KITABU CHA MORMONI

USHUHUDA MWINGINE WA
YESU KRISTO

KANISA LA
YESU KRISTO
LA WATAKATIFU
WA SIKU ZA MWISHO

KITABU CHA MORMONI

Ushuhuda Mwingine wa Yesu Kristo

Kimechapishwa na
Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho
Jiji la Salt Lake, Utah, Marekani

Toleo la kwanza kwa Kiingereza lilichapishwa
Palmyra, New York, Marekani, mwaka 1830

Tafadhali wasilisha mwitiko au mapendekezo kwa
scriptures@ChurchofJesusChrist.org au itume kwa posta kwenda
Scriptures Coordination, 50 East North Temple Street, 24th Floor,
Salt Lake City, UT 84150-3220 USA.

© 2020 by Intellectual Reserve, Inc.
All rights reserved.

Tafsiri: 5/21
Tafsiri ya the Book of Mormon
Swahili
Printed in the United States of America 09/2023

Pakua
Aplikesheni ya Kitabu cha Mormoni

KITABU CHA MORMONI

HISTORIA ILIYOANDIKWA KWA

MKONO WA MORMONI

KWENYE MABAMBA

YALIYOCHUKULIWA KUTOKA KATIKA MABAMBA YA NEFI

Kwa hivyo, huu ni ufupisho wa maandishi ya watu wa Nefi, na pia ya Walamani—Ulioandikiwa Walamani, ambao ni baki la nyumba ya Israeli; na pia kwa Myahudi na kwa Myunani—Uliandikwa kutokana na amri, na pia kwa roho ya unabii na ufunuo—Uliandikwa na kufungwa, na kufichwa katika Bwana, ili usiharibiwe—Upate kutolewa kwa karama na uwezo wa Mungu na hata utafsiri wake—Ulifungwa kwa mkono wa Moroni, na kufichwa katika Bwana, ili uje utolewe wakati wa kufaa kupitia Myunani—Na kutafsiriwa kwa karama ya Mungu.

Na pia ufupisho kutoka kitabu cha Etheri, ambao ni maandishi kuhusu watu wa Yaredi, ambao walitawanyishwa wakati Bwana alipochanganya lugha za watu, walipokuwa wakijenga mnara ili wafike mbinguni—Ambao ni kuonyesha baki la nyumba ya Israeli vitu vikubwa ambavyo Bwana aliwatendea baba zao; na ili waje maagano ya Bwana, kuwa hawakutupiliwa mbali milele—Na pia kuwathibitishia Myahudi na Myunani kwamba Yesu ndiye Kristo, Mungu wa Milele, anayejidhihirisha kwa mataifa yote—Na sasa, kama kuna makosa ni mapungufu ya wanadamu; kwa hivyo, usilaumu vitu vya Mungu, ili usipatikane na doa kwenye kiti cha hukumu cha Kristo.

TAFSIRI ASILI YA KIINGEREZA KUTOKA KWENYE MABAMBA
NA JOSEPH SMITH, MDOGO

YALIYOMO

Utangulizi vii
Ushuhuda wa Mashahidi Watatu ix
Ushuhuda wa Mashahidi Wanane ix
Ushuhuda wa Nabii Joseph Smith xi
Maelezo Mafupi xv
Picha xvii
1 Nefi 1
2 Nefi 64
Yakobo 143
Enoshi 165
Yaromu 169
Omni 171
Maneno ya Mormoni 174
Mosia 176
Alma 251
Helamani 454
3 Nefi 503
4 Nefi 575
Mormoni 579
Etheri 603
Moroni 642
Mwongozo wa Maandiko 1
Wendo 229
Upatanifu wa Injili 235

VIFUPISHO

Agano la Kale

Mwa.	Mwanzo
Ku.	Kutoka
Law.	Walawi
Hes.	Hesabu
Kum.	Kumbukumbu la Torati
Yos.	Joshua
Amu.	Waamuzi
Rut.	Ruthu
1 Sam.	1 Samweli
2 Sam.	2 Samweli
1 Fal.	1 Wafalme
2 Fal.	2 Wafalme
1 Nya.	1 Mambo ya Nyakati
2 Nya.	2 Mambo ya Nyakati
Ezra	Ezra
Neh.	Nehemia
Esta	Esta
Ayu.	Ayubu
Zab.	Zaburi
Mit.	Mithali
Mh.	Mahubiri
Wim.	Wimbo wa Suleimani
Isa.	Isaya
Yer.	Yeremia
Omb.	Maombolezo
Eze.	Ezekieli
Dan.	Danieli
Hos.	Hosea
Yoe.	Yoeli
Amo.	Amosi
Oba.	Obadia
Yon.	Yona
Mik.	Mika
Nah.	Nahamu
Hab.	Habakuki
Sef.	Sefania
Hag.	Hagai
Zek.	Zakaria
Mal.	Malaki

Agano Jipya

Mt.	Mathayo
Mk.	Marko
Lk.	Luka
Yn.	Yohana
Mdo.	Matendo
Rum.	Warumi
1 Kor.	1 Wakorintho
2 Kor.	2 Wakorintho
Gal.	Wagalatia
Efe.	Waefeso
Flp.	Wafilipi
Kol.	Wakolosai
1 The.	1 Wathesalonike
2 The.	2 Wathesalonike
1 Tim.	1 Timotheo
2 Tim.	2 Timotheo
Tit.	Tito
Flm.	Filemoni
Ebr.	Waebrania
Yak. (Bib.)	Yakobo (Bib.)
1 Pet.	1 Petro
2 Pet.	2 Petro
1 Yoh.	1 Yohana
2 Yoh.	2 Yohana
3 Yoh.	3 Yohana
Yuda	Yuda
Ufu.	Ufunuo

Kitabu cha Mormoni

1 Ne.	1 Nefi
2 Ne.	2 Nefi
Yak. (KM)	Yakobo (KM)
Eno.	Enoshi
Yar.	Yaromu
Omni	Omni
M. ya Morm.	Maneno ya Mormoni
Mos.	Mosia
Alma	Alma
Hel.	Helamani
3 Ne.	3 Nefi
4 Ne.	4 Nefi
Morm.	Mormoni
Eth.	Etheri
Moro.	Moroni

Mafundisho na Maagano

M&M	Mafundisho na Maagano
TR	Tamko Rasmi

Lulu ya Thamani Kuu

Musa	Musa
Ibr.	Ibrahimu
JS—M	Joseph Smith—Mathayo
JS—H	Joseph Smith—Historia ya
M ya I	Makala ya Imani

Vifupisho na Maelezo Mengine

TJS	Tafsiri ya Joseph Smith
MWM	Mwongozo wa Maandiko
EBR	Tafsiri mbadala kutoka katika Kiebrania
TMKIG	Tafsiri mbadala kutoka kwa Kiyunani
MY	Ufafanuzi wa nahau na miundo migumu ya sentensi
AU	Huonyesha kwamba maneno mbadala yanafuata ili kubainisha maana ya semi za kale

UTANGULIZI

Kitabu cha Mormoni ni juzuu ya maandiko matakatifu sawa sawa na Biblia. Ni kumbukumbu ya matendo ya Mungu kwa kikundi cha wakazi wa kale wa bara la Marekani na inayo utimilifu wa injili isiyo na mwisho.

Kitabu hiki kiliandikwa na manabii wengi wa kale kwa roho ya unabii na ufunuo. Maneno yao, yaliyoandikwa kwenye mabamba ya dhahabu, yalinukuliwa na kufupishwa na mwanahistoria nabii aliyeitwa Mormoni. Kumbukumbu hii inaelezea kuhusu historia ya mataifa mawili makubwa. Moja lilitoka Yerusalemu katika mwaka wa 600 K.K. na baadaye kugawanyika kuwa mataifa mawili, ambayo yalijulikana kama Wanefi na Walamani. Lingine lilikuja mapema zaidi wakati Bwana alipovuruga lugha katika Mnara wa Babeli. Kikundi hiki kinajulikana kama Wayaredi. Baada ya maelfu ya miaka, wote waliangamizwa isipokuwa Walamani, na hawa ni miongoni mwa mababu wakuu wa Wahindi wa Kiamerika.

Tukio kuu lililoandikwa katika Kitabu cha Mormoni ni huduma binafsi ya Bwana Yesu Kristo miongoni mwa Wanefi mara baada ya ufufuko Wake. Kinaeleza mafundisho ya injili, kinafafanua juu ya mpango wa wokovu, na kuwaambia binadamu mambo wanayopaswa kuyafanya ili wapate amani katika maisha haya na wokovu wa milele katika maisha yanayokuja.

Baada ya Mormoni kukamilisha maandishi yake, akamkabidhi mwanawe Moroni historia hiyo, ambaye naye akaongeza maneno yake machache na kuficha mabamba hayo katika Kilima Kumora. Mnamo 21 Septemba 1823, Moroni huyo huyo, sasa akiwa ametukuzwa, kiumbe mfufuka, akamtokea Nabii Joseph Smith na kumpa maelekezo kuhusu kumbukumbu hiyo ya kale na hatima ya tafsiri yake katika lugha ya Kiingereza.

Wakati ulipofika mabamba hayo yalitolewa kwa Joseph Smith, ambaye aliyatafsiri kwa karama na uwezo wa Mungu. Kumbukumbu hii sasa imechapishwa katika lugha nyingi kama ushuhuda mpya na wa nyongeza kuwa Yesu Kristo ndiye Mwana wa Mungu aliye hai na kwamba wote ambao watakuja Kwake na kutii sheria na ibada za injili Yake wataokolewa.

Kuhusu maandishi haya Nabii Joseph Smith Nabii alisema: "Niliwaambia ndugu kwamba Kitabu cha Mormoni ndicho kitabu sahihi duniani, na ndicho jiwe la katikati la teo la dini yetu, na kuwa mwanadamu angemkaribia Mungu zaidi kwa kufuata mafundisho yake, zaidi ya kitabu kingine."

Pamoja na Joseph Smith, Bwana aliwachagua wengine kumi na moja kujionea mabamba yale ya dhahabu na kuwa mashahidi maalum wa ukweli na utakatifu wa kitabu cha Mormoni. Ushuhuda

wao wameuandika na umechapishwa hapa na kujulikana kama "Ushuhuda wa Mashahidi Watatu" na "Ushuhuda wa Mashahidi Wanane."

Tunawakaribisha watu wote kutoka kila mahali kusoma Kitabu cha Mormoni, kutafakari mioyoni mwao ujumbe wake, na kisha kumuuliza Mungu, Baba wa Milele, katika jina la Kristo kama hiki kitabu ni cha kweli. Wale ambao watafuata njia hii na kuuliza kwa imani watapata ushuhuda wa ukweli na utakatifu wake kwa nguvu za Roho Mtakatifu. (Soma Moroni 10:3–5.)

Wale ambao wanapata ushuhuda huu mtakatifu kutoka kwa Roho Mtakatifu watakuja pia kujua kwa uwezo huo huo kwamba Yesu Kristo ndiye Mwokozi wa ulimwengu, na kwamba Joseph Smith ndiye mfunuzi na nabii Wake katika siku hizi za mwisho, na kwamba Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho ni ufalme wa Bwana ambao kwa mara nyingine tena umekuja duniani kwa ajili ya matayarisho ya Ujio wa Pili wa Masiya.

USHUHUDA WA MASHAHIDI WATATU

Ijulikane kwa mataifa yote, makabila, lugha, na watu, ambao kwao kazi hii itawajia: Kwamba sisi, kwa neema ya Mungu Baba, na Bwana wetu Yesu Kristo, tumeyaona mabamba ambayo yana kumbukumbu hiyo, ambayo ni historia ya watu wa Nefi, na pia ya Walamani, ndugu zao, na pia ya watu wa Yaredi, ambao walitoka kwenye ule mnara ambao tayari umezungumziwa. Na pia sisi tunajua kwamba yametafsiriwa kwa karama na nguvu ya Mungu, kwani sauti yake imetutangazia hayo; kwa hivyo tunajua kwa uhakika kwamba kazi hii ni ya kweli. Na pia tunashuhudia kwamba tumeona michoro ambayo iko juu ya mabamba hayo; na tumeonyeshwa haya kwa uwezo wa Mungu, wala sio wa binadamu. Na tunatangaza kwa maneno ya kiasi, kwamba malaika wa Mungu aliteremka kutoka mbinguni, na akaleta na kulaza mbele ya macho yetu, na tukatazama na kuona mabamba hayo, na michoro yake; na tunajua kwamba ni kwa neema ya Mungu Baba, na ya Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba tuliona na tunashuhudia kwamba vitu hivi ni vya kweli. Na ni ya kustaajabisha machoni mwetu. Walakini, sauti ya Bwana ilituamuru kwamba tuishuhudie; kwa hivyo, kwa kutii amri za Mungu, tunatoa ushuhuda wa mambo haya. Na tunajua kuwa kama tutakuwa waaminifu katika Kristo, tutatakasa mavazi yetu kutokana na damu ya watu wote, ili tusipatikane na doa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, na tutaishi na yeye milele mbinguni. Na utukufu uwe kwa Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu, ambao ni Mungu mmoja. Amina.

Oliver Cowdery
David Whitmer
Martin Harris

USHUHUDA WA MASHAHIDI WANANE

Ijulikane kwa mataifa yote, makabila, lugha, na watu, ambao kwao kazi hii itawajia: Kwamba Joseph Smith, Mdogo, mfasiri wa kazi hii, ametuonyesha mabamba ambayo tayari yameelezwa, ambayo yana muonekeno wa dhahabu; na tumegusa kwa mikono yetu kurasa ambazo yeye Smith ametafsiri; na pia kuona michoro juu yake, vyote vikiwa na muonekeno wa kazi ya kale, na ya ustadi wa hali ya juu. Na kwa hili tunatoa ushuhuda kwa maneno ya kiasi, kwamba Smith aliyetajwa ametuonyesha, kwani sisi tumeyaona

na kuyainua, na kujua kwa uhakika kwamba Smith aliyetajwa anayo mabamba ambayo tayari tumeyaeleza. Na tunaupatia ulimwengu majina yetu, ili kushuhudia kwa ulimwengu yale ambayo tumeyaona. Na hatudanganyi, Mungu akishuhudia hili.

Christian Whitmer	Hiram Page
Jacob Whitmer	Joseph Smith, Mkubwa
Peter Whitmer, Mdogo	Hyrum Smith
John Whitmer	Samuel H. Smith

USHUHUDA WA NABII JOSEPH SMITH

Maneno yenyewe ya Nabii Joseph Smith kuhusu ufunuo wa Kitabu cha Mormoni ni haya:

"Na kisha, jioni ya siku . . . yaani tarehe ishirini na moja ya Septemba [1823] . . . nilifanya sala na maombi kwa Mwenyezi Mungu. . . .

"Wakati nikiwa katika kumlingana Mungu, niligundua mwangaza ukitokeza chumbani mwangu, mwangaza ambao uliendelea kuongezeka hadi chumba chote kikawa na mwanga mkali zaidi kuliko jua la saa sita mchana, na hatimaye mara mtu alionekana kuwa amesimama kando ya kitanda changu, amesimama hewani, kwani miguu yake haikugusa sakafu.

"Alikuwa amevaa joho kubwa jeupe zuri sana. Weupe wake ulikuwa weupe upitao kitu chochote cha kidunia nilichopata kukiona; wala siamini kwamba kitu chochote cha kidunia chaweza kufanywa kionekane cheupe na kiangavu kama hilo. Viganja vyake vilikuwa wazi, na mikono yake pia, juu kidogo ya kifundo; hivyo, pia, nyayo zake zilikuwa wazi, kama ilivyokuwa miguu yake, hadi juu kidogo ya vifundo. Kichwa chake na shingo pia vilikuwa wazi. Niliweza kugundua kuwa hakuwa na nguo nyingine aliyoivaa ila joho hili, kwa sababu lilikuwa wazi, kwani niliweza kuyaona maungo yake.

"Siyo tu joho lake lilikuwa jeupe zaidi, lakini hata kiwiliwili chake kilikuwa na utukufu usioelezeka, na uso wake hakika uling'ara kama radi. Chumba kikajawa na mwangaza, lakini siyo sana kama ilivyokuwa kuzunguka pale alipokuwa yeye. Mara ya kwanza nilipomwangalia, niliogopa; lakini mara woga ukanitoka.

"Aliniita kwa jina, na kuniambia kwamba alikuwa mjumbe aliyetumwa kwangu kutoka uwepo wa Mungu, na kwamba jina lake lilikuwa Moroni; kwamba Mungu alikuwa na kazi ambayo mimi ningefanya; na kwamba jina langu litafikiriwa kwa mema na maovu miongoni mwa mataifa yote, makabila, na lugha, au lingetajwa kwa wema na kwa uovu miongoni mwa watu wote.

"Alisema kulikuwepo na kitabu kilichohifadhiwa, kilichoandikwa kwenye mabamba ya dhahabu, chenye kutoa historia ya wakazi wa zamani wa bara hili, na asili yao walikotokea. Yeye pia alisema kwamba utimilifu wa Injili isiyo na mwisho ulikuwepo ndani yake, kama ilivyoletwa na Mwokozi kwa wakazi hao wa kale;

"Pia, kwamba yalikuwepo mawe mawili katika pinde za fedha—na mawe haya, yalifungwa kwenye dera ya kifua, yalifanya kitu kinachoitwa Urimu na Thumimu—yamehifadhiwa pamoja na mabamba; na umiliki na utumiaji wa mawe haya ndiyo yalifanya watu waitwe 'waonaji' katika nyakati za kale au zilizopita; na kwamba Mungu alikuwa ameyatengeneza kwa ajili ya madhumuni ya kutafsiri kitabu. . . .

"Tena, akanieleza, kwamba nitakapoyapata mabamba hayo ambayo ameyasema—kwa maana wakati ambao yanapaswa kupatikana ulikuwa bado haujatimia—nisiyaonyeshe kwa mtu yeyote; wala dera ya kifua pamoja na Urimu na Thumimu; isipokuwa kwa wale tu ambao nitaamriwa niwaonyeshe; kama nitayaonyesha nitaangamizwa. Wakati alipokuwa akizungumza nami juu ya mabamba, ono lilifunguliwa akilini mwangu kwamba nikaweza kuona mahali ambapo mabamba yale yalihifadhiwa, na kwamba kila kitu nilikiona vizuri na kwa uwazi zaidi kiasi kwamba nilipajua mahali pale tena wakati nilipopatembelea.

"Baada ya mazungumzo haya, nikaona mwanga katika chumba ukianza mara moja kumzingira mtu ambaye alikuwa akizungumza nami, na ukaendelea kufanya hivyo, hadi chumba kikawa tena na giza, isipokuwa tu mahali alipokuwa amesimama, mara, nikaona, ni kama njia imefunguka hadi mbinguni, na yeye akapanda nayo hadi akatoweka kabisa, na chumba kikaachwa kama vile kilivyokuwa kabla ya mwanga huu wa mbinguni haujatokea.

"Nililala huku nikiwaza juu ya upekee wa hilo jambo, na nikishangazwa sana na yale niliyokuwa nimeambiwa na huyu mjumbe asiye wa kawaida; na halafu, katikati ya tafakuri yangu, nikagundua kwa ghafla kwamba chumba changu kilianza tena kuangazwa, na ikawa kwamba mara moja, kama ilivyokuwa, mjumbe yule yule wa mbinguni alikuwa tena kando ya kitanda changu.

"Akaanza, kuniambia tena vitu vile vile kama alivyofanya hapo awali, bila tofauti yoyote; baada ya kufanya hivyo, akanijulisha kuhusu hukumu kali ambazo zilikuwa zinakuja ulimwenguni, pamoja na ukiwa mkubwa utakaoletwa na njaa, upanga, na tauni; na kwamba hizi hukumu kali zitakuja ulimwenguni katika kizazi hiki. Baada ya kusimulia vitu hivi, akapanda juu tena kama alivyokuwa amefanya hapo awali.

"Kwa wakati huu, mawazo mazito yalikuwa yamejengwa akilini mwangu, kiasi kwamba usingizi ulitoroka machoni mwangu, nami nililala nikiwa nimezidiwa na mshangao kwa yale niliyokwisha kuyaona na kusikia. Lakini mshangao wangu ulikuwa ni wakati nilipomwona tena mjumbe yule yule kando ya kitanda changu, na nikamsikia akirejea au kurudia tena kwangu mambo yale yale kama hapo awali; na kuongeza tahadhari kwangu, akinieleza kwamba Shetani angejaribu kunishawishi (kutokana na hali ya ufukara wa familia ya baba yangu), ili kupata mabamba haya kwa madhumuni ya kupata utajiri. Hili alinikataza, akisema kwamba ni lazima nisiwe na lengo jingine lolote katika nia ya kupata mabamba haya isipokuwa kwa ajili ya kumtukuza Mungu, na nisichochewe na nia nyingine yoyote zaidi ya ile ya kuujenga ufalme wake; vinginevyo nisingeliweza kuyapata.

"Baada ya kuja mara hii ya tatu, akapaa tena mbinguni kama

hapo mwanzo, na mimi tena nikaachwa nikitafakari juu ya ugeni wa yale ambayo nilikuwa nimeyashuhudia; ambapo punde tu baada ya mjumbe yule wa mbinguni kupaa mara ya tatu, jogoo akawika, na nikafahamu kwamba siku mpya ilikuwa inapambazuka, hivyo basi mahojiano yetu lazima yalikuwa yamechukua huo usiku wote.

"Muda mfupi baadaye niliamka kutoka kitandani pangu, na, kama kawaida, nilienda kufanya kazi muhimu za siku hiyo; lakini, katika kujaribu kufanya kazi kama nyakati zingine, nilijiona kuwa nguvu zangu zimeniishia hata kunifanya nisijiweze kabisa. Baba yangu, ambaye alikuwa akifanya kazi pamoja nami, aligundua kwamba nilikuwa na matatizo, na akaniambia niende nyumbani. Nilianza kwa dhamira ya kwenda nyumbani; lakini, katika kujaribu kuvuka ukingo wa shamba ambamo tulikuwepo, nguvu zangu ziliniishia kabisa, nami nilianguka chini kabisa, na kwa muda nilikuwa sijiwezi kabisa kwa chochote.

"Kitu cha kwanza ambacho ninaweza kukikumbuka kilikuwa ni sauti ikinisemesha, ikiniita kwa jina. Niliangalia juu, na nikamwona mjumbe yule yule akiwa amesimama juu ya kichwa changu, akiwa amezungukwa na mwanga kama vile awali. Kisha akayarudia tena yale yote aliyonieleza usiku uliopita, na akaniamuru niende kwa baba yangu na kumwambia juu ya lile ono na amri nilizozipokea.

"Nilitii; nikarudi kwa baba yangu shambani, na kumweleza jambo lile lote. Yeye alinijibu kwamba lilikuwa la Mungu, na akaniambia niende na kufanya kama nilivyoamriwa na yule mjumbe. Niliondoka shambani, na kwenda mahali ambapo yule mjumbe alinieleza kwamba mabamba yamehifadhiwa; na kwa sababu ya uwazi wa lile ono ambalo nililipata juu yake, nilipajua mahali pale mara baada ya kufika hapo.

"Karibu na kijiji cha Manchester, wilaya ya Ontario, New York, kimesimama kilima cha ukubwa wa wastani, na ndicho kilima kirefu kuliko chochote katika maeneo ya jirani. Upande wa magharibi ya kilima hiki, siyo mbali kutoka kileleni, chini ya jiwe la ukubwa wa wastani, yalilala mabamba, yakiwa yamehifadhiwa ndani ya kisanduku cha jiwe. Jiwe hili lilikuwa nene na la mviringo katikati juu ya upande wa juu, na jembamba zaidi kuelekea kwenye kingo, hivyo sehemu yake ya katikati ilikuwa ikionekana juu ya udongo, lakini kingo zake zote kuzunguka zilifunikwa kwa udongo.

"Baada ya kuondoa udongo, nilipata wenzo, ambayo niliitia chini ya kingo za lile jiwe, na kwa kutumia nguvu kidogo nililiinua. Niliangalia ndani, na humo hakika niliona mabamba hayo, Urimu na Thumimu, na dera ya kifuani, kama ilivyoelezwa na yule mjumbe. Lile sanduku ambalo ndani yake yaliwekwa lilitengenezwa kwa kuyapanga mawe pamoja kwa aina fulani ya saruji. Ndani, chini ya sanduku yaliwekwa mawe mawili yakikingama na sanduku, na juu

ya mawe haya yaliwekwa mabamba hayo na vitu vingine pamoja nayo.

"Nilifanya jaribio la kuvitoa nje, lakini nilikatazwa na yule mjumbe, na tena niliarifiwa kuwa wakati wa kuvichukua ulikuwa bado haujafika, wala haungefika, hadi miaka minne kutoka wakati huo; lakini alinieleza kwamba yanipasa kuja mahali pale baada ya mwaka mmoja barabara kutoka wakati ule, na kwamba atakutana nami pale, na kwamba itanipasa kuendelea kufanya hivyo hadi wakati utakapofika wa kuyapata mabamba yale.

"Hivyo, kulingana na nilivyokuwa nimeamriwa, nilikwenda kila ilipofika mwisho wa mwaka, na kila wakati nilimkuta mjumbe yule pale, na nikapokea maelekezo na maarifa kutoka kwake katika kila mahojiano yetu, juu ya yale Bwana atakayoyafanya, na namna gani na kwa jinsi gani ufalme wake utaendeshwa katika siku za mwisho. . . .

"Hatimaye wakati ulifika wa kuyachukua mabamba, Urimu na Thumimu, na dera ya kifuani. Tarehe ishirini na mbili ya Septemba, elfu moja mia nane na ishirini na saba, ikiwa nimeenda kama kawaida mwishoni mwa mwaka mwingine mahali vilipokuwa vimehifadhiwa, mjumbe yule yule wa mbinguni alinipa pamoja na amri hii: kwamba nitawajibika juu yake; kwamba kama nitayaacha yaende kwa kukosa uangalifu, au kwa uzembe wangu, nitakatiliwa mbali; lakini kama nitatumia uwezo wangu wote kuyalinda, hadi yeye, yule mjumbe, atakapoyataka, yatalindwa.

"Muda si mrefu nilitambua sababu ya mimi kupokea amri ile kali ya kuyatunza kwa usalama, na kwa nini ilikuwa mjumbe aseme hivyo kwamba nitakapokuwa nimefanya yale yaliyotakiwa kutoka kwangu, atayataka. Kwani haikuwa muda mrefu ilijulikana kwamba nilikuwa nayo, juhudi ya nguvu nyingi zaidi ilitumika ili kuyapata kutoka kwangu mimi. Kila hila ambayo iliweza kubuniwa ilitumiwa kwa dhumuni hili. Mateso yakawa machungu zaidi na makali kuliko mwanzoni, na umati ulikuwa uko tayari daima kuyachukua kutoka kwangu kama ikiwezekana. Lakini kwa hekima ya Mungu, yalibaki salama mikononi mwangu, hadi nilipoyamalizia kazi ile iliyotakiwa kutoka kwangu. Hatimaye, kulingana na mipangilio, mjumbe yule akayataka, nikampa; naye anayo katika himaya zake hadi siku hii, ikiwa siku ya pili ya Mei, elfu moja mia nane na thelathini na nane."

Kwa historia kamili, angalia Joseph Smith—Historia ya katika Lulu ya Thamani Kuu.

Historia hiyo ya kale ilitolewa kwenye ardhi kama sauti ya watu wakizungumza kutoka mavumbini, na ikatafsiriwa kwa lugha ya kisasa kwa karama na uwezo wa Mungu kama ilivyoshuhudiwa na Ushuhuda mtakatifu, ulichapishwa mara ya kwanza ulimwenguni kwa Kiingereza mwaka wa 1830 kama The Book of Mormon.

MAELEZO MAFUPI KUHUSU KITABU CHA MORMONI

Kitabu cha Mormoni ni historia takatifu ya makundi ya watu katika Marekani ya kale, na ilikuwa imechorwa kwenye mabamba ya metali. Vyanzo ambavyo kwavyo kumbukumbu hii ilikusanywa inajumuisha vifuatavyo:

1. *Mabamba ya Nefi,* ambayo yalikuwa ya aina mbili: mabamba madogo na mabamba makubwa. Ya kwanza yalikuwa hasa yamekusudiwa zaidi kwa masuala ya kiroho na huduma yake pamoja na mafundisho ya manabii, wakati haya mengine yalikuwa zaidi na historia ya kiulimwengu ya watu husika (1 Nefi 9:2–4). Tangu wakati wa Mosia, hata hivyo, mabamba makubwa pia yalijumuisha mambo yenye umuhimu mkubwa wa kiroho.
2. *Mabamba ya Mormoni,* ambayo yalikuwa na ufupisho wa Mormoni kutoka katika yale mabamba makubwa ya Nefi, pamoja na ufafanuzi mwingi. Mabamba haya pia yalikuwa na mwendelezo wa mambo ya kihistoria iliyoandikwa na Mormoni pamoja na nyongeza ya mwanawe Moroni.
3. *Mabamba ya Etheri,* ambazo zilikuwa na historia ya Kiyaredi. Historia hii ilifupishwa na Moroni, ambaye aliongeza maneno yake na kuchanganya hayo maandishi katika historia ya jumla ijulikanayo kama "Kitabu cha Etheri."
4. *Mabamba ya Shaba Nyeupe* yaliyoletwa na watu wa Lehi kutoka Yerusalemu mnamo mwaka wa 600 K.K. Haya yalikuwa na " vitabu vitano vya Musa, . . . na pia kumbukumbu ya Wayahudi tangu mwanzo, . . . hadi mwanzoni mwa utawala wa Zedekia, mfalme wa Yuda; na pia unabii wa manabii watakatifu" (1 Nefi 5:11–13). Nukuu nyingi kutoka katika mabamba haya, zikimtaja Isaya na manabii wengine wa kibiblia na manabii wasio wa kibiblia, zinaonekana katika Kitabu cha Mormoni.

Kitabu cha Mormoni kina mgawanyo au sehemu kuu kumi na tano zinazojulikana kama vitabu, isipokuwa kimoja, kwa kawaida vitabu hivi vimetajwa kwa jina la mwandishi wake mkuu. Fungu la kwanza (vitabu sita vya kwanza, cha mwisho kikiwa Omni) ni tafsiri kutoka katika mabamba madogo ya Nefi. Katikati ya vitabu vya Omni na Mosia kuna ingizo linaloitwa Maneno ya Mormoni. Ingizo hili linaunganisha kumbukumbu iliyochorwa juu ya yale mabamba madogo pamoja na ufupisho wa Mormoni wa yale mabamba makubwa.

Sehemu ambayo ni ndefu zaidi, kutoka kitabu cha Mosia hadi

Mormoni mlango wa saba, yote pamoja, ni tafsiri ya ufupisho wa Mormoni kutoka katika yale mabamba makubwa ya Nefi. Sehemu ya mwisho, kutoka Mormoni mlango wa nane, hadi mwisho wa kitabu, ilichorwa na mwana wa Mormoni ambaye, ni Moroni, ambaye baada ya kumaliza kuandika kumbukumbu ya maisha ya baba yake, alifupisha kumbukumbu ya Wayaredi (kama kitabu cha Etheri) na baadaye akaongeza sehemu zijulikanazo kama kitabu cha Moroni.

Katika au karibia mwaka wa 421 B.K., Moroni, wa mwisho katika manabii-wanahistoria wa Kinefi, alifunga kumbukumbu ile takatifu na kuificha katika Bwana, ili itolewe katika siku za baadaye, kama vile ilivyotabiriwa na sauti ya Mungu kupitia manabii Wake wa kale. Katika mwaka wa 1823 B.K., huyo huyo Moroni, akiwa mtu aliyefufuliwa, alimtokea Nabii Joseph Smith na hatimaye akamkabidhi yale mabamba yaliyochongwa maandishi.

Juu ya toleo hili; Ukurasa asili wa kwanza wenye jina la kitabu, ulio kabla tu ya ukurasa wa yaliyomo, umetolewa kutoka kwenye mabamba na ni sehemu ya maandishi matakatifu. Utangulizi katika maneno yasiyo ya kiitaliki, kama vile yalivyo katika 1 Nefi na kabla tu Mosia mlango wa 9, nayo ni sehemu ya maandishi matakatifu. Utangulizi ulio katika kiitaliki, kama vile katika vichwa vya milango, siyo maandiko ya asili hayakuwepo mwanzoni lakini ni msaada katika kujifunza yamejumuishwa ili kurahisisha katika usomaji.

Baadhi ya makosa madogo madogo katika maandishi yameendelezwa katika matoleo yaliyopita ya Kitabu cha Mormoni kilichochapishwa kwa Kiingereza. Toleo hili lina masahihisho ambayo yameonakana yanafaa katika kuileta taarifa iliyotumika katika maandiko haya katika ulinganifu na miswada iliyokuwepo kabla ya kuchapishwa na matoleo ya mwanzoni yaliyo sahihishwa na Nabii Joseph Smith.

PICHA



Bwana Yesu Kristo
Mchoraji ni Heinrich Hoffman



Nabii Joseph Smith
Mchoraji ni Alvin Gittins

Ona "Ushuhuda wa Nabii Joseph Smith," kurasa za xi–xiv

Lehi agundua Liahona
Mchoraji ni Arnold Friberg
Ona 1 Nefi 16, kurasa za 40–44

Lehi na watu wake wanawasili katika nchi ya ahadi
Mchoraji ni Arnold Friberg
Ona 1 Nefi 18, kurasa za 50–52

Alma anabatiza katika Maji ya Mormoni
Mchoraji ni Arnold Friberg
Ona Mosia 18, kurasa za 219–222

Samweli Mlamani atoa unabii
Mchoraji ni Arnold Friberg
Ona Helamani 16, kurasa za 501–503

Yesu Kristo anazuru bara za Marekani
Mchoraji ni John Scott
Ona 3 Nefi 11, kurasa za 529–533



Moroni anazika kumbukumbu ya Wanefi
Mchoraji ni Tom Lovell
Ona Mormoni 8, kurasa 594–598

KITABU CHA KWANZA CHA NEFI

UTAWALA NA HUDUMA YAKE

Historia ya Lehi na mkewe Saria, na wanawe wanne, wanaoitwa, (kuanzia kifungua mimba) Lamani, Lemueli, Samu, na Nefi. Bwana anamwonya Lehi aondoke kutoka nchi ya Yerusalemu, kwa sababu alitoa unabii kuhusu maovu ya watu nao wanatafuta kutoa uhai wake. Anaelekea nyikani na kusafiri kwa siku tatu akiwa na jamii yake. Nefi anawachukua kaka zake na kurejea nchi ya Yerusalemu kuchukua maandishi ya Wayahudi. Historia ya mateso yao. Wanawaoa mabinti za Ishmaeli. Wanachukua jamaa zao na kuelekea nyikani. Mateso na masumbuko yao wakati wakiwa nyikani. Njia zao safarini. Wanafikia maji makubwa. Kaka za Nefi wanamuasi. Anawafadhaisha, na kujenga merikebu. Walipaita pahali pa Neema. Wanavuka bahari na kufika katika nchi ya ahadi, na hali kadhalika. Haya ni kulingana na historia ya Nefi; hii ina maana kwamba, mimi, Nefi, ndiye niliyeandika maandishi haya.

MLANGO WA 1

Nefi anaanza maandishi ya watu wake—Lehi aona ono la nguzo ya moto na kusoma kutoka kitabu cha unabii—Anamsifu Mungu, anatabiri kuja kwa Masiya, na kutoa unabii kuhusu maangamizo ya Yerusalemu—Anateswa na Wayahudi. Karibia mwaka 600 K.K.

1 MIMI, [a]Nefi, nikiwa nimezaliwa na [b]wazazi [c]wema, kwa hivyo nilikuwa [d]nimefundishwa karibu yote ambayo baba yangu alijua; na baada ya kushuhudia [e]masumbuko mengi maisha mwangu, haidhuru, nikiwa nimebarikiwa na Bwana maishani mwangu; ndiyo, nikiwa nimepokea ufahamu wa wema na [f]siri za Mungu, kwa hivyo naandika [g]maandishi juu ya mambo ya maisha yangu.

2 Ndiyo, naandika maandishi kwa [a]lugha ya baba yangu, ambayo ni pamoja na elimu ya Wayahudi na lugha ya Wamisri.

3 Na ninajua kwamba maandishi ambayo ninaandika ni ya [a]kweli; na ninayaandika kwa mkono wangu; na ninayaandika kadiri nijuavyo.

4 Kwani ikawa mwanzoni mwa mwaka wa [a]kwanza wa utawala

1 1*a* MWM Nefi, Mwana wa Lehi.
b M&M 68:25, 28. MWM Wazazi.
c Mit. 22:1.
d Eno. 1:1; Mos. 1:2–3.
MWM Fundisha, Mwalimu.
e MWM Shida.
f MWM Siri za Mungu.
g MWM Maandiko.
2*a* Mos. 1:2–4; Morm. 9:32–33.
3*a* 1 Ne. 14:30; Mos. 1:6; Eth. 5:1–3; M&M 17:6.
4*a* 598 K.K.; tazama Wendo katika kiambatisho.

wa [b]Zedekia, mfalme wa Yuda, (baba yangu, Lehi, akiwa ameishi katika [c]Yerusalemu maisha yake yote); na katika mwaka huo walikuja [d]manabii wengi, wakitoa unabii na kuwaambia watu kwamba lazima watubu, au sivyo mji mkuu wa [e]Yerusalemu lazima uangamizwe.

5 Kwa hivyo ikawa baba yangu, [a]Lehi, aliendelea mbele aliomba dua kwa Bwana, ndiyo, hata na [b]moyo wake wote, kwa niaba ya watu wake.

6 Na ikawa alipokuwa akimwomba Bwana, palitokea moto mfano wa [a]nguzo na ukatua juu ya mwamba uliokuwa mbele yake; na akaona na kusikia mengi; na kwa sababu ya vitu alivyoona na kusikia alitetemeka na kutapatapa kupita kiasi.

7 Na ikawa kwamba alirejea nyumbani kwake Yerusalemu; na akajitupa kitandani mwake, akiwa [a]amelemewa na Roho na vitu alivyoviona.

8 Na ikiwa amelemewa na Roho, alichukuliwa kwa [a]ono, hata kwamba aliona [b]mbingu zikifunguka, na akadhani kuwa alimwona Mungu ameketi kwenye kiti chake cha enzi, akizingirwa na malaika wasio na idadi wakiwa katika hali ya kumwimbia na kumsifu Mungu wao.

9 Na ikawa kwamba alimwona Mmoja akishuka kutoka katikati ya mbingu, na akaona [a]mng'aro wake ulikuwa zaidi ya jua la adhuhuri.

10 Na pia akaona wengine [a]kumi na wawili wakimfuata, na mng'aro wao ulikuwa zaidi ya ule wa nyota angani.

11 Na wakaja chini na wakatembea usoni mwa dunia; na wa kwanza akaja na kusimama mbele ya baba yangu, na akampatia [a]kitabu, na akamwamuru asome.

12 Na ikawa alipokuwa akisoma, alijazwa na [a]Roho wa Bwana.

13 Na akasoma, akisema: Ole, ole kwa Yerusalemu, kwani nimeona [a]machukizo yako! Ndiyo, na vitu vingi vilisomwa na baba yangu kuhusu [b]Yerusalemu—kwamba itaangamizwa, na wenyeji wake pia; wengi wangekufa kwa upanga, na wengi [c]wangetekwa nyara na kupelekwa Babilonia.

14 Na ikawa kwamba baada

4 *b* 2 Nya. 36:10; Yer. 52:3–5; Omni 1:15.
c 1 Nya. 9:3.
d 2 Fal. 17:13–15; 2 Nya. 36:15–16; Yer. 7:25–26. MWM Nabii.
e Yer. 26:18; 2 Ne. 1:4; Hel. 8:20.
5 *a* MWM Lehi, Baba wa Nefi.
b Yak. (Bib.) 5:16.
6 *a* Ku. 13:21; Hel. 5:24, 43; M&M 29:12; JS—H 1:16.
7 *a* Dan. 10:8; 1 Ne. 17:47; Musa 1:9–10; JS—H 1:20.
8 *a* 1 Ne. 5:4. MWM Ono.
b Eze. 1:1; Mdo. 7:55–56; 1 Ne. 11:14; Hel. 5:45–49; M&M 137:1.
9 *a* JS—H 1:16–17.
10 *a* MWM Mtume.
11 *a* Eze. 2:9.
12 *a* M&M 6:15.
13 *a* 2 Fal. 24:18–20; 2 Nya. 36:14.
b 2 Fal. 23:27; 24:2; Yer. 13:13–14; 2 Ne. 1:4.
c 2 Fal. 20:17–18; 2 Ne. 25:10; Omni 1:15.

ya baba yangu kusoma na kuona vitu vingi vikubwa na vya ajabu, alipaza sauti kwa Bwana akisema vitu vingi; kama: Kazi zako ni kuu na za ajabu, Ewe Bwana Mungu Mwenyezi! Kiti chako cha enzi kiko juu mbinguni, na nguvu zako, na wema wako, na rehema zako ziko juu ya wakazi wote wa dunia; na, kwa sababu una huruma, hutakubali wale ambao [a]watakuja kwako waangamie!

15 Na baba yangu alitumia maneno kama haya kwa kumsifu Mungu wake; kwani nafsi yake ilishangilia, na moyo wake wote ulijaa furaha, kwa sababu ya vitu vile alivyokuwa ameona, ndiyo, vile Bwana alivyokuwa amemwonyesha.

16 Na sasa mimi, Nefi, siandiki maandishi yote ambayo baba yangu aliandika, kwani ameandika vitu vingi ambavyo aliona kwa maono na kwa ndoto; na pia ameandika vitu vingi ambavyo alitoa [a]unabii na kuwaambia watoto wake, ambayo mimi sitaandika yote.

17 Lakini nitaandika maandishi ya matendo yangu maishani mwangu. Tazama, [a]ninafupisha [b]maandishi ya baba yangu, na kuyaandika katika mabamba ambayo nilitengeneza kwa mikono yangu mwenyewe; kwa hivyo, baada ya kufupisha maandishi ya baba yangu ndipo nitaandika maandishi kuhusu maisha yangu.

18 Kwa hivyo, ningetaka mjue, kwamba baada ya Bwana kumwonyesha baba yangu, Lehi, vitu vingi vya ajabu, ndiyo, kuhusu [a]kuangamizwa kwa Yerusalemu, tazama alienda miongoni mwa watu, na akaanza kutoa [b]unabii na kuwatangazia vile vitu alivyokuwa ameviona na kusikia.

19 Na ikawa kwamba Wayahudi walimfanyia [a]mzaha kwa sababu ya vitu vile alivyowashuhudia; kwa kweli aliwashuhudia kuhusu uovu wao na machukizo yao; na akawashuhudia kwamba vitu vile ambavyo alivyokuwa ameviona na kusikia, na pia vitu ambavyo alikuwa amesoma katika kitabu, vilidhihirisha wazi kuja kwa [b]Masiya, na pia ukombozi wa ulimwengu.

20 Na wakati Wayahudi waliposikia vitu hivi, walimkasirikia; ndiyo, jinsi ilivyokuwa kwa manabii wa kale, ambao walikuwa [a]wamewatupa nje, na kuwapiga kwa mawe, na kuwaua; na pia walimtafuta ili watoe uhai wake. Lakini tazama, mimi, Nefi, nitawaonyesha ninyi kuwa Bwana ana [b]huruma nyororo juu ya wale ambao amewachagua, kwa sababu ya imani yao, kuwatia nguvu hata kwenye uwezo wa ukombozi.

14*a* Alma 5:33–36; 3 Ne. 9:14.
16*a* 1 Ne. 7:1.
17*a* 1 Ne. 9:2–5.
b 1 Ne. 6:1–3; 19:1–6; 2 Ne. 5:29–33; M&M 10:38–46.
18*a* 2 Ne. 25:9–10; M&M 5:20.
b MWM Toa unabii, Unabii.
19*a* 2 Nya. 36:15–16; Yer. 25:4; 1 Ne. 2:13; 7:14.
b MWM Masiya.
20*a* Hel. 13:24–26.
b Alma 34:38; M&M 46:15. MWM Rehema, enye Rehema.

MLANGO WA 2

Lehi anachukua jamii yake nyikani kando ya Bahari ya Shamu—Wanaacha mali yao—Lehi anamtolea Bwana dhabihu na anawafundisha wanawe kuweka amri—Lamani na Lemueli wananung'unika dhidi ya baba yao—Nefi ni mtiifu na anasali kwa imani; Bwana anamzungumzia na anachaguliwa kuwaongoza kaka zake. Karibia mwaka wa 600 K.K.

Kwani tazama, ikawa kuwa Bwana alimzungumzia baba yangu, ndiyo, hata katika ndoto, na akamwambia: Umebarikiwa ewe Lehi, kwa sababu ya vitu ambavyo umetenda; na kwa sababu umekuwa mwaminifu na kuwatangazia hawa watu vile vitu nilivyokuamrisha, tazama, wanakutafuta [a]watoe uhai wako.

2 Na ikawa kwamba Bwana [a]akamwamrisha baba yangu, hata kwenye [b]ndoto, kuwa [c]aichukue jamii yake na aelekee nyikani.

3 Na ikawa kwamba alikuwa [a]mtiifu kwa neno la Bwana, kwa hivyo alitenda kulingana na yale Bwana aliyomwamuru.

4 Na ikawa kwamba akatoka na kuelekea nyikani. Na akaacha nyumba yake, na nchi yake ya urithi, na dhahabu yake, na fedha yake, na vitu vyake vya thamani, na hakubeba chochote, isipokuwa jamii yake, na maakuli, pamoja na mahema, na [a]akaelekea nyikani.

5 Na akashuka mipakani karibu na ufuko wa [a]Bahari ya Shamu; na akasafiri nyikani mipakani ambayo imekaribia Bahari ya Shamu; na akasafiri nyikani na jamii yake, ambayo ilikuwa ni mama yangu, Saria, na kaka zangu wakubwa ambao walikuwa ni [b]Lamani, Lemueli, na Samu.

6 Na ikawa kwamba baada ya yeye kusafiri nyikani kwa siku tatu, alipiga hema lake [a]bondeni kando ya mto wa maji.

7 Na ikawa kwamba alijenga [a]madhabahu ya [b]mawe, na akamtolea Bwana dhabihu, na [c]kumshukuru Bwana Mungu wetu.

8 Na ikawa kwamba aliuita ule mto, Lamani, na ulitiririka ukielekea Bahari ya Shamu; na bonde lilikuwa mipakani karibu na kinywa cha huo mto.

9 Na wakati baba yangu alipoona kwamba maji ya ule mto yalitiririka kwenye chemchemi ya Bahari ya Shamu, alimzungumzia Lamani, na kusema: Ee kwamba uwe kama mto huu, daima ukitiririka kwenye chemchemi ya haki yote!

10 Na pia akamzungumzia Lemueli: Ee kwamba uwe kama bonde hili, imara na thabiti, na asiyetingishika kwa kuweka amri za Bwana!

11 Sasa aliyazungumza haya

2 1*a* 1 Ne. 7:14.
2*a* 1 Ne. 5:8; 17:44.
b MWM Ndoto.
c Mwa. 12:1; 2 Ne. 10:20; Eth. 1:42; Ibr. 2:3.
3*a* MWM Mtiifu, Tii, Utii.
4*a* 1 Ne. 10:4; 19:8.
5*a* 1 Ne. 16:14; M&M 17:1.
b MWM Lamani.
6*a* 1 Ne. 9:1.
7*a* Mwa. 12:7–8; Ku. 24:4; Ibr. 2:17.
b Ku. 20:25; Kum. 27:5–6.
c MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.

kwa sababu ya ugumu wa Lamani na Lemueli; kwani tazama [a]walinung'unika kwa vitu vingi dhidi ya [b]baba yao, kwa sababu alikuwa ni mtu wa [c]maono, na alikuwa amewatoa kutoka nchi ya Yerusalemu, kuacha nchi yao ya urithi, na dhahabu zao, na fedha zao, na vitu vyao vya thamani, kuangamia nyikani. Na wakasema alikuwa ametenda haya kwa sababu ya mafikira ya ujinga moyoni mwake.

12 Na hivyo ndivyo Lamani na Lemueli, wakiwa wakubwa, walivyonung'unika dhidi ya baba yao. Na walinung'unika kwa sababu [a]hawakujua matendo ya yule Mungu aliyewaumba.

13 Wala hawakuamini kuwa Yerusalemu, mji ule mkuu, [a]ungeangamizwa kulingana na maneno ya manabii. Na walikuwa kama Wayahudi waliokuwa Yerusalemu, ambao walimtafuta baba yangu wakitaka kumtoa uhai wake.

14 Na ikawa kwamba baba yangu akawazungumzia katika bonde la Lemueli, [a]kwa nguvu, akiwa amejazwa na Roho, hadi miili yao [b]ikatetemeka mbele yake. Na aliwafadhaisha, kwamba hawakunena lolote kinyume chake; kwa hivyo, wakatenda alivyowaamrisha.

15 Na baba yangu aliishi kwenye hema.

16 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nikiwa mdogo, ingawa nilikuwa na mwili mkubwa, na pia nikiwa na hamu ya kujua [a]siri za Mungu, kwa hivyo, nikamlilia Bwana; na tazama [b]akanijia mimi, na [c]akanigusa moyo wangu kwamba [d]nikaamini maneno yote ambayo [e]baba yangu alikuwa amezungumza; kwa hivyo, mimi sikumwasi kama kaka zangu.

17 Na nikazungumza na Samu, nikimjulisha vile vitu ambavyo Bwana alikuwa amenidhihirishia kwa Roho Mtakatifu. Na ikawa kwamba aliamini maneno yangu.

18 Lakini, tazama, Lamani na Lemueli hawakusikiza maneno yangu; na nikiwa [a]nimehuzunishwa na ugumu wa mioyo yao nikamlilia Bwana kwa niaba yao.

19 Na ikawa kwamba Bwana akanizungumzia, akisema: Umebarikiwa ewe, Nefi, kwa sababu ya [a]imani yako, maana umenitafuta kwa bidii, kwa unyenyekevu wa moyo.

20 Na kadiri utakavyozishika amri zangu, wewe [a]utafanikiwa, na utaongozwa kwa [b]nchi ya ahadi; ndiyo, hata nchi ambayo nimekutayarishia wewe; ndiyo

11 *a* 1 Ne. 17:17.
MWM Manung'uniko.
b Mit. 20:20.
c 1 Ne. 5:2–4.
12 *a* Musa 4:6.
13 *a* Yer. 13:14; 1 Ne. 1:13.
14 *a* MWM Uwezo.
b 1 Ne. 17:45.
16 *a* MWM Siri za Mungu.
b Zab. 8:4; Alma 17:10; M&M 5:16.
MWM Ufunuo.
c 1 Fal. 18:37; Alma 5:7.
d 1 Ne. 11:5.
e MWM Baba, Mwili wenye kufa; Nabii.
18 *a* Alma 31:24; 3 Ne. 7:16.
19 *a* 1 Ne. 7:12; 15:11.
20 *a* Yos. 1:7; 1 Ne. 4:14; Mos. 1:7.
b Kum. 33:13–16; 1 Ne. 5:5; 7:13; Musa 7:17–18.
MWM Nchi ya Ahadi.

nchi ambayo ni bora kuzidi nchi zingine.

21 Na kadiri kaka zako watakavyokuasi wewe, [a]watatengwa mbali na Bwana.

22 Na kadiri utakavyo weka amri zangu, wewe utakuwa [a]mtawala na mwalimu wa kaka zako.

23 Kwani tazama, katika siku ile watakaponiasi, [a]nitawalaani hata na laana kali, na hawatakuwa na uwezo juu ya uzao wako ijapokuwa pia nao waniasi.

24 Na kama wataniasi, watakuwa [a]mjeledi kwa uzao wako, kwa [b]kuwavuruga wakumbuke njia zangu.

MLANGO WA 3

Wana wa Lehi warejea Yerusalemu kupata mabamba ya shaba nyeupe—Labani anakataa kuwapa mabamba—Nefi anawasihi na kuwatia moyo kaka zake—Labani anaiba mali yao na anajaribu kuwauwa—Lamani na Lemueli wanawapiga Nefi na Samu na wanashutumiwa na malaika. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilirudi kwenye hema la baba yangu, baada ya kusema na Bwana.

2 Na ikawa kwamba akanisemesha, na kuniambia: Tazama nimeota [a]ndoto, ambapo Bwana ameniamrisha kwamba wewe na kaka zako mtarejea Yerusalemu.

3 Kwani tazama, Labani anazo kumbukumbu za Wayahudi na pia [a]nasaba ya babu zangu, na zimechorwa kwenye mabamba ya shaba nyeupe.

4 Kwa hivyo, Bwana ameniamrisha mimi kwamba wewe na kaka zako mwende nyumbani kwa Labani, mtafute hayo maandishi, na kuyaleta hapa nyikani.

5 Na sasa, tazama kaka zako wananung'unika, wakisema kuwa ni kitu kigumu ninachokihitaji kutoka kwao; lakini, tazama mimi sijahitaji hilo kwao, lakini ni amri ya Bwana.

6 Kwa hivyo nenda, mwana wangu, nawe utapendeka kwa Bwana, kwa sababu wewe [a]hujanung'unika.

7 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilimwambia baba yangu: [a]Nitaenda na kutenda vitu ambavyo Bwana ameamuru, kwani ninajua kwamba Bwana hatoi [b]amri kwa watoto wa watu, isipokua [c]awatayarishie njia ya kutimiza kitu ambacho amewaamuru.

8 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kusikia maneno haya alifurahi sana, maana alijua kuwa nimebarikiwa na Bwana.

21 *a* 2 Ne. 5:20–24; Alma 9:13–15; 38:1.
22 *a* Mwa. 37:8–11; 1 Ne. 3:29.
23 *a* Kum. 11:28; 1 Ne. 12:22–23; M&M 41:1.
24 *a* Yos. 23:13; Amu. 2:22–23.
b 2 Ne. 5:25.

3 2 *a* MWM Ndoto.
3 *a* 1 Ne. 5:14.
6 *a* MWM Kuwakubali Viongozi wa Kanisa.
7 *a* 1 Sam. 17:32; 1 Fal. 17:11–15.
MWM Amini, Imani; Mtiifu, Tii, Utii.
b MWM Amri za Mungu.
c Mwa. 18:14; Flp. 4:13; 1 Ne. 17:3, 50; M&M 5:34.

9 Na mimi, Nefi, na kaka zangu tukachukua safari nyikani, pamoja na mahema yetu, tukielekea nchi ya Yerusalemu.

10 Na ikawa kwamba tulipokuwa tumesafiri hadi nchi ya Yerusalemu, mimi na kaka zangu tulijadiliana.

11 Na [a]tukapiga kura—ni nani kati yetu ataingia nyumbani mwa Labani. Na ikawa kwamba kura ikamwangukia Lamani; na Lamani akaenda nyumbani mwa Labani, na akaongea na yeye alipokuwa ameketi nyumbani mwake.

12 Na akamwomba Labani zile kumbukumbu ambazo zilikuwa zimechorwa kwenye mabamba ya shaba nyeupe, ambazo zilikuwa na [a]nasaba ya baba yangu.

13 Na tazama, ikawa kwamba Labani alikasirika, na akamtoa nje; na asitake kumpatia yale maandishi. Kwa hivyo, akamwambia: Tazama wewe ni mnyang'anyi, na nitakuua.

14 Lakini Lamani alitoroka kutoka kwake, na akatuelezea vitu ambavyo Labani alitufanyia. Na tulishikwa na huzuni nyingi, na kaka zangu walikuwa karibu kurudi nyikani kwa baba yangu.

15 Lakini tazama nikawaambia kwamba: Kadiri Bwana aishivyo, na tuishivyo sisi, hatutarudi kwa baba yetu nyikani mpaka tukamilishe kile kitu ambacho Bwana alituamrisha sisi.

16 Kwa hivyo, tuwe waaminifu katika kushika amri za Bwana; kwa hivyo tuteremke hadi kwa nchi ya [a]urithi ya baba yetu, kwani tazama aliacha dhahabu na fedha, na kila aina ya utajiri. Na haya yote ametenda kwa sababu ya [b]amri za Bwana.

17 Kwani alijua kwamba lazima Yerusalemu [a]iangamizwe, kwa sababu ya uovu wa watu.

18 Kwani tazama, [a]wamekataa maneno ya manabii. Kwa hivyo, kama baba yangu ataishi katika nchi baada ya [b]kuamriwa atoroke nchi hiyo, tazama, pia yeye ataangamia. Kwa hivyo, inabidi lazima atoroke nchi hiyo.

19 Na tazama, ni hekima katika Mungu tupate kuchukua [a]maandishi haya, ili tuweze kuhifadhia watoto wetu lugha ya baba zetu;

20 Na pia kwamba [a]tuwahifadhie maneno yaliyonenwa kwa vinywa vya manabii watakatifu, ambayo walipewa na Roho na nguvu za Mungu, tangu mwanzo wa ulimwengu, hadi nyakati za sasa.

21 Na ikawa kwamba niliwashawishi kaka zangu kwa maneno haya, ili wawe waaminifu kwa kushika amri za Mungu.

22 Na ikawa kwamba tulishuka na kwenda katika nchi yetu ya urithi, na tukakusanya [a]dhahabu yetu, na fedha yetu, na vitu vyetu vya thamani.

11 *a* Neh. 10:34; Mdo. 1:26.
12 *a* 1 Ne. 3:3; 5:14.
16 *a* 1 Ne. 2:4.
b 1 Ne. 2:2; 4:34.
17 *a* 2 Nya. 36:16–20; Yer. 39:1–9; 1 Ne. 1:13.
18 *a* MWM Uasi.
b 1 Ne. 16:8.
19 *a* Omni 1:17; Mos. 1:2–6.
20 *a* MWM Maandiko—Maandiko yahifadhiwe.
22 *a* 1 Ne. 2:4.

23 Na baada ya kukusanya hivi vitu pamoja, tukaenda tena nyumbani mwa Labani.

24 Na ikawa kwamba tulikutana na Labani, na tukataka atupatie zile kumbukumbu ambazo zilikuwa zimechorwa kwenye [a]mabamba ya shaba nyeupe, kwa ajili hiyo nasi tungempatia dhahabu yetu, na fedha yetu, na vitu vyetu vyote vya thamani.

25 Na ikawa kwamba wakati Labani alipoona mali yetu, na kwamba ilikuwa nyingi sana, [a]aliitamani, hadi kwamba akatufukuza nje, na akatuma watumishi wake watuue, ili kwamba aweze kupata mali yetu.

26 Na ikawa kwamba tuliwakimbia watumishi wa Labani, na ikatubidi kuacha mali yetu, na ikangukia mikononi mwa Labani.

27 Na ikawa kwamba tulitorokea nyikani, na watumishi wa Labani hawakutupata, na tukajificha kwenye pango la mwamba.

28 Na ikawa kwamba Lamani alinikasirikia mimi, na baba yangu pia; na pia Lemueli, kwani alisikiliza maneno ya Lamani. Kwa hivyo Lamani na Lemueli walituzungumzia kwa maneno mengi ya [a]uchungu, sisi wadogo zao, na wakatupiga sisi hata kwa bakora.

29 Na ikawa kwamba walipokuwa wakitupiga kwa bakora, tazama [a]malaika wa Bwana alikuja na akasimama mbele yao, na akawazungumzia, akisema: Kwa nini mnampiga mdogo wenu kwa bakora? Hamjui kuwa Bwana amemchagua yeye kuwa [b]kiongozi wenu, na hii ni kwa sababu ya maovu yenu? Tazama mtarudi tena Yerusalemu, na Bwana atamkabidhi Labani mikononi mwenu.

30 Na baada ya [a]malaika kutuzungumzia, akatoweka.

31 Na baada ya malaika kutoweka, Lamani na Lemueli wakaanza [a]kunung'unika tena, wakisema: Vipi itawezekana kwamba Bwana atamkabidhi Labani mikononi mwetu? Tazama, yeye ni mtu shujaa, na anaweza kuamuru watu hamsini; ndiyo, hata kuwaua watu hamsini; je, kwa nini asituue sisi?

MLANGO WA 4

Nefi anamuua Labani kwa amri ya Bwana na kisha anayapata mabamba ya shaba nyeupe kwa werevu—Zoramu achagua kuandamana na familia ya Lehi nyikani. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na ikawa kwamba nikawazungumzia kaka zangu, nikisema: Twendeni tena Yerusalemu, na tuwe [a]waaminifu kwa kuzishika amri za Bwana; kwani tazama yeye ni [b]mkuu kupita ulimwengu wote, basi kwa nini asiwe mkuu kupita Labani na

24 *a* 1 Ne. 3:3.
25 *a* MWM Tamani.
28 *a* 1 Ne. 17:17–18.
29 *a* 1 Ne. 4:3; 7:10.
MWM Malaika.
b 1 Ne. 2:22.
30 *a* 1 Ne. 16:38.
31 *a* MWM Manung'uniko.
4 1 *a* MWM Amini, Imani; Ushujaa, enye Ushujaa.
b 1 Ne. 7:11–12.

watu wake hamsini, ndiyo, au hata kupita kumi ya maelfu?

2 Kwa hivyo twendeni; tuwe [a]hodari kama [b]Musa; kwani alinena na maji ya [c]Bahari ya Shamu nayo yakagawanyika pande mbili huku na huko, na mababu zetu wakapita, katika nchi kavu, kutoka utumwani, na majeshi ya Farao yakafuata na kuzama majini mwa Bahari ya Shamu.

3 Tazama sasa mnajua kwamba hii ni kweli; na pia mnajua kwamba [a]malaika amewazungumzia; je mnaweza kuwa na shaka? Twendeni; Bwana anaweza kutukomboa, kama baba zetu, na kumwangamiza Labani, hata kama Wamisri.

4 Sasa baada ya mimi kunena maneno haya, bado walikuwa na hasira, na wakaendelea kunung'unika; walakini walinifuata hadi tukafika nje ya kuta za Yerusalemu.

5 Na ilikuwa usiku; na nikawaambia wajifiche nje ya kuta. Na baada ya wao kujificha, mimi, Nefi, nilinyemelea hadi ndani ya mji na nikaelekea hadi nyumba ya Labani.

6 Na [a]nikaongozwa na Roho, wala [b]sikujua kimbele vitu ambavyo ningefanya.

7 Walakini niliendelea mbele, na nilipokaribia nyumba ya Labani nilimwona mtu, na alikuwa ameanguka kwenye ardhi mbele yangu, kwani alikuwa amelewa kutokana na mvinyo.

8 Na nilipomkaribia niligundua kwamba alikuwa Labani.

9 Na nikaona [a]upanga wake, na nikautoa kutoka ala wake; na mpini wake ulikuwa wa dhahabu halisi, na uumbaji wake ulikuwa mzuri sana, na nikaona upanga wake ulikuwa wa chuma chenye thamani.

10 Na ikawa kwamba Roho [a]alinishurutisha nimuue Labani; lakini nikasema moyoni mwangu: Sijawahi wakati wowote kumwaga damu ya mtu. Na nikasita na sikutaka kumuua.

11 Na Roho aliniambia tena: Tazama [a]Bwana amemkabidhi mikononi mwako. Ndiyo, na pia nilijua kwamba alikuwa amenitafuta kunitoa uhai; ndiyo, na pia hakusikiza amri za Bwana; na alikuwa pia [b]amechukua mali yetu.

12 Na ikawa kwamba Roho aliniambia tena: Muuwe, kwani Bwana amemkabidhi mikononi mwako;

13 Tazama Bwana [a]huwaua [b]waovu ili atimize madhumuni yake ya haki. [c]Yafaa mtu mmoja afe badala ya taifa kufifia na kuangamia katika kutoamini.

14 Na sasa, mimi, Nefi, niliposikia maneno haya, nikakumbuka maneno ya Bwana ambayo

2*a* Kum. 11:8.
b MWM Musa.
c Ku. 14:21; 1 Ne. 17:26; Mos. 7:19.
3*a* 1 Ne. 3:29–31; 7:10.
6*a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi; Roho Mtakatifu.
b Ebr. 11:8.
9*a* 2 Ne. 5:14; M&M 17:1.
10*a* Alma 14:11.
11*a* 1 Sam. 17:41–49.
b 1 Ne. 3:26.
13*a* 1 Ne. 17:33–38; M&M 98:31–32.
b MWM Ovu, Uovu.
c Alma 30:47.

alinizungumzia nyikani, akisema kwamba: [a]Kadiri uzao wako utakavyoshika [b]amri zangu, [c]watafanikiwa katika [d]nchi ya ahadi.

15 Ndiyo, na pia nikafikiria kwamba hawangeshika amri za Bwana kulingana na sheria za Musa, hadi wawe na hizo sheria.

16 Na pia nilijua kwamba [a]sheria ilikuwa imechorwa katika mabamba ya shaba nyeupe.

17 Na tena, nilijua kwamba Bwana alikuwa amemkabidhi Labani mikononi mwangu kwa sababu hii—kwamba nipate kuchukua yale maandishi kulingana na amri zake.

18 Kwa hivyo nikatii sauti ya Roho, na nikamshika Labani kwa nywele za kichwa chake, na nikamkata kichwa chake kwa [a]upanga wake.

19 Na baada ya kukata kichwa chake kwa upanga wake, nilichukua mavazi ya Labani na nikayavaa; ndiyo, hata kila chembe; na nikafunga vazi la vita lake kiunoni mwangu.

20 Na baada ya kutenda hivyo, nilielekea kwenye nyumba ya hazina ya Labani. Na nilipoelekea kwenye nyumba ya hazina ya Labani, tazama, nilimwona [a]mtumishi wa Labani ambaye alikuwa na funguo za nyumba ya hazina. Na nikamwamrisha nikiiga sauti ya Labani, kwamba aandamane na mimi hadi nyumba ya hazina.

21 Na akadhania kwamba mimi ni tajiri wake, Labani, kwani aliona mavazi na pia upanga nimeufunga kiunoni.

22 Na akanizungumzia kuhusu wazee wa Wayahudi, yeye akijua kwamba tajiri yake, Labani, alikuwa nje miongoni mwao usiku ule.

23 Nami nikazungumza na yeye kama kwamba nilikuwa Labani.

24 Na pia nikamwambia kwamba inanibidi kuchukua michoro, ambayo ilikuwa kwenye [a]mabamba ya shaba nyeupe, kwa kaka zangu, waliokuwa nje ya kuta.

25 Na pia nikamwamuru anifuate.

26 Na yeye, akidhania kwamba nilikuwa nikizungumza kuhusu ndugu wa kanisa, na kwamba nilikuwa Labani ambaye nilikuwa nimemuua, kwa hivyo alinifuata.

27 Na akanizungumzia mara nyingi kuhusu wazee wa Wayahudi, nilipokuwa nikielekea kwa kaka zangu, ambao walikuwa nje za kuta.

28 Na ikawa kwamba wakati Lamani aliponiona alishikwa na woga mwingi, pia Lemueli na Samu. Na walinikimbia; kwani walidhani kuwa ni Labani, na kwamba alikuwa ameniua na alikuwa anajaribu kutoa uhai wao pia.

29 Na ikawa kwamba niliwa-

14*a* Omni 1:6; Mos. 2:22; Eth. 2:7–12.
b MWM Amri za Mungu.
c 1 Ne. 2:20.
d 1 Ne. 17:13–14; Yak. (KM) 2:12.
16*a* MWM Torati ya Musa.
18*a* 1 Sam. 17:51.
20*a* 2 Ne. 1:30.
24*a* 1 Ne. 3:12, 19–24; 5:10–22.

ita, na wakanisikia; kwa hivyo wakaacha kunitoroka.

30 Na ikawa kwamba wakati mtumishi wa Labani aliona kaka zangu alianza kutetemeka, na alikuwa karibu kutoroka na kurejea katika mji wa Yerusalemu.

31 Na sasa mimi, Nefi, nikiwa mtu mwenye umbo kubwa, na pia nikiwa nimepokea [a]nguvu nyingi za Bwana, kwa hivyo nikamkamata mtumishi wa Labani, na nikamzuia, kwamba asitoroke.

32 Na ikawa kwamba nikamzungumzia, kwamba kama angesikiza maneno yangu, kama Bwana anavyoishi, na kama ninavyoishi, endapo angesikiza maneno yetu, basi tungehifadhi maisha yake.

33 Na nikamzungumzia, hata kwa [a]kiapo, kwamba asiogope; kwamba atakuwa mtu huru kama sisi ikiwa atakwenda nyikani pamoja nasi.

34 Na pia nikamzungumzia, nikisema: Kwa kweli Bwana [a]ametuamuru kutenda kitu hiki; je hatutakuwa wenye juhudi kuweka amri za Bwana? Kwa hivyo, kama utaenda nyikani kwa baba yangu utapata mahali pa kuishi pamoja nasi.

35 Na ikawa kwamba Zoramu alifarijika na maneno ambayo nilimzungumzia. Sasa [a]Zoramu lilikuwa jina lake huyo mtumishi; na akaahidi kwamba ataenda huko nyikani kwa baba yetu. Ndiyo, na pia aliapa kwamba ataishi pamoja nasi tangu wakati ule na kuendelea.

36 Sasa tulitaka aishi nasi kwa sababu hii, ili Wayahudi wasijue kuhusu ukimbizi wetu wa nyikani, na kutufuata ili watuangamize.

37 Na ikawa kwamba wakati Zoramu alitupatia [a]kiapo, hofu yetu kumhusu ikakoma.

38 Na ikawa kwamba tukayachukua mabamba ya shaba nyeupe na mtumishi wa Labani, na kuelekea nyikani, na kusafiri hadi kwenye hema ya baba yetu.

MLANGO WA 5

Saria anamnung'unikia Lehi—Wote wawili wanashangilia kurudi kwa wana wao—Wanatoa dhabihu—Mabamba ya shaba nyeupe yana maandiko ya Musa na manabii wengine—Mabamba yanamtambulisha Lehi kuwa uzao wa Yusufu—Lehi anatoa unabii kuhusu uzao wake na kuhifadhiwa kwa mabamba. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na ikawa kwamba baada ya sisi kufika nyikani kwa baba yetu, tazama, alijazwa na shangwe, na pia mama yangu, [a]Saria, alifurahi sana, kwani alikuwa ameomboleza kwa sababu yetu.

2 Kwani alikuwa amedhani kwamba tulikuwa tumeangamia nyikani; na pia alikuwa

31*a* Mos. 9:17; Alma 56:56.
33*a* MWM Kiapo.
34*a* 1 Ne. 2:2; 3:16.
35*a* 1 Ne. 16:7; 2 Ne. 5:5–6. MWM Zoramu, Wazoramu.
37*a* Yos. 9:1–21; Mh. 5:4. MWM Kiapo.

5 1*a* MWM Saria.

amemlalamikia baba yangu, akimwambia kwamba yeye ni mtu wa maono; na kusema: Tazama wewe umetuongoza kutoka nchi yetu ya urithi, na wana wangu hawapo tena, na tunaangamia nyikani.

3 Na kwa lugha ya aina hii mama yangu alimlalamikia baba yangu.

4 Na ikawa kwamba baba yangu akamzungumzia, na kusema: Najua kwamba mimi ni [a]mtu wa maono; kwani kama nisingeona vitu vya Mungu katika [b]maono nisingejua wema wa Mungu, lakini ningekaa huko Yerusalemu, na kuangamia pamoja na ndugu zangu.

5 Lakini tazama, nimepokea uthibitisho wa [a]nchi ya ahadi, vitu ambavyo kwavyo ninafurahia; ndiyo, na [b]ninajua kwamba Bwana atawakomboa wana wangu kutoka mikononi mwa Labani, na kuwaleta hapa kwetu nyikani.

6 Na kwa lugha ya aina hii baba yangu, Lehi, alimfariji mama yangu, Saria, kutuhusu, tulipokuwa tukisafiri kutoka nyikani hadi nchi ya Yerusalemu, kuchukua maandishi ya Wayahudi.

7 Na tulipokuwa tumerudi kwenye hema la baba yangu, tazama shangwe yao ilikuwa tele, na mama yangu akafarijika.

8 Na mama yangu akazungumza, akisema: Sasa najua kwa hakika kwamba Bwana [a]amemwamuru mume wangu kutorokea nyikani; ndiyo, na pia najua kwa hakika kwamba Bwana amewalinda wana wangu, na kuwakomboa kutoka mikononi mwa Labani, na kuwapatia uwezo wa [b]kutimiza kitu ambacho Bwana aliwaamuru. Na hii ndiyo lugha ambayo mama yangu alitumia.

9 Na ikawa kwamba walishangilia sana, na wakamtolea Bwana [a]dhabihu za kuteketezwa kwa moto pamoja na sadaka; na [b]kumshukuru Mungu wa Israeli.

10 Na baada ya kumshukuru Mungu wa Israeli, baba yangu, Lehi, alichukua zile kumbukumbu ambazo zilikuwa zimechorwa kwenye [a]mabamba ya shaba nyeupe, na aliyapekua tangu mwanzo.

11 Na akagundua kwamba yalikuwa na [a]vitabu vitano vya Musa, ambavyo vilieleza historia ya kuumbwa kwa dunia, na pia kwa Adamu na Hawa, ambao ndiyo wazazi wetu wa kwanza;

12 Na pia [a]maandishi ya Wayahudi kutoka mwanzo, hadi mwanzo wa utawala wa Zedekia, mfalme wa Yuda;

13 Na pia unabii wa manabii watakatifu, tangu mwanzo, hadi mwanzoni mwa utawala

4 *a* 1 Ne. 2:11.
b 1 Ne. 1:8–13.
MWM Ono.
5 *a* 1 Ne. 2:20; 18:8, 22–23.
MWM Nchi ya Ahadi.
b MWM Amini, Imani.
8 *a* 1 Ne. 2:2.
b 1 Ne. 3:7.
9 *a* Mos. 2:3; 3 Ne. 9:19–20.
MWM Torati ya Musa.
b MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
10 *a* 1 Ne. 4:24, 38; 13:23.
MWM Mabamba ya Shaba Nyeupe.
11 *a* 1 Ne. 19:23.
MWM Torati.
12 *a* 1 Nya. 9:1.
MWM Maandiko.

wa [a]Zedekia; na pia unabii mwingi ambao ulizungumzwa kutoka kinywa cha [b]Yeremia.

14 Na ikawa kwamba baba yangu, Lehi, pia alipata kwenye [a]mabamba ya shaba nyeupe nasaba ya babu zake; kwa hivyo akajua kwamba yeye ni wa kizazi cha Yusufu; ndiyo, hata yule [b]Yusufu, ambaye alikuwa mwana wa [c]Yakobo, ambaye [d]aliuzwa Misri, na ambaye [e]alihifadhiwa kwa mkono wa Bwana, ili amhifadhi baba yake, Yakobo, na wote wa jamii yake wasiangamie kwa njaa.

15 Na [a]waliongozwa pia kutoka utumwani na kutoka nchi ya Misri, na yule Mungu ambaye alikuwa amewahifadhi.

16 Na hivyo baba yangu, Lehi, aligundua nasaba ya baba zake. Na Labani pia alikuwa kizazi cha [a]Yusufu, ndipo yeye na baba zake wakaweka yale maandishi.

17 Na sasa baba yangu alipoona vitu hivi vyote, alijawa na Roho, na akaanza kutoa unabii kuhusu uzao wake—

18 Kwamba mabamba haya ya shaba nyeupe yanapaswa kupelekwa katika mataifa yote, makabila zote, lugha zote, na watu wote wa uzao wake.

19 Kwa hivyo, alisema kwamba mabamba haya ya shaba nyeupe yasiangamie [a]kamwe; wala yasichakazwe na wakati. Na akatoa unabii wa vitu vingi kuhusu uzao wake.

20 Na ikawa kwamba mpaka hapo mimi na baba yangu tulikuwa tumeweka amri ambazo Bwana alikuwa ametuamuru.

21 Na tulikuwa tumepata yale maandishi ambayo Bwana alikuwa ametuamuru, na kuyachunguza na tukagundua kwamba yalikuwa ya kupendeza; ndiyo, hata yenye [a]thamani kubwa kwetu sisi, kwani tungeweza [b]kuhifadhi amri za Bwana na kuwapa watoto wetu.

22 Kwa hivyo, ilikuwa ni hekima katika Bwana kwamba tuyabebe tulipokuwa, tukisafiri nyikani tukielekea nchi ya ahadi.

MLANGO WA 6

Nefi anaandika kuhusu vitu vya Mungu—Kusudi la Nefi ni kushawishi watu kumjia Mungu wa Ibrahimu ili waokolewe. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na sasa mimi, Nefi, sitaandika nasaba ya baba zangu katika sehemu [a]hii ya maandishi yangu; wala sitaiandika baadaye wakati wowote katika mabamba

13*a* 2 Fal. 24:18; Yer. 37:1.
b Ezra 1:1; Yer. 36:17–32; 1 Ne. 7:14; Hel. 8:20.
14*a* 1 Ne. 3:3, 12. MWM Mabamba ya Shaba Nyeupe.
b 2 Ne. 3:4; Alma 10:3. MWM Yusufu, Mwana wa Yakobo.
c MWM Yakobo, Mwana wa Isaka.
d Mwa. 37:29–36.
e Mwa. 45:4–5.
15*a* Ku. 13:17–18; Amo. 3:1–2; 1 Ne. 17:23–31; M&M 103:16–18; 136:22.
16*a* 1 Ne. 6:2.
19*a* Alma 37:4–5.
21*a* MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
b 2 Ne. 25:26.
6 1*a* 2 Ne. 4:14–15.

haya [b]mabamba ambayo ninaandika; kwani imeandikwa kwenye maandishi ambayo yamewekwa na [c]baba yangu; kwa hivyo, sitaiandika katika mabamba haya.

2 Kwani inanitosha kusema kuwa sisi ni kizazi cha [a]Yusufu.

3 Na sio muhimu kwangu kutoa taarifa kamili ya vitu vya baba yangu, kwani haviwezi kuandikwa kwenye mabamba [a]mabamba haya, kwani nahitaji nafasi ya kuandika vitu vya Mungu.

4 Kwani lengo langu kamili ni [a]kuwashawishi watu [b]waje kwa Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo ili waokolewe.

5 Kwa hivyo, sitaandika vitu vile ambavyo [a]vinafurahisha ulimwengu, bali nitaandika yale ambayo yanamfurahisha Mungu na wale wasio wa ulimwengu.

6 Kwa hivyo, nitatoa amri kwa uzao wangu, kwamba hawataandika vitu visivyo na thamani kwa watoto wa watu kwenye mabamba haya.

MLANGO WA 7

Wana wa Lehi wanarejea Yerusalemu na kumwalika Ishmaeli na jamii yake waungane nao katika safari yao—Lamani na wengine wanaasi—Nefi anawasihi kaka zake wawe na imani katika Bwana—Wanamfunga kwa kamba na kupanga njama za kumwangamiza—Anakombolewa kwa nguvu za imani—Kaka zake wanaomba msamaha—Lehi na kikundi chake wanatoa dhabihu na sadaka za kuteketezwa kwa moto. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na sasa ningetaka mjue, kwamba baada ya baba yangu, Lehi, kumaliza kutoa [a]unabii kuhusu uzao wake, ikawa kwamba Bwana akamzungumzia tena, akisema kuwa haifai yeye, Lehi, kuipeleka jamii yake pekee nyikani; lakini kwamba wanawe [b]waoe [c]mabinti, ili waweze kuendeleza uzao wa Bwana katika nchi ya ahadi.

2 Na ikawa kwamba Bwana [a]akamwamuru kwamba mimi, Nefi, na kaka zangu, turudi tena katika nchi ya Yerusalemu, na tumlete Ishmaeli na jamii yake nyikani.

3 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, pamoja na kaka zangu, [a]tena, tukaenda nyikani na kuelekea Yerusalemu.

4 Na ikawa kwamba tuliingia katika nyumba ya Ishmaeli, na Ishmaeli akakubaliana nasi, hata tukamwelezea maneno ya Bwana.

5 Na ikawa kwamba Bwana aliulainisha moyo wa Ishmaeli, pia na jamii yake, hata

1 *b* 1 Ne. 9:2.
c 1 Ne. 1:16–17; 19:1–6.
2 *a* 1 Ne. 5:14–16.
3 *a* Yak. (KM) 7:27; Yar. 1:2, 14; Omni 1:30.
4 *a* Yn. 20:30–31. Tazama ukurasa wenye jina la Kitabu cha Mormoni.
b 2 Ne. 9:41, 45, 51.
5 *a* 1 The. 2:4; M. ya Morm. 1:4.

7 1 *a* 1 Ne. 5:17–19.
b 1 Ne. 16:7.
c MWM Ndoa, Oa, Olewa.
2 *a* 1 Ne. 16:7–8.
3 *a* 1 Ne. 3:2–3.

wakasafiri pamoja nasi hadi nyikani kwenye hema la Baba yetu.

6 Na ikawa kwamba tulipokuwa tukisafiri nyikani, tazama Lamani na Lemueli, na mabinti wawili wa Ishmaeli, na wale [a]wana wawili wa Ishmaeli na jamii zao, waliasi dhidi yetu; ndiyo, dhidi yangu, Nefi, na Samu, na baba yao, Ishmaeli, na mke wake, na mabinti zake wengine watatu.

7 Na ikawa katika kuasi kwao, walitaka kurejea katika nchi ya Yerusalemu.

8 Na sasa mimi, Nefi, nikiwa [a]nimehuzunishwa na ugumu wa mioyo yao, kwa hivyo nikawazungumzia, nikisema, ndiyo, hata kwa Lamani na Lemueli: Tazama ninyi ndiyo kaka zangu wakubwa, je, kwa nini mna ugumu mioyoni mwenu, na upofu katika akili zenu, hata mnahitaji kwamba mimi mdogo wenu, niwazungumzie, ndiyo, hata kuwa kielelezo kwenu?

9 Je, kwa nini hamjasikiza neno la Bwana?

10 Je, ni vipi [a]mmesahau kwamba mliona malaika wa Bwana?

11 Ndiyo, na ni vipi kwamba mmesahau vitu vikubwa ambavyo Bwana ametutendea, katika [a]kutukomboa kutoka mikononi mwa Labani, na pia kwamba tukaweza kupata yale maandishi?

12 Ndiyo, na ni vipi kwamba mmesahau kuwa Bwana anaweza kufanya [a]vitu vyote kulingana na nia yake, kwa watoto wa watu, ikiwa watatekeleza [b]imani kwake? Kwa hivyo, tuwe waaminifu kwake.

13 Na kama tutakuwa waaminifu kwake, tutapokea [a]nchi ya ahadi; na hapo baadaye mtajua kwamba neno la Bwana litatimia kuhusu [b]kuangamizwa kwa mji wa Yerusalemu; kwani vitu vyote ambavyo Bwana amezungumza kuhusu kuangamizwa kwa Yerusalemu lazima yatimizwe.

14 Kwani tazama, Roho wa Bwana ataacha karibuni kujishughulisha nao; kwani tazama, [a]wamewakataa manabii, na wamemtia [b]Yeremia gerezani. Na wamemtafuta baba yangu kumtoa [c]uhai wake, mpaka wamemfukuza kutoka nchini.

15 Tazama sasa, nawaambia kama ninyi mtarudi Yerusalemu pia nanyi mtaangamia nao. Na sasa, mkiwa na uwezo wa kuchagua, nendeni kwenye nchi, na kumbukeni maneno ambayo nawazungumzia, kwamba kama mtaenda pia mtaangamia; kwani Roho wa Bwana ananishurutisha kuzungumza.

16 Na ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kuwazungumzia kaka zangu maneno haya, walinikasirikia. Na ikawa kwamba

6a 2 Ne. 4:10.
8a Alma 31:2; Musa 7:41.
10a Kum. 4:9; 1 Ne. 3:29; 4:3.
11a 1 Ne. 4.
12a 1 Ne. 17:50; Alma 26:12.
b 1 Ne. 3:7; 15:11.
13a 1 Ne. 2:20. MWM Nchi ya Ahadi.
b 2 Fal. 25:1–21; 2 Ne. 6:8; 25:10; Omni 1:15; Hel. 8:20–21.
14a Eze. 5:6; 1 Ne. 1:18–20; 2:13. MWM Uasi.
b Yer. 37:15–21.
c 1 Ne. 2:1.

walinikamata, kwani tazama, walikuwa na hasira nyingi, na [a]wakanifunga kwa kamba, kwani walitaka kunitoa uhai wangu, kwamba wangeniacha nyikani niliwe na wanyama wa mwituni.

17 Lakini ikawa kwamba nilimwomba Bwana, nikisema: Ewe Bwana, kulingana na imani yangu kwako, unikomboe kutoka mikononi mwa kaka zangu; ndiyo, hata unipatie nguvu ili [a]nizikate kamba ambazo nimefungwa nazo.

18 Na ikawa kwamba baada ya kusema maneno haya, tazama, kamba kwa mikono na miguu yangu zililegezwa, na nikasimama mbele za kaka zangu, na nikawazungumzia tena.

19 Na ikawa kwamba walinikasirikia tena, na wakataka kunishika; lakini tazama, mmoja wa [a]mabinti za Ishmaeli, ndiyo, na mama yake pia, na mmoja wa wana wa Ishmaeli, wakawasihi kaka zangu, hadi wakalainisha mioyo yao; na wakaacha kutaka kujaribu kutoa uhai wangu.

20 Na ikawa kwamba walihuzunishwa, kwa sababu ya uovu wao, hadi wakaniinamia, na kunisihi niwasamehe kitu ambacho walikuwa wametenda dhidi yangu.

21 Na ikawa kwamba [a]niliwasamehe kwa ukweli na moyo wangu wote kwa yote waliyofanya, na nikawahimiza kwamba wamuombe Bwana Mungu wao msamaha. Na ikawa kwamba walitenda hivyo. Na baada ya wao kumaliza kumwomba Bwana, tulisafiri tena tukielekea kwenye hema la baba yetu.

22 Na ikawa kwamba tulifika kwenye hema la baba yetu. Na baada ya mimi na kaka zangu pamoja na nyumba yote ya Ishmaeli kufika kwenye hema la baba yangu, walitoa [a]shukrani kwa Bwana Mungu wao; na wakamtolea [b]dhabihu na sadaka za kuteketezwa kwa moto.

MLANGO WA 8

Lehi anaona ono la mti wa uhai—Anakula matunda yake na kutamani jamii yake pia nao wale—Anaona fimbo ya chuma, na njia nyembamba imesonga, na ukungu wa giza ambao unafunika wanadamu—Saria, Nefi, na Samu wanakula matunda, lakini Lamani na Lemueli wanakataa. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na ikawa kwamba tulikuwa tumekusanya namna zote za mbegu za kila aina, pamoja na nafaka za kila aina, na pia mbegu za kila aina ya matunda.

2 Na ikawa kwamba wakati baba yangu alipoishi nyikani alituzungumzia, akisema: Tazama, [a]nimeota ndoto; au kwa maneno mengine, nimeona [b]ono.

3 Na tazama, kwa sababu ya

16 *a* 1 Ne. 18:11–15.
17 *a* Alma 14:26–28.
19 *a* 1 Ne. 16:7.
21 *a* MWM Samehe.
22 *a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
b 1 Ne. 5:9.
8 2 *a* MWM Ndoto; Ufunuo.
b 1 Ne. 10:17. MWM Ono.

kitu ambacho nilikuwa nimekiona, nina sababu ya kutoa shukrani kwa Bwana kwa sababu ya [a]Nefi na pia ya Samu; nina sababu ya kuamini kwamba wao, na pia wengi wa uzao wao, watakombolewa.

4 Lakini tazama, [a]Lamani na Lemueli, ninaogopa sana kwa sababu yenu; kwani tazama, nilidhania niliona ndotoni mwangu, nyika yenye giza na yenye kuhuzunisha.

5 Na ikawa kwamba niliona mtu, na alikuwa amevaa [a]joho jeupe; na akaja na kusimama mbele yangu.

6 Na ikawa kwamba alinizungumzia, na aliniamuru nimfuate.

7 Na ikawa kwamba nilipokuwa namfuata nilijiona kwamba nilikuwa katika mahali penye giza na ukiwa wa jangwa.

8 Na baada ya kusafiri kwa masaa mengi gizani, nilianza kumwomba Bwana [a]anihurumie, kulingana na wingi wa rehema na fadhili zake.

9 Na ikawa kwamba baada ya mimi kumwomba Bwana, niliona [a]uwanja mkubwa na mpana.

10 Na ikawa kwamba niliona [a]mti, ambao [b]matunda yake yalitamanika kumfurahisha mwanadamu.

11 Na ikawa kwamba nilienda na nikala [a]matunda yake; na nikagundua kwamba yalikuwa matamu, zaidi ya yote ambayo nilikuwa nimeonja. Ndiyo, na nikaona kwamba tunda lake lilikuwa leupe, kushinda [b]weupe wote ambao nilikuwa nimeuona.

12 Na nilipokula tunda lile lilijaza nafsi yangu na [a]shangwe tele; kwa hivyo, nikaanza [b]kutaka jamii yangu na wao pia wale; kwani nilijua kwamba lilikuwa tunda la [c]kupendeza zaidi ya yote.

13 Na nilipotazama hapa na pale, ili pia labda nione jamii yangu, niliona [a]mto wa maji; na ulitiririka, karibu na mti ule ambao nilikuwa nikila matunda yake.

14 Na nikatazama nione ulitoka wapi; na nikaona chimbuko lake mbali kidogo; na kwenye chimbuko nikaona mama yenu Saria, na Samu, na Nefi; na walisimama wakawa kama hawajui wanapoenda.

15 Na ikawa kwamba niliwapungia mkono; na pia kwa sauti kubwa nikawaambia wanikaribie, na wale tunda, ambalo lilikuwa la kupendeza zaidi kuliko tunda lingine.

16 Na ikawa kwamba walinikaribia na kula tunda pia.

17 Na ikawa kwamba nilitaka pia Lamani na Lemueli waje na kula tunda; kwa hivyo, nikatazama kwenye chimbuko la mto, kwamba labda niwaone.

3*a* 1 Ne. 8:14–18.
4*a* 1 Ne. 8:35–36.
5*a* JS—H 1:30–32.
8*a* MWM Rehema, enye Rehema.
9*a* Mt. 13:38.
10*a* Mwa. 2:9; Ufu. 2:7; 22:2; 1 Ne. 11:4, 8–25. MWM Mti wa Uzima.
b Alma 32:41–43.
11*a* Alma 5:34.
b 1 Ne. 11:8.
12*a* MWM Shangwe.
b Alma 36:24.
c 1 Ne. 15:36.
13*a* 1 Ne. 12:16–18; 15:26–29.

18 Na ikawa kwamba niliwaona, lakini [a]hawakunijia na kula tunda.

19 Na nikaona [a]fimbo ya chuma, na ilinyooka kando ya ukingo wa mto, mpaka kwenye mti niliposimama.

20 Na pia nikaona njia nyembamba [a]imesonga, ambayo iliambatana na fimbo ya chuma, hata hadi ambapo nilipokuwa nimesimama kwenye mti; na pia ilielekea kwenye chimbuko la chemchemi, hadi kwenye [b]uwanja mkubwa mpana, kama kwamba ni ulimwengu.

21 Na nikaona umati mkubwa wa watu usio na idadi, wengi wao ambao walikuwa wanasogea mbele, ili wapate kufikia [a]njia ambayo ilielekea kwenye mti ambapo nilikuwa nimesimama.

22 Na ikawa kwamba walifika hapo mbele, na kuipata njia iliyoelekea kwenye mti.

23 Na ikawa kwamba kulitokea [a]ukungu wa giza; ndiyo, hata ukungu mkubwa wa giza, hadi wale ambao walikuwa wametangulia njia walipotea njia, kwamba walizungukazunguka na kupotea.

24 Na ikawa kwamba niliona wengine wakisonga mbele, na wakafika mbele na wakashika mwisho wa fimbo ya chuma; na wakasonga mbele na kupenya ukungu wa giza, wakishikilia fimbo ya chuma, hadi wakafika na kula [a]matunda ya mti.

25 Na baada ya kula matunda ya mti wakatupa macho yao hapa na pale wakawa kama [a]wanaaibika.

26 Na pia nikatupa macho yangu hapa na pale, na nikaona, kwenye ng'ambo nyingine ya mto wa maji, jengo kubwa na [a]pana; na lilikuwa ni kama linaelea hewani, juu zaidi ya ardhi.

27 Na lilikuwa limejaa watu, wazee kwa vijana, wanaume kwa wanawake; na mavazi yao yalikuwa mazuri kupita kiasi; na walikuwa na [a]tabia ya kufanya mzaha na kuwaonyesha kwa vidole vyao wale ambao walikuwa wanakuja na kula matunda.

28 Na baada ya [a]kuonja matunda [b]waliaibika, kwa sababu ya wale waliokuwa wakiwadharau; na [c]wakaingia katika njia zilizokataliwa na wakapotea.

29 Na sasa mimi, Nefi, sizungumzi maneno [a]yote ya baba yangu.

30 Lakini, nikifupisha katika kuandika, tazama, aliona umati mwingine ukisonga mbele; na wakaja na kushika mwisho wa ile fimbo ya chuma; na waka-

18*a* 2 Ne. 5:20–25.
19*a* Zab. 2:9; Ufu. 12:5; TJS Ufu. 19:15 (Kiambatisho); 1 Ne. 8:30; 11:25; 15:23–24.
20*a* Mt. 7:14; 2 Ne. 31:17–20.
b Mt. 13:38.
21*a* MWM Njia.
23*a* 1 Ne. 12:17; 15:24.
24*a* 1 Ne. 8:10–12.
25*a* Rum. 1:16; 2 Tim. 1:8; Alma 46:21; Morm. 8:38.
26*a* 1 Ne. 11:35–36; 12:18.
27*a* MWM Kiburi.
28*a* 2 Pet. 2:19–22.
b Mk. 4:14–20; 8:38; Lk. 8:11–15; Yn. 12:42–43.
c MWM Ukengeufu.
29*a* 1 Ne. 1:16–17.

songa mbele, daima wameshikilia ile [a]fimbo ya chuma, hadi wakafika na kuinama na kula matunda ya ule mti.

31 Na pia akaona [a]umati mwingine ukipapasapapasa wakielekea kwa lile jengo kubwa na pana.

32 Na ikawa kwamba wengi walizama kwenye kilindi cha [a]chemchemi; na wengi wakapotea asipate kuwaona, wakizururazurura katika njia ngeni.

33 Na umati ule ulioingia kwenye lile jengo geni ulikuwa mkubwa. Na baada ya kuingia kwenye lile jengo walitufanyia ishara za [a]madharau kwa vidole vyao mimi na wale ambao walikuwa wakila matunda; lakini hatukuwasikiza.

34 Haya ndiyo maneno ya baba yangu: Kuwa wengi [a]waliowasikiza, walianguka.

35 Na [a]Lamani na Lemueli hawakula lile tunda, alisema baba yangu.

36 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kuzungumza maneno yote ya ndoto yake au ono, ambayo yalikuwa mengi, akatuambia sisi, kwa sababu ya vitu hivi vyote ambavyo alivyoona katika ono, aliwahofia kupita kiasi Lamani na Lemueli; ndiyo, alihofia wasije wakatupiliwa mbali kutoka kwenye uwepo wa Bwana.

37 Na aliwasihi kwa huruma zote za [a]mzazi mwenye upendo, kwamba wasikilize maneno yake, na pengine Bwana angewarehemu, na asiwatupilie mbali; ndiyo, baba yangu aliwahubiria.

38 Na baada ya kuwahubiria, na pia kuwatolea unabii wa vitu vingi, aliwaamuru kuweka amri za Bwana; na akakoma kuwazungumzia.

MLANGO WA 9

Nefi anaandika aina mbili za historia—Kila kimoja kinaitwa mabamba ya Nefi—Mabamba makubwa yanayo maandishi ya historia ya kiulimwengu; mabamba ndogo yanayo asili ya vitu vitakatifu. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na baba yangu aliona vitu hivi vyote, na kusikia, na kuvizungumza, alipokuwa kwenye hema, katika [a]bonde la Lemueli, na pia vitu vingi zaidi, ambavyo haviwezi kuandikwa kwenye mabamba haya.

2 Na sasa, kama nilivyosema kuhusu mabamba haya, tazama sio yale mabamba ambayo nimeyaandika historia kamili ya watu wangu; kwani [a]mabamba ambayo nimeandika historia kamili ya watu wangu nimeyaita kwa jina la Nefi; kwa hivyo, yanaitwa mabamba ya Nefi, kufuatana na jina langu; na pia mabamba haya yanaitwa mabamba ya Nefi.

30 *a* 1 Ne. 15:23–24.
31 *a* Mt. 7:13.
32 *a* 1 Ne. 15:26–29.
33 *a* MWM Mateso, Tesa.
34 *a* Ku. 23:2.
35 *a* 1 Ne. 8:17–18; 2 Ne. 5:19–24.
37 *a* MWM Familia; Wazazi.
9 1 *a* 1 Ne. 2:4–6, 8, 14–15; 16:6.
2 *a* 1 Ne. 19:2, 4; Yak. (KM) 3:13–14; M. ya Morm. 1:2–11; M&M 10:38–40.
MWM Mabamba.

3 Walakini, nimepokea amri ya Bwana kwamba niyatengeneze mabamba haya kwa [a]kusudi muhimu kwamba kuweko na historia iliyochorwa ya [b]huduma ya watu wangu.

4 Kwenye yale mabamba mengine ichorwe historia ya utawala wa wafalme, na vita na mabishano ya watu wangu; kwa hivyo mabamba haya sehemu kubwa ni ya huduma; na yale [a]mabamba mengine sehemu kubwa ni ya utawala wa wafalme na vita na pia mabishano ya watu wangu.

5 Kwa hivyo, Bwana ameniamuru kuandika mabamba haya kwa kusudi lake lenye [a]hekima, ambalo kusudi mimi silijui.

6 Lakini Bwana [a]anavijua vitu vyote kuanzia mwanzoni; kwa hivyo, anatayarisha njia ya kutimiza kazi zake zote miongoni mwa watoto wa watu; kwani tazama, ana [b]uwezo wote wa kutimiza maneno yake yote. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.

MLANGO WA 10

Lehi abashiri kwamba Wayahudi watatekwa mateka na Wababilonia—Anasimulia kuja kwa Masiya, Mwokozi, na Mkombozi, miongoni mwa Wayahudi—Lehi pia anasimulia kuhusu kuja kwa yule ataakaye mbatiza Mwanakondoo wa Mungu—Lehi anasimulia kifo na ufufuko wa Masiya—Analinganisha kutawanyika na kukusanyika kwa Israeli na mzeituni—Nefi anazungumza kuhusu Mwana wa Mungu, kipawa cha Roho Mtakatifu, na haja ya haki. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na sasa mimi, Nefi, ninaendelea kuandika historia kuhusu matendo yangu kwenye [a]mabamba haya, pamoja na utawala na huduma yangu; kwa hivyo, ili niendelee na historia yangu, lazima nizungumze machache kuhusu vitu vya baba yangu, na pia kaka zangu.

2 Kwani tazama, ikawa kwamba baada ya baba yangu kumaliza kuzungumza maneno ya [a]ndoto yake, na pia kuwasihi waendelee kwenye jitihada, aliwazungumuzia kuhusu Wayahudi—

3 Kwamba baada yao kuangamizwa, hata ule mji mkuu [a]Yerusalemu, na wengi [b]kupelekwa uhamishoni [c]Babilonia, kulingana na nyakati za Bwana, [d]watarejea tena, ndiyo, hata kurejeshwa kutoka uhamishoni; na baada ya kutolewa uhamishoni watamiliki tena nchi yao ya urithi.

4 Ndiyo, hata baada ya miaka [a]mia sita tangu baba yangu atoke

3*a* M&M 3:19.
b 1 Ne. 6:3.
4*a* Yak. (KM) 1:2–4; M. ya Morm. 1:10.
5*a* 1 Ne. 19:3; M. ya Morm. 1:7; Alma 37:2, 12, 14.
6*a* 2 Ne. 9:20; M&M 38:2; Musa 1:6, 35.
MWM Kujua yote.
b Mt. 28:18.
10 1*a* 1 Ne. 9:1–5; 19:1–6; Yak. (KM) 1:1–4.
2*a* 1 Ne. 8.
3*a* Esta 2:6; 2 Ne. 6:8; Hel. 8:20–21.
b 587 K.K.; tazama Wendo katika kiambatisho.
2 Ne. 25:10.
c Eze. 24:2; 1 Ne. 1:13; Omni 1:15.
d Yer. 29:10; 2 Ne. 6:8–9.
4*a* 1 Ne. 19:8; 2 Ne. 25:19; 3 Ne. 1:1.

Yerusalemu, Bwana Mungu atainua [b]nabii miongoni mwa Wayahudi—hata [c]Masiya, au, kwa maneno mengine, Mwokozi wa ulimwengu.

5 Na pia akazungumzia kuhusu manabii, jinsi wengi wao walivyokuwa [a]wameshuhudia vitu hivi, kuhusu Masiya ambaye alikuwa amemzungumzia, au huyu Mkombozi wa ulimwengu.

6 Kwa hivyo, wanadamu wote walikuwa wamepotea na wako katika hali ya [a]kuanguka, na watakuwa hivyo hata milele wasipomtegemea huyu Mkombozi.

7 Na alizungumza pia kuhusu [a]nabii ambaye angemtangulia Masiya, ili kumtayarishia Bwana njia yake—

8 Ndiyo, hata ataondoka mbele na kutangaza nyikani: [a]Itayarisheni njia ya Bwana, na yanyoosheni mapito yake; kwani miongoni mwenu amesimama yeye msiyemjua; na yeye ni mkuu kunishinda, ambaye mimi sistahili kuilegeza gidamu ya kiatu chake. Na baba yangu alizungumza mengi kuhusu kitu hiki.

9 Na baba yangu akasema atabatiza katika [a]Bethabara, ng'ambo ya Yordani; na pia akasema kuwa [b]atabatiza kwa maji; hata kwamba atambatiza Masiya kwa maji.

10 Na baada ya kumbatiza Masiya kwa maji, itambidi kuona na kushuhudia kwamba alimbatiza [a]Mwanakondoo wa Mungu, ambaye ataondoa dhambi za ulimwengu.

11 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kuzungumza maneno haya aliwazungumzia kaka zangu kuhusu injili ambayo itahubiriwa miongoni mwa Wayahudi, na pia kuhusu [a]kufifia kwa Wayahudi katika [b]kutoamini. Na baada ya [c]kumuua Masiya, ajaye, na baada ya kuuwawa [d]atafufuka kutoka kwa wafu, na ajidhihirishe, kupitia nguvu za [e]Roho Mtakatifu, kwa Wayunani.

12 Ndiyo, baba yangu hata alizungumza mengi kuhusu Wayunani, na pia kuhusu nyumba ya Israeli, kwamba watalinganishwa na [a]mzeituni, ambao matawi yake yatakatwa na [b]kutawanywa kote kote usoni mwa dunia.

13 Kwa hivyo, akasema ni lazima sote tuongozwe pamoja hadi kwenye [a]nchi ya ahadi, ili maneno ya Bwana yatimizwe,

4 *b* 1 Ne. 22:20–21.
c MWM Masiya.
5 *a* Yak. (KM) 7:11; Mos. 13:33; Hel. 8:19–24; 3 Ne. 20:23–24.
6 *a* MWM Anguko la Adamu na Hawa.
7 *a* 1 Ne. 11:27; 2 Ne. 31:4.
8 *a* Isa. 40:3; Mt. 3:1–3.
9 *a* Yn. 1:28.
b MWM Yohana Mbatizaji.
10 *a* MWM Mwanakondoo wa Mungu.
11 *a* Yak. (KM) 4:14–18.
b Morm. 5:14.
c MWM Kusulubiwa; Yesu Kristo.
d MWM Ufufuko.
e MWM Roho Mtakatifu.
12 *a* Mwa. 49:22–26; 1 Ne. 15:12; 2 Ne. 3:4–5; Yak. (KM) 5; 6:1–7. MWM Mzeituni; Shamba la mizabibu la Bwana.
b 1 Ne. 22:3–8. MWM Israeli—Kutawanyika kwa Israeli.
13 *a* 1 Ne. 2:20. MWM Nchi ya Ahadi.

kuwa tutawanywe kote usoni mwa dunia.

14 Na baada ya nyumba ya Israeli kutawanyika [a]watakusanyika tena pamoja; au, kwa usemi mwingine, baada ya [b]Wayunani kupokea utimilifu wa Injili, matawi ya asili ya [c]mzeituni, au mabaki ya nyumba ya Israeli, yatapandikizwa, au kumfahamu Masiya wa ukweli, Bwana wao na Mkombozi wao.

15 Na baba yangu alitumia maneno haya kwa kuwatolea kaka zangu unabii, na kuwazungumzia na pia vitu vingi mno ambavyo siandiki kwenye kitabu hiki; kwani nimeandika mengi yaliyonipasa kwa kile kitabu changu [a]kingine.

16 Na vitu hivi vyote, ambavyo nimezungumza, vilifanyika wakati baba yangu akiishi kwenye hema, katika bonde la Lemueli.

17 Na ikawa kwamba, baada ya mimi, Nefi nikiwa nimesikia [a]maneno yote ya baba yangu, kuhusu yale mambo aliyokuwa ameyaona katika [b]ono, na pia mambo yale aliyozungumza kwa nguvu za Roho Mtakatifu, nguvu alizopokea kwa imani katika Mwana wa Mungu—na Mwana wa Mungu alikuwa ndiye [c]Masiya ajaye—mimi, Nefi, nikatamani pia nipate kuona, na kusikia, na kujua juu ya mambo haya, kwa nguvu za [d]Roho Mtakatifu, ambayo ni karama ya Mungu kwa wote wale ambao humtafuta kwa [e]bidii, sio tu katika nyakati [f]zilizopita, lakini pia katika nyakati ambapo atajionyesha mwenyewe kwa watoto wa watu.

18 Kwani yeye ni [a]yule yule jana, leo, na milele; na njia imetayarishiwa wanadamu wote tangu msingi wa ulimwengu, ikiwa itakuwa kwamba watatubu na kuja kwake.

19 Kwani atafutaye kwa bidii atapata; na watafunguliwa [a]siri za Mungu, kwa nguvu ya [b]Roho Mtakatifu, kama ilivyokuwa katika nyakati hizi na nyakati za kale, na vile vile hizo nyakati za kale, na pia nyakati zijazo; kwa hivyo, [c]mpangilio wa Bwana ni mpangilio imara milele.

20 Kwa hivyo kumbuka, Ewe mwanadamu, [a]utahukumiwa kwa yale yote utendayo.

21 Kwa hivyo, kama uliteua kutenda maovu katika nyakati za [a]majaribio yako, basi utapatwa [b]mchafu mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu; na hakuna kitu kichafu chaweza kuishi na Mungu; kwa hivyo, lazima utupiliwe mbali milele.

14 *a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b 1 Ne. 13:42; M&M 14:10.
c Yak. (KM) 5:8, 52, 54, 60, 68.
15 *a* 1 Ne. 1:16–17.
17 *a* Eno. 1:3; Alma 36:17.
b 1 Ne. 8:2.
c MWM Masiya.
d MWM Roho Mtakatifu.
e Moro. 10:4–5, 7, 19.
f M&M 20:26.
18 *a* Ebr. 13:8; Morm. 9:9; M&M 20:12.
MWM Mungu, Uungu.
19 *a* MWM Siri za Mungu.
b MWM Roho Mtakatifu.
c Alma 7:20; M&M 3:2; 35:1.
20 *a* Mh. 12:14; 2 Ne. 9:46.
MWM Hukumu ya mwisho.
21 *a* Alma 34:32–35.
b 1 Kor. 6:9–10; 3 Ne. 27:19; M&M 76:50–62; Musa 6:57.

22 Na Roho Mtakatifu ananipatia mamlaka kuzungumza vitu hivi, na nisiyazuie.

MLANGO WA 11

Nefi anaona Roho wa Bwana na anaonyeshwa kwa ono mti wa uzima—Anamuona mama wa Mwana wa Mungu na kufahamu kuhusu ufadhili wa Mungu—Anaona ubatizo, huduma, na kusulibiwa kwa Mwanakondoo wa Mungu—Pia anaona mwito na huduma ya Mitume Kumi na Wawili wa Mwanakondoo. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Kwani ikawa baada ya kutamani kujua vitu ambavyo baba yangu aliona, na nikiamini kwamba Bwana anaweza kunijulisha haya kwangu, nikiwa nimekaa [a]nikiwaza moyoni mwangu [b]nilinyakuliwa na Roho wa Bwana, ndiyo, hadi kwenye [c]mlima mrefu zaidi, ambao sijawahi kuona hapo awali kamwe, na ambao juu yake sijawahi kukanyagisha mguu wangu kamwe hapo awali.

2 Na Roho akaniambia: Tazama, ni nini unachotamani?

3 Na nilisema: Natamani kuona vitu ambavyo baba yangu [a]aliona.

4 Na Roho akaniambia: Unaamini kwamba baba yako aliuona [a]mti ambao ameuzungumzia?

5 Na nikasema: Ndiyo, wewe unajua kwamba [a]ninaamini maneno yote ya baba yangu.

6 Na baada ya mimi kuzungumza maneno haya, Roho akapaza sauti, na kusema: Hosana kwa Bwana, Mungu aliye juu sana; kwani yeye ndiye Mungu juu ya [a]ardhi yote, ndiyo, hata juu ya yote. Na umebarikiwa ewe, Nefi, kwa sababu [b]unamwamini Mwana wa Mungu aliye juu sana; kwa hivyo, wewe utaona vitu ulivyotamani.

7 Na tazama utapewa kitu hiki kama [a]ishara, kwamba baada ya kuona mti ambao ulizaa tunda ambalo baba yako alionja, wewe utaona pia mtu akiteremka kutoka mbinguni, na wewe utashuhudia; na baada ya kumwona wewe [b]utashuhudia kwamba yeye ni Mwana wa Mungu.

8 Na ikawa kwamba Roho akaniambia: Tazama! Na nikatazama na kuona [a]mti; na ulikuwa kama ule mti ambao baba yangu aliuona; na urembo wake ulikuwa hauna kipimo, ndiyo, zaidi ya urembo wote; na [b]weupe wake ulizidi weupe wa theluji ivumayo.

9 Na ikawa baada ya kuona huu mti, nikamwambia Roho: Nimeona kuwa umenionyesha mti [a]ulioadimika zaidi ya yote.

11 1*a* M&M 76:19. MWM Tafakari.
b 2 Kor. 12:1–4; Ufu. 21:10; 2 Ne. 4:25; Musa 1:1.
c Kum. 10:1; Eth. 3:1.
3*a* 1 Ne. 8:2–34.
4*a* 1 Ne. 8:10–12; 15:21–22.
5*a* 1 Ne. 2:16.
6*a* Ku. 9:29; 2 Ne. 29:7; 3 Ne. 11:14; Musa 6:44.
b MWM Amini, Imani.
7*a* MWM Ishara.
b MWM Ushuhuda.
8*a* 1 Ne. 8:10.
b 1 Ne. 8:11.
9*a* 1 Ne. 11:22–25.

10 Na akaniambia: Nini unachotamani?

11 Na nikamwambia: Kufahamu [a]maana yake—kwani nilimzungumzia kama mwanadamu; kwani niliona kuwa alikuwa kwa [b]mfano wa mwanadamu; walakini, nilijua kwamba ni Roho wa Bwana; na akanizungumzia kama mwanadamu anavyozungumzia na mwingine.

12 Na ikawa kwamba akaniambia: Tazama! Na nikatazama ili nimwone, na sikumwona; kwani alikuwa ameenda kutoka machoni mwangu.

13 Na ikawa kwamba nilitazama na nikaona mji mkuu wa Yerusalemu, na pia miji mingine. Na nikaona mji wa [a]Nazareti; na katika mji wa Nazareti nikamwona [b]bikira, na alikuwa mrembo na mweupe.

14 Na ikawa kwamba niliona [a]mbingu zikifunguka; na malaika akateremka na kusimama mbele yangu; na akaniambia: nini unachokiona, Nefi?

15 Na nikamwambia: Ni bikira, ambaye ni mrembo na mtakatifu zaidi ya bikira wengine wote.

16 Na akaniambia: Je wajua ufadhili wa Mungu?

17 Na nikamwambia: Najua kwamba anawapenda watoto wake; walakini, sijui maana ya vitu vyote.

18 Na akaniambia: Tazama, [a]bikira unayemwona ni [b]mama wa Mwana wa Mungu, katika kimwili.

19 Na ikawa kwamba niliona alinyakuliwa na Roho; na baada ya kunyakuliwa na [a]Roho kwa muda, malaika akanizungumizia, akisema: Tazama!

20 Na nikatazama na kumwona yule bikira tena, akimbeba [a]mtoto mikononi mwake.

21 Na malaika akaniambia: Tazama [a]Mwanakondoo wa Mungu, ndiyo, hata [b]Mwana wa [c]Baba wa Milele! Je, unajua maana ya ule [d]mti ambao baba yako aliuona?

22 Na nikamjibu, nikasema: Ndiyo, ni [a]upendo wa Mungu, ambao umejimimina mioyoni mwa watoto wa watu, kwa hivyo, ni wa kupendeza zaidi ya vitu vyote.

23 Na akanizungumzia, na kusema: Ndiyo, na inafurahisha moyo kwa [a]shangwe.

24 Na baada ya kusema maneno haya, akaniambia: Tazama! Na nikatazama, na nikamwona Mwana wa Mungu [a]akienda miongoni mwa watoto wa watu; na nikawaona wengi wakiinama mbele ya miguu yake na kumuabudu.

---

11 *a* Mwa. 40:8.
b Eth. 3:15–16.
13 *a* Mt. 2:23.
b Lk. 1:26–27; Alma 7:10. MWM Maria, Mama wa Yesu.
14 *a* Eze. 1:1; 1 Ne. 1:8.
18 *a* Isa. 7:14; Lk. 1:34–35.
b Mos. 3:8.
19 *a* Mt. 1:20.
20 *a* Lk. 2:16.
21 *a* MWM Mwanakondoo wa Mungu.
b MWM Yesu Kristo.
c MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.
d 1 Ne. 8:10; Alma 5:62. MWM Mti wa Uzima.
22 *a* MWM Upendo.
23 *a* MWM Shangwe.
24 *a* Lk. 4:14–21.

25 Na ikawa kwamba niliona ile [a]fimbo ya chuma, ambayo baba yangu aliiona, ilikuwa neno la Mungu, na ilielekea hadi kwenye chemchemi ya [b]maji ya uhai, au kwenye [c]mti wa uzima; maji ambayo ni kielelezo cha upendo wa Mungu; na pia nikaona kwamba ule mti wa uzima ulikuwa pia kielelezo cha upendo wa Mungu.

26 Na malaika akaniambia tena: Angalia na uone [a]ufadhili wa Mungu!

27 Na nikatazama na [a]kuona Mkombozi wa ulimwengu, ambaye baba yangu alikuwa amenena kumhusu; na pia nikaona [b]nabii atakayemtayarishia njia mbele yake. Na Mwanakondoo wa Mungu akamwendea na [c]akabatizwa naye; na baada ya kubatizwa, nikaona mbingu zikifunguka, na Roho Mtakatifu akishuka kutoka mbinguni na kutua juu yake kwa mfano wa [d]njiwa.

28 Na nikaona kwamba alienda na kuwahudumia watu, kwa [a]uwezo na utukufu mkuu; na umati ukakusanyika kumsikiliza; na nikaona kwamba walimfukuza kutoka miongoni mwao.

29 Na pia nikaona wengine [a]kumi na wawili wakimfuata. Na ikawa kwamba walichukuliwa na Roho kutoka machoni mwangu, na sikuwaona.

30 Na ikawa kwamba malaika akanizungumzia tena, akisema: Angalia! Na nikaangalia, na kuona mbingu zikifunguka tena, na nikaona [a]malaika wakiwashukia watoto wa watu; na kuwahudumia.

31 Na akanizungumzia tena, akasema: Angalia! Na nikaangalia, na nikamwona Mwanakondoo wa Mungu akienda miongoni mwa watoto wa watu. Na nikaona umati wa watu waliokuwa wagonjwa, na ambao walikuwa wakiugua kutokana na aina zote za magonjwa, pamoja na [a]ibilisi na [b]pepo wachafu; na malaika akazungumza na kunionyesha hivi vitu vyote. Na [c]wakaponywa kwa nguvu za Mwanakondoo wa Mungu; na ibilisi pamoja na pepo wachafu wakafukuzwa.

32 Na ikawa kwamba malaika akanizungumzia tena, akisema: Angalia! Na nikaangalia na nikamwona Mwanakondoo wa Mungu, kwamba alikamatwa na watu; ndiyo, Mwana wa Mungu asiye na mwisho [a]alihukumiwa na ulimwengu; na niliona na kuyashuhudia.

33 Na mimi, Nefi, nikaona kwamba aliinuliwa juu ya

25*a* 1 Ne. 8:19.
b мwм Maji ya Uzima.
c Mwa. 2:9; Alma 32:40–41; Musa 4:28, 31.
26*a* 1 Ne. 11:16–33.
27*a* 2 Ne. 25:13.
b Mt. 11:10; 1 Ne. 10:7–10; 2 Ne. 31:4.
c мwм Batiza, Ubatizo.
d мwм Njiwa, Ishara ya.
28*a* M&M 138:25–26.
29*a* мwм Mtume.
30*a* мwм Malaika.
31*a* Mk. 5:15–20; Mos. 3:5–7.
мwм Ibilisi.
b мwм Roho—Pepo wachafu.
c мwм Ponya, Uponyaji.
32*a* Mk. 15:17–20.

[a]msalaba na [b]kuuawa kwa dhambi za ulimwengu.

34 Na baada ya yeye kusulubiwa nikaona umati wa dunia, ukiwa umekusanyika pamoja kupigana dhidi ya mitume wa Mwanakondoo; kwani hivi ndivyo wale kumi na wawili waliitwa na malaika wa Bwana.

35 Na umati wa dunia ulikusanyika pamoja; na nikaona kwamba walikuwa kwenye [a]jengo kubwa na pana, kama jengo lile baba yangu alililoliona. Na malaika wa Bwana akanizungumzia tena, akisema: Tazama ulimwengu na hekima yake; ndiyo, tazama nyumba ya Israeli imekusanyika pamoja kupinga mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo.

36 Na ikawa kwamba niliona na ninashuhudia, kwamba lile jengo kuu na pana lilikuwa ni [a]kiburi cha ulimwengu; na lilianguka, na muanguko wake ulikuwa mkuu zaidi. Na malaika wa Bwana akanizungumizia tena, akisema: Hivyo ndivyo mataifa yote, makabila yote, lugha zote, na watu wote, ambao wanawapinga wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo wataangamizwa.

MLANGO WA 12

Nefi anaona katika ono nchi ya ahadi; haki, uovu, na uangamizo wa wenyeji wake; kuja kwa Mwanakondoo wa Mungu miongoni mwao; jinsi wale Wanafunzi Kumi na Wawili pamoja na wale Mitume Kumi na Wawili watahukumu Israeli; na hali ya machukizo na uchafu ya wale ambao wanafifia katika kutoamini. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na ikawa kwamba malaika akaniambia: Angalia, na uone uzao wako, na pia uzao wa kaka zako. Na nikaangalia na kuona [a]nchi ya ahadi; na nikaona vikundi vya watu, ndiyo, hata hesabu yao ilikuwa nyingi kama mchanga wa bahari.

2 Na ikawa kwamba niliona vikundi vimekusanyika pamoja kupigana, moja dhidi ya mwingine; na nikaona [a]vita, na uvumi wa vita, na mauaji makuu kwa upanga miongoni mwa watu wangu.

3 Na ikawa kwamba niliona vizazi vingi vikipita, baada ya vita vya namna hii na mabishano katika nchi; na nikaona miji mingi, ndiyo, hata sikuihesabu.

4 Na ikawa kwamba niliona [a]ukungu [b]mweusi usoni mwa nchi ya ahadi; na nikaona umeme, na nikasikia radi, na mitetemeko ya ardhi, na aina zote za misukosuko na makelele; na nikaona ardhi, na miamba, kwamba ilipasuka; na nikaona milima ikivunjika vipande vipande; na nikaona tambarare za ardhi, kwamba zilipasuka; na

33*a* Yn. 19:16–19; Mos. 3:9–10; 3 Ne. 27:14. MWM Msalaba.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
35*a* 1 Ne. 8:26; 12:18.
36*a* MWM Kiburi.
12 1*a* MWM Nchi ya Ahadi.
2*a* Eno. 1:24; Morm. 8:7–8. MWM Vita.
4*a* Hel. 14:20–28.
b 1 Ne. 19:10.

nikaona miji mingi [c]imezama; na nikaona mingi iliyochomwa kwa moto; na nikaona mingi iliyoanguka chini, kwa sababu ya ile mitetemeko.

5 Na ikawa baada ya kuona vitu hivi, nikaona ule [a]ukungu wa giza, ukitoweka kutoka usoni mwa ulimwengu; na tazama, nikaona makundi ya wale ambao hawakuanguka kwa sababu ya hukumu kuu ya kuhofisha kwa Bwana.

6 Na nikaona mbingu zikifunguka, na [a]Mwanakondoo wa Mungu akiteremka kutoka mbinguni; na akashuka chini na akajionyesha kwao.

7 Na pia niliona na ninashuhudia kwamba Roho Mtakatifu aliwashukia wengine [a]kumi na wawili; na walichaguliwa na kuteuliwa, na Mungu.

8 Na malaika akanizungumzia, na kusema: Tazama wale wanafunzi kumi na wawili wa Mwanakondoo, ambao wameteuliwa kuhudumia uzao wako.

9 Na akaniambia: Je, unawakumbuka wale [a]mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo? Tazama ni wao [b]watakaohukumu yale makabila kumi na mawili ya Israeli; kwa hivyo, wale wahudumu kumi na wawili wa uzao wako watahukumiwa na wao; kwani ninyi ni wa nyumba ya Israeli.

10 Na hawa [a]wahudumu kumi na wawili uwaonao watahukumu uzao wako. Na, tazama, wao ni watakatifu milele; kwa sababu ya imani yao katika Mwanakondoo wa Mungu [b]mavazi yao yanafanywa kuwa meupe kwa damu yake.

11 Na malaika akaniambia: Angalia! Na nikaangalia, na kuona vizazi [a]vitatu vikiishi kwa haki; na mavazi yao yalikuwa meupe kama ya Mwanakondoo wa Mungu. Na malaika akaniambia: Hawa wamefanywa kuwa weupe kwa damu ya Mwanakondoo, kwa sababu ya imani yao kwake.

12 Na mimi, Nefi, pia nikaona wengi katika kizazi cha [a]nne wakiishi katika haki.

13 Na ikawa kwamba niliona vikundi vya dunia vimekusanyika pamoja.

14 Na malaika akaniambia: Tazama uzao wako, na pia uzao wa kaka zako.

15 Na ikawa kwamba niliangalia na kuona watu wa uzao wangu wamekusanyika pamoja katika vikundi [a]kupigana na uzao wa kaka zangu; na walikusanyika pamoja wapigane vita.

16 Na malaika akanizungumzia, akisema: Tazama chemchemi ya maji [a]machafu ambayo baba yako aliiona; ndiyo, hata

4 *c* 3 Ne. 8:14.
5 *a* 3 Ne. 8:20; 10:9.
6 *a* 2 Ne. 26:1, 9; 3 Ne. 11:3–17.
7 *a* 3 Ne. 12:1; 19:12–13.
9 *a* Lk. 6:13.
b Mt. 19:28; M&M 29:12.
MWM Hukumu ya mwisho.
10 *a* 3 Ne. 27:27; Morm. 3:18–19.
b Ufu. 7:14; Alma 5:21–27; 13:11–13; 3 Ne. 27:19–20.
11 *a* 2 Ne. 26:9–10; 3 Ne. 27:30–32.
12 *a* Alma 45:10–12; Hel. 13:5, 9–10; 3 Ne. 27:32; 4 Ne. 1:14–27.
15 *a* Morm. 6.
16 *a* MWM Chafu, Uchafu.

[b]mto ambao aliuzungumzia; na kilindi chake ni kilindi cha [c]jehanamu.

17 Na [a]ukungu wa giza ni majaribio ya ibilisi, [b]yanayopofusha macho, na ambayo yanashupaza mioyo ya watoto wa watu, na kuwaelekeza kwenye [c]njia pana, ili waangamie na kupotea.

18 Na [a]jengo kubwa na pana, ambalo baba yako aliliona, ni [b]mawazo yasiyofaa na [c]kiburi cha watoto wa watu. Na [d]shimo kubwa la kuhofisha linawagawanya; ndiyo, hata neno la [e]haki la Mungu wa Milele, na Masiya ambaye ni Mwanakondoo wa Mungu, ambaye anashuhudiwa na Roho Mtakatifu, tangu mwanzo wa ulimwengu hadi sasa, na tangu sasa hadi milele.

19 Na wakati malaika alipokuwa akisema maneno haya, nikatazama na kuona kwamba uzao wa kaka zangu walichokozana na uzao wangu, kulingana na maneno ya malaika; na kwa sababu ya kiburi cha uzao wangu, na [a]majaribio ya ibilisi, nikaona kwamba uzao wa kaka zangu [b]waliwashinda watu wa uzao wangu.

20 Na ikawa kwamba nilitazama, na kuona kwamba watu wa uzao wa kaka zangu waliwashinda uzao wangu; na wakendelea mbele katika vikundi kwenye uso wa nchi.

21 Na nikawaona wamekusanyika pamoja katika vikundi; na nikaona [a]vita na uvumi wa vita miongoni mwao; na nikaona vizazi vingi vikiishi kwenye vita na uvumi wa vita.

22 Na malaika akaniambia: Tazama hawa [a]watafifia katika kutoamini.

23 Na ikawa kwamba niliona, baada ya wao kufifia katika kutoamini wakawa watu wa [a]giza, wenye makuruhu, wenye [b]uchafu, waliojaa [c]uzembe na namna zote za machukizo.

MLANGO WA 13

Nefi anaona katika ono kanisa la ibilisi limeanzishwa miongoni mwa wayunani, uvumbuzi na ukoloni katika Marekani, kupotea kwa sehemu nyingi zilizo wazi na za thamani za Biblia, kama matokeo yake hali ya ukengeufu wa myunani, urejesho wa injili, kutokea kwa maandiko ya siku za mwisho, na ujenzi wa Sayuni. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na ikawa kwamba malaika akanizungumzia, akisema: Angalia! Na nikaangalia na kuona mataifa mengi na falme nyingi.

2 Na malaika akaniambia:

16 *b* 1 Ne. 8:13; 15:26–29.
c MWM Jehanamu.
17 *a* 1 Ne. 8:23; 15:24; M&M 10:20–32.
b MWM Ukengeufu.
c Mt. 7:13–14.
18 *a* 1 Ne. 8:26; 11:35–36.
b Yer. 7:24.
c MWM Kiburi.
d Lk. 16:26; 1 Ne. 15:28–30.
e MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
19 *a* MWM Jaribu, Majaribu.
b Yar. 1:10; M. ya Morm. 1:1–2.
21 *a* Morm. 8:8; Moro. 1:2.
MWM Vita.
22 *a* 1 Ne. 15:13; 2 Ne. 26:15.
23 *a* 2 Ne. 26:33.
b 2 Ne. 5:20–25.
c MWM Mvivu, Uvivu.

Nini unachoona? Na nikasema: Naona mataifa mengi na falme nyingi.

3 Na akaniambia: Haya ni mataifa na falme za Wayunani.

4 Na ikawa kwamba niliona miongoni mwa mataifa ya [a]Wayunani mwanzo wa [b]kanisa kuu.

5 Na malaika akaniambia: Tazama mwanzo wa kanisa ambalo lina machukizo mengi zaidi ya makanisa yote mengine, ambalo [a]linawaua watakatifu wa Mungu, ndiyo, na kuwatesa na kuwafunga, na kuwatia [b]nira ya chuma, na kuwapeleka utumwani.

6 Na ikawa kwamba niliona hili kanisa [a]kuu la machukizo; na nikaona [b]ibilisi, kwamba ndiye alikuwa mwanzilishi wake.

7 Na pia nikaona [a]dhahabu, na fedha, na hariri, na nguo za rangi nyekundu, na kitani nzuri, na kila aina ya nguo ya thamani; na nikaona makahaba wengi.

8 Na malaika akanizungumzia, akisema: Tazama, dhahabu, na fedha, na hariri, na nguo za rangi nyekundu, na kitani nzuri, na nguo ya thamani, na makahaba, ni [a]tamaa za kanisa hili kuu la machukizo.

9 Na pia kwa sababu ya sifa za ulimwengu [a]wanawaua watakatifu wa Mungu, na kuwapeleka utumwani.

10 Na ikawa kwamba niliangalia na kuona maji mengi; na yaliwagawanya Wayunani kutoka kwa uzao wa kaka zangu.

11 Na ikawa kwamba malaika akaniambia: Tazama ghadhabu ya Mungu iko juu ya uzao wa kaka zako.

12 Na nikaangalia na kuona mtu miongoni mwa Wayunani, ambaye alitenganishwa kutokana na uzao wa kaka zangu na yale maji mengi; na nikaona [a]Roho ya Mungu, kwamba ilishuka na kumshawishi mtu huyo; na akasafiri kwa yale maji mengi, hadi akaufikia uzao wa kaka zangu, kwenye nchi ya ahadi.

13 Na ikawa kwamba niliona Roho ya Mungu, kwamba iliwashawishi Wayunani wengine, na walitoka utumwani, na kusafiri kwenye maji mengi.

14 Na ikawa kwamba niliona [a]vikundi vingi vya Wayunani katika [b]nchi ya ahadi; na nikaona ghadhabu ya Mungu, kwamba ilikuwa juu ya uzao wa kaka zangu; na [c]wakatawanywa na Wayunani na kupigwa.

15 Na nikaona Roho wa Bwana, kwamba ilikuwa juu ya Wayunani, na wakafanikiwa na kupata [a]nchi kwa urithi wao; na nikaona kwamba walikuwa

13 4*a* MWM Wayunani.
b 1 Ne. 13:26, 34; 14:3, 9–17.
5*a* Ufu. 17:3–6; 1 Ne. 14:13.
b Yer. 28:10–14.
6*a* M&M 88:94.
MWM Ibilisi—Kanisa la ibilisi.
b 1 Ne. 22:22–23.
7*a* Morm. 8:36–38.
8*a* Ufu. 18:10–24; Morm. 8:35–38.
9*a* Ufu. 13:4–7.
12*a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi.
14*a* 2 Ne. 1:11; Morm. 5:19–20.
b MWM Nchi ya Ahadi.
c 1 Ne. 22:7–8.
MWM Israeli—Kutawanyika kwa Israeli.
15*a* 2 Ne. 10:19.

weupe, na [b]warembo zaidi, kama watu wangu kabla [c]hawajauawa.

16 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliona kwamba Wayunani waliotoka utumwani walinyenyekea kwa Bwana; nao [a]walikuwa na nguvu za Bwana.

17 Na nikaona kwamba waasili wa Wayunani walikusanyika pamoja kwenye maji, na pia kwenye ardhi, ili kupigana dhidi yao.

18 Na nikaona kwamba walikuwa na nguvu za Bwana, na pia kwamba ghadhabu ya Mungu ilikuwa juu ya wale wote waliokusanyika pamoja kupigana dhidi yao.

19 Na mimi, Nefi, nikaona kwamba wale Wayunani ambao walitoka utumwani [a]walikombolewa na nguvu za Mungu kutoka mikononi mwa mataifa mengine yote.

20 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliona kwamba walifanikiwa nchini; na nikaona [a]kitabu, ambacho walikuwa nacho miongoni mwao.

21 Na malaika akaniambia: Je, unajua maana ya hicho kitabu?

22 Na nikamjibu: Sijui.

23 Na alisema: Tazama kinatokana na kinywa cha Myahudi. Na mimi, Nefi, nikakiona; na akaniambia: [a]Kitabu unachokiona ni [b]kumbukumbu ya [c]Wayahudi, ambacho kina maagano ya Bwana, ambayo aliagana na nyumba ya Israeli; na pia kina unabii mwingi wa manabii watakatifu; na ni kumbukumbu kama michoro iliyo katika [d]mabamba ya shaba nyeupe, ila tu sio nyingi vile; walakini, yana maagano ya Bwana, ambayo aliagana na nyumba ya Israeli; kwa hivyo, yana thamani kubwa kwa Wayunani.

24 Na malaika wa Bwana akaniambia: Wewe umeona kwamba hicho kitabu kilitoka kwenye kinywa cha Myahudi; na wakati kilitoka kwenye kinywa cha Myahudi kilikuwa na utimilifu wa injili ya Bwana, ambaye anashuhudiwa na mitume kumi na wawili; na wanashuhudia kulingana na ukweli ambao uko na Mwanakondoo wa Mungu.

25 Kwa hivyo, vitu hivi vinatoka kwa usafi kutoka kwa [a]Wayahudi na kuwafikia [b]Wayunani, kulingana na ukweli wa Mungu.

26 Na baada ya kusonga mbele kwa mikono ya wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo, kutoka kwa Wayahudi [a]hadi kwa Wayunani, wewe unaona mwanzo wa lile [b]kanisa [c]kuu la machukizo, ambalo lina machukizo zaidi ya makanisa yote; kwani tazama,

15 *b* 2 Ne. 5:21.
c Morm. 6:17–22.
16 *a* M&M 101:80.
19 *a* 2 Ne. 10:10–14; 3 Ne. 21:4; Eth. 2:12.
20 *a* 1 Ne. 14:23.
23 *a* 1 Ne. 13:38; 2 Ne. 29:4–12.
b MWM Maandiko.
c 2 Ne. 3:12.
d 1 Ne. 5:10–13.
25 *a* 2 Ne. 29:4–6; M&M 3:16. MWM Wayahudi.
b MWM Wayunani.
26 *a* Mt. 21:43.
b MWM Ukengeufu—Ukengeufu wa Kanisa la awali la Kikristo.
c 1 Ne. 13:4–6; 14:3, 9–17.

[d]wameondoa kutoka kwa injili ya Mwanakondoo sehemu nyingi ambazo ni [e]wazi na zenye thamani; na pia wamepunguza maagano mengi ya Bwana.

27 Na haya yote wamefanya kwamba wachafue njia nzuri za Bwana, kwamba wapofushe macho na kushupaza mioyo ya watoto wa watu kuwa migumu.

28 Kwa hivyo, wewe umeona kwamba baada ya hicho kitabu kusonga mbele kupitia mikono ya hilo kanisa kuu la machukizo, kwamba vitu vingi vilivyo wazi na vyenye thamani vilivyondolewa kutoka kwenye hicho kitabu, ambacho ni kitabu cha Mwanakondoo wa Mungu.

29 Na baada ya hivi vitu vilivyo wazi na vyenye thamani kutolewa kiliyafikia mataifa yote ya Wayunani; na baada ya kufikia mataifa yote ya Wayunani, ndiyo, hata ng'ambo ya yale maji mengi ambayo uliona wale Wayunani wakitoka utumwani, wewe unaona—kwa sababu ya kuondolewa kwa vitu vingi vilivyo wazi na vyenye thamani kutoka hicho kitabu, ambavyo vilikuwa wazi na kueleweka na watoto wa watu, kulingana na udhahiri ulio katika Mwanakondoo wa Mungu—kwa sababu ya kuondolewa kwa vitu hivi ambavyo vimetoka kwa injili ya Mwanakondoo, wengi zaidi wamepotea, ndiyo, mpaka Shetani ana nguvu juu yao.

30 Walakini, wewe umeona kwamba wale Wayunani waliotoka utumwani, na wakainuliwa kwa nguvu za Mungu juu ya mataifa mengine yote, usoni mwa nchi ambayo ni nchi bora zaidi ya nchi zingine, ambayo ndiyo nchi Bwana Mungu aliagana na baba yako kwamba uzao wake watapata kuwa [a]nchi yao ya urithi; kwa hivyo, unaona kwamba Bwana Mungu hatakubali kwamba Wayunani wawaangamize kabisa [b]mchanganyiko wa uzao wako, ulio miongoni mwa kaka zako.

31 Wala hatakubali kwamba Wayunani [a]wauangamize uzao wa kaka zako.

32 Wala Bwana Mungu hatakubali kwamba Wayunani wataishi milele katika hali hiyo mbaya ya upofu, ambayo umeona wanayo, kwa sababu ya sehemu zilizo wazi na zenye thamani za injili ya Mwanakondoo ambazo zimefichwa na lile kanisa la [a]machukizo, ambalo umeona uanzilishi wake.

33 Kwa hivyo asema Mwanakondoo wa Mungu: Nitawarehemu Wayunani, kwa kutembelea baki la nyumba ya Israeli kwa hukumu kuu.

34 Na ikawa kwamba malaika wa Bwana akanizungumzia, akisema: Tazama, asema

26 *d* Morm. 8:33; Musa 1:41.
e 1 Ne. 14:20–26; M ya I 1:8.
30 *a* MWM Nchi ya Ahadi.
b Alma 45:10–14.
31 *a* 2 Ne. 4:7; 10:18–19; Yak. (KM) 3:5–9; Hel. 15:12; 3 Ne. 16:8–9; Morm. 5:20–21.
32 *a* MWM Ibilisi—Kanisa la ibilisi.

Mwanakondoo wa Mungu, baada ya kuadhibu [a]baki la nyumba ya Israeli—na baki hili ambalo nalizungumzia ni uzao wa baba yako—kwa hivyo, baada ya kuwaadhibu kwa hukumu, na kuwapiga kwa mkono wa Wayunani, na baada ya Wayunani [b]kupotea zaidi, kwa sababu ya kufichwa kwa sehemu za [c]injili ambazo ni muhimu na kanisa la machukizo, ambalo ni mama ya makahaba, asema Mwanakondoo—nitakuwa na huruma kwa Wayunani siku hiyo, hata kwamba [d]nitawaletea, kwa nguvu zangu, wingi wa injili yangu ambayo itakuwa wazi na yenye thamani, asema Mwanakondoo.

35 Kwani, tazama, asema Mwanakondoo: Nitajidhirihisha kwa uzao wako, kwamba wataandika vitu vingi ambavyo nitawahudumia, ambavyo vitakuwa wazi na vyenye thamani; na baada ya uzao wako kuangamizwa, na kufifia katika kutoamini, pia na uzao wa kaka zako, tazama, [a]vitu hivi vitafichwa, na kutolewa kwa Wayunani, kwa karama na nguvu za Mwanakondoo.

36 Na kwa hayo itaandikwa [a]injili yangu, asema Mwanakondoo, na [b]mwamba wangu na wokovu wangu.

37 [a]Heri wale ambao watatafuta kujenga [b]Sayuni yangu katika siku ile, kwani watapata [c]karama na nguvu za Roho Mtakatifu; na [d]wakivumilia hadi siku ya mwisho watainuliwa katika siku ya mwisho, na wataokolewa katika [e]ufalme usio na mwisho wa Mwanakondoo; na yeyote [f]atakayetangaza amani, ndiyo, habari za shangwe, jinsi gani watakavyokuwa warembo milimani.

38 Na ikawa kwamba niliona baki la uzao wa kaka zangu, na pia [a]kitabu cha Mwanakondoo wa Mungu, ambacho kilitoka kwenye kinywa cha Myahudi, kwamba kilitokana na Wayunani na [b]kuwafikia baki la uzao wa kaka zangu.

39 Na baada ya kuwafikia nikaona [a]vitabu vingine, ambavyo vilitolewa kwa nguvu za Mwanakondoo, kutoka kwa Wayunani hadi kwao, ili [b]kuwasadikisha Wayunani na baki la uzao wa kaka zangu, na pia Wayahudi waliotawanywa kote usoni mwa dunia, kwamba maandishi ya manabii na wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo ni [c]kweli.

34 *a* MWM Yusufu, Mwana wa Yakobo.
b 1 Ne. 14:1–3; 2 Ne. 26:20.
c MWM Injili.
d M&M 10:62. MWM Urejesho wa Injili.
35 *a* 2 Ne. 27:6; 29:1–2. MWM Kitabu cha Mormoni.
36 *a* 3 Ne. 27:13–21.
b Hel. 5:12; 3 Ne. 11:38–39. MWM Mwamba.
37 *a* M&M 21:9.
b MWM Sayuni.
c MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
d 3 Ne. 27:16. MWM Stahimili.
e MWM Utukufu wa Selestia.
f Isa. 52:7; Mos. 15:14–18; 3 Ne. 20:40.
38 *a* 1 Ne. 13:23; 2 Ne. 29:4–6.
b Morm. 5:15.
39 *a* MWM Maandiko—Maandiko yaliyotolewa unabii kwamba yatakuja.
b Eze. 37:15–20; 2 Ne. 3:11–12.
c 1 Ne. 14:30.

40 Na malaika akanizungumzia, akisema: [a]Maandishi haya ya mwisho, ambayo umeyaona miongoni mwa Wayunani, [b]yatathibitisha juu ya kweli kwa yale ya [c]kwanza, ambayo ni ya wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo, na yatafahamisha vitu vilivyo wazi na vyenye thamani viliyotolewa kutoka kwao; na yatafahamisha makabila yote, lugha zote, na watu wote, kwamba Mwanakondoo wa Mungu ndiye Mwana wa Baba wa Milele, na [d]Mwokozi wa ulimwengu; na kwamba lazima watu wote wamkubali yeye, kama sio hivyo, hawawezi kuokolewa.

41 Na ni lazima wamkubali kulingana na yale maneno ambayo yatanenwa kwa kinywa cha Mwanakondoo; na maneno ya Mwanakondoo yatafumbuliwa katika maandishi ya uzao wako, vile vile katika maandishi ya wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo; kwa hivyo zote mbili zitaunganishwa kuwa [a]moja; kwani kuna [b]Mungu mmoja na [c]Mchungaji mmoja ulimwenguni kote.

42 Na wakati unafika atakapojidhihirisha mwenyewe kwa mataifa yote, kwa Wayahudi na pia kwa [a]Wayunani; na baada ya kujidhihirisha mwenyewe kwa Wayahudi na pia kwa Wayunani, ndipo atajidhihirisha mwenyewe kwa Wayunani na pia kwa Wayahudi, na wa [b]mwisho atakuwa wa [c]kwanza, na wa kwanza atakuwa wa mwisho.

MLANGO WA 14

Malaika anamwambia Nefi kuhusu baraka na laana ambazo zitawateremkia Wayunani—Kuna makanisa mawili pekee: Kanisa la Mwanakondoo wa Mungu na kanisa la ibilisi—Watakatifu wa Mungu kote ulimwenguni wanateswa na lile kanisa kuu la machukizo—Mtume Yohana ataandika kuhusu mwisho wa ulimwengu. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na itakuwa kwamba, ikiwa [a]Wayunani watamsikiliza Mwanakondoo wa Mungu katika siku hiyo atajidhirishia kwa neno, pia kwa [b]nguvu, na kwa kila kitendo, kwa kuwaondolea [c]vikwazo vyao—

2 Na wasishupaze mioyo yao dhidi ya Mwanakondoo wa Mungu, watahesabiwa miongoni mwa uzao wa baba yako; ndiyo, [a]watahesabiwa miongoni mwa nyumba ya Israeli; na

40 *a* 2 Ne. 26:16–17; 29:12. MWM Kitabu cha Mormoni.
b Morm. 7:8–9.
c MWM Biblia.
d Tazama ukurasa wenye jina la Kitabu cha Mormoni. Musa 1:6.
41 *a* Eze. 37:17.
b Kum. 6:4; Yn. 17:21–23; 2 Ne. 31:21.
c MWM Mchungaji Mwema.
42 *a* M&M 90:8–9; 107:33; 112:4.
b Yak. (KM) 5:63.
c Lk. 13:30; 1 Ne. 15:13–20.

14 1 *a* 3 Ne. 16:6–13. MWM Wayunani.
b 1 The. 1:5; 1 Ne. 14:14; Yak. (KM) 6:2–3.
c Isa. 57:14; 1 Ne. 13:29, 34; 2 Ne. 26:20.
2 *a* Gal. 3:7, 29; 2 Ne. 10:18–19; 3 Ne. 16:13; 21:6, 22; Ibr. 2:9–11.

watakuwa watu wenye [b]baraka za milele katika nchi ya ahadi; hawatatiwa utumwani tena; na nyumba ya Israeli haitachanganywa tena.

3 Na lile [a]shimo kuu, walilochimbiwa na lile kanisa kuu la machukizo, ambalo lilianzishwa na ibilisi na wanawe, ili aelekeze nafsi za watu hadi jehanamu—ndiyo, lile shimo kuu ambalo limechimbwa kwa maangamizo ya watu, litajazwa na wale waliolichimba, kwa kuangamizwa kwao kabisa, asema Mwanakondoo wa Mungu; sio maangamizo ya nafsi, bali ni kutupwa katika [b]jehanamu isiyo na mwisho.

4 Kwani tazama, hii ni kulingana na utumwa wa ibilisi, na pia kulingana na haki ya Mungu, kwa wale wote watakaotenda uovu na machukizo mbele yake.

5 Na ikawa kwamba malaika alinizungumzia mimi, Nefi, akisema: Wewe umeona kwamba Wayunani wakitubu itakuwa vyema kao; na pia wewe unajua kuhusu maagano ya Bwana na nyumba ya Israeli; na pia wewe umesikia kwamba yeyote [a]asiyetubu lazima aangamie.

6 Kwa hivyo, [a]ole kwa Wayunani ikiwa watashupaza mioyo yao dhidi ya Mwanakondoo wa Mungu.

7 Kwani wakati unafika, asema Mwanakondoo wa Mungu, kwamba nitatenda kazi kuu na ya [a]maajabu miongoni mwa watoto wa watu; kazi ambayo haitakuwa na mwisho, pengine kwa upande mmoja au kwa mwingine—labda kuwasadikisha kwa amani na [b]uzima wa milele, au kwa kuwakabidhi kwa ugumu wa mioyo yao na upofu wa fikira zao na kuwatia utumwani, na pia katika maangamizo, ya kimwili na kiroho, kulingana na [c]utumwa wa ibilisi, ambao nimeuzungumzia.

8 Na ikawa kwamba wakati malaika alipokuwa amenizungumzia maneno haya, akaniambia: Wewe unakumbuka [a]maagano ya Baba na nyumba ya Israeli? Nikamwambia, Ndiyo.

9 Na ikawa kwamba akaniambia: Angalia, na tazama lile kanisa kuu na la machukizo, ambalo ni mama wa machukizo, ambaye mwanzilishi wake ni [a]ibilisi.

10 Na akaniambia: Tazama kuna ila tu makanisa [a]mawili pekee; moja ni kanisa la Mwanakondoo wa Mungu, na [b]lingine ni kanisa la ibilisi; kwa hivyo, yule ambaye sio wa kanisa la Mwanakondoo wa Mungu ni wa kanisa lile kuu, ambalo ni

2 *b* 2 Ne. 6:12; 10:8–14; 3 Ne. 16:6–7; 20:27.
3 *a* 1 Ne. 22:14; M&M 109:25.
b MWM Hukumu; Jehanamu.
5 *a* MWM Toba, Tubu.
6 *a* 2 Ne. 28:32.
7 *a* Isa. 29:14; 1 Ne. 22:8; 2 Ne. 27:26; 29:1–2; M&M 4:1. MWM Urejesho wa Injili.
b MWM Uzima wa Milele.
c 2 Ne. 2:26–29; Alma 12:9–11.
8 *a* MWM Agano la Ibrahimu.
9 *a* 1 Ne. 15:35; M&M 1:35. MWM Ibilisi.
10 *a* 1 Ne. 22:23.
b 1 Ne. 13:4–6, 26.

mama wa machukizo; na yeye ni [c]kahaba wa ulimwengu wote.

11 Na ikawa kwamba niliangalia na kuona kahaba wa ulimwengu wote, na aliketi kwenye [a]maji mengi; na [b]alikuwa na mamlaka ulimwenguni kote, miongoni mwa mataifa yote, makabila yote, lugha zote, na watu.

12 Na ikawa kwamba niliona kanisa la Mwanakondoo wa Mungu, na hesabu yake ilikuwa [a]chache, kwa sababu ya uovu na machukizo ya kahaba aliyeketi kwenye maji mengi; walakini, nikaona kwamba kanisa la Mwanakondoo, ambao walikuwa ni watakatifu wa Mungu, pia nao walikuwa [b]kote usoni mwa dunia; na utawala wao usoni mwa dunia yalikuwa madogo, kwa sababu ya uovu wa yule kahaba mkuu niliyemuona.

13 Na ikawa kwamba niliona kuwa yule mama mkuu wa machukizo alikusanya pamoja vikundi usoni mwote mwa dunia, miongoni mwa mataifa yote ya Wayunani, ili [a]kupigana dhidi ya Mwanakondoo wa Mungu.

14 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliona nguvu za Mwanakondoo wa Mungu, kwamba ziliwashukia watakatifu wa kanisa la Mwanakondoo, na kwa watu wa agano wa Bwana, ambao walitawanyika kote usoni mwa dunia; na walikuwa wamejikinga kwa haki na kwa [a]nguvu za Mungu katika utukufu mkuu.

15 Na ikawa kwamba ghadhabu ya Mungu [a]iliiliteremkia lile kanisa kuu la machukizo, hata kukawa na vita na uvumi wa vita miongoni mwa [b]mataifa yote na makabila yote duniani.

16 Na kulipoanza kuwa na [a]vita na uvumi wa vita miongoni mwa mataifa yote ambayo yalikuwa ya mama wa machukizo, malaika akanizungumzia, akisema: Tazama, ghadhabu ya Mungu imemteremkia mama wa makahaba; na tazama, wewe unaona vitu hivi vyote—

17 Na siku itakapofika [a]wakati [b]ghadhabu ya Mungu itamteremkia mama wa makahaba, ambalo ni lile kanisa kuu la machukizo ulimwenguni mwote, ambaye mwanzilishi wake ni ibilisi, katika siku ile, [c]kazi ya Baba itaanza, katika kutayarisha matimizo ya [d]maagano yake, ambayo ameagana na watu wake ambao ni wa nyumba ya Israeli.

18 Na ikawa kwamba malaika akanizungumzia, akisema: Angalia!

10 *c* Ufu. 17:5, 15; 2 Ne. 10:16.
11 *a* Yer. 51:13; Ufu. 17:15.
b M&M 35:11.
12 *a* Mt. 7:14; 3 Ne. 14:14; M&M 138:26.
b M&M 90:11.
13 *a* Ufu. 17:1–6; 18:24; 1 Ne. 13:5; M&M 123:7–8.
14 *a* Yak. (KM) 6:2; M&M 38:32–38.
15 *a* M&M 1:13–14.
b Mk. 13:8; M&M 87:6.
16 *a* 1 Ne. 22:13–14; Morm. 8:30.
17 *a* MWM Siku za Mwisho.
b 1 Ne. 22:15–16.
c 3 Ne. 21:7, 20–29. MWM Urejesho wa Injili.
d Morm. 8:21, 41. MWM Agano la Ibrahimu.

19 Na nikaangalia na kumwona mtu, na alikuwa amevalia joho leupe.

20 Na malaika akaniambia: Tazama [a]mmoja wa wale mitume kumi na wawili wa Mwanakondoo.

21 Tazama, ataona na kuandika vitu hivi vilivyobaki; ndiyo, na pia vitu hivi vingi vilivyokuwepo.

22 Na pia ataandika kuhusu mwisho wa ulimwengu.

23 Kwa hivyo, vitu hivyo atakavyoandika ni vya haki na kweli; na tazama vimeandikwa kwenye [a]kitabu ulichoona kikitoka kwenye kinywa cha Myahudi; na wakati kwenye kinywa cha Myahudi, au, wakati kitabu kilitoka kinywani mwa Myahudi, vitu vilivyoandikwa vilikuwa wazi na vitakatifu, na vyenye [b]thamani na rahisi kueleweka na watu wote.

24 Na tazama, vitu ambavyo huyu [a]mtume wa Mwanakondoo ataandika ni vitu vingi ambavyo umeona; na tazama, vilivyosalia wewe utaviona.

25 Lakini vitu utakavyoona baadaye wewe hutaviandika; kwani Bwana Mungu amemchagua mtume wa Mwanakondoo wa Mungu [a]aviandike.

26 Na pia wengine ambao wameishi, kwao amewaonyesha vitu vyote, na wameviandika; na [a]vimefungwa na vitatokea kwa usafi, kulingana na ukweli ulio na Mwanakondoo, na hivi vitakuwa katika wakati wa Bwana, kwa nyumba ya Israeli.

27 Na mimi, Nefi, nilisikia na ninashuhudia, kwamba jina la yule mtume wa Mwanakondoo lilikuwa ni [a]Yohana, kulingana na neno la malaika.

28 Na tazama, mimi, Nefi, nimekatazwa kwamba nisiandike vitu vilivyokuwa vimebaki ambavyo niliviona na kusikia; kwa hivyo vitu ambavyo nimeandika vimenitosha; na nimeandika sehemu ndogo tu ya yale niliyoona.

29 Ninashuhudia kwamba niliona vile vitu ambavyo [a]baba yangu aliviona, na malaika wa Bwana alinifahamisha hayo.

30 Na sasa ninakoma kuzungumza kuhusu mambo ambayo niliyaona nilipokuwa nimenyakuliwa katika Roho; na kama mambo yote ambayo niliyaona hayajaandikwa, mambo haya ambayo nimeyaandika ni ya [a]kweli. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.

MLANGO WA 15

Uzao wa Lehi utapokea injili kutoka kwa Wayunani katika siku za mwisho—Kusanyiko la Israeli unafananishwa na mti wa mzeituni ambao matawi yake ya asili yatapandikizwa tena—Nefi anatafsiri ono la mti wa uzima na anazungumza kuhusu haki ya

20*a* Ufu. 1:1–3; 1 Ne. 14:27.
23*a* 1 Ne. 13:20–24; Morm. 8:33.
b 1 Ne. 13:28–32.
24*a* Eth. 4:16.
25*a* Yn. 20:30–31; Ufu. 1:19.
26*a* 2 Ne. 27:6–23; Eth. 3:21–27; 4:4–7; M&M 35:18; JS—H 1:65.
27*a* Ufu. 1:1–3.
29*a* 1 Ne. 8.
30*a* 2 Ne. 33:10–14.

Mungu katika kuwatenga waovu kutoka kwa watakatifu. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kunyakuliwa katika Roho, na kuona mambo haya yote, nilirudi kwenye hema la baba yangu.

2 Na ikawa kwamba niliona kaka zangu, na walikuwa wakibishana kuhusu vile vitu ambavyo baba yangu aliwazungumzia.

3 Kwa kweli aliwazungumzia vitu vikubwa, vilivyokuwa vigumu [a]kueleweka, isipokuwa mtu amuulize Bwana; na wao wakiwa wagumu mioyoni mwao, kwa hivyo hawakumtazama Bwana jinsi ilivyowapasa.

4 Na sasa mimi, Nefi, nilihuzunika kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao, na pia, kwa sababu ya vitu ambavyo niliviona, na nilijua lazima vitimizwe kwa sababu ya uovu mkuu wa wanadamu.

5 Na ikawa kwamba nililemewa na [a]masumbuko yangu, kwa maana nilidhani kwamba masumbuko yangu yalizidi yote, kwa sababu ya [b]kuangamia kwa watu wangu, kwani nilikuwa nimeona kuanguka kwao.

6 Na ikawa kwamba baada ya kupokea [a]nguvu nikawazungumzia kaka zangu, nikitaka kujua chanzo cha ugomvi wao.

7 Na wakasema: Tazama, hatuwezi kuelewa maneno ambayo baba yetu amesema kuhusu matawi ya asili ya mti wa mzeituni, na pia kuhusu Wayunani.

8 Na nikawaambia: [a]Je mmemuuliza Bwana?

9 Na wakasema: Hapana; kwani Bwana hatujulishi vitu hivi.

10 Tazama, nikawaambia: Kwa nini hamtii amri za Bwana? Kwa nini mwangamie, kwa sababu ya [a]ugumu wa mioyo yenu?

11 Kwani hamkumbuki vitu ambavyo Bwana amesema?—Kama hamtashupaza mioyo yenu, na [a]mniulize kwa imani, mkiamini kwamba mtapokea, kwa bidii katika kutii amri zangu, kwa kweli vitu hivi vitafanywa vijulikane kwenu.

12 Tazama, nawaambia, kuwa nyumba ya Israeli ililinganishwa na mti wa mzeituni, na Roho wa Bwana aliyekuwa ndani ya baba yetu; na tazama si sisi tumetokana na nyumba ya Israeli, na si sisi ni [a]tawi la nyumba ya Israeli?

13 Na sasa, kitu ambacho baba yetu anamaanisha kuhusu kupandikizwa kwa matawi ya asili kwa kupitia utimilifu wa Wayunani, ni, kwamba katika siku za baadaye, wakati uzao wetu utakuwa [a]umefifia katika kutoamini, ndiyo, kwa muda wa miaka mingi, na vizazi

15 3*a* 1 Kor. 2:10–12; Alma 12:9–11.
5*a* MWM Shida.
b Eno. 1:13; Morm. 6:1.
6*a* Musa 1:10; JS—H 1:20, 48.
8*a* Mos. 26:13; Alma 40:3. MWM Sala.
10*a* MWM Ukengeufu.
11*a* Yak. (Bib.) 1:5–6; Eno. 1:15; Moro. 7:26; M&M 18:18.
MWM Omba.
12*a* Mwa. 49:22–26; 1 Ne. 10:12–14; 19:24. MWM Lehi, Baba wa Nefi.
13*a* 1 Ne. 12:22–23; 2 Ne. 26:15.

vingi baada ya [b]Masiya kudhihirishwa katika mwili kwa watoto wa watu, ndipo utimilifu wa [c]injili ya Masiya utawafikia [d]Wayunani, na kutoka kwa Wayunani hadi kwa baki la uzao wetu—

14 Na katika siku ile baki la [a]uzao wetu litajua kwamba wao ni wa nyumba ya Israeli, na kwamba wao ni watu wa [b]agano la Bwana; na kisha watajua na pia kupata [c]ufahamu wa babu zao, na pia ufahamu wa injili ya Mkombozi wao, ambayo aliwahudumia babu zao; kwa hivyo, watamfahamu Mkombozi wao na mambo halisi ya mafundisho yake, ili waweze kujua jinsi ya kumkaribia na waokolewe.

15 Na basi katika siku ile, si watashangilia na kumsifu Mungu asiye na mwisho, [a]mwamba wao na wokovu wao? Ndiyo, katika siku ile, si watapokea nguvu na malisho kutoka kwa ule [b]mizabibu wa kweli? Ndiyo, si wataungana na zizi la kweli la Mungu?

16 Na tazama, nawaambia, Ndiyo; watakumbukwa tena miongoni mwa nyumba ya Israeli; [a]watapandikizwa ndani, wakiwa tawi la asili la mti wa mzeituni, kwenye mti wa mzeituni wa kweli.

17 Na hii ndiyo baba yetu anamaanisha; na anamaanisha kwamba haitatimizwa hadi watawanywe na Wayunani; na anamaanisha itatimizwa na Wayunani, ili Bwana awaonyeshe Wayunani nguvu zake, na kwa sababu hii [a]atakataliwa na Wayahudi, au na nyumba ya Israeli.

18 Kwa hivyo, baba yetu hajazungumza juu ya uzao wetu pekee, lakini pia nyumba yote ya Israeli, akilenga agano ambalo litatimizwa katika siku za baadaye; agano ambalo Bwana aliagana na baba yetu Ibrahimu, akisema: Kwa [a]uzao wako makabila yote ya dunia yatabarikiwa.

19 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwaambia mengi kuhusu vitu hivi; ndiyo, niliwaambia kuhusu [a]uamsho wa Wayahudi katika siku za baadaye.

20 Na nikawasimulia maneno ya [a]Isaya, ambaye alizungumza kuhusu kurudi kwa Wayahudi, au nyumba ya Israeli; na baada ya wao kuamshwa hawatachanganyika tena, wala kutawanyika tena. Na ikawa kwamba niliwaelezea kaka zangu maneno mengi, hata kwamba waliridhika na [b]wakajinyenyekeza mbele ya Bwana.

21 Na ikawa kwamba wali-

13 *b* MWM Masiya.
c MWM Injili.
d 1 Ne. 13:42; 22:5–10; M&M 14:10.
MWM Wayunani.
14 *a* 2 Ne. 10:2; 3 Ne. 5:21–26; 21:4–7.
b MWM Agano la Ibrahimu.
c 2 Ne. 3:12; 30:5; Morm. 7:1, 9–10; M&M 3:16–20.
Tazama pia ukurasa wenye jina la Kitabu cha Mormoni.
15 *a* MWM Mwamba.
b Mwa. 49:11; Yn. 15:1.
16 *a* Yak. (KM) 5:60–68.
17 *a* MWM Kusulubiwa.
18 *a* Mwa. 12:1–3; Ibr. 2:6–11.
19 *a* 1 Ne. 19:15.
MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
20 *a* 1 Ne. 19:23.
b 1 Ne. 16:5, 24, 39.

nizungumzia tena, wakisema: Kitu hiki kinamaanisha nini ambacho Baba yetu alikiona ndotoni? Nini maana ya ule [a]mti aliouona?

22 Na nikawaambia: Ni kielelezo cha [a]mti wa uzima.

23 Na wakaniambia: Nini maana ya [a]fimbo ya chuma ambayo baba aliona, ikielekeza kwenye ule mti?

24 Na nikawaambia kwamba ilikuwa [a]neno la Mungu; na yeyote atakayesikiza hilo neno la Mungu, na [b]alizingatie, hataangamia; wala [c]majaribu na [d]mishale ya moto ya [e]adui kuwalemea na kuwapofusha, ili kuwaelekeza kwenye maangamio.

25 Kwa hivyo, mimi, Nefi, niliwasihi [a]wasikize neno la Bwana; ndiyo, niliwasihi kwa nguvu zote za nafsi yangu, na kwa uwezo wote ambao nilikuwa nao, kwamba wasikilize neno la Mungu na wakumbuke kutii amri zake kila wakati katika vitu vyote.

26 Na wakaniuliza: Nini maana ya ule [a]mto ambao baba yetu aliuona?

27 Na nikawaambia kwamba yale [a]maji ambayo baba aliona ni [b]uchafu; na mawazo yake yalikuwa yamemezwa katika vitu vingine kwamba hakuona uchafu wa yale maji.

28 Nikawaambia kwamba lilikuwa ni [a]shimo la kuogopesha, ambalo liligawanya waovu kutokana na mti wa uzima, na pia kutoka kwa watakatifu wa Mungu.

29 Nikawaambia kwamba ilikuwa kielelezo cha ile [a]jehanamu ya kuogopesha, ambayo yule malaika aliniambia imetayarishwa kwa waovu.

30 Na nikawaambia kwamba baba yetu pia aliona kwamba [a]haki ya Mungu imewatenga waovu kutoka kwa watakatifu; na mng'aro wake ulikuwa ni kama mng'aro wa moto, ambao unapaa kwa Mungu milele na milele, bila mwisho.

31 Na wakaniambia: Je, hii inamaanisha mateso ya mwili wakati wa [a]majaribio, au hali ya mwisho ya nafsi baada ya [b]kifo cha mwili, au inazungumza kuhusu vitu ambavyo ni vya muda?

32 Na ikawa kwamba niliwaambia kuwa ilikuwa ni kielelezo cha vitu ambavyo ni vya muda na kiroho; kwa maana siku itafika watakapohukumiwa kulingana na [a]matendo yao, ndiyo, hata matendo yaliyotendwa katika mwili wa

21 *a* 1 Ne. 8:10–12.
22 *a* 1 Ne. 11:4, 25; Musa 3:9.
23 *a* 1 Ne. 8:19–24.
24 *a* MWM Neno la Mungu.
b 1 Ne. 8:30; 2 Ne. 31:20.
c 1 Ne. 8:23. MWM Jaribu, Majaribu.
d Efe. 6:16; M&M 3:8; 27:17.
e MWM Ibilisi.
25 *a* M&M 11:2; 32:4; 84:43–44.
26 *a* 1 Ne. 8:13.
27 *a* 1 Ne. 12:16.
b MWM Chafu, Uchafu.
28 *a* Lk. 16:26; 1 Ne. 12:18; 2 Ne. 1:13.
29 *a* MWM Jehanamu.
30 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
31 *a* Alma 12:24; 42:10; Hel. 13:38.
b Alma 40:6, 11–14.
32 *a* MWM Matendo.

muda katika siku zao za majaribio.

33 Kwa hivyo, [a]wakifa katika uovu wao lazima [b]watupwe pia, kulingana na vitu vya kiroho, ambavyo vinalingana na haki; kwa hivyo, lazima waletwe kusimama mbele ya Mungu, [c]wahukumiwe kulingana na [d]matendo yao; na kama matendo yao yalikuwa machafu lazima wao wawe wachafu; na kama wao ni [e]wachafu lazima iwe kwamba hawawezi [f]kuishi katika ufalme wa Mungu; au ikiwa hivyo, ufalme wa Mungu lazima uwe mchafu pia.

34 Lakini tazama, nawaambia, ufalme wa Mungu sio [a]mchafu, na hakuna kitu chochote kichafu kiwezacho kuingia katika ufalme wa Mungu; kwa hivyo lazima pawe na mahali pa uchafu ambapo pametayarishiwa yale ambayo ni machafu.

35 Na kuna pahali pametayarishwa, ndiyo, hata ile [a]jehanamu ya kuogofya ambayo nimeizungumzia, na [b]ibilisi ndiye mtayarishaji; kwa hivyo hali ya mwisho ya nafsi za wanadamu ni kuishi katika ufalme wa Mungu, au kutupwa nje kwa sababu ya ile [c]haki ambayo nimezungumzia.

36 Kwa hivyo, waovu wamekataliwa kutoka kwa watakatifu, na pia kutoka kwa [a]mti wa uzima, ambao matunda yake ni yenye thamani na [b]bora zaidi ya matunda mengine; ndiyo, na ni karama ya Mungu ambayo ni [c]kuu zaidi ya [d]karama zote. Na hivyo ndivyo nilivyowazungumzia kaka zangu. Amina.

MLANGO WA 16

Waovu wanachukua ukweli kuwa mgumu—Wana wa Lehi wanaoa mabinti za Ishmaeli—Liahona inawaongoza njiani huko nyikani—Ujumbe kutoka kwa Bwana unaandikwa kwenye Liahona mara kwa mara—Ishmaeli anafariki; jamii yake inanung'unika kwa sababu ya masumbuko. Karibia mwaka 600–592 K.K.

Na sasa ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kumaliza kuwazungumzia kaka zangu, tazama wakaniambia: Wewe umetuelezea vitu vigumu, kuliko tunavyoweza kuvumilia.

2 Na ikawa kwamba niliwaambia kuwa nilijua kwamba nilikuwa nimezungumza vitu vigumu kinyume cha waovu, kulingana na ukweli; na nilikuwa nimewathibitisha wenye haki, na kushuhudia kwamba watainuliwa katika siku ya mwisho; kwa hivyo, wenye

33 *a* Mos. 15:26; Moro. 10:26.
b Alma 12:12–16; 40:26.
c MWM Hukumu ya mwisho.
d 3 Ne. 27:23–27.
e 2 Ne. 9:16; M&M 88:35.
f Zab. 15; 24:3–4; Alma 11:37; M&M 76:50–70; Musa 6:57.

34 *a* MWM Chafu, Uchafu.

35 *a* 2 Ne. 9:19; Mos. 26:27. MWM Jehanamu.
b 1 Ne. 14:9; M&M 1:35.
c MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.

36 *a* Mwa. 2:9; 2 Ne. 2:15.
b 1 Ne. 8:10–12; Alma 32:42.
c M&M 6:13.
d M&M 14:7. MWM Uzima wa Milele.

[a]hatia huchukua [b]ukweli kuwa mgumu, kwani [c]huwakata hadi sehemu zao za ndani.

3 Na sasa kaka zangu, kama ninyi mngekuwa watakatifu na mngetaka kusikiza ukweli, na kuufuata, ili [a]mtembee imara mbele ya Mungu, basi hamngenung'unika kwa sababu ya ukweli, mkisema: Unazungumza vitu vigumu dhidi yetu.

4 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwasihi kaka zangu, kwa bidii zote, watii amri za Bwana.

5 Na ikawa kwamba [a]walijinyenyekeza kwa Bwana; hata kwamba nikawa na shangwe na matumaini mengi, kwamba watatembea katika njia za haki.

6 Sasa, vitu hivi vyote vilizungumziwa na kufanyika vile baba yangu alipoishi kwenye hema katika bonde alilioliita Lemueli.

7 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilimchukua [a]binti mmoja wa Ishmaeli kuwa [b]mke wangu, na pia kaka zangu wakaoa mabinti za Ishmaeli; na pia [c]Zoramu akamwoa binti mkubwa wa Ishmaeli.

8 Na hivyo baba yangu alitimiza amri zote ambazo alipewa na Bwana. Na pia, mimi, Nefi, nilibarikiwa na Bwana zaidi.

9 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana ikazungumza na baba yangu usiku, na kumwamuru kwamba kesho yake aanze kusafiri nyikani.

10 Na ikawa kwamba wakati baba yangu alipoamka asubuhi, na akaenda mlangoni mwa hema, kwa mshangao wake mkuu, akaona hapo chini [a]mpira wa ufundi maalumu; na ulikuwa wa shaba nyeupe ya hali ya juu. Na ndani ya huu mpira kulikuwa na mishale miwili; na moja ilionyesha njia tutakayofuata nyikani.

11 Na ikawa kwamba tulikusanya pamoja vitu ambavyo tungebeba nyikani, na pia mabaki ya maakuli ambayo Bwana alikuwa ametupatia; na tukachukua mbegu za kila aina ili tubebe nyikani.

12 Na ikawa kwamba tulichukua hema zetu na kuelekea nyikani, na tukavuka ng'ambo ya mto Lamani.

13 Na ikawa kwamba tulisafiri kwa muda wa siku nne, tukielekea karibu upande wa kusini-kusini-mashariki, na tukapiga hema zetu tena; na tukaita mahali pale Shazeri.

14 Na ikawa kwamba tulichukua pinde zetu na mishale yetu, na kwenda nyikani kuwindia jamii zetu; na baada ya kuwindia jamii zetu chakula tulirejea tena kwa jamii zetu huko nyikani, mahali palipoitwa Shazeri. Na tulisafiri tena nyikani, tukielekea upande ule ule, tukifuata

16 2*a* Yn. 3:20; 2 Ne. 33:5; Eno. 1:23; Hel. 14:10. MWM Hatia.
b Mit. 15:10; 2 Ne. 1:26; 9:40; Hel. 13:24–26.
c Mdo. 5:33; Mos. 13:7.
3*a* M&M 5:21. MWM Tembea, Tembea na Mungu.
5*a* 1 Ne. 16:24, 39; 18:4.
7*a* 1 Ne. 7:1.
b MWM Ndoa, Oa, Olewa.
c 1 Ne. 4:35; 2 Ne. 5:5–6.
10*a* Alma 37:38–46. MWM Liahona.

sehemu ambazo zilikuwa nzuri nyikani, ambazo zilikuwa mipakani mwa [a]Bahari ya Shamu.

15 Na ikawa kwamba tulisafiri kwa muda wa siku nyingi, tukiwinda chakula chetu njiani, kwa pinde zetu na mishale yetu na mawe yetu na kwa kombeo zetu.

16 Na tulifuata [a]majira ya ule mpira, ambayo ilituelekeza katika sehemu zenye rutuba zaidi nyikani.

17 Na baada ya kusafiri kwa muda wa siku nyingi, tukapiga hema zetu kwa muda mfupi, ili tujipumzishe tena na tutafutie jamii zetu chakula.

18 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilipoenda kuwinda, tazama, nikavunja upinde wangu, ambao ulikuwa umetengenezwa kwa [a]chuma nyororo; na baada ya kuvunja upinde wangu, tazama, ndugu zangu walinikasirikia kwa kupotelewa na upinde wangu, kwa sababu hatukupata chakula chochote.

19 Na ikawa kwamba tulirudi kwa jamii zetu bila chakula, na wakiwa wamechoka zaidi, kwa sababu ya kusafiri, waliteseka sana kwa kutaka chakula.

20 Na ikawa kwamba Lamani na Lemueli na wana wa Ishmaeli walianza kunung'unika zaidi, kwa sababu ya mateso yao na masumbuko huko nyikani; na pia baba yangu alianza kumnung'unikia Bwana, Mungu wake; ndiyo, na wote walikuwa na huzuni zaidi, hata wakamnung'unikia Bwana.

21 Sasa ikawa kwamba mimi, Nefi, nikiwa nimeumizwa na kaka zangu kwa sababu ya kupotelewa na upinde wangu, na pinde zao zikiwa zimelegea na zimenyumbuka, ilianza kuwa shida zaidi, ndiyo, hata tukakosa chakula.

22 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwazungumzia kaka zangu, kwa sababu walikuwa wameshupaza mioyo yao tena, hata [a]wakamnung'unikia Bwana Mungu wao.

23 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nikatengeneza upinde kutoka kwa mbao, na kutoka kwa kijiti kinyoofu, nikatengeneza mshale; kwa hivyo, nikajiami kwa upinde, na mshale, kombeo na mawe. Na nikamuuliza [a]baba yangu: Niende kuwinda wapi?

24 Na ikawa kwamba [a]akamuomba Bwana, kwani walijinyenyekeza kwa sababu ya maneno yangu; kwani niliwaambia vitu vingi kwa nguvu za nafsi yangu.

25 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana ikamjia baba yangu; na [a]akakemewa kwa kweli kwa kumnung'unikia Bwana, hadi akadhilika kwa huzuni nyingi.

26 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana ikamwambia: Angalia kwenye ule mpira, na uone vitu vilivyoandikwa.

14*a* M&M 17:1.
16*a* 1 Ne. 16:10, 16, 26; 18:12; Alma 37:38–46.
18*a* 2 Sam. 22:35.
22*a* Ku. 16:8; Hes. 11:1.
23*a* Ku. 20:12; Mos. 13:20.
24*a* MWM Sala.
25*a* Eth. 2:14. MWM Rudi, Kurudiwa.

27 Na ikawa kwamba wakati baba yangu alipoona vitu vilivyoandikwa kwenye mpira, aliogopa na kutetemeka sana, pia na kaka zangu, na wana wa Ishmaeli na wake zetu.

28 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliona kwamba vile vyuma vilivyokuwa kwenye mpira, vilifanya kazi kulingana na [a]imani na bidii na utiifu, ambao tulivipatia.

29 Na pia paliandikwa juu yao maandishi mengine mapya, ambayo yalikuwa rahisi kwa kusomwa, ambayo yalitupatia [a]ufahamu kuhusu njia za Bwana; na yaliandikwa na kubadilishwa mara kwa mara, kulingana na imani na bidii ambayo tuliipatia. Na hivyo tunaona kwamba kwa njia [b]ndogo Bwana anaweza kuleta vitu vikubwa.

30 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilienda juu ya mlima, kulingana na maelezo yaliyokuwa kwenye mpira.

31 Na ikawa kwamba niliwinda wanyama wa mwitu, hata nikapata chakula cha jamii zetu.

32 Na ikawa kwamba nilirudi kwenye hema zetu, nikibeba wanyama ambao niliwinda; na sasa walipoona nilikuwa nimepata chakula, walifurahia sana! Na ikawa kwamba walijinyenyekeza kwa Bwana, na wakamtolea shukrani.

33 Na ikawa kwamba tulianza safari yetu tena, tukisafiri kwa majira karibu kama mwanzoni, na baada ya kusafiri kwa muda wa siku nyingi tulipiga hema zetu tena, ili tukae kwa muda.

34 Na ikawa kwamba [a]Ishmaeli alifariki, na akazikwa mahali palipoitwa Nahomu.

35 Na ikawa kwamba mabinti za Ishmaeli waliomboleza zaidi, kwa sababu ya kifo cha baba yao, na kwa sababu ya [a]masumbuko yao nyikani; na wakamnung'unikia baba yangu, kwa sababu aliwatoa nchi ya Yerusalemu, wakisema: Baba yetu amekufa; ndiyo, na tumezunguka sana nyikani, na tumepata masumbuko mengi, njaa, kiu, na uchovu; na baada ya haya mateso yote tutaangamia nyikani kwa njaa.

36 Na hivyo wakalalamika dhidi ya baba yangu, na pia dhidi yangu; na wakataka kurudi tena Yerusalemu.

37 Na Lamani akamwambia Lemueli na pia wana wa Ishmaeli: Tazama, [a]tumuue baba yetu, na pia ndugu yetu Nefi, ambaye amejifanya kuwa [b]mtawala na mwalimu wetu, sisi ambao ni kaka zake wakubwa.

38 Na sasa, anasema kwamba Bwana amemzungumzia, na pia kwamba [a]malaika wamemhudumia. Lakini tazama, tunajua kwamba anatudanganya; na anatuambia vitu hivi, na

28 *a* Alma 37:40. MWM Amini, Imani.
29 *a* MWM Ufahamu.
b 2 Fal. 5:13; Yak. (Bib.) 3:4; Alma 37:6–7, 41; M&M 123:16.
34 *a* 1 Ne. 7:2–6.
35 *a* MWM Shida.
37 *a* 1 Ne. 17:44. MWM Mauaji.
b Mwa. 37:9–11; 1 Ne. 2:22; 18:10.
38 *a* 1 Ne. 3:30–31; 4:3.

anatenda vitu vingi kwa ujanja wake, ili atufunike macho yetu, akidhani, kwamba, labda atatuelekeza kwenye nyika ya ugeni; na baada ya kufanya hivyo, amepanga kujifanya mfalme na mtawala wetu, ili atutendee kulingana na nia na mapenzi yake. Na jinsi hii ndivyo kaka yangu Lamani alivyochochea hasira mioyoni mwao.

39 Na ikawa kwamba Bwana alikuwa pamoja nasi, ndiyo, hata sauti ya Bwana ikaja na [a]kuwazungumzia maneno mengi, na ikawakemea zaidi; na baada ya kukemewa na sauti ya Bwana wakaacha hasira yao, na wakatubu dhambi zao, hata kwamba Bwana akatubariki tena kwa chakula, kwamba hatukuangamia.

MLANGO WA 17

Nefi anaamriwa kujenga merikebu—Kaka zake wanampinga—Anawasihi kwa kuwaelezea vile Mungu alivyoitendea Israeli katika historia—Nefi anajazwa na nguvu za Mungu—Kaka zake wanakatazwa wasimguse, au sivyo watanyauka kama nyasi iliyokauka. Karibia mwaka 592–591 K.K.

Na ikawa kwamba tulianza safari yetu tena nyikani; na tulisafiri tukielekea mashariki tangu tangu wakati ule na kuendelea. Na tulisafiri na kupitia mateso mengi huko nyikani; na wanawake zetu walizaa watoto nyikani.

2 Na baraka kuu za Bwana zilikuwa nasi, kwamba wakati tulipoishi kwa nyama [a]mbichi huko nyikani, wanawake wetu walitoa maziwa mengi ya kutosha ya kunyonyesha watoto wao, na walikuwa na nguvu, ndiyo, hata kama wanaume; na wakaanza kusafiri bila kunung'unika.

3 Na hivyo tunaona kwamba lazima amri za Mungu zitimizwe. Na kama watoto wa watu [a]watatii amri za Mungu atawalisha, na kuwatia nguvu, na kuwapatia uwezo ili wakamilishe kitu ambacho amewaamuru; kwa hivyo, [b]alitupatia uwezo tulipopitia nyikani.

4 Na tulipitia nyikani kwa muda wa miaka mingi, ndiyo, hata miaka minane nyikani.

5 Na tulifika nchi ambayo tuliita Neema, kwa sababu ya matunda yake mengi na asali ya mwitu; na vitu hivi vyote vilitayarishwa na Bwana ili tusiangamie. Na tukaona bahari, ambayo tuliita Ireantumu, ambayo, maana yake, ni maji mengi.

6 Na ikawa kwamba tulipiga hema zetu pwani, ingawaje tulipata [a]mateso na masumbuko mengi, ndiyo, hata mengi zaidi kwamba hatuwezi kuandika yote, tulishangilia sana wakati tulipofika pwani; na tukaita pahali pale Neema, kwa sababu ya matunda yake mengi.

7 Na ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kuwa katika nchi ya

39 *a* MWM Rudi, Kurudiwa.
17 2 *a* 1 Ne. 17:12.
3 *a* Mos. 2:41; Alma 26:12. MWM Mtiifu, Tii, Utii.
b 1 Ne. 3:7.
6 *a* 2 Ne. 4:20.

Neema kwa muda wa siku nyingi, sauti ya Bwana ikanijia na kuniambia: Ondoka, na uende mlimani. Na ikawa kwamba niliinuka na kwenda mlimani, na nikamlilia Bwana.

8 Na ikawa kwamba Bwana akanizungumzia, na kusema: Wewe utajenga merikebu, kulingana na [a]vile nitakavyokuonyesha, ili niwavushe watu wako maji haya.

9 Na nikasema: Bwana, ni wapi nitakapoenda ili nipate mawe yenye madini ya kuyeyusha, ili nijenge vifaa vya kutengenezea merikebu jinsi vile umenionyesha?

10 Na ikawa kwamba Bwana akanieleza pa kwenda ili nipate mawe yenye madini, ili nijenge vifaa.

11 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nilitengeneza mivuo ya kupuliza moto, kwa ngozi za wanyama; na baada ya kutengeneza mivuo, ya kupuliza moto, niligongesha mawe mawili pamoja ili nipate moto.

12 Kwani Bwana hakuturuhusu tuwashe moto mwingi, tulipokuwa tukisafiri nyikani; kwani alisema: Nitafanya chakula chenu kiwe kitamu, hata [a]hamtakipika;

13 Na pia nitakuwa nuru yenu huko nyikani; na [a]nitawatayarishia njia, kama mtatii amri zangu; kwa hivyo, vile mtakavyotii amri zangu mtaongozwa hadi kwenye [b]nchi ya ahadi; na [c]mtajua kwamba ni mimi ninayewaongoza.

14 Ndiyo, na Bwana pia akasema kwamba: Baada ya kuwasili katika nchi ya ahadi, [a]mtajua kwamba mimi, Bwana, ndiye [b]Mungu; na kwamba mimi, Bwana, niliwakomboa kutoka maangamizoni; ndiyo, kwamba niliwatoa kutoka nchi ya Yerusalemu.

15 Kwa hivyo, mimi, Nefi, nilijaribu kutii amri za Bwana, na nikawasihi kaka zangu wawe waaminifu na wenye jitihada.

16 Na ikawa kwamba nilitengeneza vifaa kutoka kwa mawe yenye madini ambayo nilikuwa nimeyayeyusha kutoka kwenye mwamba.

17 Na wakati kaka zangu walipoona kwamba niko karibu [a]kujenga merikebu, walianza kunung'unika dhidi yangu, na kusema: Ndugu yetu ni mjinga, kwani anafikiri kuwa anaweza kujenga merikebu; ndiyo, na anafikiri pia kwamba anaweza kuvuka maji haya makuu.

18 Na hivyo ndivyo kaka zangu walilalamika dhidi yangu, na hawakutaka kufanya kazi, kwani hawakuamini kwamba ningejenga merikebu; wala hawakuamini kuwa nilifundishwa na Bwana.

19 Na sasa ikawa kwamba mimi, Nefi, nilikuwa na huzuni zaidi kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao, na sasa walipoona kwamba nilianza kuwa

8 *a* 1 Ne. 18:2.
12 *a* 1 Ne. 17:2.
13 *a* Alma 37:38–39.
b 1 Ne. 2:20; Yak. (KM) 2:12.
c Ku. 6:7.
14 *a* 2 Ne. 1:4. MWM Ushuhuda.
b M&M 5:2.
17 *a* 1 Ne. 18:1–6.

na huzuni walifurahi mioyoni mwao, hata [a]wakanishangilia kwa kusema: Tulijua kwamba huwezi kujenga merikebu, kwani tulijua ulipungukiwa na mawazo; kwa hivyo, wewe huwezi kutimiza kazi kubwa hivyo.

20 Nawe uko kama baba yetu, aliyepotoshwa na [a]mawazo ya ujinga moyoni mwake; ndiyo, ametutoa kutoka nchi ya Yerusalemu, na tumezunguka nyikani kwa hii miaka mingi; na wanawake wetu wamefanya kazi ya kuchosha, wakiwa wajawazito; na wamezaa watoto nyikani na kuteseka kwa vitu vyote, ila kifo tu; na ingekuwa vyema wafe kabla ya kutoka Yerusalemu badala ya kuteseka na haya masumbuko.

21 Tazama, hii miaka mingi tumeteseka nyikani, na pengine huu wakati tungefurahia mali yetu na nchi yetu ya urithi; ndiyo, na pengine tungekuwa na furaha.

22 Na tunajua kwamba wale watu waliokuwa katika nchi ya Yerusalemu walikuwa watu [a]watakatifu; kwani walitii masharti na hukumu za Bwana, na amri zake zote, kulingana na sheria ya Musa; kwa hivyo, tunajua kwamba ni watu watakatifu; na baba yetu amewahukumu, na ametupotosha kwa sababu tulisikiza maneno yake; ndiyo, na kaka yetu ni kama yeye. Na kwa lugha kama hii, kaka zangu walinung'unika na kulalamika dhidi yetu.

23 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, nikawazungumzia nikasema: Je, mnaamini kwamba baba zetu, ambao walikuwa wana wa Israeli, wangekombolewa kutoka mikononi mwa Wamisri kama hawakutii maneno ya Bwana?

24 Ndiyo, mnadhania kwamba wangetolewa utumwani, kama Bwana hakumwamuru Musa [a]awatoe utumwani?

25 Sasa mnajua kwamba wana wa Israeli walikuwa [a]utumwani; na mnajua kwamba walikuwa na [b]mizigo mizito, ambayo ilikuwa migumu kuvumilia; kwa hivyo, mnajua kwamba lazima iwe ilikuwa kitu kizuri kwao, kutolewa utumwani.

26 Sasa mnajua kwamba [a]Musa aliamriwa na Bwana kutenda ile kazi kuu; na mnajua kwamba kwa [b]maneno yake, maji ya Bahari ya Shamu yaligawanyika huku na kule, na wakapitia nchi kavu.

27 Lakini mnajua Wamisri walizama katika Bahari ya Shamu, ambao walikuwa majeshi la Farao.

28 Na pia mnajua kwamba walilishwa kwa [a]mana kutoka mbinguni huko nyikani.

29 Ndiyo, na pia mnajua kwamba Musa, kwa neno lake

19 *a* MWM Mateso, Tesa.
20 *a* 1 Ne. 2:11.
22 *a* 1 Ne. 1:13.
24 *a* Ku. 3:2–10; 1 Ne. 19:10; 2 Ne. 3:9; 25:20.
25 *a* Mwa. 15:13–14.
b Ku. 1:11; 2:11.
26 *a* Mdo. 7:22–39.
b Ku. 14:21–31; 1 Ne. 4:2; Mos. 7:19; Hel. 8:11; M&M 8:3; Musa 1:25.
28 *a* Ku. 16:4, 14–15, 35; Hes. 11:7–8; Kum. 8:3; Mos. 7:19.

kulingana na nguvu za Mungu ambazo alikuwa nazo, [a]aligonga mwamba, na pakatiririka maji, ili wana wa Israeli watulize kiu yao.

30 Na ijapokuwa waliongozwa, na Bwana Mungu wao, Mkombozi wao, akiwatangulia, akiwaongoza mchana na kuwapatia nuru usiku, na kuwafanyia yote [a]yaliyompasa mwanadamu kupokea, waliposhupaza mioyo yao na kupofusha mawazo yao, na [b]wakamtusi Musa pamoja na Mungu anayeishi na wa kweli.

31 Na ikawa kwamba [a]aliwaangamiza kulingana na neno lake; na [b]akawaongoza kulingana na neno lake; na aliwatendea vitu vyote kulingana na neno lake; na hakuna lolote lililotendwa ila tu kulingana na neno lake.

32 Na baada ya kuvuka mto Yordani aliwatia nguvu za [a]kuwafukuza wana wa nchi ile, ndiyo, hata kuwatawanya kwa maangamizo.

33 Na sasa, mnadhani kuwa wana wa nchi hii, waliokuwa kwenye nchi ya ahadi, waliofukuzwa na babu zetu, mnadhani kuwa walikuwa watakatifu? Tazama, nawaambia, Hapana.

34 Je, mnadhania kwamba Baba zetu wangekuwa bora zaidi yao, kama wangekuwa watakatifu? Ninawaambia, Hapana.

35 Tazama, Bwana anawapenda [a]watu wote sawa sawa; yule ambaye ni [b]mtakatifu [c]anapendelewa na Mungu. Lakini tazama, hawa watu walikataa kila neno la Mungu, na walikuwa wamekomaa kwenye maovu; na utimilifu wa ghadhabu ya Mungu ulikuwa juu yao; na Bwana akalaani nchi dhidi yao, na akaibariki kwa babu zetu; ndiyo, alitamka laana dhidi yao kwa maangamizo yao, na akaibariki kwa baba zetu ili wapate mamlaka juu yake.

36 Tazama, Bwana [a]ameumba [b]dunia ili watu [c]waishi ndani yake; na ameumba wanawe ili wairithi.

37 Na [a]huinua taifa takatifu, na kuangamiza mataifa maovu.

38 Na anawaongoza watakatifu kwenye [a]nchi za thamani, na waovu [b]anawaangamiza, na kulaani nchi kwa sababu yao.

39 Anatawala juu mbinguni, kwani ndicho kiti chake cha enzi, na dunia ni [a]kiti chake cha kuegemesha miguu.

40 Na anawapenda wale

29 *a* Ku. 17:6; Hes. 20:11; Kum. 8:15; 1 Ne. 20:21.
30 *a* M&M 18:18; 88:64–65.
b Ku. 32:8; Hes. 14:2–3; Eze. 20:13–16; M&M 84:23–25.
31 *a* Hes. 26:65.
b 1 Ne. 5:15; M&M 103:16–18.
32 *a* Hes. 33:52–53; Yos. 24:8.
35 *a* Mdo. 10:15, 34; Rum. 2:11; 2 Ne. 26:23–33.
b Zab. 55:22; 1 Ne. 22:17.
c 1 Sam. 2:30; Zab. 97:10; 145:20; Alma 13:4; M&M 82:10.
36 *a* MWM Umba, Uumbaji.
b MWM Dunia.
c Isa. 45:18; Ibr. 3:24–25.
37 *a* Mit. 14:34; 1 Ne. 4:13; Eth. 2:10; M&M 117:6.
38 *a* MWM Nchi ya Ahadi.
b Law. 20:22.
39 *a* Isa. 66:1; M&M 38:17; Ibr. 2:7.

ambao watamkubali awe Mungu wao. Tazama, aliwapenda baba zetu na [a]akaagana nao, ndiyo, hata na Ibrahimu, [b]Isaka, na [c]Yakobo; na akakumbuka maagano aliyoagana nao; kwa hivyo, akawatoa kutoka nchi ya [d]Misri.

41 Na aliwanyosha kwa fimbo yake huko nyikani; kwani [a]walishupaza mioyo yao, hata kama ninyi; na Bwana aliwanyosha kwa sababu ya uovu wao. Aliwatumia [b]nyoka wakali warukao miongoni mwao; na baada ya wao kuumwa akawatayarishia njia ya [c]kuponywa; na lile waliopaswa kutenda ni kutazama; na kwa sababu ya [d]wepesi wa njia, au urahisi wake, kulikuwa na wengi walioangamia.

42 Na walishupaza mioyo yao mara kwa mara, na [a]wakamwasi [b]Musa, na pia Mungu; walakini, mnajua kuwa waliongozwa kwa nguvu zake zisizoshindikana hadi wakafika katika nchi ya ahadi.

43 Na sasa, baada ya vitu hivi vyote, wakati umefika kwamba wamekuwa waovu, ndiyo, kupita kiasi; na nafikiri inawezekana leo wanakaribia kuangamizwa; kwani najua siku itafika ambayo lazima waangamizwe, ila tu wachache, ambao watapelekwa utumwani.

44 Kwa hivyo, Bwana [a]alimwamuru baba yangu kukimbilia nyikani; na Wayahudi pia wakajaribu kumtoa uhai; ndiyo, [b]nanyi pia mmejaribu kumtoa uhai wake; kwa hivyo, ninyi ni wauaji mioyoni mwenu na ninyi mnafanana na wao.

45 Ninyi ni [a]wepesi kwa kutenda maovu lakini wanyonge kumkumbuka Bwana Mungu wenu. Mmeona [b]malaika, na akawazungumzia; ndiyo, mmesikia sauti yake mara kwa mara; na amewazungumzia kwa sauti ndogo tulivu, lakini mlikuwa mmekufa [c]ganzi, kwamba hamkupata yale maneno yake; kwa hivyo, amewazungumzia kwa sauti kama radi, ambayo ilisababisha dunia kutetemeka kama ambayo inapasuka.

46 Na pia mnajua kwamba kwa [a]nguvu za neno lake kuu anaweza kusababisha dunia imalizike; ndiyo, na mnajua kwamba kwa neno lake anaweza kusababisha palipopotoka pawe pamenyooka, na paliponyooka pavunjike. Je, kwa nini, basi, muwe wagumu mioyoni mwenu?

47 Tazama, nafsi yangu imevunjwa na uchungu kwa sababu yenu, na moyo wangu unaumwa; nina hofu kwamba mtatupwa milele. Tazama,

40*a* MWM Agano la Ibrahimu.
b Mwa. 21:12; M&M 27:10.
c Mwa. 28:1–5.
d Kum. 4:37.
41*a* 2 Fal. 17:7–23.
b Hes. 21:4–9; Kum. 8:15; Alma 33:18–22.
c Yn. 3:13–15; 2 Ne. 25:20.
d Alma 37:44–47; Hel. 8:15.
42*a* Hes. 14:1–12. MWM Uasi.
b M&M 84:23–24.
44*a* 1 Ne. 2:1–2.
b 1 Ne. 16:37.
45*a* Mos. 13:29.
b 1 Ne. 4:3.
c Efe. 4:19.
46*a* Hel. 12:6–18.

[a]nimejazwa na Roho mtakatifu wa Mungu, hata kwamba kiwiliwili changu [b]hakina nguvu.

48 Na sasa ikawa kwamba nilipozungumza maneno haya walinikasirikia, na walitaka kunitupa katika kilindi cha bahari; na walipokuja kunikamata nikawazungumzia, nikisema: Katika jina la Mwenyezi Mungu, ninawaamuru [a]msiniguse, kwani nimejazwa na [b]nguvu za Mungu, hata kwamba kiwiliwili changu chaweza kuungua; na yeyote atakayenigusa [c]atakauka kama nyasi iliyokauka; na atakuwa bure mbele ya nguvu za Mungu, kwani Mungu atamwadhibu.

49 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwaambia wasilalamike tena juu ya baba yao; wala wasikatae kunitumikia, kwani Mungu aliniamuru nijenge merikebu.

50 Na nikawaambia: [a]Kama Mungu aliniamuru kutenda vitu vyote ningevifanya. Kama ataniamuru niyaambie maji haya, yawe ardhi, yangekuwa ardhi; na kama nikisema, ingetendeka.

51 Na sasa, ikiwa Bwana anazo nguvu nyingi hivyo, na amefanya miujiza mingi miongoni mwa watoto wa watu, je, kwa nini hawezi [a]kunishauri, kwamba nijenge merikebu?

52 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwaambia kaka zangu vitu vingi, mpaka wakafadhaishwa wasiweze kubishana na mimi; wala hawakuthubutu kunigusa kwa mikono yao au vidole vyao, kwa muda wa siku nyingi. Sasa hawakuthubutu kufanya hivyo ili wasikauke mbele yangu, kwani [a]Roho ya Mungu alikuwa na nguvu nyingi; hata wakaguswa.

53 Na ikawa kwamba Bwana aliniambia: Nyosha mkono wako tena kwa kaka zako, na hawatakauka mbele yako, lakini nitawashitua, asema Bwana, na nitafanya hivi, ili wajue kwamba mimi ndimi Bwana Mungu wao.

54 Na ikawa kwamba niliwanyoshea kaka zangu mkono wangu, na hawakukauka mbele yangu; lakini Bwana aliwashitua, kulingana na neno ambalo alikuwa amelizungumza.

55 Na sasa, wakasema: Tunajua kwa hakika kwamba Bwana yuko nawe, kwani tunajua kwamba ni nguvu za Bwana zimetushitua. Na wakainama mbele yangu, na walikuwa karibu [a]kuniabudu, lakini sikuwaruhusu, nikisema: Mimi ni mdogo wenu, ndiyo, hata mdogo wenu mdogo; kwa hivyo, mwabuduni Bwana Mungu wenu, na mheshimu baba yenu na mama yenu, ili [b]maisha yenu yawe marefu katika nchi ambayo Bwana Mungu wenu atawapatia.

47 *a* Mik. 3:8.
b 1 Ne. 19:20.
48 *a* Mos. 13:3.
b 2 Ne. 1:26–27.
MWM Uwezo.
c 1 Fal. 13:4–7.
50 *a* Flp. 4:13; 1 Ne. 3:7.
51 *a* Mwa. 6:14–16; 1 Ne. 18:1.
52 *a* MWM Roho Mtakatifu.
55 *a* Mdo. 14:11–15.
b Ku. 20:12; Mos. 13:20.

MLANGO WA 18

Merikebu inamalizika—Kuzaliwa kwa Yakobo na Yusufu kunatajwa—Kundi lapakia kuelekea nchi ya ahadi—Wana wa Ishmaeli na wake zao wanaungana kwa kuasi na ugomvi—Nefi anafungwa, na merikebu inarudishwa nyuma na dhoruba kubwa—Nefi anaachiliwa huru, na kwa sala zake dhoruba inatulia—Watu wanawasili katika nchi ya ahadi. Karibia mwaka 591–589 K.K.

Na ikawa kwamba walimuabudu Bwana, na wakajiunga na mimi; na tukaunda mbao kwa ufundi maalumu. Na Bwana alinionyesha mara kwa mara namna ya kuunda zile mbao za merikebu.

2 Sasa mimi, Nefi, sikuunda mbao kulingana na njia zilizofahamika kwa watu, wala sikujenga merikebu kulingana na njia za watu; lakini niliijenga kulingana na vile Bwana alivyonionyesha; kwa hivyo, haikuwa kulingana na njia za wanadamu.

3 Na mimi, Nefi, nilienda mlimani mara nyingi, na [a]nilimuomba Bwana mara nyingi; kwa hivyo Bwana [b]alinionyesha vitu vikubwa.

4 Na ikawa kwamba baada ya mimi kumaliza kujenga merikebu, kulingana na neno la Bwana, ndugu zangu waliona kwamba ni nzuri, na ufundi wake ulikuwa stadi; kwa hivyo, [a]wakajinyenyekeza tena kwa Bwana.

5 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana ikamjia baba yangu, kwamba tuinuke na kuingia kwenye merikebu.

6 Na ikawa kwamba kesho yake, baada ya kutayarisha vitu vyote, matunda mengi na [a]nyama kutoka nyikani, na asali nyingi, na maakuli kulingana na yale Bwana aliyotuamuru, tuliingia kwenye merikebu, pamoja na mizigo yetu yote na mbegu zetu, na kitu chochote ambacho tulileta nasi, kila mmoja kulingana na umri wake; kwa hivyo, tuliingia sote kwenye merikebu, pamoja na wake zetu na watoto wetu.

7 Na sasa, baba yangu alikuwa amepata watoto wawili nyikani; mkubwa aliitwa [a]Yakobo na mdogo alikuwa ni [b]Yusufu.

8 Na ikawa kwamba baada ya sisi sote kuingia kwenye merikebu, na kuchukua maakuli yetu na vitu ambavyo tuliamriwa, tulitweka [a]baharini na tukaendeshwa mbele na upepo tukielekea [b]nchi ya ahadi.

9 Na baada ya sisi kuendeshwa na upepo kwa muda wa siku nyingi, tazama, kaka zangu na wana wa Ishmaeli pia na wake zao walianza kujifurahisha, hata wakaanza kucheza ngoma, na kuimba, na kuzungumza kwa ujeuri sana, ndiyo, hata kwamba wakasahau kwa nguvu gani waliletwa hapo; ndiyo, waliinuliwa zaidi kwa ujeuri.

18 3*a* MWM Sala.
b MWM Ufunuo.
4*a* 1 Ne. 16:5.
6*a* 1 Ne. 17:2.
7*a* 2 Ne. 2:1.
b 2 Ne. 3:1.
8*a* 2 Ne. 10:20.
b 1 Ne. 2:20.
MWM Nchi ya Ahadi.

10 Na mimi, Nefi, nikaanza kuogopa zaidi kwamba Bwana atatukasirikia, na atupige kwa sababu ya uovu wetu, hata tuzame kwenye kilindi cha bahari; kwa hivyo, mimi, Nefi, nilianza kuwazungumzia kwa makini; lakini tazama [a]walinikasirikia, wakisema: Hatutakubali kuwa mdogo wetu awe [b]mtawala wetu.

11 Na ikawa kwamba Lamani na Lemueli walinikamata na kunifunga kwa kamba, na wakawa wakali sana kwangu; walakini, Bwana [a]alikubali haya ili aonyeshe nguvu zake, kwa kutimiza maneno yake aliyosema kuhusu wale waovu.

12 Na ikawa kwamba waliponifunga hata nisingeweza kutembea, [a]dira, ambayo Bwana alikuwa ameitayarisha, ilikoma kufanya kazi.

13 Kwa hivyo, hawakujua njia gani ambayo wangeelekeza merikebu, hata mpaka kukawa na dhoruba kubwa, ndiyo, dhoruba kuu na kali, na [a]tukarudishwa nyuma majini kwa muda wa siku tatu; na wakaanza kuogopa kupita kiasi kwamba watazama baharini; walakini hawakunifungua.

14 Na baada ya kurudishwa nyuma kwa siku nne, dhoruba ilianza kuwa kali zaidi.

15 Na ikawa kwamba tulikuwa karibu kumezwa kilindini mwa bahari. Na baada ya kurudishwa nyuma katika maji kwa muda wa siku nne, kaka zangu wakaanza [a]kuona kwamba hukumu za Mungu zilikuwa juu yao, na kwamba lazima wafe kama hawatatubu maovu yao; kwa hivyo, wakanijia na kunifungua kamba ambazo zilikuwa kwenye viwiko vyangu, na tazama vilikuwa vimefura zaidi; na pia vifundo vyangu vilivimba sana, na uchungu ulikuwa mwingi.

16 Walakini, nilimtazama Mungu wangu, na [a]nilimsifu siku yote nzima; na sikumlalamikia Bwana kwa sababu ya masumbuko yangu.

17 Sasa baba yangu, Lehi, alikuwa amewaambia vitu vingi, na pia kwa wana wa [a]Ishmaeli; lakini, tazama, walitoa vitisho vingi kwa yeyote ambaye alinitetea; na wazazi wangu wakiwa na umri mkuu, na wakiwa wameteseka kwa hofu kuu kwa sababu ya wana wao, walilemewa, ndiyo, hadi wakaugulia vitandani.

18 Kwa sababu ya hofu yao na huzuni nyingi, na maovu ya kaka zangu, walikaribia kukutana na Mungu wao; ndiyo, mvi zao zilikaribia kulazwa mavumbini; ndiyo, hata karibu watupwe na huzuni katika kaburi la maji.

19 Na Yakobo na Yusufu pia, wakiwa wachanga, na wakihitaji kulishwa sana, walihu-

10*a* 1 Ne. 17:17–55.
b Mwa. 37:9–11; 1 Ne. 16:37–38; 2 Ne. 1:25–27.
11*a* Alma 14:11.
12*a* 1 Ne. 16:10, 16, 26; 2 Ne. 5:12; Alma 37:38–47; M&M 17:1.
13*a* Mos. 1:17.
15*a* Hel. 12:3.
16*a* Alma 36:28.
17*a* 1 Ne. 7:4–20.

zunishwa na masumbuko ya mama yao; pia na [a]mke wangu na machozi yake na sala, na pia watoto wangu, hawakulainisha mioyo ya kaka zangu ili wanifungue.

20 Na hapakuwa chochote ila nguvu za Mungu, zilizowatisha na maangamizo, kingelainisha mioyo yao; kwa hivyo, walipoona kwamba walikuwa karibu kuzama baharini walitubu kwa kitu kile ambacho walitenda, hata wakanifungua.

21 Na ikawa kwamba baada ya wao kunifungua, tazama, nilichukua dira, na ilitenda nilivyotaka. Na ikawa kwamba nikamwomba Bwana; na baada ya mimi kusali, upepo ulikoma, na dhoruba ikaisha, na kukawa na utulivu mkuu.

22 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliendesha merikebu, hata tukasafiri tena tukielekea nchi ya ahadi.

23 Na ikawa kwamba baada ya kusafiri kwa muda wa siku nyingi tuliwasili katika [a]nchi ya ahadi; na tukatembea kwenye ardhi, na tukapiga hema zetu; na tukaiita nchi ya ahadi.

24 Na ikawa kwamba tulianza kulima ardhi, na tukaanza kupanda mbegu; ndiyo, tulitia mbegu zetu zote udongoni, tulizokuwa tumebeba kutoka nchi ya Yerusalemu. Na ikawa kwamba zilimea zaidi; kwa hivyo, tukapata baraka tele.

25 Na ikawa kwamba tuliposafiri nyikani, tulipata katika nchi ya ahadi, wanyama huko porini wa kila aina, ngombe na dume, na punda na farasi, na mbuzi wa nyumbani na mbuzi wa kichaka, na kila aina ya wanyama wa mwitu, ambao walimfaidisha mwanadamu. Na tukapata kila aina ya mawe yenye madini, ya dhahabu, na ya fedha, na shaba nyekundu.

MLANGO WA 19

Nefi anatengeneza mabamba ya madini na kuandika historia ya watu wake—Mungu wa Israeli atakuja baada ya miaka mia sita tangu Lehi kutoka Yerusalemu—Nefi anaelezea kuhusu mateso Yake na kusulubiwa Kwake—Wayahudi watadharauliwa na kutawanywa hadi siku za baadaye, wakati watamrudia Bwana. Karibia mwaka 588–570 K.K.

Na ikawa kwamba Bwana akaniamuru, kwa hivyo nilitengeneza mabamba ya mawe yenye madini ili nichore juu yake maandishi ya watu wangu. Na kwenye yale [a]mabamba ambayo nilitengeneza, niliandika maandishi ya baba yangu, na pia safari zetu nyikani, na unabii wa [b]baba yangu; na pia unabii wangu mwingi mwenyewe nimeuandika hapo.

2 Na sikujua ule wakati nilipoyatengeneza kwamba nitaamriwa na Bwana kuyatengeneza [a]mabamba haya; kwa hivyo, maandishi ya baba yangu, na nasaba ya baba zake, na mengi kuhusu yaliyotupata huko nyikani yamechorwa kwenye

19*a* 1 Ne. 7:19; 16:7.
23*a* MWM Nchi ya Ahadi.

19 1*a* MWM Mabamba.
b 1 Ne. 1:16–17; 6:1–3.

2*a* 2 Ne. 5:30.

yale mabamba ya kwanza nilizoyazungumzia; kwa hivyo, vitu vilivyotukia kabla ya kutengeneza [b]mabamba haya, kwa kweli, vimeelezwa zaidi kwenye yale mabamba ya kwanza.

3 Na baada ya kutengeneza mabamba haya kwa amri, mimi, Nefi, nilipokea amri kwamba ile huduma na unabii, sehemu zake zilizo wazi zaidi na zenye thamani, ziandikwe katika [a]mabamba haya; na kwamba vitu vilivyoandikwa vihifadhiwe kwa kuwashauri watu wangu, ambao watamiliki nchi, na pia kwa sababu zingine zenye [b]hekima, sababu ambazo zinajulikana na Bwana.

4 Kwa hivyo, mimi, Nefi, niliandika maandishi kwenye yale mabamba mengine, ambayo yanaeleza, au ambayo yanafafanua zaidi kuhusu vita na mabishano na maangamizo ya watu wangu. Na nimetenda hivi, na kuwaamuru watu wangu kile watakachofanya baada mimi kuaga dunia; na kwamba mabamba haya yapitishwe kutoka kizazi kimoja hadi kingine, au kutoka nabii mmoja hadi kwa mwingine, mpaka Bwana atakapoamuru vingine.

5 Na maelezo ya [a]utengenezaji wa mabamba haya utaelezwa hapo baadaye; na kisha, tazama, nitaendelea kulingana na yale ambayo nimezungumza; na ninafanya haya ili yale ambayo ni matakatifu zaidi [b]yahifadhiwe kwa ufahamu wa watu wangu.

6 Walakini, siandiki chochote kwenye mabamba haya, ila tu kile ambacho nafikiri ni [a]kitakatifu. Na sasa, kama nitakosea, wale nao ambao walinitangulia walikosea; sio ati kwamba nitajihalalisha mwenyewe kwa sababu ya watu wengine, lakini ni kwa sababu ya [b]unyonge ulio ndani yangu, kulingana na mwili, nitajihalalisha.

7 Kwani vitu ambavyo watu wengine wanafikiria ni vya thamani kuu, kwa mwili na kwa nafsi, wengine [a]wanavidharau na kuvikanyaga miguuni mwao. Ndiyo, hata yule Mungu wa Israeli watu [b]humkanyaga miguuni; nasema, kumkanyaga miguuni mwao lakini ningezungumza kwa maneno mengine—wanamdharau, na hawasikilizi sauti ya mawaidha yake.

8 Na tazama [a]anakuja, kulingana na maneno ya malaika, baada ya miaka [b]mia sita tangu baba yangu alipotoka Yerusalemu.

9 Na ulimwengu, kwa sababu ya uovu wao, utamhukumu kuwa jambo la dharau; kwa

2*b* 1 Ne. 9:1–5.
3*a* Yak. (KM) 1:1–4; 3:13–14; 4:1–4.
b 1 Ne. 9:4–5; M. ya Morm. 1:7; M&M 3:19–20; 10:1–51.
5*a* 2 Ne. 5:28–33.
b MWM Maandiko—Maandiko yahifadhiwe.
6*a* Tazama ukurasa wenye jina la Kitabu cha Mormoni. MWM Takatifu.
b Morm. 8:13–17; Eth. 12:23–28.
7*a* 2 Ne. 33:2; Yak. (KM) 4:14.
b MWM Uasi.
8*a* MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.
b 1 Ne. 10:4; 2 Ne. 25:19.

hivyo wanampiga kwa mijeledi, na anavumilia; na wanamchapa, na anavumilia. Ndiyo, na [a]wanamtemea mate, na anavumilia, kwa sababu ya upendo wake mkarimu na subira yake kwa watoto wa watu.

10 Na [a]Mungu wa baba zetu, ambao [b]walitolewa Misri, kutoka utumwani, na pia wakahifadhiwa nyikani na yeye, ndiyo, [c]Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka, na Mungu wa Yakobo, kulingana na maneno ya malaika, kama mtu, [d]anajikabidhi mikononi mwa watu waovu, ili [e]ainuliwe, kulingana na maneno ya [f]Zenoki, na [g]kusulubiwa, kulingana na maneno ya Neumu, na kuzikwa [h]kaburini, kulingana na maneno ya [i]Zeno, ambayo alizungumza kuhusu zile siku tatu za [j]giza, ambazo zitakuwa ni ishara imetolewa ya kifo chake kwa wale watakaoishi katika visiwa vya bahari, muhimu zaidi itatolewa kwa wale ambao ni wa [k]nyumba ya Israeli.

11 Kwa hivyo alizungumza nabii: Kwa hakika Bwana Mungu [a]atatembelea nyumba yote ya Israeli katika siku ile, wengine kwa sauti yake, kwa sababu ya haki yao, kwa shangwe yao kuu na wokovu wao, na wengine kwa [b]radi na umeme wa nguvu zake, kwa dhoruba, kwa moto, na kwa moshi, na ukungu wa [c]giza, na kwa upasukaji wa [d]ardhi, na kwa [e]milima ambayo itainuliwa.

12 Na hivi vitu [a]vyote lazima vitimizwe, asema nabii [b]Zeno. Na [c]miamba ya ardhi lazima ipasuke; na kwa sababu ya mingurumo ya dunia, wafalme wengi wa visiwa vya bahari watashawishiwa na Roho ya Mungu, kupaza sauti: Mungu wa asili anateseka.

13 Na kwa wale ambao watakuwa Yerusalemu, asema nabii, [a]watapigwa kwa mijeledi na watu wote, kwa sababu [b]wanamsulubu Mungu wa Israeli, na kugeuza mioyo yao upande, wakikataa ishara na maajabu, na nguvu na utukufu wa Mungu wa Israeli.

14 Na kwa sababu wanageuza mioyo yao upande, asema nabii, na [a]wamemdharau yule

9 *a* Isa. 50:5–6; Mt. 27:30.
10 *a* 2 Ne. 26:12; Mos. 7:27; 27:30–31; Alma 11:38–39; 3 Ne. 11:14–15.
b Ku. 3:2–10; 6:6; 1 Ne. 5:15; M&M 136:22.
c Mwa. 32:9; Mos. 7:19; M&M 136:21. MWM Yehova.
d MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
e 3 Ne. 27:14.
f Alma 33:15; 34:7; Hel. 8:19–20; 3 Ne. 10:15–16. MWM Maandiko—Maandiko yaliyopotea; Zenoki.
g 2 Ne. 6:9; Mos. 3:9. MWM Kusulubiwa.
h Mt. 27:60; Lk. 23:53; 2 Ne. 25:13.
i Yak. (KM) 6:1; Hel. 15:11. MWM Zeno.
j 1 Ne. 12:4–5; Hel. 14:20, 27; 3 Ne. 8:3, 19–23; 10:9.
k 3 Ne. 16:1–4.
11 *a* 3 Ne. 9; M&M 5:16.
b Hel. 14:20–27; 3 Ne. 8:5–23.
c Lk. 23:44–45; 3 Ne. 8:19–20.
d 2 Ne. 26:5.
e 3 Ne. 8:10.
12 *a* Hel. 14:20–28.
b Yak. (KM) 5:1.
c Mt. 27:51.
13 *a* Lk. 23:27–30.
b 2 Ne. 10:3.
14 *a* Isa. 53:3–6; Mos. 14:3–6.

Mtakatifu wa Israeli, wataran-daranda maishani mwao, na kuangamia, na kuwa wa [b]kufanyiwa mzaha na [c]kutukanwa, na kuchukiwa miongoni mwa mataifa yote.

15 Walakini, wakati siku ile itafika, asema nabii, kwamba [a]hawatageuza tena mioyo yao upande kinyume cha yule Mtakatifu wa Israeli, ndipo atakumbuka [b]maagano ambayo aliagana na baba zao.

16 Ndiyo, ndipo atakumbuka [a]visiwa vya bahari; ndiyo, na watu wote ambao ni wa nyumba ya Israeli [b]nitawakusanya, asema Bwana, kutoka pembe nne za ulimwengu, kulingana na maneno ya nabii Zeno.

17 Ndiyo, na ulimwengu wote [a]utaona wokovu wa Bwana, asema nabii; kila taifa, kabila, lugha, na watu watabarikiwa.

18 Na mimi, Nefi, nimewaandikia watu wangu vitu hivi, ili pengine niwashawishi wamkumbuke Bwana Mkombozi wao.

19 Kwa hivyo, nazungumza kwa nyumba yote ya Israeli, kama watapokea [a]hivi vitu.

20 Kwani tazama, nina jambo rohoni, ambalo limenichosha hata kwamba viungo vyangu vyote vimenyong'onyea, kwa wote ambao wako Yerusalemu; kwani ikiwa Bwana hakuwa na huruma, na kunionyesha yaliyowahusu, kama hata wale manabii wa kale, pia nami ningeangamia.

21 Na kwa hakika aliwaonyesha [a]manabii wa kale vitu vyote [b]vilivyowahusu; na pia alionyesha wengi yaliyotuhusu; kwa hivyo, ni lazima tujue yaliyowahusu kwani yameandikwa katika mabamba ya shaba nyeupe.

22 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwafundisha kaka zangu vitu hivi; na ikawa kwamba niliwasomea vitu vingi, vilivyochorwa kwenye yale [a]mabamba ya shaba nyeupe, ili wajue kuhusu vitendo vya Bwana katika nchi zingine, miongoni mwa watu wa kale.

23 Na niliwasomea vitu vingi ambavyo viliandikwa kwenye [a]vitabu vya Musa; lakini ili niwashawishi kabisa wamwamini Bwana Mkombozi wao niliwasomea yale ambayo yaliandikwa na nabii [b]Isaya; kwani [c]nililinganisha maandiko yote nasi, ili [d]yatufaidishe na kutuelimisha.

24 Kwa hivyo niliwazungumzia, nikisema: Sikizeni maneno ya nabii, ninyi ambao ni baki la nyumba ya Israeli, [a]tawi ambalo

14 *b* MWM Wayahudi.
c Kum. 28:37; 1 Fal. 9:7; 3 Ne. 16:9.
15 *a* 1 Ne. 22:11–12.
b MWM Agano la Ibrahimu.
16 *a* 1 Ne. 22:4; 2 Ne. 10:21.
b Isa. 49:20–22. MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
17 *a* Isa. 40:4–5.
19 *a* Eno. 1:16; Morm. 5:12; 7:9–10.
21 *a* 2 Fal. 17:13; Amo. 3:7. MWM Nabii.
b 3 Ne. 10:16–17.
22 *a* 1 Ne. 22:1.
23 *a* Ku. 17:14; 1 Ne. 5:11; Musa 1:40–41.
b 1 Ne. 15:20; 2 Ne. 25:4–6; 3 Ne. 23:1.
c MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
d 2 Ne. 4:15.
24 *a* Mwa. 49:22–26; 1 Ne. 15:12; 2 Ne. 3:4–5.

wamevunjwa; sikilizeni maneno ya nabii, ambayo yaliandikiwa nyumba yote ya Israeli, na myalinganishe nanyi, ili mpate matumaini vile vile na ndugu zenu ambao mlitawanyika kutoka kwao; kwani hivi ndivyo nabii ameandika.

MLANGO WA 20

Bwana anafunua makusudi Yake kwa Israeli—Israeli imechaguliwa kutoka katika tanuri la masumbuko na linapaswa kuondoka kutoka Babeli—Linganisha Isaya 48. Karibia mwaka 588–570 K.K.

Sikilizeni na msikie haya, Ee nyumba ya Yakobo, ambao wanajulikana kwa jina la Israeli, na wametoka katika maji ya Yuda, au kutoka kwenye maji ya [a]ubatizo, ambao wanaapa kwa jina la Bwana, na kutaja Mungu wa Israeli, walakini hawaapi kwa ukweli wala kwa haki.

2 Walakini, wanajiita wakaazi wa [a]mji mtakatifu, lakini hawamtegemei Mungu wa Israeli, ambaye ni Bwana wa Majeshi; ndiyo, jina lake ni Bwana wa Majeshi.

3 Tazama, nimetangaza vitu vilivyokuja [a]awali kutoka mwanzoni; na yalitoka kinywani mwangu, na niliyadhihirisha. Niliyadhihirisha kwa ghafla.

4 Na niliitenda kwa sababu nilijua kwamba [a]wewe ni mkaidi, na shingo yako ni ngumu kama chuma, na paji lako kama shaba nyeupe;

5 Na nimekutangazia hata tangu mwanzo, kabla hayajakuwa niliyaonyesha kwako; na nilikuonyesha usije ukasema—[a]Sanamu yangu imezitenda, na mfano uliochongwa wangu, na mfano ulioyeyushwa wangu ndiyo imeziamuru.

6 Umeona na kusikia haya yote; na je wewe hutayatangaza? Na kwamba nimekuonyesha vitu vipya tangu wakati huu, hata vitu vilivyofichwa, na wewe hukuvijua.

7 Yameumbwa sasa, na si tangu mwanzo, hata kabla ya ile siku ambayo hukuyasikia yalikuwa yametangazwa kwako, ili usiseme—Tazama niliyajua.

8 Ndiyo, na wewe hukusikia; ndiyo, wewe hukujua; ndiyo, tangu ule wakati sikio lako halikufunguliwa; maana nilijua kwamba ungetenda uhaini, na ulikuwa [a]mvunja sheria kutoka tumboni.

9 Walakini, kwa sababu ya heshima ya [a]jina langu nitazuia ghadhabu yangu, na kwa sababu ya sifa zangu nitajizuia kutokana nawe, kwamba nisikuangamize.

10 Kwani, tazama, nimekutakasa, nimekuchagua kutoka karibu ya [a]masumbuko.

11 Kwa heshima yangu, ndiyo, kwa heshima yangu nitatenda hii, kwani sitakubali [a]jina

20 1*a* MWM Batiza, Ubatizo.
2*a* Isa. 52:1.
MWM Yerusalemu.
3*a* Isa. 46:9–10.
4*a* MY Israeli.
5*a* MWM Kuabudu sanamu.
8*a* Zab. 58:3.
9*a* 1 Sam. 12:22; Zab. 23:3; 1 Yoh. 2:12.
10*a* MWM Shida.
11*a* Yer. 44:26.

langu lichafuliwe, na [b]sitampatia mwingine utukufu wangu.

12 Nisikilize mimi, Ee Yakobo, na Israeli wateule wangu, kwani Mimi ndimi yeye; Mimi ndimi wa [a]kwanza, na pia Mimi ndimi wa mwisho.

13 Mkono wangu pia [a]umejenga msingi wa dunia, na mkono wangu wa kuume umetandaza mbingu. Naziita na zinasimama pamoja.

14 Ninyi nyote, kusanyikeni, na msikie; ni nani miongoni mwao amewatangazia vitu hivi? Bwana amempenda; ndiyo, na [a]atatimiza neno lake ambalo amesema kupitia kwao; na atatendea [b]Babilonia nia yake, na mkono wake utanyoshewa Wakaldayo.

15 Pia, Bwana asema; mimi, Bwana, ndiyo, nimesema; ndiyo, nimemuita kutangaza, nimemleta, na atafanikiwa katika njia zake.

16 Njooni karibu na mimi; sijazungumza kwa [a]siri; tangu mwanzo, tangu ilipotangazwa nimezungumza; na Bwana Mungu, na Roho yake, amenituma.

17 Na hivyo ndivyo asemavyo Bwana, [a]Mkombozi wenu, Mtakatifu wa Israeli; nimemtuma, Bwana Mungu wenu anayekufundisha kufaidika, ambaye [b]anakuongoza katika njia inayokupasa, ameitenda.

18 Ee kwamba ungesikiliza [a]amri zangu—basi amani yako ingekuwa kama mto, na haki yako ungekuwa kama mawimbi ya bahari.

19 [a]Uzao wako ungekuwa pia kama mchanga; na kizazi cha matumbo yenu ingekuwa kama changarawe yake; jina lake halingetupiliwa mbali wala kuangamizwa kutoka mbele yangu.

20 [a]Tokeni kutoka Babilonia, waondokeeni Wakaldayo, kwa sauti ya kuimba tangazeni ninyi, semeni haya, ambieni hadi mwisho wa ulimwengu; semeni ninyi; Bwana amemkomboa [b]mtumishi wake Yakobo.

21 Na hawakuona [a]kiu; aliwaongoza katika majangwa; akasababisha maji kutiririka kutoka kwenye [b]mwamba kwa sababu yao; alipasua mwamba pia na maji yakatoka.

22 Ingawa ametenda haya yote, na makuu pia, hakuna [a]amani, asema Bwana, kwa waovu.

MLANGO WA 21

Masiya atakuwa nuru ya Wayunani na atawafungua wafungwa—Israeli itakusanywa kwa uwezo katika siku za mwisho—Wafalme

11 *b* Isa. 42:8; Musa 4:1–4.
12 *a* Ufu. 1:17; 22:13. MWM Alfa na Omega; Mzaliwa wa Kwanza.
13 *a* Zab. 102:25. MWM Umba, Uumbaji.
14 *a* 1 Fal. 8:56; M&M 64:31; 76:3.
b MWM Babeli, Babilonia.
16 *a* Isa. 45:19.
17 *a* MWM Mkombozi.
b MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi; Ufunuo.
18 *a* Mh. 8:5.
19 *a* Mwa. 22:15–19; Hos. 1:10.
20 *a* Yer. 51:6; M&M 133:5–14.
b Isa. 44:1–2, 21.
21 *a* Isa. 41:17–20.
b Ku. 17:6; Hes. 20:11; 1 Ne. 17:29; 2 Ne. 25:20.
22 *a* MWM Amani.

watakuwa baba zao walezi—Linganisha Isaya 49. Karibia mwaka 588–570 K.K.

Na tena: Sikiliza, Ee ninyi nyumba ya Israeli, nyote ambao mmetenganishwa na kufukuzwa kwa sababu ya uovu wa wachungaji wa watu wangu; ndiyo, ninyi nyote ambao mmetenganishwa, na kutawanywa ugenini, wale ambao ni wa watu wangu, Ee nyumba ya Israeli. Sikilizeni, Ee [a]visiwa, nisikilizeni mimi, na watu walio [b]mbali pia sikilizeni; Bwana ameniita kabla sijazaliwa, kutoka tumboni mwa mama yangu, ametaja jina langu.

2 Na amefanya kinywa changu kuwa kama upanga mkali; amenificha katika kivuli cha mkono wake, na akanifanya mshale uliong'aa; amenificha katika podo lake.

3 Na akaniambia: Wewe ndiye [a]mtumishi wangu, Ee Israeli, ambaye nitatukuzwa ndani yake.

4 Kisha nikasema, nimefanya kazi bure, nimetumia nguvu zangu bure na bila faida; kwa hakika hukumu yangu iko na Bwana, na vitendo vyangu na Mungu wangu.

5 Na sasa, asema Bwana—ambaye [a]aliniumba kutoka tumboni ili niwe mtumishi wake, kumrejesha Yakobo kwake tena—ingawa Israeli haijakusanyika, bado nitakuwa mwenye utukufu machoni mwa Bwana, na Mungu wangu atakuwa nguvu yangu.

6 Na alisema: Ni kitu rahisi kuwa wewe uwe mtumishi wangu ili uinue [a]makabila ya Yakobo, na kurudisha waliohifadhiwa kutoka Israeli. Nitakufanya pia uwe [b]nuru kwa [c]Wayunani, kwamba uwe wokovu wangu hadi mwisho wa ulimwengu.

7 Hivyo ndivyo asemavyo Bwana, Mkombozi wa Israeli, Mtakatifu wake, kwa yule anayechukiwa na watu, kwa yule anaye dharauliwa na mataifa, kwa mtumishi wa watawala: Wafalme wataona na kuinuka, wana wa wafalme pia wataabudu, kwa sababu ya Bwana ambaye ni mwaminifu.

8 Hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Kwa wakati uliokubalika nimekusikia, Ee visiwa vya bahari, na kwa siku ya wokovu nilikusaidia; na nitakuhifadhi, na ninakupatia [a]mtumishi wangu uwe agano la watu, kuimarisha nchi, kuwasababisha kurithi makao yaliokuwa yenye ukiwa.

9 Ili uwaambie [a]wafungwa: Ondokeni; kwa wale ambao wanaketi [b]gizani: Jidhihirisheni. Watakula njiani, na [c]malisho yao yatakuwa juu ya majabali.

21 1*a* 1 Ne. 22:4; 2 Ne. 10:20–22.
b M&M 1:1.
3*a* Law. 25:55; Isa. 41:8; M&M 93:45–46.
5*a* Isa. 44:24.
6*a* MWM Israeli—Makabila kumi na mawili ya Israeli.
b M&M 103:8–10; Ibr. 2:10–11.
c 3 Ne. 21:11.
8*a* 2 Ne. 3:6–15; 3 Ne. 21:8–11; Morm. 8:16, 25.
9*a* MWM Wokovu kwa ajili ya Wafu.
b 2 Ne. 3:5.
c Eze. 34:14.

10 Hawataona njaa wala kiu, wala joto au jua kuwachoma; kwani yule anayewarehemu atawaongoza, hata kwenye chemchemi za maji atawaongoza.

11 Na nitafanya milima yangu yote iwe [a]njia, na njia zangu zitainuliwa.

12 Na kisha, Ee nyumba ya Israeli, tazama, [a]haya yatatoka mbali; na tazama, haya kutoka kaskazini na kutoka magharibi; na haya kutoka nchi ya Sinimu.

13 [a]Imbeni, Ee mbingu; na ushangilie, Ee dunia; kwani miguu ya wale ambao wako mashariki itaimarishwa; na anzeni kuimba, Ee milima; kwani hawatapigwa tena; kwani Bwana amewafariji watu wake, na atawarehemu wanaosumbuka.

14 Lakini, tazama, Sayuni imesema: Bwana ameniacha, na Bwana wangu amenisahau—lakini ataonyesha kwamba hajafanya hivyo.

15 Kwani [a]mwanamke anaweza kusahau mtoto wake ambaye anamnyonyesha, kwamba asiwe na huruma kwa mwana wa tumbo lake? Ndiyo, wanaweza [b]kusahau, lakini sitakusahau, Ee nyumba ya Israeli.

16 Tazama, nimekuchora [a]viganjani mwa mikono yangu; kuta zako daima ziko mbele yangu.

17 Watoto wako wataharakisha dhidi ya waharibifu wako; na wale [a]waliokuharibu wataondoka kutoka kwako.

18 Inua macho yako pande zote na utazame; hawa wote [a]wanakusanyika pamoja, na watakuja kwako. Na vile ninavyoishi, Bwana asema, wewe utajivika na wao wote, kama pambo, na kujifunga kwao kama bibi arusi.

19 Kwani utupu wako na kwenye ukiwa, na nchi yako ya maangamizo, itakuwa hata sasa nyembamba kwa sababu ya wakazi; na wale ambao walikumeza watakuwa mbali.

20 Watoto utakaopata, baada ya kupoteza wale wa kwanza, watasema tena masikioni mwako: Hapa mahali ni [a]padogo sana kwangu; nipe mahali ili niishi.

21 Kisha [a]utasema moyoni mwako: Nani alinizalia hawa, akiona nimepoteza watoto wangu, na nina [b]ukiwa, mtumwa, na akizurura hapa na pale? Nani amelea hawa? Tazama, niliachwa pekee yangu; hawa, walikuwa wapi?

22 Hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu: Tazama, nitawanyooshea [a]Wayunani mkono wangu, na nitapeperusha [b]bendera yangu miongoni mwa watu; na wataleta wana wako kwa [c]mikono yao, na mabinti zako watabebwa mabegani mwao.

11 *a* Isa. 62:10; M&M 133:23–32.
12 *a* Isa. 43:5–6.
13 *a* Isa. 44:23.
15 *a* MWM Mwanamke, Wanawake.
b Isa. 41:17; Alma 46:8; M&M 61:36.
16 *a* Zek. 13:6.
17 *a* 3 Ne. 21:12–20.
18 *a* Mik. 4:11–13.
20 *a* AU yenye kubana, au nyembamba.
21 *a* MY Sayuni.
b Isa. 54:1; Gal. 4:27.
22 *a* Isa. 66:18–20.
b Isa. 11:12; 18:3.
c 1 Ne. 22:8; 2 Ne. 10:8–9.

23 Na [a]wafalme watakuwa baba zako walezi, nao malkia wao watakuwa mama zako [b]walezi; watainama mbele yako nyuso zao zikiielekea ardhi, na kuramba mavumbi ya miguu yako; na utajua kwamba mimi ni Bwana; kwani hawataaibika [c]wanaoningojea.

24 Kwani mateka watanyakuliwa kutoka kwa shupavu, au [a]watumwa halali kukombolewa?

25 Lakini hivyo ndivyo asemavyo Bwana, hata watumwa wa shupavu watachukuliwa, na mateka wa wale walio wa kutisha watakombolewa; kwani nitashindana na yule anayeshindana nawe, na nitaokoa watoto wako.

26 Na [a]nitawalisha wanaokudhulumu kwa nyama yao wenyewe; watalewa kwa damu yao wenyewe kama kwa mvinyo mtamu; na watu wote [b]watajua kwamba mimi, Bwana, ni Mwokozi wenu na Mkombozi wenu, [c]Mwenyezi Mkuu wa Yakobo.

MLANGO WA 22

Israeli itatawanyika kote usoni mwa ulimwengu—Wayunani watalea na kulisha Israeli kwa injili katika siku za mwisho—Israeli itakusanywa na kuokolewa, na waovu wataungua kama kapi—Ufalme wa ibilisi utaangamizwa, na Shetani atafungwa. Karibia mwaka 588–570 K.K.

Na sasa ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kuvisoma vitu hivi vilivyochorwa kwenye [a]mabamba ya shaba nyeupe, kaka zangu walinijia na kuniambia: Nini maana ya vitu hivi ambavyo umevisoma? Tazama, je, vitaeleweka kulingana na vitu vya kiroho, ambavyo vitatimizwa kulingana na roho na sio mwili?

2 Na mimi, Nefi, niliwaambia: Tazama [a]vilidhirihishwa kwa nabii kwa sauti ya [b]Roho; kwani kwa Roho vitu vyote vinafunuliwa kwa [c]manabii, ambavyo vitawajia watoto wa watu kulingana na mwili.

3 Kwa hivyo, vitu ambavyo nimesoma ni vitu vinavyolingana na vitu vya [a]muda na vya kiroho; kwani inaonekana kwamba nyumba ya Israeli, sasa au baadaye, [b]itatawanyika usoni mwote mwa dunia, na pia miongoni mwa mataifa yote.

4 Na tazama, tayari kuna wengi ambao wamepotea kutokana na ufahamu wa wale ambao walioko Yerusalemu. Ndiyo, sehemu kubwa ya [a]makabila

23*a* Isa. 60:16.
b 1 Ne. 22:6.
c 2 Ne. 6:13; M&M 98:2; 133:10–11, 45.
24*a* 1 Ne. 21:25.
26*a* 1 Ne. 22:13–14.
b Mos. 11:22.
c MWM Yehova.

22 1*a* 1 Ne. 19:22; 2 Ne. 4:2.
2*a* 2 Pet. 1:19–21.
b MWM Roho Mtakatifu.
c MWM Toa unabii, Unabii.
3*a* M&M 29:31–34.
b 1 Ne. 10:12–14; 2 Ne. 25:14–16.
MWM Israeli—Kutawanyika kwa Israeli.
4*a* MWM Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea.

yote [b]yamepotoshwa; na yametawanyika hapa na pale katika [c]visiwa vya bahari; na pale yalipo hakuna yeyote baina yetu ajuaye, ila tunajua kwamba yamepotoshwa.

5 Na kwa vile wamepotoshwa, vitu hivi vimetabiriwa juu yao, na pia kuhusu wale wote ambao watatawanywa baadaye na kuchanganyika, kwa sababu ya yule Mtakatifu wa Israeli; kwani watashupaza mioyo yao dhidi yake; kwa hivyo, watatawanywa miongoni mwa mataifa yote na [a]watachukiwa na watu wote.

6 Walakini, baada ya wao [a]kulelewa na [b]Wayunani, na Bwana kunyoshea Wayunani mkono wake na kuwainua kama bendera, na [c]watoto wao wamebebwa mikononi mwao, na mabinti zao wamebebwa mabegani mwao, tazama vitu hivi ambavyo vimezungumziwa ni vya muda; kwani hayo ndiyo maagano ya Bwana na baba zetu; na inatuhusu katika siku zijazo, na pia kaka zetu wote ambao ni wa nyumba ya Israeli.

7 Na inamaanisha kwamba wakati unafika kwamba baada ya nyumba yote ya Israeli kutawanywa na kuchanganywa, kwamba Bwana Mungu atainua taifa shupavu miongoni mwa [a]Wayunani, ndiyo, hata usoni mwa nchi hii; na kwa wao uzao wetu [b]utatawanywa.

8 Na baada ya uzao wetu kutawanywa Bwana Mungu ataanza kutenda kazi ya [a]maajabu miongoni mwa [b]Wayunani, ambayo itakuwa ya [c]thamani kubwa kwa uzao wetu; kwa hivyo, unalinganishwa na wao wakilishwa na Wayunani na wakibebwa mikononi mwao na mabegani mwao.

9 Na pia itakuwa yenye [a]thamani kwa Wayunani; na sio tu kwa Wayunani lakini [b]kwa [c]nyumba yote ya Israeli, kwa kujulisha [d]maagano ya Baba wa Mbingu kwa Ibrahimu, akisema: Katika [e]uzao wako makabila yote ya dunia [f]yatabarikiwa.

10 Na ningetaka, kaka zangu, kwamba mngejua kwamba makabila yote ya dunia hayawezi kubarikiwa isipokuwa aweke mkono wake [a]wazi machoni mwa mataifa.

11 Kwa hivyo, Bwana Mungu ataendelea kuweka mkono wake wazi machoni mwa mataifa yote, katika kutimiza maagano yake na injili yake kwa wale ambao ni wa nyumba ya Israeli.

4 *b* 2 Ne. 10:22.
c 1 Ne. 21:1; 2 Ne. 10:8, 20.
5 *a* 1 Ne. 19:14.
6 *a* 1 Ne. 21:23.
b MWM Wayunani.
c 1 Ne. 15:13.
7 *a* 3 Ne. 20:27.
b 1 Ne. 13:12–14; 2 Ne. 1:11.
8 *a* Isa. 29:14; 1 Ne. 14:7; 2 Ne. 27:26. MWM Urejesho wa Injili.
b 2 Ne. 10:10–11; 3 Ne. 16:4–7; Morm. 5:19.
c 1 Ne. 15:13–18; 3 Ne. 5:21–26; 21:7.
9 *a* 1 Ne. 14:1–5.
b 2 Ne. 30:1–7.
c 2 Ne. 29:13–14.
d Kum. 4:31.
e MWM Agano la Ibrahimu.
f Mwa. 12:2–3; 3 Ne. 20:27; Ibr. 2:9–11.
10 *a* Isa. 52:10.

12 Kwa hivyo, atawatoa tena utumwani, na [a]watakusanyika pamoja katika nchi yao ya urithi; na watatolewa kutoka fumboni na kutoka [b]gizani; na watajua kwamba [c]Bwana ni [d]Mwokozi wao na Mkombozi wao, [e]Mwenyezi Mkuu wa Israeli.

13 Na damu ya lile kanisa kuu na la [a]machukizo, ambalo ni kahaba wa ulimwengu wote, itakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe; kwani [b]watapigana wenyewe kwa wenyewe, na upanga wa mikono [c]yao utaangukia vichwa vyao vyenyewe, na watalewa kwa damu yao wenyewe.

14 Na kila [a]taifa ambalo litapigana nawe, Ee nyumba ya Israeli, watageukiana mmoja dhidi ya mwingine, na [b]wataanguka kwenye shimo walilochimba kutega watu wa Bwana. Na wote [c]watakaopigana dhidi ya Sayuni wataangamizwa, na yule kahaba mkuu, ambaye ameharibu njia sahihi za Bwana, ndiyo, lile kanisa kuu la machukizo, litaanguka [d]mavumbini na muanguko wake utakuwa mkuu.

15 Kwani tazama, asema nabii, wakati unafika kwa haraka kwamba Shetani hatakuwa na nguvu yoyote mioyoni mwa watoto wa watu; maana siku inafika kwamba wote wenye kiburi na wale wanaotenda maovu watakuwa kama [a]kapi; na siku inafika ambayo lazima [b]wachomwe.

16 Kwani wakati unafika mapema ambapo utimilifu wa [a]ghadhabu ya Mungu utakuwa juu ya watoto wa watu wote; kwani hatakubali kwamba waovu wawaangamize walio watakatifu.

17 Kwa hivyo, [a]atawahifadhi walio wa [b]haki kwa nguvu zake, hata kama ghadhabu yake timilifu ije, na watakatifu wahifadhiwe, hata katika maangamizo ya maadui wao kwa moto. Kwa hivyo, watakatifu hawapaswi kuogopa; na hivyo ndivyo asemavyo nabii, wataokolewa, hata kama ni kwa moto.

18 Tazama, kaka zangu, nawaambia, kwamba vitu hivi lazima vitimizwe karibuni; ndiyo, hata damu, na moto, na ukungu wa moshi lazima uje; na ni lazima itendeke usoni mwa dunia hii; na inawajia binadamu kulingana na mwili ikiwa watashupaza mioyo yao dhidi ya yule Mtakatifu wa Israeli.

19 Kwani tazama, watakatifu hawataangamia; kwani wakati

12*a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b MWM Giza, Kiroho.
c 2 Ne. 6:10–11.
d MWM Mwokozi.
e MWM Yehova.
13*a* MWM Ibilisi—Kanisa la ibilisi.
b 1 Ne. 14:3, 15–17.
c 1 Ne. 21:26.
14*a* Lk. 21:10.
b Isa. 60:12; 1 Ne. 14:3; M&M 109:25.
c 2 Ne. 10:13; 27:3.
d Isa. 25:12.
15*a* Isa. 5:23–24; Nah. 1:10; Mal. 4:1; 2 Ne. 15:24; 26:4–6; M&M 64:23–24; 133:64.
b Zab. 21:9; 3 Ne. 25:1; M&M 29:9.
MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
16*a* 1 Ne. 14:17.
17*a* 2 Ne. 30:10; Musa 7:61.
b 1 Ne. 17:33–40.

lazima kwa hakika ufike kuwa wale ambao wanapinga Sayuni wataondolewa mbali.

20 Na Bwana kwa kweli atawatayarishia watu wake njia, kwa kutimiza maneno ya Musa, ambayo alizungumza, akisema: Bwana Mungu wenu atawainulia nabii, kama mimi, yeye mtamsikiliza kwa vitu vyote atakavyowaambia. Na itakuwa kwamba wale wote ambao hawatamsikiliza [a]nabii [b]wataondolewa kutoka miongoni mwa watu.

21 Na sasa mimi, Nefi, ninawatangazia, kwamba huyu [a]nabii aliyetajwa na Musa ni yule Mtakatifu wa Israeli; kwa hivyo, atapitisha [b]hukumu kwa haki.

22 Na watakatifu hawapaswi kuogopa, kwani wao hawatachanganyika. Lakini ni ufalme wa ibilisi, ambao utajengwa miongoni mwa watoto wa watu, ambao ni ufalme ulioimarishwa miongoni mwa wale wanaoishi—

23 Kwani kwa haraka wakati utafika ambapo [a]makanisa yote ambayo yamejengwa ili kupata faida, na wote waliojengwa kwa kupata mamlaka juu ya mwili, na wale ambao walijengwa ili wapate [b]sifa machoni mwa ulimwengu, na wale wanaotafuta tamaa za mwili na vitu vya ulimwengu, na kutenda kila aina ya uovu; ndiyo, mwishowe, wale wote ambao ni wa ufalme wa ibilisi ndiyo wanapaswa kuogopa, na kutetemeka, na [c]kutapatapa; wao ndiyo lazima washushwe chini mavumbini; wao ndiyo lazima [d]watachomwa kama kapi; na haya ni kulingana na maneno ya nabii.

24 Na wakati unafika kwa haraka kwamba wale watakatifu lazima waongozwe kama [a]ndama wa zizini, na yule Mtakatifu wa Israeli lazima atawale kwa mamlaka, na uwezo, na nguvu, na utukufu mkuu.

25 Na [a]anawakusanya watoto wake kutoka pembe nne za ulimwengu; na anahesabu kondoo wake, na wanamjua; na kutakuwa na zizi moja na [b]mchungaji mmoja; na atalisha kondoo wake, na kwake watapata [c]malisho.

26 Na kwa sababu ya haki ya watu wake, [a]Shetani hana nguvu; kwa hivyo, hawezi kufunguliwa kwa muda wa [b]miaka mingi; kwani hana nguvu juu ya mioyo ya watu, kwani wanaishi katika haki, na yule Mtakatifu wa Israeli [c]anatawala.

20 *a* Yn. 4:19; 7:40.
b M&M 133:63.
21 *a* Kum. 18:15, 18; Mdo. 3:20–23; 1 Ne. 10:4; 3 Ne. 20:23.
b Zab. 98:9; Musa 6:57.
23 *a* 1 Ne. 14:10; 2 Ne. 26:20. MWM Ukuhani wa uongo.
b Lk. 6:26; Alma 1:3.
c 2 Ne. 28:19.
d 2 Ne. 26:6.
24 *a* Amo. 6:4; Mal. 4:2; 3 Ne. 25:2.
25 *a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b MWM Mchungaji Mwema.
c Zab. 23.
26 *a* Ufu. 20:2; Alma 48:17; M&M 43:31; 45:55; 88:110; 101:28. MWM Ibilisi.
b Yak. (KM) 5:76.
c MWM Milenia.

27 Na sasa tazama, mimi, Nefi, ninawaambia kwamba lazima vitu hivi vyote vitimizwe kulingana na mwili.

28 Lakini, tazama, mataifa yote, makabila yote, lugha zote, na watu wote wataishi salama katika Yule Mtakatifu wa Israeli ikiwa [a]watatubu.

29 Na sasa mimi, Nefi, ninakoma; kwani sitathubutu kuzungumza zaidi kuhusu vitu hivi.

30 Kwa hivyo, kaka zangu, ningetaka mfikirie kwamba vile vitu vilivyoandikwa kwenye [a]mabamba ya shaba nyeupe ni vya kweli; na vinashuhudia kwamba lazima mtu atii amri za Mungu.

31 Kwa hivyo, msidhani kwamba mimi na baba yangu ndiyo pekee tumeshuhudia, na kuyafundisha. Kwa hivyo, kama mtatii [a]amri, na kuvumilia hadi mwisho, mtaokolewa katika siku ya mwisho. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.

KITABU CHA PILI CHA NEFI

Historia ya kifo cha Lehi. Kaka za Nefi wanamwasi. Bwana anamwonya Nefi akimbilie nyikani. Safari zake nyikani na kadhalika.

MLANGO WA 1

Lehi atoa unabii kuhusu nchi ya uhuru—Uzao wake utatawanywa na kuchapwa kama utamkataa yule Mtakatifu wa Israeli—Anawasihi wanawe wajivike mavazi ya silaha ya haki. Karibia mwaka 588–570 K.K.

NA ikawa kwamba baada ya mimi, Nefi, kumaliza kufundisha kaka zangu, [a]baba yetu, Lehi, naye pia aliwaelezea vitu vingi, na akawaambia, jinsi Bwana alivyowafanyia mambo makuu kwa kuwatoa kutoka nchi ya Yerusalemu.

2 Na aliwazungumzia kuhusu [a]maasi yao majini, na huruma za Mungu katika kuhifadhi maisha yao, kwamba hawakuzama.

3 Na pia aliwaelezea kuhusu nchi ya ahadi, ambayo walipokea—jinsi Bwana alivyokuwa na huruma katika kutuonya kwamba tukimbie kutoka nchi ya Yerusalemu.

4 Kwani, tazama, alisema, nimeona [a]ono, ambalo najua kwamba Yerusalemu imeangamizwa; na kama tungebaki [b]Yerusalemu tungekuwa [c]tumeangamia pia.

28 *a* MWM Samehe; Toba, Tubu.
30 *a* 2 Ne. 4:2.
31 *a* Mt. 19:17.
MWM Amri za Mungu.

[2 NEFI]
1 1 *a* MWM Kipatriaki, Patriaki.
2 *a* 1 Ne. 18:9–20.
4 *a* MWM Ono.

b 2 Fal. 24:14–15; Yer. 44:2; 1 Ne. 1:4; Hel. 8:20.
c Alma 9:22.

5 Lakini, akasema, ingawa tumepata masumbuko, tumepokea [a]nchi ya ahadi, nchi ambayo ni [b]bora zaidi ya nchi zingine zote; nchi ambayo Bwana Mungu ameagana na mimi kwamba itakuwa urithi wa uzao wangu. Ndiyo, Bwana [c]ameagana na mimi kuhusu nchi hii, na kwa watoto wangu milele, na pia wale wote ambao watatolewa kutoka nchi zingine kwa mkono wa Bwana.

6 Kwa hivyo, mimi, Lehi, natoa unabii kulingana na mahimizo ya Roho aliye ndani yangu, kwamba hakuna [a]yeyote atakayekuja katika nchi hii ila tu wale ambao wataletwa na mkono wa Bwana.

7 Kwa hivyo, [a]nchi hii imewekwa wakfu kwa yule atakayeletwa na yeye. Na ikiwa kwamba watamtumikia kulingana na amri ambazo amewapatia, itakuwa nchi ya [b]uhuru kwao; kwa hivyo, hawatatekwa nyara kamwe; au sivyo, itakuwa ni kwa sababu ya uovu; kwani uovu ukiwepo, nchi [c]italaaniwa kwa sababu yao, lakini kwa wale watakatifu itabarikiwa milele.

8 Na tazama, ni hekima kwamba hii nchi ifichwe kutokana na ufahamu wa mataifa mengine; kwani tazama, mataifa mengi yangeinyakua hii nchi, hata kwamba pasiwe na mahali pa kurithiwa.

9 Kwa hivyo, mimi, Lehi, nimepokea ahadi, kwamba [a]kama wale ambao Bwana Mungu atawatoa kutoka nchi ya Yerusalemu watatii amri zake, [b]watafanikiwa katika nchi hii; na watafichwa kutokana na mataifa mengine, ili wapokee nchi hii. Na kama [c]watatii amri zake watabarikiwa usoni mwa nchi hii, na hakuna yeyote atakayewaudhi, wala kuwanyang'anya nchi yao ya urithi; na wataishi salama milele.

10 Lakini tazama, wakati ukitimia watakapofifia katika kutoamini, baada ya kupokea baraka nyingi kutoka mkono wa Bwana—wakiwa na ufahamu wa uumbaji wa dunia, na watu wote, wakielewa kazi kuu na ya maajabu ya Bwana tangu uumbaji wa ulimwengu; na wakipewa nguvu za kutenda vitu vyote kwa imani; wakiwa na amri zote tangu mwanzo, na wakiwa wameletwa kwa wema wake usio na kikomo katika nchi hii ya ahadi—tazama, nasema, kama siku itafika ambapo watamkataa yule Mtakatifu wa Israeli, yule [a]Masiya wa kweli, Mkombozi wao na Mungu wao, tazama, hukumu za yule mwenye haki zitakuwa juu yao.

11 Ndiyo, atawaletea [a]mataifa mengine, na atayapatia nguvu, na ataondoa kutoka kwao nchi ile ambayo ni mali yao, na

5*a* MWM Nchi ya Ahadi.
b Eth. 2:9–10.
c MWM Agano.
6*a* 2 Ne. 10:22.
7*a* Mos. 29:32; Alma 46:10, 20.
b 2 Ne. 10:11.
MWM Huru, Uhuru.
c Alma 45:10–14, 16; Morm. 1:17; Eth. 2:8–12.
9*a* 2 Ne. 4:4; Alma 9:13.
b Kum. 29:9.
c MWM Mtiifu, Tii, Utii.
10*a* MWM Masiya.
11*a* 1 Ne. 13:12–20; Morm. 5:19–20.

atawasababishia [b]kutawanywa na kupigwa.

12 Ndiyo, wakati kizazi kitakapopita hadi kingine kutakuwa na [a]umwagaji wa damu, na mapigo makali miongoni mwao; kwa hivyo, wana wangu, ningetaka mkumbuke; ndiyo, ningetaka kwamba msikilize maneno yangu.

13 Ee kwamba ninyi mngezinduka; zindukeni kutoka usingizi mzito, ndiyo, hata kutoka usingizi wa [a]jehanamu, na mjifungue [b]minyororo ambayo mmefungiwa, ambayo ni minyororo inayowafunga watoto wa watu, kwamba wanachukuliwa mateka hadi kwenye lile [c]shimo la milele lenye mateso na huzuni.

14 Zindukeni! na muinuke kutoka mavumbini, na msikie maneno ya [a]mzazi dhaifu, ambaye viungo vyake hivi karibuni lazima mvitie kwenye [b]kaburi kimya lenye baridi, ambalo hakuna msafiri yeyote anayeweza kurejea kutoka humo; siku chache zimebaki na nitaenda [c]njia ya ulimwengu wote.

15 Lakini tazama, Bwana [a]ameikomboa nafsi yangu kutoka jehanamu; nimeuona utukufu wake, na nimezingirwa milele katika [b]mikono ya [c]upendo wake.

16 Na ninatamani kwamba mkumbuke kuchunguza [a]sheria na hukumu za Bwana; tazama, huu ndiyo wasiwasi wa nafsi yangu tangu mwanzoni.

17 Moyo wangu umechoshwa na huzuni mara kwa mara, kwani naogopa kwamba kutokana na ugumu wa mioyo yenu Bwana Mungu wenu atawateremkia kwa [a]ghadhabu yake timilifu, hata kwamba [b]mtengwe na kuangamizwa milele.

18 Au, kwamba laana itawapata kwa muda wa [a]vizazi vingi; na muadhibiwe kwa upanga, na kwa njaa, na mchukiwe, na kuongozwa kulingana na nia na utumwa wa [b]ibilisi.

19 Enyi wana wangu, kwamba vitu hivi visiwajie, lakini kwamba muwe watu [a]wateule na wa kuheshimika na Bwana. Lakini tazama, nia yake itendeke; kwani [b]njia zake ni takatifu milele.

20 Na amesema kwamba: [a]Kama mtashika [b]amri zangu [c]mtafanikiwa nchini; lakini kama mtakataa amri zangu mtatengwa kutokana na uwepo wangu.

21 Na sasa ili nafsi yangu ifurahi ndani yenu, na ili moyo wangu uondoke ulimwengu huu ukifurahishwa nanyi, kwamba

11 *b* 1 Ne. 22:7.
12 *a* Morm. 1:11–19; 4:11.
13 *a* MWM Jehanamu.
b Alma 12:9–11.
c 1 Ne. 15:28–30; Hel. 3:29–30.
14 *a* MWM Wazazi.
b MWM Mauti ya Kimwili.
c Yos. 23:14.
15 *a* Alma 36:28.
MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
b Yak. (KM) 6:5; Alma 5:33; 3 Ne. 9:14.
c Rum. 8:39.
MWM Upendo.
16 *a* Kum. 4:5–8; 2 Ne. 5:10–11.
17 *a* 2 Ne. 5:21–24; Alma 3:6–19.
b Mos. 12:8.
18 *a* 1 Ne. 12:20–23.
b MWM Ibilisi.
19 *a* MWM Teule, Wateule.
b Hos. 14:9.
20 *a* Yar. 1:9; Mos. 1:6–7; Alma 9:13–14.
b Law. 26:3–14; Yoe. 2:23–26.
c Zab. 67:6; Mos. 2:21–25.

nisishushwe chini kaburini kwa hofu na huzuni, basi, inukeni kutoka mavumbini, wana wangu, na muwe [a]wanaume, na muamue kwa mawazo na kwa moyo [b]mmoja, mkiungana kwa vitu vyote, ili msiingie utumwani;

22 Ili msilaaniwe kwa laana kali; na pia, ili msijiletee ghadhabu ya Mungu wa [a]haki, kwa kuangamizwa, ndiyo, kuangamizwa milele kwa roho na mwili.

23 Zindukeni, wana wangu; jivikeni [a]silaha za haki. Jifungueni minyororo ambayo imewafunga, na mtoke fumboni, na muinuke kutoka mavumbini.

24 Msimwasi ndugu yenu tena, ambaye maono yake yamekuwa matukufu, na ambaye ametii amri tangu wakati tulipoondoka Yerusalemu; na ambaye amekuwa chombo mikononi mwa Mungu, katika kutuleta hadi kwenye nchi ya ahadi; kwani kama sio yeye, lazima tungeangamia kwa [a]njaa huko nyikani; walakini, mlitaka [b]kumtoa uhai wake; ndiyo, na ameteseka kwa hofu nyingi kwa sababu yenu.

25 Na ninaogopa na kutetemeka zaidi kwa sababu yenu, kwamba atateseka tena; kwani tazama, mmemlaumu kwamba alitaka awe na uwezo na mamlaka juu yenu; lakini najua kwamba hakutaka awe na uwezo wala [a]mamlaka juu yenu, lakini alitaka kumtukuza Mungu, na ustawi wenu wa milele.

26 Na mmenung'unika kwa sababu amekuwa wazi kwenu. Mmesema kwamba ametumia [a]ukali; na mnasema kwamba amewakasirikia; lakini tazama, ukali wake ulikuwa ukali wa nguvu za neno la Mungu, ambalo lilikuwa ndani yake; na lile mnaloliita hasira lilikuwa ukweli, kulingana na ule ulio ndani ya Mungu, ambao hangezuia, akidhihirisha kwa ujasiri kuhusu maovu yenu.

27 Na ni lazima kwamba [a]nguvu za Mungu ziwe na yeye, hata kwamba lazima mtii akiwaamrisha. Lakini tazama, sio yeye, bali ilikuwa [b]Roho wa Bwana iliyokuwa ndani yake, ambayo [c]ilifungua kinywa chake ili azungumze hata kwamba hangefunga kinywa chake.

28 Na sasa mwana wangu, Lamani, na pia Lemueli na Samu, na pia wana wangu ambao ni wana wa Ishmaeli, tazama, kama mtasikiliza sauti ya Nefi hamtaangamia. Na kama mtamsikiliza nitawaachia [a]baraka, ndiyo, hata baraka yangu ya kwanza.

29 Lakini ikiwa hamtamsikiza ninaondoa baraka yangu ya [a]kwanza, ndiyo, hata baraka yangu, na itakuwa juu yake.

30 Na sasa, Zoramu, nakuzu-

21*a* 1 Sam. 4:9; 1 Fal. 2:2.
b Musa 7:18.
22*a* M&M 3:4.
23*a* Efe. 6:11–17.
24*a* 1 Ne. 16:32.
b 1 Ne. 16:37.
25*a* Mwa. 37:9–11.
26*a* Mit. 15:10; 1 Ne. 16:2; Moro. 9:4; M&M 121:41–43.
27*a* 1 Ne. 17:48.
b M&M 121:43.
c M&M 33:8.
28*a* MWM Haki ya Kuzaliwa.
29*a* Ibr. 1:3.

ngumzia wewe: Tazama, wewe ni [a]mtumishi wa Labani; walakini, wewe umetolewa kutoka nchi ya Yerusalemu, na ninajua kwamba wewe ni rafiki wa kweli wa mwana wangu Nefi, milele.

31 Kwa hivyo, kwa vile umekuwa mwaminifu uzao wako utabarikiwa [a]pamoja na mbegu yake, hata kwamba wataishi kwa mafanikio kwa muda mrefu katika nchi hii; na hakuna chochote, ila tu ni uovu miongoni mwao, kitakachowadhulumu au kusumbua mafanikio yao usoni mwa nchi hii milele.

32 Kwa hivyo, kama utatii amri za Bwana, Bwana ameweka nchi hii wakfu kwa usalama wa uzao wako na uzao wa mwana wangu.

MLANGO WA 2

Ukombozi unatokana na Masiya Mtakatifu—Uhuru wa kuamua ni muhimu kwa kuishi na kwa maendeleo—Adamu alianguka ili wanadamu wawe—Wanadamu wako huru kuchagua uhuru na uzima wa milele. Karibia mwaka 588–570 K.K.

Na sasa, Yakobo, ninasema nawe: Wewe ndiye [a]mzaliwa wa kwanza wangu katika siku za taabu yangu nyikani. Na tazama, katika utoto wako umeteseka kwa masumbuko na huzuni nyingwa sababu ya ujeuri wa ndugu zako.

2 Walakini, Yakobo, mzaliwa wa kwanza wangu nyikani, wewe unajua ukuu wa Mungu; na ataweka wakfu masumbuko yako kwa faida yako.

3 Kwa hivyo, nafsi yako itabarikiwa, na wewe utaishi salama na kaka yako, Nefi; na utamtumikia Mungu wako maishani mwako. Kwa hivyo, najua kwamba wewe umekombolewa, kwa sababu ya haki ya Mkombozi wako; kwani wewe umeona kwamba katika wakati mtimilifu yeye atakuja kuwaletea wanadamu wokovu.

4 Na wewe [a]umeona ujanani mwako utukufu wake; kwa hivyo, wewe umebarikiwa kama wale atakaowahudumia katika mwili; kwani Roho ni sawa, jana, leo, na milele. Na njia imetayarishwa tangu kuanguka kwa mwanadamu, na wokovu ni [b]bure.

5 Na wanadamu wanashauriwa kikamilifu kwamba [a]wajue mema na maovu. Na wanadamu wanapewa sheria. Na hakuna yeyote [b]anayekubalika kwa sheria; au, kwa sheria wanadamu [c]wanatengwa. Ndiyo, walitengwa kwa sheria ya muda; na pia, kwa sheria ya kiroho wanaangamizwa kutokana na yale yalio mema, na wanadhoofika milele.

30 *a* 1 Ne. 4:20, 35.
31 *a* 2 Ne. 5:6.
2 1 *a* 1 Ne. 18:7.
4 *a* 2 Ne. 11:3; Yak. (KM) 7:5.
b MWM Neema.
5 *a* Moro. 7:16.
b Rum. 3:20; 2 Ne. 25:23; Alma 42:12–16. MWM Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki.
c 1 Ne. 10:6; 2 Ne. 9:6–38; Alma 11:40–45; 12:16, 24; 42:6–11; Hel. 14:15–18.

6 Kwa hivyo, [a]ukombozi unakuja kupitia [b]Masiya Mtakatifu; kwani amejaa [c]neema na kweli.

7 Tazama, anajitoa kuwa [a]dhabihu ya dhambi, kutimiza masharti ya sheria, kwa wale wote wenye moyo uliopondeka na roho iliyovunjika; na hakuna mwingine yeyote anayeweza kutimiza [b]masharti ya sheria.

8 Kwa hivyo, ni muhimu sana kuwajulisha wakazi wa dunia kuhusu vitu hivi, ili wajue hakuna binadamu anayeweza kuishi karibu na Mungu, [a]bila fadhila, na rehema, na neema za Masiya Mtakatifu, ambaye anatoa maisha yake mwilini, na kuyachukua tena kwa uwezo wa Roho, ili alete [b]ufufuo wa wafu, akiwa wa kwanza kufufuka.

9 Kwa hivyo, yeye ni malimbuko kwa Mungu, kwani [a]atawaombea watoto wa watu wote; na wale watakaomwamini wataokolewa.

10 Na kwa sababu ya [a]maombi kwa wote, watu wote wanamjia Mungu; kwa hivyo, wanasimama kwenye uwepo wake, ili [b]kuhukumiwa na yeye kulingana na ukweli na [c]utakatifu ulioko ndani yake yeye. Kwa hivyo, masharti ya sheria ambayo yule Mtakatifu ametoa, yatalingana na adhabu na mapigo yake, adhabu hii ni kinyume cha furaha ya kutii amri, ili kutimiza masharti ya [d]upatanisho—

11 Kwani lazima, kuwe na [a]upinzani katika mambo yote. Kama sio hivyo, mzaliwa wa kwanza wangu nyikani, haki haingeweza kupatikana, wala uovu, wala utakatifu au taabu, wala uzuri au ubaya. Kwa hivyo, mambo yote lazima yawe kitu kimoja; kwa hivyo, kama ni kitu kimoja lazima kikae kama kimekufa, bila uhai wala kifo, si uharibifu wala kutoharibika, si furaha wala taabu, si kufahamu wala kutofahamu.

12 Kwa hivyo, itakuwa kwamba kiliumbwa bure; kwa hivyo itakuwa kwamba hakuna [a]kusudi la kuumbwa kwake. Kwa hivyo, kitu hiki kinaangamiza hekima ya Mungu na makusudi yake ya milele, na pia nguvu, na rehema, na [b]haki ya Mungu.

13 Na kama mtasema [a]hakuna sheria, mtasema pia hakuna dhambi. Kama mtasema hakuna dhambi, mtasema pia hakuna haki. Na kama hakuna

6 *a* 1 Ne. 10:6; 2 Ne. 25:20; Alma 12:22–25. MWM Mpango wa Ukombozi.
b MWM Masiya.
c Yn. 1:14, 17; Musa 1:6.
7 *a* MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
b Rum. 10:4.
8 *a* 2 Ne. 25:20; 31:21; Mos. 4:8; 5:8; Alma 38:9.
b 1 Kor. 15:20; Alma 7:12; 12:24–25; 42:23. MWM Ufufuko.
9 *a* Isa. 53; Mosia 14:12; 15:8–9.
10 *a* MWM Mkombozi.
b MWM Hukumu ya mwisho.
c MWM Utakatifu.
d 2 Ne. 9:7, 21–22, 26; Alma 22:14; 33:22; 34:9.
11 *a* M&M 29:39; 122:5–9. MWM Shida.
12 *a* M&M 88:25–26. MWM Dunia—Iliumbwa kwa ajili ya mwanadamu.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
13 *a* 2 Ne. 9:25.

haki hakuna furaha. Na kama hakuna haki wala furaha basi hakuna adhabu wala huruma. Na kama vitu hivi havipo basi hakuna Mungu. Na kama [b]hakuna Mungu basi sisi hatupo, wala dunia; kwani hakungekuwa na uumbaji wa vitu, wala kutenda au kutendewa; kwa hivyo, vitu vyote lazima vingetokomea.

14 Na sasa, wana wangu, nawaambia vitu hivi kwa faida yenu na elimu; kwani kuna Mungu, na [a]ameumba vitu vyote, mbingu na dunia, na vitu vyote vilivyomo, vitu vya kutenda na vitu vya [b]kutendewa.

15 Na kutimiza [a]makusudio yake ya milele katika kikomo cha mwanadamu, baada ya kuumba wazazi wetu wa kwanza, na wanyama wa porini na ndege wa hewani, na mwishowe, vitu vyote vilivyoumbwa, ilibidi lazima kuwe na upinzani, hata [b]tunda [c]lililokataliwa kinyume cha [d]mti wa uzima; mmoja ukiwa mtamu na mwingine ukiwa chungu.

16 Kwa hivyo, Bwana Mungu amemruhusu mwanadamu [a]kujitendea mwenyewe. Kwa hivyo, mwanadamu hangeweza kujitendea mwenyewe bila [b]kuvutiwa na moja au nyingine.

17 Na mimi, Lehi, kulingana na mambo ambayo nimesoma, lazima niwaze kwamba [a]malaika wa Mungu, kulingana na lile lililoandikwa, [b]alianguka kutoka mbinguni; kwa hiyo, akawa ibilisi, kwani alitafuta kile ambacho kilikuwa ni uovu mbele za Mungu.

18 Na kwa sababu alianguka kutoka mbinguni, na kuhuzunika milele, [a]aliwatakia wanadamu nao pia wahuzunike. Kwa hivyo, akamwambia [b]Hawa, ndiyo, hata yule nyoka wa zamani, ambaye ni ibilisi, ambaye ni baba wa [c]uwongo wote, kwa hivyo akasema: Kuleni tunda lililokatazwa, na hamtakufa, lakini mtakuwa kama Mungu, [d]mkifahamu mema na maovu.

19 Na baada ya Adamu na Hawa [a]kula tunda lililokatazwa walifukuzwa kutoka bustani ya [b]Edeni, ili walime ardhi.

20 Na wamezaa watoto; ndiyo, hata [a]jamii ya dunia yote.

21 Na maisha ya watoto wa [a]watu yaliongezewa, kulingana na nia ya Mungu, ili waweze [b]kutubu wakiwa hai; kwa hivyo, hali yao ikawa hali

13 *b* Alma 42:13.
14 *a* MWM Umba, Uumbaji.
b M&M 93:30.
15 *a* Isa. 45:18; Alma 42:26; Musa 1:31, 39.
b Mwa. 3:6; Alma 12:21–23.
c Mwa. 2:16–17; Musa 3:17.
d Mwa. 2:9; 1 Ne. 15:22, 36; Alma 32:40.
16 *a* 2 Ne. 10:23; Alma 12:31. MWM Haki ya uamuzi.
b M&M 29:39–40.
17 *a* MWM Ibilisi.
b Isa. 14:12; 2 Ne. 9:8; Musa 4:3–4; Ibr. 3:27–28.
18 *a* 2 Ne. 28:19–23; 3 Ne. 18:18; M&M 10:22–27.
b MWM Hawa.
c 2 Ne. 28:8; Musa 4:4.
d Mwa. 3:5; Alma 29:5; Moro. 7:15–19.
19 *a* Alma 12:31. MWM Anguko la Adamu na Hawa.
b MWM Edeni.
20 *a* M&M 138:38–39.
21 *a* Alma 12:24; Musa 4:23–25.
b Alma 34:32. MWM Toba, Tubu.

ya [c]majaribio, na wakati wao ukaongezewa, kulingana na amri ambazo Bwana Mungu aliwapatia watoto wa watu. Kwani alitoa amri kwamba lazima wanadamu wote watubu; kwani alionyesha wanadamu wote kwamba [d]walipotea, kwa sababu wazazi wao walivunja sheria.

22 Na sasa, tazama, kama Adamu hangevunja sheria hangeanguka, bali angeishi katika bustani ya Edeni. Na vitu vyote vilivyoumbwa vingebaki katika hali yao ya kwanza baada ya kuumbwa; na vingebaki vivyo hivyo milele, na kuwa bila mwisho.

23 Na hawangezaa [a]watoto; na hivyo wangeishi katika hali ya kitoto, bila shangwe, kwani hawakufahamu dhiki; bila kutenda mema, kwani hawakujua dhambi.

24 Lakini tazama, vitu vyote vimetendwa kwa hekima ya yule [a]ajuaye vitu vyote.

25 [a]Adamu [b]alianguka ili wanadamu wawe; na wanadamu [c]wapo, ili wapate [d]shangwe.

26 Na [a]Masiya anakuja katika wakati mtimilifu, ili [b]awakomboe watoto wa watu kutokana na mwanguko. Na kwa sababu wamekombolewa kutokana na mwanguko wamekuwa [c]huru milele, wakielewa mema na maovu; kujitendea wenyewe na sio kutendewa, ila tu katika kuadhibiwa na [d]sheria katika siku ile kuu ya mwisho, kulingana na amri ambazo Mungu amezitoa.

27 Kwa hivyo, wanadamu wana [a]uhuru wanapoishi; na wamepewa vitu vyote ambavyo ni muhimu kwa mwanadamu. Na wana haki [b]kuchagua uhuru na [c]uzima wa milele, kupitia yule Mpatanishi mkuu wa wanadamu wote, au kuchagua utumwa na kifo, kulingana na utumwa na nguvu za ibilisi; kwani anataka wanadamu wote wawe na dhiki kama yeye.

28 Na sasa, wana wangu, ningetaka mtazame yule [a]Mpatanishi mkuu, na msikilize amri zake kuu; na muwe waaminifu kwa maneno yake, na mchague uzima wa milele, kulingana na mapenzi ya Roho Mtakatifu wake.

29 Na msichague kifo cha milele, ambacho ni kulingana na nia ya mwili na uovo ulio ndani yake, ambayo inaipatia roho ya ibilisi nguvu za [a]kuteka nyara, na kukuleta [b]jehanamu, ili awatawale katika ufalme wake.

30 Nimewazungumzia ninyi

21 *c* MWM Hali ya Kufa, enye Kufa.
d Yak. (KM) 7:12.
23 *a* Musa 5:11.
24 *a* MWM Mungu, Uungu.
25 *a* MWM Adamu.
b Musa 6:48. MWM Anguko la Adamu na Hawa.
c MWM Hali ya Kufa, enye Kufa.
d Musa 5:10. MWM Mwanadamu, Wanadamu; Shangwe.
26 *a* MWM Masiya.
b MWM Mpango wa Ukombozi.
c Alma 42:27; Hel. 14:30.
d MWM Sheria.
27 *a* Gal. 5:1; Musa 6:56.
b MWM Haki ya uamuzi.
c MWM Uzima wa Milele.
28 *a* MWM Mpatanishi.
29 *a* Rum. 6:16–18; Alma 12:11.
b MWM Jehanamu.

nyote, wana wangu, maneno haya machache, katika siku zangu za mwisho za majaribio; na nimechagua sehemu njema, kulingana na maneno ya nabii. Na sina lengo lingine lolote ila ustawi wenu usio na mwisho wa nafsi zenu. Amina.

MLANGO WA 3

Yusufu akiwa Misri aliona Wanefi kwenye ono—Alitoa unabii kuhusu Joseph Smith, mwonaji wa siku za mwisho; kuhusu Musa, ambaye atakomboa Israeli; na kutokea kwa Kitabu cha Mormoni. Karibia mwaka 588–570 K.K.

Na sasa nakuzungumzia wewe, Yusufu, [a]kitinda mimba wangu. Wewe ulizaliwa huko nyikani nikisumbuka; ndiyo, katika siku za msiba wangu mkuu mama yako alikuzaa.

2 Na Bwana akuwekee wakfu [a]nchi hii pia, ambayo ni nchi bora zaidi, kwa urithi wako na kwa urithi wa uzao wako na kaka zako, kwa usalama wako milele, kama utatii amri za yule aliye Mtakatifu wa Israeli.

3 Na sasa, Yusufu, kitinda mimba wangu ambaye nimekuzaa huko nyikani nikisumbuka, Bwana akubariki milele, kwani uzao wako [a]hautaangamizwa kabisa.

4 Kwani tazama, wewe ni matunda ya kiuno changu; na mimi ni uzao wa [a]Yusufu [b]aliyeuzwa Misri. Na makubwa yalikuwa maagano ya Bwana ambayo alimfanyia Yusufu.

5 Kwa hivyo, Yusufu kwa hakika [a]aliona siku yetu. Na akapokea ahadi kwa Bwana, kwamba kutoka matunda ya viuno vyake Bwana Mungu angeinulia nyumba ya Israeli, [b]tawi [c]takatifu; sio [d]Masiya, lakini tawi ambalo lingekatwa, walakini, kukumbukwa katika maagano ya Bwana kwamba Masiya angethirihishwa kwao katika siku za baadaye, katika roho ya nguvu, ya kuwatoa [e]gizani hadi kwenye nuru—ndiyo, kutoka maficho ya giza na kutoka utumwani hadi kwenye uhuru.

6 Kwani Yusufu alishuhudia kwa hakika, akisema: Bwana Mungu wangu atainua [a]mwonaji, ambaye atakuwa mwonaji bora kwa uzao wa [b]viuno vyangu.

7 Ndiyo, Yusufu kwa hakika alisema: Hivi ndivyo anisemavyo Bwana: Ni [a]mwonaji bora nitakaye mwinua kutoka matunda ya viuno vyako; na ataheshimiwa zaidi miongoni mwa matunda ya viuno vyako. Naye nitamwamurisha afanyie

3 1*a* 1 Ne. 18:7.
2*a* 1 Ne. 2:20.
MWM Nchi ya Ahadi.
3*a* 2 Ne. 9:53.
4*a* Mwa. 39:1–2; 45:4; 49:22–26; 1 Ne. 5:14–16.
b Mwa. 37:29–36.
5*a* TJS Mwa. 50:24–38 (Kiambatisho); 2 Ne. 4:1–2.
b Mwa. 49:22–26; 1 Ne. 15:12; 19:24.
MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
c Yak. (KM) 2:25.
d 2 Ne. 6:14; M&M 3:16–20.
e Isa. 42:16.
6*a* 3 Ne. 21:8–11; Morm. 8:16.
MWM Mwonaji.
b M&M 132:30.
7*a* MWM Smith, Joseph, Mdogo.

matunda ya viuno vyako kazi, ndugu zake, ambayo itakuwa ya thamani kuu kwao, hata kwa kuwafahamisha ufahamu wa maagano ambayo nimeagana na baba zenu.

8 Na nitampatia amri kwamba [a]asitende kazi nyingine, ila ile kazi nitakayomwamuru. Na nitamuinua juu machoni mwangu; kwani atafanya kazi yangu.

9 Na atakuwa mkuu kama [a]Musa, ambaye nimesema nitamuinulia, [b]kukomboa watu wangu, Enyi nyumba ya Israeli.

10 Na nitamuinua Musa, ili akomboe watu wako kutoka nchi ya Misri.

11 Lakini nitamuinua mwonaji kutoka matunda ya viuno vyako; na nitampatia [a]nguvu za kuleta neno langu kwa uzao wa viuno vyako—na sio tu kuwaletea neno langu pekee, asema Bwana, lakini hata kwa kuwathibitishia wao neno langu, ambalo watakuwa wamelipata awali.

12 Kwa hivyo, uzao wa viuno vyako [a]utaandika; na uzao wa viuno vya [b]Yuda [c]utaandika; na yale yatakayoandikwa na uzao wa viuno vyako, na pia yale yatakayo andikwa na uzao wa viuno vya Yuda, yatakua pamoja, kwa [d]kufadhaisha mafundisho ya uwongo na kutatua mabishano, na kuimarisha amani miongoni mwa uzao wa viuno vyako, na [e]kuwapatia [f]ufahamu wa baba zao katika siku za mwisho, na pia kufahamu maagano yangu, asema Bwana.

13 Na kutoka kwa unyonge atapewa nguvu, katika siku ile ambayo kazi yangu itaanza miongoni mwa watu wangu, kwa kuwarudisha ninyi, Enyi nyumba ya Israeli, asema Bwana.

14 Na hivi ndivyo Yusufu alivyotoa unabii, akisema: Tazama, Bwana atambariki yule mwonaji; na wale ambao wanataka kumwangamiza watateketezwa; kwani ahadi hii, ambayo nimepokea kutoka kwa Bwana, kuhusu uzao wa viuno vyangu, itatimizwa. Tazama, nina hakika kwamba ahadi hii itatimizwa;

15 Na [a]jina lake litakuwa kama langu; na litakuwa sawa na [b]jina la baba yake. Na atakuwa kama mimi; kwani kuwa kitu, ambacho Bwana atakileta kwa mkono wake, kwa uwezo wa Bwana atawaleta watu wangu kwenye wokovu.

16 Ndiyo, hivi ndivyo Yusufu alivyotoa unabii: Nina uhakika kwa kitu hiki, hata vile nilivyo na uhakika wa ahadi ya Musa; kwani Bwana ameniambia, [a]nitaihifadhi uzao wako milele.

17 Na Bwana amesema: Nitamuinua Musa mmoja; na nitampatia nguvu kwa fimbo;

8 *a* M&M 24:7, 9.
9 *a* Musa 1:41.
b Ku. 3:7–10; 1 Ne. 17:24.
11 *a* M&M 5:3–4.
12 *a* MWM Kitabu cha Mormoni.
b 1 Ne. 13:23–29.
c MWM Biblia.
d Eze. 37:15–20; 1 Ne. 13:38–41; 2 Ne. 29:8; 33:10–11.
e Moro. 1:4.
f 1 Ne. 15:14; 2 Ne. 30:5; Morm. 7:1, 5, 9–10.
15 *a* M&M 18:8.
b JS—H 1:3.
16 *a* Mwa. 45:1–8.

na nitampatia hukumu katika maandishi. Lakini sitalegeza ulimi wake, ili aweze kuzungumza mengi, kwani sitamfanya awe hodari kwa mazungumzo. Lakini [a]nitamuandikia sheria zangu, kwa kidole cha mkono wangu; na nitampatia [b]mnenaji.

18 Na Bwana aliniambia pia: Nitainua uzao wa viuno vyako; na nitampatia mnenaji. Na mimi, tazama, nitamwezesha kwamba aandike maandishi ya uzao wa viuno vyako, kwa uzao wa viuno vyako; na mnenaji wa viuno vyako ataitangaza.

19 Na maneno atakayoandika yatakuwa maneno ambayo kwa hekima yangu ni lazima yafikie [a]mazao ya viuno vyako. Na itakuwa ni kama uzao wa viuno vyako uliwalilia [b]kutoka mavumbini; kwani ni najua imani yao.

20 Na [a]watalia kutoka mavumbini; ndiyo, hata toba kwa ndugu zao, hata baada ya vizazi vingi kuwapitia. Na itakuwa kwamba kilio chao kitapita, hata kulingana na wepesi wa maneno yao.

21 Kwa sababu ya imani yao [a]maneno yao yatatoka kutoka kinywa changu hadi kwa ndugu zao ambao ni uzao wa viuno vyako; na katika unyonge wa maneno yao nitawatia nguvu kwa imani, ya kukumbuka agano langu ambalo niliagana na baba zako.

22 Na sasa, tazama, mwana wangu Yusufu, hivi ndivyo baba yangu wa kale alitoa [a]unabii.

23 Kwa hivyo, kwa sababu ya hili agano umebarikiwa; kwani uzao wako hautaangamizwa, kwani watatii maneno ya hicho kitabu.

24 Na atainuka mmoja miongoni mwao ambaye atakuwa shujaa, ambaye atatenda mema mengi, kwa maneno na kwa vitendo, akiwa chombo mikononi mwa Mungu, mwenye imani kuu, kutenda maajabu makuu, na kutenda kile kitu ambacho ni kikuu machoni mwa Mungu, kwa kutimiza ufufuo wa nyumba ya Israeli, pamoja na uzao wa kaka zako.

25 Na sasa, Yusufu, umebarikiwa. Tazama, wewe ni mchanga; kwa hivyo sikiliza maneno ya kaka yako, Nefi, na utatendewa kulingana na yale maneno ambayo nimezungumza. Kumbuka maneno ya baba yako anayekufa. Amina.

MLANGO WA 4

Lehi anashauri na kubariki uzao wake—Anafariki na kuzikwa—Nefi anashangilia wema wa Mungu—Nefi anamwamini Bwana milele. Karibia mwaka 588–570 K.K.

Na sasa, mimi, Nefi, ninazungumza kuhusu ule unabii ambao baba yangu alitaja,

17 *a* Kum. 10:2, 4; Musa 2:1.
b Ku. 4:16.
19 *a* M&M 28:8.
b Isa. 29:4; 2 Ne. 27:13; 33:13; Morm. 9:30; Moro. 10:27.
20 *a* 2 Ne. 26:16; Morm. 8:23.
21 *a* 2 Ne. 29:2.
22 *a* 2 Ne. 3:5.

kuhusu [a]Yusufu, ambaye alipelekwa hadi Misri.

2 Kwani tazama, kwa kweli alitoa unabii kuhusu uzao wake wote. Na hakuna [a]unabii mwingi mkubwa, zaidi ya yale aliyoandika. Na alitoa unabii kutuhusu sisi, na vizazi vyetu vya baadaye; na umeandikwa kwenye mabamba ya shaba nyeupe.

3 Kwa hivyo, baada ya baba yangu kukoma kuzungumza kuhusu unabii wa Yusufu, akaita wana wa Lamani, wanawe, na mabinti zake, na akawaambia: Tazameni, wana wangu, na mabinti zangu, ambao ni wana na mabinti za [a]mzaliwa wa kwanza wangu, ningependa kwamba ninyi msikilize maneno yangu.

4 Kwani Bwana Mungu amesema kwamba: [a]Kadiri mtakavyo tii amri zangu mtafanikiwa nchini; na msipotii amri zangu mtatengwa kutokana na uwepo wangu.

5 Lakini tazameni, wana wangu na mabinti zangu, siwezi kufa kabla sijawapatia [a]baraka; kwani tazameni, ninajua kwamba kama mtalelewa kulingana na [b]njia inayo wapasa hamtaiacha.

6 Kwa hivyo, kama mmelaaniwa, tazameni, ninawaachia baraka yangu, kwamba ile laana iondolewe kwenu na iwe [a]juu ya wazazi wenu.

7 Kwa hivyo, kwa sababu ya baraka yangu Bwana Mungu [a]hatakubali kwamba mwangamie; kwa hivyo, [b]atawarehemu ninyi na uzao wenu milele.

8 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kumaliza kuzungumzia wana na mabinti za Lamani, alisababisha wana na mabinti za Lemueli kusimama mbele yake.

9 Na akawazungumzia, akisema: Tazama, wana wangu na mabinti zangu, ambao ni wana na mabinti za mwana wangu wa pili; tazama ninawapatia baraka kama ile ambayo niliwapatia wana na mabinti za Lamani; kwa hivyo, ninyi hamtaangamizwa kabisa; lakini uzao wenu utabarikiwa mwishowe.

10 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu kukoma kuwazungumzia, tazama, aliwazungumzia wana wa [a]Ishmaeli, ndiyo, na hata nyumba yake yote.

11 Na baada ya kukoma kuwazungumzia, alimwambia Samu, akisema: Heri wewe, na uzao wako; kwani wewe utarithi nchi kama vile kaka yako Nefi. Na uzao wako utahesabiwa na uzao wake; na wewe utakuwa kama kaka yako, na uzao wako kama uzao wake; na wewe utabarikiwa katika siku zako zote.

12 Na ikawa kwamba baada ya baba yangu, Lehi, kumaliza kuzungumzia jamaa yake yote, kulingana na mawazo ya moyo

4 1*a* Mwa. 39:1–2.
2*a* 2 Ne. 3:5.
3*a* MWM Mzaliwa wa Kwanza.
4*a* 2 Ne. 1:9.
5*a* MWM Baraka za Kipatriaki.
b Mit. 22:6.
6*a* M&M 68:25–29.
7*a* 2 Ne. 30:3–6; M&M 3:17–18.
b 1 Ne. 13:31; 2 Ne. 10:18–19; Yak. (KM) 3:5–9; Hel. 15:12–13.
10*a* 1 Ne. 7:6.

wake na Roho wa Bwana ambaye alikuwa ndani yake, akawa mzee. Na ikawa kwamba alifariki, na akazikwa.

13 Na ikawa kwamba muda mfupi baada ya kifo chake, Lamani na Lemueli pamoja na wana wa Ishmaeli walinikasirikia kwa sababu walirudiwa na Bwana.

14 Kwani mimi, Nefi, nilishurutishwa kuwazungumzia, kulingana na neno lake; kwani nilikuwa nimewazungumzia vitu vingi, na pia baba yangu, kabla ya kifo chake; maneno mengi ambayo yameandikwa kwenye [a]mabamba yangu mengine; kwani sehemu kubwa zaidi ya historia imeandikwa kwenye mabamba yangu mengine.

15 Na katika [a]haya ninaandika mambo ya nafsi yangu, na maandiko mengi ambayo yamechorwa kwenye mabamba ya shaba nyeupe. Kwani moyo wangu unayafurahia maandiko, na moyo wangu [b]huyatafakari, na kuyaandika kwa [c]ajili ya kujifunza na faida ya watoto wangu.

16 Tazama, [a]nafsi yangu hufurahia vitu vya Bwana; na [b]moyo wangu huyatafakari mara kwa mara vitu ambavyo nimeviona na kuvisikia.

17 Walakini, ingawa Bwana ana [a]wema mkubwa, hata kunionyesha kazi yake kuu na ya maajabu, moyo wangu unalia: Ewe mimi mtu [b]mwovu! Ndiyo, moyo wangu unahuzunishwa kwa sababu ya mwili wangu; moyo wangu unahofishwa na dhambi zangu.

18 Nimezingirwa, kwa sababu ya majaribio na dhambi ambazo [a]zinaninasa kwa urahisi.

19 Na ninapotaka kushangilia, moyo wangu huugua kwa sababu ya dhambi zangu; walakini, ninajua ninayemwamini.

20 Mungu wangu amekuwa tegemeo langu; amenionggoza katika masumbuko yangu nyikani; na amenihifadhi hata kutoka kilindi kikuu cha maji.

21 Amenijaza [a]upendo wake, hata kwa kumaliza mwili wangu.

22 Amewafadhaisha [a]maadui wangu, hata kuwasababisha kutetemeka mbele yangu.

23 Tazama, amesikia kilio changu mchana, na kunipatia ufahamu usiku kwa [a]maono.

24 Na kwa mchana [a]nimesali kwa ujasiri; ndiyo, nimepaza sauti yangu juu; na malaika wakateremka na kunihudumia.

25 Na kwenye mabawa ya Roho yake mwili wangu [a]umebebwa na kuchukuliwa kwenye milima mirefu zaidi. Na macho yangu yameona vitu vikuu, ndiyo, hata vikuu sana kwa mwanadamu; kwa hivyo niliamriwa kwamba nisiviandike.

26 Ee basi, kama nimeona

14 *a* 1 Ne. 1:16–17; 9:4.
15 *a* 1 Ne. 6:4–6.
b MWM Maandiko; Tafakari.
c 1 Ne. 19:23.
16 *a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
b MWM Moyo.
17 *a* 2 Ne. 9:10; M&M 86:11.
b Rum. 7:24.
18 *a* Rum. 7:21–23; Ebr. 12:1; Alma 7:15.
21 *a* MWM Upendo.
22 *a* 1 Ne. 17:52.
23 *a* MWM Ono.
24 *a* Yak. (Bib.) 5:16; 1 Ne. 2:16.
25 *a* 1 Ne. 11:1; Musa 1:1–2.

mambo makuu hivi, kama Bwana katika ufadhili wake kwa watoto wa watu amewafariji wanadamu kwa huruma kuu hivi, [a]kwa nini moyo wangu ulie na nafsi yangu kusita katika bonde la hofu, na mwili wangu kuwa mnyonge, na nguvu zangu kufifia, kwa sababu ya masumbuko yangu?

27 Na kwa nini [a]nitumikie dhambi, kwa sababu ya mwili wangu? Ndiyo, kwa nini niyakubali [b]majaribio, hata kwamba yule mwovu apate nafasi moyoni mwangu ya kuangamiza [c]amani na kusumbua nafsi yangu? Kwa nini nikasirishwe na adui yangu?

28 Amka, nafsi yangu! Usilemewe na dhambi tena. Shangilia, Ewe moyo wangu, na usimpatie [a]adui wa nafsi yangu mahali.

29 Usikasirike tena kwa sababu ya maadui zangu. Usipungukiwe na nguvu kwa sababu ya masumbuko yangu.

30 Shangilia, Ewe moyo wangu, na umlilie Bwana, na kusema: Ewe Bwana, nitakusifu milele; ndiyo, nafsi yangu itashangilia ndani yako, Mungu wangu, na [a]mwamba wa wokovu wangu.

31 Ewe Bwana, je, utaikomboa nafsi yangu? Je, utaniopoa kutoka mikononi mwa maadui zangu? Je, utanifanya kwamba nitetemeke nikiona [a]dhambi?

32 Na milango ya jehanamu ifungwe mbele yangu daima, kwa sababu [a]moyo wangu umevunjika na nafsi yangu imepondeka! Ewe Bwana, je, usiifunge milango ya haki yako mbele yangu, ili [b]nitembee katika mapito ya bonde iliyo chini, hata niwe mkali kwenye njia iliyo wazi!

33 Ewe Bwana, je, utanizingira na joho la haki yako! Ewe Bwana, je, utanitayarishia njia ya kutorokea maadui wangu! Je, utaninyooshea mapito yangu! Je, utaniwekea kikwazo kwa njia yangu—lakini kwamba unifanyie njia zangu ziwe wazi, na usizibe njia yangu, lakini njia za adui yangu.

34 Ewe Bwana, nimekuamini, na [a]nitakuamini milele. Sitaweka [b]tumaini langu kwenye mkono wa mwanadamu; kwani ninajua amelaaniwa yule anayeweka [c]tumaini lake kwa mkono wa mwanadamu. Ndiyo, amelaaniwa yule anayeweka tumaini lake kwa mwanadamu au amfanyaye kuwa mkono wake.

35 Ndiyo, ninajua kwamba Mungu humsaidia anayeomba bila [a]kizuizi. Ndiyo, Mungu wangu atanipatia, [b]nikiomba [c]bila kasoro; kwa hivyo nitakupazia sauti yangu; ndiyo, nitakulilia, Mungu wangu, mwamba wa haki yangu. Tazama, nitakupa-

26*a* Zab. 43:5.
27*a* Rum. 6:13.
b MWM Jaribu, Majaribu.
c MWM Amani.
28*a* MWM Ibilisi.
30*a* 1 Kor. 3:11. MWM Mwamba.
31*a* Rum. 12:9; Alma 13:12.
32*a* MWM Moyo Uliovunjika.
b MWM Tembea, Tembea na Mungu.
34*a* MWM Tegemea.
b Zab. 44:6–8.
c Yer. 17:5; Morm. 3:9; 4:8.
35*a* Yak. (Bib.) 1:5.
b MWM Sala.
c Hel. 10:5.

zia sauti yangu milele, [d]mwamba wangu na Mungu wangu asiye na mwisho. Amina.

MLANGO WA 5

Wanefi wajitenga kutoka kwa Walamani, wanatii sheria ya Musa, na kujenga hekalu—Kwa sababu ya kutoamini kwao, Walamani wanaondolewa kutoka uwepo wa Bwana, wanalaaniwa, na wanakuwa mjeledi kwa Wanefi. Karibia mwaka 588–559 K.K.

Tazama, ikawa kwamba mimi, Nefi, nilimlilia Bwana Mungu wangu, kwa sababu ya [a]hasira ya kaka zangu.

2 Lakini tazama, hasira yao ilinizidia, hata wakataka kunitoa uhai.

3 Ndiyo, walininung'unikia, wakisema: Mdogo yetu anataka [a]kututawala; na tumepatwa na majaribu mengi kwa sababu yake; kwa hivyo, tumuue sasa, ili tusisumbuke tena kwa sababu ya maneno yake. Kwani tazama, hatutakubali awe mtawala wetu; kwani utawala ni wetu, sisi ambao ni kaka zake wakubwa, kuwatawala hawa watu.

4 Sasa mimi siandiki kwenye mabamba haya maneno yote ambayo walininung'unikia. Lakini inatosha mimi kusema, kwamba walitaka kunitoa uhai wangu.

5 Na ikawa kwamba Bwana [a]alinionya, mimi, [b]Nefi, kwamba niwaondokee na nikimbilie huko nyikani, pamoja na wale wote watakaonifuata.

6 Kwa hivyo, ikawa kwamba mimi, Nefi, nilichukua jamaa yangu pia na [a]Zoramu na jamaa yake, na Samu, kaka yangu mkubwa, na jamaa yake, na Yakobo na Yusufu, kaka zangu wadogo, pia na dada zangu, na wale wote ambao wangenifuata. Na wale wote ambao wangenifuata ni wale ambao waliamini [b]maonyo na ufunuo wa Mungu; kwa hivyo, walitii maneno yangu.

7 Na tukachukua hema zetu na vitu ambavyo viliwezekana kwetu, na tukasafiri nyikani kwa muda wa siku nyingi. Na baada ya kusafiri kwa muda wa siku nyingi tulipiga hema zetu.

8 Na watu wangu walitaka tupaite pahali pale [a]Nefi; kwa hivyo, tulipaita Nefi.

9 Na wale wote waliokuwa na mimi waliamua kujiita [a]watu wa Nefi.

10 Na tuliendelea kutii hukumu, maagizo na amri za Bwana katika vitu vyote, kulingana na [a]sheria ya Musa.

11 Na Bwana alikuwa pamoja nasi; na tulifanikiwa zaidi; kwani tulipanda mbegu, na tukavuna kwa wingi. Na tukaanza kufuga mifugo, na makundi, na kila aina ya wanyama.

35 *d* Kum. 32:4.
5 1 *a* 2 Ne. 4:13–14.
3 *a* 1 Ne. 16:37–38; Mos. 10:14–15.
5 *a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi.
b Mos. 10:13.
6 *a* 1 Ne. 4:35; 16:7; 2 Ne. 1:30–32.
b MWM Onya, Onyo.
8 *a* Omni 1:12, 27; Mos. 9:1–4; 28:1.
9 *a* Yak. (KM) 1:13–14.
10 *a* 2 Ne. 11:4.
MWM Torati ya Musa.

12 Na mimi, Nefi, nilikuwa nimeleta pia kumbukumbu ambazo zilikuwa zimechorwa kwenye [a]mabamba ya shaba nyeupe; pamoja na [b]mpira, au [c]dira, ambayo baba yangu alitayarishiwa na mkono wa Bwana, kulingana na yale ambayo yameandikwa.

13 Na ikawa kwamba tulianza kufanikiwa zaidi, na kuongezeka katika nchi.

14 Na mimi, Nefi, nilichukua [a]upanga wa Labani, na nikatengeneza panga nyingi kwa umbo lake, nikishuku kwamba wale watu ambao sasa walikuwa wanaitwa [b]Walamani watatushukia na kutuangamiza; kwani nilijua chuki waliyokuwa nayo kwangu na kwa watoto wangu na kwa wale walioitwa watu wangu.

15 Na niliwafundisha watu wangu kujenga majengo, na kutengeneza vitu vya kila aina kwa kutumia mbao, na kwa [a]chuma, na kwa shaba nyekundu, na kwa shaba nyeupe, na kwa pua, na kwa dhahabu, na kwa fedha, na kwa mawe ya thamani, ambayo yalikuwa kwa wingi.

16 Na mimi, Nefi, nilijenga [a]hekalu; na nilijenga kwa umbo la [b]hekalu la Sulemani ila tu halikujengwa na vitu vingi vya [c]thamani; kwani havikupatikana nchini, kwa hivyo, haingejengeka kikamilifu kama hekalu la Sulemani. Lakini umbo la mjengo ulikuwa kama hekalu la Sulemani; na ujenzi wake ulikuwa wa hali ya juu.

17 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, niliwasababisha watu wangu kuwa na [a]bidii, na kutenda kazi kwa mikono yao.

18 Na ikawa kwamba walitaka niwe [a]mfalme wao. Lakini mimi, Nefi, sikutaka wapate mfalme; walakini, niliwatendea kulingana na yale ambayo yalikuwa kwenye uwezo wangu.

19 Na tazama, maneno ya Bwana yametimia kwa ndugu zangu ambayo alisema juu yao, kwamba nitakuwa [a]mtawala wao na [b]mwalimu wao. Kwa hivyo, nilikuwa mtawala wao na mwalimu wao, kulingana na amri za Bwana, hadi ule wakati ambao walitaka kunitoa uhai.

20 Kwa hivyo, neno la Bwana lilitimizwa ambalo alinizungumzia, akisema: Kadiri [a]watakapokataa kusikiliza maneno yako watatolewa kwenye uwepo wa Bwana. Na tazama, [b]waliondolewa kutoka uwepo wake.

21 Na akasababisha [a]laana iwashukie, ndiyo, hata laana

12 *a* Mos. 1:3–4. MWM Mabamba.
b Mos. 1:16.
c 1 Ne. 16:10, 16, 26; 18:12, 21; Alma 37:38–47; M&M 17:1.
14 *a* 1 Ne. 4:9; Yak. (KM) 1:10; M. ya Morm. 1:13.
b MWM Walamani.
15 *a* Eth. 10:23.
16 *a* MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
b 1 Fal. 6; 2 Nya. 3.
c M&M 124:26–27.
17 *a* Mwa. 3:19; M&M 42:42.
18 *a* Yak. (KM) 1:9, 11.
19 *a* 1 Ne. 2:22.
b MWM Fundisha, Mwalimu.
20 *a* 2 Ne. 2:21.
b Alma 9:14.
21 *a* MWM Laani, Laana.

kali, kwa sababu ya uovu wao. Kwani tazama, walishupaza mioyo yao kwake, kwamba wakawa kama gumegume; kwa hivyo, vile walikuwa weupe, na wenye ngozi nyororo na ya kuvutia na [b]kupendeza, ili wasiwashawishi watu wangu Bwana Mungu alisababisha wawe na [c]ngozi ya nyeusi.

22 Na hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu: Nitasababisha kwamba wawe [a]chukizo kwa watu wako, wasipotubu maovu yao.

23 Na italaaniwa uzao wa yule [a]atakayechanganyika na uzao wao; kwani watalaaniwa kwa laana kama ile. Na Bwana akainena, na ikatendeka.

24 Na kwa sababu ya laana yao ambayo ilikuwa juu yao wakawa watu [a]wavivu, walijawa na ujanja na udanganyifu, na waliwinda wanyama wa mwituni huko nyikani.

25 Na Bwana Mungu akaniambia: Watakuwa mjeledi kwa uzao wako, kuwachochea wao kunikumbuka; na wasiponikumbuka, na kusikiza maneno yangu, watawapiga hadi kuwaangamiza.

26 Na ikawa kwamba mimi, Nefi, [a]niliwatenga Yakobo na Yusufu, kwamba wawe makuhani na walimu katika nchi ya watu wangu.

27 Na ikawa kwamba tuliishi kwa furaha.

28 Na miaka thelathini ilikuwa imepita tangu tutoke Yerusalemu.

29 Na mimi, Nefi, nilikuwa nimeandika maandishi ya watu wangu, hadi ule wakati, kwenye yale mabamba nilizokuwa nimetengeneza.

30 Na ikawa kwamba Bwana Mungu akaniambia: Tengeneza [a]mabamba mengine; nawe utaandika vitu vingi kwenye mabamba ambavyo ni vyema machoni mwangu, kwa manufaa ya watu wako.

31 Kwa hivyo, mimi, Nefi, kwa kuwa ni mtiifu kwa amri za Bwana, nilienda na kutengeneza [a]mabamba haya ambayo nimeandikia vitu hivi.

32 Na niliandika yale ambayo yalimpendeza Mungu. Na kama watu wangu watafurahishwa na vitu vya Mungu watafurahishwa na maandishi yangu ambayo yako kwenye mabamba haya.

33 Na kama watu wangu wanataka kujua kikamilifu historia ya watu wangu lazima wasome yale mabamba yangu mengine.

34 Na inanitosha kusema kwamba miaka arobaini ilikuwa imepita, na tayari tulikuwa na vita na mabishano dhidi ya kaka zangu.

MLANGO WA 6

Yakobo aeleza historia ya Wayahudi: Uhamisho wa Kibabilonia

21 *b* 4 Ne. 1:10.
c 2 Ne. 26:33; 3 Ne. 2:14–16.
22 *a* 1 Ne. 12:23.
23 *a* MWM Ndoa, Oa, Olewa—Ndoa ya imani mbili.
24 *a* MWM Mvivu, Uvivu.
26 *a* Yak. (KM) 1:18–19; Mos. 23:17.
30 *a* 1 Ne. 19:1–6.
31 *a* MWM Mabamba.

na marejeo; huduma na kusulubiwa kwa yule Mtakatifu wa Israeli; msaada uliopokelewa kutokana na Wayunani; na uamsho wa siku za mwisho kwa Wayahudi watakapomwamini Masiya. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Maneno ya Yakobo, kaka yake Nefi, ambayo aliwazungumzia watu wa Nefi:

2 Tazameni, ndugu zangu wapendwa, mimi, Yakobo, nikiwa nimeitwa na Mungu, na kutawazwa wake mtakatifu, na nikiwa nimetawazwa na kaka yangu Nefi, ambaye mnamtegemea kama [a]mfalme au mlinzi, na ambaye pia mnamtegemea kwa usalama, tazameni mnajua kwamba nimewazungumzia vitu vingi zaidi.

3 Walakini, nawazungumzia tena; kwani ninajali ustawi wa nafsi zenu. Ndiyo, wasiwasi wangu ni mkubwa kwenu; na ninyi mnajua imekuwa hivyo tangu mwanzo. Kwani nimewashauri kwa bidii zote; na nimewafundisha maneno ya baba yangu; na nimewazungumzia ninyi kuhusu vitu vyote vilivyoandikwa, tangu kuumbwa kwa ulimwengu.

4 Na sasa, tazameni, ningewazungumzia kuhusu vitu vilivyo, na vile vitakavyokuja; kwa hivyo, nitawasomea maneno ya [a]Isaya. Na ni maneno yale ambayo kaka yangu anataka niwasomee. Na ninawazungumzia kwa manufaa yenu, ili mjifunze na kulitukuza jina la Mungu wenu.

5 Na sasa, maneno ambayo nitasoma ni yale ambayo Isaya alizungumza kuhusu nyumba yote ya Israeli; kwa hivyo, yanaweza kulinganishwa nanyi, kwani ninyi ni wa nyumba ya Israeli. Na kuna vitu vingi ambavyo vimezungumzwa na Isaya ambavyo vinaweza kulinganishwa nanyi, kwa sababu ninyi ni wa nyumba ya Israeli.

6 Na sasa, haya ndiyo maneno: [a]Hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu: Tazama, nitawainulia Wayunani mkono wangu, na kuwapeperushia watu [b]bendera yangu; na watawaleta wana wenu mikononi mwao, na kuwabeba mabinti zenu mabegani mwao.

7 Na wafalme watakuwa baba walezi wenu, na malkia wao watakuwa mama walezi wenu; watainamisha nyuso zao mbele zenu zikielekea udongoni, na kuramba mavumbi ya miguu yenu; nanyi mtajua kwamba Mimi ni Bwana; kwani wale [a]wanaonisubiri hawataaibika.

8 Na sasa mimi, Yakobo, nitazungumza kuhusu maneno haya. Kwani tazama, Bwana amenionyesha kwamba wale waliokuwa [a]Yerusalemu, kule tulipotoka, wameuawa na [b]kupelekwa utumwani.

6 2*a* Yak. (KM) 1:9, 11.
4*a* 3 Ne. 23:1.
6*a* Isa. 49:22–23.
b MWM Bendera.
7*a* M&M 133:45; Musa 1:6.
8*a* Esta 2:6; 1 Ne. 7:13; 2 Ne. 25:10; Omni 1:15; Hel. 8:20–21.
b 2 Fal. 24:10–16; 25:1–12.
MWM Israeli—Kutawanyika kwa Israeli.

9 Walakini, Bwana amenionyesha kwamba [a]watarejea tena. Na pia amenionyesha kwamba Bwana Mungu, aliye Mtakatifu wa Israeli, atajidhihirisha kwao katika mwili; na baada ya kujidhihirisha watampiga na [b]kumsulubu, kulingana na maneno ya malaika aliyenizungumzia.

10 Na baada ya wao kushupaza mioyo yao na kukaza shingo zao kwa yule Mtakatifu wa Israeli, tazama [a]hukumu za yule aliye Mtakatifu wa Israeli zitawateremkia. Na siku inakuja kwamba watachapwa na kusumbuliwa.

11 Kwa hivyo, baada ya wao kufukuzwa hapa na pale, kwani hivyo ndivyo asemavyo malaika, wengi watasumbuka sana mwilini, na hawatakubaliwa kuangamia, kwa sababu ya sala za walio waaminifu; watatawanywa, na kupigwa, na kuchukiwa; walakini, Bwana atawarehemu, kwamba [a]wakati [b]watakapomfahamu Mkombozi wao, [c]watakusanywa pamoja tena katika nchi yao ya urithi.

12 Na heri [a]Wayunani, wale ambao nabii ameandika juu yao; kwani tazama, kama watatubu na hawapigani na Sayuni, na wasijiunge na lile kanisa kuu la [b]machukizo, wataokolewa; kwani Bwana Mungu atatimiza [c]maagano yake aliyoagana na watoto wake; na ni kwa sababu hii nabii ameandika maneno haya.

13 Kwa hivyo, wale wanaopigana dhidi ya Sayuni na watu wa agano la Bwana wataramba mavumbi ya miguu yao; na watu wa Bwana [a]hawataaibika. Kwani watu wa Bwana ni wale [b]wanaomsubiri; kwani bado wanangoja kuja kwa Masiya.

14 Na tazama, kulingana na maneno ya nabii, Masiya ataanza tena kwa mara ya [a]pili kuwakomboa; kwa hivyo, [b]atajidhihirisha kwao kwa uwezo na utukufu mkuu, kwa [c]kuangamiza maadui wao, wakati siku ile itakapofika ambapo watamwamini; na hatamuangamiza yeyote yule atakayemwamini.

15 Na wale wasiomwamini yeye [a]wataangamizwa, kwa [b]moto, na kwa dhoruba, na kwa matetemeko ya ardhi, na kwa vita, na kwa [c]tauni, na kwa njaa. Na watajua kwamba Bwana ni Mungu, yule Mtakatifu wa Israeli.

16 [a]Kwani mawindo yatanyang'anywa kutoka wale wenye

9a 1 Ne. 10:3.
b 1 Ne. 19:10, 13; Mos. 3:9; 3 Ne. 11:14–15. MWM Kusulubiwa.
10a Mt. 27:24–25.
11a 1 Ne. 22:11–12; 2 Ne. 9:2.
b Hos. 3:5.
c MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
12a 1 Ne. 14:1–2; 2 Ne. 10:9–10.
b MWM Ibilisi—Kanisa la ibilisi.
c MWM Agano la Ibrahimu.
13a 3 Ne. 22:4.
b Isa. 40:31; 1 Ne. 21:23; M&M 133:45.
14a Isa. 11:11; 2 Ne. 25:17; 29:1.
b 2 Ne. 3:5.
c 1 Ne. 22:13–14.
15a 2 Ne. 10:16; 28:15; 3 Ne. 16:8. MWM Siku za Mwisho.
b Yak. (KM) 6:3.
c M&M 97:22–26.
16a Isa. 49:24–26.

nguvu, au [b]mateka halali kukombolewa?

17 Lakini Bwana asema hivi: Hata [a]mateka wa shujaa watanyakuliwa, na mawindo ya waovu kukombolewa; kwani [b]Mwenyezi Mungu [c]atawakomboa watu wake wa agano. Kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Nitashindana na wale wanaoshindana nawe—

18 Na nitawalisha wale wanaowadhulumu, kwa miili yao wenyewe; na watalewa kwa damu yao wenyewe kama vile kwa mvinyo mtamu; na miili yote itafahamu kwamba mimi Bwana ndiye Mwokozi wako na [a]Mkombozi wako, yule [b]Mwenye Enzi wa Yakobo.

MLANGO WA 7

Yakobo anaendelea kusoma kutoka katika Isaya: Isaya azungumza kimasiya—Masiya atakuwa na ulimi wa aliyeelimika—Atawapa mgongo Wake wale wampigao—Hatafadhaishwa—Linganisha Isaya 50. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Ndiyo, kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Je, nimekuweka kando, au kukutenga milele? Na hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Cheti cha talaka cha mama yako kiko wapi? Kwa nani nimekuweka, au ni kwa nani anayenidai nimekuuza? Ndiyo, kwa nani nimekuuza? Tazama, ni kwa uovu wenu [a]mmejiuza, na ni kwa makosa yenu mama yenu ametengwa.

2 Kwa hivyo, nilipokuja, hakukuwepo mtu yeyote; [a]nilipoita, ndiyo, hakukuwepo na yeyote wa kujibu. Ee nyumba ya Israeli, je, mkono wangu umefupishwa kwamba siwezi kukomboa, au sina uwezo wa kukomboa? Tazama, kwa kukemea kwangu ninakausha [b]bahari, ninafanya [c]mito yao kuwa nyika na [d]samaki wao kunuka kwa sababu maji yao yamekauka, na wanakufa kwa sababu ya kiu.

3 Ninavisha mbingu na [a]weusi, na kusababisha [b]gunia iwe mavazi yao.

4 Bwana Mungu amenipatia [a]ulimi wa aliyeelimika, kwamba niweze kujua jinsi ya kuwazungumzia katika majira, Ee nyumba ya Israeli. Wakati mmechoka anaamka asubuhi kwa asubuhi. Anaamsha sikio langu kusikia kama yule aliyeelimika.

5 Bwana Mungu amefungua [a]sikio langu, na sikuasi wala kurudi nyuma.

6 Niliwapatia [a]walionipiga mgongo wangu, na mashavu

16 *b* MY watu wa agano wa Bwana, kama ilivyoelezwa katika aya 17.
17 *a* 1 Ne. 21:25.
b MWM Yehova.
c 2 Fal. 17:39.
18 *a* MWM Mkombozi.
b Mwa. 49:24; Isa. 60:16.

7 1 *a* MWM Ukengeufu.
2 *a* Mit. 1:24–25; Isa. 65:12; Alma 5:37.
b Ku. 14:21; Zab. 106:9; M&M 133:68–69.
c Yos. 3:15–16.
d Ku. 7:21.
3 *a* Ku. 10:21.
b Ufu. 6:12.
4 *a* Lk. 2:46–47.
5 *a* M&M 58:1.
6 *a* Mt. 27:26; 2 Ne. 9:5.

yangu kwa waliong'oa nywele. Sikuuficha uso wangu kutokana na aibu na kutemewa mate.

7 Kwani Bwana Mungu atanisaidia, kwa hivyo sitafadhaishwa. Kwa hivyo nimekaza uso wangu kama jiwe, na ninajua kwamba sitaaibishwa.

8 Na Bwana yuko karibu, na ananitetea. Nani atashindana na mimi? Tusimame pamoja. Nani adui yangu? Anikaribie mimi, na nitampiga kwa nguvu za kinywa changu.

9 Kwani Bwana Mungu atanisaidia. Na wale [a]watakaonihukumu, tazama, wote watakuwa wazee kama nguo, na kuliwa na nondo.

10 Ni nani miongoni mwenu anayemwogopa Bwana, anayetii [a]sauti ya mtumishi wake, anayetembea kwa giza bila nuru?

11 Tazameni nyote mnaowasha moto, ambao mnajizingira kwa chembe za moto, tembeeni katika nuru ya moto [a]wenu na kwa chembe za moto mnaowasha. Mtapata haya kutoka mkono wangu—mtalala chini kwa huzuni.

MLANGO WA 8

Yakobo anaendelea kusoma kutoka katika Isaya: Katika siku za mwisho, Bwana ataifariji Sayuni na kukusanya Israeli—Walioko-mbolewa watakuja Sayuni kwa shangwe kuu—Linganisha Isaya 51 na 52:1–2. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Nisikizeni mimi, ninyi ambao mnatafuta haki. Tazameni [a]mwamba kutoka ambapo mlichongwa, na kwenye shimo mlikotolewa.

2 Tazameni Ibrahimu, [a]baba yenu, na [b]Sara, aliyewazaa; kwani nimemwita pekee, na kumbariki.

3 Kwani Bwana atafariji [a]Sayuni, atafariji sehemu zake zote zenye ukiwa; na atasababisha [b]nyika yake kuwa kama Edeni, na jangwa lake kama bustani ya Bwana. Shangwe na furaha itakuwa ndani yake, pia na shukrani na sauti ya uimbaji.

4 Nisikilizeni, watu wangu; na mnipe sikio, Ee taifa langu; kwani [a]sheria itatoka kwangu, na nitafanya hukumu zangu kubaki kama [b]mwangaza kwa watu.

5 Utakatifu yangu iko karibu; [a]wokovu wangu umesonga mbele, na mkono wangu utahukumu watu. [b]Visiwa vitaningoja, na watauamini mkono wangu.

6 Elekezeni macho yenu mbinguni, na mtazame huko chini duniani; kwani [a]mbingu [b]zitatoweka kama moshi, na dunia [c]itazeeka kama vazi; na wale wanaoishi ndani yake watakufa

9 *a* Rum. 8:31.
10 *a* M&M 1:38.
11 *a* Amu. 17:6.
8 1 *a* MWM Mwamba.
2 *a* Mwa. 17:1–8; M&M 132:49.
b Mwa. 24:36.
3 *a* MWM Sayuni.
b Isa. 35:1–2, 6–7.
4 *a* AU fundisho. Isa. 2:3. MWM Injili.
b MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
5 *a* MWM Wokovu.
b 2 Ne. 10:20.
6 *a* 2 Pet. 3:10.
b EBR kutawanywa. Zab. 102:25–27.
c EBR oza.

vivyo hivyo. Lakini wokovu wangu utakuwa milele, na haki yangu haitaondolewa.

7 Nisikilizeni mimi, ninyi ambao mnajua haki, wale watu ambao nimeandika sheria yangu moyoni mwao, [a]msiogope mzaha wa wanadamu, wala msiogope matusi yao.

8 Kwani nondo atawala kama vazi, na mchango kuwala kama manyoya. Lakini haki yangu itakuwa milele, na wokovu wangu utakuwa kutoka kizazi hadi kizazi.

9 Inuka, inuka! Vaa [a]nguvu, Ee mkono wa Bwana; inuka kama katika siku za kale. Kwani wewe sio yule aliyemchinja Rahabu, na kuumiza joka?

10 Kwani wewe sio yule ambaye amekausha bahari, maji ya kilindi kikuu; ambaye amesababisha kilindi cha bahari kuwa [a]njia ya wale waliokombolewa kupitia?

11 Kwa hivyo, wale [a]waliokombolewa na Bwana watarejea, na kuja Sayuni [b]wakiimba; na shangwe isiyo na mwisho na utakatifu itakuwa juu ya vichwa vyao, na watapokea furaha na shangwe; huzuni na [c]kuomboleza zitatoweka.

12 [a]Mimi ndimi; ndiyo, mimi ndimi yule anayekufariji. Tazama, wewe ni nani, kwamba [b]umwogope mwanadamu, atakayekufa, na mwanadamu, ambaye atafanywa kuwa kama [c]nyasi?

13 Na [a]kumsahau Bwana muumba wako, ambaye ametandaza mbingu, na kujenga msingi wa dunia, na ameendelea kuogopa kila siku, kwa sababu ya hasira ya mdhalimu, kama aliye tayari kukuangamiza? Na hasira ya mdhalimu iko wapi?

14 Mateka mkimbizi anaharakisha, ili afunguliwe, na kwamba asife shimoni, wala kwamba asikose mkate wake.

15 Lakini mimi ni Bwana Mungu wako, ambaye [a]mawimbi yake yalizuka; Bwana wa Majeshi ni jina langu.

16 Na nimeweka maneno yangu kinywani mwako, na kukuficha katika kivuli cha mkono wangu, ili nipande mbingu na kujenga msingi wa dunia, na kuambia Sayuni: Tazama, ninyi ni [a]watu wangu.

17 Inuka, inuka, simama wima, Ee Yerusalemu, ambaye amekunywa kutoka mkono wa Bwana [a]kikombe cha [b]hasira yake—umekunywa mabaki ya kikombe cha kuogopesha—

18 Na hakuna yeyote miongoni mwa wanawe wote aliozaa anayeweza kumwongoza; wala yule anayemchukua kwa mkono wake, miongoni mwa wana wale wote aliolea.

19 Hawa [a]wana wawili wamekujia, ambao watakuhurumia—

7a Zab. 56:4, 11; M&M 122:9.
9a M&M 113:7–8.
10a Isa. 35:8.
11a MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
b Isa. 35:10.
c Ufu. 21:4.
12a M&M 133:47; 136:22.
b Yer. 1:8.
c Isa. 40:6–8; 1 Pet. 1:24.
13a Yer. 23:27.
15a 1 Ne. 4:2.
16a 2 Ne. 3:9; 29:14.
17a Isa. 29:9; Yer. 25:15.
b Lk. 21:24.
19a Ufu. 11:3.

ukiwa na uangamizo wako, na njaa na upanga—na ni kwa kupitia nani nitakayekufariji?

20 Wana wako wamezimia, ila tu hawa wawili; wanangoja kwenye njia zote; kama ndume wa kichakani kwenye wavu, wamejaa hasira ya Bwana, kemeo la Mungu wako.

21 Kwa hivyo sikiliza haya sasa, wewe uliyesumbuka, na [a]kulewa, na sio kwa mvinyo:

22 Hivyo ndivyo asemavyo Bwana wako, Bwana na Mungu wako [a]anatetea maslahi ya watu wake; tazama, nimeondoa mkononi mwako kikombe cha kuogopesha, mabaki ya kikombe cha hasira yangu; wewe hutakinywa tena.

23 Lakini [a]Mimi nitakiweka mkononi mwa wale wanaokusumbua; wale ambao wameiambia nafsi yako: Inama chini, ili tupite juu—na wewe umelaza mwili wako chini na ukawa kama njia kwa wale waliopita.

24 [a]Inuka, inuka, vaa [b]nguvu zako, Ee [c]Sayuni; vaa mavazi yako maridadi, Ee Yerusalemu, mji mtakatifu; kwani tangu sasa wasiotahiriwa na walio wachafu [d]hawatakuingia.

25 Jitingishe kutoka mavumbini; [a]inuka, kaa chini, Ee Yerusalemu; jifungue kutokana na [b]vifungo vya shingo lako, Ee binti mateka wa Sayuni.

MLANGO WA 9

Yakobo anaelezea kwamba Wayahudi watakusanywa katika nchi zao zote za ahadi—Upatanisho ni ukombozi wa mwanadamu kutokana na Anguko—Miili ya wafu itafufuka kutoka kaburini, na roho zao zitatoka jehanamu na peponi—Watahukumiwa—Upatanisho unaokoa kutokana na kifo, jehanamu, ibilisi na mateso yasiyo na mwisho—Wenye haki wataokolewa katika ufalme wa Mungu—Adhabu ya dhambi yaelezwa—Yule Mtakatifu wa Israeli ni mlinzi wa mlango. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na sasa, ndugu zangu wapendwa, nimesoma vitu hivi ili mfahamu kuhusu yale [a]maagano ya Bwana aliyoagana na nyumba yote ya Israeli—

2 Kwamba amezungumza kwa Wayahudi, kwa kinywa cha manabii wake watakatifu, hata tangu mwanzo hadi chini, kizazi kwa kizazi, mpaka wakati ufike [a]watakaporejeshwa kwa lile kanisa la kweli na zizi la Mungu; wakati [b]watakapokusanywa nyumbani kwenye [c]nchi zao za urithi, na wataimarishwa katika nchi zao zote za ahadi.

3 Tazameni, ndugu zangu wapendwa, nawazungumzia vitu hivi ili kwamba mshangilie,

21 *a* 2 Ne. 27:4.
22 *a* Yer. 50:34.
23 *a* Zek. 12:9.
24 *a* Isa. 52:1–2.
b M&M 113:7–8.
c MWM Sayuni.
d Yoe. 3:17.
25 *a* MY Inuka kutoka mavumbini na uketi katika heshima, ukiwa umekombolewa hatimaye.
b M&M 113:9–10.

9 1 *a* MWM Agano la Ibrahimu.
2 *a* 2 Ne. 6:11.
MWM Urejesho wa Injili.
b MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
c 2 Ne. 10:7–8.
MWM Nchi ya Ahadi.

na [a]muinue vichwa vyenu juu milele, kwa sababu ya baraka ambazo Bwana Mungu atawateremshia watoto wenu.

4 Kwani najua kwamba wengi wenu, mmetafuta sana, kujua vitu vijavyo; kwa hivyo najua kwamba mnajua kuwa [a]miili yetu lazima izeeke na kufa; walakini, katika miili yetu tutamuona Mungu.

5 Ndiyo, najua kwamba mnajua kwamba atajidhihirisha kimwili kwa wale walio Yerusalemu, kule tulikotoka; kwani ni lazima iwe miongoni mwao; kwani ilimpasa [a]Muumba mkuu akubali kuwa chini ya mwanadamu katika mwili, na afe kwa wanadamu [b]wote, ili wanadamu wote wawe chini yake.

6 Kwani kifo kimewapata wanadamu wote, ili kutimiza [a]mpango wa huruma wa Muumba mkuu, inahitajika lazima pawe na nguvu ya [b]ufufuo, na inahitajika lazima ufufuo umfikie mwanadamu kwa sababu ya [c]mwanguko; na mwanguko ulitokana na kosa; na kwa sababu mwanadamu alianguka [d]alitengwa kutokana na uwepo wa Bwana.

7 Kwa hivyo, unahitajika uwe [a]upatanisho [b]usio na kipimo—bila huu upatanisho usio na kipimo huu uharibifu hauwezi kuvaa kutoharibika. Kwa hivyo, hukumu ya [c]kwanza iliyompata mwanadamu lazima [d]ingekuwa kwa muda usio na mwisho. Na kama ni hivyo, miili hii lazima ingelala chini kuoza na kurudi mavumbini ilipotoka, bila kufufuka tena.

8 Ee [a]hekima ya Mungu, [b]huruma zake na [c]neema! Kwani tazama, kama [d]miili haifufuki tena roho zetu lazima ziwe chini ya yule malaika [e]aliyeanguka kutoka uwepo wa Mungu wa Milele, na akawa [f]ibilisi, bila kufufuka tena.

9 Na roho zetu lazima zingekuwa kama yeye, na tuwe mashetani, [a]malaika kwa ibilisi, [b]kutengwa na uwepo wa Mungu wetu, na kuishi na baba wa [c]uwongo, katika huzuni, kama yeye mwenyewe; ndiyo, kwa kile kiumbe [d]kilichodanganya wazazi wetu wa kwanza, ambaye [e]hujigeuza kuwa [f]malaika wa

3 *a* TJS Zab. 24:7–10 (Kiambatisho).
4 *a* Ayu. 19:26; Alma 11:41–45; 42:23; Hel. 14:15; Morm. 9:13.
5 *a* MWM Umba, Uumbaji.
b Yn. 12:32; 2 Ne. 26:24; 3 Ne. 27:14–15.
6 *a* MWM Mpango wa Ukombozi.
b MWM Ufufuko.
c MWM Anguko la Adamu na Hawa.
d 2 Ne. 2:5.
7 *a* MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
b Alma 34:10.
c Mos. 16:4–5; Alma 42:6, 9, 14.
d Mos. 15:19.
8 *a* Ayu. 12:13; Ibr. 3:21. MWM Hekima.
b MWM Rehema, enye Rehema.
c MWM Neema.
d M&M 93:33–34.
e Isa. 14:12; 2 Ne. 2:17–18; Musa 4:3–4; Ibr. 3:27–28.
f MWM Ibilisi.
9 *a* Yak. (KM) 3:11; Alma 5:25, 39.
b Ufu. 12:7–9.
c MWM Kusema uongo.
d Mwa. 3:1–13; Mos. 16:3; Musa 4:5–19.
e 2 Kor. 11:14; Alma 30:53.
f M&M 129:8.

nuru, na huvuruga watoto wa watu kuwa na [g]makundi maovu ya siri na ya mauaji na kila aina ya kazi za siri za giza.

10 Ee jinsi gani ulivyo mkuu wema wa Mungu wetu, anayetutayarishia njia ya kuepuka kunaswa na huyu mnyama mwovu; ndiyo, huyo mnyama, [a]kifo na [b]jehanamu, ambayo naita kifo cha mwili, na pia kifo cha roho.

11 Na kwa sababu ya njia ya [a]ukombozi wa Mungu wetu, Mtakatifu wa Israeli, hiki [b]kifo, ambacho nimetaja, ambacho ni cha muda, kitaachilia wafu wake; kifo ambacho ni kaburi.

12 Na [a]kifo hiki ambacho nimetaja, ambacho ni kifo cha kiroho, kitaachilia wafu wake; kifo cha kiroho ambacho ni [b]jehanamu; kwa hivyo, kifo na jehanamu lazima ziachilie wafu wao, na jehanamu lazima iachilie roho zake zilizo utumwani, na kaburi lazima liachilie miili yake iliyo utumwani, na miili na [c]roho za wanadamu [d]itaunganishwa tena; na ni kwa nguvu za ufufuo za yule Mtakatifu wa Israeli.

13 Ee jinsi gani ulivyo mkuu [a]mpango wa Mungu wetu! Kwani katika njia nyingine, [b]peponi ya Mungu lazima iachilie roho za walio haki, na kaburi iachilie miili ya walio haki; na roho na mwili [c]kuunganishwa tena, na wanadamu wote wawe [d]wasioharibika, na wasiokufa, na wao ni nafsi zinazoishi, wakiwa na [e]ufahamu [f]kamili kama sisi tulio na miili, ila tu ufahamu wetu utakuwa kamili.

14 Kwa hivyo, tutakuwa na [a]ufahamu kamili wa [b]hatia zetu, na uchafu wetu, na [c]uchi wetu; na walio haki watakuwa na ufahamu kamili wa furaha yao, na [d]haki yao, wakiwa [e]wamevishwa [f]usafi, ndiyo, hata kwa [g]joho la haki.

15 Na itakuwa kwamba baada ya wanadamu wote kupita mauti haya ya kwanza na kupata uzima, jinsi vile wamekuwa wasiokufa, lazima watasimama mbele ya kiti cha [a]hukumu cha yule Mtakatifu wa Israeli; na kisha [b]hukumu itafika, na kisha lazima wahukumiwe kulingana na hukumu takatifu ya Mungu.

16 Na kwa hakika, kama Bwana anavyoishi, kwani Bwana Mungu amelizungumza, na ni [a]neno lake la milele, ambalo halikosi [b]kutimizwa, kwamba

9 *g* MWM Makundi maovu ya siri.
10 *a* Mos. 16:7–8; Alma 42:6–15.
b MWM Jehanamu.
11 *a* MWM Mwokozi.
b MWM Mauti ya Kimwili.
12 *a* MWM Mauti ya Kiroho.
b M&M 76:81–85.
c MWM Roho.
d MWM Ufufuko.
13 *a* MWM Mpango wa Ukombozi.
b M&M 138:14–19. MWM Peponi.
c Alma 11:43.
d MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
e M&M 130:18–19.
f MWM Kamilifu.
14 *a* Mos. 3:25; Alma 5:18.
b MWM Hatia.
c Morm. 9:5.
d MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
e Mit. 31:25.
f MWM Safi na Isiyo safi.
g M&M 109:76.
15 *a* MWM Hukumu ya mwisho.
b Zab. 19:9; 2 Ne. 30:9.
16 *a* 1 Fal. 8:56; M&M 1:38; Musa 1:4.
b M&M 56:11.

wale walio haki bado watakuwa haki, na wale walio [c]waovu bado watakuwa [d]waovu; kwa hivyo, wale ambao ni waovu ni [e]ibilisi na malaika wake; na watatupwa kwenye moto usio na [f]mwisho, waliotayarishiwa; na mateso yao ni kama [g]ziwa la moto na kiberiti ambacho ndimi zake zinapanda juu milele na daima bila mwisho.

17 Ee jinsi gani ilivyo kuu [a]haki ya Mungu wetu! Kwani anatimiza maneno yake yote, na yametoka kinywani mwake, na sheria yake lazima itimizwe.

18 Lakini, tazama, [a]watakatifu, wale wateule wa yule Mtakatifu wa Israeli, wale ambao wamemwamini yule Mtakatifu wa Israeli, wale ambao wamevumilia [b]misalaba ya ulimwengu, na kudharau aibu yake, [c]watarithi [d]ufalme wa Mungu, ambao walitayarishiwa [e]tangu mwanzo wa dunia, na shangwe yao itakuwa tele [f]milele.

19 Ee jinsi gani ilivyo kuu rehema ya Mungu wetu, yule Mtakatifu wa Israeli! Kwani [a]huwakomboa watakatifu wake kutokana na yule mnyama [b]mwovu yaani ibilisi, na kifo, na [c]jehanamu, na lile ziwa la moto na kiberiti, ambalo ni mateso yasiyo na mwisho.

20 Ee jinsi gani ulivyo mkuu [a]utakatifu wa Mungu wetu! Kwani [b]anafahamu vitu vyote, na hakuna jambo lolote asilolijua.

21 Na anakuja ulimwenguni ili [a]awaokoe wanadamu wote kama watakubali sauti yake; kwani tazama, anapokea [b]maumivu ya wanadamu wote, ndiyo, maumivu ya kila kiumbe kinachoishi, waume kwa wake, na watoto, ambao ni wa jamii ya [c]Adamu.

22 Na anakubali haya ili ufufuo uwafikie wanadamu wote, ili wote wasimame mbele yake katika siku ile kuu ya hukumu.

23 Na anawaamuru wanadamu wote kwamba lazima [a]watubu, na [b]wabatizwe katika jina lake, wakiwa na imani kamili katika yule Mtakatifu wa Israeli, au kama sivyo hawawezi kuokolewa katika ufalme wa Mungu.

24 Na kama hawatatubu na kuamini katika [a]jina lake, na kubatizwa kwa jina lake, na [b]kuvumilia hadi mwisho, lazima wapate [c]laana ya milele; kwani Bwana Mungu, yule Mtakatifu wa Israeli, amezungumza.

25 Kwa hivyo, ametoa [a]sheria;

16 *c* MWM Chafu, Uchafu.
d 1 Ne. 15:33–35; Alma 7:21; Morm. 9:14; M&M 88:35.
e MWM Ibilisi.
f Mos. 27:28.
g Ufu. 21:8; 2 Ne. 28:23; M&M 63:17.

17 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.

18 *a* MWM Mtakatifu.
b Lk. 14:27.
c M&M 45:58; 84:38.
d MWM Kuinuliwa.
e Alma 13:3.
f MWM Uzima wa Milele.

19 *a* M&M 108:8.
b 1 Ne. 15:35.
c MWM Jehanamu.

20 *a* MWM Utakatifu.
b Alma 26:35; M&M 38:2.

21 *a* MWM Wokovu.
b M&M 18:11; 19:18.
c MWM Adamu.

23 *a* MWM Toba, Tubu.
b MWM Batiza, Ubatizo.

24 *a* MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
b MWM Stahimili.
c MWM Hukumu.

25 *a* Yak. (Bib.) 4:17. MWM Sheria.

na ambapo [b]hakuna sheria imetolewa hakuna adhabu; na pasipo adhabu hakuna hukumu; na pasipo hukumu rehema za yule Mtakatifu wa Israeli zinawadai, kwa sababu ya upatanisho; kwani wanakombolewa kwa nguvu zake.

26 Kwani [a]upatanisho unatimiza madai yake ya [b]haki kwa wale ambao [c]hawakupatiwa [d]sheria, kwamba wanakombolewa kutokana na yule mnyama mwovu, kifo na jehanamu, na yule ibilisi, na ziwa la moto na kiberiti, ambalo ni mateso bila mwisho; na wanarejeshwa kwa yule Mungu aliyewapatia [e]pumzi, ambaye ni yule Mtakatifu wa Israeli.

27 Lakini ole kwa yule ambaye alipewa [a]sheria, ndiyo, aliye na sheria zote za Mungu, kama sisi, na huzivunja, na yule anayepoteza siku za majaribio yake, kwani hali yake ni mbovu!

28 Ee ule [a]mpango wa ujanja wa yule mwovu! Ee [b]utupu, na ugoigoi, na upumbavu wa wanadamu! [c]Wanapoelimika wanadhani kwamba wana [d]hekima, na hawasikii [e]mawaidha ya Mungu, kwani wanaiweka kando, wakifikiria kwamba wanajua wenyewe, kwa hivyo, hekima yao ni ujinga na haiwafaidi. Na wataangamia.

29 Lakini kuelimika ni vyema ikiwa [a]watatii [b]mawaidha ya Mungu.

30 Lakini ole kwa [a]matajiri, ambao ni matajiri kwa vitu vya ulimwengu. Kwani kwa sababu wao ni matajiri wanachukia walio [b]masikini, na wanawatesa wale wapole, na mioyo yao iko kwenye hazina yao; kwa hivyo, hazina yao ni mungu wao. Na tazama, hazina yao itaangamia nao pia.

31 Na ole kwa viziwi wale [a]wasiosikia; kwani wataangamia.

32 Ole pia kwa wale walio vipofu wasioona; kwani nao pia wataangamia.

33 Ole kwa wale wasiotairiwa moyoni, kwani ufahamu wa maovu yao utawasonga katika siku ya mwisho.

34 Ole kwa aliye [a]mdanganyifu, kwani atatupwa [b]jehanamu.

35 Ole kwa muuaji [a]anayeua akitaka, kwani [b]atakufa.

36 Ole kwa wale wanaotenda

25 *b* Rum. 4:15; 2 Ne. 2:13; Alma 42:12–24. MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
26 *a* 2 Ne. 2:10; Alma 34:15–16. MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
c Mos. 3:11.
d Mos. 15:24; M&M 137:7.
e Mwa. 2:7; M&M 93:33; Ibr. 5:7.
27 *a* Lk. 12:47–48.
28 *a* Alma 28:13.
b MWM Majivuno, Siofaa.
c Lk. 16:15; 2 Ne. 26:20; 28:4, 15.
d Mit. 14:6; Yer. 8:8–9; Rum. 1:22. MWM Hekima; Kiburi.
e Alma 37:12. MWM Ushauri.
29 *a* 2 Ne. 28:26.
b Yak. (KM) 4:10.
30 *a* Lk. 12:34; 1 Tim. 6:10; M&M 56:16.
b MWM Maskini.
31 *a* Eze. 33:30–33; Mt. 11:15; Mos. 26:28; M&M 1:2, 11, 14; Musa 6:27.
34 *a* Mit. 19:9. MWM Kusema uongo; Mwaminifu, Uaminifu.
b MWM Jehanamu.
35 *a* Ku. 20:13; Mos. 13:21.
b MWM Adhabu Kuu.

[a]ukahaba, kwani watatupwa jehanamu.

37 Ndiyo, ole kwa wale [a]wanaoabudu masanamu, kwani ibilisi wa ibilisi wote huwafurahia.

38 Na, mwishowe, ole kwa wale wote wanaokufa katika dhambi zao; kwani [a]watamrejea Mungu, na kuona uso wake, na kubaki katika dhambi zao.

39 Ee, ndugu zangu wapendwa, kumbukeni uovu wa kumkosea yule Mungu Mtakatifu, na pia uovu wa kukubali ushawishaji wa yule [a]mwovu. Kumbukeni, kufikiria [b]kimwili ni [c]kifo, na kufikiria kiroho ni [d]uzima wa [e]milele.

40 Ee, ndugu zangu wapendwa, sikilizeni maneno yangu. Kumbukeni ukuu wa yule Mtakatifu wa Israeli. Msiseme kwamba nimezungumza vitu vigumu dhidi yenu; kwani mkifanya hivyo, mtaasi kinyume cha [a]ukweli; kwani nimenena maneno ya Muumba wenu. Najua kwamba maneno ya kweli ni [b]makali kwa uchafu wote; lakini walio haki hawayaogopi, kwani wanapenda ukweli na hawatingishwi.

41 Kisha, Ee ndugu zangu wapendwa, [a]njooni kwa Bwana, yule Mtakatifu. Kumbuka kwamba mapito yake ni matakatifu. Tazama, [b]njia ya mwanadamu ni [c]nyembamba, lakini imenyooka mbele yake, na [d]mlinzi wa mlango ni yule Mtakatifu wa Israeli; na haajiri mtumishi yeyote pale; na hakuna njia nyingine yoyote isipokuwa kwa mlango; kwani hawezi kudanganywa, kwani Bwana Mungu ndilo jina lake.

42 Na kwa yeyote anayebisha, kwake yeye atamfungulia; na kwa wenye [a]hekima, na walioelimika, na wale walio matajiri, ambao [b]wanajidai kwa sababu ya elimu yao, na hekima yao, na utajiri wao—ndiyo, hao ndiyo anaochukia; na wasipoacha vitu hivi, na wajichukue kama [c]wajinga mbele ya Mungu, na [d]kunyenyekea, hatawafungulia.

43 Lakini vitu vya wenye hekima na walio werevu [a]vitafichwa kwao milele—ndiyo, furaha ile iliyotayarishiwa watakatifu.

44 Ee, ndugu zangu wapendwa, kumbukeni maneno yangu. Tazama, navua mavazi

36 *a* 3 Ne. 12:27–29. MWM Usafi wa Kimwili.
37 *a* MWM Kuabudu sanamu.
38 *a* Alma 40:11, 13.
39 *a* 2 Ne. 28:20–22; 32:8; Mos. 2:32; 4:14; Alma 30:53.
b Rum. 8:6. MWM Tamaa za kimwili.
c MWM Mauti ya Kiroho.
d Mit. 11:19.
e MWM Uzima wa Milele.
40 *a* MWM Ukweli.
b 1 Ne. 16:2; 2 Ne. 28:28; 33:5.
41 *a* 1 Ne. 6:4; Yak. (KM) 1:7; Omni 1:26; Moro. 10:30–32.
b 2 Ne. 31:17–21; Alma 37:46; M&M 132:22, 25.
c Lk. 13:24; 2 Ne. 33:9; Hel. 3:29–30.
d 2 Ne. 31:9, 17–18; 3 Ne. 14:13–14; M&M 43:7; 137:2.
42 *a* Mt. 11:25.
b MWM Kiburi.
c 1 Kor. 3:18–21.
d MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
43 *a* 1 Kor. 2:9–16.

yangu, na kuzisukasuka mbele yenu; Naomba kwamba Mungu wa wokovu wangu anitazame na jicho lake linaloona [a]kila mahali; kwa hivyo, mtajua katika siku ile ya mwisho, wakati wanadamu wote watakapo hukumiwa kulingana na kazi zao, kwamba Mungu wa Israeli alishuhudia kwamba [b]nilijitoa mzigo wa maovu yenu kutoka nafsi yangu, na kwamba nasimama kwa usafi mbele yake, na kwamba damu yenu [c]haiko juu yangu.

45 Ee, ndugu zangu wapendwa, acheni dhambi zenu; jifungueni [a]minyororo ya yule atakayewafunga; njooni kwa yule Mungu aliye [b]mwamba wa wokovu wenu.

46 Tayarisheni nafsi zenu kwa siku ile ya [a]utukufu ambapo wale walio watakatifu watahudumiwa kwa haki, hata siku ile ya [b]hukumu, kwamba msitetemeke kwa woga; na kwamba msikumbuke [c]hatia yenu ya uovu katika ukamilifu, na mlazimishwe kulia: Takatifu, takatifu ni hukumu zako, Ee Bwana Mungu [d]Mwenyezi—lakini najua hatia yangu; nilivunja sheria yako, na makosa yangu ni yangu; na ibilisi amenipata, na kwamba mimi ni mawindo kwa huzuni yake mbovu.

47 Lakini tazameni, ndugu zangu, je, ni lazima niwafahamishe huu ukweli wa kutisha wa vitu hivi? Je, ningesumbua nafsi zenu kama mawazo yenu yangekuwa mema? Ningekuwa wazi kwenu kulingana na udhahiri wa kweli kama mngepata uhuru wa dhambi?

48 Tazama, kama mngekuwa watakatifu ningewazungumzia kuhusu utakatifu; lakini kwa vile ninyi sio watakatifu, na mnanitegemea mimi kama mwalimu, lazima [a]niwafundishe kuhusu matokeo ya [b]dhambi.

49 Tazama, nafsi yangu inachukia dhambi, na moyo wangu unafurahishwa na haki; na [a]nitalisifu jina takatifu la Mungu wangu.

50 Njooni, ndugu zangu, kila mmoja aliye na kiu, njooni kwenye [a]maji; na yule asiye na pesa, njoo ununue na ule; ndiyo, njooni mnunue mvinyo na maziwa bila [b]pesa na bei.

51 Kwa hivyo, msitumie pesa zenu kwa yale yasiyo na thamani, wala [a]nguvu zenu kwa yale yasiyotosheleza. Mnisikilize kwa makini, na mkumbuke yale maneno ambayo nimezungumza; na mje kwa yule Mtakatifu wa Israeli, na [b]mle yale yasiyoangamia, wala kuharibiwa, na mruhusu nafsi zenu zifurahie unono.

52 Tazameni, ndugu zangu wapendwa, kumbukeni maneno

44*a* Yak. (KM) 2:10.
b Yak. (KM) 1:19.
c Yak. (KM) 2:2; Mos. 2:28.
45*a* 2 Ne. 28:22; Alma 36:18.
b MWM Mwamba.
46*a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b MWM Hukumu ya mwisho.
c Mos. 3:25.
d 1 Ne. 1:14; Musa 2:1.
48*a* Alma 37:32.
b MWM Dhambi.
49*a* 1 Ne. 18:16.
50*a* MWM Maji ya Uzima.
b Alma 42:27.
51*a* Isa. 55:1–2.
b 2 Ne. 31:20; 32:3; 3 Ne. 12:6.

ya Mungu wenu; muombeni bila kukoma kwa mchana, na [a]mshukuru jina lake takatifu kwa usiku. Acheni mioyo yenu ishangilie.

53 Na tazameni jinsi gani yalivyo makuu [a]maagano ya Bwana, na jinsi gani ulivyo mkuu ufadhili wake kwa watoto wa watu; na kwa sababu ya ukuu wake, na neema yake na [b]rehema, ametuahidi kwamba uzao wetu hautaangamizwa kabisa, kimwili, lakini kwamba atawahifadhi; na katika vizazi vya baadaye watakuwa [c]tawi takatifu kwa nyumba ya Israeli.

54 Na sasa, ndugu zangu, ningewazungumzia zaidi; lakini kesho nitawaelezea maneno yangu yaliyosalia. Amina.

MLANGO WA 10

Yakobo anaeleza kwamba Wayahudi watamsulubisha Mungu wao—Watatawanywa mpaka waanze kumwamini Yeye—Marekani itakuwa nchi ya uhuru ambako hakuna mfalme yeyote atakayetawala—Jipatanisheni na Mungu na pokeeni wokovu kwa neema Yake. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na sasa mimi, Yakobo, nawazungumzia tena, ndugu zangu wapendwa, kuhusu [a]tawi hili takatifu ambalo nimelitaja.

2 Kwani tazama, ahadi ambazo tumepokea ni [a]ahadi kwetu kuhusu kimwili; kwa hivyo, kwa vile nimeonyeshwa kwamba watoto wetu wengi wataangamia kimwili kwa sababu ya kutoamini, walakini, Mungu atawarehemu wengi; na watoto wetu watarejeshwa, ili wapokee kile ambacho kitawapatia ufahamu wa kweli wa Mkombozi wao.

3 Kwa hivyo, kama vile nilivyowaambia, lazima inahitajika kwamba Kristo—kwani usiku uliopita [a]malaika aliniambia kwamba hili litakuwa jina lake—[b]atakuja miongoni mwa Wayahudi, miongoni mwa wale ambao ni waovu zaidi ulimwenguni; na [c]watamsulubu—hivyo ndivyo ilimpasa Mungu wetu, na hakuna taifa lingine duniani ambalo [d]lingemsulubu [e]Mungu wao.

4 Kwani [a]miujiza mikuu ingetendwa miongoni mwa mataifa mengine wangetubu, na wangejua kwamba yeye ni Mungu wao.

5 Lakini kwa sababu ya [a]ukuhani wa uongo, walio Yerusalemu watamkazia shingo zao, hata mpaka asulubiwe.

6 Kwa hivyo, kwa sababu ya uovu wao, maangamizo, njaa, tauni, na umwagaji wa damu

52*a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
53*a* MWM Agano.
b MWM Rehema, enye Rehema.
c MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
10 1*a* 1 Ne. 15:12–16; 2 Ne. 3:5; Yak. (KM) 5:43–45.
2*a* 1 Ne. 22:8; 3 Ne. 5:21–26; 21:4–7.
3*a* 2 Ne. 25:19; Yak. (KM) 7:5; Moro. 7:22.
b MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.
c 1 Ne. 11:33; Mos. 3:9; M&M 45:52–53.
d Lk. 23:20–24.
e 1 Ne. 19:10.
4*a* MWM Muujiza.
5*a* Lk. 22:2. MWM Ukuhani wa uongo.

zitawapata; na wale ambao hawataangamizwa [a]watatawanywa miongoni mwa mataifa yote.

7 Lakini tazama, hivyo ndivyo asemavyo [a]Bwana Mungu: Siku [b]itakapofika watakaponiamini, kwamba mimi ni Kristo, basi nimeagana na baba zao kwamba watarejeshwa kimwili, duniani, kwenye nchi za urithi wao.

8 Na itakuwa kwamba [a]watakusanywa kutoka mtawanyiko wao wa muda mrefu, kutoka [b]visiwa vya bahari, na kutoka sehemu nne za dunia; na mataifa ya Wayunani yatakuwa makuu machoni mwangu, asema Mungu, kwa [c]kuwapeleka katika nchi zao za urithi.

9 [a]Ndiyo, wafalme wa Wayunani watakuwa baba zao walezi, na malkia wao watakuwa mama walezi; kwa hivyo, [b]ahadi za Bwana ni kuu kwa Wayunani, kwani ameizungumza, na nani anayeweza kubisha?

10 Lakini tazama, nchi hii, Mungu alisema, itakuwa nchi ya urithi wako, na [a]Wayunani watabarikiwa katika nchi hii.

11 Na nchi hii itakuwa nchi ya [a]uhuru kwa Wayunani, na hakutakuwa na [b]wafalme katika nchi hii, ambao watainuka juu ya Wayunani.

12 Na nitaimarisha nchi hii dhidi ya nchi zingine zote.

13 Na yule [a]anayepigana na Sayuni [b]ataangamia, asema Mungu.

14 Kwani yule anayeniinulia mfalme ataangamia, kwani mimi, Bwana, [a]mfalme wa mbingu, nitakuwa mfalme wao, na nitakuwa [b]nuru kwao milele, kwa wale wanaosikia maneno yangu.

15 Kwa hivyo, kwa sababu hii, ili [a]maagano yangu niliyoagana na watoto wa watu yaweze kutimizwa, yale nitakayowatendea kimwili, lazima niangamize kazi za [b]siri za [c]giza, na za mauaji, na za machukizo.

16 Kwa hivyo, yule anayepigana dhidi ya [a]Sayuni, Myahudi na Myunani, mateka na walio huru, waume kwa wake, wataangamia; kwani [b]wao ndiyo makahaba wa dunia yote; kwani [c]wale [d]wasio wangu wako [e]dhidi yangu, asema Mungu.

17 Kwani [a]nitatimiza ahadi zangu ambazo niliagana na wanadamu, kwamba nitawatendea kimwili—

18 Kwa hivyo, ndugu zangu

6*a* 1 Ne. 19:13–14. MWM Israeli—Kutawanyika kwa Israeli.
7*a* MWM Bwana.
b 2 Ne. 25:16–17.
8*a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b 1 Ne. 22:4; 2 Ne. 10:20–22; M&M 133:8.
c 1 Ne. 22:8.
9*a* Isa. 49:22–23.
b 1 Ne. 22:8–9; M&M 3:19–20.
10*a* 2 Ne. 6:12.
11*a* MWM Huru, Uhuru.
b Mos. 29:31–32.
13*a* 1 Ne. 22:14, 19.
b Isa. 60:12.
14*a* Alma 5:50; M&M 38:21–22; 128:22–23; Musa 7:53.
b MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
15*a* MWM Agano.
b Hel. 3:23. MWM Makundi maovu ya siri.
c MWM Giza, Kiroho.
16*a* MWM Sayuni.
b 1 Ne. 13:4–5.
c 1 Ne. 14:10.
d 1 Ne. 22:13–23; 2 Ne. 28:15–32; 3 Ne. 16:8–15; Eth. 2:9.
e Mt. 12:30.
17*a* M&M 1:38.

wapendwa, hivyo ndivyo asemavyo Mungu wetu: Nitasumbua uzao wenu kwa mkono wa [a]Wayunani; walakini, nitalainisha mioyo ya Wayunani, kwamba watakuwa kama baba kwao; kwa hivyo, Wayunani [b]watabarikiwa na [c]kuhesabiwa miongoni mwa nyumba ya Israeli.

19 Kwa hivyo, nitaiwekea [a]wakfu uzao wako hii nchi, na wale watakao hesabiwa miongoni mwa uzao wako, milele, kuwa nchi yao ya urithi; kwani ni nchi bora, Mungu ananiambia, zaidi ya nchi zingine zote, kwa hivyo nitawataka wanadamu wote wanaoishi juu yake kwamba wataniabudu, asema Mungu.

20 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, kwa vile Mungu wetu wa huruma ametupatia ufahamu mkuu hivyo kuhusu vitu hivi, hebu tumkumbuke, na kuacha dhambi zetu, na tusiinamishe vichwa vyetu, kwani hatujatupwa; walakini, [a]tumefukuzwa kutoka nchi yetu ya urithi; lakini tumeongozwa hadi nchi ile iliyo [b]bora zaidi, kwani Bwana amesababisha bahari kuwa [c]njia yetu, na tuko kwenye [d]kisiwa cha bahari.

21 Lakini kubwa ni ahadi za Bwana kwa wale walio kwenye [a]visiwa vya bahari; kwa hivyo kama vile inavyosema visiwa, lazima pawe na zaidi ya haya, na pia wale wanaoishi humo ni ndugu zetu.

22 Kwani tazama, Bwana Mungu [a]ametoa kutoka nyumba ya Israeli mara kwa mara, kulingana na nia na furaha yake. Na sasa tazama, Bwana hukumbuka wale wote waliotengwa, kwa hivyo anatukumbuka pia sisi.

23 Kwa hivyo, changamsheni mioyo yenu, na kumbukeni kwamba mko [a]huru [b]kujitendea—[c]kuchagua njia ya kifo kisicho na mwisho au njia ya uzima wa milele.

24 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, jipatanisheni na nia ya Mungu, na sio kwa nia ya ibilisi na mwili; na kumbukeni, baada ya kupatanishwa na Mungu, kwamba ni kwa kupitia [a]neema ya Mungu pekee [b]mnaokolewa.

25 Kwa hivyo, Mungu awafufue kutoka kwa wafu kwa nguvu za ufufuo, na pia kutoka kifo kisicho na mwisho kwa nguvu za [a]upatanisho, kwamba mpokelewe katika ufalme wa milele wa Mungu, kwamba mmsifu kwa neema takatifu. Amina.

MLANGO WA 11

Yakobo alimwona Mkombozi

18*a* Lk. 13:28–30; M&M 45:7–30.
b Efe. 3:6.
c Gal. 3:7, 29; 1 Ne. 14:1–2; 3 Ne. 16:13; 21:6, 22; 30:2; Ibr. 2:9–11.

19*a* 2 Ne. 3:2.

20*a* 1 Ne. 2:1–4.
b 1 Ne. 2:20. MWM Nchi ya Ahadi.
c 1 Ne. 18:5–23.
d Isa. 11:10–12.

21*a* 1 Ne. 19:15–16; 22:4.

22*a* 1 Ne. 22:4.

23*a* MWM Haki ya uamuzi.
b 2 Ne. 2:16.
c Kum. 30:19.

24*a* MWM Neema.
b MWM Wokovu.

25*a* MWM Lipia dhambi, Upatanisho.

wake—Sheria ya Musa inamwakilisha Kristo na kuthibitisha kwamba Yeye atakuja. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na sasa, [a]Yakobo aliwaambia watu wangu vitu vingi zaidi katika ule wakati; walakini ni hivi vitu pekee nimesababisha [b]viandikwe, kwani vitu nilivyoandika vimenitosha.

2 Na sasa mimi, Nefi, naandika maneno zaidi ya [a]Isaya, kwani nafsi yangu inafurahia maneno yake. Kwani nitalinganisha maneno yake kwa watu wangu, na nitayatuma kwa watoto wangu wote, kwani kweli alimwona [b]Mkombozi wangu, kama vile nilivyomwona.

3 Na kaka yangu, Yakobo, pia [a]amemwona vile nilivyomwona; kwa hivyo, nitayatuma maneno yao kwa watoto wangu kuwathibitishia wao kwamba maneno yangu ni ya kweli. Kwa hivyo, Mungu amesema, kwa maneno ya [b]watatu, nitaimarisha neno langu. Walakini, Mungu huwatuma mashahidi wengi, na anathibitisha maneno yake yote.

4 Tazama, nafsi yangu inafurahia [a]kuwathibitishia watu wangu ukweli wa [b]kuja kwa Kristo; kwani, ni kwa lengo hili kwamba [c]sheria ya Musa imetolewa; na vitu vyote vilivyopewa na Mungu tangu mwanzo wa dunia, kwa mwanadamu, ni kielelezo chake.

5 Na pia nafsi yangu inafurahia [a]maagano ya Bwana aliyoagana na baba zetu; ndiyo, moyo wangu unafurahia neema yake, na katika haki yake, na nguvu, na rehema zilizo katika mpango mkuu wa milele wa ukombozi kutoka mauti.

6 Na nafsi yangu inafurahia kuwathibitishia watu wangu kwamba [a]ijapokuwa Kristo aje lazima wanadamu wote waangamie.

7 Kwani kama hakuna Kristo [a]hakuna Mungu; na kama hakuna Mungu basi nasi hatupo, kwani hakungekuwa na [b]uumbaji. Lakini kuna Mungu, na yeye ni Kristo, na atakuja katika utimilifu wa wakati wake mwenyewe.

8 Na sasa naandika baadhi ya maneno ya Isaya, ili wowote wa watu wangu watakaoona maneno haya wangeinua mioyo yao na kufurahia kwa wanadamu wote. Sasa haya ndiyo maneno, na mnaweza kuyalinganisha nanyi na kwa wanadamu wote.

MLANGO WA 12

Isaya anaona hekalu la siku za mwisho, kusanyiko la Israeli, na hukumu ya milenia na amani—Walio na kiburi na waovu

11 1*a* 2 Ne. 6:1–10.
b 2 Ne. 31:1.
2*a* 3 Ne. 23:1.
b MWM Mkombozi.
3*a* 2 Ne. 2:3; Yak. (KM) 7:5.
b 2 Ne. 27:12; Eth. 5:2–4; M&M 5:11.
4*a* 2 Ne. 31:2.
b Yak. (KM) 4:5; Yar. 1:11; Alma 25:15–16; Eth. 12:19.
c 2 Ne. 5:10.
5*a* MWM Agano la Ibrahimu.
6*a* Mos. 3:15.
7*a* 2 Ne. 2:13.
b MWM Umba, Uumbaji.

watashushwa chini katika Ujio Wake wa Pili—Linganisha Isaya 2. Karibia mwaka 559–545 K.K.

NENO ambalo [a]Isaya, mwana wa Amozi, [b]aliona kuhusu Yuda na Yerusalemu:

2 Na itakuwa kwamba katika siku za mwisho, wakati [a]mlima wa [b]nyumba ya Bwana utajengwa kileleni mwa [c]milima, na utainuliwa juu ya vilima, na mataifa yote yataitiririkia.

3 Na watu wengi wataenda na kusema, Njooni ninyi, na hebu twende juu ya mlima wa Bwana, kwenye nyumba ya Mungu wa Yakobo; na atatufundisha njia zake, na [a]tutatembea katika mapito yake; kwani kutoka Sayuni itatokea [b]sheria, na neno la Bwana kutoka Yerusalemu.

4 Na [a]atahukumu miongoni mwa mataifa, na kukemea watu wengi: na watafua panga zao kuwa majembe, na mikuki yao itakuwa visu vya kupogoa—taifa halitainua upanga kwa taifa lingine, wala hawatajifunza vita tena.

5 Ee nyumba ya Yakobo, njooni na tutembee katika nuru ya Bwana; ndiyo, njooni, kwani nyote [a]mmepotea, kila moja katika njia zake mbovu.

6 Kwa hivyo, Ee Bwana, wewe umewaacha watu wako, nyumba ya Yakobo, kwa sababu [a]wamejaa na mila za mashariki, na wanatii wachawi kama [b]Wafilisti, na [c]wanajifurahisha na watoto wa wageni.

7 Nchi yao pia imejaa fedha na dhahabu, wala hakuna mwisho wa hazina zao; nchi yao pia imejaa farasi, wala hakuna mwisho wa magari yao makubwa.

8 Nchi yao pia imejaa [a]sanamu; wanaabudu kazi ya mikono yao yenyewe, yale ambayo vidole vyao vyenyewe vimeunda.

9 Na mtu wa kawaida hainami [a]chini, na yule mtu aliye jasiri hanyenyekei, kwa hivyo, usimsamehe.

10 Ee ninyi mlio waovu, ingieni kwenye mwamba, na [a]mjifiche wenyewe kwenye mavumbi, kwani woga wa Bwana na utukufu wa nguvu zake utawachapa.

11 Na itakuwa kwamba kiburi cha mwanadamu kita-

12 1*a* Isaya mlango wa 2–14 imenukuliwa kutoka katika mabamba ya shaba nyeupe na Nefi katika 2 Ne. 12–24; kuna tofauti za maneno ambazo inabidi zizingatiwe.
b EBR *kaza*, maana yake "iliyoonwa." Maana yake Isaya alipokea ujumbe wake kupitia ono kutoka kwa Bwana.
2*a* Yoe. 3:17. MWM Sayuni.
b MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
c M&M 49:25.
3*a* MWM Tembea, Tembea na Mungu.
b EBR fundisho. MWM Injili.
4*a* 2 Ne. 21:2–9.
5*a* 2 Ne. 28:14; Mos. 14:6; Alma 5:37.
6*a* MY wamejazwa, wamepewa, mafundisho, imani zisizo za kweli. Zab. 106:35.
b MWM Wafilisti.
c EBR kubaliana, au fanya agano.
8*a* MWM Kuabudu sanamu.
9*a* MY kwa Mungu; huabudu sanamu badala yake.
10*a* Alma 12:14.

nyenyekeshwa, na maringo ya wanadamu yatashushwa, na Bwana pekee ndiye atainuliwa katika siku ile.

12 Kwani [a]siku ya Bwana wa Majeshi hivi punde itatukia kwa mataifa yote, ndiyo, katika kila mmoja; ndiyo, kwa wale walio na [b]kiburi na maringo, na kwa kila mmoja aliyejiinua, na atashushwa chini.

13 Ndiyo, na siku ya Bwana itateremkia mierezi yote ya Lebanoni, kwani iko juu na kuinuliwa; na juu ya mialoni yote ya Bashani;

14 Na juu ya milima yote mirefu, na juu ya vilima vyote, na juu ya mataifa yote yaliyoinuliwa, na juu ya kila watu;

15 Na juu ya kila mnara mrefu, na juu ya kila ukuta uliozungushwa;

16 Na juu ya meli zote za [a]bahari, na juu ya meli zote za Tarshishi, na juu ya picha zote nzuri.

17 Na kiburi cha mwanadamu kitashushwa, na maringo ya wanadamu kuteremshwa; na Bwana pekee ndiye atayeinuliwa katika [a]siku ile.

18 Na ataangamiza sanamu kabisa.

19 Na zitaingia katika mashimo ya miamba, na mapango ya dunia, kwani woga wa Bwana utawafikia na utukufu wa fahari yake utawapiga, atakapoinuka kusukasuka ulimwengu vikali.

20 Katika siku ile mwanadamu atatupa sanamu zake za fedha, na sanamu zake za dhahabu, ambazo alijiundia mwenyewe kwa kuabudu, kwa fuko na kwa popo;

21 Kuingia katika mianya ya miamba, na vilele vya miamba iliyopasuka, kwani woga wa Bwana utawajia na fahari ya utukufu wake utawachapa, atakapoinuka kusukasuka ulimwengu vikali.

22 [a]Achaneni ninyi na mwanadamu, ambaye pumzi yake iko katika pua zake; kwani ni katika nini yeye atawajibika?

MLANGO WA 13

Yuda na Yerusalemu zitaadhibiwa kwa sababu ya maasi yao—Bwana hutetea na huhukumu watu Wake—Mabinti wa Sayuni wanalaaniwa na kusumbuliwa kwa sababu ya kupenda anasa—Linganisha Isaya 3. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Kwani tazama, Bwana, Bwana wa Majeshi, huondoa kutoka Yerusalemu, na Yuda, kijiti na bakora, bakora yote ya mkate, na kijiti chote cha maji—

12*a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
b Mal. 4:1; 2 Ne. 23:11; M&M 64:24.
16*a* Toleo la Kiyunani (Septuaginto) lina kifungu kimoja cha maneno ambacho Kiebrania haina, na Kiebrania ina kifungu kimoja cha maneno ambacho Kiyunani haina; lakini 2 Ne 12:16 ina vyote.
Zab. 48:7; Eze. 27:25.
17*a* MY siku ya ujio wa Bwana katika utukufu.
22*a* MY Acha kumtegemea mwanadamu aliye katika mwili wenye kufa; ni mwenye uwezo kidogo akilinganishwa na Mungu.
Musa 1:10.

2 Mwanadamu aliye shujaa, na mwanadamu aliye wa vita, mwamuzi, na nabii, na aliye na hekima, na mzee;

3 Kapteni wa wanajeshi hamsini, na yule anayeheshimika, na mshauri, na mganga mwerevu, na mzungumzaji shujaa.

4 Na nitawapatia watoto kuwa wafalme wao, na watoto wachanga watawatawala.

5 Na watu watadhulumiwa, kila mmoja na mwingine, na kila mmoja na jirani yake; watoto watajivunia wazee, na mshenzi kwa anayeheshimika.

6 Wakati mtu atamkumbatia kaka yake wa nyumba ya baba yake, na kusema: Wewe unayo mavazi, kuwa kiongozi wetu, na usikubali haya [a]maangamizo kushukia kwa mkono wako—

7 Katika siku ile ataapa, akisema: Mimi sitakuwa [a]mponyaji; kwani nyumbani mwangu hamna mkate wala mavazi; msinifanye kiongozi wa watu.

8 Kwani Yerusalemu [a]imeangamizwa, na Yuda [b]imeanguka, kwa sababu ndimi zao na matendo yao yamekuwa kinyume cha Bwana, kwa kuchokoza utukufu wa macho yake.

9 Umbo la nyuso zao linashuhudia dhidi yao, na kutangaza kwamba dhambi yao ni kama ya [a]Sodoma, na hawawezi kuificha. Ole kwa nafsi zao, kwani wamejilipiza kwa uovu!

10 Waambieni walio haki kwamba wako [a]salama; kwani watakula matunda ya matendo yao.

11 Ole kwa wale walio waovu, kwani wataangamia; kwani malipo ya mikono yao yatakuwa juu yao!

12 Na watu wangu, wanadhulumiwa na watoto, na kutawaliwa na wanawake. Ee watu wangu, wale [a]wanaowaongoza wanawasababisha kukosa na kuangamiza njia ya mapito yenu.

13 Bwana husimama [a]kuwatetea, na husimama kuhukumu watu.

14 Bwana atawahukumu wazee wa watu wake na wana wa [a]wafalme wao; kwani [b]mmekula shamba la [c]mizabibu na [d]mali ya [e]maskini nyumbani mwenu.

15 Mnamaanisha nini? Mnawapiga watu wangu kuwa vipande, na kusaga nyuso za maskini, asema Bwana Mungu wa Majeshi.

16 Zaidi ya hayo, Bwana asema: Kwa sababu mabinti za Sayuni wanaringa, na kutembea na shingo mbele na macho ya tamaa, na mwendo wa [a]kiburi,

13 6*a* Isa. 3:6.
7*a* EBR ufungaji (wa jeraha); m.y., siwezi kutatua matatizo yako.
8*a* Yer. 9:11.
b Omb. 1:3.
9*a* Mwa. 19:1, 4–7, 24–25.
MWM Tabia ya Ubasha.
10*a* Kum. 12:28.
12*a* Isa. 9:16.
13*a* EBR bisha. Mik. 6:2; M&M 45:3–5.
14*a* EBR watawala, au viongozi.
b EBR unguzwa, au chomwa.
c Isa. 5:7.
d MY kipato kwa njia ya udanganyifu.
e 2 Ne. 28:12–13.
16*a* MY kutembea kwa hatua fupi, za haraka haraka katika namna ya uongo.

na kuliza sauti ya njuga kwa miguu yao—

17 Kwa hivyo Bwana atachapa kipaji cha mabinti za Sayuni, kwa kigaga, na Bwana [a]atagundua sehemu zao za siri.

18 Na katika siku ile Bwana ataondoa urembo wa pambo zao, na [a]kofia zao zilizoshonwa, na ushanga na [b]duara ya mviringo kama mwezi.

19 Mikufu na bangili, na [a]buibui za vito;

20 Kofia, na mavazi ya miguu, na vitambaa vya kichwa, na marashi, na vipuli vya masikio;

21 Na pete, na vipuli vya pua;

22 Na [a]mavazi mengi mazuri, na kanzu, na shali, na vibeti;

23 Na [a]vioo, na kitani dhaifu, na shela, na setiri.

24 Na itakuwa kwamba, badala ya kunukia utamu kutakuwa na uvundo; na badala ya mshipi, [a]kiraka; na badala ya nywele, upara; na badala ya [b]nguo nzuri, mshipi wa gunia; [c]kuchomeka badala ya urembo.

25 Wanaume wako wataanguka kwa upanga na mashujaa wako kwa vita.

26 Na milango yake italia na kuomboleza; na atakuwa na ukiwa, na atakaa ardhini.

MLANGO WA 14

Sayuni na mabinti zake watakombolewa na kutakaswa katika siku ya milenia—Linganisha Isaya 4. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na katika siku ile, wanawake saba watamshika mwanaume mmoja, wakisema: Tutakula mkate wetu wenyewe, na kuvaa mavazi yetu wenyewe; turuhusu tu tuitwe kwa jina lako ili tuondolewe [a]aibu yetu.

2 Katika siku ile [a]tawi la Bwana litakuwa la urembo na tukufu; matunda ya udongo yatakuwa mema na ya kupendeza kwa wale waliokimbia kutoka Israeli.

3 Na itakuwa kwamba, wale waliobaki Sayuni na kubaki Yerusalemu wataitwa watakatifu, kila mmoja aliyeandikwa miongoni mwa wale walio hai Yerusalemu—

4 [a]Wakati Bwana [b]atakapokuwa ameuosha uchafu wa mabinti za Sayuni, na kuisafisha damu ya Yerusalemu kutoka kati yake kwa roho ya hukumu na kwa roho ya [c]kuchoma.

5 Na Bwana ataumba juu ya kila makao ya mlima wa Sayuni, na juu ya kila mkusanyiko

17 *a* EBR fichua; msemo unaomaanisha "kuwaabisha."
18 *a* Yawezekana wavu wa kufungia nywele. Wataalamu hawakubaliana mara zote kuhusu asili ya mapambo ya kike yaliyoorodheshwa katika aya ya 18–23.
b MY mapambo yaliyo na umbo kama la mwezi mwandamo.
19 *a* EBR shela.
22 *a* EBR mavazi ya kupendeza.
23 *a* AU mavazi yenye kuangaza.
24 *a* EBR nguo chakavu.
b AU joho.
c AU mhuri (ishara ya utumwa).
14 1 *a* MY waa la kutoolewa na kutokuwa na mtoto.
2 *a* Isa. 60:21; 2 Ne. 3:5; Yak. (KM) 2:25.
4 *a* MY Wakati Bwana atakapokuwa ameitakasa dunia.
b MWM Osha, Oshwa, Uoshaji.
c Mal. 3:2–3; 4:1.

wake, [a]wingu na moshi mchana na mng'aro wa miale ya moto usiku; kwani juu ya utukufu wote wa Sayuni kutakuwa na ulinzi.

6 Na kutakuwa na hema kwa kivuli mchana kwa sababu ya joto, na mahali [a]pakukimbilia, na kujificha nyakati za dhoruba na mvua.

MLANGO WA 15

Shamba la mizabibu la Bwana (Israeli) litakuwa lenye ukiwa, na watu Wake watatawanywa—Shida zitawajia katika hali yao ya ukengeufu na hali ya kutawanyika—Bwana atainua bendera na kuwakusanya Israeli—Linganisha Isaya 5. Karibia mwaka 559–545 K.K.

NA kisha nitamuimbia mpenzi wangu [a]wimbo wa mpenzi wangu, kuhusu shamba lake la mizabibu. Mpenzi wangu analo shamba la mizabibu katika kilima kinono sana.

2 Na alilizingira kwa ua, na akayatoa mawe yake, na akapanda [a]mizabibu iliyo bora, na akajenga mnara katikati yake, na akajenga pia kishinikizo ndani yake; na akategemea kwamba litazaa zabibu, nalo likazaa zabibu-mwitu.

3 Na sasa, Ee wakazi wa Yerusalemu, nanyi watu wa Yuda, nawasihi, amueni, kati yangu na shamba langu la mizabibu.

4 Ni nini kingefanywa zaidi katika shamba langu la mizabibu ambacho sijafanya ndani yake? Kwa hivyo, nilipotumaini kwamba itazaa zabibu ikazaa zabibu-mwitu.

5 Na sasa basi; nitawaambia nitakachotenda kwenye shamba langu la mizabibu—[a]nitaondoa ua hili, nalo litaliwa; na nitabomoa ukuta wake, nao utakanyagwa;

6 Na nitaliharibu; halitapogolewa wala kulimwa; lakini litamea [a]mbigili na miiba; mimi nitaamuru pia mawingu kwamba [b]yasinyeshe mvua juu yake.

7 Kwani [a]shamba la mizabibu la Bwana wa Majeshi ni nyumba ya Israeli, na watu wa Yuda ndiyo mmea wake wa kupendeza; na alitafuta [b]hukumu, na tazama, dhuluma; kwa haki, lakini tazama, kilio.

8 Ole kwa wale wanaoungana [a]nyumba hadi nyumba, mpaka pasiwe na mahali, kwamba [b]wawekwe peke yao katikati ya dunia!

9 Katika masikio yangu, alisema Bwana wa Majeshi, hakika nyumba nyingi zitaku-

5*a* Ku. 13:21.
6*a* Isa. 25:4; M&M 115:6.

15 1*a* MY Nabii anatunga wimbo au mfano wa kishairi wa shamba la mzabibu, akionyesha rehema ya Mungu na ukaidi wa Israeli.
2*a* Yer. 2:21.
5*a* Zab. 80:12.
6*a* Isa. 7:23; 32:13.
b Yer. 3:3.
7*a* MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
b AU haki.
8*a* Mik. 2:1–2.
b MY kuachwa uishi peke yako. Wamiliki ardhi matajiri wameyameza mashamba madogo madogo ya masikini.

wa zenye ukiwa, na miji mikuu na mizuri itakuwa haina mtu.

10 Ndiyo, ekari kumi za shamba la mizabibu zitazaa [a]bathi moja, na mbegu ya homeri itatoa efa tu.

11 Ole wao waamkao alfajiri, ili [a]watafute pombe kali, wanaoendelea hadi usiku wa manane, mpaka [b]mvinyo unawachoma kama moto!

12 Na kinubi, na zeze, matari, na filimbi, na mvinyo ziko katika karamu zao; lakini [a]hawashughuliki na kazi ya Bwana, wala kuyafikiri matendo ya kazi yake.

13 Kwa hivyo, watu wangu wamepelekwa utumwani, kwa sababu hawana [a]ufahamu; na watu wao wanao heshimika wana njaa, na wengi wao wamekauka kwa kiu.

14 Kwa hivyo, jehanamu imejipanua, na kufungua kinywa chake bila kipimo; na utukufu wao, na wingi wao, na fahari yao, na yule anayefurahia, atateremka ndani yake.

15 Na mtu wa kawaida atashushwa chini, na yule mtu shujaa atanyenyekeshwa, na macho ya aliye na kiburi yatanyenyekeshwa.

16 Lakini Bwana wa Majeshi atainuliwa katika [a]hukumu, na Mungu aliye mtakatifu atatakaswa katika haki.

17 Kisha wanakondoo watakula kama kawaida yao, na mahali palipoharibiwa pawale wanono pataliwa na wageni.

18 Ole kwa wale wavutao uovu kwa kamba za [a]ubatili, na dhambi [b]kama kwa kamba ya gari;

19 Wanaosema: Hebu [a]afanye haraka, aihimize kazi yake, ili [b]tuione; na hebu mawaidha ya yule Mtakatifu wa Israeli yaharakishwe na kutukia, ili tuyafahamu.

20 Ole kwa wale [a]wanaoita uovu wema, na wema uovu, watiao [b]giza badala ya nuru, na nuru badala ya giza, watiao ukali badala ya utamu, na utamu badala ya ukali!

21 Ole kwa wao walio wenye [a]hekima katika macho yao wenyewe, na wenye busara katika fikira zao wenyewe!

22 Ole kwa wale hodari wa kunywa mvinyo, na wanaume walio shujaa katika kuchanganya pombe;

23 Wanaompatia mwovu haki kwa kupokea zawadi, na [a]kumwondolea haki yule aliye haki!

24 Kwa hivyo, kama vile [a]moto

10 *a* Eze. 45:10–11.
11 *a* Mit. 23:30–32.
b MWM Neno la Hekima.
12 *a* Zab. 28:5.
13 *a* Hos. 4:6.
MWM Maarifa.
16 *a* MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
18 *a* MWM Majivuno, Siofaa.
b MY Wamefungwa na dhambi zao kama wanyama na mizigo yao.
19 *a* Yer. 17:15.
b MY Hawataamini katika Masiya hadi watakapomwona Yeye.
20 *a* Moro. 7:14, 18; M&M 64:16; 121:16.
b 1 Yoh. 1:6.
21 *a* Mit. 3:5–7; 2 Ne. 28:15.
23 *a* MY kumnyima haki zake za kisheria.
24 *a* Oba. 1:18; Mal. 4:1–2; 2 Ne. 20:17.

uchomavyo [b]mabua makavu, na mwali wa moto humaliza [c]nyasi kavu, mzizi wao utaoza, na maua yao yatapeperushwa kama vumbi; kwa sababu wameitupa sheria ya Bwana wa Majeshi, na [d]kudharau neno la yule Mtakatifu wa Israeli.

25 Kwa hivyo, [a]hasira ya Bwana imewawakia watu wake, na amewanyoshea mkono wake dhidi yao, na kuwachapa; na vilima vilitetemeka, na mizoga yao ilipasuliwa katikati ya njia. Lakini bado hasira yake haijakoma, bado amenyosha mkono wake.

26 Na atayainulia mataifa kutoka mbali [a]bendera, na atawapigia [b]miunzi tokea mwisho wa dunia; na tazama, [c]watakuja mbio upesi sana; hakuna yeyote miongoni mwao atakayechoka wala kujikwaa.

27 Hakuna yeyote atakayesinzia wala kulala; wala mshipi wa viuno vyao kulegea, wala kamba za viatu vyao kukatika;

28 Mishale yao itakuwa mikali, na pinde zao zote kupindika, na kwato za farasi zao zitahesabika kama gumegume, na gurudumu zao kama kimbunga, na ngurumo zao kama simba.

29 Watanguruma kama wana-[a]simba; ndiyo, watanguruma, na kukamata mawindo, na kuyachukua kwa usalama, na hakuna yeyote atakayeokoa.

30 Na siku ile watawangurumia kama ngurumo ya bahari; na kama watatazama nchini, tazama, giza na huzuni, na nuru itatiwa giza katika mbingu zake.

MLANGO WA 16

Isaya anamwona Bwana—Isaya anasamehewa dhambi zake—Anaitwa kutoa unabii—Anatoa unabii kuhusu kukataliwa kwa mafundisho ya Kristo na Wayahudi—Baki litarejea—Linganisha Isaya 6. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Katika [a]mwaka ule mfalme Uzia alifariki, nilimwona Bwana pia akikalia kiti cha enzi, kilicho juu na kuinuliwa, na [b]pindo za vazi lake zilijaza hekalu.

2 Na juu yake walisimama [a]maserafi; kila mmoja alikuwa na mabawa sita; kwa mawili alifunika uso wake, na kwa mawili alifunika miguu yake, na kwa mawili aliruka.

3 Na mmoja alimwitia mwingine, na akasema: Mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu, ni Bwana wa Majeshi; dunia yote imejaa utukufu wake.

4 Na [a]vizingiti vya mlango

24 *b* Yoe. 2:5; 1 Ne. 22:15, 23; 2 Ne. 26:4, 6; M&M 64:23–24; 133:64.
c Lk. 3:17; Mos. 7:29–31.
d 2 Sam. 12:7–9.
25 *a* M&M 63:32; Musa 6:27.
26 *a* MWM Bendera.
b AU mbinja; m.y. ita kusanyiko. Isa. 7:18; 2 Ne. 29:2.
c MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
29 *a* 3 Ne. 21:12–13.
16 1 *a* MY karibu mwaka ya 750 K.K.
b MY upindo wa vazi lake, au sketi yake.
2 *a* MWM Makerubi.
4 *a* EBR misingi ya vizingiti ilitikisika.

vilitetemeka kwa sauti ya yule aliyelia, na nyumba ilijaa moshi.

5 Kisha nikasema: Ole wangu! kwani [a]nitaangamizwa; kwa sababu mimi ni mtu mwenye midomo michafu; na ninaishi miongoni mwa watu wenye midomo michafu; kwani macho yangu yamemwona Mfalme, Bwana wa Majeshi.

6 Kisha mmoja wa wale maserafi aliruka na akanikaribia, akiwa na kaa la [a]moto hai mkononi mwake, ambalo alikuwa amelitoa kwenye madhabahu kwa makoleo;

7 Na akaliweka kwenye kinywa changu, na kusema: Tazama, hili limegusa midomo yako; na [a]uovu wako umeondolewa, na dhambi zako kuoshwa.

8 Pia nilisikia sauti ya Bwana, ikisema: Nitamtuma nani, na ni nani atakayeenda kwa niaba yetu? Kisha nikasema: Niko hapa; nitume mimi.

9 Na akasema: Enenda na uwambie watu hawa—Kwa kweli mlisikiliza, lakini hamkufahamu, mliona, lakini hamkuelewa.

10 Kinaisha moyo wa watu hawa uwe mgumu, na fanya masikio yao yawe mazito, na funga macho yao—wasije wakaona kwa macho yao, na [a]kusikia kwa masikio yao, na kufahamu kwa moyo wao, na waongoke na kuponywa.

11 Kisha nikasema: Bwana, hadi lini? Na akasema: Hadi miji hii itakapokuwa na ukiwa bila mkazi, na nyumba bila wanadamu, na nchi itakapokuwa ganjo;

12 Na Bwana [a]amewahamisha watu mbali, kwani kutakuwa na uhamisho mkuu miongoni mwa nchi.

13 Lakini itasalia sehemu ya kumi, na watarejea, na kuliwa, kama mvinje, na kama mwaloni ambao nguvu zake ziko ndani yake wakati majani yanaanguka; kwa hivyo mbegu takatifu itakuwa [a]nguvu yake.

MLANGO WA 17

Efraimu na Shamu wanashambulia Yuda—Kristo atazaliwa na Bikira—Linganisha Isaya 7. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na ikawa katika siku za Ahazi mwana wa Yothamu, mwana wa Uzia, mfalme wa Yuda, kwamba Resini, mfalme wa Shamu, na Peka mwana wa Remalia, mfalme wa Israeli, walienda kushambulia Yerusalemu, lakini hawakuiweza.

2 Na nyumba ya Daudi, ikaambiwa: Shamu imeungana na [a]Efraimu. Na moyo wake

5*a* EBR tenga; m.y., alielemewa na ufahamu wa dhambi zake na dhambi za watu wake.
6*a* MY ishara ya kutakaswa.
7*a* MWM Ondoleo la Dhambi.
10*a* Mt. 13:14–15.
12*a* 2 Fal. 17:18, 20.
13*a* MY Kama mti, japokuwa majani yake yametawanywa uhai na uwezo wa kuzaa mbegu bado unabakia ndani yake.
17 2*a* MY Israeli yote ya kaskazini iliitwa kwa jina la Efraimu, kabila kuu la kaskazini.

ukatetemeka, na moyo wa watu wake, jinsi vile miti ya kichaka hupeperushwa na upepo.

3 Kisha Bwana akamwambia Isaya: Nenda sasa ukamlaki Ahazi, wewe na mwana wako [a]Shear-yashubu, huko mwisho wa mfereji wa dimbwi la juu katika njia kuu ya uwanja wa dobi;

4 Na umwambie: Sikiliza, na utulie; [a]usiogope, wala usifadhaike moyoni kwa sababu ya hii mikia miwili ya mwenge itokayo moshi, kwa sababu ya hasira kali ya Resini na Shamu, na ya mwana wa Remalia.

5 Kwa sababu Shamu, Efraimu, na mwana wa Remalia, wamekusudia maovu juu yako, wakisema:

6 Hebu twende dhidi ya Yuda na kuichokoza, na tuigawanye kati yetu, na tuweke mfalme kati yake, ndiyo, mwana wa Tabeeli.

7 Hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu: Haitasimama, wala kutimika.

8 Kwani kichwa cha Shamu ni Dameski, na kichwa cha Dameski, Resini; na katika muda wa miaka sitini na tano Efraimu itaangamizwa isiwe tena kikundi cha watu.

9 Na kichwa cha Efraimu ni Samaria, na kichwa cha Samaria ni mwana wa Remalia. Kama [a]hamtaamini kwa hakika hamtaimarishwa.

10 Tena, Bwana akazungumza zaidi na Ahazi, akamwambia:

11 Itisha [a]ishara kutoka kwa Bwana Mungu wako; iwe chini kwenye shimo, au juu kwenye mawingu.

12 Lakini Ahazi akasema: Sitaitisha, wala [a]sitamjaribu Bwana.

13 Na akasema: Sikilizeni sasa, Enyi nyumba ya Daudi; Je, ni kitu kidogo kwenu kuwachosha wanadamu, hata mkataka kumchosha Mungu wangu pia?

14 Kwa hivyo, Bwana mwenyewe atakupatia ishara—Tazama, [a]Bikira atapata mimba, na atazaa mwanamume, na atamwita kwa jina [b]Imanueli.

15 Atakula siagi na asali, ili ajue kukataa maovu na kuchagua mema.

16 Kwani kabla huyo [a]mtoto hajajua kukataa maovu na kuchagua mema, nchi ile ambayo unaichukia itakataliwa na wafalme wake [b]wawili.

17 Bwana [a]atakuteremshia, na juu ya watu wako, na juu ya nyumba ya baba yako, nyakati ambazo hazijawahi kuoneka tangu siku ile [b]Efraimu alipoondoka kutoka Yuda, mfalme wa Ashuru.

18 Na itakuwa kwamba katika siku ile Bwana ataipigia [a]miunzi nzi aliye sehemu za mbali za

3*a* EBR Masalia watarudi.
4*a* MY Usiogopeshwe na shambulio; wafalme hao wawili wamebakiwa na nguvu kidogo.
9*a* 2 Nya. 20:20.
11*a* MWM Ishara.
12*a* MY pima au thibitisha.
14*a* MWM Bikira.
b EBR Pamoja nasi yu Mungu.
MWM Imanueli.
16*a* 2 Ne. 18:4.
b 2 Fal. 15:30; 16:9.
17*a* 2 Nya. 28:19–21.
b 1 Fal. 12:16–19.
18*a* AU mbinja; m.y., ashiria mwito. Isa. 5:26.

Misri, na kwa nyuki aliye katika nchi ya Ashuru.

19 Na watakuja, na watapumzika wote katika mabonde yaliyo na ukiwa, na katika mashimo ya miamba, na kwenye miiba yote, na juu ya vichaka vyote.

20 Na siku ile ile Bwana [a]atawanyoa kwa wembe ulioajiriwa, na hao ng'ambo ya mto, na [b]mfalme wa Ashuru, kichwa, na malaika wa miguu; na pia atamaliza ndevu.

21 Na itakuwa kwamba katika siku ile, mtu [a]atalisha ng'ombe mmoja na kondoo wawili;

22 Na itakuwa kwamba, kwa wingi wa maziwa watakayotoa atakula siagi; kwani kila mmoja aliyesalia katika nchi ile atakula siagi na asali.

23 Na itakuwa kwamba katika siku ile, kila mahali patakuwa, ambapo palikuwa mizabibu elfu inayo gharama [a]fedha elfu, ambapo patakuwa na mbigili na miiba.

24 Na watu wataenda huko na mishale na pinde, kwa sababu nchi yote itakuwa mbigili na miiba.

25 Na vilima vyote vitakavyolimwa kwa jembe, hapatafika huko woga wa mbigili na miiba; lakini hapo patakuwa mahali pa kuelekeza ng'ombe, na mahali pa kukanyagwa na [a]kondoo.

MLANGO WA 18

Kristo atakuwa kama jiwe la kujikwaa na mwamba wa kuchukiza—Mtafute Bwana, sio mlio wa wachawi—Tegemea sheria na ushuhuda kwa maongozo—Linganisha Isaya 8. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Tena, neno la Bwana liliniambia: Chukua hati ndefu, na uandike juu yake kwa kalamu ya mwanadamu, kuhusu [a]Maher-shalal-hash-bazi.

2 Na nilichukua [a]mashahidi waaminifu ili waandike, Uria yule kuhani, na Zekaria mwana wa Yeberekia.

3 Na nilimwendea huyo [a]nabii wa kike; na akapata mimba na akazaa mwana wa kiume. Kisha Bwana akaniambia: Muite jina lake, Maher-shalal-hash-bazi.

4 Kwani tazama, kabla ya huyo [a]mtoto [b]hajajua kulia, baba yangu, na mama yangu, utajiri wa Dameski na [c]mateka ya Samaria yatachukuliwa na mfalme wa Ashuru.

5 Bwana alinizungumzia tena, akisema:

6 Kwa vile watu hawa wameyakataa maji ya [a]Shiloa yapitayo

20*a* MY Nchi itatiwa ukiwa na mvamizi wa nje.
b 2 Fal. 16:5–9.
21*a* MY Wabakiaji wachache tu watakaojimudu watasalia.
23*a* AU vipande vya fedha.
25*a* EBR kondoo, au mbuzi.
18 1*a* EBR Kuchukua mateka, aliharakisha mawindo.
2*a* MWM Shahidi, Ushahidi.
3*a* MY mke wake.
4*a* 2 Ne. 17:16.
b Isa. 8:4.
c 2 Fal. 15:29.
6*a* Mwa. 49:10; TJS Mwa. 50:24 (Kiambatisho).

polepole, na wanafurahia [b]Resini na mwana wa Remalia;

7 Kwa hivyo sasa, tazama, Bwana ataleta [a]juu yao maji ya huo mto, yenye nguvu, na mengi, hata mfalme wa Ashuru na utukufu wake wote; atakuja na kupita juu ya mifereji yake yote, na kingo zake zote.

8 Na [a]yeye atapita Yuda; atafurika na kuwa zaidi, atafika hata shingoni; na atakaponyosha mabawa yake yatajaa upana wa nchi, Ewe [b]Imanueli.

9 [a]Jiunganishe, Ee ninyi watu, na mtavunjwa vipande vipande; na sikiliza ninyi nyote mtokao nchi za mbali; jiwekeni tayari na silaha, na mtavunjwa vipande vipande; jiwekeni tayari na silaha, na mtavunjwa vipande vipande.

10 Fanyeni shauri pamoja, na hamtafanikiwa; nena neno, na halitatimia; [a]kwani Mungu yu pamoja nasi.

11 Kwani Bwana alinizungumzia hivyo kwa kunionya vikali, na akanishauri kuwa nisitembee katika njia za watu hawa, akisema:

12 Msiseme, [a]Muungano, kwa wale wote ambao hawa watu watasema, Muungano; wala msiogope woga wao, wala kuogopa.

13 Mtakaseni Bwana wa Majeshi mwenyewe, na [a]acheni yeye awe hofu yenu, na acheni yeye awe tisho lenu.

14 Na atakuwa [a]kimbilio; lakini [b]jiwe la kujikwaa, na mwamba wa kuchukiza kwa nyumba zote mbili za Israeli, na mtego na tanzi kwa wakazi wa Yerusalemu.

15 Na wengi miongoni mwao [a]watajikwaa na kuanguka, na kuvunjwa, na kutegwa, na kukamatwa.

16 Ufunge huo ushuhuda, na ufunge [a]sheria miongoni mwa wanafunzi wangu.

17 Na nitamngojea Bwana, ambaye [a]huficha uso wake kutoka kwa nyumba ya Yakobo, na nitamtafuta.

18 Tazama, mimi na watoto ambao Bwana amenipatia ni kwa [a]ishara na maajabu katika Israeli kutoka kwa Bwana wa Majeshi, yule anayekaa katika Mlima Sayuni.

19 Na watakapokuambia: Tafuta ushauri kwa watu wenye [a]pepo wa utambuzi, na kwa [b]wachawi wanaochungulia na kunong'ona—je, haiwapasi

6 *b* Isa. 7:1.
7 *a* MY juu ya Israeli ya kaskazini kwanza.
8 *a* MY Ashuru itaipenya Yuda pia.
b MWM Imanueli.
9 *a* MY Anzisha mashirikiano.
10 *a* MY Juda (nchi ya Emanueli) itahurumiwa. Zab. 46:7.
12 *a* MY Yuda asitegemee mipango ya siri na wengine kwa usalama.
13 *a* MY Uchaji na unyenyekevu mbele ya Mungu.
14 *a* Eze. 11:15–21.
b 1 Pet. 2:4–8; Yak. (KM) 4:14–15.
15 *a* Mt. 21:42–44.
16 *a* EBR mafundisho. MWM Injili.
17 *a* Isa. 54:8.
18 *a* MY Majina ya Isaya na watoto wake wa kiume yana maana ya "Yehova anaokoa"; "Salio atarudi"; na "kuchukua mateka, aliharakisha mawindo." 2 Ne. 17:3; 18:3.
19 *a* Law. 20:6.
b MY wachawi, watabiri.

watu kutafuta ushauri [c]kutoka kwa Mungu ili wanaoishi wasikie [d]kutoka kwa wafu?

20 Kwa sheria na kwa ushuhuda; na [a]wao wasiponena kulingana na neno hili, ni kwa sababu hakuna nuru ndani yao.

21 Nao [a]wao watapita katikati yake wamedhikika na wakiwa na njaa; na itakuwa kwamba watakapopata njaa, watajikasirisha wenyewe, na kumlaani mfalme wao na Mungu wao na kutazama juu.

22 Na watatazama ardhi na kutazama shida, na giza, kufa moyo, na wataingizwa gizani.

MLANGO WA 19

Isaya anazungumza kiumasiya—Watu wale walio gizani wataona nuru kuu—Kwetu sisi mtoto amezaliwa—Atakuwa Mwana Mfalme wa Amani na atatawala kwenye kiti cha enzi cha Daudi—Linganisha Isaya 9. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Walakini, giza halitakuwa kubwa kama ilipokuwa katika dhiki yake aliposhambuliwa, wakati hapo mwanzoni alitesa kidogo [a]nchi ya Zabuloni, na nchi ya Naftali, na baadaye kwa uzito akapitia kwa njia ya Bahari ya Shamu ng'ambo ya Yordani katika Galilaya ya mataifa.

2 Watu wale waliotembea [a]gizani wameona nuru kuu; wale wanaoishi katika nchi ya kivuli cha kifo, wameangaziwa na nuru.

3 Umeliongeza taifa, na [a]kuzidisha shangwe—wanajaa shangwe mbele yako kulingana na shangwe ya mavuno, na kama vile watu wanavyofurahia wanapogawana nyara.

4 Kwani umevunja nira ya mzigo wake, na gogo la bega lake, fimbo ya yule anayemdhulumu.

5 Kwani kila vita vya askari shujaa huunganishwa na makelele, na mavazi yaliyovingirishwa kwenye damu; lakini hii itakuwa ni ya kuchomwa na kuwa makaa ya moto.

6 Kwani kwetu sisi [a]mtoto amezaliwa, kwetu tumepewa mwana; na [b]serikali itakuwa kwenye bega lake; nalo jina lake litaitwa, Ajabu, Mshauri, [c]Mwenyezi Mungu, [d]Baba asiye na mwisho, Mwana Mfalme wa [e]Amani.

7 Na [a]hakuna mwisho wa upanuzi wa [b]serikali na amani, katika kiti cha enzi cha Daudi, na juu ya utaratibu wa ufalme wake, na kuiimarisha kwa hukumu na kwa haki tangu

19 *c* 1 Sam. 28:6–20.
d AU kwa niaba ya.
20 *a* MY mtu anayewasiliana na mapepo (pia katika aya 21–22).
21 *a* MY Israeli atachukuliwa utumwani kwa sababu hakutaka kusikia.
19 1 *a* Mt. 4:12–16.
2 *a* "Giza" lilikuwa ni ukengeufu na ufungwa; "nuru kuu" ni Kristo.
3 *a* Isa. 9:3.
6 *a* Isa. 7:14; Lk. 2:11.
b Mt. 28:18.
c Tit. 2:13–14.
d Alma 11:38–39, 44.
e Yn. 14:27.
7 *a* Dan. 2:44.
b MWM Utawala.

sasa, na hata milele. Bidii ya Bwana wa Majeshi itatenda haya.

8 Bwana alimtumia Yakobo neno lake na limemulikia [a]Israeli.

9 Na watu wote watajua, hata Efraimu na wakazi wa Samaria, wanaosema kwa kiburi na ugumu wa moyo:

10 Matofali yameanguka chini, lakini sisi tutajenga kwa mawe yaliyochongwa; mikuyu imekatwa, lakini sisi tutaibadilisha iwe mierezi.

11 Kwa hivyo Bwana atawainua maadui wa [a]Resini dhidi yake, na kuwaunganisha maadui wake pamoja;

12 Waashuri mbele yao na Wafilisti nyuma yao; na [a]watamla Israeli kwa kinywa kilicho wazi. Lakini hata baada ya haya [b]hasira yake haitapungua, lakini bado amenyoosha mkono wake.

13 Kwani watu [a]hawatamrejea aliyewapiga, wala kumtafuta Bwana wa Majeshi.

14 Kwa hivyo Bwana atakata kutoka Israeli kichwa na mkia, tawi na tete katika siku moja.

15 Mzee, ndiye kichwa; na nabii anayefundisha uwongo, ndiye mkia.

16 Kwani viongozi wa watu hawa wanawasabisha wakose; na wale wanaoongozwa nao wanaangamia.

17 Kwa hivyo Bwana [a]hatakuwa na shangwe katika vijana wao, wala hatawahurumia yatima wao na wajane wao; kwani kila mmoja wao ni mnafiki na mwovu, na kila mdomo unanena [b]upumbavu. Kwa haya yote hasira yake haitapungua, lakini bado amenyoosha [c]mkono wake.

18 Kwani uovu huteketea kama moto; itaila mibigili na miiba, na itawasha vichaka vya mwitu, na yatapaa juu kama kuinuka kwa moshi.

19 Kwa kupitia ghadhabu ya Bwana wa Majeshi nchi inatiwa giza, na watu hao watakuwa kama makaa ya moto; [a]hakuna mtu yeyote atakayemhurumia kaka yake.

20 Na atapokonya upande wa mkono wa kulia na kuwa na njaa; na [a]atakula kwa upande wa mkono wa kushoto na hawatatosheka; kila mtu atakula nyama ya mkono wake mwenyewe—

21 [a]Manase dhidi ya [b]Efraimu; na Efraimu dhidi ya Manase; wao wawili pamoja watamshambulia [c]Yuda. Kwa haya yote hasira yake haitapungua, lakini bado amenyoosha mkono wake.

MLANGO WA 20

Maangamizo ya Ashuru ni kiele-

8*a* MY Ujumbe wa kinabii ambao unafuatia (aya ya 8–21) ilikuwa ni onyo kwa makabila kumi ya kaskazini, yanayoitwa Israeli.

11*a* 2 Fal. 16:5–9.

12*a* 2 Fal. 17:6, 18.
b Isa. 5:25; 10:4.

13*a* Amo. 4:6–12.

17*a* MWM Rehema, enye Rehema.
b 2 Ne. 9:28–29.
c Yak. (KM) 5:47; 6:4.

19*a* Mik. 7:2–6.

20*a* Kum. 28:53–57.

21*a* MWM Manase.
b MWM Efraimu.
c MWM Yuda.

lezo cha maangamizo ya waovu wakati wa Ujio Wake wa Pili—Watu wachache watasalia baada ya Bwana kurudi—Baki la Yakobo litarejea katika siku ile—Linganisha Isaya 10. Karibia mwaka 559–545 K.K.

OLE wao ambao huweka maagizo yasiyo ya haki, na wale waandikao sheria ngumu ambazo wameweka;

2 Kuwageuza walio na mahitaji kutokana na haki, na kuwanyang'anya watu wangu maskini haki yao, ili [a]wajane wawe mateka wao, na ili wawaibie mayatima!

3 Nanyi mtafanya nini katika siku ya [a]hukumu, na katika ukiwa utokao mbali? mtamkimbilia nani awasaidie? na mtaacha wapi utukufu wenu?

4 Bila mimi watainamia wafungwa, na watakufa miongoni mwa waliouawa. Lakini kwa haya yote hasira yake haitapungua, lakini bado amenyoosha mkono wake.

5 Ee Mwashuri, fimbo ya hasira yangu, na bakora iliyo mkononi mwao ni ghadhabu [a]yao.

6 Nitamtuma [a]dhidi ya taifa la wanafiki, na dhidi ya watu wa ghadhabu yangu nitamwamuru kuchukua mateka, na kuchukua mawindo, na kuwakanyaga kama matope ya barabara.

7 Lakini hivyo sivyo akusudiavyo, wala sivyo moyo wake unavyowaza; lakini katika moyo wake anakusudia kuangamiza na kutenga mataifa na sio machache tu.

8 Kwani anasema: Si wakuu wangu wote ni wafalme?

9 Je, Kalno si kama Karkemishi? Si Hamathi ni kama Arpadi? Si Samaria ni kama Dameski?

10 Kama vile [a]mkono wangu ulijenga falme za sanamu, ambazo sanamu zake za kuchongwa zilikuwa bora kuliko za Yerusalemu na za Samaria;

11 Je, si nitatendea Samaria na sanamu zake, kama vile niliyvotendea Yerusalemu na sanamu zake?

12 Kwa hivyo itakuwa kwamba baada ya Bwana kutenda kazi yake yote kwenye Mlima Sayuni na kwenye Yerusalemu, nitaadhibu [a]matunda ya moyo thabiti wa mfalme wa [b]Ashuru, na utukufu wa majivuno ya macho yake.

13 Kwani [a]yeye anasema: Kwa nguvu za mkono wangu na hekima yangu nimetenda vitu hivi; kwani mimi ni mwerevu; na nimesogeza mipaka ya watu, na kuiba hazina zao, na kuwaangusha wenyeji kama mtu shujaa;

14 Na mkono wangu umegundua kwamba utajiri wa watu ni kama kiota cha ndege;

20 2*a* MWM Mjane.
3*a* MY adhabu.
5*a* Isa. 10:5.
6*a* MY dhidi ya Israeli.
10*a* MY mkono wa mfalme wa Ashuru (aya ya 10–11).
12*a* MY majivuno yenye kiburi.
b Sef. 2:13.
13*a* MY mfalme wa Ashuru (aya ya 13–14).

na kama vile mtu hukusanya mayai yalioachwa ndivyo nimekusanya dunia yote; na hakuna yeyote aliyetikisa bawa, au kufungua kinywa, au kulia.

15 Je, [a]shoka [b]litajisifu dhidi ya yule ambaye hukata nalo? Je, msumeno utajitukuza dhidi ya yule anayeutingisha? Ni kama fimbo ingejitikisa yenyewe dhidi ya waiinuayo, au ni kama bakora ingejiinua ni kama sio mbao!

16 Kwa hivyo Bwana, Bwana wa Majeshi, atawatumia walionona, kukonda; na kwa [a]utukufu wake atawasha uteketeo kama uteketezo wa moto.

17 Na nuru ya Israeli itakuwa kama moto, na Mtakatifu wake atakuwa kama muwako wa moto, na atachoma na kumaliza miiba yake na mbigili zake katika siku moja;

18 Na [a]atauteketeza utukufu wa msitu wake, na shamba lake linalostawi, zote mbili roho na mwili; nao watakuwa kama vile yule mshika bendera anazimia.

19 Na miti ya msitu wake [a]inayosalia itakuwa michache, hata mtoto ataweza kuihesabu.

20 Na itakuwa kwamba katika [a]siku ile, kwamba baki la Israeli, na wale walioepuka wa [b]nyumba ya Yakobo, hawatamtegemea tena yeye aliyewapiga, lakini watamtegemea Bwana, yule Mtakatifu wa Israeli, kwa ukweli.

21 [a]Baki litarejea, ndiyo, hata baki la Yakobo, kwa mwenyezi Mungu.

22 Kwani ingawa watu wako Israeli ni wengi kama mchanga wa bahari, lakini bado baki lao litarejea; [a]maangamizo yaliyowekwa [b]yatafurika kwa haki.

23 Kwani Bwana Mungu wa Majeshi [a]atafanya maangamizo, kugeuza nchi yote.

24 Kwa hivyo, hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu wa Majeshi: Enyi watu wangu muishio Sayuni, msimwogope Mwashuri; yeye atawapiga kwa fimbo, na atainua gongo lake dhidi yenu, kama [a]jinsi walivyofanya Misri.

25 Kwani bado kwa muda mfupi, na ghadhabu itaisha, na hasira yangu katika maangamizo yao.

26 Na Bwana wa Majeshi atamsukumia mjeledi kama vile alivyoua [a]Midiani katika jabali la Orebu; na jinsi fimbo yake ilivyoinuliwa juu ya bahari,

15*a* MY Je, mfalme anaweza kufanikiwa dhidi ya Mungu?
b Sitiari zote katika aya hii zinauliza swali moja; Mwanadamu (kwa mfano mfalme wa Ashuru) kumshinda Mungu?
16*a* MY mfalme wa Ashuru (pia aya ya 17–19).
18*a* MY Ashuru itatoweka moja kwa moja.
19*a* MY masalia ya jeshi la Ashuru.
20*a* MY siku za mwisho.
b Amo. 9:8–9.
21*a* Isa. 11:11–12.
22*a* M&M 63:34. MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
b MY Hata wakati adhabu inapokuja, rehema hupatikana.
23*a* MY sababisha angamizo lililotamkwa.
24*a* MY kama Wamisri walivyofanya katika nyakati za awali. Ku. 1:13–14.
26*a* Mwa. 25:1–2; Amu. 7:25.

hivyo hivyo jinsi ataiinua jinsi alivyofanyia Misri.

27 Na itakuwa kwamba katika siku ile [a]mzigo wake utaondolewa kutoka bega lako, na nira yake kutoka shingo yako, na nira itaharibiwa kwa sababu ya [b]kupakwa mafuta.

28 [a]Yeye Amefika Ayathi, amepitia Migroni; na ameweka magari yake huko Mikmashi.

29 Wamevuka kipito; wamelala Geba; Rama anaogopa; Gibea wa Shauli amekimbia.

30 Paza sauti, Ewe binti wa Galimu; na ifanye isikike hadi Laisha, Ee Anathothi maskini.

31 Madmena amehamishwa; wakazi wa Gebimu wamejikusanya ili wakimbie.

32 Lakini bado siku ile atabaki Nobu; atatikisa mkono wake dhidi ya mlima wa binti wa Sayuni, kilima cha Yerusalemu.

33 Tazama, Bwana, Bwana wa Majeshi atayakata matawi kwa mtisho; na walio na [a]ukubwa watakatwa; na waliojiinua watanyenyekeshwa.

34 Na atavikata vichaka vya msitu kwa chuma, na Lebanoni itaangushwa na mwenye nguvu.

MLANGO WA 21

Shina la Yese (Kristo) litahukumu kwa haki—Elimu ya Mungu itafunika dunia katika Milenia—Bwana atainua bendera na kukusanya Israeli—Linganisha Isaya 11. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na patatokea mbele [a]fimbo kutoka [b]Shina la [c]Yese, na tawi litamea kutoka mizizi yake.

2 Na [a]Roho wa Bwana itakuwa juu yake, roho ya hekima na ufahamu, roho ya mashauri na uwezo, roho ya elimu na ya kumcha Bwana;

3 Na atamsababisha aweze kufahamu kwa haraka katika kumcha Bwana; na [a]hatahukumu kulingana na maono ya macho yake, wala kukemea kulingana na kusikia kwa masikio yake.

4 Lakini kwa [a]haki atahukumu walio maskini, na [b]akemee kwa adili walio [c]wanyenyekevu wa dunia; na ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake, na kwa pumzi ya midomo yake atawaua walio waovu.

5 Na haki itakuwa mshipi wa viuno vyake, na uaminifu mshipi wa [a]mafigo yake.

6 Pia mbwa-mwitu ataishi na mwanakondoo, na chui atalala na mwana mbuzi, na ndama na mwana simba na ng'ombe mnono pamoja; na mtoto mchanga atawaongoza.

27*a* Isa. 14:25.
b MWM Mpakwa mafuta.
28*a* MY Kusonga mbele kwa majeshi ya Ashuru kunafuatiliwa; kisha (aya ya 33–34) tendo la Bwana dhidi yao linaelezewa katika lugha ya picha.
33*a* Hel. 4:12–13.
21 1*a* M&M 113:3–4.
b M&M 113:1–2.
c Yese alikuwa baba wa Daudi; inatajwa nasaba ya kifalme ya Daudi ambamo ndani yake hatimaye Yesu anazaliwa. Mik. 5:2; Ebr. 7:14.
MWM Yese.
2*a* Isa. 61:1–3.
3*a* Yn. 7:24.
4*a* Zab. 72:2–4; Mos. 29:12.
b EBR amua.
c MWM Pole, Upole.
5*a* AU kiuno.

7 Na ng'ombe na dubu watakula pamoja; watoto wao watalala chini pamoja; na simba atakula majani kama ng'ombe.

8 Na mtoto anayenyonya atacheza kwenye tundu la [a]nyoka, na mtoto aliyeachishwa kunyonya atatia mkono wake kwenye pango la [b]fira.

9 [a]Hawatadhuru wala kuharibu katika mlima wangu wote mtakatifu, kwani dunia yote itajaa [b]elimu ya Bwana, kama vile maji yanavyoifunika bahari.

10 Na katika [a]siku ile kutakuwa na [b]mzizi wa Yese, ambao utasimama kama bendera ya watu; na [c]Wayunani [d]watautafuta; na pumziko lake litakuwa takatifu.

11 Na itakuwa kwamba katika siku ile Bwana atanyoosha mkono wake tena mara ya [a]pili kurudisha baki la watu wake litakalobaki, kutoka Ashuru, na kutoka Misri, na kutoka Pathrosi, na kutoka Kushi, na kutoka Elamu, na kutoka Shinari, na kutoka Hamathi, na kutoka visiwa vya bahari.

12 Na atawainulia mataifa [a]bendera, na kuwakusanya watu wa Israeli [b]waliofukuzwa, na [c]kuwakusanya pamoja wale waliotawanywa wa Yuda kutoka pembe nne za dunia.

13 Na [a]wivu wa Efraimu pia utaondoka, na maadui wa Yuda watatengwa; [b]Efraimu hatamwonea wivu [c]Yuda, na Yuda hatamuudhi Efraimu.

14 Lakini wao [a]watashambulia juu ya mabega ya Wafilisti kuelekea upande wa magharibi; watawapora wale kutoka mashariki pamoja; watainyooshea Edomu na Moabu mkono wao; na watoto wa Amoni watawatii.

15 Na Bwana [a]atauangamiza ulimi wa bahari ya Misri; na kwa upepo wake mkali atatingisha mkono wake juu ya mto, na kuugawanya uwe vijito saba, na kuwavusha watu kwa miguu mikavu.

16 Na kutakuwa [a]barabara kuu kwa baki la watu wake waliosalia, kutoka Ashuru, kama vile ilivyokuwa katika Israeli katika siku ile waliyotoka nje ya nchi ya Misri.

---

8 *a* nyoka mdogo mwenye sumu wa Misri.
b nyoka mwingine mwenye sumu.
9 *a* Isa. 2:4.
MWM Milenia.
b M&M 101:32–33; 130:9.
10 *a* MY siku za mwisho.
JS—H 1:40.
b Rum. 15:12; M&M 113:5–6.
c M&M 45:9–10.
d AU kwake.
11 *a* 2 Ne. 6:14; 25:17; 29:1.
12 *a* MWM Bendera.
b 3 Ne. 15:15; 16:1–4.
c Neh. 1:9; 1 Ne. 22:10–12; M&M 45:24–25.
MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
13 *a* Yer. 3:18.
b Makabila yakiongozwa na Yuda na Efraimu yalikuwa ni maadui kihistoria (baada ya matukio ya 1 Fal. 12:16–20). Katika siku za mwisho uadui huu utaponywa.
Eze. 37:16–22.
MWM Husuda.
c MWM Yuda.
14 *a* MY shambulia mabonde ya magharibi ambayo yalikwa ni himaya ya Wafilisti.
15 *a* Zek. 10:11.
16 *a* Isa. 35:8; M&M 133:27.

MLANGO WA 22

Katika siku ile ya milenia watu wote watamsifu Bwana—Ataishi miongoni mwao—Linganisha Isaya 12. Karibia mwaka 559–545 K.K.

NA katika siku ile utasema: Ee Bwana, nitakusifu; ingawa ulinikasirikia hasira yako imegeuka, na unanifariji.

2 Tazama, Mungu ni wokovu wangu; [a]nitatumaini, na wala sitaogopa; kwani Bwana [b]YEHOVA ndiye nguvu yangu na wimbo wangu; pia amekuwa wokovu wangu.

3 Kwa hivyo, kwa shangwe utateka [a]maji kutoka visima vya wokovu.

4 Na katika siku ile utasema: [a]Msifuni Bwana, liiteni jina lake, tangazeni matendo yake miongoni mwa watu, taja jina lake ili liinuliwe.

5 [a]Mwimbieni Bwana; kwani ametenda vitu vyema; haya yanajulikana ulimwenguni kote.

6 Pazeni sauti na [a]mlie, ewe mkazi wa Sayuni; kwani mkuu ni yule Mtakatifu wa Israeli aliye baina yenu.

MLANGO WA 23

Maangamizo ya Babilonia ni mfano wa maangamizo katika wakati wa Ujio wa Pili—Itakuwa siku ya ghadhabu na kulipiza kisasi—Babilonia (ulimwengu) itaanguka milele—Linganisha Isaya 13. Karibia mwaka 559–545 K.K.

[a]MZIGO WA [b]Babilonia, ambao Isaya mwana wa Amozi aliuona.

2 Inueni [a]bendera juu ya mlima mrefu, wapazieni sauti, [b]wapungieni mkono, ili waingie milangoni mwa wakuu.

3 Nimewaamuru wale wangu [a]waliotakaswa, pia nimewaita mashujaa wangu, kwani hasira yangu haipo juu ya wote wanaofurahia ukuu wangu.

4 Kelele za umati huko milimani ni kama za watu wengi, ngurumo na kelele za [a]falme za mataifa [b]zilizokusanyika, Bwana wa Majeshi anapanga jeshi kwa vita.

5 Wanatoka nchi ya mbali, kutoka mwisho wa mbingu, ndiyo, Bwana, na silaha za ghadhabu yake; ili kuangamiza nchi yote.

6 Pigeni yowe, kwani siku ya Bwana iko karibu; itakuja kama maangamizo kutoka kwa Mwenyezi.

7 Kwa hivyo mikono yote

22 2*a* Mos. 4:6; Hel. 12:1.
b Ku. 15:2; Zab. 83:18. MWM Yehova.
3*a* MWM Maji ya Uzima.
4*a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
5*a* M&M 136:28.
6*a* Isa. 54:1; Sef. 3:14.
23 1*a* MY ujumbe wa angamizo.
b Angamizo la kihistoria la Babiloni ovu lililotabiriwa katika Isa. 13 na 14, linafananishwa na angamizo la mwisho la ulimwengu wote muovu. M&M 133:5, 7, 14. MWM Babeli, Babilonia.
2*a* MWM Bendera.
b MY toa ishara.
3*a* MY Watakatifu.
4*a* Zek. 14:2–3.
b Zek. 12:3.

italegea, moyo wa kila mtu utayeyuka;

8 Na wataogopa; watashikwa na kichomi na huzuni; watashangaa mmoja kwa mwingine; nyuso zao zitakuwa kama ndimi za moto.

9 Tazama, siku ya Bwana inafika, pamoja na ukali na ghadhabu na hasira kuu, kuifanya nchi iwe na ukiwa; [a]na atawaangamiza wenye dhambi kutoka ndani yake.

10 Kwa maana nyota za mbingu na makundi ya nyota hayatatoa nuru yao; [a]jua litatiwa giza wakati wa mwendo wake, na mwezi hautasababisha nuru yake kumulika.

11 Na [a]nitauadhibu ulimwengu kwa sababu ya uovu, na waovu kwa sababu ya maovu yao; nitakomesha fahari ya wenye [b]kiburi, na nitayalaza chini majivuno ya watishao.

12 Nitamfanya [a]mtu mmoja kuadimika kuliko dhahabu safi; na hata watu kuliko kabari ya dhahabu ya Ofiri.

13 Kwa hivyo, nitatingisha mbingu, na [a]kuiondoa dunia mahali pake, katika ghadhabu ya Bwana wa Majeshi, na katika siku ya hasira yake kali.

14 Na itakuwa kama paa [a]anayekimbizwa, na kama kondoo asiyechungwa; na kila mtu atarudi kwa watu wake wenyewe, na kila mmoja kukimbilia nchi yake.

15 Kila mtu ambaye ana kiburi atadungwa kwa upanga; ndiyo, na yule ambaye ameungana na mwovu atauawa kwa upanga.

16 Watoto wao watararuliwa vipande mbele ya macho yao; nyumba zao zitaporwa na wake zao watanajisiwa.

17 Tazama, nitawachochea Wamedi dhidi yao, ambao hawatafikiri fedha na dhahabu, wala hawatazifurahia.

18 Na pinde zao zitawakatakata vijana vipande vipande; na hawatahurumia matunda ya tumbo; macho yao hayata waacha watoto.

19 Na Babilonia, utukufu wa falme, na [a]urembo wa ubora wa Wakaldayo, itakuwa kama wakati Mungu alivyopindua [b]Sodoma na Gomora.

20 [a]Hautakaliwa tena, wala watu hawataishi ndani yake tangu kizazi hadi kizazi: wala Mwarabu kupiga hema hapo; wala wachungaji hawatalaza makundi yao huko.

21 Lakini wanyama [a]wakali wa jangwani watalala huko; na nyumba zao zitajaa wanyama wa kuhuzunisha; na bundi wataishi huko, na [b]mbuzi wa mwitu watacheza huko.

22 Na nyumbu wa visiwani

9 *a* MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
10 *a* MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
11 *a* Mal. 4:1.
b M&M 64:24.
12 *a* Isa. 4:1–4.
13 *a* MWM Dunia—Hali ya mwisho ya dunia.
14 *a* AU paa anayewindwa.
19 *a* MY isiyofaa.
b Mwa. 19:24–25; Kum. 29:23; 2 Ne. 13:9.
20 *a* Yer. 50:3, 39–40.
21 *a* Isa. 34:14–15.
b EBR mbuzi dume, au pepo wachafu.

watabweka katika [a]nyumba zao zilizo na ukiwa, na [b]majoka katika ngome zao nzuri; na wakati wake unakaribia, na siku yake haitaongezeka. Kwani nitamwangamiza kwa haraka; ndiyo, kwani nitawarehemu watu wangu, lakini waovu wataangamia.

MLANGO WA 24

Israeli itakusanywa na kufurahia pumziko la Milenia—Lusiferi alifukuzwa kutoka mbinguni kwa sababu ya maasi—Israeli itashinda Babilonia (ulimwengu)—Linganisha Isaya 14. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Kwani Bwana atamrehemu Yakobo, na hata hivyo [a]atachagua Israeli, na kuwaweka katika nchi yao wenyewe; na [b]wageni wataunganishwa na wao, na kuungana na nyumba ya Yakobo.

2 [a]Na watu watawachukua na kuwaleta mahali pao; ndiyo, kutoka mbali hadi miisho ya dunia; nao watarejea katika [b]nchi zao za ahadi. Na nyumba ya Israeli itawamiliki, na nchi ya Bwana itakuwa kwa ajili ya [c]watumishi na wajakazi; na watawachukua wafungwa wale waliowafunga; na watatawala juu ya watesi wao.

3 Na itakuwa kwamba katika siku ile kwamba Bwana atakupatia [a]pumziko, kutoka kwa huzuni yako, na kutoka woga wako, na kutoka ufungwa mgumu ambao ulifanywa kutumika.

4 Na itakuwa kwamba katika siku ile, kwamba utarudia methali hii dhidi ya mfalme wa [a]Babilonia, na kusema: Jinsi gani mwenye kudhulumu amekoma, na mji wa dhahabu kukoma!

5 Bwana amelivunja gongo la waovu, dalili za enzi za watawala.

6 Yeye aliyewapiga watu katika ghadhabu kwa mapigo yasiyokoma, yeye ambaye alitawala mataifa kwa hasira, ana adhibiwa, na hakuna yeyote atakayezuia.

7 Ulimwengu wote unapumzika, na umekuwa kimya; wanaanza [a]kuimba.

8 Ndiyo, [a]misunobari inakusherekea, na pia mierezi ya Lebanoni, ikisema: Tangu wewe [b]ulazwe chini hakuna [c]yeyote amekuja dhidi yetu.

9 [a]Jehanamu imetaharuki kukulaki utakapokuja; inawaamsha [b]wafu kwa sababu yako, hata walio wakuu wote wa dunia; imewainua kutoka viti vyao vya enzi wafalme wote wa mataifa.

22 *a* EBR makasri.
b EBR (pengine) mbweha, au mbwa mwitu.

24 1 *a* Zek. 1:17.
b Isa. 60:3–5, 10.
2 *a* MY Mataifa mengine yataisaidia Israeli.
b MWM Nchi ya Ahadi.
c Isa. 60:14.
3 *a* Yos. 1:13; M&M 84:24.
4 *a* MWM Babeli, Babilonia.
7 *a* Isa. 55:12.
8 *a* EBR mvinje.
b MY katika kifo.
c EBR kikata mti hakijaja dhidi yetu.
9 *a* MWM Jehanamu.
b MY roho ambazo haziko katika mwili.

10 Wote watanena na kukwambia: Je, nawe pia umekuwa mnyonge kama sisi? Je, nawe umekuwa kama sisi?

11 Fahari yako imeshushwa chini kaburini; na kelele ya mazeze yako haisikiki; funza ametandazwa chini yako, na funza wamekufunika.

12 [a]Jinsi gani umeanguka kutoka mbinguni, Ee [b]Lusiferi, mwana wa asubuhi! Je, umekatwa chini, ambaye alidhoofisha mataifa!

13 Kwani umesema moyoni mwako: [a]Mimi nitapanda mbinguni, nitainua kiti changu cha enzi juu ya nyota za Mungu; nitaketi pia juu ya mlima wa mkutano, katika pande za [b]kaskazini;

14 Nitapanda kupita vimo vya mawingu; nitakuwa kama yeye Aliye Juu Sana.

15 Bado wewe utashushwa chini jehanamu, hadi pande za [a]shimo.

16 Wale watakaokuona watakukazia macho kwa [a]makini, na kukufikiria, na watasema: Je huyu ni yule mtu aliyetetemesha dunia, aliyetingisha falme?

17 Na kufanya ulimwengu kama nyika, na kuangamiza miji iliyomo ndani yake, na hakufungua nyumba za wafungwa wake?

18 Wafalme wote wa mataifa, ndiyo, wote, wamezikwa kwa utukufu, kila mmoja wao katika [a]nyumba yake mwenyewe.

19 Lakini wewe umetupwa mbali na kaburi lako kama [a]tawi linalochukiza, na baki la wanaouawa, wanaodungwa kwa upanga, ambao wanashuka chini hadi kwenye [b]mawe ya shimo; kama mzoga uliokanyagwa chini miguuni.

20 Wewe hutaunganishwa na wao katika mazishi, kwa sababu umeangamiza nchi yako na kuwaua watu wako; [a]uzao wa [b]waovu hautaheshimiwa kamwe.

21 Tayarisheni machinjo kwa watoto wao kwa sababu ya [a]maovu ya baba zao, ili wasije wakainuka, wala kumiliki nchi, wala kujaza uso wa dunia na miji.

22 Kwani nitainuka dhidi yao, asema Bwana wa Majeshi, na kutenga kutoka Babilonia [a]jina, na baki, na mwana, na [b]mpwa, asema Bwana.

23 Pia nitaifanya [a]makao ya ngojamaliko, na maziwa ya maji; na nitaifagia kwa ufagio wa maangamizo, asema Bwana wa Majeshi.

12*a* M&M 76:26.
b EBR nyota ya asubuhi, mwana wa alfajiri. Mtawala wa ulimwengu muovu (Babiloni) anazungumziwa kama Lusiferi, mtawala wa uovu wote. MWM Ibilisi; Lusiferi.
13*a* Musa 4:1–4.
b MY makazi ya miungu kulingana na imani ya Kibabiloni. Zab. 48:2.
15*a* 1 Ne. 14:3.
16*a* EBR akutupie jicho na akuwazie.
18*a* MY kaburi la familia yake.
19*a* MY tawi lililokataliwa, lilipogolewa na kutupwa.
b MY chini kabisa.
20*a* Zab. 21:10–11; 37:28.
b MWM Ovu, Uovu.
21*a* Ku. 20:5.
22*a* Mit. 10:7.
b Ayu. 18:19.
23*a* Isa. 34:11–15.

24 Bwana wa Majeshi ameapa, akisema: Kwa kweli vile nimefikiria, hivyo yatatimia; na yale niliyoamua, ndiyo yatabaki imara—

25 Kwamba nitamleta [a]Mwashuri nchini mwangu, na kwenye [b]milima yangu nitamkanyaga chini ya miguu; kisha [c]nira yake itawaondokea, na mzigo wake kuondoka kutoka mabega yao.

26 [a]Hili ndilo kusudi lililonuiwa duniani kote; na huu ndiyo mkono ambao umenyooshwa kwa mataifa yote.

27 Kwani Bwana wa Majeshi amenuia, na nani atakayelibatilisha? Na mkono wake umenyooshwa, na nani atakayeurudisha nyuma?

28 Katika ule [a]mwaka ambao mfalme [b]Ahazi alikufa kulikuwa na mzigo huu.

29 Usifurahi ewe, Ufilisti wote, kwa sababu fimbo ya aliyekupiga imevunjika; kwani kutoka mzizi wa nyoka atatoka fira, na uzao wake utakuwa nyoka wa moto arukaye.

30 Na mzaliwa wa kwanza wa maskini watakula, na walio na shida watalala kwa usalama; na nitaua mzizi wako kwa njaa, na yeye ataua baki lako.

31 Pigeni yowe, Ee lango; lia, Ee mji, wewe, Ufilisti wote, umeyeyuka; kwani kutoka kaskazini kutakuja moshi, na hakuna yeyote atakayekuwa pekee mahali alipopangiwa.

32 Nini hapo kitakacho wajibu wajumbe wa mataifa? Kwamba Bwana ameimarisha [a]Sayuni, na walio [b]maskini wa watu wake [c]wataitumaini.

MLANGO WA 25

Nefi anautukuza unyoofu—Unabii wa Isaya utafahamika katika siku za mwisho—Wayahudi watarejea kutoka Babilonia, watamsulubu Masiya, na watatawanywa na kuadhibiwa—Watarudishwa wakimwamini Masiya—Atakuja kwanza miaka mia sita tangu Lehi aondoke Yerusalemu—Wanefi wanatii sheria ya Musa na kumwamini Kristo, aliye Mtakatifu wa Israeli. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Sasa mimi, Nefi, nasema machache kuhusu maneno ambayo nimeandika, ambayo yamenenwa na kinywa cha Isaya. Kwani tazama, Isaya alizungumza vitu vingi ambavyo vilikuwa [a]vigumu kufahamika na watu wangu; kwani hawajui kuhusu mtindo wa kutoa unabii miongoni mwa Wayahudi.

2 Kwani mimi, Nefi, sijawafundisha vitu vingi kuhusu

25 *a* Mazungumzo yanabadilika kuwa shambulio la Ashuru na kuanguka kwa Yuda, 701 K.K. (aya ya 24–27). 2 Fal. 19:32–37; Isa. 37:33–38.
b MY milima ya Yuda na Israeli.
c Isa. 10:27.
26 *a* MY Hatimaye mataifa yote ya ulimwengu yataangushwa hivi.
28 *a* MY Karibu mwaka 720 K.K. mzigo huu au ujumbe wa maangamizo ulitabiriwa kuhusu Wafilisti, wakati Yuda atakuwa.
b 2 Fal. 16:20.
32 *a* MWM Sayuni.
b Sef. 3:12.
c AU tafuta kimbilio ndani yake.
25 1 *a* 2 Ne. 25:5–6.

desturi za Wayahudi; [a]kwani kazi zao zilikuwa kazi za giza, na matendo yao yalikuwa matendo ya machukizo.

3 Kwa hivyo, ninawaandikia watu wangu, kwa wale wote watakaopokea hapo baadaye vitu hivi ambavyo ninaandika, ili wajue hukumu za Mungu, kwamba zinashukia mataifa yote, kulingana na neno ambalo amenena.

4 Kwa hivyo, sikilizeni, Enyi watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli, na msikilize maneno yangu; kwani kwa sababu maneno ya Isaya sio wazi kwenu, walakini ni wazi kwa wale wote ambao wamejazwa na [a]roho ya [b]unabii. Lakini nawapatia unabii, kulingana na roho aliye ndani yangu; kwa hivyo nitatoa unabii kulingana na [c]unyofu uliokuwa na mimi tangu wakati nitoke Yerusalemu na baba yangu; kwani tazama, nafsi yangu inafurahia unyofu kwa watu wangu, ili wajifunze.

5 Ndiyo, na nafsi yangu inafurahia maneno ya [a]Isaya, kwani nilitoka Yerusalemu, na macho yangu yameona vitu vya [b]Wayahudi, na ninajua kwamba Wayahudi wanafahamu vitu vya manabii, na hakuna watu wengine wanaofahamu vitu vilivyonenwa Wayahudi kama wao, ila tu kwamba wawe wamefundishwa desturi ya vitu vya Wayahudi.

6 Lakini tazama, mimi, Nefi, sijafundisha watoto wangu desturi za Wayahudi; lakini tazama, mimi, mwenyewe, nimeishi Yerusalemu, kwa hivyo najua kuhusu eneo karibu inayoizingira; na nimewatajia watoto wangu kuhusu hukumu za Mungu, ambazo [a]zimefanyika miongoni mwa Wayahudi, kwa watoto wangu, kulingana na yale yote ambayo Isaya amezungumza, na siyaandiki.

7 Lakini tazama, ninaendelea na unabii wangu, kulingana na [a]unyofu wangu; ambamo kwayo najua kwamba hakuna mtu yeyote anayeweza kukosea; walakini, katika siku ambazo unabii wa Isaya utatimizwa watu watajua kwa hakika, wakati yatatimizwa.

8 Kwa hivyo, yana [a]thamani kwa watoto wa watu, na kwa yule anayedhani kwamba hayana, kwa hawa nitawazungumzia zaidi, na kuyatilia mkazo kwa watu [b]wangu; kwani ninajua kwamba yatawafaidi sana katika [c]siku za mwisho; kwani katika siku hizo watayafahamu; kwa hivyo, ni kwa faida yao nimeyaandika.

9 Na kama vile kizazi kimoja miongoni mwa Wayahudi

2 *a* 2 Fal. 17:13–20.
4 *a* MWM Roho Mtakatifu.
b MWM Toa unabii, Unabii.
c 2 Ne. 31:3; 33:5–6; Yak. (KM) 4:13.
5 *a* 1 Ne. 19:23; 3 Ne. 23:1.
b MWM Wayahudi.
6 *a* 2 Ne. 6:8; Hel. 8:20–21.
7 *a* 2 Ne. 32:7; Alma 13:23.
8 *a* MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
b Eno. 1:13–16; Morm. 5:12–15; M&M 3:16–20.
c MWM Siku za Mwisho.

[a]kimeangamizwa kwa sababu ya uovu, hata hivyo wameangamizwa kutoka kizazi hadi kizazi kulingana na maovu yao; na hakuna aliyeangamizwa bila [b]kuaguliwa na manabii wa Bwana.

10 Kwa hivyo, walikuwa wameelezewa kuhusu maangamizo yatakayowajia, mara tu baada ya baba yangu alipotoka Yerusalemu; walakini, walishupaza mioyo yao; na kulingana na unabii wangu [a]wameangamizwa, ijapokuwa wale [b]waliopelekwa utumwani huko Babilonia.

11 Na sasa haya nazungumza kwa sababu ya roho iliyo ndani yangu. Na ingawaje wamehamishwa watarejea tena, na kumiliki nchi ya Yerusalemu; kwa hivyo, [a]watarudishwa tena katika nchi yao ya urithi.

12 Lakini, tazama, watakuwa na vita, na uvumi wa vita; na wakati siku inafika ambayo [a]Mzaliwa Pekee wa Baba, ndiyo, hata Baba wa mbingu na dunia, atajithirihisha mwenyewe kwao katika mwili, tazama, watamkataa, kwa sababu ya maovu yao, na ugandamizo wa mioyo yao, na ugumu wa shingo zao.

13 Tazama, [a]watamsulubu; na baada ya kulazwa katika [b]ziara kwa muda wa siku [c]tatu [d]atafufuka kutoka kwa wafu, na uponyaji katika mabawa yake; na wale wote watakaoamini kwa jina lake wataokolewa katika ufalme wa Mungu. Kwa hivyo, nafsi yangu inafurahia kutoa unabii kumhusu, kwani [e]nimeona siku yake, na moyo wangu unatukuza jina lake takatifu.

14 Na tazama itakuwa kwamba baada ya [a]Masiya kufufuka kutoka kwa wafu, na kujithirihisha kwa watu wake, kwa wengi kadiri watakavyoliamini jina lake, tazama, Yerusalemu [b]itaangamizwa tena; kwani ole kwa wale wanaopigana dhidi ya Mungu na watu wa kanisa lake.

15 Kwa hivyo, [a]Wayahudi [b]watatawanywa miongoni mwa mataifa yote; ndiyo, na [c]Babilonia pia itaangamizwa; kwa hivyo, Wayahudi watatawanywa na mataifa mengine.

16 Na baada ya wao kutawanywa, na Bwana Mungu kuwapiga kwa mataifa mengine kwa muda wa vizazi vingi, ndiyo, hata chini kutoka kizazi hadi kizazi mpaka watashawishiwa [a]kumwamini Kristo, Mwana wa Mungu, na upatanisho,

9*a* Yer. 39:4–10; Mt. 23:37–38.
b Amo. 3:7; 1 Ne. 1:13.
10*a* 1 Ne. 7:13; 2 Ne. 6:8; Omni 1:15; Hel. 8:20–21.
b 2 Fal. 24:14; Yer. 52:3–16.
11*a* Ezra 1:1–4; Yer. 24:5–7.
12*a* MWM Mzaliwa Pekee.
13*a* Lk. 23:33.
b Yn. 19:41–42; 1 Ne. 19:10.
c Lk. 24:6–7; Mos. 3:10.
d MWM Ufufuko.
e 1 Ne. 11:13–34.
14*a* MWM Masiya.
b Lk. 21:24; JS—M 1:1–18.
15*a* MWM Wayahudi.
b Neh. 1:8–9; 2 Ne. 10:6.
c MWM Babeli, Babilonia.
16*a* 2 Ne. 10:6–9; 30:7; Morm. 5:14.

ambao ni kwa wanadamu wote bila kikomo—na wakati ile siku itakapofika kwamba watamwamini Kristo, na kumwabudu Baba katika jina lake, na mioyo mweupe na mikono safi, na wasimtazamie Masiya mwingine, kisha, katika ule wakati, siku itafika ambapo itakuwa lazima waamini vitu hivi.

17 Na Bwana atanyoosha mkono wake tena mara ya pili [a]kuwarudisha watu wake kutoka kwa hali yao ya kupotea na kuanguka. Kwa hivyo, ataendelea kutenda kazi [b]kuu na maajabu miongoni mwa watoto wa watu.

18 Kwa hivyo, atawaletea maneno yake, [a]maneno yale [b]yatakayowahukumu katika siku ya mwisho, kwani yatapewa kwao kwa lengo la [c]kuwasadikisha kuhusu Masiya wa kweli, aliyekataliwa nao; na kuwasadikishia kwamba hawana haja tena kumtazamia Masiya mwingine aje, kwani hakuna mwingine atakayekuja, ila tu awe [d]Masiya wa bandia atakayewadanganya watu; kwani kuna Masiya mmoja tu anayezungumziwa na manabii, na huyo Masiya ndiye yule atakayekataliwa na Wayahudi.

19 Kwani kulingana na maneno ya manabii, [a]Masiya atakuja baada ya miaka [b]mia sita tangu baba yangu atoke Yerusalemu; na kulingana na maneno ya manabii, na pia neno la [c]malaika wa Mungu, jina lake litakuwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu.

20 Na sasa, ndugu zangu, nimezungumza wazi ili msikosee. Na jinsi aishivyo Bwana Mungu [a]aliyewatoa Israeli kutoka nchi ya Misri, na akampatia Musa uwezo kwamba [b]aponye mataifa baada ya wao kuumwa na [c]nyoka wenye sumu, kama wangemtazama nyoka ambaye aliinuliwa mbele yao, na pia akampa uwezo kwamba agonge [d]mwamba na maji yatokee; ndiyo, tazama nawaambia, kwamba jinsi vile hivi vitu ni kweli, na jinsi Bwana Mungu aishivyo, hakuna [e]jina lingine ambalo limetolewa chini ya mbingu ila tu awe huyu Yesu Kristo, ambalo nimelizungumzia, ambalo kwamba mwanadamu anaweza kuokolewa.

21 Kwa hivyo, kwa sababu hii Bwana Mungu ameniahidi kwamba hivi vitu ambavyo [a]ninaandika vitawekwa

17 *a* 2 Ne. 21:11–12; 29:1. MWM Urejesho wa Injili.
b Isa. 29:14; 2 Ne. 27:26; 3 Ne. 28:31–33.
18 *a* 2 Ne. 29:11–12; 33:11, 14–15.
b MWM Hukumu ya mwisho.
c 2 Ne. 26:12–13.
d MWM Mpinga Kristo.
19 *a* MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.
b 1 Ne. 10:4; 3 Ne. 1:1, 13.
c 2 Ne. 10:3.
20 *a* Ku. 3:7–10; 1 Ne. 17:24, 31; 19:10.
b Yn. 3:14; 1 Ne. 17:41.
c Hes. 21:8–9; Alma 33:19; Hel. 8:14–15.
d Ku. 17:6; Hes. 20:11; 1 Ne. 17:29; 20:21.
e Hos. 13:4; Mdo. 4:10–12; Mos. 5:8; Musa 6:52. MWM Mwokozi.
21 *a* 2 Ne. 27:6–14.

na kuhifadhiwa, na kutolewa kwa uzao wangu, kutoka kizazi hadi kizazi, ili ahadi atimiziwe Yusufu, kwamba uzao wake [b]hautaangamia kamwe kadiri dunia itakavyosimama.

22 Kwa hivyo, hivi vitu vitaendelea kutoka kizazi kimoja hadi kizazi kingine kadiri dunia itakavyokuwepo; na vitaendelea kulingana na njia na mapenzi ya Mungu; na mataifa yatakayovimiliki [a]yatahukumiwa kwavyo kulingana na maneno ambayo yameandikwa.

23 Kwani tunajitahidi kuandika, [a]kuwashawishi watoto wetu, na pia ndugu zetu, kumwamini Kristo, na kupatanishwa na Mungu; kwani tunajua kwamba ni kwa [b]neema kwamba tunaokolewa, baada ya [c]kutenda yote tunayoweza.

24 Na, ingawa tunamwamini Kristo, [a]tunatii sheria ya Musa, na kutazama mbele kwa uthabiti kwa Kristo, hadi sheria itakapotimizwa.

25 Kwani, ni kwa kusudi hili [a]sheria ilitolewa; kwa hivyo sheria [b]imekufa kwetu, na tumefanywa hai katika Kristo kwa sababu ya imani yetu; lakini bado tunatii sheria kwa sababu ya amri.

26 Na [a]tunazungumza kuhusu Kristo, tunafurahia katika Kristo, tunahubiri kuhusu Kristo, tunatoa [b]unabii kumhusu Kristo, na tunaandika kulingana na unabii wetu, ili [c]watoto wetu wajue asili ya kutegemea [d]msamaha wa dhambi zao.

27 Kwa hivyo, tunazungumza kuhusu sheria ili watoto wetu wajue mauti ya sheria; na wao, kwa kujua mauti ya sheria; watatazama mbele kwa ule uhai ulio katika Kristo, na wafahamu ni kwa kusudi gani sheria ilitolewa. Na baada ya sheria kutimizwa katika Kristo, kwamba wasishupaze mioyo yao dhidi yake wakati sheria itakapotakiwa kuwekwa kando.

28 Na sasa tazama, watu wangu, ninyi ni watu wa [a]shingo ngumu; kwa hivyo, nimewazungumzia kwa uwazi, ili msielewe vibaya. Na maneno ambayo nimezungumza yatabaki kama [b]ushuhuda dhidi yenu; kwani yanatosha [c]kumfundisha mtu yeyote njia iliyo sawa; kwani njia iliyo sawa ni kuamini katika Kristo na kutomkana kwani kwa kumkana unawakana pia manabii na sheria.

29 Na sasa tazama, nawaambia kwamba njia iliyo sawa ni kuamini katika Kristo, na kutomkana; na Kristo ndiye

21 *b* Amo. 5:15; 2 Ne. 3:16; Alma 46:24–27.
22 *a* 2 Ne. 29:11; 33:10–15; 3 Ne. 27:23–27.
23 *a* MWM Mtoto, Watoto.
b Rum. 3:23–24; 2 Ne. 2:4–10; Mos. 13:32; Alma 42:12–16; M&M 138:4. MWM Neema.
c Yak. (Bib.) 2:14–26. MWM Matendo.
24 *a* Yak. (KM) 4:4–5.
25 *a* MWM Torati ya Musa.
b Rum. 7:4–6.
26 *a* Yak. (KM) 4:12; Yar. 1:11; Mos. 3:13.
b Lk. 10:23–24.
c MWM Mtoto, Watoto.
d MWM Ondoleo la Dhambi.
28 *a* Mos. 3:14.
b MWM Ushuhuda.
c 2 Ne. 33:10.

Mtakatifu wa Israeli; kwa hivyo lazima msujudu mbele yake, na mmwabudu kwa [a]uwezo wenu wote, akili, na nguvu, na nafsi zenu zote; na mkifanya hivi, hamtatengwa kwa njia yoyote.

30 Na, kadiri itakavyohitajika, lazima utii matendo na [a]masharti ya Mungu hadi sheria aliyopewa Musa itakapotimizwa.

MLANGO WA 26

Kristo atawahudumia Wanefi—Nefi anaona mbele maangamizo ya watu wake—Watazungumza kutoka mavumbini—Wayunani watajenga makanisa ya bandia na makundi maovu ya siri—Bwana anawakataza wanadamu wasifanye ukuhani wa uongo. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na baada ya Kristo [a]kufufuka kutoka kwa wafu [b]atajidhihirisha kwenu ninyi, watoto wangu, na ndugu zangu wapendwa; na maneno atakayowazungumzia yatakuwa [c]sheria mtakayoitii.

2 Kwani tazama, nawaambia kwamba nimeona kwamba vizazi vingi vitapita, na kutakuwa na vita kuu na mabishano miongoni mwa watu wangu.

3 Na baada ya Masiya kuja watu wangu watapewa [a]ishara kuhusu [b]kuzaliwa kwake, na pia kuhusu kifo chake na kufufuka kwake; na siku ile itakuwa kuu na mbovu kwa wale walio waovu, kwani wataangamia; na wanaangamia kwa sababu waliwafukuza manabii, na watakatifu, na kuwapiga mawe, na kuwaua; kwa hivyo kilio cha [c]damu ya watakatifu kitapanda kwa Mungu kutoka chini dhidi yao.

4 Kwa hivyo, wale wote walio na kiburi, na watendao maovu, siku itakayofika [a]itawachoma, asema Bwana wa Majeshi, kwani watakuwa kama makapi.

5 Na wale wanaoua manabii, na watakatifu, [a]watamezwa na kina cha ardhi, asema Bwana wa Majeshi; na [b]milima itawafunika, na vimbunga vitawabeba, na majengo kuwaangukia na kuwavunja kwa vipande na kuwasaga kama unga.

6 Na wataadhibiwa kwa radi, na umeme, na matetemeko ya ardhi, na kila aina ya maangamizo, kwani moto wa hasira ya Bwana utawawakia, na watakuwa kama makapi, na ile siku inayokuja itawamaliza, asema Bwana wa Majeshi.

7 Ee uchungu, na maumivu ya nafsi yangu kwa sababu ya watu wangu waliopotea kwa kuuawa! Kwani mimi, Nefi, nimeiona, na inakaribia kunimaliza katika uwepo wa Bwana; lakini lazima nimlilie Mungu wangu: Njia zako ni za [a]haki.

8 Lakini tazama, wenye haki

29*a* Kum. 6:5; Mk. 12:29–31.
30*a* MWM Ibada.
26 1*a* 3 Ne. 11:1–12.
b 1 Ne. 11:7; 12:6.
c 3 Ne. 15:2–10.
3*a* 1 Ne. 12:4–6. MWM Ishara.
b MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.
c Mwa. 4:10; 2 Ne. 28:10; Morm. 8:27.
4*a* 3 Ne. 8:14–24; 9:3, 9.
5*a* 1 Ne. 19:11; 3 Ne. 10:14.
b 3 Ne. 8:10; 9:5–8.
7*a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.

wanaotii maneno ya manabii, na bila kuwaangamiza, lakini wanamtazamia Kristo kwa uthabiti na ishara zinazotolewa, ingawa [a]mateso hayo yote—tazama, wao ndiyo wao ambao [b]hawataangamia.

9 Lakini Mwana wa Uadilifu [a]atawatokea; na [b]atawaponya, na watakuwa na [c]amani na yeye, hadi vizazi [d]vitatu vitakuwa vimepita, na wengi wa kizazi cha [e]nne watakuwa wamepita kwa uadilifu.

10 Na wakati vitu hivi vimepita [a]maangamizo ya haraka yatawajia watu wangu; kwani ingawa nafsi yangu ina uchungu, nimeiona; kwa hivyo, najua kwamba itatimia; na wanajiuza bure; kwani, kwa zawadi ya kiburi chao na upumbafu wao watavuna maangamizo; kwani kwa sababu watajitolea ibilisi na kuchagua kazi za giza badala ya nuru, kwa hivyo lazima waende chini [b]jehanamu.

11 Kwani Roho wa Bwana daima [a]haitajishughulisha na wanadamu. Na wakati Roho anakoma kujishughulisha na wanadamu basi maangamizo ya haraka yanakuja, na hii inahuzunisha nafsi yangu.

12 Na kama nilivyosema kuhusu [a]kuwasadikisha [b]Wayahudi, kwamba Yesu ndiye [c]yule Kristo, inahitajika lazima kwamba Wayunani pia nao wasadikishiwe kwamba Yesu ndiye Kristo, Mungu wa Milele;

13 Na kwamba anajidhihirisha kwa wale wote wanaomwamini, kwa nguvu za [a]Roho Mtakatifu; ndiyo, kwa kila taifa, kabila, lugha, na watu, akifanya maajabu makuu, ishara, na miujiza, miongoni mwa watoto wa watu kulingana na imani yao.

14 Lakini tazama, nawatolea unabii kuhusu [a]siku za mwisho; kuhusu siku zile Bwana Mungu [b]atakapowaletea watoto wa watu vitu hivi.

15 Baada ya uzao wangu na uzao wa kaka zangu kufifia katika kutoamini, na watakuwa wamepigwa na Wayunani; ndiyo, baada ya Bwana Mungu kuwazingira, na kuwa husuru kwa kilima, na kuinua ngome dhidi yao; na baada ya wao kushushwa chini mavumbini, hadi wamalizwe kabisa, bado maneno ya wenye haki yataandikwa, na sala za waumini yatasikika, na wale wote ambao wamefifia katika kutoamini hawatasahaulika.

16 Kwani wale watakaoangamizwa [a]watawazungumzia kutoka ardhini, na sauti yao itakuwa sauti kunjufu kutoka

8 *a* MWM Mateso, Tesa.
b 3 Ne. 10:12–13.
9 *a* 3 Ne. 11:8–15.
b 3 Ne. 17:7–9.
c 4 Ne. 1:1–4.
d 1 Ne. 12:11–12; 3 Ne. 27:30–32.
e Alma 45:10–12; Hel. 13:9–10.
10 *a* Alma 45:9–14; Morm. 8:1–9.
b MWM Jehanamu.
11 *a* Eth. 2:15.
12 *a* 2 Ne. 25:18.
b 2 Ne. 30:7; Morm. 5:14. MWM Wayahudi.
c Morm. 3:21.
13 *a* MWM Roho Mtakatifu.
14 *a* MWM Siku za Mwisho.
b MWM Urejesho wa Injili.
16 *a* Isa. 29:4; Moro. 10:27; Musa 7:62. MWM Kitabu cha Mormoni.

mavumbini, na sauti yao itakuwa kama moja ambayo ina pepo ya utambuzi; kwani Bwana Mungu atampatia uwezo, kwamba anong'one juu yao, hata iwe ni kama kutoka ardhini; na sauti yao itanong'ona kutoka mavumbini.

17 Kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu: [a]Wataandika vile vitu vitakavyotendwa miongoni mwao, na vitaandikwa na kutiwa muhuri katika kitabu, na wale waliofifia katika kutoamini hawatavipokea, kwani wanajaribu [b]kutafuta kuharibu vitu vya Mungu.

18 Kwa hivyo, kwa kuwa wale walioangamizwa wameangamizwa kwa haraka; na kundi la watu watishao watakuwa kama [a]makapi yapitayo—ndiyo, hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu: Itakuwa kwa muda, ghafla—

19 Na itakuwa, kwamba wale waliofifia katika kutoamini [a]watapigwa kwa mkono wa Wayunani.

20 Na Wayunani wamejiinua kwa [a]kiburi cha macho yao, na [b]wamejikwaa, kwa sababu ya [c]kikwazo kikuu, kwamba wamejenga [d]makanisa mengi; walakini, wanadharau uwezo na miujiza ya Mungu, na kujihubiria wao wenyewe hekima yao na [e]elimu yao, ili wafaidike na [f]kuseta uso wa maskini.

21 Na kuna makanisa mengi ambayo yamejengwa yanayosababisha [a]wivu, na ubishi, na chuki.

22 Na pia kuna [a]makundi maovu ya siri, hata kama siku za kale, kulingana na makundi ya ibilisi, kwani yeye ndiye chanzo cha vitu hivi vyote; ndiyo, chanzo cha mauaji, na kazi za giza; ndiyo, na huwaongoza kwa shingo na mkanda wa kitani, hadi anawafunga kwa mikanda yake milele.

23 Kwani tazama, ndugu zangu wapendwa, nawaambia kwamba Bwana Mungu hatendi kazi yake gizani.

24 Hafanyi chochote ila tu kwa manufaa ya ulimwengu; kwani [a]anapenda ulimwengu, hata kwamba anatoa maisha yake ili awavute wanadamu [b]wote kwake. Kwa hivyo, hamwamuru yeyote asipokee wokovu wake.

25 Tazama, je yeye hulilia yeyote, na kusema: Niondokeeni? Tazama, nawaambia, Hapana; lakini husema: [a]Njooni kwangu nyote kutoka pande zote za mwisho wa ulimwengu, [b]nunueni maziwa na asali, bila pesa na bila bei.

26 Tazama, je amemwamuru yeyote kutoka katika masinagogi, au kutoka nyumba za ibada? Tazama, nawaambia, Hapana.

27 Je, amewaamuru wowote

17*a* 2 Ne. 29:12.
b Eno. 1:14.
18*a* Morm. 5:16–18.
19*a* 3 Ne. 16:8–9; 20:27–28.
20*a* MWM Kiburi.
b 1 Ne. 13:29, 34. MWM Ukengeufu.
c Eze. 14:4.
d 1 Ne. 14:10; 22:23; Morm. 8:28.
e 2 Ne. 9:28; Morm. 9:7–8.
f Isa. 3:15; 2 Ne. 13:15.
21*a* MWM Husuda.
22*a* MWM Makundi maovu ya siri.
24*a* Yn. 3:16.
b 3 Ne. 27:14–15.
25*a* Alma 5:33–35; 3 Ne. 9:13–14.
b Isa. 55:1–2.

wasipokee [a]wokovu wake? Tazama nawaambia, Hapana; lakini [b]ameutoa bure kwa wanadamu wote; na amewaamuru watu wake kwamba wawashawishi wanadamu wote [c]watubu.

28 Tazama, je, Bwana amewaamuru wowote wasipokee wema wake? Tazama nawaambia, Hapana; lakini wanadamu [a]wote wana haki sawa, na hakuna yeyote anayekatazwa.

29 Anaamuru kwamba kusiwe na [a]ukuhani wa uongo; kwani, tazama, ukuhani wa uongo ni kwamba wanadamu wanahubiri na kujiinua wawe nuru ya ulimwengu, ili wafaidike na wapate [b]sifa za ulimwengu; lakini hawajali ustawi wa Sayuni.

30 Tazama, Bwana amekataza kitu hiki; kwa hivyo, Bwana Mungu ametoa amri kwamba wanadamu wote wawe na hisani, [a]hisani ambayo ni [b]upendo. Na bila kuwa na hisani wao sio chochote. Kwa hivyo, kama wangekuwa na hisani hawangekubali mtumishi wa Sayuni kuangamia.

31 Lakini mtumishi wa Sayuni atatumikia [a]Sayuni; kwani kama watatumikia kwa sababu ya [b]pesa wataangamia.

32 Na tena, Bwana Mungu [a]ameamuru kwamba wanadamu wasiue; kwamba wasidanganye; kwamba wasiibe; kwamba wasiape [b]bure kwa jina la Bwana Mungu wao; kwamba wasiwe na wivu; kwamba wasiwe na chuki; kwamba wasibishane wao; kwamba kwa wao wasifanye uasherati; na kwamba wasitende vyovyote vya vitu hivi; kwani yeyote atakayevitenda ataangamia.

33 Kwani hakuna yoyote ya haya maovu yatokayo kwa Bwana; kwani anatenda yale ambayo ni mema miongoni mwa watoto wa watu; na hatendi lolote lisilo wazi kwa watoto wa watu; na anawakaribisha wote kuja kwake na kupokea wema wake; na [a]hamkatazi yeyote anayemjia, mweusi na mweupe, wafungwa na walio huru, mwanaume na mwanawake; na anawakumbuka [b]kafiri; na [c]wote ni sawa kwa Mungu, wote wawili, Myahudi na Myunani.

MLANGO WA 27

Giza na ukengeufu yataufunika ulimwengu katika siku za mwisho—Kitabu cha Mormoni kitatokea—Mashahidi watatu watakishuhudia kitabu—Mtu aliyeelimika atasema hawezi kukisoma kitabu kilichotiwa muhuri—Bwana atatenda kazi kuu na ya maajabu—Linganisha Isaya 29. Karibia mwaka 559–545 K.K.

27 *a* MWM Wokovu.
b Efe. 2:8; 2 Ne. 25:23.
c MWM Toba, Tubu.
28 *a* Rum. 2:11; 1 Ne. 17:33–35.
29 *a* MWM Ukuhani wa uongo.
b M&M 121:34–37.
30 *a* Moro. 7:47–48. MWM Hisani.
b MWM Upendo.
31 *a* MWM Sayuni.
b Yak. (KM) 2:17–19; M&M 11:7; 38:39.
32 *a* MWM Amri za Mungu.
b MWM Lugha chafu.
33 *a* Mdo. 10:9–35, 44–45.
b Alma 26:37.
c Rum. 2:11; 1 Ne. 17:35.

Lakini, tazama, katika [a]siku za mwisho, au katika siku za Wayunani—ndiyo, tazama mataifa yote ya Wayunani na pia Wayahudi, wote watakaokuja katika nchi hii na wale watakaokuwa katika nchi zingine, ndiyo, hata katika nchi zote za dunia, tazama, watalewa kwa maovu na aina zote za machukizo—

2 Na siku ile itakapofika wataadhibiwa na Bwana wa Majeshi, kwa radi na kwa mtetemeko wa ardhi, na kwa ngurumo, na kwa dhoruba, na kwa tufani, na kwa [a]mwale wa moto unaounguza.

3 Na [a]mataifa yote [b]yapiganayo dhidi ya Sayuni, na yale yanayomuudhi, yatakuwa ni kama ndoto ya maono usiku; ndiyo, itakuwa kwao, hata kama mtu mwenye njaa aotaye, na tazama anakula lakini anaamka na nafsi yake ni tupu; au kama mtu aliye na kiu aotaye, na tazama anakunywa lakini anaamka na tazama anazirai, na nafsi yake ina hamu; ndiyo, hata hivyo ndivyo utakavyokuwa umati wa mataifa yote yapiganayo dhidi ya Mlima Sayuni.

4 Kwani tazama, nyote mnaotenda maovu, kaeni mlipo na mstaajabu, kwani mtalia, na kulia; ndiyo, mtalewa lakini sio kwa mvinyo, mtayumbayumba lakini sio kwa pombe kali.

5 Kwani tazama, Bwana amewamwagia roho ya usingizi. Kwani tazama, mmefunga macho yenu, na mmewakataa manabii; na watawala wenu, na waonaji amewafunika kwa sababu ya uovu wenu.

6 Na itakuwa kwamba Bwana Mungu atawaletea [a]ninyi maneno ya [b]kitabu, na yatakuwa maneno ya waliokufa.

7 Na tazama, hicho kitabu kitakuwa kimetiwa [a]muhuri; na katika kitabu hicho patakuwa na [b]ufunuo kutoka kwa Mungu, tangu mwanzo wa dunia hadi [c]mwisho wake.

8 Kwa hivyo, kwa sababu ya vitu ambavyo vimetiwa [a]muhuri, vitu viliyotiwa muhuri [b]havitatolewa katika siku za uovu na machukizo ya watu. Kwa hivyo kitabu hicho kitawekwa mbali nao.

9 Lakini kitabu hicho atapewa [a]mtu, na atapewa maneno ya kitabu hicho, ambayo ni maneno ya wafu walio mavumbini, na atatoa maneno haya kwa [b]mwingine;

10 Lakini maneno yaliyotiwa muhuri hatatoa, wala hatatoa hicho kitabu. Kwani kitabu hicho kitatiwa muhuri kwa nguvu za Mungu, na ufunuo uliotiwa muhuri utawekwa kitabuni humo hadi wakati mkamilifu wa Bwana utimie, kwamba yajulikane; kwani tazama, yana-

27 1 *a* mwm Siku za Mwisho.
2 *a* Isa. 24:6; 66:15–16; Yak. (KM) 6:3; 3 Ne. 25:1.
3 *a* Isa. 29:7–8.
b 1 Ne. 22:14.
6 *a* Yar. 1:2; Morm. 5:12–13.
b 2 Ne. 26:16–17; 29:12. mwm Kitabu cha Mormoni.
7 *a* Isa. 29:11–12; Eth. 3:25–27; 4:4–7.
b Mos. 8:19.
c Eth. 13:1–12.
8 *a* Eth. 5:1.
b 3 Ne. 26:9–12; Eth. 4:5–6.
9 *a* M&M 17:5–6.
b JS—H 1:64–65.

funua vitu vyote tangu msingi wa ulimwengu hadi mwisho wake.

11 Na siku inafika ambapo yale maneno ya kile kitabu yaliyotiwa muhuri yatasomwa kutoka juu ya nyumba; na yatasomwa kwa uwezo wa Kristo; na vitu vyote [a]vitafunuliwa watoto wa watu vile vilivyokuwa miongoni mwa watoto wa watu, na vile vitakavyokuwa hata hadi mwisho wa dunia.

12 Kwa hivyo, katika siku ile ambayo hicho kitabu kitatolewa kwa yule mtu ambaye nimemtaja, kitabu hicho kitafichwa kutokana na macho ya ulimwengu, kwamba hakuna macho yoyote yatakayokiona ila tu [a]mashahidi [b]watatu watakiona, kwa nguvu za Mungu, na kwa yule ambaye atapewa kitabu hicho; na watashuhudia ukweli wa kitabu hicho na kwa vitu vilivyomo.

13 Na hakuna yeyote atakayekiona, ila tu wachache kulingana na nia ya Mungu, kushuhudia kuhusu neno lake kwa watoto wa watu; kwani Bwana Mungu amesema kwamba maneno ya waaminifu yatanena ni kama [a]kutoka kwa wafu.

14 Kwa hivyo, Bwana Mungu ataendelea kutoa maneno ya kitabu hicho; na kwa vinywa vya mashahidi wengi kama apendavyo ataimarisha neno lake; na ole ni kwa yule [a]anayekataa neno la Mungu!

15 Lakini tazama, itakuwa kwamba Bwana Mungu atamwambia yule aliyempa hicho kitabu: Chukua maneno haya ambayo hayajawekwa muhuri na umpatie mwingine, ili amwonyeshe aliyeelimika, akisema: [a]Soma hii, nakusihi. Na aliyeelimika atasema: Leta hapa kitabu, na nitayasoma.

16 Na sasa, kwa sababu ya utukufu wa ulimwengu na kupata [a]faida watasema haya, na sio kwa utukufu wa Mungu.

17 Na yule mtu atasema: Siwezi kuleta hicho kitabu, kwani kimetiwa muhuri.

18 Kisha aliyeelimika atasema: Siwezi kukisoma.

19 Kwa hivyo itakuwa kwamba, Bwana Mungu atatoa tena kitabu hicho na maneno haya kwa yule asiye elimika; na yule mtu asiye elimika atasema: Mimi sina elimu.

20 Kisha Bwana Mungu atamwambia: Walioelimika hawatayasoma, kwani wameyakataa, na ninaweza kufanya kazi yangu mwenyewe; kwa hivyo wewe utasoma yale maneno nitakayokupatia.

21 [a]Usiguse vitu vilivyotiwa muhuri, kwani nitavitoa katika wakati wangu mkamilifu; kwani nitawaonyesha watoto wa watu kwamba ninaweza

11*a* Lk. 12:3; Morm. 5:8; M&M 121:26–31.
12*a* Kum. 19:15.
b 2 Ne. 11:3; Eth. 5:2–4; M&M 5:11, 15; 17:1.
13*a* 2 Ne. 3:19–20; 33:13–15; Moro. 10:27.
14*a* 2 Ne. 28:29–30; Eth. 4:8.
15*a* Isa. 29:11–12; JS—H 1:65.
16*a* MWM Ukuhani wa uongo.
21*a* Eth. 5:1.

kufanya kazi yangu mwenyewe.

22 Kwa hivyo, ukishamaliza kusoma maneno yale niliyokuamuru, na kupata wale [a]mashahidi ambao nilikuahidi, basi utakitia kile kitabu muhuri tena, na kukificha kwangu, ili niyahifadhi maneno ambayo hujasoma, hadi nitakapotaka katika hekima yangu kuwafunulia watoto wa watu mambo yote.

23 Kwani tazama, mimi ni Mungu; na mimi ni Mungu wa [a]miujiza; na nitauonyesha ulimwengu kwamba Mimi [b]ndimi yule jana, leo, na milele; na kwamba mimi sitendi lolote miongoni mwa watoto wa watu ila tu [c]kulingana na imani yao.

24 Na tena itakuwa kwamba Bwana atamwambia yule atakayesoma yale maneno atakayopewa:

25 [a]Kwa sababu watu hawa wananikaribia kwa kinywa chao, na kwa midomo yao [b]wananisifu, lakini mioyo yao iko mbali nami, na hofu yao kwangu mimi inafundishwa kwa [c]njia ya wanadamu—

26 Kwa hivyo, nitaendelea kufanya kazi ya [a]kushangaza miongoni mwa watu hawa, ndiyo, kazi ya [b]kushangaza na ya maajabu, kwani hekima ya walio werevu na wenye elimu itaangamia, na ufahamu wa wapiga ramli wao utafichwa.

27 Na [a]ole kwa wale wanaojaribu kumficha Bwana mashauri yao! Na matendo yao yako gizani; na wanasema: Nani anayetuona, na nani anayetujua? Na pia wanasema: Kwa hakika, upinduzi wako wa vitu juu chini utahesabiwa kama udongo wa [b]mfinyanzi. Lakini tazama, nitawaonyesha, asema Bwana wa Majeshi, kwamba najua matendo yao yote. Kwani kitu kitamwambia aliyekiunda, kwamba hakuniunda? Au kitu kilichojengwa kitamwambia mjenzi, hakuwa na ufahamu?

28 Lakini tazama, asema Bwana wa Majeshi: Nitaonyesha watoto wa watu kwamba ni muda kidogo uliobaki kwamba Lebanoni itageuzwa kuwa shamba lizaalo; na shamba lizaalo litakuwa kama msitu.

29 [a]Na katika siku ile viziwi watasikia maneno ya kitabu, na macho ya vipofu yataona kutoka fumboni na giza.

30 Na [a]wapole pia nao wataongezeka, na [b]shangwe yao itakuwa katika Bwana, na walio masikini miongoni mwa wanadamu watashangilia katika yule Mtakatifu wa Israeli.

31 Kwa hakika jinsi Bwana aishivyo wataona kwamba yule ambaye [a]hutisha atakuwa bure,

22*a* MWM Mashahidi wa Kitabu cha Mormoni.
23*a* MWM Muujiza.
b Ebr. 13:8.
c Ebr. 11; Eth. 12:7–22.
25*a* Isa. 29:13.
b Mt. 15:8.
c 2 Ne. 28:31.
26*a* 1 Ne. 22:8; 2 Ne. 29:1–2. MWM Urejesho wa Injili.
b Isa. 29:14; 2 Ne. 25:17.
27*a* Isa. 29:15.
b Yer. 18:6.
29*a* Isa. 29:18.
30*a* MWM Pole, Upole.
b M&M 101:36.
31*a* Isa. 29:20.

na mwenye kudharau ameangamizwa, na kwamba wale wote wanaotafuta uovu wanatengwa;

32 Na wale [a]wanaomkosesha mtu kwa neno, na kumtegea mtego yule anayekemea [b]langoni, na [c]kumkataa mwenye haki kwa kitu kisichofaa.

33 Kwa hivyo, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, aliyemkomboa Ibrahimu, kuhusu nyumba ya Yakobo: Sasa Yakobo hataaibika, wala uso wake kugeuka rangi uwe mweupe.

34 Lakini [a]atakapoona watoto wake, ambao ni kazi ya mikono yangu, kati yake, watatakasa jina langu, na kumtakasa yule Mtakatifu wa Yakobo, na watamheshimu Mungu wa Israeli.

35 Wale nao pia [a]waliokosea katika roho watafahamu, na wale walionung'unika [b]watajifunza mafundisho ya dini.

MLANGO WA 28

Makanisa mengi ya bandia yatajengwa katika siku za mwisho—Yatafundisha mafundisho ya uwongo, yasiyofaidi, na ya kipumbavu—Ukengeufu utaendelea kwa sababu ya walimu wa bandia—Ibilisi atavuma katika mioyo ya wanadamu—Atafundisha kila aina ya mafundisho ya uwongo. Karibia mwaka 559–545 K.K.

28 Na sasa, tazameni, ndugu zangu, nimewazungumzia, kulingana na vile Roho ameniongoza; kwa hivyo, najua kwamba kwa kweli lazima yatimizwe.

2 Na vitu ambavyo vitaandikwa kutoka kwenye [a]kitabu hicho vitakuwa vya [b]dhamana kuu kwa watoto wa watu, na hasa kwa uzao wetu, ambayo ni baki la nyumba ya Israeli.

3 Kwani itakuwa kwamba katika siku ile [a]makanisa ambayo yamejengwa, na siyo kwa Bwana, wakati mmoja italiambia nyingine: Tazama, Mimi, Mimi ni wa Bwana; na jingine litasema: Mimi, Mimi ni wa Bwana; na kila mmoja aliyejenga makanisa, yasiyo ya Bwana atasema hivyo—

4 Na watabishana mmoja na mwingine; na makuhani wao watabishana mmoja na mwingine, na watafundisha kulingana na [a]elimu yao, na watamkana Roho Mtakatifu, anayetoa maneno.

5 Na [a]wanakana [b]nguvu za Mungu, yule Mtakatifu wa Israeli; na kuwaambia watu: Tusikilizeni sisi, na sikiliza mawaidha yetu; kwani tazama [c]hakuna Mungu leo, kwani Bwana na Mkombozi ametenda kazi yake, na amewapatia wanadamu uwezo wake;

6 Tazameni, sikilizeni mawaidha yangu; kama watasema

32*a* Lk. 11:54.
b Amo. 5:10.
c 2 Ne. 28:16.
34*a* Isa. 29:23–24.
35*a* 2 Ne. 28:14; M&M 33:4.
b Dan. 12:4.

28 2*a* MWM Kitabu cha Mormoni.
b 1 Ne. 13:34–42; 22:9; 3 Ne. 21:6.
3*a* 1 Kor. 1:10–13; 1 Ne. 22:23; 4 Ne. 1:25–29; Morm. 8:28, 32–38.
4*a* 2 Ne. 9:28.
5*a* 2 Ne. 26:20.
b 2 Tim. 3:5.
c Alma 30:28.

kuna muujiza uliotendwa kwa mkono wa Bwana, msiamini; kwani leo yeye sio Mungu wa [a]miujiza; ametenda kazi yake.

7 Ndiyo, na kutakuwa na wengi ambao watasema: [a]Kuleni, kunyweni, na mshangilie, kwani kesho tutakufa; na sisi tutakuwa salama.

8 Na kutakuwa pia na wengi ambao watasema: Kuleni, kunyweni na mshangilie; walakini, mwogopeni Mungu—[a]ataturuhusu kutenda dhambi kidogo; ndiyo, [b]danganya kidogo, tumieni wengine kwa sababu ya maneno yao, mchimbie jirani yako [c]shimo; hakuna hatia kwa haya; na mtende vitu hivi vyote, kwani kesho tutakufa, na kama tutakuwa na hatia, Mungu atatuadhibu kwa mijeledi michache, na mwishowe tutaokolewa katika ufalme wa Mungu.

9 Ndiyo, na kutakuwa na wengi watakaofundisha kwa namna hii, uwongo na yasiyofaa na [a]mafundisho ya [b]kipumbavu, na watajifurisha mioyoni mwao, na watajitahidi kumfichia Bwana mashauri yao; na matendo yao yatakuwa gizani.

10 Na [a]damu ya watakatifu italia kutoka chini dhidi yao.

11 Ndiyo, wote wamepotea [a]njia; [b]wameharibika.

12 Kwa sababu ya [a]kiburi, na kwa sababu ya walimu bandia, na mafundisho ya bandia, makanisa yao yameharibika, na makanisa yao yamejiinua; kwa sababu ya kiburi yamefura.

13 [a]Wanawapora [b]maskini kwa sababu ya makutaniko yao mazuri; wanawapora maskini kwa sababu ya mavazi yao mazuri; na kuwatesa walio wapole na maskini katika moyo, kwa sababu katika [c]kiburi chao wamefura.

14 [a]Wanakaza shingo zao na kufanya vichwa vyao kuwa na kiburi; ndiyo, na kwa sababu ya kiburi, na uovu, na machukizo, na uasherati, wote [b]wamepotea ila tu wachache, ambao ni wafuasi wanyenyekevu wa Kristo; walakini, wanaongozwa, na inakuwa kwamba katika wakati mwingi wanakosea kwa sababu wanafundishwa kwa mawaidha ya wanadamu.

15 Ee wenye [a]hekima, na walioelimika, na matajiri, ambao wanajivuna kwa [b]kiburi cha roho zao, na wale wote wanaofundisha mafundisho ya bandia, na wale wote wanaofanya uasherati, na kupindua njia zilizo sawa za Bwana, [c]ole, ole, ole ni kwao, asema Bwana Mungu Mwenyezi, kwani watatupwa jehanamu!

6*a* Morm. 8:26; 9:15–26.
7*a* 1 Kor. 15:32; Alma 30:17–18.
8*a* Morm. 8:31.
b M&M 10:25; Musa 4:4. MWM Kusema uongo.
c Mit. 26:27; 1 Ne. 14:3.
9*a* Mt. 15:9.
b Eze. 13:3; Hel. 13:29.
10*a* Ufu. 6:9–11; 2 Ne. 26:3; Morm. 8:27; Eth. 8:22–24; M&M 87:7.
11*a* Hel. 6:31.
b Morm. 8:28–41; M&M 33:4.
12*a* Mit. 28:25.
13*a* Eze. 34:8.
b Hel. 4:12.
c Alma 5:53.
14*a* Mit. 21:4.
b Isa. 53:6.
15*a* Mit. 3:5–7.
b MWM Kiburi.
c 3 Ne. 29:5.

16 Ole kwa wale [a]wanaokataa la haki kwa kitu kisichofaa na kushutumu kilicho chema, na kusema kwamba hakina thamani! Kwani siku inafika ambapo Bwana Mungu ataadhibu wakazi wa dunia kwa haraka; na katika siku ile ambayo watakuwa wameiva [b]kabisa katika maovu wataangamia.

17 Lakini tazama, kama wakazi wa dunia watatubu uovu wao na machukizo hawataangamizwa, asema Bwana wa Majeshi.

18 Lakini tazama, kanisa lile kuu la machukizo, yule [a]kahaba wa ulimwengu wote, lazima [b]aporomoke duniani, na kubwa utakuwa muanguko wake.

19 Kwani ufalme wa ibilisi lazima [a]utetemeke, na wale ambao ni wake lazima wavurugwe hadi watubu, au [b]ibilisi atawafunga kwa [c]minyororo yake isiyo na mwisho, na wavurugwe, kwa hasira na waangamie.

20 Kwani tazama, katika siku ile [a]atavuma mioyoni mwa watoto wa watu, na awavuruge wakasirikie yale ambayo ni mema.

21 Na wengine [a]atawapatanisha, na awapatie usalama wa kimwili, kwamba watasema: Yote yako salama Sayuni; ndiyo, Sayuni inafanikiwa, yote ni mema—na hivyo [b]ibilisi anadanganya roho zao, na kuwapeleka kwa makini hadi jehanamu.

22 Na tazama, wengine atawadanganya, na kuwaambia kwamba hakuna [a]jehanamu; na kuwaambia: Mimi sio ibilisi, kwani hakuna yeyote—na anawanong'onezea hivyo masikioni mwao, hadi awashike na [b]minyororo yake miovu, kutoka ambapo hakuna ukombozi.

23 Ndiyo, wamefungwa na mauti, na jehanamu; na mauti, na jehanamu, na ibilisi, na wale wote ambao wameshikwa na hao lazima watasimama mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, na [a]wahukumiwe kulingana na matendo yao, na kutoka hapo lazima waende mahali walipotayarishiwa, hata kwenye [b]ziwa la moto na kiberiti, ambayo ni mateso yasiyo na mwisho.

24 Kwa hivyo, ole kwa yule anayestarehe Sayuni!

25 Ole kwa yule anayetangaza: Yote yako salama!

26 Ndiyo, ole kwa yule [a]anayetii mawaidha ya wanadamu, na kukana nguvu za Mungu, na kipawa cha Roho Mtakatifu!

27 Ndiyo, ole kwa yule anayesema: Tumepokea, na [a]hatuhitaji zaidi!

28 Na mwishowe, ole kwa wale wote wanaotetemeka, na [a]wanakasirika kwa sababu ya

16 *a* Isa. 29:21.
b Eth. 2:9–10.
18 *a* Ufu. 19:2.
b 1 Ne. 14:3, 17.
19 *a* 1 Ne. 22:23.
b Alma 34:35.
c Alma 12:11.
20 *a* M&M 10:20–27.
21 *a* Morm. 8:31.
b 2 Ne. 9:39.
22 *a* MWM Jehanamu.
b Alma 36:18.
23 *a* MWM Hukumu ya mwisho; Yesu Kristo—Mwamuzi.
b 2 Ne. 9:16, 19, 26.
26 *a* 2 Ne. 9:29.
27 *a* Alma 12:10–11.
28 *a* 2 Ne. 9:40; 33:5.
MWM Uasi.

ukweli wa Mungu! Kwani tazama, yule ambaye amejengwa katika [b]mwamba huyapokea kwa furaha; na yule aliyejengwa kwenye msingi wa mchanga hutetemeka asije akaanguka.

29 Ole kwa yule atakayesema: Tumepokea neno la Mungu, na [a]hatuhitaji [b]mengine zaidi ya maneno ya Mungu, kwani tuna ya kutosha!

30 Kwani tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu: Nitawapatia watoto wa watu mstari juu ya mstari, [a]amri juu ya amri, hapa kidogo na pale kidogo; na heri wale wanaosikiliza kanuni zangu, na kutegea sikio mashauri yangu, kwani watajifunza [b]hekima; kwani kwa yule ambaye [c]hupokea nitampatia [d]zaidi; na kutoka kwa wale watakaosema, Tuna ya kutosha, watapokonywa hata kile walichonacho.

31 Amelaaniwa yule ambaye anaweka [a]imani yake kwa mwanadamu, au amfanyaye kuwa mkono wake, au kusikiliza kanuni za wanadamu, isipokuwa kanuni zao zitolewe na nguvu ya Roho Mtakatifu.

32 [a]Ole kwa Wayunani, asema Bwana Mungu wa Majeshi! Ingawa nitawanyoshea [b]mkono wangu siku kwa siku, watanikana; walakini, nitawarehemu, asema Bwana Mungu, kama watatubu na kunijia mimi; kwani mkono wangu umenyooshwa siku yote, asema Bwana Mungu wa Majeshi.

MLANGO WA 29

Wayunani wengi watakataa Kitabu cha Mormoni—Watasema, Hatuhitaji Biblia zaidi—Bwana huzungumzia mataifa mengi—Atahukumu ulimwengu kutoka vitabu vitakavyoandikwa. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Lakini tazama, kutakuwa na wengi—katika siku ile ambayo nitaanza kutenda kazi ya [a]maajabu miongoni mwao, kwamba nikumbuke [b]maagano yangu ambayo nilifanya na watoto wa watu, kwamba ninyooshe mkono wangu tena mara ya [c]pili kurudisha watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli.

2 Na pia, ili nikumbuke ahadi nilizokuahidi wewe, Nefi, na pia kwa baba yako, kwamba nitakumbuka uzao wako; na kwamba [a]maneno ya uzao wako utatoka kinywani mwangu hadi kwa uzao wako; na maneno yangu yatapigwa [b]miunzi hadi mwisho wa dunia, kwani itakuwa [c]bendera kwa

28 *b* Mt. 7:24–27.
MWM Mwamba.
29 *a* 2 Ne. 29:3–10.
b 2 Ne. 27:14; Eth. 4:8.
30 *a* Isa. 28:9–13; M&M 98:12.
b MWM Hekima.
c Lk. 8:18.
d Alma 12:10; M&M 50:24.
31 *a* M&M 1:19–20.
32 *a* 1 Ne. 14:6.
b Yak. (KM) 5:47; 6:4.
29 1 *a* 2 Ne. 27:26.
MWM Urejesho wa Injili.
b MWM Agano la Ibrahimu.
c 2 Ne. 6:14; 21:11–12; 25:17.
MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
2 *a* 2 Ne. 3:18–21.
b Isa. 5:26; 2 Ne. 15:26; Moro. 10:28.
c 1 Ne. 21:22.
MWM Bendera.

watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli.

3 Na kwa sababu maneno yangu yatapigwa miunzi mbele—Wayunani wengi watasema: [a]Biblia! Biblia! Tunayo Biblia, na hakuwezi kuwako na Biblia nyingine.

4 Lakini hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu: Enyi wajinga, watapata Biblia; na itatoka kwa [a]Wayahudi, watu wangu wa kale wa maagano. Na shukrani gani wameitoa ya nini kwa Wayahudi kwa ajili ya ile [b]Biblia waliyoipokea kutoka kwao? Ndiyo, Wayunani wanamaanisha nini? Je, wanakumbuka machungu, na mateso, na maumivu ya Wayahudi, na bidii yao kwangu mimi, katika kuwaletea Wayunani wokovu?

5 Ee ninyi Wayunani, je, mmekumbuka Wayahudi, watu wangu wa kale wa maagano? Hapana; lakini mmewalaani, na [a]kuwachukia, na hamkutaka kuwarudisha. Lakini tazama, nitarudisha vitu hivi vyote juu ya vichwa vyenu wenyewe; kwani mimi Bwana sijasahau watu wangu.

6 Ewe mjinga, utakayesema: [a]Biblia, tunayo Biblia, na hatuhitaji Biblia nyingine. Je, umepokea Biblia isipokuwa kwa Wayahudi?

7 Je, hujui kwamba kuna mataifa mengi zaidi ya moja? Je, hujui kwamba Mimi, Bwana Mungu wako, [a]nimeumba wanadamu wote, na kwamba nawakumbuka wale ambao wako katika [b]visiwa vya bahari; na kwamba ninatawala juu mbinguni na chini duniani; na kwamba nitaleta mbele neno langu kwa watoto wa watu, ndiyo, hata katika mataifa yote ya ulimwengu?

8 Kwa hivyo unanung'unika, kwa sababu mtapokea maneno yangu zaidi? Je, hamjui kwamba ushuhuda wa mataifa [a]mawili ni [b]ushahidi kwenu kwamba mimi ni Mungu, na kwamba nakumbuka taifa moja kama lingine? Kwa hivyo, nazungumzia taifa moja maneno sawa na lingine. Na wakati [c]mataifa mawili yatakapoishi pamoja ushuhuda wa hayo mataifa mawili utaenda pia pamoja.

9 Ninafanya haya ili niwathibitishie wengi kwamba Mimi ndimi [a]yule yule jana, leo, na milele; na kwamba ninazungumza maneno yangu nipendavyo. Na kwa sababu nimenena [b]neno moja hamna haja kudhani kwamba siwezi kunena lingine; kwani kazi yangu bado haijakamilika; wala haitakamilika hadi mwisho wa mwanadamu, wala kutoka wakati huo hadi milele.

3 *a* 1 Ne. 13:23–25. MWM Biblia; Kitabu cha Mormoni.
4 *a* M&M 3:16. MWM Wayahudi.
b MWM Yuda—Kijiti cha Yuda.
5 *a* 3 Ne. 29:8.
6 *a* 1 Ne. 13:38.
7 *a* MWM Umba, Uumbaji.
b 1 Ne. 22:4.
8 *a* Eze. 37:15–20; 1 Ne. 13:38–41; 2 Ne. 3:12.
b Mt. 18:16. MWM Shahidi, Ushahidi.
c Hos. 1:11.
9 *a* Ebr. 13:8.
b MWM Ufunuo.

10 Kwa hivyo, kwa sababu mna Biblia msidhani kwamba inayo [a]maneno yangu yote; wala hamna haja kudhani kwamba sijasababisha mengine kuandikwa.

11 Kwani ninawaamuru wanadamu [a]wote, kutoka mashariki na magharibi, na kaskazini, na kusini, na katika visiwa vya bahari, kwamba [b]wataandika maneno ambayo nitawazungumzia; kwani kutoka kwa [c]vitabu ambavyo vitaandikwa [d]nitahukumu ulimwengu, kila mwanadamu kulingana na matendo yake, kulingana na yale yaliyoandikwa.

12 Kwani tazama, nitawazungumzia [a]Wayahudi na wataiandika; na pia nitawazungumzia Wanefi na [b]wataiandika; na pia nitazungumzia makabila mengine ya nyumba ya Israeli, ambayo nimeyaongoza mbali, na wataiandika; na pia nitazungumzia mataifa [c]yote ya dunia na wataiandika.

13 Na itakuwa kwamba [a]Wayahudi watapokea maneno ya Wanefi, na Wanefi watapokea maneno ya Wayahudi; na Wanefi na Wayahudi watapokea maneno ya makabila ya Israeli [b]yaliyopotea; na makabila ya Israeli yaliyopotea yatapokea maneno ya Wanefi na Wayahudi.

14 Na itakuwa kwamba watu wangu, ambao ni wa [a]nyumba ya Israeli, watakusanywa nyumbani katika nchi zao za kumiliki; na pia neno langu litakusanywa [b]pamoja. Na nitawaonyesha wale ambao wanapigana dhidi ya neno langu na dhidi ya watu wangu, ambao ni wa [c]nyumba ya Israeli, kwamba mimi ni Mungu, na kwamba [d]niliagana na Ibrahimu kwamba nitakumbuka [e]uzao wake [f]milele.

MLANGO WA 30

Wayunani walioongoka watahesabika kuwa watu wa maagano—Walamani wengi na Wayahudi wataliamini neno na kuwa wema—Israeli itarudishwa na walio waovu kuangamizwa. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na sasa tazama, ndugu zangu wapendwa, nitawazungumzia; kwani mimi, Nefi, sitakubali kwamba ninyi mdhani kuwa ninyi ni watakatifu zaidi ya vile Wayunani watakavyokuwa. Kwani tazameni, msipotii amri za Mungu wote mtaangamia pia; na kwa sababu ya maneno ambayo yamezungumzwa

10 *a* MWM Maandiko—Maandiko yaliyotolewa unabii kwamba yatakuja.
11 *a* Alma 29:8.
b 2 Tim. 3:16.
c MWM Kitabu cha Uzima.
d 2 Ne. 25:22; 33:11, 14–15.
MWM Hukumu ya mwisho.
12 *a* 1 Ne. 13:23–29.
b 1 Ne. 13:38–42; 2 Ne. 26:17.
c 2 Ne. 26:33.
13 *a* Morm. 5:12–14.
b MWM Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea.
14 *a* Yer. 3:17–18.
b Eze. 37:16–17.
c 1 Ne. 22:8–9.
d Mwa. 12:1–3; 1 Ne. 17:40; 3 Ne. 20:27; Ibr. 2:9.
MWM Agano la Ibrahimu.
e M&M 132:30.
f Mwa. 17:7.

msidhani kwamba Wayunani wameangamizwa kabisa.

2 Kwani tazama, nawaambia kwamba kadiri Wayunani watakavyotubu wao wanakuwa watu wa [a]maagano wa Bwana; na kadiri wengi [b]Wayahudi wasivyotubu watatengwa; kwani Bwana haagani na yeyote ila tu wale [c]wanaotubu na kumwamini Mwana wake, ambaye ndiye Mtakatifu wa Israeli.

3 Na sasa, nitatoa unabii mchache zaidi kuhusu Wayahudi na Wayunani. Kwani baada ya kitabu kile nilichokizungumzia kutokea, na kuandikiwa Wayunani, na kutiwa muhuri tena katika Bwana, kutakuwa na wengi ambao [a]wataamini maneno yaliyoandikwa; na [b]wao watayapelekea baki la uzao wetu.

4 Na kisha baki la uzao wetu litajua kutuhusu, vile tulivyotoka Yerusalemu, na kwamba wao ni ukoo wa Wayahudi.

5 Na injili ya Yesu Kristo itatangazwa miongoni [a]mwao; kwa hivyo, [b]wao watarejeshwa tena kwa ufahamu wa baba zao, na pia kwa [c]ufahamu wa Yesu Kristo, ambao ulikuwa miongoni mwa baba zao.

6 Na kisha watashangilia; kwani watajua kwamba ni baraka kwao kutoka mkono wa Mungu; na magamba yao ya giza yataanza kuanguka kutoka macho yao; na vizazi vingi havitapita miongoni mwao, ila tu watakuwa safi na watu [a]wema.

7 Na itakuwa kwamba [a]Wayahudi waliotawanyika [b]wataanza kumwamini Kristo; na wataanza kukusanyika katika uso wa nchi; na kadiri wengi watakavyomwamini Kristo pia nao watakuwa watu wema.

8 Na itakuwa kwamba Bwana Mungu ataanza kazi yake miongoni mwa mataifa yote, makabila, lugha, na watu, kuleta marejesho ya watu wake katika dunia.

9 Na kwa haki [a]Bwana Mungu [b]atawahukumu maskini, na kuwakemea kwa kiasi kwa walio [c]wapole duniani. Na ataipiga dunia kwa fimbo ya kinywa chake; na kwa pumzi ya midomo yake atawaua walio waovu.

10 Kwani [a]wakati unafika upesi ambapo Bwana Mungu atasababisha [b]mgawanyiko mkuu miongoni mwa watu, na ataangamiza waovu; na [c]atawahurumia watu wake, ndiyo, hata kama lazima [d]aangamize waovu kwa moto.

11 Na [a]haki itakuwa mshipi

30 2*a* Gal. 3:26–29.
b Mt. 8:10–13.
MWM Wayahudi.
c MWM Toba, Tubu.
3*a* 3 Ne. 16:6–7.
b 1 Ne. 22:8–9.
5*a* 3 Ne. 21:3–7, 24–26.
b M&M 3:20.
c 1 Ne. 15:14; 2 Ne. 3:12; Morm. 7:1, 9–10.
6*a* M&M 49:24; 109:65.
7*a* 2 Ne. 29:13–14.
b 2 Ne. 25:16–17.
9*a* Isa. 11:4–9.
b 2 Ne. 9:15.
c MWM Pole, Upole.
10*a* MWM Siku za Mwisho.
b M&M 63:53–54.
c Musa 7:61.
d 1 Ne. 22:15–17, 23.
MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
11*a* Isa. 11:5–9.

wa viuno vyake, na uaminifu utakuwa mshipi wa mafigo yake.

12 [a]Na kisha mbwa mwitu ataishi na mwanakondoo; na chui atalala na mwanambuzi, na ndama, na mwana-simba, na kinono, pamoja; na mtoto mdogo atawaongoza.

13 Na ng'ombe na dubu watakula; na watoto wao watalala pamoja; na simba atakula majani kama ng'ombe.

14 Na mtoto anayenyonya atachezea katika tundu la nyoka sumu, na mtoto aliyeachishwa atatia mkono wake kwenye pango la fira.

15 Hawatadhuru wala kuharibu katika mlima wangu wote mtakatifu; maana dunia itajawa na ufahamu wa Bwana kama vile maji yanavyofunika baharini.

16 Kwa hivyo, vitu vya mataifa [a]yote [b]vitajulikana; ndiyo, vitu vyote vitajulikana na watoto wa watu.

17 Hakuna jambo ambalo ni la siri ambalo [a]halitafunuliwa; hakuna kazi ya giza ambayo haitafunuliwa katika nuru; na hakuna jambo lolote ambalo limetiwa muhuri duniani ambalo halitafunguliwa.

18 Kwa hivyo, vitu vyote ambavyo vimewahi kufunuliwa watoto wa watu katika siku ile vitafunuliwa; na Shetani [a]hatakuwa na nguvu juu ya mioyo ya watoto wa watu tena, kwa muda mrefu. Na sasa, ndugu zangu wapendwa, namalizia maneno yangu hapo.

MLANGO WA 31

Nefi anaeleza ni kwa nini Kristo alibatizwa—Wanadamu lazima wamfuate Kristo, wabatizwe, wampokee Roho Mtakatifu, na wavumilie hadi mwisho ili waokolewe—Toba na ubatizo ndiyo lango la kuingia katika njia ile nyembamba na iliyosonga—Uzima wa milele huja kwa wale wanaotii zile amri baada ya ubatizo. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na sasa mimi, Nefi, namaliza kuwatolea [a]unabii, ndugu zangu wapendwa. Na siwezi kuandika isipokuwa tu vitu vichache, ambavyo najua kwa hakika lazima vitatimia; wala siwezi kuandika isipokuwa tu maneno machache ya kaka yangu Yakobo.

2 Kwa hivyo, vitu ambavyo nimeandika vimenitosha, ila tu maneno machache ambayo lazima niyazungumze kuhusu [a]mafundisho ya Kristo; kwa hivyo, nitawazungumzia kwa uwazi, kulingana na unyofu wangu ninapotoa unabii.

3 Kwani nafsi yangu inafurahia unyoofu; kwani kwa namna hii ndivyo Bwana Mungu anavyotenda kazi miongoni mwa wanadamu. Kwani Bwana Mungu hutoa [a]nuru kwa ufahamu; kwani huzungumza na

12*a* Isa. 65:25. MWM Milenia.
16*a* M&M 101:32–35; 121:28–29.
b Eth. 4:6–7.
17*a* M&M 1:2–3.
18*a* Ufu. 20:1–3; Eth. 8:26.
31 1*a* 2 Ne. 25:1–4.
2*a* 2 Ne. 11:6–7.
3*a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.

wanadamu kulingana na [b]lugha yao, kwa ufahamu wao.

4 Kwa hivyo, ningependa mkumbuke kwamba nimewahi kuwazungumzia kuhusu yule [a]nabii ambaye Bwana alinionyesha, kwamba atambatiza [b]Mwanakondoo wa Mungu, ambaye ataondoa dhambi za ulimwengu.

5 Na sasa, kama Mwanakondoo wa Mungu, akiwa mtakatifu, alihitaji [a]kubatizwa kwa maji, ili kutimiza haki yote, Ee basi, jinsi gani tunahitaji zaidi sisi, tusio watakatifu, kubatizwa, ndiyo, hata kwa maji!

6 Na sasa, ningewauliza ninyi, ndugu zangu wapendwa, ni vipi Mwanakondoo wa Mungu alitimiza haki yote alipobatizwa kwa maji?

7 Je, hamjui kwamba alikuwa mtakatifu? Lakini ingawa alikuwa mtakatifu, anawaonyesha watoto wa watu kwamba, kulingana na mwili anajinyenyekeza mbele ya Baba, na kumshuhudia Baba kwamba yeye atakuwa [a]mwaminifu kwake katika kutii amri zake.

8 Kwa hivyo, baada ya kubatizwa kwa maji Roho Mtakatifu alimshukia katika [a]umbo la [b]njiwa.

9 Na tena, inaonyesha watoto wa watu unyofu wa njia, na wembamba wa [a]lango, ambalo wataliingilia, baada ya yeye kuwatolea mfano.

10 Na akawaambia watoto wa watu: [a]Nifuateni mimi. Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, je, tunaweza [b]kumfuata Yesu tusipokubali kushika amri za Baba?

11 Na Baba alisema: Tubuni, tubuni, na mbatizwe katika jina la Mwana wangu Mpendwa.

12 Na pia, sauti ya Mwana ilinijia, ikisema: Yule anayebatizwa katika jina langu, [a]atapewa Roho Mtakatifu na Baba, kama mimi; kwa hivyo, [b]nifuateni, na mfanye vitu ambavyo mmeniona nikifanya.

13 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, najua kwamba kama mtamtii Mwana, kwa moyo wa lengo moja, bila unafiki na udanganyifu mbele yake Mungu, lakini kwa kusudi kamili, na kutubu dhambi zenu, mkishuhudia kwa Baba kwamba mnataka kujivika juu yenu jina la Kristo, kwa [a]ubatizo—ndiyo, kwa kumfuata Bwana wenu na Mwokozi wenu chini majini, kulingana na neno lake, tazameni, ndipo mtapokea Roho Mtakatifu; ndiyo, kisha [b]ubatizo wa moto na Roho Mtakatifu

3 *b* M&M 1:24.
4 *a* 1 Ne. 10:7; 11:27. MWM Yohana Mbatizaji.
b MWM Mwanakondoo wa Mungu.
5 *a* Mt. 3:11–17. MWM Batiza, Ubatizo.
7 *a* Yn. 5:30. MWM Mtiifu, Tii, Utii.
8 *a* 1 Ne. 11:27.
b MWM Njiwa, Ishara ya.
9 *a* 2 Ne. 9:41; 3 Ne. 14:13–14; M&M 22:4.
10 *a* Mt. 4:19; 8:22; 9:9.
b Moro. 7:11; M&M 56:2.
12 *a* MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
b Lk. 9:57–62; Yn. 12:26.
13 *a* Gal. 3:26–27.
b MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu; Moto.

unakuja; na kisha mtaweza kuzungumza kwa [c]lugha ya malaika, na kupiga kelele za sifa kwa yule Mtakatifu wa Israeli.

14 Lakini, tazama, ndugu zangu wapendwa, hivyo sauti ya Mwana ilinijia, ikisema: Baada ya kutubu dhambi zenu, na kushuhudia Baba kwamba mko tayari kutii amri zangu, kwa ubatizo wa maji, na kupokea ubatizo wa moto na wa Roho Mtakatifu, na kuzungumza kwa lugha mpya, ndiyo, hata lugha ya malaika, na baada ya haya [a]mnikane, ingekuwa [b]vyema kama hamkunifahamu.

15 Na nikasikia sauti kutoka kwa Baba, ikisema: Ndiyo, maneno ya Mpendwa wangu ni ya kweli na maaminifu. Yule atakayevumilia hadi mwisho, huyo ataokolewa.

16 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, najua kwamba bila ya mwanadamu [a]kuvumilia hadi mwisho, kwa kufuata [b]mfano wa Mwana wa Mungu aliye hai, hawezi kuokolewa.

17 Kwa hivyo, fanyeni vitu ambavyo nimewaambia nimeona kwamba Bwana wenu na Mkombozi wenu atatenda; kwani, nimeonyeshwa haya kwa lengo hili, ili mjue ni kwa lango gani mtakaloingilia. Kwani lango ambalo mtaingilia ni toba na [a]ubatizo kwa maji; na kisha unakuja [b]msamaha wa dhambi zenu kwa moto kwa Roho Mtakatifu.

18 Na kisha mnaingia katika [a]njia hii nyembamba [b]iliyosonga ambayo inaelekea uzima wa milele; ndiyo, mmeingia kwa hilo lango; mmetenda kulingana na amri za Baba na Mwana; na mmempokea Roho Mtakatifu, ambaye [c]anawashuhudia Baba na Mwana, katika kutimiza ahadi ambayo ametoa, kwamba mkiingia kwa njia mtapokea.

19 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, baada yenu kuingia katika njia hii nyembamba na iliyosonga, nauliza je, yote [a]yamekamilishwa? Tazama, nawaambia, Hapana; kwani hamjafika hapa ila tu kwa neno la Kristo na kwa [b]imani isiyotingishika ndani yake, [c]mkitegemea kabisa ustahili wa yule aliye mkuu kuokoa.

20 Kwa hivyo, lazima [a]msonge mbele mkiwa na imani imara katika Kristo, mkiwa na mng'aro mkamilifu wa [b]tumaini, na [c]upendo kwa Mungu na wanadamu wote. Kwa hivyo, kama mtasonga mbele, mkila na kusherekea neno la Kristo,

13 *c* 2 Ne. 32:2–3.
14 *a* Mt. 10:32–33; Alma 24:30; M&M 101:1–5. MWM Dhambi isiyo sameheka.
b 2 Pet. 2:21.
16 *a* Alma 5:13; 38:2; M&M 20:29.
b MWM Yesu Kristo—Mfano wa Yesu Kristo.
17 *a* Mos. 18:10. MWM Batiza, Ubatizo.
b MWM Ondoleo la Dhambi.
18 *a* Mit. 4:18. MWM Njia.
b 1 Ne. 8:20.
c Mdo. 5:29–32.
19 *a* Mos. 4:10.
b MWM Amini, Imani.
c M&M 3:20.
20 *a* MWM Tembea, Tembea na Mungu.
b MWM Tumaini.
c MWM Upendo.

na [d]mvumilie hadi mwisho, tazama, hivyo ndivyo asemavyo Baba: Mtapokea uzima wa milele.

21 Na sasa, tazama, ndugu zangu wapendwa, hii ndiyo [a]njia; na [b]hakuna [c]njia nyingine wala jina lililotolewa chini ya mbingu ambalo mwanadamu anaweza kuokolewa katika ufalme wa Mungu. Na sasa, tazama, hili ndilo [d]fundisho la Kristo, na fundisho pekee na la kweli la [e]Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu, ambao ni [f]Mungu mmoja, bila mwisho. Amina.

MLANGO WA 32

Malaika wanazungumza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu—Wanadamu lazima wasali na kupokea ufahamu kwa wao wenyewe kutoka kwa Roho Mtakatifu. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na sasa, tazama, ndugu zangu wapendwa, nadhani kwamba mnawaza machache mioyoni mwenu kuhusu yale mtakayotenda baada ya kuingia kwa njia hiyo. Lakini, tazama, kwa nini mnawaza vitu hivi mioyoni mwenu?

2 Je, hamkumbuki kwamba niliwaambia kwamba baada ya [a]kupokea Roho Mtakatifu mngezungumza kwa [b]lugha ya malaika? Na sasa, vipi mngezungumza kwa lugha ya malaika bila Roho Mtakatifu?

3 [a]Malaika wanazungumza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu; kwa hivyo, wanazungumza maneno ya Kristo. Kwa hivyo, niliwaambia, [b]shiriki maneno ya Kristo; kwani tazama, maneno ya Kristo yatawaelezea vitu vyote mnavyostahili kutenda.

4 Kwa hivyo, na sasa baada ya kuzungumza maneno haya, kama hamwezi kuyafahamu, ni kwa sababu [a]hamuombi, wala kubisha; kwa hivyo, hamjaletwa kwenye nuru, lakini lazima mwangamie gizani.

5 Kwani tazama, tena nawaambia kwamba kama mtaingia kwa njia hiyo, na kupokea Roho Mtakatifu, atawaonyesha vitu vyote ambavyo mnastahili kutenda.

6 Tazameni, haya ndiyo mafundisho ya Kristo, na hakutakuwa na mafundisho mengine yatakayotolewa hadi [a]atakapojidhihirisha kwenu katika mwili. Na atakapojithirihisha kwenu katika mwili, mtachunguza na kufanya vile vitu atakavyowaambia.

7 Na sasa mimi, Nefi, siwezi kuzungumza zaidi; Roho anayokomesha mazungumzo yangu, na ninaachwa kuo-

20 *d* MWM Stahimili.
21 *a* Mdo. 4:10–12; 2 Ne. 9:41; Alma 37:46; M&M 132:22, 25.
b Mos. 3:17.
c MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
d Mt. 7:28; Yn. 7:16–17.
e MWM Mungu, Uungu.
f 3 Ne. 11:27, 35–36. MWM Umoja.

32 2 *a* 3 Ne. 9:20.
b 2 Ne. 31:13.
3 *a* MWM Malaika.
b Yer. 15:16.
4 *a* MWM Omba.
6 *a* 3 Ne. 11:8.

mboleza kwa sababu ya [a]kutoamini, na uovu, na ujinga, na majivuno ya wanadamu; kwani hawatatafuta ufahamu, wala kuelewa ufahamu wa juu, wanapoelezewa wazi [b]wazi, hata wazi vile neno linaweza kuwa.

8 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, naona kwamba bado mnatafakari mioyoni mwenu; na inanihuzunisha kwamba lazima nizungumze kuhusu kitu hiki. Kwani ikiwa mtasikiliza Roho ambaye anawafundisha wanadamu [a]kusali, mtajua kwamba lazima msali, kwani [b]roho mchafu hawafundishi mwanadamu kusali, lakini humfundisha kwamba lazima asisali.

9 Lakini tazameni, nawaambia kwamba lazima [a]msali kila wakati, na msife moyo; na kwamba msifanye lolote kwa Bwana bila kumuomba Baba kwa [b]jina la Kristo, kwamba awatakasie matendo yenu, kwamba matendo yenu yawe ni kwa [c]ajili ya ustawi wa nafsi yako.

MLANGO WA 33

Maneno ya Nefi ni ya kweli—Yanamshuhudia Kristo—Wale ambao wanamwamini Kristo wataamini maneno ya Nefi, ambayo yatasimama kama shahidi mbele ya baraza la hukumu. Karibia mwaka 559–545 K.K.

Na sasa mimi, Nefi, siwezi kuandika vitu vyote ambavyo vilifundishwa miongoni mwa watu wangu; wala mimi sio [a]shujaa kwa kuandika, kama nilivyo katika mazungumzo; kwani mwanadamu [b]anapozungumza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu uwezo wa Roho Mtakatifu huyapeleka katika mioyo ya watoto wa watu.

2 Lakini tazama, kuna wengi [a]wanaoshupaza mioyo yao dhidi ya Roho Mtakatifu, kwamba hana nafasi ndani yao; kwa hivyo, wanatupa vitu vingi ambavyo vimeandikwa na kuvichukua kama vitu visivyofaa.

3 Lakini mimi, Nefi, nimeandika yale ambayo nimeandika, na kuyachukua kuwa yenye [a]thamani kuu, na zaidi kwa watu wangu. Kwani [b]nawaombea siku zote kwa mchana, na macho yangu huitia mto maji usiku, kwa sababu yao; na ninamlilia Mungu wangu kwa imani, na ninajua kwamba atasikia kilio changu.

4 Na ninajua kwamba Bwana Mungu ataweka wakfu sala zangu kwa faidha ya watu wangu. Na maneno ambayo nimeandika kwa unyonge yatatiwa [a]nguvu kwao; kwani [b]inawashawishi kutenda mema;

7 *a* MWM Kutoamini.
b 2 Ne. 31:2–3; Yak. (KM) 4:13.
8 *a* MWM Sala.
b Mos. 4:14. MWM Ibilisi.
9 *a* 3 Ne. 20:1; M&M 75:11.
b Musa 5:8.
c Alma 34:27.
33 1 *a* Eth. 12:23–24.
b M&M 100:7–8.
2 *a* Hel. 6:35–36.
3 *a* MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
b Eno. 1:9–12; M. ya Morm. 1:8.
4 *a* Eth. 12:26–27.
b Moro. 7:13.

inawafahamisha wao kuhusu babu zao; na inazungumza kuhusu Yesu, na kuwashawishi kumwamini, na kuvumilia hadi mwisho, ambao ni uzima wa [c]milele.

5 Na inazungumza kwa [a]ukali dhidi ya dhambi, kulingana na vile ukweli ulivyo [b]wazi; kwa hivyo, hakuna mtu yeyote atakayekasirikia maneno ambayo nimeandika ila tu awe na roho ya ibilisi.

6 Nafurahia kwa uwazi; nafurahia ukweli; namfurahia Yesu wangu, kwani [a]ameikomboa nafsi yangu kutoka jehanamu.

7 Nina [a]hisani kwa watu wangu, na imani kuu katika Kristo kwamba nitakutana na nafsi nyingi zisizokuwa na mawaa katika kiti chake cha hukumu.

8 Nina hisani kwa Myahudi—nasema [a]Myahudi, kwa sababu nina maana kwamba nilitoka huko.

9 Na pia nina hisani kwa [a]Wayunani. Lakini tazama, siwezi kuwatumainia ila tu wao [b]wapatanishwe na Kristo, na kuingia katika lile lango [c]jembamba, na [d]watembee katika njia ile [e]iliyosonga inayoelekeza uzima wa milele, na waendelee katika njia hiyo hadi mwisho wa siku ya majaribio.

10 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, na pia Myahudi, na ninyi nyote mlio pande zote za ulimwengu, sikilizeni maneno haya na mwamini katika Kristo; na kama hamwamini katika maneno haya [a]aminini katika Kristo. Na kama mtamwamini Kristo mtaamini katika [b]maneno haya, kwani ni [c]maneno ya Kristo, na ameyapatia kwangu; na [d]yanafundisha wanadamu wote kwamba wafanye mema.

11 Na kama sio maneno ya Kristo, amueni ninyi—kwani Kristo atawaonyesha, kwa [a]uwezo na utukufu mkuu, kwamba ni maneno yake, katika siku ya mwisho; na wewe na mimi [b]tutasimama uso kwa uso kwenye baraza lake; na utajua kwamba nimeamriwa na yeye kuandika vitu hivi, ingawa mimi ni mnyonge.

12 Na ninamuomba Baba kwa jina la Kristo kwamba wengi wetu, kama sio wote, waokolewe katika [a]ufalme wake siku ile kuu ya mwisho.

13 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, wale wote ambao ni wa nyumba ya Israeli, na nyote hadi mwisho wa ulimwengu, nawazungumzia kama sauti [a]inayolia kutoka mavumbini:

4 *c* MWM Uzima wa Milele.
5 *a* 1 Ne. 16:1–3; 2 Ne. 9:40.
b 2 Ne. 31:3; Yak. (KM) 4:13.
6 *a* MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
7 *a* MWM Hisani.
8 *a* MWM Wayahudi.
9 *a* MWM Wayunani.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
c 2 Ne. 9:41.
d MWM Tembea, Tembea na Mungu.
e Hel. 3:29–30; M&M 132:22.
10 *a* MWM Amini, Imani.
b MWM Kitabu cha Mormoni.
c Moro. 10:27–29.
d 2 Ne. 25:28.
11 *a* Eth. 5:4; Moro. 7:35.
b Ufu. 20:12; Moro. 10:34.
12 *a* MWM Utukufu wa Selestia.
13 *a* Isa. 29:4; 2 Ne. 26:16.

Kwa herini hadi siku ile kuu itakapofika.

14 Na wewe usiyekubali kupokea wema wa Mungu, na kuheshimu maneno ya Wayahudi, na pia [a]maneno yangu, na [b]maneno yatakayotoka kutoka kinywa cha Mwanakondoo wa Mungu, tazama, nakupigia kwaheri isiyo na mwisho, kwani maneno haya [c]yatakuhukumu siku ya mwisho.

15 Kwani yale ambayo ninayatia muhuri duniani, yatatetwa dhidi yako katika baraza la [a]hukumu; kwani Bwana ameniamuru hivi, na ni lazima nitii. Amina.

KITABU CHA YAKOBO

MDOGO WA NEFI

Maneno aliyowahubiria ndugu zake. Anamfadhaisha mtu aliyetaka kupindua mafundisho ya Kristo. Maneno machache kuhusu historia ya watu wa Nefi.

MLANGO WA 1

Yakobo na Yusufu wanatafuta kuwashawishi wanadamu kumwamini Kristo na kushika amri Zake—Nefi anafariki—Uovu unazidi miongoni mwa Wanefi. Karibia mwaka 544–421 K.K.

KWANI tazama, ikawa kwamba miaka hamsini na mitano ilikuwa imepita tangu Lehi atoke Yerusalemu; kwa hivyo, Nefi alinipatia mimi, [a]Yakobo, [b]amri kuhusu mabamba yale [c]madogo, ambako vitu hivi vimechorwa.

2 Na akanipatia mimi, Yakobo, amri kwamba niandike kwenye mabamba haya vitu vichache ambavyo nilivifikiria kuwa vyenye thamani; na kwamba nisiguse, ila kidogo tu, kuhusu historia ya hawa watu wanaoitwa watu wa Nefi.

3 Kwani alisema kwamba historia ya watu wake iandikwe kwenye yale mabamba yake mengine, na kwamba nihifadhi mabamba haya na kupokelezea uzao wangu, kutoka kizazi hadi kizazi.

4 Na kama kulikuwa na mahubiri yaliyo matakatifu, au ufunuo ulio mkuu, au kutoa unabii, kwamba nichore yaliyo muhimu katika mabamba haya, na niyagusie sana kama iwezekanavyo, kwa ajili ya Kristo, na kwa faida ya watu wetu.

5 Kwani kwa sababu ya imani na wasiwasi mwingi, kwa

14 *a* MWM Biblia.
b MWM Kitabu cha Mormoni.
c 2 Ne. 29:11; Eth. 4:8–10.

15 *a* M. ya Morm. 1:11.

[YAKOBO]
1 1 *a* MWM Yakobo, Mwana wa Lehi.
b Yak. (KM) 7:27.
c 2 Ne. 5:28–33; Yak. (KM) 3:13–14. MWM Mabamba.

hakika tulidhihirishiwa, kuhusu vile vitu [a]vitakavyowapata watu wetu.

6 Na pia tulikuwa na ufunuo mwingi, na roho ya unabii mwingi; kwa hivyo, tulijua kuhusu [a]Kristo na ufalme wake, utakaokuja.

7 Kwa hivyo tulifanya kazi kwa bidii miongoni mwa watu wetu, kwamba tuwashawishi [a]waje kwa Kristo, na waonje wema wa Mungu, ili waingie katika [b]pumziko lake, na ili kwa njia yoyote asiape katika ghadhabu yake kwamba [c]hawataingia ndani, kama walivyomtia [d]hasira katika siku za majaribio wakati wana wa Israeli walipokuwa [e]nyikani.

8 Kwa hivyo, tunatamani kutoka kwa Mungu kama ingewezekana kwamba tungewashawishi wanadamu wote [a]wasimwasi Mungu, kumtia [b]hasira, lakini kwamba watu wote wangemwamini Kristo, na kutafakari kuhusu kifo chake, na kubeba [c]msalaba wake na kuchukua aibu ya ulimwengu; kwa hivyo, mimi, Yakobo, najichukulia kutimiza amri ya kaka yangu Nefi.

9 Sasa Nefi akaanza kuzeeka, na akajua kwamba anakaribia [a]kufariki; kwa hivyo, [b]akamtia mtu mafuta awe mfalme na mtawala juu ya watu wake sasa, kulingana na utawala wa [c]wafalme.

10 Watu walikuwa wamempenda Nefi sana, kwa vile alikuwa mlinzi wao mkuu, na kuupunga [a]upanga wa Labani kwa ulinzi wao, na alikuwa ametumikia kwa ustawi wao katika maisha yake yote—

11 Kwa hivyo, watu walitaka kulikumbuka jina lake. Na yeyote atakayetawala baada yake watu walimwita, Nefi wa pili, Nefi wa tatu, na kadhalika, kulingana na utawala wa wafalme; na hivyo ndivyo walivyoitwa na watu, haidhuru jina lolote walilokuwa nalo.

12 Na ikawa kwamba Nefi alifariki.

13 Sasa wale watu ambao hawakuwa [a]Walamani walikuwa [b]Wanefi; walakini, waliitwa Wanefi, Wayakobo, Wayusufu, [c]Wazoramu, Walamani, Walemueli, na Waishmaeli.

14 Lakini mimi, Yakobo, hapa baadaye sitawapambanua kwa majina haya, lakini wale wanaotaka kuangamiza watu wa Nefi [a]nitawaita Walamani, na wale ambao ni marafiki wa Nefi

5 *a* 1 Ne. 12.
6 *a* 1 Ne. 10:4–11; 19:8–14.
7 *a* 2 Ne. 9:41; Omni 1:26; Moro. 10:32.
b MWM Pumzika.
c Hes. 14:23; Kum. 1:35–37; M&M 84:23–25.
d Ebr. 3:8.
e Hes. 26:65; 1 Ne. 17:23–31.
8 *a* MWM Uasi.
b 1 Ne. 17:30; Alma 12:36–37; Hel. 7:18.
c TJS Mt. 16:25–26 (Kiambatisho); Lk. 14:27.
9 *a* 2 Ne. 1:14.
b MWM Paka mafuta.
c 2 Ne. 6:2; Yar. 1:7.
10 *a* 1 Ne. 4:9; 2 Ne. 5:14; M. ya Morm. 1:13; Mos. 1:16; M&M 17:1.
13 *a* Eno. 1:13; M&M 3:18.
b MWM Wanefi.
c 1 Ne. 4:35; 4 Ne. 1:36–37.
14 *a* Mos. 25:12; Alma 2:11.

nitawaita [b]Wanefi, au [c]watu wa Nefi, kulingana na utawala wa wafalme.

15 Na sasa ikawa kwamba watu wa Nefi, chini ya utawala wa mfalme wa pili, walianza kuwa wagumu mioyoni mwao, na kujihusisha katika matendo maovu, kama vile Daudi wa kale wakitamani [a]wake wengi na makahaba, na pia mwana wake, Sulemani.

16 Ndiyo, na hata pia wakaanza kutafuta dhahabu na fedha nyingi, na wakaanza kuinuliwa katika kiburi.

17 Kwa hivyo mimi, Yakobo, niliwapatia maneno haya nilipowafundisha katika [a]hekalu, nikiwa nimepokea kwanza [b]mwito wangu kutoka kwa Bwana.

18 Kwani mimi, Yakobo, na kaka yangu Yusufu tulikuwa [a]tumetengwa tuwe makuhani na walimu kwa watu hawa, kwa mkono wa Nefi.

19 Na tuliadhimisha [a]ofisi yetu kwa Bwana, tukijichukulia [b]jukumu, na wajibu wa dhambi za watu vichwani mwetu kama hatungewafundisha neno la Mungu kwa bidii yote; kwa hivyo, tulitumikia kwa uwezo wetu ili [c]damu yao isiwe katika mavazi yetu; la sivyo, damu yao ingekuwa katika mavazi yetu, na hatungepatikana bila alama katika siku ile ya mwisho.

MLANGO WA 2

Yakobo anashutumu tamaa ya utajiri, kiburi, na uasherati—Wanadamu wamekubaliwa kutafuta utajiri kwa kusudi la kuwasaidia wanadamu wenzao—Bwana anaamuru kwamba hakuna mtu miongoni mwa Wanefi anayeruhusiwa kuwa na zaidi ya mke mmoja—Bwana anafurahia katika usafi wa kimwili wa wanawake. Karibia mwaka 544–421 K.K.

Maneno ambayo Yakobo, kaka wa Nefi, aliwazungumzia watu wa Nefi, baada ya kifo cha Nefi:

2 Sasa, ndugu zangu wapendwa, mimi, Yakobo, kulingana na jukumu langu kwa Mungu, kutukuza ofisi yangu kwa ufahamu, na ili niyaondolee mavazi yangu dhambi zenu, naja hapa hekaluni siku hii ili niwatangazie neno la Mungu.

3 Na ninyi mnajua mpaka sasa kwamba nimekuwa na bidii katika ofisi niliyoitiwa; lakini siku ya leo nimelemewa sana kwa hamu na wasiwasi wa ustawi wa nafsi zenu zaidi ya vile nilivyokuwa hapo awali.

4 Kwani tazama, hadi sasa, mmekuwa watiifu kwa neno la Bwana, ambalo nimewapatia.

5 Lakini tazama, nisikilizeni mimi, na mjue kwamba kwa usaidizi wa Muumba wa mbingu na dunia na aliye na uwezo wote naweza kuwaambia kuhusu [a]mawazo yenu, jinsi

14 *b* 2 Ne. 4:11.
c 2 Ne. 5:9.
15 *a* M&M 132:38–39.
17 *a* 2 Ne. 5:16.
MWM Hekalu, Nyumba ya Bwana.
b MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
18 *a* 2 Ne. 5:26.
19 *a* MWM Ofisa, Ofisi.
b M&M 107:99–100.
MWM Msimamizi, Usimamizi.
c 2 Ne. 9:44.
2 5 *a* Alma 12:3; M&M 6:16.
MWM Mungu, Uungu.

vile mmeanza kutumikia katika dhambi, dhambi ambayo ni ya machukizo zaidi kwangu, ndiyo, na ya machukizo kwa Mungu.

6 Ndiyo, inahuzunisha nafsi yangu na kunisababisha nijitenge kwa aibu mbele ya uwepo wa Muumbaji wangu, kwamba lazima niwashuhudie kuhusu uovu wa mioyo yenu.

7 Na pia inanihuzunisha kwamba lazima nitumie maneno [a]makali nikizungumza kuwahusu, mbele za wake zenu na watoto wenu, ambao wengi wao mawazo yao ni mepesi sana na yenye [b]unyoofu na ya kuvutia mbele ya Mungu, kitu ambacho ni cha kupendeza kwa Mungu;

8 Na nimedhania kwamba wamekuja kusikia [a]neno la kupendeza la Mungu, ndiyo, neno ambalo linaponya nafsi iliyojeruhiwa.

9 Kwa hivyo, inahuzunisha nafsi yangu kwamba ninashurutishwa, kwa sababu ya amri kali ambayo nimepokea kutoka kwa Mungu, kuwaonya kulingana na makosa yenu, kupanua vidonda vya wale ambao wamejeruhiwa, badala ya kuwafariji na kuponya vidonda vyao; na wale ambao hawajajeruhiwa, badala ya kujiburudisha kwa neno la kupendeza la Mungu wamewekewa visu vidunge nafsi zao na kujeruhi mawazo yao mepesi.

10 Lakini, ingawa kazi hii ni kuu, lazima nitende kulingana na [a]amri kali za Mungu, na niwaambie kuhusu uovu wenu na machukizo yenu, katika uwepo wa walio safi moyoni, na moyo uliopondeka, na chini ya tazamo la jicho lenye [b]kupenya la Mwenyezi Mungu.

11 Kwa hivyo, lazima niwaambie ukweli kulingana na [a]udhahiri wa neno la Mungu. Kwani tazama, nilipokuwa nikimuomba Bwana, neno likanijia hivi, likisema: Yakobo, kesho uende hekaluni, na uwatangazie watu neno nitakalokupatia.

12 Na sasa tazameni, ndugu zangu, hili ndilo neno ambalo nawatangazia, kwamba wengi wenu mmeanza kutafuta dhahabu, na fedha, na kila aina ya mawe yenye [a]madini, ambayo yamejaa tele, katika nchi hii, ambayo ni [b]nchi ya ahadi kwenu na kwa uzao wenu.

13 Na mkono wa majaliwa umewapendelea sana, hata kwamba mmepata utajiri mwingi; na kwa sababu wengine wenu mmepata tele zaidi kuliko ndugu zenu [a]mmejiinua juu kwa kiburi cha mioyo yenu, na kukaza shingo zenu na kuinua vichwa vyenu kwa sababu ya mavazi yenu yenye gharama, na kuwatesa ndugu zenu kwa sababu mnadhani kwamba ninyi ni bora kuliko wao.

14 Na sasa, ndugu zangu, je, mnadhani kwamba Mungu

7 *a* M&M 121:43.
b MWM Wema.
8 *a* Alma 31:5.
10 *a* MWM Amri za Mungu.
b 2 Ne. 9:44.
11 *a* 2 Ne. 25:4; 31:2–3.
12 *a* 1 Ne. 18:25; Hel. 6:9–11; Eth. 10:23.
b 1 Ne. 2:20.
MWM Nchi ya Ahadi.
13 *a* Morm. 8:35–39.

anawakubalia katika jambo hili? Tazama, nawaambia, Hapana. Lakini anawahukumu, na mkiendelea katika mambo hili lazima hukumu zake ziwateremkie kwa haraka.

15 Ee kwamba angewaonyesha kuwa anaweza kuwadunga, na kwa tazamo moja la jicho lake anaweza kuwaangusha mchangani!

16 Ee kwamba angewaondolea uovu huu na chukizo. Na, Ee kwamba mngesikiliza neno la amri zake, na msikubali hiki [a]kiburi cha mioyo yenu kuangamiza nafsi zenu.

17 Fikirieni ndugu zenu jinsi mnavyojifikiria ninyi wenyewe, na mfanye urafiki na wote na muwe wakarimu katika [a]utajiri wenu, ili [b]nao wawe matajiri kama ninyi.

18 Lakini kabla ya kutafuta [a]utajiri, tafuteni [b]ufalme wa Mungu.

19 Na baada ya kupokea tumaini katika Kristo mtapokea utajiri, kama mtautafuta; na mtautafuta kwa kusudi la [a]kutenda mema—kuvisha walio uchi, na kulisha wenye njaa, na kuwakomboa wafungwa, na kuwatolea msaada walio wagonjwa na wanaoteseka.

20 Na sasa, ndugu zangu, nimewazungumzia kuhusu kiburi; na wale wenu ambao mmetesa jirani yenu, na kumdhulumu kwa sababu mlikuwa na kiburi mioyoni mwenu, kwa sababu ya vitu vile ambavyo Mungu amewapatia, je, mnasema nini?

21 Je, hamdhani kwamba vitu kama hivi ni vya kuchukiza kwa yule aliyeumba watu wote? Na mwanadamu mmoja ni mwenye thamani machoni mwake kama mwingine. Na wanadamu wote wametoka mavumbini; na aliwaumba kwa kusudi moja, kwamba watii [a]amri zake na kumtukuza milele.

22 Na sasa ninakoma kuwazungumzia kuhusu kiburi hiki. Na kama sio lazima kwamba niwazungumzie kuhusu makosa makuu zaidi, moyo wangu ungeweza kushangilia sana kwa sababu yenu.

23 Lakini neno la Mungu linanipatia mzigo kwa sababu ya dhambi zenu kuu: Kwani tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Watu hawa wanaanza kutenda uovu; hawafahamu maandiko, kwani wanatafuta kisingizio cha kutenda uasherati, kwa sababu ya vile vitu vilivyoandikwa kuhusu Daudi, na Sulemani mwana wake.

24 Tazama, Daudi na [a]Sulemani kwa hakika walikuwa na wake [b]wengi na makahaba, kitu ambacho kilikuwa cha kuchukiza mbele yangu, asema Bwana.

16 *a* MWM Kiburi.
17 *a* MWM Sadaka, Utoaji sadaka; Ustawi.
b 4 Ne. 1:3.
18 *a* 1 Fal. 3:11–13; Mk. 10:17–27; 2 Ne. 26:31; M&M 6:7. MWM Ukwasi.
b Lk. 12:22–31.
19 *a* Mos. 4:26.
21 *a* M&M 11:20; Ibr. 3:25–26.
24 *a* 1 Fal. 11:1; Neh. 13:25–27.
b 1 Fal. 11:1–3; Ezra 9:1–2; M&M 132:38–39.

25 Kwa hivyo, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, nimewaongoza watu hawa kutoka nchi ya Yerusalemu, kwa uwezo wa mkono wangu, ili niinue tawi [a]takatifu kutoka kwa matunda ya viuno vya Yusufu.

26 Kwa hivyo, mimi Bwana Mungu sitakubali kwamba watu hawa watende kama wale wa kale.

27 Kwa hivyo, ndugu zangu, nisikilizeni, na mtii neno la Bwana: Kwani hakuna mtu yeyote miongoni mwenu ambaye atakuwa na mke zaidi ya [a]mmoja; wala hatakuwa na masuria;

28 Kwani mimi, Bwana Mungu, nafurahia [a]usafi wa kimwili wa wanawake. Na ukahaba ni chukizo mbele yangu; hivyo ndivyo asemavyo Bwana wa Majeshi.

29 Kwa hivyo, watu hawa watatii amri zangu, asema Bwana wa Majeshi, la sivyo nchi [a]italaaniwa kwa sababu yao.

30 Kwani kama, nitainua [a]kizazi kwangu, asema Bwana wa Majeshi, nitawaamuru watu wangu; la sivyo, watatii vitu hivi.

31 Kwani tazama, mimi, Bwana, nimeona huzuni, na kusikia maombolezi ya mabinti za watu wangu katika nchi ya Yerusalemu, ndiyo, na katika nchi zote za watu wangu, kwa sababu ya uovu na machukizo ya mabwana wao.

32 Na sitakubali, asema Bwana wa Majeshi, kwamba vilio vya mabinti wazuri wa hawa watu, ambao niliwaongoza kutoka nchi ya Yerusalemu, kunifikia mimi kwa sababu ya wanaume wa watu wangu, asema Bwana wa Majeshi.

33 Kwani hawatawapeleka utumwani mabinti za watu wangu kwa sababu ya upole wao, la sivyo nitawaadhibu kwa laana kali, hata kuwaangamiza; kwani hawatatenda [a]uasherati, kama wale wa kale, asema Bwana wa Majeshi.

34 Na sasa tazameni, ndugu zangu, mnajua kwamba amri hizi zilitolewa kwa baba yetu, Lehi; kwa hivyo, mlizijua hapo awali; na mmepokea hukumu kuu; kwani mmetenda vitu hivi ambavyo hamkustahili kutenda.

35 Tazama, mmetenda maovu [a]makuu kuliko Walamani, ndugu zetu. Mmevunja mioyo ya wake zenu wapole, na kuvunja tumaini la watoto wenu, kwa sababu ya mifano miovu mbele yao; na vilio vya mioyo yao kwa sababu yenu vinamfikia Mungu. Na kwa sababu ya ukali wa neno la Mungu, unaoshuka dhidi yenu, mioyo mingi ilikufa, ikiwa imedungwa na vidonda vikubwa.

25*a* Mwa. 49:22–26; Amo. 5:15; 2 Ne. 3:5; Alma 26:36. MWM Lehi, Baba wa Nefi.
27*a* M&M 42:22; 49:16.
28*a* MWM Usafi wa Kimwili.
29*a* Eth. 2:8–12.
30*a* Mal. 2:15; M&M 132:61–66. MWM Ndoa, Oa, Olewa.
33*a* MWM Kupenda anasa, Matamanio ya anasa; Utovu wa maadili ya kujamiiana.
35*a* Yak. (KM) 3:5–7.

MLANGO WA 3

Walio safi moyoni wanapokea neno la kupendeza la Mungu—Utakatifu wa Walamani unazidi ule wa Wanefi—Yakobo anaonya kuhusu uasherati, tamaa, na kila dhambi. Karibia mwaka 544–421 K.K.

Lakini tazama, mimi, Yakobo, nitawazungumzia wale walio safi moyoni. Mtegemeeni Mungu kwa mawazo yenu yote, na mmuombe, kwa imani kuu, na atawafariji katika mateso yenu, na atatetea kesi yenu, na kuwateremshia hukumu wale wanaotaka kuwaangamiza.

2 Ee ninyi nyote mlio safi moyoni, inueni vichwa vyenu na kupokea neno la kupendeza la Mungu, na kusherekea upendo wake; kwani mnaweza, kama mawazo yenu yatakuwa [a]imara, daima.

3 Lakini, ole, ole, kwa ninyi msio safi moyoni, wale ambao ni [a]wachafu mbele ya Mungu leo; kwani msipotubu nchi italaaniwa kwa sababu yenu; na Walamani, ambao sio wachafu kama ninyi, walakini [b]wamelaaniwa kwa laana kali, watawadhulumu hadi wawaangamize.

4 Na wakati unafika haraka, kwamba msipotubu watamiliki nchi yenu ya urithi, na Bwana Mungu [a]atawaondoa wenye haki miongoni mwenu.

5 Tazameni, Walamani ndugu zenu, ambao mnawachukia kwa sababu ya uchafu wao na laana ambayo imeshika ngozi zao, ni watakatifu zaidi yenu; kwani [a]hawajasahau amri ya Bwana, ambayo ilipewa kwa baba yetu—kwamba waoe mke mmoja pekee, na wasiwe na makahaba, na wasitende uasherati miongoni mwao.

6 Na sasa, wanatii amri hii kwa bidii; kwa hivyo, kwa sababu ya huu utiifu, katika kuweka amri hii, Bwana Mungu hatawaangamiza, lakini [a]atawarehemu; na siku moja watakuwa watu wenye baraka.

7 Tazama, mabwana zao [a]wanawapenda wake zao, na wake zao wanawapenda mabwana zao; na mabwana zao na wake zao wanawapenda watoto wao; na kutoamini kwao na chuki yao kwenu ni kwa sababu ya uovu wa baba zao; kwa hivyo, je, ninyi ni wema zaidi yao, machoni pa Muumba wenu mkuu?

8 Enyi ndugu zangu, nawahofia kwamba msipotubu dhambi zenu ngozi zao zitakuwa nyeupe zaidi yenu, mtakapoletwa pamoja na wao mbele ya kiti cha enzi cha Mungu.

9 Kwa hivyo, nawapa amri, ambayo ni neno la Mungu, kwamba msiwachukie tena kwa sababu ya weusi wa ngozi zao; wala hamtawachukia kwa sababu ya uchafu wao; lakini mtakumbuka uchafu wenu wenyewe, na kukumbuka kwamba uchafu wao ulitokana na baba zao.

3 2*a* Alma 57:26–27.
3*a* MWM Chafu, Uchafu.
b 1 Ne. 12:23.
4*a* Omni 1:5–7, 12–13.
5*a* Yak. (KM) 2:35.
6*a* 2 Ne. 4:3, 6–7; Hel. 15:10–13.
7*a* MWM Familia; Upendo.

10 Kwa hivyo, mtakumbuka [a]watoto wenu, jinsi mlivyodhulumu mioyo yao kwa sababu ya mfano mliowapatia; na pia, kumbukeni kwamba mnaweza, kwa sababu ya uchafu wenu, kuwatia watoto wenu katika maangamizo, na dhambi zao zitakuwa vichwani vyenu katika siku ya mwisho.

11 Ee ndugu zangu, sikilizeni maneno yangu; amsheni fahamu za nafsi zenu; jitingisheni ili [a]muamke kutoka katika usingizi wa kifo; na mjifungue kutoka katika uchungu wa [b]jehanamu ili msiwe [c]malaika wa ibilisi, na kutupwa katika ziwa la moto na kiberiti ambalo ni [d]mauti ya pili.

12 Na sasa mimi, Yakobo, niliwazungumzia watu wa Nefi vitu vingi zaidi nikiwaonya wasitende [a]uasherati na [b]tamaa, na kila aina ya dhambi, na kuwaelezea matokeo yao.

13 Na haiwezekani kuandika hata asilimia moja ya yale yaliotendwa na watu hawa, ambao waliongezeka kuwa wengi, katika [a]mababmba haya; lakini matendo yao mengi yameandikwa katika yale mababmba makubwa, na vita vyao, na mabishano yao, na utawala wa wafalme wao.

14 Mababmba haya yanaitwa mababmba ya Yakobo, na yalitengenezwa kwa mkono wa Nefi. Na ninakoma kuzungumza maneno haya.

MLANGO WA 4

Manabii wote walimwabudu Baba katika jina la Kristo—Sadaka ya Ibrahimu ya kumtoa Isaka ilikuwa katika mfano wa Mungu na Mwana Wake wa Pekee—Wanadamu wanapaswa kujipatanisha wenyewe na Mungu kwa njia ya Upatanisho—Wayahudi watalikataa jiwe la msingi. Karibia mwaka 544–421 K.K.

Tazama sasa, na ikawa kwamba mimi, Yakobo, nikiwa nimewahudumia watu wangu sana kwa kunena, (na siwezi kuandika ila tu maneno machache, kwa sababu ya ugumu wa kuchora maneno yetu kwenye mababmba) na tunajua kwamba vitu ambavyo tunaandika kwenye mababmba haya lazima vitadumu;

2 Lakini vitu vyovyote tunavyoandika kwenye kitu kingine isipokuwa kwenye mababmba lazima viangamie na kutoweka; lakini tunaweza kuandika maneno machache kwenye mababmba, ambayo yatawapatia watoto wetu, na pia ndugu zetu wapendwa, kiasi kidogo cha ufahamu kutuhusu sisi, au kuhusu baba zao—

3 Sasa tunafurahia kitu hiki; na tunatumikia kwa bidii kuchora maneno haya kwenye mababmba, tukitumai kwamba ndugu zetu wapendwa na watoto wetu watayapokea kwa mioyo ya shukrani, na kuyatazamia ili

10 *a* MWM Mtoto, Watoto.
11 *a* Alma 5:6–9.
b MWM Jehanamu.
c 2 Ne. 9:8–9.
d MWM Mauti ya Kiroho.
12 *a* MWM Uasherati.
b MWM Ovu, Uovu; Tamaa mbaya.
13 *a* 1 Ne. 19:1–4; Yak. (KM) 1:1–4.

wajifunze kwa shangwe na sio kwa huzuni, wala kwa dharau, yanayowahusu wazazi wao wa kwanza.

4 Kwani, kwa madhumuni haya tumeandika vitu hivi, ili wajue kwamba [a]tulijua kuhusu Kristo, na tulikuwa na matumaini ya utukufu wake miaka mia mingi kabla ya kuja kwake; na sio tu sisi pekee tuliokuwa na tumaini la utukufu wake, lakini pia [b]manabii wote wataka tifu ambao walikuwa mbele yetu.

5 Tazama, walimwamimi Kristo na [a]kumwabudu Baba katika jina lake, na pia sisi tunamwabudu Baba katika jina lake. Na kwa madhumuni haya tunatii [b]sheria ya Musa, ambayo [c]inaelekeza nafsi zetu kwake; na kwa lengo hili imetakaswa kwetu sisi ili tuwe wenye haki, hata kama vile ilivyochukuliwa kwa Ibrahimu huko nyikani awe mtiifu kwa amri za Mungu kwa kumtoa mwana wake Isaka awe sadaka, ambayo ilikuwa ni mfano wa Mungu na [d]Mwana wake wa Pekee.

6 Kwa hivyo, tunawachunguza manabii, na tunao ufunuo mwingi na roho ya [a]unabii; pamoja na [b]mashahidi hawa wote tunapokea tumaini, na imani yetu haiwezi kutingishwa, hadi kwamba kwa kweli tunaweza [c]kuamuru katika [d]jina la Yesu na miti itutii, au milima, au mawimbi ya bahari.

7 Walakini, Bwana Mungu hutuonyesha [a]unyonge wetu ili tujue kwamba ni kwa neema yake, na ufadhili wake mkuu kwa watoto wa watu, kwamba tunao uwezo wa kutenda vitu hivi.

8 Tazama, kazi za Bwana ni kuu na za kushangaza. Jinsi gani [a]zilivyofichika [b]siri zake; na haiwezekani kwamba mwanadamu agundue njia zake zote. Na hakuna mwanadamu yeyote [c]ajuaye [d]njia zake bila kufunuliwa kwake; kwa hivyo, ndugu, msidharau ufunuo wa Mungu.

9 Tazama kwani, kwa nguvu za [a]neno lake [b]mwanadamu alikuja usoni mwa dunia, dunia ambayo iliumbwa kwa nguvu za neno lake. Kwa hivyo, kama Mungu aliweza kuzungumza na ulimwengu ukawepo, na kuzungumza na mwanadamu akaumbwa, Ee basi, kwa nini asiweze kuamuru [c]dunia, au kazi ya mikono yake usoni mwa

4 4*a* MWM Yesu Kristo.
b Lk. 24:25–27; Yak. (KM) 7:11; Mos. 13:33–35; M&M 20:26.
5*a* Musa 5:8.
b 2 Ne. 25:24; Yar. 1:11; Mos. 13:27, 30; Alma 25:15–16. MWM Torati ya Musa.
c Gal. 3:24.
d Mwa. 22:1–14; Yn. 3:16–18. MWM Mzaliwa Pekee.
6*a* MWM Toa unabii, Unabii.
b MWM Shahidi, Ushahidi.
c MWM Uwezo.
d Mdo. 3:6–16; 3 Ne. 8:1.
7*a* Eth. 12:27.
8*a* Rum. 11:33–36.
b M&M 19:10; 76:114. MWM Siri za Mungu.
c 1 Kor. 2:9–16; Alma 26:21–22. MWM Maarifa.
d Isa. 55:8–9.
9*a* Morm. 9:17; Musa 1:32.
b MWM Mwanadamu, Wanadamu; Umba, Uumbaji.
c Hel. 12:8–17.

ulimwengu, kulingana na nia yake na raha yake?

10 Kwa hivyo, ndugu, msijaribu [a]kumshauri Bwana, lakini mpokee ushauri kutoka mkono wake. Kwani tazama, ninyi wenyewe mnajua kwamba anatoa ushauri juu ya kazi yake yote kwa [b]hekima, na kwa haki, na kwa rehema kuu.

11 Kwa hivyo, ndugu wapendwa, patanishweni na yeye kwa [a]upatanisho wa Kristo, [b]Mwana wake wa Pekee, na mnaweza kupokea [c]ufufuo, kulingana na nguvu za ufufuo ambazo zimo katika Kristo, na mkabidhiwe kama [d]malimbuko ya Kristo kwa Mungu, mkiwa na imani, na kupokea tumaini jema la utukufu kwake kabla hajajidhihirisha katika mwili.

12 Na sasa, wapendwa, msishangae kwamba ninawaambia vitu hivi; kwani kwa nini [a]isizungumziwe upatanisho wa Kristo, na kupata ufahamu kamili kwake, ili kupokea ufahamu wa ufufuo na ulimwengu ujao?

13 Tazameni, ndugu zangu, yule anayetoa unabii, hebu yeye atoe unabii wa kuleleweka na wanadamu; kwani [a]Roho huzungumza ukweli wala sio uwongo. Kwa hivyo, huzungumza kuhusu vile vitu [b]vilivyo, na vile vitu vitavyokuwa; kwa hivyo, tunadhihirishiwa vitu hivi [c]wazi wazi, kwa wokovu wa nafsi zetu. Lakini tazama, sisi sio mashahidi wa pekee katika vitu hivi; kwani Mungu alivizungumza pia kwa manabii wa kale.

14 Lakini tazama, Wayahudi walikuwa ni watu wenye [a]shingo ngumu; na [b]walidharau maneno yaliyokuwa wazi, na wakawaua manabii, na wakatafuta vitu ambavyo hawakuweza kufahamu. Kwa hivyo, kwa sababu ya [c]upofu wao, upofu ambao ulitokana na kuangalia zaidi ya lengo, lazima waanguke; kwani Mungu ameuondoa udhahiri wake kutoka kwao, na kuwapatia wao vitu vingi ambavyo [d]hawawezi kufahamu, kwa sababu walivitamani. Na kwa sababu walivitamani Mungu alivitenda, ili wajikwaze.

15 Na sasa mimi, Yakobo, naongozwa na Roho kwa kutoa unabii; kwani ninahisi kwa matendo ya Roho aliye ndani yangu, kwamba kwa [a]kujikwaa kwa Wayahudi [b]watalikataa [c]jiwe ambalo wangejenga juu yake na kuwa na msingi salama.

16 Lakini tazama, kulingana na maandiko, [a]jiwe hili litakuwa

10 *a* 2 Ne. 9:28–29; Alma 37:12, 37; M&M 3:4, 13.
b MWM Hekima; Kujua yote.
11 *a* MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
b Ebr. 5:9.
c MWM Ufufuko.
d Mos. 15:21–23; 18:9; Alma 40:16–21.
12 *a* 2 Ne. 25:26.
13 *a* MWM Roho Mtakatifu; Ukweli.
b M&M 93:24.
c Alma 13:23.
14 *a* Mt. 23:37–38; 2 Ne. 25:2.
b 2 Kor. 11:3; 1 Ne. 19:7; 2 Ne. 33:2.
c Isa. 44:18; Rum. 11:25.
d 2 Ne. 25:1–2.
15 *a* Isa. 8:13–15; 1 Kor. 1:23; 2 Ne. 18:13–15.
b 1 Ne. 10:11.
c MWM Jiwe la pembeni; Mwamba.
16 *a* Zab. 118:22–23.

lile kuu, na la mwisho, na [b]msingi wa kweli ambao ni wa pekee, ambao Wayahudi kuweza kujenga juu yake.

17 Na sasa, wapendwa wangu, itawezekanaje, baada ya hawa kukataa msingi wa kweli, [a]kuweza kujenga juu yake, kwamba uwe kichwa cha pembe yao?

18 Tazameni, ndugu zangu wapendwa, nitawafunulia siri hii; kama sitatingishwa, vyovyote, kutokana na msimamo wangu wa Roho, na kujikwaa kwa sababu ya wasiwasi wangu juu yenu.

MLANGO WA 5

Yakobo anamdondoa Zeno kuhusu fumbo la miti ya mizabibu ya kiasili na iliyofugwa—Ni mfano wa Israeli na Wayunani—Kutawanywa na kusanyiko la Israeli kunawaziwa mbele—Wanefi na Walamani na nyumba ya Israeli yote wanatajwa kijuujuu—Wayunani watapandikizwa katika Israeli—Hatimaye shamba la mizabibu litachomwa. Karibia mwaka 544–421 K.K.

Tazameni, ndugu zangu, hamkumbuki mliposoma maneno ya nabii [a]Zeno, ambayo alizungumzia nyumba ya Israeli, akisema.

2 Sikilizeni, Ee ninyi nyumba ya Israeli, na msikie maneno yangu, nabii wa Bwana.

3 Kwani tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, nitakulinganisha, Ee nyumba ya [a]Israeli, na [b]mzeituni uliochukuliwa na mtu na akaulisha [c]shambani mwake la mizabibu; na ukakua, na kuzeeka, na ukaanza [d]kuoza.

4 Na ikawa kwamba bwana wa shamba la mizabibu akaenda mbele, na akaona kwamba mzeituni wake ulianza kuoza; na akasema: Nitaupogoa, na kuupalilia, na kuulisha, ili pengine uchipuke matawi yaliyo mazuri, na usiangamie.

5 Na ikawa kwamba aliupogoa, na kuupalilia, na kuulisha kulingana na neno lake.

6 Na ikawa kwamba baada ya siku nyingi ukaanza kutoa matawi machache, machanga na yaliyo nyororo; lakini tazama, kilele chake kikaanza kuangamia.

7 Na ikawa kwamba mwenye shamba la mizabibu akaliona, na akamwambia mtumishi wake: inanihuzunisha kwamba nitaupoteza mti huu; kwa hivyo, nenda ukate matawi kutoka [a]mchekele, na uyalete hapa kwangu; na tutayagoboa yale matawi yake ya kati ambayo yameanza kukauka, na tutayatia motoni ili yachomeke.

8 Na tazama, asema Bwana wa shamba la mizabibu, ninaondoa matawi haya mengi yaliyo machanga na miororo, na nitayapandikiza popote ninapotaka;

16*b* Isa. 28:16; Hel. 5:12.
17*a* Mt. 19:30; M&M 29:30.
5 1*a* MWM Zeno.
3*a* Eze. 36:8. MWM Israeli.
b Rum. 11:17–24. MWM Mzeituni.
c M&M 101:44. MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
d MWM Ukengeufu.
7*a* Rum. 11:17, 24.

na haidhuru kama mzizi wa mti huu utaangamia, Nitajihifadhia matunda yake; kwa hivyo, nitachukua matawi haya machanga na miororo, na nitayapandikiza popote nitakapo.

9 Chukua ewe matawi mchekele, na uyapandikize, [a]badala yake; na haya ambayo nimeyagoboa nitayatupa motoni na kuyachoma, ili yasikwaze mchanga wa shamba langu la mizabibu.

10 Na ikawa kwamba mtumishi wa Bwana wa shamba la mizabibu alitenda kulingana na neno la Bwana wa shamba, na akapandikiza matawi [a]mchekele.

11 Na Bwana wa shamba la mizabibu akasababisha kwamba ipaliliwe, na ipogolewe, na ilishwe, akimwambia mtumishi wake: Inanihuzunisha kwamba nitaupoteza mti huu; kwa hivyo, ili pengine nihifadhi mizizi yake ili isiangamie, na ili nijihifadhie, nimetenda kitu hiki.

12 Kwa hivyo, fuata njia yako; chunga mti, na uulishe, kulingana na maneno yangu.

13 Na haya [a]nitayaweka katika sehemu ya mbali shambani mwangu la mizabibu, mahali popote nitakapo, na haikuhusu wewe; na ninaitenda ili nijihifadhie matawi ya asili ya ule mti; na pia, kwamba nijiwekee, akiba ya matunda wakati wa majira; kwani inanihuzunisha kwamba nitapotelewa na mti huu na matunda yake.

14 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu akaenda njia zake, na akaficha matawi ya kiasili ya ule mzeituni sehemu za mbali za shamba la mizabibu, mingine hapa na mingine pale, kulingana na nia yake na raha yake.

15 Na ikawa kwamba muda mrefu ukapita, na Bwana wa shamba la mizabibu akamwambia mtumishi wake: Njoo, hebu twende shambani la mizabibu, ili tufanye kazi shambani la mizabibu.

16 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu, na pia yule mtumishi, walienda shambani la mizabibu kufanya kazi. Na ikawa kwamba yule mtumishi akamwambia bwana wake: Tazama, angalia hapa; tazama ule mti.

17 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu aliangalia na kuona ule mti ambao yale matawi ya mchekele yalikuwa yamepandikizwa; na ulikuwa umeanza kuota na kuanza kuzaa [a]matunda. Na akaona kwamba ni mazuri; na matunda yake yalikuwa kama matunda ya kawaida.

18 Na akamwambia yule mtumishi: Tazama, matawi ya ule mti wa mwituni yametoa umande kutoka mzizi wake, kwamba mzizi wake umeleta nguvu nyingi; na kwa sababu ya nguvu hizo nyingi za mzizi yale matawi ya mwituni yamezaa matunda ya kinyumbani. Sasa, kama hatungepandikiza haya matawi, ule mti ungeangamia.

9*a* Rum. 1:13.
10*a* MWM Wayunani.
13*a* 1 Ne. 10:12.
17*a* Yn. 15:16.

Na sasa, tazama, nitaweka matunda mengi, ambayo yamezaliwa na ule mti; na matunda yake nitajiwekea akiba, kwa wakati wa majira.

19 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu akamwambia mtumishi: Njoo, twende katika sehemu za mbali za shamba, na tutazame kama matawi ya mti hayajazaa matunda mengi pia, ili nijiwekee akiba, mimi mwenyewe.

20 Na ikawa kwamba walienda pale pahali ambapo yule bwana alikuwa ameficha matawi ya ule mti wa kawaida, na akamwambia yule mtumishi: Tazama haya; na akaona ule wa [a]kwanza kwamba ulikuwa umezaa matunda mengi; na akaona pia kwamba yalikuwa mazuri. Na akamwambia yule mtumishi: Chukua matunda yake, na uyaweke kama akiba wakati wa majira, ili nijihifadhie, kwani tazama, akasema, nimeulisha kwa muda huu wote, na umezaa matunda mengi.

21 Na ikawa kwamba yule mtumishi akamwambia bwana wake: Kwa nini ulikuja kupanda mti huu hapa, au tawi la mti huu? Kwani tazama, palikuwa ndipo pahali pabovu katika shamba lako la mizabibu.

22 Na Bwana wa shamba la mizabibu akamwambia: Usinipatie mawaidha; nilijua kwamba palikuwa ni pahali pabovu shambani; ndivyo, nikakwambia, nimeulisha huu muda mrefu, na wewe unaona kwamba umezaa matunda mengi.

23 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu akamwambia mtumishi wake: Tazama hapa; tazama nimepanda tawi lingine la mti pia; na wewe unajua kwamba pahali hapa ni pabovu zaidi ya pale pa mwanzo. Lakini, tazama mti. Nimeulisha kwa muda huu mrefu, na umezaa matunda mengi; kwa hivyo, uyavune, na uyaweke kama hazina wakati wa majira, ili nijiihifadhie mimi mwenyewe.

24 Na ikawa kwamba yule Bwana wa shamba la mizabibu akamwambia tena mtumishi wake: Tazama hapa; na uone [a]tawi lingine, ambalo pia nimelipanda; tazama nimelilisha pia, na limezaa matunda.

25 Na akamwambia mtumishi: Tazama hapa na uone la mwisho. Tazama, nimepanda hili pahali [a]pema pa shamba; na nimelilisha kwa muda huu mrefu, na sehemu moja pekee ya mti imezaa matunda ya kinyumbani, na sehemu [b]ingine ya mti imezaa matunda ya mwituni; tazama, nimeulisha mti huu kama yale mengine.

26 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu akamwambia mtumishi wake: Chuma yale matawi ambayo hayajazaa [a]matunda mema, na uyatupe motoni.

27 Lakini tazama, yule mtumishi akamwambia: Hebu tuupo-

20 *a* Yak. (KM) 5:39.
24 *a* Eze. 17:22–24; Alma 16:17; 3 Ne. 15:21–24.
25 *a* 1 Ne. 2:20.
b 3 Ne. 10:12–13.
26 *a* Mt. 7:15–20; Alma 5:36; M&M 97:7.

goe, na tuupalilie, na tuulishe kwa muda mwingine mrefu kidogo tena, kwamba pengine utakuzalia matunda mema, yale ambayo unaweza kujiwekea akiba wakati wa majira.

28 Na ikawa kwamba yule Bwana wa shamba la mizabibu na mtumishi wa Bwana wa shamba walilisha matunda yote ya shamba la mizabibu.

29 Na ikawa kwamba muda mrefu ulipita, na Bwana wa shamba akamwambia [a]mtumishi wake: Njoo, twende kule shambani la mizabibu, ili tufanye kazi tena shambani la mizabibu. Kwani tazama, [b]wakati unakaribia, na [c]mwisho unafika hivi karibuni; kwa hivyo, lazima nijiwekee akiba, wakati wa majira.

30 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu na mtumishi wake walienda shambani; na wakafika kwenye ule mti ambao matawi yake ya kawaida yalivunjwa, na matawi ya mwituni kupandikizwa; na tazama matunda ya kila [a]aina yaliufunika ule mti.

31 Na ikawa kwamba yule Bwana wa shamba la mizabibu alionja yale matunda, kila aina kulingana na wingi wake: Na yule Bwana wa shamba la mizabibu akasema: Tazama, kwa muda huu mrefu tumeulisha mti huu, na nimejiwekea akiba kwa wakati wa majira.

32 Lakini tazama, wakati huu umezaa matunda mengi, na [a]hakuna yoyote ambayo ni mazuri. Na tazama, kuna kila aina ya matunda mabaya; na hainifaidi chochote, ingawa tumeuchokea sana; na sasa inanihuzunisha kwamba nitapoteza mti huu.

33 Na Bwana wa shamba la mizabibu akamwambia yule mtumishi: Tutaufanya nini mti huu, ili nijihifadhie mimi mwenyewe matunda mazuri?

34 Na yule mtumishi akamwambia bwana wake: Tazama, kwa sababu wewe ulipandikiza matawi ya mchekele, yamelisha mizizi, hata iwe hai na isiangamie; kwa hivyo wewe unaona kwamba bado ni mizuri.

35 Na ikawa kwamba Bwana wa lile shamba la mizabibu akamwambia mtumishi wake: Huu mti haunifaidi chochote, na mizizi yake hainifaidi chochote ikiwa utazaa matunda maovu.

36 Walakini, najua kwamba mizizi yake ni mizuri, na kwa shauri langu nimeihifadhi; na kwa sababu ya nguvu yao imezaa, kutoka kwa matawi ya mwituni, matunda mazuri.

37 Lakini tazama, yale matawi ya mwituni yamekua [a]zaidi ya mizizi yake; na kwa sababu matawi ya mwituni yamezidi mizizi yake umezaa matunda mengi maovu; na kwa sababu umezaa matunda mengi maovu wewe unaona kwamba umeanza kuangamia; na utaoza hivi karibuni, na kutupwa motoni, tusipotenda jambo ili kuuhifadhi.

29 *a* M&M 101:55; 103:21.
b MWM Siku za Mwisho.
c 2 Ne. 30:10; Yak. (KM) 6:2.
30 *a* MWM Ukengeufu.
32 *a* JS—H 1:19.
37 *a* M&M 45:28–30.

38 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba akamwambia mtumishi wake: Twende kule sehemu za ndani ya shamba la mizabibu, na tuone kama matawi ya kawaida pia nayo yamezaa matunda maovu.

39 Na ikawa kwamba walienda katika sehemu za ndani za lile shamba. Na ikawa kwamba waliona kuwa yale matunda ya matawi ya kiasili pia nayo yalikuwa yameharibika; ndiyo ya [a]kwanza na ya pili na ya mwisho pia; na yote yalikuwa yameharibika.

40 Na matunda ya [a]mwituni ya ule wa mwisho yalizidi sehemu ile ya mti ambayo ilizaa matunda mema, hata kwamba lile tawi likanyauka na kuangamia.

41 Na ikawa kwamba yule Bwana wa shamba la mizabibu alilia, na akamwambia mtumishi wake: Je, ningefanya [a]nini zaidi kuhusu shamba langu la mizabibu?

42 Tazama, nilijua kwamba matunda yote ya lile shamba la mizabibu, isipokuwa haya, yalikuwa yameharibika. Na sasa hii ambayo hapo awali ilizaa matunda mema pia imeharibika; na sasa miti yote ya shamba langu la mizabibu hainifaidi chochote ila kukatwa na kutiwa motoni.

43 Na tazama huu wa mwisho, ambao tawi lake limekauka, nilikuwa nimeupanda katika sehemu [a]nzuri; ndiyo, hata ile ambayo ilikuwa ni bora zaidi ya sehemu zingine za shamba langu la mizabibu.

44 Na wewe uliona pia kwamba nilikata ile [a]iliyofunika sehemu hii, ili nipande mti huu pahala pake.

45 Na wewe uliona kwamba sehemu moja ilizaa matunda mema, na sehemu ingine ikazaa matunda ya mwituni; na kwa sababu sikung'oa matawi yake na kuyatupa motoni, tazama, yamelemea tawi lile njema hata kwamba likakauka.

46 Na sasa, tazama, ingawa tulilitunza sana shamba langu la mizabibu, miti yake imeharibika, hata kwamba haizai matunda mema; na nilikuwa nimetarajia kuihifadhi, na kujiwekea hazina, wakati wa majira. Lakini, tazama, imekuwa kama ule mchekele, na haina faida ila tu [a]kukatwa na kutupwa motoni; na inanihuzunisha kwamba nitaipoteza.

47 Lakini ningefanya nini zaidi shambani langu la mizabibu? Je nimelegeza mkono wangu, hata kwamba sikuulisha? Hapana, nimeulisha, na kuupalilia, na kuupogoa, na nimeutia mbolea; na [a]nimeunyosha mkono wangu karibu siku yote, na [b]mwisho unakaribia. Na inanihuzunisha kwamba nitakata miti yote ya shamba langu la mizabibu, na kuitupa motoni ili ichomeke. Ni nani aliyeharibu shamba langu la mizabibu?

39 *a* Yak. (KM) 5:20, 23, 25.
40 *a* Morm. 6:6–18.
41 *a* 2 Ne. 26:24.
43 *a* 2 Ne. 1:5.
44 *a* Eth. 13:20–21.
46 *a* 3 Ne. 27:11.
47 *a* 2 Ne. 28:32; Yak. (KM) 6:4.
b MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.

48 Na ikawa kwamba yule mtumishi akamwambia bwana wake: Je, sio kiburi cha shamba lako la mizabibu—kwamba matawi yake yamezidi mizizi ambayo ni mizuri? Na kwa sababu yale matawi yamezidi mizizi yake, tazama yalikua zaidi ya nguvu ya mizizi, na kujichukulia nguvu. Tazama, nasema, je, si hii ndiyo sababu ya uharibifu wa miti ya shamba lako?

49 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu akamwambia mtumishi wake: Hebu twende na tukate miti ile ya shamba la mizabibu na tuitupe motoni, ili isifunike ardhi ya shamba langu, kwani nimeshatenda yote. Je, ni yapi mengine ningeutendea shamba langu la mizabibu?

50 Lakini, tazama, yule mtumishi akamwambia Bwana wa shamba la mizabibu: Liache kwa [a]muda mdogo zaidi.

51 Na Bwana akasema: Ndiyo, nitaliacha kwa muda mdogo zaidi, kwani inanihuzunisha kwamba nitapoteza miti ya shamba langu la mizabibu.

52 Kwa hivyo, hebu tukate [a]matawi mengine ya hii ambayo nimepanda katika sehemu za ndani za shamba langu la mizabibu, na hebu tuyapandikize katika ule mti ambao yalitolewa; na hebu tung'oe matawi kutoka ule mti ambao matunda yake ni machungu zaidi, na badala yake tupandikize matawi ya kawaida.

53 Na nitatenda haya ili ule mti usiangamie, ili, pengine, nijihifadhie mizizi yake kwa matumizi yangu.

54 Na, tazama, mizizi ya yale matawi ya mti ambao nimeupanda popote nipendapo bado ingali hai; kwa hivyo, ili nijihifadhie hayo pia kwa matumizi yangu mwenyewe, nitaondoa matawi ya mti huu, na [a]nitayapandikiza ndani yake. Ndiyo, nitayapandikiza katika matawi ya mti mzazi wao, ili nijihifadhie pia hiyo mizizi, ili itakapopokea nguvu za kutosha pengine itanizalia matunda mema, na ili bado nitukuzwe na matunda ya shamba langu la mizabibu.

55 Na ikawa kwamba walichukua kutoka mti wa kawaida ambao ulikuwa umegeuka kuwa wa mwituni, na kupandikiza katika miti ya kawaida, ambayo pia ilikuwa imegeuka kuwa ya mwituni.

56 Na pia wakachukua kutoka miti ya kawaida ambayo ilikuwa imegeuka kuwa ya mwituni, na kupandikiza katika ule mti mzazi wao.

57 Na Bwana wa shamba la mizabibu akamwambia mtumishi wake: Using'oe yale matawi ya mwituni kutoka ile miti, ila tu yale ambayo ni machungu zaidi; na utapandikiza ndani yao kulingana na yale ambayo nimesema.

58 Na tutalisha tena ile miti ya shamba la mizabibu, na tutachenga matawi yake; na tutang'oa kutoka hiyo miti yale matawi yaliyooza, ambayo

50*a* Yak. (KM) 5:27.
52*a* мwм Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
54*a* 1 Ne. 15:12–16.

lazima yaangamie, na kuyatupa motoni.

59 Na nitatenda haya ili, pengine, mizizi yake ipokee nguvu kwa sababu ya ubora wao; na kwa sababu ya mabadiliko ya matawi, kwamba wema uzidi ubaya.

60 Na kwa sababu ya kwamba nimehifadhi yale matawi ya kawaida na mizizi yake, na ya kwamba nimepandikiza matawi ya kawaida tena katika ule mti mzazi wao, na nimehifadhi mizizi ya ule mti mzazi wao, ili, pengine, miti ya shamba langu la mizabibu izae tena [a]matunda mema; na ili nishangilie tena kwa matunda ya shamba langu la mizabibu, na, ili, nishangilie zaidi ya kwamba nimehifadhi mizizi na matawi ya malimbuko—

61 Kwa hivyo, nenda, ulete [a]watumishi, ili tufanye [b]kazi shambani la mizabibu kwa bidii na kwa nguvu zetu, ili tuitayarishe njia, ili nirejeshe tena lile tunda la kawaida, tunda la kawaida ambalo ni bora zaidi ya matunda mengine yote.

62 Kwa hivyo, hebu twende na tutumike kwa nguvu zetu mara hii ya mwisho, kwani tazama mwisho unakaribia, na hii ndiyo mara ya mwisho ambayo nitapogoa shamba langu la mizabibu.

63 Pandikizeni matawi; anzeni na ya [a]mwisho ili yawe ya kwanza, na kwamba ya kwanza yawe ya mwisho, na mlime miongoni mwa miti, iliyo mchanga na iliyokomaa, ya kwanza na ya mwisho; na ya mwisho na ya kwanza, ili yote ilishwe tena kwa mara ya mwisho.

64 Kwa hivyo, chimbeni miongoni mwao, na muipogoe, na kuitia mbolea mara nyingine, kwa mara ya mwisho, kwani mwisho unakaribia. Na kama haya mapandikizo ya mwisho yatakua, na kuzaa matunda ya kawaida, basi mtayatayarishia njia, ili yakue.

65 Na itakapoanza kukua mtaondoa matawi yanayozaa matunda machungu, kulingana na nguvu na kipimo cha uzuri wake; na [a]hamtaondoa yaliyo mabaya kwa ghafla, isiwe kwamba mizizi yake inazidi nguvu ya lile pandikizo, na pandikizo hilo liangamie, na nipoteze miti ya shamba langu la mizabibu.

66 Kwani inanihuzunisha kwamba nitapoteza miti ya shamba langu la mizabibu; kwa hivyo mtafyeka iliyo miovu kulingana na vile iliyo mizuri itakavyomea, ili mizizi na kilele ziwe na nguvu sawa, hadi iliyo nzuri izidi iliyo mbovu, na iliyo mbovu ikatwe na kutiwa motoni, ili isifunike ardhi ya shamba langu; na hivyo ndivyo nitaufagia uovu kutoka shamba langu.

67 Na matawi ya mti wa kawaida nitayapandikiza tena kwenye mti ule wa kawaida;

68 Na matawi ya mti wa kawaida nitayapandikiza katika matawi ya kawaida ya ule mti;

60 *a* Isa. 27:6.
61 *a* Yak. (KM) 6:2; M&M 24:19.
b M&M 39:11, 13, 17.
63 *a* 1 Ne. 13:42; Eth. 13:10–12.
65 *a* M&M 86:6–7.

na ndivyo nitakavyoiunganisha pamoja tena, ili izae matunda ya kawaida, na iwe kitu kimoja.

69 Na iliyo mbovu [a]itatupwa mbali, ndiyo, hata kutoka ardhi yote ya shamba langu la mizabibu; kwani tazama, ni kwa hii mara moja tu nitakayopogoa shamba langu la mizabibu.

70 Na ikawa kwamba Bwana wa shamba la mizabibu alimtuma [a]mtumishi wake; na mtumishi akaenda na kutenda kulingana na vile alivyoamriwa na Bwana, na akaleta watumishi wengine; na walikuwa [b]wachache.

71 Na Bwana wa shamba la mizabibu akawaambia: Nendeni, na [a]mkatumikie shamba la mizabibu, kwa uwezo wenu. Kwani tazama, hii ndiyo [b]mara ya mwisho nitakayolisha shamba langu la mizabibu; kwani mwisho unakaribia, na wakati unafika kwa haraka; na kama mtanitumikia na mimi kwa nguvu zenu [c]mtakuwa na shangwe katika matunda nitakayojiwekea kwa wakati unaokaribia.

72 Na ikawa kwamba watumishi walienda na kutumikia kwa nguvu zao; na Bwana wa shamba la mizabibu akatumikia shambani pia nao; na wakatii amri za Bwana wa shamba la mizabibu katika vitu vyote.

73 Na matunda ya kawaida yakaanza kukua tena pale shambani la mizabibu; na matawi ya kawaida yakaanza kukua na kufanikiwa sana; na matawi ya mwituni yakapobolewa na kutupwa mbali; na wakaweka mizizi yake na kilele chake kuwa sawa, kulingana na nguvu zake.

74 Na wakatumikia hivyo, kwa bidii zote, kulingana na amri za Bwana wa shamba la mizabibu, hadi iliyo mibovu ikatolewa shambani la mizabibu, na Bwana alikuwa amejihifadhia kwamba ile miti ilikuwa matunda ya kawaida tena; na ikawa kama [a]kitu kimoja; na matunda yalikuwa sawa; na yule Bwana wa shamba la mizabibu alikuwa amejihifadhia mwenyewe matunda ya kawaida, ambayo yalikuwa bora zaidi tangu hapo mwanzoni.

75 Na ikawa kwamba wakati yule Bwana wa shamba la mizabibu alipoona kuwa matunda yake ni mazuri, na kwamba shamba lake la mizabibu halikuwa haribifu tena, aliwaita watumishi wake, na kuwaambia: Tazama, tumelilisha shamba langu la mizabibu kwa mara hii ya mwisho; na ninyi mmeona kwamba nimetenda kulingana na nia yangu; na nimehifadhi matunda ya kawaida, na ni mazuri, kama vile yalivyokuwa hapo mwanzoni. Na [a]heri ninyi; kwani kwa sababu mmekuwa na bidii katika kutumikia na mimi katika shamba langu la mizabibu, na mmetii

69 *a* 1 Ne. 22:15–17, 23; 2 Ne. 30:9–10.
70 *a* M&M 101:55; 103:21.
b 1 Ne. 14:12.
71 *a* Mt. 21:28; Yak. (KM) 6:2–3; M&M 33:3–4.
b M&M 39:17; 43:28–30.
c M&M 18:10–16.
74 *a* M&M 38:27.
75 *a* 1 Ne. 13:37.

amri zangu, na kuniletea tena matunda ya [b]kawaida, kwamba shamba langu sio bovu tena, na iliyo mibovu imetupwa mbali, tazama mtapokea shangwe na mimi kwa sababu ya matunda ya shamba langu la mizabibu.

76 Kwani tazama, kwa muda [a]mrefu nitajiwekea matunda ya shamba langu la mizabibu kwa wakati wa majira, unaokaribia kwa haraka; na nimelisha shamba langu la mizabibu kwa mara ya mwisho, na kulipogoa, na kulilimia, na kulitia mbolea; kwa hivyo nitajiwekea matunda, kwa muda mrefu, kulingana na yale ambayo nimezungumza.

77 Na wakati ule utakapofika ambao matunda maovu yatakuja tena katika shamba langu la mizabibu, basi nitasababisha yale yaliyo mazuri na mabaya kukusanywa; na yale mazuri nitajiwekea, na yale mabaya nitayatupa mahali pake. Na kisha wakati wa [a]majira utafika na mwisho; na nitasababisha shamba langu la mizabibu [b]lichomwe kwa moto.

MLANGO WA 6

Bwana ataifufua Israeli katika siku za mwisho—Ulimwengu utachomwa kwa moto—Lazima wanadamu wamfuate Kristo ili kuepuka ziwa la moto na kiberiti. Karibia mwaka 544–421 K.K.

Na sasa, tazameni, ndugu zangu, kama vile nilivyowaambia kwamba nitatoa unabii, tazama, huu ndiyo unabii wangu—kwamba vile vitu ambavyo huyu nabii [a]Zeno alizungumza, kuhusu nyumba ya Israeli, ambapo aliwalinganisha na mzeituni, lazima vitimie.

2 Na siku ambayo atanyoosha mkono wake tena mara ya pili ili [a]kuwaokoa watu wake, ni siku ile, ndiyo, hata mara ya mwisho, ambayo [b]watumishi wa Bwana wataenda mbele kwa [c]nguvu zake, [d]kulisha na kupogoa [e]shamba lake la mizabibu; na baada ya hayo [f]mwisho utafika.

3 Na heri wale ambao wametumikia shamba lake la mizabibu kwa bidii; na jinsi gani watakavyolaaniwa wale ambao watatupwa mahala pao! Na ulimwengu [a]utachomwa kwa moto.

4 Na jinsi gani alivyoturehemu sisi Mungu wetu, kwani anakumbuka nyumba ya [a]Israeli, mizizi pamoja na matawi; na anawanyoshea [b]mikono yake siku yote na ni watu wenye [c]shingo ngumu na ubishi; lakini

75 *b* MWM Israeli.
76 *a* 1 Ne. 22:24–26. MWM Milenia.
77 *a* Ufu. 20:2–10; M&M 29:22–24; 43:29–33; 88:110–116.
b MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.

6 1 *a* Yak. (KM) 5:1.
2 *a* 1 Ne. 22:10–12; M&M 110:11. MWM Urejesho wa Injili.
b Yak. (KM) 5:61.
c 1 Ne. 14:14.
d Yak. (KM) 5:71.
e MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
f 2 Ne. 30:10.
3 *a* 2 Ne. 27:2; Yak. (KM) 5:77; 3 Ne. 25:1.
4 *a* 2 Sam. 7:24.
b Yak. (KM) 5:47.
c Mos. 13:29.

wale wote ambao hawatashupaza mioyo yao wataokolewa katika ufalme wa Mungu.

5 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, ninawasihi kwa maneno ya kiasi kwamba mtubu, na mje kwa moyo wa lengo moja, na [a]mjishikilie kwa Mungu kama vile anavyowashikilia. Na msishupaze mioyo yenu, wakati amewanyoshea [b]mkono wake wa huruma mchana.

6 Ndiyo, leo, kama mtasikia sauti yake, msishupaze mioyo yenu; kwani, kwa nini [a]mfe?

7 Kwani tazama, baada yenu kulishwa kwa neno jema la Mungu kwa siku yote, je, mtazaa matunda maovu, ili [a]mkatwe na kutupwa motoni?

8 Tazameni, je, mtayakataa maneno haya? Je, mtayakataa maneno ya manabii; na je, mtayakataa maneno yote ambayo yamezungumzwa kuhusu Kristo, baada ya wengi sana kuzungumza kumhusu yeye; na kukana neno jema la Kristo, na nguvu ya Mungu, na [a]kipawa cha Roho Mtakatifu, na kuzimisha Roho Mtakatifu, na kufanyia mzaha ule mpango mkuu wa ukombozi, ambao mmepangiwa ninyi?

9 Je, hamjui kwamba mkitenda vitu hivi, kwamba nguvu za ukombozi na ufufuo, ambazo ziko katika Kristo, zitawaleta kusimama katika [a]kiti cha hukumu cha Mungu kwa aibu na [b]hatia kuu?

10 Na kulingana na nguvu za [a]haki, kwani haki haiwezi kuzuiwa, lazima mtupwe kwenye lile [b]ziwa la moto na kiberiti, ambalo ndimi zake za moto hazizimiki, na ambalo moshi wake unapaa juu milele na milele, ambalo ziwa la moto na kiberiti ni [c]mateso [d]yasiyo na mwisho.

11 Ee basi, ndugu zangu wapendwa, tubuni ninyi, na muingie katika [a]mlango uliosonga, na mwendelee katika njia ambayo ni nyembamba, hadi mtakapopokea uzima wa milele.

12 Ee muwe wenye [a]hekima; niseme nini zaidi?

13 Mwishoni, nawaaga kwa heri, hadi nitakapokutana nanyi kwa furaha katika kiti cha enzi cha Mungu, kiti ambacho kinawatia walio waovu woga na hofu ya [a]kutisha. Amina.

MLANGO WA 7

Sheremu anamkana Kristo, anabishana na Yakobo, anadai ishara, na anapigwa na Mungu—Manabii wote wamezungumza kuhusu Kristo na Upatanisho Wake—Wanefi waliishi maisha yao kama wahamaji, wakizaliwa matesoni na kuchukiwa na Walamani. Karibia mwaka 544–421 K.K.

Na sasa ikawa kwamba baada ya miaka kadhaa kupita, pali-

5 *a* MWM Umoja.
b Alma 5:33–34; 3 Ne. 9:14.
6 *a* Eze. 18:21–23.
7 *a* Alma 5:51–52; 3 Ne. 27:11–12.
8 *a* MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
9 *a* MWM Hukumu ya mwisho.
b Mos. 15:26. MWM Hatia.
10 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b 2 Ne. 28:23. MWM Jehanamu.
c MWM Hukumu.
d M&M 19:10–12.
11 *a* 2 Ne. 9:41.
12 *a* Morm. 9:28.
13 *a* Alma 40:14.

tokea mtu miongoni mwa watu wa Nefi, aliyeitwa Sheremu.

2 Na ikawa kwamba alianza kuhubiri miongoni mwa wale watu, na kuwatangazia kwamba hakutakuwa na Kristo. Na akahubiri vitu vingi ambavyo vilikuwa vya kupendeza kwa watu; na alifanya hivi ili apindue mafundisho ya Kristo.

3 Na akatumika kwa bidii ili apotoshe mioyo ya watu, hadi akapotosha mioyo mingi; na yeye akijua kwamba mimi, Yakobo, nilikuwa na imani kwa Kristo atakayekuja, alitafuta nafasi ili anijie.

4 Na alikuwa ameelimika, hata kwamba alifahamu kikamilifu lugha ya wale watu; kwa hivyo, angerairai, na alikuwa na uwezo wa kuzungumza sana, kulingana na nguvu ya ibilisi.

5 Na alikuwa anatumaini kwamba ataniondoa kutoka imani, ingawa nilikuwa na [a]ufunuo mwingi na vitu vingi ambavyo nilikuwa nimeona kuhusu vitu hivi; kwani kwa kweli nilikuwa nimewaona malaika, na walikuwa wamenihudumia. Na pia, nilikuwa nimesikia sauti ya Bwana ikinizungumzia kwa maneno dhahiri, mara kwa mara; kwa hivyo, singetetemeshwa.

6 Na ikawa kwamba alinijia, na akanizungumzia hivi, akisema: Kaka Yakobo, nimetafuta nafasi ili nikuzungumzie; kwani nimesikia na pia ninajua kwamba wewe unasafiri sana, ukihubiri ile ambayo unaiita injili, au mafundisho ya Kristo.

7 Na umepotosha watu hawa wengi kwamba wamegeuza njia ile sawa ya Mungu, na [a]hawatii amri ya Musa ambayo ndiyo njia sawa; na kubadili sheria ya Musa kuwa ibada ya mtu ambaye unasema kwamba atakuja baada ya miaka mia na mia. Na sasa tazama, mimi, Sheremu, nakutangazia wewe kwamba huu ni ukufuru; kwani hakuna mtu anayejua vitu hivi; kwani [b]hawezi kuzungumza kuhusu vitu vile vitakavyokuwepo. Na Sheremu alibishana na mimi katika njia hii.

8 Lakini tazama, Bwana Mungu alinishushia [a]Roho wake katika nafsi yangu, hadi nikamfadhaisha katika maneno yake yote.

9 Na nikamwambia: Je, wewe unamkana Kristo ambaye atakuja? Na akasema: kama Kristo atakuwepo, singemkana; lakini najua kwamba hakuna Kristo, wala hajakuwepo, wala hatakuwepo.

10 Na nikamwambia: Je, wewe unaamini maandiko? Na akasema, Ndiyo.

11 Na nikamwambia: Basi hauyafahamu; kwani yanashuhudia Kristo kwa kweli. Tazama, nakuambia kwamba hakuna manabii walioandika, wala kutoa [a]unabii, bila kuzungumza kuhusu huyu Kristo.

12 Na haya sio yote—imedhi-

7 5*a* 2 Ne. 11:3; Yak. (KM) 2:11.
7*a* Yak. (KM) 4:5.
b Alma 30:13.
8*a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi.
11*a* Ufu. 19:10; 1 Ne. 10:5; Yak. (KM) 4:4; Mos. 13:33–35; M&M 20:26.
MWM Yesu Kristo.

hirishwa kwangu mimi, kwani nimesikia na kuona; na pia imedhihirishwa kwangu kwa [a]nguvu za Roho Mtakatifu; kwa hivyo, najua kama hakuna upatanisho wanadamu wote [b]watapotea.

13 Na ikawa kwamba aliniambia: Nionyeshe [a]ishara kwa nguvu hizi za Roho Mtakatifu ambazo zinakuwezesha kujua haya mengi.

14 Na nikamwambia: Mimi ni nani ili nimjaribu Mungu akuonyeshe ishara kwa kitu unachokijua kwamba ni [a]kweli? Lakini bado wewe unalikana, kwa sababu wewe ni wa [b]ibilisi. Walakini, nia yangu isitendeke; lakini kama Mungu atakupiga, hebu hiyo na iwe ishara kwako kwamba ana nguvu, mbinguni na duniani; na pia, kwamba Kristo atakuja. Na nia yako, Ewe Bwana, itendeke, sio yangu.

15 Na ikawa kwamba wakati mimi, Yakobo, nilizungumza maneno haya, nguvu za Bwana zikamshukia, hadi akainama kwenye ardhi. Na ikawa kwamba alilishwa kwa muda wa siku nyingi.

16 Na ikawa kwamba aliwaambia watu: Kusanyikeni pamoja hapo kesho, kwani nitafariki; kwa hivyo, natamani kuzungumza na watu kabla sijafariki.

17 Na ikawa kwamba umati ulikusanyika pamoja kesho yake; na akazungumza kwao wazi wazi na akakana vile vitu alivyokuwa amewafundisha, na akamkiri Kristo, na nguvu za Roho Mtakatifu, na huduma ya malaika.

18 Na akawazungumzia wazi, kwamba alikuwa [a]amedanganywa na nguvu ya [b]ibilisi. Na akazungumza kuhusu jehanamu, na umilele, na adhabu ya milele.

19 Na akasema: Nahofia kwamba nimetenda [a]dhambi isiyosamehewa, kwani nimesema uwongo mbele ya Mungu; kwani nilimkana Kristo, na nikasema kwamba niliamini maandiko; na kwa kweli yanamshuhudia yeye. Na kwa sababu nimemdanganya Mungu naogopa kwamba hali yangu itakuwa [b]mbaya; lakini ninatubu kwa Mungu.

20 Na ikawa kwamba baada ya kusema maneno haya hakuweza tena kusema mengine, na [a]akafariki.

21 Na umati uliposhuhudia kwamba alizungumza vitu hivi akiwa karibu ya kufariki, walishangazwa sana; hadi nguvu za Mungu zikawashukia, na [a]wakazidiwa na kuinama ardhini.

22 Sasa, kitu hiki kilinifurahisha mimi, Yakobo, kwani nilikuwa nimemwomba Baba yangu aliye mbinguni; kwani

12 *a* MWM Mungu, Uungu—Mungu Roho Mtakatifu; Roho Mtakatifu.
b 2 Ne. 2:21.
13 *a* Mt. 16:1–4; Alma 30:43–60. MWM Ishara.
14 *a* Alma 30:41–42.
b Alma 30:53.
18 *a* Alma 30:53. MWM Danganya, Kudanganya, Udanganyifu.
b MWM Ibilisi.
19 *a* MWM Dhambi isiyo sameheka.
b Mos. 15:26.
20 *a* Yer. 28:15–17.
21 *a* Alma 19:6.

alisikia kilio changu na kujibu sala yangu.

23 Na ikawa kwamba amani na upendo wa Mungu ulirejeshwa tena miongoni mwa watu; na [a]wakasoma maandiko, na hawakutii tena maneno ya huyu mtu mwovu.

24 Na ikawa kwamba mbinu nyingi zilitumiwa [a]kuwarejesha Walamani ili wapate ufahamu wa kweli; lakini yote yalikuwa ni [b]bure, kwani walifurahia [c]vita na umwagaji wa [d]damu, na walikuwa na [e]chuki ya milele kwetu sisi, ndugu zao. Na wakataka kwa uwezo wao wa silaha kutuangamiza daima.

25 Kwa hivyo, watu wa Nefi wakajiimarisha dhidi yao kwa silaha zao, na kwa nguvu zao zote, wakimwamini Mungu na [a]mwamba wa wokovu wao; kwa hivyo, wakawa, washindi wa maadui zao.

26 Na ikawa kwamba mimi, Yakobo, nilianza kuzeeka; na maandishi ya watu hawa yakiwa yameandikwa katika yale [a]mabamba mengine ya Nefi, kwa hivyo, namaliza historia hii, nikikiri kwamba nimeandika kulingana na ufahamu wangu kamili, na kusema kwamba wakati ulipita pamoja nasi, na pia [b]maisha yetu yalipita kama ndoto, sisi tukiwa watu wenye upweke na unadhiri, wahamaji, tuliotupwa nje kutoka Yerusalemu, tukizaliwa kwenye mateso, kwenye nyika, na kuchukiwa na ndugu zetu, ambao walisababisha vita na mabishano; kwa hivyo, tuliomboleza maisha yetu.

27 Na mimi, Yakobo, nikafahamu kwamba lazima hivi karibu niende kaburini; kwa hivyo, nikamwambia mwana wangu [a]Enoshi: Chukua mabamba haya. Na nilimwambia vile vitu ambavyo kaka yangu Nefi [b]aliniamuru, na akaahidi kutii zile amri. Na ninamaliza kuandika katika mabamba haya, uandishi ambao umekuwa mfupi; na kwa msomaji nakuaga kwa heri, nikitumaini kwamba ndugu zangu wengi watasoma maneno haya. Ndugu, Mungu awe nanyi.

KITABU CHA ENOSHI

Enoshi anasali kwa bidii na kupokea msamaha wa dhambi zake—Anaisikia sauti ya Bwana mawazoni mwake ikiahidi wokovu kwa Walamani katika siku za hapo usoni—Wanefi walijaribu kuwakomboa Walamani—Enoshi anamshangilia Mkombozi wake. Karibia mwaka 420 K.K.

23 *a* Alma 17:2.
24 *a* Eno. 1:20.
b Eno. 1:14.
c Mos. 10:11–18.
d Yar. 1:6; Alma 26:23–25.
e 2 Ne. 5:1–3; Mos. 28:2.
25 *a* MWM Mwamba.
26 *a* 1 Ne. 19:1–6; Yar. 1:14–15.
MWM Mabamba.
b Yak. (Bib.) 4:14.
27 *a* Eno. 1:1.
b Yak. (KM) 1:1–4.

TAZAMA, ikawa kwamba mimi, [a]Enoshi, nikijua kwamba Baba yangu [b]alikuwa mtu wa haki—kwani [c]alinifundisha kwa lugha yake, na pia katika [d]malezi na maonyo ya Bwana—na jina la Mungu wangu libarikiwe kwa hayo—

2 Na nitakuelezea kuhusu [a]mweleka ambao niliupata nao mbele ya Mungu, kabla ya kupokea [b]msamaha wa dhambi zangu.

3 Tazama, nilienda kuwinda wanyama porini; na maneno ambayo nilikuwa nimezoea kumsikia baba yangu akizungumza kuhusu uzima wa milele, na [a]shangwe ya watakatifu, [b]yakapenya ndani ya moyo wangu.

4 Na nafsi yangu ikapata [a]njaa; na nikapiga [b]magoti mbele ya Muumba wangu, na nikamlilia kwa [c]sala kuu na nikamsihi kwa nafsi yangu; na kwa siku nzima nikamlilia; ndiyo, na wakati usiku ulipofika bado nilipaza sauti yangu hata ikafika mbinguni.

5 Na [a]sauti ikanijia, ikisema: Enoshi, umesamehewa dhambi zako, na wewe utabarikiwa.

6 Na mimi, Enoshi, nilijua kwamba Mungu hawezi kusema uwongo; kwa hivyo, hatia yangu iliondolewa mbali.

7 Na nikasema: Bwana, je, inafanywa vipi?

8 Na akaniambia: Kwa sababu ya [a]imani yako katika Kristo, ambaye wewe hujamwona kamwe wala kumsikia. Na miaka mingi itapita kabla yeye hajajidhihirisha katika mwili; kwa hivyo, nenda, imani yako imekufanya [b]mkamilifu.

9 Sasa, ikawa kwamba baada ya kusikia maneno haya nilianza [a]kushughulika na ustawi wa ndugu zangu, Wanefi; kwa hivyo, [b]nilimlilia Mungu kwa nafsi yangu yote kwa niaba yao.

10 Na nilipokuwa nikishindana na hivyo rohoni, tazama, sauti ya Bwana ikanijia [a]mawazoni mwangu tena, ikisema: Nitagawanyia ndugu zako kulingana na bidii yao katika kutii amri zangu. [b]Nimewapatia nchi hii, na hii ni nchi takatifu; na siwezi [c]kuilaani ila tu kwa sababu ya dhambi; kwa hivyo, nitagawanyia ndugu zako kulingana na yale ambayo nimesema; na nitawateremshia juu ya vichwa vyao wenyewe huzuni ya dhambi zao.

11 Na baada ya mimi, Enoshi, kusikia maneno haya, imani yangu kwa Bwana ikawa haitikisiki; na nikamwomba kwa

1 1*a* MWM Enoshi, Mwana wa Yakobo.
b 2 Ne. 2:2–4.
c 1 Ne. 1:1–2.
d Efe. 6:4.
2*a* Mwa. 32:24–32; Alma 8:10.
MWM Toba, Tubu.
b MWM Ondoleo la Dhambi.
3*a* MWM Shangwe.
b 1 Ne. 10:17–19; Alma 36:17–21.
4*a* 2 Ne. 9:51; 3 Ne. 12:6.
b MWM Uchaji.
c MWM Sala.
5*a* MWM Ufunuo.
8*a* Eth. 3:12–13.
MWM Amini, Imani.
b Mt. 9:22.
9*a* 1 Ne. 8:12; Alma 36:24.
b 2 Ne. 33:3; M. ya Morm. 1:8; Alma 34:26–27.
10*a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi; Nia.
b 1 Ne. 2:20.
c Eth. 2:7–12.

vilio vingi kwa niaba ya ndugu zangu, Walamani.

12 Na ikawa kwamba baada ya [a]kuomba na kumtumikia kwa bidii, Bwana akaniambia: Kwa sababu ya imani yako, nitakutendea kulingana na [b]mahitaji yako.

13 Na sasa tazama, hii ndiyo ilikuwa tamaa ambayo niliyotamani kutoka kwake—kwamba kama hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa, kwamba watu wangu, Wanefi, wataanguka katika uvunjifu wa sheria, na kwa njia yo yote [a]waangamizwe, na, Walamani wasiangamizwe, kwamba Bwana Mungu [b]angehifadhi kumbu kumbu ya watu wangu, Wanefi; hata kama ni kwa nguvu za mkono wake mtakatifu, ili katika siku za usoni [c]ifunuliwe kwa Walamani, ili, pengine, waweze [d]kuletwa katika wokovu—

14 Kwani kwa sasa majaribio yetu ya kuwarudisha katika imani ya kweli yalikuwa ni [a]bure. Na wakaapa katika hasira zao, kwamba, kama itawezekana, [b]wataangamiza maandishi yetu pamoja nasi, na pia desturi zote za baba zetu.

15 Kwa hivyo, mimi nikijua kwamba Bwana Mungu anaweza [a]kuhifadhi maandishi yetu, nilimlilia sana bila kukoma, kwani alikuwa ameniambia: Chochote utakachoomba kwa imani, ukiamini kwamba utapokea kwa jina la Kristo, utakipokea.

16 Na nilikuwa na imani, na nikamlilia Mungu kwamba [a]angehifadhi yale [b]maandishi; na akaagana na mimi kwamba [c]atayafunua kwa Walamani katika wakati wake.

17 Na mimi, Enoshi, nilijua kwamba itakuwa kulingana na agano alilofanya; kwa hivyo nafsi yangu ikapumzika.

18 Na Bwana akaniambia: Baba zako nao pia wameniomba kitu hiki; na kitatendwa kulingana na imani yao; kwani imani yao ilikuwa kama yako.

19 Na sasa ikawa kwamba mimi, Enoshi, nilienda miongoni mwa watu wa Nefi, nikitoa unabii kuhusu vitu vitakavyokuja, na nikishuhudia kuhusu vitu ambavyo nilikuwa nimevisikia na kuona.

20 Na ninashuhudia kwamba watu wa Nefi walijaribu kwa bidii kuwarejesha Walamani katika imani ya kweli ya Mungu. Lakini [a]kazi zetu zilikuwa bure; na chuki yao ilikuwa imeimarishwa, na walitawaliwa na maumbile yao maovu na wakawa wachokozi, wakali, na watu wapendao

12 *a* Morm. 5:21; 9:36.
b Zab. 37:4; 1 Ne. 7:12; Hel. 10:5.
13 *a* Morm. 6:1, 6.
b M. ya Morm. 1:6–11; Alma 37:2.
c Alma 37:19; Eth. 12:22; M&M 3:18.
d Alma 9:17.
14 *a* Yak. (KM) 7:24.
b Morm. 6:6.
15 *a* MWM Maandiko—Maandiko yahifadhiwe.
16 *a* 3 Ne. 5:13–15; M&M 3:19–20; 10:46–50.
b MWM Kitabu cha Mormoni.
c 2 Ne. 27:6.
20 *a* Moro. 9:6.

[b]umwagaji wa damu na kuabudu [c]sanamu na uchafu; wakila wanyama wa porini; na kuishi katika mahema, na kuzunguka nyikani, na kuvaa ngozi za wanyama viunoni mwao na kunyoa nywele zao; na ustadi wao ulikuwa ni wa [d]upinde, na upanga, na shoka. Na wengi wao hawakula chochote isipokuwa nyama mbichi, na walijaribu kila mara kutuangamiza.

21 Na ikawa kwamba watu wa Nefi walilima ardhi, na [a]kupanda kila aina ya nafaka, na matunda, na makundi ya wanyama, na makundi yote ya kila aina ya ngombe, na mbuzi, na mbuzi wa mwitu, na pia farasi wengi.

22 Na kulikuwa na [a]manabii wengi sana miongoni mwetu. Na watu walikuwa watu wenye [b]shingo ngumu, wagumu katika kufahamu.

23 Na hakukuwa na chochote ila [a]ukali mwingi, [b]mahubiri na kutoa unabii kuhusu vita, na mabishano, na maangamizo, na [c]kuwakumbusha kila mara kuhusu mauti, na kipindi cha umilele, na hukumu na nguvu za Mungu, na hivi vitu vyote—kuwavuruga [d]kila mara ili wamwogope Bwana. Nasema hapakuwa na mambo chini ya vitu hivi, na mazungumzo dhahiri, ili kuwafanya wasiangamie kwa haraka. Na ninaandika jinsi hii juu yao.

24 Na niliona vita vingi miongoni mwa Wanefi na Walamani maishani mwangu.

25 Na ikawa kwamba nilianza kuzeeka, na miaka mia moja, sabini na tisa ilikuwa imepita tangu baba yetu Lehi [a]aondoke Yerusalemu.

26 Na nikaona kwamba ni lazima ninakaribia kuelekea kaburini, nikiwa nimewezeshwa na nguvu za Mungu ili nihubiri na niwatolee watu hawa unabii, na nitangaze neno kulingana na ukweli ulio katika Kristo. Na nimeutangaza katika maisha yangu yote, na nimeufurahia zaidi ya yote ulimwenguni.

27 Na hivi karibuni naelekea mahala pa [a]pumziko langu, ambapo ni pamoja na Mkombozi wangu; kwani najua kwamba nitapumzika na yeye. Na ninafurahia siku ile ambayo huu mwili wenye [b]kutokufa [c]utajivika, na kusimama mbele yake, kisha nitaona uso wake kwa furaha, na ataniambia: Njoo kwangu, heri wewe, umetayarishiwa mahali katika [d]nyumba za Baba yangu. Amina.

---

20 *b* Yar. 1:6.
c Mos. 9:12. MWM Kuabudu sanamu.
d Mos. 10:8.
21 *a* Mos. 9:9.
22 *a* M. ya Morm. 1:16–18.
b Yar. 1:3.
23 *a* 1 Ne. 16:2; 2 Ne. 33:5.
b MWM Hubiri.
c Hel. 12:3.
d Yar. 1:12; Alma 31:5.
25 *a* 1 Ne. 2:2–4.
27 *a* MWM Pumzika.
b MWM Hali ya Kufa, enye Kufa.
c MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
d Yn. 14:2–3; Eth. 12:32–34; M&M 72:4; 98:18.

KITABU CHA YAROMU

Wanefi wanatii sheria ya Musa, wanatazamia kuja kwa Kristo, na wanafanikiwa nchini—Manabii wengi wanatumikia ili kuwafanya watu waishi katika njia ya kweli. Karibia mwaka 399–361 K.K.

SASA tazama, mimi, Yaromu, naandika maneno machache kulingana na amri ya baba yangu, Enoshi, ili [a]nasaba yetu iwekwe.

2 Na kwa vile [a]mabamba haya ni [b]ndogo, na kwa vile vitu hivi [c]vimeandikwa kwa madhumuni ya kuwafaidi ndugu zetu [d]Walamani, kwa hivyo, ni lazima niandike machache; lakini sitaandika vitu kuhusu utoaji wa unabii wangu, wala kuhusu ufunuo wangu. Kwani naweza kuandika nini zaidi ya yale baba zangu waliyoandika? Kwani siwamefunua kuhusu mpango wa wokovu? Nawaambia, Ndiyo; na hii inanitosheleza.

3 Tazama, ni lazima mengi yatendwe miongoni mwa watu hawa, kwa sababu ya [a]ugumu wa mioyo yao; na uziwi wa masikio yao, na upofu wa mawazo yao, na ugumu wa shingo zao; walakini, Mungu anawarehemu sana, na bado [b]hajawaondoa usoni mwa nchi.

4 Na kuna wengi miongoni mwetu ambao wana [a]ufunuo mwingi, kwani sio wote wanye shingo ngumu. Na kwa wale wengi ambao hawana ugumu wa shingo na wana imani, wana [b]ushirika na Roho Mtakatifu, ambaye anawadhihirishia watoto wa watu, kulingana na imani yao.

5 Na sasa, tazama, miaka mia mbili ilikuwa imepita, na watu wa Nefi walikuwa wamepata nguvu katika nchi. Walitia bidii [a]kutii sheria ya Musa na pia siku ya [b]Sabato kuwa takatifu kwa Bwana. Wala [c]hawakutusi; au [d]kukufuru. Na sheria za nchi zilikuwa kali sana.

6 Na walitawanyika sana usoni mwa nchi, na pia Walamani. Na walikuwa ni wengi zaidi ya Wanefi; na walipenda [a]mauaji na hata kunywa damu ya wanyama.

7 Na ikawa kwamba walitushambulia mara nyingi sisi, Wanefi, ili tupigane. Lakini [a]wafalme na viongozi wetu walikuwa ni watu mashujaa kwa imani ya Bwana; na wakafundisha watu njia za Bwana; kwa hivyo, tuliwapiga Walamani na kuwaondoa kutoka nchi [b]yetu, na tukaanza kujenga nyua miji

1 1*a* 1 Ne. 3:12; 5:14.
2*a* Yak. (KM) 3:14; Omni 1:1.
b 1 Ne. 6.
c MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
d 2 Ne. 27:6; Morm. 5:12.
3*a* Eno. 1:22–23.
b Eth. 2:8–10.
4*a* Alma 26:22; Hel. 11:23; M&M 107:18–19.
MWM Ufunuo.
b MWM Roho Mtakatifu.
5*a* 2 Ne. 25:24; Alma 34:13–14.
b Ku. 35:2.
MWM Siku ya Sabato.
c MWM Lugha chafu.
d MWM Kukufuru, Kufuru.
6*a* Yak. (KM) 7:24; Eno. 1:20.
7*a* Yak. (KM) 1:9, 11, 15.
b M. ya Morm. 1:14.

yetu, au mahali popote pa urithi wetu.

8 Na tukaongezeka sana, na tukatawanyika usoni mwa nchi, na tukatajirika sana kwa dhahabu, na kwa fedha, na katika vitu vyenye thamani, na katika kazi nzuri za mbao, katika majengo, na katika mitambo, na pia katika chuma na shaba nyekundu, na shaba nyeupe na chuma, na kutengeneza kila aina ya vyombo vya kulima, na [a]silaha za vita—ndiyo, mshale mkali, na podo, na kiparara, na sagai, na matayarisho yote ya vita.

9 Na hivyo tukiwa tayari kukutana na Walamani, wao hawakufanikiwa dhidi yetu. Lakini neno la Bwana lilithibitishwa, ambalo aliwazungumzia Baba zetu, akisema kwamba: Kadiri mtakavyo tii amri zangu ndivyo mtakavyofanikiwa nchini.

10 Na ikawa kwamba manabii wa Bwana waliwatisha watu wa Nefi, kulingana na neno la Mungu, kwamba kama hawakutii amri, lakini waanguke dhambini, [a]wangeangamizwa kutoka usoni mwa nchi.

11 Kwa hivyo, manabii, na makuhani, na walimu, walitumikia kwa bidii, wakiwaonya watu kwa subira watie bidii; wakifundisha [a]sheria ya Musa, na kwa madhumuni gani ilitolewa; kuwashawishi [b]wamtazamie Masiya, na wamwamini yeye atakayekuja [c]kama vile tayari yuko. Na hivi ndivyo walivyowafundisha.

12 Na ikawa kwamba kwa kufanya hivyo waliwazuia watu [a]wasiangamizwe kutoka usoni mwa nchi; kwani [b]waliwadunga mioyo yao kwa neno, kila mara na kuwavuruga ili watubu.

13 Na ikawa kwamba miaka mia mbili, thelathini na minane ilikuwa imepita—kwa muda mkubwa wa huu wakati kulikuwa na vita, mabishano, na mafarakano.

14 Na mimi, Yaromu, sitaandika mengine, kwani mabamba ni ndogo. Lakini tazameni, ndugu zangu, mnaweza kusoma yale [a]mabamba mengine ya Nefi; kwani tazama, maandishi kuhusu vita vyetu yako humo na yameandikwa, kulingana na maandiko ya wafalme, au yale ambayo waliamuru yaandikwe.

15 Na ninamkabidhi mwana wangu Omni mabamba haya, ili yawekwe kulingana na [a]amri za baba zangu.

8*a* Mos. 10:8.
10*a* 1 Ne. 12:19–20; Omni 1:5.
11*a* Yak. (KM) 4:5; Alma 25:15–16.
b 2 Ne. 11:4; Eth. 12:18–19.
c 2 Ne. 25:24–27; Mos. 3:13; 16:6.
12*a* Eth. 2:10.
b Alma 31:5.
14*a* 1 Ne. 9:2–4.
15*a* Yak. (KM) 1:1–4.

KITABU CHA OMNI

Omni, Amaroni, Kemishi, Abinadomu, na Amaleki, kila mmoja, anaweka yale maandishi—Mosia anavumbua watu wa Zarahemla, ambao walitoka Yerusalemu katika siku za Zedekia—Mosia anafanywa kuwa mfalme wao. Wazao wa Muleki katika Zarahemla walikuwa wamevumbua Koriantumuri, Myaredi wa mwisho—Mfalme Benjamini anamrithi Mosia—Inafaa wanadamu wamtolee Kristo nafsi zao kama sadaka. Karibia mwaka 323–130 K.K.

TAZAMA, ikawa kwamba mimi, Omni, nikiwa nimeamriwa na baba yangu, Yaromu, kwamba niandike kwenye mabamba haya, ili nasaba yetu ihifadhiwe—

2 Kwa hivyo, ningetaka mjue kwamba, katika maisha yangu, nilipigana sana kwa upanga ili kuwahifadhi watu wangu, Wanefi, wasianguke mikononi mwa maadui wao, Walamani. Lakini tazama, mimi mwenyewe ni mtu mwovu, na sijatii amri za Bwana na sheria zake kama vile ilivyonipasa.

3 Na ikawa kwamba miaka mia mbili, sabini na sita ilikuwa imepita, na tulikuwa na vipindi vingi vya amani; na tulikuwa na vipindi vingi vya vita na umwagaji wa damu. Ndiyo, na kwa ufupi, miaka mia mbili, themanini na miwili ilikuwa imepita, na nilikuwa nimeweka mabamba haya kulingana na [a]amri za baba zangu; na nikampatia mwana wangu Amaroni mabamba haya. Na ninakoma hapa.

4 Na sasa mimi, Amaroni, naandika vitu ambavyo ninaandika, ambavyo ni vichache, katika kitabu cha baba yangu.

5 Tazama, na ikawa kwamba miaka mia tatu na ishirini ilikuwa imepita, na sehemu kubwa ya Wanefi waovu [a]ikaangamizwa.

6 Kwani Bwana hangeruhusu, baada ya kuwaongoza kutoka nchi ya Yerusalemu na kuwahifadhi wasianguke mikononi mwa maadui zao, ndiyo, hangekubali kwamba yale maneno ambayo aliwaambia baba zetu, yasithibitishwe, akisema kwamba: Msipotii amri zangu hamtafanikiwa nchini.

7 Kwa hivyo, Bwana aliwaadhibu kwa hukumu kuu; walakini, aliwaokoa wenye haki kwamba wasiangamie, lakini aliwakomboa kutoka mikononi mwa maadui zao.

8 Na ikawa kwamba nilimpatia Kemishi kaka yangu yale mabamba.

9 Sasa mimi, Kemishi, naandika vitu vichache, katika kitabu sawa na kaka yangu; kwani tazama, niliona ya mwisho aliyoandika, kwamba aliandika kwa mkono wake mwenyewe; na aliyaandika siku ile aliyonipatia. Na tunaweka maandishi katika njia hii, kwani ni kulingana

1 3*a* Yak. (KM) 1:1–4; Yar. 1:15. 5*a* Yar. 1:9–10.

na amri za baba zetu. Na ninakoma hapo.

10 Tazama, mimi, Abinadomu, ni mwana wa Kemishi. Tazama, ikawa kwamba mimi niliona vita vingi na ubishi kati ya watu wangu, Wanefi, na Walamani; na mimi, kwa upanga wangu mwenyewe, nimeondoa maisha ya Walamani wengi kwa ulinzi wa ndugu zangu.

11 Na tazama, maandishi ya watu hawa yameandikwa katika mabamba ambayo yamekuwa na wafalme, kulingana na vizazi; na sijui ufunuo wowote ambao haujaandikwa, wala unabii; kwa hivyo, yaliyoandikwa yametosha. Na ninakoma hapo.

12 Tazama, mimi ni Amaleki, mwana wa Abinadomu. Tazama, nitawazungumzia kuhusu Mosia, ambaye alitawazwa mfalme katika nchi ya Zarahemla; kwani tazama, yeye akiwa ameonywa na Bwana kwamba atoroke kutoka nchi ya [a]Nefi, na wale wengi watakaotii sauti ya Bwana pia nao [b]waondoke nchini na yeye, na waelekee nyikani—

13 Na ikawa kwamba alitenda kulingana na vile Bwana alivyomwamuru. Na walitoka nchi ile na kuelekea nyikani, wote ambao walisikiliza sauti ya Bwana; na waliongozwa kwa mahubiri mengi na unabii. Na wakaonywa kila mara kwa neno la Mungu; na waliongozwa kwa nguvu za mkono wake, huko nyikani hadi wakafika katika nchi inayoitwa nchi ya Zarahemla.

14 Na wakawavumbua watu, walioitwa watu wa [a]Zarahemla. Sasa, kulikuwa na furaha kuu miongoni mwa watu wa Zarahemla; na pia Zarahemla alifurahi sana, kwa sababu Bwana alikuwa ametuma watu wa Mosia pamoja na [b]mabamba ya shaba nyeupe ambayo yalikuwa na maandishi ya Wayahudi.

15 Tazama, na ikawa kwamba Mosia alivumbua kuwa [a]watu wa Zarahemla waliondoka Yerusalemu wakati [b]Zedekia, mfalme wa Yuda, alipohamishwa Babilonia utumwani.

16 Na wakasafiri nyikani, na wakavushwa kwa mkono wa Bwana katika yale maji makuu, hadi katika nchi ile ambayo Mosia aliwavumbua, na wakaishi katika nchi ile tangu tangu wakati ule na kuendelea.

17 Na ule wakati Mosia alipowavumbua, walikuwa wamekuwa wengi sana. Walakini, walikuwa wamekuwa na vita vingi na mabishano makubwa, na walikuwa wameanguka kwa upanga mara kwa mara; na lugha yao ilikuwa imechafuka; na hawakuwa wamebeba [a]maandishi yoyote; na walikana uwepo wa Muumba wao; na Mosia, wala watu wa Mosia, hawakuweza kuwaelewa.

18 Lakini ikawa kwamba Mosia akasababisha kwamba wafundishwe kwa lugha yake. Na

12*a* 2 Ne. 5:6–9.
b Yak. (KM) 3:4.
14*a* MWM Zarahemla.
b 1 Ne. 3:3, 19–20; 5:10–22.
15*a* Mos. 25:2.
b Yer. 39:1–10; Hel. 8:21.
17*a* Mos. 1:2–6.

ikawa kwamba baada ya kufundishwa lugha ya Mosia, Zarahemla akatoa nasaba ya baba zake, kulingana na ukumbuko wake; na yameandikwa, lakini sio katika mabamba haya.

19 Na ikawa kwamba watu wa Zarahemla, na watu wa Mosia, [a]waliungana pamoja; na [b]Mosia akateuliwa kuwa mfalme wao.

20 Na ikawa kwamba katika siku za Mosia, aliletewa jiwe kubwa lililokuwa na maandishi juu yake; na [a]akatafsiri hayo maandishi kwa karama na nguvu za Mungu.

21 Na yalieleza historia ya mmoja aliyeitwa [a]Koriantumuri, na mauaji ya watu wake. Na Koriantumuri alivumbuliwa na watu wa Zarahemla; na akaishi nao kwa muda wa miezi tisa.

22 Na pia ilizungumza maneno machache kuhusu babu zake. Na wazazi wake wa kwanza walitoka katika ule [a]mnara, wakati Bwana [b]alipochanganya lugha za watu; na mapigo ya Bwana yaliwashukia kulingana na hukumu zake, ambazo ni za haki; na [c]mifupa yao ilitawanyika katika nchi za kaskazini.

23 Na tazama, mimi, Amaleki, nilizaliwa katika siku za Mosia; na nimeishi kuona kifo chake; na mwana wake, [a]Benjamini anatawala mahali pake.

24 Na tazama, nimeona, katika siku za mfalme Benjamini, vita vikali na umwagaji wa damu miongoni mwa Wanefi na Walamani. Lakini tazama, Wanefi walipata ushindi juu yao; ndiyo, hadi mfalme Benjamini akawafukuza kutoka nchi ya Zarahemla.

25 Na ikawa kwamba nilianza kuzeeka; na nikiwa sina uzao, na nikijua kwamba mfalme [a]Benjamini alikuwa mwenye haki kwa Bwana, kwa hivyo, [b]nitamkabidhi mabamba haya, nikiwasihi wanadamu wote wamjie Mungu, yule Mtakatifu wa Israeli, na kuamini katika unabii, na katika ufunuo, na kuhudumu kwa malaika, na katika kipawa cha kunena kwa ndimi, na katika kipawa cha kutafsiri ndimi, na katika vitu vyote vilivyo [c]vyema; kwani hakuna lolote jema lisilotokana na Bwana: na kwamba yale yaliyo maovu yanatokana na ibilisi.

26 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, natamani [a]mje kwa Kristo, ambaye ni Mtakatifu wa Israeli, na mpokee wokovu wake, na nguvu za ukombozi wake. Ndiyo, njooni kwake, na [b]mumtolee nafsi zenu kama [c]sadaka kwake, na muendelee katika [d]kufunga na kusali, na kuvumilia hadi mwisho; na kama vile Bwana anavyoishi mtaokolewa.

19 *a* Mos. 25:13.
b Omni 1:12.
20 *a* Mos. 8:13–19.
MWM Mwonaji.
21 *a* Eth. 12:1.
MWM Koriantumuri.
22 *a* Eth. 1:1–5.
b Mwa. 11:6–9; Mos. 28:17; Eth. 1:33.
c Mos. 8:8.
23 *a* M. ya Morm. 1:3.
25 *a* M. ya Morm. 1:17–18; Mos. 29:13.
b M. ya Morm. 1:10.
c Alma 5:40; Eth. 4:12; Moro. 7:15–17.
26 *a* Yak. (KM) 1:7; Alma 29:2; Moro. 10:32.
b MWM Dhabihu.
c 3 Ne. 9:20.
d MWM Funga, Kufunga.

27 Na sasa nitazungumza machache kuhusu wengine walioelekea nyikani ili kurejea katika nchi ya Nefi; kwani kulikuwa na wengi waliotamani kumiliki nchi yao ya urithi.

28 Kwa hivyo, walielekea nyikani. Na kiongozi wao akiwa mtu mwenye nguvu na shujaa, na mtu mwenye shingo ngumu, kwa hivyo alisababisha ubishi miongoni mwao; na wote [a]wakauawa, huko nyikani, isipokuwa hamsini, na wakarejea katika nchi ya Zarahemla.

29 Na ikawa kwamba waliwachukua wengine pia, na wakaelekea katika safari nyingine huko nyikani.

30 Na mimi, Amaleki, nilikuwa na kaka yangu, ambaye pia alienda pamoja nao; na tokea hapo sijajua lolote juu yao. Na sasa ninakaribia kulala katika kaburi langu; na [a]mabamba haya yamejaa. Na ninamaliza mazungumzo yangu.

MANENO YA MORMONI

Mormoni anafupisha mabamba makubwa ya Nefi—Anaweka mabamba yale madogo na mabamba yale mengine—Mfalme Benjamini anaimarisha amani nchini. Karibia mwaka 385 B.K.

NA sasa mimi, [a]Mormoni, nikikaribia kuyakabidhi yale maandishi ambayo nimeandika mikononi mwa mwana wangu Moroni, tazama nimeshuhudia karibu maangamizo yote ya watu wangu, Wanefi.

2 Na ni baada ya miaka mia [a]kadha baada ya kuja kwa Kristo ninapompatia mwana wangu maandishi haya; na ninadhani kwamba atashuhudia maangamizo yote ya watu wangu. Lakini na Mungu amjalie aweze kuishi, ili aandike juu yao, na kwa vyovyote kuhusu Kristo, ili pengine [b]wafaidike katika nyakati zingine.

3 Na sasa, ninazungumza kuhusu yale ambayo nimeandika; kwani baada ya kufanya [a]ufupisho kutoka yale [b]mabamba ya Nefi, hadi utawala wa huyu mfalme Benjamini, ambaye alizungumziwa na Amaleki, nilipekua miongoni mwa [c]maandishi haya niliyopewa, na nikapata mabamba haya, ambayo yalikuwa na historia hii ndogo ya manabii, kutoka Yakobo hadi utawala huu wa mfalme [d]Benjamini, na pia maneno mengi ya Nefi.

28 *a* Mos. 9:1–4.
30 *a* 1 Ne. 6.

[Maneno ya Mormoni]
1 1 *a* 3 Ne. 5:9–12; Morm. 1:1–4; 8:1, 4–5.
MWM Mormoni, Nabii Mnefi.
2 *a* Morm. 6:5–6.
b M&M 3:16–20.
3 *a* M&M 10:44.
b M&M 10:38–40.
c Mos. 1:6; Hel. 3:13–15; Morm. 4:23.
d Omni 1:23.

4 Na vitu ambavyo vimo katika mabamba haya [a]vinanifurahisha, kwa sababu ya unabii wa kuja kwa Kristo; na baba zangu wakijua kwamba vingi vimetimizwa; ndiyo, na pia najua kwamba vingi vilivyobashiriwa kutuhusu sisi hadi siku hii vimetimizwa, na vingi ambavyo vitazidi leo lazima kwa ukweli vitatokea—

5 Kwa hivyo, nachagua [a]vitu hivi, ili nimalize maandishi yangu juu yao, maandishi ambayo nitatoa kutoka [b]mabamba ya Nefi; na siwezi kuandika hata sehemu moja ya [c]mia ya vitu vya watu wangu.

6 Lakini tazama, nitachukua mabamba haya, ambayo yana unabii na ufunuo, na kuyaweka pamoja na mabaki ya yale maandishi yangu, kwani ni bora kwangu; na ninajua kwamba yatakuwa bora kwa ndugu zangu.

7 Na ninatenda haya kwa madhumuni ya [a]busara; kwani ninanong'onezewa, kulingana na kazi za Roho wa Bwana aliye ndani yangu. Na sasa, sijui mambo yote; lakini Bwana [b]anajua vitu vyote vitakavyokuja; kwa hivyo, anafanya kazi ndani yangu ili nitende kulingana na nia yake.

8 Na [a]sala yangu kwa Mungu ni kuhusu ndugu zangu, kwamba wamfahamu Mungu tena, ndiyo, ukombozi wa Kristo; ili tena wawe watu [b]wema.

9 Na sasa mimi, Mormoni, namalizia maandishi yangu, ambayo ninayatoa kutoka mabamba ya Nefi; na ninayaandika kulingana na maarifa na ufahamu ambao Mungu amenipatia.

10 Kwa hivyo, ikawa kwamba baada ya Amaleki [a]kumpatia mfalme Benjamini mabamba haya, aliyachukua na kuyaweka pamoja na yale [b]mabamba mengine, ambayo yalikuwa na maandishi ambayo yalitolewa na [c]wafalme, kutoka kizazi hadi kizazi mpaka siku za Benjamini.

11 Na yalipitishwa kutoka mfalme Benjamini, kutoka kizazi hadi kizazi mpaka zikafika [a]mikononi mwangu. Na mimi, Mormoni, naomba Mungu kwamba yahifadhiwe tangu sasa. Na ninajua kwamba yatahifadhiwa; kwani kuna mambo makuu ambayo yameandikwa juu yake, ambayo [b]yatahukumu watu wangu na ndugu zao katika siku ile kuu ya mwisho, kulingana na neno la Mungu ambalo limeandikwa.

12 Na sasa, kuhusu huyu mfalme Benjamini—alikuwa na mabishano fulani miongoni mwa watu wake.

13 Na ikawa kwamba pia majeshi ya Walamani yaliondoka [a]nchi ya Nefi, ili yapigane na

4 *a* 1 Ne. 6:5.
5 *a* MY mambo yanayomfurahisha, yametajwa katika aya ya 4.
b 1 Ne. 9:2.
c 3 Ne. 5:8–11; 26:6–12.
7 *a* 1 Ne. 9:5; 19:3; M&M 3:12–20; 10:1–19, 30–47.
b MWM Kujua yote.
8 *a* 2 Ne. 33:3–4; Eno. 1:11–12.
b 2 Ne. 30:6.
10 *a* Omni 1:25, 30.
b 1 Ne. 9:4.
c Yar. 1:14.
11 *a* 3 Ne. 5:8–12; Morm. 1:1–5.
b 2 Ne. 25:18; 29:11; 33:11–15; 3 Ne. 27:23–27.
13 *a* Omni 1:12.

watu wake. Lakini tazama, mfalme Benjamini alikusanya pamoja majeshi yake, na akawapinga; na alipigana kwa nguvu ya mkono wake mwenyewe, akitumia [b]upanga wa Labani.

14 Na kwa nguvu za Bwana walipigana dhidi ya maadui wao, hadi wakawaua maelfu mengi ya Walamani. Na ikawa kwamba walipigana na Walamani hadi wakawaondoa kutoka nchi yao yote ya urithi wao.

15 Na ikawa kwamba baada ya kuwa na [a]Kristo wengi bandia, na vinywa vyao vikafungwa, na wakaadhibiwa kulingana na makosa yao;

16 Na baada ya kuwepo na manabii wa bandia, na wahubiri bandia na walimu bandia miongoni mwa watu, na hawa wote wakiwa wameadhibiwa kulingana na makosa yao; na baada ya kuwepo na ubishi mwingi na ukengeufu mwingi kwa Walamani, tazama, ikawa kwamba mfalme Benjamini, kwa msaada wa [a]manabii watakatifu waliokuwa miongoni mwa watu wake—

17 Kwani tazama, mfalme Benjamini alikuwa mtu [a]mtakatifu, na alitawala watu wake kwa haki; na kulikwa na watu wengi watakatifu nchini ile, na walinena neno la Mungu kwa [b]nguvu na mamlaka; na walitumia [c]ukali mwingi kwa sababu ya utukutu wa wale watu—

18 Kwa hivyo, kwa msaada wa hawa, mfalme Benjamini, kwa kutumikia kwa nguvu zote za mwili wake na uwezo wa nafsi yake yote, na pia manabii, aliimarisha tena amani katika nchi ile.

KITABU CHA MOSIA

MLANGO WA 1

Mfalme Benjamini anafundisha wanawe lugha na unabii wa babu zao—Dini yao na utamaduni wao zimehifadhiwa kwa sababu ya maandishi yaliyowekwa kwenye mabamba mbali mbali—Mosia anateuliwa kuwa mfalme na kupewa jukumu la kuhifadhi yale maandishi na vitu vingine. Karibia mwaka 130–124 K.K.

NA sasa kulikuwa hakuna ubishi katika [a]nchi yote ya Zarahemla, miongoni mwa watu wote wa mfalme Benjamini, hata kwamba mfalme Benjamini akawa na amani katika siku zake zote zilizo salia.

2 Na ikawa kwamba alipata wana watatu; na akawaita majina yao, Mosia, na Helorumu, na Helamani. Na akasababisha kwamba [a]wafundishwe kwa

13 *b* 1 Ne. 4:9; 2 Ne. 5:14; Yak. (KM) 1:10; Mos. 1:16; M&M 17:1.
15 *a* MWM Mpinga Kristo.
16 *a* Eno. 1:22.
17 *a* Alma 13:26.
b Alma 17:2–3.
c Moro. 9:4; M&M 121:41–43.

[MOSIA]
1 1 *a* Omni 1:13.
2 *a* Mos. 4:14–15; M&M 68:25, 28.

[b]lugha yote ya babu zake, ili wawe watu wenye ufahamu; na ili wajue kuhusu unabii uliokuwa umezungumzwa kwa vinywa vya babu zao, ambao ulikuwa umetolewa na mkono wa Bwana.

3 Na pia akawafundisha kuhusu kumbukumbu ambazo zilikuwa zimechorwa kwenye yale mabamba ya shaba nyeupe, akisema: Wana wangu, nataka mkumbuke kwamba kama sio [a]mabamba haya, ambayo yana kumbukumbu hizi na amri hizi, lazima tungeteseka kwa [b]kutojua, mpaka wakati huu, kwa kutojua siri za Mungu.

4 Kwani haingewezekana kwamba baba yetu Lehi, angevikumbuka vitu hivi vyote, kuvifundisha kwa watoto wake, bila usaidizi wa mabamba haya; kwani yeye alikuwa amefundishwa kwa [a]lugha ya Wamisri kwa hivyo yeye aliweza kusoma michoro hii, na kuwafundisha watoto wake, ili nao wawafundishe watoto wao, na hivyo kutimiza amri za Mungu, hadi wakati huu.

5 Nawaambia, wana wangu, kama sio kwa sababu ya vitu hivi, ambavyo vimewekwa na [a]kuhifadhiwa kwa mkono wa Mungu, ili [b]tusome na tufahamu [c]siri zake, na tuwe na amri zake kila mara machoni mwetu, hata kwamba baba zetu wangefifia katika kutoamini, na tungekuwa kama ndugu zetu, Walamani, ambao hawajui lolote kuhusu vitu hivi, au hata kwamba hawaviamini wanapofundishwa, kwa sababu ya [d]desturi za baba zao, ambazo sio sawa.

6 Enyi wana wangu, ningependa mkumbuke kwamba hii misemo ni ya kweli, na pia kwamba maandishi haya ni ya [a]kweli. Na tazama, pia mabamba ya Nefi, ambayo yana maandishi na misemo ya baba zetu tangu walipotoka Yerusalemu hadi sasa, na ni za kweli; na tunaweza kujua ukweli wao kwa sababu ziko mbele machoni mwetu.

7 Na sasa, wana wangu, ningependa kwamba [a]myapekue kwa bidii, ili mfaidike; na ningependa kwamba [b]mtii amri za Mungu, ili [c]mfanikiwe nchini kulingana na [d]ahadi ambazo Bwana aliwafanyia babu zetu.

8 Na ni vitu vingi zaidi ambavyo mfalme Benjamini aliwafundisha wanawe, ambavyo havijaandikwa kwenye kitabu hiki.

9 Na ikawa kwamba baada ya mfalme Benjamini kumaliza kuwafundisha wanawe, kwamba alizeeka, na akaona kwamba lazima hivi karibuni aelekee katika ile njia ya ulimwengu wote; kwa hivyo,

2 *b* Morm. 9:32.
3 *a* MWM Mabamba.
b Alma 37:8–9.
4 *a* JS—H 1:64.
5 *a* MWM Maandiko—Maandiko yahifadhiwe.
b Kum. 6:6–8.
c MWM Siri za Mungu.
d Mos. 10:11–17.
6 *a* 1 Ne. 1:3; 2 Ne. 33:10–11; Moro. 10:27.
7 *a* MWM Maandiko.
b Mos. 2:22; Alma 50:20–22.
c Zab. 122:6; 1 Ne. 2:20.
d Alma 9:12–14.

akadhani kwamba ni muhimu aukabidhi ufalme wake kwa mmoja wa wanawe.

10 Kwa hivyo, akasababisha Mosia asimamishwe mbele yake; na haya ndiyo maneno ambayo alimzungumzia, akisema: Mwana wangu, nataka utangaze kote nchini hii miongoni mwa watu hawa wote, au [a]watu wa Zarahemla, na watu wa Mosia ambao wanaishi katika nchi hii, kwamba wakusanyike pamoja; kwani kesho nitawatangazia watu wangu kwa kinywa changu kwamba wewe ni [b]mfalme na mtawala juu ya hawa watu, ambao Bwana Mungu wetu ametupatia.

11 Na juu ya hayo, nitawapatia watu hawa [a]jina, ili waweze kutofautishwa kutokana na watu wote ambao Bwana Mungu aliwatoa kutoka nchi ya Yerusalemu; na hivi ninatenda kwa sababu wamekuwa watu wa bidii kwa kutii amri za Bwana.

12 Na ninawapa jina ambalo halitafutwa, ila tu kwa [a]dhambi.

13 Ndiyo, na zaidi ninakwaambia, kwamba ikiwa watu hawa walioheshimiwa na Bwana zaidi wataanguka kwenye [a]dhambi, na wawe waovu na watu wazinifu, kwamba Bwana atawatoa, ili wawe [b]wanyonge kama ndugu zao; na [c]hatawalinda tena kwa nguvu zake zisizokuwa na kipimo; kama vile alivyowahifadhi babu zetu.

14 Kwani ninakwambia, kwamba kama hangenyosha mkono wake kuwahifadhi babu zetu lazima wangeanguka mikononi mwa Walamani, na waumie kwa sababa ya chuki yao.

15 Na ikawa kwamba baada ya mfalme Benjamini kumaliza kumzungumzia mwana wake, kwamba aliweka mikononi mwake mambo yote ya ufalme.

16 Na zaidi ya hayo, aliweka mikononi mwake kuhusu zile kumbukumbu ambazo ziliyochorwa kwenye [a]mabamba ya shaba nyeupe; na pia mabamba ya Nefi; na pia, [b]upanga wa Labani, na [c]mpira au kielekezo, ambacho kiliwaelekeza babu zetu kupita nyikani, ambacho kilitayarishwa na mkono wa Bwana ili waelekezwe, kila mmoja kulingana na utiifu na bidii waliompatia.

17 Kwa hivyo, kwa vile hawakuwa waaminifu hawakufanikiwa wala kuendelea katika safari yao, lakini [a]walirudishwa nyuma, na kujiteremshia hasira ya Mungu juu yao; na kwa hivyo walipigwa kwa njaa na maumivu makali, ili kuwavuruga wakumbuke jukumu lao.

18 Na sasa, ikawa kwamba Mosia alienda na kutenda kulingana na yale baba yake aliyomwamuru, na kuwatangazia watu wote waliokuwa katika nchi ya Zarahemla kwamba

10 *a* Omni 1:14.
b Mos. 2:30.
11 *a* Mos. 5:8–12.
12 *a* MWM Dhambi.
13 *a* Ebr. 6:4–6.
b Hel. 4:24–26.
c M&M 103:8–10.
16 *a* Mos. 1:3.
b 1 Ne. 4:8–19; M. ya Morm. 1:13; M&M 17:1.
c 1 Ne. 16:10.
17 *a* 1 Ne. 18:12–13.

wajikusanye pamoja, ili waende kwenye hekalu kusikiliza maneno ambayo baba yake atawazungumzia.

MLANGO WA 2

Mfalme Benjamini anahutubia watu wake—Anawakumbusha kuhusu haki, wema, na ustawi wa kiroho wa utawala wake—Anawashauri wamtumikie Mfalme wao wa Mbinguni—Wale ambao wanamuasi Mungu, watateseka kwa huzuni iliyo kama moto usiozimika. Karibia mwaka 124 K.K.

Na ikawa kwamba baada ya Mosia kutenda kulingana na vile baba yake alivyomwamuru, na kutangaza nchini kote, kwamba watu walikusanyika pamoja nchini kote, ili waende kwenye hekalu kusikia maneno ambayo mfalme Benjamini atawaelezea.

2 Na walikuwa idadi kubwa, hata kuwa wengi sana kwamba hawakuhesabika; kwani walikuwa wameongezeka zaidi na kuwa wengi katika nchi.

3 Na pia walichukua [a]malimbuko ya mifugo yao, ili watoe [b]dhabihu na [c]sadaka za kuteketezwa kwa moto [d]kulingana na sheria ya Musa;

4 Na pia kwamba wamtolee Bwana Mungu wao shukrani, ambaye alikuwa amewaleta kutoka nchi ya Yerusalemu, na ambaye alikuwa amewakomboa kutoka mikono ya maadui zao, na [a]kuwachagulia watu wenye haki kuwa [b]walimu wao, na pia mtu mwenye haki kuwa mfalme wao, ambaye alikuwa ameanzisha amani katika [c]nchi ya Zarahemla, na ambaye aliwafundisha [d]kutii amri za Mungu, ili washangilie na kujazwa na [e]upendo kwa Mungu na kwa watu wote.

5 Na ikawa kwamba walipowasili kwenye hekalu, walipiga hema zao kando yake, kila mtu kulingana na [a]jamii yake, akiwa na mke wake, na wanawe, na mabinti zake, na wana wao, na mabinti zao, kutoka mkubwa hadi kwa aliye mdogo, kila jamii ikiwa imetengana na nyingine.

6 Na wakapiga hema zao na kuizingira hekalu, kila mtu akielekeza mlango wa [a]hema lake kwenye hekalu, ili wakae ndani ya hema zao na kusikia maneno ambayo mfalme Benjamini angewazungumzia;

7 Kwani umati ulikuwa mkubwa sana hata kwamba mfalme Benjamini hangeweza kuwafundisha wote katika kuta za hekalu, kwa hivyo akaamuru mnara ujengwe, ili watu wake wasikie maneno ambayo angewazungumzia.

8 Na ikawa kwamba alianza kuwazungumzia watu wake kutoka mnarani; na wote hawangeweza kusikia maneno

2 3*a* Mwa. 4:4.
b MWM Dhabihu.
c 1 Ne. 5:9.
d 2 Ne. 25:24; Alma 30:3; 34:13–14.
4*a* MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
b Mos. 18:18–22. MWM Fundisha, Mwalimu.
c Omni 1:12–15.
d Yn. 15:10.
e MWM Upendo.
5*a* MWM Familia.
6*a* Ku. 33:8–10.

yake kwa sababu ya wingi wa umati; kwa hivyo akasababisha kwamba maneno aliyozungumza yaandikwe na kupelekwa miongoni mwa wale ambao hawakuwa karibu na sauti yake, ili wao pia wapokee maneno yake.

9 Na haya ndiyo maneno [a]aliyozungumza na kusababisha yaandikwe, akisema: Ndugu zangu, nyote ambao mmekusanyika pamoja, ninyi ambao mtasikia maneno yangu ambayo nitawazungumzia leo; kwani sijawaamrisha kuja hapa ili [b]kuchezacheza na maneno ambayo nitawazungumzia, lakini kwamba [c]mnisikilize, na mfungue masikio yenu ili msikie, na [d]mioyo yenu ili mfahamu, na [e]akili zenu ili [f]siri za Mungu zifunguliwe machoni mwenu.

10 Sijawaamuru kuja hapa ili [a]mniogope, au kwamba mnidhanie kwamba mimi mwenyewe ni zaidi ya binadamu.

11 Lakini mimi niko kama ninyi, kwa unyonge wa kila aina mwilini na akilini; walakini nimechaguliwa na watu hawa, na kutakaswa na baba yangu, na nikaruhusiwa kwa mkono wa Bwana kwamba niwe mtawala na mfalme wa watu hawa; na nimelindwa na kuhifadhiwa kwa uwezo wake usio na kipimo, ili niwatumikie kwa uwezo wote, na nguvu ambazo Bwana amenipatia.

12 Ninawaambia kwamba kwa vile nimekubaliwa kuwatumikia ninyi maishani mwangu, hata hadi sasa, na sijatazamia kupata faida ya [a]dhahabu au fedha au aina yoyote ya utajiri kutoka kwenu;

13 Wala sijaruhusu kwamba mfungwe gerezani, wala ninyi wenyewe kuwafanya wengine watumwa, wala kuua, au kupora, au kuiba, au kuzini; wala hata mimi sijawaruhusu kwamba mtende aina yoyote ya uovu, na nimewafundisha ninyi kwamba mtii amri za Bwana, katika vitu vyote ambavyo amewaamuru—

14 Na hata mimi, mwenyewe, [a]nimefanya kazi kwa mikono yangu mwenyewe ili niwatumikie ninyi, na kwamba msilemewe na makodi, na kwamba msipatwe na chochote ambacho hamuwezi kuvumilia—na ninyi ni mashahidi leo, kwa vitu vyote ambavyo nimewazungumzia siku hii.

15 Lakini, ndugu zangu, sijatenda vitu hivi ili nijivune, wala sisemi vitu hivi ili niwalaumu; lakini nawaambia vitu hivi ili mjue kwamba sina lawama katika [a]dhamira yangu mbele ya Mungu siku ya leo.

16 Tazama, nawaambia kwamba kwa sababu niliwaambia kuwa nimewatumikia maishani mwangu, sitamani kujivuna, kwani nimekuwa tu katika utumishi wa Mungu.

9 *a* Mos. 8:3.
b M&M 6:12.
c MWM Sikiliza.
d Mos. 12:27; 3 Ne. 19:33.
e MWM Nia.
f MWM Siri za Mungu.
10 *a* MWM Hofu.
12 *a* Mdo. 20:33–34.
14 *a* 1 Kor. 9:18.
15 *a* MWM Dhamiri.

17 Na tazama, nawaambia vitu hivi ili mpate [a]hekima; ili mjifunze kwamba [b]mnapowatumikia wanadamu [c]wenzenu mnamtumikia tu Mungu wenu.

18 Tazama, mmeniita mfalme wenu; na kama mimi, ambaye mnaniita mfalme wenu, ninajichosha [a]kuwatumikia, je, haiwapasi nanyi kujichosha kutumikiana?

19 Na tazama pia, kama mimi, ambaye mnaita mfalme wenu, ambaye amewatumikia siku zake zote ninyi, na walakini amekuwa katika utumishi wa Mungu, ninastahili shukrani kutoka kwenu, Je, inawapasa jinsi gani ninyi [a]kumshukuru Mfalme wenu wa mbinguni!

20 Ninawaambia, ndugu zangu, kwamba kama mtamtolea shukrani zote na [a]sifa ambazo nafsi zenu zote zina uwezo wa kuwa nazo, [b]Mungu aliyewaumba, na aliyewaweka na kuwahifadhi, na kuwasababisha ninyi kufurahi, na kuwezesha kwamba ninyi muishi kwa amani kati yenu—

21 Ninawaambia kwamba kama mtamtumikia yule ambaye aliwaumba tangu mwanzo, na anawahifadhi siku kwa siku, kwa kuwaazima pumzi, kwamba muishi na mtembee na kutenda kulingana na [a]nia zenu, na hata kuwasaidia muda kwa muda—nasema, kama mtamtumikia kwa nafsi zenu zote kwa jumla bado mtakuwa watumishi [b]wasioleta faida.

22 Na tazama, yote ambayo anahitaji kutoka kwenu ni [a]kutii [b]amri zake; na amewaahidi kwamba kama mtatii amri zake mtafanikiwa nchini; na kamwe [c]hageuki kutoka kwa yale aliyosema; kwa hivyo, kama [d]mtatii amri zake atawabariki na kuwafanikisha.

23 Na sasa, kwanza, amewaumba, na kuwapatia uhai wenu, ambao anawadai.

24 Na cha pili, anahitaji kwamba ninyi mtende yale ambayo amewaamuru; kwani kama mtatenda hivyo, [a]atawabariki papo hapo; na kwa hivyo amewalipa. Na hivyo basi bado anawadai, na hata sasa, na baadaye hadi milele na milele; kwa hivyo, je, mna nini ambacho mnajivunia?

25 Na sasa nauliza, je mnaweza kujiongezea chochote wenyewe? Ninawajibu, Hapana. Hamwezi kusema mko hata kuzidi mavumbi ya dunia; ingawa [a]mliumbwa kutoka [b]mavumbi ya dunia; lakini tazama, ni yake yule aliyewaumba.

26 Na mimi, hata mimi, ambaye mnaniita mfalme wenu,

17 *a* MWM Hekima.
b Mt. 25:40; Yak. (Bib.) 1:27; M&M 42:29–31. MWM Utumishi.
c MWM Dada; Kaka, Ndugu.
18 *a* Mt. 20:26–27.
19 *a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
20 *a* 1 Ne. 18:16.
b MWM Mungu, Uungu.
21 *a* MWM Haki ya uamuzi.
b Lk. 17:7–10.
22 *a* Law. 25:18–19; 2 Ne. 1:9.
b MWM Amri za Mungu.
c M&M 3:1–2.
d M&M 14:7; 58:2–3.
24 *a* MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
25 *a* MWM Umba, Uumbaji.
b Mwa. 3:19; Yak. (KM) 2:21.

sio bora zaidi ya vile mlivyo; kwani mimi pia nilitoka katika mavumbi. Na mnaona kwamba mimi ni mzee, na ninakaribia kuupeleka mwili huu kwenye udongo.

27 Kwa hivyo, kama vile nilivyowaambia kwamba niliwatumikia, [a]nikiwa na dhamira iliyo safi kwa Mungu, hata hivyo wakati huu mimi nimesababisha kwamba mkusanyike pamoja, ili nisipatikane na lawama, na kwamba [b]damu yenu isiwe juu yangu, nitakaposimama mbele ya Mungu ili nihukumiwe kwa vile vitu alivyoniamrisha kuwahusu.

28 Nawaambia kwamba nimesababisha mkusanyike pamoja ili [a]nitoe damu yenu kutoka mavazi yangu, wakati huu ambao ninakaribia kaburi langu, ili niende kwa amani, na [b]roho yangu isiyokufa iungane na [c]kwaya za juu katika kuimba sifa za Mungu aliye wa haki.

29 Na zaidi ya hayo, ninawaambia kwamba nimesababisha mkusanyike pamoja, ili niwatangazie kwamba siwezi kuendelea kuwa mwalimu wenu, wala mfalme wenu;

30 Kwani hata sasa, mwili wangu wote unatetemeka ninapojaribu kuwazungumzia; lakini Bwana Mungu ananisaidia, na ameniruhusu niwazungumzie, na ameniamuru kwamba niwatangazie leo, kwamba mwana wangu Mosia ni mfalme na mtawala wenu.

31 Na sasa, ndugu zangu, nataka mtende kama vile tayari mmetenda. Hadi sasa mmetii amri zangu, na pia amri za baba yangu, na mmefanikiwa, na mmelindwa kwamba msiangukie mikono ya maadui wenu, hata hivyo mkitii amri za mwana wangu, au amri za Mungu ambazo mtapewa naye, mtafanikiwa nchini, na maadui wenu hawatapata uwezo juu yenu.

32 Lakini, Enyi watu wangu, jihadharini kwamba pasiwe na [a]mabishano miongoni mwenu, na mchague kutii pepo mchafu, ambaye alizungumziwa na baba yangu Mosia.

33 Kwani tazama, ole kwa yule anayechagua kumtii huyo pepo; kwani akichagua kumtii, na kuishi na afariki katika dhambi zake, yeye anakunywa [a]adhabu kwa nafsi yake; kwani yeye hupokea kwa mshahara wake adhabu isiyo na [b]mwisho, kwa sababu ya kuvunja sheria ya Mungu kinyume cha ufahamu wake.

34 Ninawaambia, kwamba hakuna yeyote miongoni mwenu, ila tu watoto wenu wadogo ambao hawajafunzwa kuhusu vitu hivi, asiyejua kwamba mnadaiwa milele na Baba wenu wa mbinguni, kumtolea yote mliyo nayo na vile mlivyo; na pia mmefundishwa kuhusu maandishi ambayo yana unabii ambao umezungumziwa na manabii watakatifu, hata hadi

27 *a* MWM Tembea, Tembea na Mungu.
b Yak. (KM) 1:19.

28 *a* Yak. (KM) 2:2.
b MWM Roho.
c Morm. 7:7.

32 *a* 3 Ne. 11:29–30.

33 *a* MWM Hukumu.
b M&M 19:6, 10–12.

wakati baba yetu, Lehi, alipotoka Yerusalemu;

35 Na pia, yote ambayo yamezungumzwa na baba zetu hadi sasa. Na tazama, pia, walizungumza yale ambayo waliamriwa na Bwana; kwa hivyo, ni ya haki na kweli.

36 Na sasa, nawaambia, ndugu zangu, kwamba baada ya kujua na kufundishwa vitu hivi vyote, kama mtakosa na kutenda kinyume cha yale yaliyozungumzwa, kwamba mnajitenga na Roho wa Bwana, kwamba hana nafasi ndani yenu ili awaongoze katika njia za hekima ili mpate baraka, mafanikio, na kuhifadhiwa—

37 Ninawaambia, kwamba, yule mtu anayetenda haya, huyo ndiye ambaye [a]anamuasi Mungu kiwazi; kwa hivyo anachagua kumtii pepo mchafu, na kuwa adui wa haki yote; kwa hivyo, Bwana hana nafasi ndani yake, kwani yeye haishi katika hekalu [b]zisizo takatifu.

38 Kwa hivyo kama mtu huyu [a]hatatubu, na aishi na afe akiwa adui wa Mungu, matakwa ya [b]haki takatifu huzindua nafsi yake isiyokufa kwa [c]hatia yake mwenyewe, ambayo humsababisha kutetemeka mbele ya Bwana, na hujaza kifua chake na hatia, na uchungu, na huzuni, ambayo ni kama moto usiozimika, ambao miale yake hupaa juu milele na milele.

39 Na sasa ninawaambia, kwamba [a]huruma haina dai juu ya mtu huyo; kwa hivyo hukumu yake ya mwisho ni kuvumilia mateso yasiyo na mwisho.

40 Ee ninyi, watu wote wazee, na pia ninyi vijana, na ninyi watoto wachanga mnaoweza kuelewa maneno yangu, kwani nimezungumza wazi kwenu ili muweze kuelewa, naomba kwamba muamke kwa [a]ukumbusho wa mahali pa kuogofya ya wale walioanguka kwenye dhambi.

41 Na zaidi, ningetamani mtafakari juu ya hali ya baraka na yenye [a]furaha ya wale wanaotii amri za Mungu. Kwani tazama, [b]wanabarikiwa katika vitu vyote, vya muda na vya kiroho; na kama watavumilia kwa [c]uaminifu hadi mwisho watapokewa [d]mbinguni, kwamba hapo waishi na Mungu katika hali ya furaha isiyo na mwisho. Enyi kumbukeni, kumbukeni kwamba vitu hivi ni vya kweli; kwani Bwana Mungu ameyazungumza.

MLANGO WA 3

Mfalme Benjamini anaendelea na hotuba yake—Bwana Mwenyezi atahudumia miongoni mwa wanadamu katika hema ya udongo—Damu itatiririka kutoka kila kinyweleo Yeye atakapokuwa aki-

37 *a* Mos. 3:12; Hel. 8:24–25. MWM Uasi.
b Alma 7:21.
38 *a* MWM Toba, Tubu.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
c MWM Hatia.
39 *a* Alma 34:8–9, 15–16. MWM Rehema, enye Rehema.
40 *a* Alma 5:18.
41 *a* 4 Ne. 1:15–18. MWM Shangwe.
b MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
c M&M 6:13.
d MWM Mbinguni.

lipia dhambi za ulimwengu—Jina lake ndilo jina pekee ambalo kwalo wokovu unakuja—Wanadamu wanaweza kumvua yule mtu wa asili na kuwa watakatifu kwa njia ya Upatanisho—Mateso ya wale waovu yatakuwa ni kama ziwa la moto na kiberiti. Karibia mwaka 124 K.K.

Na tena ndugu zangu, nataka mnisikilize, kwani nina mengine ya kuwazungumzia; kwani tazama, nina vitu vya kuwaambia kuhusu vile vitakavyokuja.

2 Na vile vitu nitakavyowaambia nimejulishwa hivyo na [a]malaika wa Mungu. Na aliniambia: Amka; na nikaamka, na tazama alisimama mbele yangu.

3 Na akaniambia: Amka, na usikilize yale maneno nitakayokuambia; kwani tazama, nimekuja kukutangazia habari [a]njema ya shangwe kuu.

4 Kwani Bwana amesikia sala zako, na ameihukumu haki yako, na amenituma kwako nikutangazie kwamba ushangilie; na kwamba wewe uwatangazie watu wako, kwamba wao wajazwe na shangwe.

5 Kwani tazama, wakati unakuja, na sio mbali sana, kwamba kwa uwezo, [a]Bwana Mwenyezi ambaye anatawala, ambaye alikuwa, na yuko kutoka milele yote hadi milele yote, atashuka chini kutoka mbinguni miongoni mwa watoto wa watu, na ataishi katika [b]hema takatifu ya udongo, na ataenda miongoni mwa watu, akitenda [c]miujiza mikuu, kama kuponya wagonjwa, kufufua wafu, kusababisha viwete kutembea, vipofu kupata kuona, na viziwi kusikia, na kuponya kila aina ya magonjwa.

6 Na atatoa [a]mashetani, au pepo wachafu wanaoishi katika mioyo ya watoto wa watu.

7 Na lo, atavumilia [a]majaribu, na maumivu ya mwili, [b]njaa, kiu, na uchovu, hata zaidi ya vile mtu anaweza [c]kuteseka, ila tu hadi kifo; kwani tazama, [d]damu inatiririka kutoka kwa kila kinyweleo, [e]mateso yake yatakuwa makuu kwa sababu ya maovu na machukizo ya watu wake.

8 Na ataitwa [a]Yesu Kristo, [b]Mwana wa Mungu, [c]Baba wa mbingu na dunia, Muumba wa vitu vyote tangu mwanzo; na [d]mama yake ataitwa [e]Mariamu.

9 Na lo, anawajia walio wake, ili [a]wokovu uwafikie watoto wa watu hata kupitia [b]imani kwa jina lake; na hata baada ya haya yote bado watamdhania kuwa

3 2*a* MWM Malaika.
3*a* Lk. 2:10–11.
5*a* MWM Yehova.
b Mos. 7:27; Alma 7:9–13.
c Mt. 4:23–24; Mdo. 2:22; 1 Ne. 11:31. MWM Muujiza.
6*a* Mk. 1:32–34.
7*a* MWM Jaribu, Majaribu.
b Mt. 4:1–2.
c M&M 19:15–18.
d Lk. 22:44.
e Isa. 53:4–5.
8*a* MWM Mungu, Uungu—Mungu Mwana.
b Alma 7:10.
c Hel. 14:12; 3 Ne. 9:15.
d Mt. 1:16; 1 Ne. 11:14–21.
e MWM Maria, Mama wa Yesu.
9*a* MWM Wokovu.
b MWM Amini, Imani.

yeye ni mwanadamu, na kusema kwamba amepagawa na [c]ibilisi, na [d]kumpiga, na [e]kumsulubu.

10 Na [a]atafufuka siku ya [b]tatu kutoka kwa wafu; na tazama, anasimama kuhukumu ulimwengu; na tazama, vitu hivi vyote vinafanyika ili [c]hukumu takatifu iwashukie watoto wa watu.

11 Kwani tazama, na pia [a]damu yake [b]inalipiza dhambi za wale ambao [c]wameanguka kwa sababu ya dhambi ya Adamu, ambao wameaga dunia bila kuelewa nia ya Mungu juu yao, au ambao wametenda dhambi [d]bila kujua.

12 Lakini ole, ole kwa yule anayefahamu kwamba [a]anamuasi Mungu! Kwani wokovu haumjii yeyote ila tu kwa kutubu na kwa imani katika [b]Bwana Yesu Kristo.

13 Na Bwana Mungu amewatuma manabii wake watakatifu miongoni mwa watoto wa watu, kutangaza vitu hivi kwa kila kabila, taifa, na lugha, ili hapo kwamba yeyote atakayeamini kwamba Kristo atakuja, hao watapokea [a]msamaha wa dhambi, na kushangilia kwa shangwe kuu zaidi, [b]kama vile tayari amekuja miongoni mwao.

14 Lakini Bwana Mungu aliona kwamba watu wake walikuwa wenye shingo ngumu, na akawapatia sheria, hata [a]sheria ya Musa.

15 Na ishara nyingi, na maajabu, na [a]mifano, na vivuli aliwaonyesha kwao, kuhusu kuja kwake; na pia manabii watakatifu waliwazungumzia kuhusu kuja kwake; na bado walishupaza mioyo yao, na hawakufahamu kuwa [b]sheria ya Musa haifaidi chochote isipokuwa kupitia upatanisho wa damu yake.

16 Na hata kama ingewezekana kwamba [a]watoto wadogo wangetenda dhambi hawangeweza kuokolewa; lakini ninakuambia [b]wamebarikiwa; kwani tazama, kama vile katika Adamu, au kwa maumbile, wanaanguka, hata hivyo damu ya Kristo inalipiza dhambi zao.

17 Na zaidi ya hayo, ninawaambia, kwamba [a]hakuna jina lingine litatolewa wala njia ingine wala mbinu yoyote ambayo [b]wokovu utawashukia watoto wa watu, ila katika na

9 *c* Yn. 8:48.
d Mk. 15:15.
e Lk. 18:33; 1 Ne. 19:10; 2 Ne. 10:3. MWM Kusulubiwa.
10 *a* MWM Ufufuko.
b Mt. 16:21; 2 Ne. 25:13; Hel. 14:20–27.
c MWM Amua, Hukumu.
11 *a* MWM Damu.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
c MWM Anguko la Adamu na Hawa.
d 2 Ne. 9:25–26.
12 *a* Mos. 2:36–38; Hel. 8:25. MWM Uasi.
b MWM Bwana.
13 *a* MWM Ondoleo la Dhambi.
b 2 Ne. 25:24–27; Yar. 1:11.
14 *a* MWM Torati ya Musa.
15 *a* MWM Yesu Kristo—Mifano au ishara za Kristo.
b Mos. 13:27–32.
16 *a* MWM Mtoto, Watoto.
b Moro. 8:8–9.
17 *a* Mdo. 4:10–12; 2 Ne. 31:21.
b MWM Wokovu.

kupitia jina la [c]Kristo pekee, Bwana Mwenyezi.

18 Kwani tazama anahukumu, na hukumu yake ni ya haki; na mtoto mchanga anayefariki uchangani mwake haangamii; lakini wanadamu hunywa adhabu kwa nafsi yao isipokuwa wajinyenyekeze na [a]kuwa kama watoto wadogo, na kuamini kwamba wokovu ulikuwa, na upo, na utakuja, kwa na katika [b]upatanisho wa damu ya Kristo, Bwana Mwenyezi.

19 Kwani mwanadamu wa [a]asili ni adui kwa Mungu, na amekuwa tangu [b]anguko la Adamu, na atakuwa hivyo, milele na milele, [c]asipokubali ushawishi wa [d]Roho Mtakatifu, na kumvua mtu wa asili na kuwa [e]mtakatifu kupitia upatanisho wa Kristo aliye Bwana, na kuwa kama [f]mtoto, mtiifu, mpole, mnyenyekevu, mvumilivu, mwenye upendo tele, aliye tayari kukubali vitu vyote ambavyo Bwana anaona sahihi kuyaweka juu yake, hata kama vile mtoto hunyenyekea kwa baba yake.

20 Na zaidi ya hayo, ninakuambia, kwamba wakati unakaribia ambako [a]ufahamu wa Mwokozi utapenya [b]kila taifa, kabila, lugha, na watu.

21 Na tazama, wakati huo utakapofika, hakuna yeyote atakayepatikana bila [a]lawama mbele ya Mungu, isipokuwa watoto wadogo, isipokuwa tu kupitia toba na imani katika jina la Bwana Mungu Mwenyezi.

22 Na hata wakati huu, wakati utakapokuwa umewafundisha watu wako vitu vile ambavyo Bwana Mungu wako amekuamuru, hata hivyo bado hawatapatikana na lawama machoni mwa Mungu, tu kulingana na yale maneno ambayo nimekuzungumzia.

23 Na sasa nimezungumza maneno ambayo Bwana Mungu ameniamuru.

24 Na Bwana asema hivi: Watasimama kama ushuhuda ung'arao kinyume cha watu hawa, siku ile ya hukumu; ambako watahukumiwa, kila mtu kulingana na matendo yake, kama ni mema, au kama ni maovu.

25 Na kama ni maovu watatolewa kwa [a]mawazo mabaya ya hatia yao na machukizo, ambayo inawasababisha kukimbia kutoka uwepo wa Bwana na kuingia katika hali ya [b]hofu na mateso yasiyo na mwisho, kutoka ambapo hawawezi kurejea tena; kwa hivyo wanajiletea hukumu ya milele katika nafsi zao.

26 Kwa hivyo, wamekunywa kutoka kikombe cha ghadhabu

17 *c* MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
18 *a* Mt. 18:3.
b Mos. 4:2; Hel. 5:9.
19 *a* 1 Kor. 2:11–14; Mos. 16:2–3.
MWM Mwanadamu wa Tabia ya Asili.
b MWM Anguko la Adamu na Hawa.
c 2 Nya. 30:8.
d Moro. 10:4–5.
MWM Roho Mtakatifu.
e MWM Mtakatifu.
f 3 Ne. 9:22.
20 *a* M&M 3:16.
b MWM Kazi ya kimisionari.
21 *a* MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
25 *a* Alma 5:18; 12:14–15.
b Morm. 8:38.

ya Mungu, haki ambayo haiwezi kuwazuia kama vile haingezuia [a]Adamu aanguke kwa sababu ya kula [b]tunda lililokatazwa; kwa hivyo, hawawezi kupokea [c]huruma milele.

27 Na [a]mateso yao ni kama [b]ziwa la moto na kiberiti, ambalo miale yake haiwezi kuzimika, na moshi wake hupaa juu milele na milele. Na hivi ndivyo Bwana ameniamuru mimi. Amina.

MLANGO WA 4

Mfalme Benjamini anaendelea katika hotuba yake—Wokovu unapatikana kwa sababu ya Upatanisho—Muamini Mungu ili uokolewe—Hifadhi msamaha wa dhambi zako kwa uaminifu—Shirikiana na walio masikini kwa mali yako—Tenda vitu vyote kwa hekima na mpango. Karibia mwaka 124 K.K.

Na sasa, ikawa kwamba baada ya mfalme Benjamini kumaliza kuzungumza maneno ambayo alikuwa amepewa na malaika wa Bwana, kwamba alitupa macho kwenye umati, na tazama walikuwa wameinama ardhini, kwani [a]woga wa Bwana ulikuwa umewajia.

2 Na walikuwa wamejiona wenyewe katika hali yao ya [a]kimwili, hata kuwa [b]ndogo zaidi ya mavumbi ya dunia. Na wote wakalia kwa sauti moja, wakisema: Ewe tuhurumie, na utumie damu ya [c]upatanisho wa Kristo kwamba tupokee msamaha wa dhambi zetu, na mioyo yetu isafishwe; kwani tunamwamini Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, [d]aliyeumba mbingu na dunia, na vitu vyote; ambaye atashuka chini miongoni mwa watoto wa watu.

3 Na ikawa kwamba baada ya wao kuzungumza maneno haya Roho wa Bwana aliwashukia, na wakajazwa na shangwe, wakiwa wamepokea [a]msamaha wa [b]dhambi zao, na kupata amani katika dhamira zao, kwa sababu ya [c]imani tele waliyokuwa nayo katika Yesu Kristo atakayekuja, kulingana na maneno ambayo mfalme Benjamini aliwazungumzia.

4 Na mfalme Benjamini tena akafungua kinywa chake na kuanza kuwazungumzia, akisema: Marafiki zangu na ndugu zangu, ukoo wangu na watu wangu, naomba tena mnisikilize, kwamba msikie na kufahamu maneno yangu yaliyosalia.

5 Kwani tazama, ikiwa ufahamu wa wema wa [a]Mungu wakati huu umewaamsha kwa kuona udhaifu wenu, na kwamba hamna thamani katika hali yenu ya kuanguka—

26 *a* Morm. 9:12.
b Mwa. 3:1–12; 2 Ne. 2:15–19; Alma 12:21–23.
c MWM Rehema, enye Rehema.
27 *a* MWM Hatia.
b 2 Ne. 9:16; Yak. (KM) 6:10; M&M 76:36.
4 1 *a* MWM Hofu.
2 *a* MWM Tamaa za kimwili.
b Hel. 12:7–8.
c Mos. 3:18; Hel. 5:9.
d MWM Umba, Uumbaji.
3 *a* MWM Ondoleo la Dhambi.
b MWM Dhamiri.
c MWM Amini, Imani.
5 *a* Musa 1:10.

6 Ninawaambia, kama mmepokea [a]ufahamu wa wema wa Mungu, na nguvu zake zisizo na kifani, na hekima yake, na subira yake, na uvumilivu wake kwa watoto wa watu; na pia, [b]upatanisho uliotayarishwa tangu [c]msingi wa ulimwengu, ili wokovu umshukie yeyote [d]atakayemwamimi Bwana, na awe mwenye bidii katika kushika amri zake, na kuendelea katika imani hata hadi mwisho wa maisha yake, ninamaanisha maisha ya mwili wa muda—

7 Ninasema, kwamba huyu ndiye yule mtu anayepokea wokovu, kupitia kwa upatanisho ambao ulitayarishwa tangu msingi wa ulimwengu kwa wanadamu wote, ambao walikuwa wakati wowote tangu [a]kuanguka kwa Adamu, au wale walio, au wale watakaokuwepo wakati wowote, hata hadi mwisho wa ulimwengu.

8 Na hii ndiyo njia ambayo kwayo wokovu unakuja. Na [a]hakuna wokovu mwingine ila huu ambao umezungumziwa; wala hakuna masharti mengine ambayo kwayo mwanadamu anaweza kuokolewa ila tu masharti yale ambayo nimewaambia.

9 Mwamini Mungu; amini kwamba yupo, na kwamba aliumba vitu vyote, katika mbingu na katika ardhi, amini kwamba ana [a]hekima yote, na uwezo wote, mbinguni na ardhini; mwamini kwamba mwanadamu [b]hafahamu vitu vyote ambavyo Bwana anavyoweza kufahamu.

10 Na tena, mwamini kwamba lazima [a]mtubu dhambi zenu na kuziacha, na kujinyenyekeza mbele ya Mungu; na muombe kutoka moyo wa kweli ili [b]awasamehe; na sasa, kama [c]mnaamini hivi vitu vyote hakikisheni kwamba [d]mnavitenda.

11 Na tena nawaambia vile nilivyosema awali, kwamba kama vile mmefahamu utukufu wa Mungu, au kama mmejua wema wake na [a]kuonja upendo wake, na kupokea [b]msamaha wa dhambi zenu, ambao unawaletea shangwe tele nafsini mwenu, hata hivyo nataka mkumbuke, na kila wakati mshikilie ukumbusho, wa ukuu wa Mungu, na [c]unyonge wenu, na [d]wema wake na subira yake kwenu ninyi; viumbe vinyonge, na mjinyenyekee kwa [e]unyenyekevu mwingi, [f]mkililingana jina la Bwana kila siku, na kusimama imara katika imani kwa yale yanayokuja, ambayo yalizungumzwa kwa kinywa cha malaika.

12 Na tazama, ninawaambia

6a MWM Mungu, Uungu.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
c Mos. 15:19.
d Zab. 36:7; 2 Ne. 22:2; Hel. 12:1. MWM Tegemea.
7a MWM Anguko la Adamu na Hawa.
8a Mdo. 4:12; 2 Ne. 31:21; Mos. 3:17.
9a Rum. 11:33–34; Yak. (KM) 4:8–13.
b Isa. 55:9.
10a MWM Toba, Tubu.
b M&M 61:2.
c Mt. 7:24–27.
d 2 Ne. 31:19–21.
11a Alma 36:24–26.
b MWM Ondoleo la Dhambi.
c Musa 1:10.
d Ku. 34:6; Moro. 8:3.
e MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
f MWM Sala.

kwamba kama mtafanya haya mtapokea furaha daima, na kujazwa na [a]upendo wa Mungu, na daima [b]kuhifadhi msamaha wa dhambi zenu; na mtaendelea mkiwa katika ufahamu wa utukufu wa yule aliyewaumba, au katika ufahamu wa yale yaliyo ya haki na kweli.

13 Na hamtataka kuumizana, lakini mtaishi kwa [a]amani, na kumpatia kila mtu anachostahili.

14 Na hamtakubali [a]watoto wenu kupatwa na njaa, au kukaa uchi; wala hamtakubali kwamba wavunje sheria za Mungu, na [b]kupigana na kutetanisha moja kwa mwingine, na kumtumikia ibilisi, ambaye ni bwana wa dhambi, au aliye pepo mchafu ambaye alizungumziwa na babu zetu, yeye akiwa adui wa haki yote.

15 Lakini ninyi [a]mtawafundisha [b]kutembea katika njia za kweli na za kiasi; mtawafundisha [c]kupendana, na kutumikiana.

16 Na pia, wenyewe [a]mtawasaidia wale wanaohitaji usaidizi wenu; mtawatolea misaada wale wanaohitaji; na hamtakubali kwamba maombi ya [b]mwombaji kuwa bure, na kumfukuza ili aangamie.

17 Pengine wewe [a]utasema: Huyu mtu amejiletea taabu; kwa hivyo nitazuia mkono wangu, na sitampatia chakula changu, wala kumtolea msaada ili asiteseke, kwani maadhibio yake ni ya haki—

18 Lakini nakwambia, Ewe mwanadamu, yeyote anayefanya hivyo basi huyo anayo sababu kuu ya kutubu; na asipotubu hilo ambalo ametenda ataangamia milele, na hana haja na ufalme wa Mungu.

19 Kwani tazama, si sisi wote ni waombaji? Je, si sisi sote tunamtegemea yule Mmoja, aliye Mungu, kwa mali yote tuliyo nayo, kwa chakula na mavazi, na kwa dhahabu, na kwa fedha, na kwa kila utajiri tulio nao?

20 Na tazama, hata sasa hivi, mmekuwa mkililingana jina lake, na mkiomba msamaha wa dhambi zenu. Na je amefanya muombe bure? La; amewashushia roho yake, na kusababisha kwamba mioyo yenu ijae [a]shangwe, na kusababisha vinywa vyenu vifungwe ili msipate kuongea, kwa sababu ya ile shangwe yenu tele.

21 Na sasa, kama Mungu, aliyewaumba, ambaye mnamtegemea kwa mahitaji yenu na kwa yote mlio nayo na vile mlivyo, huwapatia chochote mnacho omba kilicho sahihi, kwa imani, mkiamini kwamba mtapokea, Ee hata, inawapasa

12 *a* MWM Upendo.
b Mos. 4:26; Alma 4:13–14; 5:26–35; M&M 20:31–34.
13 *a* MWM Msuluhishi.
14 *a* 1 Tim. 5:8; M&M 83:4.
b MWM Ushindani.
15 *a* M&M 68:25–28; Musa 6:58. MWM Fundisha, Mwalimu.
b MWM Tembea, Tembea na Mungu.
c Mos. 18:21.
16 *a* MWM Hisani; Utumishi.
b Kum. 15:7–11; Mit. 21:13; Isa. 10:1–2.
17 *a* Mit. 17:5.
20 *a* MWM Shangwe.

ninyi [a]kusaidiana mmoja kwa mwingine.

22 Na kama [a]unamhukumu mtu yule anayekulilia kwa msaada ili asiangamie, na kumshutumu, jinsi gani hukumu yako itakuwa ya haki kwa sababu ya [b]kuzuia msaada wako, ambao sio wako bali ni wa Mungu, ambaye pia maisha yako ni yake; na walakini humlilii, wala kutubu kwa kile kitu ambacho umetenda.

23 Ninawaambia, ole kwa yule mtu, kwani ataangamia na mali yake; na sasa, ninasema vitu hivi kwa wale walio [a]matajiri kwa vitu vya ulimwengu huu.

24 Na tena, nawaambia walio masikini, ninyi ambao hamna lakini mnayo ya kutosha, kwamba muishi siku kwa siku; namaanisha ninyi nyote ambao mnawanyima mwombaji, kwa sababu hamna; ningetaka mseme mioyoni mwenu kwamba: Simpi kwa sababu sina, lakini kama ningekuwa nayo, [a]ningempa.

25 Na sasa, kama mtasema hivi mioyoni mwenu mtakuwa hamna hatia, la sivyo [a]mmehukumiwa; na hukumu yenu ni ya haki kwa sababu mnatamani yale ambayo hamjapokea.

26 Na sasa, kwa sababu ya vitu hivi ambavyo nimewazungumzia—kwamba, ili mhifadhi msamaha wa dhambi zenu siku kwa siku, ili [a]mtembee bila hatia mbele ya Mungu—ningetaka kwamba [b]muwapatie [c]masikini mali yenu, kila mtu kulingana na ile aliyo nayo, kwa mfano [d]kulisha wenye njaa, kuvisha walio uchi, kuwatembelea wagonjwa na kuwahudumia katika haja zao, kiroho na kimwili, kulingana na matakwa yao.

27 Na mhakikishe kwamba vitu hivi vyote vinafanywa kwa hekima na mpango; kwani haimpasi mwanadamu kukimbia [a]zaidi kuliko nguvu zake. Na tena, ni lazima awe na bidii, ili ashinde zawadi; kwa hivyo, vitu vyote lazima vitendeke kwa mpango.

28 Na ningependa mkumbuke, kwamba yeyote miongoni mwenu anayeazima chochote kutoka kwa jirani yake lazima arudishe kile alicho kiazima, kulingana na vile alivyokubali, la sivyo utatenda dhambi; na pengine wewe utamsababisha jirani yako kutenda dhambi pia.

29 Na mwishowe, siwezi kuwaelezea vitu vyote ambavyo vinaweza kuwasababisha kutenda dhambi; kwani kuna njia nyingi na mbinu, nyingi sana hata kwamba siwezi kuzihesabu.

30 Lakini kwa haya naweza kuwaambia hivi, kwamba [a]msipojichunga wenyewe, na

21 *a* MWM Ustawi; Utumishi.
22 *a* Mt. 7:1–2; Yn. 7:24.
b 1 Yoh. 3:17.
23 *a* M&M 56:16.
24 *a* Mk. 12:44.
25 *a* M&M 56:17.
26 *a* MWM Tembea, Tembea na Mungu.
b Yak. (KM) 2:17–19.
c Zek. 7:10; Alma 1:27. MWM Sadaka, Utoaji sadaka.
d Isa. 58:10–11; M&M 104:17–18.
27 *a* M&M 10:4.
30 *a* Alma 12:14. MWM Kesha, Walinzi.

[b]mawazo yenu, na [c]maneno yenu, na matendo yenu, na kufuata sheria za Mungu, na kuendelea kwa imani katika mambo yale mmesikia kuhusu kuja kwa Bwana, hadi mwisho wa maisha yenu, lazima mtaangamia. Na sasa, Ee mwanadamu, kumbuka, na usiangamie.

MLANGO WA 5

Watakatifu huwa wana na mabinti wa Kristo kwa imani—Kisha wanaitwa kwa jina la Kristo—Mfalme Benjamini anawaonya wawe imara na wasiotingishika katika matendo mema. Karibia mwaka 124 K.K.

Na sasa, ikawa kwamba wakati mfalme Benjamini alipomaliza kuwazungumzia watu wake, alituma ujumbe miongoni mwao, akitamani kujua kama watu wake wameyaamini maneno ambayo alikuwa amewazungumzia.

2 Na wote wakalia kwa sauti moja, wakisema: Ndiyo, tunaamini maneno yote ambayo umetuzungumzia; na pia, tunajua uhakika na ukweli wao, kwa sababu ya Roho wa Bwana Mwenyezi, ambaye ameleta [a]mabadiliko makuu ndani yetu, au mioyoni mwetu, hata kwamba hatuna tamaa ya kutenda [b]maovu tena, lakini kutenda mema daima.

3 Na sisi, wenyewe, pia, kwa wema mkuu wa Mungu, na madhihirisho ya Roho wake, tunayo maono makuu ya yale yatakayokuja; na kama ingefaa, tungetoa unabii wa vitu vyote.

4 Na ni kwa imani katika vitu vile ambavyo mfalme wetu ametuzungumzia ambavyo vimetuletea ufahamu huu mkuu, ambayo kwayo tunasherekea kwa shangwe kuu sana.

5 Na tunataka [a]tuagane na Mungu wetu ili tutende nia yake, na tuwe watiifu kwa amri zake kwa vitu vyote atakavyotuamuru, katika maisha yetu yaliyosalia, kwamba tusijiletee sisi wenyewe mateso [b]yasiyo na mwisho, kama vile alivyosema [c]malaika, kwamba tusinywe kutoka kile kikombe cha ghadhabu ya Mungu.

6 Na sasa, haya ndiyo maneno ambayo mfalme Benjamini aliwatakia; na kwa hivyo akawaambia; Mmezungumza maneno yale ambayo nilitaka; na agano ambalo mmefanya ni agano takatifu.

7 Na sasa, kwa sababu ya agano lile ambalo mmefanya mtaitwa [a]watoto wa Kristo, wanawe, na mabinti zake; kwani tazama, siku hii [b]amewazaa kiroho; kwani mnasema kwamba [c]mioyo yenu inabadilishwa kwa imani katika jina lake; kwa hivyo, [d]amewazaa na mkawa [e]wanawe na mabinti zake.

30 *b* Mk. 7:18–23.
MWM Mawazo.
c Mt. 15:18–20.
MWM Lugha chafu.
5 2 *a* Alma 5:14.
MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
b Alma 19:33.
5 *a* Mos. 18:10.
b Mos. 3:25–27.
c Mos. 3:2.
7 *a* Mos. 27:24–26; Musa 6:64–68.
MWM Wana na Mabinti za Mungu.
b MWM Zaliwa.
c MWM Moyo.
d Mos. 15:10–11.
MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
e M&M 11:30.

8 Na chini ya jina hili mmefanywa [a]huru, na [b]hakuna jina lingine ambalo linaweza kuwafanya muwe huru. Hakuna [c]jina lingine ambalo kwalo huleta wokovu; kwa hivyo, ningependa [d]mjivike juu yenu jina la Kristo, nyote ambao mmeingia katika agano na Mungu kwamba mtakuwa watiifu hadi mwisho wa maisha yenu.

9 Na itakuwa kwamba yeyote atakayefanya hivi atakuwa katika mkono wa kulia wa Mungu, kwani atajua jina ambalo anaitwa; kwani ataitwa kwa jina la Kristo.

10 Na sasa itakuwa kwamba, yeyote asiyejitundika jina la Kristo lazima aitwe kwa jina [a]lingine; kwa hivyo, anajikuta kwenye mkono wa [b]kushoto wa Mungu.

11 Na nataka pia mkumbuke, kwamba hili ndilo [a]jina ambalo nilisema kwamba nitawapatia ambalo kamwe halitafutwa, ila tu kwa dhambi; kwa hivyo, jichungeni kwamba msianguke dhambini, kwamba jina hilo lisifutwe kutoka mioyo yenu.

12 Ninawaambia, nataka kwamba mkumbuke [a]kudumisha jina ambalo limeandikwa mioyoni mwenu, kwamba msipatikane kwenye mkono wa kushoto wa Mungu, lakini kwamba msikie na kujua sauti ambayo itawaita, na pia, lile jina ambalo atawaita.

13 Kwani ni vipi mtu [a]atamjua yule bwana ambaye hajamtumikia, na aliye mgeni kwake, na yuko mbali katika mawazo na nia za moyo wake?

14 Na tena, je mtu huchukua punda wa jirani yake, na kumweka? Ninawambia, La; hatakubali hata ale miongoni mwa mifugo yake, lakini atamfukuza, nakumtupilia mbali. Nawambia, itakuwa hivyo nanyi msipojua ni kwa jina gani mtakaloitwa.

15 Kwa hivyo, nataka muwe imara na msiotingishika, daima mkitenda matendo mema, ili Kristo, Bwana Mungu Mwenyezi, awaweke [a]muhuri wake, ili mletwe mbinguni, ili mpokee wokovu usio na mwisho na uzima wa milele, kwa hekima, na uwezo, na haki na rehema za yule [b]aliyeumba vitu vyote, mbinguni na ardhini, ambaye ni Mungu juu ya yote. Amina.

MLANGO WA 6

Mfalme Benjamini anaandika majina ya watu na kuwateua makuhani wa kuwafundisha—Mosia anatawala akiwa mfalme wa haki. Karibia mwaka 124–121 K.K.

Na sasa, mfalme Benjamini alifikiria ni vyema, baada ya kumaliza kuongea kwa watu wake, kwamba [a]achukue majina ya wale wote ambao walikuwa

8 *a* Rum. 6:18; Gal. 5:1; Hel. 14:30.
b Mdo. 4:10, 12; Alma 21:9.
c Mos. 26:18.
d Mdo. 11:26; Alma 46:15.

10 *a* Alma 5:38–39.
b Mt. 25:33.

11 *a* Mos. 1:11–12. MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.

12 *a* M&M 18:23–25.

13 *a* Mos. 26:24–27.

15 *a* MWM Utakaso; Wito na Uteuzi.
b Kol. 1:16; Mos. 4:2; Alma 11:39.

6 1 *a* M&M 128:8.

wameingia kwenye agano na Mungu kutii amri zake.

2 Na ikawa kwamba hapakuwa yeyote, ila tu watoto wadogo, ambao hawakuingia kwenye agano na kujitundika jina la Kristo.

3 Na tena, ikawa kwamba wakati mfalme Benjamini alipomaliza vitu hivi vyote, na kumtawaza mwana wake [a]Mosia kuwa mtawala na mfalme wa watu wake, na kumpatia masharti yote kuhusu ule ufalme, na pia [b]kuteua makuhani [c]wafundishe watu, ili wasikie na kujua amri za Mungu, na kuwachochea ili wakumbuke kile [d]kiapo walichofanya, akalikiza ule umati, na wakarejea, kila mmoja, kulingana na jamii zao, manyumbani kwao.

4 Na [a]Mosia akaanza kutawala badala ya baba yake. Na alianza kutawala alipokuwa na umri wa miaka thelathini, ikatimia, miaka mia nne, sabini na sita [b]tangu Lehi aondoke Yerusalemu.

5 Na mfalme Benjamini akaishi miaka mitatu na kufariki.

6 Na ikawa kwamba mfalme Mosia alifuata njia za Bwana, na kufuata hukumu zake na maagizo yake, na kutii amri zake katika vitu vyote alivyomwamuru.

7 Na mfalme Mosia akasababisha watu wake kulima ardhi. Na pia yeye, mwenyewe, akalima ardhi, ili [a]asiwe mzigo kwa watu wake, na kwamba atende kulingana na vile baba yake alivyotenda katika vitu vyote. Na hapakuwa na ubishi miongoni mwa watu wake wote kwa kipindi cha miaka mitatu.

MLANGO WA 7

Amoni agundua nchi ya Lehi-Nefi, ambapo Limhi ni mfalme—Watu wa Limhi wako utumwani kwa Walamani—Limhi anaeleza historia yao—Nabii (Abinadi) alikuwa amewashuhudia kwamba Kristo ni Mungu na Baba wa vitu vyote—Wale ambao wanapanda uchafu watavuna tufani, na wale wanaomwamini Bwana watakombolewa. Karibia mwaka 121 K.K.

Na sasa, ikawa kwamba baada ya mfalme Mosia kuwa na amani kwa kipindi cha miaka mitatu, alitaka kujua kuhusu wale watu [a]walioenda kuishi katika nchi ya Lehi-Nefi, au katika mji wa Lehi-Nefi; kwani watu wake hawakusikia chochote kutoka kwao tangu waondoke nchi ya [b]Zarahemla; kwa hivyo, walimchokesha kwa maswali yao.

2 Na ikawa kwamba mfalme Mosia akaruhusu vijana wao kumi na sita wenye nguvu waende katika nchi ya Lehi-Nefi, kupeleleza kuhusu ndugu zao.

3 Na ikawa kwamba kesho yake walianza safari yao, wakiwa na mmoja aliyeitwa Amoni, yeye akiwa mtu mwenye

3 *a* Mos. 1:10; 2:30.
b MWM Kutawaza, Kutawazwa.
c Alma 4:7.
d Mos. 5:5–7.
4 *a* MWM Mosia, Mwana wa Benjamini.
b 1 Ne. 1:4.
7 *a* 2 Kor. 11:9.
7 1 *a* Omni 1:27–30.
b Omni 1:13.

nguvu na shujaa, na uzao wa Zarahemla; na alikuwa pia kiongozi wao.

4 Na sasa, hawakujua njia watakayosafiria huko nyikani ili wafike nchi ya Lehi-Nefi; kwa hivyo walizungukazunguka huko nyikani kwa siku nyingi, hata siku arubaini walizozunguka.

5 Na walipozunguka siku arubaini walifika kwenye kilima, ambacho kiko kaskazini mwa nchi ya [a]Shilomu, na hapo wakapiga hema zao.

6 Na Amoni akawachukua ndugu zake watatu, na majina yao yalikuwa Amaleki, Helemu, na Hemu, na wakaelekea katika nchi ya [a]Nefi.

7 Na tazama, wakakutana na mfalme wa watu waliokuwa katika nchi ya Nefi, na katika nchi ya Shilomu; na wakazingirwa na walinzi wa mfalme, na wakakamatwa, na kufungwa, na kuwekwa gerezani.

8 Na ikawa kwamba baada ya kuwa gerezani siku mbili waliletwa tena mbele ya mfalme, na mafungo yao yakafunguliwa; na wakasimama mbele ya mfalme, na walikubaliwa, kwa usahihi zaidi kuamriwa, kwamba wajibu maswali ambayo atawauliza.

9 Na akawaambia: Tazama, mimi ni [a]Limhi, mwana wa Nuhu, ambaye alikuwa mwana wa Zenivu, ambaye alitoka nchi ya Zarahemla kurithi nchi hii, ambayo ilikuwa nchi ya baba zao, ambaye aliteuliwa kuwa mfalme kwa sauti ya watu.

10 Na sasa, nataka kujua kwa nini mlikuwa jasiri hata mkakaribia kuta za mji, wakati mimi, mwenyewe, nilikuwa na walinzi wangu huko nje?

11 Na sasa, ni kwa kusudi hili nimeruhusu mhifadhiwe, ili niwaulize, au kama sio hivyo ningeamuru kwamba walinzi wangu wawaue. Mmeruhusiwa kuongea.

12 Na sasa, wakati Amoni alipofahamu kwamba ameruhusiwa kuongea, alisogea mbele na kuinama mbele ya mfalme; na akainuka na kusema: Ee mfalme, ninamshukuru Mungu leo kwamba bado niko hai, na nimeruhusiwa kuongea; na nitajaribu kuongea kwa ujasiri;

13 Kwani nina hakika kwamba kama ungenijua hungeruhusu kwamba nifungwe kwa kamba hizi. Kwani mimi ni Amoni, na mimi ni uzao wa [a]Zarahemla, na nimekuja kutoka nchi ya Zarahemla kupeleleza kuhusu ndugu zetu, ambao Zenivu aliwatoa kutoka nchi hiyo.

14 Na sasa, ikawa kwamba baada ya Limhi kusikia maneno ya Amoni, alikuwa na furaha tele, na akasema: Sasa, najua kwa hakika kwamba ndugu zangu ambao walikuwa katika nchi ya Zarahemla bado wako hai. Na sasa, nitasherehekea; na kesho nitawasababisha watu wangu washerehekee pia.

15 Kwani tazama, sisi tuko utumwani mwa Walamani, na

5*a* Mos. 9:6, 8, 14.
6*a* 2 Ne. 5:8.
9*a* Mos. 11:1.
13*a* Omni 1:12–15.

[a]tunatozwa kodi ambayo ni ngumu kuvumilia. Na sasa, tazama, ndugu zetu watatukomboa kutoka huu utumwa wetu, au kutoka mikononi mwa Walamani, na tutakuwa watumwa wao; kwani ni afadhali tuwe watumwa wa Wanefi badala ya kulipa kodi kwa mfalme wa Walamani.

16 Na sasa, mfalme Limhi akawaamuru walinzi wake kwamba wasimfunge tena Amoni wala ndugu zake, lakini akawasababisha kwenda katika kilima kile kilichokuwa kaskazini mwa Shilomu, na kuleta ndugu zake mjini, ili wale, na kunywa, na wajipumzishe kutoka uchovu wa safari yao; kwani walikuwa wameteseka katika vitu vingi; walikuwa wamepata mateso ya njaa, kiu, na uchovu.

17 Na sasa, ikawa kwamba kesho yake mfalme Limhi akatuma tangazo miongoni mwa watu wake, kwamba wakusanyike pamoja kwenye [a]hekalu, ili wasikie maneno ambayo angewazungumzia.

18 Na ikawa kwamba walipokusanyika pamoja aliwazungumzia hivi, akisema: Ee ninyi, watu wangu, inueni vichwa vyenu na mfarijiwe; kwani tazameni, wakati umewadia, au hauko mbali sana, ambapo hatutakuwa chini ya utawala wa maadui zetu tena, ijapokuwa jitihada zetu nyingi, ambazo zimekuwa za bure; lakini naamini kwamba bado tunaweza kupata ushindi.

19 Kwa hivyo, inueni vichwa vyenu, na msherehekee, na muweke imani yenu kwa [a]Mungu, katika huyo Mungu ambaye alikuwa ni Mungu wa Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo; na pia, yule Mungu [b]aliyewatoa wana wa Israeli kutoka nchi ya Misri, na kusababisha kwamba watembee katika Bahari ya Shamu kwa nchi kavu, na kuwalisha [c]mana ili wasiangamie huko nyikani; na aliwatendea vitu vingi zaidi.

20 Na tena, huyo Mungu amewatoa babu zetu [a]kutoka nchi ya Yerusalemu, na amewaweka na kuwahifadhi watu wake hadi sasa; na tazameni, ni kwa sababu ya maovu na machukizo yetu kwamba ametuleta utumwani.

21 Na nyote ni mashahidi siku ya leo, kwamba Zenivu, ambaye alifanywa kuwa mfalme wa watu hawa, yeye akiwa mwenye [a]bidii nyingi kwa kurithi nchi ya babu zake, kwa hivyo alidaganyika kwa ujanja na hila za mfalme Lamani, ambaye baada ya kuingia katika mkataba na mfalme Zenivu, na baada ya kumpatia sehemu ya ile nchi, au hata mji wa Lehi-Nefi, na mji wa Shilomu; na ardhi iliyoizingira—

22 Na alitenda haya yote, kwa kusudi moja, la [a]kuwatia hawa watu chini au utumwani.

15*a* Mos. 19:15.
17*a* 2 Ne. 5:16.
19*a* Ku. 3:6; 1 Ne. 19:10.
b Ku. 12:40–41; Alma 36:28.
c Ku. 16:15, 35; Hes. 11:7–8; Yos. 5:12.
20*a* 1 Ne. 2:1–4.
21*a* Mos. 9:1–3.
22*a* Mos. 10:18.

Na tazameni, sasa sisi tunalipa ushuru kwa mfalme wa Walamani, ambayo ni nusu ya mahindi yetu, na shayiri yetu, na hata kila aina ya nafaka yetu, na nusu ya mazao ya mifugo na wanyama wetu; na hata nusu ya chochote ambacho tunacho mfalme wa Walamani hutudai, au maisha yetu.

23 Na sasa, si hii ni vigumu kuvumiliwa? Na je, si haya maumivu yetu, ni makuu? Tazameni sasa, jinsi gani tuna sababu kuu ya kuomboleza.

24 Ndiyo, nawaambia, sababu za kuomboleza kwetu ni kuu; kwani tazameni, ni ndugu zetu wangapi wameuawa, na damu yao kumwagwa bure, na yote kwa sababu ya dhambi.

25 Kwani kama watu hawa hawangeanguka dhambini Bwana hangeruhusu kwamba ovu hili kubwa liwashukie. Lakini tazameni, hawakusikiza maneno yake; lakini mabishano yalitokea miongoni mwao, hata kwamba wakamwaga damu miongoni mwao.

26 Na wamemuua [a]nabii wa Bwana; ndiyo, mtu aliyeteuliwa na Mungu, ambaye aliwaelezea kuhusu uovu wao na machukizo yao, na kutoa unabii wa vitu vingi vitakavyokuja, ndiyo, hata kuja kwa Kristo.

27 Na kwa sababu aliwaambia kwamba Kristo ndiye [a]Mungu, Baba wa vitu vyote, na kusema kwamba atajichukulia [b]mfano wa mwanadamu, na utakuwa ni ule mfano ambao mwanadamu alikuwa ameumbwa nao tangu mwanzo; au kwa maneno mengine, alisema kwamba mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa [c]Mungu, na kwamba Mungu atashuka chini miongoni mwa watoto wa watu, na atachukua juu yake mwili na damu, na aende usoni mwa dunia—

28 Na sasa, kwa sababu alisema hivi, walimuua; na walifanya vitu vingi ambavyo viliwashushia ghadhabu ya Mungu. Kwa hivyo, ni nani anayeshangaa kwamba wako utumwani, na kwamba wamepigwa kwa mateso makali?

29 Kwani tazameni, Bwana amesema: Mimi [a]sitawafariji watu wangu katika siku ile ya dhambi zao; lakini mimi nitazuia njia zao kwamba wasifanikiwe; na matendo yao yatakuwa ni kama kizuizi mbele yao.

30 Na tena, anasema: Kama watu wangu watapanda [a]uchafu [b]watavuna makapi katika tufani; na matokeo yake ni sumu.

31 Na tena anasema: Kama watu wangu watapanda uchafu watavuna [a]upepo wa mashariki, ambao huleta maangamizo ya ghafla.

32 Na sasa, tazameni, ahadi ya Bwana imetimizwa, na mmepigwa na kusumbuliwa.

26 *a* Mos. 17:12–20.
27 *a* MWM Mungu, Uungu.
b Mwa. 1:26–28; Eth. 3:14–17; M&M 20:17–18.
c Mos. 13:33–34; 15:1–4.
29 *a* 1 Sam. 12:15; 2 Nya. 24:20.
30 *a* MWM Chafu, Uchafu.
b Gal. 6:7–8; M&M 6:33.
MWM Mavuno.
31 *a* Yer. 18:17; Mos. 12:6.

33 Lakini kama [a]mtamrudia Bwana kwa moyo wa lengo moja, na kumwamini, na kumtumikia kwa bidii yote akilini, kama mtafanya hivi, yeye atawaokoa, kutoka utumwani, kulingana na nia yake na mapenzi yake.

MLANGO WA 8

Amoni anawafundisha watu wa Limhi—Anajulishwa kuhusu yale mabamba ishirini na nne ya Kiyaredi—Maandishi ya kale yanaweza kutafsiriwa na waonaji—Hakuna kipawa kikuu kuliko uonaji. Karibia mwaka 121 K.K.

Na ikawa kwamba baada ya mfalme Limhi kumaliza kuwazungumzia watu wake, kwani aliwazungumzia vitu vingi na ni vichache tu nilivyoandika katika kitabu hiki, aliwaambia watu wake vitu vyote kuhusu ndugu zao waliokuwa katika nchi ya Zarahemla.

2 Na akasababisha Amoni asimame mbele ya ule umati, na kuwaelezea yale yote ambayo yaliwapata ndugu zao tangu Zenivu aondoke kutoka nchi ile hadi ule wakati ambao yeye mwenyewe aliondoka kutoka nchi ile.

3 Na pia akakariri yale maneno ya mwisho ambayo mfalme Benjamini aliwafundisha, na akayafafanua kwa watu wa mfalme Limhi, ili wafahamu yale maneno yote ambayo alizungumza.

4 Na ikawa kwamba baada ya kufanya haya yote, kwamba mfalme Limhi alilikiza ule umati, na kusababisha kila mmoja arudi nyumbani kwake.

5 Na ikawa kwamba alisababisha yale mabamba ambayo yalikuwa na [a]maandishi ya watu wake tangu watoke nchi ya Zarahemla, yaletwe mbele ya Amoni, ili ayasome.

6 Sasa, baada ya Amoni kusoma yale maandishi, mfalme alimuuliza kama anajua kutafsiri lugha, na Amoni akamwambia kwamba hangeweza.

7 Na mfalme akamwambia: Nikiwa nimehuzunishwa na masumbuko ya watu wangu, nilisababisha watu wangu arubaini na watatu wasafiri nyikani, ili pengine waweze kuipata nchi ya Zarahemla, ili tuwaombe ndugu zetu watukomboe kutoka utumwani.

8 Na walipotea huko nyikani kwa muda wa siku nyingi, lakini bado walikuwa na bidii, na hawakuipata ile nchi ya Zarahemla lakini walirejea katika nchi hii, baada ya kusafiri katika nchi iliyo miongoni mwa maji mengi, wakiwa wamegundua nchi iliyojaa mifupa ya wanadamu, na ya wanyama, na pia ilijaa mabaki ya majengo ya kila aina, wakiwa wamegundua nchi iliyomilikiwa na watu waliokuwa wengi kama Waisraeli.

9 Na ili kuthibitisha kwamba vitu walivyosema ni vya kweli wameleta mabamba [a]ishirini na nne ambayo yamejaa michoro, na ni ya dhahabu kamili.

10 Na tazama, pia, wameleta

33*a* Morm. 9:6.

8 5*a* Mos. 9–22.

9*a* Eth. 1:1–2.

[a]dirii, ambazo ni kubwa, na ni za [b]shaba nyeupe na shaba nyekundu, na zingali nzuri.

11 Na tena, wameleta panga, ambazo mipini yake imeharibika, na ndimi zake kupata kutu; na hakuna yeyote nchini anayeweza kutafsiri ile lugha au michoro iliyo kwenye mabamba. Kwa hivyo nilikuuliza: Je unaweza kutafsiri?

12 Nakuambia tena: Je, unajua yeyote anayeweza kutafsiri? Kwani natamani kwamba maandishi haya yatafsiriwe katika lugha yetu; kwani, pengine, yatatupatia ufahamu wa baki la wale watu walioangamizwa, kule maandishi haya yalikotokea; au, pengine, yatatupatia ufahamu wa hawa watu ambao wameangamizwa; na natamani kujua sababu ya kuangamizwa kwao.

13 Sasa Amoni akamwambia: Naweza kukuambia kwa uhakika hivi, Ee mfalme, kuna mtu ambaye anaweza [a]kutafsiri maandishi haya; kwani kuna kitu ambacho anaweza kutazama, na kutafsiri maandishi yote ya kale; na ni kipawa kutoka kwa Mungu. Na hivyo vitu vinaitwa [b]vitafsiri, na hakuna mtu yeyote anayeweza kutazama ndani yake bila kuamriwa, la sivyo ataona yale asiyostahili na aangamie. Na yeyote anayeamrishwa kutazama ndani yake, huyo anaitwa [c]mwonaji.

14 Na tazama, mfalme wa watu walio katika nchi ya Zarahemla ndiye yule mtu ambaye ameamriwa kufanya vitu hivi, na aliye na kipawa hiki cha juu kutoka kwa Mungu.

15 Na mfalme akasema kwamba mwonaji ni mkuu zaidi ya nabii.

16 Na Amoni akasema kwamba mwonaji ni mfunuzi na nabii pia; na hakuna kipawa kingine kikuu ambacho mwanadamu anaweza kupata, ila kuwa na uwezo wa Mungu, na hakuna yeyote anayeweza; walakini mwanadamu anaweza kupokea uwezo mkuu kutoka kwa Mungu.

17 Lakini mwonaji anaweza kujua vitu vilivyopita, na pia vitu vitakavyokuja, na kupitia kwao vitu vyote vitafunuliwa, kwa usahihi zaidi, vitu vya siri vitadhihirishwa, na vitu vilivyofichwa kuletwa katika nuru, na vitu visivyojulikana vitajulishwa na kwao, na pia vitu ambavyo havingejulikana vitajulishwa na wao.

18 Kwa hivyo Mungu ametoa njia ili mwanadamu, kwa imani, aweze kutenda miujiza mikuu; kwa hivyo anafaidi zaidi binadamu wenzake.

19 Na sasa, wakati Amoni alipomaliza kuzungumza maneno haya mfalme alifurahia sana, na akamshukuru Mungu, akisema: Bila shaka kuna siri [a]kuu iliyo katika mabamba haya, na vitafsiri hivi bila shaka vilitayarishwa kwa

10 *a* Eth. 15:15.
b Eth. 10:23.
13 *a* Mos. 28:10–17.
b MWM Urimu na Thumimu.
c MWM Mwonaji.
19 *a* Eth. 3:21–28; 4:4–5.

madhumani ya kufunua siri zote za aina hii kwa watoto wa watu.

20 Jinsi gani kazi za Bwana zilivyo za kushangaza, na ni kwa muda gani mrefu ambao anawasubiri watu wake; ndiyo, na jinsi gani watoto wa watu walivyopofuka na hawawezi kupenyeka katika fahamu zao; kwani hawatatafuta hekima, wala hawataki kwamba [a]yeye awatawale wao.

21 Ndiyo, wako kama mifugo wenye kichaa wanaomtoroka mchungaji, na kutawanyika, na kupotea, na kuliwa na wanyama wa mwituni.

Maandishi ya Zenivu—Historia ya watu wake, tangu waondoke nchi ya Zarahemla hadi ule wakati waliokombolewa kutoka mikononi mwa Walamani.

Yenye milango ya 9 hadi 22.

MLANGO WA 9

Zenivu aongoza kikundi kutoka nchi ya Zarahemla ili wamiliki nchi ya Lehi-Nefi—Mfalme wa Walamani anawakubalia kurithi nchi—Kuna vita kati ya Walamani na watu wa Zenivu. Karibia mwaka 200–187 K.K.

Mimi, Zenivu, nikiwa nimefundishwa kwa lugha yote ya Wanefi, na nikiwa ninajua [a]nchi ya Nefi, au nchi ya kwanza ya urithi wa baba zetu, na nikiwa nimetumwa kama mpelelezi miongoni mwa Walamani kwamba nipeleleze jeshi lao, ili jeshi letu liwashambulie na kuwaangamiza—lakini nilipoona yale yaliyokuwa mazuri miongoni mwao sikutaka waangamizwe.

2 Kwa hivyo, nikabishana na ndugu zangu nyikani, kwani nilitaka mtawala wetu afanye mkataba nao; lakini yeye akiwa mwenye ukali na mtu aliyependa kumwaga damu aliamuru kwamba niuawe; lakini niliokolewa kwa umwagaji wa damu nyingi; kwani kulikuwa na vita kati ya baba kwa baba, na kaka kwa kaka, hadi sehemu kubwa ya jeshi letu likaangamizwa huko nyikani; na tukarejea, wale kati yetu waliopona, katika nchi ya Zarahemla, kuelezea watoto wao na mabibi zao kuhusu ule mkasa.

3 Na bado, mimi nikiwa na uharara mkuu wa kurithi nchi ya baba zetu, niliwakusanya wengi waliotaka kwenda na kuimiliki ile nchi, na tukaanza tena safari yetu ya nyikani kuelekea ile nchi; lakini tulipatwa na njaa na mateso makali; kwani hatukumkumbuka Bwana Mungu wetu.

4 Walakini, baada ya kuzunguka huko nyikani siku nyingi tulipiga hema zetu mahali pale ndugu zetu walipouawa, ambapo palikuwa ni karibu na nchi ya babu zetu.

---

20 *a* MY Hekima, jina la kike katika Kiebrania na Kigiriki.

Mit. 9:1; Mt. 11:19.

9 1 *a* 2 Ne. 5:5–8; Omni 1:12.

5 Na ikawa kwamba nilienda tena mjini na watu wangu wanne, kwa mfalme, ili nijue hali ya yule mfalme, na ili nijue kama nitakubaliwa kuingia nchi ile pamoja na watu wangu na kuimiliki kwa amani.

6 Na nikamwendea mfalme, na akaagana na mimi kwamba niimiliki nchi ya Lehi-Nefi, na nchi ya Shilomu.

7 Na pia akaamuru kwamba watu wake waondoke kutoka nchi ile, na mimi na watu wangu tukaingia nchi ile ili tuimiliki.

8 Na tukaanza kujenga majengo, na kurekebisha kuta za mji, ndiyo, hata kuta za mji wa Lehi-Nefi, na mji wa Shilomu.

9 Na tukaanza kulima ile ardhi, ndiyo, kwa kila aina ya mbegu, kwa mbegu za mahindi, na ngano, na shayiri, na nizi, na sheumu, na mbegu za matunda ya aina zote; na tukaanza kuongezeka na kufanikiwa katika nchi ile.

10 Sasa ilikuwa ni ujanja na werevu wa mfalme Lamani, [a]kuwatia watu wangu utumwani, ndipo akaacha nchi ile ili tuimiliki.

11 Kwa hivyo ikawa kwamba, baada ya sisi kuishi katika nchi ile kwa kipindi cha miaka kumi na miwili kwamba mfalme Lamani alianza kuwa na wasiwasi, kwamba watu wangu watakuwa wenye nguvu nyingi katika nchi ile, na kwamba hawangeweza kuwalemea na kuwatia utumwani.

12 Sasa walikuwa watu wavivu na wenye kuabudu [a]sanamu; kwa hivyo walitamani kutuweka utumwani, ili wajikinaishe na jasho la mikono yetu; ndiyo, ili wafanye karamu kwa mifugo ya mashamba yetu.

13 Kwa hivyo ikawa kwamba mfalme Lamani alianza kuwachochea watu wake kwamba wabishane na watu wangu; kwa hivyo kulianza kuwa na vita na mabishano katika nchi ile.

14 Kwani, katika mwaka wa kumi na tatu wa utawala wangu katika nchi ya Nefi, mbali kusini mwa nchi ya Shilomu, wakati watu wangu walipokuwa wanalisha na kunywesha mifugo yao, na kulima mashamba yao, kikundi kikubwa cha Walamani kiliwashukia na kuanza kuwaua, na kuchukua mifugo yao, na nafaka ya mashamba yao.

15 Ndiyo, na ikawa kwamba wale wote ambao hawakupatwa, walitoroka, hadi mji wa Nefi, na wakaniomba ulinzi.

16 Na ikawa kwamba niliwapa silaha kama vile pinde, mishale, panga, na visu, na rungu, na kombeo, na kila aina ya silaha ambayo tungevumbua, na mimi na watu wangu tukaenda kupigana na Walamani.

17 Ndiyo, kwa nguvu za Bwana tulienda kupigana na Walamani; kwani mimi na watu wangu tulimlilia Bwana kwa nguvu ili atukomboe kutoka mikononi mwa maadui zetu, kwani tulikumbushwa kuhusu ukombozi wa babu zetu.

10*a* Mos. 7:21–22.
12*a* Eno. 1:20.

MWM Kuabudu sanamu.

18 Na Mungu [a]alisikia vilio vyetu na akajibu sala zetu; na tukaendelea kwa nguvu zake; ndiyo, tuliwashambulia Walamani, na kwa mchana mmoja na usiku tuliwaua elfu tatu, arubaini na tatu; tuliwaua hadi tukawafukuza kutoka nchi yetu.

19 Na mimi, mwenyewe, kwa mikono yangu, nilisaidia kuzika wafu wao. Na tazama, kwa huzuni yetu kuu na maombolezo, ndugu zetu mia mbili sabini na tisa waliuawa.

MLANGO WA 10

Mfalme Lamani anafariki—Watu wake wanakuwa wakaidi na wakorofi na kuamini mila za uwongo—Zenivu na watu wake wanawalemea. Karibia mwaka 187–160 K.K.

Na ikawa kwamba tulianza tena kuimarisha ufalme na kumiliki nchi ile kwa amani. Na nilisababisha kwamba silaha za kila aina zitengenezwe, ili niwe na silaha kwa watu wangu wakati Walamani wangetushambulia.

2 Na nikaweka walinzi waizingire ile nchi, ili Walamani wasituvamie tena kwa ghafla na kutuangamiza; na hivyo ndivyo nilivyowalinda watu wangu na mifugo yangu, na kuwachunga wasianguke mikononi mwa maadui wetu.

3 Na ikawa kwamba tulirithi nchi ya baba zetu kwa miaka mingi, ndiyo, kwa kipindi cha miaka ishirini na miwili.

4 Na nikasababisha kwamba wanaume walime ardhi, na kupanda kila aina ya [a]nafaka na matunda ya kila aina.

5 Na nikasababisha kwamba wanawake wasokote, na kujitahidi, na kufanya kazi, na kushona kila aina ya kitani bora, ndiyo, na [a]nguo za kila aina, ili tuvishe uchi wetu; na hivyo tulifanikiwa nchini—na hivyo tukaendelea kupata amani nchini kwa kipindi cha miaka ishirini na miwili.

6 Na ikawa kwamba mfalme [a]Lamani alifariki, na mwana wake akaanza kutawala badala yake. Na akaanza kuwachochea watu wake ili wazushe uasi dhidi ya watu wangu; kwa hivyo wakaanza kujitayarisha kwa vita, na kuja kuwashambulia watu wangu.

7 Lakini niliwatuma wapelelezi wangu karibu na nchi ya [a]Shemloni, ili nigundue mipango yao, na kwamba nijikinge na wao, ili wasiwashambulie watu wangu, na kuwaangamiza.

8 Na ikawa kwamba walikuja na kufika kaskazini mwa nchi ya Shilomu, na umati wao mkubwa, wanaume wakiwa [a]wamebeba [b]pinde, na mishale, na panga, na sime, na mawe, na kombeo; na vichwa vyao vilikuwa vimenyolewa kwamba walikuwa uchi; na walikuwa wamejifunga mishipi ya ngozi viunoni mwao.

9 Na ikawa kwamba nilisaba-

18 *a* Mos. 29:20.
10 4 *a* Mos. 9:9.
5 *a* Alma 1:29.
6 *a* Mos. 9:10–11; 24:3.
7 *a* Mos. 11:12.
8 *a* Yar. 1:8.
b Alma 3:4–5.

bisha kwamba wake na watoto wa watu wangu wafichwe nyikani; na pia nikasababisha kwamba wanaume wangu wote wazee ambao wangeweza kubeba silaha, na pia vijana wangu wote ambao wangeweza kubeba silaha, wakusanyike pamoja ili wapigane na Walamani; na nikawapanga kwa mistari, kila mtu kulingana na umri wake.

10 Na ikawa kwamba tulienda kupigana dhidi ya Walamani; na mimi, hata mimi, katika uzee wangu, nilienda kupigana dhidi ya Walamani. Na ikawa kwamba tulienda kwa [a]nguvu za Bwana kupigana.

11 Sasa, Walamani hawakujua lolote kuhusu Bwana, wala nguvu za Bwana, kwa hivyo walitegemea nguvu zao wenyewe. Lakini walikuwa watu wenye nguvu, kulingana na nguvu za wanadamu.

12 Walikuwa [a]wakaidi, na wakorofi, na watu wapendao kumwaga damu, wakiamini [b]mila ya baba zao, ambayo ndiyo hii—Kuamini kwamba walifukuzwa kutoka nchi ya Yerusalemu kwa sababu ya maovu ya baba zao, na kwamba walikosewa huko nyikani na ndugu zao, na kwamba pia walikosewa walipokuwa wakivuka bahari;

13 Na tena, kwamba walikosewa walipokuwa katika nchi ya urithi wao wa [a]kwanza, baada ya kuvuka bahari, na haya yote ni kwa sababu Nefi alikuwa mwaminifu katika kutii amri za Bwana—kwa hivyo, [b]alipendelewa na Bwana, kwani Bwana alisikia sala zake na kuzijibu, na aliwaongoza kwenye safari yao huko nyikani.

14 Na kaka zake walimkasirikia kwa sababu [a]hawakufahamu njia za Bwana; na pia [b]walimkasirikia huko majini kwa sababu walishupaza mioyo yao dhidi ya Bwana.

15 Na tena, walimkasirikia walipowasili katika nchi ya ahadi, kwa sababu walisema kwamba aliondoa [a]utawala wa watu mikononi mwao; na wakajaribu kumuua.

16 Na tena, walimkasirikia kwa sababu alikimbilia nyikani kama vile Bwana alivyokuwa amemwamuru, na akachukua [a]kumbukumbu ambayo iliyokuwa yamechorwa kwenye mabamba ya shaba nyeupe, kwani walisema kwamba [b]aliwapora.

17 Kwa hivyo wamewafundisha wana wao kwamba wawachukie, na kwamba wawaue, na kwamba wawaibie na kuwapora, na kutenda yale yote waliyoweza ili wawaangamize; kwa hivyo wana chuki ya milele kwa wana wa Nefi.

18 Ni kwa sababu hii mfalme Lamani, kwa ujanja wake, na werevu wake, na ahadi zake nzuri, alinidanganya, hata kwamba nikawaleta watu hawa

10*a* MWM Tegemea.
12*a* Alma 17:14.
b 2 Ne. 5:1–3.
13*a* 1 Ne. 18:23.
b 1 Ne. 17:35.
14*a* 1 Ne. 15:7–11.
b 1 Ne. 18:10–11.
15*a* 2 Ne. 5:3.
16*a* 2 Ne. 5:12.
b Alma 20:10, 13.

wangu katika nchi hii, ili wawaangamize; ndiyo, na tumeteseka miaka hii mingi katika nchi.

19 Na sasa mimi, Zenivu, baada ya kuvisema vitu hivi vyote kwa watu wangu kuhusu Walamani, niliwachechemua waende vitani kwa nguvu zao, wakimwamini Bwana; kwa hivyo, tulipigana nao, ana kwa ana.

20 Na ikawa kwamba tuliwafukuza tena kutoka nchi yetu; na tuliwauwa wengi, hata kwamba hatukuweza kuwahesabu.

21 Na ikawa kwamba tulirejea tena kwenye nchi yetu, na watu wangu wakaanza tena kufuga mifugo yao, na kulima mashamba yao.

22 Na sasa mimi, nikiwa mzee, nilitunukia ufalme wangu juu ya mwana wangu mmoja; kwa hivyo, sisemi mengine. Na Bwana awabariki watu wangu. Amina.

MLANGO WA 11

Mfalme Nuhu anatawala kwa uovu—Anajifurahisha kwa maisha ya ulevi pamoja na wake zake na makahaba—Abinadi atoa unabii kwamba hao watu watapelekwa utumwani—Mfalme Nuhu anataka kumuua. Karibia mwaka 160–150 K.K.

Na sasa ikawa kwamba Zenivu aliutawaza ufalme juu ya Nuhu, mmoja wa wanawe; kwa hivyo Nuhu akaanza kutawala badala yake; na hakutembea katika njia za baba yake.

2 Kwani tazama, hakutii amri za Mungu, walakini alifuata tamaa za moyo wake. Na alikuwa na wake wengi na [a]makahaba. Na [b]alisababisha watu wake kutenda dhambi, na kutenda yale ambayo yalikuwa yanamchukiza Bwana. Ndiyo, na walifanya [c]ukahaba na kila aina ya uovu.

3 Na aliwatoza kodi fungu la tano kwa chochote walichokuwa nacho, fungu la tano kwa dhahabu yao na kwa fedha yao, na fungu la tano la [a]zifu yao, na shaba nyekundu yao, na shaba nyeupe yao, na chuma yao; na fungu la tano la mifugo yao; na pia fungu la tano la nafaka yao yote.

4 Na alitenda haya yote ili ajisaidie mwenyewe, na wake zake na makahaba wake; na makuhani wake, na wake zao na masuria wao; na hivyo alibadilisha mipango ya ule ufalme.

5 Kwani aliwateremsha makuhani wote ambao walikuwa wameteuliwa na baba yake, na kuteua wengine wapya mahali pao, na wao walikuwa wamejiinua kwa kiburi cha mioyo yao.

6 Ndiyo, na hivi ndivyo walisaidiwa katika uvivu wao, na ukafiri wao, na ukahaba wao, kwa zile kodi ambazo mfalme Nuhu aliwatoza watu wake;

11 2*a* Yak. (KM) 3:5.
b 1 Fal. 14:15–16; Mos. 29:31.
c 2 Ne. 28:15.

3*a* EBR maneno yanayohusiana: kivumishi, "inayong'aa"; kitenzi, "kuzungushia au kupakaa madini ya chuma."

kwa hivyo watu wafanya kazi mno kusaidia uovu.

7 Ndiyo, na pia wakawa wanaabudu masanamu, kwa sababu walidanganywa na maneno ya bure na ya kusifu ya uongo ya mfalme na makuhani; kwani waliwazungumzia vitu vya ubembelezaji.

8 Na ikawa kwamba mfalme Nuhu alijenga mijengo mingi mizuri na mikubwa; na akairembesha kwa vitu vizuri vya mbao, na kila aina ya vitu vyenye thamani, vya dhahabu, na vya fedha, na vya chuma, na vya shaba nyeupe, na vya zifu, na vya shaba nyekundu;

9 Na pia alijijengea ikulu kubwa, na hapo katikati kiti cha enzi, ambayo yote yalikuwa ya mbao bora na kurembeshwa kwa dhahabu na fedha na vitu vyenye thamani.

10 Na pia akawaamuru mafundi wake lazima wafanye kazi kwa namna yote ya kupendeza kuta za hekalu, kwa mbao nzuri, na shaba nyekundu, na shaba nyeupe.

11 Na viti ambavyo vilikuwa vimewekewa wale makuhani wakuu, ambavyo vilikuwa juu ya viti vingine vyote, alivirembesha kwa dhahabu kamili; na akasababisha vijengewe ua mbele yao, ili wapumzishe miili yao na mikono yao wanapowazungumzia watu wake maneno ya uwongo na yasiyo na busara.

12 Na ikawa kwamba alijenga mnara karibu na hekalu; ndiyo, [a]mnara mrefu sana, hata mrefu sana kwamba angesimama juu yake na kuona nchi ya Shilomu, na pia nchi ya Shemloni, ambayo ilikuwa imemilikiwa na Walamani; na hata angeona nchi yote ambayo ilikuwa imewazingira.

13 Na ikawa kwamba alisababisha mijengo mingi ijengwe katika nchi ya Shilomu; na akasababisha mnara mkubwa ujengwe katika kilima kilichokuwa kaskazini mwa nchi ya Shilomu, ambayo ilikuwa ni kimbilio kwa watoto wa Nefi walipotoroka kutoka nchi ile; na haya alitenda kwa utajiri alioupata kwa kuwatoza watu wake kodi.

14 Na ikawa kwamba aliutia moyo wake katika utajiri wake, na aliutumia wakati wake katika maisha ya anasa na wake zake na masuria wake; na pia makuhani wake waliutumia wakati wao kwa makahaba.

15 Na ikawa kwamba alipanda mizabibu kote nchini mle; na akajenga vishinikizo, na kutegeneza divai kwa wingi; na kwa hivyo akawa [a]mlevi, na pia watu wake.

16 Na ikawa kwamba Walamani walianza kuwashambulia watu wake, kwa vikundi vidogo, na kuwaua mashambani mwao, na walipokuwa wakilisha mifugo yao.

17 Na mfalme Nuhu akatuma walinzi wake nchini kuwafukuza; lakini hakutuma hesabu ya kutosha, na Walamani waliwashambulia na kuwaua, na kuwanyang'anya

12*a* Mos. 19:5–6.

15*a* MWM Neno la Hekima.

mifugo yao kutoka nchini; na hivyo Walamani walianza kuwaangamiza, na kuwafanyia chuki.

18 Na ikawa kwamba mfalme Nuhu aliwatumia jeshi lake; na walisukumwa nyuma, au waliwasukuma nyuma kwa muda; kwa hivyo, walirejea wakifurahia mateka wao.

19 Na sasa, kwa sababu ya ushindi huu mkuu walijiinua sana kwa kiburi cha mioyo yao; [a]walijivunia nguvu zao, wakisema kwamba kikosi chao cha wanajeshi hamsini kiliweza kupigana na wanajeshi maelfu ya Walamani; na hivyo ndivyo walijivuna, na kufurahia damu, na umwagaji wa damu ya ndugu zao, na hii kwa sababu ya uovu wa mfalme wao na makuhani wao.

20 Na ikawa kwamba kulikuwa na mtu miongoni mwao aliyeitwa [a]Abinadi; na alienda miongoni mwao, na akaanza kutoa unabii, akisema: Tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, na ameniamuru hivi, akisema, Nenda, na uwaambie watu hawa, hivi asema Bwana—Ole kwa watu hawa, kwani nimeona machukizo yao, na maovu yao, na ukahaba wao; na wasipotubu nitawatembelea kwa ghadhabu yangu.

21 Na wasipotubu na kumrejea Bwana Mungu wao, tazama, nitawakabidhi mikononi mwa maadui wao; ndiyo, na watawekwa [a]utumwani; na watanyanyaswa kwa mkono wa maadui wao.

22 Na itakuwa kwamba watajua kuwa mimi ni Bwana Mungu wao, na mimi ni Mungu mwenye [a]hamasa, na huadhibu maovu ya watu wangu.

23 Na itakuwa kwamba hawa watu wasipotubu na kumrejea Bwana Mungu wao, watawekwa utumwani; na hakuna yeyote atakayewakomboa, ila tu Bwana Mwenyezi Mungu.

24 Ndiyo, na itakuwa kwamba watakaponililia, [a]nitakawia kusikia vilio vyao; ndiyo, na nitaruhusu maadui wao wawapige.

25 Na wasipotubu kwa gunia na majivu, na wamlilie kwa nguvu Bwana Mungu wao, [a]sitasikia sala zao, wala sitawakomboa kutoka kwa masumbuko yao; na hivyo ndivyo asemavyo Bwana, na ameniamuru hivyo.

26 Na ikawa kwamba wakati Abinadi alipowazungumzia maneno haya walimkasirikia, na walitaka kumtoa uhai wake; lakini Bwana alimkomboa kutoka mikono yao.

27 Sasa wakati mfalme Nuhu aliposikia maneno ambayo Abinadi aliwazungumzia watu wale, na yeye pia alikasirika; na akauliza: Je, Abinadi ni nani, kwamba ahukumu watu wangu na mimi, au Bwana ni [a]nani, hata kwamba ateremshie watu wangu mateso makuu hivi?

28 Nawaamuru kwamba

19 *a* M&M 3:4. MWM Kiburi.
20 *a* MWM Abinadi.
21 *a* Mos. 12:2; 20:21; 21:13–15; 23:21–23.
22 *a* Ku. 20:5; Kum. 6:15; Mos. 13:13.
24 *a* Mik. 3:4; Mos. 21:15.
25 *a* Isa. 1:15; 59:2.
27 *a* Ku. 5:2; Mos. 12:13.

mmlete Abinadi hapa, ili nimuue, kwani amesema vitu hivi ili awachochee watu wangu wakasirikiane mmoja kwa mwingine, na kuzusha mabishano miongoni mwa watu wangu; kwa hivyo nitamuua.

29 Sasa macho ya watu yalikuwa [a]yamepofuka; kwa hivyo [b]walishupaza mioyo yao dhidi ya maneno ya Abinadi, na tangu wakati huo walijaribu kumkamata. Na mfalme Nuhu alishupaza moyo wake dhidi ya neno la Bwana, na hakutubu matendo yake maovu.

MLANGO WA 12

Abinadi atiwa gerezani kwa sababu ya kutoa unabii kuhusu maangamizo ya wale watu na kifo cha Mfalme Nuhu—Makuhani wa uwongo wanataja maandiko na kudai kwamba wanatii amri za Musa—Abinadi anaanza kuwafundisha Amri Kumi. Karibia mwaka 148 K.K.

Na ikawa kwamba baada ya kipindi cha miaka miwili kwamba Abinadi alikuja miongoni mwao kwa kujificha, na hawakumjua, na akaanza kutoa unabii miongoni mwao, akisema: Bwana ameniamuru hivi, akisema—Abinadi, enda ukawatolee watu hawa wangu unabii, kwani wameshupaza mioyo yao dhidi ya maneno yangu; hawajatubu matendo yao maovu; kwa hivyo, [a]nitawatembelea kwa ghadhabu yangu, ndiyo, katika ghadhabu yangu kali nitawaadhibu kwa sababu ya uovu na machukizo yao.

2 Ndiyo, ole kwa uzao huu! Na Bwana akaniambia: Nyosha mkono wako na utoe unabii, ukisema: hivyo ndivyo asemavyo Bwana, itakuwa kwamba uzao huu, kwa sababu ya uovu wao, watatiwa [a]utumwani, na watapigwa [b]shavuni; ndiyo, na watafukuzwa na watu, na kuuawa; na koho wa angani, na mbwa, ndiyo, na wanyama wa mwituni, watakula miili yao.

3 Na itakuwa kwamba [a]maisha ya mfalme Nuhu yatakuwa na thamani kama nguo iliyo katika [b]tanuru, kwani atajua kwamba Mimi ni Bwana.

4 Na itakuwa kwamba nitawapiga watu wangu hawa kwa mapigo makali, ndiyo, kwa njaa na [a]tauni; na nitawasababisha [b]walie siku yote.

5 Ndiyo, na nitafanya wabebe [a]mizigo migongoni mwao; na wataendeshwa kama punda bubu.

6 Na itakuwa kwamba nitateremsha mvua ya mawe miongoni mwao, na itawapiga; na pia watapigwa na [a]upepo wa mashariki; na [b]wadudu watasumbua nchi yao pia, na kuharibu nafaka yao.

7 Na watapigwa kwa maradhi makuu—na nitatenda haya

29 *a* Musa 4:4.
b Alma 33:20; Eth. 11:13.
12 1 *a* Isa. 65:6.
2 *a* Mos. 11:21; 20:21; 21:13–15; 23:21–23.
b Mos. 21:3–4.
3 *a* Mos. 12:10.
b Mos. 19:20.
4 *a* M&M 97:26.
b Mos. 21:9–10.
5 *a* Mos. 21:3.
6 *a* Yer. 18:17; Mos. 7:31.
b Ku. 10:1–12.

yote kwa sababu ya [a]maovu yao na machukizo yao.

8 Na itakuwa kwamba wasipotubu [a]nitawaangamiza kutoka uso wa dunia; walakini wataacha [b]maandishi yao nyuma, na nitayahifadhi kwa mataifa mengine ambayo yataimiliki nchi; ndiyo, nitafanya haya ili niyadhihirishie mataifa mengine machukizo ya watu hawa. Na Abinadi alitoa unabii wa vitu vingi dhidi ya watu hawa.

9 Na ikawa kwamba walimkasirikia; na wakamchukua na kumpeleka mbele ya mfalme akiwa amefungwa, na wakamwambia mfalme: Tazama, tumemleta mtu mbele yako ambaye ametoa unabii mwovu kuhusu watu wako, na kusema kwamba Mungu atawaangamiza.

10 Na pia anatoa unabii mwovu kuhusu maisha yako, na kusema kwamba maisha yako yatakuwa kama nguo iliyo katika tanuru la moto.

11 Na tena, anasema utakuwa kama ubua, hata kama ubua wa shambani uliokauka, ambao unakimbiwa na wanyama na kukanyagwa kwa miguu.

12 Na tena, anasema wewe utakuwa kama maua ya mwiba, ambayo, kama limeiva, na kama upepo ukivuma, linapeperushwa kokote usoni mwa nchi. Na anadai kwamba Bwana ameyasema. Na anasema kwamba haya yote yatakupata usipotubu, na haya ni kwa sababu ya maovu yako.

13 Na sasa, Ee mfalme, ni uovu gani mkuu uliotenda, au ni dhambi gani kuu ambazo watu wako wametenda, hata kwamba tuhukumiwe na Mungu au tuhukumiwe na mtu huyu?

14 Na sasa, Ee mfalme, tazama, hatuna hatia, na wewe, Ee mfalme, hujatenda dhambi; kwa hivyo, mtu huyu amesema uwongo kukuhusu, na ametoa unabii wa bure.

15 Na tazama, tuna nguvu, hatutatiwa utumwani, au kutekwa nyara na maadui wetu; ndiyo, na wewe umefanikiwa nchini, na wewe pia utafanikiwa.

16 Tazama, mtu huyo ndiye huyu hapa, tunamkabidhisha mikononi mwako; unaweza kufanya utakavyo naye.

17 Na ikawa kwamba mfalme Nuhu aliamuru kwamba Abinadi atiwe gerezani; na akaamuru kwamba [a]makuhani wakusanyike pamoja ili wafanye baraza na yeye kuhusu kile atakachomtendea.

18 Na ikawa kwamba walimwambia mfalme: Mlete hapa ili tumwulize maswali; na mfalme akaamuru kwamba aletwe mbele yao.

19 Na wakaanza kumwuliza maswali, ili wamfanye ajikanushe, ili wapate sababu ya kumlaumu; lakini akawajibu kwa ujasiri, na kujibu maswali yao yote, ndiyo, kwa mshangao wao; kwani [a]alivumilia maswali yao yote, na kuwaduwaza katika maneno yao yote.

20 Na ikawa kwamba mmoja

7 *a* M&M 3:18.
8 *a* Alma 45:9–14.
b Morm. 8:14–16.
17 *a* Mos. 11:11.
19 *a* M&M 100:5–6.

wao alimuuliza: Je, nini maana ya maneno ambayo yameandikwa, na ambayo yamefundishwa na baba zetu, yakisema:

21 [a]Jinsi gani ilivyo vizuri juu ya milima miguu yake aletaye habari njema; anayeleta amani; anayeleta habari njema ya mambo mema; aletaye wokovu; anayeiambia Sayuni, Mungu wako anatawala;

22 Walinzi wako watapaza sauti; kwa sauti moja wote wataimba; kwani wataona jicho kwa jicho Bwana atakapoleta tena Sayuni;

23 Shangilieni kwa shangwe; imbeni pamoja enyi mahali pa ukiwa pa Yerusalemu; kwani Bwana amefariji watu wake, amekomboa Yerusalemu;

24 Bwana ameuweka [a]mkono wake mtakatifu wazi mbele ya macho ya mataifa yote, na nchi zote za ulimwengu zitauona wokovu wa Mungu?

25 Na sasa Abinadi akawaambia: Je, ninyi ni [a]makuhani, na mnadai kwamba mnafundisha watu hawa, na kwamba mnafahamu roho ya kutoa unabii, na bado mnataka kujua kutoka kwangu maana ya vitu hivi?

26 Nawaambia, ole wenu kwa sababu ya kuchafua njia za Bwana! Kwani kama mmefahamu vitu hivi hamjavifundisha; kwa hivyo, mmechafua njia za Bwana.

27 Hamjajitolea mioyo yenu kwa [a]ufahamu; kwa hivyo, hamjawa wenye hekima. Kwa hivyo, ni kitu gani ambacho mnawafundisha watu hawa?

28 Na wakasema: Tunafundisha sheria ya Musa.

29 Na tena akawaambia: Ikiwa mnafundisha [a]sheria ya Musa kwa nini hamuitii? Kwa nini mnaweka mioyo yenu kwa utajiri? Kwa nini mnatenda [b]ukahaba na kupoteza nguvu zenu na makahaba, ndiyo, na kufanya watu hawa watende dhambi, kwamba Bwana ana sababu ya kunituma nitoe unabii kinyume cha watu hawa, ndiyo, hata uovu mkuu dhidi ya watu hawa?

30 Je, hamjui kwamba nazungumza ukweli? Ndiyo, mnajua kwamba nazungumza ukweli; na inawapasa kutetemeka mbele ya Mungu.

31 Na itakuwa kwamba mtapigwa kwa sababu ya maovu yenu, kwani mmesema kwamba mnafundisha sheria ya Musa. Na nini mnachoelewa kuhusu sheria ya Musa? [a]Je, wokovu unakuja kwa sheria ya Musa? Mnasema nini?

32 Na wakamjibu kwamba wokovu unakuja kwa sheria ya Musa.

33 Lakini sasa Abinadi akawaambia: Najua kwamba mkitii amri za Mungu mtaokolewa; ndiyo, kama mtatii amri ambazo Bwana alimpatia Musa katika mlima wa [a]Sinai, akisema:

34 [a]Mimi ndimi Bwana Mungu

21 *a* Isa. 52:7–10; Nah. 1:15.
24 *a* 1 Ne. 22:11.
25 *a* Mos. 11:5.
27 *a* MWM Ufahamu.
29 *a* MWM Torati ya Musa.
b MWM Uzinzi.
31 *a* Mos. 3:15; 13:27–32; Alma 25:16.
33 *a* Ku. 19:9, 16–20; Mos. 13:5.
34 *a* Ku. 20:2–4.

wako, [b]aliyekutoa kutoka nchi ya Misri, kutoka nyumba ya utumwa.

35 Usiwe na Mungu [a]mwingine zaidi yangu.

36 Usijifanyie sanamu ya kuchonga, au mfano wa chochote kilicho juu mbinguni, au vitu vilivyo chini duniani.

37 Sasa Abinadi akawauliza, Je, mmefanya haya yote? Nawaambia ninyi, La, hamjafanya. Na [a]mmewafundisha hawa watu watende vitu hivi vyote? Nawaambia, La, hamjafanya hivyo.

MLANGO WA 13

Abinadi analindwa kwa nguvu takatifu—Anafundisha Amri Kumi—Wokovu hauji kwa sheria ya Musa pekee—Mungu Mwenyewe atafanya upatanisho na awakomboe watu Wake. Karibia mwaka 148 K.K.

Na sasa mfalme alipoyasikia maneno haya, aliwaambia makuhani wake: Mwondolee huyu mtu mbali, na mwuueni; kwani tutafanya nini na yeye, kwani ana kichaa.

2 Na wakasimama na kumsogelea na kujaribu kumkamata; lakini aliwazuia, na akawaambia:

3 Msiniguse, kwani Mungu atawapiga mkinishika, kwani sijatoa ujumbe ambao Bwana alinituma kuutoa; wala sijawaambia yale ambayo [a]mliniuliza niwaambie; kwa hivyo, Mungu hatakubali kwamba niangamizwe sasa.

4 Lakini lazima nitimize amri ambazo Mungu ameniamuru; na kwa sababu nimewaambia ukweli mnanikasirikia. Na tena, kwa sababu nimezungumza neno la Mungu mmenihukumu kuwa mimi nina kichaa.

5 Na sasa ikawa kwamba baada ya Abinadi kuzungumza maneno haya watu wa mfalme Nuhu hawakumkamata tena, kwani Roho wa Bwana alikuwa na yeye; na uso wake [a]ulimetameta kwa mng'aro mkuu, hata vile uso wa Musa ulivyong'ara katika mlima wa Sinai, alipokuwa akizungumza na Bwana.

6 Na alizungumza kwa [a]uwezo na mamlaka kutoka kwa Mungu; na akaendelea na maneno yake, akisema:

7 Mnaona kwamba hamna uwezo wa kuniua, kwa hivyo namaliza ujumbe wangu. Ndiyo, na ninaona kwamba [a]inawakera mioyoni yenu kwa sababu nimewaambia ukweli kuhusu maovu yenu.

8 Ndiyo, na maneno yangu yanawajaza na mshangao na bumbuwazi, na hasira.

9 Lakini namaliza ujumbe wangu; na kisha haijalishi ni wapi nitakapoenda, ikiwa kama nitaokolewa.

10 Lakini nawaambia haya, yale mtakayonifanyia, baada ya haya, yatakuwa ni kama [a]mfano

34*b* Ku. 12:51; 1 Ne. 17:40; Mos. 7:19.
35*a* Hos. 13:4.
MWM Kuabudu sanamu.
37*a* Mos. 13:25–26.
13 3*a* Mos. 12:20–24.
5*a* Ku. 34:29–35.
6*a* MWM Uwezo.
7*a* 1 Ne. 16:2.
10*a* Mos. 17:13–19; Alma 25:10.

au kivuli cha vitu vitakavyokuja.

11 Na sasa nitawasomea [a]amri za Mungu zilizosalia, kwani nahisi kwamba hazijaandikwa mioyoni yenu; nahisi kwamba mmesoma na kufundisha uovu kwa muda mrefu maishani mwenu.

12 Na sasa, mnakumbuka kwamba niliwaambia: Hamtajitengenezea sanamu ya kuchonga, au mfano wa vitu vyovyote vilivyo juu mbinguni, au vilivyo chini ardhini, au vilivyo majini chini ya ardhi.

13 Na tena: Hamtaviinamia, wala kuvitumikia; kwani mimi Bwana Mungu wako ni Mungu wa hamasa, niteremshiaye watoto maovu ya babu zao, kwa kizazi cha tatu na cha nne kwa wale wanaonichukia;

14 Na kuonyesha rehema kwa maelfu ya wale wanaonipenda na kutii amri zangu.

15 Usichukue jina la Bwana Mungu wako bure; kwani Bwana hatamfikiria kama asiye na hatia yule anayechukua jina lake bure.

16 Kumbuka siku ya [a]sabato, kuiweka takatifu.

17 Utafanya kazi kwa siku sita, na kufanya kazi yako yote.

18 Lakini siku ya saba, sabato ya Bwana Mungu wako, usifanye kazi yoyote, wewe, wala mwana wako, wala binti wako, wala mtumishi wako wa kiume, wala mjakazi wako, wala mifugo yako, wala mgeni wako anayeishi nawe;

19 Kwani kwa siku [a]sita Bwana aliumba mbingu na dunia, na bahari, na vyote vilivyo ndani yake; kwa hivyo Bwana aliibariki siku ya sabato, na kuitakasa.

20 [a]Heshimu baba yako na mama yako, ili maisha yako yawe marefu katika ya nchi ambayo Bwana Mungu wako amekupatia.

21 [a]Usiue.

22 [a]Usizini. [b]Usiibe.

23 Usitoe [a]ushahidi wa uwongo dhidi ya jirani yako.

24 [a]Usitamani nyumba ya jirani yako, usitamani mke wa jirani yako, wala mfanyi kazi wake, wala mjakazi wake, wala dume wake, wala punda wake, wala chochote cha jirani yako.

25 Na ikawa kwamba baada ya Abinadi kumaliza kusema maneno haya kwamba akawaambia: Mmewafundisha watu hawa kutii vitu hivi vyote ili watii amri hizi?

26 Nawaambia, La; kwani kama mngekuwa mmefanya hivyo, Bwana hangenisababisha nije na nitoe unabii wa uovu kuhusu watu hawa.

27 Na sasa mmesema kwamba wokovu huja kwa [a]sheria ya Musa. Nawaambia kwamba ni muhimu mtii sheria ya Musa sasa;lakininawaambia,kwamba

11 *a* Ku. 20:1–17.
16 *a* MWM Siku ya Sabato.
19 *a* Mwa. 1:31.
20 *a* Mk. 7:10.
21 *a* Mt. 5:21–22; M&M 42:18.
MWM Mauaji.
22 *a* MWM Uzinzi.
b MWM Iba, Wizi.
23 *a* Mit. 24:28.
MWM Kusema uongo.
24 *a* MWM Tamani.
27 *a* MWM Torati ya Musa.

wakati utafika ambapo [b]haitakuwa muhimu kutii sheria ya Musa.

28 Na juu ya hayo, nawaambia, kwamba [a]wokovu hauji kwa [b]sheria pekee; na kama sio kwa sababu ya [c]upatanisho, ambao Mungu atautoa kwa sababu ya dhambi na uovu wa watu wake, kwamba lazima waangamie, ingawa sheria ya Musa ipo.

29 Na sasa nawaambia kwamba ilikuwa lazima kwamba wana wa Israeli wapewe sheria, ndiyo, sheria iliyo [a]ngumu, kwani walikuwa watu wenye shingo ngumu, walio na [b]haraka ya kutenda maovu, na wavivu kwa kumkumbuka Bwana Mungu wao;

30 Kwa hivyo kulikuwa na [a]sheria ambayo walipewa, ndiyo, sheria ya sherehe na [b]masharti, sheria ambayo walitakiwa [c]kuitii siku kwa siku, ili kuwakumbusha Mungu na jukumu lao kwake.

31 Lakini tazama, nawaambia, kwamba vitu hivi vyote vilikuwa ni [a]mfano wa vile vitakavyokuja.

32 Na sasa, je, walifahamu sheria? Nawaambia, La, wote hawakufahamu ile sheria; na hii ni kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao; kwani hawakufahamu kwamba hakuna yeyote angeokolewa [a]ila tu kwa ukombozi wa Mungu.

33 Kwani tazama, si Musa aliwatolea unabii kuhusu kuja kwa Masiya, na kwamba Mungu atawakomboa watu wake? Ndiyo, na hata manabii [a]wote ambao wametoa unabii tangu mwanzo wa ulimwengu—Je, hawajanena mengi au machache kuhusu vitu hivi?

34 Je, hawajasema kwamba [a]Mungu mwenyewe atashuka chini miongoni mwa watoto wa watu, na ajivike hali ya mwanadamu, na atembee usoni mwa dunia kwa uwezo mkuu?

35 Ndiyo, na je, hawakusema pia kwamba atawezesha [a]ufufuo wa wafu, na kwamba yeye, mwenyewe, atanyanyaswa na kusumbuliwa?

MLANGO WA 14

Isaya huzungumza kuhusu Masiya—Manyanyaso na mateso ya Masiya yanafafanuliwa—Anatoa nafsi Yake kama malipo ya dhambi na kutetea wanaovunja sheria—Linganisha Isaya 53. Karibia mwaka 148 K.K.

Ndiyo, si hata Isaya anasema: Ni nani ambaye ameamini ujumbe wetu, na ni kwa nani mkono wa Bwana umefunuliwa?

2 Kwani atakua mbele yake

27 *b* 3 Ne. 9:19–20; 15:4–5.
28 *a* Gal. 2:16.
MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi; Wokovu.
b Gal. 2:21; Mos. 3:14–15; Alma 25:15–16.
c MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
29 *a* Yos. 1:7–8.
b Alma 46:8.
30 *a* Ku. 20.
b MWM Ibada.
c Yak. (KM) 4:5.
31 *a* Mos. 16:14; Alma 25:15.
MWM Uashiriaji.
32 *a* 2 Ne. 25:23–25.
33 *a* 1 Ne. 10:5; Yak. (KM) 4:4; 7:11.
34 *a* Mos. 7:27; 15:1–3.
MWM Mungu, Uungu.
35 *a* Isa. 26:19; 2 Ne. 2:8.

kama mmea mwororo, na kama mzizi kutoka nchi kavu; hana umbo nzuri wala urembo; na tutakapomuona hana urembo wa kutuvutia.

3 Amechukiwa na kukataliwa na watu; mtu wa huzuni, na aliyezoea huzuni; na tukaficha nyuso zetu kutoka kwake; alichukiwa, na hatukumheshimu.

4 Kwa hakika [a]amechukua [b]ghamu zetu, na kubeba huzuni zetu; na tulimdhania kuwa amepigwa, na Mungu, na kuteswa.

5 Lakini alijeruhiwa kwa [a]makosa yetu, alichubuliwa kwa maovu yetu; adhabu ya amani yetu ilikuwa juu yake; na kwa mapigo yake [b]tunaponywa.

6 Sisi sote, kama [a]kondoo, tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake; na Bwana amemwekea maovu yetu sisi sote.

7 Alidhulumiwa, na aliteswa, lakini hakufungua kinywa chake; [a]yeye analetwa kama [b]mwanakondoo machinjoni, na kama vile kondoo ni bubu mbele ya wanaokata manyoya yake hakufungua kinywa chake.

8 Alichukuliwa kutoka gerezani na kutoka kwenye hukumu; na ni nani atatangaza uzazi wake? Kwani aliondolewa kutoka nchi ya wanaoishi; kwa makosa ya watu wangu alipigwa.

9 Na kaburi lake lilikuwa pamoja na waovu, na [a]matajiri kifoni mwake; kwa sababu hakuwa ametenda [b]uovu wowote, wala hapakuwa na uwongo wowote kinywani mwake.

10 Lakini Bwana alipendezwa kumchubua; amemhuzunisha; utakapotoa nafsi yake kuwa dhabihu ya dhambi ataona [a]uzao wake, ataongeza siku zake, na mapenzi ya Bwana yatafanikiwa mkononi mwake.

11 Ataona taabu ya nafsi yake, na kuridhika; kwa maarifa yake mtumishi wangu mwenye haki atawafanya wengi kuwa wenye haki; kwani [a]atayachukua maovu yao.

12 Kwa hivyo nitamgawia sehemu pamoja na wakuu, na atagawanya nyara pamoja na mashujaa; kwa sababu ametoa nafsi yake hata kufa; na akahesabiwa na wenye dhambi; na alibeba dhambi za wengi, na [a]kuwatetea wenye dhambi.

MLANGO WA 15

Vile Kristo alivyo Baba na Mwana—Atawatetea na kujitwika uvunjifu wa sheria wa Watu—Wao na manabii wote watakatifu ni uzao Wake—Analeta Ufufuo—Watoto wadogo wana uzima wa milele. Karibia mwaka 148 K.K.

Na sasa Abinadi akawaambia:

14 4*a* Alma 7:11–12.
b Mt. 8:17.
5*a* Mos. 15:9; Alma 11:40.
b 1 Pet. 2:24–25.
6*a* Mt. 9:36; 2 Ne. 28:14; Alma 5:37.
7*a* Mk. 15:3. MWM Yesu Kristo.
b MWM Mwanakondoo wa Mungu; Pasaka.
9*a* Mt. 27:57–60; Mk. 15:27, 43–46. MWM Yusufu wa Arimathaya.
b Yn. 19:4.
10*a* Mos. 15:10–13.
11*a* Law. 16:21–22; 1 Pet. 3:18; M&M 19:16–19.
12*a* 2 Ne. 2:9; Mos. 15:8; Moro. 7:27–28.

Nataka mfahamu kwamba [a]Mungu mwenyewe atashuka miongoni mwa watoto wa watu, na [b]atawakomboa watu wake.

2 Na kwa sababu [a]anaishi katika mwili ataitwa Mwana wa Mungu, na akiwa ameweka mwili kuwa chini ya mapenzi ya [b]Baba, akiwa Baba na Mwana—

3 Baba, kwa [a]sababu [b]alizaliwa kwa nguvu za Mungu; na Mwana, kwa sababu ya mwili; kwa hivyo akawa Baba na Mwana—

4 Na wao ni [a]Mungu mmoja, ndiyo, yule yule [b]Baba wa [c]Milele wa mbingu na wa dunia.

5 Na hivyo mwili ukiwa chini ya Roho, au Mwana kwa Baba, wakiwa Mungu mmoja, [a]anateswa kwa majaribio, na hakubali majaribio, lakini anakubali afanyiwe mzaha, na [b]kupigwa, na kutupwa nje, na [c]kukataliwa na watu wake.

6 Na baada ya haya yote, baada ya kutenda miujiza mingi mikuu miongoni mwa watoto wa watu, ataongozwa, ndiyo, hata [a]kama vile Isaya aliposema, kama vile kondoo huwa bubu mbele ya yule anayemnyoa, kwa hivyo [b]hakufungua kinywa chake.

7 Ndiyo, hata hivyo ataongozwa, [a]asulubiwe, na kuuawa, mwili ule ukinyenyekea hata hadi mauti, [b]nia ya Mwana ikimezwa na nia ya Baba.

8 Na hivyo ndivyo Mungu anavyokata [a]kamba za kifo, baada ya [b]kushinda mauti; akimpa Mwana uwezo wa [c]kutetea watoto wa watu—

9 Baada ya kupaa mbinguni, na kuwa na moyo wa rehema; akiwa amejawa na upendo kwa watoto wa watu; na kusimama kati yao na haki; baada ya kukata kamba za kifo, na kujitwika [a]mwenyewe maovu yao na makosa yao, baada ya kuwakomboa, na [b]kutosheleza madai ya haki.

10 Na sasa nawaambia, ni nani atakayetangaza kizazi chake? Tazama, nawaambia, kwamba baada ya nafsi yake kutolewa kama dhabihu ya dhambi ataona [a]uzao wake. Na sasa mnasema nini? Na ni nani atakuwa uzao wake?

11 Tazama nawaambia, kwa-

15 1*a* 1 Tim. 3:16; Mos. 13:33–34. MWM Yesu Kristo.
b MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
2*a* Mos. 3:5; 7:27; Alma 7:9–13.
b Isa. 64:8; Yn. 10:30; 14:8–10; Mos. 5:7; Alma 11:38–39; Eth. 3:14.
3*a* M&M 93:4.
b Lk. 1:31–33; Mos. 3:8–9; Alma 7:10; 3 Ne. 1:14.
4*a* Kum. 6:4; Yn. 17:20–23. MWM Mungu, Uungu.
b Mos. 3:8; Hel. 14:12; 3 Ne. 9:15; Eth. 4:7.
c Alma 11:39.
5*a* Lk. 4:2; Ebr. 4:14–15.
b Yn. 19:1.
c Mk. 8:31; Lk. 17:25.
6*a* Isa. 53:7.
b Lk. 23:9; Yn. 19:9; Mos. 14:7.
7*a* MWM Kusulubiwa.
b Lk. 22:42; Yn. 6:38; 3 Ne. 11:11.
8*a* Mos. 16:7; Alma 22:14.
b Hos. 13:14; 1 Kor. 15:55–57.
c 2 Ne. 2:9.
9*a* Isa. 53; Mos. 14:5–12.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
10*a* Isa. 53:10; Mos. 5:7; 27:25; Moro. 7:19.

mba yeyote ambaye amesikia maneno ya [a]manabii, ndiyo, manabii wote watakatifu ambao wametoa unabii kuhusu kuja kwa Bwana—Nawaambia, kwamba wale wote ambao wamesikia maneno yao, na kuamini kwamba Bwana atawakomboa watu wake, na kuitazamia siku ile kwa msamaha wa dhambi zao, nawaambia, kwamba hawa ni uzao wake, au ndiyo warithi wa [b]ufalme wa Mungu.

12 Kwani hawa ndiyo wale dhambi zao [a]amebeba; hawa ndiyo aliwafia, kuwakomboa kutoka kwa makosa yao. Na sasa, je, wao sio uzao wake?

13 Ndiyo, je, na sio manabii, kila mmoja aliyefungua kinywa chake kutoa unabii, na hajaanguka kwenye makosa, namaanisha manabii wote watakatifu tangu mwanzo wa ulimwengu? Nawaambia kwamba wao ni uzao wake.

14 Na hawa ndiyo [a]wameitangaza amani, walioleta habari njema ya mambo mazuri, ambao wametangaza wokovu; na kuiambia Sayuni: Mungu wako anatawala!

15 Na Ee jinsi gani miguu yao ilivyo mizuri juu ya milima!

16 Na tena, jinsi gani ilivyo mizuri juu ya milima miguu ya wale ambao bado wanatangaza amani!

17 Na tena, jinsi gani ilivyo mizuri juu ya milima miguu ya wale watakaoitangaza amani baadaye, ndiyo, kutoka wakati huu hadi milele!

18 Na tazama, nawaambia, hii sio yote. Kwani Ee jinsi gani ilivyo rembo juu ya milima [a]miguu ya yule anayeleta habari njema, ambaye ni mwanzilishi wa [b]amani, ndiyo, hata Bwana, ambaye amewakomboa watu wake; ndiyo, yule ambaye amewapatia watu wake wokovu;

19 Kwani kama sio kwa sababu ya ukombozi aliowatolea watu wake, ambao ulitayarishwa tangu [a]msingi wa ulimwengu, nawaambia, kama sio kwa sababu hii, wanadamu wote lazima [b]wangeangamia.

20 Lakini tazama, kamba za kifo zitakatwa, na Mwana anatawala, na ana nguvu juu ya wafu; kwa hivyo, anawezesha ufufuo wa wafu.

21 Na kutakuja ufufuo, hata [a]ufufuo wa kwanza; ndiyo, hata ufufuo wa wale ambao walikuwa, na ambao wapo, na wale watakaokuwa, hadi hata ufufuo wa Kristo—kwani ataitwa hivyo.

22 Na sasa, ufufuo wa manabii wote, na wale wote ambao wameamini maneno yao, au wale wote ambao wametii amri za Mungu, watakuja mbele wakati wa ufufuo wa kwanza; kwa

11 *a* M&M 84:36–38.
b MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni; Wokovu.
12 *a* Mos. 14:12; Alma 7:13; 11:40–41.
14 *a* Isa. 52:7; Rum. 10:15; 1 Ne. 13:37; Mos. 12:21–24. MWM Kazi ya kimisionari.
18 *a* 3 Ne. 20:40; M&M 128:19.
b Yn. 16:33. MWM Amani.
19 *a* Mos. 4:6.
b 2 Ne. 9:6–13.
21 *a* Alma 40:16–21.

hivyo, wao ndiyo ufufuo wa kwanza.

23 Wanainuliwa ili [a]waishi na Mungu ambaye amewakomboa; kwa hivyo wanao uzima wa milele kupitia Kristo, ambaye [b]amekata kamba za kifo.

24 Na hawa ndiyo wale ambao wana nafasi katika ufufuo wa kwanza; na hawa ndiyo wale waliokufa mbele ya kuja kwa Kristo, walipokuwa hawajui, na hawakuwa wamehubiriwa [a]wokovu. Na hivi ndivyo Bwana huleta uamsho wa hawa; na wanayo nafasi katika ufufuo wa kwanza, au wanao uzima wa milele, baada ya kukombolewa na Bwana.

25 Na [a]watoto wachanga nao pia wana uzima wa milele.

26 Lakini tazama, na [a]uogope, na utetemeke mbele ya Mungu, kwani inakubidi kutetemeka; kwani Bwana hawakomboi wale [b]wanaomuasi na [c]kufa katika dhambi zao; ndiyo, hata wale wote ambao wameangamia katika dhambi zao tangu mwanzo wa ulimwengu, wale ambao kwa hiari yao wamemuasi Mungu, wale ambao wamezijua amri za Mungu, na hawazitii; [d]hawa ndiyo wale ambao [e]hawana nafasi katika ufufuo wa kwanza.

27 Kwa hivyo haiwapasi kutetemeka? Kwani wokovu hauji kwa kama hawa; kwani Bwana hajakomboa kama hawa; ndiyo, wala Bwana hawezi kukomboa kama hawa; kwani hawezi kujikanusha; kwani hawezi kuzuia [a]haki inapohitajika.

28 Na sasa nawaambia kwamba wakati unafika ambapo wokovu wa Bwana [a]utatangazwa katika kila taifa, kabila, lugha, na watu.

29 Ndiyo, Bwana, [a]walinzi wako watapaza sauti yao; kwa sauti pamoja wataimba; kwani wataonana ana kwa ana, wakati Bwana atakapoleta tena Sayuni.

30 Shangilieni, imbeni pamoja, enyi mahali pa ukiwa pa Yerusalemu; kwani Bwana amewafariji watu wake, amekomboa Yerusalemu.

31 Bwana ameuweka mkono wake wazi mbele ya macho ya mataifa yote; na nchi zote za ulimwengu zitaona wokovu wa Mungu wetu.

MLANGO WA 16

Mungu hukomboa wanadamu kutoka hali yao ya kuanguka—Wale ambao wana tamaa za kimwili wanaishi kama kwamba hakuna ukombozi—Kristo husababisha kutimizwa ufufuo kwa maisha ya milele au laana ya milele. Karibia mwaka 148 K.K.

Na sasa, ikawa kwamba baada

23 *a* Zab. 24:3–4; 1 Ne. 15:33–36; M&M 76:50–70.
b MWM Mauti ya Kimwili.
24 *a* 2 Ne. 9:25–26; M&M 137:7.
25 *a* M&M 29:46; 137:10. MWM Wokovu—Wokovu wa watoto.
26 *a* Kum. 5:29; Yak. (KM) 6:9.
b 1 Ne. 2:21–24.
c Eze. 18:26; 1 Ne. 15:32–33; Moro. 10:26.
d Alma 40:19.
e M&M 76:81–86.
27 *a* Alma 34:15–16; 42:1.
28 *a* MWM Kazi ya kimisionari.
29 *a* MWM Kesha, Walinzi.

ya Abinadi kuzungumza maneno haya alinyosha mkono wake na kusema: Wakati utakuja ambapo wote wataona [a]wokovu wa Bwana; wakati kila taifa, kabila, lugha, na watu wataona ana kwa ana na [b]kutubu kwa Mungu kwamba hukumu zake ni za haki.

2 Na kisha waovu [a]watatupwa nje, na watakuwa na sababu ya kupiga makelele, na [b]kulia, na kuomboleza, na kusaga meno yao; na haya ni kwa sababu hawakutii sauti ya Bwana; kwa hivyo Bwana hatawakomboi.

3 Kwani wana [a]tamaa na uibilisi, na [b]ibilisi ana uwezo juu yao; ndiyo, hata yule nyoka wa kale [c]aliyewadanganya wazazi wetu wa kwanza, ambayo ilikuwa ni sababu ya [d]kuanguka kwao; ambayo ni sababu ya wanadamu wote kuwa na tamaa, tamaa za kimwili, uibilisi, [e]kujua uovu na wema, na kujitolea kwa ibilisi.

4 Hivyo wanadamu wote [a]walipotea; na tazama, wangekuwa wamepotea daima kama sio kwamba Mungu aliwakomboa watu wake kutoka hali yao ya upotevu.

5 Lakini kumbuka kwamba yule anayeendelea na kufuata hali yake ya [a]tamaa, na kuendelea katika njia za dhambi na kumuasi Mungu, hubaki katika hali yake ya kuanguka na ibilisi ana uwezo wote juu yake. Kwa hivyo kwake yeye ni kama [b]ukombozi haukufanywa, akiwa adui kwa Mungu; na pia ibilisi ni adui wa Mungu.

6 Na sasa kama Kristo hangekuja ulimwenguni, akizungumza kuhusu vitu vitakavyokuja [a]kama tayari vimeshakuja, hakungekuwa na ukombozi.

7 Na kama Kristo hangefufuka kutoka kwa wafu, au kuvunja kamba za kifo kwamba kaburi lisiwe na ushindi, na kwamba kifo kisiwe na [a]uchungu, hakungekuwa na ufufuo.

8 Lakini kuna [a]ufufuo, kwa hivyo kaburi halina ushindi, na uchungu wa [b]kifo umemezwa katika Kristo.

9 Yeye ni [a]nuru na uzima wa ulimwengu; ndiyo, nuru isiyo na mwisho, ambayo haiwezi kuwekwa giza; ndiyo, na pia uzima usio na mwisho, kwamba hakutakuwa tena na kifo.

10 Hata huu mwili wenye kufa utajivika [a]kutokufa, na

16 1*a* MWM Wokovu.
b Mos. 27:31.
2*a* M&M 63:53–54.
b Mt. 13:41–42; Lk. 13:28; Alma 40:13.
3*a* Gal. 5:16–25; Mos. 3:19. MWM Mwanadamu wa Tabia ya Asili.
b 2 Ne. 9:8–9. MWM Ibilisi.
c Mwa. 3:1–13; Musa 4:5–19.
d MWM Anguko la Adamu na Hawa.
e 2 Ne. 2:17–18, 22–26.
4*a* Alma 42:6–14.
5*a* Alma 41:11. MWM Tamaa za kimwili.
b MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
6*a* Mos. 3:13.
7*a* Hos. 13:14; Mos. 15:8, 20.
8*a* Alma 42:15. MWM Ufufuko.
b Isa. 25:8; 1 Kor. 15:54–55; Morm. 7:5.
9*a* M&M 88:5–13. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
10*a* Alma 40:2. MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.

hii iharibikayo itavaa isiyoharibika, na italetwa [b]kusimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, [c]kuhukumiwa na yeye kulingana na matendo yao kama ni mema au kama ni maovu—

11 Kama ni wema, watafufuliwa katika maisha na furaha [a]isiyo na mwisho; na kama ni waovu, watafufuliwa katika laana ya [b]milele, na kuwekwa kwa ibilisi, ambaye amewatawala, ambayo ni laana—

12 Kwa vile walienda kulingana na nia zao za tamaa na tamaa za kimwili; wakiwa wamekosa kumlingana Bwana waliponyoshewa mikono ya rehema; kwani walinyoshewa mikono ya [a]rehema, na hawakukubali; wao wakiwa wameonywa kuhusu uovu wao lakini hawakuuacha; na waliamriwa watubu lakini hawakutubu.

13 Na sasa, haiwapasi ninyi kutetemeka na kutubu dhambi zenu, na kukumbuka kwamba ni kwa na katika Kristo pekee mnakoweza kuokolewa?

14 Kwa hivyo, kama mnafundisha [a]sheria ya Musa, fundisheni pia kwamba ni kivuli cha vile vitu vitakavyokuja—

15 Wafundishe kwamba ukombozi huja kwa Kristo aliye Bwana, ambaye ni [a]Baba kamili hasa wa Milele. Amina.

MLANGO WA 17

Alma anaamini na kuandika maneno ya Abinadi—Abinadi anafariki kwa kuchomwa kwa moto—Anatoa unabii wa ugonjwa na mauti kwa moto juu ya wauaji wake. Karibia mwaka 148 K.K.

Na sasa ikawa kwamba baada ya Abinadi kumaliza mazungumzo haya, kwamba mfalme aliamuru kwamba [a]makuhani wamkamate na kumuua.

2 Lakini kulikuwa na mmoja miongoni mwao ambaye jina lake lilikuwa [a]Alma, yeye pia akiwa uzao wa Nefi. Na alikuwa kijana, na [b]aliamini maneno ambayo Abinadi alizungumza, kwani alijua kuhusu ule uovu ambao Abinadi alikuwa ameshuhudia dhidi yao; kwa hivyo akaanza kumsihi mfalme kwamba asimkasirikie Abinadi, lakini kwamba amruhusu aende kwa amani.

3 Lakini mfalme alipandwa na hasira zaidi, na akaamuru kwamba Alma aondolewe kutoka miongoni mwao, na kuwatuma watumishi wake wamfuate ili wamuue.

4 Lakini alitoroka na kujificha hata kwamba hawakumpata. Na yeye akiwa amejifichiwa kwa siku nyingi, [a]aliyaandika maneno yote ambayo Abinadi alikuwa ameyazungumza.

5 Na ikawa kwamba mfalme

10 *b* MWM Hukumu ya mwisho.
c Alma 41:3–6.
11 *a* MWM Uzima wa Milele.
b MWM Hukumu.
12 *a* MWM Rehema, enye Rehema.
14 *a* MWM Torati ya Musa.
15 *a* Mos. 3:8; 5:7; Eth. 3:14.
17 1 *a* Mos. 11:1, 5–6.
2 *a* Mos. 23:6, 9–10. MWM Alma Mzee.
b Mos. 26:15.
4 *a* MWM Maandiko.

alisababisha walinzi wake wamzingire Abinadi na kumkamata; na wakamfunga na kumtia gerezani.

6 Na baada ya siku tatu, baada ya kushauriana na makuhani wake, aliamuru tena kwamba aletwe mbele yake.

7 Na akamwambia: Abinadi, tumekupata na lawama, na wewe unastahili kifo.

8 Kwani wewe umesema kwamba [a]Mungu mwenyewe atashuka miongoni mwa watoto wa watu; na sasa, kwa sababu hii utauliwa usiporudisha yale maneno yote maovu ambayo umezungumza kunihusu na watu wangu.

9 Sasa Abinadi akamwambia: ninakwambia, sitarudisha maneno ambayo nimekuzungumzia kuhusu watu hawa, kwani ni ya kweli; na ili ujue uhakika wa maneno haya nimekubali kuanguka mikononi mwako.

10 Ndiyo, na nitateseka hadi kifo, na sitarudisha maneno yangu, na yatakuwa ushahidi dhidi yenu. Na mkiniua mtamwaga damu [a]isiyo na hatia, na hii nayo pia itakuwa ni ushahidi dhidi yenu siku ya mwisho.

11 Na sasa mfalme Nuhu alikuwa karibu kumwachilia huru, kwani aliogopa maneno yake; kwani aliogopa kwamba hukumu za Mungu zitamshukia.

12 Lakini makuhani walipiga makelele, na kuanza kumshutumu, wakisema: Amemtusi mfalme. Kwa hivyo mfalme alimkasirikia, na akamtoa ili auawe.

13 Na ikawa kwamba walimkamata na kumfunga, na kumpiga ngozi yake kwa kuni za moto, ndiyo, hata akafariki.

14 Na sasa wakati miale ya moto ilianza kumchoma, aliwalilia, akisema:

15 Tazameni, hata vile mmenifanyia, ndivyo itakavyokuwa kwamba uzao wenu utawafanya wengi kuteseka kwa uchungu kama ule ambao mmenitesa nao, hata uchungu wa [a]kifo kwa moto; na haya ni kwa sababu wanaamini wokovu wa Bwana Mungu wao.

16 Na itakuwa kwamba mtasumbuliwa na aina zote za magonjwa kwa sababu ya maovu yenu.

17 Ndiyo, na [a]mtapigwa kutoka kila mkono, na mtafukuzwa na kutawanywa hapa na pale, hata kama vile mifugo ya mwituni hukimbizwa na wanyama katili na wakali.

18 Na katika siku ile mtawindwa, na kukamatwa kwa mikono ya maadui zenu, na kisha mtateseka, kama vile ninavyoteseka, uchungu wa [a]kifo kwa moto.

19 Na hivyo ndivyo Mungu hulipiza [a]kisasi juu ya wale wanaowaangamiza watu wake. Ee Mungu, pokea nafsi yangu.

20 Na sasa, baada ya Abinadi kusema maneno haya, alianguka chini, akiwa amepata mateso ya kifo kwa moto; ndiyo, akiwa

8a Mos. 13:25, 33–34. Alma 25:4–12.
10a Alma 60:13.
15a Mos. 13:9–10; Alma 25:4–12.
17a Mos. 21:1–5, 13.
18a Mos. 19:18–20.
19a MWM Kisasi.

ameuawa kwa sababu alikataa kukana amri za Mungu, akiwa ametilia muhuri ukweli wa maneno yake kwa kifo chake.

MLANGO WA 18

Alma anahubiri kwa siri—Anaeleza kuhusu agano la ubatizo na anabatiza katika maji ya Mormoni—Anaanzisha Kanisa la Kristo na kuwateua makuhani—Wanajisaidia wenyewe na kufundisha watu—Alma na watu wake wanakimbia kutoka kwa Mfalme Nuhu na kwenda nyikani. Karibia mwaka 147–145 K.K.

Na sasa, ikawa kwamba Alma, ambaye alikuwa ametoroka kutoka kwa watumishi wa Mfalme Nuhu, [a]alitubu dhambi zake na maovu yake, na akaenda kwa siri miongoni mwa watu, na kuanza kufundisha maneno ya Abinadi—

2 Ndiyo, kuhusu yale ambayo yatakuja, na pia kuhusu ufufuo wa wafu, na [a]ukombozi wa watu, ambao ungewezeshwa kwa [b]uwezo, na mateso, na kifo cha Kristo, na ufufuko wake na kupaa mbinguni.

3 Na kwa wengi waliotaka kusikiliza neno lake aliwafundisha. Na aliwafundisha kwa siri, ili mfalme asijue. Na wengi waliamini maneno yake.

4 Na ikawa kwamba wengi waliomwamini walienda [a]mahali palipoitwa Mormoni, kwani paliitwa kwa jina la mfalme, pakiwa mpakani mwa nchi ambayo ilikuwa imejaa, wanyama wa mwitu nyakati zote.

5 Sasa, hapo Mormoni palikuwa na chemchemi ya maji safi, na Alma alikimbilia hapo, kwani karibu na maji hayo palikuwa na kichaka cha miti midogo, na alijificha hapo wakati wa mchana ili asipatikane na misako ya mfalme.

6 Na ikawa kwamba wale wengi waliomwamini walienda hapo kusikia maneno yake.

7 Na ikawa kwamba baada ya siku nyingi kulikuwa na kikundi kikubwa kimekusanyika pamoja mahali pa Mormoni, ili kusikia maneno ya Alma. Ndiyo, wote walioamini neno lake walikusanyika pamoja, kumsikiliza. Na [a]aliwafundisha, na akawahubiria toba, na ukombozi, na imani kwa Bwana.

8 Na ikawa kwamba aliwaambia: Tazameni, hapa kuna maji ya Mormoni (kwani hivi ndivyo yaliitwa) na sasa, kwa vile [a]mnatamani kujiunga na [b]zizi la Mungu, na kuitwa watu wake, na mko [c]radhi kubeba mizigo ya mmoja na ya mwingine, ili iwe miepesi;

9 Ndiyo, na mko tayari kuomboleza na wale wanaoomboleza; ndiyo, na kufariji wale ambao wanahitaji kufarijiwa, na kusimama kama [a]mashahidi wa Mungu nyakati zote na

18 1*a* Mos. 23:9–10.
2*a* MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
4*a* Alma 5:3.
7*a* Alma 5:11–13.
8*a* M&M 20:37.
b MWM Kanisa la Yesu Kristo.
c MWM Huruma.
9*a* MWM Kazi ya kimisionari; Shahidi, Ushahidi; Shuhudia.

katika vitu vyote, na katika mahali popote mlipo, hata hadi kifo, ili muweze kukombolewa na Mungu, na kuhesabiwa pamoja na wale wa [b]ufufuko wa kwanza, ili mpokee [c]uzima wa milele—

10 Sasa ninawaambia, ikiwa hili ndilo pendo la mioyo yenu, ni nini mnacho dhidi ya [a]kubatizwa kwa jina la Bwana, kama ushahidi mbele yake kwamba mmeingia kwenye [b]agano na yeye, kwamba mtamtumikia na kushika amri zake, ili awateremshie Roho yake juu yenu zaidi?

11 Na sasa wakati watu waliposikia maneno haya, walipiga makofi kwa shangwe, na wakasema kwa nguvu: Hili ndilo pendo la mioyo yetu.

12 Na sasa ikawa kwamba Alma alimchukua Helamu, yeye akiwa wa kwanza, na kwenda na kusimama majini, na kupaza sauti yake, akisema: Ee Bwana, mteremshie mtumishi wako Roho wako, ili afanye kazi hii kwa utakatifu wa moyo.

13 Na aliposema maneno haya, [a]Roho wa Bwana alishuka juu yake, na akasema: Helamu, [b]nakubatiza wewe, nikiwa na [c]mamlaka kutoka kwa Mwenyezi Mungu, kama ushahidi kwamba umeingia kwenye agano kumtumikia hadi utakapokufa katika mwili; na Roho wa Bwana akuteremkie; na akupe uzima wa milele, kupitia kwa [d]ukombozi wa Kristo, ambaye amemtayarisha tangu [e]msingi wa ulimwengu.

14 Na baada ya Alma kusema maneno haya, Alma pamoja na Helamu [a]walizikwa majini; na wakainuka na wakatoka majini wakishangilia wakiwa wamejazwa na Roho.

15 Na tena, Alma akamchukua mwingine, na kuingia majini mara ya pili, na akambatiza kama yule wa kwanza, lakini hakujizika kwa maji tena.

16 Na hivi ndivyo alivyobatiza kila mmoja aliyeenda mahali pa Mormoni; na walikuwa watu mia mbili na nne; ndiyo, na [a]walibatizwa katika maji ya Mormoni, na wakajazwa na [b]neema ya Mungu.

17 Na waliitwa [a]kanisa la Mungu, au kanisa la Kristo, kutoka siku ile na kuendelea mbele. Na ikawa kwamba yeyote aliyebatizwa kwa uwezo na mamlaka ya Mungu aliongezwa katika kanisa lake.

18 Na ikawa kwamba Alma, akiwa na [a]mamlaka kutoka kwa Mungu, aliwateua makuhani; hata kuhani mmoja kwa

9 *b* Mos. 15:21–26.
c MWM Uzima wa Milele.
10 *a* 2 Ne. 31:17. MWM Batiza, Ubatizo.
b MWM Agano.
13 *a* MWM Roho Mtakatifu.
b 3 Ne. 11:23–26; M&M 20:72–74.
c M ya I 1:5. MWM Ukuhani.
d MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
e Musa 4:2; 5:9.
14 *a* MWM Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa kuzamishwa.
16 *a* Mos. 25:18.
b MWM Neema.
17 *a* 3 Ne. 26:21; 27:3–8. MWM Kanisa la Yesu Kristo.
18 *a* MWM Ukuhani.

kila kikundi cha hamsini aliwatawaza kuwahubiria, na [b]kuwafundisha kuhusu vitu vya ufalme wa Mungu.

19 Na akawaamuru kwamba wasifundishe chochote ila tu vitu vile ambavyo alikuwa amewafundisha, na ambavyo vilikuwa vimezungumzwa na manabii watakatifu.

20 Ndiyo, hata aliwaamuru kwamba [a]wasihubiri chochote ila tu toba na imani kwa Bwana, ambaye alikuwa amewakomboa watu wake.

21 Na akawaamuru kwamba wasiwe na [a]ubishi wao kwa wao, lakini kwamba watazame kwa jicho [b]moja, kwa imani moja ubatizo mmoja, na mioyo yao ikiwa imeunganishwa pamoja kwa [c]umoja na kwa kupendana wao kwa wao.

22 Na hivi ndivyo alivyowaamuru kuhubiri. Na hivyo wakawa [a]watoto wa Mungu.

23 Na akawaamuru kwamba waiheshimu siku ya [a]sabato, na kuiweka iwe takatifu, na pia kwamba wamshukuru Bwana Mungu wao kila siku.

24 Na pia akawaamuru kwamba makuhani wale ambao alikuwa amewateua wafanye [a]kazi kwa mikono yao ili wajitegemee.

25 Na kulikuwa na siku moja kwa kila juma ambayo ilitengwa ili wakusanyike pamoja kuwafundisha watu, na [a]kumuabudu Bwana Mungu wao, na pia, mara kwa mara kama walivyo na uwezo, kukusanyika pamoja.

26 Na makuhani wasitegemee watu kwa chakula chao; lakini watapokea [a]neema ya Mungu kwa sababu ya utumishi wao, ili wapokee nguvu za Roho, na [b]kumfahamu Mungu, ili wafundishe kwa uwezo na mamlaka kutoka kwa Mungu.

27 Na tena Alma akaamuru kwamba watu wa kanisa watoe mali yao, [a]kila mmoja kulingana na kile alichokuwa nacho; kama yuko na tele basi na yeye atoe kwa wingi; na kwa yule ambaye ana chache, basi chache ndizo zitahitajika; na yule ambaye hana basi naye apewe.

28 Na hivyo watoe mali yao kwa hiari yao na nia njema kwa Mungu, na kwa wale makuhani waliohitaji, ndiyo, na kwa kila mtu aliyehitaji, na aliye uchi.

29 Na hivi aliwaambia, akiwa ameamriwa na Mungu; na [a]walitembea imara mbele ya Mungu, [b]wakisaidiana kimwili na kiroho kulingana na mahitaji yao na matakwa yao.

30 Na sasa ikawa kwamba haya yote yalifanywa katika

18 *b* MWM Fundisha, Mwalimu.
20 *a* M&M 15:6; 18:14–16.
21 *a* 3 Ne. 11:28–30. MWM Ushindani.
b Mt. 6:22; M&M 88:67–68.
c MWM Umoja.
22 *a* Mos. 5:5–7; Musa 6:64–68.
23 *a* Mos. 13:16–19; M&M 59:9–12.
24 *a* Mdo. 20:33–35; Mos. 27:3–5; Alma 1:26.
25 *a* MWM Kuabudu.
26 *a* MWM Neema.
b MWM Maarifa.
27 *a* Mdo. 2:44–45; 4 Ne. 1:3.
29 *a* MWM Tembea, Tembea na Mungu.
b MWM Ustawi.

Mormoni, ndiyo, karibu na [a]maji ya Mormoni, katika mwitu uliokuwa karibu na maji ya Mormoni; ndiyo, mahali pa Mormoni, maji ya Mormoni, mwitu wa Mormoni, jinsi gani yalivyo na wema machoni mwa wale ambao walimfahamu Mkombozi wao hapo; ndiyo, na jinsi gani wamebarikiwa, kwani wataimba sifa zake milele.

31 Na vitu hivi vilifanywa [a]mipakani mwa nchi, ili visijulikane na mfalme.

32 Lakini tazama, ikawa kwamba mfalme, akiwa amegundua kuwa kuna njama miongoni mwa watu, alituma watumishi wake kuwachunguza. Kwa hivyo siku ile waliyokuwa wanakusanyika pamoja kusikia neno la Bwana waligunduliwa kwa mfalme.

33 Na sasa mfalme akasema kuwa Alma alikuwa anawachochea watu ili wamuasi; kwa hivyo alituma jeshi lake kuwaangamiza.

34 Na ikawa kwamba Alma na watu wa Bwana [a]walijulishwa kuhusu uvamizi wa jeshi la mfalme; kwa hivyo walichukua hema zao na jamii zao na kukimbilia nyikani.

35 Na walikuwa hesabu ya watu karibu mia nne na hamsini.

MLANGO WA 19

Gideoni anajaribu kumuua Mfalme Nuhu—Walamani wanavamia nchi—Mfalme Nuhu anauawa kwa kuchomwa na moto—Limhi atawala akiwa mfalme alipaye kodi kwa mfalme mwingine. Karibia mwaka 145–121 K.K.

Na ikawa kwamba jeshi, la mfalme lilirejea, baada ya msako wao wa watu wa Bwana kukosa kufua dafu.

2 Na sasa tazama, vikosi vya mfalme vilikuwa vidogo, vikiwa vimepunguzwa, na pakaanza kuwa na mgawanyiko miongoni mwa watu waliosalia.

3 Na ile sehemu ndogo ikaanza kumtolea mfalme vitisho, na kukawa na ubishi mkuu miongoni mwao.

4 Na sasa miongoni mwao kulikuwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa Gideoni, na yeye akiwa mtu mwenye nguvu na adui wa mfalme, kwa hivyo alichomoa upanga wake, na kuapa kwa hasira kwamba atamuua mfalme.

5 Na ikawa kwamba alipigana na mfalme; na mfalme alipoona kwamba alikuwa karibu kushindwa, alikimbia na kupanda kwenye [a]mnara uliokuwa karibu na hekalu.

6 Na Gideoni alimkimbiza na alikaribia kupanda ule mnara ili amuue mfalme, na mfalme akatazama nchi ya Shemloni, na tazama, jeshi la Walamani lilikuwa mipakani mwa nchi.

7 Na sasa mfalme alilia kwa maumivu ya nafsi yake, na kusema: Gideoni, nisamehe, kwani Walamani wanatushambulia,

30*a* Mos. 26:15.
31*a* Mos. 18:4.
34*a* Mos. 23:1.
19 5*a* Mos. 11:12.

na watatuangamiza; ndiyo, wataangamiza watu wangu.

8 Na sasa mfalme hakujali watu wake kama vile alivyojali maisha yake; walakini, Gideoni aliyaokoa maisha yake.

9 Na mfalme akaamuru watu wake kwamba wawakimbie mbele Walamani, na yeye mwenyewe akawaongoza, na wakakimbilia nyikani, pamoja na wake zao na watoto wao.

10 Na ikawa kwamba Walamani waliwafuata, na kuwafikia, na kuanza kuwaua.

11 Sasa ikawa kwamba mfalme aliamuru wanaume wote kwamba wawaache wake zao na watoto wao, na wawatoroke Walamani.

12 Sasa kulikuwa na wengi ambao hawakuwaacha, lakini waliona vizuri kubaki nao na kuangamia nao. Na wengine waliacha wake zao na watoto wao na kukimbia.

13 Na ikawa kwamba wale waliobaki na wake zao na watoto wao waliwafanya mabinti zao walio warembo kusimama mbele ya Walamani na kuwasihi kwamba wasiwaue.

14 Na ikawa kwamba Walamani waliwaonea huruma, kwani walivutiwa na urembo wa wanawake wao.

15 Kwa hivyo Walamani waliokoa maisha yao, na kuwachukua kama mateka na kuwapeleka katika nchi ya Nefi, na kuwaruhusu kwamba warithi nchi ile, na kuwapatia masharti kwamba watamkabidhi mfalme Nuhu mikononi mwa Walamani, na kutoa mali yao, hata nusu ya yote waliyokuwa nayo; nusu ya dhahabu yao, na fedha yao, na vitu vyao vyote vyenye thamani, na hivyo ndivyo watalipa ushuru kwa mfalme wa Walamani mwaka kwa mwaka.

16 Na sasa kulikuwa na mmoja wa wana wa mfalme miongoni mwa wale waliochukuliwa kama mateka, aliyeitwa kwa jina la [a]Limhi.

17 Na sasa Limhi hakutaka baba yake aangamizwe; walakini, Limhi hakukosa kuona maovu ya baba yake, yeye mwenyewe akiwa mtu mwenye haki.

18 Na ikawa kwamba Gideoni alituma watu nyikani kwa siri, kumsaka mfalme na wale waliokuwa na naye. Na ikawa kwamba waliwapata watu wote nyikani, ila tu mfalme na makuhani wake.

19 Sasa walikuwa wameapa mioyoni mwao kwamba watarejea katika nchi ya Nefi, na kama wake zao na watoto wao wameuawa, na pia wale waliobaki nao, kwamba wangelipiza kisasi, na pia kuangamia nao.

20 Na mfalme akawaamuru kwamba wasirejee; na walimkasirikia mfalme, na kusababisha kwamba [a]afariki, kwa moto.

21 Na walikuwa karibu ya kuwakamata makuhani pia na kuwaua, na waliwatoroka.

22 Na ikawa kwamba walikuwa karibu ya kurejea katika nchi ya Nefi, na wakakutana na watu wa Gideoni. Na watu

16*a* Mos. 7:9. | 20*a* Mos. 17:13–19; Alma 25:11.

wa Gideoni wakawaelezea yale yaliyowapata wake zao na watoto wao; na kwamba Walamani walikuwa wamewaruhusu kumiliki nchi kwa kulipa kodi kwa Walamani kiasi cha nusu ya mali yote waliyokuwa nayo.

23 Na wale watu wakawaambia watu wa Gideoni kwamba walikuwa wamemuua mfalme, na makuhani wake walikuwa wametorokea nyikani.

24 Na ikawa kwamba baada ya wao kumaliza ile sherehe, kwamba walirejea katika nchi ya Nefi, wakishangilia, kwa sababu wake zao na watoto wao hawakuwa wameuawa; na wakamwambia Gideoni yale waliyokuwa wamemfanyia mfalme.

25 Na ikawa kwamba mfalme wa Walamani alikula [a]kiapo na wao, kwamba watu wake hawatawaua.

26 Na pia Limhi, akiwa mwana wa mfalme, akiwa amepewa ufalme [a]na watu, aliapa kwa mfalme wa Walamani kwamba watu wake watamlipa ushuru, kiasi cha nusu ya chochote walicho nacho.

27 Na ikawa kwamba Limhi alianza kuimarisha ufalme na kudumisha amani miongoni mwa watu wake.

28 Na mfalme wa Walamani aliweka walinzi waizingire nchi, ili awaweke watu wa Limhi katika nchi ile, ili wasiondoke na kwenda nyikani; na aliwalisha walinzi wake kwa ushuru aliopokea kutoka kwa Wanefi.

29 Na sasa mfalme Limhi alikuwa na amani katika ufalme wake kwa kipindi cha miaka miwili, kwamba Walamani hawakuwavamia wala kutaka kuwaangamiza.

MLANGO WA 20

Baadhi ya mabinti za Walamani wanatekwa nyara na makuhani wa Nuhu—Walamani wanamvamia Limhi na watu wake kwa vita—Walamani wavamizi wanakomeshwa na kutulizwa. Karibia mwaka 145–123 K.K.

Sasa palikuwa na pahali katika Shemloni ambapo mabinti za Walamani walikusanyika pamoja kuimba, na kucheza, na kujifurahisha.

2 Na ikawa kwamba siku moja kikundi chao kidogo kilikusanyika pamoja ili waimbe na wacheze.

3 Na sasa makuhani wa mfalme Nuhu, wakiona aibu ya kurejea katika mji wa Nefi, ndiyo, na pia wakiogopa kwamba watu watawaua, kwa hivyo hawakuwarudia wake zao na watoto wao.

4 Na baada ya kungoja nyikani, na baada ya kugundua mabinti za Walamani, walijificha na kuwatazama;

5 Na wakati walikuwa ni wachache tu waliokusanyika pamoja kucheza, waliondoka pahali pao pa siri na kuwashika na kuwapeleka nyikani; ndiyo, mabinti ishirini na nne wa Walamani waliwapeleka nyikani.

25*a* Mos. 21:3.
26*a* Mos. 7:9.

6 Na ikawa kwamba Walamani walipogundua kwamba mabinti zao walikuwa wamepotea, walikasirikia watu wa Limhi, kwani walidhani kuwa ni watu wa Limhi.

7 Kwa hivyo walituma majeshi yao; ndiyo, hata mfalme aliongoza watu wake; na wakaelekea nchi ya Nefi kuwaangamiza watu wa Limhi.

8 Na sasa Limhi alikuwa amewaona kutoka kwenye mnara, hata matayarisho yao yote ya vita alikuwa ameyaona; kwa hivyo aliwakusanya watu wake, na akawangoja huko mwituni na vichakani.

9 Na ikawa kwamba Walamani walipokuja, wale watu wa Limhi walianza kuwashambulia kutoka pahali pao pa kujificha, na kuanza kuwaua.

10 Na ikawa kwamba vita vilipamba moto, kwani walipigana kama simba kwenye mawindo yao.

11 Na ikawa kwamba watu wa Limhi walianza kuwakimbiza Walamani; ingawa hawakuwa wengi kama Walamani. Lakini [a]walipigania maisha yao, na wake zao, na watoto wao; kwa hivyo walijitahidi na wakapigana kama joka.

12 Na ikawa kwamba walimpata mfalme wa Walamani miongoni mwa wafu wao; walakini hakuwa amefariki, akiwa amejeruhiwa na kuachiliwa chini, kwani watu wake walitoroka kwa haraka.

13 Na wakamchukua na kufunga majeraha yake, na kumpeleka mbele ya Limhi, na kusema: Tazama, hapa kuna mfalme wa Walamani; alijeruhiwa na akawa ameanguka miongoni mwa wafu wao, na wamemuacha; na tazama, tumemleta mbele yako; na sasa hebu tumuue.

14 Lakini Limhi akawaambia: Hamtamuua, lakini mleteni hapa ili nimuone. Na wakamleta. Na Limhi akamwambia: Ni sababu gani iliyokufanya kushambulia watu wangu? Tazama, watu wangu hawajavunja [a]kiapo nilichofanya nawe; kwa hivyo, kwa nini uvunje kiapo ulichofanya na watu wangu?

15 Na sasa mfalme akasema: Nimevunja kiapo kwa sababu watu wako waliwachukua mabinti za watu wangu; kwa hivyo, kwa hasira yangu niliwafanya watu wangu wawashambulie watu wako.

16 Na sasa Limhi hakuwa amesikia lolote kuhusu jambo hili; kwa hivyo akasema: Nitatafuta miongoni mwa watu wangu na yeyote ambaye ametenda kitu hiki ataangamia. Kwa hivyo akaamuru msako ufanywe miongoni mwa watu wake.

17 Sasa [a]Gideoni aliposikia vitu hivi, yeye akiwa kapteni wa mfalme, alienda na kumwambia mfalme: Nakuomba usubiri na usiwasake watu hawa, na usiwashutumu kwa kitu hiki.

20 11*a* Alma 43:45. | 14*a* Mos. 19:25–26. | 17*a* Mos. 19:4–8.

18 Kwani hukumbuki makuhani wa baba yako, ambao watu hawa walitaka kuwaangamiza? Na je, hawako huko nyikani? Na je, si wao ndiyo waliowachukua mabinti za Walamani?

19 Na sasa, tazama, mwambie mfalme kuhusu vitu hivi, ili awaambie watu wake na ili watulizwe nasi; kwani tazama tayari wanajitayarisha kutuvamia; na tazama sisi ni wachache.

20 Na tazama, wanakuja na majeshi yao; na ijapokuwa mfalme awasihi kwa niaba yetu lazima tuangamie.

21 Kwani si maneno ya Abinadi [a]yanatimizwa, yale aliyotoa unabii dhidi yetu—na haya yote kwa sababu hatukutii maneno ya Bwana, na kuacha maovu yetu?

22 Na sasa hebu tumtulize mfalme, na tutimize kiapo ambacho tulifanya kwake; kwani ni afadhali tuwe utumwani badala ya kupoteza maisha yetu; kwa hivyo, hebu tukomeshe umwagaji wa damu nyingi.

23 Na sasa Limhi akamwambia mfalme vitu vyote kuhusu baba yake, na [a]makuhani waliokimbilia nyikani, na akawashutumu kwa kuwachukua mabinti zao.

24 Na ikawa kwamba mfalme alitulizwa na watu wake; na akawaambia: Hebu twende tukalaki watu wangu, bila silaha; na ninaapa kwa kiapo kwamba watu wangu hawatawaua watu wako.

25 Na ikawa kwamba walimfuata mfalme, na wakaenda kuwalaki Walamani bila silaha. Na ikawa kwamba walikutana na Walamani; na mfalme wa Walamani akainama mbele yao, na kuwatetea watu wa Limhi.

26 Na Walamani walipoona watu wa Limhi, kwamba hawakuwa na silaha, waliwaonea [a]huruma na wakatulizwa na wao, na wakarejea na mfalme wao kwa amani nchini mwao.

MLANGO WA 21

Watu wa Limhi wanashambuliwa na kushindwa na Walamani—Watu wa Limhi wanakutana na Amoni na kubadilishwa—Wanamwambia Amoni kuhusu yale mabamba ishirini na nne ya Kiyaredi. Karibia mwaka 122–121 K.K.

Na ikawa kwamba Limhi na watu wake walirejea katika mji wa Nefi, na wakaanza kuishi tena kwa amani katika nchi.

2 Na ikawa kwamba baada ya siku nyingi Walamani walianza tena kuwachokoza wakasirike Wanefi, na wakaanza kusogea karibu na mipaka iliyozingira nchi.

3 Sasa hawakuthubutu kuwaua, kwa sababu ya kile kiapo ambacho mfalme wao alikuwa amemuapia Limhi; walakini waliwacharaza makofi kwenye [a]mashavu, na kuwa na mamlaka juu yao; na kuwabebesha [b]mizigo mizito kwenye migongo yao, na kuwakimbiza kama vile wanavyomfanyia punda bubu—

21*a* Mos. 12:1–8.
23*a* Mos. 19:21, 23.
26*a* MWM Huruma.
21 3*a* Mos. 12:2.
b Mos. 12:5.

4 Ndiyo, haya yote yalifanywa ili neno la Bwana litimizwe.

5 Na sasa mateso ya Wanefi yalikuwa ni makuu, na hapakuwa na njia yoyote ya kujikomboa kutoka mikononi mwao, kwani Walamani waliwazingira kwa kila upande.

6 Na ikawa kwamba watu walianza kumnung'unikia mfalme kwa sababu ya mateso yao; na wakaanza kutamani kupigana nao. Na walimsumbua mfalme kwa malalamiko yao; kwa hivyo akawaruhusu wafanye kulingana na tamaa yao.

7 Na wakakusanyika pamoja tena, na kuvaa silaha zao, na kuwaendea Walamani ili wawafukuze kutoka nchi yao.

8 Na ikawa kwamba Walamani waliwapiga, na kuwasukuma nyuma, na kuwaua wengi wao.

9 Na sasa kulikuwa na [a]maombolezo makuu na kilio miongoni mwa watu wa Limhi, mjane akiomboleza mume wake, mwana na binti wakiomboleza baba yao, na kaka kwa ndugu zao.

10 Sasa kulikuwa na wajane wengi nchini, na walilia sana siku kwa siku, kwani woga mkuu wa Walamani uliwaingia.

11 Na ikawa kwamba vilio vyao viliwachochea wale watu waliobaki wa Limhi kuwakasirikia Walamani; na wakaenda vitani tena, lakini walisukumwa nyuma tena, na wakapata maafa makubwa.

12 Ndiyo, walienda tena mara ya tatu, na wakateseka kama hapo awali; na wale ambao hawakuuawa walirejea tena katika nchi ya Nefi.

13 Na wakanyenyekea mpaka mavumbini, na kujitoa kwa nira ya utumwa, na kukubali kupigwa, na kukimbizwa hapa na pale, na kulemeshwa, kulingana na matakwa ya maadui wao.

14 Na [a]walinyenyekea chini kabisa na hata kuwa chini ya unyenyekevu; na walimlilia Mungu sana; ndiyo, hata siku yote walimlilia Mungu wao kwamba awakomboe kutokana na mateso yao.

15 Na sasa Bwana alikuwa [a]mzito wa kusikia kilio chao kwa sababu ya maovu yao; hata hivyo Bwana alisikia vilio vyao, na akaanza kulainisha mioyo ya Walamani kiasi kwamba wakaanza kupunguza mizigo yao; walakini Bwana hakuonelea vyema kuwakomboa kutoka utumwani.

16 Na ikawa kwamba walianza kufanikiwa nchini kidogo kidogo, na wakaanza kupanda nafaka kwa wingi, na mifugo, na wanyama, kwamba hawakuteseka kwa njaa.

17 Sasa kulikuwa na wanawake wengi, zaidi ya wanaume; kwa hivyo mfalme Limhi akaamuru kwamba kila mwanaume [a]atoe ili [b]wajane na watoto wao wapate kusaidiwa, na ili wasiangamie kwa njaa; na walitenda haya kwa sababu ya wingi wa hao waliouwawa.

9*a* Mos. 12:4.
14*a* Mos. 29:20.
MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
15*a* Mit. 15:29; Mos. 11:23–25; M&M 101:7–9.
17*a* Mos. 4:16, 26.
b MWM Mjane.

18 Sasa watu wa Limhi walishi kwa kikundi kama ilivyowezekana, na kulinda nafaka yao na mifugo yao;

19 Na mfalme mwenyewe alihofia maisha yake nje ya ukuta wa mji, isipokuwa awe na walinzi wake na yeye, akiogopa kwamba ingewezekana aanguke mikononi mwa Walamani.

20 Na akasababisha watu wake washike zamu kila mahali nchini, ili ikiwezekana wawakamate makuhani ambao walikuwa wametorokea nyikani, ambao walikuwa wamewachukua [a]mabinti za Walamani, na ambao walikuwa wamesababisha maangamizi makuu kuwapata.

21 Kwani walitamani kuwakamata na kuwaadhibu; kwa sababu walikuwa wameingia katika nchi ya Nefi wakati wa usiku, na kuiba nafaka yao na vitu vyao vingi vyenye thamani; kwa hivyo walijificha na kuwangoja.

22 Na ikawa kwamba hakukuwa na ghasia yoyote miongoni mwa Walamani na watu wa Limhi, hadi ule wakati ambao [a]Amoni na ndugu zake walipowasili katika nchi.

23 Na mfalme akiwa nje ya lango la mji na walinzi wake, aliwaona Amoni na ndugu zake; na akidhani kwamba wao ni makuhani wa Nuhu, kwa hivyo aliamrisha kwamba washikwe, na kufungwa, na kuwekwa [a]gerezani. Na kama wangekuwa makuhani wa Nuhu, angeamuru wauawe.

24 Lakini alipofahamu kwamba sio wao, walakini walikuwa ndugu zake, waliotoka nchi ya Zarahemla, alijazwa na shangwe kuu.

25 Sasa mfalme Limhi alikuwa ametuma, kikundi [a]kidogo cha watu [b]kutafuta nchi ya Zarahemla, kabla ya kuwasili kwa Amoni; lakini hawakuipata, na walipotea huko nyikani.

26 Walakini, walipata nchi ambamo watu walikuwa wameishi; ndiyo, nchi ambayo ilijaa [a]mifupa iliyokauka; ndiyo, nchi ambayo watu walikuwa wameishi na ambao walikuwa wameangamizwa; na wao, wakidhani kuwa ni nchi ya Zarahemla, walirejea katika nchi ya Nefi, wakiwa wamewasili mipakani mwa nchi siku chache kabla ya kufika kwa Amoni.

27 Na walileta maandishi, hata maandishi ya watu wale ambao walipata mifupa yao; na yalikuwa yamechorwa kwenye mabamba ya chuma.

28 Na sasa Limhi alijawa shangwe tena alipoambiwa kwa kinywa cha Amoni kwamba mfalme Mosia alikuwa na [a]karama kutoka kwa Mungu, ambayo ingemwezesha kutafsiri michoro kama ile; ndiyo, na hata Amoni pia alifurahi.

29 Walakini Amoni na ndugu zake walijawa na huzuni kwa sababu ndugu zao wengi walikuwa wameuawa;

20 *a* Mos. 20:5.
22 *a* Mos. 7:6–13.
23 *a* Hel. 5:21.
25 *a* Mos. 8:7.
b Mos. 7:14.
26 *a* Mos. 8:8.
28 *a* Omni 1:20–22; Mos. 28:11–16.

30 Na pia kwamba mfalme Nuhu na makuhani wake walikuwa wamewafanya watu kumtendea Mungu dhambi nyingi na maovu; na pia waliomboleza [a]kifo cha Abinadi; na pia [b]kuondoka kwa Alma na watu walioenda na yeye, ambao walikuwa wameanzisha kanisa la Mungu kwa nguvu na uwezo wa Mungu, na kwa imani katika yale maneno yaliozungumzwa na Abinadi.

31 Ndiyo, waliomboleza kuondoka kwao, kwani hawakujua walikotorokea. Sasa wangeungana nao bila kusita, kwani wao wenyewe walikuwa wameingia kwenye agano na Mungu kwamba watamtumikia na kutii amri zake.

32 Na sasa tangu kuwasili kwa Amoni, mfalme Limhi pia alikuwa ameingia kwenye agano na Mungu, na pia watu wake wengi, kumtumikia na kutii amri zake.

33 Na ikawa kwamba mfalme Limhi na watu wake wengi walitamani kubatizwa; lakini hapakuwa na yeyote katika nchi ile aliyekuwa na [a]mamlaka kutoka kwa Mungu. Na Amoni alikataa kufanya kitu hiki, akijidhania kwamba yeye ni mtumishi asiyestahili.

34 Kwa hivyo wakati ule hawakujipanga pamoja kama kanisa, wakimsubiri Roho wa Bwana. Sasa walitamani kuwa kama Alma na ndugu zake, ambao walikuwa wametorokea nyikani.

35 Walitamani kubatizwa kama ushahidi na ushuhuda kwamba wako tayari kumtumikia Mungu kwa mioyo yao yote; walakini waliongeza wakati; na maelezo ya ubatizo wao [a]yatatolewa hapo baadaye.

36 Na sasa mawazo yote ya Amoni na watu wake, na mfalme Limhi na watu wake, yalikuwa ni jinsi ya kujikomboa kutoka mikono ya Walamani na kutoka utumwa.

MLANGO WA 22

Mipango inatayarishwa ili watu watoroke kutoka utumwa wa Walamani—Walamani wanaleweshwa—Watu wanatoroka, na kurejea Zarahemla, na kutawaliwa na mfalme Mosia. Karibia mwaka 121–120 K.K.

Na sasa ikawa kwamba Amoni na mfalme Limhi walishauriana na watu jinsi ya kujikomboa kutoka utumwani; na hata walisababisha kwamba watu wote wakusanyike pamoja; na walifanya hivi ili wapate sauti ya watu kuhusu jambo hili.

2 Na ikawa kwamba hawakupata njia yoyote ya kujitoa utumwani, ila tu wawachukue wake zao na watoto wao, na mifugo yao, na wanyama wao, na hema zao, na kwenda nyikani; kwani Walamani wakiwa wengi mno, ilikuwa haiwezekani kwa watu wa Limhi kupigana nao, wakifikiria kujikomboa kutoka utumwani kwa upanga.

3 Na sasa ikawa kwamba

30 *a* Mos. 17:12–20.
b Mos. 18:34–35.

33 *a* MWM Mamlaka.

35 *a* Mos. 25:17–18.

Gideoni alienda na kusimama mbele ya mfalme, na kumwambia: Sasa Ee mfalme, wewe umekuwa ukisikiliza maneno yangu mara nyingi wakati tulipokuwa tunabishana na ndugu zetu, Walamani.

4 Na sasa Ee mfalme, kama wewe hujaniona kuwa mimi ni mtumishi asiyeleta faida, au kama wewe umesikiliza maneno yangu kwa kiasi chochote, na yamekuwa yenye huduma kwako, hata hivyo natamani kwamba usikilize maneno yangu wakati huu, na nitakuwa mtumishi wako na kuwakomboa watu hawa kutoka utumwani.

5 Na mfalme akamruhusu kwamba azungumze. Na Gideoni akamwambia:

6 Tazama ule mlango wa nyuma, kupitia ukuta wa nyuma ulio upande wa nyuma wa mji. Walamani, au walinzi wa Walamani, huwa wamelewa usiku; kwa hivyo hebu tutume tangazo miongoni mwa watu hawa kwamba wakusanye pamoja mifugo yao na wanyama wao, ili wawapeleke kwa usiku huko nyikani.

7 Na nitaenda kulingana na amri yako ili nilipe ushuru wa mwisho wa mvinyo kwa Walamani, na watalewa; na tutapitia mlango wa siri ulio kushoto mwa kambi yao watakapokuwa wamelewa na kulala.

8 Na hivyo tutaondoka na wake zetu na watoto wetu, mifugo yetu, na wanyama wetu na kwenda nyikani; na tutasafiri kando ya nchi ya Shilomu.

9 Na ikawa kwamba mfalme alisikiliza maneno ya Gideoni.

10 Na mfalme Limhi alisababisha kwamba watu wake wakusanye mifugo yao pamoja; na akatuma ushuru wa mvinyo kwa Walamani; na pia alituma mvinyo zaidi, kama zawadi kwao; na walikunywa kwa wingi ule mvinyo uliotumwa kwao na mfalme Limhi.

11 Na ikawa kwamba watu wa mfalme Limhi waliondoka usiku na kwenda nyikani pamoja na mifugo yao na wanyama wao, na walizunguka nchi ya Shilomu nyikani, na wakapinda njia yao na kuelekea nchi ya Zarahemla, wakiongozwa na Amoni na ndugu zake.

12 Na walikuwa wamechukua dhahabu yao yote, na fedha, na vitu vyao vya thamani, vile ambavyo waliweza kubeba, na pia maakuli yao, na kwenda nyikani; na wakaendelea na safari yao.

13 Na baada ya kuwa nyikani kwa siku nyingi walifika katika nchi ya Zarahemla, na kuungana na watu wa Mosia, na kuwa watu wake.

14 Na ikawa kwamba Mosia aliwapokea kwa shangwe; na pia alipokea [a]maandishi yao, na pia [b]maandishi ambayo yalipatwa na watu wa Limhi.

15 Na sasa ikawa kwamba wakati Walamani walipogundua kwamba watu wa Limhi walikuwa wameondoka nchini

22 14*a* Mos. 8:5. | *b* Mos. 8:9.

usiku, walituma jeshi huko nyikani kuwafuata;

16 Na baada ya kuwafuata kwa siku mbili, hawangefuata nyayo zao tena; kwa hivyo walipotea huko nyikani.

Historia ya Alma na watu wa Bwana, ambao walikimbizwa nyikani na watu wa Mfalme Nuhu.

Yenye milango ya 23 na 24.

MLANGO WA 23

Alma anakataa kuwa mfalme—Anatumika kama kuhani mkuu—Bwana huwarudi watu Wake, na Walamani wananyakua nchi ya Helamu—Amuloni, kiongozi wa makuhani waovu wa mfalme Nuhu, anatawala chini ya mfalme wa Walamani. Karibia mwaka 145–121 K.K.

Sasa Alma, akiwa ameonywa na Bwana kwamba majeshi ya mfalme Nuhu yatawavamia, na baada ya kujulisha watu wake, kwa hivyo walikusanya pamoja mifugo yao, na kuchukua nafaka yao, na wakaondoka na kuelekea nyikani mbele ya majeshi ya mfalme Nuhu.

2 Na Bwana aliwaongezea nguvu, kwamba watu wa mfalme Nuhu wasiwafikie na kuwaangamiza.

3 Na wakasafiri kwa muda wa siku nane huko nyikani.

4 Na wakaja katika nchi, ndiyo, nchi iliyo mzuri sana na yenye kupendeza, nchi ya maji safi.

5 Na wakapiga hema zao, na wakaanza kulima ardhi, na kuanza kujenga majengo; ndiyo, walikuwa wenye bidii, na walifanya kazi sana.

6 Na watu walitaka kwamba Alma awe mfalme wao, kwani alipendwa na watu wake.

7 Lakini aliwaambia: Tazameni, haistahili kwamba tuwe na mfalme; kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana: [a]Hamtatukuza mwili mmoja zaidi ya mwingine, au mtu asidhani kwamba yuko juu zaidi ya mwingine; kwa hivyo nawaambia haistahili muwe na mfalme.

8 Walakini, kama ingewezekana muwe na watu wenye haki nyakati zote wawe wafalme wenu ingekuwa ni vyema kwenu muwe na mfalme.

9 Lakini kumbukeni [a]maovu ya mfalme Nuhu na makuhani wake; na mimi mwenyewe [b]nilinaswa katika mtego, na nilifanya vitu vingi ambavyo vilikuwa vinachukiza machoni mwa Bwana, na vilinisababishia shida kuu ya kutubu;

10 Walakini, baada ya [a]shida nyingi, Bwana alisikia vilio vyangu, na akajibu sala zangu, na amenifanya kuwa chombo mikononi mwake cha kuwezesha wengi wenu [b]sana kuwa na ufahamu wa ukweli wake.

11 Walakini, kwa hii mimi sijitukuzi, kwani mimi sistahili kujitukuza mwenyewe.

---

23 7*a* Mos. 27:3–5. 9*a* Mit. 16:12; Mos. 11:1–15. *b* Mos. 17:1–4. 10*a* M&M 58:4. *b* Mos. 18:35.

12 Na sasa nawaambia, mmedhulumiwa na mfalme Nuhu, na mmekuwa utumwani kwake na kwa makuhani wake, na kuwekwa kwenye uovu nao; kwa hivyo mlifungwa kwa [a]kanda za maovu.

13 Na sasa kwa vile mmekombolewa kwa nguvu za Mungu kutoka kwa hii minyororo; ndiyo, kutoka kwa mikono ya mfalme Nuhu na watu wake, na pia kutoka kwa minyororo ya maovu, hata hivyo ninataka [a]msimame imara kwenye huo [b]uhuru ambao kwa hii mmekombolewa, na kwamba [c]msimwamini mtu yeyote kuwa mfalme juu yenu.

14 Na pia msimwamini yeyote kuwa [a]mwalimu wenu wala mhubiri wenu, ila tu awe mtu wa Mungu, anayetembea katika njia zake na kutii amri zake.

15 Hivi ndivyo Alma alivyowafundisha watu wake, kwamba kila mtu [a]ampende jirani yake jinsi anavyojipenda mwenyewe, kwamba kusiwe na [b]ubishi miongoni mwao.

16 Na sasa, Alma alikuwa [a]kuhani wao mkuu, yeye akiwa mwanzilishi wa kanisa lao.

17 Na ikawa kwamba hakuna yeyote aliyepokea [a]mamlaka ya kuhubiri au kufundisha ila tu kwa yule wa kutoka kwa Mungu. Kwa hivyo aliwatakasa makuhani wao wote na walimu wao wote; na hakuna yeyote aliyetakaswa ila tu wale wanadamu waliokuwa wenye haki.

18 Kwa hivyo waliwalinda watu wao, na [a]kuwalisha vitu vilivyohusu haki.

19 Na ikawa kwamba walianza kufanikiwa sana nchini; na wakaiita nchi ile Helamu.

20 Na ikawa kwamba waliongezeka na kufanikiwa sana katika nchi ya Helamu; na wakajenga mji, ambao waliuita mji wa Helamu.

21 Walakini Bwana anaonelea vyema [a]kuwarekebisha watu wake; ndiyo, anajaribu [b]subira na imani yao.

22 Walakini—yeyote atakayeweka [a]imani yake kwake, yeye [b]atainuliwa juu siku ya mwisho. Ndiyo, na hivi ndivyo ilivyokuwa na watu hawa.

23 Kwani tazama, nitakuonyesha kwamba walitiwa utumwani, na hakuna yeyote ambaye angewakomboa ila tu Bwana Mungu wao, ndiyo, hata Mungu wa Ibrahimu na Isaka na wa Yakobo.

24 Na ikawa kwamba aliwakomboa, na akawaonyesha uwezo wake mkuu, na walifurahi sana.

25 Kwani tazama, ikawa kwamba walipokuwa katika nchi ya Helamu, ndiyo, katika mji wa Helamu, walipokuwa wakilima ardhi ambayo imeizingira, tazama jeshi la Walamani lilikuwa katika mipaka ya nchi.

12 *a* 2 Ne. 28:19–22.
13 *a* Gal. 5:1.
b MWM Huru, Uhuru.
c Mos. 29:13.
14 *a* Mos. 18:18–22.
15 *a* MWM Upendo.
b 3 Ne. 11:28–29.
16 *a* Mos. 26:7.
17 *a* MWM Mamlaka; Ukuhani.
18 *a* 1 Tim. 4:6.
21 *a* Hel. 12:3; M&M 98:21.
MWM Rudi, Kurudiwa.
b MWM Subira.
22 *a* MWM Tegemea.
b 1 Ne. 13:37.

26 Sasa ikawa kwamba ndugu za Alma walitoroka kutoka mashamba yao, na kujikusanya pamoja kwenye mji wa Helamu; na walikuwa na woga mwingi kwa sababu ya kuonekana kwa Walamani.

27 Na Alma aliwaendea na kusimama miongoni mwao, na kuwasihi kwamba wasiogope, lakini kwamba wamkumbuke Bwana Mungu wao na atawakomboa.

28 Kwa hivyo wakatuliza woga wao, na kuanza kumlilia Bwana kwamba alainishe mioyo ya Walamani, ili wawahurumie, na wake zao, na watoto wao.

29 Na ikawa kwamba Bwana alilainisha mioyo ya Walamani. Na Alma na ndugu zake wakaenda na kujitoa mikononi mwao; na Walamani wakamiliki nchi ya Helamu.

30 Sasa majeshi ya Walamani, yaliokuwa yamefuata watu wa mfalme Limhi, yalipotea nyikani kwa siku nyingi.

31 Na tazama, waliwapata wale makuhani wa mfalme Nuhu, katika mahali walipoita Amuloni; na walikuwa wameanza kumiliki nchi ya Amuloni na kuanza kulima ardhi.

32 Sasa jina la yule kiongozi wa makuhani lilikuwa Amuloni.

33 Na ikawa kwamba Amuloni aliwasihi Walamani; na pia akawatuma wake zao, ambao walikuwa [a]mabinti za Walamani, kusihi ndugu zao, kwamba wasiwaangamize waume wao.

34 Na Walamani waliwaonea [a]huruma Amuloni na ndugu zake, na hawakuwaangamiza, kwa sababu ya wake zao.

35 Na Amuloni na ndugu zake waliungana na Walamani, na walikuwa wakisafiri nyikani wakitafuta nchi ya Nefi walipoigundua nchi ya Helamu, ambayo ilikuwa imemilikiwa na Alma na ndugu zake.

36 Na ikawa kwamba Walamani wakawaahidi Alma na ndugu zake, kwamba kama wangewaonyesha njia ya kuelekea hadi nchi ya Nefi wangeokoa maisha yao na kuwapatia uhuru wao.

37 Lakini baada ya Alma kuwaonyesha njia iliyoelekea hadi nchi ya Nefi Walamani hawakutimiza ahadi yao; lakini waliwawekea Alma na ndugu zake [a]walinzi, kuizingira nchi ya Helamu.

38 Na waliosalia walienda katika nchi ya Nefi; na wengine wao walirejea katika nchi ya Helamu, na pia kuwaleta wake na watoto wa walinzi walioachwa katika nchi.

39 Na mfalme wa Walamani alikuwa amemruhusu Amuloni kwamba awe mfalme na mtawala wa watu wake, ambao walikuwa katika nchi ya Helamu; walakini hakuwa na uwezo wa kufanya lolote ambalo lilikuwa kinyume cha matakwa ya mfalme wa Walamani.

MLANGO WA 24

Amuloni anawatesa Alma na

33*a* Mos. 20:3–5. | 34*a* MWM Huruma. | 37*a* Mos. 24:8–15.

watu wake—Watauawa kama watasali—Bwana anaifanya mizigo yao iwe miepesi—Anawokomboa kutoka utumwani, na wanarajea Zarahemla. Karibia mwaka 145–120 K.K.

NA ikawa kwamba Amuloni alipendelewa na mfalme wa Walamani; kwa hivyo, mfalme wa Walamani aliwaruhusu yeye na ndugu zake wateuliwe kuwa walimu wa watu wake, ndiyo, hata juu ya watu waliokuwa katika nchi ya Shemloni, na katika nchi ya Shilomu, na katika nchi ya Amuloni.

2 Kwani Walamani walikuwa wamemiliki nchi hizi zote; kwa hivyo, mfalme wa Walamani alikuwa amewateua wafalme katika nchi hizi.

3 Na sasa jina la mfalme wa Walamani lilikuwa Lamani, akiitwa kwa jina la baba yake; na kwa hivyo aliitwa mfalme Lamani. Na alikuwa mfalme wa watu wengi.

4 Na aliwateua walimu wa ndugu za Amuloni katika kila nchi iliyomilikiwa na watu wake; na hivyo lugha ya Nefi ilianza kufundishwa miongoni mwa watu wote wa Walamani.

5 Na walikuwa watu ambao walipendana wao kwa wao, walakini hawakumjua Mungu; wala ndugu za Amuloni hawakuwafundisha chochote kuhusu Bwana Mungu wao, wala sheria ya Musa; wala hawakuwafundisha maneno ya Abinadi;

6 Lakini waliwafundisha kuhifadhi maandishi yao, na kwamba waandikiane wao kwa wao.

7 Na hivyo Walamani wakaanza kufanikiwa kwa utajiri, na wakaanza kufanya biashara wao kwa wao na kuwa na nguvu, na wakaanza kuwa wajanja na watu wenye hekima, kulingana na hekima ya ulimwengu, ndiyo, watu wenye ujanja mwingi, na kufurahishwa na kila aina ya uovu na uporaji, ila tu miongoni mwa ndugu zao.

8 Na sasa ikawa kwamba Amuloni alianza [a]kuwanyanyasa Alma na ndugu zake, na kuanza kumtesa na kuwasababisha watoto wake kuwatesa watoto wao.

9 Kwani Amuloni alikuwa amemjua Alma, kwamba alikuwa [a]mmoja wa makuhani wa mfalme, na kwamba ni yeye aliyeamini maneno ya Abinadi na kufukuzwa kutoka mbele ya mfalme, na kwa hivyo alikasirishwa na yeye; kwani alikuwa chini ya mfalme Lamani, na bado aliwanyanyasa, na kuwafanyisha kazi [b]ngumu, na kuwawekea manyapara.

10 Na ikawa kwamba mateso yao yalikuwa makubwa hata kwamba wakaanza kumlilia Mungu.

11 Na Amuloni akawaamuru kwamba waache vilio vyao; na aliwawekea walinzi kuwalinda, kwamba yeyote atakayepatikana akimlingana Mungu auawe.

24 8*a* M&M 121:39. | 9*a* Mos. 17:1–4; 23:9. | *b* Mos. 21:3–6.

12 Na Alma na watu wake hawakupaza sauti zao kwa Bwana Mungu wao, lakini [a]walimfunulia mioyo yao; na alijua mawazo ya mioyo yao.

13 Na ikawa kwamba sauti ya Bwana iliwafikia katika mateso yao, ikisema: lnueni vichwa vyenu na msherehekee, kwani ninajua agano ambalo mlinifanyia; na nitaagana na watu wangu na kuwakomboa kutoka utumwani.

14 Na pia nitawapunguzia mizigo ambayo imewekwa mabegani yenu, hata kwamba hamtaisikia kamwe migongoni mwenu, hata mkiwa utumwani; na nitafanya haya ili muwe [a]mashahidi wangu hapo baadaye, na kwamba mjue kwa hakika kwamba mimi, Bwana Mungu, huwatembelea watu wangu katika [b]mateso yao.

15 Na sasa ikawa kwamba mizigo ambayo ilikuwa wamewekewa Alma na ndugu zake ilipunguzwa; ndiyo, Bwana aliwapatia [a]nguvu kwamba wabebe [b]mizigo yao kwa urahisi, na walinyenyekea kwa furaha na [c]subira kwa mapenzi ya Bwana.

16 Na ikawa kwamba imani yao na subira yao ilikuwa kuu sana hata kwamba sauti ya Bwana ikawajia tena, ikisema: Shangilieni, kwani hapo kesho nitawakomboa kutoka utumwani.

17 Na akamwambia Alma: Wewe utaenda mbele ya hawa watu, na nitaenda nawe na kuwakomboa watu hawa kutoka [a]utumwani.

18 Na sasa ikawa kwamba Alma na watu wake walikusanya mifugo yao pamoja usiku, na pia nafaka yao; ndiyo, hata usiku wote walikusanya mifugo yao pamoja.

19 Na asubuhi Bwana alisababisha [a]usingizi mzito uwapate Walamani, ndiyo, na manyapara wao wote walilala usingizi mzito.

20 Na Alma na watu wake walienda nyikani; na walipokuwa wamesafiri mchana wote walipiga mahema zao katika bonde, na wakaliita lile bonde Alma, kwa sababu aliwaongoza njiani wakielekea nyikani.

21 Ndiyo, na katika bonde la Alma walimpigia [a]shukrani wao kwa Mungu kwa sababu amekuwa mwenye huruma kwao, na kupunguza mizigo yao, na kuwakomboa kutoka utumwani, kwani walikuwa utumwani, na hakuna yeyote ambaye angewakomboa ila tu Bwana Mungu wao.

22 Na wakamshukuru Mungu, ndiyo, waume wao wote na wake zao wote na watoto wao wote ambao waliweza kuzungumza walipaza sauti zao na kumshukuru Mungu wao.

23 Na sasa Bwana akamwa-

12*a* MWM Sala.
14*a* MWM Shahidi, Ushahidi.
b MWM Shida.
15*a* Mt. 11:28–30.
b Alma 31:38; 33:23.
c M&M 54:10. MWM Subira.
17*a* MWM Ufungwa.
19*a* 1 Sam. 26:12.
21*a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.

mbia Alma: Jiharakishe wewe na utoe watu hawa kutoka nchi hii, kwani Walamani wameamka na wanakufuata; kwa hivyo jiondoe kutoka nchi hii, na nitawazuia Walamani katika bonde hili ili wasiwafuate watu hawa.

24 Na ikawa kwamba waliondoka bondeni, na kuelekea nyikani.

25 Na baada ya kuwa nyikani kwa siku kumi na mbili walifika katika nchi ya Zarahemla; na mfalme Mosia aliwapokea kwa shangwe.

MLANGO WA 25

Wazawa wa Muleki katika Zarahemla wanakuwa Wanefi—Wanajifundisha kuhusu watu wa Alma na Zenivu—Alma anawabatiza Limhi na watu wake wote—Mosia anamruhusu Alma kuanzisha Kanisa la Mungu. Karibia mwaka 120 K.K.

Na sasa mfalme Mosia alisababisha kwamba watu wote wakusanyike pamoja.

2 Sasa hakukuwa na watoto wa Nefi wengi, au wale wengi waliokuwa uzao wa Nefi, kama vile wale [a]watu wa Zarahemla, ambaye alikuwa ni wa uzao wa [b]Muleki, na wale ambao walikuja na yeye nyikani.

3 Na watu wa Nefi na watu wa Zarahemla hawakuwa wengi kama Walamani; ndiyo, hata hawakuwa nusu yao.

4 Na sasa watu wote wa Nefi walikuwa wamekusanyika pamoja, na pia watu wote wa Zarahemla, na walikuwa wamekusanyika pamoja kwa vikundi viwili.

5 Na ikawa kwamba Mosia alisoma, na akasababisha kusomwa, kwa maandishi ya Zenivu kwa watu wake; ndiyo, alisoma maandishi ya watu wa Zenivu, tangu ule wakati walipoondoka kutoka nchi ya Zarahemla hadi ule wakati waliporejea tena.

6 Na pia alisoma historia ya Alma na ndugu zake, na mateso yao yote, tangu waondoke nchi ya Zarahemla hadi ule wakati ambao walirejea tena.

7 Na sasa, Mosia alipomaliza kusoma yale maandishi, watu wake ambao walikuwa wamebaki katika nchi ile walijazwa na mshangao na kustaajabu.

8 Kwani hawakujua la kufikiria; kwani walipotazama wale ambao walikuwa wamekombolewa [a]kutoka utumwani walikuwa wamejazwa na shangwe kuu zaidi.

9 Na tena, walipofikiri kuhusu vile ndugu zao walivyouawa na Walamani walijazwa na huzuni, na hata kumwaga machozi mengi ya huzuni.

10 Na tena, walipofikiri kuhusu wema wa Mungu ulio kamili, na uwezo wake katika kuwakomboa Alma na ndugu zake kutoka mikono ya Walamani na utumwa, walipaza sauti zao na kumshukuru Mungu.

11 Na tena, walipofikiri juu ya Walamani, ambao walikuwa ni ndugu zao, jinsi walivyokuwa

25 2*a* Omni 1:13–19.
b Hel. 6:10.
MWM Muleki.
8*a* Mos. 22:11–13.

katika hali ya dhambi na iliyochafuka, walijazwa na [a]uchungu na maumivu kwa sababu ya ustawi wa [b]nafsi zao.

12 Na ikawa kwamba wale ambao walikuwa watoto wa Amuloni na ndugu zake, ambao walikuwa wamewachukua mabinti za Walamani kuwa wake zao, hawakufurahishwa na tabia za babu zao, na hawakutaka waitwe tena kwa majina ya babu zao, kwa hivyo walijichukulia jina la Nefi, ili waitwe watoto wa Nefi na kuhesabiwa miongoni mwa wale walioitwa Wanefi.

13 Na sasa watu wote wa Zarahemla [a]walihesabiwa pamoja na Wanefi, na hii ni kwa sababu ufalme haukukabidhiwa yeyote ila tu wale waliokuwa wa uzao wa Nefi.

14 Na sasa ikawa kwamba Mosia alipomaliza kuzungumza na kusomea watu, alitaka Alma pia azungumzie watu.

15 Na Alma aliwazungumzia, walipokusanyika pamoja katika vikundi vikubwa, na alienda kutoka kwa kikundi kimoja hadi kingine, akiwahubiria watu toba na imani katika Bwana.

16 Na akawasihi watu wa Limhi na ndugu zake, wale wote ambao walikuwa wamekombolewa kutoka utumwani, kwamba wakumbuke kuwa ni Bwana ambaye alikuwa amewakomboa.

17 Na ikawa kwamba baada ya Alma kuwafundisha watu vitu vingi, na kumaliza kuwazungumzia, kwamba mfalme Limhi alitaka abatizwe; na watu wake wote pia walitaka kubatizwa.

18 Kwa hivyo, Alma aliingia katika maji na [a]kuwabatiza; ndiyo, aliwabatiza jinsi alivyobatiza ndugu zake katika yale [b]maji ya Mormoni; ndiyo, na wale wote aliobatiza waliingia katika kanisa la Mungu; na hii ilikuwa ni kwa sababu yao kuamini maneno ya Alma.

19 Na ikawa kwamba mfalme Mosia alimruhusu Alma kuanzisha makanisa kote katika nchi ya Zarahemla; na akampa [a]uwezo wa kuwatawaza makuhani na walimu katika kila kanisa.

20 Sasa haya yalitendeka kwa sababu kulikuwa na watu wengi hata kwamba hawangetawaliwa na mwalimu mmoja; wala hawangesikia neno la Mungu wakiwa katika kikundi kimoja;

21 Kwa hivyo walikusanyika pamoja katika vikundi tofauti, na kuitwa makanisa; kila kanisa likiwa na makuhani wake na walimu wake, na kila kuhani akihubiri neno kulingana na vile lilivyotolewa kwa kinywa cha Alma.

22 Na hivyo, licha ya kuwa na makanisa mengi, yote yalikuwa [a]kanisa moja, ndiyo, hata kanisa la Mungu; kwani hakuna lingine lolote lililohubiriwa

11 *a* Mos. 28:3–4; Alma 13:27.
b MWM Nafsi— Thamani ya nafsi.
13 *a* Omni 1:19.
18 *a* Mos. 21:35.
b Mos. 18:8–17.
19 *a* MWM Ukuhani.
22 *a* Mos. 18:17.

makanisani ila tu toba na imani katika Mungu.

23 Na sasa kulikuwa na makanisa saba katika nchi ya Zarahemla. Na ikawa kwamba wowote waliotaka kulichukua [a]jina la Kristo, au la Mungu, walijiunga na makanisa ya Mungu;

24 Na waliitwa [a]watu wa Mungu. Na Bwana aliwateremshia Roho wake juu yao, na wakabarikiwa, na kufanikiwa katika nchi.

MLANGO WA 26

Washirika wengi wa Kanisa wanaelekezwa dhambini na wasioamini—Alma anaahidiwa uzima wa milele—Wale ambao wanatubu na kubatizwa wanapokea msamaha—Washirika wa Kanisa ambao wako katika dhambi wakitubu na kuungama kwa Alma na kwa Bwana watasamehewa; la sivyo, hawatahesabiwa miongoni mwa watu wa Kanisa. Karibia mwaka 120–100 K.K.

Sasa ikawa kwamba kulikuwa na wengi wa uzao mchanga ambao hawakufahamu maneno ya mfalme Benjamini, kwani walikuwa watoto wadogo alipowazungumzia watu wake; na hawakuamini mila za babu zao.

2 Hawakuamini yale ambayo yalikuwa yamezungumzwa kuhusu ufufuo wa wafu, wala hawakuamini kuhusu kuja kwa Kristo.

3 Na sasa kwa sababu ya kutokuamini kwao [a]hawakufahamu neno la Mungu; na mioyo yao ilikuwa imeshupazwa.

4 Na hawakubatizwa; wala hawakujiunga na kanisa. Na walikuwa watu tofauti kulingana na imani yao, na walishi hivyo daima, katika hali yao ya [a]kimwili na yenye dhambi; kwani hawakumkimbilia Bwana Mungu wao.

5 Na sasa katika utawala wa Mosia hawakuwa nusu ya wingi wa watu wa Mungu; lakini kwa sababu ya [a]mafarakano miongoni mwa ndugu waliongezeka.

6 Kwani ikawa kwamba waliwadaganya wengi kwa maneno yao ya kusifu ya uongo, ambao walikuwa kanisani, na kuwasababisha kutenda dhambi nyingi; kwa hivyo ilibidi wale ambao walikuwa kanisani, na kutenda dhambi, [a]waonywe na kanisa.

7 Na ikawa kwamba waliletwa mbele ya makuhani, na kukabidhiwa kwa makuhani na walimu; na makuhani wakawaleta mbele ya Alma, ambaye alikuwa ni [a]kuhani mkuu.

8 Sasa mfalme Mosia alikuwa amempatia Alma mamlaka juu ya kanisa.

9 Na ikawa kwamba Alma hakujua mengi juu yao; lakini kulikuwa na mashahidi wengi kinyume chao; ndiyo, watu walisimama na kushuhudia sana kuhusu uovu wao.

23*a* MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
24*a* MWM Agano.
26 3*a* MWM Ufahamu.
4*a* MWM Mwanadamu wa Tabia ya Asili.
5*a* MWM Ukengeufu; Ushindani.
6*a* Alma 5:57–58; 6:3. MWM Onya, Onyo.
7*a* Mos. 29:42.

10 Sasa kulikuwa kitu kama hicho hakijawahi kutendeka kanisani; kwa hivyo Alma alisononeka rohoni mwake, na akasababisha kwamba waletwe mbele ya mfalme.

11 Na akamwaambia mfalme: Tazama, hapa kuna wengi ambao tumewaleta mbele yako, na ambao wameshtakiwa na ndugu zao; ndiyo, na wamepatikana katika maovu mengi. Na hawatubu maovu yao; kwa hivyo tumewaleta mbele yako, ili uwahukumu kulingana na hatia zao.

12 Lakini mfalme Mosia alimwambia Alma: Tazama, mimi sitawahukumu; kwa hivyo [a]nawakabidhi mikononi mwako ili wahukumiwe.

13 Na sasa roho ya Alma ilisononeka tena; na akaenda na kumwuliza Bwana yale atakayotenda kuhusu jambo hili, kwani aliogopa kwamba atafanya vibaya mbele ya Mungu.

14 Na ikawa kwamba baada ya kumfunulia Mungu nafsi yake yote, sauti ya Bwana ilimjia, na kusema:

15 Heri wewe, Alma, na heri wale ambao walibatizwa katika [a]maji ya Mormoni. Wewe umebarikiwa kwa sababu ya [b]imani yako kuu katika maneno pekee ya mtumishi wangu Abinadi.

16 Na wamebarikiwa wao kwa sababu ya imani yao kuu katika yale maneno ambayo umewazungumzia.

17 Na wewe umebarikiwa kwa sababu umeanzisha [a]kanisa miongoni mwa watu hawa; na wataimarishwa, na watakuwa watu wangu.

18 Ndiyo, heri watu hawa kwa sababu wako tayari kulichukua [a]jina langu; kwani wataitwa kwa jina langu; na watakuwa wangu.

19 Na kwa sababu wewe umeniuliza kuhusu mwenye dhambi, wewe umebarikiwa.

20 Wewe ni mtumishi wangu; na ninaagana na wewe kwamba utapokea [a]uzima wa milele; na utanitumikia na kuendelea mbele kwa jina langu, na utakusanya pamoja kondoo wangu.

21 Na yule atakayesikia sauti yangu atakuwa [a]kondoo wangu; na yeye utampokea kanisani, na pia mimi nitampokea.

22 Kwani tazama, hili ni kanisa langu; yeyote [a]atakayebatizwa atabatizwa ubatizo wa toba. Na yeyote utakayempokea ataliamini jina langu; na yeye [b]nitamsamehe bila sharti.

23 Kwani ni mimi ambaye [a]najichukulia dhambi za ulimwengu juu yangu; kwani ni mimi ambaye [b]niliwaumba; na ni mimi ambaye nampatia yule anayeamini hadi mwisho mahali kwa mkono wangu wa kuume.

12 *a* M&M 42:78–93.
15 *a* Mos. 18:30.
b Mos. 17:2.
MWM Amini, Imani.
17 *a* Mos. 25:19–24.
18 *a* Mos. 1:11; 5:8.
MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
20 *a* MWM Teule, Wateule; Uteuzi; Uzima wa Milele.
21 *a* MWM Mchungaji Mwema.
22 *a* 2 Ne. 9:23.
MWM Batiza, Ubatizo.
b MWM Ondoleo la Dhambi; Samehe.
23 *a* MWM Mkombozi.
b MWM Umba, Uumbaji.

24 Kwani tazama, kwa jina langu wanaitwa; na ikiwa [a]wananijua watakuja mbele, na watapata mahali pa milele kwa mkono wangu wa kuume.

25 Na itakuwa kwamba tarumbeta ya [a]pili itakapopigwa, basi wale ambao hawajawahi [b]kunijua watakuja mbele na kusimama mbele yangu.

26 Na ndipo watajua kwamba mimi ni Bwana Mungu wao, na kwamba mimi ni Mkombozi wao; lakini hawakutaka kukombolewa.

27 Na kisha nitakiri kwao kwamba [a]sikuwajua; na [b]wataelekea kwenye moto usio na [c]mwisho ambao umetayarishiwa ibilisi na malaika wake.

28 Kwa hivyo nakwaambia, kwamba yule ambaye [a]hatasikia sauti yangu, huyo hutampokea katika kanisa langu, kwani yeye sitampokea katika siku ya mwisho.

29 Kwa hivyo nakuambia, Nenda; na yeyote ambaye ananikosea, huyo [a]utamhukumu [b]kulingana na dhambi ambazo ametenda; na kama [c]ataungama dhambi zake mbele yako na mimi, na [d]atubu kwa moyo wake kwa kweli, [e]utamsamehe, na pia nitamsamehe.

30 Ndiyo, na [a]kila mara watu wangu [b]watatubu, nitawasamehe makosa yao dhidi yangu.

31 Na pia ninyi [a]mtasameheana makosa yenu; kwa kweli nawaambia, yule ambaye hatamsamehe jirani yake makosa anaposema kuwa ametubu, huyu amejiweka chini ya hukumu.

32 Sasa nakwambia, Nenda; na yeyote asiyetubu dhambi zake, huyo hatahesabiwa miongoni mwa watu wangu; na hii itafuatwa kutoka wakati huu na daima.

33 Na ikawa kwamba wakati Alma alipokuwa amesikia maneno haya aliyaandika chini ili awe nayo, na kwamba aweze kuwahukumu watu wa kanisa lile kulingana na amri za Mungu.

34 Na ikawa kwamba Alma alienda na kuwahukumu wale ambao walikuwa wamepatikana na maovu, kulingana na neno la Bwana.

35 Na yeyote ambaye alitubu dhambi zake na [a]kuungama, aliwahesabu wao miongoni mwa watu wa kanisa;

36 Na wale ambao hawakutubu dhambi zao na maovu yao, wao hawakuhesabiwa miongoni mwa watu wa kanisa, na majina yao [a]yalifutwa.

37 Na ikawa kwamba Alma

24 *a* Yn. 17:3.
25 *a* M&M 88:99, 109.
b M&M 76:81–86.
27 *a* Mt. 7:21–23.
b Lk. 13:27.
c M&M 76:43–44.
28 *a* 2 Ne. 9:31; M&M 1:14.
29 *a* MWM Amua, Hukumu.
b MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
c 3 Ne. 1:25. MWM Kiri, Kukiri.
d MWM Toba, Tubu.
e MWM Samehe.
30 *a* Moro. 6:8.
b Eze. 33:11, 15–16; Mdo. 3:19–20; Mos. 29:19–20.
31 *a* 3 Ne. 13:14–15; M&M 64:9–10.
35 *a* MWM Kiri, Kukiri.
36 *a* Ku. 32:33; Alma 1:24. MWM Kitabu cha Uzima; Kutengwa na Kanisa.

aliongoza mambo yote ya kanisa; na wakaanza tena kupata amani na kufanikiwa sana katika mambo ya kanisa, wakitembea kwa uangalifu mbele ya Mungu, wakipokea wengi, na kubatiza wengi.

38 Na sasa hivi vitu vyote ndivyo vile ambavyo Alma na watumishi wenzake waliokuwa juu ya kanisa walifanya, wakitembea kwa uangalifu, wakifundisha neno la Mungu katika vitu vyote, wakiteseka kila aina ya mateso, na kuteswa na wale wote ambao hawakuwa wa kanisa la Mungu.

39 Na waliwaonya ndugu zao; na pia nao [a]walionywa, kila mmoja wao kwa neno la Mungu, kulingana na dhambi zake, au dhambi ambazo alikuwa ametenda, na kuamriwa na Mungu [b]wasali bila [c]kukoma, na kushukuru kwa vitu vyote.

MLANGO WA 27

Mosia anakomesha mateso na anaamrisha usawa—Alma mdogo na wana wanne wa Mosia wanajaribu kuangamiza Kanisa—Malaika anawatokea na kuwaamuru waache mwenendo wao wa uovu—Alma anapigwa na kuwa bubu—Wanadamu wote lazima wazaliwe tena ili kupata wokovu—Alma na wana wa Mosia wanahubiri habari njema. Karibia mwaka 100–92 K.K.

Na sasa ikawa kwamba yale mateso ambayo yaliwekelewa kanisa na wasioamini yalikuwa makuu hata kwamba kanisa likaanza kunung'unika, na kulalamikia viongozi wao kuhusu hilo jambo; na walimlalamikia Alma. Na Alma akamwelezea mfalme wao, Mosia, hii kesi. Na Mosia alishauriana na makuhani wake.

2 Na ikawa kwamba mfalme Mosia alituma tangazo kote nchini kwamba wale wasioamini [a]wasiwatese wale ambao walikuwa wa kanisa la Mungu.

3 Na kulikuwa na amri kali katika makanisa yote kwamba kusiwe na mateso miongoni mwao, na kwamba kuwe na [a]usawa miongoni mwa watu wote;

4 Kwamba wasikubali kiburi au maringo kuharibu [a]amani yao; kwamba kila mtu [b]amheshimu jirani yake jinsi anavyojiheshimu, na kufanya kazi kwa mikono yao wenyewe ili waishi.

5 Ndiyo, na makuhani wao wote na walimu wao wote iliwabidi kufanya [a]kazi kwa mikono yao ili waweze kuishi, katika kila hali isipokuwa wanapougua, au wakiwa na taabu nyingi; na kwa kufanya vitu hivi, walipokea [b]neema ya Mungu.

6 Na kukawa na amani kubwa tena katika nchi; na watu wakaanza kuongezeka sana, na wakaanza kutawanyika huku na kule usoni mwa dunia, ndiyo, kaskazini na kusini, mashariki

39 *a* MWM Onya, Onyo.
b 2 Ne. 32:8–9.
c MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.

27 2 *a* MWM Mateso, Tesa.
3 *a* Mos. 23:7; 29:32.
4 *a* MWM Amani.
b MWM Tukuza.
5 *a* Mos. 18:24, 26.
b MWM Neema.

na magharibi, wakijenga miji mikubwa na vijiji katika sehemu zote za nchi.

7 Na Bwana aliwatembelea na kuwafanikisha, na wakawa watu wengi na matajiri.

8 Sasa wana wa Mosia walihesabiwa miongoni mwa wale makafiri; na pia [a]mwana mmoja wa Alma alihesabiwa miongoni mwao, yeye akiitwa Alma, kama baba yake; walakini, akawa mtu mwovu na mwenye kuabudu [b]sanamu. Na alikuwa mtu wa maneno mengi, na aliwaelezea watu maneno mengi ya mzaha; kwa hivyo aliwaongoza watu wengi watende maovu kama yake.

9 Na akawa pingamizi kuu kwa mafanikio ya kanisa la Mungu; [a]akiiba mioyo ya watu; akisababisha mafarakano miongoni mwa watu; na kumpatia adui wa Mungu nafasi ya kuwatawala kwa uwezo wake.

10 Na ikawa kwamba alipokuwa akienda hivyo ili aangamize kanisa la Mungu, kwani alienda hivyo kwa kisiri na wana wa Mosia ili waangamize kanisa, na kuwapotosha watu wa Bwana, kinyume cha amri za Mungu, au hata mfalme—

11 Na kama vile nilivyowaelezea, jinsi vile [a]walivyomuasi Mungu, tazama, [b]malaika wa Bwana [c]aliowatokea; na alishuka kama kwa wingu; na alizungumza kwa sauti kama radi, iliyosababisha ardhi kutetemeka pale waliposimama;

12 Na walikuwa na mshangao mkuu, hata kwamba wakainama kwenye ardhi, na hawakufahamu maneno yale ambayo aliwazungumzia.

13 Walakini alipaza sauti tena, akisema: Alma, inuka na usimame, kwa nini wewe unalitesa kanisa la Mungu? Kwani Bwana amesema: [a]Hili ni kanisa langu, na nitalijenga; na hakuna lolote litakalolipinga, ila tu watu wangu watende dhambi.

14 Na tena, malaika akasema: Tazama, Bwana amesikia [a]sala za watu wake, na pia sala za mtumishi wake, Alma, ambaye ni baba yako; kwani ameomba kwa imani kubwa kukuhusu ili upate kuelimika kwa ukweli; kwa hivyo, ni kwa sababu hii nimekuja kukusadikisha kuhusu uwezo na mamlaka ya Mungu, kwamba [b]sala za watumishi wake zijibiwe kulingana na imani yao.

15 Na sasa tazameni, je unaweza kupinga nguvu za Mungu? Kwani tazama, si sauti yangu inatingisha ardhi? Na pia hunioni mbele yako? Na nimetumwa kutoka kwa Mungu.

16 Sasa nakwambia: Nenda, na ukumbuke utumwa wa babu zako katika nchi ya Helamu, na katika nchi ya Nefi; na kumbuka vile vitu vikuu ambavyo amewatendea; kwani walikuwa

8*a* MWM Alma, Mwana wa Alma.
b MWM Kuabudu sanamu.
9*a* 2 Sam. 15:1–6.
11*a* MWM Uasi.
b MWM Malaika.
c Mdo. 9:1–9; Alma 8:15.
13*a* MWM Yesu Kristo—Kichwa cha Kanisa.
14*a* Alma 10:22.
b Morm. 9:36–37.

utumwani, na [a]amewakomboa. Na sasa nakuambia wewe, Alma, enda njia yako, na usijaribu kuangamiza kanisa tena, ili sala zao zijibiwe, na hivi hata kama wewe mwenyewe utataka kutupiliwa mbali.

17 Na sasa ikawa kwamba haya ndiyo yalikuwa maneno ya mwisho ambayo malaika alimwambia Alma, na akaondoka.

18 Na sasa Alma na wale wengine aliokuwa nao waliinama tena kwenye ardhi kwani mshangao wao ulikuwa mkuu; kwani kwa macho yao walikuwa wameona malaika wa Bwana; na sauti yake ilikuwa kama radi, ambayo ilitingisha ulimwengu; na walijua kwamba hakuna kingine chochote ila tu nguvu za Mungu ambazo zingetingisha ulimwengu mpaka ionekane kama itapasuka.

19 Na sasa mshangao wa Alma ulikuwa mkubwa sana kwamba akawa bubu, asiweze kufungua kinywa chake; ndiyo, na akawa mnyonge, hata kwamba hakuweza kunyosha mikono yake; kwa hivyo alibebwa na wale ambao walikuwa na yeye, akiwa hajiwezi, hata mpaka walipomweka mbele ya baba yake.

20 Na wakamwambia baba yake yote ambayo yaliwatokea; na baba yake alifurahi, kwani alijua kwamba ulikuwa ni uwezo wa Mungu.

21 Na akasababisha kwamba umati ukusanywe pamoja ili ushuhudie yale ambayo Bwana alikuwa amemtendea mwana wake, na pia kwa wale ambao walikuwa na yeye.

22 Na akasababisha kwamba makuhani wakusanyike pamoja; na wakaanza kufunga, na kumwomba Bwana Mungu wao kwamba afungue kinywa cha Alma, ili azungumze, na pia kwamba viungo vyake vipokee nguvu—kwamba macho ya watu yafunuliwe ili waone na watambue wema na utukufu wa Mungu.

23 Na ikawa kwamba baada ya wao kufunga na kuomba kwa muda wa siku mbili kuchwa, viungo vya Alma vilipokea nguvu, na akasimama na akaanza kuwazungumzia, na kuwaalika kwamba wawe na faraja:

24 Kwani, alisema, nimetubu dhambi zangu, na [a]kukombolewa na Bwana; tazama nimezaliwa kwa Roho.

25 Na Bwana akaniambia: Usishangae kwamba wanadamu wote, ndiyo, wanaume na wanawake, mataifa yote, makabila, lugha na watu, lazima [a]wazaliwe mara ya pili; ndiyo, wazaliwe na Mungu, [b]wabadilishwe kutoka hali yao ya [c]kimwili na ya kuanguka, kwa hali ya haki, na kukombolewa na Mungu, na kuwa wana na mabinti zake;

16 *a* Mos. 23:1–4.
24 *a* 2 Ne. 2:6–7. MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
25 *a* Rum. 6:3–11; Mos. 5:7; Alma 5:14; Musa 6:59. MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
b Mos. 3:19; 16:3.
c MWM Tamaa za kimwili.

26 Na hivyo wanakuwa viumbe vipya; na wasipofanya hivi, [a]hawawezi kwa vyovyote kurithi ufalme wa Mungu.

27 Nawaambia, isipokuwa hivi, lazima watengwe; na hii najua, kwa sababu karibu mimi nitengwe.

28 Walakini, baada ya kupitia mateso mengi, na kukaribia kifo kwa kutubu, Bwana kwa rehema zake ameonelea kwamba ni vyema kuninyakua ili nisiungue [a]milele, na nimezaliwa na Mungu.

29 Nafsi yangu imekombolewa kutoka nyongo ya uchungu na vifungo vya uovu. Nilikuwa katika shimo la giza nyingi; lakini sasa naona mwangaza wa ajabu wa Mungu. Nafsi yangu [a]ilisononeshwa na uchungu usio na mwisho; lakini nimenyakuliwa, na nafsi yangu haina maumivu tena.

30 Nilimkataa Mkombozi wangu, na kuyakana yale ambayo yalizungumzwa na babu zetu; lakini sasa ili waone kuwa atakuja, na kwamba yeye hukumbuka kila kiumbe ambacho ameumba, atajidhihirisha kwa wote.

31 Ndiyo, [a]kila goti litainama, na kila ulimi utakiri mbele yake. Ndiyo, hata katika siku ya mwisho, ambapo wanadamu wote watasimama [b]kuhukumiwa na yeye, kisha watakiri kwamba yeye ni Mungu; na kisha watakiri, wale ambao wanaishi ulimwenguni [c]bila Mungu, kwamba hukumu ya adhibio isiyo na mwisho ambayo iko juu yao ni ya haki; na watatetemeka, na kutikisika, na kuogopa mbele ya tazamo la jicho lake ambalo huona [d]kote.

32 Na sasa ikawa kwamba Alma alianza kutoka wakati huu na kwenda mbele kufundisha watu, na wale ambao walikuwa na Alma wakati ambao malaika aliwatokea, wakisafiri kote nchini, wakiwatangazia watu wote vitu vile ambavyo walikuwa wameona na kusikia, na kuhubiri neno la Mungu kwa mateso mengi, wakiteswa sana na wale wasioamini, na wakipigwa na wengi wao.

33 Licha ya haya yote, walilifariji kanisa sana, na kuthibitisha imani yao, na kuwaonya kwa subira kuu na uchungu wazitii amri za Mungu.

34 Na wanne wao walikuwa ni [a]wana wa Mosia; na majina yao yalikuwa ni Amoni, na Haruni, na Omneri, na Himni; haya ndiyo yalikuwa majina ya wana wa Mosia.

35 Na walisafiri katika nchi yote ya Zarahemla, na miongoni mwa watu wote ambao walitawaliwa na mfalme Mosia, wakijibidiisha kuponya majeraha yote ambayo walikuwa wamelifanyia kanisa, wakitubu dhambi zao zote, na kutangaza vitu vyote ambavyo walikuwa wameona, na wakieleza unabii

26*a* Yn. 3:5.
28*a* 2 Ne. 9:16.
29*a* Mos. 2:38.
31*a* Flp. 2:9–11; Mos. 16:1–2; M&M 88:104.
b MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
c Alma 41:11.
d MWM Mungu, Uungu.
34*a* MWM Amoni, Mwana wa Mosia.

na maandiko kwa wote ambao walitaka kuyasikia.

36 Na hivyo walikuwa vyombo mikononi mwa Mungu kwa kuwezesha wengi kufahamu ukweli, ndiyo, kwa ufahamu wa Mkombozi wao.

37 Na jinsi gani walivyobarikiwa! Kwani [a]walitangaza amani; walitangaza [b]habari njema ya mambo mema; na waliwatangazia watu kwamba Bwana anatawala.

MLANGO WA 28

Wana wa Mosia wanaenda kuwahubiria Walamani—Akitumia yale mawe mawili ya mwonaji, Mosia anatafsiri mabamba ya Kiyaredi. Karibia mwaka 92 K.K.

Sasa ikawa kwamba baada ya [a]wana wa Mosia kufanya vitu hivi vyote, walichukua kikundi kidogo na kurejea kwa baba yao, mfalme, na wakataka waruhusiwe, wao pamoja na wale ambao walikuwa wamewateua, kwamba waende hadi katika nchi ya [b]Nefi ili wahubiri vitu vile ambavyo walikuwa wamesikia, na ili wawapatie ndugu zao, Walamani, neno la Mungu—

2 Ili pengine wawafahamishe kuhusu Bwana Mungu wao, na kuwasadikisha kuhusu maovu ya baba zao; na ili pengine waponye [a]chuki yao kwa Wanefi, ili pia wawezeshwe kumshere-hekea Bwana Mungu wao, ili wawe marafiki wao kwa wao, kwamba kusiwe na mabishano katika nchi yote ambayo Bwana Mungu wao alikuwa amewapatia.

3 Sasa walitamani kwamba wokovu utangaziwe kila kiumbe, kwani [a]hawangevumilia kwamba [b]nafsi ya mwanadamu yeyote iangamie; ndiyo, hata mafikira kwamba kuna nafsi yoyote itakayopata kuteswa kwa [c]milele iliwafanya kutetemeka na kutikisika.

4 Na hivyo ndivyo Roho wa Bwana alivyowatendea, kwani wao ndiyo waliokuwa wenye dhambi [a]mbaya mno. Na Bwana katika [b]rehema yake aliona kwamba inafaa awaachilie; walakini waliteseka sana katika nafsi zao kwa sababu ya maovu yao, wakiteseka sana na kuogopa kwamba watatengwa milele.

5 Na ikawa kwamba walimsihi baba yao kwa siku nyingi ili waende katika nchi ya Nefi.

6 Na mfalme Mosia akaenda kumwuliza Bwana ili ajue kama atawaruhusu wanawe waende kuhubiria neno miongoni mwa Walamani.

7 Na Bwana akamwaambia Mosia: Waruhusu waende, kwani wengi wataamini maneno yao, na watapokea uzima wa milele; na [a]nitawakomboa

37 *a* Isa. 52:7; Mos. 15:14–17.
mwm Hubiri.
b *mwm* Injili.

28 1 *a* Mos. 27:34.
b Omni 1:12–13; Mos. 9:1.

2 *a* Yak. (KM) 7:24.

3 *a* Alma 13:27; 3 Ne. 17:14; Musa 7:41.
b *mwm* Nafsi—Thamani ya nafsi.
c Yak. (KM) 6:10; M&M 19:10–12.

4 *a* Mos. 27:10.
b *mwm* Rehema, enye Rehema.

7 *a* Alma 19:22–23.

wana wako kutoka mikono ya Walamani.

8 Na ikawa kwamba Mosia aliwaruhusu waende na kutenda kulingana na haja yao.

9 Na [a]wakasafiri nyikani ili wahubiri neno miongoni mwa Walamani; na nitatoa [b]historia ya matendo yao hapo baadaye.

10 Sasa mfalme Mosia hakuwa na yeyote wa kumkabidhi ufalme wake, kwani hakukuwa na yeyote miongoni mwa wanawe aliyekubali ufalme.

11 Kwa hivyo alichukua kumbukumbu ambazo zilikuwa zimechorwa katika [a]mabamba ya shaba nyeupe, na pia mabamba ya Nefi, na vitu vyote alivyokuwa ameweka na kuhifadhi kulingana na amri za Mungu, baada ya kutafsiri na kusababisha kuandikwa kumbukumbu ambazo zilikuwa kwenye [b]mabamba ya dhahabu ambayo yalikuwa yamegunduliwa na watu wa Limhi, na ambayo alipewa kwa mkono wa Limhi;

12 Na alifanya hivi kwa sababu ya wasiwasi mkuu wa watu wake; kwani walitamani sana kujua kuhusu wale watu ambao walikuwa wameangamizwa.

13 Na sasa alizitafsiri kwa kuyatumia yale [a]mawe mawili ambayo yalikuwa yamefungiliwa katika ile mizingo miwili ya pinde.

14 Sasa hivi vilikuwa vimetayarishwa tangu mwanzo, na vilipitishwa kutoka kizazi hadi kizazi, kwa lengo la kutafsiri lugha;

15 Na vimewekwa na kuhifadhiwa kwa mkono wa Bwana, ili afichulie kila kiumbe ambacho kitamiliki nchi maovu na machukizo ya watu wake;

16 Na yeyote aliye na vitu hivi anaitwa [a]mwonaji, kama zile nyakati za kale.

17 Sasa baada ya Mosia kumaliza kutafsiri maandishi haya, tazama, yalieleza historia ya watu ambao [a]waliangamizwa, kutoka ule wakati walioangamizwa hadi ule wakati ule [b]mnara mkuu uliojengwa, ule wakati ambao Bwana [c]alichanganya lugha ya watu na wakatawanywa kote usoni mwa ulimwengu, ndiyo, na hata kutoka wakati huo kurudi nyuma hadi uumbaji wa Adamu.

18 Sasa historia hii iliwafanya watu wa Mosia kuomboleza sana, ndiyo, walijazwa na hofu; walakini iliwapa ufahamu mwingi, ambao uliwafurahisha.

19 Na historia hii itaandikwa hapo baadaye; kwani tazama, ni muhimu watu wote kujua vitu ambavyo vimeandikwa katika historia hii.

20 Na sasa, kama vile nilivyowaambia, kwamba baada ya mfalme Mosia kutenda vitu hivi, alichukua yale mabamba

9 *a* Alma 17:6–9.
b Alma 17–26.
11 *a* MWM Mabamba ya Shaba Nyeupe.
b MWM Mabamba ya Dhahabu.
13 *a* MWM Urimu na Thumimu.
16 *a* Mos. 8:13–18. MWM Mwonaji.
17 *a* Mos. 8:7–12.
b Eth. 1:1–5.
c Mwa. 11:6–9.

ya [a]shaba nyeupe, na vitu vyote ambavyo alikuwa ameweka, na kumkabidhi Alma, ambaye alikuwa ni mwana wa Alma; ndiyo, maandishi yote, na pia [b]vitafsiri, na kumpatia yeye, na akamwamuru kwamba aviweke na [c]avihifadhi, na pia aweke maandishi ya wale watu, na kuvipitisha kutoka kizazi hadi kizazi, hata kama vile vilikuwa vimepitishwa tangu ule wakati Lehi alipoondoka Yerusalemu.

MLANGO WA 29

Mosia anashauri kwamba waamuzi wachaguliwe badala ya mfalme—Wafalme wasio na haki wanaongoza watu wao kwenye dhambi—Alma mdogo anachaguliwa kuwa mwamuzi mkuu kwa sauti ya watu—Yeye pia ni kuhani mkuu wa Kanisa—Alma mkubwa na Mosia wanafariki. Karibia mwaka 92–91 K.K.

Sasa baada ya Mosia kufanya hivi alituma ujumbe kote nchini, miongoni mwa watu wote, akitaka kujua walitaka nani awe mfalme wao.

2 Na ikawa kwamba sauti ya watu ilikuja, ikisema: Tunataka mwana wako Haruni awe mfalme wetu na mtawala wetu.

3 Sasa Haruni alikuwa ameenda katika nchi ya Nefi, kwa hivyo mfalme hangempatia ufalme; wala Haruni hakukubali ufalme; wala hakuna yeyote miongoni mwa [a]wana wa Mosia aliyetaka kuchukua ufalme.

4 Kwa hivyo mfalme Mosia alituma tena ujumbe miongoni mwa watu; ndiyo, alituma miongoni mwa watu kwa maandishi. Na haya ndiyo maneno yalioandikwa, ya kisema:

5 Tazameni, Ee ninyi watu wangu, au ndugu zangu, kwani nawaheshimu hivyo, nataka mfikirie jambo ambalo mnatakiwa kufikiria—kwani mnatamani kupata [a]mfalme.

6 Sasa nawatangazia kwamba yule anayestahili kupokea ufalme amekataa, na hatauchukua ufalme.

7 Na sasa kama kuna mwingine atakayeteuliwa badala yake, tazama naogopa kwamba kutazuka mabishano miongoni mwenu. Na ni nani ajuaye kama mwana wangu, ambaye ufalme ni wake, atakasirika na kuchukua sehemu ya watu hawa, ambayo itasababisha vita na mabishano miongoni mwenu, ambayo itasababisha umwagaji wa damu nyingi na kuchafua njia za Bwana, ndiyo, na kuangamiza nafsi za watu wengi.

8 Sasa nawaambia, hebu tuwe na hekima na tuwaze vitu hivi, kwani hatuna haki ya kumwangamiza mwana wangu, wala hatuna haki ya kumwangamiza mwingine kama atachaguliwa badala yake.

9 Na kama mwana wangu atarudia kiburi chake atakumbuka vitu vile alivyokuwa amesema, na adai haki yake katika

20 *a* Alma 37:3–10.
b MWM Urimu na Thumimu.
c MWM Maandiko—Maandiko yahifadhiwe.
29 3 *a* Mos. 27:34.
5 *a* 1 Sam. 8:9–19.

ufalme, ambayo itamsababisha yeye na pia watu hawa kutenda dhambi.

10 Na sasa hebu tuwe na hekima na tutazamie vitu hivi, na tufanye lile ambalo litawaletea watu hawa amani.

11 Kwa hivyo nitakuwa mfalme wenu katika siku zangu ambazo zimesalia; walakini, hebu [a]tuchague [b]waamuzi, ili wahukumu watu hawa kulingana na sheria yetu; na tutapanga upya mambo ya watu hawa, kwani tutachagua watu wenye hekima kuwa waamuzi, ambao watahukumu watu hawa kulingana na amri za Mungu.

12 Sasa ni afadhali mwanadamu ahukumiwe na Mungu badala ya mwanadamu, kwani hukumu za Mungu ni za haki daima, lakini hukumu za mwanadamu sio za haki daima.

13 Kwa hivyo, kama ingewezekana muwe na watu wenye [a]haki wawe wafalme wenu, ambao wangeimarisha sheria za Mungu, na kuhukumu hawa watu kulingana na amri zake, ndiyo, kama mngekuwa na watu wawe wafalme wenu ambao wangetenda kama baba yangu [b]Benjamini alivyowatendea watu hawa—Nawaambia, kama ingekuwa hivi daima basi ingekuwa inafaa daima muwe na wafalme wa kuwatawala.

14 Na hata mimi mwenyewe nimetumika kwa nguvu zote na uwezo ambao ninao, kuwafundisha amri za Mungu, na kuimarisha amani kote nchini, kwamba kusiwe na vita wala mabishano, wala kuiba, wala uporaji, wala uuaji, wala uovu wa aina yoyote;

15 Na yeyote ambaye ametenda maovu, [a]nimemuadhibu kulingana na hatia ile ambayo ametenda, kulingana na sheria ambayo tumepewa na baba zetu.

16 Sasa nawaambia, kwamba kwa sababu sio wanadamu wote walio wenye haki, haifai muwe na mfalme au wafalme kuwatawala.

17 Kwani tazama, jinsi vile mfalme mmoja [a]mwovu anavyosababisha [b]uovu mkuu kutendwa, ndiyo, na ni mashaka makuu!

18 Ndiyo, kumbuka mfalme Nuhu, uovu wake na machukizo yake, na pia [a]uovu na machukizo ya watu wake. Tazama jinsi yale maangamizo makuu yalivyowapata; na pia kwa sababu ya maovu yao waliwekwa [b]utumwani.

19 Na kama sio kwa sababu ya kuingilia kwa Muumba wao mwenye hekima, na haya kwa sababu ya kutubu kwao kwa kweli, wangekuwa lazima wanaishi utumwani hadi sasa.

20 Lakini tazama, aliwakomboa kwa sababu [a]walijinyenyekeza mbele yake; na kwa sababu [b]walimlilia sana aliwakomboa

11 *a* Mos. 29:25–27.
b Ku. 18:13–24.
13 *a* Mos. 23:8, 13–14.
b M. ya Morm. 1:17–18.
15 *a* Alma 1:32–33.
17 *a* Mos. 23:7–9.
b Alma 46:9–10.
18 *a* Mos. 11:1–15.
b 1 Sam. 8:10–18; Mos. 12:1–8; Eth. 6:22–23.
20 *a* Mos. 21:13–15.
b Ku. 2:23–25; Alma 43:49–50.

kutoka utumwani; na hivi ndivyo Bwana anavyotenda katika hali zote kwa uwezo wake miongoni mwa watoto wa watu, na kuunyosha mkono wake wa [c]rehema kwa wale wote ambao [d]wanamwamini.

21 Na tazama, sasa nawaambia ninyi, hamuwezi kumpindua mfalme mwovu ila tu kwa ubishi mwingi, na umwagaji wa damu nyingi.

22 Kwani tazama, ana [a]marafiki wake katika uovu, na anajizingira na walinzi; na anavunja sheria za wale ambao walitawala kwa haki kabla yake; na huzikanyaga chini ya miguu yake amri za Mungu.

23 Na hutoa sheria mpya, na kuzituma miongoni mwa watu wake, ndiyo, sheria ambazo zinafuata [a]uovu wake; na yeyote ambaye hatii amri zake anasababisha aangamizwe; na yeyote ambaye anamuasi anatumia majeshi yake kumpiga, na kama anaweza, atawaangamiza; na hivyo ndivyo mfalme mwovu huchafua njia za haki.

24 Na sasa tazama nawaambia, haifai kwamba machukizo kama haya yawapate.

25 Kwa hivyo, chagueni kwa sauti ya watu hawa, waamuzi, kwamba mhukumiwe kulingana na sheria ambazo mlipewa na baba zetu, ambazo ni za kweli, na ambazo zilitolewa kwao na mkono wa Bwana.

26 Sasa sio kawaida kwamba sauti ya watu itake lile ambalo ni kinyume cha lile lililo la haki; lakini ni kawaida kwa sehemu ndogo ya watu kutaka lile lisilo la haki; kwa hivyo mtafuata hii na kuifanya iwe sheria yenu—kufanya shughuli zenu kulingana na sauti ya watu.

27 Na [a]kama utafika wakati ambao sauti ya watu itachagua maovu, basi huo ndiyo wakati ambao hukumu za Mungu zitawashukia; ndiyo, kisha atawatembelea kwa maangamizo makuu kama vile ameshatembelea nchi hii.

28 Na sasa kama mtakuwa na waamuzi, na hawawahukumu kulingana na sheria ambayo imetolewa, mnaweza kufanya wahukumiwe na waamuzi mkuu.

29 Kama waamuzi wenu wakuu hawahukumu kwa haki, mtawakusanya waamuzi wenu wadogo kwa kikundi, na watawahukumu waamuzi wenu wakuu, kulingana na sauti ya watu.

30 Na ninawaamuru kutenda vitu hivi kwa kumuogopa Bwana; na ninawaamuru mtende vitu hivi, na kwamba msiwe na mfalme; ili kama watu hawa wakitenda dhambi na maovu, yatakuwa juu ya vichwa vyao wenyewe.

31 Kwani tazama nawaambia, dhambi za watu wengi zimesababishwa na maovu ya wafalme wao; kwa hivyo maovu yao yanadaiwa juu ya vichwa vya wafalme wao.

20 *c* Eze. 33:11, 15–16; Mos. 26:30.
d MWM Tegemea.

22 *a* 1 Fal. 12:8–14.

23 *a* MWM Ovu, Uovu.

27 *a* Alma 10:19.

32 Na sasa sitaki [a]ubaguzi huu uwe tena katika nchi hii, hasa miongoni mwa watu wangu hawa; lakini nahitaji kwamba nchi hii iwe nchi ya [b]uhuru, na [c]kila mtu afurahie haki zake na heshima zake kwa usawa, kadiri vile Bwana atakavyoonelea ni vyema tuishi na kurithi nchi hii, ndiyo, hata kadiri vile uzao wetu utaishi katika nchi hii.

33 Na vitu vingi vingine mfalme Mosia aliwaandikia, na kuwafungulia majaribio na shida zote za mfalme mtakatifu, ndiyo, mateso yote ya nafsi kwa niaba ya watu wao, na pia malalamiko ya watu kwa mfalme wao; na akawaelezea yote.

34 Na akawaambia kwamba lazima mambo haya hayatakiwi kuweko; lakini kwamba uzito lazima uwe kwa watu wote, na kwamba kila mtu abebe sehemu yake.

35 Na pia akawaelezea kuhusu shida ambazo watakuwa nazo, wakitumikia chini ya utawala wa mfalme mwovu;

36 Ndiyo, uovu wake wote na machukizo, na vita vyote, na mabishano, na umwagaji wa damu, na wizi, na uporaji, na kutenda uasherati, na kila aina ya maovu ambayo hayawezi kuhesabika—akiwaambia kwamba lazima vitu hivi havitakiwi kuwepo, na kwamba vilikuwa ni kinyume cha amri za Mungu.

37 Na sasa ikawa kwamba, baada ya mfalme Mosia kutuma vitu hivi miongoni mwa watu walisadiki kuhusu ukweli wa maneno yake.

38 Kwa hivyo waliacha haja yao ya mfalme, na wakataka kila mtu apate nafasi yake katika nchi yote; ndiyo, na kila mtu akawa tayari kuchukua wajibu wa dhambi zake.

39 Kwa hivyo, ikawa kwamba walijikusanya kwa vikundi katika nchi, ili wapige kura na kuchagua waamuzi wao, watakaowahukumu kulingana na [a]sheria ambayo walipewa; na walifurahi sana kwa sababu ya [b]uhuru ambao walipewa.

40 Na waliendelea kumpenda Mosia sana; ndiyo, walimheshimu zaidi ya mtu mwingine yeyote; kwani hawakumchukua kama mkorofi aliyetaka kupata faida, ndiyo, kwa mapato ya aibu yanayochafua nafsi; kwani hakuwa amewanyang'anya utajiri, wala kufurahia umwagaji wa damu; lakini alikuwa ameimarisha [a]amani katika nchi, na alikuwa amewaruhusu watu wake wakombolewe kutoka kila aina ya utumwa; kwa hivyo walimheshimu, ndiyo, kupita kipimo.

41 Na ikawa kwamba walichagua [a]waamuzi wa kuwatawala, au kuwahukumu kulingana na sheria; na walifanya haya kote katika nchi.

42 Na ikawa kwamba Alma alichaguliwa kuwa mwamuzi mkuu wa kwanza, pia akiwa kuhani mkuu, baada ya baba yake kumpatia ofisi hio, na

32 *a* Alma 30:11.
b 2 Ne. 1:7; 10:11.
MWM Huru, Uhuru.
c Alma 27:9.
39 *a* Alma 1:14.
b MWM Huru, Uhuru.
40 *a* MWM Msuluhishi.
41 *a* Mos. 29:11.

baada ya kumpatia jukumu juu ya shughuli zote za kanisa.

43 Na sasa ikawa kwamba Alma [a]alitembea katika njia za Bwana, na akatii amri zake, na alitoa hukumu za haki; na amani ikaimarika kote katika nchi.

44 Na hivyo utawala wa waamuzi ukaanza kote katika nchi ya Zarahemla, miongoni mwa watu wote walioitwa Wanefi; na Alma alikuwa mwamuzi mkuu na wa kwanza.

45 Na sasa ikawa kwamba baba yake alifariki, akiwa na umri wa miaka themanini na miwili, baada ya kuishi na kutimiza amri za Mungu.

46 Na sasa ikawa kwamba Mosia akafariki pia, katika mwaka wa thelathini na tatu wa utawala wake, akiwa na umri wa miaka [a]sitini na mitatu; ikiwa miaka mia tano na tisa tangu Lehi aondoke Yerusalemu.

47 Na hivyo utawala wa wafalme ukaisha kwa watu wa Nefi; na hivyo siku zikaisha za Alma, ambaye alikuwa mwanzilishi wa kanisa lao.

KITABU CHA ALMA

MWANA WA ALMA

Historia ya Alma, ambaye alikuwa mwana wa Alma, mwamuzi mkuu wa kwanza juu ya watu wa Nefi, na pia kuhani mkuu wa Kanisa. Historia kuhusu utawala wa waamuzi, na vita na mabishano miongoni mwa wale watu. Na pia historia ya vita miongoni mwa Wanefi na Walamani, kulingana na maandishi ya Alma, mwamuzi mkuu wa kwanza.

MLANGO WA 1

Nehori anafundisha mafundisho ya uwongo, anaanzisha kanisa, anaanzisha ukuhani wa uongo, na anamuua Gideoni—Nehori anauawa kwa sababu ya hatia zake—Ukuhani wa uongo na mateso yanaenea miongoni mwa watu—Makuhani wanajilisha, watu wanawajalia wale walio masikini, na Kanisa linafanikiwa. Karibia mwaka 91–88 K.K.

SASA ikawa kwamba katika mwaka wa kwanza wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, tangu wakati huu na kuendelea mbele, mfalme Mosia akiwa [a]ameelekea njia ya ulimwengu wote, akiwa amepigana vita vyema, akiwa ametembea wima mbele ya Mungu, akiwa hajaacha yeyote kutawala badala yake; walakini alikuwa ameanzisha [b]sheria, na zilikubaliwa na watu; kwa

43*a* MWM Tembea, Tembea na Mungu.
46*a* Mos. 6:4.

[ALMA]
1 1*a* Mos. 29:46.
b Yar. 1:5; Alma 4:16; Hel. 4:22.

hivyo iliwabidi kuishi kulingana na sheria alizokuwa ameweka.

2 Na ikawa kwamba katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Alma katika kiti cha hukumu, kulikuwa na [a]mtu mmoja ambaye aliletwa mbele yake ili ahukumiwe, mtu aliyekuwa mkubwa, na alifahamika kwa sababu ya nguvu zake nyingi.

3 Na alikuwa ameenda miongoni mwa watu, akiwa amewahubiria yale ambayo [a]aliita neno la Mungu, [b]akipinga kanisa; akiwatangazia watu kwamba inafaa kila kuhani na kila mwalimu awe [c]mashuhuri; na [d]haifai wafanye kazi kwa mikono yao, lakini kwamba inafaa walishwe na watu.

4 Na alishuhudia kwa watu pia kwamba wanadamu wote wataokolewa katika siku ya mwisho, na kwamba haistahili waogope au kubabaika, lakini kwamba wainue vichwa vyao na washangilie; kwani Bwana alikuwa ameumba wanadamu wote, na pia kuwakomboa wanadamu wote; na, mwishowe, wanadamu wote watapokea uzima wa milele.

5 Na ikawa kwamba alifundisha vitu hivi sana hata kwamba wengi waliamini maneno yake, wengi sana hata wakaanza kumlisha na kumpatia pesa.

6 Na akaanza kujiinua kwa kiburi cha moyo wake, na kuvaa mavazi ya thamani nyingi, ndiyo, na hata akaanza kuanzisha [a]kanisa kulingana na mafundisho yake.

7 Na ikawa kwamba alipokuwa akienda, kuhubiria wale walioamini neno lake, alikutana na mtu ambaye alikuwa wa kanisa la Mungu, ndiyo, hata mmoja wa walimu wao; na akaanza kubishana na yeye kwa ukali, ili awapotoshe watu wa kanisa; lakini yule mtu alimpinga, na kumuonya kwa [a]maneno ya Mungu.

8 Sasa jina la yule mtu lilikuwa [a]Gideoni; na ni yeye ndiye aliyekuwa chombo mikononi mwa Mungu cha kuwakomboa watu wa Limhi kutoka utumwani.

9 Sasa, kwa sababu Gideoni alimpinga kwa maneno ya Mungu alimkasirikia Gideoni, na akauchomoa upanga wake na akaanza kumjeruhi. Sasa Gideoni alikuwa amelemewa kwa umri mkuu, kwa hivyo hakuweza kuvumilia mapigo yake, kwa hivyo [a]aliuawa kwa upanga.

10 Na mtu aliyemuua alichukuliwa na watu wa kanisa, na kuletwa mbele ya Alma, [a]kuhukumiwa kulingana na kosa alilotenda.

11 Na ikawa kwamba alisimama mbele ya Alma na kujitetea kwa ujasiri mwingi.

12 Lakini Alma akamwambia: Tazama, hii ndiyo mara

2*a* Alma 1:15.
3*a* Eze. 13:3.
b MWM Mpinga Kristo.
c Lk. 6:26; 1 Ne. 22:23.
d Mos. 18:24, 26; 27:5.
6*a* 1 Ne. 14:10.
7*a* MWM Neno la Mungu.
8*a* Mos. 20:17; 22:3.
9*a* Alma 6:7.
10*a* Mos. 29:42.

ya kwanza kwamba [a]ukuhani wa uongo umeletwa miongoni mwa watu hawa. Na tazama, hatia yako sio tu ya ukuhani wa uongo, lakini umejaribu kuulazimisha kwa upanga; na kama ukuhani wa uongo utalazimishwa miongoni mwa watu hawa utathibitisha maangamizo yao kabisa.

13 Na wewe umemwaga damu ya mtu mwenye haki, ndiyo, mtu ambaye ametenda wema mwingi miongoni mwa watu hawa; na kama tutakuachilia basi damu yake itatujia kulipiza [a]kisasi.

14 Kwa hivyo [a]umehukumiwa kufa, kulingana na sheria ambayo tulipewa na Mosia, mfalme wetu wa mwisho; na imekubaliwa na watu hawa; kwa hivyo lazima watu hawa waishi kulingana na sheria hiyo.

15 Na ikawa kwamba walimchukua; na jina lake lilikuwa [a]Nehori; na wakambeba na kumpeleka juu ya kilima Manti, na hapo akalazimishwa, kwa usahihi zaidi akakubali, kati ya mbingu na ardhi, kwamba yale ambayo alikuwa amefundisha watu yalikuwa kinyume cha neno la Mungu; na hapo akapata [b]kifo cha aibu.

16 Walakini, hii haikukomesha kuenea kwa ukuhani wa uongo katika nchi; kwani kulikuwa na wengi ambao walipenda vitu vya ulimwengu visivyo na faida, na wakaendelea kuhubiri mafundisho ya uwongo; na walitenda haya ili wapate [a]utajiri na heshima.

17 Walakini, hawakuthubutu [a]kudanganya, kama ingejulikana, kwa kuogopa sheria, kwani waongo waliadhibiwa; kwa hivyo walidai kwamba walikuwa wanahubiri kulingana na imani yao; na sasa sheria haikuwa na uwezo wowote juu ya [b]imani ya mtu yeyote.

18 Na hawakuthubutu [a]kuiba, kwani waliogopa sheria, kwani kama hao waliadhibiwa; wala hawakupora, wala kuua, kwani yule [b]aliyeua alihukumiwa [c]kifo.

19 Lakini ikawa kwamba yeyote ambaye hakuwa wa kanisa la Mungu alianza kuwatesa wale ambao walikuwa wa kanisa la Mungu, na waliokuwa wamejivika jina la Kristo.

20 Ndiyo, waliwatesa, na kuwasumbua kwa maneno ya kila aina, na haya yalikuwa ni kwa sababu ya unyenyekevu wao; kwa sababu hawakuwa na majivuno katika macho yao wenyewe, na kwa sababu walifundishana neno la Mungu, wao kwa wao, bila kutozana [a]pesa na bila gharama.

21 Sasa kulikuwa na sheria kali miongoni mwa watu wa kanisa, kwamba kusiwe na mtu yeyote,

12*a* 2 Ne. 26:29. MWM Ukuhani wa uongo.
13*a* MWM Kisasi.
14*a* MWM Adhabu Kuu.
15*a* Alma 1:2.
b Kum. 13:1–9.
16*a* MWM Majivuno, Siofaa; Ukwasi.
17*a* MWM Kusema uongo; Mwaminifu, Uaminifu.
b Alma 30:7–12; M ya I 1:11.
18*a* MWM Iba, Wizi.
b MWM Mauaji.
c MWM Adhabu Kuu.
20*a* Isa. 55:1–2.

miongoni mwa washiriki wa kanisa, atakayeinuka na [a]kuwatesa wale ambao sio washiriki wa kanisa, na kwamba kusiwe na mateso miongoni mwao.

22 Walakini, kulikuwa na wengi miongoni mwao ambao walianza kuwa na kiburi, na kuanza kubishana vikali na wapinzani wao, hata wakapigana kwa ngumi; ndiyo, walipigana kwa ngumi wao kwa wao.

23 Sasa hii ilikuwa katika mwaka wa pili wa utawala wa Alma, na ilikuwa ni chanzo cha mateso mengi kwa kanisa; ndiyo, ilikuwa ni chanzo cha majaribio mengi kwa kanisa.

24 Kwani mioyo ya wengi ilishupazwa na majina yao [a]yalifutwa, hata kwamba hawakukumbukwa tena miongoni mwa watu wa Mungu. Na pia wengi [b]walijiondoa kutoka miongoni mwao.

25 Sasa hili lilikuwa ni jaribio kuu kwa wale ambao walikuwa wamesimama imara katika imani; walakini, walikuwa wameimarishwa na hawangeondolewa katika kutii amri za Mungu, na walivumilia kwa [a]subira mateso yale waliyotundikwa.

26 Na wakati makuhani walipoacha [a]kazi zao ili watoe neno la Mungu kwa watu, watu nao pia waliacha kazi zao ili wasikie neno la Mungu. Na makuhani walipomaliza kuwafundisha neno la Mungu wote walirudia kazi zao kwa bidii; na kuhani, hakujiinua zaidi ya wale ambao walimsikiliza, kwani mhubiri hakuwa bora zaidi kuliko wale ambao walimsikiliza, wala mwalimu hakuwa bora kuliko mwanafunzi; na hivyo wote walikuwa sawa, na wote walifanya kazi, kila mtu [b]kulingana na nguvu zake.

27 Na [a]walipeana mali yao, kulingana na uwezo wao, kwa [b]masikini, na waliohitaji, na wagonjwa, na walioteswa; na hawakuvaa mavazi ya thamani kubwa, lakini walikuwa wasafi na wa kuvutia.

28 Na hivyo waliimarisha mambo ya kanisa; na hivyo wakaanza kuwa na amani bila kikomo tena, ingawa walikuwa wamepata mateso mengi.

29 Na sasa, kwa sababu ya uthabiti wa kanisa walianza [a]kutajirika sana, wakipokea kwa utele vitu vyote walivyohitaji—utele katika mifugo na wanyama, na vinono vya kila aina, na pia utele wa nafaka, na wa dhahabu, na wa fedha, na wa vitu vya thamani, na utele wa [b]hariri na kitani nzuri, na kila aina ya nguo ya kuvutia.

30 Na hivyo, hata katika hali yao ya [a]kufanikiwa, hawakumfukuza yeyote aliyekuwa [b]uchi, au walio na njaa, au walio na

21 *a* MWM Mateso, Tesa.
24 *a* Ku. 32:33; Mos. 26:36; Alma 6:3. MWM Kutengwa na Kanisa.
b Alma 46:7. MWM Ukengeufu.
25 *a* MWM Subira.
26 *a* Mos. 18:24, 26; 27:3–5.
b Mos. 4:27; M&M 10:4.
27 *a* MWM Sadaka, Utoaji sadaka.
b Lk. 18:22; Mos. 4:26; M&M 42:29–31.
29 *a* MWM Ukwasi.
b Alma 4:6.
30 *a* Yak. (KM) 2:17–19.
b MWM Maskini.

kiu, au wale ambao walikuwa wagonjwa, au wale ambao hawakuwa wamelishwa; na hawakuweka mioyo yao katika utajiri; kwa hivyo walikuwa wakarimu kwa wote, wote wazee kwa vijana, wote watumwa na walio huru, wote wanaume kwa wanawake, washiriki wa kanisa na wale wasio washiriki wa kanisa, bila [c]kuwabagua wale wote walio na shida.

31 Na hivyo walifanikiwa na wakawa matajiri zaidi ya wale ambao hawakuwa washiriki wa kanisa.

32 Kwani wale ambao hawakuwa washiriki wa kanisa walijishughulisha na uchawi, na kuabudu [a]sanamu au [b]uvivu, na [c]kusengenyana, na [d]wivu na kuzusha mzozo; wakivaa mavazi yaliyo ghali; [e]wakijiinua kwa kiburi machoni mwao; kutesana, kusema uwongo, kuiba, kupora, kufanya ukahaba, na kuua, na kila aina ya uovu; walakini, sheria ilitimizwa kwa wale wote ambao waliivunja, kwa vyovyote ilivyowezekana.

33 Na ikawa kwamba kwa kutimiza amri juu yao, kila mtu akiteseka kulingana na yale ambayo alitenda, wakawa watulivu zaidi, na hawakutenda uovu wowote ikiwa ungegunduliwa; kwa hivyo, kulikuwa na amani kuu miongoni mwa watu wa Nefi hadi mwaka wa tano wa utawala wa waamuzi.

MLANGO WA 2

Amlisi anataka kuwa mfalme na anakataliwa na kura ya watu—Wafuasi wake wanamtawaza kuwa mfalme—Waamlisi wanapigana na Wanefi na kushindwa—Walamani na Waamlisi wanaungana na kushindwa—Alma anamuua Amlisi. Karibia mwaka 87 K.K.

Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa tano wa utawala wao kulianza kuwa na ubishi miongoni mwa watu; kwani mtu fulani, aliyekuwa anaitwa Amlisi, yeye akiwa mjanja sana, ndiyo, mtu mwenye hekima kulingana na hekima ya ulimwengu, yeye akiwa mfano wa yule mtu aliyemuua [a]Gideoni kwa upanga, ambaye aliuawa kulingana na sheria—

2 Sasa huyu Amlisi, kwa ujanja wake, alikuwa amewavutia watu wengi; wengi sana hata kwamba wakaanza kuwa wenye nguvu; na wakaanza kujaribu kumfanya Amlisi awe mfalme wa watu.

3 Sasa hii ilikuwa ni ya kuogofya kwa watu wa kanisa, na pia kwa wote ambao hawakuwa wamevutiwa na vishawishi vya Amlisi; kwani walijua kwamba kulingana na sheria yao vitu kama hivi lazima vithibitishwe kwa [a]kura ya watu.

4 Kwa hivyo, kama ingewezekana kwamba Amlisi apate kura za watu, yeye akiwa mtu

30 *c* Alma 16:14; M&M 1:35.
32 *a* MWM Kuabudu sanamu.
b MWM Mvivu, Uvivu.
c MWM Kusema uovu.
d MWM Husuda.
e Yak. (KM) 2:13; Alma 31:25; Morm. 8:28. MWM Kiburi.
2 1 *a* Alma 1:8.
3 *a* Mos. 29:25–27; Alma 4:16.

mwovu, [a]angewanyang'anya haki zao na heshima za kanisa; kwani ilikuwa nia yake kuangamiza kanisa la Mungu.

5 Na ikawa kwamba watu walikusanyika pamoja kote nchini, kila mtu kulingana na mawazo yake, kama ilikuwa wanamtaka au wanampinga Amlisi, katika vikundi tofauti, wakipingana sana na kuwa na [a]mabishano ya kushangaza wao kwa wao.

6 Na hivyo walikusanyika pamoja ili wapige kura kuhusu jambo hilo; na wakasimama mbele ya waamuzi.

7 Na ikawa kwamba kura za watu zilikuwa kinyume cha Amlisi, kwamba hakufanywa mfalme wa watu.

8 Sasa hii ilisababisha wale ambao walimpinga wawe na shangwe tele mioyoni mwao; lakini Amlisi aliwachochea wale ambao walimtaka wawakasirikie wale ambao walikuwa wanampinga.

9 Na ikawa kwamba walijikusanya pamoja, na kumteua Amlisi awe mfalme wao.

10 Sasa Amlisi alipofanywa kuwa mfalme wao aliwaamuru kwamba wachukue silaha dhidi ya ndugu zao; na alifanya hivi ili wawe chini yake.

11 Sasa watu wa Amlisi walijulikana kwa jina la Amlisi, wakiitwa [a]Waamlisi; na waliobakia waliitwa [b]Wanefi, au watu wa Mungu.

12 Kwa hivyo watu wa Wanefi walitambua nia ya Waamlisi, na kwa hivyo walijitayarisha kupambana nao; ndiyo, walijiami kwa mapanga, na kwa vitara, na kwa pinde na kwa mishale, na kwa mawe, na kwa kombeo, na kwa kila aina ya [a]silaha za vita, za kila namna.

13 Na hivyo ndivyo walivyojitayarisha kukabiliana na Waamlisi wakati watakapowasili. Na waliwachagua makapteni, na makapteni wa juu, na makapteni wakuu, kulingana na wingi wao.

14 Na ikawa kwamba Amlisi aliwahami wanaume wake kwa kila namna ya silaha za vita; na pia akawachagua watawala na viongozi juu ya watu wake, kuwaongoza ili wapigane na ndugu zao.

15 Na ikawa kwamba Waamlisi waliwasili katika kilima cha Amnihu, ambacho kilikuwa mashariki mwa [a]mto wa Sidoni, ambao ulipita kando ya [b]nchi ya Zarahemla, na hapo wakaanza kushambuliana na Wanefi.

16 Sasa Alma, akiwa [a]mwamuzi mkuu na mtawala wa watu wa Nefi, kwa hivyo alienda juu na watu wake, ndiyo, na makapteni wake, na makapteni wakuu wake, ndiyo, mbele ya majeshi yake, kupigana dhidi ya Waamlisi kwa vita.

17 Na walianza kuwaua Waamlisi katika kilima kilichokuwa mashariki mwa Sidoni. Na Waamlisi walikabiliana na Wanefi

4 *a* Alma 10:19; Hel. 5:2.
5 *a* 3 Ne. 11:29.
11 *a* Alma 3:4.
b Yak. (KM) 1:13–14; Mos. 25:12; Alma 3:11.
12 *a* Mos. 10:8; Hel. 1:14.
15 *a* Alma 3:3.
b Omni 1:13–15.
16 *a* Mos. 29:42.

kwa uwezo mkuu, hata kwamba Wanefi wengi wakaanguka mbele ya Waamlisi.

18 Walakini Bwana aliutia nguvu mkono wa Wanefi, kwamba wakawaua Waamlisi kwa mauaji mengi, hata kwamba wakaanza kutoroka kutoka kwao.

19 Na ikawa kwamba Wanefi waliwafuata Waamlisi siku hiyo yote, na kuwauwa kwa mauaji makuu, hata kwamba Waamlisi elfu kumi na wawili, mia tano thelathini na wawili [a]walikufa; na Wanefi elfu sita, mia tano sitini na wawili walikufa.

20 Na ikawa kwamba wakati Alma hangewafuata Waamlisi zaidi, alisababisha watu wake wapige hema zao katika [a]bonde la Gideoni; bonde hilo likiitwa kwa jina la Gideoni ambaye aliuawa kwa upanga kwa mkono wa [b]Nehori; na Wanefi walipiga hema zao katika bonde hili usiku ule.

21 Na Alma alituma wapelelezi kufuata baki la Waamlisi, ili ajue mipango yao na mitego yao, ili ajilinde kutokana nao, na ili awahifadhi watu wake wasiangamizwe.

22 Sasa wale ambao alikuwa amewatuma kwenda katika kambi ya Waamlisi waliitwa Zeramu, na Amnori, na Manti, na Limheri; hawa ndiyo waliokwenda na watu wao kupeleleza kambi ya Waamlisi.

23 Na ikawa kwamba kesho yake walirejea katika kambi ya Wanefi kwa haraka kuu, wakiwa wameshangaa zaidi, na kujawa na woga mkuu, wakisema:

24 Tazama, tulifuata kambi ya [a]Waamlisi, na kwa mshangao wetu mkuu, katika nchi ya Minoni, ambayo iko juu ya nchi ya Zarahemla, katika njia inayoelekea hadi nchi ya [b]Nefi, tuliona mkusanyiko mkuu wa Walamani; na tazama, Waamlisi wameungana nao;

25 Na wamewashambulia ndugu zetu katika nchi ile; na wanatoroka kutoka mbele yao na mifugo yao, na wake zao, na watoto wao, na wanaelekea katika mji wetu; na tusipoharakisha watateka mji wetu, na baba zetu, na wake zetu, na watoto wetu watauawa.

26 Na ikawa kwamba watu wa Nefi walichukua hema zao, na kuondoka katika bonde la Gideoni na kuelekea katika mji wao, ambao ulikuwa ni mji wa [a]Zarahemla.

27 Na tazama, walipokuwa wakivuka mto wa Sidoni, Walamani na Waamlisi, wakiwa [a]wengi, kama mchanga ya bahari, waliwavamia ili wawaangamize.

28 Walakini, Wanefi wakiwa wameongezwa [a]nguvu na mkono wa Bwana, baada ya kumwomba sana kwamba awakomboe kutoka mikononi mwa maadui zao, kwa hivyo Bwana alisikia vilio vyao, na akawapa nguvu, na Walamani na Waamlisi wakaanguka mbele yao.

29 Na ikawa kwamba Alma

19*a* Alma 3:1–2, 26; 4:2.
20*a* Alma 6:7.
b Alma 1:7–15; 14:16.
24*a* Alma 3:4, 13–18.
b 2 Ne. 5:8.
26*a* Omni 1:14, 18.
27*a* Yar. 1:6.
28*a* Kum. 31:6.

alipigana na Amlisi kwa upanga, ana kwa ana; na walipigana kwa nguvu sana, mmoja kwa mmoja.

30 Na ikawa kwamba Alma akiwa mtu wa Mungu, aliyekuwa na [a]imani kubwa, alipaza sauti, na kusema: Ee Bwana unirehemu na uokoe maisha yangu, ili niwe chombo mikononi mwako cha kuokoa na kuhifadhi watu hawa.

31 Sasa baada ya Alma kunena maneno haya alipigana tena na Amlisi; na akapewa nguvu, hata kwamba akamuua Amlisi kwa upanga.

32 Na pia alipigana na mfalme wa Walamani; lakini mfalme wa Walamani alitoroka kutoka mbele ya Alma na akatuma walinzi wake kupigana na Alma.

33 Lakini Alma, pamoja na walinzi wake, alipigana na walinzi wa mfalme wa Walamani hadi akawaua na kuwasukuma nyuma.

34 Na hivyo alifagia uwanja, kwa usahihi zaidi ufuo, uliokuwa magharibi mwa mto wa Sidoni, na kutupa maiti za Walamani waliokuwa wameuawa katika maji ya Sidoni, ili watu wake wapate nafasi ya kuvuka na kupigana na Walamani na Waamlisi magharibi mwa mto wa Sidoni.

35 Na ikawa kwamba baada ya wao wote kuvuka mto wa Sidoni kwamba Walamani na Waamlisi walianza kutoroka kutoka mbele yao, ingawa walikuwa wengi hata kwamba hawangehesabika.

36 Na wakakimbia kutoka mbele ya Wanefi na kuelekea nyika ambayo ilikuwa magharibi na kaskazini, mbali na mipaka ya nchi; na Wanefi waliwafuata kwa nguvu yao, na kuwaua.

37 Ndiyo, walikamatwa kwa kila upande, na kuuawa na kukimbizwa, hadi wakatawanywa magharibi, na kaskazini, hadi walipoifiki nyika, ambayo iliitwa Hermantsi; na ilikuwa ni sehemu ile ambayo ilikuwa imejaa wanyama wa mwitu ambao ni wakali.

38 Na ikawa kwamba wengi wao walikufa nyikani kutokana na majeraha yao, na wakaliwa na wanyama hao na pia tai wa angani; na mifupa yao imepatikana, na imerundikwa ardhini.

MLANGO WA 3

Waamlisi walikuwa wamejiweka alama kulingana na neno la unabii—Walamani walikuwa wamelaaniwa kwa sababu ya kuasi kwao—Wanadamu hujiletea laana wenyewe—Wanefi wanashinda kikosi kingine cha Walamani. Karibia mwaka 87–86 K.K.

Na ikawa kwamba Wanefi ambao hawakuwa [a]wameuawa kwa silaha za vita, baada ya kuzika wale ambao walikuwa wameuawa—sasa idadi ya wale ambao walikuwa wamekufa haingehesabika, kwa sababu nambari yao ilikuwa kubwa—baada ya kuzika watu wao wote walirejea katika mashamba yao, na kwa nyumba zao, na wake zao, na watoto wao.

30*a* MWM Amini, Imani. | **3** 1*a* Alma 2:19; 4:2.

2 Sasa wanawake wengi na watoto walikuwa wameuawa kwa upanga, na pia mifugo yao na wanyama wao; na pia mashamba yao mengi ya nafaka yaliangamizwa, kwani yalikanyagwa na majeshi.

3 Na sasa Walamani wengi na Waamlisi waliuawa kando ya mto wa Sidoni na kutupwa katika [a]mto wa Sidoni; na tazama mifupa yao iko katika kilindi cha [b]bahari, na ni mingi.

4 Na [a]Waamlisi walitambulika kutoka kwa Wanefi, kwani walikuwa wamejiweka [b]alama nyekundu katika vipaji vyao kwa kuiga Walamani; walakini hawakuwa wamenyoa vichwa vyao kama Walamani.

5 Sasa vichwa vya Walamani vilikuwa vimenyolewa; na walikuwa [a]uchi, ila tu ngozi ambayo walikuwa wamejifunga viunoni mwao, na pia silaha zao, ambazo walikuwa wamejizungushia, na pinde zao, na mishale yao, na mawe yao, na kombeo zao, na kadhalika.

6 Na ngozi ya Walamani ilikuwa nyeusi, kulingana na alama iliyowekwa juu ya babu zao, ambayo ilikuwa ni [a]laana juu yao kwa sababu ya makosa yao na maasi yao dhidi ya kaka zao, ambao walikuwa ni Nefi, Yakobo, na Yusufu, na Samu, ambao walikuwa ni watu waadilifu na watakatifu.

7 Na kaka zao walitazamia kuwaua, kwa hivyo walilaaniwa; na Bwana Mungu akawaweka [a]alama, ndiyo, juu ya Lamani na Lemueli, na pia wana wa Ishmaeli, na wanawake wa Kiishmaeli.

8 Na hii ilifanywa ili uzao wao uweze kutambulika kutokana na uzao wa ndugu zao, ili Bwana Mungu angewahifadhi watu wake, kwamba [a]wasichanganyike na kuamini [b]mila zisizokuwa halali na ambazo zingewaangamiza.

9 Na ikawa kwamba yeyote aliyechanganya uzao wake na Walamani aliuteremshia uzao wake laana ile.

10 Kwa hivyo, yeyote aliyekubali kupotoshwa na Walamani alijulikana kwa jina lile, na alama iliwekwa juu yake.

11 Na ikawa kwamba yeyote ambaye hakuamini [a]mila za Walamani, lakini aliamini maandishi yale ambayo yalitolewa kutoka nchi ya Yerusalemu, na pia mila za babu zao, ambazo zilikuwa halali, na ambao waliziamini amri za Mungu na kuzitii, waliitwa Wanefi, au watu wa Nefi, tangu wakati ule na kuendelea—

12 Na ni wao ambao wamehifadhi maandishi ya watu wao ambayo ni ya [a]kweli, na pia ya watu wa Walamani.

13 Sasa tutarudi tena kwa Waamlisi, kwani nao pia walikuwa na alama juu yao; ndiyo,

3 *a* Alma 2:15.
b Alma 44:22.
4 *a* Alma 2:11.
b Alma 3:13–19.
5 *a* Eno. 1:20; Mos. 10:8; Alma 42:18–21.
6 *a* 2 Ne. 5:21; 26:33. MWM Laani, Laana.
7 *a* 1 Ne. 12:23.
8 *a* MWM Ndoa, Oa, Olewa—Ndoa ya imani mbili.
b Mos. 10:11–18; Alma 9:16.
11 *a* Alma 17:9–11.
12 *a* Mos. 1:6; Eth. 4:6–11.

walijiweka [a]alama wao wenyewe, ndiyo, hata alama nyekundu katika vipaji vyao.

14 Na hivyo neno la Mungu limetimizwa, kwani haya ndiyo maneno ambayo alimwambia Nefi: Tazama, nimewalaani Walamani, na nitawaweka alama juu yao ili wao na uzao wao watengwe kutoka kwako na uzao wako, tangu sasa hadi milele, isipokuwa watubu uovu wao na [a]wanirudie ili niwarehemu.

15 Na tena: Nitamweka alama yeyote atakayechanganya uzao wake na wa ndugu yako, ili nao pia walaaniwe.

16 Na tena: Nitaweka alama kwa yeyote atakayepigana na wewe na uzao wako.

17 Na tena, ninasema kwamba yeyote atakayekutoroka hatakuwa tena uzao wako; na nitakubariki, pamoja na yeyote atakayeitwa uzao wako, tangu sasa hadi milele; na hizi ndizo zilizokuwa ahadi za Bwana kwa Nefi na uzao wake.

18 Sasa Waamlisi hawakujua kwamba walikuwa wakitimiza maneno ya Mungu walipoanza kujiweka alama katika vipaji vyao; hata hivyo walikuwa [a]wamemwasi Mungu waziwazi; kwa hivyo ililazimika kwamba laana iwateremkie.

19 Sasa ningetaka mjue kwamba walijiletea [a]laana wao wenyewe; na hata hivyo kila mtu anayelaaniwa hujiletea laana yake mwenyewe.

20 Na sasa ikawa kwamba baada ya siku chache tangu vita vilivyokuwa katika nchi ya Zarahemla, na Walamani na Waamlisi, kwamba jeshi lingine la Walamani liliwashambulia watu wa Nefi, katika mahali [a]pale ambapo jeshi la kwanza lilikutana na Waamlisi.

21 Na ikawa kwamba kulikuwa na jeshi ambalo lilitumwa kuwakimbiza kutoka nchi yao.

22 Sasa Alma mwenyewe akiwa [a]amejeruhiwa hakwenda wakati huu kupigana na Walamani;

23 Lakini alituma jeshi kubwa dhidi yao; na walienda na kuwaua Walamani wengi, na kuwafukuza waliobaki kutoka mipaka ya nchi yao.

24 Na kisha wakarudi tena na kuanza kuimarisha amani katika nchi, bila kusumbuliwa tena kwa muda na maadui wao.

25 Sasa hivi vitu vyote vilifanywa, ndiyo, vita hivi vyote na mabishano yalianza na kukoma katika mwaka wa tano wa utawala wa waamuzi.

26 Na katika mwaka mmoja, kumi ya maelfu ya nafsi zilitumwa katika ulimwengu wa milele, kwamba wavune [a]zawadi zao kulingana na kazi zao, kama zilikuwa njema au kama zilikuwa mbaya, kuvuna furaha ya milele au huzuni ya milele, kulingana na roho ambayo walichagua kutii, kama ni roho nzuri au mbaya.

13*a* Alma 3:4.
14*a* 2 Ne. 30:4–6.
18*a* 4 Ne. 1:38.
MWM Uasi.
19*a* 2 Ne. 5:21–25; Alma 17:15.
20*a* Alma 2:24.
22*a* Alma 2:29–33.
26*a* MWM Matendo.

27 Kwani kila mtu hupokea [a]mshahara kutoka kwa yule anayemchagua [b]kutii, na haya ni kulingana na maneno ya roho ya unabii; kwa hivyo hebu na iwe kulingana na ukweli. Na hivyo ukaisha mwaka wa tano wa utawala wa waamuzi.

MLANGO WA 4

Alma anabatiza maelfu ya waumini—Uovu unaingia kanisani, na maendeleo ya Kanisa yanacheleweshwa—Nefiha anachaguliwa kuwa mwamuzi mkuu—Alma, kama kuhani mkuu, anajitolea kwa huduma. Karibia mwaka 86–83 K.K.

Sasa ikawa kwamba katika mwaka wa sita wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, hakukuwa na mabishano wala vita katika [a]nchi ya Zarahemla;

2 Lakini watu walisumbuliwa, ndiyo, walisumbuliwa sana kwa [a]kupoteza ndugu zao, na pia hasara ya mifugo yao na wanyama wao, na pia hasara ya mashamba yao ya nafaka, ambayo ilikanyagwa kwa miguu na kuangamizwa na Walamani.

3 Na masumbuko yao yalikuwa makuu sana hata kwamba kila nafsi ilisababishwa kuomboleza; na waliamini kwamba ilikuwa ni hukumu ya Mungu juu yao kwa sababu ya uovu wao na machukizo yao; kwa hivyo walikumbushwa jukumu lao.

4 Na wakaanza kuimarisha sana kanisa; ndiyo, na wengi [a]walibatizwa katika maji ya Sidoni na wakaunganishwa kwa kanisa la Mungu; ndiyo, walibatizwa kwa mkono wa Alma, ambaye alikuwa ametengwa kuwa [b]kuhani mkuu juu ya watu wa kanisa, kwa mkono wa baba yake Alma.

5 Na ikawa kwamba katika mwaka wa saba wa utawala wa waamuzi nafsi elfu tatu na mia tano zilijiunga na [a]kanisa la Mungu na kubatizwa. Na hivyo mwaka wa saba wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi uliisha; na kulikuwa na amani daima kwa wakati huo wote.

6 Na ikawa kwamba katika mwaka wa nane wa utawala wa waamuzi, kwamba watu wa kanisa walianza kupata kiburi, kwa sababu ya [a]utajiri wao wa [b]kupita kiasi, na hariri zao za kuvutia, na vitani vyao vilivyovutia, na kwa sababu ya mifugo yao na wanyama wao wengi, na dhahabu yao na fedha yao, na kila aina ya vitu vya thamani, ambavyo walikuwa wamepata kwa sababu ya bidii yao; na katika vitu hivi vyote walijivuna kwa macho yao, kwani walianza kuvaa mavazi ya bei ghali.

7 Sasa hii ilimsumbua Alma

27 *a* Mos. 2:31–33; Alma 5:41–42.
b Rum. 6:16; Hel. 14:29–31.
MWM Mtiifu, Tii, Utii.

4 1 *a* Omni 1:12–19.
2 *a* Alma 2:19; 3:1–2, 26.
4 *a* Mos. 18:10–17.
b Mos. 29:42.
5 *a* Mos. 25:18–23; 3 Ne. 26:21.
6 *a* MWM Ukwasi.
b Alma 1:29.

sana, ndiyo, na pia watu wengi ambao Alma alikuwa [a]amewatenga wawe walimu, na makuhani, na wazee wa kanisa; ndiyo, wengi wao walianza kuhuzunishwa na uovu ambao waliona umeanza kuwa miongoni mwa watu wao.

8 Kwani waliona na wakahuzunika sana kwamba watu wa kanisa walianza kujiinua kwa [a]kiburi machoni mwao, na kuweka mioyo yao katika utajiri na vitu vya ulimwengu visivyofaidisha, kwamba walianza kufanyiana madharau, wao kwa wao, na wakaanza kuwatesa wale ambao [b]hawakuamini kulingana na nia yao na mapenzi yao.

9 Na hivyo, katika mwaka huu wa nane wa utawala wa waamuzi, kulianza kuwa na [a]mabishano mengi miongoni mwa watu wa kanisa; ndiyo, kulikuwa na [b]wivu, na mzozo, na chuki, na mateso, na kiburi, hata kuzidi kiburi cha wale ambao hawakuwa washiriki wa kanisa la Mungu.

10 Na hivyo mwaka wa nane wa utawala wa waamuzi ulikwisha; na uovu wa kanisa ulikuwa ni kikwazo kikuu kwa wale ambao hawakuwa washiriki wa kanisa; na hivyo kanisa likaanza kukosa kuendelea.

11 Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa tisa, Alma aliona uovu wa kanisa, na pia akaona kwamba [a]mfano wa kanisa ulianza kuwaongoza wale wasioamini kutoka uovu mmoja hadi mwingine, hivyo kuwaletea watu maangamizo.

12 Ndiyo, aliona ukosefu wa usawa miongoni mwa watu, wengine wakijiinua juu kwa kiburi chao, wakidharau wengine, wakikataa kuwasaidia wale ambao walikuwa na [a]shida na walio uchi na wale ambao walikuwa na [b]njaa, na wale ambao walikuwa na kiu, na wale ambao walikuwa wagonjwa na waliosumbuka.

13 Sasa hii ilikuwa ni sababu kuu ya maombolezi miongoni mwa watu, wakati wengine walikuwa wanajinyenyekeza, wakiwasaidia wale ambao walihitaji msaada, kama vile [a]kupeana mali yao kwa wale ambao walikuwa masikini na wenye shida, wakiwalisha wenye njaa, na kuteseka kwa kila aina ya [b]masumbuko, kwa [c]sababu ya Kristo, ambaye angekuja kulingana na roho ya unabii;

14 Wakitazamia mbele kwenye siku ile, na hivyo [a]wakidumisha msamaha wa dhambi zao; wakijazwa na [b]shangwe kuu kwa sababu ya ufufuo wa wafu, kulingana na nia na uwezo na ukombozi wa Yesu Kristo kutoka kamba za kifo.

7 *a* MWM Mamlaka.
8 *a* MWM Kiburi; Majivuno, Siofaa.
b Alma 1:21.
9 *a* MWM Ushindani.
b MWM Husuda.
11 *a* 2 Sam. 12:14; Alma 39:11.
12 *a* Isa. 3:14; Yak. (KM) 2:17.
b Mos. 4:26.
13 *a* MWM Sadaka, Utoaji sadaka.
b MWM Shida.
c 2 Kor. 12:10.
14 *a* Mos. 4:12; Alma 5:26–35. MWM Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki.
b MWM Shangwe.

15 Na sasa ikawa kwamba Alma, baada ya kuona masumbuko ya wafuasi wanyenyekevu wa Mungu, na mateso ambayo walibandikwa na watu wake waliobaki, na kuona ukosefu wa [a]usawa wao wote, alianza kuhuzunika sana; walakini Roho wa Bwana hakumwacha.

16 Na akamchagua mtu mwenye hekima miongoni mwa wazee wa kanisa, na akampatia nguvu kulingana na [a]kura ya watu, kwamba apate uwezo wa kuandika [b]sheria kulingana na sheria ambazo zilikuwa zimetolewa, na kuzitekeleza kulingana na uovu na uhalifu wa watu.

17 Sasa jina la mtu huyu lilikuwa Nefiha, na alichaguliwa kuwa [a]mwamuzi mkuu; na alikaa katika kiti cha hukumu na kuwahukumu na kuwatawala watu.

18 Sasa Alma hakumkabidhi ofisi ya kuhani mkuu wa kanisa, lakini alijihifadhia ofisi ya kuhani mkuu; lakini akamkabidhi Nefiha kiti cha hukumu.

19 Na hii alifanya ili yeye [a]mwenyewe aende miongoni mwa watu wake, au watu wa Nefi, kwamba awahubirie [b]neno la Mungu, [c]kuwasisimua [d]wakumbuke wajibu wao, na kwamba ashushe chini, kwa neno la Mungu, kiburi chao chote na ujanja na mabishano yaliyokuwa miongoni mwa watu wake, kwani hakuona njia nyingine ya kuwaokoa watu wake isipokuwa kwa kuwashawishi [e]ushuhuda halisi.

20 Na hivyo katika mwanzo wa mwaka wa tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, Alma alimkabidhi [a]Nefiha kiti cha hukumu, na akajitolea mwenyewe kabisa kwa ule [b]ukuhani mkuu ulio mpango mtakatifu wa Mungu, kwa ushuhuda wa neno, kulingana na roho ya ufunuo na unabii.

Maneno ambayo Alma, Kuhani Mkuu kulingana na mpango mtakatifu wa Mungu, aliwatolea watu katika miji yao na vijiji vyao kote katika nchi.

Kuanzia mlango wa 5.

MLANGO WA 5

Kupata wokovu, lazima wanadamu watubu na kushika amri, wazaliwe tena, waoshe mavazi yao kwa damu ya Kristo, wawe wanyeyekevu na wajivue kiburi na wivu, na watende vitendo vya haki—Mchungaji Mwema huwaita watu Wake—Wale ambao wanafanya vitendo viovu ni watoto wa ibilisi—Alma anashuhudia kuhusu ukweli wa mafundisho yake na kuwaamuru watu kutubu—Majina ya wale wenye haki yataandikwa katika kitabu cha uzima. Karibia mwaka 83 K.K.

15 *a* M&M 38:27; 49:20.
16 *a* Alma 2:3–7.
b Alma 1:1, 14, 18.
17 *a* Alma 50:37.
19 *a* Alma 7:1.
b Alma 31:5; M&M 11:21–22.
c Eno. 1:23.
d Mos. 1:17; Hel. 12:3.
e MWM Ushuhuda.
20 *a* Alma 8:12.
b Mos. 29:42; Alma 5:3, 44, 49.

Sasa ikawa kwamba Alma alianza [a]kuwatolea watu neno la [b]Mungu, kuanzia katika nchi ya Zarahemla, na kuenea kote katika nchi.

2 Na haya ndiyo maneno aliyowaelezea watu katika kanisa lililokuwa limeanzishwa katika nchi ya Zarahemla, kulingana na maandishi yake mwenyewe, akisema:

3 Mimi, Alma, baada ya kuwekwa [a]wakfu na baba yangu, Alma, kuwa [b]kuhani mkuu wa kanisa la Mungu, yeye akiwa na uwezo na [c]mamlaka kutoka kwa Mungu ya kutenda vitu hivi, tazama, ninawaambia kwamba alianza kuimarisha kanisa katika [d]nchi ambayo ilikuwa mipakani mwa Nefi; ndiyo, nchi ambayo iliitwa nchi ya Mormoni; ndiyo, na alibatiza ndugu zake katika maji ya Mormoni.

4 Na tazama, ninawaambia, [a]walikombolewa kutoka mikono mwa mfalme Nuhu, kwa rehema na uwezo wa Mungu.

5 Na tazama, baadaye, walitiwa [a]utumwani na mikono ya Walamani huko nyikani; ndiyo, ninawaambia, walikuwa katika utumwa, na tena Bwana [b]aliwakomboa kutoka utumwani kwa uwezo wa neno lake; na tukaletwa katika nchi hii, na hapa tulianza kuimarisha kanisa la Mungu kote katika nchi hii pia.

6 Na sasa tazama, ninawaambia, ndugu zangu, ninyi ambao ni washiriki wa kanisa hili, je, mngali mnakumbuka ya kutosha utumwa wa babu zenu? Ndiyo, na bado mngali mnakumbuka ya kutosha rehema zake na uvumilivu wake kwao? Na zaidi, je, mngali mnakumbuka ya kutosha kwamba amezikomboa nafsi zao kutoka jehanamu?

7 Tazama, alibadilisha mioyo yao; ndiyo, aliwaamsha kutoka usingizi mzito, na wakaamka katika Mungu. Tazama, walikuwa katikati ya giza; walakini, nafsi zao ziliangazwa na nuru ya neno lisilo na mwisho; ndiyo, walizingirwa na [a]kamba za kifo; na [b]minyororo ya jehanamu, na maangamizo yasiyo na mwisho yaliwangojea.

8 Na sasa ninawauliza, ndugu zangu, je, waliangamizwa? Tazama, ninawaambia, hapana, hawakuangamizwa.

9 Na tena ninauliza, kamba za kifo zilikatwa, na minyororo ya jehanamu ambayo iliwazingira, je, ilifunguliwa? Ninawaambia, Ndiyo, ilifunguliwa, na nafsi zao zikapanuka, na wakaimba upendo unaokomboa. Na ninawaambia kwamba wameokolewa.

10 Na sasa ninawauliza ni kwa masharti gani [a]wanayookolewa? Ndiyo, ni masharti gani waliyokuwa nayo kutumaini wokovu? Ni sababu gani ya

5 1*a* Alma 4:19.
b Alma 5:61.
3*a* MWM Kutawaza, Kutawazwa.
b Alma 4:4, 18, 20.
c Mos. 18:13; 3 Ne. 11:25.
d Mos. 18:4; 3 Ne. 5:12.
4*a* Mos. 23:1–3.
5*a* Mos. 23:37–39; 24:8–15.
b Mos. 24:17.
7*a* Mos. 15:8.
b Alma 12:11; M&M 138:23.
10*a* MWM Mpango wa Ukombozi; Wokovu.

wao kufanywa huru kutokana na kamba za kifo, ndiyo, na pia minyororo ya jehanamu?

11 Tazama, ninaweza kuwaambia—si baba yangu Alma aliamini maneno ambayo yalizungumzwa kwa kinywa cha [a]Abinadi? Na si yeye alikuwa nabii mtakatifu? Si yeye alizungumza maneno ya Mungu, na baba yangu Alma kuyaamini?

12 Na kulingana na imani yake [a]badiliko kuu likafanyika katika moyo wake. Tazama ninawaambia kwamba haya yote ni ukweli.

13 Na tazama, [a]aliwahubiria babu zenu neno, na mabadiliko makuu yakafanyika katika mioyo yao, na wakajinyenyekeza na kuweka [b]tumaini lao katika Mungu wa kweli na [c]anayeishi. Na tazama, walikuwa waaminifu hadi [d]mwisho; kwa hivyo waliokolewa.

14 Na sasa tazama, ninawauliza, ndugu zangu wa kanisa, je, [a]mmezaliwa kiroho katika Mungu? Mmepokea mfano wake katika nyuso zenu? Mmeshuhudia [b]mabadiliko haya makuu katika mioyo yenu?

15 Mnaweka imani yenu ya ukombozi kwa yule [a]aliyewaumba? Mnatazamia mbele kwa macho ya imani na kuona mwili huu wenye kufa ukifufuliwa katika kutokufa, na uharibifu huu [b]ukiinuliwa katika kutoharibika, kusimama mbele ya Mungu [c]kuhukumiwa kulingana na vitendo ambavyo vilitendwa katika miili inayokufa?

16 Ninawaambia, mnaweza kuwaza kwamba mnasikia sauti ya Bwana, siku ile, ikiwaambia: Njooni kwangu [a]mliobarikiwa, kwani tazameni, kazi zenu zimekuwa kazi za haki usoni mwa dunia?

17 Au mnawaza kwenu ninyi kwamba mtamdanganya Bwana katika siku ile, na [a]kusema—Bwana, kazi zetu zimekuwa kazi za haki usoni mwa dunia—na kwamba atawaokoa?

18 Au kwa vingine, mnaweza kuwaza ninyi wenyewe kwamba mmeletwa mbele ya baraza la hukumu ya Mungu na nafsi zenu zimejaa hatia na majuto, [a]mkikumbuka hatia zenu zote, ndiyo, ukumbusho ulio kamili wa maovu yenu yote, ndiyo, ukumbusho kwamba mliziasi amri za Mungu?

19 Ninawaambia, mnaweza kumtazama Mungu siku ile kwa moyo safi na mikono safi? Ninawaambia, mnaweza kutazama juu, mkiwa na [a]mfano wa Mungu umechorwa katika nyuso zenu?

20 Ninawaambia, mnaweza

11 *a* Mos. 17:1–4.
12 *a* MWM Mwongofu, Uongofu.
13 *a* Mos. 18:7.
b MWM Tegemea.
c Morm. 9:28; M&M 20:19.
d MWM Stahimili.
14 *a* Mos. 27:24–27; Alma 22:15.
MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
b Rum. 8:11–17; Mos. 5:2; Musa 6:65.
MWM Mwongofu, Uongofu.
15 *a* MWM Umba, Uumbaji.
b MWM Ufufuko.
c MWM Hukumu ya mwisho.
16 *a* Mt. 25:31–46.
17 *a* 3 Ne. 14:21–23.
18 *a* Eze. 20:43; 2 Ne. 9:14; Mos. 3:25; Alma 11:43.
19 *a* 1 Yoh. 3:1–3.

kutumaini wokovu baada ya kujitolea kuwa [a]wafuasi wa ibilisi?

21 Ninawaambia, mtajua katika siku ile kwamba hamwezi [a]kuokolewa; kwani mwanadamu yeyote hawezi kuokolewa bila [b]mavazi yake kuoshwa na kuwa meupe; ndiyo, lazima mavazi yake [c]yatakaswe hadi yaoshwe kutokana na mawaa yote, kwa kupitia damu ya yule ambaye alizungumziwa na babu zetu, ambaye atakuja kuwakomboa watu wake kutoka dhambi zao.

22 Na sasa ninawauliza, ndugu zangu, mtahisi vipi, kama mtasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, mavazi yenu yakiwa yamechafuliwa na [a]damu na kila aina ya [b]uchafu? Tazama, vitu hivi vitashuhudia nini dhidi yenu?

23 Tazama si [a]yatawashuhudia kwamba ninyi ni wauaji, ndiyo, na pia kwamba ninyi mna hatia kwa sababu ya uovu wa kila namna?

24 Tazama, ndugu zangu, mnadhani kwamba kama huyo atapata nafasi ya kuketi chini katika ufalme wa Mungu, pamoja na [a]Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, na pia manabii wote watakatifu, ambao mavazi yao yameoshwa, na hayana doa, safi na meupe?

25 Ninawaambia, Hapana; isipokuwa mumfanye Muumba wetu mwongo tangu mwanzo, au mdhani kwamba yeye ni mwongo tangu mwanzo, hamwezi kudhani kwamba kama huyo anaweza kupata nafasi katika ufalme wa mbinguni; lakini watatupwa nje kwa sababu wao ni [a]watoto wa ufalme wa ibilisi.

26 Na sasa tazama, ninawambia, ndugu zangu, ikiwa mmepata [a]mabadiliko ya moyo, na ikiwa mmesikia kuimba [b]wimbo wa upendo wa ukombozi, ningeuliza, [c]mnaweza kuhisi hivyo sasa?

27 Mmetembea, na mkijiweka bila [a]lawama mbele ya Mungu? Mngeweza kusema, kama mngetakiwa kufa wakati huu, ndani mioyo yenu, kwamba mlikuwa [b]wanyenyekevu wa kutosha? Kwamba mavazi yenu yameoshwa na kufanywa meupe kwa damu ya Kristo, ambaye atakuja [c]kuwakomboa watu wake kutoka dhambi zao?

28 Tazama, mmevuliwa [a]kiburi? Ninawaambia, kama bado, hamko tayari kukutana na Mungu. Tazama lazima mjitayarishe haraka; kwani ufalme wa mbinguni u karibu, na kama huyu hana uzima wa milele.

29 Tazama, nawaambia, kuna

20 *a* Mos. 2:32.
21 *a* MWM Wokovu.
b 1 Ne. 12:10; Alma 13:11–13; 3 Ne. 27:19–20.
c MWM Safi na Isiyo safi.
22 *a* Isa. 59:3.
b MWM Chafu, Uchafu.
23 *a* Isa. 59:12.
24 *a* Lk. 13:28.
25 *a* 2 Ne. 9:9.
26 *a* MWM Mwongofu, Uongofu.
b Alma 26:13.
c Mos. 4:12; M&M 20:31–34.
27 *a* MWM Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki.
b MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
c MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
28 *a* MWM Kiburi.

yeyote miongoni mwenu ambaye hajavuliwa [a]wivu? Ninawaambia kwamba huyu hayuko tayari; na ningetaka kwamba ajitayarishe haraka, kwani wakati u karibu, na hajui ni wakati gani utakapofika; kwani kama huyo hatakosa hatia.

30 Na tena ninawauliza, kuna yeyote miongoni mwenu ambaye humfanyia ndugu yake [a]mzaha, au yule ambaye anambandika mateso?

31 Ole kwa huyo, kwani hayuko tayari, na wakati u karibu ambao lazima atubu au hawezi kuokolewa!

32 Ndiyo, hata ole ninyi [a]watendaji wote wa uovu; tubuni, tubuni, kwani Bwana Mungu ameizungumza!

33 Tazama, yeye huwatumia wanadamu [a]wote mwaliko, kwani [b]mikono ya huruma imenyoshwa kwao, na anasema: Tubuni, na nitawapokea.

34 Ndiyo, anasema: [a]Njooni kwangu na mtakula [b]matunda ya mti wa uzima; ndiyo, mtakula na kunywa [c]mkate na maji ya uhai [d]bure;

35 Ndiyo, njooni kwangu na mlete kazi za haki, na hamtakatwa na kutupwa motoni—

36 Kwani tazama, wakati uko mkononi ambao yeyote ambaye [a]haleti matunda mema, au yeyote ambaye hatendi kazi za haki, huyo ana sababu ya kulia na kuomboleza.

37 Ee ninyi watendaji wa uovu; ninyi ambao mmejazwa na vitu vya ulimwengu [a]visivyo na maana, ninyi ambao mnakiri kwamba mnajua njia za haki walakini [b]mmepotea, kama [c]kondoo ambao hawana mchungaji, ingawa mchungaji [d]aliwaita na angali anawaita, lakini [e]hamtasikia sauti yake!

38 Tazama, ninawaambia, kwamba [a]mchungaji mwema anawaita, ndiyo, na kwa jina lake mwenyewe anawaita, ambalo ni jina la Kristo; na kama [b]hamtasikia sauti ya [c]mchungaji mwema, kwa [d]jina ambalo mnaitwa nalo, tazama, ninyi sio kondoo wa mchungaji mwema.

39 Na sasa kama ninyi sio kondoo wa mchungaji mwema, ninyi ni wa [a]zizi gani? Tazama, nawaambia, kwamba [b]ibilisi ndiye mchungaji wenu, na ninyi ni wa zizi lake; na sasa, nani ambaye anaweza kukana haya? Tazama, nawaambia, yeyote

29 *a* MWM Husuda.
30 *a* MWM Kusema uovu.
32 *a* Zab. 5:5.
33 *a* Alma 19:36; 3 Ne. 18:25.
b Yak. (KM) 6:5; 3 Ne. 9:14.
34 *a* 2 Ne. 26:24–28; 3 Ne. 9:13–14.
b 1 Ne. 8:11; 15:36.
c MWM Mkate wa Uzima.
d 2 Ne. 9:50–51; Alma 42:27.
36 *a* Mt. 3:10; 7:15–20; 3 Ne. 14:19; M&M 97:7.
37 *a* MWM Majivuno, Siofaa.
b 2 Ne. 12:5; 28:14; Mos. 14:6.
c Mt. 9:36.
d Mit. 1:24–27; Isa. 65:12.
e Yer. 26:4–5; Alma 10:6.
38 *a* MWM Mchungaji Mwema.
b Law. 26:14–20; M&M 101:7.
c 3 Ne. 15:24; 18:31.
d Mos. 5:8; Alma 34:38.
39 *a* Mt. 6:24; Lk. 16:13.
b Mos. 5:10. MWM Ibilisi.

ambaye anakana haya ni [c]mwongo na ni [d]mtoto wa ibilisi.

40 Kwani ninawaambia kwamba chochote ambacho ni [a]kizuri kinatoka kwa Mungu, na chochote ambacho ni kiovu kinatoka kwa ibilisi.

41 Kwa hivyo, kama mtu anatenda [a]kazi njema yeye husikiliza sauti ya mchungaji mwema, na humfuata; lakini yeyote ambaye anatenda kazi mbovu, huyo huwa [b]mtoto wa ibilisi, kwani husikiliza sauti yake, na kumfuata.

42 Na yeyote ambaye anatenda haya lazima apokee [a]mshahara wake kwake; kwa hivyo, kwa [b]mshahara wake hupokea [c]mauti, kulingana na vitu vya haki, kwani huwa amekufa kwa kazi zote nzuri.

43 Na sasa, ndugu zangu, ningetaka kwamba mnisikize, kwani ninazungumza na nguvu za nafsi yangu; kwani tazama, nimewazungumzia waziwazi ili msikosee, au nimenena kulingana na amri za Mungu.

44 Kwani nimeitwa kunena jinsi hii, kulingana na [a]mpango mtakatifu wa Mungu, ambao umo katika Kristo Yesu; ndiyo, nimeamriwa nisimame na kushuhudia kwa watu hawa vitu ambavyo vilisemwa na babu zetu kuhusu vitu vitakavyokuja.

45 Na hii sio yote. Hamfikirii kwamba mimi mwenyewe [a]najua vitu hivi? Tazama, nawashuhudia kwamba mimi najua kuwa vitu hivi ambavyo nimezungumza ni vya kweli. Na mnadhaniaje kwamba ninajua ukweli wao?

46 Tazama, ninawaambia kwamba yamesababishwa [a]kujulikana kwangu na Roho Mtakatifu wa Mungu. Tazama, [b]nimefunga na kusali siku nyingi ili nivijue vitu hivi mimi mwenyewe. Na sasa ninavijua mwenyewe kuwa ni vya kweli; kwani Bwana Mungu amevidhihirisha kwangu kwa Roho wake Mtakatifu; na hii ni roho ya [c]ufunuo ambayo iko ndani yangu.

47 Na zaidi, ninawaambia kwamba imefunuliwa kwangu, kwamba maneno ambayo yalizungumzwa na babu zetu ni ya kweli, hata hivyo kulingana na roho ya unabii iliyo ndani yangu, ambayo pia ni dhihirisho la Roho wa Mungu.

48 Ninawaambia, kwamba ninajua mwenyewe ya kuwa lolote nitakalowaambia, kuhusu yale ambayo yatakayokuja, ni ya kweli; na ninawaambia, kwamba ninajua kuwa Yesu Kristo atakuja, ndiyo, Mzaliwa Pekee wa Baba, amejaa neema, na rehema, na ukweli. Na tazama, ni yeye ambaye anakuja kuondoa dhambi za ulimwengu, ndiyo, dhambi za kila mtu ambaye daima analiamini jina lake.

39 *c* 1 Yoh. 2:22.
d 2 Ne. 9:9.
40 *a* Omni 1:25; Eth. 4:12; Moro. 7:12, 15–17.
41 *a* 3 Ne. 14:16–20. MWM Matendo.
b Mos. 16:3–5; Alma 11:23.
42 *a* Alma 3:26–27; M&M 29:45.
b Rum. 6:23.
c Hel. 14:16–18. MWM Mauti ya Kiroho.
44 *a* Alma 13:6.
45 *a* MWM Ushuhuda.
46 *a* 1 Kor. 2:9–16.
b MWM Funga, Kufunga.
c MWM Ufunuo.

49 Na sasa ninawaambia kwamba huu ndiyo [a]mpango ambao nimeitiwa, ndiyo, kuwahubiria ndugu zangu wapendwa, ndiyo, na kila mmoja ambaye anaishi katika nchi; ndiyo, kuwahubiri kwa wote, wazee na vijana, wafungwa na walio huru; ndiyo, ninawaambia mliozeeka, na pia wenye umri wa kiasi, na kizazi kinachoinukia; ndiyo, kuwaambia kwamba lazima watubu na [b]kuzaliwa tena.

50 Ndiyo, hivyo ndivyo asemavyo Roho: Tubuni, ninyi kote ulimwenguni, kwani ufalme wa mbinguni umo mkononi; ndiyo, Mwana wa Mungu anakuja katika [a]utukufu wake mkuu, kwa nguvu zake, fahari, uwezo, na utawala. Ndiyo, ndugu zangu wapendwa, ninawaambia, kwamba Roho anasema: Tazama utukufu wa [b]Mfalme wa ulimwengu wote; na pia Mfalme wa mbinguni hivi karibuni utametameta miongoni mwa wanadamu.

51 Na pia Roho inaniambia, ndiyo, alipaaza sauti kwangu na kwa sauti kuu, ikisema: Nenda na uwaambie watu hawa—Tubuni, kwani msipotubu hamwezi kurithi kwa vyovyote ufalme wa [a]mbinguni.

52 Na tena ninawaambia, Roho inasema: Tazama, [a]shoka limewekwa kwenye mzizi wa mti; kwa hivyo kila mti ambao hauzai matunda mema [b]utakatwa na kutupwa katika moto, ndiyo, moto ambao hauwezi kuisha, hata moto usiozimika. Tazama, na mkumbuke, Yule Mtakatifu ameisema.

53 Na sasa ndugu zangu wapendwa, ninawaambia, mnaweza kuvumilia misemo hii; ndiyo, mnaweza kuweka vitu hivi kando, na [a]mumkanyage Yule Mtakatifu miguuni mwenu; ndiyo, mnaweza kujazwa na [b]kiburi cha mioyo yenu; ndiyo, mtaendelea kuvaa mavazi ya [c]bei na kuiweka mioyo yenu katika vitu vya ulimwengu visivyo na busara, na [d]utajiri wenu?

54 Ndiyo, mtaendelea kujidhania kwamba ninyi ni bora zaidi ya wengine; ndiyo, mtaendelea kuwatesa ndugu zenu, ambao ni wanyenyekevu na hufuata mpango mtakatifu wa Mungu, ambao umewaleta katika kanisa hili, [a]wakishatakaswa na Roho Mtakatifu, na hutenda kazi njema ya toba—

55 Ndiyo, na mtaendelea kuwageukia wale ambao ni [a]masikini, na wenye shida, na kuzuia misaada yenu kwao?

49*a* MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito; Ukuhani.
b MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
50*a* MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo; Utukufu.
b Zab. 24; Mt. 2:2; Lk. 23:2; 2 Ne. 10:14; M&M 38:21–22; 128:22–23; Musa 7:53. MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni; Yesu Kristo.
51*a* MWM Mbinguni.
52*a* Lk. 3:9; M&M 97:7.
b Yak. (KM) 5:46; 6:7; 3 Ne. 27:11–12.
53*a* 1 Ne. 19:7.
b MWM Kiburi.
c 2 Ne. 28:11–14; Morm. 8:36–39.
d Zab. 62:10; M&M 56:16–18.
54*a* MWM Utakaso.
55*a* Zab. 109:15–16; Yak. (KM) 2:17; Hel. 6:39–40.

56 Na mwishowe, nyote ambao mnaendelea katika uovu wenu, ninawaambia kwamba hawa ndiyo wale ambao watakatwa na kutupwa motoni wasipotubu kwa haraka.

57 Na sasa ninawaambia, nyote ambao mnatamani kufuata sauti ya [a]mchungaji mwema, ondokeni kutoka kwa waovu, na [b]mjitenge, na msiguse vitu vyao vichafu; na tazama, majina yao [c]yatafutwa, kwamba majina ya waovu hayatahesabiwa miongoni mwa majina ya wale wenye haki, ili neno la Mungu litimizwe, ambalo linasema: Majina ya waovu hayatachanganywa na majina ya watu wangu;

58 Kwani majina ya wale wenye haki yataandikwa katika [a]kitabu cha uzima, na kwao nitawapatia urithi katika mkono wangu wa kulia. Na sasa, ndugu zangu, nini mtakachosema kinyume cha hivi? Ninawaambia, mkizungumza kinyume cha hivi, haijalishi, kwani lazima neno la Mungu litimizwe.

59 Kwani ni mchungaji gani miongoni mwenu ambaye ana kondoo wengi na hawachungi, ili mbwa mwitu wasiingie na kuwararua mifugo yake? Na tazama, kama mbwa mwitu anashambulia mifugo yake hamfukuzi nje? Ndiyo, na mwishowe, akiweza, atamwangamiza.

60 Na sasa ninawaambia kwamba mchungaji mwema anawaita; na ikiwa mtaisikiliza sauti yake atawaleta katika zizi lake, na ninyi ni kondoo wake; na anawaamuru kwamba msikubali mbwa mwitu aliye na njaa aingie miongoni mwenu, ili msiangamizwe.

61 Na sasa mimi, Alma, ninawaamuru ninyi kwa lugha ya [a]yule ambaye ameniamuru, kwamba mtie bidii katika kutii maneno ambayo nimewazungumzia.

62 Nazungumza kwa njia ya amri kwenu ambao mnashiriki katika kanisa; na kwa wale wasio washiriki wa kanisa nawazungumzia kwa njia ya kuwaalika, na kusema: Njooni na mpate kubatizwa ubatizo wa toba, ili pia nanyi mshiriki katika kula tunda la [a]mti wa uzima.

MLANGO WA 6

Kanisa katika Zarahemla linatakaswa na kupangwa—Alma anaenda Gideoni ili ahubiri. Karibia mwaka 83 K.K.

Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kumaliza kuwazungumzia watu wa kanisa, ambalo lilikuwa limeanzishwa katika mji wa Zarahemla, [a]aliwatawaza makuhani na [b]wazee, kwa kuwawekea [c]mikono kulingana na mpango wa Mungu, kusimamia na [d]kuchunga kanisa.

57 *a* MWM Mchungaji Mwema.
b Ezra 6:21; 9:1; Neh. 9:2; 2 The. 3:6; M&M 133:5, 14.
c Kum. 29:20; Moro. 6:7; M&M 20:8.
58 *a* MWM Kitabu cha Uzima.
61 *a* Alma 5:44.
62 *a* 1 Ne. 8:10; 11:21–23.
6 1 *a* MWM Kutawaza, Kutawazwa.
b MWM Mzee.
c MWM Mikono, Kuweka juu ya.
d M&M 52:39.

2 Na ikawa kwamba yeyote ambaye hakuwa mshiriki wa kanisa ambaye alitubu dhambi zake [a]alibatizwa ubatizo wa toba, na akapokelewa katika kanisa.

3 Na ikawa kwamba wale ambao walikuwa washiriki wa kanisa na [a]hawakutubu uovu wao na kunyenyekea mbele ya Mungu—ninamaanisha wale ambao walikuwa wamejiinua kwa [b]kiburi cha mioyo yao—wao walikataliwa, na majina yao [c]kufutwa, kwamba majina yao yasihesabiwe miongoni mwa wale ambao ni wenye haki.

4 Na hivyo walianza kuimarisha mpango wa kanisa katika mji wa Zarahemla.

5 Sasa ningetaka mfahamu kwamba neno la Mungu lilikuwa huru kwa wote, na kwamba hakuna yeyote aliyenyimwa nafasi ya kukusanyika pamoja ili kusikia neno la Mungu.

6 Walakini watoto wa Mungu waliamriwa kwamba wakusanyike pamoja mara kwa mara, na waungane katika [a]kufunga na sala kuu kwa niaba ya ustawi wa nafsi ambazo hazikumjua Mungu.

7 Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kutoa masharti haya aliondoka kutoka kwao, ndiyo, kutoka kanisa ambalo lilikuwa katika mji wa Zarahemla, na akaenda mashariki mwa mto Sidoni, katika [a]bonde la Gideoni, palipojengwa mji, ambao uliitwa mji wa Gideoni, ambao ulikuwa katika bonde lililoitwa Gideoni, kwani lilitungwa yule mtu ambaye [b]aliuawa kwa mkono wa Nehori kwa upanga.

8 Na Alma alienda na kuanza kutangaza neno la Mungu katika kanisa ambalo lilikuwa limeanzishwa katika bonde la Gideoni, kulingana na ufunuo wa ukweli wa neno ambao ulizungumzwa na babu zake, na kulingana na roho ya unabii ambayo ilikuwa ndani yake, kulingana na [a]ushuhuda wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ambaye atakuja kuwakomboa watu wake kutoka dhambi zao, na ule mpango mtakatifu ambao aliitiwa. Na hivyo imeandikwa. Amina.

Maneno ya Alma ambayo aliwakabidhi watu wa Gideoni, kulingana na maandishi yake mwenyewe.

Yenye mlango wa 7.

MLANGO WA 7

Kristo atazaliwa na Mariamu—Atafungua kamba za mauti na kubeba dhambi za watu Wake—Wale ambao wanatubu, wanabatizwa, na kushika amri watakuwa na

2*a* MWM Batiza, Ubatizo.
3*a* Mos. 26:6.
b MWM Kiburi.
c Ku. 32:33; Mos. 26:36; Alma 1:24; 5:57–58. MWM Kutengwa na Kanisa.
6*a* MWM Funga, Kufunga.
7*a* Alma 2:20.
b Alma 1:9.
8*a* Ufu. 19:10.

uzima wa milele—Uchafu hauwezi kurithi ufalme wa Mungu—Unyenyekevu, imani, tumaini, na hisani vinahitajika. Karibia mwaka 83 K.K.

TAZAMA ndugu zangu wapendwa, kwa kuwa nimeruhusiwa kuja kwenu, kwa hivyo nitajaribu [a]kuwazungumzia kwa lugha yangu; ndiyo, kwa kinywa changu mwenyewe, nikiona kwamba hii ndiyo mara yangu ya kwanza ya kuwazungumzia kwa maneno ya kinywa changu, kwani nilikuwa nimefungiwa kwa [b]kiti cha hukumu, nikiwa na shughuli nyingi kwamba sikuweza kuwatembelea.

2 Na hata singeweza kuja sasa kwa wakati huu, ijapokuwa kiti cha hukumu [a]kimepewa mwingine, atawale badala yangu; na Bwana katika rehema nyingi amewezesha kwamba niwatembelee.

3 Na tazama, nimekuja kwa matumaini mengi kwamba niwapate kwamba mmejinyenyekeza mbele ya Mungu, na kwamba mlikuwa mnaendelea kuomba neema yake, na kwamba niwapate hamna lawama mbele yake, na kwamba nisiwapate mkiwa katika hali ya kuhofisha kama ile ndugu zetu waliyokuwa nayo huko Zarahemla.

4 Lakini jina la Mungu libarikiwe, kwani amenijulisha nijue, ndiyo, amenipatia shangwe kuu ya kujua kwamba wamejiimarisha tena katika haki yake.

5 Na ninatumai, kulingana na Roho wa Mungu aliye ndani yangu, kwamba pia nitakuwa na shangwe juu yenu; walakini sitamani kwamba shangwe yangu kwenu ninyi ije kwa mateso mengi na huzuni kama ile niliyokuwa nayo kwa ndugu huko Zarahemla, kwani tazama, shangwe yangu juu yao inakuja baada ya kupitia mateso mengi na huzuni.

6 Lakini tazama, ninatumai kwamba hamko katika hali ya kutoamini kama vile waliyokuwa ndugu zenu; ninatumaini kwamba hamjainuliwa kwa kiburi cha mioyo yenu; ndiyo, ninatumaini kwamba hamjaweka mioyo yenu katika utajiri na vitu vya ulimwengu visivyo na busara; ndiyo, ninatumaini kwamba hamwabudu [a]sanamu, lakini mnamwabudu Mungu wa kweli na [b]anayeishi, na kwamba mnatazamia msamaha wa dhambi zenu, kwa imani isiyo na mwisho, inayokuja.

7 Kwani tazama, ninawaambia kuna vitu vingi vitakavyokuja; na tazama, kuna kitu kimoja ambacho ni muhimu kuliko vyote—kwani tazama, [a]wakati hauko mbali ambao Mkombozi ataishi miongoni mwa watu wake.

8 Tazama, sisemi kwamba atakuja kati yetu ule wakati atakaokuwa akiishi katika hema ya mwili; kwani tazama, Roho

7 1*a* Alma 4:19.
b Mos. 29:42.
2*a* Alma 4:16–18.
6*a* 2 Ne. 9:37; Hel. 6:31.
b Dan. 6:26.
7*a* Alma 9:26.

hajaniambia kwamba itakuwa hivyo. Sasa kitu hiki sikijui; lakini ninajua haya, kwamba Bwana Mungu ana uwezo wa kutenda vitu vyote ambavyo vinalingana na neno lake.

9 Lakini tazama, Roho ameniambia haya, akisema: Watangazie watu hawa, ukisema—[a]Tubuni ninyi, na mtayarishie Bwana njia, na mfuate njia zake, ambazo ni nyoofu; kwani tazama, ufalme wa mbinguni u karibu, na Mwana wa Mungu [b]atakuja usoni mwa dunia.

10 Na tazama, [a]atazaliwa na [b]Mariamu, huko Yerusalemu ambayo ni [c]nchi ya babu zetu, yeye akiwa [d]bikira, chombo cha thamani na kilichochaguliwa, ambaye atawezeshwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kupata [e]mimba, na kumzaa mwana, ndiyo, hata Mwana wa Mungu.

11 Na atakwenda, na kuteseka maumivu na [a]masumbuko na majaribio ya kila aina; na hii kwamba neno litimizwe ambalo linasema atabeba maumivu na magonjwa ya watu wake.

12 Na atajichukulia [a]kifo, ili afungue kamba za kifo ambazo zinafunga watu wake; na atajichukulia unyonge wao, ili moyo wake ujae rehema, kulingana na mwili, ili ajue kulingana na mwili jinsi ya [b]kuwasaidia watu wake kulingana na unyonge wao.

13 Sasa Roho [a]anajua vitu vyote; walakini Mwana wa Mungu anateseka katika mwili ili [b]achukue dhambi za watu wake, kwamba aondoe uvunjaji wao wa sheria kulingana na nguvu za ukombozi wake; na sasa tazama, huu ndiyo ushuhuda ulio ndani yangu.

14 Sasa nawaambia kwamba lazima mtubu, na [a]mzaliwe tena; kwani Roho anasema kuwa msipozaliwa tena hamwezi kurithi ufalme wa mbinguni; kwa hivyo njooni mbatizwe ubatizo wa toba, ili msafishwe kutoka kwa dhambi zenu, ili muwe na imani katika Mwanakondoo wa Mungu, anayeondoa dhambi za ulimwengu, ambaye anaweza kuokoa na kuosha kutokana na uovu wote.

15 Ndiyo, ninawaambia njooni na msiogope, na muweke kando kila dhambi, ambayo [a]inawasumbua, ambayo inawatia katika maangamizo, ndiyo, njooni na msonge mbele na mmwonyeshe Mungu wenu kwamba mnatamani kutubu dhambi zenu na kuingia kwenye agano naye kuweka amri zake, na kushuhudia kwake siku hii kwa kuingia kwenye maji ya ubatizo.

16 Na yeyote atakayefanya

9 *a* Mt. 3:2–4; Alma 9:25.
b Mos. 3:5; 7:27; 15:1–2.
10 *a* Isa. 7:14; Lk. 1:27.
b Mos. 3:8. MWM Maria, Mama wa Yesu.
c 1 Nya. 9:3; 2 Nya. 15:9; 1 Ne. 1:4; 3 Ne. 20:29.
d 1 Ne. 11:13–21.
e Mt. 1:20; Mos. 15:3.
11 *a* Isa. 53:3–5; Mos. 14:3–5.
12 *a* 2 Ne. 2:8; Alma 12:24–25. MWM Kusulubiwa.
b Ebr. 2:18; 4:15; M&M 62:1.
13 *a* MWM Mungu, Uungu.
b Mos. 15:12. MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
14 *a* MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
15 *a* 2 Ne. 4:18.

hivi, na atii amri za Mungu tangu leo, huyu atakumbuka kwamba nilimwambia, ndiyo, atakumbuka kwamba nimemwambia, atapokea uzima wa milele, kulingana na ushuhuda wa Roho Mtakatifu, ambaye anashuhudia ndani yangu.

17 Na sasa ndugu zangu wapendwa, mnaamini vitu hivi? Tazama, ninawaambia, ndiyo, ninajua kwamba mnaviamini; na jinsi ile ninayojua kwamba mnaviamini ni kwa dhihirisho la Roho aliye ndani yangu. Na sasa kwa sababu imani yenu ina nguvu kuhusu hayo, ndiyo, kuhusu vile vitu ambavyo nimezungumza, shangwe yangu ni kuu.

18 Kwani kama vile nilivyosema kwenu hapo mwanzo, kwamba nilitamani msiwe katika hali ile ya dharura kama ndugu zenu, hata hivyo nia yangu imependezwa.

19 Kwani ninahisi kwamba mko katika njia za haki; ninahisi kwamba mko katika njia ile inayoelekea katika ufalme wa Mungu; ndiyo, ninahisi kwamba mnanyoosha [a]njia zake.

20 Ninahisi kwamba imefanywa kujulikana kwenu, kwa ushuhuda wa neno lake, kwamba yeye hawezi [a]kupita katika njia kombo; wala habadilishi yale ambayo amesema; wala hana kivuli cha kugeukia kushoto au kulia, au kutoka kwa mema na kuingilia yale maovu; kwa hivyo, njia zake ni za milele.

21 Na haishi katika hekalu zilizo [a]chafu; wala uchafu au chochote ambacho kisicho safi hakiwezi kupokewa katika ufalme wa Mungu; kwa hivyo ninawaambia kwamba wakati utafika, ndiyo, na itakuwa siku ya mwisho, kwamba yule aliye [b]mchafu atabaki katika uchafu wake.

22 Na sasa ndugu zangu wapendwa, nimewaambia vitu hivi ili niwaamshe mjue wajibu wenu kwa Mungu, ili mtembee bila lawama mbele yake, ili mtembee kulingana na mpango mtakatifu wa Mungu, ambayo kwayo mmepokelewa.

23 Na sasa ningetaka kwamba muwe [a]wanyenyekevu, na muwe wapole na waungwana; wepesi kusihiwa; wenye utele wa subira na uvumilivu; wenye kiasi katika vitu vyote, wenye bidii katika kutii amri za Mungu wakati wote; mkiomba kwa vyovyote mnavyohitaji, vya kiroho na vya kimwili; na kila wakati kumshukuru Mungu kwa vyovyote mnavyopokea.

24 Na mhakikishe kwamba mna [a]imani, tumaini, na hisani, na kisha mtadumu katika kazi nzuri.

25 Na Bwana awabariki, na ahifadhi mavazi yenu yasiwe

19*a* Mt. 3:3.
20*a* 1 Ne. 10:19; Alma 37:12; M&M 3:2.
21*a* 1 Kor. 3:16–17; 6:19; Mos. 2:37; Alma 34:36.
b 1 Ne. 15:33–35; 2 Ne. 9:16; Morm. 9:14; M&M 88:35.
23*a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
24*a* 1 Kor. 13; Eth. 12:30–35; Moro. 7:33–48.

na doa, ili mwishowe mletwe mkae chini na Ibrahimu, Isaka, na Yakobo, na manabii watakatifu ambao wameishi tangu ulimwengu uumbwe, mkiwa na mavazi yenu yasiyo na [a]doa kama vile mavazi yao hayana doa, katika ufalme wa mbinguni bila kutoka nje tena.

26 Na sasa ndugu zangu wapendwa, nimewazungumzia mambo haya kulingana na Roho anayeshuhudia ndani yangu; na nafsi yangu inafurahi sana, kwa sababu ya bidii nyingi na utiifu ambao mmelipatia neno langu.

27 Na sasa, [a]amani ya Mungu iwe nanyi, na kwa nyumba zenu na mashamba yenu, na mifugo yenu na wanyama wenu, na yote ambayo mnamiliki, wake zenu na watoto wenu, kulingana na imani yenu na kazi njema, tangu sasa hadi milele. Na hivyo nimesema. Amina.

MLANGO WA 8

Alma anahubiri na kubatiza katika Meleki—Anakataliwa katika Amoniha na kuondoka—Malaika anamwamuru arudi na kuhubiria watu toba—Anapokelewa na Amuleki, na wao wawili wanahubiri katika Amoniha. Karibia mwaka 82 K.K.

Na sasa ikawa kwamba Alma alirudi kutoka [a]nchi ya Gideoni, baada ya kuwafundisha watu wa Gideoni vitu vingi ambavyo haviwezi kuandikwa, baada ya kuimarisha mpangilio wa kanisa, kulingana na vile alivyokuwa amefanya katika nchi ya Zarahemla, ndiyo, alirejea katika nyumba yake Zarahemla kujipumzisha kutokana na ile kazi aliyokuwa ametenda.

2 Na hivyo mwaka wa tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi ulikwisha.

3 Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa kumi wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, kwamba Alma aliondoka kutoka huko na kusafiri katika nchi ya Meleki, magharibi kando mwa [a]mto Sidoni, magharibi kando mwa mipaka ya nyika.

4 Na akaanza kuwafundisha watu katika nchi ya Meleki kulingana na [a]mpango mtakatifu wa Mungu, ambao alikuwa ameitwa kwake; na akaanza kufundisha watu kote katika nchi ya Meleki.

5 Na ikawa kwamba watu walimjia kutoka mipaka yote ya nchi ambayo ilikuwa kando ya nyika. Na wakabatizwa kote katika nchi;

6 Kwa hivyo baada ya kukamilisha kazi yake katika Meleki aliondoka huko, na akasafiri muda wa siku tatu kaskazini mwa nchi ya Meleki; na akafika katika mji ulioitwa Amoniha.

7 Sasa ilikuwa ni desturi ya watu wa Nefi kuita nchi zao, na miji yao, na vijiji vyao, ndiyo, na hata vijiji vyao vyote vidogo, kwa jina la yule ambaye

25 *a* 2 Pet. 3:14.
27 *a* MWM Amani.
8 1 *a* Alma 2:20; 6:7.
3 *a* Alma 16:6–7.
4 *a* M&M 107:2–4.
MWM Ukuhani wa Melkizedeki.

aliimiliki kwanza; na ilikuwa hivyo katika nchi ya Amoniha.

8 Na ikawa kwamba baada ya Alma kuwasili katika mji wa Amoniha alianza kuwahubiria neno la Mungu.

9 Sasa Shetani alikuwa [a]amekamata mioyo ya watu wa mji wa Amoniha; kwa hivyo hawakusikiliza maneno ya Alma.

10 Walakini Alma alitia [a]bidii sana katika roho, [b]akipambana na Mungu katika [c]sala kuu, ili awateremshie watu waliokuwa katika mji Roho wake; kwamba akubali kwamba awabatize katika toba.

11 Walakini, walishupaza mioyo yao, na kumwaambia: Tazama, tunajua kwamba wewe ni Alma; na tunajua kwamba wewe ni kuhani mkuu wa kanisa ambalo wewe umeanzisha katika sehemu nyingi za nchi, kulingana na mila zako; na sisi sio washirika wa kanisa lako, na hatuamini mila za kishenzi kama hizo.

12 Na sasa tunajua kwamba kwa sababu sisi sio washirika wa kanisa lako tunajua kwamba huna mamlaka juu yetu; na wewe umemkabidhi [a]Nefiha kiti cha hukumu; kwa hivyo wewe si mwamuzi mkuu juu yetu.

13 Sasa baada ya watu kunena haya, na kuyapinga maneno yake yote, na kumfanyia mzaha, na kumtemea mate, na kumsababisha kwamba atupwe nje ya mji wao, aliondoka hapo na akafunga safari yake akielekea mji ambao uliitwa Haruni.

14 Na ikawa kwamba alipokuwa akisafiri huko, na kuzidiwa sana na huzuni, na kupambana na [a]mateso mengi na kusononeka sana katika nafsi, kwa sababu ya uovu wa watu ambao walikuwa katika mji wa Amoniha, ikawa kwamba wakati ambao Alma alikuwa amezidiwa na huzuni, tazama [b]malaika wa Bwana alimtokea, na kusema:

15 Heri wewe, Alma; kwa hivyo, inua kichwa chako na ufurahi, kwani una sababu kubwa ya kufurahi; kwani umekuwa mwaminifu katika kutii amri za Mungu tangu ule wakati ambao ulipokea ujumbe wako mara ya kwanza kutoka kwake. Tazama, Mimi ndimi yule [a]niliyewaletea.

16 Na tazama, nimetumwa kukuamuru kwamba urudi katika mji wa Amoniha, na uwahubirie tena watu wa mji huo; ndiyo, uwahubirie. Ndiyo, uwaambie, wasipotubu Bwana Mungu [a]atawaangamiza.

17 Kwani tazama, wanapanga kwa wakati huu jinsi ya kuangamiza uhuru wa watu wako, (kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana) ambayo ni kinyume cha maagizo, na hukumu, na amri ambazo amewapatia watu wake.

18 Sasa ikawa kwamba baada ya Alma kupokea ujumbe wake kutoka kwa malaika wa Bwana

9*a* 2 Ne. 28:19–22; M&M 10:20.
10*a* Alma 17:5.
b Eno. 1:1–12.
c 3 Ne. 27:1. MWM Sala.
12*a* Alma 4:20.
14*a* MWM Shida.
b Alma 10:7–10, 20. MWM Malaika.
15*a* Mos. 27:11–16.
16*a* Alma 9:12, 18, 24.

alirudi kwa haraka katika nchi ya Amoniha. Na akaingia katika mji kwa njia nyingine, ndiyo, kwa njia iliyo kusini mwa mji wa Amoniha.

19 Na alipoingia mjini alikuwa na njaa, na akamwambia mtu fulani: Waweza kumpatia mtumishi mnyenyekevu wa Mungu kitu cha kula?

20 Na yule mtu akamwambia: Mimi ni Mnefi, na ninajua kwamba wewe ni nabii mtakatifu wa Mungu, kwani wewe ndiye yule mtu ambaye [a]malaika alisema katika ono: Wewe utampokea. Kwa hivyo, njoo na mimi katika nyumba yangu na nitakupatia chakula changu; na ninajua kwamba wewe utakuwa baraka kwangu mimi na nyumba yangu.

21 Na ikawa kwamba yule mtu alimkaribisha katika nyumba yake; na yule mtu aliitwa [a]Amuleki; na akaleta mkate na nyama na kumpakulia Alma.

22 Na ikawa kwamba Alma alikula mkate na kushiba; na [a]akambariki Amuleki na nyumba yake, na akamshukuru Mungu.

23 Na baada ya kula na kushiba akamwambia Amuleki: Mimi ni Alma, na mimi ni [a]kuhani mkuu wa kanisa la Mungu kote nchini.

24 Na tazama, nimeitwa kuhubiri neno la Mungu miongoni mwa watu hawa wote, kulingana na roho ya ufunuo na unabii; na nilikuwa katika nchi hii na hawakunipokea, lakini [a]walinifukuza na karibu niiache nchi hii milele.

25 Lakini tazama, nimeamuriwa kwamba nirudi tena na niwatolee watu hawa unabii, ndiyo, na kuwashuhudia dhidi ya maovu yao.

26 Na sasa, Amuleki, kwa sababu umenilisha na kunipokea, umebarikiwa; kwani nilikuwa mwenye njaa, kwa kufunga siku nyingi.

27 Na Alma akaishi siku nyingi na Amuleki kabla ya kuanza kuwahubiria watu.

28 Na ikawa kwamba watu waliendelea kuwa wabaya zaidi katika uovu wao.

29 Na neno likamjia Alma, likisema: Nenda; na pia umwambie mtumishi wangu Amuleki, nenda mbele na uwatolee watu hawa unabii, uwaambie—[a]Tubuni, kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana, msipotubu nitawatembelea watu hawa kwa ghadhabu yangu; ndiyo, na sitabadilisha ghadhabu yangu kali kutoka kwao.

30 Na Alma akaenda, pamoja na Amuleki, miongoni mwa watu, kuwatangazia neno la Mungu; na walijazwa na Roho Mtakatifu.

31 Na wakapewa uwezo, hata ikawa kwamba haingewezekana wao kufungwa katika magereza; wala mtu yeyote kuweza kuwaua; walakini hawakutumia [a]uwezo wao hadi walipofungwa kwa kamba na kutupwa gerezani. Sasa, haya yalifanywa

20 *a* Alma 10:7–9.
21 *a* MWM Amuleki.
22 *a* Alma 10:11.
23 *a* Alma 5:3, 44, 49; 13:1–20.
24 *a* Alma 8:13.
29 *a* Alma 9:12, 18. MWM Toba, Tubu.
31 *a* 1 Ne. 1:20.

ili Bwana adhihirishe [b]uwezo wake ndani yao.

32 Na ikawa kwamba walienda na wakaanza kuhubiria watu na kuwatolea unabii, kulingana na roho na uwezo ambao Bwana alikuwa amewapatia.

Maneno ya Alma, na pia maneno ya Amuleki, ambayo yalitangaziwa kwa watu waliokuwa katika nchi ya Amoniha. Na pia wanatupwa gerezani, na kukombolewa kwa nguvu za miujiza ya Mungu ambayo ilikuwa ndani yao, kulingana na maandishi ya Alma.

Yenye milango ya 9 hadi 14.

MLANGO WA 9

Alma anawaamuru watu wa Amoniha watubu—Bwana atawarehemu Walamani katika siku za mwisho—Wanefi wakiacha nuru, wataangamizwa na Walamani—Mwana wa Mungu atakuja hivi karibuni—Atawakomboa wale ambao watatubu, kubatizwa, na kuwa na imani katika jina Lake. Karibia mwaka 82 K.K.

Na tena, mimi, Alma, baada ya kuamriwa na Mungu kwamba nimchukue Amuleki na kwenda tena na kuhubiria watu hawa, au watu waliokuwa katika mji wa Amoniha, ikawa kwamba nilipoanza kuwahubiria, nao wakaanza kubishana na mimi, wakisema:

2 Nani wewe? Unadhani kwamba tutaamini ushuhuda wa mtu [a]mmoja, hata ikiwa atatuhubiria kuwa dunia itakwisha?

3 Sasa hawakufahamu yale ambayo walizungumza; kwani hawakujua kwamba dunia itakwisha.

4 Na wakasema pia: Hatutaamini maneno yako kama utatoa unabii kwamba mji huu mkuu utaangamizwa katika siku [a]moja.

5 Sasa hawakujua kwamba Mungu angeweza kufanya vitendo vya ajabu kama hivyo, kwani walikuwa watu wenye mioyo migumu na shingo ngumu.

6 Na wakasema: Mungu ni [a]nani, ambaye [b]hatumi mamlaka zaidi ya mtu mmoja miongoni mwa watu hawa, kuwatangazia ukweli wa vitu vikuu na vya ajabu kama hivi?

7 Na wakasonga mbele ili wanikamate; lakini tazama, hawakuweza. Na nikasimama kwa ujasiri ili niwatangazie, ndiyo, niliwashuhudia kwa ujasiri, nikisema:

8 Tazameni, Ee ninyi [a]kizazi kiovu na kibaya, ni vipi mmesahau mila za babu zenu; ndiyo, vipi mara moja mmesahau amri za Mungu.

9 Hamkumbuki kwamba baba yetu, Lehi, alitolewa Yerusalemu kwa [a]mkono wa Mungu? Hamkumbuki kwamba wote waliongozwa na yeye kupitia nyikani?

31 *b* Alma 14:17–29.
9 2 *a* Kum. 17:6.
4 *a* Alma 16:9–10.
6 *a* Ku. 5:2; Mos. 11:27; Musa 5:16.
b Alma 10:12.
8 *a* Alma 10:17–25.
9 *a* 1 Ne. 2:1–7.

10 Na mmesahau haraka vipi kwamba aliwakomboa babu zetu mara nyingi kutoka mikononi mwa maadui wao, na akawahifadhi kutokana na maangamizo, hata kwa mikono ya ndugu zao wenyewe?

11 Ndiyo, na kama sio kwa uwezo wake usio na kipimo, na rehema yake, na subira yake kwetu sisi, tungekuwa tumetengwa kutoka usoni mwa dunia kitambo sana kabla ya wakati huu, na pengine tungekuwa tumewekwa kwa hali ya taabu na hofu [a]isiyo na mwisho.

12 Tazama, sasa nawaambia kwamba anawaamuru mtubu; na msipotubu, hamwezi kurithi ufalme wa Mungu. Lakini tazama, haya sio yote—amewaamuru kwamba mtubu, au [a]atawaangamiza kabisa kutoka usoni mwa dunia; ndiyo; atawatembelea katika ghadhabu yake, na katika ghadhabu yake [b]kali hatawarehemu.

13 Tazama, hamkumbuki maneno ambayo alimzungumzia Lehi, akisema kwamba: [a]Kadiri mtakavyoweka amri zangu, ndivyo mtakavyofanikiwa katika nchi? Na tena imesemwa kwamba: Kadiri vile msiposhika amri zangu ndivyo mtakavyotengwa kutoka uwepo wa Bwana.

14 Sasa ningetaka kwamba mkumbuke, kwamba jinsi Walamani wamekosa kushika amri za Mungu, [a]wamekatwa kutokana na uwepo wa Bwana. Sasa tunaona kwamba neno la Bwana limethibitishwa katika kitu hiki, na Walamani wametengwa kutoka uwepo wake, tangu mwanzo wa uasi wao katika nchi hii.

15 Walakini nawaambia, kwamba itakuwa [a]afadhali kwao katika siku ya hukumu kuliko ninyi, ikiwa mtabaki katika dhambi zenu, ndiyo, na hata ya kuvumilika zaidi katika maisha haya, msipotubu.

16 Kwani kuna ahadi nyingi ambazo Walamani [a]wamenyooshewa; kwani ni kwa sababu ya [b]mila za babu zao ambazo ziliwasababisha kuishi katika hali yao ya [c]kutojua; kwa hivyo Bwana atawahurumia na [d]azidishe maisha yao katika nchi.

17 Na wakati utafika ambao [a]watawezeshwa kuamini neno lake, na kujua kasoro za mila za babu zao; na wengi wao wataokolewa, kwani Bwana atawarehemu wote ambao [b]wataliita jina lake.

18 Lakini tazama, nawaambia kwamba mkiendelea katika uovu wenu siku zenu hazitazidishwa katika nchi, kwani [a]Walamani watatumwa kuwashambulia; na msipotubu watakuja katika wakati ambao hamjui, na mtatembelewa na

11 *a* Mos. 16:11.
12 *a* Alma 8:16; 10:19, 23, 27.
b Alma 8:29.
13 *a* 2 Ne. 1:20; Mos. 1:7; Alma 37:13.
14 *a* 2 Ne. 5:20–24; Alma 38:1.
15 *a* Mt. 11:22, 24.
16 *a* Alma 17:15.
b Mosia 10:12 (tazama aya 11–17).
c Mos. 3:11.
d Hel. 15:10–12.
17 *a* Eno. 1:13.
b Alma 38:5; M&M 3:8.
18 *a* Alma 16:2–3.

maangamizo [b]makuu; na itakuwa kulingana na [c]ghadhabu kali ya Bwana.

19 Kwani hatakubali kwamba muishi katika maovu yenu, kuangamiza watu wake. Ninawaambia, Hapana; atawaruhusu Walamani [a]wawaangamize watu wake wote ambao wanaitwa watu wa Nefi, ikiwa ingewezekana kwamba [b]wangeanguka katika dhambi na maovu, baada ya kupokea nuru nyingi na ufahamu mwingi kutoka kwa Bwana Mungu wao;

20 Ndiyo, baada ya kuwa watu waliopendelewa sana na Bwana; ndiyo, baada ya kupendelewa zaidi ya taifa, kabila, lugha, au watu wengine; baada ya [a]kujulishwa vitu vyote kulingana na kutaka kwao, na imani yao, na sala, za yale ambayo yamekuwa, na ambayo yako, na ambayo yatakuja;

21 Baada ya kutembelewa na Roho wa Mungu; baada ya kuzungumza na malaika, na baada ya kuzungumziwa na sauti ya Bwana; na kuwa na roho ya unabii, na roho ya ufunuo, na pia vipawa vingi, na kipawa cha kunena kwa lugha, kipawa cha kuhubiri, na kipawa cha Roho Mtakatifu, na kipawa cha [a]utafsiri;

22 Ndiyo, na baada ya [a]kukombolewa na Mungu kutoka nchi ya Yerusalemu, kwa mkono wa Bwana; baada ya kuokolewa kutokana na njaa, na kutoka ugonjwa, na kila aina ya magonjwa ya aina yote; na baada ya wao kupata nguvu katika vita, ili wasiangamizwe; baada ya wao kutolewa kutoka [b]utumwa mara kwa mara, na baada ya kuwekwa na kuhifadhiwa hadi sasa; na wamefanikishwa hadi wakapata utajiri kwa aina yote ya vitu—

23 Na sasa tazama nawaambia, kwamba kama hawa watu, ambao wamepokea baraka nyingi kutoka mkono wa Bwana, watakosea kulingana na nuru na ufahamu ambao wamepokea, ninawaambia kwamba kama itakuwa hivyo, kwamba ikiwa wataanguka kwenye makosa, itakuwa ni [a]heri kwa Walamani kuliko wao.

24 Kwani tazama, [a]ahadi za Bwana zimenyooshewa Walamani, lakini sio zenu mkivunja sheria; kwani si Bwana ameahidi waziwazi na kutanganza kwa uthabiti, kwamba mkimuasi mtaangamizwa kutoka usoni mwa dunia?

25 Na sasa kwa sababu hii, kwamba msiangamizwe, Bwana ametuma malaika wake kuwatembelea wengi wa watu wake, akiwaambia kwamba lazima waende na kuwatanganzia watu hawa, wakisema: [a]Tubuni ninyi, kwani ufalme wa mbinguni upo karibu;

26 Na [a]sio baada ya siku nyingi

18 *b* Alma 16:9.
c Alma 8:29.
19 *a* 1 Ne. 12:15, 19–20; Alma 45:10–14.
b Alma 24:30.
20 *a* MWM Ufunuo.
21 *a* Omni 1:20; Mos. 8:13–19; 28:11–17.
22 *a* 2 Ne. 1:4.
b Mos. 27:16.
23 *a* Mt. 11:22–24.
24 *a* 2 Ne. 30:4–6; M&M 3:20.
25 *a* Alma 7:9; Hel. 5:32.
26 *a* Alma 7:7.

kwamba Mwana wa Mungu atakuja katika utukufu wake; na utukufu wake utakuwa utukufu wa yule [b]Mzaliwa Pekee wa Baba, aliyejaa [c]neema, haki, na ukweli, mwenye subira, [d]rehema, na uvumilivu, mwepesi [e]kusikia vilio vya watu wake na kujibu sala zao.

27 Na tazama, anakuja [a]kukomboa wale ambao [b]watabatizwa ubatizo wa toba, kupitia imani katika jina lake.

28 Kwa hivyo, tayarisheni ninyi njia ya Bwana, kwani wakati umo mkononi kwamba watu wote watavuna zawadi za [a]kazi zao, kulingana na vile walivyokuwa—kama wamekuwa wenye haki [b]watavuna wokovu wa nafsi zao, kulingana na uwezo na ukombozi wa Yesu Kristo; na kama wamekuwa waovu watavuna [c]mauti ya nafsi zao, kulingana na uwezo na utumwa wa ibilisi.

29 Sasa tazama, hii ni sauti ya malaika, inayowatangazia watu.

30 Na sasa, ndugu zangu [a]wapendwa, kwani ninyi ni ndugu zangu, na inafaa muwe wapendwa, na inafaa mtende vitendo vya toba, nikiona kwamba mioyo yenu imeshupazwa kupita kiasi dhidi ya neno la Mungu, na nikiona kwamba ninyi ni watu ambao [b]wamepotea na kuanguka.

31 Sasa ikawa kwamba wakati mimi, Alma, nilipozungumza maneno haya, tazama, watu walinikasirikia kwa sababu niliwaambia kwamba wao walikuwa watu wenye mioyo migumu na [a]shingo ngumu.

32 Na pia kwa sababu niliwaambia kwamba walikuwa watu waliopotea na walioanguka, walinikasirikia, na wakatafuta jinsi ya kunikamata, ili wanitupe gerezani.

33 Lakini ikawa kwamba Bwana hakuwaruhusu wanichukue ule wakati na kunitupa gerezani.

34 Na ikawa kwamba Amuleki alienda, na akaanza kuwahubiria pia. Na sasa [a]maneno yote ya Amuleki hayajaandikwa, walakini sehemu ya maneno yake yameandikwa katika kitabu hiki.

MLANGO WA 10

Lehi ni wa uzao wa Manase—Amuleki anaelezea jinsi malaika alivyomwamuru kwamba amhudumie Alma—Sala za watu wenye haki zinawaokoa watu—Mawakili na Waamuzi wasio wenye haki wanaanza kupanga maangamizo ya watu. Karibia mwaka 82 K.K.

Sasa haya ndiyo [a]maneno ambayo [b]Amuleki aliwahubiria watu ambao walikuwa katika nchi ya Amoniha, akisema:

2 Mimi ni Amuleki; mimi ni

26 *b* MWM Mzaliwa Pekee.
c MWM Neema.
d MWM Rehema, enye Rehema.
e Kum. 26:7.
27 *a* MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
b MWM Batiza, Ubatizo.
28 *a* M&M 1:10; 6:33.
b Zab. 7:16.
c MWM Hukumu.
30 *a* 1 Yoh. 4:11.
b Alma 12:22.
31 *a* 2 Ne. 25:28; Mos. 3:14.
34 *a* Alma 10.
10 1 *a* Alma 9:34.
b Alma 8:21–29.

mwana wa Gidona, ambaye alikuwa mwana wa Ishmaeli, ambaye alikuwa uzao wa Aminadi; na alikuwa ni huyo Aminadi ambaye alitafsiri maandiko ambayo yalikuwa kwenye ukuta wa hekalu, ambayo yaliandikwa kwa kidole cha Mungu.

3 Na Aminadi alikuwa uzao wa Nefi, ambaye alikuwa ni mwana wa Lehi, ambaye alitoka nchi ya Yerusalemu, ambaye alikuwa uzao wa [a]Manase, ambaye alikuwa mwana wa [b]Yusufu [c]aliyeuzwa Misri kwa mikono ya kaka zake.

4 Na tazama, mimi pia sio mtu aliye na heshima ndogo miongoni mwa wote ambao wananijua; ndiyo, na tazama, nina jamaa na [a]marafiki wengi, na pia nimepokea utajiri mwingi kutokana na bidii ya mikono yangu.

5 Walakini, hata baada ya haya yote, sijaelewa sana kuhusu njia za Bwana, na [a]siri zake na nguvu zake za ajabu. Nilisema kuwa sikuwahi kujua mengi kuhusu vitu hivi; lakini tazama, nimekosea, kwani nimeona siri zake nyingi na nguvu zake za ajabu; ndiyo, hata katika kuhifadhiwa kwa maisha ya watu hawa.

6 Walakini, nilishupaza moyo wangu, kwani [a]niliitwa mara nyingi lakini [b]sikusikia; kwa hivyo nilijua kuhusu vitu hivi, lakini nisingeweza kuvifahamu; kwa hivyo nikaendelea kumuasi Mungu, katika uovu wa moyo wangu, hadi siku ya nne ya mwezi huu wa saba, ambao uko katika mwaka wa kumi wa utawala wa waamuzi.

7 Nilipokuwa nikisafiri kumuona mmoja wa jamaa yangu wa karibu, tazama [a]malaika wa Bwana alinitokea na kuniambia: Amuleki, rudi nyumbani kwako, kwani utamlisha nabii wa Bwana; ndiyo, mtu mtakatifu, ambaye amechaguliwa na Mungu; kwani [b]amefunga siku nyingi kwa sababu ya dhambi za watu hawa, na ana njaa, na [c]utamkaribisha katika nyumba yako na utamlisha, na atakubariki wewe na nyumba yako; na baraka ya Bwana itakuwa juu yako na nyumba yako.

8 Na ikawa kwamba nilitii sauti ya malaika, na nikarudi nyumbani kwangu. Na nilipokuwa nikienda hapo nilimpata [a]mtu ambaye malaika alikuwa ameniambia: Wewe utampokea katika nyumba yako—na tazama ni huyu mtu ambaye amekuwa akiwazungumzia kuhusu vitu vya Mungu.

9 Na malaika aliniambia kuwa yeye ni mtu [a]mtakatifu; kwa hivyo najua kwamba yeye ni mtu mtakatifu kwa sababu ilisemwa na malaika wa Mungu.

10 Na tena, najua kwamba vitu ambavyo ameshuhudia ni

3*a* Mwa. 41:51; 1 Nya. 9:3.
b MWM Yusufu, Mwana wa Yakobo.
c Mwa. 37:29–36.
4*a* Alma 15:16.
5*a* MWM Siri za Mungu.
6*a* Alma 5:37.
b M&M 39:9.
7*a* Alma 8:20.
b Alma 5:46; 6:6. MWM Funga, Kufunga.
c Mdo. 10:30–35.
8*a* Alma 8:19–21.
9*a* MWM Takatifu.

vya kweli; kwani tazama nawaambia, jinsi vile Bwana anavyoishi, hata hivyo amemtuma [a]malaika wake kufanya vitu hivi vidhihirishwe kwangu; na amefanya haya wakati huyu Alma [b]alipoishi katika nyumba yangu.

11 Kwani tazama, ameibariki nyumba yangu, [a]amenibariki, na wanawake wangu, na watoto wangu, na baba yangu na jamaa yangu; ndiyo, ameibariki jamaa yangu yote, na baraka za Bwana zimekaa juu yetu kulingana na maneno ambayo alizungumza.

12 Na sasa, Amuleki alipokuwa amezungumza maneno haya watu walianza kustaajabu, wakiona kwamba kulikuwa na shahidi [a]zaidi ya mmoja ambaye alishuhudia kuhusu vitu ambavyo walishutumiwa, na pia kuhusu vitu ambavyo vitakuja, kulingana na roho ya unabii iliyokuwa ndani yao.

13 Walakini, kulikuwa na wengine miongoni mwao ambao walitaka kuwauliza maswali, ili wawanase katika maneno yao kwa [a]mitego, ili wapate ushuhuda dhidi yao, ili wawapeleke mbele ya waamuzi wao ili wahukumiwe kulingana na sheria, na ili wauawe au kutiwa gerezani, kulingana na makosa ambayo wangewasingizia au kushuhudia kinyume chao.

14 Sasa ilikuwa ni wale watu ambao walijaribu kuwaangamiza, ambao walikuwa ni [a]mawakili, ambao waliajiriwa au kuchaguliwa na watu kutekeleza sheria wakati wao wa hukumu, au katika hukumu ya makosa ya watu mbele ya waamuzi.

15 Sasa hawa mawakili walikuwa na elimu ya udanganyifu na ujanja wa watu; na hii ni kuwawezesha wawe na ustadi katika kazi yao.

16 Na ikawa kwamba walianza kumuuliza Amuleki maswali, ili wamfanye achanganye maneno yake, au kukanusha maneno ambayo angezungumza.

17 Sasa hawakujua kwamba Amuleki angeweza kujua mipango yao. Lakini ikawa kwamba walipoanza kumuuliza maswali, [a]alihisi mawazo yao, na akawaambia: Ee ninyi [b]kizazi kiovu na kibaya, ninyi mawakili na wanafiki, kwani mnajenga msingi wa ibilisi; kwani mnaweka [c]mitego ya kunasa walio watakatifu wa Mungu.

18 Mnapanga mipango ya [a]kuchafua njia za wenye haki, na kuteremsha ghadhabu ya Mungu juu ya vichwa vyenu, hata kwa maangamizo ya watu hawa.

19 Ndiyo, si ni Mosia, ambaye alikuwa mfalme wetu wa mwisho, aliyesema alipokaribia kutoa ufalme, na hakuwa na yeyote angestahili kupewa, na akasababisha kwamba watu hawa watawaliwe kwa sauti ya watu—ndiyo, alisema kwamba

10 *a* Alma 11:30–31.
b Alma 8:27.
11 *a* Alma 8:22.
12 *a* Alma 9:6.
13 *a* Alma 11:21.
14 *a* Alma 10:24; 11:20–21; 14:18.
17 *a* Alma 12:3; 18:20, 32; M&M 6:16.
b Mt. 3:7; Alma 9:8.
c M&M 10:21–27.
18 *a* Mdo. 13:10.

kama wakati utafika ambao sauti ya watu [a]itachagua uovu, yaani, wakati ukifika ambao watu hawa wataanguka katika dhambi, watakuwa tayari kuangamizwa.

20 Na sasa ninawaambia kwamba Bwana anahukumu maovu yenu vyema; na anawalilia watu hawa vyema, kwa sauti ya [a]malaika wake: Tubuni ninyi, tubuni, kwani ufalme wa mbinguni u karibu.

21 Ndiyo, kwa wema analia, kwa sauti ya malaika wake kwamba: [a]Mimi nitashuka chini miongoni mwa watu wangu, na usawa na haki mikononi mwangu.

22 Ndiyo, na ninawaambia kwamba kama sio [a]sala za wenye haki, walio katika nchi hii sasa, kwamba mngekuwa mmetembelewa kwa maangamizo kamili; lakini haingekuwa kwa [b]mafuriko, kama watu katika siku za Nuhu, lakini ingekuwa kwa njaa, na kwa tauni, na kwa upanga.

23 Lakini ni kwa [a]sala za wale wenye haki kwamba mmeachiliwa; sasa kwa hivyo, kama mtawafukuza wale wenye haki kutoka miongoni mwenu basi Bwana hatauzuia mkono wake; lakini katika ghadhabu yake atawateremkia; kisha mtapigwa kwa njaa, na kwa tauni, na kwa upanga; na [b]wakati u karibu msipotubu.

24 Na sasa ikawa kwamba watu walimkasirikia Amuleki zaidi, na wakalia, na kusema: Huyu mtu anadharau sheria zetu ambazo ni za haki, na mawakili wetu wenye busara ambao tumewachagua.

25 Lakini Amuleki aliwanyoshea mkono wake, na kusema kwa nguvu: Ee ninyi kizazi kiovu, mbona Shetani ameingia katika mioyo yenu jinsi hii? Kwa nini mnajitoa kwake na kumruhusu awe na uwezo juu yenu, [a]kufunga macho yenu, kwamba hamfahamu maneno ambayo yamezungumzwa, kulingana na ukweli wao?

26 Kwani tazama, nimezungumza kinyume cha sheria yenu? Ninyi hamfahamu; mnasema kwamba nimezungumza kinyume cha sheria yenu; lakini sikufanya hivyo, lakini nimeisifu sheria yenu, ambayo inawahukumu.

27 Na sasa tazama, nawaambia, kwamba msingi wa maangamizo ya watu hawa umeanza kujengwa na [a]mawakili wenu na waamuzi wenu ambao hawana haki.

28 Na sasa ikawa kwamba baada ya Amuleki kuzungumza maneno haya watu walipaza sauti yao dhidi yake, na kusema: Sasa tunajua kwamba huyu mtu ni mtoto wa ibilisi, kwani [a]ametudanganya; kwani ameishutumu sheria yetu. Na

19 *a* Mos. 29:27; Alma 2:3–7; Hel. 5:2.
20 *a* Alma 8:14–16; 13:22.
21 *a* Mos. 13:34.
22 *a* Yak. (Bib.) 5:16; Mos. 27:14–16.
b Mwa. 8:21; 3 Ne. 22:8–10. MWM Gharika katika Wakati wa Nuhu.
23 *a* MWM Sala.
b Alma 34:32–35.
25 *a* 2 Kor. 4:4; Alma 14:6.
27 *a* Lk. 11:45–52.
28 *a* Alma 14:2.

sasa anasema kwamba hajaishutumu.

29 Na tena, amewashutumu mawakili wetu, na waamuzi wetu.

30 Na ikawa kwamba mawakili waliweka vitu hivi katika mioyo yao ili wavikumbuke dhidi yake.

31 Na kulikuwa na mmoja miongoni mwao ambaye jina lake lilikuwa Zeezromu. Sasa yeye alikuwa wa mbele [a]kumshtaki Amuleki na Alma, yeye akiwa mwenye ujuzi mwingi miongoni mwao, na alikuwa na shughuli nyingi miongoni mwa watu.

32 Sasa lengo la mawakili hawa lilikuwa ni kupata faida; na walipata faida kulingana na kazi yao.

MLANGO WA 11

Wanefi wanatekeleza utaratibu wa fedha zao—Amuleki anabishana na Zeezromu—Kristo hataokoa watu katika dhambi zao—Wale tu ambao wanarithi ufalme wa mbinguni ndiyo wanaookolewa—Wanadamu wote watafufuka katika miili isiyokufana mwisho—Hakuna kifo baada ya Ufufuo. Karibia mwaka 82 K.K.

Sasa ilikuwa kwenye sheria ya Mosia kwamba kila mtu ambaye alikuwa mwamuzi wa sheria, au wale waliochaguliwa kuwa waamuzi, wapokee mshahara kulingana na muda ule ambao waliutumia katika kufanya uamuzi kwa wale walioletwa mbele yao kuhukumiwa.

2 Sasa kama mtu alidaiwa na mwingine, na akakataa kulipa deni ambalo alidaiwa, alishitakiwa kwa mwamuzi; na mwamuzi alitekeleza uwezo wake, na akawatuma askari ili yule mtu aletwe mbele yake; na akamhukumu yule mtu kulingana na sheria na ushahidi uliotolewa dhidi yake, na hivyo mtu huyo alilazimishwa kulipa deni lake, au avuliwe, au aondolewe miongoni mwa watu kama mwizi na mporaji.

3 Na mwamuzi alipokea kwa mshahara wake kulingana na wakati aliotumia—senina ya dhahabu kwa siku, au senumu ya fedha, ambayo ni sawa na senina ya dhahabu; na hii ni kulingana na sheria ambayo ilitolewa.

4 Sasa haya ndiyo majina ya vipande vyao tofauti vya dhahabu, na fedha zao, kulingana na thamani yao. Na majina yalitungwa na Wanefi, kwani hawakufuata mpango wa Wayahudi ambao walikuwa Yerusalemu; wala hawakupima kulingana na mpango wa Wayahudi; lakini walibadilisha vipimo vyao na mpango wao, kulingana na mawazo na hali ya watu, katika kila kizazi, hadi utawala wa waamuzi, ambao [a]waliimarishwa na mfalme Mosia.

5 Sasa mpango huo ulikuwa huu—senina ya dhahabu, seoni ya dhahabu, shumu ya dhahabu, na limnahi ya dhahabu.

6 Senumu ya fedha, amnori ya fedha, ezromu ya fedha, na onti ya fedha.

31 *a* Alma 11:20–36.

11 4 *a* Mos. 29:40–44.

7 Senumu ya fedha ilikuwa ni sawa na senina ya dhahabu, na zote zilikuwa ni sawa na kipimo kimoja cha shayiri, na pia kipimo cha kila aina ya nafaka.

8 Sasa kiasi cha seoni ya dhahabu kilikuwa na thamani mara mbili ya senina.

9 Na shumu ya dhahabu ilikuwa na thamani mara mbili ya seoni.

10 Na limnahi ya dhahabu ilikuwa na thamani ya hizo zote.

11 Na amnori ya fedha ilikuwa kuu kama senumu mbili.

12 Na ezromu ya fedha ilikuwa kuu kama senumu nne.

13 Na onti ilikuwa kuu kama hizo zote.

14 Sasa hivi ndivyo vipimo vya chini vya mpango wao—

15 Shibloni ni nusu ya senumu; kwa hivyo, shibloni moja kwa nusu kipimo cha shayiri.

16 Na shiblumu ni nusu ya shibloni.

17 Na lea ni nusu ya shiblumu.

18 Sasa hii ndiyo idadi yao, kulingana na mpango wao.

19 Sasa antioni ya dhahabu ilikuwa ni sawa na shibloni tatu.

20 Sasa, ilikuwa ni kwa lengo la kufaidika, kwa sababu walipokea mshahara wao kulingana na kazi yao, kwa hivyo, waliwachochea watu kufanya ghasia, na kila aina ya fujo na uovu, ili wapate kazi nyingi, ili [a]wapate pesa kulingana na kesi ambazo zililetwa mbele yao; kwa hivyo waliwachochea watu dhidi ya Alma na Amuleki.

21 Na huyu Zeezromu alianza kumhoji Amuleki, akisema: Je, utaweza kunijibu maswali machache ambayo nitakuuliza? Sasa Zeezromu alikuwa ni mtu aliyekuwa na ujuzi katika [a]mipango ya ibilisi, ili aangamize yale ambayo yalikuwa mema; kwa hivyo, akamwambia Amuleki: Utajibu maswali ambayo nitakuuliza?

22 Na Amuleki akamwaambia: Ndiyo, kama itakuwa kulingana na [a]Roho wa Bwana, aliye ndani yangu; kwani sitasema chochote ambacho ni kinyume cha roho wa Bwana. Na Zeezromu akamwambia: Tazama, hapa kuna onti sita za fedha, na nitakupa hizi zote ukikana uwepo wa Kiumbe Mkuu.

23 Sasa Amuleki alisema: Ewe [a]mtoto wa jehanamu, kwa nini [b]unanijaribu? Hujui kwamba wale wenye haki hawakubali majaribio kama haya?

24 Unaamini kwamba hakuna Mungu? Nakuambia, La, wewe unajua kwamba Mungu yupo, lakini unapenda [a]pesa zaidi yake.

25 Na sasa wewe umenidanganya mbele ya Mungu wangu. Unaniambia—Tazama hizi onti sita ambazo zina thamani kuu, nitakupatia—wakati ulikuwa umepanga moyoni mwako kuziweka kutoka kwangu; na ilikuwa ni haja yako tu kwamba mimi nimkane Mungu wa kweli na anayeishi, ili uwe na sababu ya kuniangamiza. Na

20*a* Alma 10:32.
21*a* Alma 10:13.
22*a* MWM Roho Mtakatifu.
23*a* Alma 5:41.
b MWM Jaribu, Majaribu.
24*a* 1 Tim. 6:10; Tit. 1:11.

sasa tazama, kwa sababu ya huu uovu mkuu utapokea upatanisho wako.

26 Na Zeezromu akamwambia: Wewe unasema kwamba kuna Mungu wa kweli na anayeishi?

27 Na Amuleki akasema: Ndiyo, kuna Mungu wa kweli na anayeishi.

28 Sasa Zeezromu akasema: Kuna zaidi ya Mungu mmoja?

29 Na akajibu, Hapana.

30 Sasa Zeezromu akamwambia tena: Unajuaje mambo haya?

31 Na akasema: [a]Malaika amenijulisha.

32 Na Zeezromu akasema tena: Ni nani atakayekuja? Ni Mwana wa Mungu?

33 Na akamwambia, Ndiyo.

34 Na Zeezromu akasema tena: Ataokoa watu wake [a]katika dhambi zao? Na Amuleki akajibu na kumwambia: Nakwambia kwamba hatafanya hivyo, kwani yeye hawezi kukana neno lake.

35 Sasa Zeezromu akawaambia watu: Hakikisha kwamba mnakumbuka hivi vitu; kwani alisema kwamba kuna Mungu mmoja pekee; na bado amesema kwamba Mwana wa Mungu atakuja, lakini kwamba hataokoa watu wake—kama vile alikuwa na mamlaka ya kumwamuru Mungu.

36 Sasa Amuleki akamwambia tena: Tazama umesema uwongo, kwani umesema kwamba nilizungumza kama vile nilikuwa na mamlaka ya kumwamuru Mungu kwa sababu nilisema kwamba hataokoa watu wake katika dhambi zao.

37 Na ninakwambia tena kwamba yeye hawezi kuwaokoa katika [a]dhambi zao; kwani siwezi kukanusha neno lake, na amesema kwamba [b]hakuna kitu chochote kichafu kitakachorithi [c]ufalme wa mbinguni; kwa hivyo, vipi mtakavyookolewa, msiporithi ufalme wa mbinguni? Kwa hivyo, hamwezi kuokolewa katika dhambi zenu.

38 Sasa Zeezromu akamwambia tena: Mwana wa Mungu ni yule Baba wa Milele?

39 Na Amuleki akamwambia: Ndiyo, yeye ndiye [a]Baba wa Milele wa mbingu na dunia, na vitu [b]vyote vilivyo ndani yao; yeye ndiye mwanzo na mwisho, wa kwanza na wa mwisho;

40 Na atakuja ndani ya [a]ulimwengu [b]kuwakomboa watu wake; na [c]atajitwaa dhambi za wale wanaoamini katika jina lake; na hawa ndiyo watakaopokea uzima wa milele, na wokovu hautamjia mwingine yeyote.

41 Kwa hivyo waovu wataishi

31 *a* Alma 10:7–10.
34 *a* Hel. 5:10–11.
37 *a* 1 Kor. 6:9–10.
b 1 Ne. 15:33; Alma 40:26; 3 Ne. 27:19.
MWM Sio mcha mungu.
c MWM Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni.
39 *a* Isa. 9:6.
b Kol. 1:16; Mos. 4:2.
40 *a* MWM Ulimwengu.
b Rum. 11:26–27.
c Ku. 34:6–7; Isa. 53:5; 1 Yoh. 2:2; Mos. 14:5; 15:12; M&M 19:16–19.

kama kwamba [a]hapakuweko na ukombozi, ila tu kufanywa huru kutokana na kamba za kifo; kwani tazama, siku inakuja ambayo [b]wote watafufuka kutoka kwa wafu na kusimama mbele ya Mungu, na [c]watahukumiwa kulingana na kazi zao.

42 Sasa, kuna kifo ambacho kinaitwa kifo cha muda; na kifo cha Kristo kitafungua [a]kanda za kifo hiki cha muda, ili wote wafufuliwe kutoka kifo hiki cha muda.

43 Roho na mwili [a]vitaungwa tena katika hali yake ya ukamilifu; viungo vyote vitarudishwa katika sehemu zao kamili, kama vile tulivyo sasa; na tutaletwa kusimama mbele ya Mungu, tukijua kama vile tujuavyo sasa, na [b]kukumbuka [c]hatia zetu zote.

44 Sasa, huu urejesho utakuwa kwa wote, wote wazee na vijana, wote wafungwa na huru, waume na wake, wote waovu na wenye haki; na hakuna hata unywele wa vichwa vyao utakaopotea; lakini kila kitu [a]kitarejeshwa mahali pake kamili, kama vile ilivyo sasa, au katika mwili, na utaletwa na kusimamishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo Mwana, na Mungu [b]Baba, na Roho Mtakatifu, ambao ni [c]Mungu mmoja wa Milele, [d]kuhukumiwa kulingana na vitendo vyao, kama ni vyema au ni viovu.

45 Sasa, tazama, nimekuzungumzia kuhusu kifo cha mwili huu wa muda, na pia kuhusu [a]ufufuo wa mwili huu wa muda. Ninakwambia kwamba mwili huu wa kufa [b]utafufuliwa na kwa mwili [c]usiokufa, yaani kutoka kifo, hata kufufuka kifo cha kwanza hadi katika uhai, kwamba [d]wasife tena; roho zao zikiungana na miili yao, wala hazitatenganishwa tena; hivyo mtu mzima atakuwa wa [e]kiroho na asiyekufa, kwamba hawataona uharibifu tena.

46 Sasa, Amuleki alipomaliza kuzungumza maneno haya watu walianza kustaajabia tena, na pia Zeezromu akaanza kutetemeka. Na hivyo maneno ya Amuleki yakamalizika, au haya ndiyo yote ambayo nimeandika.

MLANGO WA 12

Alma anaongea na Zeezromu—Siri za Mungu zinaweza kutolewa tu kwa wale ambao ni waaminifu—Wanadamu watahukumiwa kulingana na mawazo yao, imani, maneno, na vitendo—Waovu watateseka kwa kifo cha kiroho—Maisha haya katika mwili wenye kufa ni hali ya majaribio—Mpango

41 *a* Alma 12:18; M&M 88:33.
b Ufu. 20:12–13; Alma 42:23.
c MWM Hukumu ya mwisho.
42 *a* Alma 12:16.
43 *a* 2 Ne. 9:13; Alma 40:23.
b 2 Ne. 9:14; Mos. 3:25; Alma 5:18.
c MWM Hatia.
44 *a* Alma 41:12–15.
b MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.
c 3 Ne. 11:27, 36. MWM Mungu, Uungu.
d Ufu. 20:12–13.
45 *a* Alma 40:23; M&M 88:16.
b MWM Ufufuko.
c MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
d Ufu. 21:4; M&M 63:49; 88:116.
e 1 Kor. 15:44.

wa ukombozi huleta Ufufuo na, kwa kupitia imani, ondoleo la dhambi—Wale wanaotubu wana haki ya kupokea msamaha kupitia Mwana wa Pekee. Karibia mwaka 82 K.K.

Sasa Alma, alipoona kwamba maneno ya Amuleki yalimnyamazisha Zeezromu, kwani aliona kwamba Amuleki alimpata katika [a]uwongo wake na ujanja wake ili amwangamize, na alipoona kwamba alianza kutetemeka katika [b]dhamira yake ya hatia, alifungua kinywa chake na akaanza kumzungumzia, na kuimarisha maneno ya Amuleki, na kumwelezea mambo zaidi, au kuyafungua maandiko zaidi ya vile Amuleki alivyokuwa amefanya.

2 Sasa maneno ambayo Alma alimwelezea Zeezromu yalisikika na watu waliokuwa karibu; kwani umati ulikuwa mkuu, na alisema hivi:

3 Sasa Zeezromu, nikiona kwamba wewe umeshikwa katika uwongo na ujanja wako, kwani wewe hukudanganya watu pekee lakini wewe umemdanganya Mungu; kwani tazama, anajua [a]mawazo yako yote, na unaona kwamba mawazo yako yamefanywa kujulikana kwetu na Roho yake;

4 Na wewe unaona kwamba tunajua kuwa mpango wako ulikuwa ni mpango wa hila, kama hila ya ibilisi, kwani ulitaka kudanganya na kulaghai watu hawa ili uwafanye wawe dhidi yetu, na watufanyie dharau na kututupa nje—

5 Sasa huu ulikuwa ni [a]mpango wa adui wako, na ameitumia nguvu yake ndani yako. Sasa nataka ukumbuke kwamba yale ambayo ninakwambia pia nawaambia wote.

6 Na tazama nakwambia kwamba huu ulikuwa ni mtego wa adui, ambao ameutega ili awanase watu hawa, ili akutie katika utumwa wake, ili akuzingire na [a]minyororo yake, ili akufunge chini kwa maangamizo yasiyo na mwisho, kulingana na nguvu za utumwa wake.

7 Sasa Alma alipokuwa amezungumza maneno haya, Zeezromu alianza kutetemeka zaidi, kwani alisadikishwa zaidi kuhusu nguvu za Mungu; na pia alisadikishwa kwamba Alma na Amuleki walimfahamu, kwani alisadikishwa kwamba walijua mawazo na nia za moyo wake; kwani walipewa uwezo kwamba wajue vitu hivi kulingana na roho ya unabii.

8 Na Zeezromu akaanza kuwauliza kwa bidii, ili aweze kujua zaidi kuhusu ufalme wa Mungu. Na akamwambia Alma: Ni nini maana ya haya ambayo Amuleki amesema kuhusu ufufuo wa wafu, kwamba wote watafufuka kutoka kwa wafu, wenye haki na wasio na haki, na kwamba watasimamishwa mbele ya Mungu ili wahukumiwe kulingana na vitendo vyao?

12 1*a* Alma 11:20–38.
b MWM Dhamiri.
3*a* Yak. (KM) 2:5; Alma 10:17; M&M 6:16.
5*a* MWM Ibilisi.
6*a* Alma 5:7–10.

9 Na sasa Alma akaanza kumwelezea vitu hivi, akisema: Imepewa kwa wengi kujua [a]siri za Mungu; walakini wamewekwa chini ya amri kali kwamba hawatatoa zaidi ya yale maneno ambayo amewapatia watoto wa watu, kulingana [b]tu na utiifu na bidii ambayo wanampatia.

10 Na kwa hivyo, yule ambaye [a]atashupaza moyo wake, huyo atapokea sehemu [b]ndogo ya neno; na yule ambaye [c]hatashupaza moyo wake, huyo [d]anapewa sehemu kubwa ya neno, hadi awezeshwe kufahamu siri za Mungu hadi azielewe kikamilifu.

11 Na wale watakaoshupaza mioyo yao, wao watapewa [a]sehemu ndogo ya neno hadi [b]wasijue lolote kuhusu siri zake; na kisha wanatekwa nyara na ibilisi, na kuongozwa kwa pendekezo lake katika maangamizo. Sasa hii ndiyo maana ya [c]minyororo ya [d]jehanamu.

12 Na Amuleki amezungumza waziwazi kuhusu [a]mauti, na kufufuliwa kutoka hali hii ya muda hadi katika hali ya mwili usiokufa, na kusimamishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, [b]tuhukumiwe kulingana na vitendo vyetu.

13 Kisha kama mioyo yetu imeshupazwa, ndiyo, kama tumeshupaza mioyo yetu dhidi ya neno, kadiri kwamba halipo ndani yetu, hapo hali yetu itakuwa mbaya, kwani ndipo tutahukumiwa.

14 Kwani [a]maneno yetu yatatuhukumu, ndiyo, vitendo vyetu vyote vitatuhukumu; hatutakuwa bila waa; na pia mawazo yetu yatatuhukumu; na hatutaweza kumwangalia Mungu wetu katika hali hii mbaya; na tutakuwa na furaha kama tungeweza kuamuru miamba na [b]milima ituangukie ili [c]itufiche kutoka kwa uwepo wake.

15 Lakini hii haiwezekani; lazima tuje na kusimama mbele yake katika utukufu wake, na katika nguvu zake, na uwezo wake, fahari, na mamlaka, na kukubali kwa [a]aibu yetu isiyo na mwisho kwamba [b]hukumu zake zote ni za haki; kwamba yeye ni wa haki katika kazi zake zote, na kwamba yeye huwarehemu watoto wa watu, na kwamba ana nguvu zote za kumwokoa kila mtu ambaye anaamini kwa jina lake na kuzaa matunda ya toba.

16 Na sasa tazama, nawaambia ndipo [a]mauti yanakuja,

9*a* Alma 26:22.
MWM Siri za Mungu.
b Yn. 16:12; Alma 29:8; 3 Ne. 26:8–11; Eth. 4:7.
10*a* 2 Ne. 28:27; Eth. 4:8.
b M&M 93:39.
c MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
d 2 Ne. 28:30; M&M 50:24.
11*a* Mt. 25:29.
b MWM Ukengeufu.
c Yn. 8:34; 2 Ne. 28:19.
d Mit. 9:18; 2 Ne. 2:29.
MWM Jehanamu.
12*a* Alma 11:41–45.
b MWM Hukumu ya mwisho.
14*a* Mt. 12:36; Yak. (Bib.) 3:6; Mos. 4:29–30.
b Hos. 10:8; 2 Ne. 26:5.
c Ayu. 34:22; 2 Ne. 12:10.
15*a* Mos. 3:25.
b 2 Pet. 2:9.
MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
16*a* MWM Mauti ya Kiroho.

hata mauti ya pili, ambayo ni mauti ya kiroho; halafu itakuwa wakati kwamba yeyote atakayefariki katika dhambi zake, kama vile [b]mauti ya muda, [c]atakufa pia mauti ya kiroho; ndiyo, atafariki kulingana na vitu vya haki.

17 Kisha ndiyo wakati ambao mateso yao yatakuwa kama [a]ziwa la moto na kibereti, ambalo ndimi zake hupaa juu milele na milele; na kisha utakuwa wakati ambao watafungwa chini katika maangamizo yasiyo na mwisho, kulingana na nguvu na utumwa wa Shetani, yeye akiwa amewasalimisha kulingana na nia yake.

18 Kisha, nawaambia, watakuwa ni kama [a]hapakuwa na ukombozi uliofanywa; kwani hawawezi kukombolewa kulingana na haki ya Mungu; na hawawezi [b]kufa; kwani hakutakuwa na uharibifu;

19 Sasa ikawa kwamba baada ya Alma kumaliza kuzungumza maneno haya, watu walianza kustaajabika zaidi;

20 Lakini kulikuwa na mmoja ambaye aliitwa Antiona, ambaye alikuwa ni mtawala mkuu miongoni mwao, alikuja mbele na kumwambia: Ni nini hii ambayo umesema, kwamba mwanadamu atafufuliwa kutoka kwa wafu na kubadilishwa kutoka hii hali ya muda hadi katika hali ya mwili [a]usiokufa, kwamba nafsi haitakufa?

21 Maandiko yanamaanisha nini, ambayo yanasema kwamba Mungu aliweka [a]makerubi na upanga unaowaka moto mashariki mwa bustani ya [b]Edeni, isiwe wazazi wetu wa kwanza waingie na kula tunda la mti wa uzima, na kuishi milele? Na hivyo tunaona kwamba haikuwezekana kwamba wawe na nafasi ya kuishi milele.

22 Sasa Alma akamwambia: Hiki ndicho kitu ambacho nilikaribia kuelezea. Sasa tunaona kuwa Adamu [a]alianguka kwa kula [b]tunda lililokatazwa, kulingana na neno la Mungu; na hivyo tunaona, kwamba kwa kuanguka kwake, wanadamu wote wakawa watu [c]waliopotea na walioanguka.

23 Na sasa tazama, nakuambia kama ingewezekana Adamu [a]kula tunda la mti wa uzima wakati ule, hakungekuwa na mauti, na neno lingekuwa bure, na kumfanya Mungu mwongo, kwani alisema: [b]Iwapo utakula hakika utakufa.

24 Na tunaona kwamba mauti yanampata mwanadamu, ndiyo, [a]mauti ambayo yamezungumziwa na Amuleki, ambayo

16 *b* Alma 11:40–45.
c 1 Ne. 15:33; Alma 40:26.
17 *a* Ufu. 19:20; 21:8; Mos. 3:27.
18 *a* Alma 11:41.
b Ufu. 21:4; Alma 11:45; M&M 63:49.
20 *a* MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
21 *a* Mwa. 3:24; Alma 42:2; Musa 4:31. MWM Makerubi.
b MWM Edeni.
22 *a* MWM Anguko la Adamu na Hawa.
b Mwa. 3:6; 2 Ne. 2:15–19; Mos. 3:26.
c Mos. 16:4–5.
23 *a* Alma 42:2–9.
b Mwa. 2:17.
24 *a* MWM Mauti ya Kimwili.

ni mauti ya muda; walakini [b]mwanadamu alipewa nafasi ya kutubu; kwa hivyo maisha haya yakawa hali ya kujaribiwa; wakati wa [c]kujitayarisha kukutana na Mungu; wakati wa kujitayarisha kwa ile hali isiyo na mwisho ambayo imezungumziwa nasi, ambayo ni baada ya ufufuo wa wafu.

25 Sasa, kama hakungekuwa na [a]mpango wa ukombozi, ambao ulipangwa tangu msingi wa ulimwengu, hakungekuwa na [b]ufufuo wa wafu; lakini kulikuwa na mpango wa ukombozi ambao ulipangwa, ambao utawezesha ufufuo wa wafu, ambao tayari umezungumziwa.

26 Na sasa tazama, kama ingewezekana kwamba wazazi wetu wa kwanza wale kutoka kwa [a]mti wa uzima wangekuwa wenye taabu milele, bila kuwa na hali ya matayarisho; na hivyo [b]mpango wa ukombozi ungeangamizwa, na neno la Mungu lingekuwa bure, bila matokeo.

27 Lakini tazama, haikuwa hivyo; lakini [a]ilipangiwa kwamba lazima wanadamu wafariki; na baada ya kifo, lazima [b]wahukumiwe, hata hukumu ile ambayo tumeizungumzia, ambayo ni mwisho.

28 Na baada ya Mungu kupanga kwamba hivi vitu lazima vimpate mwanadamu, tazama, akaona kwamba ilikuwa inafaa mwanadamu ajue kuhusu vile vitu ambavyo alikuwa amewapangia;

29 Kwa hivyo aliwatuma [a]malaika wazungumze nao, ambao walisababisha wanadamu kuona utukufu wake.

30 Na wakaanza tangu wakati ule na kuendelea kuliita jina lake; kwa hivyo Mungu [a]alizungumza na wanadamu, na akawafahamisha [b]mpango wa ukombozi, ambao ulikuwa umetayarishwa tangu [c]msingi wa ulimwengu; na aliwafahamisha haya kulingana na imani yao na toba na vitendo vyao vitakatifu.

31 Kwa hivyo, akawapa wanadamu [a]amri, baada ya wao kuvunja amri za [b]kwanza zilizokuwa za vitu vya muda, na kuwa kama miungu, [c]wakifahamu mema na maovu, na kujiweka katika hali ya [d]kutenda, au kuwekwa katika hali ya kutenda kulingana na nia zao na furaha yao, kama kutenda maovu au kutenda mema—

32 Kwa hivyo Mungu aliwapa amri, baada ya [a]kuwafahamisha mpango wa ukombozi,

24 *b* 2 Ne. 2:21; Musa 5:8–12.
c Alma 34:32–35.
25 *a* MWM Mpango wa Ukombozi.
b 2 Ne. 2:8; Alma 7:12; 42:23.
26 *a* Mwa. 2:9; 1 Ne. 15:36; Alma 32:40.
b Alma 34:8–16; 42:6–28; Musa 6:59–62.
27 *a* Ayu. 7:1; Ebr. 9:27; M&M 42:48.
b MWM Hukumu ya mwisho.
29 *a* Moro. 7:25, 31; M&M 29:42.
30 *a* Musa 5:4–5; 6:51.
b MWM Mpango wa Ukombozi.
c Mos. 18:13; Alma 13:3, 5, 7–8.
31 *a* MWM Amri za Mungu.
b Mwa. 2:16–17; 2 Ne. 2:18–19.
c Mwa. 3:22–23; Musa 4:11.
d 2 Ne. 2:16. MWM Haki ya uamuzi.
32 *a* Musa 5:4–9.

ili wasitende maovu, adhabu yake ikiwa ni [b]mauti ya pili, ambayo ni mauti yasiyo na mwisho kulingana na vitu vya haki; kwani kama huo mpango wa ukombozi haungekuwa na nguvu, kwani vitendo vya [c]haki havingeweza kuangamizwa, kulingana na wema wa juu wa Mungu.

33 Lakini Mungu aliwaita wanadamu, kwa jina la Mwana wake, (huu ukiwa mpango wa ukombozi ambao ulikuwa umepangwa) akisema: Ikiwa mtatubu, na msishupaze mioyo yenu, nitawarehemu, kwa Mwana wangu wa Pekee;

34 Kwa hivyo, yeyote atakayetubu, na asishupaze moyo wake, atakuwa na haki ya kupokea [a]rehema kwa Mwana wangu wa Pekee, kwa [b]ondoleo la dhambi zake; na hawa wataingia katika [c]pumziko langu.

35 Na yeyote atakayeshupaza moyo wake na kutenda maovu, tazama, naapa katika ghadhabu yangu kwamba hataingia katika pumziko langu.

36 Na sasa, ndugu zangu, tazameni, nawaambia, kwamba ikiwa mtashupaza mioyo yenu hamtaingia katika pumziko la Bwana; kwa hivyo dhambi zenu zinamchokoza na kumfanya awateremshie ghadhabu yake kama vile alivyochokozwa mara ya [a]kwanza, ndiyo, kulingana na neno lake katika uchokozi wa mwisho na wa kwanza, kwa [b]maangamizo yasiyo na mwisho ya nafsi zenu; kwa hivyo, kulingana na neno lake, hadi kifo cha mwisho, na pia kile cha kwanza.

37 Na sasa, ndugu zangu, mkiona tunajua hivi vitu, na ni vya kweli, hebu tutubu, na tusishupaze mioyo yetu, kwamba [a]tusimkasirishe Bwana Mungu wetu akateremsha ghadhabu yake juu yetu katika amri zake za pili ambazo ametupatia; lakini hebu tuingie katika [b]pumziko la Mungu, ambalo limetayarishwa kulingana na neno lake.

MLANGO WA 13

Wanaume wanaitwa kama makuhani wakuu kwa sababu ya imani yao kuu na matendo mema—Watapaswa kufundisha amri—Kupitia haki wanatakaswa na kuingia katika pumziko la Bwana—Melkizedeki alikuwa mmoja wa hawa—Malaika wanatangaza habari njema kote nchini—Watatangaza ujio halisi wa Kristo. Karibia mwaka 82 K.K.

Na tena, ndugu zangu, ningetaka nikumbushe fikira zenu kuhusu ule wakati ambao Bwana Mungu aliwapatia watoto wake amri hizi; na ningetaka mkumbuke kwamba Bwana Mungu [a]aliwatawaza makuhani, kulingana na mpango wake mtakatifu, ambao ni ule mpango wa

32 *b* MWM Mauti ya Kiroho.
c Mos. 15:27; Alma 34:15–16; 42:15.
34 *a* MWM Rehema, enye Rehema.
b MWM Ondoleo la Dhambi.
c MWM Pumzika.
36 *a* Yak. (KM) 1:7–8; Alma 42:6, 9, 14.
b MWM Hukumu.
37 *a* 1 Ne. 17:30; Yak. (KM) 1:8; Hel. 7:18.
b Alma 13:6–9.
13 1 *a* Ibr. 2:9, 11.

Mwana wake, kufundisha watu vitu hivi.

2 Na makuhani hao walitawazwa kulingana na [a]mpango wa Mwana wake, katika [b]hali ambayo watu wangejua ni vipi watakavyomtumainia Mwana wake kwa ukombozi.

3 Na hivi ndivyo jinsi walivyotawazwa—[a]wakiitwa na [b]kutayarishwa tangu [c]msingi wa ulimwengu kulingana na [d]ufahamu wa mbeleni wa Mungu, kwa ajili ya imani yao kuu na vitendo vyao vyema; mwanzoni wakiruhusiwa [e]kuchagua baina ya mema na maovu; kwa hivyo wao wakiwa wamechagua mema, na kufanya mazoezi ya imani [f]kuu, [g]wameitwa kwa mwito mtakatifu, ndiyo, kwa ule mwito mtakatifu ambao ulitayarishwa, na kulingana na, matayarisho ya ukombozi wao.

4 Na hivyo [a]wameitwa kwa mwito huu mtakatifu kwa ajili ya imani yao, wakati wengine wangemkataa Roho wa Mungu kwa ajili ya ugumu wa mioyo yao na upofu wa fikira zao, wakati, kama isingekuwa kwa sababu hii wangekuwa na [b]mamlaka makuu kama ndugu zao.

5 Au kwa kifupi, hapo mwanzoni walikuwa katika hali [a]sawa na ndugu zao; hivyo mwito huu mtakatifu ukiwa umetayarishwa tangu msingi wa ulimwengu kwa wale ambao hawangeshupaza mioyo yao, kupitia na katika upatanisho wa Mwana wa Pekee, ambaye alitayarishwa—

6 Na hivyo kuitwa na mwito huu mtakatifu, na kutawazwa ukuhani mkuu wa mpango mtakatifu wa Mungu, kufundisha watoto wa watu amri zake, ili nao pia waingie katika [a]pumziko lake—

7 Ukuhani huu mkuu ukiwa kwa ule mpango wa Mwana wake, mpango ambao ulikuwa tangu msingi wa ulimwengu; au kwa maneno mengine, [a]hakukuwa na mwanzo wa siku au mwisho wa miaka, ukiwa ulitayarishwa tangu milele hadi milele, kulingana na [b]ufahamu wake wa mbele wa vitu vyote—

8 Sasa [a]walitawazwa kwa njia hii—wakiwa wameitwa kwa mwito mtakatifu, na kutawazwa kwa agizo takatifu, na kuchukua ukuhani mkuu juu yao wa mpango mtakatifu, ambao ni mwito, na agizo, na ukuhani mkuu, usio na mwanzo au mwisho—

9 Hivyo wakawa [a]makuhani wakuu milele, kulingana na mpango mtakatifu wa Mwana wa Pekee wa Baba, ambaye hana mwanzo wa siku au mwisho wa

2 *a* M&M 107:2–4.
b Alma 13:16.
3 *a* M&M 127:2.
MWM Uteuzi; Uteuzi kabla.
b M&M 138:55–56.
c Alma 12:25, 30.
MWM Maisha kabla ya kuzaliwa.
d M&M 38:2.
e MWM Haki ya uamuzi.
f MWM Amini, Imani.
g MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito; Ukuhani.
4 *a* Eth. 12:10.
b 1 Ne. 17:32–35.
5 *a* 2 Ne. 26:28.
6 *a* Alma 12:37; 16:17.
MWM Pumzika.
7 *a* Ebr. 7:3.
b MWM Mungu, Uungu.
8 *a* M&M 84:33–42.
MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
9 *a* MWM Kuhani Mkuu.

miaka, ambaye amejaa [b]neema, ukweli, na haki. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.

10 Sasa, kama vile nilivyosema kuhusu mpango huu mtakatifu, au huu [a]ukuhani mkuu, kulikuwa na wengi ambao walitawazwa na kuwa makuhani wakuu wa Mungu; na ilikuwa kwa ajili ya imani yao kuu na [b]toba, na haki yao mbele ya Mungu, wao wakichagua kutubu na kutenda haki badala ya kuangamia;

11 Kwa hivyo waliitwa kulingana na mpango huu mtakatifu, na [a]wakatakaswa, na [b]mavazi yao yakaoshwa na kuwa meupe kupitia damu ya Mwanakondoo.

12 Na wao, baada ya [a]kutakaswa na [b]Roho Mtakatifu, na mavazi yao kufanywa meupe, yakiwa [c]safi na bila doa mbele ya Mungu, hawangetazama [d]dhambi bila [e]kukerwa; na kulikuwa na wengi, wengi sana, ambao walifanywa safi na kuingia katika pumziko la Bwana Mungu wao.

13 Na sasa, ndugu zangu, ningetaka kwamba mjinyeyekeze mbele ya Mungu, na mzae [a]matunda yanayostahili toba, ili ninyi pia muingie katika hilo pumziko.

14 Ndiyo, jinyenyekeeni hata kama wale watu waliokuwa katika siku za [a]Melkizedeki, ambaye pia alikuwa kuhani mkuu kulingana na ule mpango ambao nimeuzungumzia, ambaye pia aliuchukua ukuhani mkuu milele.

15 Na ilikuwa ni kwa huyu Melkizedeki ambaye [a]Ibrahimu alilipa [b]zaka; ndiyo, hata baba yetu Ibrahimu alilipa zaka ya fungu la kumi ya mali yote aliyokuwa nayo.

16 Sasa haya [a]maagizo yalitolewa kwa namna hii, ili watu wamtazamie Mwana wa Mungu, ambayo ikiwa ni [b]mfano wa mpango wake, au ukiwa mpango wake, na ili wamtazamie mbele kwake kwa ondoleo la dhambi zao, ili waingie katika pumziko la Bwana.

17 Sasa huyu Melkizedeki alikuwa mfalme katika nchi ya Salemu; na watu wake walikuwa wametumbukia katika uovu na machukizo; ndiyo, wote walikuwa wamepotea njia; walikuwa wamejaa kila aina ya uovu;

18 Lakini Melkizedeki akiwa na imani kuu, na kuipokea ofisi ya ukuhani mkuu kulingana na [a]mpango mtakatifu wa Mungu, aliwahubiria watu wake toba. Na tazama, walitubu; na Melkizedeki aliimarisha amani nchini

9 *b* 2 Ne. 2:6.
MWM Neema.
10 *a* M&M 84:18–22.
b MWM Toba, Tubu.
11 *a* Musa 6:59–60.
b 1 Ne. 12:10; Alma 5:21–27; 3 Ne. 27:19–20.
12 *a* Rum. 8:1–9.
MWM Utakaso.
b MWM Roho Mtakatifu.
c MWM Safi na Isiyo safi.
d Mos. 5:2; Alma 19:33.
e Mit. 8:13; Alma 37:29.
13 *a* Lk. 3:8.
14 *a* TJS Mwa. 14:25–40 (Kiambatisho); M&M 84:14.
MWM Melkizedeki.
15 *a* MWM Ibrahimu.
b Mwa. 14:18–20; Mal. 3:8–10.
MWM Lipa zaka, Zaka.
16 *a* MWM Ibada.
b MWM Uashiriaji.
18 *a* MWM Ukuhani wa Melkizedeki.

katika siku zake; kwa hivyo alitwa mwana mfalme wa amani, kwani alikuwa mfalme wa Salemu; na alitawala chini ya baba yake.

19 Sasa, kulikuwa na [a]wengi mbele yake, na pia kulikuwa na wengi baadaye, lakini [b]hapakuwa na yeyote aliyekuwa mkuu zaidi; kwa hivyo, wamemtaja yeye zaidi.

20 Sasa hakuna haja ya kurudia jambo hili; yale ambayo nimesema yametosha. Tazama, [a]maandiko yako mbele yenu; [b]mkiyapinga itakuwa ni kwa maangamizo yenu.

21 Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kusema maneno haya kwao, alinyosha mkono wake kwao na kuongea kwa sauti kuu, akisema: Sasa ndiyo wakati wa [a]kutubu, kwani siku ya wokovu inakaribia;

22 Ndiyo, na sauti ya Bwana, kwa [a]mdomo wa malaika, inatangazia mataifa yote; ndiyo, inaitangaza, kwamba wawe na habari njema kuu ya shangwe kuu; ndiyo, anaitangaza habari hii njema miongoni mwa watu wake wote, ndiyo, hata kwa wale ambao wametawanyika kote usoni mwa dunia kwa hivyo wametujia.

23 Na wametufahamisha kwa misemo iliyo [a]wazi, ili tufahamu, ili tusikose; na hii ni kwa sababu sisi ni [b]wazururaji katika nchi ngeni; kwa hivyo, tumeheshimiwa zaidi, kwani tumeelezewa habari hii njema katika pande zote za shamba letu la mizabibu.

24 Kwani tazama, [a]malaika wanawatangazia wengi sasa katika nchi yetu; na hii ni kwa lengo la kutayarisha mioyo ya watoto wa watu ili wapokee neno lake atakaporudi katika utukufu wake.

25 Na sasa tunasubiri tu kusikia habari njema tukihubiriwa kwa mdomo wa malaika, kuhusa kuja kwake; kwani wakati unakuja, na [a]hatujui ni lini. Namwomba Mungu kwamba iwe katika siku zangu; lakini ikiwa sasa au baadaye, nitaifurahia.

26 Na itafahamishwa kwa watu wenye [a]haki na watakatifu, kwa mdomo wa malaika, wakati wa kuja kwake, kwamba maneno ya babu zetu yatimizwe, kulingana na yale ambayo waliyozungumza kumhusu, ambayo yalikuwa ni kulingana na roho ya unabii iliyokuwa ndani yao.

27 Na sasa, ndugu zangu, [a]natamani kutoka sehemu za ndani kabisa za moyo wangu, ndiyo, kwa wasiwasi mwingi na hata kwa uchungu, kwamba msikilize maneno yangu, na mtupe dhambi zenu, na kwamba msiahirishe siku ya toba yenu;

28 Lakini kwamba mtajinye-

19*a* Hel. 8:18; M&M 84:6–16; 107:40–55.
b M&M 107:1–4.
20*a* MWM Maandiko.
b 2 Pet. 3:16; Alma 41:1.
21*a* MWM Toba, Tubu.
22*a* Alma 10:20.
23*a* 2 Ne. 25:7–8; 31:3; 32:7; Yak. (KM) 4:13; Eth. 12:39.
b Yak. (KM) 7:26.
24*a* Alma 10:10; 39:19.
25*a* 1 Ne. 10:4; 3 Ne. 1:13.
26*a* Amo. 3:7; Lk. 2:8–11.
27*a* Mos. 28:3.

nyekeza mbele ya Bwana, na mliite jina lake takatifu, na [a]kukesha na kusali daima, kwamba [b]msijaribiwe zaidi ya yale ambayo mnaweza kuvumilia, na hivyo mwongozwe na Roho Mtakatifu, katika kuwa wanyenyekevu, [c]wapole, watiifu, wenye subira, wenye upendo na wenye uvumilivu;

29 [a]Mkimwamini Bwana; mkitumaini kwamba mtapokea uzima wa milele; mkiwa na [b]upendo wa Mungu daima katika mioyo yenu, kwamba muinuliwe katika siku ya mwisho na muingie katika [c]pumziko lake.

30 Na ikiwezekana Bwana awape toba, kwamba msijiteremshie ghadhabu yake, kwamba msifungiwe na minyororo ya [a]jehanamu, kwamba msipate [b]mauti ya pili.

31 Na Alma aliwazungumzia watu maneno mengi, ambayo hayajaandikwa katika kitabu hiki.

MLANGO WA 14

Alma na Amuleki wanafungwa na kupigwa—Waumini na maandiko yao matakatifu wanachomwa kwa moto—Bwana anawapokea mashahidi hawa kwa utukufu—Kuta za gereza zinapasuka na kuanguka—Alma na Amuleki wanakombolewa, na wadhalimu wao kuuawa. Karibia mwaka 82–81 K.K.

Na ikawa kwamba baada ya kumaliza kuzungumzia watu wengi wao waliamini maneno yake, na wakaanza kutubu, na kupekua [a]maandiko.

2 Lakini sehemu yao kubwa ilitaka kuwaangamiza Alma na Amuleki; kwani walimkasirikia Alma, kwa sababu ya vile alivyomzungumzia Zeezromu maneno [a]waziwazi; na pia walisema kwamba Amuleki alikuwa [b]amewadanganya, na alikuwa amedharau sheria yao na pia mawakili wao na waamuzi wao.

3 Na pia waliwakasirikia Alma na Amuleki; na kwa sababu waliwashuhudia uovu wao waziwazi, walitaka kuwaondoa kwa siri.

4 Lakini ikawa kwamba hawakufanya hivyo; lakini waliwachukua na kuwafunga kwa kamba imara, na kuwapeleka mbele ya mwamuzi mkuu wa nchi.

5 Na watu wakaenda na kushuhudia dhidi yao—wakishuhudia kwamba walikuwa wameidharau sheria, na mawakili wao na waamuzi wa nchi, na pia watu wote ambao walikuwa katika nchi; na pia wakashuhudia kwamba kuna Mungu mmoja pekee, na kwamba atamtuma Mwana wake miongoni mwa watu, lakini kwamba hatawaokoa; na watu waliwasingizia Alma na Amuleki vitu vingi kama hivi. Sasa

28 *a* MWM Kesha, Walinzi; Sala.
b 1 Kor. 10:13.
c MWM Pole, Upole; Subira.
29 *a* Alma 7:24.
b M&M 20:31; 76:116. MWM Hisani.
c M&M 84:24.
30 *a* MWM Hukumu; Jehanamu.
b MWM Mauti ya Kiroho.
14 1 *a* 2 Fal. 22:8–13. MWM Maandiko.
2 *a* Alma 12:3–7.
b Alma 10:27.

haya yalifanywa mbele ya mwamuzi mkuu wa nchi.

6 Na ikawa kwamba Zeezromu alishangazwa na maneno ambayo yalikuwa yamezungumzwa; na pia alijua kuhusu upofu wa mawazo, ambao alikuwa amesababisha miongoni mwa watu kwa maneno yake ya uwongo; na nafsi yake ikaanza [a]kukerwa na [b]dhamira yake kuhusu hatia zake; ndiyo, alianza kuzingirwa na uchungu wa jehanamu.

7 Na ikawa kwamba alianza kuwalilia watu, akisema: Tazameni, mimi nina [a]hatia, na watu hawa hawana lawama mbele ya Mungu. Na akaanza kuwatetea tangu wakati ule na kuendelea; lakini walimfanyia dharau, wakisema: Je, wewe nawe pia umepagawa na ibilisi? Na wakamtemea mate, na [b]kumtupa nje kutoka miongoni mwao, na pia wale wote ambao walikuwa wameamini maneno ambayo yalikuwa yamezungumzwa na Alma na Amuleki; na wakawatupa nje, na kutuma watu kuwapiga mawe.

8 Na wakawaleta wake na watoto wao pamoja, na yeyote aliyeamini au aliyekuwa amefundishwa kuliamini neno la Mungu walisababisha kwamba atupwe motoni; na pia walileta kumbukumbu zao zilizokuwa na maandiko, na kuyatupa motoni pia, ili yachomwe na kuangamizwa kwa moto.

9 Na ikawa kwamba waliwachukua Alma na Amuleki, na kuwabeba na kuwapeleka mahali pa mateso, ili washuhudie wale ambao waliangamizwa kwa kuchomwa kwa moto.

10 Na Amuleki alipoona wanawake na watoto wakiungua kwenye moto, na yeye pia alipatwa na maumivu; na akamwambia Alma: Kwa nini tunashuhudia mkasa huu mwovu? Kwa hivyo tunyooshe mikono yetu, na tutumie [a]nguvu za Mungu tulizo nazo, na tuwaokoe kutoka ndimi za moto.

11 Lakini Alma akamwambia: Roho inanizuia kwamba nisinyooshe mkono wangu; kwani tazama Bwana mwenyewe anawapokea, kwa [a]utukufu; na anakubali wafanye kitu hiki, au kwamba watu wafanye kitu hiki kwao, kulingana na ugumu wa mioyo yao, ili [b]hukumu ambayo atawateremshia katika ghadhabu yake iwe ya haki; na [c]damu ya wale ambao hawana [d]hatia itakuwa ushahidi dhidi yao, ndiyo, na italia sana dhidi yao katika siku ya mwisho.

12 Sasa Amuleki akamwambia Alma: Tazama, pengine watatuchoma sisi pia.

13 Na Alma akasema: Hebu na iwe kulingana na nia ya Bwana. Lakini, tazama, kazi yetu haijakwisha; kwa hivyo hawawezi kutuchoma.

14 Sasa ikawa kwamba baada

6 *a* Alma 15:5.
b MWM Dhamiri.
7 *a* Alma 11:21–37.
b Alma 15:1.
10 *a* Alma 8:30–31.
11 *a* MWM Utukufu.
b Zab. 37:8–13; Alma 60:13; M&M 103:3. MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
c MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
d Mos. 17:10.

ya miili ya wale ambao walikuwa wametupwa motoni kuungua, na pia yale maandishi ambayo yalikuwa yametupwa pamoja nao, mwamuzi mkuu wa nchi alikuja na kusimama mbele ya Alma na Amuleki, wakiwa wamefungwa; na akawapiga makofi katika mashavu yao, na kuwaambia: Baada ya yale ambayo mmeona, bado mtahubiria watu hawa, kwamba watatupwa katika [a]ziwa la moto na kiberiti?

15 Tazama, mnaona kwamba hamkuwa na uwezo wa kuwaokoa wale ambao walikuwa wametupwa motoni; wala Mungu hakuwaokoa kwa sababu walikuwa wa imani yenu. Na mwamuzi akawapiga tena katika mashavu yao, na kuwauliza: Je, mna nini cha kujisemea?

16 Sasa huyu mwamuzi alikuwa mfuasi wa dini na imani ya [a]Nehori, ambaye alimuua Gideoni.

17 Na ikawa kwamba Alma na Amuleki hawakumjibu chochote; na akawapiga tena, na akawakabidhi kwa polisi ili watupwe gerezani.

18 Na walipokuwa wametupwa gerezani kwa siku tatu, kulitokea [a]mawakili wengi, na waamuzi, na makuhani, na walimu, ambao walikuwa waumini wa Nehori; na walikuja gerezani kuwaona, na kuwauliza maswali kuhusu maneno mengi; lakini hawakuwajibu lolote.

19 Na ikawa kwamba mwamuzi alisimama mbele yao, na kusema: Kwa nini hamjibu maneno ya watu hawa? Hamjui kwamba nina uwezo wa kuwatupa kwenye moto? Na akawaamuru wazungumze; lakini hawakujibu lolote.

20 Na ikawa kwamba waliondoka na kwenda zao, lakini walirudi kesho yake; na yule mwamuzi pia akawapiga tena katika mashavu yao. Na wengi walikuja pia, na kuwapiga, wakisema: Je, mtasimama tena na kuhukumu watu hawa, na kushutumu sheria yetu? Kama mnao uwezo huu mkuu kwa nini [a]hamjiokoi?

21 Na waliwaambia vitu vingi kama hivi, wakiwasagia meno yao, na kuwatemea mate, na kusema: Tutakuwa je tukilaaniwa?

22 Na vitu vingi kama hivi, ndiyo, kila aina ya vitu hivi waliwaambia; na hivyo wakawafanyia mzaha kwa siku nyingi. Na waliwanyima chakula ili wapate njaa, na maji ili wapate kiu; na pia waliwavua nguo zao ili wawe uchi; na hivyo walifungwa kwa kamba imara, na kuzuiliwa gerezani.

23 Na ikawa kwamba baada ya wao kuteseka siku nyingi, (na iliikuwa ni siku ya kumi na mbili, mwezi wa kumi, katika mwaka wa kumi wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi) kwamba mwamuzi mkuu katika nchi ya Amoniha na wengi wa walimu wao na mawakili wao walikwenda gerezani

14*a* Alma 12:17.
16*a* Alma 1:7–15.
18*a* Alma 10:14; 11:20.
20*a* Mt. 27:39–43.

ambamo Alma na Amuleki walikuwa wamefungwa kwa kamba.

24 Na mwamuzi mkuu akasimama mbele yao, na kuwapiga tena, na kuwaambia: Kama mnazo nguvu za Mungu jikomboeni kutoka kwa kamba hizi, na kisha tutaamini kwamba Bwana atawaangamiza hawa watu kulingana na maneno yenu.

25 Na ikawa kwamba wote walienda na kuwapiga, na kuyarudia yale maneno, hata hadi yule wa mwisho; na wakati yule wa mwisho aliwazungumzia [a]nguvu za Mungu zikawateremkia Alma na Amuleki, na wakainuka na kusimama kwa miguu yao.

26 Na Alma akalia, na akisema: Ni kwa muda gani ambao tutateseka kwa [a]masumbuko haya makuu, Ee Bwana? Ee Bwana, tupatie nguvu kulingana na imani yetu katika Kristo, ambayo itatukomboa. Na wakakata kamba ambazo walikuwa wamefungwa nazo; na wakati watu walipoona haya, walianza kutoroka, kwani woga wa kuagamizwa uliwajia.

27 Na ikawa kwamba woga wao ulikuwa mwingi hata kwamba wakainama kwenye ardhi, na hawakuufikia mlango wa nje wa [a]gereza; na ardhi ikatetemeka sana, na kuta za gereza zikabomolewa na kuwa sehemu mbili, na hivyo zikaanguka kwenye ardhi; na yule mwamuzi mkuu, na mawakili, na makuhani, na walimu, wale ambao walikuwa wamewapiga Alma na Amuleki, waliuawa katika ule mwanguko.

28 Na Alma na Amuleki wakaondoka gerezani, na hawakuumizwa; kwani Bwana alikuwa amewapatia uwezo, kulingana na imani yao katika Kristo. Na wakatoka gerezani moja kwa moja; na [a]wakafunguliwa kamba zao; na gereza ilikuwa imeanguka kwenye ardhi, na kila nafsi ambayo ilikuwa ndani ya zile kuta, ila tu Alma na Amuleki, waliuawa; na wakaingia moja kwa moja kwenye mji.

29 Sasa baada ya watu kusikia kelele nyingi walikuja mbio kwa makundi ili wajue chanzo chake; na walipoona Alma na Amuleki wakitoka nje ya gereza, na kwamba kuta zake zilikuwa zimeanguka kwenye ardhi, walipatwa na woga mwingi, na wakakaimbia kutoka uwepo wa Alma na Amuleki hata kama vile mbuzi na wana mbuzi wake wakimbiavyo simba wawili; na hivyo walikimbia kutoka uwepo wa Alma na Amuleki.

MLANGO WA 15

Alma na Amuleki wanaenda Sidomu na kuanzisha kanisa—Alma anamponya Zeezromu, ambaye anajiunga na Kanisa—Wengi wanabatizwa, na Kanisa

25*a* Alma 8:31.
26*a* Yak. (Bib.) 5:10–11; Mos. 17:10–20; M&M 121:7–8.
27*a* Mdo. 16:26; Eth. 12:13.
28*a* Yak. (KM) 4:6; 3 Ne. 28:19–22.

linafanikiwa—Alma na Amuleki wanaenda Zarahemla. Karibia mwaka 81 K.K.

Na ikawa kwamba Alma na Amuleki waliamriwa waondoke kutoka ule mji; na wakaondoka, na kufika hata katika nchi ya Sidomu; na tazama, kule waliwapata watu wote ambao walikuwa wametoka nchi ya [a]Amoniha, na ambao walikuwa [b]wametupwa nje na kupigwa kwa mawe, kwa sababu walikuwa wameamini maneno ya Alma.

2 Na wakawaelezea yale yote ambayo yalikuwa yamefanyika kwa [a]wake na watoto wao, na pia kuwahusu wao wenyewe, na [b]nguvu za ukombozi.

3 Na pia Zeezromu aliugua huko Sidomu, kwa homa kali, ambayo ilisababishwa na masumbuko mengi akilini mwake kwa sababu ya [a]uovu wake, kwani alidhani kwamba Alma na Amuleki walikuwa hawako tena; na alidhani kwamba walikuwa wameuliwa kwa sababu ya uovu wake. Na dhambi hii kubwa, na dhambi zake zingine nyingi, zilimsumbua katika mawazo yake hadi zikawa kama vidonda vikubwa, kwani hakuwa na ukombozi; kwa hivyo aliaanza kuchomwa kwa joto kali.

4 Sasa, aliposikia kwamba Alma na Amuleki walikuwa katika nchi ya Sidomu, moyo wake ulianza kupata ujasiri; na akawatumia ujumbe mara moja, akihitaji wamtembelee.

5 Na ikawa kwamba walikwenda mara moja, kwani walitii ule ujumbe ambao alikuwa amewatumia; na wakaenda ndani ya nyumba ya Zeezromu; na wakamkuta kitandani mwake, akiwa mgonjwa, akiwa mnyonge kwa homa kali; na alikuwa na maumivu mengi katika akili yake kwa sababu ya maovu yake; na alipowaona, aliunyosha mkono wake, na kuwasihi kwamba wamponye.

6 Na ikawa kwamba Alma alimwambia, akimchukua kwa mkono wake: Je, [a]unaziamini nguvu za wokovu za Kristo?

7 Na akajibu kwa kusema: Ndiyo, ninaamini maneno yote ambayo mmefundisha.

8 Na Alma akasema: Kama unaamini katika ukombozi wa Kristo wewe unaweza [a]kuponywa.

9 Na akasema: Ndiyo, ninaamini kulingana na maneno yako.

10 Na ndipo Alma akamlilia Bwana, na kusema: Ee Bwana Mungu wetu, mrehemu mtu huyu, na [a]umponye kulingana na imani yake ambayo iko katika Kristo.

11 Na Alma aliposema maneno haya, Zeezromu [a]aliinuka kwa miguu yake, na kuanza kutembea; na hii ilifanywa kwa mshangao wa watu wote; na

15 1*a* Alma 16:2–3, 9, 11.
b Alma 14:7.
2*a* Alma 14:8–14.
b Alma 14:28.
3*a* Alma 14:6–7.
6*a* Mk. 9:23.
8*a* MWM Ponya, Uponyaji.
10*a* Mk. 2:1–12.
11*a* Mdo. 3:1–11.

kitendo hiki kilijulikana kote katika nchi ya Sidomu.

12 Na Alma akambatiza Zeezromu katika Bwana; na akaanza tangu wakati ule na kuendelea kuwahubiria watu.

13 Na Alma alianzisha kanisa katika nchi ya Sidomu, na akawaweka makuhani na walimu wakfu katika nchi, wabatize yeyote aliyetaka kubatizwa katika Bwana.

14 Na ikawa kwamba walikuwa wengi; kwani walikusanyika kutoka sehemu zote za Sidomu, na wakabatizwa.

15 Lakini kwa watu waliokuwa katika nchi ya Amoniha, bado walibaki na mioyo migumu na shingo ngumu; na hawakutubu dhambi zao, wakifikiria nguvu za Alma na Amuleki kuwa za ibilisi; kwani walikuwa wafuasi wa dini ya [a]Nehori, na hawakuamini katika kutubu dhambi zao.

16 Na ikawa kwamba Alma na Amuleki, Amuleki akiwa [a]ameiacha dhahabu yake yote, na fedha, na vitu vyake vya thamani, vilivyokuwa katika nchi ya Amoniha, kwa neno la Mungu, yeye [b]akikataliwa na wale ambao walikuwa marafiki zake kitambo, na pia na baba yake na jamaa yake;

17 Kwa hivyo, baada ya Alma kuimarisha kanisa katika Sidomu, na kuona [a]zuio kuu, ndiyo, akiona kwamba watu walizuiliwa kutokana na kiburi kilichokuwa katika mioyo yao, na wakaanza [b]kunyenyekea mbele ya Mungu, na wakaanza kujikusanya pamoja katika makao yao matakatifu [c]kumwabudu Mungu mbele ya madhabahu, wakiwa [d]waangalifu na wakiomba daima, kwamba wakombolewe kutokana na Shetani, na kutoka [e]kifo, na kutoka maangamizo—

18 Sasa kama nilivyosema, baada ya Alma kuona hivi vitu vyote, kwa hivyo alimchukua Amuleki na kuvuka katika nchi ya Zarahemla, na akampeleka katika nyumba yake mwenyewe, na kumhudumia katika mateso yake, na kumtia nguvu katika Bwana.

19 Na hivyo mwaka wa kumi wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi uliisha.

MLANGO WA 16

Walamani wanawaangamiza watu wa Amoniha—Zoramu anawaongoza Wanefi kuwashinda Walamani—Alma na Amuleki na wengine wengi wanahubiri neno—Wanafundisha kwamba baada ya Ufufuko Wake Kristo atawatokea Wanefi. Karibia mwaka 81–77 K.K.

Na ikawa kwamba katika mwaka wa kumi na moja wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, katika siku ya tano mwezi wa pili, baada ya kuwepo na amani nyingi katika nchi ya Zarahemla,

15 *a* Alma 1:2–15.
16 *a* Lk. 14:33; Alma 10:4.
b MWM Mateso, Tesa.
17 *a* Alma 16:21.
b MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
c MWM Kuabudu.
d MWM Kesha, Walinzi; Sala.
e MWM Mauti ya Kiroho.

kukiwa hakuna vita au mabishano kwa muda wa miaka kadhaa, hata hadi siku ya tano ya mwezi wa pili katika mwaka wa kumi na moja, mlio wa vita ulisikika kote katika nchi.

2 Kwani tazama, majeshi ya Walamani yalikuwa yameingia mipakani mwa nchi, kutoka upande wa nyika, hata katika mji wa [a]Amoniha, na wakaanza kuwaua watu na kuangamiza ule mji.

3 Na sasa ikawa kwamba, kabla ya Wanefi kuunda jeshi la kutosha kuwaondoa katika nchi, walikuwa [a]wameangamiza watu ambao walikuwa katika mji wa Amoniha, na pia wengine katika mipaka ya Nuhu, na kuwachukua wengine mateka huko nyikani.

4 Sasa ikawa kwamba Wanefi walitamani kuwakomboa wale ambao walikuwa wamepelekwa utumwani huko nyikani.

5 Kwa hivyo, yule ambaye alikuwa amechaguliwa kapteni mkuu wa majeshi ya Wanefi, (na jina lake lilikuwa Zoramu, na alikuwa na wana wawili, Lehi na Aha)—sasa Zoramu na wanawe wawili, wakijua kwamba Alma alikuwa kuhani mkuu juu ya kanisa, na wakiwa wamesikia kwamba alikuwa na roho ya unabii, kwa hivyo walimwendea wakitaka kujua kama Bwana alitaka kwamba waende nyikani kutafuta ndugu zao, ambao walikuwa wamefanywa watumwa na Walamani.

6 Na ikawa kwamba Alma [a]alimwuliza Bwana kuhusu jambo hilo. Na Alma akarejea na kuwaambia: Tazama, Walamani watavuka mto Sidoni kusini mwa nyika, mbali na mipaka ya nchi ya Manti. Na tazama mtakutana nao kule, mashariki mwa mto Sidoni, na kule ndipo Bwana atawakomboa ndugu zenu waliofanywa watumwa na Walamani.

7 Na ikawa kwamba Zoramu na wanawe walivuka mto wa Sidoni, na majeshi yao, na wakasafiri mbali na mipaka ya Manti kusini mwa nyika, ambayo ilikuwa upande wa mashariki wa mto wa Sidoni.

8 Na wakayafikia majeshi ya Walamani, na Walamani walitawanywa na kupelekwa nyikani; na wakachukua ndugu zao ambao walikuwa wamewekwa utumwani na Walamani, na hakukuwa na hata nafsi moja iliyopotea miongoni mwa wale ambao waliwekwa utumwani. Na wakaletwa na ndugu zao kumiliki nchi zao.

9 Na hivyo mwaka wa kumi na moja wa waamuzi ulikwisha, baada ya Walamani kuondolewa nchini, na watu wa Amoniha [a]waliangamizwa; ndiyo, kila nafsi iliyo hai ya Waamoniha [b]iliangamizwa, na pia mji wao mkuu, ambao walisema Mungu hangeweza kuuangamiza, kwa sababu ya ukubwa wake.

10 Lakini tazama, katika siku [a]moja ilifanywa kuwa ukiwa;

16 2*a* Alma 15:1, 15–16.
3*a* Alma 9:18.
6*a* Alma 43:23–24.
9*a* Alma 8:16; 9:18–24; Morm. 6:15–22.
b Alma 25:1–2.
10*a* Alma 9:4.

na maiti wakaliwa na mbwa na wanyama wa mwitu wa nyika.

11 Walakini, baada ya siku nyingi maiti wao walirundikwa usoni mwa ardhi, na wakafunikwa kwa mchanga mdogo. Na uvundo ulikuwa mwingi sana hata kwamba watu hawakuingia kumiliki nchi ya Amoniha kwa miaka mingi. Na uliitwa Ukiwa wa Wanehori; kwani walikuwa wafuasi wa [a]Nehori, ambao waliuawa; na nchi zao zikabaki na ukiwa.

12 Na Walamani hawakuja tena kupigana vita na Wanefi hadi mwaka wa kumi na nne wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi. Na hivyo kwa miaka mitatu watu wa Nefi walikuwa na amani katika nchi yote.

13 Na Alma na Amuleki wakaenda na kuhubiri toba kwa watu katika [a]mahekalu yao, na mahali pao patakatifu, na pia katika [b]masinagogi yao, ambayo yalikuwa yamejengwa kulingana na desturi za Wayahudi.

14 Na kadiri wengi waliosikiliza maneno yao, kwao walifundisha neno la Mungu, bila [a]ubaguzi wa watu, daima.

15 Na hivyo Alma na Amuleki waliendelea mbele, na pia wengi ambao walikuwa wamechaguliwa kwa ile kazi, kuhubiri neno kote nchini. Na uwekaji wa kanisa ukaenea kote nchini, katika sehemu zote za nchi, miongoni mwa watu wote wa Wanefi.

16 Na [a]hakukuwa na ukosefu wa usawa miongoni mwao; Bwana aliteremsha Roho wake juu ya uso wa nchi ili kutayarisha mawazo ya watoto wa watu, au kutayarisha [b]mioyo yao kupokea neno ambalo lingefundishwa miongoni mwao wakati wa kuja kwake—

17 Ili wasishupazwe dhidi ya neno, ili wasikose kuamini, na kwenda katika maangamizo, lakini kwamba wapokee neno kwa shangwe, na kama [a]tawi waunganishwe na ule [b]mizabibu wa kweli, ili waweze kuingia katika [c]pumziko la Bwana Mungu wao.

18 Sasa wale [a]makuhani ambao walienda miongoni mwa watu walihubiri kinyume cha uwongo wote, na [b]udanganyifu, na [c]wivu, na vita, na dharau, na matusi, na wizi, unyang'anyi, uporaji, mauaji, uzinzi, na kila aina ya matusi, wakisema kwamba hivi vitu havistahili kuwa hivyo—

19 Na kuwaelezea vitu ambavyo vitakuja; ndiyo, kuwaelezea kuhusu [a]kuja kwa Mwana wa Mungu, mateso yake na kifo chake, na pia ufufuo wa wafu.

20 Na watu wengi waliuliza kuhusu mahali pale ambapo

11 *a* Alma 1:15; 24:28–30.
13 *a* 2 Ne. 5:16.
b Alma 21:4–6, 20.
14 *a* Alma 1:30.
16 *a* Mos. 18:19–29; 4 Ne. 1:3.
b MWM Moyo Uliovunjika.
17 *a* Yak. (KM) 5:24.
b MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
c Alma 12:37; 13:10–13.
18 *a* Alma 15:13.
b MWM Danganya, Kudanganya, Udanganyifu.
c MWM Husuda.
19 *a* MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.

Mwana wa Mungu atakuja; na walifundishwa kwamba [a]atawatokea [b]baada ya ufufuo wake; na watu waliyapokea haya kwa shangwe kuu na furaha.

21 Na sasa baada ya kanisa kuanzishwa kote nchini—baada ya kupata [a]ushindi juu ya ibilisi, na neno la Mungu likihubiriwa katika usafi wake kote nchini, na Bwana akiwateremshia watu baraka zake—na hivyo mwaka wa kumi na nne wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi ulikwisha.

Historia ya wana wa Mosia, ambao walizikataa haki zao za kumiliki ufalme kwa ajili ya neno la Mungu, na wakaenda mpaka nchi ya Nefi kuwahubiria Walamani; mateso yao na ukombozi wao—kulingana na maandishi ya Alma.

Yenye milango ya 17 hadi 27.

MLANGO WA 17

Wana wa Mosia wana roho ya unabii na ufunuo—Wanaenda njia zao mbalimbali na kuwahubiria Walamani neno—Amoni anaenda katika nchi ya Ishmaeli na kuwa mtumishi wa mfalme Lamoni—Amoni anaokoa mifugo ya mfalme na kuwauwa maadui wake katika maji ya Sebo. Aya ya 1 hadi ya 3, karibia mwaka 77 K.K.; aya ya 4, karibia mwaka 91–77 K.K.; na aya ya 5 hadi 39, karibia mwaka 91 K.K.

Na sasa ikawa kwamba wakati Alma alipokuwa anasafiri kutoka nchi ya Gideoni iliyo kusini, mbali kwa nchi ya Manti, tazama, kwa mshangao wake, [a]alikutana na [b]wana wa Mosia wakielekea nchi ya Zarahemla.

2 Sasa hawa wana wa Mosia walikuwa na Alma ule wakati ambao malaika alimtokea mara ya [a]kwanza; kwa hivyo Alma alijawa shangwe alipowaona ndugu zake; na lile ambalo liliongezea furaha yake, ni kwamba walikuwa bado ndugu zake katika Bwana; ndiyo, na walikuwa wameongezwa nguvu kwa ufahamu wa ukweli; kwani walikuwa watu ambao wana ufahamu mwema na walikuwa [b]wameyapekua maandiko kwa bidii, ili wajue neno la Mungu.

3 Lakini haya sio yote; kwani walikuwa wamejitoa kwa [a]sala, na kufunga; kwa hivyo walikuwa na roho ya unabii, na roho ya ufunuo, na [b]walipofundisha, walifundisha kwa uwezo na mamlaka ya Mungu.

4 Na walikuwa wamefundisha neno la Mungu kwa muda wa miaka kumi na nne miongoni mwa Walamani, wakiwa [a]wamefanikiwa sana [b]kuwaleta wengi katika ufahamu wa ukweli;

20 *a* 2 Ne. 26:9; 3 Ne. 11:7–14.
b 1 Ne. 12:4–6.
21 *a* Alma 15:17.
17 1 *a* Alma 27:16.
b Mos. 27:34.
2 *a* Mos. 27:11–17.
b MWM Maandiko.
3 *a* MWM Funga, Kufunga; Sala.
b MWM Fundisha, Mwalimu—Kufundisha kwa Roho.
4 *a* Alma 29:14.
b MWM Kazi ya kimisionari.

ndiyo, kwa uwezo wa maneno yao wengi walisimama mbele ya madhabahu ya Mungu, ili wamlingane na [c]kutubu dhambi zao mbele yake.

5 Sasa hii ndiyo hali ambayo iliwapata katika safari yao, kwani walipata masumbuko mengi; waliteseka sana, katika mwili na mawazo, kama vile njaa, kiu na uchovu, na pia [a]kazi katika roho.

6 Sasa hizi ndizo zilikuwa safari zao: Baada ya [a]kupata ruhusa kwa baba yao, Mosia, katika mwaka wa kwanza wa waamuzi; baada ya [b]kukataa ufalme ambao baba yao alitamani kuwakabidhi, na pia hii ndiyo ilikuwa katika mawazo ya watu;

7 Walakini waliondoka kutoka nchi ya Zarahemla, na wakachukua panga zao, na mikuki yao, na pinde zao, na mishale yao, na kombeo zao; na walifanya haya ili wajitafutie chakula wakiwa huko nyikani.

8 Na hivyo wakaelekea nyikani pamoja na umati ambao walikuwa wameuchagua, ili waende katika nchi ya Nefi, kuwahubiria Walamani neno la Mungu.

9 Na ikawa kwamba walisafiri kwa siku nyingi nyikani, na wakafunga sana na [a]kuomba sana kwamba Bwana angewapatia sehemu ya roho yake ili iende pamoja nao, na kuishi nao, ili wawe [b]chombo mikononi mwa Mungu kuwaleta kama ingewezekana, ndugu zao, Walamani, wawafahamishe, kuhusu ufahamu wa ukweli, na ufahamu wa uovu wa [c]mila za babu zao, ambazo hazikuwa za haki.

10 Na ikawa kwamba Bwana [a]aliwatembelea kwa [b]Roho wake, na kuwaambia: Pateni [c]faraja. Na wakafarijika.

11 Na Bwana akawaambia pia: Nendeni miongoni mwa Walamani, ndugu zenu, na muimarishe neno langu; walakini mtakuwa wenye [a]subira kwa uvumilivu na mateso, kwamba muwatolee mfano mwema ndani yangu, na nitawafanya muwe chombo katika mikono yangu cha kuokoa nafsi nyingi.

12 Na ikawa kwamba mioyo ya wana wa Mosia, na pia wale ambao walikuwa nao, ilijipatia ujasiri wa kwenda kwa Walamani na kuwatangazia neno la Mungu.

13 Na ikawa kwamba walipofika katika mipaka ya nchi ya Walamani, [a]walijigawanya na kuachana, wakimwamini Bwana kwamba watakutana tena baada ya [b]mavuno yao; kwani walidhani kwamba walikuwa na kazi kubwa sana.

14 Na kwa hakika ilikuwa kubwa, kwani walikuwa wamechukua jukumu la kuhubiri neno la Mungu kwa watu [a]wakaidi na wagumu na wakali;

4 *c* MWM Kiri, Kukiri.
5 *a* Alma 8:10.
6 *a* Mos. 28:1, 5–9.
b Mos. 29:3.
9 *a* Alma 25:17.
MWM Sala.
b Mos. 23:10; Alma 26:3.
c Alma 3:10–12.
10 *a* M&M 5:16.
b MWM Roho Mtakatifu.
c Alma 26:27.
11 *a* Alma 20:29.
MWM Subira.
13 *a* Alma 21:1.
b Mt. 9:37.
14 *a* Mos. 10:12.

watu ambao walifurahia kuwaua Wanefi, na kuwanyang'anya na kuwapora; na mioyo yao ilikuwa katika utajiri, au katika dhahabu na fedha, na mawe ya thamani; lakini walitafuta kupata hivi vitu kwa kuua na unyang'anyi, ili wasijichoshe kupata kwa mikono yao.

15 Na hivyo walikuwa watu wavivu, wengi wao wakiabudu sanamu, na [a]laana ya Mungu iliwateremkia kwa sababu ya [b]mila za babu zao; ingawa walikuwa wamenyooshewa ahadi za Bwana wakitubu.

16 Kwa hivyo, hili ndilo lilikuwa [a]lengo ambalo wana wa Mosia walikuwa wamejitakia kazi, ili pengine wawalete katika toba; ili pengine waweze kuwafahamisha kuhusu mpango wa ukombozi.

17 Kwa hivyo walijigawanya mmoja kutoka kwa mwingine, na wakaenda miongoni mwao, kila mtu peke yake, kulingana na nguvu za Mungu ambazo alipewa.

18 Sasa Amoni akiwa kiongozi miongoni mwao, kwa usahihi zaidi aliwahudumia, na akaondoka kutoka kwao, baada ya [a]kuwabariki kulingana na vyeo vyao tofauti, baada ya kuwazungumzia neno la Mungu, au kuwabariki kabla ya kuondoka kwake; na hivyo wakaanza safari zao kadha kote nchini.

19 Na Amoni alikwenda katika nchi ya Ishmaeli, kwani nchi hiyo ilitungwa baada ya wana wa [a]Ishmaeli, ambao pia nao walibadilika na kuwa Walamani.

20 Na wakati Amoni alipoingia katika nchi ya Ishmaeli, Walamani walimchukua na kumfunga, kama ilivyokuwa desturi yao ya kuwafunga Wanefi wote walioangukia mikononi mwao, na kuwapeleka mbele ya mfalme; na hivyo ilikuwa ni juu ya mfalme kuwaua, au kuwafanya watumwa, au kuwatupa gerezani, au kuwafukuza kutoka nchi yake, kulingana na nia yake na matakwa yake.

21 Na hivyo Amoni alipelekwa mbele ya mfalme aliyekuwa juu ya nchi ya Ishmaeli; na jina lake lilikuwa Lamoni; na alikuwa wa uzao wa Ishmaeli.

22 Na mfalme akamwuliza Amoni kama alitaka kuishi katika nchi miongoni mwa Walamani, au miongoni mwa watu wake.

23 Na Amoni akamwambia: Ndiyo, natamani kuishi miongoni mwa watu hawa kwa muda; ndiyo, na pengine hadi siku ile nitakapoaga dunia.

24 Na ikawa kwamba mfalme Lamoni alifurahishwa sana na Amoni, na akaamuru kwamba kamba zake zifunguliwe; na akataka kwamba Amoni amchukue mmoja wa mabinti zake awe mke wake.

25 Lakini Amoni akamwambia: La, lakini nitakuwa mtumishi wako. Kwa hivyo Amoni akawa mtumishi wa mfalme

15 *a* Alma 3:6–19; 3 Ne. 2:15–16.
b Alma 9:16–24; 18:5.

16 *a* Mos. 28:1–3.

18 *a* MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.

19 *a* 1 Ne. 7:4–6.

Lamoni. Na ikawa kwamba alipewa kazi ya kuchunga mifugo ya Lamoni pamoja na watumishi wengine, kulingana na desturi ya Walamani.

26 Na baada ya kuwa katika utumishi wa mfalme kwa siku tatu, alipokuwa na watumishi wa Kilamani wakipeleka mifugo yao mahali pa maji, ambapo paliitwa maji ya Sebo, na Walamani wote walikuwa wakileta mifugo yao hapa, ili inywe maji—

27 Kwa hivyo, wakati Amoni na watumishi wa mfalme walipokuwa wakipeleka mifugo yao mahali hapo pa maji, tazama, kikundi fulani cha Walamani, ambacho kilikuwa kimeleta mifugo yao kwenye maji, kilisimama na kutawanya mifugo ya Amoni na watumishi wa mfalme, na wakawatawanya hadi wakatorokea njia nyingi.

28 Sasa watumishi wa mfalme wakaanza kunung'unika, wakisema: Sasa mfalme atatuua, kama alivyowaua ndugu zetu kwa sababu mifugo yao ilitawanywa kwa uovu wa watu hawa. Na wakaanza kulia sana, wakisema: Tazama, mifugo yetu tayari imetawanywa.

29 Sasa walilia kwa sababu ya woga wa kuuawa. Sasa Amoni alipoona haya moyo wake ulifurahi sana ndani yake kwa sababu ya shangwe; kwani, alisema, nitawafunulia hawa watumishi wenzangu nguvu zangu, au nguvu iliyo ndani yangu, katika kumrejeshea mfalme mifugo hii, ili niweze kupendeza mioyo ya hawa watumishi wenzangu, ili waweze kuamini maneno yangu.

30 Na sasa, haya ndiyo yalikuwa mawazo ya Amoni, alipoona mateso ya wale ambao aliwaita ndugu zake.

31 Na ikawa kwamba aliwafanyia utani kwa maneno yake, na kusema: Ndugu zangu, jitieni moyo na twende tukatafute mifugo, na tutaikusanya pamoja na tuilete katika mahali penye maji; na hivyo tutaihifadhi mifugo ya mfalme na hatatuua.

32 Na ikawa kwamba walienda kutafuta ile mifugo, na wakamfuata Amoni, na wakaenda kwa kasi kubwa na kuikusanya mifugo ya mfalme, na kuirudisha tena mahali penye maji.

33 Na watu wale wakataka kuitawanya ile mifugo tena; lakini Amoni akawaambia ndugu zake: Izingireni mifugo ili isitawanyike; na nitakwenda na kukabiliana na hawa watu wanaotawanya mifugo yetu.

34 Kwa hivyo, wakafanya vile Amoni alivyowaamuru, na akaenda na kukabiliana na wale ambao walisimama karibu na maji ya Sebo; na idadi yao haikuwa ndogo.

35 Kwa hivyo hawakumwogopa Amoni, kwani walidhani kwamba mmoja wa watu wao angemuua kulingana na furaha yao, kwani hawakujua kwamba Bwana alikuwa amemwahidi Mosia kwamba "angewakomboa wanawe kutoka mikononi mwao; wala hawakujua chochote kumhusu Bwana; kwa

35*a* Mos. 28:7; Alma 19:22–23.

hivyo walifurahia maangamizo ya ndugu zao; na kwa sababu hii walisimama kuitawanya mifugo ya mfalme.

36 Lakini [a]Amoni akasimama na akaanza kuwatupia mawe kwa kombeo yake; ndiyo, alitupa mawe kwa nguvu nyingi miongoni mwao; na [b]akawaua wengi wao hadi wakaanza kustaajabishwa na nguvu yake; walakini walikasirishwa kwa sababu ya ndugu zao waliokuwa wameuawa, na walikata kauli kwamba lazima aanguke; kwa hivyo, wakiona kwamba [c]hawakuweza kumgonga kwa mawe, walimjia kwa rungu zao ili wamuue.

37 Lakini tazama, kila mtu aliyeinua rungu lake kumgonga Amoni, alikata mikono yao kwa upanga wake; kwani alizuia mapigo yao kwa kukata mikono yao kwa ncha ya upanga wake, hadi kwamba wakaanza kustaajabia, na wakaanza kukimbia; ndiyo, na idadi yao haikuwa ndogo; na akawasababisha wakimbie kwa nguvu za mkono wake.

38 Sasa sita ya wao waliangushwa kwa kombeo, lakini hakuwaua wengine isipokuwa kiongozi wao kwa upanga wake; na alikata mikono ya wengi walioinua mikono yao kumpiga; na hawakuwa wachache.

39 Na wakati alipokuwa amewakimbiza, alirudi na kunywesha mifugo yao maji na kuirudisha katika malisho ya mfalme, na kumwendea mfalme, wakibeba mikono ile ambayo ilikuwa imekatwa kwa upanga wa Amoni, ya wale ambao walijaribu kumuua; na ikapelekwa mbele ya mfalme kama ushahidi wa vitu ambavyo walikuwa wamefanya.

MLANGO WA 18

Mfalme Lamoni anawaza kwamba Amoni ni Roho Mkuu—Amoni anamfundisha mfalme kuhusu Uumbaji, matendo ya Mungu kwa wanadamu, na kuhusu ukombozi unaokuja kwa njia ya Kristo—Lamoni anaamini na kuanguka chini kana kwamba amekufa. Karibia mwaka 90 K.K.

Na ikawa kwamba mfalme Lamoni alisababisha kwamba watumishi wake wasimame na washuhudie kuhusu vitu vyote walivyokuwa wameviona kuhusu jambo lile.

2 Na wote walipokuwa wameshuhudia vitu ambavyo walikuwa wameona, na alikuwa amejulishwa vile Amoni alivyokuwa mwaminifu katika kuhifadhi mifugo yake, na pia kwa nguvu zake kuu za kukabiliana na wale ambao walitaka kumuua, alistaajabu sana, na kusema: Kwa kweli, huyu ni zaidi ya mwanadamu. Tazama, si huyu ndiye Roho Mkuu anawateremshia watu hawa adhabu kwa sababu ya mauaji yao?

3 Na wakamjibu mfalme, na kusema: Hatujui kama yeye ndiye ile Roho Kuu, au mwanadamu; lakini tunajua haya, kwamba [a]hawezi kuuawa na

36*a* Eth. 12:15.
b Alma 18:16.
c Alma 18:3.
18 3*a* Alma 17:34–38.

maadui wa mfalme; wala hawawezi kutawanya mifugo ya mfalme akiwa pamoja na sisi, kwa sababu ya uhodari wake na nguvu zake kuu; kwa hivyo tunajua kwamba yeye ni rafiki wa mfalme. Na sasa, Ee mfalme, hatuamini kwamba mwanadamu anazo nguvu kama hizo, kwani tunajua kwamba hawezi kuuawa.

4 Na sasa, mfalme aliposikia maneno haya, aliwaambia: Sasa ninajua kwamba ni Roho Mkuu; na ameshuka chini wakati huu kuhifadhi maisha yenu, ili [a]nisiwaue vile nilivyowafanya ndugu zenu. Sasa huyu ndiye Roho Mkuu ambaye babu zetu walimzungumzia.

5 Sasa hii ndiyo ilikuwa desturi ya Lamoni, ambayo alikuwa amepokea kutoka kwa baba yake, kwamba kulikuwa na [a]Roho Mkuu. Ingawa waliamini katika Roho Mkuu, bado walidhani kwamba yoyote ambayo walitenda yalikuwa ni sawa; walakini, Lamoni alianza kuogopa sana, na aliogopa kwamba alikuwa ametenda mabaya kwa kuwaua watumishi wake;

6 Kwani alikuwa ameua wengi wao kwa sababu ndugu zao walikuwa wametawanya mifugo yao mahali pa maji; na hivyo, kwa sababu mifugo yao ilitawanywa waliuawa.

7 Sasa ilikuwa ni desturi ya Walamani hawa kusimama karibu na maji ya Sebo kutawanya mifugo ya watu, wafukuze wale wengi ambao walikuwa wametawanywa katika nchi yao, hii ikiwa ni desturi yao ya kupora miongoni mwao.

8 Na ikawa kwamba mfalme Lamoni aliwauliza watumishi wake, akisema: Yuko wapi huyu mtu ambayo ana uwezo kama huu mkuu?

9 Na wakamwambia: Tazama, analisha farasi wako. Sasa mfalme alikuwa amewaamuru watumishi wake, kabla ya kupeleka mifugo kunywa maji, kwamba watayarishe farasi wake na magari yale yanayovutwa, na wamsindikize hadi nchi ya Nefi; kwani kulikuwa na sherehe kubwa iliyoandaliwa katika nchi ya Nefi, na baba ya Lamoni, ambaye alikuwa mfalme katika nchi yote.

10 Sasa wakati mfalme Lamoni aliposikia kwamba Amoni alikuwa anatayarisha farasi wake na magari yake yanayovutwa alistaajabu zaidi, kwa sababu ya uaminifu wa Amoni, akisema: Kwa hakika hakuna mtumishi mwingine miongoni mwa watumishi wangu ambaye amekuwa mwaminifu kama mtu huyu; kwani hata anakumbuka kutii amri zangu zote na kuzitekeleza.

11 Sasa kwa hakika najua kwamba huyu ndiye Roho Mkuu, na ninatamani kwamba aje ndani kwangu, lakini sithubutu.

12 Na ikawa kwamba wakati Amoni alipomaliza kutayarisha farasi na magari ya mfalme na watumishi wake, alimwendea mfalme, na akaona kwamba uso wa mfalme ulikuwa ume-

4*a* Alma 17:28–31. | 5*a* Alma 19:25–27. | MWM Mungu, Uungu.

badilika; kwa hivyo alikaribia kuondoka katika uwepo wake.

13 Na mtumishi mmoja wa mfalme akamwambia, Rabana, ambayo, tafsiri yake, ni mwenye nguvu au mfalme mkuu, wakifikiria wafalme wao kuwa wenye nguvu; na hivyo akamwambia: Rabana, mfalme anataka ukae.

14 Kwa hivyo Amoni akamgeukia mfalme, na kumwambia: Ni nini unachotaka nikufanyie, Ee mfalme? Na mfalme hakumjibu kwa muda wa saa moja, kulingana na wakati wao, kwani hakujua la kumwambia.

15 Na ikawa kwamba Amoni alimwambia tena: Nini unahitaji kwangu? Lakini mfalme hakumjibu.

16 Na ikawa kwamba Amoni, akiwa amejawa na Roho wa Mungu, kwa hivyo alihisi [a]mawazo ya mfalme. Na akamwambia: Ni kwa sababu umesikia kwamba niliwakinga watumishi wako na mifugo yako, na kuwaua ndugu zao saba kwa kombeo na upanga, na kukata mikono ya wengine, ili kulinda mifugo yako na watumishi wako; tazama, ni haya ndiyo yanayosababisha kushangaa kwako?

17 Nakwambia, ni nini, ambacho kimefanya mshangao wako uwe mkuu? Tazama, mimi ni mwanadamu, na mimi ni mtumishi wako; kwa hivyo, chochote utakachotaka ambacho ni chema, nitatenda.

18 Sasa wakati mfalme aliposikia maneno haya, alishangaa tena, kwani aliona kwamba Amoni angeweza [a]kupambanua mawazo yake; lakini licha ya haya, mfalme Lamoni alifungua kinywa chake, na kumwambia: Wewe ni nani? Wewe ni yule Roho Mkuu, [b]anayejua vitu vyote?

19 Amoni akamjibu na kumwambia: Mimi siye.

20 Na mfalme akasema: Vipi unajua mawazo ya moyo wangu? Unaweza kuzungumza kwa ujasiri, na uniambie kuhusu vitu hivi; na pia uniambie ni kwa nguvu gani uliwaua na kukata mikono ya ndugu zangu ambao waliotawanya mifugo yangu—

21 Na sasa, kama utanielezea kuhusu vitu hivi, chochote utakachoniuliza nitakupa; na kama itahitajika, nitakulinda na majeshi yangu; lakini najua kwamba wewe una nguvu kuliko hao wote; walakini, chochote unacho kitaka nitakupa.

22 Sasa Amoni akiwa mwenye hekima, lakini mpole, alimwambia Lamoni: Utasikiliza maneno yangu, nikikuelezea ni kwa nguvu gani ninafanya vitu hivi? Na hiki ndicho kitu ambacho ninataka kutoka kwako.

23 Na mfalme akamjibu, na kusema: Ndiyo, nitaamini maneno yako yote. Na hivyo akanaswa kwa werevu.

24 Na Amoni akaanza kumzungumzia kwa [a]ujasiri, na akamwambia: Unaamini kwamba Mungu yupo?

25 Na akamjibu, na kusema: Mimi sijui maana ya hayo.

16*a* Alma 12:3.
18*a* MWM Utambuzi,
Kipawa cha.
b MWM Mungu, Uungu.
24*a* Alma 38:12.

26 Na kisha Amoni akasema: Unaamini kwamba kuna Roho Mkuu?

27 Na akasema, Ndiyo.

28 Na Amoni akasema: Huyu ndiye Mungu. Na Amoni akamwambia tena: Unaamini kwamba huyu Roho Mkuu, ambaye ni Mungu, aliumba vitu vyote vilivyo mbinguni na duniani?

29 Na akasema: Ndiyo, naamini kwamba aliumba vitu vyote vilivyo ulimwenguni; lakini si juu mbinguni.

30 Na Amoni akamwambia: Mbinguni ni mahali ambapo Mungu anaishi pamoja na malaika wake wote watakatifu.

31 Na mfalme Lamoni akasema: Iko juu ya ulimwengu?

32 Na Amoni akasema: Ndiyo, na anatazama chini kwa binadamu wote; na anafahamu [a]mawazo yote na nia zote za moyo; kwani kwa mkono wake, wote waliumbwa kutoka mwanzo.

33 Na mfalme Lamoni akasema: Naamini vitu hivi vyote ambavyo umezungumza. Wewe umetumwa kutoka kwa Mungu?

34 Amoni akamwambia: Mimi ni mwanadamu; na hapo mwanzo [a]mwanadamu aliumbwa kwa mfano wa Mungu, na nimeitwa na Roho Mtakatifu wake ili [b]niwafundishe watu hawa vitu hivi, ili waweze kujua yale yaliyo ya haki na kweli;

35 Na sehemu ya [a]Roho huyo anaishi ndani yangu, ambaye hunipatia [b]ufahamu, na pia uwezo kulingana na imani yangu na nia iliyo katika Mungu.

36 Sasa baada ya Amoni kusema maneno haya, alianzia tangu kuumbwa kwa ulimwengu, na pia kuumbwa kwa Adamu, na kumwambia vitu vyote kuhusu kuanguka kwa mwanadamu, na [a]kumwelezea na kumfunulia maandishi na [b]maandiko ya watu, ambayo yalikuwa yamezungumzwa na [c]manabii, hata hadi ule wakati ambao baba yao, Lehi, alipotoka Yerusalemu.

37 Na pia akawasimulia (kwani ilikuwa kwa mfalme na watumishi wake) safari zote za babu zao huko nyikani, na mateso yao yote ya njaa na kiu, na mateso yao, na kadhalika.

38 Na pia akawasimulia kuhusu maasi ya Lamani na Lemueli, na wana wa Ishmaeli, ndiyo, aliwaeleza kuhusu maasi yao yote; na akawaelezea maandishi na maandiko yote tangu ule wakati ambao Lehi aliondoka Yerusalemu hadi ule wakati wa sasa.

39 Lakini haya sio yote; kwani aliwaelezea kuhusu [a]mpango wa ukombozi, ambao ulitayarishwa tangu msingi wa ulimwengu; na pia akawaelezea kuhusu kuja kwa Kristo, na aliwajulisha kuhusu matendo yote ya Bwana.

32*a* Amo. 4:13; 3 Ne. 28:6; M&M 6:16.
34*a* Mos. 7:27; Eth. 3:13–16.
b MWM Fundisha, Mwalimu—Kufundisha kwa Roho.
35*a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi.
b MWM Maarifa.
36*a* Mos. 1:4; Alma 22:12; 37:9.
b MWM Maandiko.
c Mdo. 3:18–21.
39*a* MWM Mpango wa Ukombozi.

40 Na ikawa kwamba baada yake kusema vitu hivi vyote, na kumwelezea mfalme, kwamba mfalme aliamini maneno yake yote.

41 Na akaanza kumlilia Bwana, akisema: Ee Bwana, nihurumie; kulingana na [a]rehema zako tele ambazo umewaonyesha watu wa Nefi, nihurumie mimi, na watu wangu.

42 Na sasa, baada ya kusema haya, alianguka ardhini, kama vile alikuwa amekufa.

43 Na ikawa kwamba watumishi wake walimchukua na kumpeleka kwa mke wake, na wakamlaza kitandani; na akalala kama aliyekufa kwa muda wa siku mbili na kucha mbili; na mke wake, na wanawe, na mabinti zake walimwomboleza, kama ilivyokuwa desturi ya Walamani, wakiomboleza sana kifo chake.

MLANGO WA 19

Lamoni anapokea nuru ya uzima usio na mwisho na kumwona Mkombozi—Nyumba yake yote inaota ndoto, na wengi waona malaika—Amoni anahifadhiwa kiajabu—Anabatiza wengi na kuimarisha kanisa miongoni mwao. Karibia mwaka 90 K.K.

Na ikawa kwamba baada ya siku mbili usiku na mchana walikaribia kuchukua mwili wake na kuuzika kaburini, ambalo walikuwa wametayarisha kwa kusudi la kuzika wafu wao.

2 Sasa malkia akiwa amesikia sifa za Amoni, kwa hivyo alituma na akataka kwamba aje kwake.

3 Na ikawa kwamba Amoni alifanya vile alivyoamriwa, na akamwendea malkia, na akahitaji kujua yale aliyotaka atende.

4 Na akamwambia: Watumishi wa bwana wangu wamenijulisha kwamba wewe ni [a]nabii wa Mungu mtakatifu, na kwamba wewe una uwezo wa kutenda vitendo vikuu katika jina lake;

5 Kwa hivyo, kama hivi ndivyo ilivyo, ningetaka uende na umwone bwana wangu, kwani amelazwa kitandani mwake kwa muda wa siku mbili na kucha mbili; na wengine wanasema kwamba hajafariki, lakini wengine wanasema kwamba amefariki na kwamba ananuka, na kwamba anastahili kuzikwa kaburini; lakini kwangu mimi, hanuki.

6 Sasa, hili ndilo Amoni alilotaka, kwani alijua kwamba mfalme Lamoni alikuwa chini ya nguvu za Mungu; alijua kwamba [a]pazia la giza ya kutoamini lilikuwa limeondolewa mawazoni mwake, na [b]nuru ile ambayo iliangaza mawazo yake, ambayo ilikuwa ni nuru ya utukufu wa Mungu, ambayo ilikuwa ni nuru ya ajabu ya wema wake—ndiyo, nuru hii ilikuwa imejaza nafsi yake na shangwe, wingu la giza likiwa limeondolewa, na kwamba nuru ya uzima usio na mwisho ya Kristo.

41 *a* MWM Rehema, enye Rehema.
19 4 *a* MWM Nabii.
6 *a* 2 Kor. 4:3–4. MWM Pazia.
b MWM Nuru, Nuru

ilikuwa imewashwa katika nafsi yake, ndiyo, alijua kwamba mwili wake ulikuwa umelemewa na haya, na alikuwa amebebwa na Mungu—

7 Kwa hivyo, yale malkia aliyohitaji yalikuwa ni matakwa yake. Kwa hivyo, akaenda ndani kumwona mfalme kama vile malkia alivyomhitajia; na alimwona mfalme, na alijua kwamba hajafariki.

8 Na akamwambia malkia: Yeye hajafariki, lakini amelala katika Mungu, na kesho atainuka tena; kwa hivyo usimzike.

9 Na Amoni akamwambia: Wewe unaamini haya? Na akamwambia: Sijapata ushahidi mwingine ijapokuwa neno lako, na neno la watumishi wetu; walakini naamini kwamba itakuwa kulingana na yale ambayo umesema.

10 Na Amoni akamwambia: Wewe umebarikiwa kwa sababu ya imani yako nyingi; nakwambia wewe, mwanamke, hakujawahi kuwa na [a]imani kuu kama hii miongoni mwa Wanefi.

11 Na ikawa kwamba alilinda kitanda cha bwana wake, tangu wakati ule hadi kesho yake ule wakati ambao Amoni alikuwa amepanga kwamba atainuka.

12 Na ikawa kwamba aliinuka, kulingana na maneno ya Amoni; na alipoinuka, alinyosha mkono wake kwa mwanamke wake, na kusema: Jina la Mungu libarikiwe, na wewe umebarikiwa.

13 Kwani kwa hakika kama vile unavyoishi, tazama, nimemwona Mkombozi wangu; na atakuja, na [a]atazaliwa na [b]mwanamke, na atakomboa wanadamu wote ambao wanaamini jina lake. Sasa, aliposema maneno haya, moyo wake ulifura tena ndani yake, na akazama tena kwa shangwe; na malkia pia akazama, akiwa amelemewa na Roho.

14 Sasa Amoni akiona kwamba Roho wa Bwana aliteremshwa kulingana na [a]sala zake kwa Walamani, ndugu zake, ambao walikuwa wamesababisha maombolezo makuu miongoni mwa Wanefi, au miongoni mwa watu wote wa Mungu kwa sababu ya maovu yao na [b]mila zao, alipiga magoti, na akaanza kutoa nafsi yake kwa sala na kumshukuru Mungu kwa roho yake yote kwa sababu ya yale yote ambayo alikuwa amewatendea ndugu zake; na pia alilemewa na [c]shangwe; na hivyo wote watatu walikuwa [d]wameanguka ardhini.

15 Sasa, wakati watumishi wa mfalme walipoona kwamba walikuwa wameinama, nao pia walianza kumlilia Mungu, kwani woga wa Bwana ulikuwa umewaingia nao pia, kwani [a]wao ndiyo walikuwa wamesimama mbele ya mfalme na

10*a* Lk. 7:9.
MWM Amini, Imani.
13*a* MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.
b 1 Ne. 11:13–21.
14*a* M&M 42:14.
b Mos. 1:5.
c MWM Shangwe.
d Alma 27:17.
15*a* Alma 18:1–2.

kumshuhudia kuhusu nguvu kuu za Amoni.

16 Na ikawa kwamba waliliita jina la Bwana, kwa uwezo wao wote, hadi wote wakaanguka ardhini, isipokuwa tu mwanamke mmoja wa Kilamani, ambaye jina lake lilikuwa Abishi, ambaye alikuwa amemgeukia Bwana kwa muda wa miaka mingi, iliyotokana na ono la kushangaza la baba yake—

17 Hivyo, baada ya kumgeukia Bwana, na hakuwa amewahi kumjulisha yeyote, kwa hivyo, alipoona kwamba watumishi wote wa Lamoni walikuwa wameanguka ardhini, na pia bibi yake, malkia, na mfalme, na Amoni kwamba walikuwa wamelala katika ardhi kifudifudi, alijua kwamba ni uwezo wa Mungu; na akidhani kwamba nafasi hii, kwa kufahamisha watu kuhusu yale yaliyokuwa yametendeka miongoni mwao, kwamba kwa kuona kisa hiki [a]itawasababishia kuamini kwa nguvu za Mungu, kwa hivyo akakimbia kutoka nyumba kwa nyumba, akiwafahamisha watu.

18 Na walianza kukusanyika wenyewe pamoja katika nyumba ya mfalme. Na ulikaja umati mkubwa, na kwa mmfalme mshangao wao wakaona mfalme wao, na malkia, na watumishi wao wamelala kifudifudi ardhini, na wote walikuwa wamelala pale kama vile walikuwa wamekufa; na pia wakamwona Amoni, na tazama, alikuwa Mnefi.

19 Na sasa watu wakaanza kunung'unika miongoni mwao; baadhi wakisema kwamba ulikuwa uovu mkubwa uliokuwa umewateremkia, au juu ya mfalme na nyumba yake, kwa sababu alikuwa ameruhusu Mnefi anapaswa [a]kuishi katika nchi ile.

20 Lakini wengine waliwakemea, wakisema: Mfalme ameteremshia nyumba yake uovu huu, kwa sababu aliwaua watumishi wake ambao mifugo yao ilitawanywa katika [a]maji ya Sebo.

21 Na pia walikemewa na wale watu ambao walikuwa wamesimama katika maji ya Sebo na [a]kutawanya mifugo ya mfalme, kwani walimkasirikia Amoni kwa sababu ya idadi ambayo alikuwa ameua ya ndugu zao katika maji ya Sebo, alipokuwa akilinda mifugo ya mfalme.

22 Sasa, mmoja wao, ambaye kaka yake alikuwa [a]ameuawa kwa upanga wa Amoni, akiwa amemkasirikia Amoni sana, alitoa upanga wake ili amwangushie Amoni, amuue; na alipoinua upanga wake ili amkate, tazama, alianguka chini na kufariki.

23 Sasa tunaona kwamba Amoni hangeuawa, kwani [a]Bwana alikuwa amemwambia Mosia, baba yake: Nitamhifadhi, na itakuwa juu yake kulingana na

17 *a* Mos. 27:14.
19 *a* Alma 17:22–23.
20 *a* Alma 17:26; 18:7.
21 *a* Alma 17:27; 18:3.
22 *a* Alma 17:38.
23 *a* Mos. 28:7; Alma 17:35.

imani yako—kwa hivyo, Mosia [b]alimtumainia Bwana.

24 Na ikawa kwamba ule umati ulipoona kwamba yule mtu alikuwa ameanguka na kufariki, aliyekuwa ameinua upanga kumuua Amoni, woga uliwapata wote, na hawakuthubutu kuweka mikono yao kwake au kwa wale ambao walikuwa wameanguka; na wakaanza tena kustaajabu miongoni mwao ni nini kilichosababisha nguvu hizi kuu, au maana ya vitu hivi vyote.

25 Na ikawa kwamba kulikuwa na wengi miongoni mwao waliosema kwamba Amoni alikuwa ni yule [a]Roho Mkuu, na wengine wakasema kwamba ametumwa na Roho Mkuu;

26 Lakini wengine waliwakemea wote, wakisema kwamba alikuwa ni jitu, ambalo lilikuwa limetumwa na Wanefi kuwatesa.

27 Na kulikuwa na wengine ambao walisema kwamba Amoni alikuwa ametumwa na yule Roho Mkuu kuwatesa kwa sababu ya maovu yao; na kwamba ilikuwa ni yule Roho Mkuu aliyekuwa anawasaidia Wanefi daima, ambaye alikuwa amewakomboa kutoka mikononi mwao; na wakasema kwamba ni huyu Roho Mkuu ambaye alikuwa amewaangamiza ndugu zao wengi, Walamani.

28 Na hivyo ubishi ukazidi kuwa mkali miongoni mwao. Na walipokuwa wakibishana, yule mtumishi [a]mwanamke ambaye alikuwa amesababisha umati ukusanyike pamoja alifika, na alipoona ule ubishi uliokuwa miongoni mwa umati alihuzunika sana, hadi akalia machozi.

29 Na ikawa kwamba alienda na kumchukua malkia kwa mkono wake, ili pengine amuinue kutoka ardhini; na alipougusa mkono wake aliinuka na kusimama kwa miguu yake, na kulia kwa sauti kubwa, akisema: Ee Yesu uliyebarikiwa, uliyeniokoa kutoka [a]jehanamu! Ee Mungu uliyebarikiwa, [b]warehemu watu hawa!

30 Na aliposema haya, alifunga mikono yake, akiwa amejazwa na shangwe, na kuzungumza maneno mengi ambayo hayakufahamika; na alipofanya haya, alimchukua mfalme, Lamoni, kwa mkono, na tazama aliinuka na kusimama kwa miguu yake.

31 Na yeye, papo hapo, akiona ubishi uliokuwa miongoni mwa watu wake, alianza kuwakemea, na kuwafundisha [a]maneno aliyoyasikia kutoka kinywa cha Amoni; na wengi walisikia maneno yake na kuyaamini, na wakamgeukia Bwana.

32 Lakini kulikuwa na wengi miongoni mwao ambao hawakutaka kuyasikia maneno yake; kwa hivyo walienda zao.

33 Na ikawa kwamba wakati

23 *b* MWM Tegemea.
25 *a* Alma 18:2–5.
28 *a* Alma 19:16.
29 *a* 1 Ne. 14:3.
b MWM Rehema, enye Rehema.
31 *a* Alma 18:36–39.

Amoni alipoinuka, na yeye pia aliwahudumia, na pia watumishi wote wa Lamoni; na wote waliwatangazia watu kitu sawa—kwamba mioyo yao ilikuwa [a]imebadilishwa; kwamba hawakutamani tena kutenda [b]maovu.

34 Na tazama, wengi waliwatangazia watu kwamba walikuwa wameona [a]malaika na kuzungumza nao; na hivyo walikuwa wamewaambia vitu vya Mungu, na haki yake.

35 Na ikawa kwamba kulikuwa na wengi walioamini katika maneno yao; na wengi walioamini [a]walibatizwa; na wakawa watu wenye haki, na wakaanzisha kanisa miongoni mwao.

36 Na hivyo kazi ya Bwana ikaanza miongoni mwa Walamani; hivyo Bwana alianza kuteremsha Roho wake juu yao; na tunaona kwamba mkono wake umenyooshwa kwa watu [a]wote ambao watatubu na kuamini katika jina lake.

MLANGO WA 20

Bwana anamtuma Amoni Midoni kuwakomboa kaka zake waliofungwa—Amoni na Lamoni wanakutana na baba ya Lamoni, ambaye ni mfalme katika nchi yote—Amoni anamshurutisha mfalme mzee awaachilie kaka zake. Karibia mwaka 90 K.K.

Na ikawa kwamba baada ya wao kuanzisha kanisa katika nchi hiyo, mfalme Lamoni alimtaka Amoni aende pamoja na yeye katika nchi ya Nefi, ili amwonyeshe kwa baba yake.

2 Na sauti ya Bwana ikamjia Amoni, ikisema: Hutaenda katika nchi ya Nefi, kwani tazama, mfalme atataka kukutoa uhai wako; lakini utaenda katika nchi ya Midoni; kwani tazama, kaka yako Haruni, na pia Muloki na Ama wako gerezani.

3 Sasa ikawa kwamba Amoni aliposikia haya, alimwambia Lamoni: Tazama, kaka yangu na jamaa zangu wako gerezani huko Midoni, na ninaenda ili niwakomboe.

4 Sasa Lamoni akamwambia Amoni: Najua, kwamba kwa [a]nguvu za Bwana wewe unaweza kufanya vitu vyote. Lakini tazama, nitaenda na wewe katika nchi ya Midoni; kwani mfalme wa nchi ya Midoni, ambaye jina lake ni Antiomno, ni rafiki yangu; kwa hivyo nitaenda katika nchi ya Midoni, ili nimtanie mfalme wa nchi, na atawatoa ndugu zako kutoka [b]gerezani. Sasa Lamoni akamwambia: Nani aliyekwambia kwamba ndugu zako wako gerezani?

5 Na Amoni akamwambia: Hakuna yeyote aliyeniambia, ijapokuwa Mungu; na aliniambia—Nenda ukawakomboe ndugu zako, kwani wako gerezani katika nchi ya Midoni.

6 Sasa Lamoni aliposikia haya aliamuru kwamba watumishi

33 *a* MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
b Mos. 5:2; Alma 13:12.

34 *a* MWM Malaika.

35 *a* MWM Batiza, Ubatizo.

36 *a* 2 Ne. 26:33; Alma 5:33.

20 4 *a* Alma 26:12.
b Alma 20:28–30.

wake watayarishe [a]farasi wake na magari yake.

7 Na akamwambia Amoni: Njoo, nitaenda nawe katika nchi ya Midoni, na huko nitamsihi mfalme ili awatoe ndugu zako gerezani.

8 Na ikawa kwamba Amoni na Lamoni walipokuwa wakisafiri huko, walikutana na baba ya Lamoni, ambaye alikuwa ni mfalme [a]katika nchi yote.

9 Na tazama, baba ya Lamoni akamwambia: Kwa nini hukuja kwa [a]sherehe siku ile kuu niliyoandaa kwa wana wangu, na watu wangu?

10 Na pia akasema: Unaenda wapi na huyu Mnefi, ambaye ni mmoja wa wana wa [a]mwongo?

11 Na ikawa kwamba Lamoni akamwelezea kule alikokuwa akienda, kwani aliogopa kumkasirisha.

12 Na pia akamwelezea sababu zake za kukawia katika ufalme wake, na kwa nini hakwenda kwa sherehe ambayo baba yake alikuwa ameandaa.

13 Na sasa wakati Lamoni alipomwelezea vitu hivi vyote, tazama, kwa mshangao wake, baba yake alimkasirikia, na kusema: Lamoni, wewe unaenda kuwakomboa hawa Wanefi, ambao ni wana wa mwongo. Tazama, aliwaibia babu zetu; na sasa watoto wake nao pia wamekuja kati yetu, ili kwa ujanja wao na uwongo wao, watudanganye, ili watuibie mali zetu tena.

14 Sasa baba ya Lamoni alimwamuru kwamba amuue Amoni kwa upanga. Na pia akamwamuru kwamba asiende katika nchi ya Midoni, lakini kwamba arudi na yeye katika nchi ya [a]Ishmaeli.

15 Lakini Lamoni akamwambia: Mimi sitamuua Amoni, wala sitarudi katika nchi ya Ishmaeli, lakini nitaenda katika nchi ya Midoni ili niwakomboe ndugu za Amoni, kwani najua kwamba wao ni watu wenye haki na manabii watakatifu wa Mungu wa kweli.

16 Sasa wakati baba yake aliposikia maneno haya, alimkasirikia, na akatoa upanga wake ili amwangushe chini.

17 Lakini Amoni akasonga mbele na kumwambia: Tazama, huwezi kumuua mwana wako; walakini, [a]heri yeye aanguke chini badala yako, kwani tazama, [b]ametubu dhambi zake; lakini wewe ukianguka wakati huu, katika hasira yako, nafsi yako haiwezi kuokolewa.

18 Na tena, inafaa ujizuie; kwani [a]ukimuua mwana wako, na yeye ni mtu ambaye hana hatia, damu yake itamlilia Bwana Mungu wake kutoka ardhini, kulipiza kisasi kwake; na pengine wewe utapoteza [b]nafsi yako.

19 Sasa wakati Amoni alipomwambia maneno haya, alimjibu, akisema: Najua kwamba nikimuua mwana wangu, kwamba nitamwaga damu isiyo na

6*a* Alma 18:9–10.
8*a* Alma 22:1.
9*a* Alma 18:9.
10*a* Mos. 10:12–17.
14*a* Alma 17:19.
17*a* Alma 48:23.
b Alma 19:12–13.
18*a* MWM Mauaji.
b M&M 42:18.

hatia; kwani wewe ndiye umetaka kumwangamiza.

20 Na akanyoosha mkono wake ili amuue Amoni. Lakini Amoni alivumilia mapigo yake, na pia akaupiga mkono wake kwamba hakuweza kuutumia tena.

21 Sasa mfalme alipoona kwamba Amoni angemuua, alianza kumlilia Amoni kwamba aokoe maisha yake.

22 Lakini Amoni akainua upanga wake, na kumwambia: Tazama, nitakuua usipokubali ndugu zangu watolewe gerezani.

23 Sasa mfalme, akiogopa kwamba atapoteza uhai wake, alisema: Ukiniokoa nitakupa chochote utakachoniuliza, hata kama ni nusu ya ufalme.

24 Sasa Amoni alipoona kwamba mfalme mzee amekubali matakwa yake, alimwambia: Ukikubali kwamba ndugu zangu watolewe gerezani, na pia kwamba Lamoni amiliki ufalme wake, na kwamba usimkasirikie, lakini kwamba umruhusu atende kulingana na nia yake kwa kitu [a]chochote anachofikiria, ndipo nitakuokoa; la sivyo nitakuangusha chini.

25 Sasa Amoni aliposema maneno haya, mfalme akaanza kufurahi kwa sababu ya maisha yake.

26 Na alipoona kwamba Amoni hakuwa na haja ya kumwangamiza, na pia alipoona jinsi alivyompenda mwana wake Lamoni, alishangaa sana, na kusema: Kwa sababu haya pekee ndiyo umetaka, kwamba niwaachilie ndugu zako, na kwamba nimruhusu mwana wangu Lamoni amiliki ufalme wake, tazama, nitamruhusu mwana wangu amiliki ufalme wake kutoka sasa hadi milele; na sitamtawala tena—

27 Na pia nitakubali kwamba ndugu zako waondolewe gerezani, na wewe na ndugu zako mnaweza kunijia, katika ufalme wangu; kwani nitatamani kukuona. Kwani mfalme alistaajabia sana kwa yale maneno aliyozungumza, na pia yale maneno ambayo mwana wake Lamoni alikuwa amezungumza, kwa hivyo [a]alitaka kujifunza.

28 Na ikawa kwamba Amoni na Lamoni waliendelea na safari yao ya kuelekea nchi ya Midoni. Na Lamoni alipata fadhila za mfalme wa nchi; kwa hivyo ndugu za Amoni waliondolewa gerezani.

29 Na Amoni alipowaona alikuwa na huzuni sana, kwani tazama walikuwa uchi, na ngozi zao zilikuwa zimenyauka sana kwa sababu ya kufungwa kwa kamba nzito. Na pia walikuwa wamepatwa na njaa, kiu, na kila aina ya mateso; walakini [a]walivumilia mateso yao yote.

30 Na, kama vile ilivyotendeka, ilikuwa ni mkosi wao kuchukuliwa na mikono ya watu ambao walikuwa ni wagumu zaidi, na wenye shingo ngumu zaidi; kwa hivyo

24*a* Alma 21:21–22.
27*a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
29*a* Alma 17:11.

hawangesikiliza maneno yao, na waliwafukuza, na kuwapiga, na kuwakimbiza kutoka nyumba hadi nyumba, na kutoka mahali hadi mahali, hadi wakafika katika nchi ya Midoni; na hapo walichukuliwa na kutupwa gerezani, na kufungwa kwa kamba [a]nzito, na kuwekwa gerezani kwa siku nyingi, na wakakombolewa na Lamoni na Amoni.

Maandishi ya mahubiri ya Haruni, na Muloki, na ndugu zao, kwa Walamani.

Yenye milango ya 21 hadi 25.

MLANGO WA 21

Haruni anawafundisha Waamaleki juu ya Kristo na Upatanisho Wake—Haruni na ndugu zake wanafungwa Midoni—Baada ya kukombolewa kwa, wanafundisha katika masinagogi na kuwafanya wengi kuwa waongofu—Lamoni anatoa uhuru wa dini kwa watu wa nchi ya Ishmaeli. Karibia mwaka 90–77 K.K.

Sasa wakati Amoni na ndugu zake [a]walijigawanya katika mipaka ya nchi ya Walamani, tazama Haruni alisafiri kuelekea nchi iliyoitwa na Walamani, Yerusalemu, ambayo iliitwa kulingana na nchi ya kuzaliwa ya babu zao; na ilikuwa na mipaka ya Mormoni.

2 Sasa Walamani na Waamaleki na watu wa [a]Amuloni walikuwa wamejenga mji mkubwa, ambao uliitwa Yerusalemu.

3 Sasa Walamani wenyewe walikuwa ni wagumu kabisa, lakini Waamaleki na Waamuloni walikuwa ni wagumu zaidi; kwa hivyo wakawasababisha Walamani washupaze mioyo yao, kwamba waendelee na maovu yao na machukizo yao.

4 Na ikawa kwamba Haruni alifika katika mji wa Yerusalemu, na kwanza akaanza kuwahubiria Waamaleki. Na akaanza kuwahubiria katika masinagogi yao, kwani walikuwa wamejenga masinagogi [a]kulingana na desturi za Wanehori; kwani wengi wa Waamaleki na Waamuloni walikuwa wafuasi wa Wanehori.

5 Kwa hivyo, Haruni alipoingia katika moja ya masinagogi yao ili awahubirie watu, na alipokuwa akiwazungumzia, tazama Mwamaleki mmoja alisimama na akaanza kubishana na yeye, akisema: Ni nini ambacho wewe umeshuhudia? Wewe umeona [a]malaika? Kwa nini malaika hawatutokei sisi? Tazama si watu hawa ni wema kama watu wako?

6 Wewe pia unasema, tusipotubu tutaangamia. Jinsi gani wewe unajua mawazo na nia ya mioyo yetu? Jinsi gani unavyojua kwamba tunayo sababu ya kutubu? Jinsi gani unavyojua kwamba sisi sio watu wenye haki? Tazama, tumejenga makao matakatifu, na sisi huwa

30*a* Alma 26:29.
21 1*a* Alma 17:13, 17.
2*a* Mos. 24:1; Alma 25:4–9.
4*a* Alma 1:2–15.
5*a* Mos. 27:11–15.

tunakusanyika pamoja kumwabudu Mungu. Tunaamini kwamba Mungu ataokoa wanadamu wote.

7 Sasa Haruni akamwambia: Unaamini kwamba Mwana wa Mungu atakuja kuwakomboa wanadamu kutoka dhambi zao?

8 Na yule mtu akamwambia: Hatuamini kwamba wewe unajua kitu kama hicho. Hatuamini katika desturi za kijinga kama hizi. Hatuamini kwamba wewe unajua [a]vitu vile vitakavyokuja, wala hatuamini kwamba baba zako na pia kwamba baba zetu walijua kuhusu vitu vile walivyozungumza, yaani vile vitakavyokuja.

9 Sasa Haruni akaanza kuwafungulia maandiko kuhusu kuja kwa Kristo, na pia kuhusu ufufuo wa wafu, na kwamba [a]hakutakuwa na ukombozi kwa wanadamu ila tu kwa mauti na mateso ya Kristo, na [b]upatanisho wa damu yake.

10 Na ikawa kwamba alipoanza kuwafafanulia vitu hivi walimkasirikia, na wakaanza kumfanyia mzaha; na hawakutaka kusikia maneno aliyozungumza.

11 Kwa hivyo, alipoona kwamba hawakutaka kusikia maneno yake, aliondoka katika sinagogi yao, na akaenda katika kitongoji kilichoitwa Ani-Anti, na hapo akampata Muloki akiwahubiria neno; na pia Ama na ndugu zake. Na wakabishana na wengi kuhusu neno.

12 Na ikawa kwamba waliona kuwa watu watashupaza mioyo yao, kwa hivyo wakaondoka na kufika katika nchi ya Midoni. Na wakahubiri neno kwa wengi, na wachache wakaamini maneno ambayo walifundisha.

13 Walakini, Haruni na idadi fulani ya ndugu zake walishikwa na kutupwa gerezani, na waliosalia wakatoroka nchi ya Midoni na kuelekea katika sehemu zile zilizoizingira.

14 Na wale ambao walitupwa gerezani [a]waliteseka kwa vitu vingi, na walikombolewa kwa mkono wa Lamoni na Amoni, na wakalishwa na kuvishwa.

15 Na wakaenda tena kutanganza neno, na hivyo walikombolewa mara ya kwanza kutoka gerezani, na hivyo waliteseka.

16 Na walienda popote walipoongozwa na [a]Roho wa Bwana, wakihubiri neno la Mungu katika kila sinagogi la Waamaleki, au katika kila kusanyiko la Walamani lililowakaribisha.

17 Na ikawa kwamba Bwana alianza kuwabariki, hata wakaweza kuleta wengi kwa ufahamu wa ukweli; ndiyo, [a]waliwasadikisha wengi kuhusu dhambi zao, na desturi za babu zao, ambazo hazikuwa sawa.

18 Na ikawa kwamba Amoni na Lamoni walirudi kutoka katika nchi ya Midoni na kwenda katika nchi ya Ishmaeli, ambayo ilikuwa ni nchi yao ya urithi.

19 Na mfalme Lamoni hange-

8*a* Yak. (KM) 7:1–8.
9*a* Mos. 5:8; Alma 38:9.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
14*a* Alma 20:29.
16*a* Alma 22:1.
17*a* M&M 18:44.

kubali kwamba Amoni amtumikie, au awe mtumishi wake.

20 Lakini alisababisha kwamba masinagogi yajengwe katika nchi ya Ishmaeli; na akasababisha kwamba watu wake, au watu wale waliokuwa chini ya utawala wake, wakusanyike pamoja.

21 Na alifurahi juu yao, na akawafundisha vitu vingi. Na pia aliwatangazia kwamba wao ni watu waliokuwa chini ya utawala wake, na kwamba walikuwa watu huru, na kwamba walikuwa huru kutokana na udhalimu wa mfalme, baba yake; kwani baba yake alikuwa amemruhusu atawale watu waliokuwa katika nchi ya Ishmaeli, na katika sehemu iliyowazingira.

22 Na pia akawaambia kwamba wangekuwa na [a]uhuru wa kumwabudu Bwana Mungu wao kulingana na mahitaji yao, katika mahali popote walipo, ikiwa ilikuwa katika nchi ile iliyokuwa chini ya utawala wa mfalme Lamoni.

23 Na Amoni akawahubiria watu wa mfalme Lamoni; na ikawa kwamba aliwafundisha vitu vyote vilivyohusu vitu vya haki. Na akawaonya kila siku, kwa bidii zote; na wakasikiza neno lake, na walikuwa na bidii ya kushika amri za Mungu.

MLANGO WA 22

Haruni anamfundisha baba ya Lamoni kuhusu Uumbaji na Anguko la Adamu, na mpango wa ukombozi kupitia Kristo—Mfalme na nyumba yake yote wanaongolewa—Mgawanyo wa ardhi kati ya Wanefi na Walamani unaelezwa. Karibia mwaka 90–77 K.K.

Sasa, vile Amoni alikuwa hivyo alikuwa anafundisha watu wa Lamoni bila kikomo, tutarudia historia ya Haruni na ndugu zake; kwani baada ya kuondoka kutoka kwenye nchi ya Midoni [a]aliongozwa na Roho hadi kwenye nchi ya Nefi, hata kwenye nyumba ya mfalme ambaye alikuwa anasimamia nchi yote [b]isipokuwa nchi ya Ishmaeli; na alikuwa baba ya Lamoni.

2 Na ikawa kwamba alimwendea kwenye nyumba ya mfalme, na ndugu zake, na akasujudu mbele ya mfalme, na kusema kwake: Tazama, Ee mfalme, sisi ni ndugu za Amoni, ambaye [a]ulimwachilia huru kutoka gerezani.

3 Na sasa, Ee mfalme, ikiwa utasalimisha maisha yetu, tutakuwa watumishi wako. Na mfalme akawaambia: Amkeni, kwani nitamruhusu muishi, na sitakubali muwe watumishi wangu; lakini nitasisitiza kwamba mnitumikie, kwani nimesumbuliwa kidogo rohoni mwangu kwa sababu ya ukarimu mkuu wa maneno ya ndugu yako Amoni; na ninatamani kujua sababu iliyomfanya asitoke na ninyi Midoni.

4 Na Haruni akamwambia mfalme: Tazama, Roho wa

22*a* M&M 134:1–4; M ya I 1:11.
MWM Huru, Uhuru.
22 1*a* Alma 21:16–17.
b Alma 21:21–22.
2*a* Alma 20:26.

Bwana amemtuma mahali pengine; ameenda kwenye nchi ya Ishmaeli, kuwafundisha watu wa Lamoni.

5 Sasa mfalme akamwambia: Ni nini hiki ambacho mmekisema kuhusu Roho wa Bwana? Tazama, hiki ni kitu ambacho kinanisumbua.

6 Na pia, ni nini hiki ambacho Amoni alikisema—[a]Ikiwa mtatubu mtasamehewa, na ikiwa hamtatubu, mtatupiliwa mbali siku ya mwisho?

7 Na Haruni akamjibu na kumwambia: Unaamini wewe kwamba kuna Mungu? Na mfalme akasema: Ninajua kwamba Waamaleki wanasema kwamba kuna Mungu, na nimewaruhusu kwamba wajenge makanisa, kwamba wangekusanyika pamoja kumwabudu. Na sasa ikiwa unasema kuna Mungu, tazama, [a]nitaamini.

8 Na sasa Haruni aliposikia hivi, moyo wake ulianza kufurahi, na akasema: Tazama, kwa hakika vile unavyoishi, Ee mfalme, kuna Mungu.

9 Na mfalme akasema: Mungu ni yule [a]Roho Mkuu aliyewaleta babu zetu kutoka nchi ya Yerusalemu?

10 Na Haruni akamwambia: Ndiyo, ni yule Roho Mkuu, na [a]aliumba vitu vyote mbinguni na ardhini. Unaamini hivi wewe?

11 Na akasema: Ndiyo, ninaamini kuwa Roho Mkuu aliumba vitu vyote, na ninataka kwamba uniambie kuhusu hivi vitu vyote, na [a]nitaamini maneno yako.

12 Na ikawa kwamba wakati Haruni alipoona kwamba Mfalme angeamini maneno yake, alianzia tangu Adamu alivyoumbwa, [a]akisoma maandiko kwa mfalme—vile Mungu alivyomuumba mwanadamu kwa mfano wake mwenyewe, na kwamba Mungu alimpatia amri, na kwa sababu ya dhambi, binadamu alikuwa ameanguka.

13 Na Haruni akamwelezea maandiko kuanzia [a]uumbaji wa Adamu, akimwelezea binadamu alivyoanguka, na hali ya kimwili sasa na pia [b]mpango wa ukombozi, ambao ulitayarishwa [c]tangu uumbaji wa ulimwengu, kupitia kwa Kristo, kwa wote ambao wataamini katika jina lake.

14 Na kwa sababu binadamu alikuwa [a]ameanguka hangeweza [b]kustahili chochote mwenyewe; isipokuwa mateso na kifo cha Kristo [c]hulipia dhambi zao, katika imani na kutubu, na vingine; na kwamba hukata kamba za kifo, kwamba [d]kaburi halitakuwa na ushindi, na kwamba uchungu wa kifo utashindwa katika matumaini ya utukufu; na Haruni alieleza hivi vitu vyote kwa mfalme.

6*a* Alma 20:17–18.
7*a* M&M 46:13–14.
9*a* Alma 18:18–28.
10*a* MWM Umba, Uumbaji.
11*a* MWM Amini, Imani.
12*a* 1 Ne. 5:10–18; Alma 37:9.
13*a* Mwa. 1:26–28.
b MWM Mpango wa Ukombozi.
c 2 Ne. 9:18.
14*a* MWM Anguko la Adamu na Hawa.
b 2 Ne. 25:23; Alma 42:10–25.
c Alma 34:8–16. MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
d Isa. 25:8; 1 Kor. 15:55.

15 Na ikawa kwamba baada ya Haruni kumwelezea hivi vitu, mfalme alisema: Nitafanya [a]nini ili nipate uzima wa milele ambao umeuzungumzia? Ndiyo, nitafanya nini ili [b]nizaliwe kwa Mungu, ili hii roho mbovu ing'olewe nje ya mwili wangu, na nipokee Roho yake, ili niweze kujazwa na shangwe, ili nisitupiliwe nje siku ya mwisho? Tazama, alisema, nitatoa umiliki wangu [c]wote, ndiyo, nitaacha ufalme wangu, ili nipokee hii shangwe kuu.

16 Lakini Haruni alimwambia: Ikiwa [a]unatamani kitu hiki, ikiwa utamsujudia Mungu, ndiyo, ikiwa utatubu dhambi zako zote, na umsujudie Mungu, na umlingane kwa imani, ukiamini kwamba utapokea, ndipo utakapopokea [b]matumaini ambayo unatamani.

17 Na ikawa kwamba Haruni aliposema maneno haya, mfalme [a]alisujudu mbele ya Bwana, kwa magoti yake; ndiyo, hata akajilaza kifudifudi ardhini, na [b]kulia kwa nguvu, akisema:

18 Ee Mungu, Haruni ameniambia kwamba kuna Mungu; na ikiwa kuna Mungu, na ikiwa wewe ni Mungu, unaweza kujitambulisha kwangu, na nitaacha dhambi zangu zote ili nikujue wewe, na kwamba niinuliwe kutoka kwa wafu, na niokolewe siku ya mwisho. Na sasa wakati mfalme alipokuwa amesema maneno haya, alianguka akawa kama amekufa.

19 Na ikawa kwamba wafanyi kazi wake walikimbia na kumwambia malkia yote ambayo yalikuwa yametendeka kwa mfalme. Na akaja mahali ambapo mfalme alikuwa; na alipomwona amelala kama aliyekufa, na pia Haruni na ndugu zake wakisimama kama ndiyo waliosababisha kuanguka kwake, aliwakasirikia, na kuamuru kwamba watumishi wake, au watumishi wa mfalme, wawachukue na kuwaua.

20 Sasa watumishi walikuwa wameona kilichosababisha mfalme kuanguka, kwa hivyo hawakuthubutu kumshika Haruni na ndugu zake; na wakamsihi malkia wakisema: Kwa nini unatuamrisha tuue watu hawa, ikiwa tazama, mmoja wao yu [a]mkuu kuliko sisi zote? Kwa hivyo wanaweza kutuua.

21 Sasa wakati malkia aliona woga wa watumishi, yeye pia alianza kuogopa sana, kwamba maovu yasimjie. Na akawaamrisha watumishi wake kwamba waende na kuita watu, ili wawaue Haruni na ndugu zake.

22 Sasa Haruni alipoona kusudi la malkia, yeye, pia akijua ugumu wa mioyo ya watu, aliogopa kwamba umati utakusanyika pamoja, na kuwe na ubishi mwingi na msukosuko miongoni mwao; kwa hivyo alinyosha mkono wake na

15*a* Mdo. 2:37.
b Alma 5:14, 49.
c Mt. 13:44–46; 19:16–22.

16*a* MWM Mwongofu, Uongofu.
b Eth. 12:4.

17*a* M&M 5:24.
b MWM Sala.

20*a* Alma 18:1–3.

kumuinua mfalme kutoka chini, na akamwambia: Simama. Na akasimama, miguu yake ikipata nguvu zake.

23 Sasa hii ilifanyika machoni mwa malkia na watumishi wengi. Na walipoiona walishangaa sana, na kuanza kuogopa. Na mfalme alisimama mbele, na kuanza [a]kuwahudumia. Na aliwahudumia, jinsi kwamba jamii yake yote [b]ilimgeukia Bwana.

24 Sasa kulikuwa na umati uliokusanyika kwa sababu ya amri ya malkia, na kukawa na manung'uniko mengi miongoni mwao kwa sababu ya Haruni na ndugu zake.

25 Lakini mfalme alisimama mbele miongoni mwao na kuanza kuwahudumia. Na walitulizwa juu ya Haruni na wale ambao walikuwa na yeye.

26 Na ikawa kwamba wakati mfalme aliona kwamba watu wametulia, alisababisha kwamba Haruni na ndugu zake wasimame na kusogea katikati ya umati, na kwamba wawahubirie neno.

27 Na ikawa kwamba mfalme alitoa [a]tangazo nchini kote, miongoni mwa watu wake wote ambao walikuwa kwenye nchi yake yote, ambao walikuwa ndani ya mikoa yote iliyokaribiana, hata karibu na bahari, upande wa mashariki na upande wa magharibi, na ambayo ilitengwa kutoka nchi ya [b]Zarahemla na kipande chembamba cha nyika, ambayo ilinyooka kutoka mashariki ya bahari hadi magharibi ya bahari, karibu na mipaka ya pwani, na mipaka ya nyika ambao ulikuwa kaskazini karibu na nchi ya Zarahemla, kupitia mipaka ya Manti, kupitia kando ya mto wa Sidoni, kutoka mashariki hadi magharibi—na hivyo ndivyo Walamani na Wanefi walivyotenganishwa.

28 Sasa, sehemu kubwa ya Walamani ambao walikuwa [a]wazembe waliishi nyikani, na kuishi kwenye hema; na walikuwa wametawanyika upande wa magharibi, katika nchi ya Nefi; ndiyo, na pia kwenye magharibi ya nchi ya Zarahemla, kwenye sehemu ya ukingo wa bahari, na magharibi kwenye nchi ya Nefi, mahali ambapo babu zao walirithi mbeleni, na hivyo ikipakana na ukingo wa bahari.

29 Na pia kulikuwa na Walamani wengi mashariki karibu na ukingo wa bahari, ambapo Wanefi waliwasukuma. Na hivyo Wanefi walizingirwa na Walamani; ingawaje Wanefi walikuwa wamemiliki sehemu ya kaskazini mwa nchi inayopakana na nyika, kwenye chimbuko ya mto Sidoni, kutoka mashariki, hadi magharibi, ikizunguka upande wa nyika; upande wa kaskazini, hata wakaja kwa nchi ambayo waliita [a]Neema.

30 Na ilikuwa imepakana na

23 *a* MWM Fundisha, Mwalimu; Hubiri; Kuhudumu.
b MWM Mwongofu, Uongofu.
27 *a* Alma 23:1–4.
b Omni 1:13–17.
28 *a* 2 Ne. 5:22–25.
29 *a* Alma 52:9; 63:5.

nchi waliyoiita [a]Ukiwa, ikiwa mbali sana kaskazini kwamba iliingia katika nchi iliyokaliwa na watu na kuharibiwa, ambayo [b]mifupa yake tumeizungumzia, ambayo iligunduliwa na watu wa Zarahemla, ikawa mahali ambapo walishukia [c]kwanza.

31 Na walikuja kutokea kule juu hadi kwenye nyika ya kusini. Hivyo nchi ya kaskazini iliitwa [a]Ukiwa, na nchi ya kusini iliitwa Neema, ilikuwa nyika ambayo imejazwa na wanyama wa kila aina, ambao wengi wao walitoka katika nchi ya kaskazini kwa ajili ya chakula.

32 Na sasa, ilikuwa tu [a]mwendo wa siku moja na nusu kwa usafiri wa Mnefi, kwenye mpaka miongoni mwa Neema na nchi ya Ukiwa, kutoka mashariki hadi kwenye bahari ya magharibi; na hivyo nchi ya Nefi na nchi ya Zarahemla zilikuwa karibu zimezingirwa na maji, kukiwa na [b]kijisehemu cha nchi katikati ya nchi iliyo kaskazini na nchi iliyo kusini.

33 Na ikawa kwamba Wanefi walikuwa wameimiliki nchi ya Neema, hata kutokea mashariki hadi kwenye bahari ya magharibi, na hivyo Wanefi kwa hekima yao, na walinzi wao na majeshi yao, walikuwa wamewafungia Walamani upande wa kusini, kwa hivyo wasiwe tena na umiliki kaskazini, ili wasiweze kupita na kuleta vita kaskazini.

34 Kwa hivyo Walamani hawangemiliki kitu kingine isipokuwa tu nchi ya Nefi, na nyika iliyokuwa karibu. Sasa hii ilikuwa hekima kwa Wanefi—kwani Walamani walikuwa maadui kwao, hawangekubali mateso yao yatokee kila upande, na pia ili wapate nchi ambayo wangekimbilia, kulingana na mahitaji yao.

35 Na sasa mimi baada ya kusema haya, narudia tena historia ya Amoni na Haruni, Omneri na Himni, na ndugu zao.

MLANGO WA 23

Uhuru wa dini unatangazwa—Walamani kwenye nchi na miji saba waokoka—Wanajiita wenyewe Waanti-Nefi-Lehi na wanakuwa huru kutokana na laana—Waamaleki na Waamuloni wanakataa ukweli. Karibia mwaka 90–77 K.K.

Tazama, sasa ikawa kwamba mfalme wa Walamani alituma [a]tangazo miongoni mwa watu wake wote, kwamba wasimuumize Amoni, au Haruni, au Omneri, au Himni, wala mmoja wao wa ndugu zao ambao ataenda mbele na kuhubiri neno la Mungu, mahali popote watakaokuwa, kwenye sehemu yoyote ya nchi yao.

2 Ndiyo, alitoa amri miongoni mwao, kwamba wasiwashike na kuwafunga mikono yao, au kuwatupa gerezani; wala wasiwatemee mate, wala kuwapiga,

30 *a* Alma 50:34; Morm. 4:1–3.
b Mos. 8:7–12; 28:11–19.
c Hel. 6:10.
31 *a* Hel. 3:5–6.
32 *a* Hel. 4:7.
b Alma 50:34.
23 1 *a* Alma 22:27.

wala kuwatupa nje ya masinagogi yao, wala kuwaadhibu; wala wasiwatupie mawe, lakini kwamba waruhusiwe kwenye nyumba zao, na pia kwenye mahekalu yao, na mahali pao patakatifu.

3 Na hivyo wangeweza kwenda mbele, na kuhubiri neno kulingana na kutaka kwao, kwani mfalme alikuwa amemgeukia Bwana, na jamii yake yote; kwa hivyo alitoa tangazo lake nchini kote kwa watu, kuwa neno la Mungu lisizuiliwe, lakini kwamba lingeenda kote kwenye nchi yote, kwamba watu wake wangesadikishwa kuhusu [a]mila mbovu za babu zao, na kwamba wangesadikishwa kwamba wote walikuwa ndugu, na kwamba wanapaswa wasiue, wala kunyang'anya, wala kuiba, wala wasitende uzinzi, wala kutenda aina yoyote ya maovu.

4 Na sasa ikawa kwamba mfalme alipotuma mbele hili tangazo, kwamba Haruni na ndugu zake walienda kutoka mji mmoja hadi mwingine, na kutoka kwenye nyumba moja ya ibada hadi nyingine, wakianzisha makanisa, na wakiweka wakfu makuhani na walimu kote nchini miongoni mwa Walamani, kuhubiri na kufundisha neno la Mungu miongoni mwao; na hivyo walianza kufanikiwa kwa wingi.

5 Na maelfu waliletwa kwenye ufahamu wa Bwana, ndiyo, maelfu waliletwa kuamini [a]desturi za Wanefi; na walifundishwa [b]maandiko na unabii ambao ulikuwa umetolewa tangu zamani hadi wakati huu.

6 Na kwa kweli kama vile Bwana anavyoishi, kwa hakika vile wengi walivyoamini, au vile wengi walielimishwa kwa ukweli, kupitia kwa uhubiri wa Amoni na ndugu zake, kulingana na roho ya ufunuo na ya unabii, na uwezo wa Mungu ukifanya miujiza ndani yao—ndiyo, nawaambia ninyi, vile Bwana anavyoishi, vile wengi wa Walamani walivyoamini kuhubiri kwao, na [a]wakamgeukia Bwana, [b]hawakuanguka kamwe kutoka kanisa.

7 Kwani walipata kuwa watu wenye haki na wakaweka chini silaha zao za uasi, kwamba hawangeweza kupigana na Mungu tena, wala dhidi ya yeyote wa ndugu zao.

8 Sasa, hawa ndiyo [a]wale waliomgeukia Bwana:

9 Watu wa Walamani ambao walikuwa kwenye nchi ya Ishmaeli;

10 Na pia watu wa Walamani ambao walikuwa kwenye nchi ya Midoni;

11 Na pia watu wa Walamani ambao walikuwa kwenye mji wa Nefi;

12 Na pia watu wa Walamani ambao walikuwa kwenye nchi ya [a]Shilomu, na katika nchi ya Shemloni, na katika mji wa

3a Alma 26:24.
5a Alma 37:19.
b Alma 63:12.
MWM Maandiko.
6a MWM Mwongofu, Uongofu.
b Alma 27:27.
8a Alma 26:3, 31.
12a Mos. 22:8, 11.

Lemueli, na katika mji wa Shimnilomu.

13 Na haya ndiyo majina ya miji ya Walamani ambayo [a]ilimgeukia Bwana; na hii ndiyo iliweka chini silaha zao za uasi, ndiyo, silaha zao zote za vita; na wote walikuwa Walamani.

14 Na Waamaleki [a]hawakuongoka, isipokuwa tu mmoja; wala hapakuweko yeyote kwa [b]Waamuloni; lakini walishupaza mioyo yao, na pia mioyo ya Walamani kwenye hiyo sehemu ya nchi popote walipoishi, ndiyo, na kwenye vijiji vyao vyote na miji yao yote.

15 Kwa hivyo, tumeitaja miji yote ya Walamani ambamo walitubu na kupata ufahamu wa ukweli, na wakageuka.

16 Na sasa ikawa kwamba mfalme na wote ambao waligeuka walitaka kwamba wawe na jina, ambalo lingewatofautisha na ndugu zao; kwa hivyo mfalme akashauriana na Haruni na wengi wa makuhani, kuhusu jina ambalo wangejiita, ili waweze kujitambulisha.

17 Na ikawa kwamba walijiita [a]Anti-Nefi-Lehi; na waliitwa kwa jina hili na hawakuitwa tena Walamani.

18 Na walianza kuwa watu wenye kushika kazi sana; ndiyo, na wakawa marafiki wa Wanefi; kwa hivyo, wakaanza mawasiliano nao, na [a]lawama ya Mungu haikuwa kwao tena.

MLANGO WA 24

Walamani wanawashambulia watu wa Mungu—Waanti-Nefi-Lehi wanafurahi ndani ya Kristo na wanatembelewa na malaika—Wanaamua kuuawa kuliko kujikinga wenyewe—Walamani zaidi waokolewa. Karibia mwaka 90–77 K.K.

Na ikawa kwamba Waamaleki na Waamuloni na Walamani ambao walikuwa katika nchi ya Amuloni, na pia kwenye nchi ya Helamu, na waliokuwa kwenye nchi ya [a]Yerusalemu, na kwa kifupi, kwenye nchi yote karibu, ambao hawakuwa wamegeuka na hawakuwa wamechukua jina la [b]Anti-Nefi-Lehi, walichochewa na Waamaleki na Waamuloni kuwakasirikia ndugu zao.

2 Na chuki yao ilikuja kuwa jeraha kubwa juu yao, hata kwa kiasi kwamba walianza kuasi juu ya mfalme wao, hata ikawa hawataki awe mfalme wao; kwa hivyo, walichukua silaha na kuwakabili watu wa Anti-Nefi-Lehi.

3 Sasa mfalme alimpa mwana wake ufalme, na akamuita jina la Anti-Nefi-Lehi.

4 Na mfalme akafariki mwaka huo huo ambao Walamani walianza kufanya matayarisho ya kukabiliana na watu wa Mungu.

5 Sasa Amoni na ndugu zake na wote waliokuja na yeye

13*a* Alma 53:10.
14*a* Alma 24:29.
b Mos. 23:31–39.
17*a* MWM Waanti-Nefi-Lehi.
18*a* 1 Ne. 2:23; 2 Ne. 30:5–6; 3 Ne. 2:14–16.

24 1*a* Alma 21:1.
b Alma 25:1, 13.

walipoona matayarisho ya Walamani kuwaangamiza ndugu zao, walienda mbele kwenye nchi ya Midiani, na huko Amoni alikutana na ndugu zake wote; na kutokea hapo walienda kwa nchi ya Ishmaeli ili wawe na [a]baraza na Lamoni na pia kaka yake Anti-Nefi-Lehi, wajue cha kufanya kujikinga kutokana na Walamani.

6 Sasa hakukuwa hata mtu mmoja miongoni mwa wote waliokuwa wamemgeukia Bwana ambaye angechukua silaha dhidi ya ndugu zao; hapana, hawangeweza kufanya matayarisho ya vita; ndiyo, hata mfalme wao aliwaamuru wasifanye hivyo.

7 Sasa haya ndiyo maneno ambayo aliwaambia watu kuhusu hili tatizo: Ninamshukuru Mungu wangu, wapendwa wangu, kwamba Mungu wetu mkuu kwa wema amewatuma hawa ndugu zetu, Wanefi, kwetu kutuhubiria, na kutusadikisha sisi kwa [a]desturi za babu zetu waovu.

8 Na tazama, ninamshukuru Mungu wangu mkuu kwamba ametushawishi na roho yake na kulainisha mioyo yetu, kwamba tumeanza mawasiliano na hawa ndugu Wanefi.

9 Na tazama, pia ninamshukuru Mungu wangu, kwamba kwa kuanzisha mawasiliano tumesadikishwa [a]dhambi zetu, na mauaji mengi ambayo tumetenda.

10 Na pia ninamshukuru Mungu wangu, ndiyo, Mungu wangu mkuu, kwamba ametujalia kwetu sisi kwamba tutubu juu ya vitu hivi, na pia kwamba [a]ametusamehe sisi kwa hizo dhambi zetu na mauaji mengi ambayo tumetenda, na kututolea mbali [b]hatia kutoka kwenye mioyo yetu, kupitia kwa matendo mema ya Mwana wake.

11 Na sasa tazama, ndugu zangu, vile imekua yote ambayo tungetenda (kwa vile sisi tulikuwa wapotevu zaidi miongoni mwa wanadamu wote) kutubu dhambi zetu na mauaji mengi tuliyotenda, na kupata Mungu [a]kuziondoa kutoka mioyo yetu, kwani ni hii tu tungefanya kutubu ya kutosha mbele ya Mungu kwamba angeondolea mbali hatia yetu—

12 Sasa, ndugu zangu wapendwa sana, vile Mungu ametuondolea mbali hatia zetu, na panga zetu, zimekuwa safi, basi tusichafue panga zetu tena na damu ya ndugu zetu.

13 Tazama, ninawambia ninyi, Hapana, acheni tuhifadhi panga zetu ili zisichafuliwe tena na damu ya ndugu zetu; kwani huenda kama tunachafua panga zetu tena [a]hazitaoshwa tena na kuwa safi kupitia kwa damu ya Mwana wa Mungu wetu mkuu, ambayo itatiririka kwa upatanisho wa dhambi zetu.

14 Na Mungu mkuu amekuwa na huruma kwetu, na kusabisha hivi vitu kujulikana kwetu

5*a* Alma 27:4–13.
7*a* Mos. 1:5.
9*a* M&M 18:44.
10*a* Dan. 9:9.
b MWM Hatia.
11*a* Isa. 53:4–6.
13*a* Ufu. 1:5.

ili tusiangamie; ndiyo, na amesababisha hivi vitu kujulikana kwetu mbeleni, kwa sababu anapenda [a]nafsi zetu vile anapenda watoto wetu; kwa hivyo, kwa rehema yake hututembelea sisi kupitia malaika wake, ili [b]mpango wa wokovu usababishwe kujulikana kwetu na pia uzazi ujao.

15 Ee, jinsi gani Mungu wetu ana huruma! Na sasa tazameni, vile imekuwa kazi ngumu kutoa dhambi kutoka kwetu, na panga zetu zimefanywa safi, acha tuzifiche mbali ili zibaki ziking'ara, kama ushuhuda kwa Mungu wetu katika siku ya mwisho, ama katika siku ambayo tutaletwa kusimama mbele yake kuhukumiwa, kwamba hatujazichafua panga zetu na damu ya ndugu zetu tangu atoe neno lake kwetu na kwa hivyo kutufanya sisi tuwe safi.

16 Na sasa, ndugu zangu, ikiwa ndugu zetu wanatutafuta kutuangamiza, tazama, tutaficha panga zetu mbali, ndiyo, hata kuzizika udongoni, ili zihifadhiwe zikiwa safi, kama ushuhuda kwamba hatujazitumia, katika siku ya mwisho; na ikiwa ndugu zetu watatuangamiza, tazama, [a]tutaenda kwa Mungu wetu na tutaokolewa.

17 Na sasa ikawa kwamba mfalme alipokuwa amemaliza kuzungumza hii misemo, na watu wote walikuwa wamekusanyika pamoja, walichukua panga zao, na silaha zote ambazo zilitumiwa kwa kumwaga damu ya wanadamu, na [a]wakazizika chini mchangani.

18 Na hivi walifanya, ikiwa kwa maoni yao ushuhuda kwa Mungu, na pia kwa binadamu, kwamba [a]hawatatumia silaha tena kumwaga damu ya binadamu; na hivi walifanya, ili kudhibitisha na [b]kuagana na Mungu, kwamba badala ya kumwaga damu ya ndugu zao [c]wangetoa maisha yao; na badala ya kuchukua kutoka kwa ndugu wangepeana kwake na badala ya kukaa bila kufanya kitu wangefanya kazi kwa bidii kwa mikono yao.

19 Na hivyo tunaona kwamba, wakati hawa Walamani walipoelekezwa kujua ukweli, walikuwa [a]imara, na wangeumia hata kwenye kifo kuliko kutenda dhambi; na hivyo tunaona kwamba walizika silaha zao za amani, au walizika silaha za vita, kwa amani.

20 Na ikawa kwamba ndugu zao, Walamani, walijiandaa kwa vita, na wakaja kwenye nchi ya Nefi kwa nia ya kumwangamiza mfalme, na kumweka mwingine badala yake, na pia kuwaangamiza watu wa Anti-Nefi-Lehi wasiwepo nchini.

21 Sasa wakati walipoona kwamba wanakabiliwa waliondoka

14 *a* MWM Nafsi—Thamani ya nafsi.
b MWM Mpango wa Ukombozi.
16 *a* Alma 40:11–15.
17 *a* Hel. 15:9.
18 *a* Alma 53:11.
b MWM Agano.
c MWM Dhabihu.
19 *a* MWM Amini, Imani.

na kukutana nao, na [a]kujilaza mchangani mbele yao, na kuanza kulilingana kwa jina la Bwana; na hivyo walikuwa katika hali ile wakati Walamani walipoanza kuwashambulia, na wakaanza kuwachinja kwa upanga.

22 Na hivyo bila kuwa na pingamizi, waliwachinja elfu moja na watano wao; na tunajua kwamba wamebarikiwa, kwani wameenda kuishi na Mungu wao.

23 Sasa wakati Walamani waliona kwamba ndugu zao hawakimbii kutoka kwa upanga, wala hawageuki upande wa kulia au kushoto, lakini kwamba wangelala chini na [a]kuangamia, na kumsifu Mungu hata wakifa kwa upanga—

24 Sasa Walamani walipoona hivi [a]waliacha kuwachinja; na kulikuwa wengi ambao mioyo yao ilikuwa [b]imevimba ndani yao kwa ajili ya ndugu zao ambao waliangukiwa na upanga, hata wakatubu kwa vitu ambavyo walikuwa wamefanya.

25 Na ikawa kwamba walitupa silaha zao za vita chini, na hawangezichukua tena, kwani walikuwa na uchungu kwa mauaji ambayo walikuwa wamefanya; na walilala chini kama ndugu zao, wakitegemea huruma ya wale silaha zao zilizokuwa zimeinuliwa kuwachinja.

26 Na ikawa kwamba watu wa Mungu waliungana siku ile na wengi kuliko idada ya wale ambao walikuwa wameuawa; na wale ambao waliuawa walikuwa watu wenye haki, kwa hivyo hatuna sababu ya kuwa na shaka kwamba [a]waliokolewa.

27 Na hakukuwa na mtu mwovu aliyechinjwa miongoni mwao; lakini kulikuwa na zaidi ya elfu moja walioelimishwa kwa ukweli; hivyo tunaona kwamba Bwana hutumia [a]njia nyingi ili kuokoa watu wake.

28 Sasa idadi kubwa sana ya wale Walamani ambao waliua ndugu zao wengi walikuwa Waamaleki na Waamuloni, idadi kubwa ambayo ilikuwa kulingana na [a]shirika la [b]Wanehori.

29 Sasa, miongoni mwa wale ambao walijiunga na watu wa Bwana, [a]hakukuwepo na Waamaleki au Waamuloni, au ambao walikuwa na desturi ya Nehori, lakini walikuwa hasa watoto wa Lamani na Lemueli.

30 Na hivyo tunaweza kuona wazi, kwamba baada ya watu [a]kuelimishwa na Roho wa Mungu, na wana [b]ufahamu mkuu wa vitu ambavyo vinahusikana na haki, na tena [c]waingie tena kwenye makosa na dhambi, wanakuwa wagumu zaidi, na hivyo hali yao huwa [d]mbaya zaidi kama kwamba hawakujua vitu hivi.

21 *a* Alma 27:3.
23 *a* Alma 26:32.
24 *a* Alma 25:1.
b MWM Huruma.
26 *a* Ufu. 14:13.
27 *a* Isa. 55:8–9; Alma 37:6–7.
28 *a* Alma 21:4.
b Alma 1:15; 2:1, 20.
29 *a* Alma 23:14.
30 *a* Mt. 12:45.
b Ebr. 10:26; Alma 47:36.
c 2 Ne. 31:14; Alma 9:19.
MWM Ukengeufu.
d 2 Pet. 2:20–21.

MLANGO WA 25

Ujeuri wa Walamani unasambaa—Uzao wa makuhani wa Nuhu unaangamia vile nabii Abinadi alipobashiri—Walamani wengi wanageuka na kuungana na watu wa Anti-Nefi-Lehi—Wanaamini katika Kristo na kuhifadhi sheria ya Musa. Karibia mwaka 90–77 K.K.

NA tazama, sasa ikawa kwamba wale Walamani walikuwa na hasira sana kwa sababu walikuwa wamewaua ndugu zao; kwa hivyo waliapa kulipiza kisasi juu ya Wanefi; na hawakujaribu mara nyingine tena kuua watu wa [a]Anti-Nefi-Lehi kwa wakati huo.

2 Lakini walichukua majeshi yao na wakaenda juu kwenye mipaka ya nchi ya Zarahemla, na kuwashambulia watu ambao walikuwa kwenye nchi ya Amoniha na [a]kuwaangamiza.

3 Na baada ya hayo, walikuwa na vita vingi na Wanefi, ambako walikimbizwa na kuuawa.

4 Na miongoni mwa Walamani ambao waliuawa karibu wote walikuwa [a]uzao wa Amuloni na ndugu zake, ambao walikuwa makuhani wa Nuhu, na waliuawa kwa mikono ya Wanefi;

5 Na waliosalia, wakikimbilia kwenye nyika ya mashariki, na wakijitwalia uwezo na mamlaka juu ya Walamani, walisababisha kwamba wengi wa Walamani [a]waangamizwe kwa moto kwa sababu ya imani yao—

6 Kwa sababu wengi [a]wao, baada ya kuumia kwa hasara nyingi na mateso mengi, walianza kuvurugwa na kukumbuka [b]maneno ambayo Haruni na ndugu zake waliwahubiria nchini mwao; kwa hivyo, walianza kutoamini [c]desturi za babu zao, na kuamini katika Bwana, na kwamba aliwapa Wanefi uwezo mwingi; na hivyo kulikuwa na wengi wao ambao waligeuka nyikani.

7 Na ikawa kwamba wale watawala ambao walikuwa baki la watoto wa [a]Amuloni walisababisha kwamba [b]wauawe, ndiyo, wale wote ambao waliamini katika vitu hivi.

8 Sasa haya mauaji yalisababisha kwamba wengi wa ndugu zao wachochewe na kukasirika; na kukaanza kuwa na ubishi nyikani; na Walamani wakaanza [a]kufuata uzao wa Amuloni na ndugu zake na kuanza kuwaua; na wakakimbilia upande wa mashariki ya nyika.

9 Na tazama wanatafutwa hadi siku hii na Walamani. Hivyo maneno ya Abinadi yalitimizwa, ambayo alisema kuhusu uzao wa makuhani ambao walisababisha kwamba ateswe na kifo kwa moto.

10 Kwa sababu aliwaambia:

25 1*a* MWM Waanti-Nefi-Lehi.
2*a* Alma 8:16; 16:9.
4*a* Mos. 23:35.
5*a* Mos. 17:15.
6*a* MY Walamani.
b Alma 21:9.
c Alma 26:24.
7*a* Alma 21:3; 24:1, 28–30.
b MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
8*a* Mos. 17:18.

Yale [a]mtakayonifanyia yatakuwa mfano wa vitu vitakavyokuja.

11 Na sasa Abinadi alikuwa wa kwanza aliyeumia [a]kifo kwa moto kwa sababu ya kuamini kwake katika Mungu; sasa hivi ndivyo alivyomaanisha, kwamba wengi wataumia kifo kwa moto, kulingana na vile alivyoumia.

12 Na akawaambia makuhani wa Nuhu kwamba uzao wao utasababisha wengi wauawe, kwa njia sawa vile alivyokuwa, na kwamba watatawanyika nje na kuuawa, hata vile kondoo huwa kama hawana mlinzi hukimbizwa na kuuawa na wanyama wa mwitu; na sasa tazama, maneno haya yalithibitishwa, kwani walikimbizwa na Walamani, na waliwindwa, na kuuawa.

13 Na ikawa kwamba Walamani walipoona kwamba hawangeweza kuwashinda Wanefi walirudi tena kwenye nchi yao; na wengi wao walienda kuishi kwenye nchi ya Ishmaeli na nchi ya Nefi, na wakaungana na watu wa Mungu, ambao walikuwa watu wa [a]Anti-Nefi-Lehi.

14 Na pia [a]walizika silaha zao za vita, vile ndugu zao walivyofanya, na wakaanza kuwa watu wenye haki; na wakatembea kwa njia za Bwana, na kuchunguza na kuweka amri zake na sheria zake.

15 Ndiyo, na walihifadhi [a]sheria ya Musa; kwani ilikuwa ya manufaa kwamba wahifadhi sheria ya Musa bado, kwani yote ilikuwa haijatimizwa. Lakini ijapokuwa sheria ya Musa, walitazamia kuja kwa Kristo, wakifikiri kwamba sheria ya Musa ilikuwa [b]mfano wa kuja kwake, na kuamini kwamba lazima wahifadhi kutenda mambo [c]mengine hadi wakati ambao atafichuliwa kwao.

16 Sasa hawakufikiria kwamba [a]wokovu ulikuja kwa [b]sheria ya Musa; lakini sheria ya Musa ilitumika kwa kuweka nguvu imani yao kwa Kristo; na hivyo waliweka [c]matumaini kupitia imani, kwa wokovu wa milele, wakitegemea roho ya unabii, ambayo ilizungumzia vitu vinavyokuja.

17 Na sasa tazama, Amoni, na Haruni, na Omneri, na Himni, na ndugu zao walifurahi sana, kwa ushindi ambao waliupata miongoni mwa Walamani, wakiona kwamba Bwana alikuwa amewakubalia kulingana na [a]sala zao, na kwamba alikuwa amethibitisha neno lake kwao kwa jumla.

MLANGO WA 26

Amoni anashangilia katika Bwana—Waaminifu hupewa nguvu na Bwana na kupewa ufahamu—Kwa imani binadamu

10*a* Mos. 13:10.
11*a* Mos. 17:13.
13*a* Alma 23:16–17.
14*a* Alma 24:15; 26:32.
15*a* Yak. (KM) 4:5; Yar. 1:11. MWM Torati ya Musa.
b Mos. 3:14–15; 16:14.
c Mos. 13:29–32.
16*a* Mos. 12:31–37; 13:27–33.
b 2 Ne. 11:4.
c 1 The. 5:8–9.
17*a* Alma 17:9.

wangewaleta watu wengi kutubu—Mungu ana uwezo wote na anafahamu vitu vyote. Karibia mwaka 90–77 K.K.

Na sasa, haya ndiyo maneno ya Amoni kwa ndugu zake, ambayo yanasema hivi: Ndugu zangu na jamaa zangu, tazama nawambia ninyi, ni sababu kiasi gani tunayo ya kutufanya tufurahi; kwani tungejuaje wakati [a]tulipoanza safari yetu kutoka Zarahemla kwamba Mungu angetubariki sisi hivi kwa wingi?

2 Na sasa, nauliza, ni baraka gani kubwa ambayo ametupatia sisi? Mnaweza kunena?

3 Tazama, ninajibu kwa niaba yenu; kwani ndugu zetu, Walamani, walikuwa gizani, ndiyo, hata kwenye shimo la giza kubwa sana, lakini tazama, ni [a]wangapi miongoni mwao wameletwa kuona mwangaza wa ajabu wa Mungu! Na hii ndiyo baraka ambayo tumeteremshiwa, kwamba tumetengenezwa kuwa [b]vyombo mikononi mwa Mungu kuimarisha kazi hii kubwa.

4 Tazama, [a]maelfu miongoni mwao wanafurahi, na kuletwa kwenye zizi la Mungu.

5 Tazama, [a]shamba lilikuwa bivu, na heri ninyi, kwani mlisukuma [b]pepeto, na mkavuna kwa nguvu, ndiyo, siku yote nzima mlifanya kazi; na tazama idadi ya [c]miganda yenu! Na itakusanywa kwenye maghala, ili isiharibiwe.

6 Ndiyo, haitaangushwa na dhoruba ya mvua siku ya mwisho; ndiyo, wala haitatawanyishwa na vimbunga; lakini [a]dhoruba itakapokuja itakusanywa pamoja, kwamba dhoruba isiweze kuipenya; ndiyo, wala haitasukumwa na upepo mkali popote adui atakapotaka kuipeleka.

7 Lakini tazama, wamo mikononi mwa Bwana wa [a]mavuno, na ni wake; na [b]atawainua katika siku ya mwisho.

8 Libarikiwe jina la Mungu wetu; acheni [a]tuimbe kwa sifa yake, ndiyo, wacha [b]tulishukuru jina lake takatifu, kwani yeye hufanya kazi ya haki milele.

9 Kwani kama hatungekuja kutoka kwa nchi ya Zarahemla, hawa ndugu zetu wapendwa, ambao wametupenda sana, wangekuwa bado wanasumbuliwa na [a]chuki juu yetu, ndiyo, na wangekuwa pia wageni kwa Mungu.

10 Na ikawa kwamba baada ya Amoni kusema maneno haya, ndugu yake Haruni alimkemea, akisema: Amoni, ninaogopa kwamba shangwe yako imekusababisha kuelekea kujisifu.

26 1*a* Mos. 28:9; Alma 17:6–11.
3*a* Alma 23:8–13.
b 2 Kor. 4:5; Mos. 23:10.
4*a* Alma 23:5.
5*a* Yn. 4:35–37; M&M 4:4.
b Yoe. 3:13.
c M&M 33:7–11; 75:2, 5.
6*a* Hel. 5:12; 3 Ne. 14:24–27.
7*a* MWM Mavuno.
b Mos. 23:22; Alma 36:28.
8*a* M&M 25:12.
b MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
9*a* Mos. 28:1–2.

11 Lakini Amoni alimwambia: Mimi [a]sijisifu kwa nguvu yangu, wala kwa hekima yangu; lakini tazama, [b]shangwe yangu ni tele, ndiyo, moyo wangu umejawa na shangwe, na nitafurahi ndani ya Mungu wangu.

12 Ndiyo, najua kwamba mimi si kitu; kulingana na nguvu zangu mimi ni mlegevu; kwa hivyo sitaweza [a]kujivuna mwenyewe, lakini nitajivuna katika Mungu wangu, kwani kwa [b]nguvu zake naweza kufanya vitu vyote; ndiyo, tazama, miujiza mingi mikuu tumetenda kwenye nchi hii, ambayo kwayo tutasifu jina lake milele.

13 Tazama, ni maelfu mangapi ya ndugu zetu ambao amewaachilia kutoka kwa uchungu wa [a]jehanamu; na wamefanywa [b]kuimba upendo ukomboao, na haya kwa sababu ya uwezo wa neno lake, ambao uko ndani yetu, kwa hivyo, si tuna sababu kuu ya kufurahi?

14 Ndiyo, tuna sababu ya kumsifu milele, kwani yeye ni Mungu Aliye Juu Sana, na amewafungua ndugu zetu kutoka kwenye [a]minyororo ya jehanamu.

15 Ndiyo, walizungukwa na giza lisilo na mwisho na uharibifu; lakini tazama, amewaleta kwenye [a]mwangaza usio na mwisho, ndiyo, kwenye wokovu usio na mwisho; na wamezungukwa na ukarimu usiolinganishwa wa mapenzi yake; ndiyo, na tumekuwa vyombo mikononi mwake vya kufanya kazi hii kuu na ya kushangaza.

16 Kwa hivyo, wacha [a]tusifu, ndiyo, [b]tutamsifu Bwana; ndiyo, tutafurahi, kwani shangwe yetu imejaa; ndiyo, tutamsifu Mungu wetu milele. Tazama, ni nani anayeweza kufurahia sana kwa Bwana? Ndiyo, ni nani anaweza kuongea sana juu ya uwezo wake mkuu, na [c]huruma yake, na uvumilivu wake kwa watoto wa watu? Tazama nasema kwenu, siwezi kusema sehemu ndogo ya yale ambayo ninahisi.

17 Ni nani ambaye angefikiria kwamba Mungu wetu angekuwa na huruma nyingi hivyo ili kutuokoa kutoka kwenye hali yetu chafu, ya kutisha, na yenye dhambi?

18 Tazama, tulienda mbele, kwa hasira na vitisho vingi [a]kuangamiza kanisa lake.

19 Ee basi, kwa nini hakutuweka sisi kwenye maangamizo ya kutisha, ndiyo, kwa nini hakuachilia panga lake la haki kutuangukia, na kutulaani sisi kwa kutukatisha tamaa milele?

20 Ee, nafsi yangu, kama ilivyo, iko karibu kukimbia kutoka kwa wazo hilo. Tazama, hakutumia haki yake kwetu, lakini kwa hekima yake kuu

11 *a* 2 Kor. 7:14.
b M&M 18:14–16. MWM Shangwe.
12 *a* Yer. 9:24; Alma 29:9.
b Zab. 18:32–40; Flp. 4:13; 1 Ne. 17:3.
13 *a* MWM Jehanamu.
b Alma 5:26.
14 *a* Alma 12:11.
15 *a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
16 *a* Rum. 15:17; 1 Kor. 1:31.
b 2 Kor. 10:15–18; M&M 76:61.
c Zab. 36:5–6.
18 *a* Mos. 27:8–10.

ametuleta sisi nje ya [a]shimo lile lisilo na mwisho la kifo na taabu, hata kwenye wokovu wa nafsi zetu.

21 Na sasa tazama, ndugu zangu, ni mtu gani wa [a]kawaida ambaye anajua vitu hivi? Nawaambia ninyi, hakuna yeyote ambaye [b]anaelewa hivi vitu, isipokuwa wenye kutubu.

22 Ndiyo, yule ambaye [a]anatubu na kutimiza [b]imani, na kutenda kazi nzuri, na kuomba wakati wote bila kikomo—kwa hawa wamepewa kujua [c]siri za Mungu; ndiyo, kwa hawa wamepawa kufunua vitu ambavyo havijawahi kufunuliwa; ndiyo, na watapaswe kupewa maelfu ya nafsi kwenye toba, kama vile tulivyopewa sisi kuwaleta ndugu zetu hawa kwenye toba.

23 Sasa mnakumbuka, ndugu zangu, kwamba tuliwaambia ndugu zetu kwenye nchi ya Zarahemla, tunaenda kwenye nchi ya Nefi, tuhubirie ndugu zetu, Walamani, na wakatucheka kwa madharau?

24 Kwani walituambia: Mnafikiri kwamba mnaweza kuwafahamisha Walamani ukweli? Mnafikiri mnaweza kuwasadikisha Walamani makosa ya [a]desturi za babu zao, wakiwa watu wenye [b]shingo ngumu vile walivyo; ambao mioyo yao hufurahia kwa umwagaji wa damu; ambao siku zao zimetumika kwa maovu mabaya sana; ambao njia zao zimekuwa njia za mhalifu tangu mwanzo? Sasa ndugu zangu, mnakumbuka kwamba hii ndiyo ilikuwa lugha yao.

25 Na tena walisema: Acha tuchukue silaha dhidi yao, ili tuwaangamize na maovu yao kutoka nchini, kwa maana wanaweza kutupita na kutuua.

26 Lakini tazama, ndugu zangu wapendwa, tulikuja nyikani sio na nia ya kuwaangamiza ndugu zetu, lakini nia ilikuwa labda tungeponya wachache wao.

27 Sasa wakati mioyo yetu ilihuzunishwa, na tukawa karibu kurudi, tazama, Bwana [a]alitufariji, na kusema: Nendeni miongoni mwa ndugu zenu, Walamani, na mvumilie [b]mateso yenu kwa [c]subira, na nitawapatia mafanikio.

28 Na sasa tazama, tumekuja, na tumekuwa miongoni mwao; na tumekuwa wavumilivu kwenye maumivu yetu, na tumevumilia aina yote ya masumbuko; ndiyo, tumesafiri kutoka nyumba hadi nyingine, tukitegemea huruma ya walimwengu—sio huruma ya walimwengu pekee lakini juu ya huruma za Mungu.

29 Na tumeingia kwenye nyumba zao na kuwafundisha, na tumewafundisha kwenye njia za miji yao; ndiyo, na tumewafundisha kwenye vilima vyao;

20 *a* 2 Ne. 1:13; Hel. 3:29–30.
21 *a* MWM Mwanadamu wa Tabia ya Asili.
b 1 Kor. 2:9–16; Yak. (KM) 4:8.
22 *a* Alma 36:4–5. MWM Toba, Tubu.
b MWM Amini, Imani.
c MWM Siri za Mungu.
24 *a* Mos. 10:11–17.
b Mos. 13:29.
27 *a* Alma 17:9–11.
b Alma 20:29–30. MWM Shida.
c MWM Subira.

na pia tumeingia kwenye hekalu zao na masinagogi yao na kuwafundisha; na tumetupwa nje, na kufanyiwa mzaha, na kutemewa mate, na kupigwa kwenye mashavu ya uso; na tumepigwa na mawe, na kuchukuliwa na kufungwa kwa kamba za nguvu, na kutupwa gerezani; na kupitia kwa nguvu na hekima wa Mungu tumekombolewa tena.

30 Na tulivumilia aina yote ya mateso, na tulifanya haya yote, kwamba labda tungepata njia ya kuponya watu; na tulifikiri kwamba [a]shangwe yetu ingejaa ikiwa labda tungekuwa na njia ya kuwaokoa wengine.

31 Sasa tazama, tungeweza kuona mbele na kuona matunda ya kazi zetu, na ni wachache? Ninawaambia: Hapana, ni [a]wengi; ndiyo, na tunaweza kushuhudia uaminifu wao, kwa sababu ya mapenzi yao juu ya ndugu zao na pia sisi.

32 Kwani tazama, [a]wangejitolea dhabihu maisha yao kuliko kuwaua adui wao; na [b]wamezika silaha zao za vita udongoni, kwa sababu ya mapenzi yao juu ya ndugu zao.

33 Na sasa tazama, nawaambia ninyi, kumewahi kuwa na mapenzi makuu hivi nchini kote? Tazama, nawaambia, La, hakujakuwepo, hata miongoni mwa Wanefi.

34 Kwani tazama, wangechukua silaha dhidi ya ndugu zao; hawangevumilia wenyewe wauawe. Lakini tazameni ni wangapi baina ya hawa ambao wametoa maisha yao; na tunajua kwamba wameenda kwa Mungu wao, kwa sababu ya mapenzi yao na kwa sababu ya chuki yao kwa dhambi.

35 Sasa si tunayo sababu ya kufurahi? Ndiyo, nasema kwenu, hakujakuwa na watu ambao walikuwa na sababu kubwa hivyo ya kufurahi kama sisi, tangu mwanzo wa dunia; ndiyo, na shangwe yangu imenichukua mbali, hata kwa majivuno kwa Mungu wangu; kwani ana [a]uwezo wote, hekima yote, na akili yote; [b]anaelewa vitu vyote, na ni Kiumbe cha [c]huruma, hata kwenye wokovu, kwa wale ambao watatubu na kuamini kwa jina lake.

36 Sasa kama hii ni kujivuna, na hata iwe hivyo nitajivuna; kwani haya ni maisha yangu na mwangaza wangu, shangwe yangu na wokovu wangu, na ukombozi wangu kutoka kwa taabu usio na mwisho. Ndiyo, libarikiwe jina la Mungu wangu, ambaye amewajali watu hawa, ambao ni [a]tawi la mti wa Israeli, na limepotea kutoka kwenye shina lake kwenye nchi ngeni; ndiyo, ninasema, heri jina la Mungu wangu, ambaye amekuwa mwangalifu kwetu, [b]wazururaji kwenye nchi geni.

37 Sasa ndugu zangu, tunaona

30 *a* M&M 18:15–16.
31 *a* Alma 23:8–13.
32 *a* Alma 24:20–24.
b Alma 24:15.
35 *a* MWM Uwezo.
b M&M 88:41.
c MWM Rehema, enye Rehema.
36 *a* Mwa. 49:22–26; Yak. (KM) 2:25; 5:25.
b Yak. (KM) 7:26.

kwamba Mungu ni mwangalifu kwa kila [a]watu, nchi yoyote ambayo wangekuwa ndani; ndiyo, huhesabu watu wake, na ana huruma za kutosha kwa ulimwengu wote. Sasa hii ndiyo shangwe yangu, na shukrani yangu nyingi; ndiyo, na nitatoa shukrani kwa Mungu wangu milele. Amina.

MLANGO WA 27

Bwana anamwamuru Amoni awaongoze watu wa Anti-Nefi-Lehi kwenye usalama—Wakati anakutana na Alma, shangwe ya Amoni inapunguza nguvu zake—Wanefi wanagawia wa Anti-Nefi-Lehi nchi ya Yershoni—Wanaitwa watu wa Amoni. Karibia mwaka 90–77 K.K.

Sasa ikawa kwamba wakati wale Walamani ambao walikuwa wameanzisha vita na Wanefi walipata, baada ya kujaribu mara nyingi kuwaangamiza, kwamba ilikuwa ni bure kutazamia kuwaangamiza, walirudi tena kwa nchi ya Nefi.

2 Na ikawa kwamba Waamaleki, kwa sababu ya hasara yao, walikasirika kupita kiasi. Na walipoona kwamba hawangelipiza kisasi kwa Wanefi, walianza kuwavuruga watu kuwa na hasira dhidi ya [a]ndugu zao, watu wa [b]Anti-Nefi-Lehi; kwa hivyo walianza tena kuwaangamiza.

3 Sasa hawa watu walikataa [a]tena kutwaa silaha zao, na wakavumilia wenyewe wauawe vile maadui wao walivyotaka.

4 Sasa Amoni na ndugu zake walipoona hii kazi ya mauaji baina ya wale ambao waliwapenda sana, na kati ya wale waliowapenda—kwani walikuwa wanatendewa kama kwamba ni malaika waliotumwa kutoka kwa Mungu kuwaokoa kutoka kwa maangamizo yasiyo na mwisho—kwa hivyo, Amoni na ndugu zake walipoona kazi hii kubwa ya mauaji, walivurugwa na huruma, na [a]wakamwambia mfalme:

5 Acha tukusanye pamoja hawa watu wa Bwana, na acha sisi tuteremke kwenye nchi ya Zarahemla mahali pa ndugu zetu Wanefi, na tutoroke kutoka mikono ya maadui wetu, ili tusiuawe.

6 Lakini mfalme aliwambia: Tazama, Wanefi watatuangamiza, kwa sababu ya mauaji mengi na dhambi ambazo tumetenda dhidi yao.

7 Na Amoni akasema: Nitaenda kuuliza kutoka kwa Bwana, na ikiwa atatuambia, nendeni mahali ndugu zenu wapo, je, utaenda?

8 Na mfalme akamwambia: Ndiyo, ikiwa Bwana atatuambia twende, tutaenda chini kwenye ndugu zetu, na tutakuwa watumwa wao hadi tutakapowalipa mauaji mengi na dhambi ambazo tumetenda dhidi yao.

9 Lakini Amoni aliwaambia: Ni kinyume cha sheria ya ndugu

37*a* Mdo. 10:34–35; 2 Ne. 26:33.
27 2*a* Alma 43:11.
b Alma 25:1. MWM Waanti-Nefi-Lehi.
3*a* Alma 24:21–26.
4*a* Alma 24:5.

zetu, ambayo ilianzishwa na baba yangu, kwamba kusiwe na [a]watumwa baina yao; kwa hivyo acha twende chini na kutegemea juu ya rehema ya ndugu zetu.

10 Lakini mfalme aliwambia: Mwulize Bwana, na ikiwa atatuambia twende, tutaenda; la sivyo tutaangamia hapa nchini.

11 Na ikawa kwamba Amoni akaenda na kumwuliza Bwana, na Bwana akamwambia:

12 Toa hawa watu kutoka nchi hii, ili wasiangamie; kwani Shetani ameshikilia mioyo ya Waamaleki, ambao wanawavuruga Walamani kukasirika dhidi ya ndugu zao kuwaua; kwa hivyo nendeni ninyi nje ya nchi hii; na heri kwa watu hawa wa kizazi hiki, kwani nitawahifadhi.

13 Na sasa ikawa kwamba Amoni alienda na kumwambia mfalme maneno yote ambayo Bwana alikuwa amemwambia.

14 Na wakakusanya pamoja watu wao wote, ndiyo, watu wote wa Bwana, na walikusanya mifugo yao yote na makundi, na kutoka katika nchi, na kwenda kwenye nyika ambayo ilitenganisha nchi ya Nefi kutoka kwa nchi ya Zarahemla, na ilikuwa juu karibu na mpaka wa nchi.

15 Na ikawa kwamba Amoni aliwaambia: Tazama, mimi na ndugu zangu tutaenda mbele kwenye nchi ya Zarahemla, na mtabaki hapa mpaka tutakaporudi; na tutajaribu mioyo ya ndugu zetu, kama watakubali mje kwa nchi yao.

16 Na ikawa kwamba wakati Amoni alipokuwa anaenda mbele nchini, ndiyo yeye na ndugu zake walikutana na Alma, juu [a]mahali ambapo palikuwa pame zungumzwa; na tazama, huu ulikuwa mkutano wa furaha.

17 Sasa [a]shangwe ya Amoni ilikuwa nyingi sana hata ikajaa; ndiyo, alimezwa kwenye shangwe ya Mungu wake, hata [b]akapungukiwa na nguvu; na akainama [c]tena kwenye ardhi.

18 Sasa si hii ilikuwa shangwe kuu? Tazama, hii ni shangwe ambayo hakuna yeyote aipataye isipokuwa tu yule ambaye ametubu na anayetafuta furaha kwa unyenyekevu.

19 Sasa shangwe ya Alma kukutana na ndugu zake kwa kweli ilikuwa kubwa, na pia shangwe ya Haruni, ya Omneri, na Himni; lakini tazama shangwe yao haikuwa ya kushinda nguvu zao.

20 Na sasa ikawa kwamba Alma aliwaongoza ndugu zake kurudi kwa nchi ya Zarahemla; hata kwenye nyumba yake. Na walienda na kumwambia [a]mwamuzi mkuu vitu vyote ambavyo vilitendeka kwao kwenye nchi ya Nefi, miongoni mwa ndugu zao, Walamani.

21 Na ikawa kwamba mwamuzi mkuu alituma tangazo nchini kote, akiuliza maoni ya

9 *a* Mos. 2:13; 29:32, 38, 40.
16 *a* Alma 17:1–4.
17 *a* MWM Shangwe.
b 1 Ne. 1:7.
c Alma 19:14.
20 *a* Alma 4:16–18.

watu kuhusu kukubaliwa kwa ndugu zao, ambao walikuwa watu wa Anti-Nefi-Lehi.

22 Na ikawa kwamba sauti ya watu ilirudi, ikisema: Tazama, tutaitoa nchi ya Yershoni, ambayo iko mashariki kando ya bahari, ambayo inaungana na nchi ya Neema, ambayo iko kusini mwa nchi ya Neema; na hii nchi ya Yershoni ndiyo nchi ambayo tutawapatia ndugu zetu kwa urithi.

23 Na tazama, tutaweka majeshi yetu katikati ya nchi ya Yershoni na nchi ya Nefi, ili tuwalinde ndugu zetu kwenye nchi ya Yershoni; na hivi tunafanya kwa ajili ya ndugu zetu, kwa sababu ya woga wao wa kuchukua silaha dhidi ya ndugu zao wakihofia kutenda dhambi; na huu woga wao mwingi uliwajia kwa kutubu sana, kwa sababu ya mauaji yao mengi na maovu yao ya kutisha.

24 Na sasa tazama, hivi ndivyo tutawafanyia ndugu zetu, ili warithi nchi ya Yershoni; na tutawakinga kutoka kwa maadui wao na majeshi yetu, kwa masharti kwamba watatoa sehemu ya mazao yao kutusaidia sisi ili tudumishe majeshi yetu.

25 Sasa, ikawa kwamba Amoni alipokuwa amesikia hivi, alirejea kwa watu wa Anti-Nefi-Lehi, na pia akiwa na Alma, kwenye nyika, ambapo walikuwa wamepiga hema zao, na kuwajulisha hivi vitu vyote. Na Alma pia aliwaambia juu ya [a]uongofu wake, na Amoni na Haruni, na ndugu zake.

26 Na ikawa kwamba ilisababisha shangwe nyingi miongoni mwao. Na wakaelekea chini kwenye nchi ya Yershoni, na kumiliki nchi ya Yershoni; na wakaitwa na Wanefi watu wa Amoni; kwa hivyo walitambulika kwa hilo jina siku zote za baadaye.

27 Na walikuwa miongoni mwa watu wa Nefi, na pia wakahesabiwa miongoni mwa watu ambao walikuwa kwenye kanisa la Mungu. Na pia walitambulika kwa juhudi yao kwa Mungu, na pia kwa watu; kwani walikuwa wakamilifu na wa [a]kuaminiwa na wa kusimama wima kwa vitu vyote; na walikuwa [b]imara kwa imani yao ya Kristo, hadi mwisho.

28 Na waliangalia kumwaga damu ya ndugu zao ni machukizo makuu; na hawangeweza kushawishiwa kuchukua silaha dhidi ya ndugu zao; na hawakuona kifo kwa woga wowote, kwa matumaini na maoni yao nikatika Kristo na ufufuo; kwa hivyo, kifo kilimezwa kwao na ushindi wa Kristo juu yake.

29 Kwa hivyo, wangevumilia [a]kifo kwa njia ya kukasirika na kuudhika ambayo ndugu zao waliwapasha, mbele ya kuchukua panga au kitara kuwaua.

30 Na hivyo walikuwa watu wa juhudi na wapendwa, watu ambao walipendwa sana na Bwana.

25*a* Mos. 27:10–24.
27*a* MWM Mwaminifu, Uaminifu.
b Alma 23:6.
29*a* Alma 24:20–23.

MLANGO WA 28

Walamani wanashindwa kwenye vita vya kutisha—Maelfu na maelfu wauawa—Waovu wanahukumiwa wawe katika hali ya masumbuko ya milele; wenye wema wanapokea furaha isiyo na mwisho. Karibia mwaka 77–76 K.K.

Na ikawa kwamba baada ya watu wa Amoni kuimarishwa kwenye nchi ya Yershoni, na kanisa pia kuanzishwa kwenye nchi ya [a]Yershoni, na majeshi ya Wanefi kuwekwa kila mahali kwenye nchi ya Yershoni, ndiyo, kwenye mipaka yote kuzunguka nchi ya Zarahemla; tazama majeshi ya Walamani yalikuwa yamewaandama ndugu zao hadi kwenye nyika.

2 Na hivyo kulikuwa na vita vya kutisha; ndiyo, hata vita kama hivyo havikuwa vimeonekana kamwe miongoni mwa watu wote nchini kutoka Lehi alipotoka Yerusalemu; ndiyo, na maelfu na maelfu ya Walamani waliuawa na kutawanywa kila mahali.

3 Ndiyo, na pia kulikuwa na mauaji ya ajabu miongoni mwa watu wa Nefi; lakini, Walamani [a]walifukuzwa na kutawanywa, na watu wa Nefi walirudi tena kwa nchi yao.

4 Na sasa huu ulikuwa wakati ambao kulikuwa na huzuni na vilio vilivyosikika kote nchini, miongoni mwa watu wa Nefi—

5 Ndiyo, vilio vya wajane wakiomboleza mabwana zao, na pia baba wakiomboleza wana wao; na binti kwa kaka, ndiyo, kaka kwa baba; na hivyo vilio vya kuombeleza vilisikika miongoni mwao wote, wakiomboleza jamaa zao ambao waliuawa.

6 Na sasa hii ilikuwa siku ya huzuni; ndiyo, wakati wa unadhiri, na wakati wa [a]kufunga na kusali.

7 Na hivyo mwaka wa kumi na tano wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi ukaisha;

8 Na hii ni historia ya Amoni na ndugu zake, matembezi yao kwenye nchi ya Nefi, kuumia kwao nchini, masikitiko yao, na mateso yao, na shangwe yao isiyo na [a]kipimo, na makaribisho na ulinzi kutoka kwa ndugu zao kwenye nchi ya Yershoni. Na sasa Bwana, Mkombozi wa watu wote, aibariki nafsi zao milele.

9 Na hii ni historia ya vita na mabishano miongoni mwa Wanefi, na pia vita baina ya Wanefi na Walamani; na mwaka wa kumi na tano wa utawala wa waamuzi umeisha.

10 Na kutoka mwaka wa kwanza mpaka wa kumi na tano umeleta maangamizo ya maelfu ya maisha; ndiyo, umeleta vitendo vibaya vya umwagaji wa damu.

11 Na miili ya wengi imelazwa ardhini, wakati miili ya maelfu [a]inaoza kwa chunguchungu juu ya ardhi; ndiyo, na maelfu wengi [b]wanaomboleza

28 1*a* Alma 27:22; 30:1, 19.
3*a* Alma 30:1.
6*a* Alma 30:2.
8*a* Alma 27:16–19.
11*a* Alma 16:11.
b Alma 48:23; M&M 42:45–46.

kwa kupoteza jamii yao, kwa ajili wana sababu ya kuogopa, kulingana na ahadi za Bwana, kwamba wanadhainiwa masharti ya taabu ya daima.

12 Wakati maelfu wengi wa wengine kwa kweli wanaomboleza jamii yao, lakini wanafurahi na kushangilia kwa matumaini, na hata wanajua, kulingana na [a]ahadi za Bwana, kwamba wanainuliwa na kuishi kwa mkono wa kulia wa Mungu, kwa hali ya furaha daima.

13 Na hivyo tunaona vile [a]kutokuwa sawa kwingi kwa watu kwa sababu ya dhambi na makosa, na nguvu za ibilisi, ambayo huja kwa [b]mipango ya udanganyifu ambayo amefikiria kutega mioyo ya watu.

14 Na hivyo tunaona mwito mkuu wa uangalifu kwa watu kufanya kazi kwenye [a]shamba la mizabibu la Bwana; na hivyo tunaona sababu kuu ya huzuni, na pia ya kufurahi—huzuni kwa sababu ya vifo na uharibifu miongoni mwa watu, na shangwe kwa sababu ya [b]mwangaza wa Kristo ambao ni uzima.

MLANGO WA 29

Alma anatamani kuhubiri toba na juhudi ya malaika—Bwana anatoa walimu kwa mataifa yote—Alma anafurahia kazi ya Bwana na kwa kufaulu kwa Amoni na ndugu zake. Karibia mwaka 76 K.K.

Ee vile natamani ningekuwa malaika, na ningekuwa na matarajio ya moyo wangu, kwamba ningeenda mbele na kuhututubia watu na parapanda ya Mungu, na sauti ya kutingisha ulimwengu, na kuhubiri toba kwa watu wote!

2 Ndiyo, ningemtangazia kila mtu, kwa sauti kama ya radi, na mpango wa ukombozi, kwamba watubu na [a]waje kwa Mungu wetu, kwamba kusije kukawa huzuni zaidi juu ya dunia.

3 Lakini tazama, mimi ni mtu, na hukosa kwa matakwa yangu; kwani ninahitaji nitosheke na vitu ambavyo Bwana amenipatia.

4 Sitakiwi kubadilisha katika tamaa yangu amri imara na haki za Mungu, kwani najua kwamba hutoa kwa watu kulingana na [a]kutaka kwao, kama itakuwa kwenye kifo ama kwenye uhai; ndiyo, ninajua kwamba hugawanyia watu, ndiyo, huamuru kwao sheria ambazo hazibadiliki, kulingana na [b]kutaka kwao, ikiwa zitakuwa za wokovu au kwa uharibifu.

5 Ndiyo, na ninajua kwamba uzuri na uovu ulidhihirishwa mema na maovu yalidhihirisha mbele ya watu wote; yule asiyejua mema na maovu hana lawama; lakini yule [a]ajuaye uzuri

12 *a* Alma 11:41.
13 *a* 1 Ne. 17:35.
b 2 Ne. 9:28.
14 *a* MWM Shamba la mizabibu la Bwana.
b MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
29 2 *a* Omni 1:26; 3 Ne. 21:20.
4 *a* Zab. 37:4.
b MWM Haki ya uamuzi.
5 *a* 2 Ne. 2:18, 26; Moro. 7:15–19.
MWM Utambuzi, Kipawa cha.

na uovu, kwake itatolewa kulingana na matakwa yake, kama anataka uzuri au uovu, uzima au kifo, shangwe au majuto ya [b]moyo.

6 Sasa, nikiona kwamba najua hivi vitu, kwa nini nitamani kuliko vile ninavyoeza kazi ambayo nimeitiwa kufanya?

7 Kwa nini nitamani kwamba ningekuwa malaika, ili niwazungumzie watu wote wa ulimwengu?

8 Kwani tazama, Bwana huwakubali mataifa [a]yote, kila taifa na [b]lugha yake, kufundisha neno lake, ndiyo, kwa hekima, yote ambayo anaona [c]sawa wawe nayo; kwa hivyo tunaona kwamba Bwana hushauri kwa hekima, kulingana na yale ambayo ni ya haki na kweli.

9 Najua ile ambayo Bwana ameniamuru mimi, na ninatukuza ndani yake. [a]Sijitukuzi mimi mwenyewe, lakini natukuza ile ambayo Bwana ameniamuru; ndiyo, na hii ni furaha yangu, kwamba labda niwe chombo kwenye mikono ya Mungu kuleta nafsi moja katika toba; na hii ndiyo shangwe yangu.

10 Na tazama, ninapoona wengi wa ndugu zangu wametubu kweli, na kumkubali Bwana Mungu wao, ndipo nafsi yangu hujaa na shangwe; ndipo ninapokumbuka yale [a]ambayo Bwana amenifanyia mimi, ndiyo, hata kwamba amesikia sala yangu; ndiyo, ndipo ninapokumbuka mkono wake wa huruma ambao alinyosha kwangu.

11 Ndiyo, na pia nakumbuka utumwa wa babu zangu; kwani kwa kweli najua kwamba [a]Bwana aliwakomboa kutoka kwenye utumwa, na kufuatana na hayo alianzisha kanisa lake; ndiyo, Bwana Mungu, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo, aliwaokoa kutoka kwenye utumwa.

12 Ndiyo, nimekumbuka kila siku utumwa wa babu zangu; na kwamba yule Mungu ambaye [a]aliwakomboa kutoka kwa mikono ya Wamisri aliwakomboa kutoka kwa utumwa.

13 Ndiyo, na yule yule Mungu alianzisha kanisa lake miongoni mwao; ndiyo, na yule yule Mungu ameniita mimi kwa mwito mtakatifu, kuhubiri neno kwa watu wake, na amenifanikisha sana, matokeo ambayo [a]shangwe yangu imejaa.

14 Lakini mimi sijawi shangwe tu kwa [a]kufanikiwa kwangu pekee, lakini shangwe yangu imejaa zaidi kwa sababu ya kufanikiwa kwa ndugu zangu, ambao wamekuwa kwenye nchi ya Nefi.

15 Tazama, wamefanya kazi sana, na wameleta matunda mengi; na zawadi yao itakuwa kubwa aje!

16 Sasa, ninapofikiria mafani-

5*b* MWM Dhamiri.
8*a* 2 Ne. 29:12.
b M&M 90:11.
c Alma 12:9–11.
9*a* Alma 26:12.
10*a* Mos. 27:11–31.
11*a* Mos. 24:16–21; Alma 5:3–5.
12*a* Ku. 14:30–31.
13*a* M&M 18:14–16.
14*a* Alma 17:1–4.

kio ya hawa ndugu zangu roho yangu inabebwa, hata kama imetenganishwa kutoka kwa mwili, vile ilikuwa, kwani shangwe yangu ni kubwa sana.

17 Na sasa Mungu angewakubalia hawa, ndugu zangu, kwamba waketi kwenye ufalme wa Mungu; ndiyo, na pia wale ambao ni matokeo ya kazi yao kwamba wasitoke nje tena, lakini kwamba wamtukuze milele. Na afadhali Mungu akubali kwamba itendeke kulingana na maneno yangu, hata vile nilivyosema. Amina.

MLANGO WA 30

Korihori, mpinga Kristo, anamfanyia mzaha Kristo, Upatanisho, na roho ya unabii—Anafundisha kwamba hakuna Mungu, hakuna kuanguka kwa binadamu, hakuna adhabu kwa dhambi, na hakuna Kristo—Alma anashuhudia kwamba Kristo atakuja na vitu vyote vinashuhudia kuwa kuna Mungu—Korihori anadai ishara na anaangushwa na kusababishwa kuwa bubu—Ibilisi alikuwa amemtokea Korihori kama malaika na kumfundisha cha kusema—Korihori anakanyagwa chini na kufa. Karibia mwaka 76–74 K.K.

Tazama, sasa ikawa kwamba baada ya [a]watu wa Amoni kuimarishwa kwenye nchi ya Yershoni, ndiyo, na pia baada ya Walamani [b]kukimbizwa kutoka nchini, na wafu wao kuzikwa na watu wa nchi hiyo—

2 Sasa wafu wao hawakuhesabiwa kwa sababu ya wingi wa idadi yao; hata wafu wa Wanefi hawakuhesabiwa—lakini ikawa baada ya kuzika wafu wao, na pia baada ya siku za kufunga, na kuomboleza, na sala, (na ulikuwa mwaka wa kumi na sita wa utawala wa waamuzi kwa watu wa Nefi) kulianza kuwa na mfululizo wa amani kote nchini.

3 Ndiyo, na watu walijitahidi kuweka amri ya Bwana; na walikuwa wakamilifu kwa kuweka [a]masharti ya Mungu, kulingana sheria ya Musa; kwani walifundishwa [b]kutii sheria ya Musa hadi itakapotimizwa.

4 Kwa hivyo watu hawakuwa na msukosuko wowote katika mwaka wa kumi na sita wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

5 Na ikawa kwamba katika mwaka wa kumi na saba wa utawala wa waamuzi, kulikuwa na mfululizo wa amani.

6 Lakini ikawa kwenye mwisho wa mwaka wa kumi na saba, kulikuja mtu kwenye nchi ya Zarahemla, na alikuwa [a]mpinga Kristo, kwani alianza kuhubiria watu dhidi ya unabii ambao ulizungumzwa na manabii, kuhusiana na kuja kwa Kristo.

7 Sasa hakukuwa na sheria yeyote dhidi ya [a]imani ya mtu;

30 1*a* Alma 27:25–26. MWM Waanti-Nefi-Lehi. *b* Alma 28:1–3.
3*a* MWM Torati ya Musa. *b* 2 Ne. 25:24–27; Alma 25:15.
6*a* MWM Mpinga Kristo.
7*a* Alma 1:17.

kwani ilikuwa kinyume kabisa cha amri za Mungu kwamba kuwe na sheria inayoleta watu kutokuwa sawa.

8 Kwani hivyo ndivyo yasemavyo maandiko: [a]Chagua wewe siku ya leo, yule ambaye utamtumikia.

9 Sasa kama mtu alitaka kumtumikia Mungu, ilikuwa ni haki yake; kwa usahihi zaidi kama aliamini katika Mungu ilikuwa ni haki yake kumtumikia; lakini kama hakuamini kwake hakukuwa na sheria ya kumwadhibu.

10 Lakini kama aliua aliadhibiwa kwa [a]kifo; na kama alipora aliadhibiwa pia; na kama aliiba aliadhibiwa pia; na kama alizini aliadhibiwa pia; ndiyo, kwa huu uovu wote waliadhibiwa.

11 Kwani kulikuwa na sheria kwamba watu walihukumiwa kulingana na makosa yao. Walakini, hakukuwa na sheria dhidi ya imani ya mtu; kwa hivyo, mtu aliadhibiwa tu kwa makosa ambayo alikuwa amefanya; kwa hivyo watu wote walikuwa [a]sawa.

12 Na huyu mpinga Kristo, ambaye jina lake lilikuwa Korihori, (na sheria haingemshika) alianza kuhubiria watu kwamba hakutakuwa na Kristo. Na jinsi hii alihubiri, akisema:

13 Ee ninyi ambao mmefungiwa chini ya upumbavu na tumaini la bure, kwa nini mnajiweka mzigo na vitu vya upumbavu kama hivi? Kwa nini mnamtafuta Kristo? Kwani hakuna yeyote ajuaye chochote kitakachokuja.

14 Tazama, hivi vitu ambavyo mnaita unabii, ambavyo mnasema vinatolewa na manabii watakatifu, tazama, ni mila za upumbavu za baba zenu.

15 Mnajuaje ukweli wao? Tazama, hamwezi kujua vitu ambavyo [a]hamuoni; kwa hivyo hamwezi kujua kwamba kutakuwa na Kristo.

16 Mnaona mbele na kusema kwamba mnaona msamaha wa dhambi zenu. Lakini tazama, ni matokeo ya wenda wazimu wa akili; na hii michafuko ya akili yenu inawajia kwa sababu ya desturi za babu zenu, ambazo zinawaongoza mbali kwa kuamini kwa vitu ambavyo havipo.

17 Na vitu vingi vya aina hii aliwazungumzia, akiwaambia kwamba hakutakuwa na upatanisho utakaofanywa kwa dhambi za watu, lakini kila mtu hufaulu katika maisha haya kulingana na vile alijiendesha; kwa hivyo kila mtu alifanikiwa kulingana na akili yake, na kila mtu alishinda kulingana na nguvu yake; na chochote ambacho mtu alifanya si kosa.

18 Na hivyo aliwahubiria, akipotosha mbali mioyo ya wengi, na kuwafanya kubeba vichwa vyao kwa uovu, ndiyo, akidanganya wanawake wengi, na pia wanaume, kutenda ukahaba—akiwaambia kwamba mtu akifa, huo ndiyo mwisho wake.

8*a* Yos. 24:15.
MWM Haki ya uamuzi.
10*a* MWM Adhabu Kuu.
11*a* Mos. 29:32.
15*a* Eth. 12:5–6.

19 Sasa huyu mtu alienda hadi kwenye nchi ya Yershoni pia, kuhubiri vitu hivi miongoni mwa watu wa Amoni, ambao walikuwa awali watu wa Walamani.

20 Lakini tazama walikuwa werevu kuliko wengi wa Wanefi; kwani walimchukua, na kumfunga, na kumbeba na kumpeleka mbele ya Amoni, ambaye alikuwa kuhani mkuu juu ya watu hao.

21 Na ikawa kwamba alilazimisha kwamba atolewe nje ya nchi. Na akaenda kwenye nchi ya Gideoni, na akaanza kuwahubiria pia; na pale hakufaulu sana, kwani alichukuliwa na kufungwa na kupelekwa mbele ya kuhani mkuu, pia mwamuzi mkuu juu ya nchi.

22 Na ikawa kwamba kuhani mkuu alimwambia: Kwa nini unazunguka ukiharibu njia za Bwana? Kwa nini unafundisha hawa watu kwamba hakutakuwa na Kristo, kukatisha furaha yao? Kwa nini unazungumza ubaya dhidi ya unabii wote wa manabii watakatifu?

23 Sasa jina la kuhani mkuu lilikuwa Gidona. Na Korihori akamwambia: Kwa sababu sifundishi desturi za upumbavu za babu zenu, na kwa sababu sifundishi hawa kujizuia wenyewe chini ya masharti na utaratibu ambao uliwekwa na makuhani wa zamani, kujitwalia nguvu na uwezo kwao, kuwaweka katika ujinga, kwamba wasiweze kubeba vichwa vyao, lakini wawekwe chini kufuatana na maneno yako.

24 Unasema kwamba hawa watu ni watu huru. Tazama, nasema wako kwenye utumwa. Unasema kwamba ule unabii wa zamani ni wa kweli. Tazama, nasema kwamba hujui kwamba ni kweli.

25 Unasema kwamba watu hawa wana makosa na ni watu walioanguka, kwa sababu ya dhambi ya mzazi. Tazama, nasema kwamba mtoto si mkosaji kwa sababu ya wazazi wake.

26 Na unasema pia kwamba Kristo atakuja. Lakini tazama, nasema kwamba hujui kwamba kutakuwa na Kristo. Na unasema kwamba atauawa kwa sababu ya [a]dhambi za ulimwengu—

27 Na hivyo unawapoteza hawa watu kufuata desturi za upuuzi za babu zenu, na kulingana na kutaka kwako; na unawaweka chini, hata vile walivyokuwa kwenye utumwa, kwamba ujishibishe na kazi ya mikono yao, ili wasiangalie juu na ujasiri, na kwamba wasifurahie haki na mapendeleo yao.

28 Ndiyo, hawatumii ile ambayo ni yao wasije wakachukiza makuhani wao, ambao wanawataabisha kufuatana na kutaka kwao, na wamewafanya kuamini, kupitia desturi zao na ndoto zao na upuzi wao na maono yao na siri za kujifanya, kwamba, ikiwa hawafanyi kufuatana na maneno yao, watachukiza kiumbe

26*a* Isa. 53:4–7.

ambacho hakijulikani, ambaye wanasema ni Mungu—kiumbe ambacho hakijaonekana au kujulikana, ambacho hakikuwepo wala hakitakuwepo.

29 Sasa kuhani mkuu na mwamuzi mkuu walipoona ugumu wa moyo wake, ndiyo, walipoona kwamba atatukana hata Mungu, hawakumjibu lolote kwa maneno yake; lakini wakasababisha kwamba afungwe; na walimkabidhi katika mikono ya askari, na wakampeleka katika nchi ya Zarahemla, kwamba angeletwa mbele ya Alma, na mwamuzi mkuu ambaye alikuwa mtawala juu ya nchi yote.

30 Na ikawa kwamba wakati alipopelekwa mbele ya Alma na mwamuzi mkuu, aliendelea kusema kwa njia sawa vile alivyofanya kwenye nchi ya Gideoni; ndiyo, aliendelea [a]kukufuru.

31 Na aliongea maneno kwa sauti [a]kubwa mbele ya Alma, na kuwatukana makuhani na walimu, akiwashtaki kwa kuwapoteza watu kwa kufuata desturi za ujinga za babu zao, kwa nia ya kujishibisha kwa kazi ya watu.

32 Sasa Alma alimwambia: Unajua kwamba hatujishibishi sisi wenyewe kwa kazi ya watu hawa; kwani tazama nimefanya kazi hata kutokea mwanzo wa utawala wa waamuzi mpaka sasa, kwa mikono yangu kwa kujitegemea, ingawa nilikuwa na safari nyingi kuzunguka nchi nikitangaza neno la Mungu kwa watu wangu.

33 Na ingawa nimefanya kazi nyingi kanisani, sijapokea hata zaidi ya [a]senine moja kwa kazi yangu; wala hata mmoja wa ndugu zangu, isipokuwa wakati tulikuwa kwenye kiti cha kutoa hukumu; na wakati huo tumepokea tu kulingana na sheria kwa wakati wetu.

34 Na sasa, kama hatuwezi kupokea chochote kwa kazi yetu kanisani, itatufaidi nini kufanya kazi kanisani isipokuwa tu kutangaza ukweli, ili tuweze kushangilia kwa shangwe kwa [a]raha ya ndugu zetu?

35 Basi kwa nini wewe unasema kwamba tunawahubiria hawa kupata faida, wakati wewe, mwenyewe, unajua kwamba hatupati faida yoyote? Na sasa unaamini kwamba tunadanganya hawa watu, ili tusababishe shangwe ndani ya mioyo yao?

36 Na Korihori akamjibu, Ndiyo.

37 Na kisha Alma akasema kwake: Unaamini wewe kwamba kuna Mungu?

38 Na akajibu, La.

39 Sasa Alma akasema kwake: Utakataa kwamba kuna Mungu, na pia kumkana Kristo? Kwani tazama, nakwambia, najua kuna Mungu, na pia kwamba Kristo atakuja.

40 Na sasa ni ushahidi gani unao kwamba hakuna [a]Mungu, au kwamba Kristo hatakuja? Nakwambia wewe kwamba

30 *a* MWM Kukufuru, Kufuru.
31 *a* Hel. 13:22.
33 *a* Alma 11:3.
34 *a* MWM Shangwe.
40 *a* Zab. 14:1.

huna lolote, isipokuwa tu maneno yako.

41 Lakini, tazama, nina vitu vyote kama [a]ushahidi kwamba hivi vitu ni kweli; na wewe pia una vitu vyote kama ushuhuda kwako kwamba ni vya kweli; na utakana hivi vitu? Unaamini kwamba hivi vitu ni kweli?

42 Tazama, najua kwamba unaamini, lakini unaongozwa na roho wa uwongo, na umeweka mbali Roho ya Mungu ili isiwe na pahali ndani yako; lakini ibilisi ana uwezo juu yako, na anakubeba kila mahali, akifanya ujanja ili aangamize watoto wa Mungu.

43 Na sasa Korihori alimwambia Alma: Ikiwa utanionyesha [a]ishara, kwamba ningesadikishwa kuwa kuna Mungu, ndiyo, nionyeshe kwamba ana uwezo, na ndipo nitakubali ukweli wa maneno yako.

44 Lakini Alma akamwambia: Wewe umepata ishara za kutosha; utamjaribu Mungu wako? Unaweza kusema, Nionyeshe ishara, wakati una ushuhuda wa hawa ndugu zako [a]wote, na pia manabii watakatifu? Maandiko yamewekwa mbele yako, ndiyo, na vitu [b]vyote vinaonyesha kwamba kuna Mungu; ndiyo, hata [c]dunia, na vitu vyote vilivyo juu yake, ndiyo, na [d]mwendo wake, ndiyo, na pia [e]sayari zote ambazo huenda kwa utaratibu wao zinashuhudia kwamba kuna Muumba Mkuu.

45 Na bado unaenda ukizunguka, ukidanganya mioyo ya watu hawa, ukitoa ushuhuda kwamba hakuna Mungu? Na bado utakana huu ushahidi wote? Na akasema: Ndiyo, nitakana isipokuwa unionyeshe ishara.

46 Na ikawa kwamba Alma akamwambia: Tazama, nimesikitika kwa sababu ya ugumu wa moyo wako, ndiyo, kwamba utazidi kushindana na roho ya ukweli, kwamba nafsi yako iangamizwe.

47 Lakini tazama, ni [a]afadhali roho yako ipotee kuliko kwamba uwe njia ya kuleta roho nyingi kwenye maangamizo, kwa udanganyifu wako na maneno yako ya kusifu ya uongo; kwa hivyo kama utakana tena, tazama Mungu atakupiga wewe, kwamba uwe bubu, kwamba hutafungua kinywa chako mara nyingine, kwamba hutaweza kudanganya hawa watu mara nyingine.

48 Sasa Korihori akamwambia: Sikatai kuweko kwa Mungu, lakini siamini kwamba kuna Mungu; na ninasema pia, kwamba hujui kuwa kuna Mungu; na isipokuwa unionyeshe ishara, sitaamini.

49 Sasa Alma akamwambia: Hii nitakupatia kwa ishara, kwamba [a]utapigwa na kuwa

41 *a* MWM Shahidi, Ushahidi.
43 *a* Yak. (KM) 7:13–21; M&M 46:8–9. MWM Ishara.
44 *a* Mos. 13:33–34.
b Zab. 19:1; M&M 88:47.
c Ayu. 12:7–10.
d Hel. 12:11–15.
e Musa 6:63.
47 *a* 1 Ne. 4:13.
49 *a* 2 Nya. 13:20.

bubu, kufuatana na maneno yangu; na ninasema, kwamba kwa jina la Mungu, utafanywa bubu, kwamba hutatamka tena.

50 Sasa wakati Alma alipokuwa amenena maneno haya, Korihori alipigwa na akawa bubu, kwamba hangeweza kunena tena, kufuatana na maneno ya Alma.

51 Na wakati mwamuzi mkuu alipoona hivi, alinyosha mkono wake na kuandika kwa Korihori, akisema: Umesadikishwa kwa nguvu za Mungu? Kwake ambaye ulitaka Alma aonyeshe ishara? Ulitaka kwamba atese wengine, akionyesha ishara? Tazama amekuonyesha ishara; na sasa hutabishana zaidi?

52 Na Korihori alinyoosha mkono wake na kuandika, akisema: Najua kwamba mimi ni bubu, kuwa siwezi kuongea; na ninajua kwamba hakuna kingine isipokuwa nguvu ya Mungu pekee ndiyo iliyoweza kuniletea mimi haya; ndiyo, na nilikuwa kila siku [a]najua kwamba kuna Mungu.

53 Lakini tazama, ibilisi [a]amenidanganya; kwani [b]alinitokea kwa mfano wa malaika, na akaniambia; Nenda na urudishe hawa watu, kwani wote wamepotea wakifuata Mungu asiyejulikana. Na akaniambia: [c]Hakuna Mungu; ndiyo, na akanifundisha yale ambayo ninahitaji kusema. Na nimefundisha maneno yake; na niliyafundisha kwa sababu yalikuwa yanapendeza kwa akili ya [d]kimwili; na niliyafundisha, hata ikawa ninafaulu sana, hata kwamba niliamini kwamba yalikuwa ya kweli; hata mpaka nimejiletea hii laana kuu kwangu.

54 Sasa wakati alikuwa amesema haya; alimsihi Alma kwamba amuombee Mungu, kwamba laana itolewe kwake.

55 Lakini Alma alimwambia: Laana hii ikitolewa kwako utapoteza mioyo ya watu tena; kwa hivyo, itakuwa nawe hata vile Bwana atakavyohitaji.

56 Na ikawa kwamba laana haikutolewa kutoka kwa Korihori; lakini alitupwa nje, na akaenda akitembea kutoka nyumba hadi nyingine akiomba chakula.

57 Sasa ufahamu wa yaliyompata Korihori mara moja ilitangazwa kote nchini; ndiyo, tangazo lilitolewa na mwamuzi mkuu kwa watu wote nchini, ikitangaziwa wale ambao walikuwa wameamini maneno ya Korihori kwamba lazima watubu mara moja, isije hukumu sawa ikaletwa kwao.

58 Na ikawa kwamba wote walisadikishwa kwa uovu wa Korihori; kwa hivyo wote walimgeukia tena Bwana; na hii ikaweka mwisho kwa uovu wa aina ya Korihori. Na Korihori alienda kutoka moja nyumba hadi nyingine, akiomba chakula kwa kujiweka hai.

59 Na ikawa kwamba alienda miongoni mwa watu, ndiyo,

52*a* Alma 30:42.
53*a* Yak. (KM) 7:14.
b 2 Kor. 11:14; 2 Ne. 9:9.
c Zab. 10:4.
d MWM Tamaa za kimwili.

miongoni mwa watu ambao walikuwa wamejitenga kutoka kwa Wanefi na kujiita Wazoramu, wakiongozwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa Zoramu—na alipoenda miongoni mwao, tazama, alishambuliwa na kukanyagwa chini, hadi akafa.

60 Na hivyo tunaona mwisho wa yule ambaye anapotosha njia za Bwana; na hivyo tunaona kwamba [a]ibilisi [b]hatasaidia watoto wake siku ya mwisho, lakini anawachukua kwa mbio hadi [c]jehanamu.

MLANGO WA 31

Alma anaongoza ujumbe kurudisha Wazorami waliopotea—Wazoramu wanamkana Kristo, wanaamini kwa wazo la uwongo la uchaguzi, na wanaabudu kwa sala zalizopangwa—Wamisionari wanajazwa na Roho Mtakatifu—Mateso yao yanamezwa kwenye shangwe ya Kristo. Karibia mwaka 74 K.K.

Sasa ikawa kwamba baada ya mwisho wa Korihori, Alma baada ya kupata habari kwamba Wazoramu wanapotosha neno la Bwana, na kwamba Zoramu, ambaye alikuwa kiongozi wao, alikuwa akiongoza mioyo ya watu [a]kusujudu kwa [b]viumbe visivyosikia wala kusema, moyo wake tena ulianza kuwa na [c]huzuni kwa sababu ya ubaya wa watu.

2 Kwani ilikuwa chanzo cha [a]huzuni kuu kwa Alma kujua kuhusu uovu miongoni mwa watu wake; kwa hivyo moyo wake ulikuwa na huzuni sana kwa sababu ya kutenganishwa kwa Wazoramu kutoka kwa Wanefi.

3 Sasa Wazoramu walikuwa wamejikusanya pamoja kwenye nchi iliyoitwa Antionumu ambayo ilikuwa mashariki mwa nchi ya Zarahemla, ambayo ilipakana karibu na juu ya ukingo wa bahari, ambayo ilikuwa kusini mwa nchi ya Yershoni, ambayo pia ilipakana na nyika kusini, nyika ambayo ilikuwa imejaa Walamani.

4 Sasa Wanefi waliogopa kwamba Wazoramu wangeanza mawasiliano na Walamani, na kwamba ingekuwa njia ya hasara kubwa kwa upande wa Wanefi.

5 Na sasa, kwa vile [a]kuhubiri kwa [b]neno kulikuwa na maelekezo makubwa ya [c]kuongoza watu kufanya yale ambayo ni haki—ndiyo, ilikuwa na matokeo ya nguvu zaidi kwa akili za watu kuliko upanga, au kitu chochote kingine, ambacho kiliwahi kufanyika kwao—kwa hivyo Alma alifikiri ilikuwa bora

60 *a* MWM Ibilisi.
b Alma 3:26–27; 5:41–42; M&M 29:45.
c MWM Jehanamu.

31 1 *a* Ku. 20:5; Mos. 13:13.
b 2 Ne. 9:37.
MWM Kuabudu sanamu.
c Alma 35:15.

2 *a* Mos. 28:3; 3 Ne. 17:14; Musa 7:41.

5 *a* Eno. 1:23; Alma 4:19.
MWM Hubiri.
b Ebr. 4:12; Yak. (KM) 2:8; Alma 36:26.
c Yar. 1:11–12; M&M 11:2.

kwamba wangejaribu matokeo ya uwezo wa neno la Mungu.

6 Kwa hivyo aliwachukua Amoni, na Haruni, na Omneri; na Himni alimwacha kanisani Zarahemla; lakini wa kwanza watatu walienda na yeye, na pia Amuleki na Zeezromu, ambao walikuwa Meleki; na pia aliwachukua wawili wa wanawe.

7 Sasa mkubwa kwa wanawe hakwenda na yeye, na jina lake lilikuwa [a]Helamani; lakini majina ya wale ambao alienda nao yalikuwa Shibloni na Koriantoni; na haya ndiyo majina ya wale ambao walienda na yeye miongoni mwa [b]Wazoramu, kuwahubiria neno.

8 Sasa Wazoramu walikuwa [a]wamekataa mafundisho ya Wanefi; kwa hivyo walikuwa wamepata neno la Mungu kuhubiriwa kwao.

9 Lakini walianza [a]kufanya makosa makubwa, kwani hawangeweza kuchunga amri za Mungu, na sheria zake, kulingana na sheria ya Musa.

10 Wala hawangechunga heshima za kanisa, kuendelea kwa sala na maombi Mungu kila siku, kwamba wasiingie kwenye majaribio.

11 Ndiyo, kwa ufupi, waliharibu njia za Bwana kwa namna nyingi; kwa hivyo, kwa sababu hii, Alma na ndugu zake waliondoka kwenda nchini kuhubiri neno kwao.

12 Sasa, walipowasili nchini, tazama, kwa mshangao wao walipata kwamba Wazoramu walikuwa wamejenga masinagogi, na kwamba walikuwa wakikusanyika pamoja siku moja ndani ya wiki, siku ambayo waliita siku ya Bwana; na waliabudu kwa njia ambayo Alma na ndugu zake hawajawahi kuona;

13 Kwani walikuwa na mahali palipojengwa katikati ya sinagogi yao, mahali pa kusimama, ambapo palikuwa parefu kupita kichwa; na juu yake yangetosha tu mtu mmoja.

14 Kwa hivyo, yeyote ambaye alitaka [a]kuabudu alilazimika kwenda na kusimama juu yake, na kunyosha mikono yake juu kueleka mbinguni, na kupaza sauti kuu, akisema:

15 Mtakatifu, mtakatifu Mungu; tunaamini kwamba wewe ni Mungu, na tunaamini kwamba wewe u mtakatifu, na kwamba ulikuwa roho, na ungali roho, na utakuwa roho milele.

16 Mungu Mtakatifu, tunaamini kwamba umetutenganisha sisi kutoka kwa ndugu zetu; na hatuamini katika desturi ya ndugu zetu, ambayo ilikabidhiwa kwao kwa njia ya utoto wa babu zao; lakini tunaamini kwamba [a]umetuchagua sisi kuwa watoto wako [b]watakatifu; na pia umetudhihirishia kwamba hakutakuwa na Kristo.

17 Lakini wewe ni yule yule jana, na leo, na milele; na [a]umetuchagua kwamba tutaokolewa,

7 *a* MWM Helamani, Mwana wa Alma.
b Alma 30:59.
8 *a* Alma 24:30.
9 *a* MWM Ukengeufu.
14 *a* Mt. 6:1–7.
16 *a* Alma 38:13–14.
b Isa. 65:3, 5.
17 *a* MWM Majivuno, Siofaa.

wakati wote ambao wametuzunguka wamechaguliwa kutupwa kwa na ghadhabu yako kwenye jehanamu; kwa ajili ya utakatifu huu, Ee Mungu, tunakushukuru; na pia tunakushukuru kwamba umetuchagua, kwamba tusipotezwe na desturi za upumbavu za ndugu zetu, ambazo zinawafungia chini kwa imani ya Kristo, ambayo inaongoza mioyo yao kutangatanga mbali kutoka kwako, Mungu wetu.

18 Na tena tunakushukuru wewe, Ee Mungu, kwamba sisi ni wateule na watu watakatifu. Amina.

19 Sasa ikawa kwamba Alma na ndugu zake na wanawe waliposikia sala hizi, walishtuka kupita kiasi.

20 Kwani tazama, kila mtu alienda mbele na kutoa sala zilizokuwa sawa.

21 Sasa mahali pale paliitwa na hawa Rameumtomu, ambayo ikifasiriwa, ni kituo kitakatifu.

22 Sasa, kutoka kwenye jukwa hili, walitoa, kila mmoja, sala sawa kwa Mungu, wakimshukuru Mungu wao kwamba walichaguliwa na yeye, na kwamba hakuwapoteza kutoka desturi ya ndugu zao, na kwamba mioyo yao haikudanganywa kuamini kwa matukio yanayokuja, ambayo hawakujua kuhusu chochote kuvihusu.

23 Sasa, baada ya watu wote kutoa shukrani kwa njia hii, walirejea kwao, [a]bila kuzungumza maneno ya Mungu wao tena hadi wakati wa kukusanyika tena kwenye kituo kitakatifu, kutoa shukrani kwa njia yao ya kawaida.

24 Sasa Alma alipoona haya moyo wake [a]ulihuzunika; kwani aliona kwamba watu walikuwa watu waovu na wakaidi; ndiyo, aliona kwamba mioyo yao ilitamani dhahabu, na fedha, na vitu vyote vilivyotengenezwa vizuri.

25 Ndiyo, na aliona pia kwamba mioyo yao ilikuwa [a]imeinuliwa kwa kujisifu sana, kwa kiburi chao.

26 Na alipaza sauti yake kuelekea mbinguni, na [a]kulia, akisema: Ee, kwa muda gani, Ee Bwana, utakubali kwamba watumishi wako waishi hapa chini katika mwili, kuona uovu mwingi miongoni mwa watoto wa watu?

27 Tazama, Ee Mungu, [a]wanaomba kwako, na bado mioyo yao imezidiwa na kiburi chao. Tazama, Ee Mungu, wanaomba kwako na midomo yao, wakati [b]wanatamani, hivi vitu vingine vya ulimwengu, kuliko kitu kingine.

28 Tazama, Ee Mungu wangu, mavazi yao ya bei ya juu, na pete zao, na [a]mikufu yao, na mapambo yao ya dhahabu, na vitu vyao vyote vya thamani ambavyo wamejipamba navyo; na tazama, mioyo yao

23*a* Yak. (Bib.) 1:21–25.
24*a* Mwa. 6:5–6.
25*a* Yak. (KM) 2:13; Alma 1:32.
26*a* Musa 7:41–58.
27*a* Isa. 29:13.
b MWM Kiburi.
28*a* Isa. 3:16–24.

iko kwenye hivi vitu, lakini wanaomba kwako wakisema—Tunakushukuru, Ee Mungu, kwani sisi ni watu wateule kwako, wakati wengine wataangamia.

29 Ndiyo, na wanasema kwamba umewahakikishia kwamba hakutakuwa na Kristo.

30 Ee Bwana Mungu, kwa muda gani utakubali kwamba uovu wa aina hii na ukafiri uwe miongoni mwa watu? Ee Bwana, utanipa nguvu, ili nivumilie na udhaifu wangu. Kwani mimi ni dhaifu, na uovu aina hii miongoni mwa watu hawa unaumiza roho yangu.

31 Ee Bwana, moyo wangu una huzuni nyingi sana; unaweza kutuliza nafsi yangu [a]katika Kristo. Ee Bwana unaweza kunikubalia niwe na nguvu, kwamba niweze kuvumilia haya mateso ambayo yatanijia mimi, kwa sababu ya maovu ya watu hawa.

32 Ee Bwana, utafariji roho yangu, na unipatie mafanikio, na pia wafanyikazi wenzangu ambao wako pamoja na mimi—ndiyo, Amoni, na Haruni, na Omneri, na pia Amuleki na Zeezromu, na pia [a]wana wangu wawili—ndiyo, hata hawa wote uwafariji, Ee Bwana. Ndiyo, ufariji roho zao katika Kristo.

33 Uwakubalie hawa kwamba wawe na nguvu, kwamba waweze kuvumilia mateso yao ambayo yatawajia kwa sababu ya maovu ya watu hawa.

34 Ee Bwana, [a]utukubalie sisi kwamba tuwe na mafanikio kwa kuwaleta kwako tena katika Kristo.

35 Tazama, Ee Bwana, [a]roho zao ni za thamani, na wengi wao ni ndugu zetu; kwa hivyo, tupatie, Ee Bwana, uwezo na hekima kwamba tuwalete hawa, ndugu zetu, tena kwako.

36 Sasa ikawa kwamba Alma aliposema maneno haya, kwamba [a]aliwawekea [b]mikono yake wale wote ambao walikuwa na yeye. Na tazama, alipoweka mikono yake juu yao, walijazwa na Roho Mtakatifu.

37 Na baada ya hayo walitawanyika wenyewe mmoja kutoka kwa mwingine, bila [a]kujifikiria wenyewe watakula nini, au kile watakachokunywa, au kile watakachovaa.

38 Na Bwana aliwaandalia kwamba wasiwe na njaa, wala wasiwe na kiu; ndiyo, na pia akawapatia nguvu, kwamba wasiteseke kwa namna yote ya [a]mateso, isipokuwa yamezwe kwenye shangwe ya Kristo. Sasa hii ilikuwa kulingana na sala ya Alma; na hii ni kwa sababu aliomba kwa [b]imani.

MLANGO WA 32

Alma anawafundisha walio masi-

31*a* Yn. 16:33.
32*a* Alma 31:7.
34*a* 2 Ne. 26:33.
35*a* MWM Nafsi—Thamani ya nafsi.
36*a* 3 Ne. 18:36–37.
b MWM Mikono, Kuweka juu ya.
37*a* Mt. 6:25–34; 3 Ne. 13:25–34.
38*a* Mt. 5:10–12; Mos. 24:13–15; Alma 33:23.
b MWM Amini, Imani.

kini ambao mateso yao yamewanyenyekeza—Imani ni tumaini kwa lile ambalo halionekani ambalo ni kweli—Alma anatoa ushuhuda kwamba malaika huwahudumia wanaume, wanawake, na watoto—Alma analinganisha neno na mbegu—Lazima ipandwe na kulishwa—Ndipo inakua kuwa mti ambao kutoka kwake matunda ya uzima wa milele huvunwa. Karibia mwaka 74 K.K.

Na ikawa kwamba waliendelea mbele, na kuanza kuhubiri neno la Mungu kwa watu, wakiingia kwenye masinagogi yao, na kwenye nyumba zao; ndiyo, na hata walihubiri neno kwenye mitaa yao.

2 Na ikawa kwamba baada ya kazi nyingi miongoni mwao, wakaanza kuwa na mafanikio miongoni mwa watu wa vyeo vya [a]chini; kwani tazama, walitupwa nje ya masinagogi kwa sababu ya nguo zao hafifu—

3 Kwa hivyo hawakuruhusiwa kuingia katika masinagogi yao kumwabudu Mungu, wakichukuliwa kama uchafu; kwa hivyo walikuwa masikini; ndiyo, walichukuliwa na ndugu zao kama takataka; kwa hivyo walikuwa [a]masikini kulingana na vitu vya ulimwengu; na pia walikuwa masikini katika mioyo yao.

4 Sasa, Alma alipokuwa akifundisha na akizungumza na watu kwenye mlima Onida, kulitokea umati mkubwa kwake, cha wale ambao tulikuwa tukizungumza juu yao, ambao walikuwa [a]masikini moyoni, kwa sababu ya umasikini wao kulingana na vitu vya ulimwengu.

5 Na wakamjia Alma; na yule ambaye alikuwa anawaongoza akamwambia: Tazama, ni [a]nini hawa ndugu zangu watafanya, kwani wanadharauliwa na watu wote kwa sababu ya umasikini wao, ndiyo, hasa na makuhani wetu; kwani [b]wametutupa nje ya masinagogi ambayo tuliyafanyia kazi kwa wingi kujenga kwa mikono yetu; na wametutupa nje kwa sababu ya umasikini wetu mkuu; na hatuna mahali pa kumuabudia Mungu wetu; na tazama, tutafanya [c]nini?

6 Na sasa Alma aliposikia haya, alimgeuza, uso wake mara moja, na kumwangalia, kwa shangwe kubwa; kwani aliona kwamba [a]mateso yao yalikuwa yamewafanya kwa kweli kuwa [b]wanyenyekevu, na kwamba walikuwa [c]wamejiandaa kusikiliza neno.

7 Kwa hivyo hakusema mengi kwa huo umati mwingine; lakini alinyoosha mbele mkono wake, na kupaza sauti kwa wale ambao aliwaona, ambao walikuwa kwa kweli wametubu, na akawaambia;

32 2*a* MWM Maskini.
3*a* Alma 34:40.
4*a* MWM Maskini—Maskini katika roho.
5*a* Mit. 18:23.
b Alma 33:10.
c Mdo. 2:37–38.
6*a* MWM Shida.
b MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
c Alma 16:16–17; M&M 101:8.

8 Ninaona kwamba [a]mmenyenyekea moyoni; na ikiwa ni hivyo, heri kwenu.

9 Tazama ndugu yenu alisema, Tutafanya nini?—kwani tumetupwa nje ya masinagogi yetu, kwamba hatuwezi kumuabudu Mungu wetu.

10 Tazama ninawaambia, mnafikiri kwamba hamwezi [a]kumuabudu Mungu isipokuwa kwenye masinagogi yenu pekee?

11 Na zaidi ya hayo, ningewauliza, mnafikiri kwamba lazima umwabudu Mungu tu siku moja kwa juma?

12 Nawaambia, ni vyema kwamba mmetupwa nje ya masinagogi yenu, ili muwe wanyenyekevu, na ili mjifunze [a]hekima; kwani ni lazima mjifunze hekima; kwani ni kwa sababu mmetupwa nje, kwamba mmedharauliwa na ndugu zenu kwa sababu ya [b]umasikini wenu mkuu, kwamba mioyo yenu imenyenyekea; kwani mnyenyekezwa kwa lazima.

13 Na sasa, kwa sababu mmelazimishwa kunyenyekea heri ninyi; kwani mtu wakati mwingine, akilazimishwa kunyenyekea, hutafuta toba; na sasa kwa kweli, yeyote anayetubu atapata huruma; na yule ambaye anapata huruma na [a]kuvumilia hadi mwisho huyo ataokolewa.

14 Na sasa, vile nilivyowaambia ninyi, kwamba kwa sababu mlilazimishwa kunyenyekea mlibarikiwa, hamdhani kwamba wale ambao wanajinyenyekeza kwa ukweli wenyewe kwa sababu ya neno wamebarikiwa zaidi?

15 Ndiyo, yule ambaye anajinyenyekeza mwenyewe kwa ukweli, na kutubu dhambi zake, na kuvumilia hadi mwisho, huyo atabarikiwa—ndiyo, atabarikiwa zaidi ya wale ambao hulazimishwa kunyenyekea kwa sababu ya umasikini wao mwingi.

16 Kwa hivyo, heri wale ambao [a]hunyenyekea wenyewe bila kulazimishwa kunyenyekea; kwa usahihi zaidi, heri yule ambaye anaamini katika neno la Mungu, na anabatizwa bila ukaidi wa moyo, ndiyo, bila kushurutishwa kujua neno, au hata kulazimishwa kujua, kabla ya kuamini.

17 Ndiyo, kuna wengi ambao husema: ikiwa utatuonyesha [a]ishara kutoka mbinguni, ndipo tutajua kwa hakika; halafu tutaamini.

18 Sasa ninauliza; hii ni imani? Tazama, nawaambia, Hapana; kwani ikiwa mtu anajua kitu hana sababu ya [a]kuamini, kwani anakijua.

19 Na sasa, hulaaniwaje zaidi ya yule ambaye [a]anajua mapenzi ya Mungu na hayatimizi, kuliko yule ambaye huamini tu, au ana sababu ya kuamini, na kuanguka kwenye makosa?

20 Sasa, kwa kitu hiki lazima

8*a* Mt. 5:3–5.
10*a* MWM Kuabudu.
12*a* Mh. 4:13.
b Mit. 16:8.
13*a* Alma 38:2.
16*a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
17*a* MWM Ishara.
18*a* Eth. 12:12, 18.
19*a* Yn. 15:22–24.

mhukumu. Tazama, nawaambia, kwamba ni sawa mkono mmoja hata vile ilivyo kwa mwingine; na itakuwa hivyo kwa kila mtu kulingana na vitendo vyake.

21 Na sasa nilivyosema kuhusu imani—[a]imani sio kuwa na ufahamu kamili wa vitu; kwa hivyo mkiwa na imani, [b]mnatumainia vitu ambavyo [c]havionekani, ambavyo ni vya kweli.

22 Na sasa, tazama, ninawaambia, na ningetaka kwamba mkumbuke, kwamba Mungu ni mwenye hekima kwa wote wanaoamini katika jina lake; kwa hivyo, anataka kwa mara ya kwanza, kwamba mwamini, ndiyo, hata katika neno lake.

23 Na sasa, yeye huwatolea wanadamu neno lake kwa malaika, ndiyo, [a]sio tu kwa wanaume peke yao lakini pia kwa wanawake. Sasa hii si yote; [b]watoto wadogo huwa na maneno wanayopewa mara nyingi, ambayo yanawafadhaisha werevu na wasomi.

24 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, kwa vile mnatamani kujua kutoka kwangu mtafanya nini kwa sababu mnasumbuliwa na kutupwa nje—sasa sitaki mfikirie kwamba ninamaanisha kutoa hukumu kwenu isipokuwa kulingana na yale ambayo ni kweli—

25 Kwani simaanishi kwamba ninyi nyote mmelazimishwa kujinyenyekeza; kwani ninaamini kwa ukweli kwamba kuna wengine kati yenu ambao wangenyenyekea wenyewe, hata wawe katika hali gani.

26 Sasa, vile nilivyosema kuhusu imani—kwamba haikuwa ufahamu kamili—hata hivyo ni kama maneno yangu. Hamwezi kujua ukweli wao kwanza, kwa ukamilifu, vile imani si ufahamu kamili.

27 Lakini tazama, ikiwa mtaamka na kuziwasha akili zenu, hata kwenye kujaribu juu ya maneno yangu na kutumia sehemu ya imani, ndiyo, hata ikiwa hamwezi ila [a]kutamani kuamini, acha hamu hii ifanye kazi ndani yenu, hata mpaka mwamini kwa njia ambayo mtatoa nafasi kwa sehemu ya maneno yangu.

28 Sasa, tutalinganisha neno na [a]mbegu. Sasa ikiwa mtatoa nafasi, ili [b]mbegu ipandwe ndani ya [c]moyo wako, tazama, ikiwa itakuwa mbegu ya kweli, au mbegu mzuri, ikiwa hamtaitupa nje kwa [d]kutoamini kwenu, kwamba mtashindana na Roho wa Bwana, tazama, itaanza kuvimba ndani ya vifua vyenu; na wakati mtakaposikia huu mwendo wa kuvimba, mtaanza kusema ndani yenu—inawezekana kwamba hii ni mbegu mzuri, au kwamba neno ni zuri, kwani linaanza kukua ndani ya nafsi yangu; ndiyo,

21 *a* Yn. 20:29; Ebr. 11.
b MWM Tumaini.
c Eth. 12:6.
23 *a* Yoe. 2:28–29.
b Mt. 11:25; Lk. 10:21; 3 Ne. 26:14–16; M&M 128:18.
27 *a* Mk. 11:24.
28 *a* Alma 33:1.
b Lk. 8:11.
c MWM Moyo.
d Mt. 17:20.

inaanza kuangaza [e]kuelewa kwangu, ndiyo, inaanza kunipendeza.

29 Sasa tazama, si hii itaongeza imani yenu? Ninawaambia, Ndiyo; walakini haijakua kwa ufahamu kamili.

30 Lakini tazama, wakati mbegu inapovimba, na kuchipua, na kuanza kukua, ndipo mtasema kwamba mbegu ni mzuri; kwani tazama inavimba, na kuchipua, na kuanza kukua. Na sasa, tazama, si hii itaimarisha imani yenu? Ndiyo, itaimarishaa imani yenu: kwani mtasema tunajua kwamba hii ni mbegu mzuri; kwani tazama inachipuka na inaanza kukua.

31 Na sasa, tazama, mna hakika kwamba hii ni mbegu mzuri? Nawaambia, Ndiyo; kwani kila mbegu huzaa [a]mfano wake.

32 Kwa hivyo kama mbegu inakua ni mzuri, lakini kama haikui, tazama si mzuri, kwa hivyo hutupiliwa mbali.

33 Na sasa, tazama, kwa sababu mmejaribu utafiti, na kupanda mbegu, na inavimba na kumea, na kuanza kukua, lazima mjue kwamba mbegu ni nzuri.

34 Na sasa, tazama, ufahamu wenu ni kamili? Ndiyo, [a]ufahamu wenu ni kamili kwa kile kitu, na [b]imani yenu inalala; na hii ni kwa sababu mnajua, kwani mnajua kwamba neno limevimbisha nafsi zenu, na pia mnajua kwamba limemea, kwamba ufahamu wenu umeanza kuelimika, na [c]akili zenu zinaanza kupanuka.

35 Ee basi, si hii ni kweli? Nawaambia, Ndiyo, kwa sababu ni [a]nuru; na chochote ambacho ni nuru, ni kizuri, kwa sababu kinaonekana, kwa hivyo lazima mjue kwamba ni nzuri; na sasa tazama, baada ya ninyi kuonja nuru hii si ufahamu wenu ni kamili?

36 Tazama nawaambia, Hapana; wala msiweke kando imani yenu, kwani mmejaribu tu imani yenu kupanda mbegu kwamba mngejaribu utafiti kujua kama mbegu ilikuwa mzuri.

37 Na tazama, mti ukianza kukua, mtasema: Acha tuulishe kwa uangalifu mkuu, kwamba uweze kupata mizizi, kwamba upate kukua, na kututolea matunda. Na sasa tazama, ikiwa mtaulisha kwa uangalifu mwingi mtapata mizizi, na kukua, na kuleta matunda.

38 Lakini [a]mkiuachilia mti ule, na msifikirie kuulisha, tazama hautapata mzizi wowote; na wakati joto la jua linawadia na kuuchoma, kwa sababu hauna mzizi hukaukia mbali, na mtaukata na kuutupa nje.

39 Sasa, hii sio kwa sababu mbegu haikuwa mzuri, wala sio kwa sababu tunda lake halingekuwa la kutamanika; lakini ni kwa sababu [a]udongo wenu ni mkame, na hamtaweza kuulisha

28 *e* MWM Ufahamu.
31 *a* Mwa. 1:11–12.
34 *a* MWM Maarifa.
b Eth. 3:19.
c MWM Nia.
35 *a* Yn. 3:18–21. MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
38 *a* MWM Ukengeufu.
39 *a* Mt. 13:5.

mti, kwa hivyo hamwezi kupata tunda juu yake.

40 Na hivyo, ikiwa hamtalisha neno, mkingojea tu kwa imani kupata tunda juu yake, hamwezi kuchuma tunda la [a]mti wa maisha.

41 Lakini ikiwa mtalisha neno, ndiyo, lisha mti unapoanza kukua, kwa imani yenu kwa bidii kuu, na [a]uvumilivu, mkitumainia kupata tunda kwake, utamea mizizi; na tazama utakuwa mti [b]unao chipua kuelekea maisha ya milele.

42 Na kwa sababu ya [a]bidii yenu na imani yenu na uvumilivu wenu kwa neno kwa kulilisha, kwamba limee ndani yenu, tazama, baadaye mtavuna [b]matunda kwake, ambayo ni ya thamani sana, ambayo ni matamu kupita kiasi, na ambayo ni meupe kupita kiasi, ndiyo, na safi kupita kiasi; na mtakula hili tunda mpaka hata mshibe, kwamba hamtapata njaa, wala kuona kiu.

43 Kisha, ndugu zangu, mtavuna zawadi ya imani yenu, na bidii yenu, na subira, na uvumilivu, mkingojea mti kuwatolea matunda.

MLANGO WA 33

Zeno alifundisha kwamba watu waombe na kuabudu mahali popote, na kwamba hukumu zimeondolewa kwa sababu ya Mwana—Zenoki alifundisha kwamba rehema inatolewa kwa sababu ya Mwana—Musa aliinua nyikani mfano wa Mwana wa Mungu. Karibia mwaka 74 K.K.

Sasa baada ya Alma kumaliza kusema maneno haya, walimtumia mnenaji wakitamani kujua kama wangeweza kumwamini katika [a]Mungu mmoja, ili waweze kupokea hilo tunda ambalo alilizungumzia, au vile wangeweza kupanda ile [b]mbegu, au hilo neno ambalo alilizungumzia, ambalo alisema lazima lipandwe ndani ya mioyo yao; au jinsi gani wangeanza kutumia imani yao.

2 Na Alma akawaambia: Tazama, mmesema kwamba [a]hamuwezi kumwabudu Mungu wenu kwa sababu mmetupwa nje ya masinagogi yenu. Lakini tazama, ninawaambia, ikiwa mnadhani ati hamuwezi kumwabudu Mungu, mnafanya kosa kubwa, na mnahitaji kupekua [b]maandiko; ikiwa mnadhania kwamba yamewafundisha hii, ninyi hamuelewi.

3 Je, mnakumbuka mlisoma yale ambayo [a]Zeno, nabii wa kale, aliyosema kuhusu sala au [b]ibada?

4 Kwani alisema: Wewe una rehema, Ee Mungu, kwani umesikia sala yangu, hata nilipokuwa nyikani; ndiyo, ulikuwa mwenye rehema wakati

40 *a* Mwa. 2:9; 1 Ne. 15:36.
41 *a* MWM Subira.
b Alma 33:23; M&M 63:23.
42 *a* MWM Bidii.
b 1 Ne. 8:10–12.
33 1 *a* 2 Ne. 31:21; Mos. 15:2–4.
b Alma 32:28–43.
2 *a* Alma 32:5.
b Alma 37:3–10.
3 *a* MWM Maandiko—Maandiko yaliyopotea; Zeno.
b MWM Kuabudu.

niliposali kuhusu wale ambao walikuwa [a]maadui zangu, na ukawarudisha kwangu.

5 Ndiyo, Ee Mungu, na ulikuwa na rehema kwangu wakati nilipokulilia kwenye [a]shamba langu; wakati nilipokulilia kwa sala yangu, na ulinisikiliza.

6 Na tena, Ee Mungu, wakati nilipoingia kwenye nyumba yangu ulinisikia mimi kwenye sala yangu.

7 Na wakati nilipoingia katika [a]kijumba changu, Ee Bwana, na kuomba kwako, na ulinisikia.

8 Ndiyo, una huruma kwa watoto wako, wakati wanakulilia wewe, ili wasikilizwe nawe na sio na watu, na utawasikiliza.

9 Ndiyo, Ee Mungu, umekuwa na rehema kwangu, na kusikia vilio vyangu miongoni mwa umati wako.

10 Ndiyo, na pia umenisikia wakati [a]nimetupwa nje na kudharauliwa na maadui zangu; ndiyo, ulisikia vilio vyangu, na uliwakasirikia maadui zangu, na ukawatembelea kwa ghadhabu yako na maangamizo ya haraka.

11 Na wewe ulinisikia kwa sababu ya mateso yangu na uaminifu wangu; na ni kwa sababu ya Mwana wako kwamba umekuwa na rehema jinsi hivyo kwangu, kwa hivyo nitakulilia wewe katika mateso yangu yote, kwani nina shangwe ndani yako; kwani umeniondolea hukumu zako, kwa sababu ya Mwana wako.

12 Na sasa Alma aliwaambia: Mnaamini hayo [a]maandiko ambayo yaliandikwa na wale wa kale?

13 Tazama ikiwa mnayaamini, lazima mwamini yaliyosemwa na [a]Zeno; kwani tazama, alisema: Umeondoa hukumu zako kwa sababu ya Mwana wako.

14 Sasa, tazama, ndugu zangu, ningeuliza kama mmesoma maandiko? Ikiwa mmeyasoma, jinsi gani mnaweza kutomwamini Mwana wa Mungu?

15 Kwani [a]haikuandikwa kwamba Zeno pekee ndiye alisema vitu hivi, lakini [b]Zenoki pia alizungumzia vitu hivi—

16 Kwani tazama, alisema: Umewakasirikia, Ee Bwana, watu hawa, kwa sababu hawataelewa rehema zako ambazo umewapatia kwa sababu ya Mwana wako.

17 Na sasa, ndugu zangu, mnaona kwamba nabii wa pili wa kale ameshuhudia juu ya Mwana wa Mungu, na kwa sababu ya watu kutoelewa maneno yake [a]walimpiga na mawe hadi akafa.

18 Lakini tazama, haya si yote; hawa sio pekee ambao wamezungumza kuhusu Mwana wa Mungu.

19 Tazama, alizungumziwa na [a]Musa; ndiyo, na tazama [b]mfano [c]uliinuliwa nyikani, kwamba

4 *a* Mt. 5:44.
5 *a* Alma 34:20–25.
7 *a* Mt. 6:5–6; Alma 34:26.
10 *a* Alma 32:5.
12 *a* MWM Maandiko.
13 *a* Alma 34:7.
15 *a* Yak. (KM) 4:4.
b 1 Ne. 19:10; Alma 34:7.
17 *a* MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
19 *a* Kum. 18:15, 18; Alma 34:7.
b Hes. 21:9; 2 Ne. 25:20; Mos. 3:15.
c Yn. 3:14; Hel. 8:14–15.

yeyote atakayeuangalia aweze kuishi. Na wengi waliangalia na wakaishi.

20 Lakini wachache walielewa maana ya vitu hivyo, na hii ni kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao. Lakini kulikuwa na wengi ambao walikuwa wagumu kiasi kwamba hawangeangalia, kwa hivyo waliangamia. Sasa sababu yao ya kukataa kuangalia ni kwa sababu hawakuamini kwamba [a]ingewaponya.

21 Ee ndugu zangu, ikiwa mngeponywa tu kwa kuangalia na macho yenu ili muweze kuponywa, msingetazama haraka, au ni afadhali mshupaze mioyo yenu kwa kutokuamini, na kuwa wavivu, kwamba msiangalie kwa macho yenu ili mweze kuangamia?

22 Ikiwa hivyo, taabu itawapata; lakini ikiwa si hivyo, basi zungusha macho yako na uanze [a]kuamini katika Mwana wa Mungu, kwamba atakuja kukomboa watu wake, na kwamba atateseka na kufa ili [b]alipie dhambi zao; na kwamba [c]atafufuka tena kutoka kwa wafu, na kutimiza [d]ufufuo, kwamba watu wote watasimama mbele yake, kuhukumiwa katika siku ya mwisho ya hukumu, kulingana na [e]matendo yao.

23 Na sasa, ndugu zangu, natamani kwamba [a]mtapanda hili neno kwenye mioyo yenu, na itakavyoanza kumea endelea kuvimba kwa imani yenu. Na tazama, itakuwa mti, [b]ukikua ndani yako kwenye maisha yasiyo na mwisho. Na kisha Mungu akubali kwamba [c]mizigo yenu iwe miepesi, kupitia kwa shangwe inayotokana na Mwana wake. Na hata haya yote mnaweza mkafanya mkipenda. Amina.

MLANGO WA 34

Amuleki anashuhudia kwamba neno liko ndani ya Kristo ili kusababisha wokovu—Isipokuwa upatanisho ufanywe, binadamu wote lazima wapotee—Sheria yote ya Musa inaelekeza kwa dhabihu ya Mwana wa Mungu—Mpango wa milele wa ukombozi unatokana na imani na toba—Omba baraka kwa vitu vya maisha ya kimwili na vya kiroho—Haya maisha ni wakati wa binadamu kujitayarisha kukutana na Mungu—Tia bidii katika wokovu wenu kwa kumwogopa Mungu. Karibia mwaka 74 K.K.

Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kuwazungumzia maneno haya aliketi chini juu ya ardhi, na [a]Amuleki aliamka na kuanza kuwafundisha, akisema:

2 Ndugu zangu, ninadhani kwamba ni vigumu kwamba msijue vitu ambavyo vimezungumziwa kuhusu kuja kwa Kristo, ambaye tunafundisha kwamba ni Mwana wa Mungu; ndiyo, ninajua kwamba [a]hivi vitu vilifundishwa kwenu kwa

20 *a* 1 Ne. 17:40–41.
22 *a* Alma 32:27–28.
b Alma 22:14; 34:8–9.
c MWM Ufufuko.
d Alma 11:44.
e MWM Matendo.
23 *a* Alma 33:1; 34:4.
b Alma 32:41; M&M 63:23.
c Alma 31:38.
34 1 *a* Alma 8:21.
2 *a* Alma 16:13–21.

wingi kabla ya mfarakano wenu kutoka miongoni mwetu.

3 Na kwa vile mmetaka kwamba ndugu yangu mpendwa awajulishe yale mnayostahili kufanya, kwa sababu ya mateso yenu; na amewazungumzia machache ili kuzitayarisha akili zenu; ndiyo, na amewasihi muwe na imani na uvumilivu—

4 Ndiyo, hata kwamba muwe na imani nyingi hata [a]mpande neno ndani ya mioyo yenu, ili mjaribu kujua uzuri wake.

5 Na tumeona kwamba swali kubwa ambalo liko kwenye akili zenu ni kama neno liko kwa Mwana wa Mungu, au kama hakutakuweko na Kristo.

6 Na mliona kwamba ndugu yangu amewathibitishia, kwa mifano mingi, kwamba [a]neno la wokovu liko katika Kristo.

7 Ndugu yangu ametumia maneno ya Zeno, kwamba ukombozi huja kupitia Mwana wa Mungu, na pia alitumia maneno ya Zenoki; na pia amekata rufani kwa Musa, kuthibitisha kwamba hivi vitu ni vya kweli.

8 Na sasa, tazama, [a]nitawashuhudia mimi mwenyewe kwamba vitu hivi ni vya kweli. Tazama, nawaambia, kwamba najua kwamba Kristo atakuja miongoni mwa watoto wa watu, kujitwalia makosa ya watu, na kwamba [b]atalipia dhambi za ulimwengu; kwani Bwana Mungu amesema.

9 Kwani ni ya kufaa kwamba [a]upatanisho ufanywe, kwani kulingana na [b]mpango mkuu wa Mungu wa milele lazima upatanisho ufanywe, la sivyo wanadamu wote lazima bila kuepukika waangamie; ndiyo, wote wamekuwa wagumu; ndiyo, wote [c]wameanguka na wamepotea, na lazima waangamie isipokuwa wapitie kwa upatanisho ambao unafaa ufanywe.

10 Kwani ni ya kufaa kwamba kuwe na [a]dhabihu kuu na ya mwisho; ndiyo, sio dhabihu ya mtu, wala ya mnyama, wala ya aina yoyote ya ndege; kwani haitakuwa dhabihu ya binadamu; lakini lazima iwe [b]isiyo ya mwisho na [c]dhabihu ya milele.

11 Sasa hakuna mtu yeyote ambaye anaweza kutoa dhabihu ya damu yake ambayo italipia dhambi ya mwingine. Sasa, kama mtu anaua, tazama, sheria yetu, ambayo ni ya [a]haki, itachukua maisha ya kaka yake? Nasema kwenu, Hapana.

12 Lakini sheria inahitaji maisha ya yule ambaye [a]ameua; kwa hivyo hakuwezi kuwa na chochote ambacho kimepungua kuliko upatanisho usio na mwisho ambao utatosheleza dhambi za ulimwengu.

13 Kwa hivyo, ina kufaa kwamba kuwe na dhabihu kubwa

4 *a* Alma 33:23.
6 *a* Yn. 1:1, 14.
8 *a* MWM Shuhudia.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
9 *a* Alma 33:22.
b Alma 12:22–33; Musa 6:62.
c MWM Anguko la Adamu na Hawa.
10 *a* Musa 5:6–7.
b 2 Ne. 9:7.
c MWM Dhabihu.
11 *a* Kum. 24:16; Mos. 29:25.
12 *a* MWM Adhabu Kuu; Mauaji.

na ya mwisho, na ndipo kutakuweko, au ina kufaa kwamba kuweko na [a]mwisho kwa umwagaji wa damu; ndipo [b]sheria ya Musa itimizwe; ndiyo, yote itatimizwa, kila tone na chembe, na hakuna yoyote ambaye atafutiliwa mbali.

14 Na tazama, hii ndiyo [a]maana kamili ya [b]sheria, kila chembe kikielekeza kwa ile [c]dhabihu kubwa na ya mwisho; na hivyo dhabihu kubwa na ya mwisho itakuwa Mwana wa Mungu, ndiyo, isiyo ya mwisho na milele.

15 Na hivyo ataleta [a]wokovu kwa wote ambao wataamini katika jina lake; hii ikiwa kusudi la hii dhabihu ya mwisho, kufungua tumbo la rehema, ambayo hupindua haki, na kuwafungulia wanadamu njia ya kupata imani hadi toba.

16 Na hivyo [a]rehema inaridhisha mahitaji ya [b]haki, na kuwazingira kwa mikono ya usalama, wakati yule ambaye hatumii imani hadi toba anajiweka wazi kwa sheria yote ya madai ya [c]haki; kwa hivyo ni tu yule ambaye ana imani hadi toba atatimiziwa [d]mpango mkuu wa ukombozi.

17 Kwa hivyo Mungu awajalie, ndugu zangu, kwamba muanze kutumia [a]imani yenu hadi toba, kwamba muanze [b]kulilingana jina lake takatifu, ili awe na rehema kwenu;

18 Ndiyo, mlilie kwa rehema; kwani ana uwezo wa kuokoa.

19 Ndiyo, mjinyenyekeze, na kuendelea kusali.

20 Mlilie mkiwa ndani ya mashamba yenu, ndiyo, juu ya mifugo yenu yote.

21 [a]Mlilie ndani ya nyumba zenu, ndiyo, wote wa nyumba yako, asubuhi, mchana, na jioni.

22 Ndiyo, mlilie dhidi ya uwezo wa maadui wenu.

23 Ndiyo, [a]mlilie dhidi ya [b]ibilisi, ambaye ni adui wa yote yaliyo [c]haki.

24 Mlilie juu ya mimea yenu ndani ya mashamba, kwamba muweze kufanikiwa.

25 Lieni juu ya kundi la mifugo katika mashamba yenu, kwamba iongezeke.

26 Lakini hii sio yote, lazima mfungue roho zenu ndani ya [a]vijumba vyenu, na mahali penu pa siri, na kwenye nyika zenu.

27 Ndiyo, na wakati hamammlili Bwana, hebu [a]mioyo yenu [b]ijae, mdumu katika sala kwake siku zote kwa ustawi wenu, na pia kwa ustawi wa wale ambao wako karibu nanyi.

28 Na sasa tazama, ndugu zangu wapendwa, nawaambia, msidhani kwamba haya ni yote; kwani baada ya kufanya hivi vitu vyote, ikiwa mtawafukuza

13 *a* 3 Ne. 9:17, 19–20.
b 3 Ne. 15:5.
14 *a* Alma 30:3.
b MWM Torati ya Musa.
c M&M 138:35.
15 *a* MWM Wokovu.
16 *a* MWM Rehema, enye Rehema.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
c Alma 12:32.
d MWM Mpango wa Ukombozi.
17 *a* MWM Amini, Imani.
b MWM Sala.
21 *a* Zab. 5:1–3; 3 Ne. 18:21.
23 *a* 3 Ne. 18:15, 18.
b MWM Ibilisi.
c MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
26 *a* Mt. 6:5–6.
27 *a* MWM Moyo.
b MWM Tafakari.

[a]masikini, na walio uchi, na msiwatembelee wagonjwa na walioteseka, na [b]kuwagawia mali yenu, ikiwa mnayo, wale ambao wanahitaji—Ninawaambia, ikiwa hamfanyi vitu hivi, tazama, [c]sala yenu ni ya [d]bure, kwani hayatakupatia chochote, na wewe ni kama wanafiki ambao wanakana imani.

29 Kwa hivyo kama hamuwezi kukumbuka kuwa [a]wakarimu, ninyi ni kama takataka ambayo wasafishaji hutupa nje, (ikiwa haina faida) na inakanyagwa chini na miguu ya watu.

30 Na sasa, ndugu zangu, ningetaka kwamba baada ya kupokea ushahidi mwingi hivyo, mkiona kwamba maandiko matakatifu yanashuhudia mambo haya, mje mbele na mwonyeshe [a]matunda ya toba.

31 Ndiyo, ningependa kwamba mje mbele na msishupaze mioyo yenu mara nyingine; kwani tazama, sasa ndiyo wakati na [a]siku ya wokovu wenu; na kwa hivyo ikiwa mtatubu, na msishupaze mioyo yenu, mara moja mpango mkuu wa ukombozi utatimizwa kwenu.

32 Kwani tazama, maisha haya ndiyo wakati wa watu [a]kujitayarisha kukutana na Mungu; ndiyo, tazama, wakati wa maisha haya ndiyo siku ya watu kufanya kazi yao wanayohitaji.

33 Na sasa, nilivyosema kwenu awali, kwa vile mna mashahidi wengi, kwa hivyo, nawaomba [a]msiahirishe siku yenu ya [b]toba hadi mwisho; kwani baada ya siku hii ya maisha, ambayo tumepewa ya kujitayarishia milele, tazama, kama hatuwezi kutenda mema wakati tuko katika maisha haya, kutakuja [c]usiku wa [d]giza ambapo hakutakuwa chochote kitakachofanywa.

34 Huwezi kusema, wakati utakapoletwa kwenye [a]shida ile ya kutisha, kwamba nitatubu, kwamba nitamrudia Mungu wangu. Hapana, hamuwezi kusema hivi; kwani ile roho ambayo inamiliki miili yenu mkitoka katika maisha haya, roho ile ile itakuwa na uwezo wa kushika mwili wako katika ule ulimwengu wa milele.

35 Kwani tazama, ikiwa mmeahirisha siku zenu za toba hadi kifo, tazama, mmekuwa [a]chini ya roho wa ibilisi, na amewatia [b]muhuri kuwa wake, kwa hivyo, Roho wa Bwana ameandoka kwenu, na hana mahali ndani yenu, na ibilisi ana uwezo wote juu yenu; na hii ndiyo hali ya mwisho wa waovu.

36 Na ninajua haya, kwa sababu Bwana amesema haishi kwenye mahekalu [a]yasiyo matakatifu, lakini yeye huishi

28*a* MWM Maskini.
b MWM Sadaka, Utoaji sadaka.
c Mt. 15:7–8.
d Moro. 7:6–8.
29*a* MWM Hisani.
30*a* Mt. 3:8; Alma 13:13.
31*a* Rum. 13:11–12.
32*a* 2 Ne. 2:21; Alma 12:24; 42:4–6.
33*a* Hel. 13:38; M&M 45:2.
b MWM Toba, Tubu.
c Yn. 9:4; M&M 45:17.
d MWM Giza, Kiroho; Mauti ya Kiroho.
34*a* Alma 40:13–14.
35*a* 2 Ne. 28:19–23.
b 2 Ne. 9:9.
36*a* Mos. 2:37; Alma 7:21; Hel. 4:24.

kwenye mioyo ya wale wenye [b]haki; ndiyo, na pia amesema kwamba wenye haki watakaa chini katika ufalme wake, bila kwenda nje tena; lakini nguo zao sharti zifanywe nyeupe kupitia kwa damu ya mwana-kondoo.

37 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, natamani kwamba mkumbuke mambo haya, na kwamba [a]mtumikie wokovu wenu kwa woga mbele ya Mungu, na kwamba msikane tena kuja kwa Kristo;

38 Kwamba [a]msibishane tena dhidi ya Roho Mtakatifu, lakini kwamba muipokee, na mjichukulie [b]jina la Kristo; kwamba mjinyenyekeze sana hata kwenye mavumbi, na [c]kumwabudu Mungu, mahali popote mtakapokuwa, ndani ya roho na ndani ya ukweli, na kwamba muishi katika [d]kushukuru kila siku, kwa rehema nyingi na baraka ambazo anaweka kwenu.

39 Ndiyo, na pia nawasihi, ndugu zangu, kwamba muwe [a]waangalifu ndani ya sala bila kikomo, ili msipotezwe na [b]majaribio ya ibilisi, kwamba asiwashinde ninyi, kwamba msije mkawa chini yake siku ya mwisho; kwani tazama, [c]hakupatii zawadi ya kitu kizuri.

40 Na sasa ndugu zangu wapendwa, ningewasihi muwe na [a]uvumilivu, na kwamba mvumilie aina yote ya mateso; kwamba [b]msishutumu dhidi ya wale waliowatupa nje kwa sababu ya umasikini wenu mkubwa, msije kuwa wenye dhambi kama wao.

41 Lakini kwamba muwe na uvumilivu, na mvumilie yale mateso, na tumaini thabiti kwamba siku moja mtapumzika kutoka kwa mateso yenu yote.

MLANGO WA 35

Kuhubiriwa kwa neno kunaangamiza hila za Wazoramu—Wanawafukuza waliobadilika, ambao baadaye wanaungana na watu wa Amoni katika Yershoni—Alma anahuzunika kwa sababu ya uovu wa watu. Karibia mwaka 74 K.K.

Sasa ikawa kwamba Amuleki alipomaliza kuzungumza mambo hayo, waliondoka kutoka lile kundi na wakaenda kwenye nchi ya Yershoni.

2 Ndiyo, na ndugu wengine, baada ya kuhubiri neno kwa Wazoramu, pia walikuja kwenye nchi ya Yershoni.

3 Na ikawa kwamba baada ya Wazoramu wengi waliokuwa mashuhuri kushauriana pamoja kuhusu maneno ambayo yalikuwa yamehubiriwa kwao, walikasirika juu ya neno, kwani liliharibu [a]hila yao; kwa hivyo hawangesikiliza maneno.

4 Na wakawatuma na wali-

36 *b* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
37 *a* Flp. 2:12.
38 *a* MWM Ushindani.
b Mos. 5:8; Alma 5:38.
c MWM Kuabudu.
d Zab. 69:30; M&M 59:7.
MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
39 *a* MWM Kesha, Walinzi.
b MWM Jaribu, Majaribu.
c Alma 30:60.
40 *a* MWM Subira.
b M&M 31:9.
35 3 *a* MWM Ukuhani wa uongo.

wakusanya pamoja kote nchini watu wote, na kuwashauri kuhusu maneno ambayo yalikuwa yamesemwa.

5 Sasa watawala wao na makuhani wao na walimu wao hawakuwaruhusu watu kujua kuhusu nia yao; kwa hivyo waligundua kwa siri mawazo ya watu wote.

6 Na ikawa kwamba baada ya kupata mawazo ya watu wote, wale ambao waliunga mkono yale maneno ambayo yalizungumzwa na Alma na ndugu zake walitupwa nje ya nchi; na walikuwa wengi; na walikuja pia katika nchi ya Yershoni.

7 Na ikawa kwamba Alma na ndugu zake waliwahudumia.

8 Sasa watu wa Wazoramu waliwakasirikia watu wa Amoni ambao walikuwa Yershoni, na mtawala mkuu wa Wazoramu, akiwa mtu mwovu sana, alituma mjumbe kwa watu wa Amoni akiwataka wawatupe nje ya nchi yao wale wote ambao walitoka katika nchi yao.

9 Na alitoa vitisho vingi dhidi yao. Na sasa watu wa Amoni hawakuogopa maneno yao; kwa hivyo hawakuwatupa nje, lakini waliwapokea Wazoramu wote waliokuwa masikini ambao walikuja kwao; na [a]waliwalisha, na wakawavisha, na wakawapatia ardhi kwa urithi wao; na wakawahudumia kulingana na mahitaji yao.

10 Sasa hii iliwavuruga Wazoramu kuwakasirikia watu wa Amoni, na wakaanza kuchanganyika na Walamani na wakawavuruga pia kukasirika dhidi yao.

11 Na hivyo Wazoramu na Walamani walianza kujiandaa kwa vita dhidi ya watu wa Amoni, na pia dhidi ya Wanefi.

12 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na saba wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

13 Na watu wa Amoni waliondoka kutoka nchi ya Yershoni, na wakaingia katika nchi ya Meleki, na wakawapatia majeshi ya Wanefi mahali katika nchi ya Yershoni, ili wakabiliane na majeshi ya Walamani na majeshi ya Wazoramu; na hivyo vita vikaanza kati ya Walamani na Wanefi, katika mwaka wa kumi na nane wa utawala wa waamuzi; na [a]historia itatolewa kuhusu vita vyao baadaye.

14 Na Alma, na Amoni, na ndugu zao, na pia wana wawili wa Alma walirejea katika nchi ya Zarahemla, baada ya kuwa vyombo mikononi mwa Mungu kuleta [a]wengi wa Wazoramu kutubu; na vile walipoletwa katika toba, walikimbizwa kutoka katika nchi yao; lakini wana mashamba kwa urithi wao katika nchi ya Yershoni, na wametayarisha silaha zao kwa kujikinga wenyewe, na wake zao, na watoto, na mashamba yao.

15 Sasa Alma, akiwa amehuzunishwa na uovu wa watu wake, ndiyo, kwa vita, na umwagaji wa damu, na mabishano

9*a* Mos. 4:26.
MWM Ustawi.

13*a* Alma 43:3.
14*a* Alma 35:6.

ambayo yalikuwa miongoni mwao; na akiwa ameenda kutangaza neno, au kwa maneno mengine, kutangaza neno miongoni mwa watu wote katika kila mji; na akiona kwamba mioyo ya watu ilianza kuwa migumu, na kwamba walianza [a]kuudhika kwa sababu ya uhalisi wa neno, moyo wake ulihuzunika sana.

16 Kwa hivyo, alisababisha kwamba wanawe wakusanywe pamoja, ili atoe [a]maagizo tofauti, kwa kila mmoja, kuhusu vitu vinavyohusiana na haki. Na tuna historia ya amri zake, ambazo aliwapatia kulingana na maandishi yake.

Amri za Alma kwa mwana wake Helamani.

Yenye milango ya 36 na 37.

MLANGO WA 36

Alma anashuhudia kwa Helamani uongofu wake baada ya kuona malaika—Alivumilia maumivu ya roho iliyolaaniwa; akamwomba Yesu, na ndipo akazaliwa katika Mungu—Shangwe tamu iliijaza roho yake—Aliona makundi ya malaika yakimsifu Mungu—Wengi waliobadilika wameonja na kuona vile amevyonja na kuona. Karibia mwaka 74 K.K.

[a]Mwana wangu, sikiliza maneno yangu; kwani naapa kwako, kwamba kadiri utakavyoweka amri za Mungu ndivyo utafanikiwa katika nchi.

2 Ningetaka kwamba ufanye vile nimevyofanya, kwa kukumbuka [a]utumwa wa babu zetu; kwani walikuwa katika utumwa, na hapakuwa na yeyote ambaye angewaokoa isipokuwa awe [b]Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo; na kwa kweli aliwakomboa katika mateso yao.

3 Na sasa, Ee mwana wangu Helamani, tazama, wewe ni kijana, na kwa hivyo, nakuomba wewe kwamba usikilize maneno yangu na ujifunze kutoka kwangu; kwani najua kwamba wote watakaoweka imani yao katika Mungu watasaidiwa kwa [a]majaribio yao, na taabu zao, na mateso yao, na [b]watainuliwa juu katika siku ya mwisho.

4 Na sitaki kwamba ufikiri kwamba [a]nimejua mwenyewe—sio kwa [b]kimwili lakini kwa kiroho, sio kwa mawazo ya kimwili lakini ya Mungu.

5 Sasa, tazama, nakwambia, ikiwa [a]nisingezaliwa kwa Mungu [b]nisingekuwa nimejua vitu hivi; lakini Mungu, kwa mdomo wa malaika wake mtakatifu, amethibitisha vitu hivi kwangu, sio kwa sababu ya [c]wema wangu;

15*a* MWM Ukengeufu.
16*a* MWM Msimamizi, Usimamizi.
36 1*a* Hel. 5:9–14.
2*a* Mos. 23:23; 24:17–21.
b Ku. 3:6; Alma 29:11.
3*a* Rum. 8:28.
b Mos. 23:21–22.
4*a* 1 Kor. 2:11; Alma 5:45–46. MWM Maarifa.
b MWM Tamaa za kimwili.
5*a* MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
b Alma 26:21–22.
c MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki.

6 Kwani nilienda na wana wa Mosia, nikinuia [a]kuharibu kanisa la Mungu; lakini tazama, Mungu alimtuma malaika wake mtakatifu kutuzuia tulipokuwa njiani.

7 Na tazama, alituzungumzia, kwa sauti kama ya radi, na ardhi yote [a]ilitetemeka chini ya miguu yetu; na sisi sote tuliinama kwenye ardhi, kwani [b]hofu ya Bwana ilitujia.

8 Lakini tazama, sauti iliniambia: Amka. Na niliamka na kusimama wima, na nikaona malaika.

9 Na akaniambia: Ikiwa hutaki kuangamizwa mwenyewe, usijaribu tena kuangamiza kanisa la Mungu.

10 Na ikawa kwamba niliinama kwenye ardhi; na ilikuwa kwa muda wa siku [a]tatu usiku na mchana kwamba nisingefungua kinywa changu, wala kutumia viungo vyangu.

11 Na malaika alinizungumzia vitu vingi zaidi, ambavyo vilisikika na ndugu zangu, lakini mimi sikuvisikia; kwani wakati niliposikia maneno—Ikiwa hutaki kujiangamiza mwenyewe, usijaribu tena kuliangamiza kanisa la Mungu—Nilipigwa na woga mwingi sana na mshangao kwa hofu kwamba ningeangamizwa, kwamba niliinama kwenye ardhi na sikusikia tena.

12 Lakini nilisumbuliwa na adhabu ya [a]milele, kwani roho yangu iliteseka kwa kiasi kikubwa sana na kuadhibiwa kwa dhambi zangu zote.

13 Ndiyo, nilikumbuka dhambi zangu zote na uovu, kwa ajili hiyo [a]niliadhibiwa na uchungu wa jehanamu; ndiyo, niliona kwamba nimeasi dhidi ya Mungu wangu, na kwamba sikuwa nimetii amri zake.

14 Ndiyo, na nilikuwa nimeua watoto wake wengi, au kwa usahihi zaidi niliwaelekeza kwenye maangamizo; ndiyo, na kwa ufupi uovu wangu ulikuwa mwingi sana kwamba ile fikira ya kukaribia uwepo wa Mungu wangu iliiadhibu nafsi yangu kwa hofu kuu isiyoelezeka.

15 Ee, nilifikiri, kwamba [a]ningefukuzwa na kutokuwepo kwa nafsi wala mwili, kwamba nisingeletwa kusimama kwenye uwepo wa Mungu wangu, kuhukumiwa kwa [b]vitendo vyangu.

16 Na sasa, kwa siku tatu usiku na mchana niliteseka, hata na uchungu wa [a]nafsi iliyolaaniwa.

17 Na ikawa kwamba wakati nilipoteseka na maumivu mabaya, wakati [a]nilihuzunishwa na ufahamu wa dhambi zangu nyingi, tazama, nilikumbuka pia kusikia baba yangu akitoa unabii kwa watu kuhusu kuja kwa mmoja aitwaye Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kulipia dhambi za ulimwengu.

18 Sasa, nilipofikiria wazo hili,

6*a* Mos. 27:10.
7*a* Mos. 27:18.
b MWM Hofu—Hofu juu ya Mungu.
10*a* Mos. 27:19–23.
12*a* M&M 19:11–15.
13*a* MWM Hatia.
15*a* Ufu. 6:15–17; Alma 12:14.
b Alma 41:3; M&M 1:9–10.
16*a* MWM Hukumu.
17*a* 2 Kor. 7:10.

nililia ndani ya moyo wangu: Ee Yesu, wewe Mwana wa Mungu, nihurumie, mimi ambaye [a]nina uchungu, na nimezungukwa na [b]minyororo ya kifo kisicho na mwisho.

19 Na sasa, tazama, nilipofikiri hivi, sikukumbuka uchungu wangu tena; ndiyo, [a]sikuteseka na ufahamu wa dhambi zangu tena.

20 Na Ee, ni [a]shangwe gani, na ni mwangaza gani wa ajabu niliouona; ndiyo, nafsi yangu ilijazwa na shangwe ya ajabu kama vile ulivyokuwa uchungu wangu!

21 Ndiyo, nakwambia, mwana wangu, kwamba hakungekuwa na chochote kilichokuwa kikali vile na kichungu vile ulivyokuwa uchungu wangu. Ndiyo, na tena ninakwambia, mwana wangu, kwamba upande mwingine, hapawezi kuwa na kitu kizuri hivyo na kitamu kama vile ilivyokuwa shangwe yangu.

22 Ndiyo, nilidhani niliona, hata vile babu yetu [a]Lehi alivyomwona, Mungu akiketi kwenye kiti chake cha enzi, akizungukwa na umati usiohesabika wa malaika, kwa hali ya kuimbia na kumsifu Mungu wao; ndiyo, na nafsi yangu ilitamani kuwa hapo.

23 Lakini tazama, viungo vyangu vilipata [a]nguvu tena, na nilisimama kwa miguu yangu, na nikajidhihirisha kwa watu kwamba [b]nimezaliwa kwa Mungu.

24 Ndiyo, na tangu wakati huo hata hadi sasa, nimefanya kazi bila kukoma, kwamba nilete nafsi za watu kutubu; kwamba ningewaleta wapate [a]kuonja shangwe kuu ambayo niliiona; ili nao pia wazaliwe ndani ya Mungu, na [b]wajazwe na Roho Mtakatifu.

25 Ndiyo, na sasa tazama, Ee mwana wangu, Bwana hunipa shangwe kuu kwa matokeo ya kazi yangu;

26 Kwani kwa sababu ya [a]neno ambalo amenipatia, tazama, wengi wamezaliwa kwa Mungu, na wameonja vile nilivyoonja, na wameona macho kwa macho kama vile nilivyoona; kwa hivyo wanajua kuhusu vitu hivi ambavyo nimezungumzia, vile ninavyojua; na elimu ambayo ninayo ni ya Mungu.

27 Na nimesaidiwa wakati wa majaribio na taabu za kila aina, ndiyo, na kwa kila aina ya mateso; ndiyo, Mungu amenikomboa kutoka gerezani, na kutoka kufungwa, na kutoka kifo; ndiyo, na ninaweka tumaini langu ndani yake, na [a]atanikomboa.

28 Na ninajua kwamba [a]ataniinua katika siku ya mwisho, kuishi na yeye kwenye [b]utukufu; ndiyo, na nitamsifu milele, kwani [c]amewaleta babu zetu kutoka ya Misri, na amewameza

18*a* MY majuto makuu.
b 2 Ne. 9:45; 28:22; Alma 12:11; Musa 7:26.
19*a* MWM Hatia.
20*a* MWM Shangwe.
22*a* 1 Ne. 1:8.
23*a* Musa 1:10.
b Alma 5:14. MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
24*a* 1 Ne. 8:12; Mos. 4:11.
b 2 Ne. 32:5; 3 Ne. 9:20. MWM Roho Mtakatifu.
26*a* Alma 31:5.
27*a* Zab. 34:17.
28*a* 3 Ne. 15:1.
b MWM Utukufu.
c Ku. 12:51.

[d]Wamisri ndani ya Bahari ya Shamu; na aliwaongoza na uwezo wake hadi kwenye nchi ya ahadi; ndiyo, na amewakomboa kutoka kifungoni na utumwa mara kwa mara.

29 Ndiyo, na amewaleta babu zetu kutoka nchi ya Yerusalemu; na pia kwa uwezo wake usio na mwisho, [a]amewakomboa kutoka kifungoni na utumwa wao, mara kwa mara hadi wakati huu; na daima nimehifadhi ukumbusho wa utumwa wao; ndiyo, na ninyi pia inawapasa kuhifadhi ukumbusho wa utumwa wao, kama vile nilivyofanya.

30 Lakini tazama, mwana wangu, hii si yote; kwani unapaswa kujua kama vile ninavyojua kwamba [a]kadiri utakavyoshika amri za Mungu utafanikiwa nchini; na unapaswa kujua pia kwamba, kadiri utakavyoacha kutii amri za Mungu utatolewa kwenye uwepo wake. Sasa hii ni kulingana na neno lake.

MLANGO WA 37

Mabamba ya shaba nyeupe na maandiko mengine yamehifadhiwa ili kuongoza nafsi kwenye wokovu—Wayaredi waliangamizwa kwa sababu ya uovu wao—Viapo vyao vya siri na maagano lazima yaondolewe mbali kutoka kwa watu—Shauriana na Bwana kwa matendo yako yote—Kama Liahona ilivyowaongoza Wanefi, kadhalika neno la Kristo huwaongoza watu kwenye uzima wa milele. Karibia mwaka 74 K.K.

Na sasa, mwana wangu Helamani, ninakuamuru kwamba uchukue [a]maandishi ambayo [b]nilikabidhiwa;

2 Na pia ninakuamuru kwamba uandike maandishi ya hawa watu, kulingana na vile nilivyofanya, kwenye mabamba ya Nefi, na uhifadhi vitu hivi vyote vitakatifu ambavyo nimehifadhi, hata kama vile nilivyovihifadhi; kwani ni kwa sababu ya [a]busara kwamba zimewekwa.

3 Na [a]mabamba haya ya shaba nyeupe, ambayo yana michoro, ambayo yana kumbukumbu ya maandiko matakatifu juu yake, ambayo yana nasaba ya babu zetu, hata kutoka mwanzoni—

4 Tazama, unabii umetolewa na babu zetu, kwamba zihifadhiwe na kutolewa kutoka kwa kizazi kimoja hadi kingine, na ziwekwe na kulindwa na mkono wa Bwana mpaka ziwafikie kila taifa, kabila, lugha, na watu, kwamba wafahamu [a]siri zilizomo.

5 Na sasa tazama, ikiwa zitahifadhiwa lazima ziweke mng'aro wao; ndiyo, na zihifadhi mng'aro wao; ndiyo, na pia mabamba yote ambayo yana maandiko matakatifu.

6 Sasa labda unadhani kwa-

28 *d* Ku. 14:26–27.
29 *a* Mos. 24:17; 27:16; Alma 5:5–6.
30 *a* 2 Ne. 1:9–11; Alma 50:19–22.

37 1 *a* Alma 45:2–8.
b Mos. 28:20.
2 *a* Eno. 1:13–18; M. ya Morm. 1:6–11; Alma 37:9–12.

3 *a* 1 Ne. 5:10–19. MWM Mabamba ya Shaba Nyeupe.
4 *a* MWM Siri za Mungu.

mba huu ni [a]upuuzi ndani yangu; lakini tazama nakwambia, kwamba kupitia kwa vitu vilivyo [b]vidogo na rahisi vitu vikubwa hutendeka; na njia ndogo mara nyingi hufadhaisha wenye hekima.

7 Na Bwana Mungu hutumia [a]njia zake ili kutimiza kusudi lake kuu na la milele; na kwa njia [b]ndogo sana Bwana hufawadhaisha wale werevu na kutimiza wokovu wa roho nyingi.

8 Na sasa, mpaka sasa imekuwa hekima ndani ya Mungu kwamba vitu hivi vihifadhiwe; kwani tazama, [a]vimeongeza ufahamu wa watu hawa, ndiyo, na kuwasadikisha wengi kuhusu makosa ya njia zao, na kuwaleta kwenye ufahamu wa Mungu wao hadi kwa wokovu wa nafsi zao.

9 Ndiyo, nakwambia wewe, [a]isingekuwa vitu hivi ambavyo maandishi haya yanayo, ambavyo viko kwenye mabamba haya, Amoni na ndugu zake [b]hawangesadikisha maelfu wengi hivyo wa Walamani kuhusu desturi zisizo sawa za baba zao; ndiyo, haya mandishi na [c]maneno yao yaliwaleta kwenye toba; yaani, yaliwaleta kwenye ufahamu wa Bwana Mungu wao, na kufurahi katika Yesu Kristo Mkombozi wao.

10 Na nani anajua lakini kwamba watakuwa njia ya kuwaleta maelfu wengi wao, ndiyo, na pia maelfu wengi wa ndugu zetu wenye shingo ngumu, Wanefi, ambao sasa wanashupaza mioyo yao kwenye dhambi na uovu, kwa ufahamu wa Mkombozi wao?

11 Sasa siri hizi hazijafahamishwa kwangu kabisa; kwa hivyo sitaongea tena.

12 Na ingetosha kwangu kusema zimehifadhiwa kwa kusudi la busara, kusudi ambalo linajulikana na Mungu; kwani yeye [a]hushauri kwa hekima juu ya kazi yake yote, na njia zake ni nyoofu, na mwenendo wake ni ule [b]usiobadilika.

13 Ee kumbuka, kumbuka, mwana wangu Helamani, jinsi amri za Mungu zilivyo [a]kali. Na alisema: [b]Ikiwa utatii amri zangu [c]utafanikiwa nchini—lakini kama huwezi kutii amri zake utatolewa kutoka uwepo wake.

14 Na sasa kumbuka, mwana wangu, kwamba Mungu [a]amekukabidhii vitu hivi, ambavyo ni vi[b]takatifu, ambavyo amevifanya vitakatifu, na pia ambavyo ataviweka na kuvihifadhi kwa nia ya [c]busara ambayo anajua, ili aweze kuonyesha uwezo wake kwa vizazi vijavyo.

15 Na sasa tazama, nakwambia kwa roho ya unabii, kwamba ikiwa utavunja amri za Mungu,

6 *a* 1 Kor. 2:14.
b 1 Ne. 16:28–29; M&M 64:33; 123:15–17.
7 *a* Isa. 55:8–9.
b 2 Fal. 5:1–14.
8 *a* 2 Tim. 3:15–17; Mos. 1:3–5.
9 *a* Mos. 1:5.
b Alma 18:36; 22:12.
c MWM Injili.
12 *a* 2 Ne. 9:28; Yak. (KM) 4:10.
b 1 Ne. 10:19; Alma 7:20.
13 *a* 2 Ne. 9:41.
b Alma 9:13; 3 Ne. 5:22.
c Mos. 1:7; Alma 50:20.
14 *a* M&M 3:5.
b MWM Takatifu.
c 1 Ne. 9:3–6.

tazama, vitu hivi ambavyo ni wakfu vitaondoshwa kutoka kwako kwa uwezo wa Mungu, na utatolewa kwa Shetani, kwamba aweze kukuchunga kama kapi mbele ya upepo.

16 Lakini kama utatii amri za Mungu, na ufanye vitu hivi ambavyo ni vitakatifu kulingana na yale ambayo Bwana amekuamuru ufanye, (kwani lazima uombe msaada wa Bwana kwa vitu vyote ambavyo unataka kuvitumia) tazama, hakuna nguvu za ardhini au jehanamu, zinazoweza [a]kuvichukua kutoka kwako, kwani Mungu ni mwenye uwezo kwa kutimiza maneno yake yote.

17 Kwani atatimza ahadi zake zote ambazo atakuahidi, kwani ametimiza ahadi zake ambazo amewaahidi babu zetu.

18 Kwani aliwaahidi kwamba [a]atahifadhi vitu hivi kwa kusudi la busara kwake, kwamba angeweza kuonyesha nguvu yake kwa vizazi vijavyo.

19 Na sasa tazama, kusudi moja ametimiza, hata kwa kurudisha maelfu [a]wengi wa Walamani kwenye ufahamu wa ukweli; na ameonyesha tena uwezo wake kwao, na pia ataonyesha uwezo wake tena ndani yao kwa vizazi [b]vijavyo; kwa hivyo vitahifadhiwa.

20 Kwa hivyo ninakuamuru, mwana wangu Helamani, kwamba uwe na bidii kwa kutimiza maneno yangu yote, na kwamba uwe na bidii kwa kutii amri za Mungu kama zilivyoandikwa.

21 Na sasa, nitaongea na wewe kuhusu yale mabamba [a]ishirini na nne, kwamba uyahifadhi, ili siri na vitendo viovu, na kazi zao za [b]siri, au kazi za siri za wale watu ambao wemeangamizwa, zingeonyeshwa kwa watu hawa; ndiyo, mauaji yao yote, na wizi, na utekaji nyara wao, na maovu na machukizo yao yote, yangejulikana kwa hawa watu; ndiyo, na kwamba uzihifadhi [c]vitafsiri hivi.

22 Kwani tazama, Bwana aliona kwamba watu wake walianza kufanya kazi gizani, ndiyo, walifanya mauaji ya siri na machukizo; kwa hivyo Bwana alisema, ikiwa hawangetubu wangeamizwa kutoka usoni mwa dunia.

23 Na Bwana akasema: Nitamtayarisha mtumishi wangu Gazelemu, [a]jiwe, ambalo litamulika mwangaza gizani, kwamba niwafahamishe watu wangu ambao wananihudumia, kwamba ningewafahamisha kazi za ndugu zao, ndiyo, kazi zao za siri, kazi zao za gizani, na uovu wao na machukizo yao.

24 Na sasa mwana wangu, hivi vitafsiri zilitayarishwa kwamba neno la Mungu lingetimizwa, ambalo alizungumza, akisema:

25 [a]Nitatoa nje kutoka gizani hadi kwenye mwanga kazi zao za siri na machukizo yao; na

16*a* JS—H 1:59.
18*a* M&M 5:9.
19*a* Alma 23:5.
b Eno. 1:13; Morm. 7:8–10.
21*a* Eth. 1:1–5.
b MWM Makundi maovu ya siri.
c MWM Urimu na Thumimu.
23*a* Mos. 8:13.
25*a* M&M 88:108–110.

wasipotubu [b]nitawaangamiza kutoka uso wa dunia; na nitaleta kwa mwangaza siri zao zote na machukizo yao, kwa kila taifa ambalo kutoka sasa kuendelea litamiliki nchi.

26 Na sasa, mwana wangu, tunajua kwamba hawakutubu; kwa hivyo wameangamizwa, na hivyo neno la Mungu limetimizwa; ndiyo, siri zao za machukizo zimetolewa gizani na kujulikana kwetu.

27 Na sasa, mwana wangu, ninakuamuru uweke viapo vyao, na maagano yao, na mapatano yao ya siri zao za machukizo; ndiyo, na [a]ishara zao zote na miujiza ya hila utaficha kutoka kwa hawa watu, ili wasiyajue, isiwe ikawa waanguke gizani pia na waangamizwe.

28 Kwani tazama, kuna [a]laana juu ya nchi hii yote, kwamba maangamizo yatafika juu ya wale wote wanaofanya kazi gizani, kulingana na uwezo wa Mungu, wakati watakuwa wameiva; kwa hivyo natamani kwamba hawa watu wasiangamizwe.

29 Kwa hivyo utaweka hii mipango yao ya siri za [a]viapo na maagano yao kutoka kwa hawa watu, na tu maovu yao na mauaji yao na machukizo yao yatajulishwa kwao; na utawafundisha [b]kuchukia maovu na machukizo na mauaji kama hayo, na utawafundisha pia kwamba hawa watu waliangamizwa kwa sababu ya uovu wao na machukizo na mauaji yao.

30 Kwani tazama, waliwaua manabii wote wa Bwana ambao walikuja miongoni mwao kutangaza kwao kuhusu uovu; na damu ya wale ambao waliwaua ililia kutoka ardhini kwa Bwana Mungu wao kulipiza kisasi kwa wale ambao waliwaua; na hivi hukumu ya Mungu iliwajia hawa wafanyikazi wa giza na makundi maovu ya siri.

31 Ndiyo, na nchi ilaaniwe milele na milele kwa wale wafanyikazi wa gizani na makundi ya siri, hata kwenye maangamizo, isipokuwa watubu kabla ya kuwa waovu kabisa.

32 Na sasa, mwana wangu, kumbuka maneno ambayo nimekuzungumzia; usiamini ile mipango ya siri kwa watu hawa, lakini uwafundishe [a]chuki isiyo na mwisho dhidi ya dhambi na uovu.

33 [a]Wahubirie toba, na imani kwa Bwana Yesu Kristo; wafundishe kujinyenyekeza na kuwa [b]wapole, na wanyenyekevu moyoni; wafundishe kushindana na kila [c]jaribio la ibilisi, na imani yao kwa Bwana Yesu Kristo.

34 Wafundishe wasichoke na kazi nzuri daima, lakini kuwa wapole na wanyenyekevu moyoni; kwani kama hawa watapata [a]mapumziko kwa nafsi zao.

35 Ee, kumbuka, mwana

25 *b* Mos. 21:26.
27 *a* Hel. 6:22.
28 *a* Alma 45:16; Eth. 2:7–12.
29 *a* Hel. 6:25.
b Alma 13:12.
32 *a* 2 Ne. 4:31.
33 *a* MWM Hubiri.
b MWM Pole, Upole.
c MWM Jaribu, Majaribu.
34 *a* Zab. 37:4–7; Mt. 11:28–30.

wangu, na ujifunze [a]hekima katika ujana wako; ndiyo, jifunze katika ujana wako kutii amri za Mungu.

36 Ndiyo, na [a]mlilie Mungu kwa usaidizi wako wote; ndiyo, acha vitendo vyako vyote viwe kwa Bwana, na popote uendapo acha iwe kwa Bwana; ndiyo, acha fikira zako zote zielekezwe kwa Bwana; ndiyo, acha mapenzi ya moyo wako yaelekezwe kwa Bwana milele.

37 [a]Shauriana na Bwana kwenye matendo yako yote, na atakuongoza kwa yale mema; ndiyo, unapolala usiku lala katika Bwana, ili akulinde usingizini mwako; na ukiamka asubuhi hebu moyo wako ujazwe na [b]shukrani kwa Mungu; na ukifanya vitu hivi, utainuliwa katika siku ya mwisho.

38 Na sasa, mwana wangu, nina machache ya kuzungumza kuhusu kitu ambacho babu zetu wanaita mpira, au mwelekezi—au baba zetu waliita [a]Liahona, ambayo, inaamanisha dira; na Bwana aliitayarisha.

39 Na tazama, hakungekuwa na mtu ambaye angetengeneza kitu cha mtindo aina hii. Na tazama, ilitayarishwa kuwaonyesha babu zetu njia ambayo wangesafiria katika nyika.

40 Na iliwatumikia kulingana na imani yao kwa Mungu; kwa hivyo, kama walikuwa na [a]imani kuamini kwamba Mungu angesababisha hivyo vijiti vingeonyesha njia ambayo wangefuata, tazama, ilifanyika; kwa hivyo walikuwa na muujiza huu, na pia miujiza mingine mingi iliyofanyika kwa uwezo wa Mungu, siku hadi siku.

41 Walakini, kwa sababu hiyo miujiza ilitendeka kupitia kwa njia [a]rahisi iliwaonyesha kazi ya kushangaza. Walikuwa wavivu na walisahau kutumia imani yao na bidii na baadaye zile kazi za ajabu zilikoma, na hawakuendelea kwenye safari yao;

42 Kwa hivyo, walikaa nyikani, au hawakusafiri kwa njia nyoofu, na waliteswa na njaa na kiu, kwa sababu ya makosa yao.

43 Na sasa, mwana wangu, ningependa uelewe kwamba vitu hivi haviko bila mfano wa maana; kwani kwa jinsi babu zetu walivyokuwa wavivu kufuata hii dira (sasa vitu hivi vilikuwa vya muda) hawakufanikiwa; hata hivyo ndivyo ilivyo na vitu ambavyo ni vya kiroho.

44 Kwani tazama, ni rahisi kama kutii [a]neno la Kristo, ambalo litakuonyesha njia nyoofu kwa raha ya milele, kama vile ilivyokuwa kwa babu zetu kutii hii dira, ambayo ingewaonyesha njia nyoofu kuelekea nchi ya ahadi.

45 Na sasa nasema, hakuna mfano wa kitu hiki? Kwani kwa hakika vile mwongozo huu ulivyowaleta babu zetu kwa kufuata njia yake, kuelekea nchi ya

35*a* MWM Hekima.
36*a* MWM Sala.
37*a* Yak. (KM) 4:10; M&M 3:4.
b M&M 46:32.
38*a* 1 Ne. 16:10; 18:12; M&M 17:1.
40*a* 1 Ne. 16:28.
41*a* Alma 37:6–7.
44*a* Zab. 119:105; 1 Ne. 11:25; Hel. 3:29–30.

ahadi, hivyo maneno ya Kristo, ikiwa tutafuata mwelekeo wake, yatatuvukisha hili bonde la huzuni hadi mbali kwenye nchi bora ya ahadi.

46 Ee mwana wangu, usiache tuwe [a]wavivu kwa sababu ya urahisi wa [b]njia; kwani hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa babu zetu; kwani hivyo ndivyo ilivyotayarishwa kwao, kwamba ikiwa wangeangalia kwake [c]wangeishi; hata hivyo ndivyo ilivyo kwetu sisi. Njia imetayarishwa, na ikiwa tutaangalia tutaishi milele.

47 Na sasa, mwana wangu, uwe na hakika kwamba unalinda vitu hivi vitakatifu, ndiyo, ona kwamba umeelekeza jicho kwa Mungu na uishi. Waendee hawa watu na kutangaza neno, na uwe na busara. Mwana wangu, kwaheri.

Amri za Alma kwa mwana wake Shibloni.

Yenye mlango wa 38.

MLANGO WA 38

Shibloni aliteswa kwa ajili ya haki—Wokovu uko ndani ya Kristo, ambaye ni uzima na mwangaza wa ulimwengu—Jifunze kuzuia tamaa zenu. Karibia mwaka 74 K.K.

Mwana wangu, sikiliza maneno yangu, kwani ninakwambia, vile nilimwambia Helamani, kwamba ikiwa utatii amri za Mungu utafanikiwa katika nchi; na kadiri hutatii amri za Mungu utaondolewa kwenye uwepo wake.

2 Na sasa, mwana wangu, ninaamini kwamba nitakuwa na shangwe kuu juu yako, kwa sababu ya uthabiti wako na imani yako kwa Mungu; kwani kwa njia hiyo umeanza katika ujana wako kumtegemea Bwana Mungu wako, hata hivyo natarajia kwamba [a]utaendelea kutii amri zake; kwani heri yule [b]atakayevumilia hadi mwisho.

3 Nakwambia wewe, mwana wangu, kwamba tayari nimekuwa na shangwe kwako, kwa sababu ya uaminifu wako na bidii yako na subira yako na uvumilivu wako miongoni mwa watu wa [a]Wazoramu.

4 Kwani ninajua kwamba ulikuwa umefungwa; ndiyo, na pia najua kwamba ulipigwa kwa mawe kwa ajili ya kuhubiri neno; na [a]ulivumilia hivi vitu vyote kwa sababu Bwana [b]alikuwa nawe; na sasa unajua kwamba Bwana alikuokoa.

5 Na sasa mwana wangu, Shibloni, ningetaka wewe ukumbuke, kwamba kadiri utakavyoweka [a]imani yako ndani ya Mungu hata hivyo zaidi [b]utakombolewa kutoka kwenye majaribio yako, na [c]taabu zako, na

46*a* 1 Ne. 17:40–41.
b Yn. 14:5–6; 2 Ne. 9:41; 31:17–21; M&M 132:22, 25.
c Yn. 11:25; Hel. 8:15; 3 Ne. 15:9.

38 2*a* Alma 63:1–2.
b 2 Ne. 31:15–20; 3 Ne. 15:9; 27:6, 16–17.

3*a* Alma 31:7.

4*a* MWM Subira.
b Rum. 8:35–39.

5*a* Alma 36:27.
MWM Tegemea.
b Mt. 11:28–30.
c M&M 3:8; 121:7–8.

mateso yako, na utainuliwa juu siku yako ya mwisho.

6 Sasa, mwana wangu singetaka kwamba ufikirie kwamba ninajua vitu hivi kwa uwezo wangu, lakini ni Roho wa Bwana aliyo ndani yangu ndiyo anayefanya vijulikane kwangu; kwani kama [a]nisingezaliwa kwa Mungu nisingejua vitu hivi.

7 Lakini tazama, Bwana kwa rehema yake kuu alimtuma [a]malaika wake kutangaza kwangu kwamba nikome kazi ya [b]kuangamiza miongoni mwa watu wake; ndiyo, na nimemwona malaika uso kwa uso, na akazungumza na mimi, na sauti yake ilikuwa kama radi, na ikatetemesha ardhi yote.

8 Na ikawa kwamba nilikuwa kwa siku tatu usiku na mchana ndani ya uchungu mkali na maumivu ya roho; na haikuwa mpaka nilipomlilia Bwana Yesu Kristo kwa huruma, ndipo nikapata [a]kusamehewa dhambi zangu. Lakini tazama, nilimlilia na nikapata amani ndani ya roho yangu.

9 Na sasa, mwana wangu, nimekwambia hii ili ujifunze hekima, kwamba ungejifunza kutoka kwangu kwamba [a]hakuna njia nyingine au kwa vyote ambayo binadamu anaweza kuokolewa, ila tu kwa na kupitia kwa Kristo. Tazama, yeye ni uzima na [b]mwangaza wa ulimwengu. Tazama, yeye ni neno la ukweli na haki.

10 Na sasa, vile umeanza kufundisha neno hata hivyo ningetaka kwamba uendelee kufundisha; na ningetaka kwamba uwe na bidii na kiasi kwa vitu vyote.

11 Hakikisha kwamba hujiinui kwa kiburi; ndiyo, angalia kwamba [a]hujisifu kwa hekima yako mwenyewe, wala kwa nguvu zako nyingi.

12 Tumia ujasiri, lakini usiwe mjeuri; na pia uone kwamba ujifunze kuzuia tamaa zako zote, ili uweze kujazwa na mapenzi; hakikisha kwamba uepuke kutokana na uvivu—

13 Usiombe kama vile Wazoramu wanavyofanya, kwani umeona kwamba wanaomba kuonekana na watu, na kusifiwa kwa hekima yao.

14 Usiseme: Ee Mungu, ninakushukuru kwamba tu [a]wema kuliko ndugu zetu; lakini afadhali useme: Ee Bwana, unisamehe kwa [b]kutokuwa na haki kwangu, na ukumbuke ndugu zangu kwa huruma—ndiyo, kubali kutokuwa na haki kwako mbele ya Mungu wakati wote.

15 Na Bwana aibariki roho yako, na akupokee katika siku ya mwisho ndani ya ufalme wake, kukaa chini kwa amani. Sasa nenda, mwana wangu, na ukafundishe neno kwa watu

6*a* Alma 36:26; M&M 5:16. MWM Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena.
7*a* Mos. 27:11–17.
b Alma 26:17–18; 36:6–11.
8*a* MWM Ondoleo la Dhambi.
9*a* Hel. 5:9.
b Mos. 16:9.
11*a* MWM Kiburi.
14*a* Alma 31:16.
b Lk. 18:10–14.

hawa. Uwe na busara. Mwana wangu, kwaheri.

Amri za Alma kwa mwana wake Koriantoni.

Yenye milango ya 39 hadi 42.

MLANGO WA 39

Dhambi ya ngono ni machukizo—Dhambi za Koriantoni ziliwazuia Wazoramu kupokea neno—Ukombozi wa Kristo utaponya waumini ambao waliutangulia. Karibia mwaka 74 K.K.

Na sasa, mwana wangu, nina vitu vingi zaidi kukuzungumzia kuliko yale niliyomzungumzia kaka yako; kwani tazama, hujachunguza unyofu wa kaka yako, uaminifu wake, na bidii yake kwa kutii amri za Mungu? Tazama, si yeye amekuonesha mfano mzuri?

2 Kwani hukutii maneno yangu kama vile kaka yako alivyofanya, miongoni mwa watu wa [a]Wazoramu. Sasa hii ndiyo ninayo dhidi yako; uliendelea kujivuna kwa sababu ya nguvu yako na hekima yako.

3 Na hii siyo yote, mwana wangu. Ulifanya yale ambayo yalikuwa ya kusikitisha kwangu; kwani uliacha huduma, na ukaenda kwenye nchi ya Sironi ndani ya mipaka na nchi ya Walamani, kumtafuta [a]kahaba Isabeli.

4 Ndiyo, [a]aliiba mioyo ya wengi; lakini hii sio kisingizio kwako, mwana wangu. Ungeendelea kuhudumu pale ambapo uliaminiwa.

5 Hujui, mwana wangu, kwamba [a]vitu hivi ni machukizo machoni mwa Bwana; ndiyo, ni machukizo kuliko dhambi zote isipokuwa ile ya kumwaga damu ya wale wasio na hatia au kumkana Roho Mtakatifu?

6 Kwani tazama, ikiwa [a]utamkana Roho Mtakatifu wakati amekuwa ndani yako, na unajua kwamba unamkataa, tazama, hii ni dhambi ambayo [b]haiwezi kusamehewa; ndiyo, na yeyote auaye dhidi ya mwangaza na taarifa ya Mungu, si rahisi kwake kupata [c]msamaha; ndiyo, nasema kwako, mwana wangu, kwamba si rahisi kwake kupata msamaha.

7 Na sasa, mwana wangu, ningemsihi Mungu kwamba hungekuwa na [a]hatia ya kosa kubwa hivyo. Singetaka kuendelea kukuzungumzia makosa yako, na kuumiza roho yako, kama haingekuwa kwa faida yako.

8 Lakini tazama, huwezi kuficha makosa yako kwa Mungu; na isipokuwa utubu zitakuwa ushahidi dhidi yako katika siku ya mwisho.

9 Sasa mwana wangu, ningetaka kwamba utubu na kusahau dhambi zako, na usiende tena kupendeza [a]tamaa ya

39 2*a* Alma 38:3.
3*a* MWM Kupenda anasa, Matamanio ya anasa.
4*a* Mit. 7:6–27.
5*a* MWM Utovu wa maadili ya kujamiiana.
6*a* M&M 76:35–36.
b MWM Dhambi isiyo sameheka.
c M&M 64:10.
7*a* MWM Hatia.
9*a* MWM Tamaa za kimwili.
MWM Samehe.

macho yako, lakini [b]ujikataze mwenyewe kwa vitu hivi vyote; kwani usipofanya hivi huwezi kwa vyovyote kurithi ufalme wa Mungu. Ee, kumbuka, na ujichukulie juu yako, na ujikatishe mwenyewe katika vitu hivi.

10 Na nina kuamuru ujichukulie kushauriana na kaka zako wakubwa katika shughuli zako; kwani tazama, wewe ungali ndani ya ujana wako, na unahitaji kulishwa na kaka zako. Na kusikiliza ushauri wao.

11 Usiamini kudanganywa na kitu kilicho bure na cha kipumbavu; usikubali ibilisi apoteze moyo wako kufuata hao makahaba waovu. Tazama, Ee mwana wangu, ni jinsi gani uovu mkuu uliwaletea [a]Wazoramu; kwani wakati walipoona [b]mwenendo wako hawakuamini maneno yangu.

12 Na sasa Roho wa Bwana huniambia mimi: [a]Amuru watoto wako watende mema, la sivyo wataongoza mioyo ya wengi kwenye maangamizo; kwa hivyo nakuamuru, wewe mwana wangu, kwa heshima ya Mungu, kwamba ujiepushe kutoka uovu wako;

13 Kwamba umtazamie Bwana na akili, nguvu, na uwezo wako wote; kwamba usipoteze mioyo ya watu mara nyingine kwa uovu; lakini urudi kwao, na [a]kukiri makosa yako na ule ubaya ambao umetenda.

14 [a]Usitafute utajiri wala vitu visivyo vya maana vya ulimwengu huu; kwani tazama, hutavibeba wakati wa kifo.

15 Na sasa, mwana wangu, ningesema machache kwako kuhusu kuja kwa Kristo. Tazama, nakwambia, kwamba ni yeye kwa kweli atakayekuja kuondoa dhambi za ulimwengu; ndiyo, anakuja kutangaza habari njema ya wokovu kwa watu wake.

16 Na sasa, mwana wangu, hii ndiyo huduma ambayo ulitiwa, kutangaza hizi habari njema kwa watu hawa, kutayarisha akili zao; kwa usahihi zaidi afadhali kwamba wokovu uwajie, kwamba watayarishe akili za [a]watoto wao kusikiliza neno wakati wa kuja kwake.

17 Na sasa nitatuliza kidogo akili yako kwa jambo hili. Tazama, unashangaa kwa nini hivi vitu vijulikane mbele. Tazama, nakwambia, si roho wakati huu ina thamani kwa Mungu vile roho itakuwa wakati wa kuja kwake?

18 Si ni lazima mpango wa ukombozi ufunuliwe kwa watu hawa na kwa watoto wao pia?

19 Je, si ni rahisi wakati huu kwa Bwana kutuma malaika wake kututangazia habari hii njema kama vile kwa watoto wetu, au kama vile baada ya kuja kwake?

9 *b* 3 Ne. 12:30.
11 *a* Alma 35:2–14.
b Rum. 2:21–23; 14:13; Alma 4:11.
12 *a* MWM Amri za Mungu; Fundisha, Mwalimu.
13 *a* Mos. 27:34–35.
14 *a* Mt. 6:25–34; Yak. (KM) 2:18–19; M&M 6:6–7; 68:31–32.
16 *a* MWM Familia—Wajibu wa wazazi.

MLANGO WA 40

Kristo anasababisha kuwepo ufufuo wa binadamu wote—Wenye haki wakifa wataenda peponi na waovu nje gizani kungojea wakati wa ufufuo wao—Vitu vyote vitarudishwa kwa umbo lao jema na kamilifu kwenye Ufufuo. Karibia mwaka 74 K.K.

Sasa mwana wangu, hapa nina mengine mengi ningependa kukwambia; kwani nafikiria kwamba akili yako ina wasiwasi kuhusu ufufuo wa wafu.

2 Tazama, nakwambia, kwamba hakuna ufufuo—au, ningesema, kwa maneno mengine kwamba mwili wenye kufa haujiviki [a]kutokufa, ya uharibifu [b]haijiviki kutoharibika—[c]mpaka baada ya kuja kwa Kristo.

3 Tazama, anawezesha [a]ufufuo wa waliokufa kutendeka. Lakini tazama, mwana wangu, ufufuo haujatimizwa bado. Sasa, nafichua kwako siri; walakini, kuna [b]siri nyingi ambazo [c]zimefichwa, ambazo hakuna azijuaye isipokuwa Mungu mwenyewe. Lakini ninakuonyesha kitu kimoja ambacho nimemwuliza Mungu kwa bidii ili nipate kujua—ambayo inahusu ufufuo.

4 Tazama, kuna wakati ambao umewekwa kwamba wote [a]watatokea kutoka wafu. Sasa wakati huu utakapotimia hakuna ajuaye; lakini Mungu anajua wakati ambao umewekwa.

5 Sasa, kama kutakuwa wakati mmoja, au wakati wa [a]pili, au wakati wa tatu, kwamba wafu watafufuka kutoka kwa wafu, haijalishi; kwani Mungu [b]anajua hivi vitu vyote; na ninatosheka kujua kwamba hii ndiyo hali—kwamba kuna wakati ambao umechaguliwa kwamba wote watafufuka kutoka kwa wafu.

6 Sasa lazima kuwe na nafasi kati ya wakati wa kifo na wakati wa kufufuka.

7 Na sasa nitakuuliza ni nini kitatokea kwa [a]roho za binadamu kutoka wakati huu wa kifo hadi wakati uliowekwa wa kufufuka?

8 Sasa kama kutakuwa na zaidi ya wakati moja ambao umewekwa kwa watu kuamka haijalishi; kwani wote hawafi wakati mmoja, na hii haijalishi; wakati wote ni kama siku moja kwake Mungu, na wakati hupimwa tu na watu.

9 Kwa hivyo, kuna wakati ambao umewekewa watu kwamba wataamka kutoka kwa wafu; na kuna nafasi kati ya wakati wa kifo na ufufuo. Na sasa, kuhusu nafasi hii ya muda, kitakachotokea kwa roho za watu ni kitu ambacho nimeuliza kwa bidii kwa Bwana nijue; ni hiki ndicho kitu ninachojua.

10 Na wakati majira yatapofika wakati wote wataamka, ndipo watakapojua kwamba Mungu anajua wakati [a]wote ambao amewekewa mtu.

40 2*a* Mos. 16:10–13. MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
b 1 Kor. 15:53–54.
c 1 Kor. 15:20.
3*a* MWM Ufufuko.
b MWM Siri za Mungu.
c M&M 25:4; 124:41.
4*a* Yn. 5:28–29.
5*a* Mos. 26:24–25; M&M 43:18; 76:85.
b MWM Mungu, Uungu.
7*a* Alma 40:21; M&M 138. MWM Nafsi.
10*a* Mdo. 17:26.

11 Sasa, kuhusu hali ya roho kati ya [a]kifo na ufufuo—Tazama, nimejulishwa na malaika, kwamba roho za watu wote, mara zinapotoka kwa mwili huu wa muda, ndiyo, roho za watu wote, zikiwa njema au ovu, zinachukuliwa [b]nyumbani kwa yule Mungu ambaye alizipatia uhai.

12 Na ndipo itakuja kuwa kwamba roho za wale walio haki zinapokelewa kwa hali ambayo ni ya [a]furaha, ambayo inaitwa [b]peponi, hali ya [c]kupumzika, hali ya [d]amani, ambapo zitapumzikia kutoka kwa taabu zao zote na kutoka kwa mashaka yote, na masikitiko.

13 Na ndipo itakuwa kwamba, zile roho za waovu, ndiyo, ambazo ni ovu—kwani tazama, hazina kipande au sehemu ya Roho wa Bwana; kwani tazama, walichagua matendo maovu kuliko matendo mema; kwa hivyo roho wa ibilisi aliingia ndani yao, na akamiliki nyumba yao—na hawa watatupwa nje katika giza la [a]nje kabisa; huko kutakuwa na [b]kulia, na kuomboleza, na kusaga meno, na hii ni kwa sababu ya uovu wao wenyewe, wakiongozwa kifungoni kwa mapenzi ya ibilisi.

14 Sasa hii ni hali ya roho ya [a]waovu, ndiyo, kwenye giza, na kwa hali ya kutisha, na [b]kuogopesha wakitarajia hasira na uchungu wa ghadhabu ya Mungu juu yao; hivyo wanabaki kwenye [c]hali hii, na vile vile walio wenye haki huko peponi, hadi wakati wao wa ufufuko.

15 Sasa, kuna wachache ambao wanaelewa kwamba hii hali ya furaha na hii hali ya taabu ya roho, kabla ya ufufuo, ilikuwa na ufufuo wa kwanza. Ndiyo, nakubali inaweza kuitwa ufufuo, kuamka kwa roho au nafsi na upatanisho kwa furaha au taabu, kulingana na maneno yaliyozungumzwa.

16 Na tazama, imezungumziwa tena, kwamba kuna [a]ufufuo wa [b]kwanza, au ufufuo wa wale ambao wamekwisha kuwepo, au ambao wako, au watakaokuwa, hadi ufufuo wa Kristo kutoka kwa wafu.

17 Sasa, hatuwezi kudhani kwamba huu ufufuo wa kwanza, ambao umezungumziwa kwa njia hii, unaweza kuwa ufufuo wa roho na [a]upatanisho wao kwa furaha au taabu. Huwezi kudhani kwamba hii ndiyo inamaanisha.

18 Tazama, nakwambia, Hapana; lakini inaamanisha kuunganisha roho na mwili, kwa wale kutoka siku za Adamu hadi kwa [a]ufufuo wa Kristo.

19 Sasa, kama roho na miili ya wale ambao wamezungumziwa

11 *a* Lk. 16:22–26; 1 Pet. 3:18–19; 4:6; M&M 76:71–74; 138.
b Mh. 12:7; 2 Ne. 9:38.
12 *a* MWM Shangwe.
b MWM Peponi.
c MWM Pumzika.
d M&M 45:46. MWM Amani.
13 *a* MWM Jehanamu.
b Mt. 8:12; Mos. 16:2.
14 *a* M&M 138:20.
b Yak. (KM) 6:13; Musa 7:1.
c Alma 34:34.
16 *a* MWM Ufufuko.
b Yak. (KM) 4:11; Mos. 15:21–23.
17 *a* M&M 76:17, 32, 50–51.
18 *a* Mt. 27:52–53.

itaunganishwa yote mara moja, waovu sawa na wenye haki, sisemi; ni ya kutosha kwangu kusema kwamba, wote watainuka; au kwa njia nyingine, ufufuko wao utakuja kupita [a]kabla ya ufufuko wa wale ambao hufa baada ya kufufuka kwa Kristo.

20 Sasa, mwana wangu, sisemi kwamba ufufuko huja wakati wa kufufuka kwa Kristo; lakini tazama, ninatoa kama maoni yangu, kwamba roho na miili zitaunganishwa, za wale wenye haki, katika ufufuko wa Kristo, na [a]kupaa kwake mbinguni.

21 Lakini kama itakuwa wakati wa ufufuko wake au ya baadaye, sisemi; lakini hii yote nasema, kwamba kuna [a]nafasi kati ya kifo na ufufuko wa mwili, na hali ya roho ndani ya [b]furaha au [c]shida mpaka wakati ambao umechaguliwa na Mungu kwamba wafu wataamka, na kuunganishwa, vyote roho na mwili, na [d]kuletwa na kusimama mbele ya Mungu, na kuhukumiwa kulingana na vitendo vyao.

22 Ndiyo, hii italeta kurudishwa kwa vitu ambavyo vimezungumziwa na midomo ya manabii.

23 [a]Roho [b]itarudishwa kwa mwili, na [c]mwili kwa roho; ndiyo, na kila sehemu na kiungo kitarudishwa kwa mwili wake; ndiyo, hata nywele ya kichwa haitapotea; lakini vitu vyote vitarudishwa kwa umbo lake sahihi na kamilifu.

24 Na sasa, mwana wangu, huku ni kurudisha ambako [a]kumezungumzwa na midomo ya manabii—

25 Na ndipo wale wenye haki wataang'aa ndani ya ufalme wa Mungu.

26 Lakini tazama, [a]kifo cha kutisha kitawajia waovu; kwani wanakufa kulingana na vitu vilivyo vya haki; kwani hawako safi, na hakuna kitu [b]kichafu kitakachorithi ufalme wa Mungu; lakini watatupwa nje, na kutolewa kupokea matunda ya vitendo vyao au kazi zao, ambazo zimekuwa mbovu; na wanakunywa machicha ya kikombe kikali.

MLANGO WA 41

Katika ufufuko wanadamu huamka katika hali ya furaha isiyo na mwisho au huzuni isiyo na mwisho—Uovu haujawahi kuwa furaha—Watu wa tamaa za kimwili hawana Mungu ulimwenguni—Kila mtu hupokea tena kwenye Ufufuko tabia na sifa alizozichuma wakati akiwa duniani. Karibia mwaka 74 K.K.

Na sasa, mwana wangu, nina machache ya kusema kuhusu ufufuko ambao umezungumziwa; kwani tazama, wengine [a]wamegeuza maandiko,

19 *a* Mos. 15:26.
20 *a* MWM Kupaa.
21 *a* Lk. 23:39–43.
b MWM Peponi.
c MWM Jehanamu.
d Alma 42:23.

23 *a* MY Roho.
M&M 88:15–17.
MWM Nafsi.
b 2 Ne. 9:12–13; Alma 11:40–45.
c MWM Mwili.

24 *a* Isa. 26:19.
26 *a* 1 Ne. 15:33; Alma 12:16.
b Alma 11:37.
41 1 *a* 2 Pet. 1:20; 3:16; Alma 13:20.

na [b]wamepotelea mbali kwa sababu ya kitu hiki. Na ninaona kwamba akili yako imekuwa na wasiwasi kuhusu kitu hiki. Lakini tazama, nitakuelezea.

2 Ninakwambia, mwana wangu, kwamba mpango wa ufufuo ni wa lazima na haki ya Mungu; kwani ni lazima kwamba vitu vyote virudishwe kwenye kanuni zao. Tazama, ni lazima na haki, kulingana na uwezo wa kufufuka kwa Kristo, kwamba roho ya kila mtu irudishwe kwa mwili wake, na kila [a]sehemu ya mwili sharti irudishwe vile ilivyokuwa.

3 Na ni lazima na [a]haki ya Mungu kwamba binadamu [b]wahukumiwe kulingana na [c]vitendo vyao; na ikiwa vitendo vyao vilikuwa vizuri kwenye maisha haya, na nia za mioyo yao zilikuwa nzuri, ndipo pia itakuwa kwa siku ya mwisho, [d]itarudishwa kwa ile ambayo ni nzuri.

4 Na ikiwa vitendo vyao ni viovu [a]watarudishiwa uovu. Kwa hivyo, vitu vyote vitarudishwa kwa kanuni zao, kila kitu kwa asili ya umbo lake—[b]mwili wenye kufa utafufuliwa katika kutokufa, [c]vilivyoharibika kwa visivyo haribika—vikiinuliwa kwenye furaha [d]isiyo na mwisho kurithi ufalme wa Mungu, au taabu isiyo ya mwisho kurithi ufalme wa ibilisi, moja kwa upande mmoja, na mwingine kwa upande mwingine—

5 Mmoja ameinuliwa kwenye furaha kulingana na nia yake ya furaha, au uzuri kulingana na mahitaji yake ya uzuri; na mwingine kwenye ubaya kulingana na nia yake ya ubaya; kwani kwa vile ametamani kutenda maovu siku yote hata hivyo atapata zawadi yake ya uovu wakati usiku utakapoingia.

6 Na hivyo iko kwenye upande mwingine. Ikiwa ametubu dhambi zake, na kuhitaji haki mpaka mwisho wa siku zake, hata hivyo atapata zawadi kwa haki.

7 [a]Hawa ni watu ambao wamekombolewa na Bwana; ndiyo, hawa ndiyo wao ambao wametolewa nje, ambao wameokolewa kutoka kwa ule usiku wa giza la milele; na hivyo wanasimama au kuanguka; kwani tazama, wanajihukumu [b]wenyewe, kama watafanya mazuri au maovu.

8 Sasa, maagizo ya Mungu [a]hayabadiliki; kwa hivyo, njia imeandaliwa kwamba yeyote atakaye angetembea juu yake na kuokolewa.

9 Na sasa tazama, mwana wangu, usijihatarishe na kosa lingine [a]moja zaidi dhidi ya Mungu juu ya yale mambo ya mafundisho, ambayo wewe umejihatarisha sasa kwa kutenda dhambi.

10 Usidhani, kwa sababu ime-

1 *b* MWM Ukengeufu.
2 *a* Alma 40:23.
3 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b MWM Amua, Hukumu; Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
c MWM Matendo.
d Hel. 14:31.
4 *a* Alma 42:28.
b 2 Ne. 9:12–13; M&M 138:17. MWM Ufufuko.
c 1 Kor. 15:51–55.
d MWM Uzima wa Milele.
7 *a* M&M 76:50–70.
b 2 Ne. 2:26; Alma 42:27; Hel. 14:30. MWM Haki ya uamuzi.
8 *a* M&M 1:38.
9 *a* M&M 42:23–28.

zungumzwa kuhusu ufufuo, kwamba utarudishwa kutoka kwenye dhambi hadi kwenye furaha. Tazama, nakwambia, [a]uovu haujapata kuwa furaha.

11 Na sasa, mwana wangu, watu wote ambao wako kwa hali ya [a]asili, au ningesema, kwenye hali ya [b]kimwili, wako kwenye masumbuko ya uchungu na kwenye kifungo cha uovu; [c]hawako na Mungu duniani, na wameenda kinyume cha asili ya Mungu; kwa hivyo, wako kwa hali ya kinyume cha furaha.

12 Na sasa tazama, je, maana ya neno kurudisha ni kuchukua kitu cha hali ya asili na kukiweka kwenye hali isiyo asili, au kukiweka katika hali kinyume cha asili yake?

13 Ee, mwana wangu, hili silo jambo; lakini maana ya neno kurudisha ni kurejesha tena uovu kwa uovu, au mwili kwa mwili, au uibilisi kwa uibilisi—uzuri kwa lile ambalo ni zuri; haki kwa kile ambacho ni haki; adilifu kwa kile ambacho ni adilifu; rehema kwa lile ambalo lina rehema.

14 Kwa hivyo, mwana wangu, ona kwamba unawarehemu ndugu zako; tenda yaliyo [a]mazuri, toa [b]hukumu kwa haki, na [c]ufanye mema kila mara; na ikiwa utafanya vitu hivi vyote ndipo utakapopokea zawadi yako; ndiyo, utapata [d]rehema irudishwe kwako tena; utapata haki kurudishwa kwako tena; utapata hukumu ya haki kurudishwa kwako tena; na utapata zawadi nzuri kutolewa kwako tena.

15 Kwani yale ambayo unayoyapeleka nje yatarudi kwako tena, na kurudishwa kwenye asili yake tena; kwa hivyo, neno kurudisha humhukumu mwenye dhambi, na haimthibitishi hata kidogo.

MLANGO WA 42

Maisha ya duniani ni wakati wa majaribio kumwezesha mtu kutubu na kumtumikia Mungu—Anguko limeleta kifo cha kimwili na cha kiroho kwa binadamu wote—Ukombozi huja kupitia toba—Mungu Mwenyewe hulipia dhambi za ulimwengu—Rehema ni kwa wale ambao wanatubu—Wengine wote wako chini ya hukumu ya Mungu—Rehema huja kwa sababu ya Upatanisho—Ni wale tu wenye toba ya kweli wanaokolewa. Karibia mwaka 74 K.K.

Na sasa, mwana wangu, naona kuna kitu kidogo zaidi ambacho kinakusumbua akili yako, ambacho huwezi kuelewa—ambacho kinahusu [a]unyoofu wa Mungu kwa kuadhibu wenye dhambi; kwani unajaribu kudhani kwamba si haki

10 *a* Zab. 32:10; Isa. 57:20–21; Hel. 13:38.
11 *a* Mos. 3:19. MWM Mwanadamu wa Tabia ya Asili.
b MWM Tamaa za kimwili.
c Efe. 2:12.
14 *a* MWM Mwaminifu, Uaminifu.
b Yn. 7:24; M&M 11:12.
c M&M 6:13; 58:27–28.
d MWM Rehema, enye Rehema.
42 1 *a* 2 Ne. 26:7; Mos. 15:26–27. MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.

kwamba wenye dhambi watupiliwe kwenye hali ya taabu.

2 Sasa tazama, mwana wangu, nitakuelezea hiki kitu. Kwani tazama, baada ya Bwana Mungu [a]kutuma wazazi wetu wa kwanza kutoka kwenye bustani ya [b]Edeni, kulima ardhi, kutoka ambapo walipelekwa—ndiyo, alimfukuza huyo mtu, na akaweka [c]makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huku na huko, kulinda [d]mti wa uzima—

3 Sasa, tunaona kwamba yule mtu alikuwa kama Mungu, akijua wema na uovu; na ili asinyooshe mkono wake mbele, na achukue pia kwa mti wa uzima, na kula na kuishi milele, Bwana Mungu aliweka makerubi na upanga wa moto, ili asile tunda—

4 Na hivyo tunaona, kwamba kulikuwa na wakati ambao uliwekewa mwanadamu kutubu, ndiyo, [a]wakati wa majaribio, wakati wa kutubu na kumtumikia Mungu.

5 Kwani tazama, kama Adamu angenyoosha mkono wake haraka, na kula kutoka kwa mti wa uzima, angeishi milele, kulingana na neno la Mungu, kukiwa hakuna nafasi ya toba; ndiyo, na pia neno la Mungu lingekuwa bure, na mpango mkuu wa wokovu ungezuiliwa.

6 Lakini tazama, ilipangiwa mwanadamu [a]kufa—kwa hivyo, vile walitolewa mbali kutoka kwa mti wa uzima wangetolewa mbali kutoka uso wa dunia—na mwanadamu alipotea milele, ndiyo, binadamu [b]wakaanguka.

7 Na sasa, kwa hii unaona kwamba wazazi wetu wa kwanza [a]walitolewa mbali yote kimwili na kiroho kutoka kwa uwepo wa Bwana; na hivyo tunaona wakawa raia wa kufuata [b]kusudi lao.

8 Sasa tazama, haikuwa ya kufaa kwamba mwanadamu arudishwe kutoka kwa kifo chake cha mwili, kwani hiyo ingeangamiza [a]mpango mkuu wa furaha.

9 Kwa hivyo, kwa vile roho haingekufa, na [a]anguko umeleta kwa wanadamu wote kifo cha roho na pia cha mwili, inaamanisha, walitolewa mbali na uwepo wa Bwana, ilikuwa ni lazima kwamba mwanadamu arudishwe kutoka kwenye kifo hiki cha roho.

10 Kwa hivyo, tangu walipokuwa wamekuwa na [a]tamaa za kimwili, uasherati, na uibilisi, kwa [b]asili, hii [c]hali ya majaribio ilikuwa hali ya wao

2*a* Mwa. 3:23–24; Musa 4:28–31.
b MWM Edeni.
c MWM Makerubi.
d Mwa. 2:9.
4*a* Alma 34:32–33.
6*a* MWM Mauti ya Kimwili.
b Mos. 16:3–5. MWM Anguko la Adamu na Hawa.
7*a* 2 Ne. 2:5; 9:6; Hel. 14:16. MWM Mauti ya Kiroho.
b MWM Haki ya uamuzi.
8*a* Alma 34:9; Musa 6:62.
9*a* MWM Anguko la Adamu na Hawa.
10*a* MWM Tamaa za kimwili.
b MWM Mwanadamu wa Tabia ya Asili.
c MWM Hali ya Kufa, enye Kufa.

kujitayarisha; ikawa hali ya matayarisho.

11 Na sasa kumbuka, mwana wangu, kama haungekuwa mpango wa ukombozi, (kuwekwa kando) upesi vile walikufa roho zao zilikuwa [a]taabuni, ikiwa imetolewa kutoka kwa uwepo wa Bwana.

12 Na sasa, hapakuwa na njia ya kudai wanadamu kutoka hali hii ya kuanguka, ambayo mwanadamu alijiletea kwa sababu ya kutotii kwake;

13 Kwa hivyo, kulingana na haki, [a]mpango wa ukombozi haungeletwa, tu kwa tabia ya [b]toba ya wanadamu katika hali hii ya majaribio, ndiyo, hali hii ya kujitayarisha; kwani isingekuwa masharti haya, rehema haingefaa isipokuwa iangamize kazi ya haki. Sasa kazi ya haki haiengeangamizwa; ikiwa hivyo, Mungu [c]angekoma kuwa Mungu.

14 Na hivyo tunaona kwamba binadamu wote [a]walianguka, na wakawa wameshikwa na [b]haki; ndiyo, haki ya Mungu ambayo amewatolea milele watolewe kwenye uwepo wake.

15 Na sasa, mpango wa rehema haungetimizwa isipokuwa upatanisho ufanywe; kwa hivyo Mungu mwenyewe [a]hulipia dhambi za ulimwengu, kutimiza mpango wa [b]rehema, kuwezesha mahitaji ya [c]haki, kwamba Mungu angekuwa [d]mkamilifu, na Mungu mwenye haki, na Mungu wa huruma pia.

16 Sasa, toba haingewajia watu isipokuwa kuwe na adhabu, ambayo pia ilikuwa ya [a]milele kama vile uhai wa roho ulivyo, umepandikishwa kinyume na mpango wa furaha, ambao ulikuwa wa milele kama vile uhai wa roho ulivyo.

17 Sasa, mtu anaweza kutubu namna gani isipokuwa atende dhambi? Ni vipi angetenda [a]dhambi ikiwa hapakuweko na [b]sheria? Kungekuwaje sheria kusipokuwa na adhabu?

18 Sasa, kulikuwa na adhabu iliyobandikwa, na sheria ya haki ikatolewa, ambayo ilileta majuto ya [a]dhamiri kwa watu.

19 Sasa, kama sheria haingetolewa—ikiwa mtu [a]ataua sharti auawe—je, angeogopa kwamba angekufa ikiwa angeua?

20 Na pia, kama hakungekuwa na sheria kutolewa dhidi ya dhambi watu hawangeogopa kutenda dhambi.

21 Na kama sheria [a]haingetolewa, wakati watu wanatenda dhambi, haki ingefanya nini au rehema, kwani hawangekuwa na madai juu ya kiumbe?

22 Lakini sheria imetolewa, na adhabu kuwekwa, na [a]toba kukubaliwa; toba ambayo, rehema

11 *a* 2 Ne. 9:7–9.
13 *a* MWM Mpango wa Ukombozi.
b MWM Toba, Tubu.
c 2 Ne. 2:13–14.
14 *a* Alma 22:13–14.
b 2 Ne. 2:5.
15 *a* 2 Ne. 9:7–10; Mos. 16:7–8.
MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
b MWM Rehema, enye Rehema.
c MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
d 3 Ne. 12:48.
16 *a* M&M 19:10–12.
17 *a* MWM Dhambi.
b Rum. 4:15.
18 *a* MWM Dhamiri.
19 *a* MWM Mauaji.
21 *a* 2 Ne. 9:25–26; Mos. 3:11.
22 *a* MWM Toba, Tubu.

hudai; la sivyo, kazi ya haki ingedai kiumbe na kutimiza sheria, na sheria kutoa adhabu; kama sio hivyo matendo ya haki yangeangamizwa, na Mungu kukoma kuwa Mungu.

23 Lakini Mungu hakomi kuwa Mungu, na [a]rehema hudai wanaotubu, na rehema huja kwa sababu ya upatanisho; na [b]upatanisho huleta [c]ufufuo wa wafu; na ufufuo wa wafu [d]huwarudisha watu kwenye uwepo wa Mungu; na hivyo wanarudishwa kwenye uwepo wake, [e]kuhukumiwa kulingana na matendo yao, kulingana na sheria na haki.

24 Kwani tazama, haki hutekeleza madai yake yote, na pia huruma hudai yote yaliyo yake; na hivyo, hakuna ila tu waliotubu kwa ukweli watakaokolewa.

25 Ni nini, unadhani kwamba rehema inaweza kuibia [a]haki? Ninakwambia, Hapana; hata chembe kimoja. Ikiwa hivyo, Mungu atakoma kuwa Mungu.

26 Na hivyo Mungu hutimiza [a]kusudi lake kubwa na la milele, ambalo lilitayarishwa [b]kutokea msingi wa dunia. Na hivyo huja wokovu na ukombozi wa binadamu, na pia maangamizo yao na taabu.

27 Kwa hivyo, Ee mwana wangu, [a]yeyote atakeyekuja angekuja na kunywa maji ya uzima bure; yeyote atakayekataa kuja hivyo hatashurutishwa kuja; lakini katika siku ya mwisho [b]itarudishwa kwake kulingana na [c]vitendo vyake.

28 Ikiwa anatamani kufanya [a]uovu, na hajatubu katika siku zake, tazama, uovu utafanywa kwake, kulingana na kurudishwa kwa Mungu.

29 Na sasa, mwana wangu, nataka kwamba usiache vitu hivi vikusumbue mara nyingine, na ni dhambi zako tu zikusumbue, pamoja na taabu hiyo ambayo itakuleta wewe katika toba.

30 Ee mwana wangu, nataka kwamba usikane haki ya Mungu mara nyingine. Usijaribu kujisamehe mwenyewe hata kwa njia ndogo kwa sababu ya dhambi zako, kwa kukataa haki ya Mungu; lakini uache haki ya Mungu, na rehema yake, na uvumilivu wake uvume ndani ya moyo wako; na acha ikulete chini kwenye mavumbi ndani ya [a]unyenyekevu.

31 Na sasa, Ee mwana wangu, umeitwa na Mungu kuhubiri neno kwa hawa watu. Na sasa, mwana wangu, nenda njia zako, tangaza neno kwa ukweli na busara, kwamba uzilete roho kwenye toba, kwamba mpango mkuu wa rehema ungekuwa na

23*a* MWM Rehema, enye Rehema.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
c 2 Ne. 2:8; 9:4; Alma 7:12; 11:41–45; 12:24–25; Hel. 14:15–18; Morm. 9:13.
d Alma 40:21–24.
e MWM Hukumu ya mwisho.
25*a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
26*a* 2 Ne. 2:14–30; Musa 1:39.
b Alma 13:3; 3 Ne. 1:14.
27*a* Alma 5:34; Hel. 14:30. MWM Haki ya uamuzi.
b Alma 41:15.
c Isa. 59:18; Ufu. 20:12.
28*a* Alma 41:2–5.
30*a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.

madai juu yao. Na Mungu akupatie hata kulingana na maneno yangu. Amina.

MLANGO WA 43

Alma na wanawe wanahubiri neno—Wazoramu na Wanefi wengine waasi wanakuwa Walamani—Walamani wanakabiliana na Wanefi katika vita—Moroni anawapa Wanefi silaha za kujilinda—Bwana anamwonyesha Alma mkakati wa Walamani—Wanefi wanalinda miji yao, uhuru, familia, na dini—Majeshi ya Moroni na Lehi yanawazingira Walamani. Karibia mwaka 74 K.K.

Na sasa ikawa kwamba wana wa Alma walikwenda miongoni mwa watu, kutangaza neno kwao. Na Alma, pia, mwenyewe, hangepumzika, na yeye pia alienda mbele.

2 Sasa hatutazungumza mengi kuhusu kuhubiri, kwao isipokuwa kwamba walihubiri neno, na ukweli, kulingana na roho ya unabii na ufunuo; na walihubiri kulingana na [a]mpango mtakatifu wa Mungu ambao waliitiwa.

3 Na sasa narudia historia ya vita miongoni mwa Wanefi na Walamani, katika mwaka wa kumi na nane wa utawala wa waamuzi.

4 Kwani tazama, ikawa kwamba [a]Wazoramu waligeuka na kuwa Walamani; kwa hivyo, katika mwanzo wa mwaka wa kumi na nane watu wa Wanefi waliona kwamba Walamani walikuwa wanataka kuwashambulia; kwa hivyo walijiandaa kwa vita; ndiyo, walikusanya pamoja majeshi yao katika nchi ya Yershoni.

5 Na ikawa kwamba Walamani walikuja kwa maelfu; na wakaja katika nchi ya Antionumu, ambayo ni nchi ya Wazoramu; ambamo mtu kwa jina la Zerahemna alikuwa kiongozi.

6 Na sasa, kwa vile Waamaleki walikuwa watu waovu na wauaji kuliko Walamani walivyokuwa, kwao wenyewe, kwa hivyo, Zerahemna aliteua makapteni wakuu juu ya Walamani, na wote walikuwa Waamaleki na Wazoramu.

7 Sasa alifanya hivi ili kuhifadhi chuki yao kwa Wanefi, ili awamiliki na kutimiza kusudi lake.

8 Kwani tazama, kusudi lake lilikuwa kuwavuruga Walamani wawe na hasira dhidi ya Wanefi; alifanya hivi ili apate uwezo mwingi juu yao, na pia kwamba ajipatie uwezo juu ya Wanefi kwa kuwaweka katika utumwa.

9 Na sasa kusudi la Wanefi lilikuwa kulinda nchi yao, na nyumba zao, na [a]wake zao, na watoto wao, ili wawaokoe kutoka kwa mikono ya maadui wao; na pia kwamba wahifadhi haki zao na mapendeleo yao, ndiyo, na pia [b]uhuru wao, kwamba wapate kumwabudu Mungu kulingana na kutaka kwao.

10 Kwani walijua kwamba ikiwa wangeshikwa mateka na Walamani, kwamba yeyote

43 2*a* MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
4*a* Alma 35:2–14; 52:33.
9*a* Alma 44:5; 46:12.
b MWM Huru, Uhuru.

[a]atakayemwabudu Mungu kwa [b]roho na kwa ukweli, Mungu wa kweli na anayeishi Walamani wangemwangamiza.

11 Ndiyo, na walijua pia ile chuki mbaya iliyokuweko ya Walamani kwa [a]ndugu zao, ambao walikuwa watu wa Anti-Nefi-Lehi, ambao waliitwa watu wa Amoni—na hawengechukua silaha, ndiyo, walikuwa wamefanya agano ambalo hawangevunja—kwa hivyo, kama wangeanguka kwenye mikono ya Walamani wangeangamizwa.

12 Na Wanefi hawangekubali kwamba waangamizwe; kwa hivyo waliwakabidhi nchi kwa ajili ya urithi wao.

13 Na watu wa Amoni walitoa sehemu kubwa ya mali yao kwa Wanefi kusaidia majeshi yao; na hivyo Wanefi walilazimishwa, kusimama, pekee yao, dhidi ya Walamani, ambao walikuwa muungano wa Lamani na Lemueli, na wana wa Ishmaeli, na wale wote ambao hawakukubaliana na Wanefi, ambao walikuwa ni Waamaleki na Wazoramu, na [a]uzao wa makuhani wa Nuhu.

14 Sasa vile vizazi vilikuwa vingi, karibu vile na vya Wanefi walivyokuwa; na hivyo Wanefi walilazimishwa kupigana na ndugu zao, hata kwa kumwaga damu.

15 Na ikawa wakati majeshi ya Walamani yalipokuwa yamejikusanya pamoja katika nchi ya Antionumu, tazama, majeshi ya Wanefi yalikuwa yamejiandaa kukabiliana nao katika nchi ya Yershoni.

16 Sasa, kiongozi wa Wanefi, au mtu ambaye alichaguliwa kuwa kapteni mkuu juu ya Wanefi—sasa kapteni mkuu alichukua jukumu la kuamrisha majeshi yote ya Wanefi—na jina lake lilikuwa Moroni;

17 Na Moroni alijitwalia amri yote, na utawala wa vita vyao. Na alikuwa na umri wa miaka ishirini na tano tu alipochaguliwa kuwa kapteni mkuu juu ya majeshi ya Wanefi.

18 Na ikawa kwamba alikabiliana na Walamani kwenye mipaka ya Yershoni, na watu wake walijihami na panga, na vitara, na kila aina ya silaha za vita.

19 Na wakati majeshi ya Walamani yalipoona kwamba watu wa Nefi, au kwamba Moroni, ameandaa watu wake kwa dirii na ngao za vita, ndiyo, na pia ngao za kujikinga vichwa, na pia kuwa walikuwa wamevaa mavazi mazito—

20 Sasa jeshi la Zerahemna halikuwa limejitayarisha kwa kitu cha aina hii; walikuwa tu na panga zao na vitara vyao, pinde zao na mishale yao, mawe yao na kombeo zao; na walikuwa uchi, isipokuwa tu ngozi iliyofunika viuno vyao; ndiyo, wote walikuwa [a]uchi, isipokuwa Wazoramu na Waamaleki;

21 Lakini hawakuwa wamejihami dirii, wala ngao—kwa hivyo, waliogopa sana majeshi ya Wanefi kwa sababu ya silaha

10 *a* MWM Kuabudu.
b Yn. 4:23–24.

11 *a* Alma 24:1–3, 5, 20; 25:1, 13; 27:2, 21–26.

13 *a* Alma 25:4.

20 *a* Eno. 1:20.

zao, ingawaje idadi yao ilikuwa kubwa mno kuliko ya Wanefi.

22 Tazama, sasa ikawa kwamba hawakuthubutu kuwashambulia Wanefi kwenye mipaka ya Yershoni; kwa hivyo waliondoka nje ya nchi ya Antionumu hadi kwenye nyika, na kusafiri wakizingira nyika, mbali na chimbuko la mto Sidoni, ili waingie katika nchi ya Manti na kuimiliki nchi; kwani hawakutarajia kwamba majeshi ya Moroni yangejua kule walikokwenda.

23 Lakini ikawa kuwa, walipoondoka kuelekea nyikani Moroni alituma wapelelezi nyikani kuchunguza kambi yao; na Moroni, pia, akiwa anaelewa unabii wa Alma, akatuma watu kwake, akitamani kwamba amwulize Bwana [a]wapi majeshi ya Wanefi yangeenda kujikinga dhidi ya Walamani.

24 Na ikawa kwamba neno la Bwana lilimjia Alma, na Alma akawajulisha wajumbe wa Moroni, kwamba majeshi ya Walamani yalikuwa yameenda taratibu yakizunguka nyikani, ili yaingie kwenye nchi ya Manti, ili yaanzishe vita mahali ambapo watu walipungukiwa na nguvu. Na wale wajumbe walienda na kufikisha ujumbe kwa Moroni.

25 Sasa Moroni, akiacha sehemu ya jeshi lake katika nchi ya Yershoni, isiwe kwa vyovyote kwamba sehemu ya Walamani ije katika nchi hiyo na kumiliki mji, alichukua jeshi lililosalia na akaenda kwenye nchi ya Manti.

26 Na alisababisha kwamba watu wote katika sehemu hiyo wajikusanye wenyewe pamoja kukabiliana dhidi ya Walamani, [a]kulinda ardhi yao na nchi yao, haki zao na uhuru wao; kwa hivyo walijiandaa dhidi ya ule wakati ambao Walamani wangekuja.

27 Na ikawa kwamba Moroni alisababisha kwamba jeshi lake lijifiche kwenye bonde ambalo lilikuwa karibu na ufuko wa mto Sidoni, ambao ulikuwa magharibi mwa mto Sidoni katika nyika.

28 Na Moroni aliweka wapelelezi kila mahali, ili aweze kujua wakati kambi ya Walamani itapokuja.

29 Na sasa, kwa vile Moroni alijua nia ya Walamani, kwamba ilikuwa nia yao kuangamiza ndugu zao, au kuwaweka chini yao na kuwafanya watumwa ili waanzishe utawala wao nchini kote;

30 Na pia akijua kwamba ilikuwa nia ya pekee ya Wanefi kuhifadhi nchi yao, na [a]uhuru wao, na kanisa lao, kwa hivyo hakufikiri ni dhambi kuwalinda kwa werevu; kwa hivyo, aligundua kupitia kwa wapelelezi wake njia ambayo Walamani watafuata.

31 Kwa hivyo, aligawanya jeshi lake na kuleta sehemu moja kwenye bonde, na akawaficha mashariki, na kusini mwa mlima Ripla;

23*a* Alma 48:16.
26*a* M&M 134:11.
30*a* Alma 46:12, 35.

32 Na waliosalia aliwaficha kwenye bonde la magharibi, magharibi mwa mto Sidoni, na hivyo chini hadi kwenye mipaka ya nchi ya Manti.

33 Na hivyo akiwa ameweka jeshi lake kulingana na mipango yake, alikuwa tayari kukabiliana nao.

34 Na ikawa kwamba Walamani walikuja juu kaskazini mwa mlima, ambapo sehemu ya jeshi la Moroni ilijificha.

35 Na vile Walamani walikuwa wamepita mlima Ripla, na wakaja ndani ya bonde, na wakaanza kuvuka mto Sidoni, jeshi ambalo lilikuwa limefichwa kusini mwa mlima, ambalo liliongozwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa [a]Lehi, na akaongoza jeshi lake mbele na kuzingira Walamani mashariki nyuma yao.

36 Na ikawa kwamba Walamani, wakati walipoona Wanefi wakiwajia kutoka nyuma yao, waligeuka na kuanza kukabiliana na jeshi la Lehi.

37 Na kazi ya mauaji ilianza pande zote mbili, lakini ilikuwa ya kutisha zaidi kwa upande wa Walamani, kwani [a]uchi wao ulijidhihirisha kwa mapigo makubwa ya Wanefi kwa panga zao na vitara vyao, ambavyo vilileta vifo karibu kwa kila pigo.

38 Wakati kwa upande mwingine, kulikuwa na mtu mmoja hapa na pale akiuawa miongoni mwa Wanefi, kwa panga zao na kwa kupoteza damu, hawa wakiwa wemejikinga sehemu muhimu za mwili, au sehemu muhimu za mwili zikikingwa kutoka na mapigo ya Walamani, kwa [a]dirii zao, na ngao zao za mikono, na vyapeo vyao; na hivyo Wanefi waliendelea na kazi ya mauaji miongoni mwa Walamani.

39 Na ikawa kwamba Walamani waliogopa, kwa sababu ya uharibifu mkuu miongoni mwao, hata mpaka wakaanza kutoroka kuelekea mto Sidoni.

40 Na walifuatwa na Lehi na watu wake; na walikimbizwa na Lehi hadi kwenye maji ya Sidoni, na wakavuka maji ya Sidoni. Na Lehi aliweka majeshi yake kwenye ukingo wa mto Sidoni kwamba wasivuke.

41 Na ikawa kwamba Moroni na jeshi lake walikabiliana na Walamani kwenye bonde, kwa upande mwingine wa mto Sidoni, na wakaanza kuwaangukia na kuwauwa.

42 Na Walamani wakakimbia kutoka kwao, kuelekea nchi ya Manti; na wakakutana tena na majeshi ya Moroni.

43 Sasa kwa hali hii Walamani walipigana sana; ndiyo, hakujakuwa na wakati Walamani wamejulikana kwa kupigana kwa nguvu kama hii na ujasiri, la, sio hata kutoka mwanzoni.

44 Na walitiwa moyo na [a]Wazoramu na Waamaleki, ambao walikuwa makapteni wao wakuu na viongozi, na Zerahemna, ambaye alikuwa kapteni wao mkuu, au kiongozi wao

35*a* Alma 49:16.
37*a* Alma 3:5.
38*a* Alma 44:8–9.
44*a* Alma 43:6.

mkuu na amri jeshi; ndiyo, walipigana kama majoka yenye, na wengi wa Wanefi waliuawa kwa mikono yao, ndiyo, kwani walipasua kwa vipande viwili vyapeo vyao, na wakatoboa dirii zao nyingi, na wakakata mikono yao; na hivyo Walamani walikata kwa hasira yao nyingi.

45 Walakini, Wanefi waliongozwa na sababu njema, kwani hawakuwa [a]wanapigania utawala wala uwezo lakini walipigania maskani yao na [b]uhuru wao, wake zao na watoto wao, na vyote vyao, ndiyo, kwa kanuni zao za kuabudu na kanisa lao.

46 Na walifanya hayo ambayo walifikiri ni [a]jukumu ambalo waliwiwa Mungu wao; kwani Bwana alikuwa amewaambia, na pia kwa babu zao, kwamba: [b]Kwa kuwa hamna hatia kwa kosa la [c]kwanza, wala la pili, hamtakubali wenyewe kuuawa kwa mikono ya maadui wenu.

47 Na tena Bwana, amesema kwamba: [a]Mtalinda jamaa zenu hata kwa umwagaji wa damu. Kwa hivyo kwa sababu hii Wanefi walikuwa wakipigana na Walamani, kujilinda wenyewe, na jamaa zao, na nchi yao, na haki zao, na dini yao.

48 Na ikawa kwamba watu wa Moroni walipoona ukali na hasira ya Walamani, walikuwa karibu kurudi nyuma na kutoroka kutoka kwao. Na Moroni akiona kusudi lao, alituma ujumbe mbele na akavuta mioyo yao kwa mawazo haya—ndiyo, mawazo ya nchi yao, uhuru wao, ndiyo, uhuru wao kutoka utumwani.

49 Na ikawa kwamba waliwashambulia Walamani, na [a]wakapaza sauti pamoja kwa Bwana Mungu wao, kwa ungwana wao na uhuru wao kutoka utumwani.

50 Na wakaanza kusimama dhidi ya Walamani kwa nguvu; na kwenye ile saa yenyewe kwamba walimlilia Bwana kwa uhuru wao, Walamani walianza kukimbia kutoka kwao; na wakakimbia hata kwenye maji ya Sidoni.

51 Sasa Walamani walikuwa wengi zaidi, ndiyo, zaidi ya mara mbili kuliko idadi ya Wanefi; walakini, walikimbizwa sana kwamba wakajikusanya kwa kundi moja katika bonde, kando ya mto Sidoni.

52 Kwa hivyo majeshi ya Moroni yaliwazingira, ndiyo, hata pande zote mbili za mto, kwani tazama, kwa upande wa mashariki kulikuwa na watu wa Lehi.

53 Kwa hivyo wakati Zerahemna alipoona watu wa Lehi upande wa mashariki wa mto Sidoni, na majeshi ya Moroni upande wa magharibi wa mto Sidoni, kwamba walikuwa wamezingirwa na Wanefi, walishikwa na woga.

54 Sasa Moroni, alipoona woga wao, aliamuru watu wake waache kumwaga damu yao.

45*a* Alma 44:5.
b MWM Huru, Uhuru.
46*a* MWM Wajibu.
b Alma 48:14; M&M 98:33–36.
c 3 Ne. 3:21; M&M 98:23–24.
47*a* M&M 134:11.
49*a* Ku. 2:23–25; Mos. 29:20.

MLANGO WA 44

Moroni anawaamuru Walamani wafanye agano la amani au waangamizwe—Zerahemna anakataa toleo, na vita vinaanza tena—Majeshi ya Moroni yanawashinda Walamani. Karibia mwaka 74–73 K.K.

Na ikawa kwamba waliacha na wakarudi nyuma hatua kutoka kwao. Na Moroni akamwambia Zerahemna: Tazama, Zerahemna, kwamba [a]hatutamani kuwa watu wa damu. Unajua kwamba mko mikononi mwetu, na bado hatutaki kuwaua.

2 Tazama, hatukuja nje kupigana dhidi yenu ili tumwage damu yenu kwa nguvu; wala hatutaki kumweka yeyote kwenye nira ya kifungo. Lakini hii ndiyo sababu ambayo imewasababisha ninyi kutujia sisi; ndiyo, na mmetukasirikia nasi kwa sababu ya dini yetu.

3 Lakini sasa, unaona kwamba Bwana yuko pamoja nasi; na unaona kwamba amewakabidhi ninyi mikononi mwetu. Na sasa nataka wewe ujue kwamba hii imefanywa kwetu kwa sababu ya dini yetu na imani katika Kristo. Na sasa mnaona kwamba hamwezi kuiangamiza hii imani yetu.

4 Sasa unaona kwamba hii ni imani ya kweli ya Mungu; ndiyo, unaona kwamba Mungu atatusaidia, na kutuweka, na kutuhifadhi, kadiri tuwe waaminifu kwake, na kwa imani yetu, na dini yetu; na kamwe Bwana hatakubali kwamba tuangamizwe isipokuwa tuanze kufanya makosa na kukana imani yetu.

5 Na sasa, Zerahemna, nakuamuru, kwa jina la Mungu aliye na uwezo wote, ambaye ameimarisha mikono yetu kwamba tumepata uwezo juu yenu, kupitia imani yetu, kwa dini yetu, kwa [a]kanuni zetu za kuabudu, na kwa kanisa letu, na kwa kazi yetu takatifu ya kusaidia wake zetu na watoto wetu, na kwa ule [b]uhuru ambao unatuunganisha sisi kwa ardhi zetu na nchi yetu; ndiyo, na pia kwa kushikilia neno takatifu la Mungu, ambalo kwake tunawiwa furaha yetu; na kwa yote yaliyo muhimu kwetu—

6 Ndiyo, na haya siyo yote; ninakuamuru kwa tamaa yote ambayo unayo kwa kuishi, kwamba utoe silaha zako za vita kwetu, na hatutataka kumwaga damu yenu, lakini tutaokoa maisha yenu, ikiwa mtaenda zenu na msirudi tena kupigana dhidi yetu.

7 Na sasa, kama hamfanyi hivi, tazama, mko mikononi mwetu, na nitaamuru watu wangu wawaangukie, na kuwapiga vidonda vya kifo miilini mwenu, kwamba mmalizike; na ndipo tutaona ni nani atakuwa na uwezo juu ya hawa watu; ndiyo, tutaona ni nani atakayewekwa utumwani.

8 Na sasa ikawa kwamba wakati Zerahemna aliposikia misemo hii alikuja mbele na

44 1*a* Alma 43:45. | 5*a* MWM Ibada. | *b* MWM Huru, Uhuru.

kutoa upanga wake na kitara chake, na pinde yake mikononi mwa Moroni, na akamwambia: Tazama, hapa kuna silaha zetu za vita; tutazikabidhi kwenu, lakini hatutakubali wenyewe kuchukua [a]kiapo kwako, ambacho tunajua kwamba tutavunja, na watoto wetu pia; lakini chukueni silaha zetu za vita, na kubali kwamba tuondoke na kwenda nyikani; la sivyo tutabaki na panga zetu, na tutaangamia au kushinda.

9 Tazama, sisi sio wa imani yenu; hatuamini kwamba ni Mungu ambaye ametukabidhi mikononi mwenu; lakini tunaamini kwamba ni ujanja wenu ambao umewahifadhi kutoka kwa panga zetu. Tazama, ni [a]dirii zenu na ngao zenu ambazo zimewahifadhi.

10 Na sasa wakati Zerahemna alipomaliza kuzungumza maneno haya, Moroni alirejesha upanga na silaha za vita, ambazo alikuwa amepokea, kwa Zerahemna, akisema: Tazama, tutamaliza pambano.

11 Sasa siwezi kukumbuka maneno ambayo nimesema, kwa hivyo vile Bwana anavyoishi, hamtaondoka isipokuwa mwondoke na kiapo kwamba hamtarudi tena kwetu kupigana. Sasa vile mko mikononi mwetu tutamwaga damu yenu mchangani, au mkubaliane na masharti ambayo nimetoa.

12 Na sasa wakati Moroni alikuwa amesema maneno haya, Zerahemna aliweka upanga wake, na akamkasirikia Moroni, na akatimka mbele ili amuue Moroni; lakini alipoinua upanga wake, tazama, mmoja wa askari wa Moroni aliupiga hata kwenye ardhi, na ukavunjika kwenye kipini; na pia akampiga Zerahemna kwamba alitoa ngozi ya kichwa chake na ikaanguka ardhini. Na Zerahemna alijiondoa kutoka kwao kupitia katikati ya askari wake.

13 Na ikawa kwamba yule askari ambaye alikuwa amesimama karibu, yule ambaye alikata na kutoa ngozi ya kichwa cha Zerahemna, alichukua ngozi ya kichwa kutoka ardhini kwa kushika nywele, na kuiweka kwenye ncha ya upanga wake, na akaunyoosha mbele yao, akisema kwao kwa sauti kubwa:

14 Hata vile ngozi hii imeanguka ardhini, ambayo ni ngozi ya mkuu wenu, hivyo ndivyo mtaanguka ardhini isipokuwa mtoe silaha zenu za vita na kuondoka na agano la amani.

15 Sasa kulikuwa na wengi, wakati waliposikia maneno haya na kuona ngozi ya kichwa ambayo ilikuwa kwenye upanga, kwamba walishikwa na woga; na wengi walisonga mbele na kutupa chini silaha zao za vita miguuni mwa Moroni, na kufanya [a]agano la amani. Na vile wengi waliingia kwenye agano waliwakubalia waelekee nyikani.

16 Sasa ikawa kwamba

8*a* MWM Kiapo.
9*a* Alma 43:38.
15*a* 1 Ne. 4:37; Alma 50:36.

Zerahemna alighadhibika sana, na akawavuruga askari wake waliosalia kwa hasira, kukabiliana na nguvu zaidi dhidi ya Wanefi.

17 Na sasa Moroni alikasirika, kwa sababu ya ukaidi wa Walamani; kwa hivyo aliwaamuru watu wake kwamba wawaangukie na kuwaua. Na ikawa kwamba walianza kuwaua; ndiyo, na Walamani walipigana na panga zao na uwezo wao.

18 Lakini tazama, ngozi zao zilizokuwa uchi na vichwa vyao vilivyokuwa bure vilikuwa wazi kwa panga za Wanefi; ndiyo, tazama zilitobolewa na kukatwa, ndiyo, na walianguka haraka sana mbele ya panga za Wanefi; na wakaanza kufagiliwa chini, hata vile askari wa Moroni alivyokuwa amebashiri.

19 Sasa Zerahemna, alipoona kwamba walikuwa karibu kuangamizwa wote, alilia sana kwa Moroni, akiahidi kwamba ataweka maagano na pia watu wake na wao, ikiwa wataponya maisha ya waliosalia, kwamba [a]hawatarudi tena kupigana dhidi yao.

20 Na ikawa kwamba Moroni alisababisha kwamba kazi ya kifo isimamishwe tena miongoni mwa watu. Na akachukua silaha za vita kutoka kwa Walamani; na baada ya kuingia kwenye [a]agano la amani na yeye, walikubaliwa kuondoka kwenda kwenye nyika.

21 Sasa idadi ya wafu wao haikuhesabika kwa sababu ya wingi wa idadi; ndiyo, idadi ya wafu wao ilikuwa kubwa sana, kote kwa Wanefi na Walamani.

22 Na ikawa kwamba walitupa wafu wao ndani ya maji ya Sidoni, na wameenda mbele na kuzikwa kwenye kilindi cha bahari.

23 Na majeshi ya Wanefi, au ya Moroni, yalirejea na kwenda kwenye nyumba zao na nchi zao.

24 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na nane wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi. Na hivyo yakaisha maandishi ya Alma, ambayo yaliandikwa kwenye mabamba ya Nefi.

Historia ya watu wa Nefi, na vita vyao na mafarakano yao, katika siku za Helamani, kulingana na maandishi ya Helamani, ambayo aliweka katika siku zake.

Yenye milango ya 45 hadi 62.

MLANGO WA 45

Helamani anaamini maneno ya Alma—Alma anatabiri kuangamizwa kwa Wanefi—Anabariki na kulaani nchi—Inaonekana Alma alichukuliwa juu na Roho, kama vile Musa—Mfarakano unatokea kanisani. Karibia mwaka 73 K.K.

Tazama, sasa ikawa kwamba watu wa Nefi walikuwa na furaha sana, kwa sababu Bwana

19*a* Alma 47:6.

20*a* Alma 62:16–17.

alikuwa amewaokoa tena kutoka mikono ya maadui wao; kwa hivyo walitoa shukrani kwa Bwana Mungu wao; ndiyo, na [a]walifunga sana, na kuomba sana na wakamwabudu Mungu kwa shangwe kuu.

2 Na ikawa katika mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, kwamba Alma alimjia mwana wake Helamani na kumwambia: Unaamini wewe maneno ambayo nilikuzungumzia kuhusu yale [a]maandiko ambayo yamehifadhiwa?

3 Na Helamani akasema kwake: Ndiyo, naamini.

4 Na Alma akasema tena: Unaamini katika Yesu Kristo, atakayekuja?

5 Na akasema: Ndiyo, ninaamini maneno yote ambayo umesema.

6 Na Alma akasema kwake tena: [a]Utaweka amri zangu?

7 Na akasema: Ndiyo, nitatii amri zako kwa moyo wangu wote.

8 Na Alma akamwambia: Umebarikiwa wewe; na Bwana [a]atakufanikisha katika nchi hii.

9 Lakini tazama, nitakutolea [a]unabii mdogo; lakini yale ambayo nita kwako usifanye yajulikane; ndiyo, yale nitakayotabiri kwako hayatafanywa yasijulikane, hata mpaka utabiri utakavyotimizwa; kwa hivyo andika maneno ambayo nitasema.

10 Na haya ndiyo maneno: Tazama, ninaona kwamba watu hawa, Wanefi, kulingana na roho ya ufunuo ambayo iko ndani yangu, katika miaka [a]mia nne kutoka wakati ambao Yesu Kristo atajidhihirisha kwao, watafifia kwa [b]kutoamini.

11 Ndiyo, na ndipo wataona vita na maradhi ya kuambukiza, ndiyo, njaa na umwagaji wa damu, hata mpaka watu wa Nefi [a]watakapomalizika—

12 Ndiyo, na itafanyika kwa sababu watafifia katika kutoamini na kuangukia kazi za gizani, na [a]uzinzi, na aina yote ya uovu; ndiyo, nakwambia, kwamba kwa sababu watakosa dhidi ya mwangaza ulio mkubwa na hekima, ndiyo, nakwambia, kwamba kutokea siku hiyo, hata kizazi cha nne hakitapita kabla ya huu uovu kutokea.

13 Na wakati ile siku kuu itakapowadia, tazama, wakati unawadia mapema kwamba wale ambao wako sasa, au uzao wa wale ambao wamehesabiwa miongoni mwa watu wa Nefi, [a]hawatahesabiwa tena miongoni mwa watu wa Nefi.

14 Lakini yeyote atakayebaki, na haangamizwi katika ile siku kuu na ya kuogopesha, [a]atahesabiwa miongoni mwa

45 1*a* MWM Funga, Kufunga.
2*a* Alma 37:1–5; 50:38.
6*a* MWM Amri za Mungu; Mtiifu, Tii, Utii.
8*a* 1 Ne. 4:14; Alma 48:15–16, 25.
9*a* MWM Toa unabii, Unabii.
10*a* 1 Ne. 12:10–15; Hel. 13:9; Morm. 8:6–7.
b MWM Kutoamini; Ukengeufu.
11*a* Yar. 1:10; Morm. 8:2–3, 6–7.
12*a* MWM Tamaa mbaya.
13*a* Hel. 3:16.
14*a* Moro. 9:24.

Walamani, na atakuwa kama wao, wote, isipokuwa wachache ambao wataitwa wanafunzi wa Bwana; na hao Walamani watawawinda mpaka wakati [b]watakapomalizika. Na sasa, kwa sababu ya uovu, huu unabii utatimizwa.

15 Na sasa ikawa kwamba baada ya Alma kusema vitu hivi kwa Helamani, alimbariki, na pia wanawe wengine; na pia akabariki ardhi kwa wale walio [a]haki.

16 Na akasema: Hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu—Nchi [a]italaaniwa, ndiyo, nchi hii, kwa kila taifa, kabila, lugha, na watu, kwa uangamizo, ambao wanafanya uovu, wakati watakapoiva kabisa kwa uovu; na vile nimesema ndivyo itakavyokuwa; kwani hii ni laana na [b]baraka ya Mungu juu ya nchi, kwani Bwana hawezi kuangalia dhambi na kuivumilia hata [c]kidogo.

17 Na sasa, wakati Alma alipokuwa amesema maneno haya alibariki [a]kanisa, ndiyo, wale wote ambao watasimama imara katika imani kutokea wakati huo na kuendelea.

18 Na wakati Alma alipofanya haya aliondoka kutoka nchi ya Zarahemla, kama anayeenda katika nchi ya Meleki. Na ikawa kwamba hakusikika tena; hatujui kulingana kifo chake au kuzikwa kwake.

19 Tazama, haya tunajua, kwamba alikuwa mtu wenye haki; na msemo ukaenea kanisani kwamba alichukuliwa na Roho, au [a]kuzikwa kwa mkono wa Bwana, kama vile Musa. Lakini tazama, maandiko yanasema kuwa Bwana alimchukua Musa kumrudisha kwake mwenyewe; na tunadhani kwamba pia amempokea Alma katika roho, kwake mwenyewe; kwa hivyo, kwa sababu hii hatujui chochote kuhusu kifo chake wala mazishi yake.

20 Na sasa ikawa katika mwanzo wa mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, kwamba Helamani alienda miongoni mwa watu kuwatangazia neno.

21 Kwani tazama, kwa sababu ya vita vyao na Walamani na mafarakano mengi madogo na vurugu ambazo zilikuwa miongoni mwa watu, ilikuwa ni lazima kwamba [a]neno la Mungu litangazwe kwao, ndiyo, na kwamba maagizo yafanywe kokote kanisani.

22 Kwa hivyo, Helamani na ndugu zake walienda mbele na kuanzisha kanisa tena katika nchi, ndiyo, katika kila mji kote katika nchi ambao ulikuwa umemilikiwa na watu wa Nefi. Na ikawa kwamba waliteua makuhani na walimu kote nchini, juu ya makanisa yote.

23 Na sasa ikawa kwamba baada ya Helamani na ndugu zake kuteua makuhani na walimu

14*b* Moro. 1:1–3.
15*a* Alma 46:10; 62:40.
16*a* 2 Ne. 1:7; Alma 37:31; Eth. 2:8–12.
b M&M 130:21.
c M&M 1:31.
17*a* MWM Kanisa la Yesu Kristo.
19*a* MWM Viumbe waliobadilishwa.
21*a* Alma 31:5.

juu ya makanisa kwamba kukatokea [a]mfarakano miongoni mwao, na hawakusikiliza maneno ya Helamani na ndugu zake;

24 Bali walianza kuwa na kiburi, wakijiinua kwa mioyo yao, kwa sababu ya [a]utajiri wao mwingi; kwa hivyo walikuwa matajiri kwenye fikira [b]zao, na hawakusikiliza maneno yao, kutembea wima mbele ya Mungu.

MLANGO WA 46

Amalikia anakula njama kuwa mfalme—Moroni anainua bendera ya uhuru—Anaunganisha watu kulinda dini yao—Waumini wa kweli wanaitwa Wakristo—Baki la Yusufu litahifadhiwa—Amalikia na wakaidi wanatorokea nchi ya Nefi—Wale ambao hawataunga kusudi la uhuru mkono wanauawa. Karibia mwaka 73–72 K.K.

Na ikawa kwamba kadiri wengi ambao hawangesikiza maneno ya Helamani na ndugu zake walikusanywa pamoja dhidi ya ndugu zao.

2 Na sasa tazama, walikasirika sana, hata kwamba waliamua kuwaua.

3 Sasa kiongozi wa wale ambao walikasirika dhidi ya ndugu zao alikuwa mtu mkubwa na mwenye nguvu; na jina lake lilikuwa Amalikia.

4 Na Amalikia alitamani kuwa mfalme; na wale watu waliokasirika walitamani kwamba awe mfalme wao; na walikuwa wengi baina yao [a]waamuzi wa vyeo vya chini katika nchi, na waliojitafutia ukubwa.

5 Na walikuwa wameongozwa na udanganyifu wa Amalikia, kwamba ikiwa watamuunga mkono na kumsimamisha kuwa mfalme wao kwamba angewafanya kuwa watawala juu ya watu.

6 Hivyo waliongozwa na Amalikia kwa mafarakano, ijapokuwa kuhubiri kwa Helamani na ndugu zake, ndiyo, ijapokuwa utunzaji wao mkuu juu ya kanisa, kwani walikuwa makuhani wakuu juu ya kanisa.

7 Na kulikuwa na wengi kanisani ambao waliamini maneno ya kusifu uongo ya Amalikia, kwa hivyo walikataa hata kanisa; na hivyo ndivyo mambo ya watu wa Nefi yalikuwa yenye shida nyingi na ya hatari, ijapokuwa [a]ushindi wao mkuu ambao walipata juu ya Walamani, na furaha yao kubwa ambayo walipata kwa sababu ya wokovu wao kupitia mkono wa Bwana.

8 Hivyo [a]tunaona vile watoto wa watu humsahau Bwana Mungu wao haraka, ndiyo, vile hutenda maovu haraka, na kupotoshwa na yule mwovu.

9 Ndiyo, na pia tunaona ule [a]uovu mwingi ambao mtu mmoja aliye mwovu anaweza kusababisha kufanyika miongoni mwa watoto wa watu.

10 Ndiyo, tunaona kwamba

23*a* 3 Ne. 11:28–29.
24*a* MWM Ukwasi.
b MWM Kiburi.

46 4*a* Mos. 29:11, 28–29.
7*a* Alma 44:19–20.
8*a* Hel. 12:2, 4–5.
9*a* Mos. 29:17–18.

Amalikia, kwa sababu alikuwa mtu mjanja na mtu wa maneno mengi ya kusifu ya uongo, kwamba aliongoza mioyo ya watu wengi kufanya maovu; ndiyo, na kutafuta kuangamiza kanisa la Mungu, na kuangamiza msingi wa [a]uhuru ambao Mungu alikuwa amewakabidhi, au baraka ambazo Mungu alituma katika ardhi kwa ajili ya wale walio [b]haki.

11 Na sasa ikawa kwamba wakati Moroni, ambaye alikuwa amiri jeshi [a]mkuu wa majeshi ya Wanefi, aliposikia mafarakano haya, alimkasirikia Amalikia.

12 Na ikawa kwamba alipasua koti lake; na akachukua kipande chake, na kuandika juu yake—[a]Kwa ukumbusho wa Mungu wetu, dini yetu, na uhuru, na amani yetu, wake zetu, na watoto wetu—na akaifunga juu ya mwisho wa mti.

13 Na akajifunga chapeo kwenye kichwa chake, na dirii yake, na ngao yake, na akajifunga silaha yake kiunoni mwake; na akaachukua ule mti, ambao mwisho wake kulikuwa koti lake lililoraruliwa, (na akaiita bendera ya uhuru) na akajinamisha chini, na akaomba sana kwa Mungu kuwa baraka ya uhuru iwe na ndugu zake, kadiri kundi la Wakristo libaki kumiliki nchi—

14 Kwani ndivyo waumini wa kweli wa Kristo, waliokuwa ndani ya kanisa la Mungu, walivyoitwa na wale ambao hawakuwa wafuasi wa kanisa.

15 Na wale ambao walikuwa wa kanisa walikuwa waaminifu; ndiyo, wale wote ambao waliokuwa waumini wa kweli katika Kristo walijichukulia, kwa furaha, [a]jina la Kristo, au [b]Wakristo vile waliitwa, kwa sababu ya imani yao katika Kristo ambaye angekuja.

16 Na kwa hivyo, kwa wakati huu, Moroni aliomba kwamba nia ya Wakristo, na uhuru wa nchi ungependelewa.

17 Na ikawa kwamba alipokuwa ametoa roho yake yote kwa Mungu, aliita nchi yote iliyo kusini mwa [a]Ukiwa, ndiyo, na kwa ufupi, nchi yote, kaskazini na kusini—Nchi iliyochaguliwa, na nchi ya uhuru.

18 Na akasema: Kwa kweli Mungu hawezi kukubali kwamba sisi, ambao tumedharauliwa kwa sababu tumejichukulia jina la Kristo, tutakanyagwa chini na kuangamizwa, mpaka tujiletee wenyewe maangamizi kwa makosa.

19 Na Moroni aliposema maneno haya, alienda mbele miongoni mwa watu, akipepeza [a]kipande cha vazi lake kilichoraruka hewani, ili wote waone maandishi ambayo aliandika kwenye sehemu iliyoraruka, na akipaza sauti, akisema:

20 Tazama, wowote watakaohifadhi hii bendera katika nchi,

10 *a* 2 Ne. 1:7; Mos. 29:32.
b 2 Ne. 1:7.
11 *a* Alma 43:16–17.
12 *a* Neh. 4:14; Alma 44:5.
15 *a* Mos. 5:7–9.
b Mdo. 11:26; 1 Pet. 4:16.
17 *a* Alma 22:30–31.
19 *a* MWM Bendera.

hebu waje mbele kwa uwezo wa Bwana, na kufanya agano kwamba watahifadhi haki yao, na dini yao, kwamba Bwana Mungu angewabariki.

21 Na ikawa kwamba wakati Moroni alipokuwa ametangaza maneno haya, tazama, watu walikuja wakikimbia pamoja na silaha zao zikiwa zimefungwa viunoni mwao, wakirarua nguo zao kama ishara, au kama agano, kwamba hawatamwacha Bwana Mungu wao; au, kwa maneno mengine, ikiwa wataasi amri za Mungu, au kuingia kwenye makosa, na [a]wapate aibu kujichukulia jina la Kristo, Bwana angewararua hata kama vile walivyorarua nguo zao.

22 Sasa hili ndilo agano ambalo walifanya, na walitupa nguo zao miguuni mwa Moroni, wakisema: Tunaagana na Mungu wetu, kwamba tutaangamizwa, hata kama vile ndugu zetu katika nchi ya kaskazini, ikiwa tutaingia kwenye makosa; ndiyo, atutupe miguuni mwa maadui zetu, hata vile tumetupa nguo zetu miguuni mwako zikanyagwe chini ya miguu, ikiwa tutaingia kwenye makosa.

23 Moroni akawaambia: Tazama, sisi ni baki la uzao wa Yakobo; ndiyo, ni baki la [a]uzao wa [b]Yusufu, ambaye [c]koti lake liliraruliwa na kaka zake kwa vipande vingi; na sasa tazama, hebu tukumbuke kutii amri za Mungu, au nguo zetu zitararuliwa na ndugu zetu, na tutupwe gerezani, au tuuzwe, au tuuawe.

24 Ndiyo, acha tuhifadhi uhuru wetu kama [a]baki la Yusufu; ndiyo, acha tukumbuke maneno ya Yakobo, kabla ya kifo chake, kwani tazama, aliona kwamba sehemu ya baki la koti la Yusufu ilihifadhiwa na haikuwa imeoza. Na akasema—Hata vile baki la nguo ya mwana wangu limehifadhiwa hata hivyo [b]baki la uzao wa mwana wangu lihifadhiwe kwa mkono wa Mungu, na lirudishwe kwake mwenyewe, wakati baki la uzao wa Yusufu itaangamia, hata vile baki la nguo yake ilikuwa.

25 Sasa tazama, hii inaipatia nafsi yangu huzuni; walakini, nafsi yangu ina shangwe katika mwana wangu, kwa sababu ya sehemu ya uzao wake ambayo itachukuliwa kwa Mungu.

26 Sasa tazama, hii ilikuwa lugha ya Yakobo.

27 Na sasa ni nani anaweza kujua kuwa baki la uzao wa Yusufu, ambalo litaangamia kama nguo yake, ni wale ambao wametukataa sisi? Ndiyo, na hata itakuwa sisi ikiwa hatuwezi kusimama imara katika imani ya Kristo.

28 Na sasa ikawa kwamba Moroni alipokuwa amesema maneno haya alienda mbele, na pia akatuma kwenye sehemu zote za nchi ambako kulikuwa na mafarakano, na akawakusanya

21 *a* 1 Ne. 8:25–28; Morm. 8:38.
23 *a* Mwa. 49:22–26; 1 Ne. 5:14–15.
b MWM Yusufu, Mwana wa Yakobo.
c Mwa. 37:3, 31–36.
24 *a* Amo. 5:15; 3 Ne. 5:21–24; 10:17.
b 2 Ne. 3:5–24; Eth. 13:6–7.

watu wote ambao walikuwa wanatamani kuhifadhi uhuru wao pamoja, kusimama dhidi ya Amalikia na wale waliokataa, ambao waliitwa Waamalikia.

29 Na ikawa kwamba wakati Amalikia alipoona kwamba watu wa Moroni walikuwa wengi kuliko Waamalikia—na alipoona pia kwamba watu wake walikuwa na wasiwasi kuhusu haki ya njia ambayo walikuwa wamechukua—kwa hivyo, akiogopa kwamba hatafaulu katika mambo yake, alichukua wale wa watu wake ambao wangekubali na wakaondoka na kwenda kwenye nchi ya Nefi.

30 Sasa Moroni alifikiri haikuwa vyema kwamba Walamani wapate nguvu nyingine; kwa hivyo alifikiri kuwazuia watu wa Amalikia, au kuwachukua na kuwarudisha, na amuue Amalikia; ndiyo, kwani alijua kwamba angewavuruga Walamani kukasirika dhidi yao, na kuwasababisha kuja kwa vita dhidi yao; na hivi alijua kwamba Amalikia angefanya ili apate kufikia lengo zake.

31 Kwa hivyo Moroni alifikiri ilikuwa ya lazima kwamba achukue majeshi yake, ambao walikuwa wamejikusanya wenyewe pamoja, na kujihami wenyewe, na kuingia kwenye agano kuweka amani—na ikawa kwamba alichukua jeshi lake na kwenda taratibu na hema zake kwenye nyika, kuzuia mwendo wa Amalikia nyikani.

32 Na ikawa kwamba alifanya kulingana na tamaa yake, na akaenda taratibu hadi kwenye nyika, na kuuzuia mwendo wa majeshi ya Amalikia.

33 Na ikawa kwamba Amalikia alikimbia na idadi ndogo ya watu wake, na waliosalia waliwekwa kwenye mikono ya Moroni na wakarudishwa katika nchi ya Zarahemla.

34 Sasa, Moroni akiwa ni mtu [a]aliyechaguliwa na waamuzi wakuu na kwa kura ya watu, kwa hivyo alikuwa na uwezo kulingana na hiari yake na majeshi ya Wanefi, kuanzisha na kuwa na uwezo juu yao.

35 Na ikawa kwamba yeyote wa Waamalikia ambaye alikataa kuingia katika agano kuunga mkono njia ya uhuru, kwamba wangehifadhi serikali huru, alisababisha auawe; na kulikuwa tu wachache waliokataa agano la amani.

36 Na ikawa pia, kwamba alisababisha bendera ya uhuru ipeperushwe kwenye kila mnara ambao ulikuwa kote nchini, ambayo ilimilikiwa na Wanefi; na hivyo Moroni alisimika bendera ya uhuru miongoni mwa Wanefi.

37 Na wakaanza kuwa na amani tena nchini; na hivyo wakadumisha amani nchini mpaka karibu mwisho wa mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi.

38 Na Helamani na [a]makuhani wakuu pia waliimarisha utaratibu ndani ya kanisa; ndiyo, hata kwa muda wa miaka

34*a* Alma 43:16.

38*a* Alma 46:6.

minne walikuwa na amani nyingi na furaha ndani ya kanisa.

39 Na ikawa kwamba kulikuwa na wengi waliokufa, [a]wakiamini kwa uthabiti kwamba nafsi zao zimekombolewa na Bwana Yesu Kristo; hivyo walitoka duniani wakishangilia.

40 Na kulikuwa na wengi ambao walifariki kwa homa, ambayo kwa misimu fulani mwakani ilikuweko mara kwa mara nchini—lakini sio kwa wingi hivyo na homa, kwa sababu ya ubora wa [a]mimea mingi na mizizi ambayo Mungu alikuwa ametayarisha kutoa mwanzo wa maradhi, ambayo binadamu walikuwa wakishikwa nayo kwa ajili ya hali ya hewa ya nchi—

41 Lakini kulikuwa na wengi waliokufa wakiwa wamezeeka; na wale waliokufa ndani ya imani ya Kristo wanayo [a]furaha ndani yake, vile lazima tuwaze.

MLANGO WA 47

Amalikia anatumia udanganyifu, mauaji, na hila ili awe mfalme wa Walamani—Wanefi walioasi ni waovu zaidi na wakatili kuliko Walamani. Karibia mwaka 72 K.K.

Sasa tutarudia kwenye historia yetu kwa Amalikia na wale ambao [a]walitoroka na yeye kwenda nyikani; kwani, tazama, alikuwa amechukua wale ambao walienda na yeye, na akaenda katika [b]nchi ya Nefi miongoni mwa Walamani, na akawachochea Walamani kuwa na hasira dhidi ya watu wa Nefi, hata kuwa mfalme wa Walamani akatoa tangazo kote nchini mwake, miongoni mwa watu wake wote, kuwa wajikusanye pamoja tena waanze vita dhidi ya Wanefi.

2 Na ikawa kwamba wakati tangazo lilipokuwa limetolewa miongoni mwao waliogopa sana; ndiyo, waliogopa kumkasirisha mfalme, na pia waliogopa kwenda vitani dhidi ya Wanefi wasije wakapoteza maisha yao. Na ikawa kwamba hawangeweza, au sehemu yao kubwa haingeweza, kutii amri ya mfalme.

3 Na ikawa kwamba mfalme alikasirika kwa sababu ya maasi yao; kwa hivyo alimpa Amalikia amri juu ya sehemu ya jeshi lake ambalo lilitii amri zake, na akamwamuru kwamba aende mbele na kuwalazimisha kuchukua silaha.

4 Sasa tazama, hii ndiyo ilikuwa nia ya Amalikia; kwani yeye alikuwa mtu mjanja kwa kufanya maovu kwa hivyo aliweka mpango ndani ya moyo wake kumwondoa mfalme wa Walamani.

5 Na sasa alikuwa amepata utawala wa yale makundi ya Walamani ambao walikuwa wanapendelea mfalme; na akatazamia kupendelewa na wale ambao hawakuwa watiifu; kwa hivyo alienda mbele kwenye mahali palipoitwa [a]Onida, kwani hapa Walamani

39 *a* Moro. 7:3, 41.
40 *a* M&M 89:10.
41 *a* Ufu. 14:13.

47 1 *a* Alma 46:33.
b 2 Ne. 5:5–8; Omni 1:12–13.
5 *a* Alma 32:4.

wote walikuwa wamekimbilia; kwani waligundua jeshi likija, na wakidhani kwamba lilikuwa linakuja kuwaangamiza, kwa hivyo walikimbilia Onida, mahali pa silaha.

6 Na walikuwa wamemchagua mtu kuwa mfalme na kiongozi juu yao, wakiwa wamekata kauli kuwa hawatakwenda dhidi ya Wanefi.

7 Na ikawa kwamba walikuwa wamejikusanya pamoja juu ya kilele cha mlima ambao uliitwa Antipa, wakijiandaa kupigana.

8 Sasa halikuwa kusudi la Amalikia kupigana nao kulingana na amri ya mfalme; lakini tazama, lilikuwa kusudi lake kupata mapendeleo kutoka kwa majeshi ya Walamani, ili ajiweke mwenyewe juu yao na kumwondoa mfalme na kumiliki ufalme.

9 Na tazama, ikawa kwamba alisababisha jeshi lake kusimamisha hema zao kwenye bonde ambalo lilikuwa karibu na mlima Antipa.

10 Na ikawa kwamba wakati usiku ulipowadia alituma wajumbe wa siri kwenye mlima Antipa, akitaka kwamba kiongozi wa wale ambao walikuwa mlimani, ambaye jina lake lilikuwa Lehonti, kwamba aje chini ya mlima, kwani alitaka kuongea na yeye.

11 Na ikawa kwamba wakati Lehonti alipopata ujumbe hakuthubutu kwenda chini ya mlima. Na ikawa kwamba Amalikia akatuma tena mara ya pili, akitaka yeye aje chini. Na ikawa kwamba Lehonti hangeenda; na akatuma tena mara ya tatu.

12 Na ikawa kwamba wakati Amalikia alipogundua kwamba hangempata Lehonti aje chini kutoka mlimani, alipanda mlima, karibu na kambi ya Lehonti; na akatuma tena mara ya nne ujumbe wake kwa Lehonti, akitaka kwamba aje chini, na kwamba angeleta walinzi wake pamoja na yeye.

13 Na ikawa kwamba wakati Lehonti alipokuja chini na walinzi kwa Amalikia, kwamba Amalikia alitaka yeye aje chini na jeshi lake wakati wa usiku, na azingire wale watu kwenye kambi yao ambao mfalme alimpatia kuongoza, na kwamba angewasalimisha mikononi mwa Lehonti, ikiwa angemfanya (Amalikia) kiongozi wa pili juu ya jeshi lote.

14 Na ikawa kwamba Lehonti aliteremka chini na watu wake na kuwazingira watu wa Amalikia, kwamba kabla ya hao kuamka kukipambazuka walikuwa wamezingirwa na majeshi ya Lehonti.

15 Na ikawa kwamba walipoona kwamba wamezungukwa, walimwomba Amalikia kwamba awakubalie wawe pamoja na ndugu zao, ili wasiangamizwe. Sasa hiki ndicho kitu ambacho Amalikia alitaka.

16 Na ikawa kwamba aliwasalimisha watu wake, [a]kinyume cha amri ya mfalme. Sasa hiki

16*a* Alma 47:3.

ndicho Amalikia alitaka, kwamba atimize mipango yake ya kumwondoa mfalme.

17 Sasa ilikuwa desturi miongoni mwa Walamani, ikiwa kiongozi wao mkuu aliuawa, kumchagua kiongozi wao wa pili kuwa kiongozi mkuu.

18 Na ikawa kwamba Amalikia alisababisha mmoja wa watumishi wake aweke sumu kidogo kidogo kwa Lehonti, kwamba alikufa.

19 Sasa, Lehonti alipokufa, Walamani walimchagua Amalikia kuwa kiongozi wao na amiri jeshi mkuu.

20 Na ikawa kwamba Amalikia alitembea taratibu na majeshi yake (kwani alikuwa amefaulu yale aliyoyataka) hadi kwenye nchi ya Nefi, kwenye mji wa Nefi, ambao ulikuwa mji mkuu.

21 Na mfalme akaja nje kukutana na yeye pamoja na walinzi wake, kwani alidhani kwamba Amalikia ametimiza amri zake, na kwamba Amalikia alikuwa amekusanya pamoja jeshi kubwa hivyo kwenda dhidi ya Wanefi vitani.

22 Lakini tazama, vile mfalme alipokuja nje kukutana na yeye Amalikia alisababisha kwamba watumishi wake waende na kumpokea mfalme. Na wakaenda na kujiinamisha mbele ya mfalme, kama kumwonyesha heshima kwa sababu ya ukuu wake.

23 Na ikawa kwamba mfalme aliinua mkono wake juu kuwasimamisha, vile ilivyokuwa desturi ya Walamani, kama ishara ya amani, desturi ambayo waliiga kutoka kwa Wanefi.

24 Na ikawa kwamba wakati alipokuwa amemwinua wa kwanza kutoka ardhini, tazama alimdunga mfalme moyoni; na akaanguka ardhini.

25 Sasa watumishi wa mfalme walitoroka, na watumishi wa Amalikia wakapiga nduru, wakisema:

26 Tazama, watumishi wa mfalme wamemdunga moyoni, na ameanguka na wametoroka; tazama, njooni muone.

27 Na ikawa kwamba Amalikia aliamrisha majeshi yake yaende mbele na kuona kile kilichotendeka kwa mfalme; na walipofika mahali hapo, na kumpata mfalme amelala katika damu yake, Amalikia alijifanya kukasirika, na kusema: Yeyote aliyempenda mfalme ebu aende mbele, na kuwafuata watumishi wa mfalme ili wauawe.

28 Na ikawa kwamba wale wote waliompenda mfalme, waliposikia maneno haya, walikuja mbele na kuwafukuza watumishi wa mfalme.

29 Sasa watumishi wa mfalme walipoona jeshi likiwafukuza, waliogopa tena, na wakatorokea nyikani, na wakafikia nchi ya Zarahemla na kuungana na “watu wa Amoni.

30 Na jeshi ambalo lilikuwa likiwafukuza lilirudi, wakiwa wamewafukuza bila kufaulu; na hivyo Amalikia, kwa hila yake, alipata imani ya watu.

31 Na ikawa kesho yake

29*a* Alma 43:11–12.

MWM Waanti-Nefi-Lehi.

akaingia kwenye mji wa Nefi na majeshi yake, na kumiliki mji.

32 Na sasa ikawa kwamba malkia, aliposikia kwamba mfalme ameuawa—kwani Amalikia alikuwa ametuma ujumbe kwa malkia kumjulisha kwamba mfalme ameuawa na watumishi wake, kwamba aliwafukuza na jeshi lake, lakini haikuwezekana, na wakatoroka—

33 Kwa hivyo, wakati malkia alipokuwa amepokea taarifa hii alituma taarifa kwa Amalikia, akimtaka kwamba aachilie watu wa mji; na akataka aende kwake; na akahitaji kwamba aje na mashahidi kushuhudia kuhusu kifo cha mfalme.

34 Na ikawa kwamba Amalikia alimchukua yule mtumishi ambaye alimuua mfalme, na wote waliokuwa na yeye, na kumwendea malkia, mahali ambapo aliketi; na wote walishuhudia kwake kwamba mfalme aliuawa na watumishi wake mwenyewe, na pia wakasema: Wametoroka; si hii inashuhudia dhidi yao? Na hivyo walimridhisha malkia kuhusu kifo cha mfalme.

35 Na ikawa kwamba Amalikia akatafuta upendeleo ya malkia, na akamwoa kuwa mkewe; na hivyo kwa hila yake, na kwa usaidizi wa watumishi wake werevu, alipata ufalme; ndiyo, alitambuliwa mfalme kote nchini, miongoni mwa watu wa Walamani, ambao walikuwa [a]mkusanyiko wa Walamani na Walemueli na Waishmaeli, na wote waliokimbia kutoka kwa Wanefi, tangu utawala wa Nefi hadi wakati huu.

36 Sasa hawa [a]wakimbiaji, wakiwa na mafundisho sawa na elimu sawa ya Wanefi, ndiyo, wakiwa wamefundishwa kwa [b]elimu ya Bwana, walakini, ni vigumu kusimulia, sio wakati mrefu baada ya mafarakano yao walikuwa wagumu na [c]wasiotubu, na mazuzu, waovu na wakatili kuliko Walamani—wakikubali desturi za Walamani; wakijiingiza kwenye uzembe, na kila aina ya uzinifu; ndiyo, wakimsahau kabisa Bwana Mungu wao.

MLANGO WA 48

Amalikia anachochea Walamani dhidi ya Wanefi—Moroni anawatayarisha watu wake kulinda imani ya Wakristo—Anafurahia uungwana na uhuru na ni mtu mkuu wa Mungu. Karibia mwaka 72 K.K.

Na sasa ikawa kwamba, Amalikia alipopokea utawala alianza kuvuta mioyo ya Walamani dhidi ya watu wa Nefi; ndiyo, alichagua watu kuzungumzia Walamani kutoka kwa minara yao, dhidi ya Wanefi.

2 Na hivyo akavuta mioyo yao dhidi ya Wanefi, kwa wingi kwamba katika mwisho wa mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi, akiwa ametimiza mipango yake hivyo,

35*a* Yak. (KM) 1:13–14.
36*a* MWM Ukengeufu.
b Ebr. 10:26–27; Alma 24:30.
c Yer. 8:12.

ndiyo, akishafanywa mfalme juu ya Walamani, alifikiria pia kutawala nchi yote, ndiyo, na watu wote waliokuwa nchini, Wanefi na pia Walamani.

3 Kwa hivyo alikuwa ametimiza kusudi lake, kwani alikuwa ameshupaza mioyo ya Walamani na akawapofusha akilini, na kuwachochea kuwa na hasira, kwa wingi kwamba waende vitani dhidi ya Wanefi.

4 Kwani alikuwa ameamua, kwa sababu ya wingi wa watu wake, kuwashinda Wanefi na kuwaweka kifungoni.

5 Na hivyo aliweka makapteni [a]wakuu wa Wazoramu, hawa wakiwa wamezoea nguvu za Wanefi, na mahali pao pa kawaida, na sehemu dhaifu za miji yao; kwa hivyo aliwaweka kuwa makapteni wakuu wa majeshi yake.

6 Na ikawa kwamba walichukua kambi yao, na kusonga mbele kuelekea nchi ya Zarahemla katika nyika.

7 Sasa ikawa kwamba wakati Amalikia alikuwa anapokea uwezo kwa hila na udanganyifu, Moroni, kwa upande mwingine, alikuwa [a]anatayarisha akili za watu kwa uaminifu kwa Bwana Mungu wao.

8 Ndiyo, alikuwa akiimarisha majeshi ya Wanefi, na kujenga ngome ndogo, au mahali pa usalama; akitupa kuta za ardhi karibu kufunika majeshi yake, na pia kujenga kuta za mawe kuwazunguka, kuzingira miji yao na mipaka ya nchi yao; ndiyo, kila mahali nchini.

9 Na kwa udhaifu wao aliweka idadi kubwa zaidi ya watu; na hivyo aliweka nguvu na kuimarisha nchi ambayo ilimilikiwa na Wanefi.

10 Na hivyo alikuwa akijitayarisha [a]kulinda uhuru wao, nchi yao, wake zao, na watoto wao, na amani yao, na kwamba wangeishi kwa Bwana Mungu wao, na kwamba wangeshikilia ile ambayo iliitwa na maadui wao imani ya Wakristo.

11 Na Moroni alikuwa mtu mwenye nguvu na uwezo; na alikuwa mtu wa [a]kuelewa kikamilifu; ndiyo, mtu ambaye hakufurahia umwagaji wa damu; mtu ambaye nafsi yake ilijawa shangwe kwa ajili ya uungwana na uhuru wa nchi yake, na wa ndugu zake kutoka kifungo na utumwa;

12 Ndiyo, mtu ambaye moyo wake ulijaa shukrani kwa Mungu wake, kwa maendeleo mengi na baraka ambazo aliwapa watu wake; mtu ambaye alifanya kazi sana kwa [a]ustawi na usalama wa watu wake.

13 Ndiyo, na alikuwa mtu ambaye alikuwa imara katika imani ya Kristo, na [a]aliapa na kiapo kuwa atawalinda watu wake, haki zake, na nchi yake, na dini yake, hata kwenye kumwaga damu yake.

14 Sasa Wanefi walifundishwa vile wanavyoweza kujilinda wenyewe dhidi ya maadui zao, hata kwenye kumwaga damu

48 5*a* Alma 43:6.
7*a* Alma 49:8.
10*a* Alma 46:12–13.
11*a* MWM Ufahamu.
12*a* MWM Ustawi.
13*a* Alma 46:20–22.

ikiwa ilihitajika; ndiyo, na walifundishwa [a]kutodhuru, ndiyo, na kutoinua upanga isipokuwa dhidi ya adui, isipokuwa wawe wanahifadhi maisha yao.

15 Na hii ilikuwa imani yao, kwamba kwa kufanya hivyo Mungu angewafanikisha nchini, au kwa maneno mengine, wakiwa waaminifu kwa kutii amri za Mungu kwamba angewafanikisha katika nchi; ndiyo, kuwaonya watoroke, au kuwaandaa kwa vita, kulingana na hatari iliyopo;

16 Na pia, kwamba Mungu angewawezesha kujua wangeenda wapi kujilinda dhidi ya maadui zao, na kwa kufanya hivyo, Bwana angewaokoa; na hii ilikuwa imani ya Moroni, na moyo wake ulifurahi ndani yake; [a]sio kwa kumwaga damu lakini kwa kutenda mema, kwa kuhifadhi watu wake, ndiyo, kwa kutii amri za Mungu, na kuzuia uovu.

17 Ndiyo, kweli, kweli ninavyowaambia, ikiwa watu wote walikuwa, na wako, na ikiwa watakuweko daima, kama Moroni, tazama, hizo nguvu za jehanamu zingetingizika milele; ndiyo, [a]ibilisi hangekuwa na uwezo juu ya mioyo ya watoto wa watu.

18 Tazama, alikuwa mtu kama Amoni, mwana wa Mosia, ndiyo, na hata wana wengine wa Mosia, ndiyo, na pia Alma na wanawe, kwani walikuwa wote watu wa Mungu.

19 Sasa tazama, Helamani na ndugu zake hawakufanya kazi ndogo kwa watu kuliko Moroni; kwani walihubiri neno la Mungu, na walibatiza ubatizo wa toba watu wote ambao wangesikiliza maneno yao.

20 Na hivyo wakaendelea na watu [a]walijinyenyekeza kwa sababu ya maneno yao, kwamba [b]walipendelewa sana na Bwana, na hivyo wakawa huru kutokana na vita na mabishano miongoni mwao, ndiyo, hata kwa muda wa miaka minne.

21 Lakini, vile nimesema, kwenye mwisho wa mwaka wa kumi na tisa, ndiyo, ijapokuwa amani yao miongoni mwao, walilazimishwa bila kupenda kupigana na wenzao, Walamani.

22 Ndiyo, kwa kifupi, vita vyao havikukoma kamwe kwa muda wa miaka mingi na Walamani, ijapokuwa kutopendelea kwao.

23 Sasa, [a]walihuzunika kuchukua silaha dhidi ya Walamani, kwa sababu hawakupendelea umwagaji wa damu; ndiyo, na hii sio yote—walihuzunika kuwa njia ya kuondoa wengi wa ndugu zao nje ya ulimwengu huu hadi kwenye ulimwengu wa milele, kabla ya kujitayarisha kukutana na Mungu wao.

24 Walakini, hawangekubali kuweka chini maisha yao, kwamba [a]wake zao na watoto wao wachinjwe kuuwawa kinyama

14*a* Alma 43:46–47; 3 Ne. 3:20–21; Morm. 3:10–11; M&M 98:16.

16*a* Alma 55:19.

17*a* 1 Ne. 22:26; 3 Ne. 6:15.

20*a* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
b 1 Ne. 17:35.

23*a* M&M 42:45.

24*a* Alma 46:12.

kwa ukatili na ujeuri wa wale ambao walikuwa siku moja ndugu zao, ndiyo, na [b]walioasi kutoka kanisa lao, na waliwaacha na kujaribu kuwaangamiza kwa kuungana na Walamani.

25 Ndiyo, hawangevumilia kwamba ndugu zao wafurahi juu ya damu ya Wanefi, mradi kuwe na yeyote atakayetii amri za Mungu, kwani ahadi ya Bwana ilikuwa, kama watatii amri zake watafanikiwa nchini.

MLANGO WA 49

Walamani walioshambulia wanashindwa kuchukua miji ya Amoniha na Nuhu zilizoimarishwa—Amalikia anamlaani Mungu na kuapa kunywa damu ya Moroni—Helamani na ndugu zake wanaendelea kuimarisha Kanisa. Karibia mwaka 72 K.K.

Na sasa ikawa katika mwezi wa kumi na moja wa mwaka wa kumi na tisa, siku ya kumi ya mwezi, majeshi ya Walamani yalionekana yakikaribia kuelekea nchi ya Amoniha.

2 Na tazama, mji ulikuwa umejengwa upya, na Moroni alikuwa ameweka jeshi karibu na mipaka ya mji, na walikuwa wametupa udongo kuzunguka kuwakinga kutokana na mishale na mawe ya Walamani; kwani tazama, walipigana kwa mawe na mishale.

3 Tazama, nilisema kwamba mji wa [a]Amoniha ulikuwa umejengwa upya. Nakwambia, ndiyo, ilikuwa sehemu moja imejengwa upya; na kwa sababu Walamani walikuwa wameuharibu wakati mmoja kwa sababu ya uovu wa watu, walidhani kwamba ingekuwa tena mawindo rahisi kwao.

4 Lakini tazama, jinsi masikitiko ya yalivyo kuwa makubwa; kwani tazama, Wanefi walikuwa wamechimba tuta la ardhi kuwazunguka, ambalo lilikuwa refu sana kwamba Walamani hawangetupa mawe yao na mishale yao kwao kwamba ingefanya chochote, wala hawangewafikia isipokuwa wapitie kwenye lango lao la kupitia.

5 Sasa kwa wakati huu makapteni wakuu wa Walamani walishtushwa sana, kwa sababu ya hekima ya Wanefi kwa kutayarisha mahali pao pa ulinzi.

6 Sasa viongozi wa Walamani walikuwa wamedhani, kwa sababu ya wingi wa idadi yao, ndiyo, walidhani kwamba wangenufaika kuwashambulia vile walikuwa wamefanya awali; ndiyo, na walikuwa pia wamejitayarisha kwa ngao, na dirii; na walikuwa pia wamejitayarisha na nguo za ngozi, ndiyo, nguo nzito sana kwa kufunika uchi wao.

7 Na wakiwa wamejitayarisha hivyo walidhani kwamba wangeshinda kwa urahisi na kuwaweka ndugu zao katika nira ya utumwa, au kuwakata na kuwachinja kulingana na furaha yao.

8 Lakini tazama, kwa mshangao wao mkuu, walikuwa

24*b* MWM Ukengeufu.

49 3*a* Alma 16:2–3, 9, 11.

[a]wamejitayarisha kwa ajili yao, kwa njia ambayo haijajulikana miongoni mwa watoto wa Lehi. Sasa walikuwa wamejiandaa kwa ajili ya Walamani, kupigana wakifuata njia ya mafundisho ya Moroni.

9 Na ikawa kwamba Walamani, au Waamalikia, walistaajabu sana katika namna yao ya matayarisho ya vita.

10 Sasa, kama mfalme Amalikia angekuja chini kutoka [a]nchi ya Nefi, mbele ya jeshi lake, labda angesababisha Walamani kuwashambulia Wanefi katika mji wa Amoniha; kwani tazama, hakujali damu ya watu wake.

11 Lakini tazama, Amalikia hakuja chini mwenyewe kupigana. Na tazama, makapteni wake wakuu hawakuwashambulia Wanefi katika mji wa Amoniha, kwani Moroni alikuwa amebadilisha shughuli ya usimamizi miongoni mwa Wanefi, hata kuwa Walamani hawakupendezwa katika mahali pao pa kurudi nyuma na hawangewajia.

12 Kwa hivyo walirudi nyuma hadi kwenye nyika, na kuchukua kambi yao na wakaenda taratibu kuelekea nchi ya Nuhu, wakidhani kuwa pale ni pahali pazuri kwao kuja dhidi ya Wanefi.

13 Kwani hawakujua kwamba Moroni alikuwa amezuia, au alikuwa amejenga [a]ngome za ulinzi, kwa kila mji nchini kote kuzunguka; kwa hivyo, walitembea mbele taratibu hadi nchi ya Nuhu kwa juhudi imara; ndiyo, makapteni wao wakuu walikuja mbele na kula kiapo kwamba wataangamiza watu wa mji huo.

14 Lakini tazama, kwa mshangao wao, mji wa Nuhu, ambao hapo awali ulikuwa dhaifu, ulikuwa sasa, kwa juhudi za Moroni, kuwa wenye nguvu, ndiyo, hata kushinda nguvu ya mji wa Amoniha.

15 Na sasa, tazama, hii ilikuwa hekima ndani ya Moroni; kwani alidhani kwamba wangeogopa katika mji wa Amoniha; na vile mji wa Nuhu ulikuwa mpaka sasa sehemu dhaifu katika nchi, kwa hivyo wangeenda hapo kupigana; na hivyo ilikuwa kulingana na tamaa zake.

16 Na tazama, Moroni alikuwa amemweka Lehi kuwa kapteni mkuu juu ya watu wa mji huo; na alikuwa ni [a]huyo Lehi ambaye alipigana na Walamani kwenye bonde la mashariki mwa mto Sidoni.

17 Na sasa tazama ikawa kwamba wakati Walamani walipogundua kwamba Lehi alikuwa amiri jeshi wa mji, hawakupendezwa kwani walimwogopa Lehi sana; walakini makapteni wao wakuu walikuwa wameapa na kiapo kuushambulia mji; kwa hivyo, walileta majeshi yao.

18 Sasa tazama, Walamani hawangeingia katika ngome zao za ulinzi kwa njia ingine yoyote isipokuwa kwenye lango, kwa sababu ya urefu wa ukingo

8*a* Alma 48:7–10.
10*a* 2 Ne. 5:8; Omni 1:12; Alma 47:1.
13*a* Alma 48:8.
16*a* Alma 43:35.

ambao ulikuwa umejengwa, na urefu wa kwenda chini wa handaki ambalo lilikuwa limelimbwa kuzunguka hapo, isipokuwa tu kupitia kwenye lango.

19 Na hivyo Wanefi walijiandaa kuangamiza jaribio kama hilo la kupanda juu na kuingia ndani ya ngome kwa njia ingine yoyote, kwa kurusha mawe na mishale kwao.

20 Hivyo walijiandaa, ndiyo, kundi la watu wao wenye nguvu, na mapanga yao na kombeo zao, kuwauwa wote ambao wangejaribu kuja kwenye mahali pao pa ulinzi kupitia mahali pa mlango; na hivyo ndivyo walivyojiandaa kujilinda dhidi ya Walamani.

21 Na ikawa kwamba makapteni wa Walamani walileta majeshi yao mbele ya mahali pa kuingilia, na wakaanza kushambuliana na Wanefi, kuingia ndani ya mahali pao pa ulinzi; lakini tazama, waliwafukuza kila wakati kwa wingi, kwamba walichinjwa kwa uchinjaji mkuu.

22 Sasa wakati walipogundua ya kwamba hawangepata uwezo juu ya Wanefi kupitia mlangoni, walianza kuchimba chini kingo zao ili wapate njia ya kufikia majeshi yao, kwamba wapate nafasi sawa kupigana; lakini tazama, kwa haya majaribio walifagiliwa mbali kwa mawe na mishale ambayo walitupiwa; na badala ya kujaza mitaro yao kwa kubomoa kingo za mchanga, zilijazwa kwa kiwango na wafu wao na miili iliyojeruhiwa.

23 Hivyo Wanefi walikuwa na uwezo wote juu ya maadui wao; na hivyo Walamani walijaribu kuwaangamiza Wanefi mpaka makapteni wao wakuu wote wakauawa; ndiyo, na zaidi ya elfu moja ya Walamani waliuawa; wakati, kwa upande mwingine, hakukuwa hata na nafsi moja ya Wanefi ambayo iliuawa.

24 Kulikuwa na karibu hamsini ambao walijeruhiwa, ambao walikuwa wazi kwa mishale ya Walamani kupitia mlangoni, lakini walijikinga na ngao zao, na dirii zao, na vyapeo vyao, hata kwamba vidonda vyao vilikuwa kwa miguu yao, vingi ambavyo vilikuwa vibaya sana.

25 Na ikawa kwamba wakati Walamani walipoona kwamba makapteni wao wakuu wote wameuawa walikimbilia nyikani. Na ikawa kwamba walirejea kwa nchi ya Nefi, kumjulisha mfalme wao, Amalikia, ambaye alikuwa Mnefi kwa kuzaliwa, kuhusu hasara yao kubwa.

26 Na ikawa kwamba alikasirika sana na watu wake, kwa sababu hakuwa amepata matarajio yake juu ya Wanefi; hakuwa amewaweka kwa nira ya utumwa.

27 Ndiyo, alikasirika sana, na [a]akamlaani Mungu, na pia Moroni, akiapa kwa [b]kiapo kuwa atakunywa damu yake; na hii ni kwa sababu Moroni alikuwa ametii amri za Mungu kwa

27 *a* MWM Kukufuru, Kufuru. *b* Mdo. 23:12.

kutayarisha usalama wa watu wake.

28 Na ikawa kwamba kwa upande mwingine, watu wa Nefi [a]walimshukuru Bwana Mungu, kwa sababu ya nguvu yake isiyo na kifani kwa kuwakomboa kutoka mikono ya maadui zao.

29 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

30 Ndiyo, na kulikuwa na amani mfululizo miongoni mwao, na mafanikio makuu katika kanisa kwa sababu ya kusikiliza kwao na bidii ambayo walitoa kwa neno la Mungu, ambalo lilitangazwa kwao na Helamani, na Shibloni, na Koriantoni, na Amoni na ndugu zake, ndiyo, na wote ambao walikuwa wametawazwa kufuatana na [a]mpango mtakatifu wa Mungu, wakibatizwa ubatizo wa toba, na kutumwa mbele kuhubiri miongoni mwa watu.

MLANGO WA 50

Moroni anaimarisha nchi za Wanefi—Wanajenga miji mingi mipya—Vita na maangamizo yaliwaangukia Wanefi katika siku za uovu na machukizo—Moriantoni na makaidi wake wanashindwa na Teankumu—Nefiha anafariki, na mwana wake Pahorani anakalia kiti cha hukumu. Karibia mwaka 72–67 K.K.

Na sasa ikawa kwamba Moroni hakuacha kujitayarisha kwa vita, au kulinda watu wake dhidi ya Walamani; kwani alisababisha kwamba majeshi yake yaanze katika mwanzo wa mwaka wa ishirini wa utawala wa waamuzi, kwamba waanze kulima vilima vya udongo kuzunguka miji yote, kote katika nchi ambayo ilimilikiwa na Wanefi.

2 Na juu ya haya magongo ya ardhi alisababisha kwamba kuwe na mbao, ndiyo, kazi za mbao zijengwe kwa urefu wa mtu, kuzunguka miji.

3 Na akasababisha kwamba juu ya kazi hizo za mbao kuwe na ufito wa miiba ujengewe kwenye mbao kuzunguka; na zilikuwa nzito na ndefu.

4 Na akasabisha minara kujengwa ambayo iliangalia zile kuta za walinzi, na akasababisha mahali pa ulinzi kujengwa kwenye hiyo minara, ili mawe na mishale ya Walamani haingewaumiza.

5 Na walikuwa wamejitayarisha ili waweze kutupa mawe kutoka juu, kulingana na nia yao na nguvu yao, na kumuua yeyote ambaye angejaribu kuja karibu na kuta za mji.

6 Hivyo Moroni aliandaa ngome dhidi ya kuja kwa maadui wao, kuzunguka kila mji nchini.

7 Na ikawa kwamba Moroni alisababisha kwamba majeshi yake yaende mbele kwenye mashariki ya nyika; ndiyo, na wakaenda mbele na kuwakimbiza Walamani wote waliokuwa ndani ya nyika ya mashariki hadi kwenye nchi zao, ambazo

28*a* MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
30*a* Alma 43:2.

zilikuwa kusini mwa nchi ya Zarahemla.

8 Na nchi ya Nefi ilienea katika mstari mnyoofu kutokea kwenye bahari ya mashariki hadi magharibi.

9 Na ikawa kwamba Moroni alipokuwa amewafukuza Walamani wote nje ya nyika ya mashariki, ambayo ilikuwa kaskazini mwa nchi za umiliki wao, alisababisha kwamba wakaazi ambao walikuwa kwenye nchi ya Zarahemla na nchi iliyoizunguka lazima waende mbele kwenye nyika ya mashariki, hata kwenye mipaka kando ya bahari, na kumiliki nchi.

10 Na pia akaweka majeshi kusini, katika mipaka ya umiliki wao, na akawasababisha wajenge ngome kwamba wangeweka salama majeshi yao na watu wao kutoka mikono ya maadui zao.

11 Na hivyo akaondoa ngome zote za Walamani kwenye mashariki ya nyika, ndiyo, na pia kwenye magharibi, akiimarisha mpaka miongoni mwa Wanefi na Walamani, kati ya nchi ya Zarahemla na nchi ya Nefi, kutoka magharibi mwa bahari, kuenea kando ya mwanzo wa mto Sidoni—Wanefi wakimiliki nchi yote upande wa kaskazini, ndiyo, hata nchi yote ambayo ilikuwa upande wa kaskazini ya nchi ya Neema, kulingana na kupenda kwao.

12 Hivyo Moroni, na majeshi yake, ambayo yaliongezeka kila siku kwa sababu ya kuhakikishiwa na ulinzi ambao kazi yake iliwaletea, walitaka kutoa nguvu na uwezo wa Walamani kutoka nchi zao za umiliki, ili wasiwe na uwezo juu ya nchi zao za umiliki.

13 Na ikawa kwamba Wanefi walianza msingi wa mji, na wakaita jina la mji Moroni; na ulikuwa kando ya bahari ya mashariki; na ulikuwa kusini kando ya mpaka wa umiliki wa Walamani.

14 Na pia walianza msingi wa mji kati ya mji wa Moroni na mji wa Haruni, ukiungana na mipaka ya Haruni na Moroni; na wakaita jina la mji, au nchi, Nefiha.

15 Na pia wakaanza kujenga katika mwaka huo huo miji mingi kaskazini, mmoja kwenye njia fulani ambao waliuita Lehi, ambao ulikuwa kaskazini kando na mipaka ya ukingo wa bahari.

16 Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini.

17 Na kwa hii hali ya kufanikiwa waliishi watu wa Nefi katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na moja wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

18 Na walifanikiwa sana, na wakawa matajiri sana; ndiyo, na wakaongezeka na wakawa na nguvu nchini.

19 Na hivyo tunaona jinsi gani hekima na haki ni matendo yote ya Bwana, kwa kutimiza maneno yake yote kwa watoto wa watu; ndiyo, tunaweza kuona kuwa maneno yake yanathibitishwa, hata wakati huu, ambayo alimzungumzia Lehi akisema:

50 10*a* Alma 49:18–22.

20 Umebarikiwa wewe na watoto wako; na watabarikiwa ikiwa watatii amri zangu watafanikiwa nchini. Lakini kumbuka, ikiwa hawatatii amri zangu [a]watatolewa mbali kutoka uwepo wa Bwana.

21 Na tunaona kwamba ahadi hizi zimetimizwa kwa watu wa Nefi; kwani imekuwa ugomvi wao na mabishano yao, ndiyo, mauaji yao, na uporaji wao, ukafiri wao, ukahaba wao, na unyang'anyi wao, na machukizo yao, ambayo yalikuwa miongoni mwao, ambayo yalisababisha vita vyao na maangamizo yao.

22 Na wale ambao walikuwa waaminifu kwa kutii amri za Bwana walikombolewa wakati wote, wakati maelfu ya ndugu zao waovu wameachwa kwenye kifungo, au kuangamia kwa upanga, au kufifia kwa kutoamini, na kuingiliana na Walamani.

23 Lakini tazama hakujakuwa wakati wa [a]furaha miongoni mwa watu wa Nefi, tangu siku za Nefi, kuliko siku za Moroni, ndiyo, hata wakati huu, katika mwaka wa ishirini na moja wa utawala wa waamuzi.

24 Na ikawa kwamba mwaka wa ishirini na mbili wa utawala wa waamuzi pia ukaisha kwa amani; ndiyo, na pia mwaka wa ishirini na tatu.

25 Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na nne wa utawala wa waamuzi, kungekuwa pia amani miongoni mwa watu wa Nefi kama hakungekuwa [a]ubishi ambao ulikuweko miongoni mwao kuhusu nchi ya Lehi, na nchi ya Moriantoni, ambazo ziliungana katika mipaka ya Lehi; zote mbili ambazo zilikuwa kwenye mipaka kando ya ukingo wa bahari.

26 Kwani tazama, watu ambao walimiliki nchi ya Moriantoni walidai sehemu ya nchi ya Lehi; kwa hivyo kulianza kuwa na ubishi mkali miongoni mwao, hata kwamba watu wa Moriantoni walichukua silaha dhidi ya ndugu zao, na walikata kauli kuwauwa kwa upanga.

27 Lakini tazama, watu ambao walimiliki nchi ya Lehi walikimbilia kambi ya Moroni, na kumuomba usaidizi; kwani tazama hawakuwa na makosa.

28 Na ikawa kwamba wakati watu wa Moriantoni, ambao waliongozwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa Moriantoni, waligundua kwamba watu wa Lehi walikuwa wamekimbilia kambi ya Moroni, waliogopa sana isiwe jeshi la Moroni lingekuja kwao na kuwaangamiza.

29 Kwa hivyo, Moriantoni alisadikisha mioyo yao kwamba wakimbilie nchi ambayo ilikuwa kaskazini, ambayo ilikuwa imefunikwa kwa miili mikubwa ya maji, na kumiliki nchi ambayo ilikuwa upande wa kaskazini.

30 Na tazama, wangetekeleza huu mpango kwa vitendo, (ambao ungekuwa mwanzo wa

20*a* M&M 1:14. | 23*a* Mos. 2:41. | 25*a* MWM Ushindani.

masikitiko) lakini tazama, Moriantoni akiwa mtu wa juhudi kuu ya roho, kwa hivyo alimkasirikia mmoja wa wafanya kazi wake wa kike, na akamwangukia na kumpiga sana.

31 Na ikawa kwamba alitoroka, na akafikia kambi ya Moroni, na kumwambia Moroni vitu vyote kuhusu mambo hayo, na pia kuhusu mipango yao ya kukimbilia nchi ya upande wa kaskazini.

32 Sasa tazama, watu ambao walikuwa katika nchi ya Neema, kwa usahihi zaidi Moroni, waliogopa kwamba wangesikia na kufuata maneno ya Moriantoni na kuungana na watu wake, na hivyo angepata urithi wa hizo sehemu za nchi, ambao ungeweka msingi wa matokeo mabaya miongoni mwa watu wa Nefi, ndiyo, matokeo ambayo yangekuwa chanzo cha kuongoza upinduzi wa [a]uhuru wao.

33 Kwa hivyo Moroni alituma jeshi, na kambi chao, kuongoza watu wa Moriantoni, kuwazuia kukimbilia nchi ya upande wa kaskazini.

34 Na ikawa kwamba hawakuwaongoza mpaka walipofikia mipaka ya nchi ya [a]Ukiwa; na huko waliwaongoza, kwa njia ndogo ambayo ilielekea kando ya bahari hadi kwenye nchi upande wa kaskazini, ndiyo, kando ya bahari, kwenye magharibi na kwenye mashariki.

35 Na ikawa kwamba jeshi ambalo lilitumwa na Moroni, ambalo liliongozwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa Teankumu, lilikutana na watu wa Moriantoni; na watu wa Moriantoni walikuwa wakaidi sana, (wakiwa wamevutiwa na uovu wake na maneno yake ya kusifu ya uongo) kwamba vita vilianza kati yao, ambamo Teankumu alimuua Moriantoni na kushinda jeshi lake, na kuwachukua wafungwa, na kurudi kwenye kambi ya Moroni. Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na nne wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

36 Na hivyo watu wa Moriantoni walirudishwa. Na baada ya maagano ya kuweka amani walirudishwa kwenye nchi ya Moriantoni, na muungano ukafanyika miongoni mwao na watu wa Lehi; na wao pia walirudishwa katika nchi yao.

37 Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo kwamba imani iliimarishwa kwa watu wa Nefi, kwamba Nefiha, mwamuzi mkuu wa pili, alifariki, akiwa amekalia kiti cha hukumu kwa haki kamili mbele ya Mungu.

38 Walakini alikuwa amemkataza Alma kuchukua hayo maandishi na vile vitu ambavyo viliheshimiwa na Alma na baba zake kuwa vitakatifu; kwa hivyo Alma alikuwa amevipatia kwa mwana wake, Helamani.

39 Tazama, ikawa kwamba mwana wa Nefiha aliwekwa kwenye kiti cha hukumu,

32*a* MWM Huru, Uhuru. | 34*a* Alma 46:17.

badala ya baba yake; ndiyo, aliteuliwa mwamuzi mkuu na msimamizi juu ya watu, kwa kiapo na agizo takatifu kuhukumu kwa haki, na kuweka amani na uhuru wa watu, na kuwapa mapendeleo matakatifu ya kumwabudu Bwana Mungu wao, ndiyo, kusaidia na kudumisha matendo ya Mungu siku zake zote, na kuwaleta waovu kwenye hukumu kulingana na makosa yao.

40 Sasa tazama, jina lake lilikuwa Pahorani. Na Pahorani alijaza kiti cha baba yake, na akaanza utawala wake katika mwisho wa mwaka wa ishirini na nne, juu ya watu wa Nefi.

MLANGO WA 51

Watu wa mfalme wanatazamia kugeuza sheria na kumchagua mfalme—Pahorani na watu wa uhuru wanaungwa mkono kwa sauti ya watu—Moroni analazimisha watu wa mfalme kulinda nchi yao au wauawe—Amalikia na Walamani wanatega miji mingi iliyoimarishwa—Teankumu anarudisha nyuma mwingilio wa Walamani na kumuua Amalikia katika hema lake. Karibia mwaka 67–66 K.K.

Na sasa ikawa katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na tano wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, hao wakiwa wameanzisha amani miongoni mwa watu wa Lehi na watu wa Moriantoni kuhusu nchi zao, na wakiwa wameanza mwaka wa ishirini na tano kwa amani;

2 Walakini, hawakudumisha amani kwa muda mrefu nchini, kwani kulianza kuwa na ubishi miongoni mwa watu kuhusu mwamuzi mkuu Pahorani; kwani tazama, kulikuwa na sehemu ya watu ambao walitaka kwamba sehemu fulani za sheria ibadilishwe.

3 Lakini tazama, Pahorani hakubadilisha wala kukubali sheria ibadilishwe; kwa hivyo, hakuwasikiliza wale ambao walikuwa wamepeleka mashauri na maombi kuhusu kubadilishwa kwa sheria.

4 Kwa hivyo, wale ambao walitamani kwamba sheria ibadilishwe walimkasirikia, na wakataka kwamba asiwe tena mwamuzi mkuu katika nchi; kwa hivyo kulitokea ugomvi mkali kuhusu jambo hili, lakini damu haikumwagwa.

5 Na ikawa kwamba wale ambao walitaka kwamba Pahorani aondolewe kutoka kiti cha hukumu walikuwa watu wa ufalme, kwani walihitaji kwamba sheria igeuzwe kwa njia ambayo ingeiondoa serikali huru na kuweka mfalme katika nchi.

6 Na wale ambao walitaka kwamba Pahorani abaki mwamuzi mkuu juu ya nchi walijiita watu huru; na hivyo ndivyo ulikuwa mgawanyiko miongoni mwao, kwani watu huru walikuwa wameapa au kutoa agano kulinda haki yao na heshima yao ya dini kwa serikali huru.

7 Na ikawa kwamba jambo hili lao la ubishi lilitulizwa kwa sauti ya watu. Na ikawa kwamba sauti ya watu ilipendelea

watu huru, na Pahorani akabaki kwenye kiti cha hukumu, ambayo ilisababisha furaha nyingi miongoni mwa ndugu za Pahorani na pia watu wengi waliotaka uhuru, ambao pia waliwanyamazisha watu wa mfalme, kwamba hawakupinga lakini walihitajika kulinda mwendo wa uhuru.

8 Sasa wale ambao walipendelea wafalme walikuwa wale ambao ni wa [a]cheo cha juu, na walitaka kuwa wafalme; na walisaidiwa na wale ambao walitaka nguvu na uwezo juu ya watu.

9 Lakini tazama, huu ulikuwa wakati wa hatari wa mabishano kuwa miongoni mwa watu wa Nefi; kwani tazama, Amalikia alikuwa amevuruga tena mioyo ya watu wa Walamani dhidi ya watu wa Wanefi, na alikuwa akikusanya pamoja askari kutoka kila sehemu ya nchi yake, na kuwahami kwa silaha, na kuwatayarisha kwa vita kwa bidii yake yote; kwani alikuwa [a]ameapa kunywa damu ya Moroni.

10 Lakini tazama, tutaona kwamba ahadi yake aliyofanya ilikuwa ni ya upumbavu; walakini, alijitayarisha na majeshi yake kupigana dhidi ya Wanefi.

11 Sasa majeshi yake hayakuwa mengi kama vile yalivyokuwa hapo awali, kwa sababu ya maelfu wengi ambao waliuawa kwa mikono ya Wanefi; lakini ijapokuwa kupotewa kwao kwingi, Amalikia alikuwa amekusanya jeshi kubwa la ajabu, hivyo kwamba hakuogopa kuja chini kwenye nchi ya Zarahemla.

12 Ndiyo, hata Amalikia alikuja chini mwenyewe, mbele ya Walamani. Na ilikuwa katika mwaka wa ishirini na tano wa utawala wa waamuzi; na ilikuwa wakati huo ambao walikuwa wameanza kutatua mambo ya mabishano yao kuhusu mwamuzi mkuu, Pahorani.

13 Na ikawa kwamba wakati watu ambao waliitwa watu wa mfalme walipokuwa wamesikia kwamba Walamani wanakuja kupigana dhidi yao, walifurahi ndani ya mioyo yao; na wakakataa kuchukua silaha, kwani walimkasirikia sana mwamuzi mkuu, na pia [a]watu wa uhuru, kwamba hawangechukua silaha kulinda nchi yao.

14 Na ikawa kwamba Moroni alipoona hivi, na pia kwamba Walamani walikuwa wanakaribia mipaka ya nchi, alikasirika sana kwa sababu ya ukaidi wa watu wale ambao alikuwa amefanyia kazi kwa bidii nyingi kuwalinda; ndiyo, alikasirika sana; nafsi yake ilijaa hasira dhidi yao.

15 Na ikawa kwamba alituma ombi, na sauti ya watu, kwa msimamizi wa nchi, akitaka kwamba alisome, na kumpatia (Moroni) uwezo kulazimisha hao waasi kulinda nchi yao au wauawe.

16 Kwani lilikuwa jukumu

51 8*a* MWM Kiburi. | 9*a* Alma 49:26–27. | 13*a* Alma 46:10–16.

lake la kwanza kumaliza mabishano kama haya na mafarakano miongoni mwa watu; kwani tazama, hii ilikuwa mpaka sasa sababu ya maangamizo yao. Na ikawa kwamba lilikubaliwa kulingana na sauti ya watu.

17 Na ikawa kwamba Moroni aliamuru kwamba majeshi yake yaende dhidi ya watu wa ufalme, kuweka chini kiburi chao na daraja zao kubwa na kuwalainisha na ardhi, au wachukue silaha na kusaidia njia ya uhuru.

18 Na ikawa kwamba majeshi yalienda mbele dhidi yao; na yaliweka chini kiburi chao na daraja zao kubwa, hata kwamba wakati walipoinua silaha zao za vita kupigana dhidi ya watu wa Moroni waliangushwa chini na kulainishwa na ardhi.

19 Na ikawa kwamba kulikuwa na elfu nne ya wale [a]waasi ambao walitupwa chini kwa upanga; na wale baina ya viongozi wao ambao hawakuuawa vitani walichukuliwa na kutupwa gerezani, kwani hapakuweko na wakati wa majaribio yao wakati huo.

20 Na waasi waliosalia, badala ya kukatwa chini kwa upanga, walijitolea kwa bendera ya uhuru, na walilazimishwa kuinua [a]jina la uhuru kwenye minara yao, na katika miji yao, na kuchukua silaha kwa kulinda nchi yao.

21 Na hivyo Moroni alikomesha wale watu wa ufalme, kwamba hapakuwa na yeyote aliyejulikana kwa jina la watu wa ufalme; na hivyo akakomesha ukaidi na kiburi cha wale watu ambao walidai damu ya wale walio bora; lakini waliletwa chini kujinyenyekea kama ndugu zao, na kupigana kwa ushujaa kwa uhuru wao kutoka kifungoni.

22 Tazama, ikawa kwamba wakati [a]Moroni alipokuwa akiondoa vita na mabishano miongoni mwa watu wake, na kuwaweka kwa imani na utamaduni, na kutengeneza sheria kwa kujiandaa kwa vita dhidi ya Walamani, tazama, Walamani walikuwa wamekuja kwenye nchi ya Moroni, ambayo ilikuwa mipakani mwa ukingo wa bahari.

23 Na ikawa kwamba Wanefi hawakuwa na nguvu ya kutosha katika mji wa Moroni; kwa hivyo Amalikia aliwafukuza, akiua wengi. Na ikawa kwamba Amalikia alimiliki mji, ndiyo, alimiliki ngome zao zote.

24 Na wale ambao walikimbia kutoka mji wa Moroni walingia kwenye mji wa Nefiha; na pia watu wa mji wa Lehi walijikusanya pamoja, na wakafanya matayarisho na wakawa tayari kuwapokea Walamani kwa vita.

25 Lakini ikawa kwamba Amalikia hakuwaruhusu Walamani kwenda dhidi ya mji wa Nefiha kupigana, lakini akawaweka chini kando ya ukingo wa bahari, akiwaacha watu katika kila mji kuushika na kuulinda.

26 Na hivyo aliendelea, aki-

19 *a* Alma 60:16.
20 *a* Alma 46:12–13.
22 *a* MWM Moroni, Kapteni.

miliki miji mingi, mji wa Nefiha, na mji wa Lehi, na mji wa Moriantoni, na mji wa Omneri, na mji wa Gidi, na mji wa Muleki, yote ambayo ilikuwa mashariki mwa mipaka kando ya ukingo wa bahari.

27 Na hivyo Walamani walikuwa wamepata, kwa ujanja wa Amalikia, miji mingi sana, na wenyeji wasiohesabika, yote ambayo ilikuwa imelindwa kwa nguvu kwa njia ya [a]ulinzi wa Moroni; yote ambayo iliwezesha ulinzi kwa Walamani.

28 Na ikawa kwamba walienda taratibu hadi kwenye mipaka ya nchi ya Neema, wakiwafukuza Wanefi mbele yao na kuua wengi.

29 Lakini ikawa kwamba walikutana na Teankumu, ambaye alikuwa [a]amemuua Moriantoni na kuwaongoza watu wake kwa ukimbizi wake.

30 Na ikawa kwamba alimwongoza Amalikia pia, wakati alipokuwa akienda taratibu na jeshi lake la idadi kubwa kwamba angemiliki nchi ya Neema, na pia nchi upande wa kaskazini.

31 Lakini tazama alikabiliana na uchungu kwa kurudishwa nyuma na Teankumu na watu wake, kwani walikuwa mashujaa wakuu; kwani kila mtu wa Teankumu alikuwa anashinda Walamani kwa nguvu na kwa ustadi wao wa vita, hata kuwa walikuwa bora juu ya Walamani.

32 Na ikawa kwamba waliwaangamiza kwa wingi, hata kwamba waliwauwa hata mpaka kukawa na giza. Na ikawa kwamba Teankumu na watu wake walisimamisha hema zao kwenye mipaka ya nchi ya Neema; na Amalikia akasimamisha hema zake kwenye mipaka kwenye pwani kando ya ukingo wa bahari, na kwa njia hii walifukuzwa.

33 Na ikawa kwamba wakati usiku ulipowadia, Teankumu na mtumishi wake walienda nje usiku kwa kujificha, na wakaenda kwenye kambi ya Amalikia; na tazama, usingizi ulikuwa umewalemea kwa sababu ya uchovu wao mwingi, ambao ulisababishwa na kazi na joto la mchana.

34 Na ikawa kwamba Teankumu aliingia kwa siri hadi kwenye hema la mfalme, na kumchoma kwa sagai kwenye moyo wake; na akasababisha kifo cha mfalme mara moja kwamba hakuwaamusha watumishi wake.

35 Na akarudi tena kwa siri hadi kwenye kambi yake, na tazama watu wake walikuwa wanalala, na akawaamsha na kuwaambia vitu vyote ambavyo alikuwa amefanya.

36 Na akasababisha kwamba majeshi yake yasimame tayari, isiwe Walamani wawe wameamka na kuwajia.

37 Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na tano wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa

27 *a* Alma 48:8–9. | 29 *a* Alma 50:35.

Nefi; na hivyo zikaisha siku za Amalikia.

MLANGO WA 52

Amoroni anaingia mahali pa Amalikia kama mfalme wa Walamani—Moroni, Teankumu, na Lehi wanaongoza Wanefi katika vita vya kufaulu dhidi ya Walamani—Mji wa Muleki unachukuliwa, na Yakobo Mzorami anauawa. Karibia mwaka 66–64 K.K.

Na sasa, ikawa katika mwaka wa ishirini na sita wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, tazama, wakati Walamani walipoamka asubuhi ya kwanza ya mwezi wa kwanza, tazama, walipata Amalikia amekufa katika hema lake mwenyewe; na wakaona pia kwamba Teankumu alikuwa tayari kupigana nao siku hiyo.

2 Na sasa, wakati Walamani walipoona hivi waliogopa; na wakaacha kusudi lao la matembezi yao ya taratibu ya kuelekea nchi ya kaskazini, na wakarudi nyuma na majeshi yao yote katika mji wa Muleki, na wakatafuta ulinzi katika ngome zao.

3 Na ikawa kwamba kaka wa Amalikia aliwekwa kuwa mfalme juu ya watu; na jina lake lilikuwa Amoroni; kwa hivyo mfalme Amoroni, kaka wa mfalme Amalikia, aliwekwa kutawala badala yake.

4 Na ikawa kwamba aliamuru kwamba watu wake washikilie hiyo miji, ambayo waliichukua kwa kumwaga damu; kwani walikuwa hawajachukua miji yoyote isipokuwa walikuwa wamepoteza damu nyingi.

5 Na sasa, Teankumu aliona kwamba Walamani walikuwa wamekata kauli kushikilia hiyo miji ambayo walikamata, na hizo sehemu za nchi ambazo walimiliki; na pia akiona ukubwa wa idadi yao, Teankumu alidhani haikufaa kwamba ajaribu kuwashambulia kwenye ngome zao.

6 Lakini aliweka watu wake wakazingira, kama wanaojitayarisha kwa vita; ndiyo, na kweli alikuwa akijitayarisha kujilinda dhidi yao, kwa [a]kujenga kuta kuzunguka na kutayarisha mahali pa kukimbilia.

7 Na ikawa kwamba aliendelea hivyo kujitayarisha kwa vita mpaka Moroni alipotuma idadi kubwa ya watu kuimarisha jeshi lake.

8 Na Moroni pia alituma maagizo kwake kwamba aweke wafungwa wote ambao aliwakamata; kuwa kama vile Walamani walikuwa wamekamata wafungwa wengi, kwamba aweke wafungwa wote wa Walamani kama fidia kwa wale ambao Walamani wamekamata.

9 Na pia alituma maagizo kwake kwamba aweke ulinzi kwa nchi ya Neema, na achunge sehemu [a]nyembamba ambayo ilitangulia kuelekea katika nchi upande wa kaskazini, la sivyo, Walamani wangechukua mahali hapo na wawe na uwezo wa

52 6*a* Alma 50:1–6; 53:3–5. | 9*a* Alma 22:32; Morm. 2:29.

kuwahangaisha kwa kila upande.

10 Na Moroni pia alituma kwake, akitaka kwamba awe mwaminifu kwa kuweka hiyo sehemu ya nchi, na kwamba atafute kila nafasi kupinga Walamani katika hiyo sehemu, vile ingewezekana kwa nguvu yake, kwamba labda angechukua tena kwa werevu au baadhi ya njia zingine hiyo miji ambayo ilikuwa imechukuliwa kutoka kwa mikono yao; na kwamba pia angeimarisha na kuweka nguvu miji iliyokuwa karibu, ambayo ilikuwa haijaanguka katika mikono ya Walamani.

11 Na pia akamwambia, ningekuja kwako, lakini tazama, Walamani wako juu yetu kwenye mipaka ya nchi kando ya magharibi ya bahari; na tazama, ninaenda dhidi yao, kwa hivyo siwezi kuja kwako.

12 Sasa, mfalme (Amoroni) alikuwa ameondoka nje ya nchi ya Zarahemla, na alikuwa amemjulisha malkia kuhusu kifo cha kaka yake, na alikuwa amekusanya idadi kubwa ya watu, na alienda mbele kuwashambulia Wanefi kwenye mipaka kando ya bahari ya magharibi.

13 Na hivyo alikuwa anajaribu kuwahangaisha Wanefi, na kuteka sehemu ya majeshi yao hadi sehemu ya ile nchi, wakati alikuwa ameamuru wale ambao alikuwa amewaacha kumiliki miji ambayo alikuwa ameteka, kwamba wao pia wawahangaishe Wanefi, kwenye mipaka kando ya bahari ya mashariki, na wamiliki nchi yao kwa wingi vile uwezo wao ungewakubalia, kulingana na nguvu ya majeshi yao.

14 Na hivyo ndivyo walivyokuwa Wanefi katika hizo hali za hatari kwenye mwisho wa mwaka wa ishirini na sita wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

15 Lakini tazama, ikawa katika mwaka wa ishirini na saba wa utawala wa waamuzi, kwamba Teankumu, kutokana na amri ya Moroni—ambaye alikuwa ameweka majeshi kulinda kusini na magharibi mwa mipaka ya nchi, na alikuwa ameanza mwendo wake kuelekea nchi ya Neema, ili amsaidie Teankumu na watu wake kuteka miji ambayo walikuwa wameipoteza—

16 Na ikawa kwamba Teankumu alikuwa amepokea amri kushambulia mji wa Muleki, na kuuteka ikiwezekana.

17 Na ikawa kwamba Teankumu alifanya matayarisho kushambulia mji wa Muleki, na kwenda mbele na jeshi lake dhidi ya Walamani; lakini aliona kwamba ilikuwa vigumu kuwashinda kwa nguvu wakati walipokuwa kwa hali ya kujikinga; kwa hivyo aliachilia mipango yake na akarudi tena kwenye mji wa Neema, kungoja kurudi kwa Moroni, kwamba angepata nguvu kwa jeshi lake.

18 Na ikawa kwamba Moroni aliwasili na jeshi lake katika nchi ya Neema, katika mwisho wa mwaka wa ishirini na saba wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

19 Na katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na nane, Moroni na Teankumu na wengi wa makapteni wao wakuu walikuwa na baraza la vita—kutafakari ni nini wangefanya kusababisha Walamani kuja dhidi yao kupigana; au kwamba wawabembeleze kwa njia fulani watoke kwenye ngome zao, ili wapate kunufaika juu yao na kuteka tena mji wa Muleki.

20 Na ikawa wakatuma wajumbe kwa jeshi la Walamani, ambalo lililinda mji wa Muleki, kwa kiongozi wao, ambaye jina lake lilikuwa Yakobo, wakimhitaji yeye atoke nje na majeshi yake kukutana nao kwenye uwanda kati ya hiyo miji miwili. Lakini tazama, Yakobo, ambaye alikuwa Mzorami, hangekuja na jeshi lake kuwakuta kwenye uwanda.

21 Na ikawa kwamba Moroni, akiwa hana matumaini ya kukutana nao kwenye hali iliyo sawa, kwa hivyo, alifikiria mpango ambao ungewashawishi Walamani watoke nje ya ngome zao.

22 Kwa hivyo alisababisha kwamba Teankumu achukue idadi ndogo ya watu waende chini karibu na ukingo wa bahari; na Moroni na jeshi lake, usiku, walitembea katika nyika, magharibi mwa mji wa Muleki; na hivyo, kesho yake, wakati walinzi wa Walamani walipomgundua Teankumu, walikimbia na kumwambia Yakobo, kiongozi wao.

23 Na ikawa kwamba majeshi ya Walamani yalienda mbele dhidi ya Teankumu, yakidhani kwa sababu ya idadi yao yangemshinda Teankumu kwa sababu ya uchache wa idadi yake. Na Teankumu alipoona majeshi ya Walamani yakija dhidi yake alianza kurudi nyuma kando ya ukingo wa bahari upande wa kaskazini.

24 Na ikawa kwamba wakati Walamani walipoona kwamba ameanza kutoroka, walijipa moyo na kuwafuata kwa nguvu. Na wakati Teankumu alikuwa anawaongoza mbali Walamani ambao walikuwa wakiwafukuza bila kufaulu, tazama, Moroni aliamuru kwamba sehemu ya jeshi lake ambao walikuwa na yeye waende kwa utaratibu hadi kwenye mji, na kuumiliki.

25 Na hivyo ndivyo walivyofanya, na wakawachinja wale wote ambao waliachwa nyuma kuulinda mji, ndiyo, wale wote ambao hawakutaka kusalimisha silaha zao za vita.

26 Na hivyo Moroni alipata kuumiliki mji wa Muleki na sehemu ya jeshi lake, wakati alienda taratibu na waliosalia kukabiliana na Walamani wakiwa wamerudi kutoka kumfukuza Teankumu.

27 Na ikawa kwamba Walamani walimfukuza Teankumu mpaka wakaja karibu na mji wa Neema, na pale wakakutana na Lehi na jeshi dogo, ambalo lilikuwa limeachwa kulinda mji wa Neema.

28 Na sasa tazama, wakati makapteni wakuu wa Walamani walipomwona Lehi na jeshi lake

wakija dhidi yao, walikimbia kwa kuchanganyikiwa kwingi, wakiogopa labda hawataufikia mji wa Muleki kabla Lehi hajawapata; kwani walichoka kwa sababu ya mwendo wao, na watu wa Lehi walikuwa na nguvu.

29 Sasa Walamani hawakujua kwamba Moroni alikuwa nyuma yao na jeshi lake; na wale waliogopa alikuwa Lehi na watu wake.

30 Sasa Lehi hakuwa na tamaa ya kuwapita mpaka wakutane na Moroni na jeshi lake.

31 Na ikawa kwamba kabla ya Walamani kurudi nyuma mbali walizungukwa na Wanefi, na watu wa Moroni pande moja, na watu wa Lehi upande mwingine, wote ambao walikuwa na nguvu; lakini Walamani walikuwa wamechoka kwa sababu ya matembezi yao marefu.

32 Na Moroni akawaamuru watu wake kwamba wawaangukie mpaka watakapotoa silaha zao za vita.

33 Na ikawa kwamba Yakobo, akiwa kiongozi wao, pia akiwa [a]Mzorami, na akiwa na roho isiyoshindika, aliwatangulia Walamani mbele kupigana kwa ukatili mwingi dhidi ya Moroni.

34 Moroni akiwa kwa njia yao ya matembezi, kwa hivyo Yakobo alikuwa ameamua kuwaua na kukatiza njia yake hadi katika mji wa Muleki. Lakini tazama, Moroni na watu wake walikuwa na nguvu zaidi; kwa hivyo hawakujilegeza mbele ya Walamani.

35 Na ikawa kwamba walipigana kwa pande zote mbili na ghadhabu kali sana; na kulikuwa wengi waliouawa pande zote mbili; ndiyo, na Moroni alijeruhiwa na Yakobo akauawa.

36 Na Lehi aliwashambulia kutoka nyuma yao kwa nguvu sana na watu wake wenye nguvu, kwamba Walamani waliokuwa nyuma walisalimisha silaha zao za vita; na waliosalia, walichanganyikiwa, na hawakujua mahali pa kwenda au kupiga.

37 Sasa Moroni alipoona kuchanganyikiwa kwao, aliwaambia: Ikiwa mtaleta mbele silaha zenu za vita na kuzisalimisha, tazama, tutaacha kumwaga damu yenu.

38 Na ikawa kwamba wakati Walamani waliposikia maneno haya, makapteni wao wakuu, wale wote ambao hawakuuawa, walikuja mbele na kutupa chini silaha zao za vita miguuni mwa Moroni, na pia wakawaamuru watu wao kwamba wafanye hivyo.

39 Lakini tazama, kulikuwa na wengi ambao hawakufanya hivyo; na wale ambao hawakutoa panga zao walichukuliwa na kufungwa, na silaha zao za vita zilichukuliwa kutoka kwao, na walilazimishwa kutembea na ndugu zao hadi kwenye nchi ya Neema.

40 Na sasa idadi ya wafungwa ambao walikamatwa ilizidi idadi ya wale ambao waliuawa,

33*a* Alma 31:12.

ndiyo, zaidi ya wale ambao waliuawa katika pande zote mbili.

MLANGO WA 53

Wafungwa wa Walamani watumiwa kuimarisha mji wa Neema—Mafarakano miongoni mwa Wanefi yanasaidia kufaulu kwa Walamani—Helamani anaamrisha wana elfu mbili wa watu wa Amoni. Karibia mwaka 64–63 K.K.

Na ikawa kwamba waliweka walinzi juu ya wafungwa wa Walamani, na kuwalazimisha kwenda kuzika wafu wao, ndiyo, na pia wafu wa Wanefi ambao waliuawa; na Moroni aliweka watu kuwachunga wakati walipokuwa wakifanya kazi zao.

2 Na Moroni akaenda kwenye mji wa Muleki na Lehi, na akachukua mji na kuukabidhi kwa Lehi. Sasa tazama, huyu Lehi alikuwa ni mtu ambaye alikuwa pamoja na Moroni katika sehemu nyingi katika vita vyake vyote; na alikuwa na tabia [a]kama ya Moroni, na walifurahia usalama wa kila mmoja wao; ndiyo, walikuwa wanapendana, na pia kupendwa na watu wote wa Nefi.

3 Na ikawa kwamba baada ya Walamani kumaliza kuzika wafu wao na pia wafu wa Wanefi, walitembezwa na kurudishwa kwenye nchi ya Neema; na Teankumu, kwa amri ya Moroni, alisababisha kwamba waanze kufanya kazi ya kuchimba handaki kuzunguka ile nchi, au mji, wa Neema.

4 Na alisababisha kwamba wajenge ukuta wa mbao ndani ya ukingo wa shimo; na wakatupa uchafu wa shimo juu ya [a]ukuta wa mbao; na hivyo walisababisha Walamani kufanya kazi mpaka walipouzunguka mji wa Neema kwa ukuta imara wa mbao na mchanga, kwa kimo kirefu sana.

5 Na huu mji ukawa imara sana kuanzia pale kuendelea mbele; na ndani ya mji huu walilinda wafungwa wa Walamani; ndiyo, hata nyuma ya ukuta ambao waliwasababisha kujenga kwa mikono yao. Sasa Moroni alilazimishwa kusababisha Walamani kufanya kazi, kwa sababu ilikuwa rahisi kuwalinda wakiwa kazini mwao; na alihitaji majeshi yake yote wakati alipotaka kuwashambulia Walamani.

6 Na ikawa kwamba Moroni alikuwa amepata ushindi kwa mojawapo ya jeshi kubwa la Walamani, na alikuwa amemiliki mji wa Muleki, ambao ulikuwa mojawapo ya ngome imara za Walamani katika nchi ya Nefi; na hivyo alikuwa amejenga ngome imara ya kuweka wafungwa wake.

7 Na ikawa kwamba hakujaribu tena kupigana na Walamani katika mwaka huo, lakini aliweka watu wake kujitayarisha kwa vita, ndiyo, na kwa kujenga ngome za kujikinga kutokana na Walamani, ndiyo, na kwa pia kuwaokoa wake zao na watoto wao kutokana na njaa

53 2*a* Alma 48:16–17. | 4*a* Alma 50:2–3.

na mateso, na kutoa chakula kwa majeshi yao.

8 Na sasa ikawa kwamba majeshi ya Walamani, upande wa bahari ya magharibi, kusini, wakati Moroni alipokuwa hayuko kwa ajili ya hila fulani miongoni mwa Wanefi, ambayo ilisababisha mafarakano miongoni mwao, yalikuwa yamepata faida juu ya Wanefi, ndiyo, hata kwamba walikuwa wamepata kumiliki kiasi cha miji yao katika sehemu hio ya nchi.

9 Na hivyo kwa sababu ya uovu miongoni mwao, ndiyo, kwa sababu ya mafarakano na hila miongoni mwao, walikuwa wamewekwa kwenye hali mbaya sana.

10 Na sasa tazama, nina machache ya kusema kuhusu [a]watu wa Amoni, ambao, mwanzoni, walikuwa Walamani; lakini kwa sababu ya Amoni na ndugu zake, kwa usahihi zaidi kwa uwezo na neno la Mungu, walikuwa [b]wamemgeukia Bwana; na walikuwa wameletwa chini katika nchi ya Zarahemla, na tangu hapo walikuwa wamelindwa na Wanefi.

11 Na kwa sababu ya kiapo chao walikuwa wamekatazwa kuchukua silaha dhidi ya ndugu zao; kwani walikuwa wamekula kiapo kwamba [a]kamwe hawatamwaga damu; na kulingana na kiapo chao wangekuwa wameangamia; ndiyo, wangekubali wenyewe kuanguka mikononi mwa ndugu zao, kama haingekuwa huruma na mapenzi mengi ambayo Amoni na ndugu zake walikuwa nayo kwao.

12 Na kwa sababu hii waliletwa chini katika nchi ya Zarahemla; na tangu hapo daima walikuwa [a]wamelindwa na Wanefi.

13 Lakini ikawa kwamba wakati walipoona hatari, na mateso mengi na taabu ambazo Wanefi walihimili kwao, walijazwa na huruma na [a]wakataka kuchukua silaha kwa kulinda nchi yao.

14 Lakini tazama, vile walipokuwa karibu kuchukua silaha zao za vita, walisadikishwa na kushawishiwa na Helamani na ndugu zake, kwani walikuwa karibu [a]kuvunja [b]kiapo ambacho walikuwa wamefanya.

15 Na Helamani aliogopa isije wapoteze nafsi zao; kwa hivyo wale wote ambao waliingia kwenye agano hili walilazimishwa kutazama ndugu zao wakipitia kwenye mateso yao, kwenye hali yao ya hatari wakati huu.

16 Lakini tazama, ikawa kwamba walikuwa na wana wengi, ambao hawakuingia kwenye hilo agano kwamba hawatachukua silaha za vita kujilinda wenyewe dhidi ya maadui zao; kwa hivyo walijikusanya pamoja wakati huu, wengi vile wangeweza kuchukua silaha, na wakajiita Wanefi.

17 Na wakaingia katika agano

10 *a* Alma 27:24–26.
b Alma 23:8–13.
11 *a* Alma 24:17–19.
12 *a* Alma 27:23.
13 *a* Alma 56:7.
14 *a* Hes. 30:2.
b MWM Kiapo.

kupigania uhuru wa Wanefi, ndiyo, kulinda nchi hata kwa kutoa maisha yao; ndiyo, hata waliapa kwamba hawataachilia kamwe [a]uhuru wao, lakini watapigana kwa njia zote kulinda Wanefi na wenyewe kutokana na kifungo.

18 Sasa tazama, kulikuwa elfu mbili ya hao vijana, ambao walifanya agano hili na wakachukua silaha zao za vita kulinda nchi yao.

19 Na sasa tazama, kwa vile mbeleni hawakuwa zuio kwa Wanefi, walikuwa sasa katika wakati huu usaidizi mkuu; kwani walichukua silaha zao za vita, na wakataka kwamba Helamani awe kiongozi wao.

20 Na wote walikuwa vijana, na walikuwa mashujaa kwa [a]uhodari, na pia kwa nguvu na vitendo; lakini tazama, hii haikuwa yote—walikuwa watu wa [b]ukweli wakati wote kwa kitu chochote ambacho walikabidhiwa.

21 Ndiyo, walikuwa watu wa ukweli na wenye busara, kwani walikuwa wamefundishwa kutii amri za Mungu na [a]kutembea wima mbele yake.

22 Na sasa ikawa kwamba Helamani alitembea mbele ya askari wake vijana [a]elfu mbili, kwa kusaidia watu walio kuwa mipakani mwa nchi kusini kando ya bahari ya magharibi.

23 Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na nane wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

MLANGO WA 54

Amoroni na Moroni wanashauriana kwa ajili ya kubadilisha wafungwa—Moroni anataka kwamba Walamani waondoke na waache mashambulizi yao ya mauaji—Amoroni anataka kwamba Wanefi waweke chini silaha zao na wawe chini ya Walamani. Karibia mwaka 63 K.K.

Na sasa ikawa katika mwanzo wa mwaka wa ishirini na tisa wa waamuzi, kwamba [a]Amoroni alituma kwa Moroni akitaka kwamba abadilishe wafungwa.

2 Na ikawa kwamba Moroni alifurahi sana kwa ombi hili, kwani alitaka chakula ambacho kilitolewa kwa kuwasaidia wafungwa Walamani kiwe kwa kuwasaidia watu wake wenyewe; na pia aliwataka watu wake kwa kuimarisha jeshi lake.

3 Sasa Walamani walikuwa wamechukua wanawake wengi na watoto, na hapakuwa na mwanamke wala mtoto miongoni mwa wafungwa wa Moroni, au wafungwa ambao Moroni alikuwa amewakamata; kwa hivyo Moroni alikusudia kupata hila ya kupokea wafungwa wengi wa Wanefi kutoka kwa Walamani vile ingewezekana.

4 Kwa hivyo aliandika waraka, na ukapelekwa na mtumishi

17 *a* Alma 56:47.
MWM Huru, Uhuru.
20 *a* MWM Ushujaa, enye Ushujaa.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
21 *a* MWM Tembea, Tembea na Mungu.
22 *a* Alma 56:3–5.
54 1 *a* Alma 52:3.

wa Amoroni, yule yule aliyemletea Moroni waraka. Sasa haya ndiyo maneno ambayo alimwandikia Amoroni, akisema:

5 Tazama, Amoroni, nimekuandikia wewe maoni yangu kuhusu hivi vita ambavyo umepigana dhidi ya watu wangu, kwa usahihi zaidi ambavyo [a]kaka yako amepigana dhidi yao, na ambavyo bado unataka kuendelea navyo baada ya kifo chake.

6 Tazama, ningekwambia kidogo kuhusu [a]haki ya Mungu, na upanga wa ghadhabu yake kubwa, ambayo inaning'inia juu yako isipokuwa utubu na kuondoa majeshi yako na kuyapeleka kwa nchi zako, au nchi unayomiliki, ambayo ni nchi ya Nefi.

7 Ndiyo, ningekwambia vitu hivi ikiwa ungekuwa na uwezo wa kuvitii; ndiyo, ningekwambia kuhusu ile [a]jehanamu ya kutisha ambayo inangojea kupokea [b]wauaji kama wewe na kaka yako, msipotubu na kuondoa kusudi lenu la mauaji, na mrudi na majeshi yenu kwenye nchi zenu.

8 Lakini vile wakati mmoja umekataa vitu hivi, na umepigana dhidi ya watu wa Bwana, hata hivyo natazamia utafanya hivyo tena.

9 Na sasa tazama, tupo tayari kukupokea; ndiyo, na isipokuwa uondoe makusudio yako, tazama, ukashusha chini ghadhabu ya Mungu ambaye umemkataa kwako, hata kwenye uangamizo wako.

10 Lakini, vile Bwana anaishi, majeshi yetu yatawajia isipokuwa mwondoke, na hivi karibuni mtatembelewa na kifo, kwani tutahifadhi miji yetu na nchi zetu; ndiyo, na tutahifadhi dini yetu na njia ya Mungu wetu.

11 Lakini tazama, mimi nadhani kwamba ninakuzungumzia kuhusu hivi vitu bure; au nadhani kwamba wewe ni [a]mtoto wa jehanamu; kwa hivyo nitamaliza barua yangu kwa kukwambia kwamba sitabadilisha wafungwa, isipokuwa iwe kwamba utarudisha mwanaume na mkewe na watoto wake, kwa mfungwa mmoja; ikiwa hivi ndivyo itakuwa kwamba utaifanya, nitakubali.

12 Na tazama ikiwa hutafanya hivi, nitakushambulia na majeshi yangu; ndiyo, hata nitawahami wanawake wangu kwa silaha na watoto wangu, na nitakuja dhidi yako, na nitakufuata wewe hata hadi kwenye nchi yako, ambayo ilikuwa nchi ya kwanza ya urithi [a]wetu; ndiyo, na itakuwa damu kwa damu, ndiyo, uzima kwa uzima; na nitakupiga vita hata mpaka wakati utaangamizwa kutoka kwenye uso wa dunia.

13 Tazama, niko kwenye hasira yangu, na pia watu wangu; mmefikiri kutuua sisi, na sisi tumefikiri tu kujilinda wenyewe. Lakini tazama, kama

5*a* Alma 48:1.
6*a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
7*a* MWM Jehanamu.
b Alma 47:18, 22–24. MWM Mauaji.
11*a* Yn. 8:42–44.
12*a* 2 Ne. 5:5–8.

mnafikiri kutuangamiza sisi, tutatafuta kuwaangamiza; ndiyo, na tutatafuta nchi yetu, nchi ya kwanza ya urithi wetu.

14 Sasa nafunga barua yangu. Mimi ni Moroni; mimi ni kiongozi wa watu wa Wanefi.

15 Sasa ikawa kwamba Amoroni, alipopata barua hii, alikasirika; na akaandika barua ingine kwa Moroni, na haya ndiyo maneno ambayo aliandika, akisema:

16 Mimi ni Amoroni, mfalme wa Walamani; mimi ni kaka wa Amalikia ambaye [a]ulimwua. Tazama, nitalipiza damu yake kwako, ndiyo, na nitakuja kwako na majeshi yangu kwani siogopi vitisho vyako.

17 Kwani tazama, babu zenu waliwakosea kaka zao, hata kwamba wakawaibia [a]haki yao kwa serikali wakati ilikuwa ni yao.

18 Na sasa tazama, ikiwa mtaweka chini silaha zenu, na mkubali wenyewe kutawaliwa na wale ambao serikali ni yao, ndipo nitasababisha kwamba watu wangu waweke chini silaha zao na hatutakuwa na vita tena.

19 Tazama, umetoa vitisho vingi sana dhidi yangu na watu wangu; lakini tazama, hatuogopi vitisho vyako.

20 Walakini, nitakubali kubadilisha wafungwa kulingana na ombi lako, kwa furaha, kwamba niweke chakula changu kwa watu wangu wa vita; na tutapigana vita ambavyo vitakuwa vya milele, kuwaweka Wanefi chini ya utawala wetu au kwa kuangamizwa kwao kwa milele.

21 Na kuhusu yule Mungu ambaye unasema ati tumemkataa, tazama, hatujui kiumbe kama hicho; wala wewe; lakini kama kuna kiumbe kama hicho, hatujui lakini ametuumba sisi na wewe pia.

22 Na ikiwa hivyo kwamba kuna ibilisi na jehanamu, tazama si atakupeleka wewe huko upate kuishi na kaka yangu ambaye ulimuua, ambaye ulidokeza kwamba ameenda mahali kama hapo? Lakini vitu hivi havijalishi.

23 Mimi ni Amoroni, na kizazi cha [a]Zoramu, ambaye babu zako walimlemea na kumtoa nje ya Yerusalemu.

24 Na tazama, mimi ni Mlamani jasiri; tazama, hivi vita vimeanzishwa kulipiza mabaya yao, na kuhifadhi na kuweka haki zao kwa serikali; na ninafunga barua yangu kwa Moroni.

MLANGO WA 55

Moroni anakataa kubadilisha wafungwa—Walinzi wa Walamani wanashawishiwa kulewa, na Wanefi wafungwa wanakuwa huru—Mji wa Gidi unakamatwa bila kumwaga damu. Karibia mwaka 63–62 K.K.

Sasa ikawa kwamba Moroni alipopokea hii barua alikasirika zaidi, kwa sababu alijua kwamba Amoroni alikuwa na

16*a* Alma 51:34.
17*a* 2 Ne. 5:1–4; Mos. 10:12–17.
23*a* 1 Ne. 4:31–35.

fahamu kamili ya ᵃhila yake; ndiyo, alijua kwamba Amoroni alijua kwamba haikuwa sababu ya haki ambayo ilimsababisha kuanzisha vita dhidi ya watu wa Nefi.

2 Na akasema: Tazama, sitabadilisha wafungwa na Amoroni isipokuwa aondoe kusudi lake, vile nimeeleza kwenye barua yangu; kwani sitamkubalia kwamba awe na uwezo kuliko uliyonayo.

3 Tazama, najua mahali ambapo Walamani wanasimamia watu wangu ambao wamewachukua wafungwa; na kwa vile Amoroni hataki kukubaliana na barua yangu, tazama, nitampatia kulingana na maneno yangu; ndiyo, nitatafuta kifo miongoni mwao mpaka watakapoomba amani.

4 Na sasa ikawa kwamba wakati Moroni alikuwa amesema maneno haya, alisababisha kwamba msako ufanywe miongoni mwa watu wake, kwamba labda angepata mtu ambaye alikuwa wa uzao wa Lamani miongoni mwao.

5 Na ikawa kwamba walimpata mmoja, ambaye jina lake lilikuwa Lamani; na alikuwa ᵃmmojawapo wa watumishi wa mfalme ambaye aliuawa na Amalikia.

6 Sasa Moroni alisababisha kwamba Lamani na idadi ndogo ya watu wake waende mbele hadi kwenye walinzi ambao walikuwa wanalinda Wanefi.

7 Sasa Wanefi walisimamiwa kwenye mji wa Gidi; kwa hivyo Moroni alimchagua Lamani na kusababisha kwamba idadi ndogo ya watu iende na yeye.

8 Na kulipokuwa usiku Lamani aliwaendea walinzi waliokuwa juu ya Wanefi, na tazama, walimwona akija na wakamuita; lakini aliwaambia: Msiogope; tazama, mimi ni Mlamani. Tazama, tumetoroka kutoka kwa Wanefi, na wanalala; na tazama tumechukua baadhi ya divai yao na kuja nayo.

9 Sasa wakati Walamani waliposikia maneno haya walimpokea kwa shangwe; na wakamwambia: Tupatie divai yako, ili tunywe; tuna furaha kwamba ulichukua divai ukaja nayo kwani sisi tumechoka.

10 Lakini Lamani aliwaambia: Acha sisi tuweke divai yetu mpaka tutakapoenda dhidi ya Wanefi kupigana. Lakini kusema hivi kuliwafanya kuwa na tamaa zaidi ya kutaka kunywa divai;

11 Kwani, walisema: Tumechoka, kwa hivyo acha tunywe divai, na baadaye tutapata divai kwa posha yetu, ambayo itatuimarisha kwenda dhidi ya Wanefi.

12 Na Lamani akawaambia: Mnaweza kufanya kulingana na vile mnavyotaka.

13 Na ikawa kwamba walikunywa divai bila kuzuiliwa; na ilikuwa nzuri walipoionja, kwa hivyo waliinywa kwa wingi; na ilikuwa kali, ikiwa imetayarishwa na nguvu yake.

55 1*a* Alma 47:12–35. | 5*a* Alma 47:29.

14 Na ikawa walikunywa na wakafurahi, na baadaye wote walilewa.

15 Na sasa Lamani na watu wake walipoona kwamba wote wamelewa, na wamelala sana, walimrudia Moroni na kumwelezea vitu vyote vilivyotendeka.

16 Na sasa hii ilikuwa kulingana na mpango wa Moroni. Na Moroni alikuwa ametayarisha watu wake na silaha za vita; na akaenda kwenye mji wa Gidi, wakati Walamani walipokuwa katika usingizi mkubwa na wamelewa, na akawatupia wafungwa silaha za vita, mpaka walikuwa wote wamejihami kwa silaha;

17 Ndiyo, hata kwa wanawake wao, na kwa wale watoto wao wote, wote ambao wangeweza kutumia silaha ya vita, wakati Moroni alikuwa amewaami kwa silaha wale wafungwa wote; na hivyo vitu vyote vilifanyika kwa unyamavu mkuu.

18 Lakini kama wangewaamsha Walamani, tazama walikuwa wamelewa na Wanefi wangewachinja.

19 Lakini tazama, hii haikuwa tamaa ya Moroni; hakufurahia mauaji au [a]umwagaji wa damu, lakini alifurahia kuokoa watu wake kutoka maangamizo; na kwa hii sababu hakutaka kujiletea yasiyo ya haki, hakuwashambulia Walamani na kuwaangamiza katika ulevi wao.

20 Lakini alikuwa amepata mahitaji yake; kwani alikuwa amewahami kwa silaha wafungwa wa Wanefi ambao walikuwa ndani ya ukuta wa mji, na alikuwa amewapatia uwezo kupata umiliki wa zile sehemu ambazo zilikuwa ndani ya kuta.

21 Na kisha akasababisha wale watu ambao walikuwa na yeye warudi nyuma kiwango fulani kutoka kwao, na kuzunguka majeshi ya Walamani.

22 Sasa tazama hii ilifanyika wakati wa usiku, ili wakati Walamani walipoamka asubuhi waliona kwamba wamezungukwa na Wanefi nje ya ukuta, na kwamba wafungwa wao walikuwa wamejihami kwa silaha ndani.

23 Na hivyo waliona kwamba Wanefi walikuwa na nguvu juu yao; na kwa hali hii waliona kwamba haikuwa ya manufaa kupigana na Wanefi; kwa hivyo makapteni wao wakuu waliitisha silaha zao za vita, na wakazileta mbele na kuzitupa miguuni mwa Wanefi, wakiomba kuonewa huruma.

24 Sasa tazama, hili lilikuwa pendeleo la Moroni. Aliwachukua kuwa wafungwa wa vita na kuumiliki mji, na kusababisha kwamba wafungwa wote waachiliwe, ambao walikuwa Wanefi; na wakajiunga na jeshi la Moroni, na waliongeza nguvu nyingi katika jeshi lake.

25 Na ikawa kwamba alisababisha Walamani, ambao alikuwa amechukua wafungwa,

19*a* Alma 48:16.

kwamba waanze [a]kazi ya kuimarisha ulinzi kuzunguka mji wa Gidi.

26 Na ikawa kwamba alipoimarisha mji wa Gidi, kulingana na mahitaji yake, alisababisha kwamba wafungwa wake wapelekwe kwenye mji wa Neema; na pia akalinda huo mji kwa nguvu nyingi.

27 Na ikawa kwamba, licha ya hila za Walamani, waliwaweka na kuwalinda wafungwa wote ambao walikuwa wamewachukua, na pia kudumisha ardhi yote na faida ambayo walikuwa wamechukua tena.

28 Na ikawa kwamba Wanefi walianza tena kuwa washindi, na kudai haki zao na mapendeleo yao.

29 Mara nyingi Walamani walijaribu kuwazunguka usiku, lakini kwa haya majaribio walipoteza wafungwa wengi.

30 Na safari nyingi walijaribu kutoa divai kwa Wanefi, ili wawaangamize na sumu au ulevi.

31 Lakini tazama, Wanefi hawakuwa wapole [a]kumkumbuka Bwana Mungu wao kwa huu wakati wa mateso. Hawakuanguka katika mitego yao; ndiyo, hawakunywa divai yao, isipokuwa wawe wamewapatia kwanza wafungwa wa Walamani.

32 Na wakawa hivyo waangalifu kwamba sumu yoyote isitolewe miongoni mwao; kwani divai ikimuua Mlamani kadhalika itamuua Mnefi; na hivyo ndivyo walijaribu pombe yao yote.

33 Na ikawa kwamba ilikuwa ya maana kuwa Moroni afanye mipango kushambulia mji wa Moriantoni; kwani tazama, Walamani walikuwa, kwa kazi yao, wameimarisha mji wa Moriantoni mpaka ukawa wenye nguvu sana.

34 Na walikuwa kila wakati wakileta askari wapya katika mji, na pia ruzuku mpya za vyakula.

35 Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

MLANGO WA 56

Helamani anatuma barua kwa Moroni, akieleza yaliyotendeka vitani na Walamani—Antipo na Helamani wanapata ushindi mkuu juu ya Walamani—Vijana askari elfu mbili wa Helamani wanapigana na nguvu ya miujiza, na hakuna mmoja anayeuawa. Aya ya 1, karibia mwaka 62 K.K.; aya ya 2 hadi 19, karibia mwaka 66 K.K.; na aya ya 20 hadi 57, karibia mwaka 65–64 K.K.

Na sasa ikawa katika mwanzo wa mwaka wa thelathini wa utawala wa waamuzi, katika siku ya pili katika mwezi wa kwanza, Moroni alipata barua kutoka kwa Helamani, akieleza hali ya watu kwenye eneo hilo la nchi.

2 Na haya ndiyo maneno ambayo aliandika, akisema: Ndugu yangu mpendwa, Moroni, pamoja katika Bwana vile

25*a* Alma 53:3–5.

31*a* Alma 62:49–51.

ilivyo katika taabu ya vita vyetu; tazama, ndugu yangu mpendwa, nina kitu kukwambia kuhusu vita vyetu katika sehemu hii ya nchi.

3 Tazama, [a]elfu mbili ya wana wa wale watu ambao Amoni alileta kutoka nchi ya Nefi—sasa umejua kwamba hawa walikuwa zao la Lamani, ambaye alikuwa kifungua mimba wa babu yetu Lehi;

4 Sasa sihitaji kukariri kwako kuhusu desturi au kutoamini kwao, kwani unajua kuhusu vitu hivi vyote—

5 Kwa hivyo inanitosheleza kwamba nikuambie kuwa elfu mbili ya hawa vijana wamechukua silaha zao za vita, na wanataka kwamba niwe kiongozi wao; na tumekuja mbele kulinda nchi yetu.

6 Na sasa unajua pia kuhusu [a]agano ambalo baba zao walifanya, kwamba hawatachukua silaha zao za vita dhidi ya ndugu zao kumwaga damu.

7 Lakini katika mwaka wa ishirini na sita, wakati walipoona mateso yetu na taabu zetu kwao, walikuwa karibu [a]kuvunja hilo agano ambalo walikuwa wamefanya na wachukue silaha zao za vita kwa ulinzi wetu.

8 Lakini singewakubalia kwamba wavunje hili agano ambalo walilifanya, nikiamini kwamba Mungu atatupa nguvu, hivyo kwamba tusiumie zaidi kwa sababu ya kutimiza kiapo ambacho walikuwa wamechukua.

9 Lakini tazama, hapa kuna kitu kimoja ambacho kingetupatia shangwe kuu. Kwani tazama, katika mwaka wa ishirini na sita, mimi, Helamani, nilitembea mbele nikiwaongoza hawa vijana elfu mbili hadi mji wa Yuda, kumsaidia Antipo, ambaye ulikuwa umemchagua kiongozi juu ya wale watu wa sehemu ile ya nchi.

10 Na nilijiunga na wana wangu elfu mbili (kwani wanastahili kuitwa wana) kwa jeshi la Antipo, ambamo kwa nguvu hii Antipo alifurahi sana; kwani tazama, jeshi lake lilikuwa limepunguzwa na Walamani kwa sababu majeshi yao yalikuwa yameua idadi kubwa ya watu wetu, ambayo inatupatia sababu ya kuomboleza.

11 Walakini, tunaweza kujituliza kwenye jambo hili, kwamba wamefariki kwa sababu ya nchi yao na Mungu wao, ndiyo, na wana [a]furaha.

12 Na Walamani walikuwa pia wameweka wafungwa wengi, wote ambao walikuwa makapteni wakuu, kwani hakuna yeyote ambaye aliachwa mzima. Na tunadhani kwamba sasa wakati huu wako kwenye nchi ya Nefi; ni hivyo kama hawajauawa.

13 Na sasa hii ndiyo miji ambayo Walamani wamepata kumiliki kwa kumwaga damu ya wengi wa mashujaa wa watu wetu:

14 Nchi ya Manti, au mji wa Manti, na mji wa Zeezromu,

56 3*a* Alma 53:22.
6*a* Alma 24:17–18.
7*a* Alma 53:13–15.
11*a* Alma 28:12.

na mji wa Kumeni, na mji wa Antipara.

15 Na hii ndiyo miji ambayo walimiliki wakati nilipofika katika mji wa Yuda; na nilimpata Antipo na watu wake wakifanya kazi kwa bidii kuimarisha mji.

16 Ndiyo, na walikuwa wamedhoofishwa kwa mwili na roho, kwani walipigana kwa ushujaa mchana na kufanya kazi usiku kuhifadhi miji yao; na hivyo walivumilia mateso makubwa ya kila aina.

17 Na sasa walikuwa wamekata kauli washinde mahali hapa au wafe; kwa hivyo unaweza kudhani kwamba hili jeshi dogo ambalo nilileta, ndiyo, wale wana wangu, waliwapatia matumaini makubwa na shangwe nyingi.

18 Na sasa ikawa kwamba Walamani walipoona kwamba Antipo amepata nguvu nyingi zaidi kwa jeshi lake, walilazimishwa kwa amri za Amoroni kutokuja dhidi ya mji wa Yuda, au dhidi yetu kupigana.

19 Na hivyo tulibarikiwa na Bwana; kwani kama wangekuja katika wakati wa udhaifu wetu labda wangeangamiza hili jeshi letu dogo; lakini hivyo tulihifadhiwa.

20 Waliamrishwa na Amoroni kulinda hiyo miji ambayo walikuwa wameikamata. Na hivyo ukaisha mwaka wa ishirini na sita. Na kwenye mwanzo wa mwaka wa ishirini na saba tulikuwa tumeandaa mji wetu na sisi wenyewe kwa ulinzi.

21 Sasa tulikuwa tunataka kwamba Walamani watujie sisi; kwani hatukutaka kufanya mashambulizi juu yao kwenye ngome zao.

22 Na ikawa kwamba tuliweka wapelelezi nje huku na huko, kuchunguza mwenendo wa Walamani, kwamba wasitupite wakati wa usiku ama mchana kufanya mashambulizi juu ya miji yetu mingine ambayo ilikuwa upande wa kaskazini.

23 Kwani tulijua katika hiyo miji hawakuwa na nguvu ya kutosha kukutana nao; kwa hivyo tulikuwa tunatamani, kama wangepita karibu nasi, tuwavamie kutoka nyuma na hivyo kuwazuia kutoka nyuma, kwa wakati sawa walipokabiliwa kutoka mbele. Tulidhani kwamba tungewashinda; lakini tazama, hatukufanikiwa katika hii tamaa yetu.

24 Hawakuthubutu kutupita na jeshi lao lote, wala sehemu yake, isiwe wasiwe na nguvu ya kutosha na washindwe.

25 Wala hawakuthubutu kwenda chini dhidi ya mji wa Zarahemla; wala kuvuka chimbuko la Sidoni, hadi kwenye mji wa Nefiha.

26 Na hivyo, kwa majeshi yao, walikata kauli kulinda hiyo miji ambayo walikuwa wameikamata.

27 Na sasa ikawa katika mwezi wa pili wa mwaka huu, tuliletewa vyakula vingi kutoka kwa baba za wale vijana wangu elfu mbili.

28 Na pia kulitumwa watu elfu mbili kwetu kutoka Zarahemla. Na hivyo tulijitayarisha na watu elfu kumi, na vyakula

kwao, na pia kwa wake zao na watoto wao.

29 Na Walamani, hivyo wakiona majeshi yetu yakiongezeka kila siku, na vyakula vikiletwa kwa usaidizi wetu, walianza kuogopa, na walianza kutushambulia ghafla na kurudi nyuma, kama ingewezekana kukomesha kupokea kwetu chakula na nguvu.

30 Sasa wakati tulipoona kwamba Walamani wanaanza kuwa na wasiwasi kwa jinsi hii, tulitaka kutumia hila juu yao; kwa hivyo Antipo aliamuru kwamba niende mbele na wana wangu wachanga kwenye mji jirani, tukijifanya kama tunabeba vyakula hadi kwenye mji jirani.

31 Na tulipaswa kusafiri karibu na mji wa Antipara, kama tulikuwa tunaenda upande wa ng'ambo ya pili, kwenye mipaka karibu na ukingo wa bahari.

32 Na ikawa kwamba tulienda mbele, kama tuliokuwa na vyakula vyetu, kwenda kwenye mji huo.

33 Na ikawa kwamba Antipo alienda mbele na sehemu ya jeshi lake, akiacha waliosalia kulinda mji. Lakini hakwenda mbele mpaka nilipoenda mbele na jeshi langu dogo, na kuja karibu na mji wa Antipara.

34 Na sasa kwenye mji wa Antipara kulikuwa kumewekwa jeshi la Walamani la nguvu kuliko yote; ndiyo, lile kubwa sana.

35 Na ikawa kwamba walipokuwa wamearifiwa na wapelelezi wao, walikuja nje na jeshi lao kutushambulia.

36 Na ikawa kwamba tulitoroka mbele yao, kuelekea kaskazini. Na hivyo tukaongoza mbali jeshi lenye nguvu la Walamani;

37 Ndiyo, hata kwa mwendo mrefu sana, mpaka kwamba walipoona jeshi la Antipo likiwafuata kwa nguvu zao, hawakugeuka kulia wala kushoto, lakini waliendelea kutufuata, kwa mwendo mnyoofu; na, vile tunadhani, lilikuwa kusudi lao kutuua sisi kabla ya Antipo kuwapita, na hivi kwamba wasizungukwe na watu wetu.

38 Na sasa Antipo, alipoona hatari yetu, aliongeza mwendo wa jeshi lake. Lakini tazama, kulikuwa ni usiku, kwa hivyo hawakutupata, wala Antipo hakuwafikia; kwa hivyo tulipiga kambi wakati wa usiku.

39 Na ikawa kwamba kabla ya kupambazuka asubuhi, tazama, Walamani walikuwa wanatufuata. Sasa hatukuwa na nguvu kadiri ya kutosha kupigana nao; ndiyo, nisingekubali kwamba vijana wangu wadogo waanguke mikononi mwao; kwa hivyo tuliendelea na mwendo wetu, na tukachukua mwendo wetu hadi nyikani.

40 Sasa hawangethubutu kugeuka kwa kulia wala kushoto wakiogopa kuzungukwa; wala singegeuka kulia wala kushoto wasije wakanipita, na hatungeshindana nao, lakini tuuwawe, na wangetoroka; na hivyo tukakimbia hio siku yote kwenye nyika, mpaka kulipokuwa na giza.

41 Na ikawa kwamba tena, wakati mwangaza wa asubuhi

ulipotokea, tuliona Walamani walikuwa wametupata na tukawakimbia.

42 Lakini ikawa kwamba hawakutufuata mbali kabla ya wao kusimama; na ilikuwa ni asubuhi ya siku ya tatu ya mwezi wa saba.

43 Na sasa, kama walipatwa na Antipo hatukujua, lakini nikawaambia watu wangu: Tazama, hatujui lakini wamesimama kwa kusudi kwamba turudi dhidi yao, kwamba watushike kwenye mtego wao;

44 Kwa hivyo mnasema nini, ninyi wana wangu, mtaenda dhidi yao kupigana?

45 Na sasa nakwambia, ndugu yangu mpendwa Moroni, kwamba kamwe sijaona [a]ujasiri mkubwa hivyo, hapana, sio miongoni mwa Wanefi wote.

46 Kwani vile niliwaita kila siku wana wangu (kwani wote walikuwa wachanga sana) hata hivyo waliniambia: Baba, tazama Mungu wetu yuko pamoja nasi, na hatakubali kwamba tuanguke; basi twende mbele; hatungeua ndugu zetu ikiwa wangetuacha peke yetu; kwa hivyo acha twende, wasije wakashinda jeshi la Antipo.

47 Sasa walikuwa hawajawahi kupigana, na bado hawakuogopa kifo; na walifikiri zaidi juu ya [a]uhuru wa baba zao kuliko maisha yao wenyewe; ndiyo, walikuwa wamefundishwa na [b]mama zao, kwamba ikiwa hawakuwa na shaka, Mungu angewaokoa.

48 Na walirudia kwangu maneno ya mama zao, wakisema: Hatuna shaka kuwa mama zetu walijua.

49 Na ikawa kwamba nilirudi na elfu mbili wangu dhidi ya Walamani ambao walikuwa wametufukuza. Na sasa tazama, jeshi la Antipo lilikuwa limewapata, na vita vikali vilikuwa vimeanza.

50 Jeshi la Antipo wakiwa wamechoka, kwa sababu ya matembezi yao marefu kwenye huo muda mfupi hivyo, walikuwa karibu kuanguka kwa mikono ya Walamani; na kama singerudi na elfu mbili wangu wangepata madhumuni yao.

51 Kwani Antipo alikuwa ameangushwa kwa upanga, na wengi wa viongozi wake, kwa sababu ya uchovu wao, ambao ulisababishwa na mwendo wao wa kasi—kwa hivyo watu wa Antipo, wakiwa wamechanganyikiwa kwa sababu ya vifo vya viongozi wao, walianza kuanguka mbele ya Walamani.

52 Na ikawa kwamba Walamani walipata ujasiri, na wakaanza kuwafukuza; na hivyo Walamani walikuwa wakiwafukuza kwa nguvu wakati Helamani alipowatokea kwa nyuma na wale elfu mbili wake, na akaanza kuwaua sana, hadi kwamba jeshi lote la Walamani likasimama na kumgeukia Helamani.

53 Sasa wakati watu wa Antipo walipoona kwamba Walamani wamegeuka, walikusanya

45*a* Alma 53:20–21.
47*a* Alma 53:16–18.
b Alma 57:21.
MWM Mama.

pamoja watu wao na wakaja kutokea upande wa nyuma wa Walamani.

54 Na sasa ikawa kwamba sisi, watu wa Nefi, watu wa Antipo, na mimi na elfu mbili wangu, tuliwazingira Walamani, na kuwaua; ndiyo, mpaka kwamba wakalazimishwa kusalimisha silaha zao za vita na pia wenyewe kama wafungwa wa vita.

55 Na sasa ikawa kwamba wakati walipokuwa wamejisalamisha kwetu, tazama, niliwahesabu wale vijana ambao walipigana na mimi, nikiogopa kwamba wengi wao walikuwa wameuawa.

56 Lakini tazama, kwa shangwe yangu kubwa, [a]hakukuwa na hata mmoja ambaye alikuwa ameinama kwenye ardhi; ndiyo, na walikuwa wamepigana kama waliokuwa na nguvu ya Mungu; ndiyo, hakujatokea watu kujulikana kupigana na nguvu ya miujiza kama hii; na kwa uwezo mkubwa sana waliwaangukia Walamani, kwamba waliwaogofya; na kwa sababu hii Walamani walijisalimisha kama wafungwa wa vita.

57 Na kwa vile hatukuwa na mahali kwa wafungwa wetu, kwamba tungewalinda kutoka kwa majeshi ya Walamani, kwa hivyo tuliwatuma katika nchi ya Zarahemla, na sehemu ya wale watu wa Antipo ambao hawakuuawa, nao; na waliosalia niliwachukua na kuwaunganisha kwa vijana wangu [a]Waamoni, na tukarudi hadi kwenye mji wa Yuda.

MLANGO WA 57

Helamani anasimulia kuchukuliwa kwa Antipara na kujisalimisha na baadaye ulinzi kwa Kumeni—Vijana wake wa Kiamoni wanapigana kwa ushujaa; wote wanajeruhiwa, lakini hakuna aliyeuawa—Gidi anasimulia kuuawa na kutoroka kwa Walamani wafungwa. Karibia mwaka 63 K.K.

Na sasa ikawa kwamba nilipokea barua kutoka kwa Amoroni, mfalme, ikieleza kwamba ikiwa nitawaachilia wale wafungwa wa vita ambao tuliwakamata kwamba angeuachilia mji wa Antipara kwetu.

2 Lakini nilituma barua kwa mfalme, kwamba tulikuwa na hakika majeshi yetu yalikuwa yanatosha kukamata mji wa Antipara na askari wetu; na kwa kukabidhi wafungwa wetu kwa mji huo tungejidhania wenyewe kuwa bila hekima, na kwamba tungeachilia tu wafungwa wetu kwa kubadilishana.

3 Na Amoroni alikataa barua yangu, kwani hakutaka kubadilisha wafungwa; kwa hivyo tulianza matayarisho kwenda dhidi ya mji wa Antipara.

4 Lakini watu wa Antipara waliacha mji, na wakakimbilia miji yao mingine, ambayo walisimamia, kuiimarisha; na hivyo mji wa Antipara ulianguka mikononi mwetu.

5 Na hivyo ukaisha mwaka wa

56*a* Alma 57:25; 58:39.

57*a* Alma 27:26; 53:10–11, 16.

ishirini na nane wa utawala wa waamuzi.

6 Na ikawa kwamba mwanzoni mwa mwaka wa ishirini na tisa, tulipokea ruzuku ya vyakula, na pia ongezeko kwa jeshi letu, kutoka kwa nchi ya Zarahemla, na kutoka kwa nchi ya karibu, kwa idadi ya watu elfu sita, kando na sitini ya [a]wana wa Waamoni ambao walikuja kujiunga na ndugu zao, kundi langu dogo la elfu mbili. Na sasa tazama, tulikuwa na nguvu, ndiyo, na pia tulikuwa na vyakula vingi vilivyoletwa kwetu.

7 Na ikawa kwamba ilikuwa kupenda kwetu kupigana vita na jeshi ambalo liliwekwa kulinda mji wa Kumeni.

8 Na sasa tazama, nitakuonyesha kwamba tulitekeleza haja yetu; ndiyo, na jeshi letu la nguvu, au na sehemu ya jeshi letu la nguvu, tulizunguka, usiku, mji wa Kumeni, mbele kidogo kabla ya hao kupokea ruzuku ya vyakula.

9 Na ikawa kwamba tulipiga hema karibu na mji kwa kucha nyingi; lakini tulilalia panga zetu, na kulinda kwamba Walamani hawangetujia wakati wa usiku na kutuua, ambayo walijaribu wakati mwingi; lakini vile walijaribu mara nyingi damu yao ilimwagika.

10 Mwishowe vyakula vyao viliwasili, na walikuwa karibu kuingia mjini usiku. Na sisi, badala ya kuwa Walamani, tulikuwa Wanefi; kwa hivyo, tuliwachukua wao na vyakula vyao.

11 Na ingawa Walamani wakishazuiliwa kutoka kwa usaidizi wao kwa njia hii, walikuwa bado wamekata kauli kukalia mji huo; kwa hivyo ilikuwa ni muhimu kwamba tuchukue vile vyakula na kuvipeleka Yuda, na wafungwa wetu kwenye nchi ya Zarahemla.

12 Na ikawa kwamba siku nyingi zilikuwa hazijaisha kabla ya Walamani kuanza kupoteza matumaini kwa usaidizi; kwa hivyo walisalimisha mji mikononi mwetu; na kwa hivyo tulikuwa tumemaliza kusudi letu kwa kupata mji wa Kumeni.

13 Lakini ikawa kwamba wafungwa wetu walikuwa wengi kwamba, ingawa jeshi letu lilikuwa kubwa kwa idadi, tulilazimishwa kutumia majeshi yetu yote kuwalinda, au kuwaua.

14 Kwani tazama, wangetoroka kwa idadi kubwa, na wangepigana kwa mawe, na kwa rungu, au chochote ambacho wangekamata mikononi mwao, mpaka kwamba tuliua zaidi ya elfu mbili wao baada ya wao kujitolea kama wafungwa wa vita.

15 Kwa hivyo ilikuwa muhimu kwetu, kwamba tumalize maisha yao, au tuwalinde, na panga mkononi, hadi tuwafikishe nchi ya Zarahemla; na pia vyakula vyetu vilikuwa vya kutotosha tu kwa watu wetu, ijapokuwa kwamba tulikuwa tumechukua kutoka kwa Walamani.

16 Na sasa, kwa hiyo hali

57 6*a* Alma 53:16–18.

ngumu, ilikuwa ni mambo mazito sana kuamua kuhusu hawa wafungwa wa vita; walakini, tuliamua kuwapeleka chini kwa nchi ya Zarahemla; kwa hivyo tulichagua sehemu ya watu wetu, na tukawapa uwezo juu ya wafungwa kuwapeleka chini kwenye nchi ya Zarahemla.

17 Lakini ikawa kwamba kesho yake walirudi. Na sasa tazama, hatukuwauliza kuhusu wafungwa; kwani tazama, Walamani walikuwa juu yetu, na walirudi kwa wakati ufaao kutuponya kutoanguka mikononi mwao. Kwani tazama, Amoroni alikuwa ametuma kwa usaidizi wao ruzuku mpya ya vyakula na pia jeshi kubwa la watu.

18 Na ikawa kwamba wale watu ambao tuliwatuma na wafungwa waliwasili kwa wakati ufaao na kuwasimamisha, vile walivyokuwa wako karibu kutushinda.

19 Lakini tazama, kundi langu dogo la elfu mbili na sitini walipigana kwa ukali sana; ndiyo, walikuwa imara mbele ya Walamani, na walitoa kifo kwa wote ambao waliwapinga.

20 Na vile wale waliosalia wa jeshi letu walikuwa karibu kujisalimisha kwa Walamani, tazama, wale elfu mbili na sitini walikuwa imara na bila hofu.

21 Ndiyo, na walisikiliza na kuchunguza kufanya kila neno la amri kwa uhalisi; ndiyo, kulingana na imani yao walifanyiwa; na nilikumbuka maneno ambayo waliniambia kwamba [a]mama zao waliwafundisha.

22 Na sasa tazama, ni kwa hawa wana wangu, na wale watu ambao walichaguliwa kupeleka wafungwa, ndiyo tunawia huu ushindi; kwani ilikuwa hawa ndiyo waliowapiga Walamani; kwa hivyo walifukuzwa na kurudi nyuma kwenye mji wa Manti.

23 Na tukaweka mji wetu wa Kumeni, na sio wote walioangamizwa kwa upanga; walakini, tulipata hasara kubwa.

24 Na ikawa kwamba baada ya Walamani kukimbia, nilitoa amri mara moja kwamba watu wangu ambao walikuwa wamejeruhiwa watolewe miongoni mwa wafu, na kusababisha majeraha yao yafungwe dawa.

25 Na ikawa kwamba kulikuwa na mia mbili, kutoka kwa elfu mbili na sitini wangu, ambao walikuwa walegevu kwa sababu ya kupoteza damu; walakini, kulingana na wema wa Mungu, na kwa mshangao wetu, na pia shangwe ya jeshi lote, [a]hakukuwa na nafsi moja miongoni mwao ambaye aliangamia; ndiyo, na wala hakukuwa na mmoja miongoni mwao ambaye hakupata majeraha mengi.

26 Na sasa, ulinzi wao ulikuwa wa kushangaza kwa jeshi letu lote, ndiyo, kwamba walihifadhiwa wakati kulikuwa na elfu moja wa ndugu zetu ambao waliuawa. Na tuna ha-

21 *a* Alma 56:47–48. | 25 *a* Alma 56:56.

kika kwamba walikombolewa kwa [a]uwezo wa miujiza wa Mungu, kwa sababu ya [b]imani yao kubwa kwa yale ambayo walikuwa wamefundishwa kuamini—kwamba kuna Mungu mwenye haki, na yeyote asiyemshuku, kwamba watahifadhiwa na uwezo wake wa ajabu.

27 Sasa hii ilikuwa imani ya wale ambao nimezungumzia; ni wachanga, na akili zao ni imara, na wanaweka matumaini yao kwa Mungu siku zote.

28 Na sasa ikawa kwamba baada ya kushugulikia watu wetu waliojeruhiwa, na kuwazika wafu wetu na wale wa Walamani, ambao walikuwa wengi, tazama, tulimwuliza Gidi kile kilichotendeka kuhusu wafungwa ambao walianza kwenda chini kwenye mji wa Zarahemla nao.

29 Sasa Gidi alikuwa kapteni mkuu juu ya kundi ambalo lilichukuliwa kuwachunga hadi kwenye ile nchi.

30 Na sasa, haya ndiyo maneno ambayo Gidi aliniambia: Tazama, tulianza kuelekea chini kwenye nchi ya Zarahemla na wafungwa wetu. Na ikawa kwamba tulikutana na wapelelezi wa majeshi yetu, ambao walikuwa wametumwa kuchungulia kambi ya Walamani.

31 Na wakapaza sauti kwetu, wakisema—Tazama, majeshi ya Walamani yanatembea taratibu kuelekea mji wa Kumeni; na tazama, watawashambulia, ndiyo, watawaangamiza watu wetu.

32 Na ikawa kwamba wafungwa wetu walisikia mlio wao, ambao uliwasababisha kuwa na ujasiri; na wakaasi dhidi yetu.

33 Na ikawa kwa sababu ya uasi wao tulisababisha kwamba panga zetu ziwaangukie. Na ikawa kwamba kwa kikundi, walikimbilia panga zetu, ambamo matokeo yake idadi yao kubwa iliuawa; na waliosalia walipenya walinzi na kukimbia kutoka kwetu.

34 Na tazama, wakati walipokuwa wamekimbia na hatukuweza kuwapata, tulichukua matembezi yetu kwa kasi kuelekea mji wa Kumeni; na tazama, tuliwahi kufika kwamba tuwasaidie ndugu zetu kwa kuuhifadhi mji.

35 Na tazama, tumeokolewa tena kutoka mikononi mwa maadui wetu. Na heri ni jina la Mungu wetu; kwani tazama, yeye ndiye ametuokoa; ndiyo, amefanya hiki kitu kikubwa kwa niaba yetu.

36 Sasa ikawa kwamba mimi, Helamani, niliposikia maneno haya ya Gidi, nilijazwa na shangwe kuu kwa sababu ya wema wa Mungu kutuhifadhi sisi, kwamba tusiangamizwe sote; ndiyo, na ninaamini kwamba nafsi za wale ambao waliuawa [a]zimeingia kwenye mapumziko ya Mungu wao.

MLANGO WA 58

Helamani, Gidi, na Teomneri wanachukua mji wa Manti kwa

26*a* MWM Uwezo. | *b* MWM Amini, Imani. | 36*a* Alma 12:34.

hila—Walamani wanajiondoa—Wana wa watu wa Amoni wanahifadhiwa vile wanavyosimama imara kulinda uhuru wao na imani. Karibia mwaka 63–62 K.K.

Na tazama, sasa ikawa kwamba lengo letu la pili lilikuwa kushika mji wa Manti; lakini tazama, hakukuwa na njia ambayo tungewaongoza nje ya mji na makundi yetu madogo. Kwani tazama, walikumbuka yale ambayo tulikuwa tumefanya hapo awali; kwa hivyo hatungeweza [a]kuwashawishi kutoka kwenye ngome zao.

2 Na walikuwa wengi sana kuliko jeshi letu kwamba hatungeenda mbele na kuwashambulia ndani ya ngome zao.

3 Ndiyo, na ilihitajika kwamba tutumie watu wetu kuhifadhi hizo sehemu za nchi ambazo tulikuwa tumezichukua tena kwa umiliki wetu; kwa hivyo ikawa muhimu kwamba tungoje, kwamba tupate kuongezewa nguvu kutoka kwa nchi ya Zarahemla na pia tupate ruzuku mpya ya vyakula.

4 Na ikawa kwamba tulituma ujumbe kwa mtawala wa nchi yetu, kumweleza kuhusu mambo ya watu wetu. Na ikawa kwamba tulingoja kupokea vyakula na nguvu kutoka nchi ya Zarahemla.

5 Lakini tazama, hii ilitusaidia tu kidogo; kwani Walamani pia walikuwa pia wanapokea nguvu nyingi siku kwa siku, na pia vyakula vingi; na hivyo ndivyo ilikuwa hali yetu kwa wakati huo.

6 Na Walamani walikuwa wanatokea kwa nguvu dhidi yetu mara kwa mara, wakinuia kutuangamiza kwa hila; walakini hatukuweza kupigana nao, kwa sababu ya kurudi kwao nyuma na ngome zao.

7 Na ikawa kwamba tulingoja katika hii hali ngumu kwa muda wa miezi mingi, hata karibu tulipokuwa karibu kuangamia kwa ukosefu wa chakula.

8 Lakini ikawa kwamba tulipokea chakula, ambacho kililindwa kwetu na jeshi la watu elfu mbili ambalo lilikuja kutusaidia; na huu ndiyo usaidizi wote ambao tulipata, kujilinda wenyewe na nchi yetu kutoanguka mikononi mwa maadui wetu; ndiyo, kupigana na adui ambaye hahesabiki.

9 Na sasa sababu ya haya matatizo yetu, au kwa nini hawakutuletea nguvu zaidi, hatukujua; kwa hivyo tulihuzunika na pia tulijawa na woga, isiwe kwa njia yoyote hukumu ya Mungu ije kwa nchi yetu, kwa kutugeuza na kutuharibu kabisa.

10 Kwa hivyo tuliweka roho zetu kwenye sala kwa Mungu, kwamba angetuimarisha na kutukomboa kutoka kwa mikono ya maadui wetu, ndiyo, na pia kutupatia nguvu kwamba tungeweka miji yetu, na nchi zetu, na umiliki wetu, kwa kuwasaidia watu wetu.

58 1*a* Alma 52:21; 56:30.

11 Ndiyo, na ikawa kwamba Bwana Mungu wetu alitubariki na hakikisho kwamba angetukomboa; ndiyo, mpaka kwamba akazungumza amani kwa roho zetu, na kutupatia imani kubwa, na alitusababishia kwamba tuwe na matumaini kwake kwa ukombozi wetu.

12 Na tukapata ujasiri na jeshi letu dogo ambalo tulikuwa tumepokea, na tulithibitisha kusudi letu kushinda maadui zetu, na [a]kuhifadhi nchi zetu, na umiliki wetu, na wake zetu, na watoto wetu, na asili ya [b]uhuru wetu.

13 Na hivyo tulienda mbele kwa nguvu yetu yote dhidi ya Walamani, ambao walikuwa kwenye mji wa Manti; na tukapiga hema zetu kando ya upande wa nyika, ambao ulikuwa karibu na mji.

14 Na ikawa kwamba kesho yake, wakati Walamani walipoona kwamba tulikuwa kwenye mipaka kando ya nyika ambayo ilikuwa karibu na mji, kwamba walituma wapelelezi wao karibu nasi kwamba wagundue idadi na nguvu ya jeshi letu.

15 Na ikawa kwamba walipoona kwamba hatukuwa na nguvu, kulingana na idadi yetu, na wakiogopa kwamba tungewakatiza kutoka kwa tegemeo lao isipokuwa waje nje na kupigana dhidi yetu na watuue, na pia wakidhani kwamba wangetuangamiza kwa urahisi na jeshi lao kubwa, kwa hivyo walianza kujitayarisha kuja nje dhidi yetu kupigana.

16 Na wakati tuliona kwamba walikuwa wanajitayarisha kuja dhidi yetu, tazama, nilisababisha kwamba Gidi na idadi ndogo ya watu, wajifiche nyikani, na pia kwamba Teomneri na idadi ndogo ya watu wajifiche nyikani.

17 Sasa Gidi na watu wake walikuwa kwa mkono wa kulia na wengine kwa kushoto; na wakati walipokuwa wamejificha wenyewe, tazama, nilibaki, na jeshi langu lililosalia, mahali pale ambapo tulikuwa wakati wa kwanza tumepiga hema zetu tukijitayarisha wakati ule Walamani wangekuja nje kupigana.

18 Na ikawa kwamba Walamani walikuja nje na jeshi lao kubwa dhidi yetu. Na wakati walikuwa wamekuja na wako karibu kutuangukia kwa upanga, nilisababisha kwamba watu wangu, wale ambao walikuwa na mimi, warudi nyuma kwenye nyika.

19 Na ikawa kwamba Walamani walitufuata kwa mwendo wa kasi, kwani walitaka sana kutupata ili watuue; kwa hivyo walitufuata hadi nyikani; na tulipita katikati ya Gidi na Teomneri, hata kwamba hawakugunduliwa na Walamani.

20 Na ikawa kwamba Walamani walipopita, au wakati jeshi lilipokuwa limepita, Gidi na Teomneri waliinuka kutoka kwa maficho yao, na wakawazuia

12*a* Alma 46:12–13; Morm. 2:23. *b* MWM Huru, Uhuru.

wapelelezi wa Walamani ili wasirejee mjini.

21 Na ikawa kwamba wakati walipokuwa wamewazuia, walikimbia hadi kwenye mji na kushambulia walinzi ambao waliachwa kulinda mji, mpaka kwamba wakawaangamiza na wakamiliki mji.

22 Sasa hii ilifanyika kwa sababu Walamani walikuwa wameruhusu jeshi lao lote, kuongozwa nyikani, isipokuwa walinzi wachache pekee.

23 Na ikawa kwamba Gidi na Teomneri kwa njia hii walipata umiliki wa ngome zao. Na ikawa kwamba tulichukua njia yetu, baada ya kusafiri sana kwenye nyika kuelekea nchi ya Zarahemla.

24 Na wakati Walamani waliona kwamba walikuwa wanatembea kuelekea nchi ya Zarahemla, waliogopa sana, kusiwe kuna mtego umewekwa kuwaongoza kwenye maangamizo; kwa hivyo walianza kurudi nyuma hadi kwenye nyika tena, ndiyo, hata nyuma kutumia ile njia ambayo walikuja nayo.

25 Na tazama, kulikuwa usiku na wakapiga hema zao, kwani makapteni wakuu wa Walamani walidhani kwamba Wanefi wamechoka kwa sababu ya matembezi yao; na wakidhani kwamba walipeleka jeshi lao lote kwa hivyo hawakufikiri kuhusu mji wa Manti.

26 Sasa ikawa kwamba wakati usiku ulipowadia, nilisababisha kwamba watu wangu wasilale, lakini kwamba watembee mbele kwa njia nyingine kuelekea mji wa Manti.

27 Na kwa sababu ya haya matembezi yetu ya usiku, tazama, kesho yake tulikuwa mbele ya Walamani, mpaka kwamba tuliwasili kabla yao katika mji wa Manti.

28 Na hivyo ikawa kwamba, kwa werevu huu tulimiliki mji wa Manti bila kumwaga damu.

29 Na ikawa kwamba wakati majeshi ya Walamani yalipowasili karibu na mji, na kuona kwamba tulikuwa tayari kupigana nao, walistaajabu sana na wakashikwa na woga mwingi, mpaka kwamba walikimbilia kwenye nyika.

30 Ndiyo, na ikawa kwamba majeshi ya Walamani yalikimbia nje kutoka sehemu hii yote ya nchi. Lakini tazama, wamebeba nao wanawake wengi na watoto na wamewapeleka nje ya nchi.

31 Na [a]hiyo miji ambayo ilichukuliwa na Walamani, yote kwa wakati huu iko katika umiliki wetu; na baba zetu na wanawake wetu na watoto wetu wanarejea nyumbani kwao, wote isipokuwa wale ambao wamechukuliwa wafungwa na kubebwa na Walamani.

32 Lakini tazama, majeshi yetu ni machache kulinda idadi kubwa hiyo ya miji na umiliki mwingi hivyo.

33 Lakini tazama, tunamwamini Mungu wetu ambaye

31*a* Alma 56:14.

ametupatia ushindi juu ya hizo nchi, mpaka kwamba tumepata hiyo miji na hizo nchi, ambazo zilikuwa zetu.

34 Sasa hatujui kwa nini serikali haitupatii nguvu zaidi; wala watu ambao wamekuja kwetu hawajui kwa nini hatujapokea nguvu nyingi zaidi.

35 Tazama, hatujui lakini kwamba hamjashinda, na mmehitaji majeshi katika sehemu ile ya nchi; ikiwa hivyo, hatuwezi kunung'unika.

36 Na ikiwa si hivyo, tazama, tunaogopa kwamba kuna [a]ugomvi katika serikali, kwamba hawawezi kuleta watu wengi zaidi kwa usaidizi wetu; kwani tunajua kwamba wako wengi kuliko wale ambao wametuma.

37 Lakini, tazama, haitujalishi—tunaamini Mungu [a]atatukomboa, ijapokuwa majeshi yetu ni dhaifu, ndiyo, na kutukomboa kutoka kwa mikono ya maadui zetu.

38 Tazama, huu ni mwaka wa ishirini na tisa, karibu mwisho wake, na tumemiliki nchi zetu; na Walamani wamekimbia hadi kwenye nchi ya Nefi.

39 Na wale wana wa watu wa Amoni, ambao nimezungumzia kwa uzuri, wako na mimi katika mji wa Manti; na Bwana amewasaidia, ndiyo, na kuwaweka kutokana na kuuawa kwa upanga, kwa matokeo kwamba hata mtu [a]mmoja hakuuawa.

40 Lakini tazama, wamepata majeraha mengi; lakini wanasimama imara kwa huo [a]uhuru ambamo kwake Mungu amewafanya huru; na wako waangalifu kumkumbuka Bwana Mungu wao siku hadi siku; ndiyo, wanachunga kutii sheria zake, na hukumu zake, na amri zake siku zote; na imani yao iko na nguvu katika unabii kuhusu yale ambayo yatakuja.

41 Na sasa, ndugu yangu mpendwa, Moroni, naomba Bwana Mungu wetu, ambaye ametukomboa na kutufanya huru, akulinde siku zote katika uwepo wake; ndiyo, na awabariki hawa watu, hata kwamba ufaulu kwa kupata tena umiliki wa yale yote ambayo Walamani wamechukua kutoka kwetu, ambayo yalikuwa kwa usaidizi wetu. Na sasa tazama, ninamaliza barua yangu. Mimi ni Helamani, mwana wa Alma.

MLANGO WA 59

Moroni anamwuliza Pahorani ahifadhi majeshi ya Helamani—Walamani wanakamata mji wa Nefiha—Moroni anakasirikia serikali. Karibia mwaka 62 K.K.

Sasa ikawa katika mwaka wa thelathini wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, baada ya Moroni kupokea na kusoma [a]barua ya Helamani, alifurahi sana kwa sababu ya ustawi, ndiyo, kufaulu kwingi ambako Helamani alikamata nchi ambazo zilikuwa zimepotea.

2 Ndiyo, na aliwajulisha watu wake wote, katika nchi yote

36*a* Alma 61:1–5.
37*a* 2 Fal. 17:38–39.
39*a* Alma 56:56.
40*a* MWM Huru, Uhuru.
59 1*a* Alma 56:1.

karibu na ile sehemu ambayo alikuwa, kwamba wafurahi pia.

3 Na ikawa kwamba mara moja alituma [a]barua kwa [b]Pahorani, akitaka kwamba asababishe watu wajikusanye pamoja kumtia Helamani nguvu, au majeshi ya Helamani, ili aweze kulinda kwa urahisi sehemu hio ya nchi ambayo alikuwa ameipata tena kwa miujiza.

4 Na ikawa wakati Moroni alikuwa ametuma hii barua kwa nchi ya Zarahemla, alianza tena kufikiria kuweka mpango kwamba angeweza kupata tena mabaki ya umiliki na miji ambayo Walamani walikuwa wamechukua kutoka kwao.

5 Na ikawa kwamba wakati Moroni alikuwa anafanya mipango kwenda dhidi ya Walamani kupigana, tazama, watu wa Nefiha, ambao walikusanyika pamoja kutoka mji wa Moroni na mji wa Lehi na mji wa Moriantoni, walishambuliwa na Walamani.

6 Ndiyo, hata wale ambao walikuwa wamelazimishwa kukimbia kutoka nchi ya Manti, na kutoka nchi karibu, walikuwa wamekuja na kujiunga na Walamani katika sehemu hii ya nchi.

7 Na hivyo wakiwa wengi sana, ndiyo, na wakipokea nguvu siku hadi siku, kwa amri ya Amoroni walikuja mbele dhidi ya watu wa Nefiha, na wakaanza kuwaua kwa wingi.

8 Na majeshi yao yalikuwa mengi sana kwamba watu wa Nefiha waliosalia walilazimishwa kukimbia mbele yao; na wakaja hata wakaungana na jeshi la Moroni.

9 Na sasa vile Moroni alidhani kwamba kuwe na watu watumwe kwenye mji wa Nefiha, kwa usaidizi wa wale watu kulinda mji huo, na akijua kwamba ilikuwa ni rahisi kulinda mji usianguke kwenye mikono ya Walamani kuliko kuuteka kutoka kwao, alidhani kwamba wangelinda mji huo kwa urahisi.

10 Kwa hivyo aliweka majeshi yake yote kwa kuhifadhi zile sehemu ambazo alikuwa ameteka tena.

11 Na sasa, Moroni alipoona kwamba mji wa Nefiha umechukuliwa tena alikuwa na huzuni nyingi sana, na akaanza kuwa na shaka, kwa sababu ya uovu wa watu, ikiwa hawataanguka katika mikono ya ndugu zao.

12 Sasa hii ndiyo ilikuwa fikira ya makapteni wake wote wakuu. Walishuku na kustaajabu pia kwa sababu ya uovu wa watu, na hii ni kwa sababu ya kufaulu kwa Walamani juu yao.

13 Na ikawa kwamba Moroni alikasirishwa na serikali, kwa sababu ya [a]kutojali kwao kuhusu uhuru wa nchi yao.

MLANGO WA 60

Moroni anamlalamikia Pahorani kuhusu serikali kutojali majeshi—

3*a* Alma 60:1–3. | *b* Alma 50:40. | 13*a* Alma 58:34; 61:2–3.

Bwana anakubali wenye haki kuuawa—Wanefi lazima watumie nguvu zao na uwezo wao wote ili wajiokoe kutoka kwa maadui zao—Moroni anatishia kupigana na serikali majeshi yake yasipopelekewa msaada. Karibia mwaka 62 K.K.

Na ikawa kwamba alimwandikia tena mtawala wa nchi, ambaye alikuwa Pahorani, na haya ndiyo maneno ambayo aliandika, akisema: Tazama, ninaelekeza barua yangu kwa Pahorani, katika mji wa Zarahemla, ambaye ni [a]mwamuzi mkuu na mtawala wa nchi, na pia kwa wale wote ambao wamechaguliwa na hawa watu kutawala na kuendesha shughuli za vita hivi.

2 Kwani tazama, nina kitu cha kuwaambia kwa njia ya lawama; kwani tazama, ninyi wenyewe mnajua kwamba mmewekwa kukusanya watu pamoja, na kuwahami kwa mapanga, na vitara, na namna zote za silaha za vita za kila aina, na kutuma na mbele dhidi ya Walamani, kwenye hizo sehemu ambazo wangeingilia katika nchi yetu.

3 Na sasa tazama, nawaambia ninyi kwamba mimi, na pia watu wangu, na pia Helamani na watu wake, tumeumia maumivu makubwa sana; ndiyo, hata njaa, kiu, na uchovu, na namna zote za mateso ya kila aina.

4 Lakini tazama, ikiwa haya ndiyo yote tuliyoumia hatungelalamika wala kunung'unika.

5 Lakini tazama, mauaji yamekuwa makubwa miongoni mwa watu wetu; ndiyo, maelfu wameanguka kwa upanga, wakati ingekuwa vingine kama mngeyapa majeshi yetu nguvu za kutosha na usaidizi kwao. Ndiyo, kutojali kwenu kumekuwa kwingi sana kwetu.

6 Na sasa tazama, tunataka kujua chanzo cha huku kutojali sana; ndiyo, tunataka kujua sababu ya hii hali ya kutofikiri kwenu.

7 Mnaweza kufikiri kukalia viti vyenu vya enzi kwa hali ya kupotelewa na akili, wakati maadui wenu wanatambaza kazi ya vifo karibu nanyi? Ndiyo, wakati wanaua maelfu ya ndugu zenu—

8 Ndiyo, hata wale ambao wamewategemea kwa ulinzi, ndiyo, wamewaweka kwa nafasi kwamba mngewasaidia, ndiyo, mngetuma majeshi kwao, ili kuwapatia nguvu, na kuponya maelfu yao kutokana na kuanguka kwa upanga.

9 Lakini tazama, haya sio yote—mmezuia chakula kuwaendea, mpaka kwamba wengi wamepigana na wametokwa na damu na kufa kwa sababu ya mahitaji makubwa ambayo walikuwa nayo kwa sababu ya ustawi wa hawa watu; ndiyo, na hii wamefanya wakati walikuwa karibu [a]kuangamia kwa njaa, kwa sababu ya kutojali kwenu sana kuwahusu.

60 1*a* Alma 50:39–40. | 9*a* Alma 58:7.

10 Na sasa, ndugu zangu wapendwa—kwani mnahitajika kuwa wapendwa; ndiyo, na mnapaswa kujivuruga wenyewe kwa bidii kwa ustawi na uhuru wa hawa watu; lakini tazama, mmewadharau mpaka kwamba damu ya maelfu itakuwa juu ya vichwa vyenu kwa kisasi; ndiyo, kwani Mungu anafahamu vilio vyao vyote, na taabu zao—

11 Tazama, mnaweza kudhani kwamba mtaketi kwenye viti vyenu vya enzi, na kwa sababu ya uzuri mwingi wa Mungu hamngefanya chochote na atawakomboa? Tazama, kama mmedhani hivi mmedhani bure.

12 [a]Mnadhani kwamba, kwa sababu ndugu zenu wengi wameuawa ni kwa sababu ya uovu wao? Ninawaambia, ikiwa mmedhani hivyo mmedhani bure; kwani ninawaambia, kuna wengi ambao wameuawa kwa upanga; na tazama ni kwa lawama yenu;

13 Kwani Bwana anakubali wenye haki kuuawa ili [a]haki yake na hukumu ijie wale waovu; kwa hivyo hampaswi kudhani kwamba wenye haki wamepotea kwa sababu wameuawa; lakini tazama, wanaingia kwa pumziko la Bwana Mungu wao.

14 Na sasa tazama, nawaambia, ninaogopa sana kwamba hukumu za Mungu zitawajia watu hawa, kwa sababu ya uvivu wao mkuu, ndiyo, hata uvivu wa serikali yetu, na dharau zao kubwa kwa ndugu zao, ndiyo, kuelekea wale ambao wameuawa.

15 Kwani kama haingekuwa kwa [a]uovu ambao ulianzia kwa serikali yetu, tungezuia maadui wetu kwamba hawangekuwa na uwezo juu yetu.

16 Ndiyo, kama haingekuwa kwa ajili ya [a]vita ambavyo vilianza miongoni mwetu; ndiyo, kama haingekuwa kwa hawa [b]watu wa mfalme, ambao walisababisha damu nyingi kumwagika miongoni mwetu; ndiyo, wakati tulikuwa tunakabiliana miongoni mwetu, kama tungeunganisha nguvu zetu vile tulivyofanya awali; ndiyo, kama haingekuwa tamaa ya uwezo na mamlaka ambayo wale watu wa mfalme walikuwa nayo juu yetu; kama wangekuwa waaminifu katika mwanzo wa uhuru wetu, na kujiunga nasi, na kwenda mbele dhidi ya maadui wetu, badala ya kuchukua panga zao dhidi yetu, ambayo ilisababisha umwagaji wa damu nyingi miongoni mwetu; ndiyo, kama tungekuwa tumeenda dhidi yao kwa uwezo wa Bwana, tungekuwa tumewatawanya maadui zetu, kwani ingefanyika, kulingana na kutimiza neno lake.

17 Lakini tazama, sasa Walamani wanatushambulia, wakimiliki nchi zetu, na wanawaua watu wetu kwa upanga, ndiyo, wake zetu na watoto wetu, na

12*a* Lk. 13:1–5.
13*a* Alma 14:10–11; M&M 42:46–47.
15*a* Alma 51:9, 13.
16*a* Alma 51:16–19.
b Alma 51:5, 8.

pia kuwachukua kama wafungwa, wakisababisha kwamba waumie namna yote ya mateso, na hii ni kwa sababu ya uovu mkuu wa wale ambao wanatafuta uwezo na mamlaka, ndiyo, hata wale watu wa mfalme.

18 Lakini kwa nini niseme mengi kuhusu jambo hili? Kwani hatujui lakini kuwa ninyi wenyewe mnatafuta mamlaka. Hatujui lakini ninyi pia ni wasaliti kwa nchi yenu.

19 Au ni kwamba hamtujali kwa sababu mko katikati ya nchi yetu na mmezungukwa na usalama, kwamba hamsababishi vyakula viletwe kwetu, na pia watu kuimarisha majeshi yetu?

20 Mmesahau amri za Bwana Mungu wenu? Ndiyo, mmesahau utumwa wa babu zetu? Mmesahau ni mara ngapi tumekombolewa kutoka mikono ya maadui zetu?

21 Au mnadhani kwamba Bwana atatukomboa, wakati tunakalia viti vyetu vya enzi na hatutumii njia ambazo Bwana ametutolea?

22 Ndiyo, je, mtaketi bila kufanya kitu wakati mnazingirwa na maelfu ya wale, ndiyo, na kumi ya maelfu, ambao pia huketi kwenye uvivu, wakati kuna maelfu karibu katika mipaka ambao wanaanguka kwa upanga, ndiyo, wamejeruhiwa na kutokwa na damu?

23 Mnafikiri kwamba Mungu atawaona kama wasio na makosa wakati mnakaa wima na kutazama vitu hivi? Tazama nawaambia, Hapana. Sasa nataka kwamba mkumbuke kwamba Mungu amesema kwamba chombo cha [a]ndani kitasafishwa kwanza, ili nje yake nayo ipate kuwa safi.

24 Na sasa, isipokuwa mtubu kwa yale ambayo mmefanya, na kuanza kuamka na kufanya, na kutuma mbele vyakula na watu kwetu, na pia kwa Helamani, ili alinde hizo sehemu za nchi yetu ambazo amekamata tena, na ili tujirudishie tena umiliki wetu ambao umesalia katika sehemu hizi, tazama itakuwa ya kufaa kwamba tusipigane tena na Walamani mpaka kwanza tuoshe ndani ya chombo chetu, ndiyo, hata uongozi mkuu wa serikali yetu.

25 Na isipokuwa mkubali barua yangu, na mje nje kunionyesha mimi [a]roho ya kweli ya uhuru, na mjaribu kuimarisha na kuongeza nguvu ya majeshi yetu, na kuwapelekea chakula kwa usaidizi wao, tazama nitaacha sehemu ya wahuru wangu kulinda sehemu hii ya nchi yetu, na nitaacha nguvu na baraka za Mungu juu yao, kwamba nguvu nyingine isiweze kuja dhidi yao—

26 Na hii ni kwa sababu ya imani yao kubwa, na uvumilivu wao katika taabu zao—

27 Na nitakuja kwenu, na ikiwa kutakuwa yeyote miongoni mwenu ambaye ana mahitaji ya

23*a* Mt. 23:25–26.

25*a* Alma 51:6; 61:15.

uhuru, ndiyo, ikiwa kunaweza kuwa na hata chembe ya uhuru ambayo imebaki, tazama nitavuruga uasi miongoni mwenu, hata mpaka wale ambao wametaka kuchukua nguvu na mamlaka watamalizika.

28 Ndiyo, tazama siogopi nguvu zenu wala mamlaka yenu, lakini ni [a]Mungu wangu ambaye ninamwogopa; na ni kulingana na amri zake kwamba ninachukua upanga wangu kulinda mwendo wa nchi yangu, na ni kwa sababu ya uovu wenu kwamba tumeumia kwa kupoteza kwingi.

29 Tazama ni wakati, ndiyo, wakati sasa umefika, kwamba msipo jishughulisha kwenda katika ulinzi wa nchi yenu na watoto wenu, [a]upanga wa haki unaning'inia juu yenu; ndiyo, na utawaangukia na kuwaadhibu hata kwenye uangamizo wenu.

30 Tazama, nangojea usaidizi kutoka kwenu; na, msipohudumia mahitaji yetu, tazama, nakuja kwenu, hata kwa nchi ya Zarahemla, na kuwakata kwa upanga, mpaka kwamba hamtakuwa na uwezo mwingine wa kucheleweshe maendeleo ya watu hawa kwa kusudi la uhuru wetu.

31 Kwani tazama, Bwana hatakubali kwamba muishi na mzidi kuwa na nguvu kwa uovu wenu kuwaangamiza watu hawa wenye haki.

32 Tazama, mnaweza kudhani kwamba Bwana atawaachilia na atoe hukumu kwa Walamani, wakati ni desturi ya babu zao ambayo imesababisha chuki yao, ndiyo, na imeongezwa mara mbili na wale ambao wameasi kutoka kwetu, wakati uovu wenu ni kwa kusudi la mapenzi yenu ya furaha na vitu vya bure vya dunia?

33 Mnajua kwamba mnakosea sheria za Mungu, na mnajua kwamba mnazikanyaga chini ya miguu yenu. Tazama, Bwana ananiambia: Ikiwa wale ambao wamepewa utawala hawatubu dhambi zao na uovu, utaenda na kupigana nao.

34 Na sasa tazama, mimi, Moroni, nimelazimishwa, kulingana na agano ambalo nimefanya kuweka amri za Mungu; kwa hivyo nataka kwamba mjishikilie kwa neno la Mungu, na mtume kwa haraka kwangu kutoka kwenu vyakula na watu, na pia kwa Helamani.

35 Na tazama, kama hamtafanya hivi nitakuja kwenu haraka; kwani tazama, Mungu hawezi kukubali kwamba tuangamie kwa njaa; kwa hivyo atatupatia sehemu ya chakula chenu, hata kama ni kwa upanga. Sasa hakikisha kwamba mnatimiza neno la Mungu.

36 Tazama, mimi ni Moroni, kapteni wenu mkuu. [a]Sihitaji uwezo, lakini kuuweka chini. Sitafuti heshima ya ulimwengu, lakini utukufu wa Mungu wangu, na uhuru na ustawi wa nchi yangu. Na hivyo ninamaliza barua yangu.

28*a* Mdo. 5:26–29. | 29*a* Hel. 13:5; 3 Ne. 2:19. | 36*a* M&M 121:39–42.

MLANGO WA 61

Pahorani anamwambia Moroni kuhusu maasi na uhalifu dhidi ya serikali—Watu wa mfalme wanachukua Zarahemla na wanafanya mapatanano na Walamani—Pahorani anauliza usaidizi wa kijeshi dhidi ya waasi. Karibia mwaka 62 K.K.

Tazama, sasa ikawa kwamba mara baada ya Moroni kutuma barua yake kwa mtawala mkuu, alipata barua kutoka kwa [a]Pahorani, mtawala mkuu. Na haya ndiyo maneno ambayo alipokea:

2 Mimi, Pahorani, ambaye ni mtawala mkuu wa nchi hii, natuma maneno haya kwa Moroni, kapteni mkuu juu ya jeshi. Tazama, nakwambia, Moroni, kwamba sifurahii [a]mateso yako makubwa, ndiyo, inaisikitisha roho yangu.

3 Lakini tazama, kuna wale ambao wanafurahia mateso yako, ndiyo, mpaka kwamba wameinuka kwa uasi dhidi yangu, na pia dhidi ya watu wangu ambao ni watu [a]huru, ndiyo, na wale ambao wameasi ni wengi sana.

4 Na ni wale ambao wametafuta kuchukua kiti cha hukumu kutoka kwangu hiyo imekuwa sababu ya uovu huu kubwa; kwani wametumia udanganyifu mkuu, na wamepotosha mioyo ya watu wengi, ambayo itakuwa sababu ya majonzi ya kutisha miongoni mwetu; wamezuia chakula chetu, na wamewatisha watu wetu walio huru kwamba hawajafika nyinyi.

5 Na tazama, wamenikimbiza mimi mbele yao, na nimekimbilia nchi ya Gideoni, na watu wengi vile nilivyoweza kupata.

6 Na tazama, nimetuma tangazo kote katika sehemu hii ya nchi; na tazama, wanajikusanya kwetu kila siku, na silaha zao, kwa kukinga nchi yao na [a]uhuru wao, na kulipiza kisasi kwa wale waliotukosea.

7 Na wamekuja kwetu, mpaka kwamba wale ambao wameasi kwa uhalifu dhidi yetu, ndiyo, wametudharau, ndiyo, mpaka kwamba wanatuogopa na hawathubutu kuja kukabiliana nasi kwa vita.

8 Wanasimamia nchi, au mji, wa Zarahemla; wamejiwekea mfalme, na amemwandikia mfalme wa Walamani, ambamo kwake amekubali kuunda muungano na yeye; kwa muungano ambamo amekubali kulinda mji wa Zarahemla, ulinzi ambao anadhani utawezesha Walamani kushinda nchi iliyosalia, na atawekwa mfalme juu ya hawa watu wakati watashindwa chini ya Walamani.

9 Na sasa, kwenye barua yako, umenilaumu, lakini hainijalishi; sijakasirika, lakini nina furaha kwa ujasiri wa moyo wako. Mimi, Pahorani, sitafuti ukubwa, isipokuwa tu niweke kiti changu cha hukumu ili nihifadhi haki na uhuru wa watu wangu. Nafsi yangu inasimama

61 1*a* Alma 50:39–40.
2*a* Alma 60:3–9.
3*a* Alma 51:6–7.
6*a* MWM Huru, Uhuru.

imara kwa ule uhuru ambao kwake Mungu ametufanya [a]huru.

10 Na sasa, tazama, tutashindana na uovu hata kwenye umwagaji wa damu. Hatungemwaga damu ya Walamani ikiwa wangekaa katika nchi yao.

11 Hatungemwaga damu ya ndugu zetu kama hawangeasi kwa uhalifu na kuchukua upanga dhidi yetu.

12 Tungejitolea wenyewe kwenye nira ya utumwa kama ingekuwa kanuni ya Mungu, au kama angetuamuru kufanya hivyo.

13 Lakini tazama yeye hatuamuru kwamba tujitolee wenyewe kwa maadui wetu, lakini kwamba tuweke [a]imani yetu kwake, na atatukomboa.

14 Kwa hivyo, ndugu yangu mpendwa, Moroni, acha tupinge uovu, na uovu wowote ambao hatuwezi kupinga na maneno yetu, ndiyo, kama maasi na mafarakano, acha [a]tupinge kwa panga zetu, ili tuweke uhuru wetu, ili tufurahi kwenye ufanisi mkuu wa kanisa letu, na kwa njia ya Mkombozi wetu na Mungu wetu.

15 Kwa hivyo, njoo kwangu na wachache wa watu wako, na uwaache waliosalia waangalie Lehi na Teankumu; wape uwezo kuendesha vita katika sehemu hiyo ya nchi, kulingana na [a]Roho ya Mungu, ambayo pia ni roho ya uhuru ambayo iko ndani yao.

16 Tazama nimetuma vyakula vichache kwao, ili wasiangamie kabla hujakuja kwangu.

17 Kusanya pamoja jeshi lolote unaloweza wakati wa kuja kwako hapa, na tutaenda haraka dhidi ya wale wasiokubali, katika nguvu za Mungu wetu kulingana na imani ambayo iko ndani yetu.

18 Na tutautwaa mji wa Zarahemla, ili tuweze kupata chakula zaidi kuwapelekea Lehi na Teankumu; ndiyo, tutaenda mbele dhidi yao katika nguvu za Bwana, na tutamaliza huu uovu mkubwa.

19 Na sasa, Moroni, nina shangwe kwa kupata barua yako, kwani nilikuwa na wasiwasi kuhusu kile tutakacho fanya, ikiwa itakuwa haki kwetu kwenda dhidi ya ndugu zetu.

20 Lakini umesema, isipokuwa watubu Bwana amekuamuru uwashambulie.

21 Hakikisha kwamba [a]mnawaimarisha Lehi na Teankumu katika Bwana; uwaambie wasiogope, kwani Mungu atawakomboa, ndiyo, na pia wale wote wanaosimama imara katika uhuru ule ambao kwao Mungu amewafanya huru. Na sasa namaliza barua yangu kwa ndugu yangu mpendwa, Moroni.

MLANGO WA 62

Moroni anaenda kumsaidia Pahorani katika nchi ya Gideoni—Watu wa mfalme ambao wanakataa

9 *a* Yn. 8:31–36; M&M 88:86.
13 *a* MWM Amini, Imani; Tegemea.
14 *a* Alma 43:47.
15 *a* 2 Kor. 3:17.
MWM Roho Mtakatifu.
21 *a* Zek. 10:12.

kulinda nchi yao wanauawa—Pahorani na Moroni wanatwaa tena mji wa Nefiha—Walamani wengi wanajiunga na watu wa Amoni—Teankumu anamuua Amoroni na kisha anauawa pia—Walamani wanakimbizwa kutoka nchini, na amani inaanzishwa—Helamani anarudia ukasisi na kulijenga Kanisa. Karibia mwaka 62–57 K.K.

Na sasa ikawa kwamba Moroni alipopata barua hii moyo wake ulipata ujasiri, na ukajazwa na shangwe kuu kwa sababu ya uaminifu wa Pahorani, kwamba hakuwa pia [a]msaliti kwa uhuru na asili ya nchi yake.

2 Lakini pia alilia sana kwa sababu ya uovu wa wale ambao walimwondoa Pahorani kutoka kwa kiti cha hukumu, ndiyo, kabisa kwa sababu ya wale ambao waliasi dhidi ya nchi yao na pia Mungu wao.

3 Na ikawa kwamba Moroni alichukua idadi ndogo ya watu, kulingana na matakwa ya Pahorani, na kuwapatia Lehi na Teankumu amri juu ya jeshi lake lililosalia, na akaanza mwendo wake kuelekea nchi ya Gideoni.

4 Na aliinua [a]bendera ya [b]uhuru mahali popote alipoingia, na akashinda jeshi lolote alililoliweza katika mwendo wake wote wa kishaji kuelekea nchi ya Gideoni.

5 Na ikawa kwamba maelfu walifuata uongozi wake, na kuchukua panga zao kwa kulinda uhuru wao, ili wasije utumwani.

6 Na hivyo, Moroni alipokuwa amekusanya pamoja watu wote vile alivyoweza wakati wa mwendo wake, alifika nchi ya Gideoni; na akiunganisha majeshi yake na yale ya Pahorani wakawa na nguvu sana, hata na nguvu kuliko watu wa Pako, ambaye alikuwa [a]mfalme wa wale waasi ambao walikuwa wamewafukuza watu [b]huru nje ya nchi ya Zarahemla na walikuwa wamechukua umiliki wa nchi.

7 Na ikawa kwamba Moroni na Pahorani walienda chini na majeshi yao katika nchi ya Zarahemla, na wakashambulia mji, na wakakutana na watu wa Pako, mpaka kwamba wakaanza vita.

8 Na tazama, Pako aliuawa na watu wake wakachukuliwa wafungwa, na Pahorani akarudishwa kwenye kiti chake cha hukumu.

9 Na watu wa Pako walipata hukumu yao, kulingana na sheria, na pia watu wa mfalme ambao walikuwa wamechukuliwa na kutupwa gerezani; na [a]waliuawa kulingana na sheria; ndiyo, wale watu wa Pako na wale watu wa mfalme, yeyote ambaye hangechukua silaha kulinda nchi yao, lakini apigane dhidi ya nchi, waliuawa.

10 Na hivyo ikawa ni lazima kwamba hii sheria izingatiwe

62 1*a* Alma 60:18.
4*a* Alma 46:12–13, 36.
MWM Bendera.
b MWM Huru, Uhuru.
6*a* Alma 61:4–8.
b Alma 51:5–7.
9*a* MWM Adhabu Kuu.

sana kwa usalama wa nchi yao; ndiyo, na yeyote aliyepatikana akikana uhuru wao aliuawa kwa haraka kulingana na sheria.

11 Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi; Moroni na Pahorani wakiwa wamerudisha amani katika nchi ya Zarahemla, miongoni mwa watu wao, wakiwa wamesababisha kuuawa kwa wale wote ambao hawakuwa na imani kwa chanzo cha uhuru.

12 Na ikawa katika mwanzo wa mwaka wa thelathini na moja wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, Moroni kwa haraka alisababisha kwamba vyakula vipelekwe, na pia jeshi la watu elfu sita lipelekwe kwa Helamani, kumsaidia kuhifadhi ile sehemu ya nchi.

13 Na pia akasababisha kwamba jeshi la watu elfu sita, na chakula cha kutosha, wapelekwe kwa majeshi ya Lehi na Teankumu. Na ikawa kwamba hii ilifanyika kuimarisha nchi dhidi ya Walamani.

14 Na ikawa kwamba Moroni na Pahorani, baada ya kuacha kundi kubwa la watu katika nchi ya Zarahemla, walishika mwendo wao na kundi kubwa la watu na wakaelekea nchi ya Nefiha, wakiwa wamekata kauli kuwashinda Walamani katika mji huo.

15 Na ikawa kwamba walipokuwa wakitembea kuelekea ile nchi, walichukua kundi kubwa la watu wa Walamani, na wakachinja wengi wao, na kuchukua vyakula vyao na silaha zao za vita.

16 Na ikawa baada ya kuwachukua, waliwasababisha kufanya agano nao kwamba kamwe hawatachukua silaha za vita dhidi ya Wanefi.

17 Na wakati walikuwa wameingia kwenye agano hili waliwatuma kuishi na watu wa Amoni, na walikuwa idadi ya karibu elfu nne ambao walikuwa hawajauawa.

18 Na ikawa kwamba walipowakubalia waondoke waliendelea na matembezi yao kuelekea nchi ya Nefiha. Na ikawa kwamba wakati walikuwa wamefikia mji wa Nefiha, walipiga hema zao kwenye tambarare ya Nefiha, ambayo iko karibu na mji wa Nefiha.

19 Sasa Moroni alitaka kwamba Walamani waje nje wapigane dhidi yao, kwenye tambarare; lakini Walamani, wakijua kuhusu ujasiri wao mkuu, na kuona ukubwa wa idadi yao, kwa hivyo hawakuthubutu kuja nje dhidi yao; kwa hivyo hawakuja kupigana siku hio.

20 Na wakati usiku ulipofika, Moroni alienda mbele katika giza la usiku, na kupanda ukuta kupeleleza ni sehemu gani ya mji Walamani waliweka kambi ya jeshi lao.

21 Na ikawa kwamba walikuwa katika upande wa mashariki, kando ya lango; na wote walikuwa wamelala. Na sasa Moroni alirudi kwenye jeshi lake, na kuwaagiza kwamba watayarishe kwa haraka kamba

nzito na ngazi, ziteremshwe kutoka juu ya ukuta hadi sehemu ya ndani ya ukuta.

22 Na ikawa kwamba Moroni alisababisha kwamba watu wake watembee mbele na waje juu ya ukuta, na wajiteremshe ndani ya sehemu ile ya ule mji, ndiyo, hata kwenye magharibi, ambapo Walamani hawakukaa na majeshi yao.

23 Na ikawa kwamba wote waliteremshwa kwenye mji wakati wa usiku, kwa kutumia kamba zao nzito na ngazi zao; hivyo wakati kulipokucha wote walikuwa ndani ya kuta za mji.

24 Na sasa, Walamani walipoamka na kuona kwamba majeshi ya Moroni yalikuwa ndani ya kuta, waliogopa kupita kiasi, mpaka kwamba wakakimbia kupitia kwenye lango la mji.

25 Na sasa wakati Moroni alipoona kwamba wanatoroka kutoka kwake, aligiza kwamba watu wake waende dhidi yao, na kuwaua wengi, na waliwazunguka wengine wengi, na kuwachukua wafungwa; na waliosalia walikimbilia nchi ya Moroni, ambayo ilikuwa kwenye mipaka kando ya ukingo wa bahari.

26 Hivyo Moroni na Pahorani walikamata tena mji wa Nefiha bila kupoteza nafsi moja; na kulikuwepo na Walamani wengi waliouawa.

27 Sasa ikawa kwamba wengi wa Walamani waliokuwa wafungwa walitaka kujiunga na [a]watu wa Amoni na kuwa watu huru.

28 Na ikawa kwamba kadiri wengi waliotamani, kwao ilikubaliwa kulingana na mapenzi yao.

29 Kwa hivyo, wafungwa wote wa Walamani walijiunga na watu wa Amoni, na walianza kufanya kazi sana, kulima ardhi, kukuza kila namna ya nafaka, na makundi na mifugo ya kila aina; na hivyo Wanefi waliondolewa mzigo mkubwa; ndiyo, mpaka kwamba walipumzishwa kutoka kwa wafungwa wote wa Walamani.

30 Sasa ikawa kwamba, baada ya Moroni kukamata mji wa Nefiha, akiwa amechukua wafungwa wengi, ambao walipunguza majeshi ya Walamani sana, na akiwa ameokoa Wanefi ambao walikuwa wamechukuliwa wafungwa, ambao waliimarisha jeshi la Moroni sana; kwa hivyo Moroni alienda mbele kutoka kwa nchi ya Nefiha hadi nchi ya Lehi.

31 Na ikawa kwamba wakati Walamani walipoona kwamba Moroni alikuwa anakuja dhidi yao, waliogopa tena na kulitoroka jeshi la Moroni.

32 Na ikawa kwamba Moroni na jeshi lake waliwafuata kutoka mji hadi mji, mpaka walipokutana na Lehi na Teankumu; na Walamani wakakimbia kutoka kwa Lehi na Teankumu, hata mpaka chini kwenye mipaka kando ya ukingo wa bahari, mpaka walipofika nchi ya Moroni.

33 Na majeshi ya Walamani

27*a* MWM Waanti-Nefi-Lehi.

yalijikusanya pamoja, mpaka yalikuwa kikundi kimoja katika nchi ya Moroni. Sasa Amoroni, mfalme wa Walamani, alikuwa nao pia.

34 Na ikawa kwamba Moroni na Lehi na Teankumu walikaa na majeshi yao karibu na mipaka ya nchi ya Moroni, mpaka kwamba Walamani walizungukwa karibu na mipaka kando ya nyika kusini, na kwenye mipaka kando ya nyika mashariki.

35 Na hivyo waliweka kambi usiku. Kwani tazama, Wanefi na Walamani walikuwa pia wamechoka kwa sababu ya matembezi marefu; kwa hivyo hawakukata kauli ya kutenda hila yoyote wakati wa usiku, isipokuwa Teankumu; kwani alikuwa amemkasirikia Amoroni sana, mpaka alifikiria kwamba Amoroni, na Amalikia kaka yake, walikuwa *a*kiini cha vita hivi virefu kati yao na Walamani, ambavyo vilikuwa mwanzo wa vita vingi na umwagaji wa damu, ndiyo, na njaa nyingi.

36 Na ikawa kwamba Teankumu kwa hasira yake alienda kwenye kambi ya Walamani, na kujiteremsha chini kwenye ukuta wa mji. Na akaenda mbele na kamba, kutoka mahali hadi pengine, mpaka alipompata mfalme; na akatupa *a*sagai kwake, ambayo ilimchoma karibu na moyo. Lakini tazama, mfalme aliamsha watumishi wake kabla ya kufa, mpaka kwamba wakamfuata Teankumu, na kumuua.

37 Sasa ikawa kwamba wakati Lehi na Moroni walipojua kwamba Teankumu amekufa walihuzunika sana; kwani tazama, alikuwa mtu ambaye alipigana kwa ushujaa sana kwa ajili ya nchi yake, ndiyo, rafiki wa kweli wa uhuru; na aliumia mateso mabaya mengi. Lakini tazama, alikuwa amekufa, na alienda njia ya kawaida ya binadamu.

38 Sasa ikawa kwamba Moroni alienda mbele kesho yake, na kuwashambulia Walamani, mpaka kwamba waliwaua mauaji makuu; na waliwafukuza kutoka nchini; na walikimbia, hata kwamba hawakurudi wakati huo dhidi ya Wanefi.

39 Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini na moja wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi; na hivyo walikuwa wamekuwa na vita, na umwagaji wa damu, na njaa, na mateso, kwa muda wa miaka mingi.

40 Na kulikuwa na mauaji, na mabishano, na mafarakano, na kila namna yote ya uovu miongoni mwa watu wa Nefi; walakini kwa faida ya wale walio *a*haki, ndiyo, kwa sababu ya sala za walio haki, waliachiliwa.

41 Lakini tazama, kwa sababu ya muda mrefu wa vita miongoni mwa Wanefi na Walamani wengi walikuwa wamefanywa kuwa na roho ngumu, kwa sababu ya vita virefu; na wengi walilainishwa kwa sababu ya *a*mateso yao, mpaka kwamba

35*a* Alma 48:1.
36*a* Alma 51:33–34.
40*a* Alma 45:15–16.
41*a* MWM Shida.

wakajinyenyekeza mbele ya Mungu, hata unyenyekevu wa ndani.

42 Na ikawa kwamba baada ya Moroni kuimarisha hizo sehemu za nchi ambazo zilikuwa wazi zaidi kwa Walamani, mpaka walipopata nguvu ya kutosha, alirudi mji wa Zarahemla; na pia Helamani alirudi mahali pake pa urithi; na kukawa tena amani miongoni mwa watu wa Nefi.

43 Na Moroni aliweka mamlaka ya majeshi katika mikono ya mwana wake, ambaye jina lake lilikuwa Moroniha; na akastaafu na kurudi nyumbani kwake kwamba atumie siku zake za mwisho kwa amani.

44 Na Pahorani alirudia kiti chake cha hukumu; na Helamani alichukua tena jukumu la kuwahubiria watu neno la Mungu; kwani kwa sababu ya vita vingi na mabishano ilikuwa imekuwa muhimu kwamba msimamo uwekwe tena kanisani.

45 Kwa hivyo, Helamani na ndugu zake walienda mbele, na kutangaza neno la Mungu kwa uwezo mwingi kwa [a]kusadikisha watu wengi juu ya uovu wao, ambayo iliwafanya wakatubu dhambi zao na kubatizwa kwa Bwana Mungu wao.

46 Na ikawa kwamba walianzisha tena kanisa la Mungu, kote nchini.

47 Ndiyo, na msimamo uliwekwa kuhusu sheria. Na [a]waamuzi wao, na waamuzi wao wakuu walichaguliwa.

48 Na watu wa Nefi walianza [a]kufanikiwa tena katika nchi, na wakaanza kuongezeka na kuwa na nguvu sana nchini. Na wakaanza kutajirika sana.

49 Lakini ijapokuwa utajiri wao, au nguvu yao, au mafanikio yao, hawakujiinua kwa kiburi machoni mwao; wala hawakuwa wavivu wa kumkumbuka Bwana Mungu wao; lakini walijinyenyekeza sana mbele yake.

50 Ndiyo, walikumbuka vitu gani vikubwa ambavyo Bwana aliwafanyia, kwamba alikuwa amewakomboa kutoka kifo, na kutoka kifungoni, na kutoka magerezani, na kutoka kila aina ya mateso, na alikuwa amewakomboa kutoka katika mikono ya maadui zao.

51 Na waliomba kwa Bwana Mungu wao siku zote, mpaka kwamba Bwana aliwabariki, kulingana na neno lake, kwamba walikuwa na nguvu na kufanikiwa nchini.

52 Na ikawa kwamba vitu hivi vyote vilifanyika. Na Helamani akafariki, katika mwaka wa thelathini na tano wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

MLANGO WA 63

Shibloni na baadaye Helamani wanachukua maandishi matakatifu—Wanefi wengi wanasafiri kwenda katika nchi ya kaskazini—Hagothi anajenga merikebu, ambayo inaenda kwa bahari ya

45*a* M&M 18:44. | 47*a* Mos. 29:39. | 48*a* Alma 50:20.

magharibi—Moroniha anashinda Walamani kwenye vita. Karibia mwaka 56–52 K.K.

Na ikawa katika mwanzo wa mwaka wa thelathini na sita wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, kwamba [a]Shibloni alichukua hivyo vitu vyote [b]vitakatifu ambavyo vilitolewa kwa Helamani na Alma.

2 Na alikuwa mtu mwenye haki, na alitembea wima mbele ya Mungu; na alitazamia kutenda mema siku zote, kutii amri za Bwana Mungu wake; na pia kaka yake alifanya hivyo.

3 Na ikawa kwamba Moroni alifariki pia. Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini na sita wa utawala wa waamuzi.

4 Na ikawa kwamba katika mwaka wa thelathini na saba wa utawala wa waamuzi, kulikuwa na kundi kubwa la watu, hata kwa idadi ya elfu tano na mia nne ya watu, na wake zao na watoto wao, waliondoka nje ya nchi ya Zarahemla hadi kwenye nchi ambayo ilikuwa upande wa [a]kaskazini.

5 Na ikawa kwamba Hagothi, yeye akiwa mtu mchunguzi sana, kwa hivyo alienda mbele na akajenga merikebu kubwa sana, kwenye mipaka ya nchi ya Neema, kando ya nchi ya Ukiwa, na akaishusha ndani ya bahari ya magharibi, kando na [a]mkondo wa nchi ambao ulielekea nchi iliyokuwa upande wa kaskazini.

6 Na tazama, walikuwepo Wanefi wengi miongoni mwao ambao waliingia ndani na kusafiri mbele na vyakula vingi, na pia wanawake wengi na watoto; na walisafiri kuelekea kaskazini. Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini na saba.

7 Na katika mwaka wa thelathini na nane, huyu mtu alijenga merikebu zingine. Na merikebu ya kwanza pia ilirejea, na watu wengi zaidi waliingia ndani yake; na pia walichukua vyakula vingi, na kuanza safari tena kuelekea nchi ya kaskazini.

8 Na ikawa kwamba hawakusikika tena. Na tunadhani kwamba walizama ndani ya kina cha bahari. Na ikawa kwamba merikebu nyingine pia ilisafiri mbele; na mahali ilipoenda hatujui.

9 Na ikawa kwamba katika mwaka huu kulikuwa na watu wengi walioenda katika nchi upande wa [a]kaskazini. Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini na nane.

10 Na ikawa katika mwaka wa thelathini na tisa wa utawala wa waamuzi, Shibloni alikufa pia, na Koriantoni alikuwa ameenda kwenye nchi ya kaskazini ndani ya merikebu, kupeleka vyakula kwa watu ambao walikuwa wameenda katika nchi ile.

11 Kwa hivyo ilikuwa muhimu kwa Shibloni kupeleka vitu

63 1*a* Alma 38:1–2.
b Alma 37:1–12.
MWM Takatifu.
4*a* Alma 22:31.
5*a* Alma 22:32; Eth. 10:20.
9*a* Hel. 3:11–12.

hivyo vitakatifu kabla ya kifo chake, kumkabidhi mwana wa [a]Helamani, ambaye alikuwa Helamani, akiitwa baada ya jina la baba yake.

12 Sasa tazama, ile [a]michoro yote ambayo ilikuwa kwa ulinzi wa Helamani iliandikwa na kupelekwa miongoni mwa watoto wa watu kote nchini, isipokuwa hizo sehemu ambazo zilikuwa zimeamriwa na Alma [b]zisidhihirishwe.

13 Walakini, hivi vitu vilitakiwa kuwekwa wakfu, na [a]kutolewa kutoka uzao mmoja hadi mwingine; kwa hivyo, katika mwaka huu, vilikuwa vimekabidhiwa Helamani, kabla ya kifo cha Shibloni.

14 Na ikawa pia katika mwaka huu kwamba kulikuwa na waasi ambao walikuwa wamewaendea Walamani; na wakavurugwa tena na kukasirika dhidi ya Wanefi.

15 Na pia katika mwaka huo walikuja na jeshi kubwa kupigana vita dhidi ya watu wa [a]Moroniha, au dhidi ya jeshi la Moroniha, ambapo walipigwa na kurudishwa nyuma tena kwa nchi zao, wakipoteza na kuumia sana.

16 Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

17 Na hivyo ikaisha historia ya Alma, na Helamani mwana wake, na pia Shibloni, ambaye alikuwa mwana wake.

KITABU CHA HELAMANI

Historia ya Wanefi. Vita vyao na mabishano, na mafarakano yao. Na pia unabii wa manabii wengi watakatifu, kabla ya ujio wa Kristo, kulingana na maandishi ya Helamani, ambaye alikuwa mwana wa Helamani, na pia kulingana na maandishi ya wanawe, hata mpaka kuja kwa Kristo. Na pia wengi wa Walamani wanaongoka. Maelezo ya uongofu wao. Maelezo ya haki ya Walamani, na uovu na machukizo ya Wanefi, kulingana na maandishi ya Helamani na wanawe, hata mpaka ujio wa Kristo, ambacho kinaitwa kitabu cha Helamani, na kadhalika.

MLANGO WA 1

Pahorani wa pili anakuwa mwamuzi mkuu na anauawa na Kishkumeni—Pakumeni anachukua kiti cha hukumu—Koriantumuri anaongoza majeshi ya Walamani, anateka Zarahemla, na anamuua Pakumeni—Moroniha anawashinda Walamani na kuteka tena Zarahemla, na Koriantumuri anauawa. Karibia mwaka 52–50 K.K.

11 *a* Tazama kichwa cha kitabu cha Helamani.

12 *a* Alma 18:36.
b Alma 37:27–32.

13 *a* Alma 37:4.

15 *a* Alma 62:43.

NA sasa tazama, ikawa katika mwanzo wa mwaka wa arubaini wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, kulianza kuwa na taabu kubwa miongoni mwa watu wa Wanefi.

2 Kwani tazama, [a]Pahorani alikuwa amefariki, na kwenda njia ya kawaida ya ulimwengu; kwa hivyo kulianza kuwa na ubishi kuhusu ni nani atakayechukua kiti cha hukumu miongoni mwa kaka, ambao walikuwa wana wa Pahorani.

3 Sasa haya ndiyo majina ya wale ambao walishindania kiti cha hukumu, ambao pia walisababisha watu kugombana: Pahorani, Paanki, na Pakumeni.

4 Sasa hawa sio wana wote wa Pahorani (kwani alikuwa na wengi), lakini hawa ndiyo wale ambao walishindania kiti cha hukumu; kwa hivyo, walianzisha migawanyiko mitatu miongoni mwa watu.

5 Walakini, ikawa kwamba Pahorani alichaguliwa kwa [a]sauti ya watu kuwa mwamuzi mkuu na mtawala juu ya watu wa Nefi.

6 Na ikawa kwamba wakati Pakumeni alipoona kwamba hangepata kiti cha hukumu, alikubaliana na sauti ya watu.

7 Lakini tazama, Paanki, na sehemu ya watu ambao walitaka kwamba awe mtawala wao, walikasirika sana; kwa hivyo, alikuwa karibu kuwachochea hao watu kuasi dhidi ya ndugu zao.

8 Na ikawa kwamba vile alipokuwa karibu kufanya hivi, tazama, alikamatwa, na kujaribiwa kulingana na sauti ya watu, na kuhukumiwa kifo; kwani alikuwa ameasi na alitaka kuangamiza [a]uhuru wa watu.

9 Sasa wakati wale watu ambao walitaka kwamba awe mtawala wao walipoona kwamba amehukumiwa kifo, kwa hivyo walikasirika, na tazama, walimtuma mtu mmoja kwa jina la Kishkumeni, kwenda kwa kiti cha hukumu cha Pahorani, na kumuua Pahorani wakati alipokuwa amekalia kiti cha hukumu.

10 Na akafukuzwa na watumishi wa Pahorani; lakini tazama, mwendo wa Kishkumeni ulikuwa wa kasi sana kwamba mtu yeyote hangemshika.

11 Na akarudi kwa wale ambao walimtuma, na wote wakaingia katika agano, ndiyo, wakiapa kwa Muumba wao asiye na mwisho, kwamba hawatamwambia yeyote kwamba Kishkumeni alikuwa amemuua Pahorani.

12 Kwa hivyo, Kishkumeni hakujulikana miongoni mwa watu wa Nefi, kwani alikuwa amejigeuza wakati ambao alimuua Pahorani. Na Kishkumeni na kundi lake, ambao walikuwa wamefanya agano naye, walijichanganya miongoni mwa watu, kwa njia kwamba hawangeweza kupatikana; lakini wale waliopatikana walihukumiwa [a]kifo.

1 2*a* Alma 50:40.
5*a* Mos. 29:26–29.
8*a* MWM Huru, Uhuru.
12*a* MWM Adhabu Kuu.

13 Na sasa tazama, Pakumeni alichaguliwa, kulingana na sauti ya watu, kuwa mwamuzi mkuu na mtawala juu ya watu, kutawala mahali pa kaka yake Pahorani; na ilikuwa kulingana na haki yake. Na hayo yote yalifanyika katika mwaka wa arubaini wa utawala wa waamuzi; na yalikuwa na mwisho.

14 Na ikawa katika mwaka wa arubaini na moja wa utawala wa waamuzi, kwamba Walamani walikuwa wamekusanya pamoja jeshi kubwa wasiohesabika la watu, na kuwahami kwa panga, na kwa vitara na kwa pinde, na kwa mishale, na kwa vyapeo, na kwa dirii, na kwa kila namna ya ngao ya kila aina.

15 Na walikuja tena ili waanzishe vita dhidi ya Wanefi. Na waliongozwa na mtu ambaye jina lake lilikuwa Koriantumuri; na alikuwa wa uzao wa Zarahemla; na alikuwa mwasi kutoka miongoni mwa Wanefi; na alikuwa mtu mkubwa na mwenye nguvu.

16 Kwa hivyo, mfalme wa Walamani, ambaye jina lake lilikuwa Tubalothi, ambaye alikuwa mwana wa [a]Amoroni, alidhani kwamba Koriantumuri, akiwa na nguvu nyingi, angeweza kusimama dhidi ya Wanefi, na nguvu zake na pia hekima yake kuu, mpaka kwamba kwa kumtuma yeye mbele angepata uwezo juu ya Wanefi—

17 Kwa hivyo aliwachochea kuwa na hasira, na akakusanya pamoja majeshi yake, na kumweka Koriantumuri kuwa kiongozi wao, na kuwasababisha kwenda chini kwenye nchi ya Zarahemla kupigana dhidi ya Wanefi.

18 Na ikawa kwamba kwa sababu ya ubishi mwingi na taabu nyingi serikalini, kwamba hawakuwa wameweka walinzi wa kutosha katika nchi ya Zarahemla; kwani walikuwa wamefikiri kwamba Walamani hawangekuja hadi katikati ya nchi yao kushambulia huo mji mkubwa wa Zarahemla.

19 Lakini ikawa kwamba Koriantumuri alitembea mbele ya jeshi lake kubwa, na kuwafikia wakazi wa mji, na mwendo wao ulikuwa wa kasi sana kiasi kwamba hapakuweko na nafasi ya Wanefi kukusanya majeshi yao pamoja.

20 Kwa hivyo Koriantumuri aliua walinzi wa lango la mji, na akaenda mbele na jeshi lake lote hadi kwenye mji, na wakamuua yeyote aliyewapinga, mpaka kwamba wakamiliki mji wote.

21 Na ikawa kwamba Pakumeni, ambaye alikuwa mwamuzi mkuu, alitoroka mbele ya Koriantumuri, hata akafikia kuta za mji. Na ikawa kwamba Koriantumuri alimpiga kwenye ukuta, mpaka akafa. Na hivyo siku za Pakumeni zikaisha.

22 Na sasa wakati Koriantumuri alipoona kwamba amemiliki mji wa Zarahemla, na kuona kwamba Wanefi

16*a* Alma 52:3.

wamewatoroka, na wameuawa, na wamekamatwa, na wametupwa gerezani, na kwamba amepata uwezo juu ya mji wenye nguvu sana katika nchi yote, moyo wake ulipata ujasiri mpaka kwamba alikuwa karibu kwenda dhidi ya nchi yote.

23 Na sasa hakukawia kwenye nchi ya Zarahemla, lakini alienda na jeshi kubwa, hata na kuelekea kwenye mji wa Neema; kwani nia yake ilikuwa kwenda mbele na kupata njia yake kwa kutumia upanga, ili aweze kupata sehemu za kaskazini ya nchi.

24 Na, akidhani kwamba nguvu zao kubwa zilikuwa katikati ya nchi, kwa hivyo alienda mbele, bila kuwapatia nafasi ya kujikusanya wenyewe pamoja isipokuwa tu kwa vikundi vidogo; na kwa njia hii waliwashukia na kuwatupa chini ardhini.

25 Lakini tazama, huu mwendo wa Koriantumuri kupita katikati ya nchi ulimpa Moroniha faida kubwa juu yao, ingawa idadi kubwa ya Wanefi waliouawa.

26 Kwani tazama, Moroniha alikuwa amedhani kwamba Walamani hawangethubutu kuja katikati ya nchi, lakini kwamba wangeshambulia miji iliyo karibu na mipaka vile walivyokuwa wamefanya hapo awali; kwa hivyo Moroniha alikuwa ameamuru kwamba majeshi yao yenye nguvu yalinde sehemu hizo karibu na kando ya mipaka.

27 Lakini tazama, Walamani hawakuogopa kulingana na kusudi lake, lakini walikuwa wamekuja katikati ya nchi, na walikuwa wamekamata mji mkuu ambao ulikuwa Zarahemla, na walikuwa wanapitia katika sehemu nyingi kubwa za nchi, wakiwaua watu na mauaji makubwa, wote wanaume, wanawake, na watoto, wakimiliki miji mingi na ngome nyingi.

28 Lakini Moroniha alipogundua hii, mara moja alimtuma Lehi na jeshi kuwazunguka na kuwazuia kabla ya kufika nchi ya Neema.

29 Na hivyo ndivyo alivyofanya; na aliwazuia kabla ya hao kufikia nchi ya Neema, na akakabiliana nao, mpaka kwamba wakaanza kurudi nyuma kuelekea nchi ya Zarahemla.

30 Na ikawa kwamba Moroniha aliwazuia kukimbia, na akakabiliana nao, mpaka kwamba kukawa na vita vya kumwaga damu nyingi; ndiyo, wengi waliuawa, na miongoni mwa idadi ya waliouawa [a]Koriantumuri alipatikana miongoni mwao.

31 Na sasa, tazama, Walamani hawakuweza kurudi nyuma upande wowote, upande wa kaskazini, wala kusini, wala mashariki, wala magharibi, kwani walizungukwa kila upande na Wanefi.

32 Na hivyo Koriantumuri alikuwa amewatumbukiza

30*a* Hel. 1:15.

Walamani katikati ya Wanefi, mpaka kwamba walikuwa chini ya uwezo wa Wanefi, na yeye mwenyewe akauawa, na Walamani wakajisalimisha kwa Wanefi.

33 Na ikawa kwamba Moroniha alichukua tena mji wa Zarahemla, na kuamuru kwamba Walamani ambao walikuwa wameshikiliwa mahabusu wakubaliwe kutoka nchini kwa amani.

34 Na hivyo ukaisha mwaka wa arubaini na moja wa utawala wa waamuzi.

MLANGO WA 2

Helamani, mwana wa Helamani, anakuwa mwamuzi mkuu—Gadiantoni anaongoza kikundi cha Kishkumeni—Mtumishi wa Helamani anamuua Kishkumeni, na kundi la Gadiantoni linatorokea nyikani. Karibia mwaka 50–49 K.K.

Na ikawa katika mwaka wa arubaini na mbili wa utawala wa waamuzi, baada ya Moroniha kuanzisha tena amani miongoni mwa Wanefi na Walamani, tazama hakukuwa na yeyote wa kuchukua kiti cha hukumu; kwa hivyo kulianza kuwa na ubishi tena miongoni mwa watu kuhusu ni nani atakayechukua kiti cha hukumu.

2 Na ikawa kwamba Helamani, ambaye alikuwa mwana wa Helamani, alichaguliwa kuchukua kiti cha hukumu, kwa sauti ya watu.

3 Lakini tazama, [a]Kishkumeni, ambaye alimuua Pahorani, alivizia kumwangamiza Helamani pia; na alisaidiwa na kundi lake, ambao walikuwa wameingia katika agano kwamba uovu wake usijulikane na yeyote.

4 Kwani kulikuwa na mtu mmoja aliyejulikana kama [a]Gadiantoni, ambaye alikuwa stadi sana kwa maneno mengi, na pia kwa hila yake, kutenda kazi yake ya siri ya mauaji na unyang'anyi; kwa hivyo, alikuwa kiongozi wa kundi la Kishkumeni.

5 Kwa hivyo aliwadanganya, na pia Kishkumeni, kwamba ikiwa watampatia kiti cha hukumu angewakubalia wale ambao walikuwa wa kundi lake kwamba wangewekwa kwenye uwezo na mamlaka miongoni mwa watu; kwa hivyo Kishkumeni alitafuta kumwangamiza Helamani.

6 Na ikawa kwamba aliposonga mbele kuelekea kwenye kiti cha hukumu ili kumwangamiza Helamani, tazama mmoja wa watumishi wa Helamani, ambaye alikuwa nje usiku, na akiwa amepata, taarifa ya mipango hiyo kwa njia ya kujibadilisha ambayo ilikuwa imewekwa na hili kundi kumwangamiza Helamani—

7 Na ikawa kwamba alikutana na Kishkumeni, na kumwonyesha ishara; kwa hivyo Kishkumeni alitambua nia ya mahitaji yake, akitaka kwamba amsaidie

2 3*a* Hel. 1:9. | 4*a* MWM Wanyang'anyi wa Gadiantoni.

kufika kwenye kiti cha hukumu ili amuue Helamani.

8 Na wakati mtumishi wa Helamani alipojua lengo lote la Kishkumeni, na vile kusudi lake lilikuwa kuua, na pia kwamba kusudi la wote ambao walikuwa wa kundi lake lilikuwa ni kuua, na kunyang'anya, na kupata mamlaka, (na huu ulikuwa mpango wao wa [a]siri, na shirika lao) mtumishi wa Helamani akamwambia Kishkumeni: Acha twende kwenye kiti cha hukumu.

9 Sasa hii ilimpendeza Kishkumeni sana, kwani aliona kwamba atatimiza kusudi lake; lakini tazama, vile walipokuwa wanaenda mbele kwenye kiti cha hukumu, mtumishi wa Helamani alimchoma kisu Kishkumeni, hata mpaka kwenye moyo, kwamba alianguka na kufa bila kugumia. Na alikimbia na kumwambia Helamani vitu vyote ambavyo alikuwa ameviona, na kusikia, na kufanywa.

10 Na ikawa kwamba Helamani alituma walinzi kushika hili kundi la wezi na wauaji wa siri, ili wauawe kulingana na sheria.

11 Lakini tazama, wakati Gadiantoni alipogundua kwamba Kishkumeni hakurudi aliogopa kwamba asije akaangamizwa; kwa hivyo aliamuru kundi lake limfuate. Na walikimbia kutoka nchini, kwa njia ya siri, hadi kwenye nyika; na hivyo wakati Helamani alipotuma wachukuliwe hawakupatikana.

12 Na mengine ya huyu Gadiantoni yatazungumzwa baadaye. Na hivyo ukaisha mwaka wa arubaini na mbili wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

13 Na tazama, mwishoni mwa kitabu hiki mtaona kwamba [a]Gadiantoni alithibitisha upinduzi, ndiyo, karibu kuangamizwa kwote wa watu wa Nefi.

14 Tazama simaanishi mwisho wa kitabu hiki cha Helamani, lakini mwisho wa kitabu cha Nefi, ambamo nimepata historia yote ambayo nimeandika.

MLANGO WA 3

Wanefi wengi wanahamia kwenye nchi iliyopo kaskazini—Wanajenga nyumba za saruji na wanaandika kumbukumbu nyingi—Maelfu wanaongoka na kubatizwa—Neno la Mungu linawaongoza watu kwenye wokovu—Nefi mwana wa Helamani anachukua kiti cha hukumu. Karibia mwaka 49–39 K.K.

Na sasa ikawa katika mwaka wa arubaini na tatu wa utawala wa waamuzi, hakukuwa na ubishi miongoni mwa watu wa Nefi isipokuwa kiburi kidogo ambacho kilikuwa kanisani, ambacho kilianzisha mafarakano madogo miongoni mwa watu, mambo ambayo yalirekebishwa mwishoni mwa mwaka wa arubaini na tatu.

2 Na hapakuweko na ubishi

8*a* 2 Ne. 10:15.
MWM Makundi maovu ya siri.
13*a* Hel. 6:18; 4 Ne. 1:42.

miongoni mwa watu katika mwaka wa arubaini na nne; wala hapakuweko ubishi mwingi katika mwaka wa arubaini na tano.

3 Na ikawa katika mwaka wa arubaini na sita, ndiyo, kulikuwa na mafarakano mengi na ugomvi mwingi; hata kwamba kulikuwa na wengi sana ambao waliondoka nchi ya Zarahemla, na kwenda kwenye nchi ya upande wa [a]kaskazini kurithi nchi.

4 Na walisafiri kwa mwendo mrefu sana, mpaka kwamba wakafika kwenye maziwa [a]makubwa na mito mingi.

5 Ndiyo, na hata walitawanyika katika sehemu zote za nchi, katika sehemu zozote ambazo hazikuwa zimefanywa kuwa na ukiwa na bila miti, kwa sababu ya wakazi wengi ambao hapo kabla walikuwa wamerithi nchi ile.

6 Na sasa hakukuwa na sehemu yeyote ya nchi ambayo ilikuwa ya ukiwa, isipokuwa pale pasipokuwa na miti; lakini kwa sababu ya [a]kuangamizwa watu wengi walioishi nchini hapo kabla iliitwa [b]ukiwa.

7 Na kwa vile kulikuwa na miti michache tu nchini, hata hivyo watu walioenda huko walipata kuwa na ujuzi mwingi kwa kutumia saruji; kwa hivyo walijenga nyumba za saruji, ambamo waliishi.

8 Na ikawa kwamba waliongezeka na kutawanyika, na wakasonga mbele kutoka nchi ya upande wa kusini hadi nchi ya upande wa kaskazini, na wakaenea hata kwamba wakaanza kufunika uso wote wa ulimwengu, kutoka bahari ya kusini hadi bahari ya kaskazini, kutoka [a]bahari ya magharibi hadi bahari ya mashariki.

9 Na watu waliokuwa katika nchi ya upande wa kaskazini waliishi kwenye hema, na kwenye nyumba za saruji, na waliachilia mti wa aina yoyote uliomea juu ya ardhi ya nchi kwamba ukue, ili kwa muda ujao wangepata miti ya kujengea nyumba zao, ndiyo, miji yao, na mahekalu yao, na masinagogi yao, na mahali pao patakatifu, na aina yote ya majengo yao.

10 Na ikawa kwa vile miti ilikuwa michache katika nchi ya upande wa kaskazini, walisafirisha mingi kwa kutumia [a]meli.

11 Na hivyo waliwezesha watu waliokuwa kwenye nchi ya upande wa kaskazini kujenga miji mingi, yote ya miti na saruji.

12 Na ikawa kwamba kulikuwa na watu wengi wa [a]watu wa Amoni, ambao walikuwa Walamani kwa kuzaliwa, ambao pia walienda kwenye nchi hii.

13 Na sasa kuna kumbukumbu nyingi juu yao ambazo zimeandikwa za historia ya watu hawa ambazo ni mahsusi na kubwa sana kuwahusu.

14 Lakini tazama, sehemu

3 3*a* Alma 63:4.
4*a* Mos. 8:8; Morm. 6:4.
6*a* Mos. 21:25–27.
b Alma 22:31.
8*a* Alma 22:27, 32.
10*a* Alma 63:5–8.
12*a* Alma 27:21–26.

moja ya mia ya historia ya watu hawa, ndiyo, historia ya Walamani na Wanefi, na vita vyao, na mabishano, na mafarakano, na mahubiri yao, na unabii wao, na meli zao na uundaji wa meli zao, na ujenzi wao wa [a]mahekalu, na ya masinagogi yao na mahali pao patakatifu, na haki yao, na uovu wao, na mauaji yao, na uporaji wao, na unyang'anyi wao, na aina yote ya machukizo na ukahaba, hauwezi kuwekwa wote kwenye maandishi haya.

15 Lakini tazama, kuna vitabu vingi na maandishi mengi ya kila aina, na ameandikwa zaidi na Wanefi.

16 Na [a]kukabidhiana kutoka kizazi kimoja hadi kingine na Wanefi, hata mpaka wameanza kutenda dhambi na wameuawa, kuporwa, na kuwindwa, na kufukuzwa, na kuuawa, na kutawanywa usoni mwa ulimwengu, na kuchanganywa na Walamani mpaka [b]hawaitwi tena Wanefi, wakiwa waovu, na washenzi, na wakatili, ndiyo, hata kuwa Walamani.

17 Na sasa narudia tena historia yangu; kwa hivyo, yale ambayo nimyaesema yalifanyika baada ya kuweko mabishano makuu, na misukosuko, na vita, na mafarakano, miongoni mwa watu wa Nefi.

18 Mwaka wa arubaini na sita wa utawala wa waamuzi uliisha;

19 Na ikawa kwamba kulikuwa bado na ubishi mkubwa nchini, ndiyo, hata katika mwaka wa arubaini na saba, na pia mwaka wa arubaini na nane.

20 Walakini Helamani alichukua kiti cha hukumu kwa haki na uadilifu; ndiyo, alichunga na kutii sheria na uamuzi, na amri za Mungu; na alifanya kile kilichokuwa cha haki machoni mwa Mungu siku zote; na alikuwa na mwendo sawa na baba yake, mpaka kwamba alifanikiwa nchini.

21 Na ikawa kwamba alikuwa na wana wawili. Alimwita yule mkubwa kwa jina la [a]Nefi, na mdogo, kwa jina la [b]Lehi. Na walianza kukua wakimtii Bwana.

22 Na ikawa kwamba vita na mabishano yalianza kupungua, kidogo, miongoni mwa watu wa Wanefi, katika mwisho wa mwaka wa arubaini na nane wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

23 Na ikawa katika mwaka wa arubaini na tisa wa utawala wa waamuzi, kuliimarishwa amani ya kudumu katika nchi, yote isipokuwa makundi maovu ya siri ambayo [a]Gadiantoni mwizi alikuwa ameanzisha katika sehemu za nchi ambazo zilikuwa zimekaliwa kwa wingi, ambazo wakati huo hazikuwa zimejulikana kwa viongozi wa serikali; kwa hivyo hawakuangamizwa kutoka nchini.

24 Na ikawa kwamba katika

14 *a* 2 Ne. 5:16; Yak. (KM) 1:17; 3 Ne. 11:1.
16 *a* 1 Ne. 5:16–19; Alma 37:4.
b Alma 45:12–14.
21 *a* MWM Nefi, Mwana wa Helamani.
b MWM Lehi, Mmisionari wa Kinefi.
23 *a* Hel. 2:4.

mwaka huo huo kulikuwa na mafanikio mengi sana katika kanisa, kiasi kwamba kulikuwa na maelfu waliojiunga na kanisa na walibatizwa ubatizo wa toba.

25 Na mafanikio ya kanisa yalikuwa mengi sana, na baraka nyingi zilipokelewa na watu, kwamba hata makuhani wakuu na walimu wenyewe walishangaa kupita kiasi.

26 Na ikawa kwamba kazi ya Bwana ilifanikiwa na watu wengi kubatizwa na kuunganishwa kwa kanisa la Mungu, ndiyo, hata makumi ya maelfu.

27 Hivyo tunaweza kuona kwamba Bwana ana huruma kwa wote ambao, kwa uaminifu wa mioyo yao, wanaolingana kwa jina lake takatifu.

28 Ndiyo, hivyo tunaona kwamba [a]mlango wa mbinguni umefunguliwa kwa [b]wote, hata kwa wale ambao wataamini katika jina la Yesu Kristo, ambaye ni Mwana wa Mungu.

29 Ndiyo, tunaona kwamba yeyote atakaye angelishikilia [a]neno la Mungu, ambalo ni [b]jepesi na lenye nguvu, ambalo litaangamiza ujanja wote na mitego na hila za ibilisi, na kumwongoza mfuasi wa Kristo katika njia iliyosonga na [c]nyembamba mpaka ng'ambo ya [d]shimo la dhiki lisilo na mwisho ambalo limetayarishwa kumeza waovu—

30 Na kuangusha roho zao, ndiyo, roho zao zisizokufa, katika [a]mkono wa kuume wa Mungu katika ufalme wa mbinguni, kuketi chini na Ibrahimu, na Isaka, na Yakobo, na babu zetu wote watakatifu, ambako hawataondoka tena milele.

31 Na katika mwaka huu kulikuwa na furaha ya kudumu katika nchi ya Zarahemla, na katika nchi zote zilizokuwa karibu, hata kwenye nchi yote ambayo ilimilikiwa na Wanefi.

32 Na ikawa kwamba kulikuwa na amani na shangwe kubwa katika mwisho wa mwaka wa arubaini na tisa; ndiyo, na pia kulikuwa na amani ya kudumu na shangwe nyingi katika mwaka wa hamsini wa utawala wa waamuzi.

33 Na katika mwaka wa hamsini na moja wa utawala wa waamuzi kulikuwa na amani pia, isipokuwa tu kiburi ambacho kilianza kuingia kanisani—sio katika kanisa la Mungu, lakini katika mioyo ya watu ambao walidai kuwa wa kanisa la Mungu—

34 Na waliinuka kwa [a]kiburi, hata kwenye kudhulumu ndugu zao wengi. Sasa huu ulikuwa uovu mkubwa, ambao ulisababisha sehemu kubwa ya walio wanyenyekevu kuumia udhalimu mkuu, na kuvumilia mateso mengi.

35 Walakini [a]walifunga na [b]kuomba kila wakati, na wa-

28*a* 2 Ne. 31:9, 17.
b Mdo. 10:28; Rum. 2:10–11.
29*a* MWM Neno la Mungu.
b Ebr. 4:12; M&M 11:2.
c 2 Ne. 9:41; 33:9.
d 1 Ne. 15:28–30.
30*a* Mt. 25:33–34.
34*a* MWM Kiburi.
35*a* MWM Funga, Kufunga.
b MWM Sala.

kapokea nguvu kwa wingi katika [c]unyenyekevu wao, na wakawa imara zaidi na imara katika imani ya Kristo, hadi nafsi zao jikajazwa na shangwe na faraja, ndiyo, hata kwenye [d]kusafishwa na [e]utakaso wa mioyo yao, utakaso ambao huja kwa sababu ya wao [f]kumtolea Mungu mioyo yao.

36 Na ikawa kwamba mwaka wa hamsini na mbili uliisha kwa amani pia, isipokuwa kiburi kikubwa ambacho kilikuwa kimeingia katika mioyo ya watu; na ilikuwa kwa sababu ya [a]utajiri wao mwingi na kufanikiwa kwao nchini; na kiliendelea kukua ndani yao kutoka siku hadi siku.

37 Na ikawa katika mwaka wa hamsini na tatu wa utawala wa waamuzi, Helamani alifariki, na mwana wake wa kwanza Nefi akaanza kutawala badala yake. Na ikawa kwamba alichukua kiti cha hukumu kwa haki na uadilifu; ndiyo, alitii amri za Mungu, na alienenda katika njia za baba yake.

MLANGO WA 4

Wanefi walioasi na Walamani wanaunganisha majeshi na kuteka nchi ya Zarahemla—Kushindwa kwa Wanefi kunatokea kwa sababu ya uovu wao—Kanisa linafifia, na watu wanakuwa dhaifu kama Walamani. Karibia mwaka 38–30 K.K.

Na ikawa katika mwaka wa hamsini na nne kulikuwa na mafarakano mengi kanisani, na kulikuwa na [a]ubishi pia miongoni mwa watu, mpaka kwamba kukawa na umwagaji mwingi wa damu.

2 Na sehemu ile ya wahalifu waliuawa na kufukuzwa kutoka nchini, na wakamwendea mfalme wa Walamani.

3 Na ikawa kwamba walijaribu kuwa chochea Walamani kupigana dhidi ya Wanefi; lakini tazama, Walamani waliogopa sana, kiasi kwamba hawakusikiliza maneno ya wale waasi.

4 Lakini ikawa katika mwaka wa hamsini na sita wa utawala wa waamuzi, kulikuwa na [a]waasi ambao walienda kutoka kwa Wanefi na kujiunga na Walamani; na walifaulu kwa usaidizi wa wale wengine kuwachochea kuwa na hasira dhidi ya Wanefi; na walijitayarisha mwaka huo wote kwa vita.

5 Na katika mwaka wa hamsini na saba walikuja chini dhidi ya Wanefi kupigana, na walianza kazi ya mauaji; ndiyo, mpaka kwamba katika mwaka wa hamsini na nane wa utawala wa waamuzi walifaulu kupata umiliki wa nchi ya Zarahemla; ndiyo, na pia nchi zote, hata mpaka kwenye nchi iliyokuwa karibu na nchi ya Neema.

6 Na Wanefi na majeshi ya Moroniha walifukuzwa hata mpaka kwenye nchi ya Neema;

7 Na huko walijiimarisha

35 *c* MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
d MWM Safi na Isiyo safi.
e MWM Utakaso.
f 2 Nya. 30:8; Mos. 3:19.
36 *a* MWM Ukwasi.
4 1 *a* 3 Ne. 11:29.
4 *a* Hel. 5:17.

dhidi ya Walamani, kutoka bahari ya magharibi, hata mpaka wa mashariki; ikiwa safari ya siku moja kwa Mnefi, kwenye mstari ambao walikuwa wameimarisha na kuweka majeshi yao kulinda nchi yao ya kaskazini.

8 Na hivyo wale waasi wa Wanefi, kwa usaidizi wa jeshi kubwa la Walamani, walipata nchi yote ya Wanefi ambayo ilikuwa nchi ya upande wa kusini. Na hayo yote yalifanywa katika miaka ya hamsini na nane hadi ya tisa ya utawala wa waamuzi.

9 Na ikawa katika mwaka wa sitini wa utawala wa waamuzi, Moroniha alifaulu na majeshi yake kwa kushika tena sehemu nyingi za nchi; ndiyo, walipata tena miji mingi ambayo ilikuwa imeanguka mikononi mwa Walamani.

10 Na ikawa katika mwaka wa sitini na moja wa utawala wa waamuzi walifaulu kupata tena hata nusu ya umiliki wao wote.

11 Sasa hii hasara kubwa ya Wanefi, na mauaji makubwa ambayo yalifanyika miongoni mwao, haingefanyika kama haingekuwa uovu wao na machukizo yao ambayo yalikuwa miongoni mwao; ndiyo, na ilikuwa pia miongoni mwa wale ambao walidai kuwa katika kanisa la Mungu.

12 Na ilikuwa kwa sababu ya [a]kiburi cha mioyo yao, kwa sababu ya [b]utajiri wao mwingi, ndiyo, ilikuwa kwa sababu ya udhalimu wao kwa [c]maskini, wakizuia chakula chao kwa wale walio na njaa, wakizuia mavazi yao kwa wale walio uchi, na wakiwapiga ndugu zao wanyenyekevu kwenye shavu, na wakifanyia mzaha yale yaliyo matakatifu, wakikana roho ya unabii na wa ufunuo, wakiua, wakiteka nyara, wakidanganya, wakiiba, wakitenda zinaa, wakiinuka kwa mabishano makuu, na kukimbilia mbali hadi kwenye nchi ya Nefi, miongoni mwa Walamani—

13 Na kwa sababu ya uovu wao huu mkubwa, na [a]majivuno yao kwa nguvu yao, waliachwa wategemee nguvu zao; kwa hivyo hawakufanikiwa, lakini waliteswa na kuuawa, na kukimbizwa na Walamani, mpaka walipoteza karibu umiliki wa nchi yao yote.

14 Lakini tazama, Moroniha alihubiri vitu vingi kwa watu kwa sababu ya uovu wao, na pia [a]Nefi na Lehi, ambao walikuwa wana wa Helamani, walihubiri vitu vingi kwa watu, ndiyo, na walitoa unabii wa vitu vingi kwao kuhusu ubaya wao, na kile ambacho kingefanyika kwao kama hawakutubu dhambi zao.

15 Na ikawa kwamba walitubu, na kadiri walivyo tubu walianza kufanikiwa.

16 Kwani Moroniha alipoona kwamba wametubu alithubutu kuwaongoza mbele kutoka mahali pamoja hadi pengine,

12*a* Oba. 1:3–4; M&M 101:42.
b 1 Tim. 6:17; 2 Ne. 9:42.
c M&M 42:30–31.
13*a* MWM Kiburi.
14*a* Hel. 3:21.

na kutoka mji mmoja hadi mwingine, hata mpaka walipopata tena nusu ya mali yao na nusu ya nchi yao yote.

17 Na hivyo ukaisha mwaka wa sitini na moja wa utawala wa waamuzi.

18 Na ikawa katika mwaka wa sitini na mbili wa utawala wa waamuzi, kwamba Moroniha hangeweza kupata tena umiliki juu ya Walamani.

19 Kwa hivyo waliacha kusudi lao la kupata nchi yao iliyobakia, kwani Walamani walikuwa wengi sana kwamba ilikuwa vigumu kwa Wanefi kupata uwezo zaidi juu yao; kwa hivyo Moroniha alitumia majeshi yake yote kwa kulinda hizo sehemu ambazo alikuwa amekamata.

20 Na ikawa kwa sababu ya idadi kubwa ya Walamani Wanefi walikuwa na woga mwingi, wasije wakashindwa, na kukanyagwa chini, na kuuawa, na kuangamizwa.

21 Ndiyo, walianza kukumbuka unabii wa Alma, na pia maneno ya Mosia; na waliona kwamba walikuwa watu wenye shingo ngumu, na kwamba wamedharau amri za Mungu;

22 Na kwamba walikuwa wamegeuza na kuzikanyaga kwa miguu yao [a]sheria za Mosia, au kile ambacho Bwana alimwamuru awape watu; na waliona kwamba sheria zao zilikuwa zimeharibika, na kwamba walikuwa wamekuwa watu waovu, mpaka kwamba walikuwa waovu sawa na Walamani.

23 Na kwa sababu ya uovu wao kanisa lilikuwa limeanza [a]kufifia; na wakaanza kutoamini katika roho ya unabii na katika roho ya ufunuo; na hukumu za Mungu ziliwaangalia machoni.

24 Na waliona kwamba walikuwa wamekuwa [a]walegevu, kama ndugu zao, Walamani, na kwamba Roho wa Bwana hakuwaifadhi; ndiyo, ilikuwa imejiondoa kutoka kwao kwa sababu [b]Roho wa Bwana haishi kwenye mahekalu [c]yasiyo matakatifu—

25 Kwa hivyo Bwana aliacha kuwahifadhi kwa njia ya miujiza yake na uwezo wake usiolinganishwa, kwani walikuwa wameanguka kwenye hali ya [a]kutoamini na uovu wa kutisha; na waliona kwamba Walamani walikuwa wengi sana kuliko wao, na wasipo [b]jishikilia kwa Bwana Mungu wao wataangamia bila kizuizi.

26 Kwani tazama, waliona kwamba nguvu za Walamani zilikuwa nyingi kama zao, hata mtu kwa mtu. Na hivyo walikuwa wameanguka kwenye dhambi hii kuu; ndiyo, hivyo walikuwa wamekuwa wanyonge, kwa sababu ya makosa yao, kwa muda [a]usio wa miaka mingi.

22 *a* Alma 1:1.
23 *a* MWM Ukengeufu.
24 *a* Mos. 1:13.
b MWM Roho Mtakatifu.
c Mos. 2:37; Alma 7:21; 34:36.
25 *a* MWM Kutoamini.
b Yak. (KM) 6:5.
26 *a* Alma 46:8; Hel. 12:3–4.

MLANGO WA 5

Nefi na Lehi wanajitoa wenyewe kuhubiri—Majina yao yanawakumbusha kuishi maisha mazuri kama babu zao—Kristo anakomboa wale ambao wanatubu—Nefi na Lehi wanapata waongofu wengi na wanafungwa gerezani, na moto unawazingira—Wingu la giza linawafunika watu mia tatu—Ardhi inatetemeka, na sauti inawaamrisha watu watubu—Nefi na Lehi wanaongea na malaika, na umati unazingirwa na moto. Karibia mwaka 30 K.K.

NA ikawa kwamba katika mwaka huo huo, tazama, [a]Nefi alitoa kiti cha hukumu kwa mtu ambaye jina lake lilikuwa Sezoramu.

2 Kwani kwa vile sheria zao na serikali yao ilianzishwa kwa [a]sauti ya watu, na [b]waliochagua uovu walikuwa wengi sana kuliko wale waliochagua mema, kwa hivyo walikuwa wanajitayarisha kwa maangamizo, kwani sheria zilikuwa zimechafuliwa.

3 Ndiyo, na haya hayakuwa yote; walikuwa watu wa shingo ngumu, kiasi kwamba hawangetawaliwa na sheria wala haki, isipokuwa tu kwa uharibifu wao.

4 Na ikawa kwamba Nefi alikuwa amechoka kwa sababu ya uovu wao; na [a]akaacha kiti cha hukumu, na akajichagua mwenyewe kuhubiri neno la Mungu siku zake zote zilizosalia, na kaka yake Lehi pia, siku zake zote zilizosalia;

5 Kwani walikumbuka maneno ambayo baba yao Helamani aliwazungumzia. Na haya ndiyo maneno aliyosema:

6 Tazama, wana wangu, ninataka kwamba mtii amri za Mungu; na ningetaka kwamba mwatangazie watu maneno haya. Tazama, nimewapatia majina ya [a]wazazi wetu wa kwanza ambao walitoka nchi ya Yerusalemu; na nimefanya hivi ili mnapokumbuka majina yenu mtaweza kuwakumbuka; na mnapowakumbuka mngekumbuka kazi zao; na mkikumbuka kazi zao mngejua jinsi ilivyo semwa, na pia kuandikwa, kwamba walikuwa [b]wema.

7 Kwa hivyo, wana wangu, ninataka kwamba mfanye yale ambayo ni mema, ili izungumzwe juu yenu, na pia iandikwe, hata vile ilivyozungumzwa na kuandikwa juu yao.

8 Na sasa wana wangu, tazama nina kitu kingine ambacho ningetamani mfanye, kutamani ambako ni, kwamba msifanye hivi vitu ili mjisifu, lakini kwamba mfanye hivi vitu kujiwekea wenyewe [a]hazina mbinguni, ndiyo, ambayo ni ya milele, na ambayo haitafifia; ndiyo, ili mpate zawadi ya [b]thamani ya uzima wa milele, ambayo tuna sababu ya kudhani imepewa kwa babu zetu.

9 Ee kumbukeni, kumbukeni,

5 1*a* Hel. 3:37.
2*a* Mos. 29:25–27.
b Alma 10:19.
4*a* Alma 4:15–20.
6*a* 1 Ne. 1:1, 5.
b 2 Ne. 33.
8*a* 3 Ne. 13:19–21.
b M&M 14:7.

wana wangu, [a]maneno ambayo mfalme Benjamini aliwazungumzia watu wake; ndiyo, kumbukeni kwamba hakuna njia nyingine wala gharama ambayo kwayo binadamu anaweza kuokolewa, isipokuwa kupitia kwa [b]upatanisho wa damu ya Yesu Kristo, ambaye atakuja; ndiyo, kumbuka kwamba anakuja [c]kuukomboa [d]ulimwengu.

10 Na kumbuka pia [a]maneno ambayo Amuleki alimzungumzia Zeezromu, katika mji wa Amoniha; kwani alimwambia kwamba Bwana lazima atakuja kuwakomboa watu wake, lakini kwamba hatakuja kuwakomboa katika dhambi zao, lakini kuwakomboa kutoka kwenye dhambi zao.

11 Na ana uwezo aliopewa kutoka kwa Baba kuwakomboa kutoka kwenye dhambi zao kwa sababu ya toba; kwa hivyo [a]ametuma malaika wake kutangaza habari njema ya hali ya toba, ambayo inaleta uwezo wa Mkombozi, kuwezesha wokovu wa roho zao.

12 Na sasa, wana wangu, kumbukeni, kumbukeni kwamba ni juu ya [a]mwamba wa Mkombozi wetu, ambaye ni Kristo, Mwana wa Mungu, kwamba lazima mjenge [b]msingi wenu; kwamba ibilisi atakapotuma mbele pepo zake kali, ndiyo, mishale yake katika kimbunga, wakati mvua yake ya mawe na [c]dhoruba kali itapiga juu yenu, haitakuwa na uwezo juu yenu kuwavuta chini kwenye shimo la taabu na msiba usioisha, kwa sababu ya mwamba ambao juu yake ninyi mmejengwa, ambao ni msingi imara, msingi ambao watu wote wakijenga hawataanguka.

13 Na ikawa kwamba haya ndiyo maneno ambayo Helamani [a]aliwafundisha wanawe; ndiyo, aliwafundisha vitu vingi ambavyo havijaandikwa, na pia vitu vingi ambavyo vimeandikwa.

14 Na walikumbuka maneno yake; na kwa hivyo walienda mbele, wakitii amri za Mungu, kufundisha neno la Mungu miongoni mwa watu wote wa Nefi, kuanzia mji wa Neema;

15 Na baada ya hapo walienda hadi kwa mji wa Gidi; na kutoka mji wa Gidi hadi mji wa Muleki;

16 Na hata kutoka mji mmoja hadi mwingine, mpaka walipoenda mbele miongoni mwa watu wote wa Nefi ambao walikuwa katika nchi upande wa kusini; na kutoka hapo hadi kwenye nchi ya Zarahemla, miongoni mwa Walamani.

17 Na ikawa kwamba walihubiri kwa uwezo mwingi, mpaka kwamba waliwafadhaisha wengi wa wale [a]waasi ambao

9*a* Mos. 2:9.
b Mos. 3:17–18.
MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
c MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
d MWM Ulimwengu—Watu wasiotii amri.
10*a* Alma 11:34.
11*a* Alma 13:24–25.
12*a* Mt. 7:24–27; M&M 6:34; Musa 7:53.
MWM Jiwe la pembeni; Mwamba.
b Isa. 28:16; Yak. (KM) 4:16.
c 3 Ne. 14:25, 27.
13*a* Mos. 1:4.
17*a* Hel. 4:4.

walikuwa wameenda huko kutoka kwa Wanefi, mpaka kwamba walikuja mbele na kukiri dhambi zao na wakabatizwa ubatizo wa toba, na mara moja wakarudia Wanefi na kujaribu kurekebisha kwao mabaya ambayo wameyafanya.

18 Na ikawa kwamba Nefi na Lehi waliwahubiria Walamani kwa uwezo mkubwa na mamlaka, kwani walikuwa na uwezo na mamlaka waliyopewa ili waweze [a]kusema, na pia walikuwa nayo yale ambayo wangesema walioneshwa—

19 Kwa hivyo waliweza kusema kwa mshangao mkubwa wa Walamani, kuweza [a]kuwathibitishia, kwa matokeo kwamba kulikuwa Walamani elfu nane ambao walikuwa kwenye nchi ya Zarahemla na karibu na hapo walio batizwa ubatizo wa toba, na wamethibitishiwa juu ya uovu wa desturi za babu zao.

20 Na ikawa kwamba Nefi na Lehi walienda kutoka hapo mpaka kwenye nchi ya Nefi.

21 Na ikawa kwamba walikamatwa na jeshi la Walamani na kutupwa [a]gerezani; ndiyo, hata hilo hilo gerezani ambamo Amoni na ndugu zake walitupwa na watumishi wa Limhi.

22 Na baada ya kutupwa gerezani kwa siku nyingi bila chakula, tazama, walienda gerezani ili wawakamate na kuwaua.

23 Na ikawa kwamba Nefi na Lehi walizungukwa na kile kilichoonekana kama [a]moto, kiasi kwamba hawangeweza kuthubutu kuwagusa kwa mikono yao kwa kuogopa kwamba wangeungua Walakini, Nefi na Lehi hawakuungua; na walionekana kama wanasimama katikati ya moto na hawaungui.

24 Na walipoona kwamba wamezungukwa na [a]nguzo za moto, na kwamba hazikuwachoma, mioyo yao ilipata ujasiri.

25 Kwani waliona kwamba Walamani hawakuthubutu kuwagusa; wala hawangethubutu kuwakaribia, lakini walisimama kama bubu kwa mshangao.

26 Na ikawa kwamba Nefi na Lehi walisimama mbele yao na kuanza kuwazungumzia, wakisema: Msiogope, kwani tazama, ni Mungu ambaye amewaonyesha hiki kitu cha ajabu, ambamo kwayo imeonyeshwa kwenu kwamba hamwezi kutuwekea mikono yenu kutuua.

27 Na tazama, wakati wanasema maneno haya, nchi ilitetemeka sana, na kuta za gereza zilitikisika kama vile zilikaribia kuanguka ardhini; lakini tazama, hazikuanguka. Na tazama, wale ambao walikuwa gerezani walikuwa Walamani na Wanefi ambao walikuwa waasi.

28 Na ikawa kwamba walifunikwa na wingu la [a]giza, na woga wa kutisha mno uliwajia.

18*a* M&M 100:5–8. MWM Toa unabii, Unabii.
19*a* MWM Kazi ya kimisionari; Mwongofu, Uongofu.
21*a* Mos. 7:6–7; 21:23.
23*a* Ku. 3:2.
24*a* Ku. 14:24; 1 Ne. 1:6; M&M 29:12; JS—H 1:16.
28*a* Ku. 14:20.

29 Na ikawa kwamba kulisikika [a]sauti kama ilitokea juu ya wingu la giza, ikisema: Tubuni ninyi, tubuni ninyi, na msijaribu tena kuwaangamiza watumishi wangu ambao nimewatuma kwenu kutangaza habari njema.

30 Na ikawa wakati waliposikia sauti hii, na kuona kwamba haikuwa sauti ya radi, wala haikuwa sauti kubwa ya kuwachanganya, lakini tazama, ilikuwa [a]sauti tulivu na kadiri, kama mnong'ono, na ilipenya hata kwenye roho—

31 Na ijapokuwa upole wa sauti, tazama ardhi ilitetemeka sana, na kuta za gereza zikatingishika tena, kama vile zilikuwa ziko karibu kuanguka ardhini; na tazama wingu la giza, ambalo lilikuwa limewafunika, halikuondoka—

32 Na tazama sauti ilikuja tena, ikisema: Tubuni ninyi, tubuni ninyi, kwani ufalme wa mbinguni uko karibu; na msijaribu tena kuwaangamiza watumishi wangu. Na ikawa kwamba nchi ilitetemeka tena, na kuta zilitikisika.

33 Na pia tena safari ya tatu sauti ilisikika, na kuzungumza kwao maneno ya ajabu ambayo hayawezi kuzungumzwa na binadamu; na kuta zikatingisika tena, na nchi ikatetemeka kama iko karibu kugawanyika katika sehemu mbili.

34 Na ikawa kwamba Walamani hawangeweza kukimbia kwa sababu ya wingu la giza ambalo liliwafunika; ndiyo, na pia hawangetembea kwa sababu ya woga ambao uliwajia.

35 Sasa kulikuwa mmoja miongoni mwao ambaye alikuwa Mnefi kwa kuzaliwa, ambaye wakati mmoja alikuwa mtu wa kanisa la Mungu lakini akaasi kutoka kwao.

36 Na ikawa kwamba aligeuka, na tazama, aliona kupitia kwenye wingu la giza na akaona nyuso za Nefi na Lehi; na tazama, [a]ziling'ara sana, hata kama nyuso za malaika. Na akaona kwamba waliinua macho yao kuelekea mbinguni; na walikuwa kwa hali kama walikuwa wanaongea au kupaza sauti kwa kiumbe ambacho walimwangalia.

37 Na ikawa kwamba mtu huyu alipaza sauti kwa umati, kwamba wageuke na kuangalia. Na tazama, kulikuwa na uwezo uliotolewa kwao kwamba waligeuka na kutazama; na wakaona nyuso za Nefi na Lehi.

38 Na wakamwambia yule mtu: Tazama, hivi vitu vyote vinaamanisha nini, na ni nani ambaye hawa watu wanaongea naye?

39 Sasa jina la mtu huyu lilikuwa Aminadabu. Na Aminadabu aliwaambia: Wanaongea na malaika wa Mungu.

40 Na ikawa kwamba Walamani walimwambia: Tutafanya [a]nini, ili hili wingu la giza liweze kuondolewa kwamba lisitufunike?

41 Na Aminadabu akawaa-

29 *a* 3 Ne. 11:3–14.
30 *a* 1 Fal. 19:12; M&M 85:6.
36 *a* Ku. 34:29–35; Mdo. 6:15.
40 *a* Mdo. 2:37–39.

mbia: Lazima [a]mtubu, na mlilie ile sauti, hata mpaka mtakapopata [b]imani katika Kristo, ambaye mlifundishwa kumhusu na Alma, na Amuleki, na Zeezromu; na wakati mtakapofanya hivi, wingu la giza litatolewa kwa kutia kivuli kwenu.

42 Na ikawa kwamba wote walianza kulilia sauti ya yule ambaye alitetemesha nchi; ndiyo, walilia hata mpaka wingu la giza lilipoondoka.

43 Na ikawa kwamba wakati walipotupa macho yao karibu kuzunguka, na kuona kwamba wingu la giza limetoweka kutokana na kuwafunika, tazama, waliona kwamba [a]wamezingirwa, ndiyo, kila nafsi, na nguzo ya moto.

44 Na Nefi na Lehi walikuwa katikati yao; ndiyo, walizingirwa; ndiyo, walionekana kama wako katikati ya ndimi za moto, lakini hazikuwadhuru, wala hazikuchoma kuta za gereza; na walijazwa na hiyo [a]shangwe ambayo haiwezi kuzungumzwa na iliyojaa utukufu.

45 Na tazama, [a]Roho Mtakatifu wa Mungu alishuka chini kutoka mbinguni, na kuingia kwenye mioyo yao, na walijazwa kama na moto, na [b]walizungumza maneno ya ajabu.

46 Na ikawa kwamba kulisikika sauti kwao, ndiyo, sauti nzuri, kama mnong'ono, ikisema:

47 [a]Amani, amani iwe kwenu, kwa sababu ya imani yenu kwa yule Mpendwa Wangu Sana, ambaye alikuwepo tangu msingi wa dunia.

48 Na sasa, wakati waliposikia hivi walitupa macho yao ili waone kule ile sauti ilikotokea; na tazama, waliona [a]mbingu zikifunguka; na malaika wakaja chini kutoka mbinguni na kuwahudumia.

49 Na kulikuwa karibu watu mia tatu ambao waliona na kusikia hivi vitu; na waliambiwa waende na wasistajaabu, wala wasiwe na shaka.

50 Na ikawa kwamba walienda mbele, na kuhudumia watu, wakitangaza kote nchini mahali hapo vitu vyote ambavyo walisikia na kuona, mpaka kwamba sehemu kubwa ya Walamani ilisadikishwa juu yao, kwa sababu ya ushahidi mwingi ambao walikuwa wamepata.

51 Na kama wengi [a]walivyothibitishwa waliweka chini silaha zao za vita na pia chuki yao na desturi za babu zao.

52 Na ikawa kwamba waliwapatia Wanefi nchi ya umiliki wao.

MLANGO WA 6

Walamani walio wenye haki wanawahubiria wale Wanefi waovu—Watu wote wanafanikiwa wakati wa enzi ya amani na neema—Lusifa, mwanzilishi wa dhambi, huchochea mioyo ya waovu

41 *a* MWM Toba, Tubu.
b MWM Amini, Imani.
43 *a* 3 Ne. 17:24; 19:14.
44 *a* MWM Shangwe.
45 *a* 3 Ne. 9:20; Eth. 12:14.
b MWM Vipawa vya Roho.
47 *a* MWM Amani.
48 *a* 1 Ne. 1:8.
51 *a* Alma 31:5.

na wezi wa Gadiantoni katika uuaji na uovu—Wezi wanachukua serikali ya Wanefi. Karibia mwaka 29–23 K.K.

Na ikawa kwamba wakati mwaka wa sitini na mbili wa utawala wa waamuzi ulipoisha, hivi vitu vyote vilikuwa vimefanyika na wengi wa Walamani walikuwa sehemu kubwa yao, watu wenye haki, mpaka kwamba [a]haki yao ulizidi ule wa Wanefi, kwa sababu ya uthabiti wao na uadilifu wao katika imani.

2 Kwani tazama, kulikuwa na Wanefi wengi ambao walikuwa [a]wagumu na wasio tubu na waovu kupindukia, mpaka kwamba walikataa neno la Mungu na mahubiri yote na unabii ambao ulikuja miongoni mwao.

3 Walakini, watu wa kanisa walikuwa na shangwe nyingi kwa sababu ya uongofu wa Walamani, ndiyo, kwa sababu ya kanisa la Mungu, ambalo lilikuwa limeanzishwa miongoni mwao. Na [a]walishirikiana wao kwa wao, na kufurahiana wao kwa wao, na wakawa na shangwe kubwa.

4 Na ikawa kwamba wengi wa Walamani walikuja kwenye nchi ya Zarahemla, na walifundisha Wanefi njia ya [a]uongofu wao, na wakawasihi wawe na imani na kutubu.

5 Ndiyo, na wengi walihubiri kwa uwezo mwingi na mamlaka, kwa kuwaleta chini wengi wao kwenye kina cha unyenyekevu, kuwa wafuasi wanyenyekevu wa Mungu na Mwanakondoo.

6 Na ikawa kwamba wengi wa Walamani walienda kwenye nchi iliyokuwa upande wa kaskazini; na pia Nefi na Lehi walienda katika [a]nchi iliyokuwa upande wa kaskazini, kuwahubiria watu. Na hivyo uliisha mwaka wa sitini na tatu.

7 Na tazama, kulikuwa na amani kote nchini, kiasi kwamba Wanefi walienda popote nchini walipopenda, kama ni miongoni mwa Wanefi au Walamani.

8 Na ikawa kwamba Walamani pia walienda kokote walikopenda, kama ilikuwa miongoni mwa Walamani au miongoni mwa Wanefi; na hivyo walikuwa na ushirika huru miongoni mwao, kununua na kuuza, na kupata faida, kulingana na mapenzi yao.

9 Na ikawa kwamba walikuwa matajiri sana, wote Walamani na Wanefi; na walikuwa na kiasi kikubwa cha dhahabu, na cha fedha, na kila namna ya chuma ya thamani, kote nchini kusini na nchini kaskazini.

10 Sasa nchi ya kusini iliitwa Lehi, na nchi ya kaskazini iliitwa [a]Muleki, ambayo ilikuwa inaitwa baada ya mwana wa Zedekia; kwani Bwana alimleta Muleki katika nchi ya kaskazini, na Lehi katika nchi ya kusini.

11 Na tazama, kulikuwa na

6 1*a* Hel. 13:1.
2*a* Rum. 1:28–32.
3*a* MWM Ushirika.
4*a* MWM Mwongofu, Uongofu.
6*a* Alma 63:4–9; Hel. 3:11–12.
10*a* Mos. 25:2–4; Hel. 8:21.

namna yote ya dhahabu katika nchi hizi zote, na fedha, na vyuma vya thamani vya kila aina; na kulikuwa pia na mafundi wa ustadi, ambao walifanya kazi na aina yote ya chuma, na waliisafisha; hivyo wakawa matajiri.

12 Walikuza nafaka kwa wingi, kote kaskazini na kusini; na walifanikiwa sana, kote kaskazini na kusini. Na waliongezeka na kuwa na nguvu sana nchini. Na walikuza makundi mengi ya wanyama, ndiyo, ndama wengi.

13 Tazama wanawake wao walifanya kazi kwa bidii na kushona, na walitengeneza aina zote za nguo, laini za kitani na nguo za kila aina, kufunika uchi wao. Na hivyo mwaka wa sitini na nne uliisha kwa amani.

14 Na katika mwaka wa sitini na tano walikuwa pia na shangwe na amani, ndiyo, kuhubiri kwingi na unabii mwingi kuhusu yale yatakayokuja mbeleni. Na hivyo ukaisha mwaka wa sitini na tano.

15 Na ikawa kwamba katika mwaka wa sitini na sita wa utawala wa waamuzi, tazama, [a]Sezoramu aliuawa na mtu asiyejulikana wakati alipokuwa amekalia kiti cha hukumu. Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo, mwana wake, ambaye, alikuwa amechaguliwa na watu badala yake, pia aliuawa. Na hivyo ukaisha mwaka wa sitini na sita.

16 Na katika mwanzo wa mwaka wa sitini na saba watu walianza kuwa waovu sana tena.

17 Kwani tazama, Bwana alikuwa amewabariki sana na utajiri wa ulimwengu kwamba hawakuwa wamechochewa kuwa na hasira, kupigana, wala kumwaga damu; kwa hivyo walianza kuweka mioyo yao katika utajiri wao; ndiyo, walianza kutafuta kupata faida kwamba wangeinuliwa mmoja juu ya mwingine; kwa hivyo walianza kufanya mauaji ya [a]siri, na kunyang'anya na kupora, ili wapate faida.

18 Na sasa tazama, wale wauaji na waporaji walikuwa katika kikundi ambacho kilianzishwa na Kishkumeni na [a]Gadiantoni. Na sasa ilikuwa kwamba kulikuwa na wengi sana, hata miongoni mwa Wanefi, kutoka kikundi cha Gadiantoni. Lakini tazama, walikuwa wengi zaidi katika ile sehemu ovu zaidi ya Walamani. Na waliitwa waporaji na wauaji wa Gadiantoni.

19 Na hao ndiyo wale ambao walimuua mwamuzi mkuu Sezoramu, na mwana wake, wakiwa kwenye kiti cha hukumu; na tazama, hawakupatikana.

20 Na sasa ikawa kwamba wakati Walamani walipogundua kwamba kulikuwa na wezi miongoni mwao walikuwa na huzuni sana; na walitumia mbinu zote kwa uwezo wao kuwaangamiza kutoka kwa uso wa dunia.

21 Lakini tazama, Shetani alivuruga mioyo ya sehemu

15*a* Hel. 5:1. | 17*a* 3 Ne. 9:9. | 18*a* Hel. 2:4, 12–13.

kubwa ya Wanefi, mpaka kwamba wakaungana na yale makundi ya wezi, na waliungana kwa kufanya maagano yao na viapo vyao, ili wangejilinda na kujihifadhi wenyewe kwa kila hali yote ngumu ambayo wangekuwemo, kwamba wasiadhibiwe kwa mauaji yao, na uporaji wao, na wizi wao.

22 Na ikawa kwamba walikuwa na ishara zao, ndiyo, ishara zao za [a]siri, na maneno yao ya siri; na hii ili wapambanue mshiriki wa kundi lao ambaye alikuwa ameingia kwenye agano, kwamba kwa kila uovu ambao ndugu yake angefanya asiumizwe na ndugu yake, wala na wale ambao walikuwa washiriki wa kundi lake, ambao walikuwa wamefanya hili agano.

23 Na hivi wangeua, na kuteka nyara, na kuiba, na kufanya ukahaba na namna yote ya uovu, dhidi ya sheria za nchi yao na pia sheria za Mungu.

24 Na yeyote ambaye alikuwa mshiriki wa kundi lao akifichua kwa watu wengine [a]uovu wao na machukizo yao, angejaribiwa, sio kulingana na sheria za nchi yao, lakini kulingana na sheria za uovu wao, ambazo ziliwekwa na Gadiantoni na Kishkumeni.

25 Sasa tazama, ni hivi [a]viapo vya siri na maagano ambayo Alma alimwamuru mwana wake asifichue kwa ulimwengu, isije zikawa njia ya kuleta watu kwa maangamizo.

26 Sasa tazama, hivyo viapo vya [a]siri na maagano havikumfikia Gadiantoni kutoka kwa maandishi ambayo yalitolewa kwa Helamani; lakini tazama, viliwekwa ndani ya moyo wa Gadiantoni na [b]kile kile kiumbe ambacho kiliwashawishi wazazi wetu wa kwanza kula tunda lililokatazwa—

27 Ndiyo, kile kile kiumbe ambacho kilimshauri [a]Kaini, kwamba kama atamuua ndugu yake Habili haitajulikana katika ulimwengu. Na alishauriana na Kaini na wafuasi wake tangu wakati ule na kuendelea.

28 Na pia ni kile kile kiumbe ambacho kiliweka mahitaji kwa mioyo ya watu [a]kujenga mnara wa urefu wa kutosha ili waweze kufika mbinguni. Na kilikuwa kile kile kiumbe ambacho kiliongoza wale watu waliotoka kwenye mnara huo kuja katika nchi hii; ambao walisambaza kazi ya giza na machukizo kote usoni mwa nchi, mpaka alipovuta watu chini kwenye maangamizo [b]kamili, na kwenye jehanamu isiyo na mwisho.

29 Ndiyo, ni kile kile kiumbe ambacho kiliweka katika moyo wa [a]Gadiantoni haja ya kuendelea na kazi ya giza, na mauaji ya siri; na ameidhihirisha kutoka mwanzo wa binadamu hadi sasa.

30 Na tazama, ni yeye ambaye

22 *a* MWM Makundi maovu ya siri.
24 *a* MWM Ovu, Uovu.
25 *a* Alma 37:27–32.
26 *a* Musa 5:29, 49–52.
b 3 Ne. 6:28; Musa 4:6–12.
27 *a* Musa 5:18–33.
28 *a* Mwa. 11:1–4; Eth. 1:3.
b Eth. 8:9, 15–25.
29 *a* Hel. 2:4–13.

ni [a]mwanzilishi wa dhambi zote. Na tazama, huendesha kazi zake za giza na mauaji ya siri, na hutoa hila zao na viapo vyao, na maagano yao, na mipango ya uovu wa kutisha, kutoka kizazi hadi kingine kulingana na vile anavyoweza kupata mioyo ya watoto wa watu.

31 Na sasa tazama, alikuwa ameshawishi mioyo ya Wanefi; ndiyo, mpaka kwamba walikuwa wamekuwa waovu sana; ndiyo, wengi wao walikuwa wametoka kwenye njia ya haki, [a]kuzikanyaga kwa miguu yao amri za Mungu, na wakageukia njia zao wenyewe, na wakajitengenezea sanamu za dhahabu na fedha.

32 Na ikawa kwamba haya maovu yote yaliwajia kwa muda [a]usio wa miaka mingi, mpaka kwamba mengi ya haya yaliwajia katika mwaka wa sitini na saba wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

33 Na uovu wao uliongezeka katika mwaka wa sitini na nane pia, ambao ulileta huzuni kuu na kulia kwa wale walio wa haki.

34 Na hivyo tunaona kwamba Wanefi walianza kufifia katika kutoamini, na kukua kwenye uovu na machukizo, wakati Walamani nao walianza kukua zaidi katika ujuzi wa Mungu wao; ndiyo, walianza kutii sheria na amri zake, na kutembea katika ukweli na haki mbele yake.

35 Na hivyo tunaona kwamba Roho wa Bwana ilianza [a]kujiondoa kutoka kwa Wanefi, kwa sababu ya uovu wao na ugumu wa mioyo yao.

36 Na hivyo tunaona kwamba Bwana alianza kuwamwagia Walamani Roho yake, kwa sababu ya wema wao na hiari yao ya kuamini maneno yake.

37 Na ikawa kwamba Walamani walisaka lile kundi la wezi la Gadiantoni; na walihubiri neno la Mungu miongoni mwa wengi wao waliokuwa waovu, mpaka kwamba wezi hao waliangamizwa kabisa kutoka miongoni mwa Walamani.

38 Na ikawa kwa upande mwingine, kwamba Wanefi waliwajenga na kuwasaidia, kuanzia sehemu kubwa ya waliokuwa waovu sana, mpaka walipoenea kote katika nchi ya Wanefi, na walikuwa wameishawishi sehemu kubwa ya walio haki mpaka waliposhushwa na kuamini katika kazi zao na kugawana vilivyoibiwa, na kuungana nao katika mauaji yao ya siri na makundi yao.

39 Na hivyo walipata uwezo wa kuendesha serikali, mpaka kwamba waliikanyagia chini ya miguu yao na kupiga na kukataa kusaidia [a]masikini na walio watiifu, na wafuasi wanyenyekevu wa Mungu.

40 Na hivyo tunaona kwamba walikuwa katika hali ya kutisha, na [a]wakijitayarisha kwa angamizo lisilo na mwisho.

30 *a* Alma 5:39–42; Moro. 7:12, 17; Musa 4:4.
31 *a* 1 Ne. 19:7.
32 *a* Alma 46:8.
35 *a* Mos. 2:36; M&M 121:37.
39 *a* Zab. 109:16; Alma 5:54–56; M&M 56:16.
40 *a* Hel. 5:2; 11:37; M&M 18:6.

41 Na ikawa kwamba hivyo ukaisha mwaka wa sitini na nane wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

Unabii wa Nefi, mwana wa Helamani—Mungu anawatisha watu wa Nefi kwamba atawatembelea katika hasira yake, hata kwa maangamizo yao kabisa isipokuwa watubu kutokana na uovu wao. Mungu anawapiga watu wa Nefi kwa maradhi ya kuambukiza; wanatubu na kumrudia. Samweli, Mlamani, anatoa unabii kwa Wanefi.

Yenye milango ya 7 hadi 16.

MLANGO WA 7

Nefi anakataliwa kaskazini na anarudi Zarahemla—Anaomba juu ya mnara ulio ndani ya bustani yake na anawaambia watu watubu au waangamie. Karibia mwaka 23–21 k.k.

Tazama, sasa ikawa kwamba katika mwaka wa sitini na tisa wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Wanefi, kwamba Nefi, mwana wa Helamani, [a]alirejea katika nchi ya Zarahemla kutoka nchi ya kaskazini.

2 Kwani alikuwa anatembea miongoni mwa watu ambao walikuwa katika nchi ya upande wa kaskazini, na akahubiri neno la Mungu kwao, na alitabiri vitu vingi sana kwao;

3 Na walikataa maneno yake yote, mpaka kwamba hangeweza kuishi miongoni mwao, lakini alirejea tena kwenye nchi yake ya kuzaliwa.

4 Na alipoona watu wakiwa kwa hali ya uovu wa kutisha, na wale wezi wa Gadiantoni wakichukua viti vya hukumu—wakiwa wamejitwalia uwezo na mamlaka ya nchi; wakiweka amri za Mungu kando, na bila kutenda hata haki ndogo mbele yake; bila kufanya haki kwa watoto wa watu;

5 Kuhukumu wale wenye haki kwa sababu ya haki yao; kuachilia walio na hatia na waovu kwenda bila kuadhibiwa kwa sababu ya pesa yao; na juu ya hayo kupewa nafasi kubwa kwenye ofisi za serikali, kutawala na kufanya kulingana na nia zao, ili wapate faida na utukufu wa [a]ulimwengu, na juu ya hayo, kwamba wangefanya uzinifu kwa urahisi, na kuiba, na kuua, na kufanya kulingana na nia zao wenyewe—

6 Sasa huu ubaya uliwajia Wanefi, katika muda wa miaka isiyo mingi; na wakati Nefi alipoona haya, moyo wake ulifura kwa huzuni ndani ya kifua chake; na alipaza sauti kwa maumivu ya nafsi yake:

7 Ee, kwamba ningeishi katika siku ambazo babu yangu Nefi alipotoka mara ya kwanza kutoka Yerusalemu, kwamba ningefurahi na yeye katika ile nchi ya ahadi; hapo watu wake walikuwa rahisi kufundishwa, imara kutii

7 1*a* Hel. 6:6. | 5*a* Mt. 13:22; 16:26.

amri za Mungu, na sio rahisi kwa wao kuongozwa kufanya ubaya; na walikuwa wepesi kusikiliza neno la Bwana—

8 Ndiyo, kama siku zangu zingekuwa kwenye hizo siku, ndipo roho yangu ingejawa shangwe wa kwa ajili ya haki ya ndugu zangu.

9 Lakini tazama, nimewekewa kwamba hizi ndizo siku zangu, na kwamba roho yangu itajazwa na huzuni kwa sababu ya huu uovu wa ndugu zangu.

10 Na tazama, sasa ikawa kwamba ilikuwa juu ya mnara, ambao ulikuwa katika bustani ya Nefi, ambayo ilikuwa kando ya barabara kuu ambayo ilielekea soko kuu, ambalo ilikuwa katika mji wa Zarahemla; kwa hivyo, Nefi alikuwa amejisujudia mwenyewe juu ya mnara ambao ulikuwa kwenye bustani yake, mnara ambao pia ulikuwa karibu na mlango wa bustani, na kando yake kulikuwa na barabara kuu.

11 Na ikawa kwamba kulikuwa baadhi ya watu waliokuwa wakipita kando na kumwona Nefi akimimina roho yake kwa Mungu juu ya mnara; na walikimbia na kuwaambia watu kile ambacho walikuwa wameona, na walikuja pamoja kwa wingi ili wajue sababu ya maombolezi makubwa kwa uovu miongoni mwa watu.

12 Na sasa, wakati Nefi alipoinuka aliona umati wa watu ambao walijikusanya pamoja.

13 Na ikawa kwamba alifungua kinywa chake na kuwaambia: Tazama, kwa *a*nini mmejikusanya wenyewe pamoja? Ili niwaambie kuhusu ubaya wenu?

14 Ndiyo, kwa sababu nimekuja juu ya mnara wangu ili niminine nafsi yangu kwa Mungu, kwa sababu ya huzuni nyingi ya moyo wangu, ambayo ni kwa sababu ya maovu yenu!

15 Na kwa sababu ya kuomboleza kwangu na kulia mmejikusanya pamoja, na mnashangaa; ndiyo, na mna uhitaji mkubwa wa kushangaa; ndiyo, mnapaswa kushangaa kwa sababu mmetolewa ili ibilisi ameshikilia sana mioyo yenu.

16 Ndiyo, mngewezaje kujitolea kwa ushawishi wa yule ambaye anataka kutupa roho zenu chini kwenye taabu isiyo na mwisho na msiba bila mwisho?

17 Ee tubuni ninyi, tubuni ninyi! Kwa *a*nini mnataka kufa? Geukeni ninyi, Mgeukieni Bwana Mungu wenu. Kwa nini amewaacha ninyi?

18 Ni kwa sababu mmeshupaza mioyo yenu; ndiyo, hamtatii sauti ya *a*mchungaji mwema; ndiyo, *b*mmemchokoza kukasirika dhidi yenu.

19 Na tazama, badala ya *a*kuwakusanya, kama hamtatubu,

13*a* Mt. 3:5–8.
17*a* Eze. 18:23, 31–32.
18*a* Eze. 34:12; Yn. 10:14–16; Alma 5:38–41, 57–60. MWM Mchungaji Mwema.
b Yak. (KM) 1:8; Alma 12:36–37.
19*a* 3 Ne. 10:4–7.

tazama, atawatawanya kila mahali kwamba mtakuwa chakula kwa mbwa na wanyama wa mwitu.

20 Ee, jinsi gani mmemsahau Mungu wenu katika ile siku ambayo amewaokoa?

21 Lakini tazama, ni kwa sababu ya kupata faida, kusifiwa na watu, ndiyo, na kwamba mngepata dhahabu na fedha. Na mmeweka mioyo yenu juu ya utajiri na vitu visivyo na maana vya [a]ulimwengu huu, kwani kwa ajili yake mnaua, na kuteka nyara, na kuiba, na kutoa [b]ushahidi wa uwongo dhidi ya majirani zenu, na kufanya aina yote ya uovu.

22 Na kwa sababu hii ubaya utawapata isipokuwa mtubu. Kwani kama hamtatubu, tazama, huu mji mkuu, na pia hiyo miji yote mikubwa ambayo iko karibu, ambayo iko katika nchi ya umiliki wetu, itachukuliwa mbali kwamba hamtakuwa na mahali penu ndani yao; kwani tazama, Bwana hatawapatia [a]nguvu, vile alifanya hapo awali, kuwashinda maadui zenu.

23 Kwani tazama, hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Sitaonyesha nguvu zangu kwa wale waovu, wala kwa mmoja zaidi ya mwingine, isipokuwa kwa wale wanaotubu dhambi zao, na kusikiliza maneno yangu. Sasa kwa hivyo, ningetaka kwamba muelewe, ndugu zangu, kwamba itakuwa [a]bora kwa Walamani kuliko ninyi isipokuwa mtubu.

24 Kwani tazama, wao ni wenye haki kuwazidi, kwani hawajatenda dhambi dhidi ya ile elimu kubwa ambayo mmepokea; kwa hivyo, Bwana atawahurumia; ndiyo, [a]ataongeza siku zao na kuongeza uzao wao, hata baada yenu [b]kuangamizwa kabisa isipokuwa mtubu.

25 Ndiyo, msiba uwe kwenu kwa sababu ya yale machukizo ambayo yamekuja miongoni mwenu; na mmejiunga kwake, ndiyo, kwa lile kundi la [a]siri ambalo lilianzishwa na Gadiantoni!

26 Ndiyo, [a]msiba utawajia kwa sababu ya kile kiburi ambacho mmekubali kiingie kwenye mioyo yenu, ambacho kimewainua juu kupita yale yaliyo mema kwa sababu ya [b]utajiri wenu mwingi!

27 Ndiyo, taabu iwe kwenu kwa sababu ya uovu wenu na machukizo!

28 Na msipotubu mtaangamia; ndiyo, hata nchi zenu zitachukuliwa kutoka kwenu, na mtaangamizwa kutoka uso wa dunia.

29 Tazama sasa, mimi, binafsi sisemi kwamba vitu hivi vitakuwa, kwa sababu sio kwa ajili yangu kwamba [a]najua vitu hivi; lakini tazama, najua kwamba vitu hivi ni vya kweli kwa sababu Bwana Mungu

21 *a* MWM Malimwengu.
b Ku. 20:16; Mt. 15:19–20.
22 *a* Mos. 7:29.
23 *a* Hel. 15:11–15.
24 *a* Alma 9:16; M&M 5:33.
b Alma 9:19.
25 *a* Hel. 3:23.
26 *a* Isa. 5:8–25.
b Yak. (KM) 2:13.
29 *a* Alma 5:45–46.

amevidhihirisha kwangu, kwa hivyo nadhibitisha kwamba vitakuwa.

MLANGO WA 8

Waamuzi wabaya wanataka kuchochea watu dhidi ya Nefi—Ibrahimu, Musa, Zeno, Zenoki, Ezia, Isaya, Yeremia, Lehi, na Nefi wote walimshuhudia Kristo—Kwa maongozi ya Mungu Nefi anatangaza uuaji wa mwamuzi mkuu. Karibia mwaka 23–21 K.K.

Na sasa ikawa kwamba wakati Nefi alipokuwa amesema maneno haya, tazama, kulikuwa na watu ambao walikuwa waamuzi, ambao pia walikuwa wa kundi la siri la Gadiantoni, na walikasirika, na waliongea kwa sauti dhidi yake, wakiwaambia watu: Kwa nini hamwezi kumkamata huyu mtu na kumleta mbele, ili ahukumiwe kulingana na kosa ambalo ametenda?

2 Kwa nini mnamwangalia mtu huyu, na kumsikiliza akitukana hawa watu na sheria zetu?

3 Kwani tazama, Nefi alikuwa amewazungumzia kuhusu sheria yao chafu; ndiyo, Nefi alisema vitu vingi ambavyo haviwezi kuandikwa; na hakusema kitu chochote ambacho kilikuwa kinyume kwa amri za Mungu.

4 Na wale waamuzi walimkasirikia kwa sababu [a]aliongea wazi kwao kuhusu kazi zao za siri za giza; walakini, hawakuthubutu kuweka mikono yao kwake, kwani waliogopa watu wasipaze sauti dhidi yao.

5 Kwa hivyo, walilia kwa watu, wakisema: Kwa nini ninyi mvumilie huyu mtu kututukana? Kwani tazama anahukumu hawa watu wote, hata kwenye maangamizo; na pia kwamba hii miji yetu mikubwa itachukuliwa kutoka kwetu, kwamba hatutakuwa na nafasi ndani yao.

6 Na sasa tunajua kwamba hii haiwezekani, kwani tazama, tuna nguvu, na miji yetu ni mikubwa, kwa hivyo maadui zetu hawawezi kuwa na nguvu juu yetu.

7 Na ikawa kwamba waliwavuruga watu kumkasirikia Nefi, na wakaanzisha mabishano miongoni mwao; kwani kulikuwa na wengine waliopaza sauti: Acha huyu mtu pekee, kwani ni mtu mzuri, na vitu vile ambavyo amesema vitafanyika bila shaka isipokuwa tutubu;

8 Ndiyo, tazama, hukumu zote zitatujia ambazo ameshuhudia kwetu; kwani tunajua kwamba ameshuhudia sawa kwetu kuhusu uovu wetu. Na tazama ziko nyingi, na pia [a]anajua vitu vyote ambavyo vitafanyika kwetu vile anavyojua uovu wetu wote.

9 Ndiyo, na tazama, kama hangekuwa nabii hangeweza kushuhudia kuhusu hivyo vitu.

10 Na ikawa kwamba watu ambao walitaka kumwangamiza Nefi walilazimishwa kwa sababu ya woga wao, kwamba hawakuweka mikono yao kwake; kwa hivyo alianza tena kuwazungumzia, akiona kwamba

8 4*a* 1 Ne. 16:2–3. | 8*a* Hel. 7:29.

amepata mapendeleo ndani ya fikira za wengine wao, mpaka kwamba waliosalia waliogopa.

11 Kwa hivyo alilazimishwa kuzungumza zaidi kwao akisema: Tazameni, ndugu zangu, hamjasoma kwamba Mungu alitoa uwezo kwa mtu mmoja, hata Musa, kupiga juu ya maji ya [a]Bahari ya Shamu, na yakagawanyika hapa na kule, hata kwamba Waisraeli, ambao walikuwa babu zetu, walipita nchi kavu, na maji yakajifunga tena pamoja juu ya majeshi ya Wamisri na kuwameza wao?

12 Na sasa tazama, ikiwa Mungu alimpa huyu mtu uwezo kama huo, basi kwa nini ninyi mnashindana miongoni mwenu, na kusema kwamba hajanipatia mimi uwezo ambamo kwake ningejua kuhusu hukumu ambazo zitatolewa kwenu isipokuwa mtubu?

13 Lakini, tazama, hamkatai tu maneno yangu, lakini pia mnakataa maneno yote ambayo yalizungumzwa na babu zetu, na pia maneno ambayo yamezungumzwa na huyu mtu, Musa, ambaye alipewa nguvu nyingi hivyo kwake, ndiyo, maneno ambayo alizungumza kuhusu kuja kwa Masiya.

14 Ndiyo, sio yeye aliyeshuhudia kwamba Mwana wa Mungu atakuja? Na vile [a]alinua nyoka wa shaba nyeupe nyikani, hata hivyo atainuliwa yule atakayekuja.

15 Na vile wengi wangemtazama yule nyoka [a]wangeishi, hata hivyo jinsi vile wengi wataangalia juu kwa Mwana wa Mungu na imani, wakiwa na roho iliyovunjika, [b]wataishi, hata kwenye maisha ambayo ni ya milele.

16 Na sasa tazama, Musa hakushuhudia tu hivi vitu peke yake, lakini pia manabii [a]wote watakatifu, tangu siku zake hata mpaka siku za Ibrahimu.

17 Ndiyo, na tazama, [a]Ibrahimu aliona kuja kwake, na akajazwa na uchangamfu na alifurahi.

18 Ndiyo, na tazama nawaambia, kwamba Ibrahimu hakujua tu hivi vitu, lakini kulikuwa na [a]wengi kabla ya siku za Ibrahimu ambao waliitwa kwa [b]amri ya Mungu; ndiyo, hata baada ya amri ya Mwana wake; na hivi ili ionyeshwe kwa watu, miaka elfu nyingi kabla ya kuja kwake, kwamba hata ukombozi utawajia.

19 Na sasa ningetaka kwamba mjue, kwamba hata tangu siku za Ibrahimu kumekuwa na manabii wengi ambao wameshuhudia hivi vitu; ndiyo, tazama, nabii [a]Zeno alishuhudia kwa ujasiri; na kwa kufanya hivyo aliuawa.

11*a* Ku. 14:16; 1 Ne. 17:26; Mos. 7:19; M&M 8:2–3; Musa 1:25.
14*a* Hes. 21:6–9; 2 Ne. 25:20; Alma 33:19–22.
MWM Yesu Kristo—Mifano au ishara za Kristo.
15*a* 1 Ne. 17:41; Alma 37:45–47; 3 Ne. 15:9.
b Yn. 11:25.
16*a* Yak. (KM) 4:4–5; 7:11.
17*a* Mwa. 22:8–14; Yn. 8:56.
18*a* Alma 13:19; M&M 84:6–16; 136:37.
b MWM Ukuhani wa Melkizedeki.
19*a* Alma 34:7.

20 Na tazama, pia [a]Zenoki, na pia Ezia, na pia [b]Isaya, na [c]Yeremia, (Yeremia akiwa yule yule nabii ambaye alishuhudia kuharibiwa kwa [d]Yerusalemu) na sasa tunajua kwamba Yerusalemu iliangamizwa kulingana na maneno ya Yeremia. Ee basi kwa nini Mwana wa Mungu asije, kulingana na unabii wake?

21 Na sasa mtakataa kukubali kwamba [a]Yerusalemu iliharibiwa? Mtasema kwamba [b]wana wa Zedekia hawakuuawa, wote isipokuwa tu [c]Muleki? Ndiyo, na hamwoni kwamba wana wa Zedekia wako pamoja nasi, na walifukuzwa kutoka nchi ya Yerusalemu? Lakini tazama, haya sio yote—

22 Babu yetu Lehi alikimbizwa kutoka Yerusalemu kwa sababu alishuhudia hivi vitu. Nefi pia alishuhudia hivi vitu, na pia karibu babu zetu wote, hata kuja chini kwa wakati huu; ndiyo, wameshuhudia [a]kuja kwa Kristo, na wamengojea, na wamefurahia siku yake ambayo itakuja.

23 Na tazama, yeye ni Mungu, na yuko pamoja nao, na alijidhihirisha kwao, kwamba walikombolewa na yeye; na wakamtukuza, kwa sababu ya yale ambayo yatakuja.

24 Na sasa, ni wazi kuwa mnajua hivi vitu na hamwezi kuvikana isipokuwa mdanganye, kwa hivyo katika haya mmetenda dhambi, kwani mmekataa hivi vitu vyote ingawa mmepata ushuhuda mwingi; ndiyo, hata mmepokea vitu [a]vyote, vyote vitu vya mbinguni, na vitu vyote vilivyo ardhini, kama ushahidi kwamba viko kweli.

25 Lakini tazama, mmekataa ukweli, na [a]mmeasi dhidi ya Mungu wenu mtakatifu; na hata wakati huu, badala ya kujiwekea [b]hazina mbinguni, mahali ambapo hakuna chochote kitakachochafua, na ambapo hakuna kile kitakachokuja ambacho si safi, mnajirundikia ghadhabu dhidi ya siku ya [c]hukumu.

26 Ndiyo, hata wakati huu mnajiweka tayari, kwa sababu ya mauaji yenu, na [a]uasherati na uovu, kwenye uangamizo usio na mwisho; ndiyo, na isipokuwa mtubu utawajia upesi.

27 Ndiyo, tazama uko sasa hata kwenye milango yenu; ndiyo, nendeni kwenye kiti cha hukumu, na mpeleleze; na tazama, mwamuzi wenu ameuawa, na [a]analalia damu yake; na ameuawa [b]na kaka yake, ambaye anatazamia kiti cha hukumu.

28 Na tazama, wote ni wa-

20*a* 1 Ne. 19:10; 3 Ne. 10:15–16. MWM Maandiko—Maandiko yaliyopotea.
b Isa. 53.
c 1 Ne. 5:13; 7:14.
d Yer. 26:18; 1 Ne. 1:4.
21*a* 2 Ne. 6:8; Omni 1:15.
b 2 Fal. 25:7; Yer. 39:6; 52:10.
c Eze. 17:22–23; Hel. 6:10.
22*a* MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.
24*a* Alma 30:44; Musa 6:63.
25*a* Mos. 2:36–38; 3:12.
b Hel. 5:8; 3 Ne. 13:19–21.
c M&M 10:20–23; 121:23–25.
26*a* MWM Uasherati.
27*a* Hel. 9:3, 15.
b Hel. 9:6, 26–38.

shiriki wa kundi lenu la siri, ambalo [a]mwanzilishi wake ni Gadiantoni na mwovu ambaye anataka kuangamiza roho za wanadamu.

MLANGO WA 9

Wajumbe wanapata mwamuzi mkuu amekufa kwenye kiti cha hukumu—Wanawekwa gerezani na baadaye wanaachiliwa—Kwa maongozi ya Mungu, Nefi anamtambua Seantumu kama muuaji—Nefi anakubaliwa na baadhi yao kama nabii. Karibia mwaka 23–21 K.K.

Tazama, sasa ikawa kwamba wakati Nefi alipokuwa amezungumza maneno haya, baadhi ya watu ambao walikuwa miongoni mwao walikimbilia kwenye kiti cha hukumu; ndiyo, hata kulikuwa na watano ambao walienda, na wakasema baina yao, wakienda:

2 Tazama, sasa tutajua kwa kweli kama huyu mtu ni nabii na ameamriwa na Mungu kutabiri vitu vya maajabu kama hivi kwetu. Tazama, hatuamini kwamba amemwamuru; ndiyo, hatuamini kwamba yeye ni nabii; lakini, ikiwa hiki kitu ambacho amesema kuhusu mwamuzi mkuu kitakuwa cha kweli, kwamba amekufa, ndipo tutaamini kwamba yale maneno mengine ambayo amesema ni ya kweli.

3 Na ikawa kwamba walikimbia kwa nguvu vile wawezavyo, na kufikia kiti cha hukumu; na tazama, mwamuzi mkuu alikuwa ameanguka ardhini, na alikuwa [a]amelalia damu yake.

4 Na sasa tazama, wakati walipoona hivi walishangaa sana, mpaka kwamba waliinama kwenye ardhi; kwani walikuwa hawajaamini maneno ambayo Nefi alisema kuhusu mwamuzi mkuu.

5 Lakini sasa, wakati walipoona waliamini, na woga ukawajia isiwe hukumu zote ambazo Nefi alizungumzia ziwajie watu; kwa hivyo walitetemeka, na waliinama kwenye ardhi.

6 Sasa, mara mwamuzi alikuwa ameuawa—yeye akiwa amechomwa na kaka yake kwa mpango wa siri, na alitoroka, na watumishi walikimbia na kuwaambia watu, wakipasa kilio cha mauaji miongoni mwao;

7 Na tazama watu walijikusanya pamoja katika pahali pa kiti cha hukumu—na tazama, kwa kustaajabu kwao waliona wale watu watano ambao walikuwa wameinama kwenye ardhi.

8 Na sasa tazama, watu hawakuwa wamejua kuhusu umati ambao ulijikusanya pamoja kwenye [a]bustani ya Nefi; kwa hivyo walisema miongoni mwao: Hawa ndiyo watu ambao wamemuua mwamuzi, na Mungu amewalaani kwamba hawangeweza kutoroka kutoka kwetu.

9 Na ikawa kwamba waliwashika kwa ghafla, na kuwafunga

28 *a* Hel. 6:26–30.
9 3 *a* Hel. 8:27.
8 *a* Hel. 7:10.

na kuwatupa gerezani. Na matangazo yakatumwa kote kwamba mwamuzi ameuawa, na kwamba wauaji wamekamatwa na wametupwa gerezani.

10 Na ikawa kwamba kesho yake watu walijikusanya pamoja kuomboleza na [a]kufunga, katika mazishi ya mwamuzi mkuu ambaye aliuawa.

11 Na hivyo pia wale waamuzi ambao walikuwa kwenye bustani ya Nefi, na walisikia maneno yake, pia walikusanyika pamoja kwenye mazishi.

12 Na ikawa kwamba walipeleleza miongoni mwa watu, wakisema: Wako wapi wale watano ambao walitumwa kupeleleza kuhusu mwamuzi mkuu kama amekufa? Na walijibu wakisema: Kuhusu hawa watano ambao mnasema mliwatuma, hatujui; lakini kuna watano ambao ni wauaji, ambao tumewatupa gerezani.

13 Na ikawa kwamba waamuzi walitaka kwamba waletwe mbele yao; na waliletwa, na tazama walikuwa wale watu watano ambao walitumwa; na tazama waamuzi waliwahoji kujua kuhusu lile jambo, na waliwaambia yote ambayo walifanya, wakisema:

14 Tulikimbia na kuja mahali pa kiti cha hukumu, na tulipoona vitu vyote vile Nefi alipotushuhudia, tulishangaa mpaka kwamba tuliinama kwenye ardhi; na wakati tulipopata nguvu kutokana na mshangao wetu, tazama walitutupa gerezani.

15 Sasa, kuhusu mauaji ya huyu mtu, hatujui ni nani aliyeifanya; na hivi tu ndivyo tunajua, tulikimbia na kuja vile mlivyotaka, na tazama alikuwa amekufa, kulingana na maneno ya Nefi.

16 Na sasa ikawa kwamba waamuzi walielezea watu mambo haya, na walizungumza kwa sauti dhidi ya Nefi, wakisema: Tazama, tunajua kwamba huyu Nefi lazima alikuwa amekubaliana na mtu kumuua mwamuzi, na ili atutangazie, ili atubadilishe kwa imani yake, ili ajiweke kuwa mtu mkubwa, aliyechaguliwa na Mungu, na pia nabii.

17 Na sasa tazama, tutamgundua huyu mtu, na ataungama makosa yake na kutuambia mauaji wa kweli wa huyu mwamuzi.

18 Na ikawa kwamba wale watano waliachiwa kwenye siku ya mazishi. Walakini, waliwakemea waamuzi kwa sababu ya maneno ambayo walisema dhidi ya Nefi, na wakapingana nao mmoja mmoja, mpaka kwamba waliwanyamazisha.

19 Walakini, walisababisha kwamba Nefi achukuliwe na kufungwa na aletwe mbele ya umati, na wakaanza kumhoji kwa njia mbali mbali ili wamchanganyishe, ili wamshtaki kwa makosa ya kifo—

20 Wakimwambia: Wewe ni mshiriki; ni nani huyu mtu ambaye amefanya haya mauaji? Sasa tuambie, na ukubali makosa yako, ukisema: Tazama hapa kuna pesa; na pia tutakuachia

10*a* MWM Funga, Kufunga.

maisha yako ikiwa utatuambia, na ukiri makubaliano ambayo ulifanya na yeye.

21 Lakini Nefi aliwaambia: Ee ninyi [a]wajinga, ninyi msiotahiriwa moyoni, ninyi vipofu, ninyi watu wenye [b]shingo ngumu, mnajua ni muda gani Bwana Mungu atawakubalia kwamba mwendelee na njia hizi zenu za dhambi?

22 Ee mnapaswa kuanza kulia na [a]kuomboleza, kwa sababu ya maangamizo makubwa ambayo yanawangojea wakati huu, isipokuwa mtubu.

23 Tazama mnasema kwamba nilikubaliana na mtu kumuua Seezoramu, mwamuzi wetu mkuu. Lakini tazama, ninawaambia, hii ni kwa sababu nimeshuhudia kwenu kwamba mngejua kuhusu hiki kitu; ndiyo, hata kwa ushuhuda kwenu, kwamba nilijua uovu na machukizo ambayo yapo miongoni mwenu.

24 Na kwa sababu nimefanya hivi, mnasema kwamba nilikubaliana na mtu kwamba afanye hiki kitu; ndiyo, kwa sababu niliwaonyesha ishara hii mnanikasirikia, na mnataka kuangamiza maisha yangu.

25 Na sasa tazama, nitawaonyesha ishara nyingine, na nione ikiwa kwa hiki kitu mtataka kuniangamiza.

26 Tazama nawaambia: Nendeni kwa nyumba ya Seantumu, ambaye ni [a]kaka wa Seezoramu, na mmwambie—

27 Nefi, ambaye ni nabii wa kujifanya, ambaye anatoa unabii kuhusu uovu mwingi wa hawa watu, alikubaliana nawe, ili umuue Seezoramu, ambaye ni kaka yako?

28 Na tazama, atawaambia, Hapana.

29 Na mtasema kwake: Wewe umemuua kaka yako?

30 Na atasimama na woga, na hatajua la kusema. Na tazama, atakana kwenu; na atajifanya kama amestaajabu; walakini, atawaelezea kwamba hana hatia.

31 Lakini tazama, mtamjaribu, na mtapata damu upande wa chini wa kanzu yake.

32 Na wakati mtaona hivi, mtasema: Hii damu inatoka wapi? Unafikiri hatujui kama hii ni damu ya kaka yako?

33 Na ndipo atatetemeka, na kunyauka, hata kama aliyekufa.

34 Na hapo mtasema: Kwa sababu ya huu woga wako na huu ugeukaji wa rangi yako ambao umekuja kwa uso wako, tazama, tunajua kwamba una hatia.

35 Na pale woga zaidi utamjia; na hapo atakiri kwenu, na hatakana tena kwamba amefanya haya mauaji.

36 Na hapo atawaambia, kwamba mimi, Nefi, sijui chochote kuhusu jambo hili isipokuwa iwe imetolewa kwangu na uwezo wa Mungu. Na ndipo mtajua kwamba mimi ni mtu mwaminifu, na kwamba nimetumwa kwenu kutoka kwa Mungu.

37 Na ikawa kwamba walienda

21 *a* Mdo. 7:51.
b MWM Uasi.

22 *a* Mos. 7:24.

26 *a* Hel. 8:27.

na kufanya, hata kulingana na vile Nefi alivyokuwa amewaambia. Na tazama, yale maneno ambayo alikuwa amesema yalikuwa kweli; kwani kulingana na maneno alikana; na pia kulingana na maneno alikiri.

38 Na alifanywa kukiri kwamba yeye mwenyewe alikuwa muuaji, mpaka kwamba wale watano waliachiliwa huru, na pia Nefi.

39 Na kulikuwa baadhi ya Wanefi ambao waliamini maneno ya Nefi; na kulikuwa na baadhi ya wengine, walioamini kwa sababu ya ushuhuda wa wale watano, kwani walikuwa wamegeuka walipokuwa gerezani.

40 Na sasa kulikuwa na wengine miongoni mwa watu, ambao walisema kwamba Nefi alikuwa nabii.

41 Na kulikuwa na wengine ambao walisema: Tazama, yeye ni aina ya mungu, kwani kama hangekuwa mungu hangejua hivi vitu. Kwani tazama, ametuambia fikira za mioyo yetu, na pia ametuambia vitu; na hata ameleta kwenye elimu yetu muuaji wa kweli wa mwamuzi wetu mkuu.

MLANGO WA 10

Bwana anampatia Nefi, uwezo wa kuidhinisha—Anawezeshwa kufunga na kufungua duniani na mbinguni—Anaamrisha watu watubu au sivyo waangamie—Roho inambeba kutoka umati hadi mwingine. Karibia mwaka 21–20 K.K.

Na ikawa kwamba kulitokea mgawanyiko miongoni mwa watu, mpaka kwamba walijigawa hapa na pale na kwenda njia zao, wakimwacha Nefi peke yake, mahali alipokuwa amesimama katikati yao.

2 Na ikawa kwamba Nefi alijiendea njia yake kuelekea nyumba yake, [a]akitafakari juu ya vitu ambavyo Bwana alikuwa amemfichulia.

3 Na ikawa vile alipokuwa akitafakari—akiwa amehuzunishwa kwa sababu ya uovu wa watu wa Wanefi, kazi zao za siri na za giza, na mauaji yao, na utekaji nyara wao, na aina yote ya ubaya—na ikawa vile alikuwa anatafakari kwenye moyo wake, tazama, sauti ilikuja kwake ikisema:

4 Umebarikiwa ewe, Nefi, kwa hivyo vitu ambavyo umefanya; kwani nimeona vile umetangaza neno bila [a]kusita, neno ambalo nimekupatia, kwa hawa watu. Na hujawaogopa, na hujatazamia [b]maisha yako, lakini umetazamia [c]kusudi langu, na kutii amri zangu.

5 Na sasa, kwa sababu umefanya hivi bila kusita, tazama, nitakubariki milele; na nitakufanya mwenye nguvu kwa neno na vitendo, katika imani na vitendo; ndiyo, hata kwamba vitu [a]vyote vitafanyika kwako kulingana na [b]neno lako, kwani

10 2*a* MWM Tafakari.
4*a* MWM Bidii.
b MWM Dhabihu.
c 3 Ne. 11:11.
5*a* 3 Ne. 18:20; M&M 88:63–65.
b Eno. 1:12.

[c]hutauliza kile ambacho ni kinyume cha kusudi langu.

6 Tazama, wewe ni Nefi, na mimi ni Mungu. Tazama, ninatangaza kwako katika uwepo wa malaika wangu, kwamba utakuwa na uwezo juu ya hawa watu, na utalaani ardhi na [a]njaa, na ugonjwa wa kuambukiza, na uangamizo, kulingana na uovu wa hawa watu.

7 Tazama, ninakupatia uwezo, kwamba lolote [a]utakalofunga duniani litafungwa mbinguni; na lolote utakalofungua duniani litafunguliwa mbinguni; na hivyo utakuwa na uwezo miongoni mwa watu hawa.

8 Na hivyo, ikiwa utaliambia hekalu hili ligawanyike mara mbili, itafanyika.

9 Na ikiwa utauambia huu [a]mlima, Rudi chini na uwe laini, itafanyika.

10 Na tazama, ikiwa utasema kwamba Mungu atalaani hawa watu, itakuwa hivyo.

11 Na sasa, tazama, ninakuamuru, kwamba utaenda na kuwatangazia watu hawa, kwamba hivyo ndivyo asemavyo Bwana Mungu, ambaye ni Mwenyezi: Msipotubu mtapigwa, hata mpaka [a]mtakapoangamizwa.

12 Na tazama, sasa ikawa kwamba wakati Bwana alipokuwa amesema maneno haya kwa Nefi, alisimama na hakwenda kwa nyumba yake, lakini alirejea kwenye makundi ambayo yalikuwa yametawanyika nchini, na akaanza kuwatangazia neno la Bwana ambalo lilisemwa kwake, kuhusu kuangamizwa kwao kama hawakutubu.

13 Sasa tazama, ijapokuwa ule muujiza mkuu ambao Nefi alikuwa amefanya kwa kuwaambia kuhusu kifo cha mwamuzi mkuu, walishupaza mioyo yao na hawakutii maneno ya Bwana.

14 Kwa hivyo Nefi alitangaza kwao neno la Bwana, akisema: Isipokuwa mtubu, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, mtapigwa hata mpaka mtakapoangamizwa.

15 Na ikawa kwamba wakati Nefi alipowatangazia neno, tazama, bado walishupaza mioyo yao na hawakusikiliza maneno yake; kwa hivyo walitoa mashutumu dhidi yake, na walitaka kujaribu kumshika ili wamtupe gerezani.

16 Lakini tazama, nguvu za Mungu zilikuwa na yeye, na hawangemkamata na kumtupa gerezani, kwani alichukuliwa na Roho kutoka miongoni mwao na kubebwa kutoka kwao.

17 Na ikawa kwamba hivyo ndivyo alienda katika Roho, kutoka kwa umati hadi mwingine, akitangaza neno la Mungu, hata mpaka alipokuwa amewatangazia wote, au kutuma ujumbe miongoni mwa watu wote.

18 Na ikawa kwamba hawa-

5*c* 2 Ne. 4:35; M&M 46:30.
6*a* Hel. 11:4–18.
7*a* Mt. 16:19.
MWM Kufunga, Muhuri, Tia.
9*a* Mt. 17:20; Yak. (KM) 4:6; Morm. 8:24; Eth. 12:30.
11*a* Hel. 5:2.

kusikiliza maneno yake, na kukaanza kuwa na mabishano, mpaka kwamba waligawanyika dhidi yao wenyewe na wakaanza kuuana kwa upanga.

19 Na hivyo ukaisha mwaka wa sabini na moja wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

MLANGO WA 11

Nefi anamshawishi Bwana kurudisha njaa badala ya vita vyao—Watu wengi wanaangamia—Wanatubu, na Nefi anaomba Bwana alete mvua—Nefi na Lehi wanapata ufunuo mwingi—Wezi wa Gadiantoni wanajiweka katika nchi. Karibia mwaka 20–6 K.K.

Na ikawa katika mwaka wa sabini na mbili wa utawala wa waamuzi kwamba mabishano yaliongezeka, mpaka kwamba kukawa na vita kote nchini miongoni mwa watu wa Nefi.

2 Na lilikuwa hili kundi la [a]siri la wezi ambalo liliendelea na hii kazi ya uharibifu na uovu. Na hivi vita viliendelea huo mwaka wote; na katika mwaka wa sabini na tatu pia viliendelea.

3 Na ikawa kwamba katika huu mwaka Nefi alimlilia Bwana, akisema:

4 Ee Bwana, usikubali kwamba hawa watu waangamizwe kwa upanga; lakini Ee Bwana, afadhali kuwe na [a]njaa nchini, iwavuruge wakumbuke Bwana Mungu wao, na labda watatubu na kugeuka kwako.

5 Na hivyo ilifanyika, kulingana na maneno ya Nefi. Na kulikuwa na njaa kubwa sana katika nchi, miongoni mwa watu wote wa Nefi. Na hivyo katika mwaka wa sabini na nne njaa iliendelea, na kazi ya kuangamiza kwa upanga ilikwisha lakini ikawa nyingi kwa njaa.

6 Na hii kazi ya uangamizo pia iliendelea katika mwaka wa sabini na tano. Kwani nchi ililaaniwa kwamba ilikauka, na haikuzalisha nafaka wakati wa nafaka; na nchi yote ililaaniwa, hata miongoni mwa Walamani na pia miongoni mwa Wanefi, hata kwamba walipigwa kwamba waliangamia kwa maelfu katika sehemu zilizokuwa mbovu zaidi ya nchi.

7 Na ikawa kwamba watu waliona kwamba walikuwa karibu kuangamia kwa sababu ya njaa, na wakaanza [a]kumkumbuka Bwana Mungu wao; na walianza kukumbuka maneno ya Nefi.

8 Na watu walianza kupeleka hoja kwa waamuzi wakuu na viongozi wao, ili waseme kwa Nefi: Tazama, tunajua kwamba wewe ni mtu wa Mungu, kwa hivyo mlilie Bwana Mungu wetu kwamba amalize hii njaa, isiwe [a]maneno yote ambayo umesema kuhusu uangamizo wetu yaje yakafanyika.

9 Na ikawa kwamba waamuzi walimwambia Nefi, kulingana na maneno ambayo yalikuwa yanatakwa. Na ikawa kwamba wakati Nefi alipoona kwamba watu wametubu na

11 2*a* Hel. 6:18–24; 11:25–26.
4*a* 1 Fal. 17:1; Hel. 10:6.
7*a* Hel. 12:3.
8*a* Hel. 10:11–14.

kujinyenyekeza ndani ya nguo za gunia, alimlilia tena Bwana, akisema:

10 Ee Bwana, tazama hawa watu wametubu; na wamefutilia mbali kundi la Gadiantoni kutoka miongoni mwao mpaka kwamba wamemalizika, na wameficha mipango yao ya siri ardhini.

11 Sasa, Ee Bwana, kwa sababu ya huu unyenyekevu ambao wanao nakuomba uondoe hasira yako, na uache hasira yako itulizwe katika uangamizo wa wale waovu ambao kitambo umeangamiza.

12 Ee Bwana, je, utabadilisha hasira yako, ndiyo, hasira yako kali, na usababishe kwamba hii njaa iishe katika nchi hii.

13 Ee Bwana, je, utanisikiliza, na kusababisha kwamba ifanyike kulingana na maneno yangu, na utume [a]mvua juu ya dunia, kwamba izalishe matunda yake, na nafaka yake katika wakati wa nafaka.

14 Ee Bwana, ulisikiliza [a]maneno yangu, wakati nilisema, Acha kuwe na njaa, ili maradhi ya upanga ipate kuisha; na ninajua kwamba wewe; hata wakati huu, utasikiza maneno yangu, kwani ulisema kwamba: Ikiwa hawa watu watatubu nitawasamehe.

15 Ndiyo, Ee Bwana, na umeona kwamba wametubu, kwa sababu ya njaa na ugonjwa wa kuambukiza na maangamizo ambayo yamewajia.

16 Na sasa, Ee Bwana, utaacha hasira yako, na uwajaribu tena kama watakutumikia? Na ikiwa hivyo, Ee Bwana, unaweza kuwabariki kulingana na maneno yako ambayo ulisema.

17 Na ikawa kwamba katika mwaka wa sabini na sita Bwana aliondoa hasira yake kwa watu, na kusababisha [a]mvua kunyesha juu ya nchi, mpaka kwamba ikazalisha matunda yake katika majira ya matunda. Na ikawa kwamba ardhi ilileta nafaka katika majira ya nafaka.

18 Na tazama, watu walifurahi na kumtukuza Mungu, na nchi yote ilijaa na furaha; na hawakutaka tena kumwangamiza Nefi, lakini walimheshimu kama nabii [a]mkuu, na mtu wa Mungu, ambaye alikuwa na uwezo mwingi na mamlaka ambayo ilitolewa kwake kutoka kwa Mungu.

19 Na tazama, Lehi, kaka yake, hakuwa nyuma hata [a]chembe moja kwa vitu vilivyohusika na haki.

20 Na hivyo ikawa kwamba watu wa Nefi walianza kufanikiwa tena nchini, na wakaanza kujenga mahala pao palipokuwa ukiwa, na wakaanza kuongezeka na kutawanyika, hata kwamba wakawa kote nchini, kote kaskazini na kusini, kutoka kwa bahari ya magharibi hadi kwenye bahari ya mashariki.

21 Na ikawa kwamba mwaka wa sabini na sita uliisha kwa amani. Na mwaka wa sabini na

13*a* 1 Fal. 18:1, 41–46.
14*a* Hel. 11:4.
17*a* Kum. 11:13–17.
18*a* Hel. 10:5–11.
19*a* Hel. 5:36–44.

saba ukaanza kwa amani; na [a]kanisa lilienea kote nchini; na sehemu kubwa ya watu, wote Wanefi na Walamani, walikuwa ndani ya kanisa, na walikuwa na amani kubwa sana nchini; na hivyo mwaka wa sabini na saba uliisha.

22 Na pia walikuwa na amani katika mwaka wa sabini na nane, isipokuwa tu mabishano machache kuhusu mafundisho ya dini ambayo yalikuwa yameandikwa chini na manabii.

23 Na katika mwaka wa sabini na tisa kulianza kuwa na mzozo mkuu. Lakini ikawa kwamba Nefi na Lehi, na wengi wa ndugu zao ambao walijua kuhusu ukweli wa mafundisho ya dini, wakiwa na [a]mafunuo mengi kila siku, kwa hivyo waliwahubiria watu, mpaka kwamba wakaweka kikomo kwa mzozo wao katika mwaka huo huo.

24 Na ikawa kwamba katika mwaka wa themanini wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi, kulikuwa na idadi fulani ya waasi kutoka kwa watu wa Nefi, ambao miaka kadhaa iliyopita walikuwa wameenda kuishi na Walamani, na kujiita wenyewe Walamani, na pia idadi fulani ambao walikuwa kizazi halisi cha Walamani, ambao walivurugwa kukasirika na hawa, au na wale waasi, kwa hivyo walianza vita na ndugu zao.

25 Na wakafanya mauaji, na uporaji; na kisha wangerudi nyuma kwenye milima, na kwenye nyika na mahali pa siri, wakijificha ili wasipatikane, wakipokea kila siku idadi ya waasi, waliojiunga nao.

26 Na hivyo baada ya muda, ndiyo, hata kwa muhula usio wa miaka mingi, walipata kuwa kundi kubwa sana la wezi; na waligundua mipango yote ya siri ya Gadiantoni; na hivyo wakawa wezi wa Gadiantoni.

27 Sasa tazama, hawa wezi walifanya hasara kubwa sana, ndiyo, hata uharibifu mkuu miongoni mwa watu wa Nefi, na pia miongoni mwa watu wa Walamani.

28 Na ikawa kwamba ilikuwa ni muhimu kwamba kuweko na kikomo cha kazi hii ya uharibifu; kwa hivyo walituma jeshi la watu wenye nguvu katika nyika na juu ya milima kutafuta hili kundi la wezi, na kuwaangamiza.

29 Lakini tazama, ikawa kwamba katika mwaka huo huo walirudishwa nyuma hata mpaka kwenye nchi zao. Na hivyo ukaisha mwaka wa themanini wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

30 Na ikawa katika mwanzo wa mwaka wa themanini na moja walipigana tena na kundi hili la wezi, na kuangamiza wengi; na wengi wao pia waliangamizwa.

31 Na walilazimishwa tena kuondoka kwenye nyika na kuondoka kwenye milima hadi

21 *a* MWM Kanisa la Yesu Kristo.

23 *a* Alma 26:22; M&M 107:19.

kwenye nchi zao, kwa sababu ya ukubwa wa idadi ya wale wanyang'anyi ambao walitapakaa kwenye nyika na milimani.

32 Na ikawa kwamba hivyo ukaisha mwaka huu. Na wezi walizidi kuongezeka na kuwa na nguvu, mpaka kwamba wakadharau majeshi yote ya Wanefi, na pia ya Walamani; na walisababisha woga mwingi sana kwa watu nchini kote.

33 Ndiyo, kwani walishambulia sehemu nyingi za nchi, na kufanya uharibifu mwingi kwao; ndiyo, waliua wengi, na kuchukua wengine kama mateka hadi kwenye nyika, ndiyo, na hasa zaidi wanawake na watoto wao.

34 Sasa huu ubaya mkuu, ambao uliwajia watu kwa sababu ya uovu wao, uliwavuruga tena kwa kumkumbuka Bwana Mungu wao.

35 Na hivyo ukaisha mwaka wa themanini na moja wa utawala wa waamuzi.

36 Na katika mwaka wa themanini na mbili walianza [a]kumsahau tena Bwana Mungu wao. Na katika mwaka wa themanini na tatu walianza kuwa na nguvu katika uovu. Na katika mwaka wa themanini na nne hawakurekebisha njia zao.

37 Na ikawa katika mwaka wa themanini na tano walizidi kuwa na nguvu katika kiburi chao, na katika uovu wao; na hivyo walikuwa wanajitayarisha tena kwa maangamizo.

38 Na hivyo ukaisha mwaka wa themanini na tano.

MLANGO WA 12

Wanadamu si waaminifu na ni wapumbavu na ni wepesi kutenda maovu—Bwana huwarudi watu Wake—Ubure wa wanadamu unalinganishwa na uwezo wa Mungu—Katika siku ya hukumu, watu watapata maisha yasiyo na mwisho au laana isiyo na mwisho. Karibia mwaka 6 K.K.

Na hivyo tunaweza kuona vile uwongo, na pia kutoaminika kwa mioyo ya watoto wa binadamu; ndiyo, tunaweza kuona kwamba Bwana katika uzuri wake usio na mwisho hubariki na [a]kufanikisha wale ambao huweka [b]imani yao kwake.

2 Ndiyo, na tunaweza kuona kwa ule wakati anaofanikisha watu wake, ndiyo, kwa kuongeza mavuno yao, na wanyama wao na mifugo yao, na kwa dhahabu, na kwa fedha, na katika kila aina ya vitu vya thamani vya kila aina na umbo; kuachilia maisha yao, na kuwaokoa kutoka kwa mikono ya maadui wao; kugusa mioyo ya maadui wao ili wasitangaze vita dhidi yao; ndiyo, na kwa kifupi, akifanya vitu vyote kwa ustawi na furaha ya watu wake; ndiyo, na hapo ni wakati ambao [a]wanashupaza mioyo yao, na humsahau Bwana Mungu wao, na [b]kumkanyaga chini ya miguu

36 *a* Alma 46:8.

12 1 *a* 2 Nya. 26:5; Zab. 1:2–3.

b Zab. 36:7–8; 2 Ne. 22:2; Mos. 4:6. MWM Tegemea.

2 *a* MWM Ukengeufu.
b Alma 5:53; 3 Ne. 28:35.

yao yule Mtakatifu—ndiyo, na wanafanya hivi kwa sababu ya utulivu wao, na mafanikio yao makubwa sana.

3 Na hivyo tunaona kwamba Bwana [a]asipowaadhibu watu wake kwa mateso mengi, ndiyo, isipokuwa awaadhibishe kwa kifo na kwa vitisho, na kwa njaa na kwa namna yote ya magonjwa, [b]hawatamkumbuka.

4 Ee jinsi gani wapumbavu, na jinsi gani bure, na waovu, na wenye uibilisi, na jinsi gani hufanya mabaya kwa [a]urahisi, na jinsi gani watoto wa watu, hufanya mema polepole, ndiyo, huwa wepesi kuyasikia maneno ya mwovu, na kuweka [b]mioyo yao kwenye vitu vilivyo bure vya ulimwengu!

5 Ndiyo, jinsi gani kwa haraka wanainuliwa kwa [a]kiburi; ndiyo, jinsi gani ni wepesi kwa kujisifu, na kufanya kila aina ya yale ambayo ni ya uovu; na jinsi gani wana upole kumkumbuka Bwana Mungu wao, na kusikiza amri zake, ndiyo, na jinsi gani ni wapole [b]kutembea kwenye njia za hekima!

6 Tazama, hawataki kwamba Bwana Mungu wao, ambaye [a]amewaumba, aongoze na [b]kutawala juu yao; ijapokuwa uzuri wake na rehema yake kuwaelekea, wanachukua kama bure mawaidha yake, na hawataki awe kiongozi wao.

7 Ee ni kubwa jinsi gani hali ya [a]kutokuwa na kitu ya watoto wa watu; ndiyo, hata wako hafifu kuliko mavumbi ya dunia.

8 Kwani tazama, mavumbi ya dunia huvuma hapa na pale, na hata kugawanyika mbali, wakati inavyoamrishwa kufanya hivyo na Mungu wetu mkuu na asiye na mwisho.

9 Ndiyo, tazama kwa sauti yake vilima na milima hutetemeka na [a]kutapatapa.

10 Na kwa [a]uwezo wa sauti yake inavunjika, na kuwa laini, ndiyo, hata kama bonde.

11 Ndiyo, kwa uwezo wa sauti yake dunia [a]yote hutetemeka;

12 Ndiyo, kwa uwezo wa sauti yake, misingi ya miamba, hutikisika hata mpaka katikati.

13 Ndiyo, na ikiwa ataambia dunia—Songa—itasonga.

14 Ndiyo, na ikiwa ataambia [a]dunia—[b]Utarudi nyuma, ili [c]iongeze siku kwa masaa mengi—itafanyika;

15 Na hivyo, kulingana na neno lake dunia hurudi nyuma, na huonekana kwa binadamu kwamba jua linasimama mahali pamoja; ndiyo, na tazama, hivyo ndivyo ilivyo; kwani kwa kweli ni dunia ndiyo husogea na sio jua.

16 Na tazama, pia, ikiwa

3 *a* Mos. 23:21; M&M 98:21; 101:8.
b Amo. 4:6–11.
4 *a* Ku. 32:8.
b Mt. 15:19; Ebr. 3:12.
5 *a* Mit. 29:23. MWM Kiburi.
b MWM Tembea, Tembea na Mungu.
6 *a* Isa. 45:9; M&M 58:30; Musa 7:32–33.
b M&M 60:4.
7 *a* Isa. 40:15, 17; Mos. 4:19; Musa 1:10.
9 *a* 3 Ne. 22:10.
10 *a* 1 Ne. 17:46.
11 *a* Morm. 5:23; Eth. 4:9.
14 *a* Yos. 10:12–14.
b Isa. 38:7–8.
c 2 Fal. 20:8–11.

ataambia kilindi cha [a]maji ya bahari—[b]Kauka—inafanyika.

17 Tazama, ikiwa atauambia huu mlima—[a]Inuka juu, na uangukie mji huo, ili uzikwe—tazama inafanyika.

18 Na tazama, ikiwa mtu [a]anaficha hazina ndani ya ardhi, na Bwana aseme—Ebu [b]ilaaniwe, kwa sababu ya ubaya wa yule aliyeificha—tazama, italaaniwa.

19 Na ikiwa Bwana atasema—Wewe ulaaniwe, kwamba hakuna mtu yeyote atakayekupata sasa hadi milele—tazama, hakuna mtu atakayeipata kutokea hiyo siku hadi milele.

20 Na tazama, ikiwa Bwana atamwambia mtu—Kwa sababu ya uovu wako, utalaaniwa milele—itafanyika.

21 Na ikiwa Bwana atasema—Kwa sababu ya uovu wako utatolewa kutoka kwenye uwepo wangu—atasababisha kwamba itakuwa hivyo.

22 Na ole kwake yeye ambaye atamwambia hivi, kwani itakuwa kwake ambaye atafanya maovu, na hataweza kuokolewa; kwa hivyo, kwa sababu hii, kwamba binadamu wangeokolewa, toba imetangazwa.

23 Kwa hivyo, heri wale ambao watatubu na kusikiza sauti ya Bwana Mungu wao; kwani hawa ndiyo wale ambao [a]wataokolewa.

24 Na Mungu akubali, kwa utimilifu wake mkuu, kwamba watu waonyeshe nia ya kutubu na kufanya matendo mazuri, kwamba wangerudishwa kwenye [a]neema kwa neema, kulingana na vitendo vyao.

25 Na ningetaka kwamba watu wote waokolewe. Lakini tunasoma kwamba katika ile siku kuu ya mwisho kuna wengine ambao watatupwa nje, ndiyo, ambao watatolewa kwenye uwepo wa Bwana;

26 Ndiyo, ambao watawekwa kwa hali yenye taabu isiyo na mwisho, kwa kutimiza maneno ambayo yanasema: Wale ambao wametenda mema watakuwa na [a]maisha yasiyo na mwisho; na wale ambao wametenda maovu watapata [b]laana isiyo na mwisho. Na hivyo ndivyo ilivyo. Amina.

Unabii wa Samweli, Mlamani, kwa Wanefi.

Yenye milango ya 13 hadi 15.

MLANGO WA 13

Samweli Mlamani anatabiri kuangamizwa kwa Wanefi isipokuwa watubu—Hao na utajiri wao wanalaaniwa—Wanakataa na kuwapiga manabii kwa mawe, wanazingirwa na pepo mbaya, na wanatafuta furaha kwa kutenda uovu. Karibia mwaka 6 K.K.

Na ikawa katika mwaka wa themanini na sita, Wanefi walibaki kwenye uovu, ndiyo, katika

16*a* Mt. 8:27.
b Isa. 44:27; 51:10.
17*a* 3 Ne. 8:10.
18*a* Morm. 1:18; Eth. 14:1.
b Hel. 13:17.
23*a* MWM Wokovu.
24*a* MWM Neema.
26*a* Mt. 25:46; Yn. 5:28–29; Rum. 6:13.
b MWM Hukumu.

uovu mwingi, wakati [a]Walamani walitii amri za Mungu, kulingana na sheria ya Musa.

2 Na ikawa kwamba katika mwaka huu kulikuwa na mmoja aliyeitwa Samweli, Mlamani ambaye alikuja kwenye nchi ya Zarahemla, na akaanza kuhuwabiria watu. Na ikawa kwamba alihubiri, siku nyingi, toba kwa watu, na wakamtupa nje, na alikuwa karibu kurudi kwa nchi yake.

3 Lakini tazama, sauti ya Bwana ilimjia, kwamba arejee tena, na kuwatabiria hawa watu vitu vyote vitakavyomjia kwa [a]moyo wake.

4 Na ikawa kwamba hawangemkubalia kwamba aingie kwenye mji; kwa hivyo alienda na kupanda juu ya ukuta wa mji, na kunyosha mkono wake mbele na kupaza sauti, na kutabiria watu vitu vyote ambavyo Bwana aliweka moyoni mwake.

5 Na akawaambia: Tazama, mimi, Samweli, Mlamani, ninaongea maneno ya Bwana ambayo ameweka kwenye moyo wangu; na tazama ameiweka kwenye moyo wangu kuwaambia hawa watu kwamba [a]upanga wa haki unaning'inia juu ya hawa watu; na miaka mia nne haitapita kabla ya upanga wa haki kuwaangukia hawa watu.

6 Ndiyo, [a]uangamizo mzito unawangojea watu hawa, na kwa kweli utawajia watu hawa, na hakuna kitakachowaokoa watu hawa isipokuwa toba na imani kwa Bwana Yesu Kristo, ambaye kwa kweli atakuja duniani, na atavumilia vitu vingi na atauawa kwa ajili ya watu wake.

7 Na tazama, [a]malaika wa Bwana amenitangazia, na alileta habari [b]njema kwa roho yangu. Na tazama, nilitumwa kwenu niwatangazie pia, ili mpate habari njema; lakini tazama mmekataa kunisikiliza.

8 Kwa hivyo, hivyo ndivyo asemavyo Bwana: Kwa sababu ya ugumu wa mioyo ya watu hawa wa Wanefi, wasipotubu nitachukua ahadi yangu yote kutoka kwao, na [a]nitaondoa Roho yangu kutoka kwao, na sitawavumilia tena, na nitageuza mioyo ya ndugu zao dhidi yao.

9 Na miaka [a]mia nne haitapita kabla ya mimi kusababisha kwamba wauawe; ndiyo, nitawaadhibu kwa upanga na njaa na maradhi ya kuambukiza.

10 Ndiyo, nitawatembelea katika hasira yangu kali, na kutakuwa na wengine wa kizazi cha [a]nne ambao wataishi, baina ya maadui wenu, kuona kuangamizwa kwenu kabisa; na hii kwa kweli itakuja isipokuwa mtubu, Bwana anasema; na wale wa kizazi cha nne watawatembelea kwa maaangamizo.

11 Lakini ikiwa mtatubu na [a]kumrudia Bwana Mungu wenu nitabadilisha hasira yangu,

13 1*a* Hel. 15:4–5.
3*a* M&M 100:5.
5*a* Alma 60:29; 3 Ne. 2:19.
6*a* Alma 45:10–14; Hel. 15:17.
7*a* Alma 13:26.
b Isa. 52:7.
8*a* Hel. 6:35.
9*a* Alma 45:10–12.
10*a* 1 Ne. 12:12; 2 Ne. 26:9; 3 Ne. 27:32.
11*a* 3 Ne. 10:5–7.

asema Bwana; ndiyo, hivyo ndivyo asemavyo Bwana, wale watakaotubu na kurudi kwangu watabarikiwa, lakini ole kwa yule ambaye hatatubu.

12 Ndiyo, [a]ole kwa huu mji mkuu wa Zarahemla; kwani tazama, ni kwa sababu ya wale wenye haki kwamba umeokolewa; ndiyo, ole kwa mji huu mkuu, kwani ninaona, asema Bwana, kwamba kuna wengi, ndiyo, hata sehemu kubwa ya huu mji mkuu ambao watashupaza mioyo yao dhidi yangu, asema Bwana.

13 Lakini heri wale ambao watatubu, kwani hao ndiyo nitakaowasamehe. Lakini tazama, kama haingekuwa kwa wale wenye haki ambao wako kwenye mji huu mkuu, tazama, ningesababisha kwamba [a]moto uje chini kutoka mbinguni na kuuangamiza.

14 Lakini tazama, ni kwa ajili ya wale wenye haki kwamba umesamehewa. Lakini tazama, wakati unawadia, asema Bwana, kwamba wakati mtatupa walio wenye haki kutoka miongoni mwenu, ndipo mtakapokuwa tayari kwa uangamizo; ndiyo, ole kwa huu mji mkuu, kwa sababu ya uovu na machukizo ambayo yamo ndani yake.

15 Ndiyo, na ole kwa mji wa Gideoni, kwa uovu na machukizo ambayo yamo ndani yake.

16 Ndiyo, na ole kwa miji yote ambayo iko katika nchi karibu na hapa, ambayo imemilikiwa na Wanefi, kwa sababu ya uovu na machukizo ambayo yamo ndani yao.

17 Na tazama, [a]laana itakujia juu ya nchi, asema Bwana wa Majeshi, kwa sababu ya watu ambao wako nchini, ndiyo, kwa sababu ya uovu wao na machukizo yao.

18 Na itakuwa, asema Bwana wa Majeshi, ndiyo, ambaye ni Mungu wetu mkuu na wa kweli, kwamba yeyote ambaye [a]ataficha hazina ardhini hataipata tena, kwa sababu ya laana kuu ya nchi, isipokuwa awe mtu mwenye haki na aifiche kwenye Bwana.

19 Kwani ninawataka, asema Bwana, kwamba wafiche hazina zao kwangu; na laana iwe kwa wale wasioficha hazina zao kwangu; kwani hakuna yeyote ambaye huficha hazina zake kwangu isipokuwa awe mwenye haki; na yule ambaye hafichi hazina zake kwangu, amelaaniwa, na pia ile hazina, na hakuna atakayeikomboa kwa sababu ya laana ya nchi.

20 Na siku itawadia kwamba wataficha hazina zao, kwa sababu wameweka mioyo yao kwenye utajiri; na kwa sababu wameweka mioyo yao kwenye utajiri wao, na wataficha hazina zao wakati watakimbia kutoka kwa maadui wao; kwa sababu hawatazificha kwangu, walaaniwe na pia hazina zao; na katika siku hio ndipo watakapouawa, asema Bwana.

21 Tazama ninyi, watu wa huu mji mkuu, na sikilizeni

12*a* 3 Ne. 8:8, 24; 9:3.
13*a* Mwa. 19:24; 2 Fal. 1:9–16; 3 Ne. 9:11.
17*a* Hel. 12:18.
18*a* Morm. 1:18; Eth. 14:1.

maneno yangu; ndiyo, [a]sikilizeni maneno ambayo Bwana anasema; kwani tazama, anasema kwamba mmelaaniwa kwa sababu ya utajiri wenu, na pia utajiri wenu umelaaniwa kwa sababu mmeweka mioyo yenu juu yake, na hamjasikiliza maneno ya yule aliyewapatia huo utajiri.

22 Hammkumbuki Bwana Mungu wenu kwa vitu ambavyo amewabariki navyo, lakini kila siku mnakumbuka [a]utajiri wenu, bila kumshukuru Bwana Mungu wenu kwa hivyo vitu; ndiyo, mioyo yenu haimkaribii Bwana, lakini inavimba kwa [b]kiburi kikuu, kwa kujisifu, na kwa uvimbe mkuu, [c]mashindano, ukorofi, uovu, mateso, na mauaji, na kila aina ya uovu.

23 Kwa sababu hii Bwana Mungu amesababisha kwamba laana ije kwa nchi, na pia kwa utajiri wenu, na hii ni kwa sababu ya maovu yenu.

24 Ndiyo, ole kwa watu hawa, kwa sababu ya huu muda ambao umewadia, wakati [a]mnatupa nje manabii, na kuwacheka, na kuwatupia mawe, na kuwaua, na kufanya kila aina ya uovu kwao, hata vile walioishi zamani walivyofanya.

25 Na sasa mkizungumza, mnanena: Ikiwa siku zetu zingekuwa katika siku za [a]babu zetu wa zamani, hatungewaua manabii; hatungewapiga kwa mawe, na kuwatupa nje.

26 Tazama ninyi ni wabaya kuliko hao; kadiri Bwana anavyoishi, ikiwa [a]nabii anaweza kuja miongoni mwenu na kuwatangazia neno la Bwana, ambalo linashuhudia dhambi zenu na uovu, [b]mnamkasirikia, na kumtupa nje na kutafuta njia za namna zote kumwangamiza; ndiyo, mtasema kwamba ni [c]nabii wa uwongo, na kwamba ni mwenye dhambi, na mwenye kutoka kwa ibilisi, kwa sababu [d]anashuhudia kwamba vitendo vyenu ni viovu.

27 Lakini tazama, ikiwa mtu atatokea miongoni mwenu na kusema: Fanya hivi, na hakutakuweko na ubaya; fanya vile na hamtaumia; ndiyo, atasema: Tembeeni katika kiburi cha mioyo yenu yenyewe; ndiyo, tembeeni katika kiburi cha macho yenu, na fanya chochote ambacho moyo wako unapenda—na ikiwa mtu atatokea miongoni mwenu na kusema hivi, hapo mtamkubali, na kusema ni [a]nabii.

28 Ndiyo, mtamheshimu, na mtampatia mali yenu; mtampatia dhahabu yenu, na fedha yenu, na mtamvalisha mavazi ya thamani; na kwa sababu anazungumza maneno ya [a]kusifu ya uongo kwenu, na anasema kwamba yote ni mema, kwa hivyo hamtampata na makosa.

21 *a* MWM Sikiliza.
22 *a* Lk. 12:34.
MWM Malimwengu; Ukwasi.
b MWM Kiburi.
c MWM Husuda.
24 *a* 2 Nya. 36:15–16; 1 Ne. 1:20.
25 *a* Mdo. 7:51.
26 *a* 2 Nya. 18:7; Lk. 16:31.
b Isa. 30:9–10.
c Mt. 13:57.
d Gal. 4:16.
27 *a* Mik. 2:11.
MWM Ukuhani wa uongo.
28 *a* 2 Tim. 4:3–4.

29 Ee ninyi kizazi kilichopotea; ninyi watu wagumu na wenye shingo ngumu, kwa muda gani mnadhani Bwana atawavumilia? Ndiyo, kwa muda gani mtakubali kuongozwa na [a]wapumbavu na [b]vipofu? Ndiyo, kwa muda gani [c]mtachagua giza juu ya [d]mwangaza?

30 Ndiyo, tazama, ghadhabu ya Bwana imewashwa dhidi yenu; tazama, amelaani nchi kwa sababu ya uovu wenu.

31 Na tazama, wakati unawadia kwamba atalaani utajiri wenu, kwamba [a]utateleza, kwamba hamtaweza kuushika; na katika siku za umasikini wenu hamtazishika.

32 Na katika siku za umasikini wenu mtamlilia Bwana; na mtalia bure, kwani ukiwa wenu utakuwa umewajia kitambo, na uharibifu wenu umekamilishwa; na hapo mtatoa machozi na kulia wakati huo, asema Bwana wa Majeshi. Na hapo mtaomboleza, na kusema:

33 Ee [a]kwamba nilikuwa nimetubu, na sikuwaua manabii, na [b]kuwapiga kwa mawe, na kuwatupa nje. Ndiyo, katika siku hiyo mtasema: Ee kwamba tungemkumbuka Bwana Mungu wetu wakati ambapo alitupatia utajiri wetu, na hapo haungeteleza, kwamba tuupoteze; kwani tazama, utajiri wetu umetuwacha.

34 Tazama, tunaweka hapa chombo na kesho yake kimeenda; na tazama, panga zetu zinachukuliwa kutoka kwetu wakati tunapozitafuta kwa vita.

35 Ndiyo, tumeficha hazina zetu na zimeponyokea mbali kutoka kwetu, kwa sababu ya laana ya nchi.

36 Ee kwamba tulitubu wakati ambao neno la Bwana lilitujia; kwani tazama nchi imelaaniwa, na vitu vyote vimekuwa vya kuteleza, na hatuwezi kuvishika.

37 Tazama, tumezingirwa na pepo mbaya, ndiyo, tumezungukwa na malaika wa yule ambaye anataka kuangamiza roho zetu. Tazama, uovu wetu ni mkuu. Ee Bwana, huwezi kugeuza hasira yako kutoka kwetu? Na hii itakuwa lugha yenu wakati huo.

38 Lakini tazama, [a]siku zenu za majaribio zimepita; [b]mmechelewesha siku yenu ya wokovu mpaka imechelewa milele, na maangamizo yenu yamehakikishwa; ndiyo, kwani mmetafuta siku zote za maisha yenu yale ambayo hamwezi kupata; na mmetafuta [c]furaha kwa kufanya uovu, kitu ambacho ni kinyume cha asili ya haki ambayo huja kutoka kwa mkuu na Kiongozi wetu wa Milele.

39 Ee ninyi watu wa nchi, ningetaka kwamba msikilize maneno yangu! Na ninaomba kwamba hasira ya Bwana

29 *a* 2 Ne. 28:9.
b Mt. 15:14.
c Yn. 3:19.
d Ayu. 24:13.

31 *a* Morm. 1:17–18.

33 *a* Morm. 2:10–15.
b Mt. 23:37.

38 *a* Morm. 2:15.
b Alma 34:33–34.
c Alma 41:10–11.

itolewe kutoka kwenu, na kwamba mtatubu na kukombolewa.

MLANGO WA 14

Samweli anatabiri kwamba kutakuwa na mwangaza wakati wa usiku na nyota mpya wakati Kristo atakapozaliwa—Kristo anakomboa watu kutokana na kifo cha kimwili na cha kiroho—Ishara za kifo Chake zitajumuisha siku tatu za giza, kupasuka kwa miamba, na mabadiliko makubwa ya ulimwengu. Karibia mwaka 6 K.K.

Na sasa ikawa kwamba [a]Samweli, Mlamani, alitabiri vitu vingi zaidi ambavyo haviwezi kuandikwa.

2 Na tazama, aliwaambia: Tazama, ninawapatia ishara; kwani miaka mitano zaidi inakuja, na tazama, ndipo atakuja Mwana wa Mungu kuwakomboa wale wote ambao wataamini kwa jina lake.

3 Na tazama, hii nitawapatia kama [a]ishara wakati wa kuja kwake; kwani tazama, kutakuwa na mwangaza mwingi mbinguni, kiasi kwamba usiku kabla ya kuja kwake hakutakuwa na giza, mpaka kwamba itaonekana kwa binadamu kama ni mchana.

4 Kwa hivyo, kutakuwa na siku moja na usiku mmoja na siku, kama kwamba ni siku moja bila usiku; na hii itakuwa ishara kwenu kutazamia; kwani mtafahamu kutokea kwa jua na pia kutua kwake; kwa hivyo watajua kwa hakika kwamba kutakuwa na siku mbili na usiku mmoja; walakini usiku hautakuwa na giza; na itakuwa usiku kabla [a]yeye azaliwe.

5 Na tazama, [a]nyota mpya itatokea, aina moja ambayo hamjawahi kuona kamwe; na hii pia itakuwa ishara kwenu.

6 Na tazama haya si yote, kutakuwa na ishara nyingi na vituko mbinguni.

7 Na itakuwa kwamba ninyi nyote mtashangaa, na kustaajabu, kiasi kwamba [a]mtainama kwenye ardhi.

8 Na itakuwa kwamba yeyote [a]atakayeamini kwa Mwana wa Mungu, yeye atakuwa na maisha yasiyo na mwisho.

9 Na tazama, hivyo ndivyo Bwana ameniamuru, kupitia kwa malaika wake, kwamba nije na kusema hiki kitu kwenu; ndiyo, ameamuru kwamba nitabiri hivi vitu kwenu; ndiyo, amesema kwangu: Paza sauti kwa hawa watu, tubuni na mtayarishe njia ya Bwana.

10 Na sasa, kwa sababu mimi ni Mlamani, na nimewazungumzia maneno ambayo Bwana ameniamuru, na kwa sababu yalikuwa magumu dhidi yenu, mmenikasirikia na mnataka kuniangamiza, na [a]mmenitupa nje kutoka miongoni mwenu.

11 Na mtasikia maneno yangu, kwani, ni kwa sababu ya hili kusudi nimepanda ukuta wa

14 1*a* Hel. 13:2.
3*a* 3 Ne. 1:15.
4*a* MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.
5*a* Mt. 2:1–2; 3 Ne. 1:21.
7*a* 3 Ne. 1:16–17.
8*a* Yn. 3:16.
10*a* Hel. 13:2.

mji huu, ili muweze kusikia na kujua hukumu ya Mungu ambayo inawangojea kwa sababu ya uovu wenu, na pia kwamba mngejua hali ya toba;

12 Na pia kwamba mngejua kuhusu kuja kwa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, [a]Baba wa mbingu na dunia, Muumba wa vitu vyote tangu mwanzo; na kwamba mjue ishara za kuja kwake, na tumaini kwamba mngeamini katika jina lake.

13 Na ikiwa [a]mtaamini katika jina lake mtatubu dhambi zenu, kwamba kwa kufanya hivyo mngepata kusamehewa kupitia kwa [b]uzuri wake.

14 Na tazama, tena, ishara nyingine ninawapatia, ndiyo, ishara ya kifo chake.

15 Kwani tazama, lazima kwa kweli afe kwamba [a]wokovu uje; ndiyo, inampasa yeye kwa lazima kwamba afe, ili kutimiza [b]ufufuo wa wafu, kwamba kwa hiyo sababu binadamu waletwe kwenye uwepo wa Bwana.

16 Ndiyo, tazama, hiki kifo huleta kutimiza ufufuo, na [a]hukomboa binadamu wote kutokana na kifo cha kwanza—hicho kifo cha roho; kwani binadamu wote, kwa sababu ya [b]kuanguka kwa Adamu [c]wakitolewa kutoka uwepo wa Bwana, wanafikiriwa kama [d]waliokufa, kwa vitu vya kimwili na vitu vya kiroho.

17 Lakini tazama, ufufuko wa Kristo [a]unakomboa binadamu, ndiyo, hata binadamu wote, na huwarejesha kwenye uwepo wa Bwana.

18 Ndiyo, na inasababisha kutimiza hali ya toba, kwamba yeyote anayetubu yeye hatatupwa chini na kuwekwa kwenye moto; lakini yeyote ambaye hatatubu atawekwa chini na kutupwa kwenye moto; na hapo kinawajia kifo cha roho, ndiyo, kifo cha pili, kwani wametolewa tena kwa vitu vinavyohusika na haki.

19 Kwa hivyo tubuni ninyi, tubuni ninyi, isiwe kwamba kwa kuvijua hivi vitu na kutovifanya mtalaaniwa, na mtaletwa chini kwenye kifo cha pili.

20 Lakini tazama, vile niliwaambia kuhusu [a]ishara nyingine, ishara ya kifo chake, tazama, katika siku hiyo ambayo atapatwa na kifo jua litawekwa [b]giza na kukataa kutoa mwangaza wake kwenu; na pia mwezi na nyota; na hakutakuwa na mwangaza juu ya hii nchi, hata kutokea wakati atakapokufa, kwa muda wa siku [c]tatu, hadi kwenye siku atakayofufuka tena kutoka kwa wafu.

21 Ndiyo, wakati atakapokata roho kutakuwa na vishindo vya

12*a* Mos. 3:8; 3 Ne. 9:15; Eth. 4:7. MWM Yesu Kristo.
13*a* Mdo. 16:30–31.
b M&M 19:16–20.
15*a* MWM Mwokozi.
b Alma 42:23.
MWM Ufufuko.
16*a* MWM Mpango wa Ukombozi.
b MWM Anguko la Adamu na Hawa.
c Alma 42:6–9.
d MWM Mauti ya Kiroho.
17*a* MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
20*a* 3 Ne. 8:5–25.
b Lk. 23:44.
c Mos. 3:10.

[a]ngurumo na radi kwa muda wa masaa mengi, na ardhi itatingishika na kutetemeka; na miamba ambayo iko juu ya hii dunia, ambayo yote iko juu ya dunia na chini, ambayo mnajua wakati huu kama ni nzima, au sehemu yake kwa jumla ni nzima, [b]itavunjika;

22 Ndiyo, yatagawanyika mara mbili, na kutokea hapo itapatikana kwenye [a]pindo na kwenye nyufa, na kwa vipande vilivyovunjika juu ya dunia yote, ndiyo, juu ya nchi na chini yake.

23 Na tazama, kutakuwa na dhoruba kubwa, na kutakuwa na milima mingi itakayolainishwa, kama bonde, na kutakuwa na mahali pengi ambapo sasa hivi panaitwa mabonde ambayo itakuwa milima, ambayo urefu wake ni mkubwa.

24 Na barabara nyingi zitaharibiwa, na [a]miji mingi itakuwa jangwa.

25 Na [a]makaburi mengi yatafunguka, na yataachilia wengi wa wafu wao; na watakatifu wengi watajidhihirisha kwa wengi.

26 Na tazama, hivyo ndivyo [a]malaika ameniambia; kwani aliniambia kwamba kutakuwa na vishindo vya ngurumo na radi kwa muda wa masaa mengi.

27 Na aliniambia kwamba wakati vishindo vya ngurumo na radi vitakuwa vikiendelea, na dhoruba, kwamba hivi vitu vitafanyika, na kwamba [a]giza litafunika dunia yote kwa muda wa siku tatu.

28 Na malaika aliniambia kwamba wengi wataona vitu vingi kuliko hivi, kwa kusudi kwamba wapate kuamini [a]ishara hizi na maajabu haya yapate kutimizwa juu ya nchi yote, kwa kusudi kwamba kusiwe na sababu ya kutoamini miongoni mwa watoto wa watu—

29 Na hili kwa kusudi kwamba yeyote atakayeamini ataokolewa, na kwamba yeyote ambaye hataamini, [a]hukumu ya haki ingewajia; na pia wakihukumiwa hapo watajiletea wenyewe hukumu yao.

30 Na sasa kumbukeni, kumbukeni, ndugu zangu, kwamba yeyote anayeangamia, anaangamia kwa kupenda kwake; na yeyote afanyaye dhambi, anaifanya kwake mwenyewe; kwani tazama, mko [a]huru; mmekubaliwa kujichagulia; kwani tazama, Mungu amewapatia [b]elimu na amewafanya huru.

31 Amewapatia nafasi kwamba [a]mjue mema na maovu, na amewapatia kwamba [b]mchague uzima au kifo; na mnaweza kutenda mazuri na [c]mrejeshwe kwa yale yaliyo mema, au kupata yale yaliyo mema kurudishwa

21 *a* 3 Ne. 8:6.
b 3 Ne. 10:9.
22 *a* 3 Ne. 8:18.
24 *a* 3 Ne. 9:3–12.
25 *a* Mt. 27:50–54; 3 Ne. 23:9–11.
26 *a* Alma 13:26.
27 *a* 1 Ne. 19:10; 3 Ne. 8:3.
28 *a* 1 Ne. 12:4–5.
29 *a* MWM Hukumu ya mwisho.
30 *a* 2 Ne. 2:26–29; Musa 6:56.
MWM Haki ya uamuzi.
b MWM Maarifa.
31 *a* Moro. 7:16.
b 2 Ne. 2:28–29; Alma 3:26–27.
c Alma 41:3–5.

kwenu; au mnaweza kutenda maovu, na mpate yale yaliyo maovu yarudishwe kwenu.

MLANGO WA 15

Bwana aliwarudi Wanefi kwa sababu Yeye aliwapenda—Walamani walioongoka wako imara na thabiti katika imani—Bwana atakuwa na huruma kwa Walamani katika siku za mwisho. Karibia mwaka 6 K.K.

Na sasa, ndugu zangu wapendwa, tazama, ninawatangazia kwamba msipotubu nyumba zenu zitaachwa ziwe na [a]ukiwa.

2 Ndiyo, msipotubu, wanawake wenu watakuwa na sababu ya kuomboleza wakati watakapokuwa wakinyonyesha; kwani mtajaribu kukimbia lakini hakutakuwa na mahali pa kimbilio; ndiyo, na ole kwa wale ambao [a]wana mimba, kwani watakuwa wazito na hawataweza kukimbia; kwa hivyo, watakanyagwa chini na kuachwa kuangamia.

3 Ndiyo, ole kwa watu hawa ambao wanaitwa watu wa Nefi isipokuwa watubu, wakati wataona ishara hizi zote na maajabu ambayo yataonyeshwa kwao; kwani tazama, wamekuwa watu waliochaguliwa na Bwana; ndiyo, aliwapenda watu wa Nefi, na pia [a]amewakemea; ndiyo, katika siku zao za dhambi amewakemea kwa sababu anawapenda.

4 Lakini tazama ndugu zangu, amewachukia Walamani kwa sababu vitendo vyao vimekuwa viovu wakati wote, na wanafanya hivyo kwa sababu ya uovu wa [a]desturi ya babu zao. Lakini tazama, wokovu umekuja kwao kupitia kwa mahubiri ya Wanefi; na kwa kusudi hili Bwana [b]amewaongezea siku zao.

5 Na ningetaka kwamba mwone kwamba sehemu yao [a]kubwa wako kwenye kazi yao, na wanatembea kwa uangalifu mbele ya Mungu, na wanatii amri zake na sheria zake na maamuzi yake kulingana na sheria ya Musa.

6 Ndiyo, ninawaambia, kwamba sehemu yao kubwa wanafanya hivi, na wanajaribu kwa bidii bila kuchoka ili walete ndugu zao waliosalia kwa elimu ya ukweli; kwa hivyo, kuna wengi ambao wanaongeza idadi yao kila siku.

7 Na tazama, mnajua wenyewe, kwani mmejionea, kwamba vile wengi wao wanaletwa kuelimishwa ukweli, na kujua uovu na desturi za machukizo za babu zao, na wameongozwa kuamini maandiko matakatifu, ndiyo, utabiri wa manabii watakatifu, ambao umeandikwa, ambao unawaongoza kuwa na imani kwa Bwana, na kwenye toba, imani na toba ambavyo huwaletea mabadiliko katika [a]mioyo yao—

8 Kwa hivyo, vile wengi wa-

15 1*a* Mt. 23:37–38.
2*a* Mt. 24:19.
3*a* Mit. 3:12; Ebr. 12:5–11; M&M 95:1.
4*a* MWM Mapokeo.
b Alma 9:16.
5*a* Hel. 13:1.
7*a* MWM Mwongofu, Uongofu.

mekuja kwa ukweli huu, mnajua wenyewe kwamba wako [a]imara na thabiti katika imani, na pia kitu ambamo kwayo wamefanywa huru.

9 Na mnajua pia kwamba [a]wamezika silaha zao za vita, na wanaogopa kuzichukua wasije kwa njia yoyote wafanye dhambi; ndiyo, mnaona kwamba wanaogopa kutenda dhambi—kwani tazama wanakubali wenyewe kwamba wakanyagwe chini na kuuawa na maadui wao, na hawatainua panga zao dhidi yao, na hivyo kwa sababu ya imani yao kwa Kristo.

10 Na sasa, kwa sababu ya uthabiti wao wakati wanaamini kwenye hicho kitu ambacho wanaamini, kwani kwa sababu ya uthabiti wao mara wakielimishwa, tazama, Bwana atawabariki na kuongeza siku zao, ijapokuwa ubaya wao—

11 Ndiyo, hata kama wanafifia kwa kutoamini Bwana [a]ataongeza siku zao, mpaka wakati utatimia ambao umezungumzwa na babu zetu, na pia nabii [b]Zeno, na manabii wengine wengi, kuhusu [c]kurudishwa kwa ndugu zetu, Walamani, tena kwa ufahamu wa ukweli—

12 Ndiyo, nawaambia, kwamba katika siku za baadaye [a]ahadi za Bwana zimeelekezwa kwa ndugu zetu, Walamani; na ijapokuwa mateso mengi ambayo watakuwa nayo, na ingawa [b]watafukuzwa huku na kule duniani, na kuwindwa, na kushambuliwa na kutawanywa ugenini, wakiwa hawana mahali pa kimbilio, Bwana [c]atawarehemu.

13 Na hii ni kulingana na unabii, kwamba [a]watarejeshwa kwenye ufahamu wa ukweli, ambao ni ufahamu wa Mkombozi wao, na [b]mchungaji wao mkuu na wa kweli, na kuhesabiwa miongoni mwa kondoo wake.

14 Kwa hivyo nawaambia, itakuwa [a]bora kwao kuliko kwenu isipokuwa mtubu.

15 Kwani tazama, kama kazi kuu [a]zingeonyeshwa kwao ambazo zimeonyeshwa kwenu, ndiyo, kwao ambao wamefifia kwa kutoamini kwa sababu ya desturi za babu zao, mnaweza kuona wenyewe kwamba hawangeweza tena kufifia kwa kutoamini.

16 Kwa hivyo, Bwana asema: Sitawaangamiza kabisa, lakini nitasababisha kwamba wakati nitaona ni hekima kwangu watanirudia, asema Bwana.

17 Na sasa tazama, asema Bwana, kuhusu watu wa Wanefi: Kama hawatatubu, na kujaribu kufanya yale ninayotaka, [a]nitawaangamiza kabisa, asema Bwana, kwa sababu ya kutoamini kwao ijapokuwa kazi nyingi kubwa ambayo

8 *a* Alma 23:6; 27:27; 3 Ne. 6:14.
9 *a* Alma 24:17–19.
11 *a* Alma 9:16.
b Hel. 8:19.
c 2 Ne. 30:5–8.
12 *a* Eno. 1:12–13.
b Morm. 5:15.
c 1 Ne. 13:31; 2 Ne. 10:18–19; Yak. (KM) 3:5–6.
13 *a* 3 Ne. 16:12.
b MWM Mchungaji Mwema.
14 *a* Hel. 7:23.
15 *a* Mt. 11:20–23.
17 *a* Hel. 13:6–10.

nimefanya miongoni mwao; na kwa ukweli vile Bwana anavyoishi vitu hivi vitafanyika, asema Bwana.

MLANGO WA 16

Wanefi ambao wanamwamini Samweli wanabatizwa na Nefi—Samweli hawezi kuuawa kwa mishale na mawe ya Wanefi ambao hawajatubu—Wengine wanashupaza mioyo yao, na wengine wanawaona malaika—Wasiosadiki wanasema hakuna maana ya kuamini katika Kristo na kuja Kwake katika Yerusalemu. Karibia mwaka 6–1 K.K.

Na sasa, ikawa kwamba kulikuwa na wengi ambao walisikia maneno ya Samweli, Mlamani, ambayo alizungumzia kwenye ukuta wa mji. Na kadiri walivyoamini neno alilosema walienda na kumtafuta Nefi; na walipoenda na kumpata waliungama dhambi zao kwake bila kuacha dhambi yoyote nyuma, wakitaka kwamba wangebatizwa kwa Bwana.

2 Lakini kadiri ambao hawakuyaamini maneno ya Samweli walimkasirikia; na walimtupia mawe akiwa kwenye ukuta, na wengi pia walimpiga mishale wakati alipokuwa anasimama kwenye ukuta; lakini Roho wa Bwana alikuwa naye, mpaka kwamba hawangeweza kumpiga na mawe yao wala mishale yao.

3 Sasa wakati walipoona kwamba hawangeweza kumpiga, kulikuwa na wengi zaidi ambao waliamini maneno yake, mpaka kwamba walimwendea Nefi kubatizwa.

4 Kwani tazama, Nefi alikuwa anabatiza, na kutabiri, na kuhubiri, na kuwaambia kwamba watubu, akiwaonyesha ishara na maajabu, akifanya [a]miujiza miongoni mwa watu, ili wajue kwamba Kristo atazaliwa hivi [b]karibuni—

5 Akiwaambia vitu ambavyo lazima vifanyike, ili wajue na wakumbuke wakati wa kufanyika kwao kwamba imefanywa kujulikana kwao mbeleni, kwamba wangeamini; kwa hivyo jinsi vile wengi waliyaamini maneno ya Samweli walienda mbele kwake kubatizwa, kwani walikuja kutubu na kuungama dhambi zao.

6 Lakini sehemu kubwa yao hawakuyaamini maneno ya Samweli; kwa hivyo walipoona kwamba hawangeweza kumpiga kwa mawe yao na mishale yao, walipigia makapteni wao makelele, wakisema: Chukueni huyu mtu na mmfunge, kwani tazama ana ibilisi; na kwa sababu ya uwezo wa ibilisi ambao uko ndani yake hatuwezi kumpiga kwa mawe yetu na mishale yetu; kwa hivyo mkamateni na mmfunge, na kumpeleka mbali.

7 Na walipoenda mbele kumkamata, tazama, alijitupa kutoka kwenye ukuta, na kutoroka kutoka nchi yao, ndiyo, hadi kwenye nchi yake, na akaanza

16 4*a* MWM Muujiza. | *b* Hel. 14:2.

kuhubiri na kutoa unabii miongoni mwa watu wake.

8 Na tazama, hakusikika tena miongoni mwa Wanefi; na hivyo ndivyo zilikuwa shughuli za watu.

9 Na hivyo ukaisha mwaka wa themanini na sita wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

10 Na hivyo pia ukaisha mwaka wa themanini na saba wa utawala wa waamuzi, sehemu kubwa ya watu wakibaki katika kiburi chao na uovu, na sehemu ndogo ikitembea kwa uangalifu mbele ya Mungu.

11 Na hii ilikuwa hali pia, katika mwaka wa themanini na nane wa utawala wa waamuzi.

12 Na kulikuwa tu na mabadiliko machache katika shughuli za watu, isipokuwa watu walianza kujiimarisha katika uovu, na kufanya mengi ya yale yaliyo kinyume cha amri za Mungu, katika mwaka wa themanini na tisa wa utawala wa waamuzi.

13 Lakini ikawa katika mwaka wa tisini wa utawala wa waamuzi, kulikuwa na [a]ishara kubwa zilizoonyeshwa kwa watu, na maajabu; na maneno ya manabii [b]yalianza kutimizwa.

14 Na [a]malaika walionekana kwa watu, watu wenye hekima, na kuwatangazia habari njema ya shangwe kuu; hivyo katika mwaka huu maandiko yalianza kutimizwa.

15 Walakini, watu walianza kushupaza mioyo yao, wote isipokuwa sehemu yao iliyoamini zaidi, wote Wanefi na Walamani, na wakaanza kutegemea nguvu zao wenyewe na katika hekima yao [a]wenyewe, wakisema:

16 Baadhi ya vitu walibahatisha vyema, miongoni mwa vingi; lakini tazama, tunajua kwamba kazi hizi zote kubwa na za ajabu haziwezi kutimizwa, ambazo zimezungumziwa.

17 Na walianza kubishana na kushindana miongoni mwao, wakisema:

18 Kwamba [a]sio ya maana kwamba kiumbe kama Kristo kitakuja; ikiwa hivyo, na awe Mwana wa Mungu, Baba wa mbingu na dunia, vile ilizungumziwa, kwa nini asijidhihirishe kwetu kama kwa wale walio Yerusalemu?

19 Ndiyo, kwa nini hatajidhihirisha kwa nchi hii kama vile nchi ya Yerusalemu?

20 Lakini tazama, tunajua kwamba hii ni [a]desturi iliyo mbovu, ambayo imetolewa chini kwetu na babu zetu, kutusababisha kwamba tuamini kwa kitu kikubwa na cha ajabu ambacho kitakuja kutimizwa, lakini sio miongoni mwetu, lakini katika nchi iliyo mbali, nchi ambayo hatujui; kwa hivyo wanaweza kutuweka kwenye ujinga, kwani hatuwezi [b]kushuhudia kwa macho yetu kwamba ni ya kweli.

21 Na wataweza, kwa njia ya werevu na siri ya ustadi wa mwovu, kufanya siri kubwa

13 *a* 3 Ne. 1:4.
b Hel. 14:3–7.
14 *a* Alma 13:26.
15 *a* Isa. 5:21.
18 *a* Alma 30:12–13.
20 *a* MWM Mapokeo.
b Eth. 12:5–6, 19.

ambayo hatuwezi kuielewa, ambayo itatuweka chini kuwa watumwa kwa maneno yao, na pia watumishi kwao, kwani tunawategemea kutufundisha neno; na hivyo watatuweka kwenye ujinga ikiwa tutakubali kuongozwa na hao, siku zote za maisha yetu.

22 Na watu waliwaza mioyoni mwao vitu vingi sana, ambavyo vilikuwa vya upumbavu na [a]bure; na walisumbuliwa sana, kwani Shetani aliwavuruga kwa kutenda maovu siku zote; ndiyo, alizunguka akisambaza uvumi na mabishano nchini, ili ashupaze mioyo ya watu dhidi ya vile vitu ambavyo vilikuwa vizuri na dhidi ya vile ambavyo vitakuja.

23 Na ijapokuwa ishara na maajabu ambayo yalifanyika miongoni mwa watu wa Bwana, na miujiza mingi ambayo walifanya, Shetani alishikilia mioyo ya watu nchini kote.

24 Na hivyo ukaisha mwaka wa tisini wa utawala wa waamuzi juu ya watu wa Nefi.

25 Na hivyo kikamalizika kitabu cha Helamani, kulingana na maandiko ya Helamani na wanawe.

NEFI WA TATU
KITABU CHA NEFI

MWANA WA NEFI, AMBAYE ALIKUWA MWANA WA HELAMANI

Na Helamani alikuwa mwana wa Helamani, ambaye alikuwa mwana wa Alma, ambaye alikuwa mwana wa Alma, ambaye alikuwa wa uzao wa Nefi ambaye alikuwa mwana wa Lehi, ambaye alitoka Yerusalemu katika mwaka wa kwanza wa utawala wa Zedekia, mfalme wa Yuda.

MLANGO WA 1

Nefi, mwana wa Helamani, anaondoka nje ya nchi, na mwana wake Nefi anaandika maandishi—Ingawa ishara na maajabu ni mengi, walio waovu wanapanga kuwaua wenye haki—Usiku wa kuzaliwa kwa Kristo unafika—Ishara inatolewa, na nyota mpya inaonekana—Uwongo na udanganyifu unaongezeka, na wezi wa Gadiantoni wanawaua wengi. Karibia mwaka 1–4 B.K.

SASA ikawa kwamba mwaka wa tisini na moja ulikuwa umepita na ilikuwa miaka [a]mia sita tangu wakati ambao Lehi aliondoka Yerusalemu; na ilikuwa katika mwaka ambao Lakoneyo alikuwa mwamuzi

22*a* MWM Majivuno, Siofaa.

[3 NEFI]
1 1*a* 2 Ne. 25:19.

mkuu na msimamizi juu ya nchi.

2 Na Nefi, mwana wa Helamani, alikuwa ameondoka kutoka nchi ya Zarahemla, na kutoa amri kwa mwana wake [a]Nefi, ambaye alikuwa mwana wake mkubwa, kuhusu [b]mabamba ya shaba nyeupe, na kumbukumbu zote ambazo zilikuwa zimewekwa, na vitu vyote ambavyo vilichukuliwa kama vitakatifu kuanzia kuondoka kwa Lehi kutoka Yerusalemu.

3 Kisha aliondoka nje ya nchi, na [a]alikoenda, hakuna mtu yeyote ajuaye; na mwana wake Nefi alihifadhi maandishi badala yake, ndiyo, maandishi ya hawa watu.

4 Na ikawa kwamba katika mwanzo wa mwaka wa tisini na mbili, tazama, utabiri wa manabii ulianza kutimizwa zaidi kabisa; kwani kulianza kuwa na ishara kubwa na miujiza mikubwa kutokea miongoni mwa watu.

5 Lakini kulikuwa na wengine walioanza kusema kwamba wakati umepita kwa yale maneno kutimizwa, ambayo [a]yalizungumzwa na Samweli, Mlamani.

6 Na walianza kufurahia ndugu zao, wakisema: Tazama wakati umepita, na maneno ya Samweli hayajatimizwa; kwa hivyo, shangwe yenu na imani yenu katika hiki kitu imekuwa bure.

7 Na ikawa kwamba walifanya makelele mengi kote nchini; na watu walioamini walianza kuwa na huzuni sana, wakiogopa kwamba hivyo vitu ambavyo vilizungumzwa havingetimizwa.

8 Lakini tazama, walichunguza wakati wote ule mchana na ule usiku na ule mchana siku ile ambayo itakuwa ni kama siku moja kama vile hakuna usiku, kwamba wangejua kuwa imani yao haikuwa bure.

9 Sasa ikawa kwamba kulikuwa na siku ambayo iliwekwa kando na wasioamini, kwamba wale wote ambao waliamini kwenye desturi hizo [a]wangeuawa isipokuwa ishara zipate kutimizwa, ambazo zilitolewa na nabii Samweli.

10 Sasa ikawa kwamba wakati Nefi, mwana wa Nefi, aliona huu uovu wa watu hawa, moyo wake ulikuwa na huzuni sana.

11 Na ikawa kwamba alienda nje na kujiinamisha ardhini, na kuomba kwa Mungu wake kwa niaba ya watu wake, ndiyo, wale ambao walikuwa karibu kuangamizwa kwa sababu ya imani yao kwenye desturi za babu zao.

12 Na ikawa kwamba aliomba kwa nguvu kwa Bwana ile siku [a]yote; na tazama, sauti ya Bwana ilikuja kwake, ikisema:

13 Inua kichwa chako na uchangamke; kwani tazama, wakati umefika, na kwa usiku wa leo ishara itatolewa, na [a]kesho

2*a* MWM Nefi, Mwana wa Nefi, Mwana wa Helamani.
b Alma 37:3–5.
3*a* 3 Ne. 2:9.
5*a* Hel. 14:2–4.
9*a* MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.
12*a* Eno. 1:4; Alma 5:46.
13*a* Lk. 2:10–11.

nitakuja ulimwenguni, kuonyesha dunia kwamba nitatimiza yote ambayo nimesababisha [b]kuzungumzwa kwa midomo ya manabii wangu watakatifu.

14 Tazama, [a]naja kwa watu wangu, [b]kutimiza vitu vyote ambavyo nimefanya kujulikana kwa watoto wa watu tangu [c]msingi wa dunia, na kufanya mapenzi, [d]yote ya Baba na Mwana—ya Baba kwa sababu yangu, na ya Mwana kwa sababu ya mwili wangu. Na tazama, wakati umefika, na usiku huu ishara itadhihirishwa.

15 Na ikawa kwamba maneno ambayo yalimjia Nefi yalivyotimizwa, kulingana na vile yalizungumzwa; kwani tazama, wakati jua lilipotua [a]hapakuwa na giza; na watu walianza kustaajabu kwa sababu hapakuwa na giza wakati usiku ulipofika.

16 Na kulikuwa na wengi, ambao hawakuwa wameamini maneno ya manabii, ambao [a]walijilaza kwenye ardhi na wakawa kama waliokufa, kwani walijua kwamba [b]mpango mkubwa wa uangamizo ambao walikuwa wamewawekea wale ambao waliamini maneno ya manabii umezuiliwa; kwani ishara ambayo ilitolewa ilikuwa ipo.

17 Na wakaanza kujua kwamba Mwana wa Mungu lazima aonekane karibuni; ndiyo, kwa kifupi, watu wote usoni mwa ulimwengu kutoka magharibi hadi mashariki, kote katika nchi ya kaskazini na katika nchi ya kusini, walistaajabu sana kwamba walianguka ardhini.

18 Kwani walijua kwamba manabii walikuwa wameshuhudia vitu hivi kwa miaka mingi, na kwamba ishara ambayo ilitolewa ilikuwa ipo kitambo; na walianza kuogopa kwa sababu ya uovu wao na kutoamini kwao.

19 Na ikawa kwamba hapakuweko na giza usiku ule wote, lakini kulikuwa na mwangaza kama kwamba ilikuwa adhuhuri. Na ikawa kwamba jua lilitokea asubuhi tena, kulingana na utaratibu wake; na walijua kwamba ilikuwa ni siku ambayo Bwana [a]angezaliwa, kwa sababu ya ishara ambayo ilitolewa.

20 Na ikawa imekuwa, ndiyo, vitu vyote, kila chembe, kulingana na maneno ya manabii.

21 Na ikawa pia kwamba [a]nyota mpya ilitokea, kulingana na neno.

22 Na ikawa kwamba kutoka wakati huu kuendelea kulianza kuwa na udanganyifu ulioletwa na Shetani, miongoni mwa watu, kushupaza mioyo yao, kwa kusudi kwamba wasiamini kwenye hizo ishara na miujiza ambayo walikuwa wameona; lakini ingawaje kulikuwa na huu udanganyifu na uwongo sehemu kubwa ya watu iliamini, na wakamgeukia Bwana.

23 Na ikawa kwamba Nefi

13 *b* MWM Yesu Kristo—Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo.
14 *a* Yn. 1:11.
b Mt. 5:17–18.
c Alma 42:26.
d M&M 93:3–4.
15 *a* Hel. 14:3.
16 *a* Hel. 14:7.
b 3 Ne. 1:9.
19 *a* Lk. 2:1–7.
21 *a* Mt. 2:1–2; Hel. 14:5.

alienda mbele miongoni mwa watu, na pia wengine wengi, akiwabatiza ubatizo wa toba, ambamo kwake kulikuwa na [a]kusamehewa kwingi kwa dhambi. Na hivyo watu wakaanza tena kuwa na amani nchini.

24 Na hapakuweko na mabishano, isipokuwa wachache ambao walianza kuhubiri, wakijaribu kuthibitisha kutumia maandiko kwamba haikuwa tena [a]muhimu kutii sheria ya Musa. Sasa kwa kitu hiki walikosa, wakiwa hawajaelewa maandiko.

25 Lakini ikawa kwamba mara moja waligeuka, na walisadikishwa kwa makosa ambayo walikuwa nayo, kwani walifahamishwa kwamba sheria [a]haijatimizwa, na kwamba lazima itimizwe kwa kila chembe; ndiyo, neno lilikuja kwao kwamba lazima itimizwe; ndiyo, kwamba nukta moja wala chembe moja haitapita mpaka yote yatimie; kwa hivyo kwenye huu mwaka walielemishwa kwa makosa yao na [b]wakaungama makosa yao.

26 Na hivyo mwaka wa tisini na mbili ulipita, ukileta habari njema kwa watu kwa sababu ya ishara ambazo zilitimizwa, kulingana na maneno ya uaguzi wa manabii wote watakatifu.

27 Na ikawa kwamba mwaka wa tisini na tatu pia ulipita katika amani, isipokuwa [a]wezi wa Gadiantoni, ambao waliishi juu ya milima, ambao waliingilia nchi; kwani ngome zao zilikuwa na nguvu sana na mahali pao pa siri kwamba watu hawangewashinda; kwa hivyo walitenda mauaji mengi sana, na kuua wengi miongoni mwa watu.

28 Na ikawa kwamba katika mwaka wa tisini na nne walianza kuongezeka kwa idadi kubwa, kwa sababu kulikuwa na wengi wasiokubaliana na Wanefi ambao walikimbilia kwao, ambao walisababisha huzuni nyingi kwa Wanefi ambao walibaki nchini.

29 Na pia kulikuwa na sababu ya huzuni nyingi miongoni mwa Walamani; kwani tazama, walikuwa na watoto wengi ambao walikuwa na kuanza kuwa wazee katika miaka, kwamba walijitegemea wenyewe, na waliongozwa vibaya na wengine ambao walikuwa [a]Wazoramu, kwa udanganyifu wao na maneno yao ya kusifu ya uongo, kujiunga na wale wezi wa Gadiantoni.

30 Na hivyo Walamani walihuzunishwa pia, na walianza kupungukiwa na imani na haki yao, kwa sababu ya uovu wa vijana wa kizazi hiki.

MLANGO WA 2

Uovu na machukizo yanaongezeka miongoni mwa watu—Wanefi na Walamani wanaungana kujilinda dhidi ya wezi wa Gadiantoni—Walamani waliogeuka wanakuwa

23 *a* MWM Ondoleo la Dhambi.
24 *a* Alma 34:13.
25 *a* Mt. 5:17–18.
b Mos. 26:29.
27 *a* MWM Wanyang'anyi wa Gadiantoni.
29 *a* Alma 30:59.

weupe na wanaitwa Wanefi. Karibia mwaka 5–16 B.K.

Na ikawa kwamba hivyo ulisha mwaka wa tisini na tano pia, na watu wakaanza kusahau hizo ishara na maajabu ambayo walikuwa wamesikia, na wakaanza kuendelea kupungukiwa zaidi kwa mshangao katika ishara au maajabu kutoka mbinguni, mpaka kwamba walianza kushupaza mioyo yao, na kuwa vipofu ndani ya akili zao, na walianza kutoamini yote ambayo walisikia na kuona—

2 Wakikisia juu ya kitu cha bure ndani ya mioyo yao, kwamba ililetwa na watu na nguvu za ibilisi, kupoteza na [a]kudanganya mioyo ya watu; na hivyo Shetani alishawishi mioyo ya watu tena, mpaka kwamba akafunika macho yao na kuwaongoza mbali kuamini kwamba mafundisho ya Kristo yalikuwa ni upumbavu na kitu cha bure.

3 Na ikawa kwamba watu walianza kukua ndani ya uovu na machukizo; na hawakuamini kwamba kutakuwa na ishara zingine au maajabu ambayo yangetolewa; na Shetani alikuwa [a]akizunguka, akipotosha mbali mioyo ya watu, akiwajaribu na kuwasababisha kufanya uovu mkuu ndani ya nchi.

4 Na hivyo ukaisha mwaka wa tisini na sita; na pia mwaka wa tisini na saba; na pia mwaka wa tisini na nane; na pia mwaka wa tisini na tisa;

5 Na pia miaka mia moja ilikuwa imepita tangu siku za [a]Mosia, ambaye alikuwa mfalme juu ya watu wa Wanefi.

6 Na miaka mia sita na tisa ilikuwa imepita tangu Lehi aondoke Yerusalemu.

7 Na miaka tisa ilikuwa imepita kutoka wakati ambao ishara ilitolewa, ambayo ilizungumziwa na manabii, kwamba Kristo atakuja katika ulimwengu.

8 Sasa Wanefi walianza kupima wakati wao kutoka muda huu wakati ishara ilitolewa, au kutoka kwa kuja kwa Kristo; kwa hivyo, miaka tisa ilikuwa imepita.

9 Na Nefi, ambaye alikuwa baba ya Nefi, ambaye alikuwa ameaminiwa maandiko, [a]hakurudi katika nchi ya Zarahemla, na hakuonekana katika nchi yote.

10 Na ikawa kwamba watu bado walibaki kwenye uovu, ingawaje kulikuwa na kuhubiri kwingi na uaguzi ambao ulipelekwa miongoni mwao; na hivyo mwaka wa kumi ulipita pia; na mwaka wa kumi na moja pia ulipita katika uovu.

11 Na ikawa katika mwaka wa kumi na tatu kukaanza kuwa na vita na mabishano kote nchini; kwani wezi wa Gadiantoni walikuwa wengi sana, na waliwaua watu wengi, na kuharibu miji mingi, na walisambaza vifo vingi na uchinjaji kote nchini, kwamba ilikuwa muhimu kwamba watu wote, Wanefi

2 2*a* MWM Danganya, Kudanganya, Udanganyifu.
3*a* M&M 10:27.
5*a* Mos. 29:46–47.
9*a* 3 Ne. 1:2–3.

na Walamani, wachukue silaha dhidi yao.

12 Kwa hivyo, Walamani wote ambao walikuwa wamemgeukia Bwana waliungana na ndugu zao, Wanefi, na walilazimishwa, kwa usalama wa maisha yao na wanawake wao na watoto wao, kuchukua silaha dhidi ya wezi wa Gadiantoni, ndiyo, na pia kulinda haki zao, na faida ya kanisa lao na kuabudu kwao, na kwa [a]uhuru wao na [b]uungwana wao.

13 Na ikawa kwamba kabla ya mwaka wa kumi na tatu kupita Wanefi walitishwa na maangamizo makubwa kwa sababu ya vita hivi, ambavyo vilikuwa vikali sana.

14 Na ikawa kwamba wale Walamani ambao walijiunga na Wanefi walihesabiwa miongoni mwa Wanefi;

15 Na [a]laana yao ilitolewa kwao, na ngozi yao ikawa [b]nyeupe kama ya Wanefi;

16 Na vijana wao na mabinti zao wakawa warembo sana; na wakahesabiwa miongoni mwa Wanefi, na kuitwa Wanefi. Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na tatu.

17 Na ikawa katika mwaka wa kumi na nne, vita miongoni mwa wezi na watu wa Nefi viliendelea na vikawa vikali sana; walakini, watu wa Nefi walipata faida juu ya wezi, mpaka kwamba wakawarudisha nyuma kutoka nchi yao hadi kwenye milima na kwenye mahali pao pa siri.

18 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na nne. Na katika mwaka wa kumi na tano wezi walikuja dhidi ya watu wa Nefi; na kwa sababu ya uovu wa watu wa Nefi, na mabishano yao mengi na mafarakano yao, wezi wa Gadiantoni walipata faida nyingi juu yao.

19 Na hivyo ukaisha mwaka wa kumi na tano, na hivyo ndivyo watu walivyokuwa kwenye hali ya mateso mengi; na [a]upanga wa maangamizo ulining'inia juu yao, mpaka kwamba walikuwa karibu kupigwa chini nao, na hii ni kwa sababu ya uovu wao.

MLANGO WA 3

Gidianhi, kiongozi wa Gadiantoni, anataka kwa nguvu kwamba Lakoneyo na Wanefi wajisalimishe na nchi yao—Lakoneyo anamteua Gidgidoni kama kapteni mkuu wa majeshi—Wanefi wanajikusanya katika Zarahemla na Neema kujikinga. Karibia mwaka 16–18 B.K.

Na sasa ikawa kwamba katika mwaka wa kumi na sita tangu kuja kwa Kristo, Lakoneyo, msimamizi wa nchi, alipokea barua kutoka kwa kiongozi na msimamizi wa hili kundi la wezi; na haya ndiyo yalikuwa maneno ambayo yaliandikwa, yakisema:

2 Lakoneyo, mkuu sana na msimamizi mkuu wa nchi, tazama, ninakuandikia hii barua, na ninakupatia sifa nyingi sana kwa sababu ya uthabiti wako,

12*a* MWM Huru, Uhuru.
b MWM Huru, Uhuru.
15*a* Alma 17:15; 23:18.
b 2 Ne. 5:21; 30:6; Yak. (KM) 3:8.
19*a* Alma 60:29.

na pia uthabiti wa watu wako, katika kulinda kile ambacho mnadhani kuwa ni haki yenu na uhuru wenu; ndiyo, mnasimama vizuri, kama mnaosaidiwa na mungu, kwenye kulinda uhuru wenu, na mali yenu, na nchi yenu, au kile mnachoita chenu.

3 Na inaonekana kama jambo la huruma kwangu, Lakoneyo mwenye cheo kikubwa, kwamba ungekuwa mpumbavu na bure kudhani kwamba unaweza kusimama dhidi ya watu walio shujaa ambao wako chini ya amri yangu, ambao wakati huu wako tayari na silaha zao, na wanangojea kwa hamu kuu wasikie neno—Nenda chini kwa Wanefi na muwaangamize.

4 Na mimi, nikijua roho yao ya kutoshindwa, nimewajaribu kwenye uwanja wa vita, na nikijua chuki yao isiyo na mwisho dhidi yenu kwa sababu ya vitu vingi vibaya ambavyo mmewafanyia, kwa hivyo ikiwa watashuka dhidi yenu watawaangamiza kabisa.

5 Kwa hivyo nimeandika hii barua, nikiweka muhuri kwa mkono wangu, nikifikiria ustawi wenu, kwa sababu ya uthabiti wenu kwenye kile ambacho mnaamini ni haki, na kwa sababu ya roho yenu kuu katika uwanja wa vita.

6 Kwa hivyo ninakuandikia, nikitaka kwamba usalimishe kwa hawa watu wangu, miji yenu, nchi zenu, na mali yenu, kuliko kwamba wawashambulie kwa upanga na kuwaangamiza.

7 Au kwa maneno mengine, mjitolee wenyewe kwetu, na mjiunge nasi na mzoeane na kazi zetu za [a]siri, na muwe ndugu zetu kwamba muwe kama sisi—sio watumwa wetu, lakini ndugu zetu na washiriki wa mali yetu yote.

8 Na tazama, [a]naapa kwako, ikiwa mtafanya hivi, kwa kiapo, hamtaangamizwa; lakini kama hamtafanya hivi, ninaapa na kiapo, kwamba mwezi ujao nitaamuru kwamba majeshi yangu yatashuka dhidi yenu, na hawatajizuia na hawatawahurumia, lakini watawachinja, na kuachilia upanga uwaangukie hata mpaka mwangamie.

9 Na tazama, mimi ni Gidianhi; na mimi ni mtawala wa hili [a]shirika la siri la Gadiantoni; shirika ambalo na kazi ambazo najua ni [b]nzuri; na ni za [c]zamani na zimepitishwa kwetu.

10 Na ninaandika hii barua kwako wewe, Lakoneyo, na ninatumaini kwamba mtasalimisha mashamba yenu na mali yenu, bila kumwaga damu, kwamba watu wangu hawa wangepata tena haki zao na serikali yao, ambao wamewaasi kwa sababu ya uovu wenu wa kuwakataza wapokee haki za serikali, na msipofanya hivi, nitalipiza mateso yao. Ni mimi Gidianhi.

3 7*a* Hel. 6:22–26.
8*a* Eth. 8:13–14.
9*a* MWM Makundi maovu ya siri.
b Alma 30:53.
c Hel. 6:26–30; Musa 5:29, 49–52.

11 Na sasa ikawa Lakoneyo alipopata hii barua alistaajabu sana, kwa sababu ya ujasiri wa Gidianhi kudai umiliki wa nchi ya Wanefi, na pia kwa sababu ya kutisha watu na kulipiza mabaya ya wale ambao hawakuwa wamefanyiwa makosa, isipokuwa [a]walijikosea wenyewe kwa kuasi hadi kwenye hawa wezi waovu na wa kuchukiza.

12 Sasa tazama, huyu Lakoneyo, msimamizi, alikuwa mtu wenye haki, na hangeweza kutishwa na [a]mwizi; kwa hivyo hakutii barua ya Gidianhi, msimamizi wa wezi, lakini alisababisha kwamba watu wake wamwombe Bwana awapatie nguvu dhidi ya wezi wakati wangekuja chini dhidi yao.

13 Ndiyo, alipeleka tangazo miongoni mwa watu wote, kwamba wakusanye pamoja wanawake wao, na watoto wao, wanyama wao, na mifugo yao, na mali yao yote, isipokuwa nchi yao, mahali pamoja.

14 Na akasababisha kwamba ngome zijengwe kuwazunguka, na ziimarishwe ndani sana. Na akasababisha kwamba majeshi, yote ya Wanefi na ya Walamani, au ya hao wote waliohesabiwa miongoni mwa Wanefi, yawekwe kama walinzi hapo karibu kuwalinda, na kuwalinda kutokana na waporaji usiku na mchana.

15 Ndiyo, aliwaambia: Kadiri Bwana anavyoishi, isipokuwa mmetubu maovu yenu yote, na kumlilia Bwana, kwa namna yoyote ile, hamtakombolewa kwa namna yeyote ile kutoka mikononi mwa wale wanyang'anyi wa Gadiantoni.

16 Na maneno na unabii wa Lakoneyo ulikuwa mkubwa na wa ajabu kwamba yalisababisha woga kuwajia watu wote; na walijaribu kwa uwezo wao wote kufanya kulingana na maneno ya Lakoneyo.

17 Na ikawa kwamba Lakoneyo aliwateua makaptani wakuu wa majeshi yote ya Wanefi, kuwaamuru wakati wanyang'anyi watakapokuja chini kutoka nyikani dhidi yao.

18 Sasa aliyekuwa mkuu wa wote miongoni mwa makapteni wote na amri jeshi mkuu wa majeshi yote ya Wanefi aliteuliwa, na jina lake lilikuwa [a]Gidgidoni.

19 Sasa ilikuwa ni desturi miongoni mwa Wanefi wote kuwateua kama makapteni wakuu, (isipokuwa wakati ambao wao walikuwa na uovu mwingi), mtu ambaye alikuwa na roho ya ufunuo na pia ya [a]unabii; kwa hivyo, huyu Gidgidoni alikuwa nabii mkuu miongoni mwao, kama vile pia alivyokuwa mwamuzi mkuu.

20 Sasa watu walimwambia Gidgidoni: Omba kwa Bwana, na acha twende juu ya milima na kwenye nyika, ili tuwashambulie wanyang'anyi na tuwaangamize kwenye nchi zao.

21 Lakini Gidgidoni aliwaambia: Bwana [a]anakataza; kwani

11 *a* Hel. 14:30.
12 *a* Alma 54:5–11; 3 Ne. 4:7–10.
18 *a* 3 Ne. 6:6.
19 *a* MWM Toa unabii, Unabii.
21 *a* Alma 48:14.

ikiwa tutaenda juu dhidi yao Bwana [b]atatukabidhi mikononi mwao; kwa hivyo tutajitayarisha katikati ya nchi zetu, na tutakusanya majeshi yetu yote pamoja, na hatutaenda dhidi yao, lakini tutangoja mpaka watakapokuja dhidi yetu; kwa hivyo kadiri vile Bwana anavyoishi, ikiwa tutafanya hivi atawaweka mikononi mwetu.

22 Na ikawa katika mwaka wa kumi na saba, kuelekea mwisho wa mwaka, tangazo la Lakoneyo lilikuwa limeenezwa kote nchini, na walikuwa wamechukua farasi wao, na magari yao, na ng'ombe wao, na wanyama wao wote, na mifugo yao, na nafaka yao, na mali yao yote, na walisonga mbele wakiwa maelfu na maelfu, mpaka walipokuwa wameenda katika mahali ambapo palikuwa pamechaguliwa kwamba wajikusanye pamoja, kujilinda dhidi ya maadui zao.

23 Na nchi ambayo ilichaguliwa ilikuwa nchi ya Zarahemla, na nchi ambayo ilikuwa kati ya nchi ya Zarahemla na nchi ya Neema, ndiyo, kwenye mpaka ambao ulikuwa miongoni mwa nchi ya Neema na nchi ya Ukiwa.

24 Na kulikuwa na maelfu ya watu ambao waliitwa Wanefi, ambao walijikusanya pamoja katika nchi hii. Sasa Lakoneyo alisababisha kwamba wajikusanye pamoja katika nchi iliyo upande wa kusini, kwa sababu ya laana kubwa ambayo ilikuwa katika [a]nchi ya upande wa kaskazini.

25 Na walijiimarisha dhidi ya maadui zao; na wakaishi katika nchi moja, na kwenye kundi moja, na waliogopa maneno ambayo yalizungumzwa na Lakoneyo, mpaka kwamba wakatubu dhambi zao zote; na wakatoa sala zao kwa Bwana Mungu wao, kwamba [a]angewakomboa wakati ambao maadui wao watakuja chini dhidi yao kupigana.

26 Na walikuwa na huzuni sana kwa sababu ya maadui wao. Na Gidgidoni alisababisha kwamba watengeneze [a]silaha za vita za kila aina, na waimarishwe na silaha, na ngao, na vigao, kufuata maelezo ya namna yake.

MLANGO WA 4

Majeshi ya Wanefi yanawashinda wanyang'anyi wa Gadiantoni—Gidianhi anauawa, na mrithi wake, Zemnariha, ananyongwa—Wanefi wanamsifu Bwana kwa ushindi wao. Karibia mwaka 19–22 B.K.

Na ikawa kwamba mwishoni mwa mwaka wa kumi na nane yale majeshi ya wanyang'anyi yalikuwa yamejiandaa kwa vita, na walianza kuja chini na kushambulia kutokea kwenye vilima, na nje ya milima, na nyikani, na ngome zao, na pahali pao pa siri, na wakaanza kumiliki nchi, zote ambazo zilikuwa katika nchi, iliyokuwa kusini

21 *b* 1 Sam. 14:12.
24 *a* Alma 22:31.
25 *a* MWM Tegemea.
26 *a* 2 Ne. 5:14.

na ambazo zilikuwa katika nchi iliyokuwa kaskazini, na wakaanza kumiliki nchi zote zilizokuwa [a]zimeachwa na Wanefi, na miji ambayo ilikuwa imeachwa kwa hali ya ukiwa.

2 Lakini tazama, hapakuweko na wanyama wa mwitu wala mawindo katika nchi hizo ambazo ziliachwa na Wanefi, na hakukuwa na mawindo kwa wanyang'anyi isipokuwa kwenye nyika.

3 Na wanyang'anyi waliweza tu kuishi kwenye nyika, kwa uhitaji wa chakula; kwani Wanefi waliacha nchi zao zikiwa hazina kitu, na walikusanya wanyama wao na mifugo yao na mali yao yote, na walikuwa kwenye kikundi kimoja.

4 Kwa hivyo, hakukuwa na nafasi ya wanyang'anyi kupora na kupata chakula, isipokuwa wangekuja kwa vita vya wazi kupigana dhidi ya Wanefi; na Wanefi wakiwa katika kikundi kimoja, na wakiwa na idadi kubwa, na wakiwa wamejiwekea akiba ya vyakula, na farasi na ng'ombe, na wanyama wa kila aina, kwamba wangejilisha kwa muda wa miaka saba, wakati ambao walitumainia kuangamiza wanyang'anyi kutoka nchini; na hivyo mwaka wa kumi na nane ulipita.

5 Na ikawa kwamba katika mwaka wa kumi na tisa Gidianhi alipata kwamba ilikuwa muhimu kwake kwamba afanye vita dhidi ya Wanefi, kwani hakukuwa na njia ambayo wangeishi isipokuwa kupora, kuiba, na kuua.

6 Na hawangethubutu kujitapanya usoni mwa nchi ili wakuze nafaka, wasije Wanefi wakawaua; kwa hivyo Gidianhi alitoa amri kwa majeshi yake kwamba, mwaka huu waende kupigana dhidi ya Wanefi.

7 Na ikawa kwamba walikuja kupigana; na ilikuwa katika mwezi wa sita; na tazama, ile siku ambayo walikuja kupigana ilikuwa kubwa na ya kutisha; na walikuwa wamevaa kwa njia ya wanyang'anyi; na walikuwa na ngozi ya mwanakondoo viunoni mwao, na walijipaka rangi ya damu, na vichwa vyao vilinyolewa, na walikuwa na vyapeo juu yao; na majeshi ya Gidianhi yalionekana mengi na ya kuogofya, kwa sababu ya silaha zao, na kwa sababu ya kujipaka damu.

8 Na ikawa kwamba majeshi ya Wanefi, walipoona majeshi ya Gidianhi yalivyoonekana, wote walijilaza kwenye ardhi, na kumwomba Bwana Mungu wao, kwamba awahurumie na kuwakomboa kutoka mikono ya maadui wao.

9 Na ikawa kwamba majeshi ya Gidianhi yalipoona hivi walianza kupaza sauti, kwa sababu ya shangwe yao, kwani walidhani kwamba Wanefi walianguka kwa woga kwa sababu ya kuonekana kwa vitisho vya majeshi yao.

10 Lakini kwa hiki kitu walisikitika, kwani Wanefi hawaku-

4 1*a* 3 Ne. 3:13–14, 22.

waogopa; lakini [a]walimwogopa Mungu wao na walimwomba awalinde; kwa hivyo, wakati majeshi ya Gidianhi yalipowavamia walikuwa tayari kukabiliana nao; ndiyo, kwa nguvu za Bwana walikabiliana nao.

11 Na vita vilianza kwenye huu mwezi wa sita; na vilikuwa vikubwa na vya kutisha, ndiyo, uchinjaji ulikuwa mwingi na wa kutisha, mpaka kwamba hakujakuweko uchinjaji mkuu kama huo unaojulikana miongoni mwa watu wa Lehi tangu aondoke Yerusalemu.

12 Na ingawa kulikuwa na [a]vitisho na viapo ambavyo Gidianhi alikuwa amefanya, tazama, Wanefi waliwashinda mpaka kwamba wakarudi nyuma kutoka kwao.

13 Na ikawa kwamba [a]Gidgidoni aliamuru kwamba majeshi yake yawafukuze hadi kwenye mipaka ya nyika, na kwamba wasimhurumie yeyote ambaye ataanguka mikononi mwao njiani; na hivyo waliwafukuza na kuwaua, kwenye mipaka ya nyika, hata mpaka walipotimiza amri ya Gidgidoni.

14 Na ikawa kwamba Gidianhi, ambaye alisimama na kupigana kwa ujasiri, alifukuzwa wakati alipokuwa anakimbia; na akiwa amechoka kwa sababu ya kupigana kwingi alipitwa na kuuawa. Na hivyo maisha ya Gidianhi mwizi yaliisha.

15 Na ikawa kwamba majeshi ya Wanefi yalirejea tena mahali pao pa usalama. Na ikawa kwamba mwaka wa kumi na tisa ulipita, na wanyang'anyi hawakuja tena kupigana; wala hawakuja tena katika mwaka wa ishirini.

16 Na katika mwaka wa ishirini na moja hawakuja kupigana, lakini walikuja kutoka pande zote na kuwazunguka watu wa Nefi; kwani walidhani kwamba wangewazuilia mbali watu wa Nefi kutoka katika nchi zao, na kuwafungia ndani kila upande, na ikiwa wangewazuilia kutoingia kwa haki zao zote za nje, kwamba wangewasababisha wajitolee wenyewe kulingana na matakwa yao.

17 Sasa walikuwa wamejiteulia kiongozi mwingine, ambaye jina lake lilikuwa Zemnariha; kwa hivyo alikuwa Zemnariha ndiye aliyeamuru kwamba kuzingirwa kufanyike.

18 Lakini tazama, hii ilikuwa faida kwa Wanefi; kwani haingewezekana kwa wanyang'anyi kuwazingira kwa muda wa kutosha ili kuwe na matokeo kwa Wanefi, kwa sababu ya vyakula vyao vingi, ambavyo walikuwa wameweka kwenye ghala.

19 Na kwa sababu ya ukosefu wa vyakula miongoni mwa wanyang'anyi; kwani tazama, hawakuwa na chochote isipokuwa nyama kwa chakula chao, nyama ambayo walipata nyikani;

20 Na ikawa kwamba wanyama wa [a]mwitu walikuwa wachache kwenye nyika mpaka

10*a* MWM Hofu.
12*a* 3 Ne. 3:1–10.
13*a* 3 Ne. 3:18.
20*a* 1 Ne. 18:25.

kwamba wanyang'anyi walikuwa karibu kuangamia kwa njaa.

21 Na Wanefi siku zote walikuwa wakitoka nje mchana na usiku, na kuwashambulia maadui wao, na kuwaangamiza kwa maelfu na maelfu.

22 Na hivyo ikawa kupenda kwa watu wa Zemnariha kuachilia kusudi lao, kwa sababu ya uharibifu mkuu ambao uliwajia usiku na mchana.

23 Na ikawa kwamba Zemnariha aliwaamuru watu wake kwamba warudi nyuma wenyewe kutoka kwa mazingira, na waende kwenye sehemu ya mbali nchi ya upande wa kaskazini.

24 Na sasa, Gidgidoni akijua kusudi lao, na akijua udhaifu wao kwa sababu ya ukosefu wa chakula, na mauaji mengi ambayo yalifanywa miongoni mwao, kwa hivyo alituma nje majeshi yake wakati wa usiku, na akazuia njia yao ya kurudi nyuma, na akaweka majeshi yake kwenye njia yao ya kurudi nyuma.

25 Na hii ilifanywa wakati wa usiku, na walisonga na kupita mbele ya wanyang'anyi, kwamba kesho yake, wakati wanyang'anyi walipoanza kusonga, walisimamishwa na majeshi ya Wanefi kote mbele yao na nyuma yao.

26 Na wanyang'anyi ambao walikuwa kusini walizuiliwa pia kwenye sehemu zao ambazo wangefuata kwa kurudi nyuma. Na hivi vitu vyote vilifanywa kwa amri ya Gidgidoni.

27 Na kulikuwa na maelfu wengi ambao walijitoa kama wafungwa kwa Wanefi, na waliosalia waliuawa.

28 Na kiongozi wao, Zemnariha, alichukuliwa na kunyongwa kwenye mti, ndiyo, hata juu ya mti mpaka akafa. Na wakati walipomnyonga mpaka kufa, waliangusha mti ardhini, na wakapaza sauti, wakisema:

29 Bwana awahifadhi watu wake katika haki na utakatifu wa moyo, ili wasababishe kuangushwa chini wale wote ambao watataka kuwaua kwa kutumia nguvu na mashirika ya siri, kwa njia sawa kama vile huyu mtu alivyoangushwa ardhini.

30 Na walifurahi na kupiga makelele tena kwa sauti moja, wakisema: [a]Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo, awalinde hawa watu kwa haki, kadiri vile [b]watakavyo lilingana jina la Mungu wao kwa kinga.

31 Na ikawa kwamba kwa ghafla, wote pamoja waliimba, na [a]kumsifu Mungu wao kwa kitu kikubwa ambacho aliwafanyia, kwa kuwahifadhi kutoka kwa mikono ya maadui wao.

32 Ndiyo, walipiga kelele: [a]Hosana kwa Mungu Aliye Juu Sana. Na wakapiga kilele: Heri liwe jina la Bwana Mungu [b]Mwenyezi, Mungu Aliye Juu Sana.

33 Na mioyo yao ilifura kwa

30 *a* Alma 29:11.
b Eth. 4:15.
31 *a* Alma 26:8.
MWM Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani.
32 *a* MWM Hosana.
b 1 Ne. 1:14.
MWM Mungu, Uungu.

shangwe, mpaka kwenye kutoa machozi mengi, kwa sababu ya uzuri mwingi wa Mungu kuwakomboa kutoka mikono ya maadui wao; na walijua ni kwa sababu ya kutubu kwao na unyenyekevu wao kwamba walikuwa wamekombolewa kutoka kwa maangamizo yasiyo na mwisho.

MLANGO WA 5

Wanefi wanatubu na kuacha dhambi zao—Mormoni anaandika historia ya watu wake na kutangaza neno lisilo na mwisho kwao—Israeli itakusanywa kutoka kwenye tawanyiko lake. Karibia mwaka 22–26 B.K.

Na sasa tazama, hakukuwa hata nafsi moja miongoni mwa watu wote wa Wanefi ambayo ilikuwa na shaka hata kidogo katika maneno ya manabii watakatifu ambao walizungumza; kwani walijua kwamba ilikuwa muhimu kwamba yatimizwe.

2 Na walijua kwamba ni muhimu kwamba Kristo alikuwa amekuja, kwa sababu ya ishara nyingi ambazo zilikuwa zimetolewa kulingana na maneno ya manabii; na kwa sababu ya vitu ambavyo vilikuwa vimetimizwa kitambo walijua kwamba ilikuwa muhimu kwamba vitu vyote vitimizwe kulingana na yale ambayo yalikuwa yamezungumzwa.

3 Kwa hivyo waliacha dhambi zao zote, na machukizo yao, na ukahaba wao, na walimtumikia Mungu kwa bidii yote mchana na usiku.

4 Na sasa ikawa kwamba wakati walikuwa wamechukua wanyang'anyi wote kama wafungwa, mpaka kwamba hakuna aliyetoroka ambaye hakuuawa, waliwatupa wafungwa wao gerezani, na wakasababisha neno la Mungu kuhubiriwa kwao; na kadiri wengi walipotubu dhambi zao na kufanya agano kwamba hawataua tena waliachiliwa [a]huru.

5 Lakini kadiri kulipokuwa na wengi ambao hawakufanya agano, na ambao waliendelea na mauaji ya siri mioyoni mwao, ndiyo, vile wengi walipatikana wakitoa vitisho kwa ndugu zao walihukumiwa na kuadhibiwa kulingana na sheria.

6 Na hivyo walimaliza yale maovu yote, na siri, na mashirika ya machukizo, ambamo kwake kulikuwa na maovu mengi sana, na kutendeka kwa mauaji mengi.

7 Na hivyo mwaka wa [a]ishirini na mbili ulikuwa umepita, na mwaka wa ishirini na tatu pia, na wa ishirini na nne, na wa ishirini na tano; na hivyo miaka ishirini na tano ilipita.

8 Na vitu vingi vilikuwa vimetendeka ambavyo, kwa maoni ya watu kadhaa, vilikuwa vikubwa na vya kushangaza; walakini, vyote haviwezi kuandikwa kwenye kitabu hiki; ndiyo, kitabu hiki hakiwezi kutosha hata sehemu moja ya [a]mia ya yale yaliyofanyika miongoni

5 4*a* MWM Huru, Uhuru. | 7*a* 3 Ne. 2:8. | 8*a* 3 Ne. 26:6–12.

mwa watu wengi hivyo kwa muda wa miaka ishirini na tano.

9 Lakini tazama kuna [a]maandishi ambayo yana mambo yote ya hawa watu; na taarifa fupi zaidi na ya kweli ilitolewa na Nefi.

10 Kwa hivyo nimetengeneza maandishi yangu ya vitu hivi kulingana na kumbukumbu ya Nefi, ambayo ilichorwa kwenye mabamba ambayo yaliitwa mabamba ya Nefi.

11 Na tazama, ninatengeneza maandishi kwenye mabamba ambayo nimeunda kwa mikono yangu mwenyewe.

12 Na tazama, ninaitwa [a]Mormoni, nikiitwa kufuatana na [b]nchi ya Mormoni, nchi ambamo Alma alianzisha kanisa miongoni mwa watu, ndiyo, kanisa la kwanza ambalo lilianzishwa miongoni mwao baada ya uhalifu wao.

13 Tazama, mimi ni mwanafunzi wa Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Nimeitwa na yeye kutangaza neno lake miongoni mwa watu wake, ili wawe na maisha yasiyo na mwisho.

14 Na imekuwa muhimu kwamba mimi, kwa kutii mapenzi ya Mungu, kwamba sala za wale ambao wameenda mbele, ambao walikuwa watakatifu, sharti itatimizwa kulingana na imani yao, niandike [a]maandishi ya vitu hivi ambavyo vimefanywa—

15 Ndiyo, maandishi madogo ya yale mambo ambayo yamefanyika kutoka wakati ambao Lehi aliondoka Yerusalemu, hata chini mpaka wakati huu.

16 Kwa hivyo nitatengeneza maandishi yangu kutoka kwa kumbukumbu ambazo zilitolewa na wale ambao walikuwa mbele yangu, hadi mwanzo wa maisha yangu;

17 Na ndipo nafanya [a]maandishi haya ya vitu ambavyo nimeona kwa macho yangu.

18 Na ninajua maandishi ninayoandika kuwa ya haki na ya kweli; walakini kuna vitu vingi ambavyo, kwa sababu ya lugha yetu, hatuwezi [a]kuviandika.

19 Na sasa ninamaliza kuzungumza, juu yangu mwenyewe, na nitaendelea kutoa historia yangu ya vitu ambavyo vimefanyika mbele yangu.

20 Mimi ni Mormoni, na ni wa kizazi cha Lehi kamili. Ninayo sababu ya kumsifu Mungu wangu na Mwokozi wangu Yesu Kristo, kwamba aliwaleta babu zetu kutoka nchi ya Yerusalemu, (na [a]hakuna yeyote aliyeijua isipokuwa yeye tu na wale ambao aliwaleta kutoka nchi hiyo) na kwamba amenipatia mimi na watu wangu elimu nyingi katika wokovu wa nafsi zetu.

21 Kwa kweli ameibariki [a]nyumba ya [b]Yakobo, na amekuwa na [c]huruma kwa uzao wa Yusufu.

22 Na [a]ikiwa vile uzao wa Lehi

9 *a* Hel. 3:13–15.
12 *a* Morm. 1:1–5.
b Mos. 18:4; Alma 5:3.
14 *a* Eno. 1:13–18; M&M 3:19–20.
17 *a* Morm. 1:1.
18 *a* Eth. 12:25.
20 *a* 1 Ne. 4:36.
21 *a* MWM Israeli.
b Mwa. 32:28.
c Kum. 33:13–17.
22 *a* 2 Ne. 1:20.

umetii amri zake amewabariki na kuwasaidia kufanikiwa kulingana na neno lake.

23 Ndiyo, na kwa kweli ataleta [a]baki la uzao wa Yusufu [b]kuwaelemisha kuhusu Bwana Mungu wao.

24 Na kwa kweli kadiri Bwana anavyoishi, [a]atakusanya ndani kutoka katika pembe nne za dunia baki lote la uzao wa Yakobo, ambao wametawanyika ugenini kote usoni mwa nchi.

25 Na vile amefanya agano na nyumba yote ya Yakobo, hivyo hivyo agano ambalo amefanya na nyumba ya Yakobo litatimizwa kwa wakati wake mwenyewe, kwa [a]kurudisha nyumba yote ya Yakobo kwenye ujuzi wa agano ambalo amefanya nao.

26 Na hapo ndipo [a]watajua Mkombozi wao, ambaye ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu; na ndipo watakusanywa kutoka pembe nne za dunia hadi kwenye nchi zao, kutoka ambapo walitawanywa; ndiyo, kadiri Bwana aishivyo ndivyo itakavyokuwa. Amina.

MLANGO WA 6

Wanefi wanafanikiwa—Kiburi, utajiri, na tofauti ya vyeo inatokea—Kanisa linavunjwa kwa mifarakano—Shetani anaongoza watu kwenye maasi yaliyo wazi—Manabii wengi wanawaambia watu watubu na wanauawa—Wauaji wao wanafanya hila kuchukua serikali. Karibia mwaka 26–30 B.K.

Na sasa ikawa kwamba watu wa Wanefi wote walirudi kwenye nchi zao katika mwaka wa ishirini na sita, kila mtu na jamaa yake, wanyama wake, na mifugo yake, farasi wake na ngombe wake, na vitu vyote vilivyokuwa vyao.

2 Na ikawa kwamba walikuwa hawajamaliza vyakula vyao vyote; kwa hivyo walichukua hivyo vyote ambavyo walikuwa hawajala, nafaka yao yote ya kila aina, na dhahabu yao, na fedha yao, na vitu vyao vyote vya thamani, na wakarudi kwenye nchi zao na umiliki wao, kote kaskazini na kusini, kote katika nchi upande wa kaskazini na nchi ya upande wa kusini.

3 Na waliwapatia ardhi wale wanyang'anyi ambao walishiriki ndani ya agano la kuweka amani ya nchi, ambao walikuwa wamependelea kubaki Walamani, kulingana na wingi wao ili kwa bidii yao wangeweza kujilisha; na hivyo wakaimarisha amani kote nchini.

4 Na walianza tena kufanikiwa na kuwa wakubwa; na miaka ya ishirini na sita na ya saba ilipita, na kukawa na amri nchini; na wakawa wametengeneza sheria zao kulingana na usawa na haki.

5 Na sasa hakukuwa na kitu

23 *a* Alma 46:24.
b 2 Ne. 3:12.
24 *a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
25 *a* 3 Ne. 16:5.
26 *a* 2 Ne. 30:5–8; 3 Ne. 20:29–34.

chochote kote nchini cha kuwazui watu kufanikiwa siku zote, isipokuwa kama wangefanya kosa.

6 Na sasa ikawa ni Gidgidoni, na yule mwamuzi, Lakoneyo, na wale ambao walikuwa wameanzisha hii imani kuu katika nchi.

7 Na ikawa kwamba kulikuwa na miji mingi iliyojengwa upya, na kulikuwa na miji mingi ya kale iliyorekebishwa.

8 Na kulikuwa njia kuu nyingi zilizojengwa, na barabara nyingi zilizotengenezwa, ambazo zilielekea kutoka mji hadi mwingine, na kutoka nchi hadi nyingine, na kutoka mahali hadi pengine.

9 Na hivyo mwaka wa ishirini na nane ulipita, na watu walikuwa na amani siku zote.

10 Lakini ikawa katika mwaka wa ishirini na tisa, kukaanza kuwa na mabishano miongoni mwa watu; na wengine walijiinua kwa [a]kiburi na majivuno kwa sababu ya utajiri wao mkuu, ndiyo, hata kwenye kutesa wale ambao walikuwa masikini na wanyenyekevu.

11 Kwani kulikuwa na wafanyibiashara wengi katika nchi, na pia mawakili wengi, na wakuu wengi.

12 Na watu walianza kutambuliwa kwa vyeo, kulingana na [a]utajiri wao, na nafasi za kusoma; ndiyo, wengine walikuwa hawajui kwa sababu ya umasikini wao, na wengine walipata elimu nyingi kwa sababu ya utajiri wao.

13 Wengine walijiinua kwa kiburi na wengine walikuwa wanyenyekevu sana; na wengine walimtukana yeyote aliyewatusi, wakati wengine wangepata matusi na udhalimu na kila aina ya [a]mateso, na [b]hawangegeuka na kutoa matusi, lakini walikuwa wanyenyekevu na wenye kutubu mbele ya Mungu.

14 Na hivyo kulikuwa na kutokuwa na usawa ndani ya nchi yote, mpaka kwamba kanisa lilianza kugawanywa kwenye vikundi; ndiyo, mpaka kwamba katika mwaka wa thelathini, kanisa liligawanyika ndani ya nchi yote isipokuwa miongoni mwa Walamani wachache ambao waliogeukia imani ya kweli; na hawangeiacha, kwani walikuwa imara, na thabiti na wasiotingishika, na wanaotamani kwa [a]bidii yote kutii amri za Bwana.

15 Sasa kiini cha huu uovu wa watu kilikuwa hiki—Shetani alikuwa na nguvu nyingi kwa kuchochea watu kufanya aina yote ya uovu, na kujaza watu na kiburi, akiwashawishi kutafuta uwezo na mamlaka, na utajiri, na vitu vilivyo bure vya ulimwengu.

16 Na kwa hivyo Shetani alipotosha mbali mioyo ya watu kufanya aina yote ya uovu; kwa hivyo walifurahishwa na amani lakini kwa miaka michache tu.

6 10*a* MWM Kiburi.
12*a* 1 Tim. 6:17–19; Hel. 4:12.
13*a* MWM Mateso, Tesa.
b Mt. 5:39; 4 Ne. 1:34; M&M 98:23–25.
14*a* MWM Bidii.

17 Na hivyo katika mwanzo wa mwaka wa thelathini—watu wakiwa wameachiliwa kwa muda mrefu kuhangaishwa na [a]majaribio ya ibilisi mahali pote alipotaka kuwapeleka, na kufanya aina yote ya maovu aliyotaka wafanye—na hivyo mwanzoni mwa mwaka huu wa thelathini, walikuwa kwenye hali ya uovu wa kuogopesha.

18 Sasa hawakufanya dhambi [a]bila kujua, kwani walijua kile Mungu alichotaka wafanye, kwani ilikuwa imefundishwa kwao; kwa hivyo [b]waliasi kwa makusudi dhidi ya Mungu.

19 Na sasa ilikuwa katika siku za Lakoneyo, mwana wa Lakoneyo, kwani Lakoneyo alitwaa kiti cha baba yake na akasimamia watu mwaka huo.

20 Na kulianza kuwa na watu waliotumwa mbele na [a]kuongozwa kutoka mbinguni, ambao walisimama miongoni mwa watu katika nchi yote, wakihubiri na kushuhudia kwa ujasiri kwa ajili ya dhambi na uovu wa watu, na kushuhudia kwao kuhusu ukombozi ambao Bwana angewafanyia watu wake, au kwa maneno mengine, ufufuo wa Kristo; na walishuhudia kwa ujasiri [b]kifo chake na maumivu yake.

21 Sasa kulikuwa na watu wengi ambao walikasirika sana kwa sababu ya wale ambao walishuhudia vitu hivi; na wale ambao walikasirika walikuwa kwa wingi waamuzi wakuu na wale [a]waliokuwa makuhani wakuu, na mawakili hapo mbeleni; ndiyo, wale wote ambao walikuwa mawakili waliwakasirikia wale ambao walishuhudia vitu hivi.

22 Sasa hakukuwa na wakili wala mwamuzi wala kuhani mkuu ambaye alikuwa na uwezo wa kuhukumu mtu yeyote kufa isipokuwa hukumu yao iwekwe muhuri na mlinzi wa nchi.

23 Sasa kulikuwa na wengi ambao walishuhudia vitu hivi kuhusu Kristo, ambao walishuhudia kwa ujasiri, ambao walichukuliwa kisiri na kuuawa na waamuzi, kwamba vifo vyao havikujulikana na mtawala wa nchi mpaka baada ya vifo vyao.

24 Sasa tazama, hii ilikuwa kinyume cha sheria za nchi, kwamba mtu yeyote auawe isipokuwa wapate uwezo kutoka kwa msimamizi wa nchi—

25 Kwa hivyo nung'uniko lilitokea katika nchi ya Zarahemla, kwa msimamizi wa nchi, dhidi ya hawa waamuzi ambao walihukumu kufa kwa manabii wa Bwana, sio kulingana na sheria.

26 Sasa ikawa kwamba walichukuliwa na kuletwa mbele ya mwamuzi, kuhukumiwa kwa kosa ambalo walikuwa wamefanya, kulingana na [a]sheria

17 *a* MWM Jaribu, Majaribu.
18 *a* Mos. 3:11.
b MWM Uasi.
20 *a* MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi; Nabii.
b MWM Kusulubiwa; Lipia dhambi, Upatanisho.
21 *a* M&M 121:36–37. MWM Ukengeufu.
26 *a* Mos. 29:25; Alma 1:14.

ambayo ilikuwa imetolewa na watu.

27 Na ikawa kwamba hawa waamuzi walikuwa na marafiki wengi na jamaa; na waliosalia, ndiyo, hata karibu mawakili wote na makuhani wakuu, walijikusanya pamoja na kujiunga na jamaa za waamuzi ambao walikuwa wajaribiwe kulingana na sheria.

28 Na walifanya agano kila mmoja na mwingine, ndiyo, hata kwenye lile [a]agano ambalo lilitolewa na wale wa kale, agano ambalo lilitolewa na kusimamiwa na [b]ibilisi, kuungana dhidi ya wote walio haki.

29 Kwa hivyo waliungana dhidi ya watu wa Bwana, na kufanya agano kuwaangamiza, na kuokoa wale ambao walikuwa na hatia ya kuua kutokana na kufahamu haki, ambayo ilikuwa karibu kutekelezwa kulingana na sheria.

30 Na walidharau sheria na haki za nchi yao; na wakafanya agano wao wenyewe kwa wenyewe kumwangamiza msimamizi, na kumweka [a]mfalme juu ya nchi, ili nchi isiwe na uhuru lakini iwe chini ya wafalme.

MLANGO WA 7

Mwamuzi mkuu anauawa, serikali inavunjwa, na watu wanagawanyika katika makabila—Yakobo, mpinga Kristo, anakuwa mfalme wa kundi la siri—Nefi anahubiri toba na imani katika Kristo—Malaika wanamhubiria kila siku, na anamfufua kaka yake kutoka kwa wafu—Wengi wanatubu na wanabatizwa. Karibia mwaka 30–33 B.K.

Sasa tazama nitawaonyesha ninyi kwamba hawakumweka mfalme juu ya nchi, lakini katika mwaka huu huu, ndiyo, mwaka wa thelathini, walimwangamiza na kumuua mwamuzi mkuu akiwa kwenye kiti chake cha hukumu.

2 Na watu waligawanyika mmoja dhidi ya mwingine; na walijitenga mmoja kutoka kwa mwingine kwa makabila, kila mtu kulingana na jamaa yake na ukoo wake na marafiki; na hivyo wakaharibu serikali ya nchi.

3 Na kila kabila lilichagua chifu au kiongozi juu yao; na hivyo wakapata kuwa makabila na viongozi wa makabila.

4 Sasa tazama, kila mtu miongoni mwao alikuwa na wengi katika jamaa zake, na ndugu wengi na marafiki; kwa hivyo makabila yao yalikuwa makubwa sana.

5 Sasa hii yote ilifanyika, na bado hakukuwa na vita miongoni mwao; na huu uovu wote ulikuwa umewajia watu kwa sababu [a]walijisalimisha kwa nguvu ya Shetani.

6 Na sheria za serikali ziliharibiwa, kwa sababu ya [a]shirika la siri la marafiki na ukoo wa wale ambao waliwaua manabii.

28 *a* MWM Makundi maovu ya siri.
b Hel. 6:26–30.

30 *a* 1 Sam. 8:5–7; Alma 51:5.

7 5 *a* Rum. 6:13–16; Alma 10:25.

6 *a* 2 Ne. 9:9.

7 Na walisababisha ubishi mwingi nchini, mpaka kwamba sehemu kubwa ya wenye haki ilikuwa karibu yote imekuwa mbaya; ndiyo, kulikuwa tu watu wachache wenye haki miongoni mwao.

8 Na hivyo miaka sita ilikuwa haijapita tangu sehemu kubwa ya watu igeuke kutoka kwa haki, kama mbwa akiyarudia [a]matapiko yake mwenyewe au kama nguruwe aliyeoshwa akirudi kugaagaa matopeni.

9 Sasa hili shirika ovu la siri ambalo lilileta uovu mwingi juu ya watu, walijikusanya pamoja, na wakamweka mtu waliyemwita Yakobo kuwa kiongozi wao;

10 Na walimwita mfalme wao; kwa hivyo alipata kuwa mfalme wa hili kundi ovu; na alikuwa mmoja wa watu mashuhuri, ambaye alitoa sauti yake dhidi ya manabii ambao walishuhudia kuhusu Yesu.

11 Na ikawa kwamba hawakuwa wengi kama makabila ya watu, ambao waliungana pamoja isipokuwa viongozi wao waliweka sheria kila mmoja kwa kabila lake; hata hivyo walikuwa maadui; ingawa hawakuwa watu wa haki, lakini waliunganishwa katika chuki ya wale ambao walikuwa wamefanya agano kuangamiza serikali.

12 Kwa hivyo, Yakobo akiona kwamba maadui wao walikuwa wengi kuliko wao, kwa sababu alikuwa mfalme wa lile kundi, kwa hivyo aliamuru watu wake kwamba wakimbilie upande wa kaskazini kabisa ya nchi, na huko waanzishe [a]dola yao, mpaka waasi watakapojiunga nao, (kwani aliwabembeleza kwamba kutakuwa na waasi wengi) na mpaka wawe na nguvu ya kutosha kukabiliana na makabila ya watu; na walifanya hivyo.

13 Na mwendo wao ulikuwa wa kasi sana kwamba hawangesimamishwa mpaka walipokuwa wameenda mbali kupita ambapo watu wangewafikia. Na hivyo ukaisha mwaka wa thelathini; na hivyo ndivyo shughuli za watu wa Nefi zilivyokuwa.

14 Na ikawa katika mwaka wa thelathini na moja kwamba walijigawa katika makabila, kila mtu kulingana na jamaa yake, ukoo na marafiki; lakini walikuwa wamefikia mkataba kwamba hawangeanza vita tena mmoja na mwingine; lakini hawakujiunga katika sheria zao, na kila kabila lilikuwa na aina yake ya serikali, kwani zilianzishwa kufuatana na fikira za wale ambao walikuwa wakuu wao. Lakini walianzisha sheria kali sana kwamba kabila moja lisichukize lingine, mpaka kwamba kwa kiasi fulani walikuwa na amani nchini; lakini, mioyo yao iligeuka kutoka kwa Bwana Mungu wao, na wakawapiga kwa mawe, manabii na kuwatupa nje kutoka miongoni mwao.

8*a* Mit. 26:11; 2 Pet. 2:22.

12*a* 3 Ne. 6:30.

15 Na ikawa kwamba [a]Nefi—akishatembelewa na malaika, na pia sauti ya Bwana, kwa hivyo akiwa ameona malaika, na akiwa shahidi aliyeona na macho, na akiwa amepewa uwezo ili ajue kuhusu huduma ya Kristo, na pia akiwa shahidi aliyeona na macho kurudi kwao kwa haraka kutoka kwa haki hadi kwenye uovu wao na machukizo;

16 Kwa hivyo, kwa sababu ya kuhuzunishwa kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao na kutofahamu kwa akili zao—aliendelea miongoni mwao katika huo huo mwaka na kuanza kushuhudia kwa ujasiri, toba na msamaha wa dhambi kupitia imani katika Bwana Yesu Kristo.

17 Na aliwafundisha vitu vingi; na vyote haviwezi kuandikwa, na sehemu yao haiwezi kutosheleza, na kwa hivyo havijaandikwa kwenye kitabu hiki. Na Nefi alifundisha kwa [a]uwezo na mamlaka.

18 Na ikawa kwamba walimkasirikia, hata kwa sababu alikuwa na uwezo kuliko wao, kwani [a]haikuwezekana kwamba washuku neno lake, kwani imani yake kwa Bwana Yesu Kristo ilikuwa kubwa kwamba malaika walimhudumia kila siku.

19 Na katika jina la Yesu alitupa nje mashetani na [a]pepo wabaya; na hata alimfufua kaka yake kutoka kwa wafu, baada ya watu kumpiga kwa mawe na kumuua.

20 Na watu waliona, na kushuhudia kuwa ilitendeka, na walimkasirikia kwa sababu ya uwezo wake; na pia alifanya miujiza [a]mingi, machoni mwa watu, katika jina la Yesu.

21 Na ikawa kwamba mwaka wa thelathini na moja uliisha, na kulikuwa tu wachache ambao walimgeukia Bwana; lakini kadiri wengi waliogeuka walionyesha watu kwamba walitembelewa na uwezo na Roho wa Mungu, ambaye alikuwa katika Yesu Kristo, ambamo kwake waliamini.

22 Na jinsi kwa wengi ambao mashetani yalikuwa yametupwa nje yao, na magonjwa yao kuponywa, na udhaifu wao, walishuhudia kwa ukweli kwa watu kwamba waliguswa na Roho ya Mungu, na walikuwa wameponywa; na waliendelea kuonyesha ishara pia na kufanya miujiza miongoni mwa watu.

23 Hivyo mwaka wa thelathini na mbili uliisha pia. Na Nefi aliwazungumzia watu kwa sauti kubwa katika mwanzo wa mwaka wa thelathini na tatu; na aliwahubiria toba na msamaha wa dhambi.

24 Sasa nataka wewe ukumbuke pia, kwamba hakukuwa na mmoja ambaye aliletwa kwenye toba ambaye [a]hakubatizwa kwa maji.

25 Kwa hivyo walitawazwa

15*a* 3 Ne. 1:2.
17*a* MWM Uwezo.
18*a* 2 Ne. 33:1; Alma 4:19.
19*a* MWM Roho—Pepo wachafu.
20*a* 3 Ne. 8:1.
24*a* MWM Batiza, Ubatizo.

na Nefi, watu kwa huduma hii, kwamba yeyote atakayekuja kwao wangembatiza kwa maji, na walifanya hii kama ushahidi na ushuhuda mbele ya Mungu, na kwa watu, kwamba wametubu na [a]kusamehewa dhambi zao.

26 Na kulikuwa na wengi katika mwanzo wa mwaka huu ambao walibatizwa ubatizo wa toba, na hivyo sehemu kubwa ya mwaka ilipita.

MLANGO WA 8

Dhoruba, matetemeko, moto, vimbunga, na mchafuko wa ardhi ulishuhudia kusulubiwa kwa Kristo—Watu wengi wanaangamizwa—Giza linafunika nchi kwa muda wa siku tatu—Wale wanaosalia wanahuzunika kwa sababu ya majaliwa yao. Karibia mwaka 33–34 B.K.

Na sasa ikawa kwamba kulingana na maandishi yetu, na tunajua maandishi yetu kuwa ya kweli, kwani tazama, alikuwa mtu wa haki ambaye aliandika maandishi haya—kwani kweli alifanya [a]miujiza mingi katika [b]jina la Yesu; na hapakuweko na mtu yeyote ambaye angefanya miujiza katika jina la Yesu isipokuwa awe ameoshwa kila chembe kutokana na uovu wake.

2 Na sasa ikawa, kama hakukuwa na kosa lililotendwa na huyu mtu katika kuhesabu majira yetu, mwaka wa [a]thelathini na tatu ulikuwa umepita.

3 Na watu walianza kuangalia kwa bidii kwa ishara ambayo ilitolewa na nabii Samweli, Mlamani, ndiyo, kwa wakati ambao kungekuwa na [a]giza kwa muda wa siku tatu usoni mwa nchi.

4 Na kulianza kuwa na mashaka makuu na ugomvi miongoni mwa watu, ingawaje [a]ishara nyingi zilikuwa zimetolewa.

5 Na ikawa katika mwaka wa thelathini na nne, katika mwezi wa kwanza siku ya nne ya mwezi, kulitokea dhoruba kubwa, ambayo haijawahi kujulikana katika nchi yote.

6 Na kulikuwa pia tufani kubwa na ya kutisha; na kukawa na [a]radi ya kutisha, mpaka kwamba [b]ilitingisha dunia yote kama karibu kupasuka mbalimbali.

7 Na kulikuwa na umeme wa nguvu sana, ambao haujajulikana katika nchi yote.

8 Na [a]mji wa Zarahemla ulianza kuwaka moto.

9 Na mji wa Moroni ulizama kwenye kilindi cha bahari, na wakazi wake walitota.

10 Na ardhi ilifunika mji wa Moroniha, kwamba katika mahali pa mji kulitokea mlima mkubwa.

11 Na kulikuwa na uharibifu mkuu na wa kutisha katika nchi ya upande wa kusini.

25*a* M&M 20:37. MWM Ondoleo la Dhambi.

8 1*a* 3 Ne. 7:19–20; Morm. 9:18–19.
b Mdo. 3:6; Yak. (KM) 4:6.

2*a* 3 Ne. 2:8.

3*a* 1 Ne. 19:10; Hel. 14:20, 27; 3 Ne. 10:9.

4*a* MWM Kusulubiwa.

6*a* 1 Ne. 19:11; Hel. 14:21.
b Mt. 27:45, 50–51.

8*a* 4 Ne. 1:7–8.

12 Lakini tazama, kulikuwa na uharibifu mkubwa zaidi na wa kutisha katika nchi ya upande wa kaskazini; kwani tazama, sura ya nchi yote ilibadilika, kwa sababu ya tufani na kimbunga, na radi na umeme, na tetemeko kubwa la nchi yote.

13 Na barabara [a]kuu zilibomoka, na barabara laini ziliharibika, na mahali pengi laini palikwaruzwa.

14 Na miji mingi iliyojulikana [a]ilizama, na mingi ikachomwa, na mingi ilitingishwa mpaka majengo yao yakaanguka ardhini, na wakazi wa miji waliuawa, na mahali paliwachwa penye ukiwa.

15 Na kulikuwa na miji ambayo ilibaki; lakini uharibifu kwayo ulikuwa mkubwa sana, na kulikuwa na wengi ndani ya miji ambao waliuawa.

16 Na kulikuwa na wengine ambao walichukuliwa na vimbunga; na mahali walipoenda hakuna mtu anayejua, isipokuwa wanajua kwamba walipelekwa mbali.

17 Na hivyo uso wa ardhi yote uligeuzwa, kwa sababu ya tufani, na radi, na umeme, na kutingishika kwa nchi.

18 Na tazama, [a]miamba ilipasuka punde mbili; ilivunjika juu ya uso wa ardhi yote, mpaka kwamba ilipatikana katika vipande, kwa nyufa na mianya, juu ya uso wa nchi yote.

19 Na ikawa kwamba wakati radi, na umeme, na vimbunga, na tufani, na tetemeko la nchi vilipokwisha—kwani tazama, ulidumu muda wa masaa [a]matatu; na watu wengine walisema kwamba muda ulikuwa mrefu kuliko huo; walakini vitu hivi vyote vikubwa na vya kutisha vilifanyika katika muda wa masaa matatu—na kisha tazama, kulikuwa na giza juu ya nchi.

20 Na ikawa kwamba kulikuwa na giza jeusi juu ya uso wa nchi, mpaka kwamba wakazi wake ambao walikuwa hawajakufa waliweza [a]kuhisi [b]ukungu wa giza;

21 Na hakungekuwa na mwanga kwa sababu ya giza, wala mshumaa, wala mienge; wala hakungewashwa moto na miti yao mizuri na iliyokauka sana, ili hakungekuwa na mwanga kabisa;

22 Na hakukuonekana mwanga wowote, wala moto, wala mwanga kidogo, wala jua, wala mwezi, wala nyota, kwani ukungu wa giza ulikuwa mwingi sana ambao ulikuwa juu ya uso wa nchi.

23 Na ikawa kwamba ulidumu kwa muda wa siku [a]tatu kwamba hakukuwa na mwanga ambao ulionekana; na kulikuwa na maombolezo makubwa na kulia kwa hasira na kilio miongoni mwa watu wote bila kikomo; ndiyo, kulikuwa na kugumia kwingi kwa watu, kwa sababu ya giza na

13*a* Hel. 14:24; 3 Ne. 6:8.
14*a* 1 Ne. 12:4.
18*a* Hel. 14:21–22.
19*a* Lk. 23:44.
20*a* Ku. 10:21–22.
b 1 Ne. 12:5; 19:11.
23*a* 1 Ne. 19:10.

uharibifu mkubwa ambao uliwajia.

24 Na sehemu moja walisikika wakilia wakisema: Ee kwamba kama tulikuwa tumetubu kabla ya siku hii kubwa na kutisha, na ndipo ndugu zetu wangehurumiwa, na hawangechomwa katika ule mji mkuu wa [a]Zarahemla.

25 Na mahali pengine walisikika wakilia wakisema: Ee tunatamani kama tungekuwa tumetubu mbele ya hii siku kubwa ya kutisha, na kuwa hatungeua na kupiga manabii kwa mawe, na kuwatupa nje; hapo mama zetu na mabinti zetu warembo, na watoto wetu wangehurumiwa, na hawangezikwa katika mji wa Moroniha. Na hivyo vilio vya watu vilikuwa vikubwa na vya kuhofisha.

MLANGO WA 9

Katika giza, sauti ya Kristo inatangaza kuangamizwa kwa watu wengi na miji kwa sababu ya uovu wao—Anatangaza pia uungu Wake, anatangaza kwamba sheria ya Musa imetimizwa, na anawaalika watu waje Kwake na waokolewe. Karibia mwaka 34 B.K.

Na ikawa kwamba kulikuwa na [a]sauti iliyosikika miongoni mwa wakazi wa nchi, juu ya uso wa nchi hii, wakisema kwa sauti:

2 Ole, ole, ole kwa watu hawa; [a]ole kwa wakazi wa dunia nzima isipokuwa watubu; kwani ibilisi [b]hucheka, na malaika wake hufurahi, kwa sababu ya mauaji ya vijana wazuri na mabinti za watu wangu; na imefanyika kwa sababu ya uovu wao na machukizo kwamba wamekufa.

3 Tazama, nimeuchoma mji mkuu wa Zarahemla na wakazi wake kwa moto.

4 Na tazama ule mji mkuu Moroni nimeuzamisha kwenye kilindi cha bahari, na wakazi wake wamekufa maji.

5 Na tazama huo mji mkuu Moroniha nimeufunika kwa udongo, pamoja na wakazi wake, kuficha uovu wao na machukizo yao kutoka usoni mwangu, kwamba damu ya manabii na watakatifu haitarudi mara nyingine kwangu tena dhidi yao.

6 Na tazama, mji wa Gilgali nimeusababisha kuzama na wakazi wake kuzikwa kwenye kina cha ardhi.

7 Ndiyo, na mji wa Oniha na wakazi wake, na mji wa Mokumu na wakazi wake, na mji wa Yerusalemu na wakazi wake; na nimesababisha [a]maji kuja mahali ambapo walikuwa, kuficha uovu wao na machukizo kutoka mbele ya uso wangu, ili damu ya manabii na ya watakatifu haitakuja mara nyingine kwangu dhidi yao.

8 Na tazama, mji wa Gadiandi, na mji wa Gadiomna, na mji wa Yakobo, na mji wa Gimgimno, nimesababisha hiyo yote

24*a* Hel. 13:12.
9 1*a* 1 Ne. 19:11; 3 Ne. 11:10.
2*a* Mt. 11:20–21.
b Musa 7:26.
7*a* Eze. 26:19.

kuzamishwa, na kubunisha [a]vilima na mabonde katika mahali pao; na wakazi wake nimewazika kwenye kina cha ardhi, ili kuficha uovu wao na machukizo kutoka mbele ya uso wangu, kwamba damu ya manabii na ya watakatifu isije mara nyingine kwangu dhidi yao.

9 Na tazama, ule mji mkuu Yakobugathi, ambao ulikuwa na watu wa Yakobo, nimesababisha kuchomwa kwa moto kwa sababu ya dhambi zao, na uovu wao, ambao ulikuwa mwingi kuliko uovu wa dunia nzima, kwa sababu ya wauaji wao wa [a]siri na mashirika; kwani ni hao ambao waliharibu amani ya watu wangu na serikali ya nchi; kwa hivyo nilisababisha wachomwe, [b]kuwaangamiza kutoka uso wangu, kwamba damu ya manabii na ya watakatifu isije kwangu mara nyingine dhidi yao.

10 Na tazama, mji wa Lamani, na mji wa Yoshi, na mji wa Gadi, na mji wa Kishkumeni, nimesababisha kuchomwa kwa moto, na wakazi wake, kwa sababu ya uovu wao kwa kuwatupa nje manabii, na kuwapiga kwa mawe wale ambao niliwatuma kuwatangazia kuhusu uovu wao na machukizo yao.

11 Na kwa sababu waliwatupa wote nje, kwamba hakukuwa na yeyote aliyekuwa wa haki miongoni mwao, nilituma chini [a]moto na kuwaangamiza, kwamba uovu wao na machukizo yao yaweze kufichwa kutoka mbele ya uso wangu kwamba damu ya manabii na ya watakatifu ambao niliwatuma miongoni mwao isilie kwangu [b]kutoka chini dhidi yao.

12 Na nimesababisha maangamizo [a]mengi juu ya nchi hii, na juu ya hawa watu, kwa sababu ya uovu wao na machukizo yao.

13 Ee ninyi nyote ambao [a]mmeokolewa kwa sababu mlikuwa wenye haki kuliko hao, je mtarudi kwangu sasa, na kutubu dhambi zenu, na kugeuka ili [b]niwaponye?

14 Ndiyo, kwa kweli nawaambia, ikiwa [a]mtakuja kwangu, mtapata [b]uzima wa milele. Tazama, [c]mkono wangu wa rehema umenyoshwa kwenu, na yeyote atakayekuja, nitampokea; na heri ni wao ambao huja kwangu.

15 Tazama mimi ni Yesu Kristo Mwana wa Mungu. [a]Niliumba mbingu na dunia, na vitu vyote vilivyomo. Nilikuwa na Baba kutoka mwanzo. [b]Niko ndani ya Baba na Baba ndani yangu; na ndani yangu Baba ametukuza jina lake.

16 Nilikuja kwangu na walio wangu [a]hawakunipokea. Na

8 *a* 1 Ne. 19:11.
9 *a* Hel. 6:17–18, 21.
b Mos. 12:8.
11 *a* 2 Fal. 1:9–16; Hel. 13:13.
b Mwa. 4:10.
12 *a* 3 Ne. 8:8–10, 14.
13 *a* 3 Ne. 10:12.
b Yer. 3:22; 3 Ne. 18:32.
14 *a* 2 Ne. 26:24–28; Alma 5:33–36.
b Yn. 3:16.
c Alma 19:36.
15 *a* Yn. 1:1–3; Kol. 1:16; Hel. 14:12; Eth. 4:7; M&M 14:9.
b Yn. 17:20–22; 3 Ne. 11:27; 19:23, 29.
16 *a* Yn. 1:11; M&M 6:21.

maandiko kuhusu kuja kwangu yametimizwa.

17 Na vile wengi ambao wamenipokea, kwao [a]nimewapatia kufanyika wana wa Mungu; na hata hivyo nitawafanya kuwa wengi vile vile wataamini kwa jina langu, kwani tazama, kupitia kwangu, [b]ukombozi huja, na ndani yangu na kupitia kwangu [c]sheria ya Musa imetimizwa.

18 Mimi ni [a]nuru na uzima wa ulimwengu. Mimi ni [b]Alfa na Omega, mwanzo na mwisho.

19 Na [a]hamtatoa kwangu tena kumwagwa kwa damu; ndiyo, dhabihu na sadaka zenu za kuteketezwa zitakomeshwa, kwani sitakubali dhabihu na sadaku zenu zozote za kuteketezwa.

20 Na mtatoa kwangu [a]dhabihu ya moyo uliopondeka na roho iliyovunjika. Na yeyote atakayekuja kwangu na moyo uliopondeka na roho iliyovunjika, na huyo [b]nitambatiza kwa moto na Roho Mtakatifu, hata kwa njia sawa kama Walamani, kwa sababu ya imani yao kwangu wakati wa uongofu kwao, walibatizwa kwa moto na Roho Mtakatifu, na hawakujua.

21 Tazama, nimekuja duniani kuleta ukombozi ili kuokoa dunia kutoka dhambini.

22 Kwa hivyo yeyote [a]anayetubu na kuja kwangu kama [b]mtoto mdogo yeye, nitampokea, kwani hivyo ndivyo ulivyo ufalme wa Mungu. Tazama, kwa ajili ya kama hawa, [c]nimetoa maisha yangu, na nimeyachukua tena; kwa hivyo tubu, na mje kwangu ninyi nyote mlio duniani na muokolewe.

MLANGO WA 10

Kuna unyamavu katika nchi kwa saa nyingi—Sauti ya Kristo inaahidi kukusanya watu Wake kama vile kuku akusanyavyo vifaranga wake—Sehemu kubwa ya watu walio wa haki wanahifadhiwa. Karibia mwaka 34–35 B.K.

Na sasa tazama, ikawa kwamba watu wote nchini walisikia semi hizi, na walizishuhudia. Na baada ya semi hizi, kulikuwa na unyamavu nchini kwa masaa mengi;

2 Kwani mshangao wa watu ulikuwa mkubwa sana kwamba wakakoma kuomboleza na kulilia upotevu wa jamaa zao ambao walikuwa wameuawa; kwa hivyo kulikuwa na unyamavu katika nchi yote kwa muda wa masaa mengi.

3 Na ikawa kwamba kulitokea sauti tena kwa watu, na watu wote waliisikia, na wakaishuhudia ikisema:

17 *a* Yn. 1:12. MWM Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni; Wana na Mabinti za Mungu.
b MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
c 3 Ne. 12:19, 46–47; 15:2–9.
18 *a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b Ufu. 1:8. MWM Alfa na Omega.
19 *a* Alma 34:13.
20 *a* 3 Ne. 12:19; M&M 20:37.
b 2 Ne. 31:13–14.
22 *a* MWM Toba, Tubu.
b Mk. 10:15; Mos. 3:19; 3 Ne. 11:37–38.
c Yn. 10:15–18.

4 Ee ninyi watu wa miji [a]mikubwa ambayo imeanguka, ambao ni vizazi vya Yakobo, ndiyo, ambao ni wa nyumba ya Israeli, ni mara ngapi nimewakusanya kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake chini ya mbawa, na [b]nimewalisha.

5 Na tena, [a]mara ngapi ningekuwa nimewakusanyeni kama vile kuku akusanyavyo vifaranga vyake chini ya mabawa yake, ndiyo, Ee ninyi watu wa nyumba ya Israeli, ambao mmeanguka; ndiyo, Ee ninyi watu wa nyumba ya Israeli, ninyi mnaoishi Yerusalemu, kama vile wale ambao wameanguka; ndiyo, ni mara ngapi ningekuwa nimewakusanyeni kama vile kuku akusanyavyo vifaranga vyake na hamnikubali.

6 Ee ninyi nyumba ya Israeli ambao [a]nimewahurumia, ni mara ngapi nitawakusanya kama vile kuku hukusanya vifaranga wake chini ya mabawa yake, ikiwa mtatubu na [b]kunirudia kwa lengo moja la [c]moyo.

7 Lakini kama sivyo, Ee nyumba ya Israeli, mahali penu pa makao patakuwa tupu mpaka wakati wa kutimiza [a]agano nililofanya na babu zenu.

8 Na sasa ikawa kwamba baada ya watu kusikia maneno haya, tazama walianza kulia na kuzomea tena kwa sababu ya vifo vya jamaa zao.

9 Na ikawa kwamba hivyo siku tatu zilipita. Na ilikuwa asubuhi, na [a]giza likatoweka kutoka uso wa nchi, na ardhi ikakoma kutetemeka, na miamba ikakoma kupasuka, na kuzomea kwa kutisha kulikoma, na makelele yote ya ghasia yalikoma.

10 Na nchi ilishikamana tena pamoja kwamba ikaimarika; na kuomboleza, na kulia, na kulia kwa huzuni kwa watu walioachwa wazima kulikoma; na maombolezi yao yaligeuka kuwa shangwe, na kulia kwao kwa hasira kwa kusifu na kumshukuru Bwana Yesu Kristo Mkombozi wao.

11 Na hivyo kwa kiwango maandiko [a]yalitimia ambayo yalizungumzwa na manabii.

12 Na ikawa sehemu ya walio haki [a]zaidi ambao waliokolewa, na walikuwa hao ambao walipokea manabii na hawakuwapiga kwa mawe; na walikuwa hao ambao hawakumwaga damu ya watakatifu, ambao waliachwa—

13 Na walihurumiwa na hawakuzamishwa na kuzikwa ardhini; na hawakuzamishwa kwenye kina cha bahari; na hawakuchomwa kwa moto, wala hawakuangukiwa na kuvunjwa vipande hadi kufa; na hawakubebwa na tufani; wala hawakunyongwa na mvuke wa moshi na giza.

14 Na sasa yeyote asomaye,

10 4*a* 3 Ne. 8:14.
b 1 Ne. 17:3.
5*a* Mt. 23:37; M&M 43:24–25.
6*a* 3 Ne. 9:13.
b 1 Sam. 7:3; Hel. 13:11; 3 Ne. 24:7.
c Eze. 36:26.
7*a* MWM Agano.
9*a* 3 Ne. 8:19.
11*a* Mdo. 3:18–20.
12*a* 2 Ne. 26:8; 3 Ne. 9:13.

acha aelewe; yule ambaye ana maandiko, acha [a]ayapekue, na aone na kutazama ikiwa hivi vifo na maangamizo kwa moto, na kwa moshi na kwa dhoruba, na kwa tufani na kwa [b]kufunguliwa kwa ardhi kuwameza, na hivi vitu vyote havitimizi unabii wa manabii wengi watakatifu.

15 Tazama, ninawaambia, Ndiyo, wengi wameshuhudia vitu hivi wakati wa kuja kwa Kristo, na [a]waliuawa kwa sababu walishuhudia vitu hivi.

16 Ndiyo, nabii [a]Zeno pia alishuhudia vitu hivi, na pia Zenoki alizungumza kuhusu vitu hivi, kwa sababu vilishuhudia zaidi kutuhusu, ambao ni baki la uzao wao.

17 Tazama, baba yetu Yakobo pia alishuhudia kuhusu [a]baki la uzao wa Yusufu. Na tazama, sisi sio baki la uzao wa Yusufu? Na hivi vitu ambavyo vinashuhudia juu yao havikuandikwa kwenye mabamba ya shaba nyeupe ambayo baba yetu Lehi aliyaleta kutoka Yerusalemu?

18 Na ikawa kwamba mwishoni mwa mwaka wa thelathini na nne, tazama, nitawawonyesha kwamba watu wa Nefi ambao walihurumiwa, na pia wale ambao waliitwa Walamani, ambao walihurumiwa, upendeleo mwingi ulionyeshwa kwao, na baraka nyingi zilimwagwa vichwani mwao, mpaka kwamba mara baada ya [a]kupanda kwa Kristo mbinguni kwa kweli alijidhihirisha kwao—

19 [a]Akiwaonyesha mwili wake, na kuwahudumia; na historia ya huduma yake itatolewa baadaye. Kwa hivyo kwa wakati huu ninaweka kikomo kwa maneno yangu.

Yesu Kristo alijidhihirisha kwa watu wa Nefi, wakati umati ulipokuwa umejikusanya pamoja katika nchi ya Neema, na akawahubiria; na hivi ndivyo alivyojidhihirisha kwao.

Kuanzia mlango wa 11.

MLANGO WA 11

Baba anashuhudia kuhusu Mwana Wake Mpendwa—Kristo anatokea na kutangaza Upatanisho Wake—Watu wanapapasa alama za vidonda katika mikono na miguu na ubavu Wake—Wanapiga yowe Hosana—Anaanzisha utaratibu na namna ya ubatizo—Roho ya ubishi ni ya ibilisi—Mafundisho ya Kristo ni kwamba watu wanapaswa kuamini na wabatizwe na wapokee Roho Mtakatifu. Karibia mwaka 34 B.K.

Na sasa ikawa kwamba kulikuwa na umati mkubwa uliokusanyika pamoja, wa watu wa Nefi, karibu na hekalu

14 *a* MWM Maandiko—Thamani ya maandiko.
b 1 Ne. 19:11; 2 Ne. 26:5.

15 *a* MWM Kifo cha kishahidi, Mfiadini.

16 *a* Hel. 8:19–20.

17 *a* 2 Ne. 3:4–5; Alma 46:24; 3 Ne. 5:23–24.

18 *a* Mdo. 1:9–11.

19 *a* 3 Ne. 11:12–15.

ambalo lilikuwa katika nchi ya Neema; na walistaajabu na kushangaa mmoja na mwingine, na walionyeshana mabadiliko [a]makubwa na ya ajabu ambayo yalikuwa yamefanyika.

2 Na walikuwa wanamzungumzia huyu Yesu Kristo, ambaye [a]ishara zilikuwa zimetolewa kuhusu kifo chake.

3 Na ikawa kwamba wakati walipokuwa huko wakizungumza mmoja na mwingine, walisikia [a]sauti kama iliyotokea mbinguni; na wakaelekeza macho yao kila upande, kwani hawakutambua hiyo sauti ambayo walisikia; na haikuwa sauti kali, wala ya makelele; walakini, na ingawa ilikuwa sauti [b]ndogo tulivu, iliwapenya wale walioisikia hadi moyoni, mpaka kwamba hapakuweko na sehemu ya miili yao ambayo haikutetemeka; ndiyo, iliwatoboa mpaka kwenye roho yenyewe, na ikasababisha mioyo yao kuchomeka.

4 Na ikawa tena kwamba walisikia ile sauti, na hawakuitambua.

5 Na tena mara ya tatu wakasikia hiyo sauti, na wakafungua masikio yao kuisikiliza; na macho yao yakaelekea kule kulikotokea sauti; na walitazama kwa uthabiti kuelekea mbinguni, kule ambako sauti ilitokea.

6 Na tazama, mara ya tatu walielewa ile sauti ambayo walisikia; na ikawaambia:

7 Tazama [a]Mwana wangu Mpendwa ninayependezwa [b]na yeye, ambaye ndani yake nimetukuza jina langu—msikilizeni yeye.

8 Na ikawa walipofahamu, walielekeza macho yao tena mbinguni; na tazama, [a]walimwona mtu akiteremka kutoka mbinguni, na alikuwa amevaa joho refu leupe; na akaja chini na kusimama katikati yao; na macho ya umati wote yaligeuka kumwangalia, na hawakufungua vinywa vyao, hata mmoja kwa mwingine, na hawakujua kilichomaanishwa, kwani walidhani ni malaika ambaye alionekana kwao.

9 Na ikawa kwamba alinyosha mkono wake mbele na kuzungumza kwa watu akisema:

10 Tazama, Mimi ni Yesu Kristo ambaye manabii walishuhudia atakuja ndani ya ulimwengu.

11 Na tazama mimi ni [a]nuru na uzima wa ulimwengu; na nimekunywa kutoka kwa [b]kikombe kichungu ambacho Baba amenipatia, na nimemtukuza Bwana kwa [c]kujivika dhambi za ulimwengu ambamo ndani yake nimevumilia [d]mapenzi ya Baba katika vitu vyote kutoka mwanzo.

12 Na ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amesema maneno haya, umati wote

11 1*a* 3 Ne. 8:11–14.
2*a* Hel. 14:20–27.
3*a* Kum. 4:33–36; Hel. 5:29–33.
b 1 Fal. 19:11–13; M&M 85:6.
7*a* Mt. 3:17; 17:5; JS—H 1:17.
b 3 Ne. 9:15.
8*a* 1 Ne. 12:6; 2 Ne. 26:1.
11*a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b Mt. 26:39, 42.
c Yn. 1:29; M&M 19:18–19.
d Mk. 14:36; Yn. 6:38; M&M 19:2.

uliinama kwenye ardhi; kwani walikumbuka kwamba ilikuwa [a]imetabiriwa miongoni mwao kwamba Kristo atajidhihirisha kwao baada ya kupaa kwake mbinguni.

13 Na ikawa kwamba Bwana aliwazungumzia akisema:

14 Inukeni na mje kwangu, ili msukume mikono yenu na [a]muitie kwenye ubavu wangu, na pia kwamba mguse [b]alama za misumari katika mikono yangu na katika miguu yangu, ili mjue mimi ni Mungu wa Israeli, na [c]Mungu wa [d]ulimwengu wote, na nimeuawa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.

15 Na ikawa kwamba umati ulienda mbele, na kusukuma mikono yao ubavuni mwake, na wakaona alama za misumari katika mikono yake na katika miguu yake; na hivi walifanya wakienda mbele mmoja mmoja, mpaka walipoenda wote, na waliona na macho yao na kupapasa kwa mikono yao, na walijua ukweli na walishuhudia wenyewe kwamba [a]ni yeye, ambaye manabii waliandika kwamba atakuja.

16 Na wakati walipokuwa wameenda wote na kujishuhudia wenyewe, walipaza sauti kwa toleo moja wakisema:

17 Hosana! Heri liwe jina la Mungu Aliye Juu Sana! Na waliinama chini miguuni mwa Yesu na [a]kumwabudu.

18 Na ikawa kwamba alimzungumzia [a]Nefi (kwani Nefi alikuwa miongoni mwa umati) na kumwamuru kwamba aje mbele.

19 Na Nefi akainuka na kwenda mbele na kusujudu mbele ya Bwana na kubusu miguu yake.

20 Na Bwana alimwamrisha kwamba ainuke. Na aliinuka na kusimama mbele yake.

21 Na Bwana akamwambia: Ninakupatia [a]uwezo kwamba [b]utabatiza hawa watu nikiwa nimeenda tena mbinguni.

22 Na tena Bwana aliita [a]wengine, na akawaambia vile vile; na akawapatia uwezo wa kubatiza. Na akawaambia: Kwa njia hii mtabatiza; na [b]hakutakuwa na ugomvi miongoni mwenu.

23 Kweli nawaambia, kwamba yeyote atakayetubu dhambi zake kupitia [a]maneno yenu, na [b]kutaka kubatizwa katika jina langu, kwa njia hii mtawabatiza—Tazama, mtaenda chini na [c]kusimama majini, na katika jina langu mtawabatiza.

24 Na sasa tazama, haya ndiyo maneno ambayo mtasema, mkiwaita kwa jina, mkisema:

25 Nikiwa nimepewa [a]mamlaka na Yesu Kristo, ninakubatiza

12 *a* Alma 16:20.
14 *a* Yn. 20:27.
b Lk. 24:36–39; M&M 129:2.
c Isa. 45:3; 3 Ne. 15:5.
d 1 Ne. 11:6.
15 *a* MWM Yesu Kristo—Kuonekana kwa Kristo baada ya kifo.
17 *a* MWM Kuabudu.
18 *a* 3 Ne. 1:2, 10.
21 *a* MWM Uwezo.
b MWM Batiza, Ubatizo.
22 *a* 1 Ne. 12:7; 3 Ne. 12:1.
b 3 Ne. 18:34.
23 *a* 3 Ne. 12:2.
b MWM Batiza, Ubatizo—Sifa zinazotakiwa kwa ajili ya ubatizo.
c 3 Ne. 19:10–13.
25 *a* Mos. 18:13; M&M 20:73. MWM Batiza, Ubatizo—Mamlaka sahihi.

wewe katika jina la [b]Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu. Amina.

26 Na hapo [a]mtawatumbukiza katika maji, na kutoka tena nje ya maji.

27 Na kwa kufuata njia hii, mtabatiza katika jina langu; kwani tazama, kweli nawaambia kwamba, Baba, na Mwana wake, na Roho Mtakatifu wana [a]umoja; na niko ndani ya Baba, na Baba ndani yangu, na Baba na mimi tuna umoja.

28 Na kulingana na vile nimemwamuru hivyo ndivyo mtabatiza. Na hakutakuwa na [a]ugomvi miongoni mwenu, kama vile ilivyo hapa sasa; wala hakutakuwa na ugomvi miongoni mwenu kuhusu nukta za mafundisho yangu, kama vile ilivyokuwa.

29 Kwani amin, amin, nawaambia, yule ambaye ana [a]roho ya [b]ubishi siye wangu, bali ni wa ibilisi, ambaye ni baba wa ubishi, na huchochea mioyo ya watu kubishana kwa hasira wao kwa wao.

30 Tazama, hili sio fundisho langu, kuchochea mioyo ya wanadamu kwa hasira, moja dhidi ya mwingine; lakini hili ndilo fundisho langu, kwamba vitu kama hivi viondolewe mbali.

31 Tazama, amin, amin, ninawaambia, nitatangaza kwenu [a]mafundisho yangu.

32 Na haya ni [a]mafundisho yangu, na ni mafundisho ambayo Baba amenipatia; na [b]ninashuhudia mwenyewe kwa Baba, na Baba anashuhudia mwenyewe kwangu, na [c]Roho Mtakatifu anashuhudia kwa Baba na kwa Mimi, na ninashuhudia kwamba Baba huamuru watu wote, kila mahali, kutubu na kuniamini.

33 Na yeyote aaminiye ndani yangu na [a]kubatizwa, [b]ataokolewa; na hawa ndiyo [c]watakaorithi ufalme wa Mungu.

34 Na yeyote asiyeamini ndani yangu na hajabatizwa, atahukumiwa.

35 Amin, amin, nawaambia, kwamba, hili ni fundisho langu, na ninashuhudia kutoka kwa Baba; na yeyote [a]anayeamini ndani yangu anaamini kwa Baba pia, na kwake Baba atanishuhudia, kwani atamtembelea [b]na moto na [c]Roho Mtakatifu.

36 Na hivyo ndivyo Baba atakavyoshuhudia kunihusu, na Roho Mtakatifu atashuhudia kwake Baba na Mimi, kwani Baba na Mimi na Roho Mtakatifu tu wamoja.

25*b* MWM Mungu, Uungu.
26*a* MWM Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa kuzamishwa.
27*a* Yn. 17:20–22; 3 Ne. 28:10; Morm. 7:7; M&M 20:28.
28*a* 1 Kor. 1:10; Efe. 4:11–14; M&M 38:27.
29*a* 2 Tim. 2:23–24; Mos. 23:15. MWM Ushindani.
b TJS Efe. 4:26 (Kiambatisho); Mosia 2:32–33.
31*a* 2 Ne. 31:2–21.
32*a* MWM Mafundisho ya Kristo.
b 1 Yoh. 5:7.
c 3 Ne. 28:11; Eth. 5:4.
33*a* Mk. 16:16. MWM Batiza, Ubatizo—Muhimu.
b MWM Wokovu.
c MWM Utukufu wa Selestia.
35*a* Eth. 4:12.
b 3 Ne. 9:20; 12:2.
c MWM Roho Mtakatifu.

37 Na tena nawaambia, lazima mtubu na [a]muwe kama mtoto mdogo, na mbatizwe kwa jina langu, au hamtapokea vitu hivi kwa njia yoyote.

38 Na tena nawaambia, lazima mtubu na mbatizwe katika jina langu na muwe kama mtoto mchanga au hamtarithi ufalme wa Mungu kwa vyovyote.

39 Amin, amin, nawaambia, kwamba haya ni mafundisho yangu, na yeyote [a]atakayejenga juu ya mwamba wangu, na [b]milango ya jehanamu haitamshinda.

40 Na yeyote atakayetangaza mengi au madogo kuliko haya, na kuyaimarisha kuwa mafundisho yangu, yeye anatokana na uovu, na hajajenga kwenye mwamba wangu; lakini hujenga kwenye msingi wa [a]mchanga, na milango ya jehanamu husimama kupokea mtu kama huyu wakati mafuriko yakija na upepo hujipigisha juu yake.

41 Kwa hivyo muwaendee watu hawa, na mtangaze yale maneno ambayo nimezungumza, hadi mwisho wa dunia.

MLANGO WA 12

Yesu awaita na kuwapa mamlaka wale wanafunzi kumi na wawili—Anatoa hotuba kwa Wanefi sawa sawa na Mahubiri ya Mlimani—Yeye anazungumzia sifa za Heri—Mafundisho Yake yanapita na yanatangulia juu ya sheria za Musa—Watu wanaamriwa kuwa wakamilifu kama vile Yeye na Baba Yake walivyo wakamilifu—Linganisha na Mathayo 5. Karibia mwaka 34 B.K.

Na ikawa kwamba wakati Yesu alikuwa amesema maneno haya kwa Nefi, na kwa wale ambao walipokuwa wameitwa, (sasa idadi ya wale ambao walikuwa wameitwa na kupokea uwezo na mamlaka ya kubatiza, ilikuwa [a]kumi na wawili) na tazama, alinyoosha mkono wake mbele kwa umati, na kuwaambia kwa sauti kubwa akisema: [b]Heri ninyi ikiwa mtasikiliza maneno ya hawa kumi na wawili ambao [c]nimewachagua kutoka miongoni mwenu kuwahudumia, na kuwa watumishi wenu; na kwao nimewatolea uwezo kwamba wangewabatiza na maji; na baada ya hayo kwamba mmebatizwa na maji, tazama nitawabatiza kwa moto na Roho Mtakatifu; kwa hivyo heri ninyi ikiwa mtaamini katika mimi na mbatizwe, baada ya kuniona na kujua kwamba ni mimi.

2 Na tena wana heri nyingi wale ambao [a]wataamini kwa maneno haya yenu kwa sababu mtashuhudia kwamba mmeniona, na kwamba mnajua kwamba ni mimi. Ndiyo, heri kwa wale ambao wataamini katika

37*a* Mk. 10:15; Lk. 18:17; Mos. 3:19; 3 Ne. 9:22.
39*a* Mt. 7:24–29; Hel. 5:12.
MWM Mwamba.
b 3 Ne. 18:12–13.
40*a* 3 Ne. 14:24–27.
12 1*a* 3 Ne. 13:25.
b MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
c MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
2*a* M&M 46:13–14.
MWM Amini, Imani.

maneno yenu, na kujileta [b]chini kwenye unyenyekevu na kubatizwa, kwani watatembelewa [c]na moto na Roho Mtakatifu na watasamehewa dhambi zao.

3 Ndiyo, heri wale walio [a]maskini rohoni, ambao [b]wanakuja kwangu, kwani ufalme wa mbinguni ni wao.

4 Na tena heri wote walio na huzuni kwani watafarijika.

5 Na heri walio [a]wapole kwani watarithi [b]dunia.

6 Na heri wale wote walio na [a]njaa na kuwa na [b]kiu kwa ajili ya [c]haki, kwani watashibishwa na Roho Mtakatifu.

7 Na heri walio na [a]rehema kwani watapata rehema.

8 Na heri wote walio na moyo [a]mweupe, kwani [b]watamwona Mungu.

9 Na heri wote walio [a]wapatanishi, kwani wataitwa [b]watoto wa Mungu.

10 Na heri wale wote [a]wanaodhulumiwa kwa ajili ya jina langu kwani ufalme wa mbinguni ni wao.

11 Na heri ninyi, wakati watu watawatukana na kuwadhulumu, na watasema aina yoyote ya uovu dhidi yenu bila ukweli kwa ajili yangu;

12 Kwani mtakuwa na shangwe kubwa na mtakuwa wachangamfu kupita kiasi, kwani [a]thawabu yenu itakuwa kubwa mbinguni; kwani hivyo ndivyo walidhulumu hao manabii ambao walikuweko mbele yenu.

13 Amin, amin, nawaambia, ninawapatia muwe [a]chumvi ya dunia; lakini ikiwa chumvi itapoteza ladha yake, dunia itatiwa chumvi na nini? Chumvi kutokea hapo haitakuwa na uzuri wowote lakini itatupwa na kukanyagwa na miguu ya watu.

14 Amin, amin, ninawaambia, ninawapatia muwe nuru ya watu hawa. Mji uliojengwa kwenye kilima hauwezi kufichwa.

15 Tazama, je, watu huwasha [a]mshumaa na kuuweka chini ya pishi? La, lakini kwenye kinara cha mshumaa na humulika mwanga kwa wote walio ndani ya nyumba;

16 Kwa hivyo acha [a]nuru yenu iangae mbele ya hawa watu, ili wapate kuyaona matendo yenu, na kumtukuza Baba yenu aliye mbinguni.

17 Msifikirie kwamba nimekuja kuharibu sheria au manabii. Sikuja kuharibu bali kutimiza;

18 Kwani amin ninawaambia, nukta moja wala chembe moja haijaondoka kutoka kwa

2 *b* Eth. 4:13–15.
c 3 Ne. 11:35; 19:13.
3 *a* M&M 56:17–18.
MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
b Mt. 11:28–30.
5 *a* Rum. 12:16; Mos. 3:19.
MWM Pole, Upole.
b MWM Dunia.
6 *a* 2 Ne. 9:51; Eno. 1:4.
b Yer. 29:13.
c Mit. 21:21.
7 *a* MWM Rehema, enye Rehema.
8 *a* MWM Safi na Isiyo safi.
b M&M 93:1.
9 *a* MWM Msuluhishi.
b MWM Wana na Mabinti za Mungu.
10 *a* M&M 122:5–9.
MWM Mateso, Tesa.
12 *a* Eth. 12:4.
13 *a* M&M 101:39–40.
MWM Chumvi.
15 *a* Lk. 8:16.
16 *a* 3 Ne. 18:24.

[a]sheria, lakini ndani yangu yote imetimizwa.

19 Na tazama, nimewapatia sheria na amri za Baba yangu, kwamba mtaamini ndani yangu, na kwamba mtatubu dhambi zenu, na mje kwangu na [a]moyo uliopondeka na roho iliyovunjika. Tazama, mnazo amri mbele yenu, na [b]sheria imetimizwa.

20 Kwa hivyo njooni kwangu na mwokolewe; kwani amin nawaambia kwamba isipokuwa mtii amri zangu ambazo nimewaamuru wakati huu, kwa njia yoyote hamtaingia katika ufalme wa mbinguni.

21 Mmesikia kwamba ilisemekana na wale wa wakati wa kale, na pia imeandikwa mbele yenu, kwamba [a]usiue, na yeyote atakayeua atakuwa hatarini mwa hukumu ya Mungu;

22 Lakini ninawaambia kwamba, yeyote aliye na hasira na ndugu yake atakuwa hatarini ya hukumu yake. Na yeyote atakayesema kwa ndugu yake, Raka, atakuwa hatarini na baraza; na yeyote atakayesema, Wewe mjinga, atakuwa hatarini na moto wa jehanamu.

23 Kwa hivyo ikiwa utakuja kwangu, au utatamani kuja kwangu, na ukumbuke kwamba ndugu yako anacho kitu dhidi yako—

24 Nenda njia yako kwa ndugu yako, na kwanza [a]ondoa tofauti na ndugu yako, na hapo uje kwangu, na moyo wa lengo moja na nitakupokea.

25 Kubaliana na adui yako haraka, wakati uko katika njia moja na yeye, asije akupate wakati wowote na kukutupa gerezani.

26 Amin, amin, nakwambia hutatoka humo kamwe mpaka utakapolipa senti ya mwisho. Na wakati ungali upo gerezani unaweza kulipa hata [a]senti moja? Amin, amin, nakwambia, La.

27 Tazama, imeandikwa na wale wa kale, kwamba usifanye [a]uzinzi.

28 Lakini ninawaambia kwamba, yeyote ambaye anamchungulia mwanamke [a]kumtamani, huwa tayari amezini moyoni mwake.

29 Tazama, ninakupatia amri ili usikubali vitu hivi kuingia [a]moyoni mwako.

30 Kwani inawafaa kwamba mjizuie wenyewe hivi vitu, ambapo mtajitwika [a]msalaba wenu, kuliko kwamba mtupwe jehanamu.

31 Imeandikwa kwamba yeyote atakayempatia mke wake talaka, ampe cheti cha [a]talaka.

32 Amin, amin, nawaambia, kwamba yeyote atakayempatia mke wake [a]talaka, isipokuwa kwa sababu ya [b]uasherati,

18*a* MWM Torati ya Musa.
19*a* 3 Ne. 9:20.
MWM Moyo Uliovunjika.
b 3 Ne. 9:17.
21*a* Ku. 20:13; Mos. 13:21; M&M 42:18.
24*a* MWM Samehe.
26*a* Alma 11:3.
27*a* 2 Ne. 9:36; M&M 59:6.
28*a* M&M 42:23.
MWM Tamaa mbaya.
29*a* Mdo. 8:22.
30*a* Mt. 10:38; 16:24; Lk. 9:23.
31*a* MWM Talaka.
32*a* Mk. 10:11–12.
b MWM Uasherati.

humsababisha kutenda [c]uzinzi na yeyote atakayemwoa yule ambaye amepewa talaka anatenda uzinzi.

33 Na tena imeandikwa, na wale wa kale kwamba hutaapa uwongo mwenyewe, lakini utadhihirisha kwa Bwana [a]viapo vyako;

34 Lakini amin, amin ninawaambia, [a]usiape kabisa; wala kwa mbingu, kwani ni kiti cha enzi cha Mungu;

35 Wala kwa dunia, kwani ndipo mahali pa kuweka miguu yake;

36 Wala hutaapa kwa kichwa chako, kwani huwezi kutengeneza unywele wako mmoja kuwa mweusi au mweupe;

37 Lakini acha maongezi yenu yawe Ndiyo, ndiyo; La, la; kwani chochote kilicho zaidi ya haya ni ovu.

38 Na tazama, imeandikwa, jicho kwa [a]jicho, na jino kwa jino;

39 Lakini ninawaambia kwamba [a]hamtashindana na uovu, lakini yeyote atakayekupiga katika shavu la kulia, [b]mgeuzie upande mwingine pia;

40 Na ikiwa mtu yeyote atakushtaki mahakamani na achukue koti lako, mwachie achukue joho lako pia;

41 Na yeyote atakayekulazimisha kwenda maili moja, nenda na yeye mbili.

42 [a]Mpatie akuombaye, na atakayekukopa kwako usimfukuze.

43 Na tazama, imeandikwa pia na wale wa kale kwamba, utampenda jirani yako na umchukie adui wako;

44 Lakini tazama ninawaambia, wapendeni [a]maadui zenu, wabariki wanao walaani, wafanyie mazuri wale ambao wanawachukia, na [b]muwaombee wale ambao wanawatumia kwa madharau na kuwadhulumu;

45 Ili muwe watoto wa Baba yenu aliye mbinguni; kwani yeye husababisha jua kung'aa kwa waovu na kwa wenye haki.

46 Kwa hivyo vitu ambavyo vilikuwa vya kale, ambavyo vilikuwa chini ya sheria, vyote vimetimia.

47 Vitu vya [a]kale vimeachwa na vitu vyote vimekuwa vipya.

48 Kwa hivyo ningependa kwamba mngekuwa [a]wakamilifu hata kama nilivyo, au Baba yenu ambaye yuko mbinguni ni mkamilifu.

MLANGO WA 13

Yesu anawafundisha Wanefi Sala ya Bwana—Wanahitaji kuweka hazina zao mbinguni—Wale wanafunzi kumi na wawili katika huduma yao wanaamriwa kutofikiria vitu vya kidunia—Linganisha Mathayo 6. Karibia mwaka 34 B.K.

Amin, amin, nawaambia kwamba toeni [a]sadaka zenu kwa

32 *c* MWM Uzinzi.
33 *a* MWM Kiapo.
34 *a* MWM Lugha chafu.
38 *a* Law. 24:20.
39 *a* 3 Ne. 6:13; 4 Ne. 1:34; M&M 98:23–32.
b MWM Subira.
42 *a* Yak. (KM) 2:17–19; Mos. 4:22–26.
44 *a* Mit. 24:17; Alma 48:23.
b Mdo. 7:59–60.
47 *a* 3 Ne. 15:2, 7; M&M 22:1.
48 *a* Mt. 5:48; 3 Ne. 27:27. MWM Kamilifu.
13 1 *a* MWM Sadaka, Utoaji sadaka.

masikini; lakini chungeni kwamba msitoe sadaka zenu mbele ya watu kwa kuonekana nao; la sivyo hamna thawabu ya Baba yenu ambaye yuko mbinguni.

2 Kwa hivyo, wakati mtakapotoa sadaka zenu msivumishe tarumbeta mbele yenu, vile wanafiki hufanya kwenye masinagogi na katika barabara, ili wapate [a]kutukuzwa na watu. Amin nawaambia, wana thawabu yao.

3 Lakini unapotoa sadaka acha mkono wako wa kushoto usijue vile mkono wa kulia unafanya;

4 Ili sadaka zenu ziwe katika siri; na Baba yenu ambaye huona kwa siri, mwenyewe atawalipa wazi.

5 Na wakati [a]mnaomba hamtafanya kama wanafiki wanavyofanya, kwani wanapenda kuomba, wakisimama ndani ya masinagogi na kwenye pembe za barabara, ili waonekane na watu. Amin ninawaambia, wanayo thawabu yao.

6 Lakini wewe, unaposali, ingia kwenye chumba chako kidogo, na wakati umefunga mlango wako, sali kwa Baba yako ambaye yuko mafichoni; na Baba yako, ambaye huona kisiri, atakulipa wazi.

7 Lakini wakati unasali, usitumie marudio ya bure, kama walimwengu, kwani wanadhani kwamba watasikika kwa kutumia maneno mengi.

8 Kwa hivyo usiwe kama hao, kwani Baba yako [a]anajua ni vitu gani unavyohitaji kabla ya wewe kumwuliza.

9 Kwa hivyo [a]msali kwa [b]njia hii: [c]Baba yetu uliye mbinguni, jina lako litukuzwe.

10 Mapenzi yako yatimizwe duniani vile yalivyo mbinguni.

11 Na utusamehe deni zetu, kama tunavyowasamehe wadeni wetu.

12 Na [a]usituongoze kwenye majaribu, lakini utuokoe kutoka kwa maovu.

13 Kwani ufalme ni wako, na uwezo, na utukufu, milele. Amina.

14 Kwani, ikiwa [a]mtasamehe watu makosa yao Baba yenu wa mbinguni atawasamehe pia.

15 Lakini kama hamtawasamehe watu makosa yao Baba yenu hatawasamehe makosa yenu.

16 Tena [a]mnapofunga msiwe kama wanafiki, wenye nyuso za kuhuzunika, kwani hukunja nyuso zao ili waonekane wanafunga. Amin ninawaambia, wanayo thawabu yao.

17 Lakini wewe, unapofunga, paka mafuta kwa kichwa chako, na unawe uso wako;

18 Ili usionekane na watu kama unafunga, lakini kwa Baba yako, aliye sirini; na Baba yako, ambaye huona [a]sirini, atakupatia zawadi wazi.

19 Msijiwekee hazina duniani,

2*a* M&M 121:34–35.
5*a* MWM Sala.
8*a* M&M 84:83.
9*a* MWM Sala.
b Mt. 6:9–13.
c MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.
12*a* TJS Mt. 6:14 (Kiambatisho).
14*a* Mos. 26:30–31; M&M 64:9. MWM Samehe.
16*a* Isa. 58:5–7. MWM Funga, Kufunga.
18*a* M&M 38:7.

ambapo nondo na kutu huozesha, na wezi wanavunja na kuiba;

20 Lakini mjiwekee [a]hazina zenu mbinguni, ambapo nondo wala kutu haziozeshi, na ambapo wezi hawawezi kuvunja na kuingia wala kuiba.

21 Kwani mahali ambapo hazina yako ipo, pale pia moyo wako utakuwa.

22 [a]Nuru ya mwili ni jicho; kwa hivyo, ikiwa jicho lako liko moja, mwili wako wote utajaa nuru.

23 Lakini kama jicho lako ni ovu, mwili wako wote utajaa giza. Kwa hivyo, ikiwa nuru iliyopo ndani yako itakuwa giza, sio hio ni giza kuu!

24 Hakuna mtu ambaye anaweza [a]kutumikia mabwana wawili; kwani labda atamchukia mmoja na kumpenda mwingine, au kama sivyo atampenda mmoja na kumdhulumu mwingine. Huwezi kumtumikia Mungu na Mali.

25 Na sasa ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amezungumza maneno haya alielekeza macho juu ya wale kumi na wawili ambao alikuwa amewachagua, na akawaambia: Kumbukeni maneno ambayo nimezungumza. Kwani tazama, ni ninyi ambao nimechagua [a]kuwahudumia hawa watu. Kwa hivyo ninawaambia, [b]msisumbukie maisha yenu, ni nini mtakula, au ni nini mtakunywa; wala mtavaa nini, kwenye miili yenu. Je, si maisha yako zaidi ya chakula, na mwili zaidi ya mavazi?

26 Tazama ndege wa angani, kwani hawapandi, wala hawavuni, wala hawakusanyi kwenye maghala; lakini Baba yenu wa mbinguni huwalisha. Je, si ninyi ni bora kuliko wao?

27 Ni nani kati yenu kwa kufikiria anaweza kuongeza mkono mmoja kwa urefu wake?

28 Na kwa nini msumbuke kwa mavazi? Fikirieni maua ya mwituni vile yanakua; hayafanya kazi, wala hayasokoti;

29 Na bado ninawaambia, kwamba hata Sulemani, kwa enzi yake yote, hakupambwa kama moja ya hawa.

30 Kwa hivyo, ikiwa Mungu anavika nyasi ya shambani, ambayo ipo leo, na kesho itatupwa kwenye jiko, hata hivyo atakuvisha, ikiwa huna imani ndogo.

31 Kwa hivyo msisumbuke, mkisema, Tutakula nini? au, Tutakunywa nini? au, Tutavaa nini?

32 Kwani Baba yenu wa mbinguni anajua kwamba mna mahitaji ya hivi vitu vyote.

33 Lakini tafuteni kwanza [a]ufalme wa Mungu na haki yake, na hivi vitu vyote vitaongezwa kwenu.

34 Kwa hivyo msisumbuke kwa kesho, kwani kesho itajishugulisha na vitu vyake yenyewe. Kila siku ina maovu yake ya kutoshana nayo.

20 *a* Hel. 5:8; 8:25.
22 *a* M&M 88:67.
24 *a* 1 Sam. 7:3.
25 *a* MWM Kuhudumu.
b Alma 31:37–38; M&M 84:79–85.
33 *a* Lk. 12:31.

MLANGO WA 14

Yesu anaamuru: Msihukumu; ombeni Mungu; jihadhari na manabii wa uwongo—Anaahidi wokovu kwa wale wanaotenda nia ya Baba—Linganisha Mathayo 7. Karibia mwaka 34 B.K.

Na sasa ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amezungumza maneno haya aligeuka tena akaelekea umati, na kufungua kinywa chake kwao, na kusema: Kweli, kweli, ninawaambia, [a]Msihukumu, kwamba msije mkahukumiwa.

2 [a]Kwani kwa hukumu mnayo hukumia, mtahukumiwa nayo; na kipimo kile mpimiacho, ndicho mtakachopimiwa tena.

3 Na mbona wakitazama kibanzi ambacho kiko ndani ya jicho la ndugu yako, lakini hufikirii kiboriti ambacho kiko kwenye jicho lako?

4 Au utasemaje kwa ndugu yako: Acha nitoe kibanzi ndani ya jicho lako—na tazama, kiboriti kiko ndani ya jicho lako?

5 Wewe mnafiki, kwanza ondoa [a]kiboriti kutoka kwenye jicho lako; na ndipo utaona vema kukitoa kibanzi kutoka ndani ya jicho la ndugu yako.

6 Msitoe kile kilicho [a]kitakatifu kwa mbwa, wala msitupe lulu mbele ya nguruwe, wasije wakazikanyaga chini ya miguu yao, na kugeuka tena na kuwararua.

7 [a]Ombeni, na mtapewa; tafuteni na mtapata, bisheni, na mtafunguliwa.

8 Kwani kila mmoja ambaye huuliza, hupata; na yule anayetafuta, huvumbua; na yule ambaye hubisha, hufunguliwa.

9 Au kuna mtu gani kwenu, ambaye, ikiwa mwana wake anamwomba mkate, atampatia jiwe?

10 Au kama anamwomba samaki, atampatia nyoka?

11 Ikiwa ninyi, mkiwa waovu, mnajua kuwapatia watoto wenu zawadi nzuri, je, ni vipi Baba yenu aliye mbinguni atawapa vitu vizuri wale ambao humwomba?

12 Kwa hivyo, vitu vyote ambavyo mngetaka kwamba watu wawafanyie, [a]wafanyie pia wengine, kwani hii ni sheria na manabii.

13 Ingieni kwa kupitia [a]mlango mwembamba; kwani mlango ni wazi, na [b]pana ndiyo njia iongozayo kwenye uharibifu, na waiendayo ni wengi;

14 Kwa sababu [a]mlango umesonga, na njia ni [b]nyembamba, iendayo uzimani, nao waipatao ni [c]wachache.

15 Jihadharini na [a]manabii wa uwongo, ambao huwajia wakiwa wamevaa mavazi ya kondoo, lakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali.

16 Mtawatambua kwa matu-

14 1*a* TJS Mt. 7:1–2 (Kiambatisho); Yn. 7:24.
2*a* Morm. 8:19.
5*a* Yn. 8:3–11.
6*a* MWM Takatifu.
7*a* 3 Ne. 27:29. MWM Sala.
12*a* MWM Huruma.
13*a* Lk. 13:24; 3 Ne. 27:33.
b M&M 132:25.
14*a* 2 Ne. 9:41; 31:9, 17–18; M&M 22.
b 1 Ne. 8:20.
c 1 Ne. 14:12.
15*a* Yer. 23:21–32; 2 Ne. 28:9, 12, 15.

nda yao. Je, watu huchuma zabibu katika miiba, au tini katika mibaruti?

17 Hata hivyo kila mti mwema huzaa matunda mazuri; lakini mti mwovu huzaa matunda mabaya.

18 Mti mwema hauwezi kuzaa matunda mabaya wala mti mbaya kuzaa matunda mema.

19 Kila mti ambao [a]hauzai matunda mazuri hukatwa, na kutupwa motoni.

20 Kwa hivyo, kwa [a]matunda yao mtawajua.

21 Sio kila anayesema kwangu, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; lakini yule anayefanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni.

22 Wengi [a]watasema kwangu siku ile: Bwana, Bwana, si tulifanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako si tumetoa pepo wachafu, na katika jina lako kufanya miujiza mingi?

23 Na ndipo nitawaambia dhahiri: [a]Sikuwajua ninyi kamwe; [b]ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.

24 Kwa hivyo, yeyote asikiaye maneno haya yangu na kuyafanya, nitamfananisha na mtu mwenye hekima, ambaye alijenga nyumba yake juu ya [a]mwamba—

25 Na [a]mvua ilinyesha, na mafuriko yakaja, na pepo zikavuma, na zikapiga ile nyumba; na [b]haikuanguka, kwani iliwekwa kwenye mwamba.

26 Na yeyote asikiaye maneno haya yangu na hayafanyi atalinganishwa na mtu mpumbavu aliyejenga nyumba yake juu ya [a]mchanga—

27 Na mvua ilinyesha, na mafuriko yakaja, na pepo zikavuma, na zikaipiga ile nyumba; na ilianguka, na mwanguko wake ulikuwa mkubwa.

MLANGO WA 15

Yesu anatangaza kwamba sheria ya Musa imetimizwa katika Yeye—Wanefi ndiyo wale kondoo wengine ambao Yeye alizungumzia akiwa Yerusalemu—Kwa sababu ya uovu, watu wa Bwana katika Yerusalemu hawajui kuhusu kondoo waliotawanywa wa Israeli. Karibia mwaka 34 B.K.

Na sasa ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amemaliza maneno haya alizungusha macho yake karibu hapo kwa umati, na akawaambia: Tazameni, mmesikia vitu ambavyo nilifundisha kabla ya kupaa juu kwa Baba yangu; kwa hivyo, yeyote akumbukaye maneno haya yangu na [a]kuyafanya, yeye [b]nitamwinua juu katika siku ya mwisho.

2 Na ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amesema maneno haya aliona kwamba

19 *a* Mt. 3:10; Alma 5:36–41; M&M 97:7.
20 *a* Lk. 6:43–45; Moro. 7:5.
22 *a* Alma 5:17.
23 *a* Mos. 5:13; 26:24–27.
b Lk. 13:27.
24 *a* MWM Mwamba.
25 *a* Alma 26:6; Hel. 5:12.
b Mit. 12:7.
26 *a* 3 Ne. 11:40.
15 1 *a* Yak. (Bib.) 1:22.
b 1 Ne. 13:37; M&M 5:35.

kulikuwa na wengine miongoni mwao ambao walistaajabu, na kushangaa kile alichotaka kufanya na [a]sheria ya Musa; kwani hawakuelewa msemo uliosema kwamba vitu vya kale vilikuwa vimepita, na kwamba vitu vyote vilikuwa vimekuwa vipya.

3 Na akawaambia: Msistaajabu kwamba nilisema vitu vya kale vilikuwa vimepita, na kwamba vyote vilikuwa vimekuwa vipya.

4 Tazama, ninawaambia kwamba [a]sheria imetimizwa ambayo alipewa Musa.

5 Tazama, ni [a]mimi niliyempa ile sheria, na ni mimi niliyeagana na watu wangu Israeli; kwa hivyo, sheria imetimizwa ndani yangu, kwani nimekuja [b]kutimiza sheria; kwa hivyo imefika mwisho.

6 Tazama, [a]siharibu maandishi ya manabii, kwani kadiri mengi ambayo hayajatimizwa ndani yangu, kweli nawaambia, yote yatatimizwa.

7 Na kwa sababu niliwaambia kwamba vitu vya kale vimepita, siharibu ile ambayo imezungumzwa kuhusu vitu ambavyo vinakuja.

8 Kwani tazama, [a]agano ambalo nimefanya na watu wangu lote halijatimizwa; lakini sheria ambayo ilipewa Musa imemalizika kwa sababu yangu.

9 Tazama, Mimi ndiye [a]sheria, na [b]nuru. Nitazameni mimi, na mvumilie hadi mwisho wangu, na [c]mtaishi; kwani kwa yule ambaye [d]huvumilia hadi mwisho nitampatia uzima wa milele.

10 Tazama, nimewapatia amri; kwa hivyo tiini [a]amri zangu. Na hii ni sheria na maandishi ya manabii, kwani [b]walinishuhudia kwa ukweli.

11 Na sasa ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amezungumza maneno haya, aliwaambia wale kumi na wawili ambao alikuwa amewachagua:

12 Ninyi ni wanafunzi wangu; na ninyi ni nuru kwa hawa watu, ambao ni baki la nyumba ya [a]Yusufu.

13 Na tazama, hii ni [a]nchi ya urithi wenu; na Baba amewapatia.

14 Na kamwe hakuna wakati wowote ambao Baba amenipatia amri kwamba [a]niwaambie ndugu zenu katika Yerusalemu.

15 Wala katika muda wowote Baba hajanipa amri kwamba niwaambie kuhusu [a]makabila mengine ya nyumba ya Israeli, ambao Baba amewaongoza mbali kutoka nje ya nchi.

16 Hiki kiasi Baba aliniamuru, kwamba ningewaambia:

2 *a* MWM Torati ya Musa.
4 *a* Mos. 13:27–31; 3 Ne. 9:17–20.
5 *a* 1 Kor. 10:1–4; 3 Ne. 11:14. MWM Yehova.
b Alma 34:13.
6 *a* 3 Ne. 23:1–5.
8 *a* 3 Ne. 5:24–26.
9 *a* 2 Ne. 26:1.
b MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
c Yn. 11:25; M&M 84:44.
d MWM Stahimili.
10 *a* 3 Ne. 12:20.
b Mos. 13:33.
12 *a* MWM Yusufu, Mwana wa Yakobo.
13 *a* 1 Ne. 18:22–23.
14 *a* 3 Ne. 5:20.
15 *a* 3 Ne. 16:1–4. MWM Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea.

17 Kwamba kondoo wengine ninao ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta, na watasikia sauti yangu; na kutakuwa na kundi moja, na [a]mchungaji mmoja.

18 Na sasa, kwa sababu ya shingo ngumu na kutoamini, [a]hawakuelewa maneno yangu; kwa hivyo, niliamrishwa na Baba nisiwaambie zaidi kuhusu kitu hiki.

19 Lakini kweli, nawaambia kwamba Baba ameniamuru, na nawaambia kwamba mlitenganishwa kutoka miongoni mwao kwa sababu ya uovu wao; kwa hivyo ni sababu ya uovu wao kwamba hawajui chochote kuwahusu.

20 Na kweli, nawaambia tena kwamba makabila mengine yametengwa na Baba kutoka kwao; na ni kwa sababu ya uovu wao kwamba hawajui chochote kuwahusu.

21 Na kweli nawaambia, kwamba ni ninyi ambao nilisema: Kondoo [a]wengine ninao ambao sio wa zizi hili; hao nao ninapaswa kuwaleta, na watasikia sauti yangu; na kutakuwa na kundi moja, na mchungaji mmoja.

22 Na hawakunielewa, kwani walidhani kwamba nilizungumza kuhusu Wayunani; kwani hawakuelewa kwamba [a]Wayunani [b]watageuka kupitia mahubiri yao.

23 Na hawakunielewa kwamba nilisema wataelewa sauti yangu; na hawakunielewa kwamba [a]Wayunani hawataisikia sauti yangu wakati wowote—kwamba sitajidhihirisha kwao isipokuwa kupitia kwa [b]Roho Mtakatifu.

24 Lakini tazama, nyote mmesikia [a]sauti yangu, na kuniona; na ninyi ni kondoo wangu, na mmehesabiwa miongoni mwa wale ambao Baba [b]amenipatia.

MLANGO WA 16

Yesu atawatembelea kondoo wengine wa Israeli waliopotea—Katika siku za mwisho injili itawaendea Wayunani na baadaye kwa nyumba ya Israeli—Watu wa Bwana wataona ana kwa ana wakati Yeye atakapoileta tena Sayuni. Karibia mwaka 34 B.K.

Na kweli, kweli, nawaambia kwamba ninao [a]kondoo wengine, ambao si wa nchi hii, wala ya Yerusalemu, wala mahali popote katika nchi ya karibu niliyotoa huduma.

2 Kwani wale ambao ninawazungumzia ni wale ambao bado hawajasikia sauti yangu; wala sijajidhihirisha kwao.

3 Lakini nimepokea amri kutoka kwa Baba kwamba [a]niwaendee, na kwamba watasikia sauti yangu, na watahesabiwa miongoni mwa kondoo wangu, ili kuwe na kundi moja

17 *a* MWM Mchungaji Mwema.
18 *a* M&M 10:59.
21 *a* Yn. 10:14–16.
22 *a* MWM Wayunani.
b Mdo. 10:34–48.
23 *a* Mt. 15:24.
b 1 Ne. 10:11. MWM Roho Mtakatifu.
24 *a* Alma 5:38; 3 Ne. 16:1–5.
b Yn. 6:37; M&M 27:14.
16 1 *a* 3 Ne. 15:15. MWM Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea.
3 *a* 3 Ne. 17:4.

na mchungaji mmoja; kwa hivyo nitaenda kujidhihirisha kwao.

4 Na ninawaamuru kwamba mtaandika [a]maneno haya baada ya mimi kuondoka, ili ikiwa watu wangu katika Yerusalemu, hao ambao wameniona na kuwa na mimi katika huduma yangu, hawamwulizi Baba katika jina langu, kwamba wangeelemishwa kuwahusu kupitia Roho Mtakatifu, na pia kuhusu makabila mengine ambayo hawajui, kwamba maneno haya ambayo mtaandika yatahifadhiwa na yatadhihirishwa kwa [b]Wayunani, ili kupitia utimilifu wa Wayunani, baki la uzao wao, ambao utatawanyishwa kila mahali kwa uso wa dunia kwa sababu ya kutoamini kwao, wangeletwa ndani, au wangeletwa [c]kujua kunihusu mimi, Mkombozi wao.

5 Na ndipo [a]nitawakusanya kutoka sehemu nne za ulimwengu; na ndipo nitatimiza [b]agano ambalo Baba amefanya kwa watu wote wa [c]nyumba ya Israeli.

6 Na heri [a]Wayunani, kwa sababu ya imani yao kwangu, imani ambayo inatokana na [b]Roho Mtakatifu, ambaye anashuhudia kwao juu yangu na juu ya Baba.

7 Tazama, kwa sababu ya imani yao kwangu, Baba asema, na kwa sababu ya kutoamini kwenu, Ee nyumba ya Israeli, katika [a]siku ya mwisho, ukweli utawajia Wayunani, kwamba utimilifu wa hivi vitu utajulikana kwao.

8 Lakini ole, asema Baba, kwa wale Wayunani wasioamini—kwani hata ingawa wamefika juu ya nchi hii, na [a]wamewatawanya watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli; na watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli [b]wametupwa nje kutoka miongoni mwao, na wamekanyangwa chini ya miguu na hao;

9 Na kwa sababu ya rehema za Baba kwa Wayunani, na pia hukumu za Baba juu ya watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli, kweli, kweli, nawaambia, kwamba baada ya haya yote, na nimesababisha watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli [a]kuuawa, na kuteswa, na kuchinjwa, na kutupwa nje kutoka miongoni mwao, na kuchukiwa nao, na kuwa wa kufyonya na mithali miongoni mwao—

10 Na hivyo Baba anaamuru kwamba inanibidi niseme kwenu: Katika siku ile wakati Wayunani watafanya dhambi dhidi ya injili yangu, na

4*a* MWM Maandiko.
b 1 Ne. 10:14; 3 Ne. 21:6.
c Eze. 20:42–44; 3 Ne. 20:13.
5*a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b 3 Ne. 5:24–26.
c 1 Ne. 22:9; 3 Ne. 21:26–29.
6*a* 1 Ne. 13:30–42; 2 Ne. 30:3.
b 2 Ne. 32:5; 3 Ne. 11:32, 35–36. MWM Roho Mtakatifu.
7*a* MWM Urejesho wa Injili.
8*a* 1 Ne. 13:14; Morm. 5:9, 15.
b 3 Ne. 20:27–29.
9*a* Amo. 9:1–4.

watakataa utimilifu wa injili yangu, na [a]watainuliwa juu katika kiburi cha mioyo yao juu ya mataifa yote, na juu ya watu wote wa dunia, na wajazwe na kila aina ya udanganyifu, na uwongo, na madhara, na aina yote ya unafiki, na mauaji, na [b]ukuhani wa uongo, na ukahaba, na machukizo ya siri; na ikiwa watafanya vitu vile vyote, na wakatae utimilifu wa injili yangu, tazama, Baba anasema, nitachukua utimilifu wa injili yangu kutoka miongoni mwao.

11 Na ndipo [a]nitakumbuka agano ambalo nimefanya kwa watu wangu, Ee nyumba ya Israeli, na nitaleta injili yangu kwao.

12 Na nitawaonyesha, Ee nyumba ya Israeli, kwamba Wayunani hawatakuwa na uwezo juu yenu; lakini nitakumbuka agano langu na ninyi, Ee nyumba ya Israeli, na mtakuja kuwa na [a]ufahamu wa utimilifu wa injili yangu.

13 Lakini ikiwa Wayunani watatubu, na kunirudia, asema Baba, tazama [a]watahesabika miongoni mwa watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.

14 Na sitakubali watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli, kupitia miongoni mwao, na kuwakanyaga chini, anasema Baba.

15 Lakini kama hawatageuka kwangu, na kusikiliza sauti yangu, nitawakubalia, ndiyo, nitakubali watu wangu, Ee nyumba ya Israeli, kwamba watapita miongoni mwao, na [a]watawakanyaga chini, na watakuwa kama chumvi ambayo imepoteza ladha yake, ambayo kutoka hapo haiwi nzuri kwa chochote lakini ni ya kutupwa nje, na kukanyagwa na miguu ya watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.

16 Kweli, kweli, ninawaambia, hivi ndivyo Baba ameniamuru—kwamba niwape hawa watu hii nchi kwa urithi wao.

17 Na ndipo [a]maneno ya nabii Isaya yatatimizwa, ambayo yanasema:

18 [a]Walinzi [b]wenu watapaza sauti; na pamoja na sauti wataimba, kwani wataonana macho kwa macho wakati Bwana atakaporejesha tena Sayuni.

19 Pigeni kelele za shangwe, imbeni pamoja, enyi mahali pa Yerusalemu palipokuwa ukiwa; kwani Bwana amewafariji watu wake, ameikomboa Yerusalemu.

20 Bwana ameweka wazi mkono wake mtakatifu machoni mwa mataifa yote; na nchi zote za dunia zitaona wokovu wa Mungu.

MLANGO WA 17

Yesu anawaelekeza watu kutafakari maneno Yake na kuombea

10 *a* Morm. 8:35–41.
b 2 Ne. 26:29.
11 *a* 3 Ne. 21:1–11; Morm. 5:20.
12 *a* Hel. 15:12–13.
13 *a* Gal. 3:7, 29; 1 Ne. 15:13–17; 2 Ne. 10:18; 3 Ne. 30:2; Ibr. 2:9–11.
15 *a* Mik. 5:8–15; 3 Ne. 20:16–19; 21:12–21; M&M 87:5.
17 *a* 3 Ne. 20:11–12.
18 *a* Eze. 33:1–7. MWM Kesha, Walinzi.
b Isa. 52:8–10.

ufahamu—Anaponya wagonjwa wao—Anawaombea watu, akitumia lugha ambayo haiwezi kuandikwa—Malaika wanawahudumia na moto unawazingira watoto wao wadogo. Karibia mwaka 34 B.K.

Tazama, sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kuzungumza maneno haya alitazama tena kwa umati, na akasema kwao: Tazama, [a]muda wangu umewadia.

2 Ninahisi kwamba ninyi ni wadhaifu, kwamba hamwezi [a]kufahamu maneno yangu yote ambayo nimeamrishwa na Baba kuwazungumzia wakati huu.

3 Kwa hivyo, nendeni nyumbani kwenu, na [a]mfikirie vitu ambavyo nimesema, na mwulize kutoka kwa Baba, katika jina langu, ili muweze kufahamu, na [b]kutayarisha akili zenu kwa [c]kesho, na nitakuja kwenu tena.

4 Lakini sasa [a]ninaenda kwa Baba, na pia [b]kujidhihirisha kwa [c]makabila yaliyopotea ya Israeli, kwani hawajapotea kwa Baba, kwani anajua mahali ambapo aliwapeleka.

5 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kusema hivyo, alielekeza macho yake tena kwa umati, na akaona kuwa wanalia, na walikuwa wanamwangalia kwa uthabiti kama wanaotaka kumwomba akae nao kwa muda mrefu zaidi.

6 Na akawaambia: Tazama, matumbo yangu yamejawa na [a]huruma juu yenu.

7 Mnao wowote ambao ni wagonjwa miongoni mwenu? Waleteni hapa. Mnao wowote ambao ni viwete, au vipofu, au wa kupooza, au vilema, au ukoma, au walionyauka au ni viziwi, au ambao wanateseka kwa njia yoyote? Waleteni hapa na nitawaponya, kwani ninayo huruma juu yenu; matumbo yangu yamejaa na huruma.

8 Kwani ninaona kwamba mnataka kwamba niwaonyeshe kile ambacho nilifanya kwa ndugu zenu wa Yerusalemu, kwani naona kwamba [a]imani yenu ni ya [b]kutosha kwamba ningewaponya.

9 Na ikawa kwamba wakati alipokuwa amesema hivyo, umati wote, kwa lengo moja, ulisonga mbele na wagonjwa wao na waliosumbuka wao, na vilema wao, na vipofu wao, na bubu wao, na wote waliosumbuka kwa jinsi yoyote; na [a]akawaponya kila mmoja vile waliletwa kwake.

10 Na wote, ambao walikuwa wameponywa, na wale ambao walikuwa wazima, waliinama chini miguuni mwake, na kumwabudu; na kadiri wengi walivyoweza walikuja kutoka miongoni mwa umati [a]walibusu miguu yake, mpaka kwamba

17 1*a* MY kumrudia Baba. Tazama aya ya 4.
2*a* Yn. 16:12; M&M 78:17–18.
3*a* MWM Tafakari.
b M&M 132:3.
c 3 Ne. 19:2.
4*a* 3 Ne. 18:39.
b 3 Ne. 16:1–3.
c MWM Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea.
6*a* MWM Huruma.
8*a* Lk. 18:42.
b 2 Ne. 27:23; Eth. 12:12.
9*a* Mos. 3:5; 3 Ne. 26:15.
10*a* Lk. 7:38.

waliosha miguu yake na machozi yao.

11 Na ikawa kwamba aliamuru kwamba [a]watoto wao wachanga waletwe.

12 Kwa hivyo walileta watoto wao wachanga na kuwapanga chini juu ya ardhi kumzunguka, na Yesu alisimama katikati; na umati ulitoa nafasi mpaka wote walipoletwa kwake.

13 Na ikawa kwamba baada ya wote kuletwa, na Yesu kusimama katikati, aliamuru umati kwamba wapige [a]magoti chini.

14 Na ikawa kwamba baada ya hao kupiga magoti chini, Yesu alisononeka moyoni mwake, na kusema: Baba, [a]ninasumbuliwa kwa sababu ya uovu wa nyumba ya Israeli.

15 Na baada ya kusema maneno haya, yeye mwenyewe pia alipiga magoti ardhini; na tazama aliomba kwa Baba, na vitu ambavyo aliomba haviwezi kuandikwa, na umati uliomsikiliza ulishuhudia.

16 Na kwa maneno haya walishuhudia: [a]Jicho halijaona, wala sikio kusikia, hapo mbeleni, vitu vikubwa na vya ajabu vile tuliona na kusikia Yesu akisema kwa Baba;

17 Na hakuna [a]ulimi unaoweza kusema, wala haiwezi kuandikwa na mtu yeyote, wala mioyo ya watu haiwezi kufikiria vitu vikubwa na vya ajabu kama tulivyoona na kusikia Yesu akisema; na hakuna yeyote ambaye anaweza kuona shangwe iliyojaza nafsi zetu wakati tulipomsikia akituombea kwa Baba.

18 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kumaliza kuomba kwa Baba, aliinuka; lakini umati ulikuwa na [a]shangwe iliyokuwa kubwa sana kwamba walishindwa.

19 Na ikawa kwamba Yesu aliwazungumzia, na kuwaambia wasimame.

20 Na waliinuka kutoka ardhini, na akawaambia: Heri kwenu kwa sababu ya imani yenu. Na sasa tazama, shangwe yangu imetimia.

21 Na baada ya kusema maneno haya, [a]alilia, na umati ulishuhudia hii, na akachukua watoto wao wachanga, mmoja mmoja, na [b]kuwabariki, na kuomba kwa Baba juu yao.

22 Na baada ya kufanya hivi alilia tena;

23 Na alizungumza kwa umati, na kuwaambia: Tazama wachanga wenu.

24 Na walipotazama kuona walielekeza macho yao mbinguni, na wakaona mbingu zikifunguka, na wakaona malaika wakiteremka kutoka mbinguni kama wakiwa katikati ya moto; na walikuja chini na [a]kuzunguka wale wachanga, na walizungukwa na moto; na malaika waliwahudumia.

11 *a* Mt. 19:13–14; 3 Ne. 26:14, 16.
13 *a* Lk. 22:41; Mdo. 20:36.
14 *a* Musa 7:41.
16 *a* Isa. 64:4; 1 Kor. 2:9; M&M 76:10, 114–119.
17 *a* 2 Kor. 12:4.
18 *a* MWM Shangwe.
21 *a* Yn. 11:35.
b Mk. 10:14–16.
24 *a* Hel. 5:23–24, 43–45.

25 Na umati uliona na kusikia na wanashuhudia; na wanajua kwamba maandishi yao ni ya kweli kwani wote waliona na kusikia, kila mtu binafsi; na idadi yao ilikuwa karibu watu elfu mbili na mia tano; na walikuwa wanaume, wanawake, na watoto.

MLANGO WA 18

Yesu anaanzisha sakramenti miongoni mwa Wanefi—Wanaamriwa kuomba wakati wote katika jina Lake—Wale wanaokula mwili Wake na kunywa damu Yake bila kustahili wanalaaniwa—Wanafunzi wanapewa uwezo wa kutunukia Roho Mtakatifu. Karibia mwaka 34 B.K.

Na ikawa kwamba Yesu aliamuru wanafunzi kwamba walete [a]mkate na divai kwake.

2 Na walipokuwa wameenda kuleta mkate na divai, aliamuru umati kwamba ukae ardhini.

3 Na baada ya wanafunzi kurejea na [a]mkate na divai, alichukua mkate na kuumega kwa vipande na kuutakasa; na akawapatia wanafunzi na kuwaamuru kwamba wale.

4 Na baada ya kula na kushiba, aliwaamuru kwamba watoe kwa umati.

5 Na baada ya umati kula na kushiba, aliwaambia wanafunzi: Tazama kutakuwa na mmoja atakayetawazwa miongoni mwenu, na kwake nitatolea uwezo kwamba [a]atamega mkate na kuubariki na kuwapatia watu wa kanisa langu, kwa wote ambao wataamini na kubatizwa katika jina langu.

6 Na hii mtakumbuka kufanya daima, hata vile nimefanya, hata vile nimemega mkate na kuubariki na kuwapatia.

7 Na hii mtafanya kwa [a]ukumbusho wa mwili wangu, ambao nimewaonesha. Na itakuwa ushuhuda kwa Baba kwamba daima mnanikumbuka. Na ikiwa mtanikumbuka daima Roho yangu itakuwa na ninyi.

8 Na ikawa kwamba baada ya kusema maneno haya, aliwaamuru wanafunzi wake kwamba wachukue divai ndani ya kikombe na wainywe, na kwamba wawapatie umati ili wanywe.

9 Na ikawa kwamba walifanya hivyo, na wakainywa na kushiba; na kuupatia umati, na wakanywa, na wakashiba.

10 Na baada ya wanafunzi kufanya hivyo, Yesu aliwaambia: Mna heri kwa hiki kitu ambacho mmefanya, kwani hii ni kutimiza amri zangu, na hii inashuhudia kwa Baba kwamba mko tayari kufanya yale ambayo nimewaamuru.

11 Na daima mtafanya hivi kwa wale wanaotubu na kubatizwa katika jina langu; na mtafanya hivi kwa ukumbusho wa damu yangu, ambayo nilimwaga kwa ajili yenu, ili mshuhudie kwa Baba kwamba daima mnanikumbuka. Na

18 1*a* Mt. 26:26–28.
3*a* MWM Sakramenti.
5*a* Moro. 4.
7*a* Moro. 4:3.

ikiwa mnanikumbuka daima Roho yangu itukuwa na ninyi.

12 Na ninawapatia amri kwamba mtafanya hivi vitu. Na ikiwa mtafanya hivi vitu daima mna baraka, kwani mmejengwa juu ya [a]mwamba wangu.

13 Lakini yeyote miongoni mwenu ambaye atafanya zaidi au ndogo kuliko haya hajajengwa juu ya mwamba wangu, lakini wamejengwa kwenye msingi wa mchanga; na wakati mvua inateremka, na mafuriko kuja, na pepo kuvuma, na kujipigisha juu yao, [a]wataanguka, na [b]milango ya jehanamu iko tayari kuwapokea.

14 Kwa hivyo mnabaraka ninyi kama mtatii amri zangu, ambazo Baba ameniamuru kwamba nitoe kwenu.

15 Kweli, kweli, ninawaambia, lazima mjihadhari na [a]kuomba siku zote, msije mkajaribiwa na ibilisi, na mwongozwe mbali kama mateka wake.

16 Na kama vile nimeomba miongoni mwenu, basi nanyi muombe hivyo katika kanisa langu, miongoni mwa watu wangu wanaotubu na kubatizwa katika jina langu. Tazama, mimi ndimi [a]nuru; nimewapatia [b]mfano.

17 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kuzungumza maneno haya kwa wanafunzi wake, aliugeukia tena umati na kuwaambia:

18 Tazama, kweli, kweli, nawaambia: lazima mjihadhari na kusali siku zote, msije mkaingia majaribuni; kwani [a]Shetani amewataka ninyi, ili apate kuwapepeta kama vile ngano.

19 Kwa hivyo lazima msali siku zote kwa Baba katika jina langu;

20 Na [a]chochote mtakachomwomba Baba katika jina langu, ambacho ni haki, mkiamini kwamba mtapata, tazama, kitapewa kwenu.

21 [a]Ombeni katika ukoo wenu kwa Baba, daima katika jina langu, kwamba wake zenu na watoto wenu wabarikiwe.

22 Na tazama mtakutana pamoja mara kwa mara; na hamtamzuia mtu yeyote kuja kwenu wakati mnakutana pamoja, lakini wakubalie kwamba waje kwenu na msiwazuie;

23 Lakini [a]mtawaombea, na hamtawatupa nje; na ikiwa kwamba watakuja kwenu mara kwa mara, mtawaombea kwa Baba, katika jina langu.

24 Kwa hivyo, inueni juu [a]nuru yenu kwamba iangaze juu ya dunia. Tazama mimi ni [b]mwangaza ambao mtainua—kwamba mfanye yale ambayo mmeniona nikifanya. Tazama mnaona kwamba nimeomba kwa Baba, na nyote mmeshuhudia.

25 Na mnaona kwamba

12 *a* MWM Mwamba.
13 *a* MWM Ukengeufu.
b 3 Ne. 11:39.
15 *a* Alma 34:17–27.
MWM Sala.
16 *a* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
b MWM Yesu Kristo—Mfano wa Yesu Kristo.
18 *a* Lk. 22:31; 2 Ne. 2:17–18; M&M 10:22–27.
20 *a* Mt. 21:22; Hel. 10:5; Moro. 7:26; M&M 88:63–65.
21 *a* Alma 34:21.
23 *a* 3 Ne. 18:30.
24 *a* Mt. 5:16.
b Mos. 16:9.

nimeamuru kwamba yeyote miongoni mwenu [a]asiende, lakini nimeamuru kwamba mje kwangu, kwamba [b]mngenipapasa na kuniona; hata hivyo mtafanya kwa ulimwengu; na yeyote anayeasi hii amri anakubali mwenyewe kuongozwa majaribuni.

26 Na sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kusema maneno haya, aligeuza macho yake tena kuwaelekea wanafunzi ambao alikuwa amewachagua, na kuwaambia:

27 Tazameni kweli, kweli, ninawaambia, ninawapa amri ingine, na ndipo niteanda kwa [a]Baba yangu ili nitimize amri [b]zingine ambazo amenipatia.

28 Na sasa tazama, hii ndiyo amri ninayowapatia, kwamba msikubali yeyote [a]kuonja mwili wangu na damu [b]bila kustahili, wakati mtahudumu;

29 Kwani yeyote alaye na anywaye mwili wangu na [a]damu [b]asipostahili hula na kunywa lawama kwa nafsi yake; kwa hivyo kama mnajua kwamba mtu hastahili kula na kunywa mwili wangu na damu, mtamzuia.

30 Walakini, [a]hamtamtupa nje kutoka miongoni mwenu, lakini mtamhudumia na mtamwombea kwa Baba, katika jina langu; na ikiwa kwamba atatubu na kubatizwa katika jina langu, ndipo mtampokea, na mtamhudumia mwili wangu na damu yangu.

31 Lakini asipotubu hatahesabiwa miongoni mwa watu [a]wangu, ili asiharibu watu wangu, kwani tazama najua kondoo wangu, na wamehesabiwa.

32 Walakini, hamtamtupa nje ya masinagogi yenu, au mahali penu pa kuabudu, kwani kwa hawa mtaendelea kuwahudumia; kwani hamjui kama watarudi na kutubu, na kuja kwangu kwa moyo wa lengo moja, na [a]nitawaponya; na ndipo mtakuwa njia ya kuwaletea wokovu.

33 Kwa hivyo, tii maneno haya ambayo nimewaamuru kwamba msije mkawa chini ya [a]hukumu; kwani ole kwa yule ambaye Baba anamhukumu.

34 Na ninawapatia amri hizi kwa sababu ya ugomvi ambao umekuwa miongoni mwenu. Na heri ninyi kama [a]hamna ugomvi miongoni mwenu.

35 Na sasa nitaenda kwa Baba, kwa sababu ni muhimu kwamba niende kwa Baba [a]kwa ajili yenu.

36 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kumaliza maneno haya, [a]aliwagusa [b]wanafunzi

25 *a* Alma 5:33.
b 3 Ne. 11:14–17.
27 *a* MWM Mungu, Uungu—Mungu Baba.
b 3 Ne. 16:1–3.
28 *a* 1 Kor. 11:27–30.
b Morm. 9:29.
29 *a* MWM Damu; Sakramenti.
b M&M 46:4.
30 *a* M&M 46:3.
31 *a* Yn. 10:14; Alma 5:38; 3 Ne. 15:24.
32 *a* 3 Ne. 9:13–14; M&M 112:13.
33 *a* MWM Shutuma, Shutumu.
34 *a* 3 Ne. 11:28–30.
35 *a* 1 Yoh. 2:1; 2 Ne. 2:9; Moro. 7:27–28; M&M 29:5.
36 *a* MWM Mikono, Kuweka juu ya.
b 1 Ne. 12:7; 3 Ne. 19:4.

ambao alikuwa amewachagua kwa mkono wake mmoja mmoja mpaka alipowagusa wote, na aliwazungumzia akiwagusa.

37 Na umati haukusikia maneno ambayo alisema, kwa hivyo hawakushuhudia; lakini wanafunzi wanashuhudia kwamba aliwapatia [a]uwezo kutoa [b]Roho Mtakatifu. Na nitawaonyesha baadaye kwamba huu ushahidi ni wa kweli.

38 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kuwagusa wote, kulitokea [a]wingu na likafunika umati kwamba haungemwona Yesu.

39 Na wakati walipokuwa wamefunikwa aliondoka kutoka kwao, na kupaa mbinguni. Na wanafunzi waliona na wanashudia kwamba alipaa tena mbinguni.

MLANGO WA 19

Wale wanafunzi kumi na wawili wanawahudumia watu na wanaomba wapokee Roho Mtakalifu—Wanafunzi wanabatizwa na kupokea Roho Mtakatifu na kuhudumu kama malaika—Yesu anaomba akitumia maneno ambayo hayawezi kuandikwa—Anashuhudia imani kuu ya hawa Wanefi. Karibia mwaka 34 B.K.

Na sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kupaa mbinguni, umati ulitawanyika, na kila mtu alimchukua mke wake na watoto wake na kurejea nyumbani kwake.

2 Na uvumi ulienda nje miongoni mwa watu mara moja, kabla ya giza kushika, kwamba ule umati ulikuwa umemwona Yesu, na kwamba alikuwa amewahudumia, na kwamba pia atajidhihirisha kwao kesho.

3 Ndiyo, na hata usiku kucha ukavumishwa kuhusu Yesu; na kwa ukamilifu mwingi walisambaza kwa watu kwamba kulikuwa na wengi, ndiyo, idadi kubwa sana ilitembea sana usiku, ili wawe mahali ambapo Yesu atajionyesha mwenyewe kwa umati.

4 Na ikawa kwamba kesho yake baada ya umati kukusanyika pamoja, tazama Nefi na kaka yake ambaye alikuwa amefufuliwa kutoka kwa wafu, ambaye jina lilikuwa Timotheo, na pia mwana wake ambaye jina lake lilikuwa Yona, na pia Mathoni, na Mathoniha, kaka yake, na Kumeni, na Kumenonhi, na Yeremia, na Shemnoni, na Yona, na Zedekia, na Isaya—Sasa haya yalikuwa majina ya wanafunzi ambao Yesu alikuwa amewachagua—na ikawa kwamba walienda mbele na kusimama katikati ya umati.

5 Na tazama, umati ulikuwa mkubwa sana kwamba ulisababisha kwamba ugawanywe kwenye vikundi kumi na viwili.

6 Na wale kumi na wawili walifundisha umati; na tazama, walisababisha kwamba umati upige magoti chini juu ya ardhi, na waombe kwa Baba katika jina la Yesu.

37 *a* MWM Uwezo.
b MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
38 *a* Ku. 19:9, 16.

7 Na wanafunzi pia waliomba kwa Baba pia katika jina la Yesu. Na ikawa kwamba waliinuka na kuwahudumia watu.

8 Na baada ya kufundisha maneno yale yale ambayo Yesu alizungumza—bila tofauti yoyote na yale Yesu aliyazungumza—tazama, walipiga magoti tena na kuomba kwa Baba katika jina la Yesu.

9 Na waliomba wapate kile ambacho walitaka zaidi; na walitaka kwamba [a]Roho Mtakatifu apewe kwao.

10 Na baada ya kuomba hivyo, walienda chini kwenye ukingo wa maji, na umati ukawafuata.

11 Na ikawa kwamba Nefi alienda chini [a]ndani ya maji na akabatizwa.

12 Na alitoka nje kutoka ndani ya maji na kuanza kubatiza. Na alibatiza wale wote ambao Yesu aliwachagua.

13 Na ikawa baada ya wote [a]kubatizwa na kutoka nje ya maji, [b]Roho Mtakatifu aliteremka kwao, na walijazwa na Roho Mtakatifu na moto.

14 Na tazama, walionekana kama [a]waliozingirwa na moto; na ulikuja chini kutoka mbinguni, na umati ulishuhudia, na kutoa ushahidi; na malaika walikuja chini kutoka mbinguni na kuwahudumia.

15 Na ikawa kwamba malaika walipokuwa wanawahudumia wanafunzi, tazama, Yesu alikuja na kusimama miongoni mwao na kuwahudumia.

16 Na ikawa kwamba alizungumza kwa umati, na kuwaamuru kwamba wapige magoti chini ardhini tena, na pia kwamba wanafunzi wake wapige magoti chini ardhini.

17 Na ikawa kwamba walipopiga magoti chini, aliwaamuru wanafunzi wake waombe.

18 Na tazama, walianza kuomba; na waliomba kwa Yesu, wakimwita Bwana wao na Mungu wao.

19 Na ikawa kwamba Yesu aliondoka miongoni mwao, na kwenda pembeni kidogo kutoka kwao na kujiinamisha mwenyewe na kusema:

20 Baba, ninakushukuru kwamba umewapatia hawa watu ambao nimewachagua Roho Mtakatifu; na ni kwa sababu ya imani yao kwangu, kwamba nimewachagua kutoka miongoni mwa watu wa dunia.

21 Baba, nakuomba kwamba utawapatia Roho Mtakatifu wote ambao wataamini kwa maneno yao.

22 Baba, umewapatia Roho Mtakatifu kwa sababu wanaamini ndani yangu; na unaona kwamba wanaamini kwangu kwa sababu unawasikia, na wanaomba kwangu; na wanaomba kwangu kwa sababu niko nao.

23 Na sasa Baba, ninaomba kwako kwa ajili yao, na pia wale wote ambao wataamini maneno yao, kwamba wangeamini ndani yangu, ili niwe ndani yao

19 9*a* 3 Ne. 9:20.
11*a* 3 Ne. 11:23.
13*a* MWM Batiza, Ubatizo.
b 3 Ne. 12:2; Morm. 7:10. MWM Kipawa cha Roho Mtakatifu.
14*a* Hel. 5:23–24, 43–45; 3 Ne. 17:24.

[a]kama vile wewe ulivyo, Baba, ndani yangu, ili tuwe kitu [b]kimoja.

24 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kuomba hivyo kwa Baba, aliwajia wanafunzi wake, na tazama, walikuwa bado wanaendelea, bila kukoma, kuomba kwake; na [a]hawakuzidisha maneno, kwani walipewa yale ambayo [b]wangeomba, na utashi uliwajaa.

25 Na ikawa kwamba Yesu aliwabariki wakati walipokuwa wanaomba kwake; alikunjua uso kwao, na nuru ya [a]uso wake iling'aa kwao, na tazama, walikuwa [b]weupe kama uso na pia nguo ya Yesu; na tazama, weupe wake ulizidi weupe wote, ndiyo, hata hakungekuwa na kitu duniani cheupe kama weupe wake.

26 Na Yesu akasema kwao: Endeleeni kuomba; walakini, hawakukoma kuomba.

27 Na akageuka kutoka kwao tena, na akaenda kando kidogo na akainama mwenyewe ardhini; na akaomba tena kwa Baba, akisema:

28 Baba, ninakushukuru kwamba [a]umewatakasa wale ambao nimewachagua, kwa sababu ya imani yao, na ninawaombea, na pia wale ambao wataamini kwa yale wanayosema, ili watakaswe kupitia kwangu, kwa imani katika maneno yao, kama vile wanatakaswa ndani yangu.

29 Baba siombei dunia, lakini wale ambao umenipatia [a]kutoka duniani, kwa sababu ya imani yao, kwamba wangetakaswa kupitia kwangu, kwamba niwe ndani yao vile wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, ili tuwe kitu kimoja, kwamba nipate kutukuzwa ndani yao.

30 Na baada ya Yesu kusema maneno haya, alirudi tena kwa wanafunzi wake; na tazama waliomba kwa uthabiti, bila kukoma, kwake; na akakunjua uso kwao tena; na tazama, walikuwa [a]weupe, hata kama Yesu.

31 Na ikawa kwamba alienda tena kando kidogo na kuomba kwa Baba;

32 Na ulimi hauwezi kusema yale maneno ambayo aliomba wala hayawezi [a]kuandikwa na mwanadamu maneno ambayo aliomba.

33 Na umati ulisikia na walitoa ushuhuda; na mioyo yao ilifunguka na walisikia katika mioyo yao, maneno ambayo aliomba.

34 Walakini, maneno aliyoyatumia kwa kuomba yalikuwa makubwa sana na ya ajabu, kwamba hayawezi kuandikwa, wala [a]kuongelewa na mtu.

35 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kumaliza kuomba alirudi tena kwa wanafunzi, na

23 *a* 3 Ne. 9:15.
b Yn. 17:21–23.
MWM Umoja.
24 *a* Mt. 6:7.
b M&M 46:30.
25 *a* Hes. 6:23–27.
b MWM Kugeuka sura—Viumbe Waliogeuka Sura.
28 *a* Moro. 7:48; M&M 50:28–29; 88:74–75.
MWM Safi na Isiyo safi.
29 *a* Yn. 17:6.
30 *a* Mt. 17:2.
32 *a* M&M 76:116.
34 *a* 2 Kor. 12:4; 3 Ne. 17:17.

kuwaambia: Sijaona [a]imani kubwa kama hii miongoni mwa Wayahudi; kwa hivyo, sikuonyesha miujiza mikubwa kwa sababu ya [b]kutoamini kwao.

36 Kweli, ninawaambia, hakuna mmoja wao ambaye ameona vitu vikubwa sana kama vile ninyi wala hawajasikia vitu vikubwa kama vile mmesikia.

MLANGO WA 20

Yesu anatoa mkate na divai kwa miujiza na tena anatoa sakramenti kwa watu—Baki la Yakobo watakuja kujua Bwana Mungu wao na kurithi bara za Marekani—Yesu ni yule nabii kama Musa, na Wanefi ni watoto wa manabii—Watu wengine wa Bwana watakusanywa Yerusalemu. Karibia mwaka 34 B.K.

Na ikawa kwamba aliamuru umati kwamba wakome kusali na pia wanafunzi wake. Na akawaamuru kwamba wasikome [a]kusali kwenye mioyo yao.

2 Na akawaamuru kwamba wainuke na wasimame kwa miguu yao. Na waliinuka na kusimama kwa miguu yao.

3 Na ikawa kwamba alimega mkate tena na kuubariki, na kuwapa wanafunzi waule.

4 Na baada ya wao kula, aliwaamuru wamege mkate na kuwapatia umati.

5 Na baada ya wao kuwapatia umati, aliwapa divai pia kunywa na kuwaamuru kuwapatia umati.

6 Sasa hapakuweko na [a]mkate wala divai iliyoletwa na wanafunzi, wala na umati.

7 Lakini kwa kweli [a]aliwapatia mkate wale, na pia divai wanywe.

8 Na akawaambia: Yule ambaye [a]anaula huu mkate anakula mwili wangu kwa nafsi yake; na yule ainywaye hii divai, anakunywa damu yangu kwa nafsi yake; na nafsi yake haitaona njaa wala kiu, lakini itajazwa.

9 Sasa baada ya umati kunywa na kula, tazama, walijazwa na Roho; na walipiga yowe kwa sauti moja, na kumtukuza Yesu, ambaye walimwona na kumsikiza.

10 Na ikawa kwamba wakati wote walikuwa wamemtukuza Yesu, aliwaambia: Tazama sasa ninamaliza amri ambayo Baba aliniamuru kuhusu watu hawa, ambao ni baki la nyumba ya Israeli.

11 Mnakumbuka kwamba niliwazungumzia, na kusema kwamba wakati [a]maneno ya [b]Isaya yangetimizwa—tazama, yameandikwa, mnayo mbele yenu, kwa hivyo myachunguze—

12 Na kweli, kweli, ninasema kwenu; kwamba wakati yatakavyotimizwa ndipo kutatimizwa [a]agano ambalo Baba alifanya

35 *a* MWM Amini, Imani.
b Mt. 13:58.
MWM Kutoamini.
20 1 *a* 2 Ne. 32:9; Mos. 24:12.
6 *a* Mt. 14:19–21.
7 *a* Yn. 6:9–14.
8 *a* Yn. 6:50–58; 3 Ne. 18:7.
MWM Sakramenti.
11 *a* 3 Ne. 16:17–20; 23:1–3.
b 2 Ne. 25:1–5; Morm. 8:23.
12 *a* 3 Ne. 15:7–8.

na watu wake Ee nyumba ya Israeli.

13 Na ndipo [a]mabaki ambayo [b]yatatawanywa juu ya dunia, [c]yatakusanywa ndani kutoka mashariki na kutoka magharibi, na kutoka kusini na kutoka kaskazini; na wataletwa kwa [d]ufahamu wa Bwana Mungu wao, ambaye amewakomboa.

14 Na Baba ameniamuru kwamba niwapatie hii [a]nchi kwa urithi wenu.

15 Na ninawaambia kwamba kama Wayunani [a]hawatatubu baada ya baraka ambazo watapata, baada ya wao kutawanya watu wangu—

16 Ndipo ninyi ambao ni baki la nyumba ya Yakobo, mtaenda miongoni mwao; na mtakuwa miongoni mwao ambao ni wengi; na mtakuwa miongoni mwao kama simba miongoni mwa wanyama wa msitu, na kama mwana [a]simba miongoni mwa makundi ya kondoo, ambaye, ikiwa atapitia miongoni mwao [b]atawakanyagia chini na kuwararua katika vipande vipande na hakuna atakayewaokoa.

17 Mikono yenu itainuliwa dhidi ya maadui wenu, na maadui wenu wote watakatiliwa mbali.

18 Na [a]nitakusanya watu wangu vile mtu hukusanya miganda sakafuni.

19 Kwani nitachagua watu wangu ambao Baba amefanya agano nao, ndiyo, nifanye pembe yako kuwa chuma, na [a]kwato zako kuwa shaba nyeupe. Na utaponda kwenye vipande vipande watu wengi; na nitaweka wakfu faida yako kwa Bwana, na mali zao kwa Bwana wa dunia yote. Na tazama mimi ndimi, nitaifanya.

20 Na itakuwa, asema Baba, kwamba [a]upanga wa haki yangu utaning'inia juu yao siku ile; na wasipotubu, utawaangukia, anasema Baba, ndiyo, hata kwa mataifa yote ya Wayunani.

21 Na itakuwa kwamba nitaimarisha [a]watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.

22 Na tazama, hawa watu nitawaimarisha katika nchi hii, kwa kutimiza [a]agano ambalo nilifanya na babu yenu Yakobo; na itakuwa [b]Yerusalemu Mpya. Na uwezo wa mbinguni utakuwa katikati ya hawa watu; ndiyo, hata [c]mimi nitakuwa katikati yenu.

23 Tazama, ni mimi ambaye Musa alimzungumzia akisema: Bwana Mungu wenu atainua [a]nabii huyo kutoka miongoni

13*a* 3 Ne. 16:11–12; 21:2–7.
b MWM Israeli—Kutawanyika kwa Israeli.
c MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
d 3 Ne. 16:4–5.
14*a* MWM Nchi ya Ahadi.
15*a* 3 Ne. 16:10–14.
16*a* Morm. 5:24; M&M 19:27.
b Mik. 5:8–9; 3 Ne. 16:14–15; 21:12.
18*a* Mik. 4:12.
19*a* Mik. 4:13.
20*a* 3 Ne. 29:4.
21*a* 3 Ne. 16:8–15.
22*a* Mwa. 49:22–26; M&M 57:2–3.
b Isa. 2:2–5; 3 Ne. 21:23–24; Eth. 13:1–12; M&M 84:2–4. MWM Yerusalemu Mpya.
c Isa. 59:20–21; Mal. 3:1; 3 Ne. 24:1.
23*a* Kum. 18:15–19; Mdo. 3:22–23; 1 Ne. 22:20–21.

mwa ndugu zenu kama mimi; yeye ndiye mtamsikiliza kwa vitu vyote atakavyowaambia. Na itakuwa kwamba kila nafsi ambayo haitamsikiliza nabii itakatiwa mbali kutoka miongoni mwa watu.

24 Kweli, nawaambia, ndiyo, na manabii [a]wote kutokea Samweli na wale ambao wanafuata baadaye, kadiri vile wengi wamezungumza, wamenishuhudia.

25 Na tazama, ninyi ni watoto wa manabii; na ninyi ni wa nyumba ya Israeli; na ni wa [a]agano ambalo Baba alifanya na babu zenu akisema kwa Ibrahimu: Na [b]kupitia uzao wako, makabila yote ya dunia yatabarikiwa.

26 Baba alinitayarisha mimi kwanza, na kunituma niwabariki ninyi kwa [a]kugeuza kila mmoja wenu kutoka kwa uovu wake; na hivyo ni kwa sababu ninyi ni watoto wa agano—

27 Na baada ya hivyo mlibarikiwa ndipo kutimiza agano ambalo Baba alifanya na Ibrahimu, akisema: [a]Katika uzao wako, makabila yote ya dunia itabarikiwa—kwa njia ya kumwaga nje Roho Mtakatifu kupitia kwangu juu ya [b]Wayunani, baraka ambazo kwa Wayunani, zitawafanya kuwa na nguvu kuliko wote, kwa kutawanya watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.

28 Na watakuwa [a]mjeledi kwa watu wa nchi hii. Walakini, baada ya hao kupata utimilifu wa injili yangu, hapo ikiwa watashupaza mioyo yao dhidi yangu, nitarudishia uovu wao juu ya vichwa vyao, anasema Baba.

29 Na [a]nitakumbuka agano ambalo nimefanya na watu wangu; na nimeagana nao kwamba [b]nitawakusanya pamoja, katika wakati wangu mwenyewe, kwamba ningewapa tena [c]nchi ya babu zao kwa urithi, ambayo ni nchi ya [d]Yerusalemu, ambayo ni nchi ya ahadi kwao milele, anasema Baba.

30 Na itakuwa kwamba wakati utakuja ambapo utimilifu wa injili yangu utahubiriwa kwao;

31 Na [a]wataamini ndani yangu, kwamba mimi ni Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, na kuomba kwa Baba katika jina langu.

32 Ndipo [a]walinzi wao watapaza sauti zao, na kwa sauti, pamoja wataimba; kwani wataonana jicho kwa jicho.

33 Ndipo Baba atawakusanya pamoja tena na kuwapatia Yerusalemu kuwa nchi ya urithi wao.

34 Ndipo watapiga kelele za shangwe—[a]Imbeni pamoja enyi

24 *a* Mdo. 3:24–26; 1 Ne. 10:5; Yak. (KM) 7:11.
25 *a* MWM Agano la Ibrahimu.
b Mwa. 12:1–3; 22:18.
26 *a* Mit. 16:6.
27 *a* Gal. 3:8; 2 Ne. 29:14; Ibr. 2:9.
b 3 Ne. 16:6–7.
28 *a* 3 Ne. 16:8–9.
29 *a* Isa. 44:21; 3 Ne. 16:11–12.
b MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
c Amo. 9:14–15.
d MWM Yerusalemu.
31 *a* 3 Ne. 5:21–26; 21:26–29.
32 *a* Isa. 52:8; 3 Ne. 16:18–20. MWM Kesha, Walinzi.
34 *a* Isa. 52:9.

mahali pa Yerusalemu palipo na ukiwa; kwani Baba amefariji watu wake, na ameikomboa Yerusalemu.

35 Baba amefanya mkono wake mtakatifu wazi katika macho ya mataifa yote; na nchi zote za dunia zitauona wokovu wa Baba; na Baba na Mimi tu wamoja.

36 Na ndipo itakuja kutimia ile ambayo iliandikwa: [a]Amka, amka tena, na jivike nguvu yako, Ee Sayuni; jivike mavazi yako mazuri, Ee Yerusalemu, mji mtakatifu, kwani kutokea sasa hawataingia ndani yako, wasiotahiriwa na wasio safi.

37 Jikung'ute mavumbi; inuka uketi chini, Ee Yerusalemu, jifungulie kandaza za shingo, Ee binti mfungwa wa Sayuni.

38 Kwani hivyo ndivyo asemavyo Bwana; Mmejiuza bure, na mtakombolewa bila fedha.

39 Kweli, kweli, nawaambia, kwamba watu wangu watajua jina langu; ndiyo, katika siku hiyo watajua kwamba ni Mimi ndiye husema.

40 Na hapo watasema: [a]Jinsi ilivyo mizuri juu ya milima, miguu yake, aletaye habari njema kwao, yeye [b]atangazaye amani; aletaye habari njema ya mambo mema kwao, yeye atangazaye wokovu, aiambiaye Sayuni: Mungu wako anatawala!

41 Na hapo mlio utatokea: [a]Nendeni ninyi, nendeni ninyi, tokeni hapo, msiguse kile ambacho ni [b]kichafu; tokeni kati yake, muwe [c]safi ninyi mnaochukua vyombo vya Bwana.

42 Kwani [a]hamtatoka kwa haraka wala hamtakwenda kwa kukimbia; kwa sababu Bwana atawatangulia, na Mungu wa Israeli atakuwa nyuma yenu kuwalinda.

43 Tazama mtumishi wangu atatenda kwa busara; atatukuzwa na kuinuliwa juu, na kuwa juu sana.

44 Na vile wengi walistaajabu—uso wake ulikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote, na umbo lake zaidi ya wana wa watu—

45 Ndivyo [a]atakavyowanyunyizia mataifa mengi; wafalme watamfungia vinywa vyao, kwani maneno ambayo hawakuambiwa watayaona; na yale ambayo hawakusikia watayafahamu.

46 Kweli, kweli, ninawaambia, hivi vitu vyote vitafanyika, hata vile Baba ameniamrisha. Ndipo hili agano ambalo Baba ameagana na watu wake litatimizwa; na hapo [a]Yerusalemu itakaliwa tena na watu wangu, na itakuwa nchi yao ya urithi.

MLANGO WA 21

Israeli itakusanywa wakati kitabu cha Mormoni kinabainishwa—Wayunani wataimarishwa kama

36*a* Isa. 52:1–3; M&M 113:7–10. MWM Sayuni.
40*a* Isa. 52:7; Nah. 1:15; Mos. 15:13–18; M&M 128:19.
b Mk. 13:10; 1 Ne. 13:37.
41*a* Isa. 52:11–15.
b MWM Safi na Isiyo safi.
c M&M 133:5.
42*a* 3 Ne. 21:29.
45*a* Isa. 52:15.
46*a* Eth. 13:5, 11.

watu huru katika Marekani—Watakombolewa ikiwa wataamini na kutii; la sivyo, watakataliwa mbali na kuangamizwa—Israeli itajenga Yerusalemu Mpya, na makabila yaliyopotea yatarejea. Karibia mwaka 34 B.K.

Na kweli, ninawaambia, ninawapatia ishara ili mjue [a]muda ambao vitu hivi vitakuwa karibu kufanyika—kwamba nitawakusanya ndani, baada ya kutawanyika kwa muda mrefu, watu wangu, Ee nyumba ya Israeli, na nitaanzisha tena miongoni mwao Sayuni yangu.

2 Na tazama, hiki ndicho kitu ambacho nitawapatia kwa ishara—kwa kweli, ninawaambia kwamba wakati hivi vitu ambavyo nimetangaza kwenu, na ambavyo nitawatangazia baadaye mwenyewe, na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu ambaye atatolewa kwenu na Baba, vitafanywa kujulikana kwa Wayunani ili wajue kuhusu hawa watu ambao ni baki la nyumba ya Yakobo, na kuhusu hawa watu wangu ambao watatenganishwa na hao;

3 Kweli, kweli, ninawaambia, baada ya [a]hivi vitu kujulikana kwao, kutoka kwa Baba, na vitatokea kutoka kwa Baba kupitia kwao hadi kwenu.

4 Kwani ni hekima katika Baba kwamba waimarishwe katika nchi hii, na wapangwe kama watu [a]huru kwa uwezo wa Baba, kwamba hivi vitu vingekuja mbele kutoka kwao hadi kwa baki la uzao wenu, kwamba [b]agano la Baba lingetimizwa ambalo ameagana na watu wake, Ee nyumba ya Israeli.

5 Kwa hivyo, baada ya vitu hivi na vitu ambavyo vitafanywa miongoni mwenu baada ya muda huu vitakuja [a]kutoka kwa Wayunani, hadi kwa [b]uzao wenu ambao utafifia katika kutoamini kwa sababu ya uovu;

6 Kwa hivyo ndivyo Baba amepanga kwamba ije kutokea kwa [a]Wayunani, kwamba angeonyesha mbele uwezo wake kwa Wayunani, kwa sababu hii kwamba Wayunani kama hawatashupaza mioyo yao, kwamba watubu na waje kwangu na wabatizwe katika jina langu na wajue habari kamili ya mafundisho yangu, ili [b]wahesabiwe miongoni mwa watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.

7 Na wakati vitu hivi vitakapokuja kutimizwa, kwamba [a]uzao wenu utaanza kujua vitu hivi—itakuwa ishara kwao, ili wajue kwamba kazi ya Baba imeanza kitambo kwa kutimizwa kwa agano ambalo amefanya kwa watu ambao ni wa nyumba ya Israeli.

8 Na wakati hiyo siku itakapo-

21 1*a* MWM Siku za Mwisho.
3*a* Eth. 4:17; JS—H 1:34–36.
4*a* 1 Ne. 13:17–19; M&M 101:77–80.
b Morm. 5:20.
MWM Agano la Ibrahimu.
5*a* 3 Ne. 26:8.
b 2 Ne. 30:4–5; Morm. 5:15; M&M 3:18–19.
6*a* 1 Ne. 10:14; Yak. (KM) 5:54; 3 Ne. 16:4–7.
b Gal. 3:7, 29; 3 Ne. 16:13; Ibr. 2:9–11.
7*a* 3 Ne. 5:21–26.

fika, itakuwa kwamba wafalme watafunga vinywa vyao; kwani yale ambayo hawajaambiwa watayaona; na yale ambayo hawajasikia watayafikiria.

9 Kwani katika siku hiyo, kwa ajili yangu, Baba atafanya kazi ambayo itakuwa kubwa na kazi ya [a]ajabu miongoni mwao; na kutakuwa miongoni mwao wale ambao hawataiamini ingawa mtu atawatangazia.

10 Lakini tazama maisha ya mtumishi wangu yatakuwa mkononi mwangu; kwa hivyo, hawatamdhuru, ingawa [a]ataumizwa kwa sababu yao. Bado nitamponya, kwani nitawaonyesha kwamba hekima [b]yangu inazidi werevu wa ibilisi.

11 Kwa hivyo itakuwa kwamba yeyote ambaye hataamini katika maneno yangu, mimi ambaye ni Yesu Kristo, ambaye Baba atamsababishia [a]yeye kuleta mbele kwa Wayunani, na atampatia uwezo kwamba atayaleta mbele kwa Wayunani, (itafanyika hata kama Musa alivyosema) [b]watatolewa kutoka miongoni mwa watu wangu ambao ni wa agano.

12 Na watu wangu ambao ni baki la Yakobo watakuwa miongoni mwa Wayunani, ndiyo, miongoni mwao kama [a]simba miongoni mwa wanyama wa msituni, kama mwana simba miongoni mwa makundi ya kondoo, ambaye akiwa anapita katikati, [b]hukanyagakanyaga na kuraruarara, kwa vipande vipande, na hakuna wa kuokoa.

13 Mkono wao utainuliwa juu ya maadui zao, na maadui wao wote watakatiliwa mbali.

14 Ndiyo, ole kwa Wayunani isipokuwa [a]wakitubu; kwani itakuwa kwamba katika siku hiyo, asema Baba, kwamba nitatilia mbali farasi wenu, kutoka miongoni mwenu, na nitaharibu magari yenu ya vita;

15 Na nitakatilia mbali miji ya nchi yenu, na nitaangusha ngome zenu zote;

16 Na nitakatilia mbali uchawi nje ya nchi yenu, na hamtakuwa tena na wapiga ramli;

17 Nitaziharibu [a]sanamu zenu, na nguzo zenu za ibada, na hamtaabudu tena kazi ya mikono yenu;

18 Na nitaving'oa vijisitu vyenu visiwe kati yenu; hivyo nitaangamiza miji yenu.

19 Na itakuwa kwamba [a]uwongo wote na udanganyifu, na wivu, na mashindano, na ukuhani wa uongo, na ukahaba utaondelewa.

20 Kwani itakuwa, anasema Baba, kwamba katika siku ile, wote ambao hawatatubu na kuja kwa Mwana wangu Mpendwa, hao nitawakatilia mbali kutoka miongoni mwa watu wangu, Ee nyumba ya Israeli.

9*a* Isa. 29:14; Matendo 13:41; 1 Ne. 22:8. MWM Urejesho wa Injili.
10*a* M&M 135:1–3.
b M&M 10:43.
11*a* 2 Ne. 3:6–15; Morm. 8:16, 25.
b M&M 1:14.
12*a* Mik. 5:8–15; 3 Ne. 20:16.
b 3 Ne. 16:13–15.
14*a* 2 Ne. 10:18; 33:9.
17*a* Ku. 20:3–4; Mos. 13:12–13; M&M 1:16. MWM Kuabudu sanamu.
19*a* 3 Ne. 30:2.

21 Na nitamaliza ghadhabu yangu kali na kisasi juu yao, hata kama kwa wale wasio na dini, kama vile ambayo hawajasikia.

22 Lakini ikiwa watatubu na kutii maneno yangu, na wasishupaze mioyo yao, [a]nitaimarisha kanisa langu miongoni mwao, na wataingia kwenye agano na [b]kuhesabiwa miongoni mwa hili baki la Yakobo, kwa hao ambao nimewapa nchi hii kwa urithi wao.

23 Na watawasaidia watu wangu, lile baki la Yakobo, na pia wengi wa nyumba ya Israeli kama watakuja ili waweze kujenga mji, ambao utaitwa [a]Yerusalemu Mpya.

24 Na ndipo watasaidia watu wangu ili waweze kukusanywa ndani, ambao wametawanyika kote juu ya nchi, ndani ya Yerusalemu Mpya.

25 Na ndipo [a]uwezo wa mbinguni utakuja chini miongoni mwao; na pia [b]nitakuwa katikati.

26 Na ndipo kazi ya Baba [a]itaanza katika siku ile, hata wakati ambapo injili itahubiriwa miongoni mwa baki la watu hawa. Kweli, nawaambia, katika siku ile, ndipo kazi ya Baba itaanza miongoni mwa watu wangu waliotawanywa, ndiyo, hata makabila ambayo [b]yamepotea, ambayo Baba ameyaongozea mbali kutoka nje ya Yerusalemu.

27 Ndiyo, kazi itaanza miongoni mwa wale wote wa watu wangu [a]waliotawanywa, na kwa Baba kutayarisha njia ambayo kwayo wangekuja kwangu, ili wamwite Baba katika jina langu.

28 Ndiyo, ndipo kazi itakapoanza, na Baba miongoni mwa mataifa yote katika kutayarisha njia ambayo kwayo watu wake [a]wangekusanywa nyumbani katika nchi yao ya urithi.

29 Na wataenda nje kutoka kwa mataifa yote; na hawataenda nje kwa [a]haraka, wala kwenda kwa kukimbia, kwani nitaenda mbele yao, asema Baba, na nitakuwa nyuma yao.

MLANGO WA 22

Katika siku za mwisho, Sayuni na vigingi vyake vitaimarishwa, na Israeli itakusanywa kwa huruma na wororo—Watafaulu—Linganisha Isaya 54. Karibia mwaka 34 B.K.

Na ndipo ile ambayo imeandikwa itatimizwa: Imba, ewe tasa; wewe usiyepata kujifungua mtoto; anza [a]kuimba na ulie kwa sauti, wewe ambaye hukujifungua mtoto; kwani wengi ni watoto wa tasa, kuliko watoto wa mke aliyeolewa, asema Bwana.

2 Panua mahali pa hema lako, na acha watandaze mapazia

22 *a* MWM Kipindi.
b 2 Ne. 10:18–19; 3 Ne. 16:13.
23 *a* 3 Ne. 20:22; Eth. 13:1–12. MWM Yerusalemu Mpya.
25 *a* 1 Ne. 13:37.
b Isa. 2:2–4; 3 Ne. 24:1.
26 *a* 1 Ne. 14:17; 3 Ne. 21:6–7.
b MWM Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea.
27 *a* 3 Ne. 16:4–5.
28 *a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
29 *a* Isa. 52:12; 3 Ne. 20:42.
22 1 *a* MWM Imba.

ya maskani yako; tumia nafasi yote, ongeza urefu wa kamba zako, na vikaze [a]vigingi vyako;

3 Kwani utaenea kwenye upande wa kulia na kwenye upande wa kushoto na uzao wako utawamiliki [a]Wayunani na kufanya miji ya ukiwa kumilikiwa.

4 Usiogope, kwani hutaaibika; wala kuteketezwa, kwani hutawekwa [a]aibu; kwani utasahau aibu ya ujana wako, na hutakumbuka aibu ya ujana wako, na hutaweza kukumbuka mashtumu ya ujane wako tena.

5 Kwani muumba wako, mume wako, Bwana wa Majeshi ndilo jina lake; na Mkombozi wako, Mtakatifu wa Israeli—ataitwa Mungu wa dunia yote.

6 Kwani Bwana amekuita kama mke aliyeachwa na kuhuzunishwa rohoni, na mke wa ujana, wakati ulikataliwa, asema Mungu wako.

7 Kwa muda mfupi nimekuacha, lakini kwa rehema nyingi nitakurejesha.

8 Kwa ghadhabu ndogo, nilificha uso wangu kutoka kwako kwa muda mfupi, lakini kwa wema usio na mwisho nitakuwa na [a]huruma kwako, asema Bwana Mkombozi wako.

9 Kwani jambo [a]hili limekuwa kama [b]maji ya Nuhu kwangu, kwani vile nilivyoapa kwamba maji ya Nuhu hayatafunika dunia tena, kadhalika nimeapa kwamba sitakuwa na hasira nawe.

10 Kwani [a]milima itaondoka, na vilima vitaondelewa, lakini wema wangu [b]hautaondoka kutoka kwako, wala agano langu la amani liondolewe, asema Bwana ambaye ana rehema nawe.

11 Ee uliyeteseka, uliyerushwa na tufani, bila kutulizwa! Tazama, nitaweka [a]mawe yako na rangi nzuri, na kuweka msingi wako na johari ya thamani.

12 Na nitafanya madirisha yako ya akiki, na milango yako ya kito nyekundu, na mipaka yako yote ya mawe yapendezayo.

13 Na watoto wako [a]wote watafundishwa na Bwana; na amani ya watoto wako itakuwa kubwa.

14 Utathibitika katika [a]haki; utakuwa mbali na kuonewa, kwani hutaogopa, na mbali na hofu, kwani haitakuja karibu nawe.

15 Tazama, yamkini watakusanyika pamoja dhidi yako, sio kwa shauri langu; wote watakaokusanyika pamoja dhidi yako wataanguka kwa ajili yako.

16 Tazama, nimemuumba mhunzi afukutaye moto wa makaa, na ambaye huleta chombo kwa kazi yake; na nimemuumba mharibifu kuangamiza.

17 Hakuna silaha yoyote itakayotengenezwa dhidi yako

2*a* MWM Kigingi.
3*a* MWM Wayunani.
4*a* 2 Ne. 6:7, 13.
8*a* MWM Rehema, enye Rehema.
9*a* Isa. 54:9.
b MWM Gharika katika Wakati wa Nuhu.
10*a* Isa. 40:4.
b Zab. 94:14; M&M 35:25.
11*a* Ufu. 21:18–21.
13*a* Yer. 31:33–34.
14*a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.

ambayo itafaulu; na kila ulimi ambao utatukana dhidi yako, utahukumu. Huu ndiyo urithi wa watumishi wa Bwana, na haki yao inatoka kwangu, asema Bwana.

MLANGO WA 23

Yesu anasifu maneno ya Isaya—Anaamuru watu wapekue manabii—Maneno ya Samweli Mlamani kuhusu Kufufuka yanaongezwa kwa maandishi yao. Karibia mwaka 34 B.K.

Na sasa, tazama, nawaambia kwamba mnapaswa kupekua vitu hivi. Ndiyo, ninawapatia amri kwamba [a]mpekue hivi vitu kwa bidii; kwani maneno ya [b]Isaya ni makuu.

2 Kwani alizungumza akitaja vitu vyote kuhusu watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli; kwa hivyo ni muhimu kwake kwamba lazima awazungumzie Wayunani pia.

3 Na vitu vyote ambavyo alizungumza vimekuwa na [a]vitakuwa, hata kulingana na maneno ambayo alisema.

4 Kwa hivyo sikilizeni maneno yangu; andikeni vitu ambavyo niliwaambia; na kulingana na muda na mapenzi ya Baba, vitawaendea Wayunani.

5 Na yeyote atakayetii maneno yangu na kutubu na kubatizwa, yule atakombolewa. Pekua [a]manabii, kwani wengi wameshuhudia hivi vitu.

6 Na sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kusema maneno haya, aliwaambia tena, baada ya kuwaelezea maandiko ambayo walikuwa wamepokea, aliwaambia: Tazama, maandiko mengine ningetaka muandike ambayo hamjaandika.

7 Na ikawa kwamba alimwambia Nefi: Leta hapa maandishi ambayo umeweka.

8 Na baada ya Nefi kumletea hayo maandishi, na kuyaweka mbele yake, alielekeza macho yake kwayo na kusema:

9 Kweli, nawaambia, nilimwamuru mtumishi wangu [a]Samweli, yule Mlamani, kwamba ashuhudie hawa watu, kwamba katika siku ambayo Baba atatukuza jina lake ndani yangu kwamba kulikuwa [b]watakatifu [c]wengi ambao [d]wangeinuka kutoka kwa wafu, na kuonekana na wengi, na kuwahudumia. Na akawaambia: Si ilikuwa hivyo?

10 Na wanafunzi wake walimjibu na kusema: Ndiyo, Bwana, Samweli alitabiri kulingana na maneno yako, na yote yalitimizwa.

11 Na Yesu akawaambia: Imekuwaje kwamba hamjaandika kitu hiki, kwamba watakatifu wengi walifufuka na kuonekana na wengi na kuwahudumia?

12 Na ikawa kwamba Nefi alikumbuka kwamba hiki kitu hakikuwa kimeandikwa.

13 Na ikawa kwamba Yesu

23 1*a* MWM Maandiko.
b 2 Ne. 25:1–5; Morm. 8:23. MWM Isaya.
3*a* 3 Ne. 20:11–12.
5*a* Lk. 24:25–27.
9*a* Hel. 13:2.
b MWM Mtakatifu.
c Hel. 14:25.
d Mt. 27:52–53. MWM Ufufuko.

aliamuru kwamba iandikwe; kwa hivyo iliandikwa vile alivyoamuru.

14 Na sasa ikawa kwamba baada ya Yesu [a]kueleza maandiko yote pamoja, ambayo waliandika, aliwaamuru kwamba wafundishe vitu ambavyo alikuwa amewaeleza.

MLANGO WA 24

Mjumbe wa Bwana atatayarisha njia kwa Ujio wa Pili—Kristo ataketi kwenye hukumu—Israeli inaamrishwa kulipa zaka na matoleo—Kitabu cha ukumbusho kinahifadhiwa—Linganisha Malaki 3. Karibia mwaka 34 B.K.

Na ikawa kwamba aliwaamuru kwamba waandike maneno ambayo Baba alimkabidhi Malaki, ambayo angewaambia. Na ikawa kwamba baada ya kuandikwa, aliyaeleza. Na haya ndiyo maneno aliyowaambia akisema: Baba alimwambia Malaki hivi—Tazama, nitamtuma [a]mjumbe wangu, na atatayarisha njia kabla yangu, na Bwana mnayemgojea atakuja kwa ghafla kwenye hekalu lake, hata yule mjumbe wa agano ambaye mnafurahia ndani; tazama atakuja, asema Bwana wa Majeshi.

2 Lakini ni nani [a]atakayestahili siku ya kuja kwake, na ni nani atakayesimama atakapotokea? Kwani yeye yuko kama moto [b]usafishao fedha, na kama sabuni ya dobi.

3 Na ataketi kama asafishaye fedha na kuitakasa, na atawatakasa [a]wana wa Lawi, atawasafisha kama dhahabu na fedha, ili dhabihu kwa Bwana liwe [b]toleo kwa haki.

4 Ndipo dhabihu ya Yuda na Yerusalemu zitapendeza mbele ya Bwana, kama katika siku za kale, na kama katika miaka ya zamani.

5 Na nitawakaribia kwa hukumu; na nitakuwa shahidi mwepesi dhidi ya wachawi, na dhidi ya wazinzi, na dhidi ya waapao uwongo, na dhidi ya wale wamwoneao mwenye kuajiriwa kwa ajili ya mshahara wake, mjane na [a]yatima, na wale wanaompoteza mgeni, na hawaniogopi, asema Bwana wa Majeshi.

6 Kwa kuwa mimi ni Bwana, sibadiliki; kwa hivyo enyi wana wa Yakobo hamwangamizwi.

7 Hata kutoka siku za babu zenu, [a]mmegeuka upande kutoka kwa maagizo yangu, na hamjayashika. [b]Nirudieni na nitarudi kwenu, asema Bwana wa Majeshi. Lakini ninyi mwasema: Tutarudi kwa namna gani?

8 Je, mwanadamu atamwibia Mungu? Lakini mmeniibia. Lakini mnasema: Tumekuibia

14*a* Lk. 24:44–46.
24 1*a* M&M 45:9.
2*a* 3 Ne. 25:1.
b Zek. 13:9; M&M 128:24.
MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
3*a* Kum. 10:8; M&M 84:31–34.
b M&M 13.
5*a* Yak. (Bib.) 1:27.
7*a* MWM Ukengeufu.
b Hel. 13:11; 3 Ne. 10:6; Moro. 9:22.

kwa namna gani? Katika [a]zaka na [b]madhabihu.

9 Mmelaaniwa na laana, kwani mmeniibia, hata hili taifa lote.

10 Leteni [a]zaka kamili ghalani, ili kuweko chakula katika nyumba yangu; na mnijaribu sasa hivi, asema Bwana wa Majeshi, kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni, na kuwamwagia [b]baraka, kwamba kusiwe na nafasi ya kutosha ya kuipokea.

11 Na nitamkemea mlaji kwa ajili yenu, na hataharibu matunda ya ardhi yenu; wala mizabibu wenu hautapukutisha matunda yake katika ardhi kabla ya wakati wake huko shambani, asema Bwana wa Majeshi.

12 Na mataifa yote yatawaita wenye heri, kwani mtakuwa nchi ya kupendeza, asema Bwana wa Majeshi.

13 Maneno yenu yamekuwa magumu juu yangu, asema Bwana. Lakini mnasema: Tumesema nini dhidi yako?

14 Mmesema ni bure kumtumikia Mungu, na tumepata faida gani kwa kuzishika ibada zake, na kwamba tumetembea kwa huzuni mbele ya Bwana wa Majeshi.

15 Na sasa tunawaita wenye kiburi ndiyo walio heri; ndiyo, wale wanaotenda maovu na kunufaika; ndiyo, wanaomjaribu Mungu ndiyo wanaookolewa.

16 Ndipo wale wanaomcha Bwana, [a]walisemezana wao kwa wao, na Bwana akasikiliza na kusikia; na [b]kitabu cha ukumbusho kikaandikwa mbele yake kwa wao wanaomcha Bwana, na kulitafakari jina lake.

17 Na watakuwa wangu, asema Bwana wa Majeshi, katika siku ile [a]nitakapofanya vito vyangu; na nitawaachilia vile mtu huachilia mwana wake amtumikiaye.

18 Ndipo mtakaporudi, na [a]kupambanua miongoni mwa wenye haki na waovu, na miongoni mwa yule amtumikiaye Mungu na yule asiyemtumikia.

MLANGO WA 25

Katika Ujio wa Pili, wenye kiburi na waovu watateketezwa kama makapi—Eliya atarejea kabla ya ile siku kubwa na ya kutisha—Linganisha Malaki 4. Karibia mwaka 34 B.K.

Kwani tazama, ile siku inakuja ambayo [a]itawaka kama tanuru; na wote wenye [b]kiburi, ndiyo, na wote wanaotenda maovu, watakuwa makapi; na ile siku inayokuja itawateketeza, asema Bwana wa Majeshi, kwamba haitawaachia shina wala tawi.

2 Lakini kwenu mnaolicha

8a MWM Lipa zaka, Zaka.
b MWM Sadaka, Utoaji sadaka.
10a M&M 64:23; 119.
b MWM Baraka, Bariki, Barikiwa.
16a Moro. 6:5.
b M&M 85:9; Musa 6:5. MWM Kitabu cha Ukumbusho.
17a M&M 101:3.
18a MWM Utambuzi, Kipawa cha.
25 1a Isa. 24:6; 1 Ne. 22:15; 3 Ne. 24:2; M&M 29:9; 64:23–24; 133:64; JS—H 1:37. MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia.
b 2 Ne. 20:33. MWM Kiburi.

jina langu, yule [a]Mwana wa Haki atawashukia na uponyaji katika mabawa yake; na ninyi mtaenda mbele na [b]kukua kama [c]ndama zizini.

3 Na [a]mtakanyaga waovu; kwani watakuwa majivu chini ya nyayo za miguu yenu katika siku nitakayofanya hivi, asema Bwana wa Majeshi.

4 Kumbukeni ninyi sheria ya Musa, mtumishi wangu, niliyemwamuru huko [a]Horebu kwa ajili ya Waisraeli wote, na amri za hukumu.

5 Tazama, nitawatumia [a]Eliya nabii kabla ya kuja kwa ile [b]siku kubwa na ya kutisha ya Bwana.

6 Na [a]atageuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, na mioyo ya watoto iwaelekee baba zao, nisije na kupiga dunia na laana.

MLANGO WA 26

Yesu anaeleza vitu vyote kutoka mwanzo hadi mwisho—Watoto wachanga na vijana wanaongea vitu vya ajabu ambavyo haviwezi kuandikwa—Wale walio katika Kanisa la Kristo wana vitu vyote vya hali sawa miongoni mwao. Karibia mwaka 34 B.K.

NA sasa ikawa kwamba baada ya Yesu kuwaambia hivi vitu, na alivieleza kwa umati; na alieleza vitu vyote kwao, vyote vikuu na vidogo.

2 Na alisema: [a]Maandiko haya ambayo hamkuwa nayo, Baba aliamuru kwamba niwapatie; kwani ilikuwa hekima kwake kwamba yatolewe kwa vizazi vijavyo.

3 Na alieleza vitu vyote, hata kutoka mwanzo mpaka wakati ambao angekuja katika [a]utukufu wake—ndiyo, hata vitu vyote ambavyo vingekuja juu ya uso wa dunia, hata mpaka [b]vitu vya asili vitakapoyeyuka kwa joto lenye nguvu sana, na dunia [c]itakunjamana pamoja kama karatasi, na mbingu na dunia vitakwisha;

4 Na hata kwenye ile siku [a]kuu, wakati watu wote, na makabila yote, na mataifa yote, na lugha [b]watasimama mbele ya Mungu, kuhukumiwa kwa vitendo vyao, kama ni vizuri au ni viovu—

5 Ikiwa ni vizuri, kwa [a]ufufuo wa uzima usio na mwisho; na vikiwa viovu, kwa ufufuko wa laana; vikiwa sambamba, moja kwa mkono mmoja na ingine

2*a* Eth. 9:22.
b M&M 45:58.
c Amo. 6:4; 1 Ne. 22:24.
3*a* 3 Ne. 21:12.
4*a* Ku. 3:1–6.
5*a* 2 Fal. 2:1–2; M&M 2:1; 110:13–16; 128:17–18.
MWM Eliya; Kufunga, Muhuri, Tia; Wokovu kwa ajili ya Wafu.
b MWM Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.
6*a* M&M 2:2.
26 2*a* MF Mal. 3–4, Nukuu katika 3 Ne. 24–25.
3*a* MWM Yesu Kristo—Utukufu wa Yesu Kristo.
b Amo. 9:13; 2 Pet. 3:10, 12; Morm. 9:2.
MWM Dunia—Kutakaswa kwa dunia; Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
c Morm. 5:23.
4*a* Hel. 12:25; 3 Ne. 28:31.
b Mosia 16:10–11.
MWM Hukumu ya mwisho.
5*a* Dan. 12:2; Yn. 5:29.

kwa mkono mwingine, kulingana na hekima, na [b]haki, na utukufu ulio ndani ya Kristo, ambaye alikuweko [c]kabla ya ulimwengu kuanza.

6 Na sasa hakuwezi kuandikwa kwenye kitabu hiki hata sehemu moja kwa [a]mia ya vitu ambavyo Yesu aliwafundisha watu kwa ukweli;

7 Lakini tazama, [a]mabamba ya Nefi yanayo sehemu kubwa ya vitu ambavyo aliwafundisha watu.

8 Na hivi vitu nimeandika, ambavyo ni sehemu ndogo ya vitu ambavyo aliwafundisha watu; na nimeviandika kwa kusudi kwamba vingeletwa tena kwa watu hawa, [a]kutoka kwa Wayunani, kulingana na maneno ambayo Yesu ameongea.

9 Na wakati watakapokuwa wamepokea hii, ambayo ni muhimu kwamba wapate kwanza, kujaribu imani yao, na ikiwa itakuwa hivyo kwamba wataamini vitu hivi, ndipo [a]vitu vikubwa zaidi vitadhihirishwa kwao.

10 Na ikiwa itakuwa hivyo kwamba hawataamini vitu hivi, ndipo vile vikubwa zaidi [a]vitazuiliwa kwao kusababisha lawama kwao.

11 Tazama, nilikuwa karibu kuyaandika, yote ambayo yalikuwa yamechorwa kwenye mabamba ya Nefi, lakini Bwana akakataza akisema: [a]Nitajaribu imani ya watu wangu.

12 Kwa hivyo mimi, Mormoni, naandika vitu ambavyo nimeamriwa na Bwana. Na sasa mimi, Mormoni, nafikia mwisho wa kusema kwangu, na ninaendelea kuandika vitu ambavyo nimeamriwa.

13 Kwa hivyo, ningetaka kwamba muelewe kwamba Bwana kweli aliwafundisha watu, kwa muda wa siku tatu; na baada ya hapo [a]alijidhihirisha kwao mara kwa mara, na [b]alimega mkate mara kwa mara na kuubariki na kuwapatia.

14 Na ikawa kwamba aliwafundisha na kuwahudumia [a]watoto wa umati ambao umezungumziwa, na aliwapatia [b]uwezo wa kuongea, na waliwazungumzia baba zao vitu vikubwa na vya ajabu, hata vikubwa kuliko alivyokuwa amewatambulia watu; na alifungua ndimi zao kwamba wangezungumza.

15 Na ikawa kwamba baada ya kupaa mbinguni—baada ya mara ya pili kwamba alijidhihirisha mwenyewe kwao, na alikuwa ameenda kwa Baba, baada ya [a]kuponya wagonjwa

5 *b* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
c Eth. 3:14.
MWM Yesu Kristo—Kuwepo kwa Kristo kabla ya kuzaliwa duniani.
6 *a* Yn. 21:25; 3 Ne. 5:8.
7 *a* MWM Mabamba.
8 *a* 3 Ne. 21:5–6.
9 *a* Eth. 4:4–10.
10 *a* Alma 12:9–11.
11 *a* Eth. 12:6.
13 *a* Yn. 21:14.
b 3 Ne. 20:3–9.
MWM Sakramenti.
14 *a* 3 Ne. 17:11–12.
b Alma 32:23; 3 Ne. 26:16.
15 *a* 3 Ne. 17:9.
MWM Muujiza; Ponya, Uponyaji.

wao wote, na vipofu wao, na kufungua masikio ya viziwi, na baada ya kufanya aina yote ya kuponya miongoni mwao, na kufufua mtu kutoka kwa wafu, na alikuwa ameonyesha uwezo wake kwao, na alikuwa amepaa juu kwa Baba—

16 Tazama, ikawa kesho yake kwamba umati ulikusanyika pamoja, na waliona na kusikia [a]watoto hawa; ndiyo, hata watoto wachanga walifungua vinywa vyao, na kuongea vitu vya kustaajabisha; na vitu ambavyo waliongea vilikatazwa kwamba kusiwe na mtu yeyote wa kuviandika.

17 Na ikawa kwamba [a]wanafunzi ambao Yesu alikuwa amewachagua walianza tangu wakati ule na kuendelea [b]kubatiza na kufundisha wengi jinsi walivyokuja kwao; na vile wengi walibatizwa katika jina la Yesu, walijazwa na Roho Mtakatifu.

18 Na wengi wao waliona na kusikia vitu visivyosemekana ambavyo [a]havikubaliwi kuandikwa.

19 Na walifundishanana kuhudumiana; na walikuwa na vitu [a]vyote [b]sawasawa miongoni mwao, kila mtu akifanya haki mmoja kwa mwingine.

20 Na ikawa kwamba walifanya vitu vyote hata kama vile Yesu alivyowaamuru.

21 Na wale ambao walibatizwa katika jina la Yesu waliitwa [a]kanisa la Kristo.

MLANGO WA 27

Yesu anaamuru kwamba Kanisa liitwe kwa jina Lake—Misheni Yake na dhabihu ya kulipia dhambi ndivyo hufanya injili Yake—Watu wanaamrishwa kutubu na kubatizwa ili waweze kutakaswa na Roho Mtakatifu—Inawapasa wawe hata vile Yesu alivyo. Karibia mwaka 34–35 B.K.

Na ikawa kwamba vile wanafunzi wa Yesu walipokuwa wakisafiri na kuhubiri vitu ambavyo walikuwa wamesikia na kuona, na walikuwa wakibatiza katika jina la Yesu, ikawa kwamba wanafunzi walijikusanya pamoja na [a]kushirikiana kwa sala kuu na [b]kufunga.

2 Na Yesu tena [a]alijidhihirisha kwao, kwani walikuwa wanaomba kwa Baba katika jina lake; na Yesu alikuja na kusimama miongoni mwao, na kuwaambia: Ni kitu gani mnachohitaji kwamba niwapatie?

3 Na wakamwambia: Bwana tunataka kwamba utuambie jina ambalo tutaita hili kanisa; kwani kuna ugomvi miongoni mwa watu kuhusu jambo hili.

4 Na Bwana akawaambia: Amin, amin, nawaambia, kwa nini watu wananung'unika na

16*a* Mt. 11:25.
17*a* 3 Ne. 19:4–13.
b 4 Ne. 1:1.
18*a* 3 Ne. 26:11.
19*a* 4 Ne. 1:3.
b MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
21*a* Mos. 18:17. MWM Kanisa la Yesu Kristo.

27 1*a* M&M 29:6.
b Alma 6:6. MWM Funga, Kufunga.
2*a* 3 Ne. 26:13. MWM Yesu Kristo—Kuonekana kwa Kristo baada ya kifo.

kubishana kwa sababu ya kitu hiki?

5 Je, hawajasoma maandiko, ambayo yanasema, lazima mjivike juu yenu [a]jina la Kristo, ambalo ni jina langu? Kwani, kwa jina hili ndilo mtaitwa nalo katika siku ya mwisho;

6 Na yeyote atakayechukua jina langu na [a]kuvumilia hadi mwisho, huyo huyo ndiye atakayeokolewa katika siku ya mwisho.

7 Kwa hivyo chochote mtakachofanya, mfanye katika jina langu; kwa hivyo mtaliita kanisa katika jina langu; na mtalingana Baba katika jina langu ili aweze kubariki kanisa kwa ajili yangu.

8 Na linawezaje kuwa [a]kanisa [b]langu isipokuwa liitwe kwa jina langu? Kwani kanisa likiitwa kwa jina la Musa, hapo litakuwa kanisa la Musa; au likiitwa kwa jina la mtu, basi litakuwa kanisa la yule mtu; lakini likiitwa katika jina langu, hapo basi litakuwa kanisa langu, ikiwa kwamba watajengwa juu ya injili yangu.

9 Kweli, nawaambia kwamba mmejengwa juu ya injili yangu; kwa hivyo mtaita vitu vyovyote mtakavyoita katika jina langu; kwa hivyo ikiwa mnalingana kwa Baba, kwa kanisa, ikiwa katika jina langu, Baba atawasikia.

10 Na ikiwa itakuwa hivyo kwamba kanisa limejengwa juu ya injili yangu hapo Baba atafichua kazi yake ndani yake.

11 Lakini ikiwa haitajengwa juu ya injili yangu, na imejengwa kwa vitendo vya watu, au juu ya vitendo vya ibilisi, amin, nawaambia wana shangwe katika vitendo vyao kwa muda, na karibuni mwisho unakuja, na [a]wataangushwa chini na kutupwa kwenye moto, kutoka mahali ambapo hakuna kurudi nyuma.

12 Kwani vitendo vyao [a]huwafuata, kwani ni kwa sababu ya vitendo vyao kwamba wanaangushwa chini; kwa hivyo kumbuka vitu ambavyo nimewaambia.

13 Tazama, nimewapatia [a]injili yangu, na hii ndiyo injili ambayo nimewapatia—kwamba nilikuja kwenye ulimwengu kufanya [b]mapenzi ya Baba, kwa sababu alinituma.

14 Na Baba yangu alinituma ili nipate [a]kuinuliwa juu kwenye msalaba; na baada ya kuinuliwa juu kwenye msalaba, kwamba [b]ningeleta watu wote kwangu, kwamba kama nilivyoinuliwa juu na watu, hata hivyo watu wainuliwe juu na Baba, kusimama mbele yangu, na [c]kuhukumiwa kwa vitendo vyao, ikiwa vitakuwa vizuri au ikiwa vitakuwa viovu.

5 *a* MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
6 *a* 3 Ne. 15:9.
8 *a* M&M 115:4.
b MWM Yesu Kristo—Kichwa cha Kanisa.
11 *a* Alma 5:52.
12 *a* Ufu. 14:13; M&M 59:2.
13 *a* M&M 76:40–42. MWM Injili.
b Yn. 6:38–39.
14 *a* 1 Ne. 11:32–33; Musa 7:55.
b Yn. 6:44; 2 Ne. 9:5; M&M 27:18.
c MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.

15 Na kwa sababu hii [a]nimeinuliwa juu; kwa hivyo, kulingana na uwezo wa Baba, nitawaleta watu wote kwangu, ili wapate kuhukumiwa kulingana na vitendo vyao.

16 Na itakuwa kwamba yeyote [a]atakayetubu na [b]kubatizwa katika jina langu atajazwa; na ikiwa [c]atavumilia hadi mwisho, tazama, yeye hatahukumiwa kuwa na hatia mbele ya Baba yangu kwenye ile siku wakati nitakaposimama kuhukumu ulimwengu.

17 Na yule ambaye hatavumilia hadi mwisho, mtu huyo huyo ndiye ataangushwa chini na kutupwa kwenye moto, mahali ambapo hawawezi kurudi nyuma, kwa sababu ya [a]haki ya Baba.

18 Na hili ndilo neno ambalo amewapatia watoto wa watu. Na kwa sababu hii yeye hutimiza maneno ambayo ameyatoa, na hasemi uwongo bali hutimiza maneno yake yote.

19 Na [a]hakuna kitu kichafu kinachoweza kuingia kwenye ufalme wake; kwa hivyo hakuna chochote ambacho huingia kwenye [b]pumziko lake isipokuwa wale ambao [c]wameosha nguo zao ndani ya damu yangu kwa sababu ya imani yao, na kutubu kwa dhambi zao zote, na uaminifu wao hadi mwisho.

20 Sasa hii ndiyo amri: [a]Tubuni ninyi nyote katika sehemu zote za dunia, na mje kwangu na [b]mbatizwe katika jina langu kwamba muweze [c]kutakaswa kwa kupokea Roho Mtakatifu, ili msimame mbele yangu [d]bila mawaa katika siku ya mwisho.

21 Kweli, kweli, nawaambia, hii ni injili yangu; na mnajua vitu ambavyo mnahitajika kufanya katika Kanisa langu; kwani vitendo ambavyo mmeniona nikifanya, hivyo pia mtafanya; kwani yale ambayo mmeniona nikifanya hata hivyo ninyi mtafanya;

22 Kwa hivyo mkifanya hivi vitu heri kwenu, kwani mtainuliwa juu katika ile siku ya mwisho.

23 Andikeni vitu ambavyo mmeona na kusikia, isipokuwa vile ambavyo [a]vimekatazwa.

24 Andikeni vitendo vya hawa watu, ambavyo vitakuwa, hata kama vilivyoandikwa, ya yale ambayo yamekuwepo.

25 Kwani tazama, kutoka kwenye vitabu ambavyo vimeandikwa, na ambavyo vitaandikwa, hawa watu [a]watahukumiwa, kwani kutoka kwa hivyo vitabu [b]vitendo vyao vitajulikana kwa wanadamu.

26 Na tazama, vitu vyote [a]vimeandikwa na Baba; kwa hivyo

15 *a* MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
16 *a* MWM Toba, Tubu.
b MWM Batiza, Ubatizo.
c 1 Ne. 13:37.
MWM Stahimili.
17 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
19 *a* Alma 11:37.
b M&M 84:24.
MWM Pumzika.
c Ufu. 1:5; 7:14; Alma 5:21, 27; 13:11–13.
20 *a* Eth. 4:18.
b MWM Batiza, Ubatizo—Muhimu.
c MWM Utakaso.
d M&M 4:2.
23 *a* 3 Ne. 26:16.
25 *a* 2 Ne. 33:10–15; M. ya Morm. 1:11.
b 1 Ne. 15:32–33.
26 *a* 3 Ne. 24:16.
MWM Kitabu cha Uzima.

kutoka kwenye hivyo vitabu ambavyo vitaandikwa, dunia itahukumiwa.

27 Na mjue kwamba [a]ninyi mtakuwa waamuzi wa watu hawa, kulingana na hukumu ambayo nitawapatia ambayo itakuwa haki. Kwa hivyo mnapaswa kuwa watu wa [b]aina gani? Amin, nawaambia, hata [c]vile nilivyo.

28 Na sasa [a]naenda kwa Baba. Na amin, nawaambia, vitu vyovyote mtakavyomuuliza Baba katika jina langu, vitatolewa kwenu.

29 Kwa hivyo, [a]ombeni na mtapokea; bisheni na mtafunguliwa; kwani yule ambaye huuliza hupokea; na kwa yule ambaye hubisha, itafunguliwa.

30 Na sasa tazama, shangwe yangu ni kubwa, hata kwenye utimilifu, kwa sababu yenu, na pia kwa sababu ya kizazi hiki; ndiyo, na hata Baba hufurahi, na pia malaika watakatifu, kwa sababu yenu na hiki kizazi; kwani [a]hakuna mmoja wao aliyepotea.

31 Tazama, ningetaka kwamba muelewe; kwani ninaamanisha hao ambao [a]sasa ni wazima wa [b]hiki kizazi; na hakuna hata ambaye amepotea; na kwa sababu yao, nina utimilifu wa [c]shangwe.

32 Lakini tazama, inanihuzunisha kwa sababu ya kizazi cha [a]nne kutoka kwa hiki kizazi, kwani wameongozwa mbali kama mateka na yeye, hata kama vile mwana wa upotevu; kwani wataniuza kwa fedha, na dhahabu, na kwa hiyo ambayo [b]nondo huharibu na ambayo wezi huvunja na kuingia na kuiba. Na katika ile siku, nitawaadhibu, hata katika kugeuza vitendo vyao juu ya vichwa vyao.

33 Na ikawa kwamba wakati Yesu alipokuwa amemaliza maneno haya, aliwaambia wanafunzi wake: Ingieni ndani ninyi kupitia [a]mlango uliosonga; kwani mlango umesonga na njia ni nyembamba, ambayo inaenda kwa maisha, na kuna wachache ambao huipata; lakini mpana ni mlango, na pana ni njia iendayo kwenye kifo, na kuna wengi ambao huisafiria, mpaka usiku unakuja ambapo hakuna mtu atakayeweza kufanya kazi.

MLANGO WA 28

Tisa kati ya wale wanafunzi kumi na wawili wanatamani na wanaahidiwa urithi katika ufalme wa Kristo baada ya kufa kwao—Wanefi Watatu wanatamani na wanapewa uwezo juu ya kifo ili wabaki duniani hadi wakati Yesu atakaporudi tena—Wanahamishwa na kuona vitu ambavyo si

27 *a* 1 Ne. 12:9–10; Morm. 3:19.
b MWM Yesu Kristo—Mfano wa Yesu Kristo.
c Mt. 5:48; 3 Ne. 12:48.

28 *a* Yn. 20:17.

29 *a* Mt. 7:7; 3 Ne. 14:7.

30 *a* Yn. 17:12.

31 *a* 3 Ne. 9:11–13; 10:12.
b 3 Ne. 28:23.
c MWM Shangwe.

32 *a* 2 Ne. 26:9–10; Alma 45:10, 12.
b Mt. 6:19–21; 3 Ne. 13:19–21.

33 *a* Mt. 7:13–14; 3 Ne. 14:13–14; M&M 22.

halali kusema, na sasa wanahudumu miongoni mwa watu. Karibia mwaka 34–35 B.K.

Na ikawa kwamba Yesu alipokuwa amesema maneno haya, aliwazungumzia wanafunzi wake mmoja mmoja, akiwaambia: Ni kitu gani ambacho mnahitaji kutoka kwangu baada ya mimi kwenda kwa Baba?

2 Na wote walisema, isipokuwa watatu, wakisema: Tunataka kwamba baada ya kuishi umri wa binadamu, kwamba huduma yetu ambayo umetuitia, iishe, kwamba tuje kwako haraka kwenye ufalme wako.

3 Na akawaambia: Heri kwenu kwa sababu mnataka kitu hiki kutoka kwangu; kwa hivyo baada ya kuhitimu miaka sabini na miwili, mtakuja kwangu katika ufalme wangu; na mimi mtapata [a]mapumziko.

4 Na baada ya kuwazungumzia, alijigeuza kuelekea wale watatu, na kuwaambia: Ni kitu gani ambacho mnataka niwafanyie, wakati nitakapokwenda kwa Baba?

5 Na walihuzunika mioyoni mwao, kwani hawakuthubutu kuzungumza na yeye kitu ambacho walitaka.

6 Na akawaambia: Tazama, [a]najua mawazo yenu, na mmetaka kitu ambacho [b]Yohana, mpendwa wangu, ambaye alikuwa na mimi katika huduma yangu kabla ya mimi kuinuliwa juu na Wayahudi, alichotaka kwangu.

7 Kwa hivyo heri zaidi kwenu kwani [a]kamwe hamtaonja [b]kifo; lakini mtaishi kuona vitendo vyote vya Baba kwa watoto wa watu, hata mpaka vitu vyote vitatimizwa kulingana na mapenzi ya Baba, wakati nitakapokuja kwa utukufu wangu na [c]uwezo wa mbinguni.

8 Na hamtaumia uchungu wa kifo; lakini nitakapokuja katika utukufu wangu mtabadilishwa kwa nukta moja kutoka hali ya [a]kufa hadi kwa hali ya [b]kutokufa; na ndipo mtabarikiwa katika ufalme wa Baba yangu.

9 Na tena, hamtapata maumivu wakati mtakapoishi kimwili; wala huzuni isipokuwa kwa dhambi za ulimwengu; na haya yote nitafanya kwa sababu ya kitu ambacho mmetaka kutoka kwangu, kwani mmetaka kwamba [a]mlete roho za watu kwangu, wakati dunia itakaposimama.

10 Na kwa sababu hii mtapata [a]utimilifu wa shangwe; na mtaketi chini katika ufalme wa Baba yangu; ndiyo, shangwe yenu itajaa, hata vile Baba amenipatia utimilifu wa shangwe; na mtakuwa hata kama nilivyo, nami niko hata

28 3*a* MWM Pumzika.
6*a* Amo. 4:13; Alma 18:32.
b Yn. 21:21–23; M&M 7:1–4.
7*a* 4 Ne. 1:14; Morm. 8:10–11; Eth. 12:17.
b MWM Viumbe waliobadilishwa.
c 3 Ne. 20:22.
8*a* 3 Ne. 28:36–40. MWM Hali ya Kufa, enye Kufa.
b MWM Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa.
9*a* Flp. 1:23–24; M&M 7:5–6.
10*a* M&M 84:36–38.

vile Baba alivyo, na Baba nami tuko [b]wamoja.

11 Na [a]Roho Mtakatifu hushuhudia mambo ya Baba na Mimi; na Baba huwapa watoto wa watu Roho Mtakatifu kwa sababu yangu.

12 Na ikawa kwamba baada ya Yesu kuzungumza maneno haya, alimgusa kila mmoja wao kwa kidole chake isipokuwa wale watatu ambao walikuwa wa kukawia, na hapo akaondoka.

13 Na tazama, mbingu zilifunguka, na [a]walichukuliwa juu katika mbingu, na waliona na kusikiliza vitu visivyosikika.

14 Na [a]walikatazwa kwamba wasiongee; wala hawakupewa uwezo kwamba waongee juu ya vitu ambavyo waliona na kusikia;

15 Na kama walikuwa katika miili au walikuwa nje ya miili, hawakuja; kwani ilionekana kwao kama [a]kugeuka sura, kwamba waligeuzwa kutoka kwa huu mwili wa nyama hadi kwenye kutokufa, kwamba wangeweza kuona vitu vya Mungu.

16 Lakini ikawa kwamba walihubiri tena juu ya dunia; lakini hawakuhubiri juu ya vitu ambavyo walisikia na kuona kwa sababu ya amri ambayo walipewa mbinguni.

17 Na sasa, kama walikuwa mwili wenye kufa au wa kutokufa kutoka siku ya kugeuka kwao sura, sijui;

18 Lakini hiki kiasi najua, kulingana na maandishi ambayo yametolewa—walienda kote juu ya ulimwengu, na kuhubiri kwa watu wote, wakileta kwenye kanisa jinsi vile wengi walivyoamini katika mahubiri yao; wakiwabatiza, na vile wengi walibatizwa, walipokea Roho Mtakatifu.

19 Na walitupwa gerezani na wale ambao hawakuwa wa kanisa. Na [a]magereza hayangewashikilia, kwani yalipasuka katikati.

20 Na walitupwa chini ndani ya ardhi; lakini walipiga ardhi kwa neno la Mungu, mpaka kwamba kwa [a]uwezo wake walikombolewa kutoka kina cha ardhi; na kwa hivyo hawangechimba mashimo ya kutosha ya kuwazuia.

21 Na mara tatu walitupwa kwenye [a]tanuru na hawakupata majeraha.

22 Na mara mbili walitupwa kwenye [a]tundu la wanyama wa mwitu; na tazama, walicheza na hao wanyama kama mtoto na mwanakondoo, na hawakujeruhiwa.

23 Na ikawa kwamba walienda hivyo miongoni mwa watu wote wa Nefi, na walihubiri [a]injili ya Kristo kwa watu wote usoni mwa nchi; na waliomgeukia Bwana, na waliunganishwa

10 *b* Yn. 17:20–23.
11 *a* 2 Ne. 31:17–21; 3 Ne. 11:32.
13 *a* 2 Kor. 12:2–4.
14 *a* M&M 76:114–116.
15 *a* Musa 1:11. MWM Kugeuka sura.
19 *a* Mdo. 16:26; Alma 14:26–28.
20 *a* Morm. 8:24.
21 *a* Dan. 3:22–27; 4 Ne. 1:32.
22 *a* Dan. 6:16–23; 4 Ne. 1:33.
23 *a* MWM Injili.

kwa kanisa la Kristo, na hivyo ndivyo watu wa [b]kizazi hicho walivyobarikiwa, kulingana na neno la Yesu.

24 Na sasa mimi Mormoni, namaliza kuzungumza kuhusu vitu hivi kwa muda.

25 Tazama, nilikuwa karibu kuandika [a]majina ya wale ambao hawatakufa, lakini Bwana alinikataza; kwa hivyo siyaandiki, kwani yamefichwa kutoka kwa ulimwengu.

26 Lakini tazama, nimewaona na wamenihubiria.

27 Na tazama, watakuwa miongoni mwa Wayunani, na Wayunani hawatawafahamu.

28 Watakuwa pia miongoni mwa Wayahudi na Wayahudi hawatawafahamu.

29 Na itakuwa, wakati Bwana atakapoona ni vizuri kwa hekima yake, kwamba watahubiri kwa makabila yote ya Israeli [a]yaliyotawanywa, na kwa mataifa yote, makabila, lugha na watu, na kuokoa nafsi nyingi miongoni mwao kwa Yesu, ili matakwa yao yatimizwe, na pia kwa sababu ya uwezo wa Mungu wa kusadikisha ambao umo ndani yao.

30 Na wao ni kama [a]malaika wa Mungu, na ikiwa wataomba kwa Baba katika jina la Yesu, wanaweza kujidhihirisha kwa mtu yeyote ambaye wanaona ni vyema.

31 Kwa hivyo vitendo vikubwa na vya ajabu vitafanywa nao, kabla ya siku [a]kubwa inayokuja wakati watu wote lazima kwa kweli wasimame mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

32 Ndiyo, hata miongoni mwa Wayunani kutafanyika kazi [a]kubwa na ya ajabu na wao, kabla ya ile siku ya hukumu.

33 Na kama mngekuwa na maandiko yote ambayo yanatoa historia ya kazi zote za ajabu za Kristo, mngejua, kulingana na maneno ya Kristo, kwamba hivi vitu lazima vije kwa kweli.

34 Na ole kwake ambaye [a]hatasikia maneno ya Yesu, na pia kwa [b]wao ambao amechagua na kutuma miongoni mwao; kwani yeyote ambaye hatapokea maneno haya ya Yesu na maneno ya wale ambao amewatuma, hatampokea; na kwa hivyo hatawapokea katika ile siku ya mwisho;

35 Na ingelikuwa afadhali kwao kama hawangezaliwa. Kwani mnadhani kwamba mnaweza kukwepa haki ya Mungu aliyekosewa, ambaye [a]amekanyagwa chini ya miguu ya watu, ili wokovu ungekuja?

36 Na sasa tazama, vile nilisema kuhusu wale ambao Bwana amewachagua, ndiyo, hata wale watatu waliochukuliwa

23 *b* 3 Ne. 27:30–31.
25 *a* 3 Ne. 19:4.
29 *a* MWM Israeli—Kutawanyika kwa Israeli; Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea.
30 *a* MWM Malaika.
31 *a* Hel. 12:25; 3 Ne. 26:4–5.
32 *a* 2 Ne. 25:17.
34 *a* Eth. 4:8–12.
b MWM Nabii.
35 *a* Hel. 12:2.

juu katika mbingu, kwamba sikujua kama waligeuzwa kutoka mwili wa kufa hadi mwili usiokufa—

37 Lakini tazama, tangu niandike, nimemwuliza, Bwana, na ameifanya kujulikana kwangu kwamba lazima mabadiliko yaletwe kwenye miili yao, au sivyo, inahitajika kwamba lazima wapate kufa;

38 Kwa hivyo, ili wasipate kufa, kulikuwa na [a]mabadiliko yaliyofanywa kwenye miili yao, ili wasiumie na uchungu wala huzuni isipokuwa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu.

39 Sasa hili badiliko halikuwa sawa na lile ambalo litatendeka katika ile siku ya mwisho; lakini kulikuwa na badiliko lililofanywa kwao, mpaka kwamba Shetani hangekuwa na uwezo juu yao, kwamba [a]hangewajaribu; na [b]walitakaswa kimwili, kwamba walikuwa [c]watakatifu, na kwamba nguvu za dunia hazingewashika.

40 Na wangekaa kwa hali hii mpaka siku ya hukumu ya Kristo; na katika ile siku wangepokea mabadiliko makubwa kuliko mbeleni na kupokewa katika ufalme wa Baba kutotoka tena, lakini kuishi na Mungu milele mbinguni.

MLANGO WA 29

Ujio wa Kitabu cha Mormoni ni ishara kwamba Bwana ameanza kukusanya Israeli na kutimiza maagano Yake—Wale ambao wanakana mafunuo Yake ya siku za mwisho na zawadi watalaaniwa. Karibia mwaka 34–35 B.K.

Na sasa tazama, nawaambia kwamba wakati Bwana atakapoona sawa katika hekima yake, kwamba maneno haya [a]yatawajia Wayunani kulingana na neno lake, ndipo mtajua kwamba [b]agano ambalo Baba amefanya na wana wa Israeli, kuhusu kurudi kwao kwenye nchi zao za urithi, kitambo imeanza kutimizwa.

2 Na mtajua kwamba maneno ya Bwana, ambayo yamezungumzwa na manabii watakatifu, yote yatatimizwa; na hamtahitajika kusema kwamba Bwana [a]anacheleweshe kuja kwake kwa wana wa Israeli.

3 Na hamtakikani kuwaza katika mioyo yenu kwamba maneno ambayo yamezungumzwa ni ya bure, kwani tazama, Bwana atakumbuka agano lake ambalo amefanya kwa watu wake wa nyumba ya Israeli.

4 Na wakati mtakapoona maneno haya yakitokea miongoni mwenu, hamtahitaji tena kudharau mwenendo wa Bwana, kwani [a]upanga wake wa [b]haki uko ndani ya mkono wake wa kulia; na tazama, katika siku ile, ikiwa mtakataa kwa madharau, vitendo vyake, ndipo

38 *a* MWM Viumbe waliobadilishwa.
39 *a* MWM Jaribu, Majaribu.
b MWM Utakaso.
c MWM Utakatifu.
29 1 *a* 2 Ne. 30:3–8.
b Morm. 5:14, 20.
2 *a* Lk. 12:45–48.
4 *a* 3 Ne. 20:20.
b MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.

atasababisha kwamba haraka mtapitwa.

5 [a]Ole kwake ambaye [b]hukataa vitendo vya Bwana; ndiyo, ole kwake ambaye [c]atakataa Kristo na matendo yake!

6 Ndiyo, [a]ole kwa yule ambaye atakataa mafunuo ya Bwana, na ambaye atasema kuwa Bwana hafanyi kazi tena kwa kufunua au unabii, au kwa [b]karama, au kwa lugha au kwa kuponya, au kwa uwezo wa Roho Mtakatifu!

7 Ndiyo, na ole kwa yule atakayesema katika ile siku, kupata [a]faida, kwamba [b]hakuwezi kufanyika miujiza na Yesu Kristo; kwani yule atakayefanya hivi atakuwa [c]mwana wa upotevu, ambaye kwake hakukuwa na huruma kulingana na neno la Kristo!

8 Ndiyo, na hamhitaji tena [a]kufyonya, wala [b]kudharau, wala kuchezea [c]Wayahudi, wala baki lolote la nyumba ya Israeli; kwani tazama, Bwana hukumbuka agano lake kwao, na atawafanyia kulingana na yale ambayo ameapa.

9 Kwa hivyo hampaswi kudhani kwamba mnaweza kugeuza mkono wa kulia wa Bwana hadi kushoto, ili asifanye hukumu yake kwa kutimiza lile agano ambalo amefanya kwa nyumba ya Israeli.

MLANGO WA 30

Wayunani wa siku za mwisho wanaamriwa watubu, wamkubali Kristo, na wahesabiwe na nyumba ya Israeli. Karibia mwaka 34–35 B.K.

Sikizeni, Ee ninyi Wayunani, na msikie maneno ya Yesu Kristo, Mwana wa Mungu anayeishi, ambaye [a]ameniamuru kwamba nisizungumze kuwahusu kwani tazama, ameniamuru kwamba niandike nikisema:

2 Geukeni ninyi [a]Wayunani wote, kutoka kwenye njia zenu za uovu; na [b]mtubu kutoka matendo yenu maovu, kutoka kwa uwongo wenu na udanganyifu, na ukahaba wenu, na makundi yenu ya machukizo na ya siri, na sanamu zenu, na mauaji yenu, na ukuhani wa uongo, na wivu wenu, na mashindano yenu ya machukizo ya siri, na kutokana kwa uovu wenu na maovu, na mje kwangu, na mpate kubatizwa kwa jina langu, ili mpate kusamehewa dhambi zenu, na mjazwe na Roho Mtakatifu, ili [c]mhesabiwe na watu wangu ambao ni wa nyumba ya Israeli.

5 *a* 2 Ne. 28:15–16.
b Morm. 8:17; Eth. 4:8–10.
c Mt. 10:32–33.
6 *a* Morm. 9:7–11, 15.
b MWM Vipawa vya Roho.
7 *a* MWM Ukuhani wa uongo.
b 2 Ne. 28:4–6; Morm. 9:15–26.
c MWM Wana wa Upotevu.
8 *a* 1 Ne. 19:14.
b 2 Ne. 29:4–5.
c MWM Wayahudi.

30 1 *a* 3 Ne. 5:12–13.
2 *a* MWM Wayunani.
b MWM Toba, Tubu.
c Gal. 3:27–29; 2 Ne. 10:18–19; 3 Ne. 16:10–13; 21:22–25; Ibr. 2:10.

NEFI WA NNE
KITABU CHA NEFI

AMBAYE NI MWANA WA NEFI—MMOJAWAPO WA WANAFUNZI WA YESU KRISTO

Historia ya watu wa Nefi, kulingana na maandishi yake.

Wanefi na Walamani wote wanaongoka kwa Bwana—Vitu vyao vyote vinatumiwa kwa usawa, wanafanya miujiza, na wanafanikiwa nchini—Baada ya miaka mia mbili, migawanyiko, uovu, makanisa ya uwongo, na udhalimu vinatokea—Baada ya miaka mia tatu, wote Wanefi na Walamani wanakuwa waovu—Amaroni anaficha maandishi matakatifu. Karibia mwaka 35–321 B.K.

NA ikawa kwamba mwaka wa thelathini na nne ulipita, na pia mwaka wa thelathini na tano, na tazama wanafunzi wa Yesu walikuwa wameanzisha kanisa la Kristo katika eneo lote karibu. Na kadiri wengi walivyokuja kwao, na kutubu dhambi zao kwa ukweli, walibatizwa kwa jina la Yesu; na pia walipokea Roho Mtakatifu.

2 Na ikawa katika mwaka wa thelathini na sita, watu wote walimgeukia Bwana, nchini kote, wote Wanefi na Walamani, na hapakuweko na mabishano na ugomvi miongoni mwao, na kila mtu alimtendea mwingine haki.

3 Na vitu vyao [a]vyote vilitumiwa kwa usawa miongoni mwao; kwa hivyo hakukuwa na tajiri na masikini, wafungwa na walio huru, lakini wote walifanywa huru, na washiriki wa karama ya mbinguni.

4 Na ikawa kwamba mwaka wa thelathini na saba ulipita pia, na bado kukaendelea kuwa na amani katika nchi.

5 Na kulikuwa na kazi kubwa na ya ajabu iliyofanywa na wanafunzi wa Yesu, mpaka kwamba [a]waliponya wagonjwa, na kufufua wafu, na kusababisha vilema kutembea, na vipofu kupokea uwezo wa kuona, na viziwi kusikia; na walifanya kila aina ya [b]miujiza miongoni mwa watoto wa watu; na hawakufanyia miujiza isipokuwa katika jina la Yesu.

6 Na hivyo ndivyo mwaka wa thelathini na nane ulivyopita, na pia wa thelathini na tisa, na wa arubaini na moja, na wa arubaini na mbili, ndiyo, hata miaka arubaini na tisa ilipita, na pia wa hamsini na moja, na wa hamsini na mbili; ndiyo, na hata miaka hamsini na tisa ilipita.

7 Na Bwana aliwafanikisha

1 3*a* Mdo. 4:32; 3 Ne. 26:19. MWM Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu.
5*a* MWM Ponya, Uponyaji.
b Yn. 14:12. MWM Muujiza.

sana katika nchi; ndiyo, mpaka kwamba walijenga miji tena ambako miji ilichomwa.

8 Ndiyo, hata huo [a]mji mkubwa Zarahemla, walisababisha kujengwa tena.

9 Lakini kulikuwa na miji mingi ambayo ilikuwa [a]imezama, na maji kuja mahali pao; kwa hivyo, hii miji haingefanywa upya.

10 Na sasa, tazama, ikawa kwamba watu wa Nefi walipata nguvu, na wakaongezeka kwa haraka sana, na wakawa [a]weupe sana na watu wa kupendeza.

11 Na walioa, na kuolewa, na walibarikiwa kulingana na wingi wa ahadi ambazo Bwana alikuwa amefanya kwao.

12 Na hawakutembea tena kulingana na [a]vitendo na [b]sheria ya Musa; lakini walitembea kulingana na amri ambazo walipokea kutoka kwa Bwana wao na Mungu wao, wakiendelea katika [c]kufunga na sala, na kwa kukutana pamoja siku zote kuomba na kusikia neno la Bwana.

13 Na ikawa kwamba hakukuwepo na ubishi miongoni mwa watu wote, katika ile nchi yote; lakini kulikuwa na miujiza mikuu iliyofanywa na wanafunzi wa Yesu.

14 Na ikawa kwamba mwaka wa sabini na moja ulipita, na pia mwaka wa sabini na mbili, ndiyo, na kwa kifupi, mpaka mwaka wa sabini na tisa ulipopita; ndiyo, hata miaka mia moja ilikuwa imepita, na wanafunzi wa Yesu, ambao aliwachagua, wote walikuwa wameenda [a]peponi kwa Mungu, isipokuwa wale [b]watatu ambao wataendelea kuishi; na kulikuwa na [c]wanafunzi wengine ambao [d]walisimikwa mahali pao; na pia wengi wa kizazi hicho walikuwa wamekufa.

15 Na ikawa kwamba [a]hakukuwa na ubishi katika nchi, kwa sababu ya mapenzi ya Mungu ambayo yaliishi katika mioyo ya watu.

16 Na [a]hakukuwa na wivu, wala ubishi, wala misukosuko, wala ukahaba, wala uwongo, wala mauaji, wala [b]uzinifu wa aina yoyote; na kwa kweli hakujakuwa na watu ambao wangekuwa na [c]furaha zaidi miongoni mwa watu wote ambao waliumbwa na mkono wa Mungu.

17 Hakukuwa na wanyang'anyi, wala wauaji, wala hakukuwa na Walamani, wala aina yoyote ya vikundi; lakini walikuwa kitu [a]kimoja, watoto wa Kristo, na warithi wa ufalme wa Mungu.

18 Na jinsi gani walibarikiwa! Kwani Bwana aliwabariki kwa matendo yao yote; ndiyo, hata walibarikiwa na kufanikiwa

8 *a* 3 Ne. 8:8.
9 *a* 3 Ne. 9:4, 7.
10 *a* Morm. 9:6.
12 *a* 2 Ne. 25:30; 3 Ne. 15:2–8.
b MWM Torati ya Musa.
c Moro. 6:5; M&M 88:76–77.
14 *a* MWM Peponi.
b 3 Ne. 28:3–9. MWM Viumbe waliobadilishwa.
c MWM Mwanafunzi.
d MWM Kutawaza, Kutawazwa.
15 *a* MWM Amani.
16 *a* MWM Umoja.
b MWM Tamaa mbaya.
c Mos. 2:41; Alma 50:23. MWM Shangwe.
17 *a* Yn. 17:21. MWM Sayuni.

mpaka miaka mia moja na kumi ikapita; na kizazi cha kwanza kutoka Kristo kilikuwa kimepita, na hakukuwa na ubishi katika nchi yote.

19 Na ikawa kwamba Nefi, yule ambaye aliandika maandishi haya ya mwisho, (na aliyaandika kwenye [a]mabamba ya Nefi) alikufa, na mwana wake Amosi aliandika badala yake; na aliyaandika kwenye mabamba ya Nefi pia.

20 Na aliandika kwa miaka themanini na minne, na kulikuwa bado na amani nchini, isipokuwa sehemu ndogo ya watu ambao walikuwa wameasi kutoka kanisa na kujiita Walamani; kwa hivyo kulianza kuwa tena na Walamani katika nchi.

21 Na ikawa kwamba Amosi alifariki pia, (na ilikuwa miaka mia moja tisini nne kutoka kuja kwa Kristo) na mwana wake Amosi aliandika maandishi badala yake; na yeye pia aliandika kwenye mabamba ya Nefi; na ikaandikwa pia kwenye kitabu cha Nefi, ambacho ni kitabu hiki.

22 Na ikawa kwamba miaka mia mbili ilikuwa imepita; na kizazi cha pili chote kilikuwa kimepita isipokuwa wachache.

23 Na sasa mimi, Mormoni, ningetaka kwamba mjue kwamba watu walikuwa wameongezeka, mpaka kwamba walitapakaa kote usoni mwa nchi, na kwamba walikuwa wametajirika sana, kwa sababu ya kufanikiwa kwao katika Kristo.

24 Na sasa, katika mwaka huu wa mia mbili na moja kulianza kuwa miongoni mwao wale ambao waliinuliwa katika [a]kiburi, kwa kuvaa nguo za thamani, na kila aina ya lulu nzuri, na vitu vizuri vya dunia.

25 Na tangu wakati ule na kuendelea, walikuwa na mali yao na utajiri wao, na vitu vyao havikuwa [a]sawa miongoni mwao.

26 Na walianza kujigawanya kwenye vyeo; na wakaanza kujenga [a]makanisa yao kwa kujipatia [b]faida, na wakaanza kukataa kanisa la kweli la Kristo.

27 Na ikawa kwamba wakati miaka mia mbili na kumi ilipokuwa imepita kulikuwa na makanisa mengi katika nchi; ndiyo, kulikuwa na makanisa mengi ambayo yalidai kumjua Kristo, na bado [a]yalikataa sehemu kubwa ya injili yake, mpaka kwamba yalikubali aina yote ya uovu, na yalitoa kila kilicho kitakatifu kwa yule ambaye alikuwa [b]amekataliwa kwa sababu ya kutostahili.

28 Na hili [a]kanisa liliongezeka sana kwa sababu ya uovu, na kwa sababu ya nguvu ya Shetani ambaye alishikilia mioyo yao.

29 Na tena, kulikuwa na kanisa lingine ambalo lilimkana Kristo; na [a]walidhulumu kanisa

19 *a* MWM Mabamba.
24 *a* MWM Kiburi.
25 *a* 4 Ne. 1:3.
26 *a* 1 Ne. 22:23; 2 Ne. 28:3; Morm. 8:32–38.
b M&M 10:56. MWM Ukuhani wa uongo.
27 *a* MWM Ukengeufu.
b 3 Ne. 18:28–29.
28 *a* MWM Ibilisi—Kanisa la ibilisi.
29 *a* MWM Mateso, Tesa.

la kweli la Kristo, kwa sababu ya uvumilivu wao na kuamini kwao katika Kristo; na waliwadharau kwa sababu ya miujiza mingi ambayo walifanya miongoni mwao.

30 Kwa hivyo walionyesha uwezo na mamlaka juu ya wanafunzi wa Yesu ambao walibaki nao, na waliwatupa [a]gerezani; lakini kwa uwezo wa neno la Mungu, ambao ulikuwa ndani yao, magereza yalipasuka katikati, na wakaenda mbele wakifanya miujiza mikuu miongoni mwao.

31 Walakini, na ijapokuwa hii miujiza yote, watu walishupaza mioyo yao, na walitaka kuwaua, hata kama vile Wayahudi wa Yerusalemu walitafuta kumuua Yesu, kulingana na neno lake.

32 Na waliwatupa kwenye [a]majiko ya [b]moto, na wakatoka nje bila majeraha.

33 Na waliwatupa pia kwenye [a]mapango ya wanyama wa mwitu, na walicheza na wale wanyama wa mwitu hata kama vile mtoto na mwanakondoo; na walitoka kutoka miongoni mwao, bila kupata majeraha.

34 Walakini, watu walishupaza mioyo yao, kwani walionguzwa na makuhani wengi na manabii wa uwongo kuanzisha makanisa mengi, na kufanya aina yote ya uovu. Na [a]waliwapiga watu wa Yesu; lakini watu wa Yesu hawakulipiza kisasi. Na hivyo walififia katika kutoamini na uovu, kutoka mwaka mmoja hadi mwingine, hata hadi miaka mia mbili na thelathini ikapita.

35 Na sasa ikawa katika mwaka huu, ndiyo, katika mwaka wa mia mbili na thelathini na moja, kulikuwa na mgawanyiko mkubwa miongoni mwa watu.

36 Na ikawa kwamba katika mwaka huu kulitokea watu ambao waliitwa Wanefi, na walikuwa waumini wa kweli wa Kristo; na miongoni mwao kulikuwa na wale ambao waliitwa na Walamani—Wayakobo, na Wayusufu, na Wazoramu;

37 Kwa hivyo waumini wa kweli katika Kristo, na waabudu wa kweli wa Kristo, (miongoni mwao ambao walikuwa wale [a]wanafunzi watatu wa Yesu ambao watakaa) waliitwa Wanefi, na Wayakobo, na Wayusufu, na Wazoramu.

38 Na ikawa kwamba wale ambao walikataa injili waliitwa Walamani, na Walemueli, na Waishmaeli; na hawakufifia kwa kutoamini, lakini [a]waliasi makusudi dhidi ya injili ya Kristo; na waliwafundisha watoto wao kwamba wasiamini, hata vile babu zao, kutoka mwanzoni, walivyofifia.

39 Na ilikuwa kwa sababu ya uovu na machukizo ya babu zao, hata kama vile ilivyokuwa mwanzoni. Na [a]walifundishwa kuchukia watoto wa Mungu,

30 *a* 3 Ne. 28:19–20.
32 *a* 3 Ne. 28:21.
b Dan. 3:26–27.
33 *a* 3 Ne. 28:22.
34 *a* 3 Ne. 12:39; M&M 98:23–27.
37 *a* 3 Ne. 28:6–7; Morm. 8:10–11.
38 *a* MWM Uasi.
39 *a* Mos. 10:17.

hata vile Walamani walifundishwa kuwachukia watoto wa Nefi kutoka mwanzo.

40 Na ikawa kwamba miaka mia mbili na arubaini na nne ilikuwa imekwisha, na hivyo ndivyo yalikuwa mambo ya watu. Na sehemu kubwa ya watu waovu ilipata nguvu, na walikuwa wengi sana kuliko watu wa Mungu.

41 Na bado waliendelea na kujenga makanisa yao, na kuyapamba na aina yote ya vitu vya thamani. Na hivyo miaka mia mbili na hamsini ilikwisha, na pia miaka mia mbili na sitini.

42 Na ikawa kwamba sehemu ya watu waovu walianza tena kuanzisha viapo vya siri na [a]makundi maovu ya siri ya Gadiantoni.

43 Na pia watu ambao waliitwa watu wa Nefi walianza kujisifu katika mioyo yao, kwa sababu ya utajiri wao mwingi, na kuwa bure kama ndugu zao, Walamani.

44 Na kutoka wakati huu wanafunzi walianza kuhuzunika kwa sababu ya [a]dhambi za dunia.

45 Na ikawa kwamba wakati miaka mia tatu ilipokwisha, watu wote wa Nefi na Walamani walikuwa wamepata kuwa waovu sana mmoja akiwa kama mwingine.

46 Na ikawa kwamba wanyang'anyi wa Gadiantoni walitawanyika kote usoni mwa nchi; na hakukuwa wowote waliokuwa wa haki isipokuwa wanafunzi wa Yesu. Na waliweka dhahabu na fedha kwa wingi, na walifanya biashara na aina yote ya bidhaa.

47 Na ikawa kwamba baada ya miaka mia tatu na tano kupita, (na watu walibaki bado kwenye uovu) Amosi alifariki; na kaka yake, Amaroni, aliandika maandishi badala yake.

48 Na ikawa kwamba baada ya miaka mia tatu na ishirini kupita, Amaroni, akilazimishwa na Roho Mtakatifu, alificha [a]maandishi yote matakatifu—ndiyo, hata maandishi yote matakatifu yaliyotolewa kutoka kizazi hadi kizazi, ambayo yalikuwa matakatifu—hata mpaka mwaka wa mia tatu na ishirini tangu kuja kwa Kristo.

49 Na aliyaficha kwa Bwana, kwamba [a]yangekuja tena kwa baki la nyumba ya Yakobo, kulingana na unabii na ahadi za Bwana. Na huo ndiyo mwisho wa maandishi ya Amaroni.

KITABU CHA MORMONI

MLANGO WA 1

Amaroni anamuelemisha Mormoni kuhusu maandishi matakatifu—Vita vinaanza miongoni mwa Wanefi na Walamani—Wale

42*a* MWM Makundi maovu ya siri.

44*a* 3 Ne. 28:9.

48*a* Hel. 3:13, 15–16.

49*a* Eno. 1:13.

Wanefi watatu wanaondelewa—Uovu, kutoamini, uchawi, na ulozi unaenea. Karibia mwaka 321–326 B.K.

NA sasa mimi, [a]Mormoni, ninaandika [b]maandishi ya vitu ambavyo nimeona na kusikia, na kuyaita Kitabu cha Mormoni.

2 Na karibu wakati ambao [a]Amaroni alipoficha maandishi kwa Bwana, alikuja kwangu, (mimi nikiwa na umri wa karibu miaka kumi, na nilianza [b]kujifunza kidogo kulingana na namna ya kujifunza kwa watu wangu) na Amaroni akaniambia: Ninaona kwamba wewe ni mtoto mwenye heshima, na ni mwepesi kwa kusoma;

3 Kwa hivyo, wakati utakuwa karibu na umri wa miaka ishirini na nne ninataka kwamba ukumbuke vitu ambavyo umevichunguza kuhusu hawa watu; na wakati utakuwa na huo umri uende kwa nchi ya Antumu, kwenye kilima ambacho kitaitwa [a]Shimu; na hapo nimeweka kwa ulinzi wa Bwana maandishi yote matakatifu kuhusu hawa watu.

4 Na tazama, utajichukulia [a]mabamba ya Nefi, na yatakayosalia utaacha mahali hapo; na utaandika kwenye mabamba ya Nefi vitu vyote ambavyo utakuwa umeviona kuhusu hawa watu.

5 Na mimi, Mormoni, nikiwa wa kizazi cha [a]Nefi, (na jina la baba yangu lilikuwa Mormoni) nilikumbuka vitu ambavyo Amaroni aliniamuru nifanye.

6 Na ikawa kwamba mimi, nikiwa na miaka kumi na moja, nilibebwa na baba yangu hadi kwenye nchi iliyokuwa kusini, hata kwenye nchi ya Zarahemla.

7 Uso wa nchi yote ulikuwa umefunikwa na majengo, na watu walikuwa wengi, kama vile mchanga wa bahari.

8 Na ikawa katika mwaka huu kukaanza kuwa na vita miongoni mwa Wanefi, ambao walikuwa mkusanyiko wa Wanefi na Wayakobo na Wayusufu na Wazoramu; na hivi vita vilikuwa miongoni mwa Wanefi, na Walamani na Walemueli na Waishmaeli.

9 Sasa Walamani na Walemueli na Waishmaeli waliitwa Walamani, na yale makundi mawili yalikuwa Wanefi na Walamani.

10 Na ikawa kwamba vita vilianza kuwa miongoni mwao kwenye mipaka ya Zarahemla, kando ya maji ya Sidoni.

11 Na ikawa kwamba Wanefi walikuwa wamekusanya pamoja idadi kubwa ya watu, hata kupita idadi ya elfu thelathini. na ikawa kwamba kwenye huu mwaka walikuwa na vita kadhaa, ambazo Wanefi waliwashinda Walamani na waliwaua wengi wao.

12 Na ikawa kwamba Walamani waliondoa kusudi lao, na masikilizano ya amani ya-

1 1*a* MWM Mormoni, Nabii Mnefi.
b 3 Ne. 5:11–18.
2*a* 4 Ne. 1:47–49.
b Mos. 1:3–5.
3*a* Eth. 9:3.
4*a* M. ya Morm. 1:1, 11. MWM Mabamba.
5*a* 3 Ne. 5:12, 20.

kaimarishwa nchini; na amani ikadumu kwa muda wa karibu miaka minne, kwamba hakukuwepo na umwagaji wa damu.

13 Lakini uovu ulienea juu ya uso wa nchi yote, mpaka kwamba Bwana akaondoa wanafunzi wake [a]wapendwa, na kazi ya miujiza na ya uponyaji iliisha kwa sababu ya uovu wa watu.

14 Na hakukuwa na [a]vipawa kutoka kwa Bwana, na [b]Roho Mtakatifu hakumjia yeyote, kwa sababu ya uovu wao na [c]kutoamini kwao.

15 Na mimi, nikiwa na umri wa miaka kumi na mitano na nikiwa kidogo na akili timamu, kwa hivyo nilitembelewa na Bwana, na kuonja na kujua uzuri wa Yesu.

16 Na nilijaribu kuwahubiria watu hawa, lakini mdomo wangu ulifungwa, na nikakatazwa kwamba nisihubiri kwao; kwani tazama walikuwa [a]wameasi makusudi dhidi ya Mungu wao; na wale wanafunzi wapendwa [b]waliondolewa nje ya nchi, kwa sababu ya uovu wao.

17 Lakini nilibaki miongoni mwao, lakini nilikatazwa kuhubiri kwao, kwa sababu ya ugumu wa mioyo; na kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao nchi [a]ililaaniwa kwa sababu yao.

18 Na hawa wanyang'anyi wa Gadiantoni, ambao walikuwa miongoni mwa Walamani, waliingilia nchi, mpaka kwamba wakazi wa pale walianza kuficha [a]hazina zao udongoni; na zikawa zenye kuteleza, kwa sababu Bwana alikuwa amelaani nchi, kwamba hawangeweza kuzishikilia, wala kuziweka tena.

19 Na ikawa kwamba kulikuwa na uchawi, na ulozi, na uganga; na nguvu za yule mwovu zilitumiwa kote usoni mwa nchi, hata kwa kutimiza maneno yote ya Abinadi, na pia Samweli yule Mlamani.

MLANGO WA 2

Mormoni anaongoza majeshi ya Wanefi—Damu na mauaji yanajaa katika nchi—Wanefi wanalia na kuomboleza kwa huzuni ya waliolaaniwa—Siku yao ya neema imeisha—Mormoni anapata mabamba ya Nefi—Vita vinaendelea. Karibia mwaka 327–350 B.K.

Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo kulianza kuwa na vita tena miongoni mwa Wanefi na Walamani. Na ingawaje mimi nikiwa kijana mdogo, nilikuwa mkubwa kwa kimo; kwa hivyo watu wa Nefi walinichagua kwamba niwe kiongozi wao, au kingozi wa majeshi yao.

2 Kwa hivyo ikawa kwamba katika mwaka wangu wa kumi na sita nilienda mbele kuliongoza jeshi la Wanefi, dhidi ya Walamani; kwa hivyo miaka

13 *a* 3 Ne. 28:2, 12.
14 *a* Moro. 10:8–18, 24.
b MWM Roho Mtakatifu.
c MWM Kutoamini.
16 *a* MWM Uasi.
b Morm. 8:10.
17 *a* 2 Ne. 1:7; Alma 45:10–14, 16.
18 *a* Hel. 13:18–20; Eth. 14:1–2.

mia tatu na ishirini na sita ilikuwa imepita.

3 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na ishirini na saba Walamani walitushambulia kwa nguvu nyingi sana, mpaka kwamba wakayatisha majeshi yangu; kwa hivyo hawangepigana, na walianza kurudi nyuma kuelekea nchi za kaskazini.

4 Na ikawa kwamba tulifika mji wa Angola, na tukaumiliki mji huo, na kufanya matayarisho kujilinda dhidi ya Walamani. Na ikawa kwamba tuliimarisha mji kwa nguvu zetu; lakini injapokuwa kuimarika kwetu Walamani walitushambulia na wakatufukuza hadi nje ya nchi.

5 Na walitukimbiza pia kutoka nchi ya Daudi.

6 Na tulienda mbele na tukafika nchi ya Yoshua, ambayo ilikuwa kwenye mipaka ya magharibi kando ya bahari.

7 Na ikawa kwamba tulikusanya watu wetu kwa haraka iwezekanavyo, ili tungewakusanya pamoja katika kundi moja.

8 Lakini tazama, nchi ilikuwa imejaa wanyang'anyi na Walamani; na ingawaje kulikuwa na uharibifu mwingi ambao ulining'inia juu ya watu wangu, hawakutubu vitendo vyao viovu; kwa hivyo kulikuwa na usambazaji wa mauaji na maangamizo kote usoni mwa nchi, kote kwenye sehemu ya Wanefi na pia kwenye sehemu ya Walamani; na ulikuwa upinduzi mmoja mkuu kote usoni mwa nchi.

9 Na sasa, Walamani walikuwa na mfalme, na jina lake lilikuwa Haruni; na alitushambulia na jeshi la elfu arubaini na nne. Na tazama, nilimzuia na watu elfu arubaini na mbili. Na ikawa kwamba nilimpiga na jeshi langu kwamba alitoroka mbele yangu. Na tazama, haya yote yalifanyika, na miaka mia tatu na thelathini ikawa imekwisha.

10 Na ikawa kwamba Wanefi walianza kutubu dhambi zao, na wakaanza kulalamika hata kama ilivyotabiriwa na nabii Samweli; kwani tazama hakuna mtu ambaye aliweza kuweka ile ambayo ilikuwa yake, kwa sababu ya wezi, na wanyang'anyi, na wauaji, na ustadi wa uganga, na uchawi ambao ulikuwa katika nchi.

11 Hivyo kulianza kuwa na maombolezo na kulia katika nchi kwa sababu ya vitu hivi, na hasa zaidi miongoni mwa watu wa Nefi.

12 Na ikawa kwamba baada ya mimi, Mormoni, kuona kilio chao na maombolezo yao na huzuni yao mbele ya Bwana, moyo wangu ulianza kufurahi ndani yangu, kwa sababu nilijua huruma na uvumilivu wa Bwana, kwa hivyo nikidhani kwamba atakuwa na huruma kwao kwamba wangekuwa watu wa haki tena.

13 Lakini tazama hii shangwe yangu ilikuwa bure, kwani hii "huzuni yao haikuwa ya toba,

2 13*a* 2 Kor. 7:10; Alma 42:29.

kwa sababu ya uzuri wa Mungu; lakini ilikuwa sana huzuni ya [b]waliolaaniwa, kwa sababu Bwana hakuwaruhusu [c]kufurahi katika dhambi.

14 Na hawakuja kwa Yesu na [a]mioyo iliyovunjika na roho zilizopondeka, lakini [b]walimlaani Mungu, na wakataka kufa. Hata hivyo wangepigana wakitumia upanga kwa maisha yao.

15 Na ikawa kwamba huzuni yangu ilinirudia tena, na niliona kwamba [a]siku ya [b]neema [c]ilikuwa imepita na wao, kimwili pamoja na kiroho; kwani niliona maelfu wakiangushwa chini kwenye uasi wa wazi dhidi ya Mungu wao, na kurundikwa kama fungu la mbolea juu ya uso wa nchi. Na hivyo miaka mia tatu na arobaini na minne ilikuwa imepita.

16 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na hamsini na tano Wanefi walianza kutoroka mbele ya Walamani; na walifuatwa mpaka walipofika hata kwenye nchi ya Yashoni, kabla ya kuwezekana kuwazuia katika kukimbia kwao.

17 Na sasa, mji wa Yashoni ulikuwa karibu na [a]nchi ambayo Amaroni alikuwa ameficha maandishi kwa Bwana, ili yasiharibiwe. Na tazama nilikuwa nimeenda kulingana na neno la Amaroni, na kuchukua mabamba ya Nefi, na niliandika kulingana na maneno ya Amaroni.

18 Na niliandika juu ya mabamba ya Nefi nakili kamili ya uovu na machukizo yote; lakini kwenye [a]mabamba haya nilijizuia kuweka nakili kamili ya uovu wao na machukizo, kwani tazama, mfululizo wa kuonekana kwa uovu na machukizo umekuwa mbele ya macho yangu tangu nitoshee kuona mwenendo wa binadamu.

19 Na ole kwangu kwa sababu ya uovu wao; kwani moyo wangu umejawa na huzuni kwa sababu ya uovu wao, maisha yangu yote; walakini, ninajua kwamba [a]nitainuliwa juu katika siku ya mwisho.

20 Na ikawa kwamba katika mwaka huu watu wa Nefi waliwindwa na kukimbizwa. Na ikawa kwamba tulikimbizwa mbele mpaka tulipofika kaskazini kwa nchi ambayo iliitwa Shemu.

21 Na ikawa kwamba tuliimarisha mji wa Shemu, na tuliwakusanya humo watu wetu kadri ilivyowezekana, ili labda tungewaokoa kutoka kwenye maangamizo.

22 Na ikawa katika mwaka wa mia tatu na arubaini na sita walianza kutushambulia tena.

23 Na ikawa kwamba niliwazungumzia watu wangu, nikiwasihi kwa juhudi kuu, kwamba wasimame kwa ujasiri mbele ya Walamani na [a]kupigana kwa ajili ya wake zao, na

13 *b* MWM Hukumu.
c Alma 41:10.
14 *a* MWM Moyo Uliovunjika.
b MWM Kukufuru, Kufuru.
15 *a* Hel. 13:38.
b MWM Neema.
c Yer. 8:20; M&M 56:16.
17 *a* Morm. 1:1–4.
18 *a* MWM Mabamba.
19 *a* Mos. 23:22; Eth. 4:19.
23 *a* Mos. 20:11; Alma 43:45.

watoto wao, na nyumba zao, na miji yao.

24 Na maneno yangu yaliwaamsha kidogo kuwa na nguvu, mpaka kwamba hawakukimbia kutoka mbele ya Walamani, lakini walisimama kwa ujasiri dhidi yao.

25 Na ikawa kwamba tulikabiliana na jeshi la elfu thelathini dhidi ya jeshi la elfu hamsini. Na ikawa kwamba tuliwazuia na uthabiti hivyo kwamba walikimbia kutoka mbele yetu.

26 Na ikawa kwamba baada ya kukimbia tuliwafuata na majeshi yetu, na tulipigana na wao tena, na tukawashinda; walakini nguvu za Bwana hazikuwa nasi; ndiyo, tuliachwa peke yetu, kwamba Roho wa Bwana haikuwa nasi; kwa hivyo tulikuwa tumekuwa wanyonge kama ndugu zetu.

27 Na moyo wangu ulihuzunika kwa sababu ya huu msiba mkubwa wa watu wangu, kwa sababu ya uovu wao na machukizo yao. Lakini tazama, tulienda mbele dhidi ya Walamani na wale wanyang'anyi wa Gadiantoni, mpaka, tulipokuwa tena tumeimiliki nchi ya urithi wetu.

28 Na mwaka wa mia tatu na arubaini na tisa ukawa umepita. Na katika mwaka wa mia tatu na hamsini tuliweka mkataba na Walamani na wanyang'anyi wa Gadiantoni, ambamo tulipata nchi zetu za urithi kugawanywa.

29 Na Walamani walitupatia nchi ya upande wa kaskazini, ndiyo, hata [a]njia nyembamba iliyoelekea nchi ya kusini. Na tukawapatia Walamani nchi yote ya kusini.

MLANGO WA 3

Mormoni anawasihi Wanefi watubu—Wanapata ushindi mkuu na kujisifu kwa nguvu zao—Mormoni anakataa kuwaongoza, na sala zake kwa niaba yao hazina imani—Kitabu cha Mormoni kinawakaribisha makabila kumi na mawili ya Israeli kuamini injili. Karibia mwaka 360–362 B.K.

Na ikawa kwamba Walamani hawakutushambulia tena hadi miaka kumi ilipopita. Na tazama, nilikuwa nimeweka watu wangu, Wanefi, kwenye kazi, katika kutayarisha nchi yao na silaha zao dhidi ya wakati wa vita.

2 Na ikawa kwamba Bwana alisema kwangu: Walilie watu hawa—Tubuni ninyi, na mje kwangu, na mbatizwe, na mjenge tena kanisa langu, na mtasamehewa.

3 Na niliwahubiria hawa watu, lakini ilikuwa bure; na hawakufahamu kwamba Bwana ndiye aliyewarehemu, na kuwapatia nafasi ya kutubu. Na tazama walishupaza mioyo yao dhidi ya Bwana Mungu wao.

4 Na ikawa kwamba baada ya huu mwaka wa kumi kuisha, ikiwa, jumla ya miaka yote pamoja, mia tatu na sitini kutoka kuja kwa Kristo, mfalme

29*a* Alma 22:32.

wa Walamani alinitumia barua, ambayo ilinieleza kwamba walikuwa wanajitayarisha kuja kupigana dhidi yetu tena.

5 Na ikawa kwamba nilisababisha kwamba watu wangu wajikusanye pamoja katika nchi ya Ukiwa, kwa mji uliokuwa mipakani, kando ya njia nyembamba ambayo ilielekea katika nchi iliyokuwa upande wa kusini.

6 Na hapo tuliweka majeshi yetu, ili tuyazuie majeshi ya Walamani, kwamba wasimiliki yoyote ya nchi zetu; kwa hivyo tulijiimarisha dhidi yao na majeshi yetu yote.

7 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na sitini na moja Walamani walikuja chini kwenye mji wa Ukiwa kupigana nasi; na ikawa kwamba katika mwaka huo tuliwashinda, mpaka kwamba walirejea kwenye nchi zao tena.

8 Na katika mwaka wa mia tatu na sitini na mbili walikuja chini tena kupigana. Na tuliwashinda tena, na kuua idadi yao kubwa, na wafu wao walitupwa baharini.

9 Na sasa, kwa sababu ya kitu hiki kikubwa ambacho watu wangu, Wanefi, walikuwa wamefanya, walianza [a]kujisifu kwa nguvu zao, na walianza kuapa kwa mbingu kwamba watajilipizia kisasi kwa damu ya ndugu zao ambao walikuwa wameuawa na maadui zao.

10 Na waliapa kwa mbingu, na pia kwa kiti cha enzi cha Mungu, kwamba [a]wataenda juu kupigana dhidi ya maadui zao, na kuwaangamiza kabisa kutoka uso wa nchi.

11 Na ikawa kwamba mimi, Mormoni, nilikataa kabisa kutokea wakati huu kwenda mbele kuwa amiri jeshi na kiongozi wa hawa watu, kwa sababu ya uovu wao na machukizo yao.

12 Tazama, nilikuwa nimewaongoza, ijapokuwa uovu wao, nilikuwa nimewaongoza mara nyingi vitani, na niliwapenda, kulingana na [a]upendo wa Mungu ambao ulikuwa ndani yangu, na moyo wangu wote; na nafsi yangu ilikuwa imewekwa kwa sala kwa Mungu wangu siku yote nzima kwa ajili yao; walakini, ilikuwa [b]bila imani, kwa sababu ya kushupaza mioyo yao.

13 Na mara tatu nimewaokoa kutoka mikononi mwa maadui zao, na hawajatubu dhambi zao.

14 Na baada ya kuapa na yote ambayo [a]walikatazwa na Bwana wetu na Mwokozi Yesu Kristo, kwamba wangeenda kwenye maadui wao ili wapigane, na kujilipizia kisasi kwa damu ya ndugu zao, tazama sauti ya Bwana ilinijia, ikisema:

15 Kulipiza [a]kisasi ni kwangu, na [b]nitalipa; na kwa sababu hawa watu hawakutubu baada ya mimi kuwakomboa, tazama, wataangamizwa kutoka kwa uso wa dunia.

16 Na ikawa kwamba nilikataa

3 9*a* 2 Ne. 4:34.
10*a* 3 Ne. 3:20–21; Morm. 4:4.
12*a* MWM Upendo.
b Morm. 5:2.
14*a* 3 Ne. 12:34–37.
15*a* MWM Kisasi.
b M&M 82:23.

kabisa kwenda juu dhidi ya maadui zangu; na nilifanya hata vile Bwana alivyoniamuru; na nilisimama kama shahidi mzembe kushuhudia kwa ulimwengu vitu ambavyo niliona na kusikia, kulingana na ushuhuda wa Roho ambayo ilikuwa imeshuhudia kwa vitu vijavyo.

17 Kwa hivyo naandika kwenu, Wayunani, na pia [a]kwenu, nyumba ya Israeli, wakati kazi itakapoanza, kwamba mtakuwa karibu kujitayarisha kurudi kwenye nchi ya urithi wenu;

18 Ndiyo, tazama, nawaandikia wote wanaoishi ulimwenguni; ndiyo, kwenu, makabila kumi na mawili ya Israeli, ambao [a]mtahukumiwa kwa vitendo vyenu na wale kumi na wawili ambao Yesu aliwachagua kuwa wanafunzi wake katika nchi ya Yerusalemu.

19 Na pia nawaandikia baki la watu hawa, ambao pia watahukumiwa na wale [a]kumi na wawili ambao Yesu aliwachagua katika nchi hii; na watahukumiwa na wale kumi na wawili ambao Yesu aliwachagua katika nchi ya Yerusalemu.

20 Na vitu hivi Roho amenifunulia; kwa hivyo ninawaandikia ninyi nyote. Na kwa sababu hii ninaandika kwenu, ili mjue kwamba lazima nyote msimame mbele ya kiti cha [a]hukumu cha Kristo, ndiyo, kila nafsi ambayo ni ya [b]ukoo wa mwanadamu ya Adamu; na lazima msimame kuhukumiwa kwa yale matendo yenu, ikiwa yatakuwa kama mema au maovu;

21 Na pia kwamba [a]mngeamini injili ya Yesu Kristo, ambayo mtapata miongoni mwenu; na pia kwamba [b]Wayahudi, watu wa agano la Bwana, watakuwa na [c]ushahidi mwingine juu ya yule ambaye wamemwona na kumsikiliza, kwamba Yesu, ambaye walimuua, alikuwa ni [d]Kristo yule yule na Mungu yule yule.

22 Na ningetaka kwamba ningeweza kushawishi [a]kila mtu aishiye duniani atubu na ajitayarishe kusimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo.

MLANGO WA 4

Vita na mauaji vinaendelea—Wale waovu wanawaadhibu wale walio waovu—Uovu mkuu unaenea kuliko mbeleni katika Israeli yote—Wanawake na watoto wanatolewa kafara kwa sanamu—Walamani wanaanza kuwaangamiza Wanefi walio mbele yao. Karibia mwaka 363–375 B.K.

Na sasa ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na sitini na tatu Wanefi walienda na majeshi yao kupigana dhidi ya Walamani, kutoka nchi ya Ukiwa.

2 Na ikawa kwamba majeshi ya Wanefi yalilazimishwa

17 *a* 2 Ne. 30:3–8; 3 Ne. 29:1.
18 *a* Mt. 19:28; Lk. 22:29–30; M&M 29:12.
19 *a* 1 Ne. 12:9–10.
20 *a* MWM Hukumu ya mwisho.
b M&M 27:11.
21 *a* M&M 3:20.
b MWM Wayahudi.
c 2 Ne. 25:18.
d 2 Ne. 26:12; Mos. 7:27.
22 *a* Alma 29:1.

kurudi nyuma hadi kwenye nchi ya Ukiwa. Na wakati walikuwa bado wamechoka, jeshi lenye nguvu la Walamani liliwashambulia; na walikuwa na vita vibaya, mpaka kwamba Walamani walimiliki mji wa Ukiwa, na waliwachinja Wanefi wengi, na walichukua wengi wao kuwa wafungwa.

3 Na waliosalia walikimbia na kujiunga na wakazi wa mji wa Teankumu. Sasa mji wa Teankumu ulikuwa kwenye mipaka ya ukingo wa bahari; na ulikuwa pia karibu na mji wa Ukiwa.

4 Na ilikuwa kwa [a]sababu jeshi la Wanefi lilishambulia Walamani kwamba walianza kuuawa; kwani kama hawangefanya hivyo, Walamani hawangekuwa na uwezo juu yao.

5 Lakini, tazama, hukumu za Mungu zitashinda uovu; na ni kwa kupitia kwa waovu kwamba waovu [a]huadhibiwa; kwani ni waovu ambao huchochea mioyo ya watoto wa watu hadi kwenye umwagaji wa damu.

6 Na ikawa kwamba Walamani walifanya mipango ya kushambulia mji wa Teankumu.

7 Na ikawa katika mwaka wa mia tatu na sitini na nne Walamani walishambulia mji wa Teankumu, ili wamiliki mji wa Teankumu pia.

8 Na ikawa kwamba walisukumwa na kurudishwa nyuma na Wanefi. Na baada ya Wanefi kuona kwamba wamewakimbiza Walamani walijisifu tena kwa nguvu zao; na wakaenda mbele na uwezo wao wenyewe, na kukamata tena mji wa Ukiwa.

9 Na sasa vitu hivi vyote vilikuwa vimefanyika, na kulikuwa na maelfu waliouawa kwa pande zote mbili, miongoni mwa Wanefi na miongoni mwa Walamani.

10 Na ikawa kwamba mwaka wa mia tatu na ishirini na sita ukawa umepita, na Walamani walikuja tena kwa Wanefi ili wapigane; na bado Wanefi hawakutubu maovu waliyofanya, lakini waliendelea na maovu yao siku zote.

11 Na ni vigumu kwa ulimi kueleza, au kwa mtu kuandika maelezo kamili ya hofu iliyoonekana ya damu na mauaji ambayo yalikuwa miongoni mwa watu, upande wa Wanefi na upande wa Walamani, na kila moyo ulishupazwa, kwamba walifurahia umwagaji wa damu siku zote.

12 Na kulikuwa hakujakuwa na [a]uovu mkuu kama huu miongoni mwa kizazi cha Lehi, wala hata miongoni mwa nyumba ya Israeli, kulingana na maneno ya Bwana, vile ilipokuwa miongoni mwa watu hawa.

13 Na ikawa kwamba Walamani walimiliki mji wa Ukiwa, na hii ni kwa sababu [a]idadi yao ilizidi ya Wanefi.

14 Na walisonga mbele pia dhidi ya mji wa Teankumu, na kulazimisha wakazi wake kuondoka nje, na wakachukua wafungwa wengi wanawake

4 4*a* Morm. 3:10.
5*a* M&M 63:33.
12*a* Mwa. 6:5; 3 Ne. 9:9.
13*a* Morm. 5:6.

pamoja na watoto, na kuwaua kama kafara kwa [a]sanamu zao za kuabudu.

15 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na sitini na saba, Wanefi wakiwa wamekasirika kwa sababu ya Walamani kutoa kafara wake zao na watoto wao, kwamba walienda dhidi ya Walamani kwa hasira kubwa sana, hadi kwamba waliwapiga Walamani tena, na kuwafukuza kutoka nchi zao.

16 Na Walamani hawakuwashambulia Wanefi mpaka mwaka wa mia tatu na sabini na tano.

17 Na katika mwaka huu walikuja chini dhidi ya Wanefi kwa uwezo wao wote; na hawangehesabika kwa sababu ya ukubwa wa idadi yao.

18 Na [a]kutokea wakati huu kwenda mbele Wanefi hawakuwa na uwezo wowote juu ya Walamani, lakini walianza kuangamizwa na hao vile umande huwa mbele ya jua.

19 Na ikawa kwamba Walamani walishambulia mji wa Ukiwa; na kukawa na vita vikali sana vilivyopiganwa katika nchi ya Ukiwa, ambamo walishinda Wanefi.

20 Na walitoroka tena kutoka kwao, na kufikia mji wa Boazi; na hapo walizuia Walamani kwa ujasiri mkubwa, mpaka kwamba Walamani hawakushinda mpaka waliporudi tena mara ya pili.

21 Na baada ya kurudi mara ya pili, Wanefi walikimbizwa na kuchinjwa na mauaji makuu; wanawake wao na watoto wao walitolewa kafara tena kwa sanamu.

22 Na ikawa kwamba Wanefi walikimbia tena kutoka kwao, na wakasababisha wakazi wote kuandamana nao kote, mijini na vijijini.

23 Na sasa mimi, Mormoni, nilipoona kwamba Walamani wako karibu kuchukua nchi, kwa hivyo nilienda kwenye kilima cha [a]Shimu, na kuyachukua maandishi yote ambayo Amaroni alikuwa ameyaficha kwa Bwana.

MLANGO WA 5

Mormoni tena anayaongoza majeshi ya Wanefi katika vita vya damu na mauaji—Kitabu cha Mormoni kitakuja mbele kusadikisha Israeli yote kwamba Yesu ni Kristo—Kwa sababu ya kutoamini kwao, Walamani watatawanyika, na Roho itawaacha kukaa nao—Watapokea injili kutoka kwa Wayunani katika siku za baadaye. Karibia mwaka 375–384 B.K.

Na ikawa kwamba nilienda mbele miongoni mwa Wanefi, na kugeuza kile [a]kiapo ambacho nilikuwa nimefanya kwamba sitawasaidia; na wakanifanya amiri jeshi tena wa majeshi yao, kwani walinitazamia kama ningewakomboa kutoka kwa mateso yao.

2 Lakini tazama, [a]sikuwa na tumaini, kwani nilijua hukumu ya Bwana ambayo ingekuja juu

14*a* MWM Kuabudu sanamu.
18*a* Morm. 3:3.
23*a* Morm. 1:3.
5 1*a* Morm. 3:11.
2*a* Morm. 3:12.

yao; kwani hawakutubu uovu wao, lakini walipigania maisha yao bila kumlingana Yule ambaye aliwaumba.

3 Na ikawa kwamba Walamani walitushambulia vile tulivyokuwa tumekimbilia mji wa Yordani; lakini tazama, walifukuzwa na kurudishwa nyuma kwamba hawakukamata ule mji wakati huo.

4 Na ikawa kwamba walitushambulia tena, na tulihifadhi mji. Na kulikuwa na miji mingine pia ambayo ilihifadhiwa na Wanefi, ambayo ngome zao ziliwazuilia mbali kwamba hawangeingia nchi ambayo ilikuwa mbele yetu, ili wawaangamize wakazi wa nchi yetu.

5 Lakini ikawa kwamba nchi yoyote ambayo tulipitia karibu, ambayo wakazi hawakuwa wamejiunga nasi, waliangamizwa na Walamani, na miji yao, na vijiji vyao, na miji yao mikuu ilichomwa kwa moto; na hivyo miaka mia tatu na sabini na tisa ilipita mbali.

6 Na ikawa kwamba katika mwaka wa mia tatu na themanini Walamani walikuja tena dhidi yetu ili kupigana, na tuliwazuia kwa ujasiri; lakini yote ilikuwa bure, kwani idadi yao ilikuwa kubwa sana kwamba waliwakanyaga watu wa Wanefi chini ya miguu yao.

7 Na ikawa kwamba tulikimbia tena, na wale ambao ukimbizi wao ulikuwa wa upesi kuliko Walamani waliokoka, na wale ambao ukimbizi wao haukushinda Walamani walikatiwa chini na kuangamizwa.

8 Na sasa tazama, mimi, Mormoni, sitaki kuharibu roho za watu kwa kuwaelezea mambo ya kutisha ya damu na mauaji kama ilivyoonekana machoni mwangu; lakini mimi, nikijua kwamba vitu hivi lazima vidhihirishwe kujulikana, na kwamba vitu vyote ambavyo vimefichwa lazima [a]vifichuliwe wazi—

9 Na pia kwamba ufahamu wa vitu hivi lazima [a]ujie baki la watu hawa, na pia kwa Wayunani, ambao Bwana amesema [b]watawatawanya hawa watu, na watu hawa wahesabiwe kama bure miongoni mwao—kwa hivyo naandika [c]ufupisho mdogo, bila ya kuthubutu kutoa historia ya vitu ambavyo nimeona, kwa sababu ya amri ambayo nimepokea, na pia kwamba msiwe na huzuni nyingi sana kwa sababu ya uovu wa watu hawa.

10 Na sasa tazama, haya ninauzungumzia uzao wao, na pia kwa Wayunani ambao watakuwa na utunzaji kwa nyumba ya Israeli, ambao wanafahamu na kujua ni wapi baraka zao hutoka.

11 Kwani ninajua kwamba hao watahuzunika kwa msiba wa nyumba ya Israeli; ndiyo, watahuzunika kwa uharibifu wa hawa watu; watahuzunika kwamba watu hawa walikuwa hawajatubu ili wangekumbatiwa katika mikono ya Yesu.

8*a* Lk. 12:2–3; 2 Ne. 27:11; M&M 1:3.
9*a* 4 Ne. 1:49.
b 3 Ne. 16:8.
c Morm. 1:1.

12 Sasa [a]vitu hivi vimeandikiwa [b]baki la nyumba ya Yakobo; na vimeandikwa kwa njia hii, kwa sababu inafichuliwa kutoka kwa Mungu kwamba hawatajua kupitia kwa maovu; na sharti [c]zifichwe kwa Bwana ili zije mbele katika muda wao.

13 Na hii ni amri ambayo nimepokea; na tazama, vitakuja mbele kulingana na amri ya Bwana, wakati ataona inafaa, katika hekima yake.

14 Na tazama, vitaenda kwa wale [a]Wayahudi wasioamini; na kwa kusudi hili wataenda—ili [b]washawishwe kwamba Yesu ndiye Kristo, Mwana wa Mungu aishiye; kwamba Baba angetimiza, kupitia kwa Mpendwa wake, mpango wake mkuu na wa milele, kwa kuwarudisha Wayahudi, au nyumba yote ya Israeli, kwa nchi yao ya urithi, ambayo Bwana Mungu wao amewapatia, kwa kutimiza [c]agano lake;

15 Na pia kwamba uzao wa [a]watu hawa ungeamini kabisa injili yake, ambayo [b]itaenda mbele yao kutoka kwa Wayunani; kwani hawa watu [c]watatawanywa, na [d]watakuwa weusi, wachafu, na watu wa kuchukiza, nje ya mipaka ya maelezo ambayo yamewahi kuweko miongoni mwetu, ndiyo, hata ile ambayo imekuweko miongoni mwa Walamani, na hii ni kwa sababu ya kutoamini kwao na ibada ya sanamu.

16 Kwani tazama, Roho wa Bwana imekoma [a]kuwasaidia babu zao; na wako bila Kristo na Mungu katika ulimwengu; na wanapeperushwa kama [b]vumbi litimuliwalo mbele ya kibunga.

17 Walikuwa wakati mmoja watu wa kupendeza, na walikuwa na Kristo kama [a]mchungaji wao; ndiyo, walikuwa wanaongozwa hata na Mungu Baba.

18 Lakini sasa, tazama, [a]wanaongozwa na Shetani, hata vile vumbi litimuliwalo mbele ya kimbunga, au vile jahazi linavyorushwarushwa juu ya mawimbi, bila tanga wala nanga, au bila kitu chochote cha kuiendesha; na vile ilivyo, ndivyo walivyo.

19 Na tazama Bwana amewawekea baraka, ambazo wangepokea katika nchi, kwa [a]Wayunani ndiyo watakaoimiliki nchi.

20 Lakini tazama, itakuwa kwamba watakimbizwa na kutawanywa na Wayunani; na baada ya kukimbizwa na kutawanywa na Wayunani, tazama, ndipo Bwana [a]atakumbuka [b]agano ambalo alifanya kwa

12*a* Eno. 1:16; Hel. 15:11–13. MWM Kitabu cha Mormoni.
b M&M 3:16–20.
c Morm. 8:4, 13–14; Moro. 10:1–2.
14*a* 2 Ne. 29:13; 30:7–8. MWM Wayahudi.
b 2 Ne. 25:16–17.
c 3 Ne. 29:1–3.
15*a* 3 Ne. 21:3–7, 24–26.
b 1 Ne. 13:20–29, 38; Morm. 7:8–9.
c 1 Ne. 10:12–14; 3 Ne. 16:8.
d 2 Ne. 26:33. Eth. 2:15.
16*a* Mwa. 6:3; *b* Zab. 1:4.
17*a* MWM Mchungaji Mwema.
18*a* 2 Ne. 28:21.
19*a* 3 Ne. 20:27–28.
20*a* 3 Ne. 16:8–12.
b MWM Agano la Ibrahimu.

Ibrahimu na kwenye nyumba yote ya Israeli.

21 Na pia Bwana atakumbuka [a]sala za wenye haki, ambazo zimetolewa kwake kwa minajili yao.

22 Na ikiwa hivyo, Ee ninyi Wayunani, mtawezaje kusimama mbele ya uwezo wa Mungu, isipokuwa mtubu na kugeuka kutoka njia zenu mbovu?

23 Je, hamjui kwamba mko mikononi mwa Mungu? Je, hamjui kwamba anao uwezo wote, na kwa [a]amri yake kuu dunia [b]itakunjwa pamoja kama karatasi?

24 Kwa hivyo, tubuni ninyi, na mjinyenyekeze mbele yake, isije, atakuja nje katika haki dhidi yenu—isije baki la uzao wa Yakobo itaenda mbele miongoni mwenu kama [a]simba, na kuwararua vipande vipande, na hakuna atakayewaokoa.

MLANGO WA 6

Wanefi wanajikusanya kwenye nchi ya Kumora kwa vita vya mwisho—Mormoni anaficha maandishi matakatifu katika kilima cha Kumora—Walamani wanashinda, na taifa la Wanefi linaangamizwa—Mamia ya maelfu wanachinjwa kwa upanga. Karibia mwaka 385 B.K.

Na sasa ninamaliza maandishi yangu kuhusu [a]kuangamizwa kwa watu wangu, Wanefi. Na ikawa kwamba tulienda kutoka mbele ya Walamani.

2 Na mimi, Mormoni, niliandika barua kwa mfalme wa Walamani, na kumwuliza kwamba angetukubalia kwamba tukusanye watu wetu pamoja kwenye [a]nchi ya Kumora, kando na kilima kilichoitwa Kumora, na hapo tungepigana nao.

3 Na ikawa kwamba mfalme wa Walamani alinikubalia kitu ambacho nilitaka.

4 Na ikawa kwamba tulienda mbele hadi kwenye nchi ya Kumora, na tukapiga hema zetu kuzunguka karibu na kilima Kumora; na ilikuwa katika nchi ya maji mengi, mito, na visima; na hapa tulikuwa na tumaini la kufaidika juu ya Walamani.

5 Na baada ya miaka mia tatu na themanini na nne kupita, tulikuwa tumekusanya watu wote waliosalia kwenye nchi ya Kumora.

6 Na ikawa kwamba baada ya kuwakusanya watu wetu wote pamoja katika nchi ya Kumora, tazama mimi, Mormoni, nilianza kuzeeka; na nikijua kwamba ni juhudi ya mwisho ya watu wangu, na nikiwa nimeamriwa na Bwana kwamba nisiyaache maandishi ambayo yametolewa kutoka zamani na babu zetu, ambayo ni matakatifu, kuchukuliwa na Walamani, (kwani Walamani wangeyaharibu) kwa hivyo nilitengeneza [a]maandishi haya kutoka kwenye mabamba ya Nefi, na [b]nikayaficha

21 *a* Eno. 1:12–18; Morm. 9:36–37.
23 *a* Hel. 12:8–17.
b 3 Ne. 26:3.
24 *a* Mik. 5:8; 3 Ne. 20:15–16.
6 1 *a* 1 Ne. 12:19; Yar. 1:10; Alma 45:9–14; Hel. 13:5–11.
2 *a* Eth. 9:3.
6 *a* MWM Mabamba.
b Eth. 15:11.

katika kilima cha Kumora maandishi yote ambayo yalikuwa yamekabidhiwa kwangu na mkono wa Bwana, isipokuwa mabamba [c]haya chache ambayo nilimpatia mwana wangu [d]Moroni.

7 Na ikawa kwamba watu wangu, na wake zao na watoto wao, sasa waliona [a]majeshi ya Walamani yakisonga kuwaelekea; na kwa ule woga wa kutisha wa kifo ambao unajaa vifua vya waovu wote, walingoja washambuliwe.

8 Na ikawa kwamba walikuja kupigana dhidi yetu, na kila nafsi ilijawa na hofu kwa sababu ya wingi wa idadi yao.

9 Na ikawa kwamba walishambulia watu wangu kwa panga, na kwa pinde, na kwa mshale, na kwa shoka, na kwa kila aina ya silaha za vita.

10 Na ikawa kwamba watu wangu waliangushwa chini, ndiyo, hata elfu wangu kumi ambao walikuwa na mimi, na nilijeruhiwa nikaanguka katikati; na walipita kando yangu kwamba hawakumaliza maisha yangu.

11 Na baada ya kupita na kuangusha chini watu wangu [a]wote isipokuwa sisi ishirini na wanne, (miongoni ambamo kulikuwa na mwana wangu Moroni) na sisi tukiwa tumenusurika kifo cha watu wetu, tulitazamia kesho yake baada ya Walamani kurudi kwenye vituo vyao, kutoka juu ya kilima Kumora, wale watu wangu elfu kumi ambao waliangushwa chini, wakiwa wameongozwa mbele na mimi.

12 Na pia tuliona wale elfu kumi ambao waliongozwa na mwana wangu Moroni.

13 Na tazama, elfu kumi wa Gidgidona walikuwa wameanguka, na yeye pia akiwa katikati.

14 Na Lama alikuwa ameanguka na wale wake elfu kumi; na Gilgali alikuwa ameanguka na wale wake elfu kumi; na Limha alikuwa ameanguka na wale wake elfu kumi; na Yeneumu alikuwa ameanguka na wale wake elfu kumi; na Kumeniha, na Moroniha, na Antionumu, na Shiblomu, na Shemu, na Yoshi, walikuwa wameanguka kila mmoja na wale wao elfu kumi.

15 Na ikawa kwamba kulikuwa na kumi zaidi walioanguka kwa upanga, kila mmoja na elfu kumi wao; ndiyo, hata watu wangu [a]wote, isipokuwa wale ishirini na wanne waliokuwa na mimi, na pia wachache waliotorokea nchi za kusini, na wachache ambao walikimbia hadi kwa Walamani, walikuwa wameanguka; na miili yao, na mifupa, na damu vilitapakaa juu ya uso wa nchi, wakiwa wameachwa na wale ambao waliwachinja kuozea juu ya udongo, na kugeuka mavumbi na kurudi kwenye udongo walikotoka.

16 Na nafsi yangu ilipasuka kwa uchungu, kwa sababu ya

6 *c* M. ya Morm. 1:2.
d Morm. 8:1.
7 *a* 1 Ne. 12:15.
11 *a* 1 Ne. 12:19–20; Hel. 15:17.
15 *a* Alma 9:24.

mauaji ya watu wangu, na nililia:

17 Ee ninyi wenye umbo nzuri, ilikuwaje mkatoka kwenye njia ya Bwana! Ee ninyi wenye umbo nzuri, ilikuwaje mkamkataa Yesu, ambaye aliwangojea na mikono wazi kuwapokea!

18 Tazama, kama hamngefanya hivi, hamngekufa. Lakini tazama, mmekufa, na ninaomboleza kupotea kwenu.

19 Ee ninyi wana wa umbo nzuri, ninyi baba na mama, ninyi mabwana na wake, ninyi walio wazuri, vipi kwamba mmekufa!

20 Lakini tazama, mmetokomea, na huzuni yangu haiwezi kuwarejesha.

21 Na wakati unakuja upesi kwamba miili yenu yenye kufa itajivika kutokufa, na miili hii ambayo sasa inaoza kimwili lazima upesi itakuwa [a]isiyooza; na hapo lazima mtasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, kuhukumiwa kulingana na vitendo vyenu; na ikiwa kwamba ninyi ni wenye haki, hasi mmebarikiwa na babu zenu ambao wamekufa mbele yenu.

22 Ee ingekuwa kwamba mlitubu kabla ya hili angamizo kuja kwenu. Lakini tazama, mmekufa, na Baba, ndiyo, Baba wa Milele wa mbinguni, anajua hali zenu; na anawafanyia kulingana na [a]haki na [b]rehema yake.

MLANGO WA 7

Mormoni anawaalika Walamani wa siku za mwisho kuamini katika Kristo, waikubali injili Yake, na waokolewe—Wote wanaoiamini Biblia pia wataamini Kitabu cha Mormoni. Karibia mwaka 385 B.K.

Na sasa, tazama, nataka kuzungumza machache kwa [a]baki la watu hawa ambao wameachiliwa, ikiwa Mungu atawapatia maneno yangu, ili wajue kuhusu vitu vya baba zao; ndiyo, ninawazungumzia, ninyi baki la nyumba ya Israeli; na haya ndiyo maneno ambayo ninasema:

2 Nataka mjue kwamba ninyi ni wa [a]nyumba ya Israeli.

3 Nataka mjue kwamba lazima mtubu, au hamtaokolewa.

4 Nataka mjue kwamba lazima muweke chini silaha za vita, na msifurahie tena katika umwagaji wa damu, na msizichukue tena, isipokuwa kama Mungu atawaamuru.

5 Nataka mjue kwamba lazima [a]muelimike kuhusu babu zenu, na mtubu dhambi zenu zote na maovu, na [b]kuamini katika Yesu Kristo, kwamba yeye ni Mwana wa Mungu, na kwamba aliuawa na Wayahudi, na kwa uwezo wa Baba amefufuka tena, kwa kufanya hivyo amepata [c]ushindi juu ya mauti; na pia kupitia kwake uchungu wa kifo umetolewa.

21 *a* 1 Kor. 15:53–54.
22 *a* MWM Haki, Uadilifu, enye Uadilifu.
b MWM Rehema, enye Rehema.
7 1 *a* Hel. 15:11–13.
2 *a* Alma 10:3.
5 *a* 2 Ne. 3:12.
b MWM Amini, Imani.
c Isa. 25:8; Mos. 16:7–8.

6 Na anatimiza [a]ufufuo wa wafu, ambako binadamu lazima atainuliwa kusimama mbele ya [b]kiti cha hukumu.

7 Na ameleta kutimizwa [a]ukombozi wa ulimwengu, ambako yule ambaye atapatikana bila [b]makosa mbele yake katika siku ya hukumu atakubaliwa [c]kuishi kwenye uwepo wa Mungu katika ufalme wake, kuimba sifa zisizo na mwisho na jamii ya [d]waimbaji wa juu, kwa Baba, na kwa Mwana, na kwa Roho Mtakatifu, ambao ni [e]Mungu mmoja, katika hali ya [f]furaha ambayo haina mwisho.

8 Kwa hivyo tubuni, na mbatizwe katika jina la Yesu, na mkubali [a]injili ya Kristo, ambayo itawekwa mbele yenu, sio tu kwa maandishi haya lakini pia kwa [b]maandishi ambayo yatawajia Wayunani [c]kutoka kwa Wayahudi, maandishi ambayo yatatoka kwa Wayunani [d]hadi kwenu.

9 Kwani tazama, [a]haya yameandikwa kwa kusudi kwamba [b]mngeamini hayo; na mkiyaamini hayo mtaamini haya pia; na ikiwa mtaamini haya mtajua kuhusu babu zenu, na pia kazi za ajabu ambazo zimesababishwa na uwezo wa Mungu miongoni mwao.

10 Na mtajua pia kwamba ninyi ni baki la uzao wa Yakobo; kwa hivyo mmehesabiwa miongoni mwa watu wa agano la kwanza; na ikiwa itakuwa hivyo kwamba mtaamini katika Kristo, na mnabatizwa, kwanza kwa maji, halafu kwa moto na Roho Mtakatifu, mkifuata [a]mfano wa Mwokozi wetu, kulingana na alivyotuamuru, itakuwa vema nanyi katika ile siku ya hukumu. Amina.

MLANGO WA 8

Walamani wanawawinda na kuwaangamiza Wanefi—Kitabu cha Mormoni kitajitokeza kwa uwezo wa Mungu—Shida zinatamkwa juu ya wale ambao wanatoa nje ghadhabu na mzozo dhidi ya kazi ya Bwana—Maandishi ya Wanefi yatatokea mbele katika siku ya uovu, uharibifu, na ukengeufu. Karibia mwaka 400–421 B.K.

Tazama mimi, [a]Moroni, ninamaliza [b]maandishi ya baba yangu, Mormoni. Tazama, nina vitu vichache tu vya kuandika, vitu ambavyo nimeamriwa na baba yangu.

2 Na sasa ikawa kwamba baada ya vita [a]kubwa na vya kutisha katika Kumora, tazama, Wanefi ambao walitorokea katika nchi

6 *a* MWM Ufufuko.
b MWM Hukumu ya mwisho; Yesu Kristo—Mwamuzi.
7 *a* MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
b MWM Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki.
c 1 Ne. 10:21; M&M 76:62; Musa 6:57.
d Mos. 2:28.
e M&M 20:28. MWM Mungu, Uungu.
f MWM Shangwe.
8 *a* MWM Injili.
b MWM Biblia.
c 2 Ne. 29:4–13.
d 1 Ne. 13:38.
9 *a* MWM Kitabu cha Mormoni.
b 1 Ne. 13:38–41.
10 *a* 2 Ne. 31:5–9.
8 1 *a* MWM Moroni, Mwana wa Mormoni.
b MWM Mabamba.
2 *a* Morm. 6:2–15.

ya kusini waliwindwa na [b]Walamani, mpaka wote walipoangamizwa.

3 Na baba yangu pia aliuawa na hao, na ni mimi tu nimebaki [a]peke yangu kuandika kisa cha kuhuzunisha cha kuangamizwa kwa watu wangu. Lakini tazama, wameenda, na ninatimiza amri ya baba yangu. Na ikiwa wataniua, sijui.

4 Kwa hivyo nitaandika na kuficha maandiko katika ardhi; na haijalishi popote nitakapoenda.

5 Tazama, baba yangu alibuni [a]maandishi haya, na ameandika kusudi la kufanya hivyo. Na tazama, ningeyaandika pia ikiwa ningekuwa na nafasi kwenye [b]mabamba, lakini sina; na mawe ya madini sina hata moja, kwani niko peke yangu. Baba yangu ameuawa vitani, na ukoo wangu wote, na sina marafiki wala popote pa kwenda; na kwa muda gani Bwana atanikubalia kwamba niishi sijui.

6 Tazama, miaka [a]mia nne imepita tangu kuja kwa Bwana na Mwokozi wetu.

7 Na tazama, Walamani wamewawinda watu wangu, Wanefi, kutoka mji hadi mji na kutoka mahali hadi pengine, mpaka kwamba hawako tena; na [a]mwanguko wao umekuwa mkubwa; ndiyo, mkubwa na wa kustaajabisha ni kuangamizwa kwa watu wangu, Wanefi.

8 Na tazama, ni mkono wa Bwana ambao umeifanya. Na tazama pia, Walamani wako [a]vitani wenyewe kwa wenyewe; na uso wote wa nchi hii daima ni mviringo wa mauaji na umwagaji wa damu; na hakuna yeyote ajuaye mwisho wa vita.

9 Na sasa tazama, sisemi mengi kuhusu hao, kwani hakuna yeyote isipokuwa Walamani na [a]wanyang'anyi ambao wako kote usoni mwa nchi.

10 Na hakuna yeyote anayemjua Mungu wa kweli isipokuwa [a]wanafunzi wa Yesu, ambao walibaki katika nchi mpaka uovu wa watu ulipokuwa mwingi sana kwamba Bwana hakukubalia [b]wabaki na watu; na ikiwa wako juu ya uso wa dunia hakuna mtu ajuaye.

11 Lakini tazama, [a]baba yangu na mimi tumewaona, na wametuhubiria.

12 Na yeyote atakayepokea maandiko haya, na akose kuyalaumu kwa sababu ya makosa yaliyomo, basi huyo huyo atajua [a]vitu vikubwa kuliko hivi. Tazama, mimi ni Moroni; na kama ingewezekana, ningefanya vitu vyote kujulikana kwenu.

13 Tazama, namaliza kuongea kuhusu watu hawa. Mimi ni mwana wa Mormoni, na baba yangu alikuwa [a]uzao wa Nefi.

14 Na mimi ni yule [a]anayeficha maandishi haya kwa ulinzi wa Bwana; mabamba yaliyoko

2 *b* M&M 3:18.
3 *a* Moro. 9:22.
5 *a* Morm. 2:17–18.
b Morm. 6:6.
6 *a* Alma 45:10.
7 *a* 1 Ne. 12:2–3.
8 *a* 1 Ne. 12:20–23.
9 *a* Morm. 2:8.
10 *a* 3 Ne. 28:7; Eth. 12:17.
MWM Wanafunzi Watatu wa Kinefi.
b Morm. 1:16.
11 *a* 3 Ne. 28:24–26.
12 *a* 3 Ne. 26:6–11.
13 *a* 3 Ne. 5:20.
14 *a* Moro. 10:1–2.

hayana thamani, kwa sababu ya amri ya Bwana. Kwani alisema hakuna atakayeyapokea [b]kwa faida; lakini maandiko yaliyoko ni ya thamani kubwa; na yeyote atakayeyadhihirisha, yeye Bwana atambariki.

15 Kwani hakuna aliye na uwezo wa kuyadhihirisha isipokuwa akabidhiwe na Mungu; kwani Mungu hupendelea kwamba itafanyika [a]jicho likiwa kwa utukufu wake, au kwa ustawi wa wale wa kale na watu wa agano la Bwana waliotawanywa.

16 Na atabarikiwa [a]yule ambaye atadhihirisha kitu hiki; kwani [b]kitaletwa kutoka gizani hadi kwenye mwangaza, kulingana na neno la Mungu; ndiyo, kitaletwa kutoka udongoni, na kitatoa nuru kutoka gizani, na ije kwa ufahamu wa watu; na itafanyika kwa uwezo wa Mungu.

17 Na ikiwa kutakuwa na makosa, yatakuwa ni [a]makosa ya binadamu. Lakini tazama, hatujui kosa lolote; walakini Mungu anajua vitu vyote; kwa hivyo, yeyote ambaye [b]analaumu, acha ajihadhari asije akawa kwenye hatari ya moto wa jehanamu.

18 Na yule anayesema: Nionyeshe, au utauawa—acha ajihadhari asije akaamrisha ile ambayo imekatazwa na Bwana.

19 Kwani tazama, yule anayetoa [a]hukumu kwa haraka atahukumiwa kwa haraka tena; kwani kulingana na vitendo vyake, mshahara wake utakuwa hivyo; kwa hivyo yule ambaye huua atauawa tena, na Bwana.

20 Tazama maandiko husema nini—mtu hataua, wala hatahukumu; kwani hukumu ni yangu, asema Bwana, na kisasi ni changu pia, na nitalipiza.

21 Na yule atakayetoa nje ghadhabu na ugomvi dhidi ya kazi ya Bwana, na dhidi ya watu wa agano wa Bwana ambao ni wa nyumba ya Israeli, ambaye atasema: Tutaangamiza kazi ya Bwana, na Bwana hatakumbuka agano lake ambalo amefanya kwa nyumba ya Israeli—yule yule yuko hatarini kukatiwa chini na kutupwa motoni;

22 Kwani [a]kusudi la milele la Bwana litaendelea, mpaka ahadi zake zote zitakapotimizwa.

23 Pekua unabii wa [a]Isaya. Tazama, siwezi kuyaandika. Ndiyo, tazama ninawaambia, kwamba wale watakatifu ambao wameenda kabla yangu, ambao walimiliki hii nchi, [b]watalia, ndiyo, hata kutoka kwenye mavumbi watamlilia Bwana; na kadri Bwana anavyoishi atakumbuka agano ambalo amefanya nao.

24 Na hujua [a]sala zao, kwamba zilikuwa kwa niaba ya ndugu

14 *b* JS—H 1:46.
15 *a* M&M 4:5.
16 *a* 2 Ne. 3:6–7, 11, 13–14.
b Isa. 29:18; 2 Ne. 27:29.
17 *a* Morm. 9:31, 33; Eth. 12:23–28.
b 3 Ne. 29:5; Eth. 4:8.
19 *a* TJS Mt. 7:1–2 (Kiambatisho); 3 Ne. 14:1–2; Moro. 7:14.
22 *a* M&M 3:3.
23 *a* 3 Ne. 20:11; 23:1.
b Isa. 29:4; 2 Ne. 3:19–20; 26:16.
24 *a* Eno. 1:12–18; Morm. 9:36; M&M 10:46.

zao. Na hujua imani yao, kwani katika jina lake wangeondoa [b]milima, na katika jina lake wangesababisha ardhi kutetemeka; na kwa uwezo wa neno lake walisababisha [c]magereza kuanguka ardhini; ndiyo, hata kalibu ya moto mkali haingewaumiza, wala wanyama wa mwitu, wala nyoka wa sumu, kwa sababu ya uwezo wa neno lake.

25 Na tazama, [a]sala zao pia zilikuwa kwa niaba ya yule ambaye Bwana atakubalia kuleta vitu hivi mbele.

26 Na hakuna yeyote aliye na sababu ya kusema havitakuja, kwani kwa kweli vitakuja, kwani Bwana amenena; kwani vitatoka [a]kutoka kwa ardhi, kwa uwezo wa Bwana, na hakuna atakayeizuia; na itakuja katika ile siku wakati itasemekana kwamba [b]miujiza imeondolewa; na itatendeka hata kama vile mmoja anayezungumza [c]kutoka kwa wafu.

27 Na itakuja katika siku ile ambayo [a]damu ya watakatifu itakapolia kwa Bwana, kwa sababu ya [b]makundi maovu ya siri na kazi za gizani.

28 Ndiyo, itakuja katika siku wakati uwezo wa Mungu utakataliwa, na [a]makanisa yatakuwa yamechafuliwa na kujiinua kwa kiburi cha mioyo yao; ndiyo, hata katika siku ambayo viongozi wa makanisa na walimu watajiinua kwa kiburi cha mioyo yao, hata kuwaonea wivu wale ambao wako kwa makanisa yao.

29 Ndiyo, itakuja katika ile siku wakati [a]kutasikika moto, na tufani, na [b]mivuke ya moshi katika nchi za kigeni;

30 Na pia kutasikika mambo ya [a]vita, uvumi wa vita na mitetemeko mahali mbali mbali.

31 Ndiyo, itakuja katika ile siku wakati kutakuweko uchafu mwingi juu ya uso wa dunia; kutakuwa na mauaji, na unyang'anyi, na udanganyifu, na ulaghai, na ukahaba, na kila aina ya machukizo; wakati kutakuwa na wengi ambao watasema, Fanya hivi, au fanye vile, na [a]haijalishi, kwani Bwana [b]ataokoa hawa katika siku ya mwisho. Lakini ole kwa hao, kwani wako kwenye [c]nyongo ya uchungu na katika kifungo cha uovu.

32 Ndiyo, itakuja wakati kutakuwa na makanisa yatakayojengwa ambayo yatasema: Kuja kwangu, na kwa pesa yako utasamehewa dhambi zako.

33 Ee ninyi walio waovu na

24 *b* Yak. (KM) 4:6; Hel. 10:9.
c Alma 14:27–29.
25 *a* Morm. 5:21.
26 *a* Isa. 29:4; 2 Ne. 33:13.
b Morm. 9:15–26; Moro. 7:27–29, 33–37.
c 2 Ne. 26:15–16; Morm. 9:30; Moro. 10:27.
27 *a* Eth. 8:22–24; M&M 87:6–7.
b MWM Makundi maovu ya siri.
28 *a* 2 Tim. 3:1–7; 1 Ne. 14:9–10; 2 Ne. 28:3–32; M&M 33:4.
29 *a* Yoe. 2:28–32; 2 Ne. 27:2–3.
b 1 Ne. 19:11; M&M 45:39–42.
30 *a* Mt. 24:6; 1 Ne. 14:15–17.
31 *a* 2 Ne. 28:21–22.
b 2 Ne. 28:8.
c Alma 41:11.

wapotevu na watu wenye shingo ngumu, kwa nini mmejijengea makanisa kwa kupata [a]faida? Kwa nini [b]mmegeuza neno takatifu la Mungu, kwamba kwa kufanya hivyo mjiletee [c]lawama kwenye nafsi zenu? Tazama, tegemeeni unabii wa Mungu; kwani tazameni, wakati unawadia katika siku hiyo wakati vitu hivi vyote lazima vitimizwe.

34 Tazama, Bwana amenionyesha vitu vikubwa na vya ajabu kuhusu ile ambayo lazima itokee hivi karibuni, katika siku ile ambayo vitu hivi vitatokea mbele miongoni mwenu.

35 Tazama, ninawazungumzia kama vile mko hapa, lakini hamko. Lakini tazama, Yesu Kristo amenionyesha ninyi kwangu, na ninajua yale mnayofanya.

36 Na ninajua kwamba [a]mnaishi kwa kiburi cha mioyo yenu; na hakuna mmoja isipokuwa wachache ambao [b]hawajiinui katika kiburi cha mioyo yao, kwa kuvaa nguo nzuri [c]sana, kusababisha wivu, na ugomvi, na mabishano, na dhuluma, na aina yote ya maovu; na makanisa yenu, ndiyo, hata kila moja, yamechafuliwa kwa sababu ya kiburi cha mioyo yenu.

37 Kwani tazama, mnapenda [a]pesa, na vitu vyenu, na mavazi yenu mazuri, na kupambwa kwa makanisa yenu, kuliko mnavyowapenda maskini, na wanaohitaji msaada, wagonjwa na wanaoteseka.

38 Ee ninyi wachafu, ninyi wanafiki, ninyi walimu, ambao mnajiuza kwa kile ambacho kitaoza, kwa nini mmechafua kanisa takatifu la Mungu? Kwa nini [a]mnaaibika kujivika jina la Kristo? Kwa nini hamfikirii kwamba kubwa zaidi ni thamani ya furaha ya milele isiyo na kikomo kuliko ile [b]taabu ambayo haiishi kamwe—kwa sababu ya [c]sifa ya ulimwengu?

39 Kwa nini mnajipamba na vitu visivyo na uhai, na bado mnawaachilia wenye njaa, na wanaohitaji, na walio uchi, na wagonjwa na wanaoteseka kupita kando yenu, na mnajifanya hamuwaoni?

40 Ndiyo, kwa nini mnaanzisha [a]machukizo ya siri kwa kupata faida, na kusababisha wajane kuomboleza mbele ya Bwana, na pia mayatima kuombeleza mbele ya Bwana, na pia damu ya babu zao na bwana zao kulia kwa Bwana kutoka chini, kwa kisasi juu ya vichwa vyenu?

41 Tazama, upanga wa kisasi unaning'inia juu yenu; na wakati unatimia mapema kwamba atalipiza [a]kisasi cha damu ya wale watakatifu juu yenu, kwani hatavumilia kulia kwao tena.

33 *a* MWM Ukuhani wa uongo.
b 1 Ne. 13:26–29.
c MWM Hukumu.
36 *a* MWM Tembea, Tembea na Mungu.
b Yak. (KM) 2:13.
c Alma 5:53.
37 *a* 2 Ne. 28:9–16.
38 *a* Rum. 1:16; 2 Tim. 1:8; 1 Ne. 8:25–28; Alma 46:21.
b Mos. 3:25.
c 1 Ne. 13:9.
40 *a* MWM Makundi maovu ya siri.
41 *a* 1 Ne. 22:14.

MLANGO WA 9

Moroni anawahimiza wale ambao hawaamini katika Kristo watubu—Anamtangaza Mungu wa miujiza, ambaye hutoa unabii na anayetoa vipawa na ishara juu ya waumini—Miujiza hukoma kwa sababu ya kutoamini—Ishara hutolewa kwa wale ambao huamini—Watu wanashauriwa kuwa na busara na kutii amri. Karibia mwaka 401–421 B.K.

Na sasa, ninazungumza pia kuhusu wale ambao hawaamini katika Kristo.

2 Tazama, mtaamini katika siku ya hukumu yenu—tazama, wakati Bwana atakapokuja, ndiyo, hata ile [a]siku kuu wakati [b]dunia itakunjwa pamoja kama karatasi, na vitu vya asili [c]vitayeyuka kwa joto kubwa, ndiyo, katika siku ile kuu wakati mtaletwa kusimama mbele ya Mwanakondoo wa Mungu—ndipo mtasema kwamba hakuna Mungu?

3 Ndipo mtaendelea kumkana Kristo, au mnaweza kumtazama Mwanakondoo wa Mungu? Mnadhani kwamba mtaishi na yeye chini ya ufahamu wa makosa yenu? Mnadhani ya kwamba mngekuwa na furaha kuishi na kile Kiumbe kitakatifu, wakati nafsi zenu zina msukosuko na ufahamu wa makosa kwamba daima mmetusi sheria zake?

4 Tazama, ninawaambia kwamba mtakuwa na huzuni sana kuishi na Mungu aliye mtakatifu na wa haki, chini ya ufahamu wa uchafu wenu mbele yake, kuliko kuishi na nafsi [a]zilizolaaniwa katika [b]jehanamu.

5 Kwani tazama, wakati mtaletwa kuona [a]uchi wenu mbele ya Mungu, na pia utukufu wa Mungu, na utakatifu wa Yesu Kristo, itawasha mwale wa moto usiozimika juu yenu.

6 Ee basi ninyi [a]msioamini, [b]mgeukieni Bwana; lieni kwa Baba kwa nguvu katika jina la Yesu, kwamba pengine mpatikane bila waa, [c]safi, warembo, na weupe, mkiwa mmeoshwa na damu ya [d]Mwanakondoo, katika ile siku kuu na ya mwisho.

7 Na tena ninawazungumzia ninyi ambao [a]hukataa unabii wa Mungu, na kusema kwamba haifanyiki tena, kwamba hakuna ufunuo, wala unabii, wala vipawa, wala uponyaji, wala kuzungumza kwenye lugha za kigeni, na [b]kutafsiri lugha;

8 Tazama nawaambia, yule anayekana vitu hivi hajui [a]injili ya Kristo; ndiyo, hajasoma maandiko; na ikiwa ameyasoma, [b]hayaelewi.

9 2*a* Mal. 4:5; 3 Ne. 28:31.
b Morm. 5:23; M&M 63:20–21. MWM Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu.
c Amo. 9:13; 3 Ne. 26:3.
4*a* MWM Hukumu.
b MWM Jehanamu.
5*a* 2 Ne. 9:14.
6*a* MWM Kutoamini.
b Eze. 18:23, 32; M&M 98:47.
c MWM Safi na Isiyo safi.
d MWM Mwanakondoo wa Mungu.
7*a* 3 Ne. 29:6–7.
b 1 Kor. 12:7–10; M ya I 1:7.
8*a* MWM Injili.
b Mt. 22:29.

9 Kwani si tunasoma kwamba Mungu ni [a]yule yule jana, na leo, na hata milele, na kwake hakuna kubadilika wala kivuli cha kubadilika?

10 Na sasa, kama mmejiwazia, mungu anayebadilika, na ambaye ana kivuli cha kubadilika, aidha mmejidhania mungu ambaye si Mungu wa miujiza.

11 Lakini tazama, nitawaelezea Mungu wa miujiza, hata Mungu wa Ibrahimu, na Mungu wa Isaka, na Mungu wa Yakobo; na yule yule [a]Mungu aliyeumba mbingu na dunia, na vitu vyote vilivyomo.

12 Tazama, alimuumba Adamu, na kupitia kwa [a]Adamu kukatokea [b]mwanguko wa binadamu. Na kwa sababu ya mwanguko wa binadamu Yesu Kristo alikuja, ambaye ni Baba na Mwana; na kwa sababu ya Yesu Kristo [c]ukombozi wa binadamu ulitokea.

13 Na kwa sababu ya ukombozi wa binadamu, ambao ulifika kupitia kwa Yesu Kristo, wanarudishwa kwenye uwepo wa Bwana; ndiyo, hii ndiyo njia ambayo kwake watu wote wanakombolewa, kwa sababu kifo cha Kristo husababisha kutimizwa kwa [a]ufufuko, ambao husababisha kutimizwa kwa ukombozi kutoka kwa [b]usingizi wa milele, usingizi ambao watu wote wataamshwa kwa uwezo wa Mungu wakati tarumbeta itakapolia; na watatoka nje, wote wadogo na wakubwa, na wote watasimama mbele ya hukumu yake, wakikombolewa na kufunguliwa kutoka kwenye [c]kamba hii ya kifo cha milele, kifo ambacho ni kifo cha mwili.

14 Na ndipo kutatokea [a]hukumu ya Yule Mtakatifu juu yao; na ndipo kutatokea wakati ambao yule ambaye ni mchafu [b]ataendelea kuwa mchafu; na yule ambaye ni mwenye haki ataendelea kuwa mwenye haki; yule ambaye ana furaha ataendelea kuwa na furaha; na yule asiye na furaha ataendelea kuwa bila furaha.

15 Na sasa, Ee ninyi nyote ambao mmejiwazia mungu ambaye [a]hawezi kufanya miujiza, ningewauliza, je, vitu hivi vyote ambavyo nimezungumzia, vimefanyika? Je, mwisho umefika? Tazama nawaambia, Hapana; na Mungu hajakoma kuwa Mungu wa miujiza.

16 Tazama, si vitu ambavyo Mungu amefanya ni vya ajabu machoni mwetu? Ndiyo, na ni nani anayeweza kufahamu [a]kazi za ajabu za Mungu?

17 Ni nani atasema kwamba

9*a* Ebr. 13:8; 1 Ne. 10:18–19; Alma 7:20; Moro. 8:18; M&M 20:12.
11*a* Mwa. 1:1; Mos. 4:2; M&M 76:20–24. MWM Yesu Kristo.
12*a* Mos. 3:26.
b MWM Anguko la Adamu na Hawa.
c MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
13*a* Hel. 14:15–18.
b M&M 43:18.
c M&M 138:16.
14*a* MWM Hukumu ya mwisho.
b Alma 7:21; M&M 88:35.
15*a* Moro. 7:35–37; M&M 35:8. MWM Muujiza.
16*a* Zab. 40:5; M&M 76:114; Musa 1:3–5.

haikuwa miujiza ambayo kwa [a]neno lake mbingu na dunia vipo; na kwa uwezo wa neno lake mtu [b]aliumbwa kutoka kwa [c]mavumbi ya dunia; na kwa uwezo wa neno lake miujiza imefanyika?

18 Na ni nani atasema kwamba Yesu Kristo hakufanya [a]miujiza mingi mikubwa? Na kulikuwa na miujiza mingi mikubwa iliyofanywa na mitume.

19 Na ikiwa [a]miujiza ilifanyika wakati huo, kwa nini Mungu amekoma kuwa Mungu wa miujiza na bado awe kiumbe kisichobadilika? Na tazama, nawaambia habadiliki; ikiwa hivyo angekoma kuwa Mungu; na hakomi kuwa Mungu, na ni Mungu wa miujiza.

20 Na sababu ambayo inamfanya kukoma kufanya [a]miujiza miongoni mwa watoto wa watu ni kwa sababu kwamba wamefifia katika kutoamini, na kutoka kwa njia ya kweli, na hawamjui Mungu ambaye wanapaswa [b]kumwamini.

21 Tazama, ninawaambia kwamba yeyote aaminiye katika Kristo bila tashwishi, [a]chochote atakachomwomba Baba katika jina la Kristo kitatolewa kwake; na hii ahadi iko kwa wote, hata mpaka mwisho wa dunia.

22 Kwani tazama, hivi anasema Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, kwa wanafunzi wake ambao watabaki nyuma, ndiyo, na pia kwa wanafunzi wake wote, kundi lilipokuwa likisikiliza: [a]Nendeni ninyi katika ulimwengu wote, na mhubiri injili kwa kila mtu;

23 Na yule anayeamini na kubatizwa ataokolewa, lakini yule ambaye haamini [a]atalaaniwa;

24 Na [a]ishara hizi zitafuatana nao ambao huamini—katika jina langu watawatupa nje [b]mashetani; watazungumza kwa lugha ngeni; watainua nyoka; na ikiwa watakunywa kitu cha kuhatarisha hakitawadhuru; wataweka [c]mikono yao kwa wagonjwa na watapona;

25 Na yeyote atakayeamini katika jina langu, bila kuwa na shaka, kwake [a]nitamhakikishia maneno yangu yote, hata kwa sehemu zote za dunia.

26 Na sasa, tazama, ni nani anaweza kuzuia kazi ya Bwana? Ni [a]nani anayeweza kukana misemo yake? Ni nani atakayesimama dhidi ya uwezo usio na kipimo wa Bwana? Ni nani atachukia kazi za Bwana? Ni nani atachukia watoto wa Kristo? Tazama, nyote ambao [b]mnachukia kazi za Bwana, kwani mtatangatanga na kuangamia.

27 Ee basi msidharau, na

17 *a* Yak. (KM) 4:9.
b MWM Umba, Uumbaji.
c Mwa. 2:7; Mos. 2:25.
18 *a* Yn. 6:14.
19 *a* M&M 63:7–10.
20 *a* Amu. 6:11–13; Eth. 12:12–18; Moro. 7:35–37.
b MWM Tegemea.
21 *a* Mt. 21:22; 3 Ne. 18:20.
22 *a* Mk. 16:15–16. MWM Kazi ya kimisionari.
23 *a* MWM Hukumu.
24 *a* Mk. 16:17–18. MWM Ishara.
b Mdo. 16:16–18.
c MWM Huduma kwa Wagonjwa.
25 *a* MWM Ufunuo; Ushuhuda.
26 *a* 3 Ne. 29:4–7.
b Mit. 13:13.

msishangae, lakini sikilizeni maneno ya Bwana, na mmwombeni Baba katika jina la Yesu kwa vitu vyote mtakavyohitaji. Msiwe na shaka, lakini muwe mkiamini, na muanze kama wakati wa kale, na [a]mje kwa Bwana na [b]mioyo yenu yote, na [c]mtimize wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka mbele yake.

28 Muwe na [a]hekima katika siku zenu za majaribio; jiondoeni kutoka kwenye uchafu; msiulize, ili mle kwa [b]tamaa yenu, lakini ulizeni kwa uthabiti usiotingishika, kwamba msilegee kwa majaribu yoyote, lakini kwamba mheshimu Mungu wa kweli na [c]aishiye.

29 Oneni kwamba hambatizwi [a]bila kustahili; oneni kwamba msile sakramenti ya Kristo [b]bila kustahili; lakini mhakikishe kwamba mnafanya vitu vyote katika [c]ustahilifu, na mvifanye katika jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu aishiye; na mkifanya hivi, na mvumilie hadi mwisho, hamtatupwa nje kamwe.

30 Tazama, ninawazungumzia kama [a]ninayezungumza kutoka kwa wafu; kwani najua kwamba mtapokea maneno yangu.

31 Msinilaani kwa sababu ya [a]upungufu wangu, wala baba yangu, kwa sababu ya upungufu wake, wala wale ambao wameandika mbele yake; walakini mshukuruni Mungu kwa sababu amewaonyesha upungufu wetu, ili mjifunze kuwa na hekima zaidi yetu.

32 Na sasa, tazama, tumeandika maandiko haya kulingana na kujua kwetu, katika herufi ambazo zinaitwa miongoni mwetu Kimisri [a]kilichogeuzwa, ambacho kilitolewa na kugeuzwa nasi, kulingana na njia yetu ya kuongea.

33 Na ikiwa mabamba yetu yangekuwa kubwa za kutosha tungeandika katika Kihebrania, lakini Kihebrania kimegeuzwa nasi pia; na ikiwa tungeandika katika Kihebrania; tazama, hamngekuwa na upungufu katika maandishi yetu.

34 Lakini Bwana anajua vitu ambavyo tumeandika, na pia kwamba watu wengine hawajui lugha yetu; na kwa sababu hakuna watu wengine wajuao lugha yetu, kwa ajili hii ametayarisha [a]njia ya kutafsiri.

35 Na vitu hivi vimeandikwa ili tuwe huru kutoka kwa jukumu la dhambi zilizofanywa na ndugu zetu, ambao wamefifia kwa [a]kutoamini.

36 Na tazama, vitu hivi amba-

27 *a* Moro. 10:30–32.
b Yos. 22:5; M&M 64:22, 34. MWM Moyo.
c Flp. 2:12.
28 *a* Yak. (KM) 6:12.
b MWM Tamaa mbaya.
c Alma 5:13.
29 *a* MWM Batiza, Ubatizo—Sifa zinazotakiwa kwa ajili ya ubatizo.
b 1 Kor. 11:27–30; 3 Ne. 18:28–32.
c MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki.
30 *a* Morm. 8:26; Moro. 10:27.
31 *a* Morm. 8:17; Eth. 12:22–28, 35.
32 *a* 1 Ne. 1:2; Mos. 1:4.
34 *a* Mos. 8:13–18; Eth. 3:23, 28; M&M 17:1.
35 *a* 2 Ne. 26:15.

vyo [a]tumetaka kuhusu ndugu zetu, ndiyo, hata kurudishwa kwao kwa ufahamu wa Kristo, vipo kulingana na sala za watakatifu ambao waliishi katika nchi.

37 Na ninaomba Bwana Yesu Kristo awakubalie kwamba sala zao zijibiwe kulingana na imani yao; na namwomba Mungu Baba akumbuke lile agano ambalo amefanya na nyumba ya Israeli; na ninaomba awabariki milele, kupitia kwa imani kwa jina la Yesu Kristo. Amina.

KITABU CHA ETHERI

Kumbukumbu ya Wayaredi, ambayo ilichukuliwa kutoka kwenye mabamba ishirini na manne yailiyookotwa na watu wa Limhi katika siku za Mfalme Mosia.

MLANGO WA 1

Moroni anafupisha maandishi ya Etheri—Nasaba ya Etheri inatolewa—Lugha ya Wayaredi haikuchanganywa katika Mnara wa Babeli—Bwana anaahidi kuwaongoza kwenye nchi iliyochaguliwa na awafanye taifa kubwa.

NA sasa mimi, [a]Moroni, naendelea kutoa historia ya wakazi wa zamani ambao waliangamizwa na [b]mkono wa Bwana juu ya uso wa nchi hii ya kaskazini.

2 Na ninachukua historia yangu kutoka kwenye yale mabamba [a]ishirini na nne ambayo yalipatwa na watu wa Limhi, ambayo inaitwa Kitabu cha Etheri.

3 Na kwa vile ninadhani kwamba sehemu ya kwanza ya maandishi haya, ambayo inazungumza kuhusu uumbaji wa dunia, na pia wa Adamu, na historia kutoka wakati ule hata kwenye [a]mnara mkubwa, na vitu vyovyote vilivyojulikana miongoni mwa watoto wa watu hadi wakati huo, iko miongoni mwa Wayahudi—

4 Kwa hivyo siandiki mambo yale ambayo yalitokea tangu [a]siku za Adamu mpaka wakati huo; kwani yapo kwenye mabamba; na yeyote atakayeyapata, huyo huyo atakuwa na uwezo kwamba aweze kupata historia kamilifu.

5 Lakini tazama, sitatoa historia kamilifu, lakini nitatoa tu sehemu ya historia, kutokea wakati wa mnara mpaka wakati walipoangamizwa.

6 Na kwa njia hii ninatoa historia. Yule ambaye aliandika ni

36 *a* Morm. 8:24–26; M&M 10:46–49.

[Etheri]
1 1 *a* mwm Moroni, Mwana wa Mormoni.
b Morm. 5:23; M&M 87:6–7.
2 *a* Alma 37:21; Eth. 15:33.
3 *a* Omni 1:22; Mos. 28:17; Hel. 6:28.
4 *a* mf inajumuisha kipindi sawa na kile katika Mwanzo 1–10.

[a]Etheri, na alikuwa mzao wa Koriantori.
7 Koriantori alikuwa mwana wa Moroni.
8 Na Moroni alikuwa mwana wa Ethemu.
9 Na Ethemu alikuwa mwana wa Aha.
10 Na Aha alikuwa mwana wa Sethi.
11 Na Sethi alikuwa mwana wa Shibloni.
12 Na Shibloni alikuwa mwana wa Komu.
13 Na Komu alikuwa mwana wa Koriantumu.
14 Na Koriantumu alikuwa mwana wa Amnigada.
15 Na Amnigada alikuwa mwana wa Haruni.
16 Na Haruni alikuwa mzao wa Hethi, ambaye alikuwa mwana wa Hearthomu.
17 Na Hearthomu alikuwa mwana wa Libu.
18 Na Libu alikuwa mwana wa Kishi.
19 Na Kishi alikuwa mwana wa Koromu.
20 Na Koromu alikuwa mwana wa Lawi.
21 Na Lawi alikuwa mwana Kimu.
22 Na Kimu alikuwa mwana wa Moriantoni.
23 Na Moriantoni alikuwa mzao wa Riplakishi.
24 Na Riplakishi alikuwa mwana wa Shezi.
25 Na Shezi alikuwa mwana wa Hethi.
26 Na Hethi alikuwa mwana wa Komu.
27 Na Komu alikuwa mwana wa Koriantumu.
28 Na Koriantumu alikuwa mwana wa Emeri.
29 Na Emeri alikuwa mwana wa Omeri.
30 Na Omeri alikuwa mwana wa Shule.
31 Na Shule alikuwa mwana wa Kibu.
32 Na Kibu alikuwa mwana wa Oriha, ambaye alikuwa mwana wa Yaredi;
33 [a]Yaredi ambaye alitoka na kaka yake na jamaa zao, na wengine na jamaa zao, kutoka kwa mnara mkubwa, wakati Bwana [b]alipochanganya lugha za watu, na kuapa katika ghadhabu yake kwamba atawatawanya juu ya [c]uso wa dunia; na kulingana na neno la Bwana watu walitawanywa.
34 Na [a]kaka wa Yaredi akiwa mkubwa na mwenye nguvu, na mtu aliyependelewa sana na Bwana, Yaredi, kaka yake, alimwambia; msihi Bwana, kwamba asituchanganyie lugha ili tusielewane maneno yetu.
35 Na ikawa kwamba kaka wa Yaredi aliomba kwa Bwana, na Bwana alimhurumia Yaredi; kwa hivyo hakuchanganya lugha ya Yaredi, na Yaredi na kaka yake hawakuchafuliwa.
36 Halafu Yaredi akamwambia kaka yake: Omba tena kwa Bwana, na iwe kwamba asiwe na hasira kwa wale ambao ni marafiki zetu, ili asichafue lugha yao.
37 Na ikawa kwamba kaka

6*a* Eth. 12:2; 15:34.
33*a* MWM Yaredi.
b Mwa. 11:6–9.
c Mos. 28:17.
34*a* MWM Yaredi, Kaka wa.

wa Yaredi alimwomba Bwana, na Bwana akawa na huruma kwa marafiki zao na jamaa zao pia, kwamba hawakuchafuliwa.

38 Na ikawa kwamba Yaredi alimzungumzia kaka yake tena, akisema: Nenda na ukamwulize Bwana kama atatufukuza kutoka nchini, na ikiwa atatufukuza kutoka nchini, mwulize kule ambako tutaenda. Na labda Bwana atatuchukua kwenye nchi ambayo ni nchi [a]iliyochaguliwa kuliko zote duniani kote? Na ikiwa itakuwa hivyo, acha tuwe waaminifu kwa Bwana, ili tuweze kuipokea kwa urithi wetu.

39 Na ikawa kwamba kaka wa Yaredi alimwomba Bwana kulingana na yale ambayo yalizungumzwa na mdomo wa Yaredi.

40 Na ikawa kwamba Bwana alimsikiliza kaka wa Yaredi, na akawa na huruma juu yake, na kusema kwake:

41 Nenda na ukakusanye pamoja wanyama wako, wote wa kiume na wa kike wa kila namna; na pia mbegu ya udongoni ya kila namna; na [a]jamaa yako; na pia Yaredi kaka yako na jamaa yake; na pia marafiki zako na jamaa zao, na [b]marafiki za Yaredi na jamaa zao.

42 Na baada ya kufanya hivi [a]utawaongoza chini hadi kwenye bonde ambalo liko upande wa kaskazini. Na huko nitakukuta, na [b]nitakuongoza kwenye nchi ambayo ni [c]bora kuliko nchi zote duniani.

43 Na huko nitawabariki na uzao wenu, na nitauinua uzao wako kwangu, na uzao wa kaka yako, na wale ambao wataenda nawe, taifa kubwa. Na hakutakuwa taifa kubwa kuliko taifa ambalo nitakalolipa uzao wako, juu ya uso wa dunia yote. Na hii nitakufanyia kwa sababu ya muda huu mrefu ambao umeomba kwangu.

MLANGO WA 2

Wayaredi wanajiandaa kwa safari kuelekea nchi ya ahadi—Ni nchi iliyochaguliwa ambamo kwake watu lazima wamtumikie Kristo au waangamizwe—Bwana anamzungumzia kaka wa Yaredi kwa masaa matatu—Wayaredi wanajenga boti—Bwana anamwuliza kaka wa Yaredi atoe shauri jinsi boti zitakavyopata mwangaza.

Na ikawa kwamba Yaredi na kaka yake, na jamaa zao, na pia marafiki za Yaredi na kaka yake na jamaa zao, walienda chini kwenye bonde ambalo lilikuwa upande wa kaskazini, (na jina la lile bonde lilikuwa [a]Nimrodi, ikiwa liliitwa baada ya yule mwindaji mashuhuri) na wanyama wao ambao walikuwa wamewakusanya pamoja, wa kiume na wa kike, wa kila namna.

2 Na waliweka mitego na kushika ndege wa hewani; na pia walitayarisha chombo, ambamo

38 *a* MWM Nchi ya Ahadi.
41 *a* Eth. 6:20.
b Eth. 6:16.
42 *a* 1 Ne. 2:1–2; Ibr. 2:3.
b M&M 84:88.
c 1 Ne. 13:30.
2 1 *a* Mwa. 10:8.

ndani yake wangebebea samaki wa majini.

3 Na pia walijibebea desereti, ambayo, kwa tafsiri, ni nyuki wa asali; na hivyo walibeba vikundi vya nyuki, na kila aina ya kile kilichokuwako juu ya uso wa nchi, mbegu za kila aina.

4 Na ikawa kwamba baada ya hao kuja chini kwenye bonde la Nimrodi Bwana alikuja chini na kuongea na kaka wa Yaredi; na alikuwa kwenye [a]wingu, na kaka wa Yaredi hakumwona.

5 Na ikawa kwamba Bwana aliwaamuru waende mbele nyikani, ndiyo, katika ile sehemu ambako mtu hajawai kuwa. Na ikawa kwamba Bwana aliwaongoza, na alizungumza nao akiwa katika [a]wingu, na akawaonyesha njia ya kusafiri.

6 Na ikawa kwamba walisafiri nyikani, na walijenga boti, ambazo walivuka maji mengi, wakiongozwa wakati wote na mkono wa Bwana.

7 Na Bwana hangekubali kwamba wasimame mbele ya bahari nyikani, lakini alitaka kwamba waje mbele hata mpaka kwenye [a]nchi ya ahadi, ambayo ilikuwa nzuri kuliko nchi zingine zote, ambayo Bwana Mungu alikuwa amehifadhi kwa watu wenye haki.

8 Na alikuwa ameapa kwenye ghadhabu yake kwa kaka wa Yaredi, kwamba yeyote atakayemiliki nchi hii ya ahadi, kutokea wakati huo na kuendelea milele, lazima [a]amtumikie, yule Mungu wa kweli na wa pekee, au [b]waangamizwe utimilifu wa ghadhabu ya Mungu ukiwajia.

9 Na sasa, tunaweza kuona amri za Mungu kuhusu nchi hii, kwamba ni nchi ya ahadi; na taifa lolote litakaloimiliki litamtumikia Mungu, au wataangamizwa wakati utimilifu wa ghadhabu yake, utakuja juu yao. Na utimilifu wa ghadhabu yake huja juu yao baada ya wao kuwa waovu sana.

10 Kwani tazama, hii ni nchi ambayo ni nzuri kuliko nchi zingine zote; kwa hivyo yule atakayeimiliki atamtumikia Mungu au ataangamizwa; kwani ni amri isiyo na mwisho ya Mungu. Na haitakuwako mpaka [a]utimilifu wa uovu miongoni mwa watu wa nchi hii, ndipo [b]wataangamizwa.

11 Na hii itakuja kwenu, Ee ninyi [a]Wayunani, ili mjue amri za Mungu—kwamba mpate kutubu, na msiendelee mpaka utimilifu wa uovu wenu utakavyotimia, kwamba msilete utimilifu wa ghadhabu ya Mungu juu yenu kama wakazi wa nchi hii walivyofanya.

12 Tazama, hii ni nchi nzuri, na taifa lolote litakaloimiliki litakuwa [a]huru kutoka utumwa, na kutoka kifungo, na kutoka kwa mataifa mengine yote chini ya

4*a* Hes. 11:25; M&M 34:7–9; JS—H 1:68.
5*a* Ku. 13:21–22.
7*a* 1 Ne. 4:14.
MWM Nchi ya Ahadi.
8*a* Eth. 13:2.
b Yar. 1:3, 10; Alma 37:28; Eth. 9:20.
10*a* 2 Ne. 28:16.
b 1 Ne. 17:37–38.
11*a* 2 Ne. 28:32.
12*a* MWM Huru, Uhuru.

mbingu, ikiwa [b]watamtumikia Mungu wa pekee katika nchi, ambaye ni Yesu Kristo, ambaye amedhihirishwa na vitu ambavyo tumeviandika.

13 Na sasa ninaendelea na maandishi yangu; kwani tazama, ikawa kwamba Bwana alimleta Yaredi na ndugu zake mbele hata kwenye hiyo bahari kubwa ambayo inagawanya nchi. Na walipokaribia bahari walipiga hema zao; na waliita mahala pale Moriankumeri; na waliishi kwenye hema, na wakaishi katika hema kwenye ukingo wa bahari kwa muda wa miaka minne.

14 Na ikawa katika mwisho wa miaka minne kwamba Bwana alikuja tena kwa kaka wa Yaredi, na akasimama katika wingu na kuongea na yeye. Na kwa muda wa masaa matatu, Bwana aliongea na kaka wa Yaredi, na [a]kumkemea kwa sababu hakukumbuka [b]kulilingana jina la Bwana.

15 Na kaka wa Yaredi alitubu uovu aliofanya, na akalilingana jina la Bwana kwa niaba ya ndugu zake aliokuwa nao. Na Bwana akamwambia: Nitakusamehe na ndugu zako kutoka kwa dhambi zao; lakini hutafanya dhambi mara nyingine, kwani utakumbuka kwamba [a]Roho yangu [b]haitajishughulisha na mwanadamu kila mara; kwa hivyo, kama utafanya dhambi mpaka ufike mwisho, utakatiliwa mbali kutoka kwenye uwepo wa Bwana. Na hizi ndizo fikira zangu juu ya nchi ambayo nitakupatia kwa urithi; kwani itakuwa nchi [c]nzuri kuliko nchi zote.

16 Na Bwana alisema: Nenda ufanye kazi na ujenge, aina ya boti ambazo mmejenga hadi sasa. Na ikawa kwamba kaka wa Yaredi alienda kazini, na pia ndugu zake, na kujenga boti kama aina ambazo walikuwa wamejenga, kulingana na [a]mafundisho ya Bwana. Na zilikuwa madogo, na zilikuwa nyepesi juu ya maji, hata kama wepesi wa ndege arukaye juu ya maji.

17 Na zilijengwa kwa aina moja kwamba zilikuwa [a]zimekazwa sana, kwamba zingeshikilia maji kama vile sahani inavyofanya; na chini yake zilikuwa zimekazwa sana kama sahani; na pande zilikuwa zimekazwa kama sahani; na ncha zilichongoka; na juu yake zilikuwa zimekazwa kama sahani; na urefu wake ulikuwa urefu wa mti; na mlango wake, baada ya kufungwa, ulikazika kama sahani.

18 Na ikawa kwamba kaka wa Yaredi aliomba kwa Bwana, akisema: Ee Bwana, nimefanya kazi ambayo uliniamuru, na nimetengeneza boti kama vile ulivyoniongoza.

19 Na tazama, Ee Bwana, ndani yake hamna mwangaza;

12 *b* Isa. 60:12.
14 *a* MWM Rudi, Kurudiwa.
b MWM Sala.
15 *a* Eth. 15:19.
b Mwa. 6:3; 2 Ne. 26:11; Morm. 5:16.
c Eth. 9:20.
16 *a* 1 Ne. 17:50–51.
17 *a* Eth. 6:7.

tutazielekeza wapi? Na pia tutaangamia, kwani ndani yake hatuwezi kupumua, isipokuwa tu hewa iliyomo ndani yake; kwa hivyo tutaangamia.

20 Na Bwana akamwambia kaka wa Yaredi: Tazama, utatoboa tundu upande wa juu, na pia upande wa chini; na wakati mtakapokosa hewa mtafungua tundu na mpokee hewa. Na ikiwa itakuwa kwamba maji yataingia ndani kwenu, tazama, mtafunga tundu, ili msife katika mafuriko.

21 Na ikawa kwamba kaka wa Yaredi alifanya vile, kulingana na Bwana alivyomwamuru.

22 Na akaomba tena kwa Bwana akisema: Ee Bwana, tazama nimefanya hata vile ulivyoniamuru; na nimetayarisha vyombo kwa watu wangu, na tazama hakuna mwangaza ndani yake. Tazama, Ee Bwana, utakubali tuvuke maji haya mengi kwenye giza?

23 Na Bwana akamwambia kaka wa Yaredi: Ungetaka nifanye nini ili muwe na mwangaza kwenye boti zenu? Kwani tazama, hamwezi kuwa na madirisha, kwani yatavunjwa vipande vipande; wala hamwezi kubeba moto, kwani hamtaenda kwa mwanga wa moto.

24 Kwani tazama, mtakuwa kama nyangumi katikati ya bahari; kwani milima ya mawimbi yatawaangukia. Hata hivyo, nitawarudisha juu tena kutoka kwenye kilindi cha bahari; kwani [a]pepo hutoka katika mdomo wangu, na pia [b]mvua na mafuriko hutolewa na mimi.

25 Na tazama, ninawatayarisha dhidi ya vitu hivi; kwani hamwezi kuvuka hiki kilindi kikubwa isipokuwa niwatayarishe dhidi ya mawimbi ya bahari, na pepo ambazo zimevuma, na mafuriko ambayo yatakuja. Kwa hivyo unataka nikutayarishie nini ili muwe na mwangaza ndani ya kilindi cha bahari?

MLANGO WA 3

Kaka wa Yaredi anaona kidole cha Bwana Anapogusa mawe kumi na sita—Kristo anaonyesha mwili Wake wa kiroho kwa kaka wa Yaredi—Wale ambao wana elimu kamili hawawezi kuwekwa nyuma ya pazia—Zana za kufasiri zinatolewa kufanya kumbukumbu ya Wayaredi kujulikana.

Na ikawa kwamba kaka wa Yaredi, (sasa idadi ya boti ambazo zilikuwa zimetayarishwa zilikuwa nane) alienda mbele kwenye mlima, ambao waliuita mlima Shelemu, kwa sababu ya urefu wake mwingi, na akachonga mawe madogo kumi na sita kutoka kwenye mwamba; na yalikuwa meupe na safi, hata kama kioo kilicho wazi; na aliyabeba katika mikono yake hadi juu ya kilele cha mlima, na akaomba tena kwa Bwana, akisema:

2 Ee Bwana, umesema kwamba lazima tuzungukwe na mafuriko. Sasa tazama, Ee Bwana, na usiwe na hasira na mtumishi

24 *a* Eth. 6:5. *b* Zab. 148:8.

wako kwa sababu ya udhaifu wake mbele yako; kwani tunajua kwamba wewe ni mtakatifu na unaishi mbinguni, na sisi hatufai mbele yako; kwa sababu ya [a]mwanguko [b]maumbile yetu yamekuwa maovu siku zote; walakini, Ee Bwana, umetupatia amri kwamba tukulingane, kwamba kutoka kwako tungepokea mahitaji yetu.

3 Tazama, Ee Bwana, umetuadhibu kwa sababu ya uovu wetu, na umetusukuma mbele, na katika hii miaka mingi tumekuwa katika nyika; walakini, umekuwa mwenye [a]huruma kwetu. Ee Bwana, nitazame na huruma, na ugeuze hasira yako kutoka kwa watu hawa, na usikubali kwamba wavuke hii bahari katika giza; lakini tazama vitu hivi ambavyo nimechonga kutoka katika mwamba.

4 Na ninajua, Ee Bwana, kwamba una [a]uwezo wote, na unaweza kufanya chochote upendacho kwa faida ya binadamu; kwa hivyo gusa mawe haya, Ee Bwana, na kidole chako, na uyatayarishe kwamba yaangaze kwenye giza; na yatang'aa kwetu ndani ya boti ambazo tumezitayarisha, ili tuweze kuwa na mwangaza tutakapovuka bahari.

5 Tazama, Ee Bwana, unaweza kufanya hivi. Tunajua kwamba unaweza kuonyesha mbele uwezo wako mkuu, ambao [a]unaonekana mdogo katika macho ya watu.

6 Na ikawa kwamba baada ya kaka wa Yaredi kusema maneno haya, tazama, [a]Bwana alinyoosha mbele mkono wake na kugusa yale mawe moja moja kwa kidole chake. Na [b]pazia lilitolewa machoni mwa kaka wa Yaredi, na akaona kidole cha Bwana; na kilikuwa kama kidole cha mtu, sawa kama mwili na damu; na kaka wa Yaredi alianguka chini mbele ya Bwana, kwani alikumbwa na woga.

7 Na Bwana aliona kwamba kaka wa Yaredi alikuwa ameanguka chini; na Bwana akasema kwake: Amka, kwa nini umeanguka?

8 Na akamwambia Bwana: Niliona kidole cha Bwana, na nikaogopa asije akanipiga; kwani sikujua kama Bwana anao mwili na damu.

9 Na Bwana akamwambia: Kwa sababu ya imani yako umeona kwamba nitachukua juu yangu [a]mwili na damu; na hakujakuwa na mtu aliyekuja kwangu mbeleni na imani kubwa vile umefanya; kwani kama hungekuwa hivyo hungeona kidole changu. Je, uliona zaidi ya hii?

10 Na akajibu: Hapana; Bwana, jidhihirishe kwangu.

11 Na Bwana akamwambia: utaamini maneno ambayo nitasema?

12 Na akajibu: Ndiyo, Bwana,

3 2*a* MWM Anguko la Adamu na Hawa.
b Mos. 3:19.
3*a* Eth. 1:34–43.
4*a* MWM Uwezo.
5*a* Isa. 55:8–9; 1 Ne. 16:29.
6*a* MWM Yesu Kristo.
b Eth. 12:19, 21.
9*a* MWM Hali ya Kufanyika Nyama; Yesu Kristo.

najua kwamba wewe husema ukweli, kwani wewe u Mungu wa ukweli, na [a]huwezi kudanganya.

13 Na baada ya kusema maneno haya, tazama, Bwana [a]alijionyesha kwake, na kusema: Kwa [b]sababu unajua vitu hivi umekombolewa kutoka kwenye mwanguko; kwa hivyo umerudishwa kwenye uwepo wangu; kwa hivyo [c]ninajionyesha kwako.

14 Tazama, ni mimi yule aliyetayarishwa kutoka mwanzo wa dunia [a]kuokoa watu wangu. Tazama, mimi ni Yesu Kristo. Mimi ni [b]Baba na Mwana. Ndani yangu binadamu wote watapata [c]maisha, na kwamba milele, hata wale watakaoamini kwa jina langu; na watakuwa [d]wana wangu na mabinti zangu.

15 Na kamwe sijajionyesha kwa binadamu ambaye nilimuumba, kwani binadamu [a]hajaamini kwangu vile umefanya. Je, unaona kwamba uliumbwa kwa [b]mfano wangu? Ndiyo, hata watu wote waliumbwa katika mwanzo kwa jinsi ya kama maumbile yangu.

16 Tazama, huu mwili, ambao unauona sasa, ni mwili wa [a]roho yangu; na nimemuumba mtu jinsi ya mwili wangu wa roho; na hata ninavyoonekana kwako kuwa katika roho ndivyo nitakavyoonekana kwa watu wangu katika mwili.

17 Na sasa, kwa vile mimi, Moroni, nilisema siwezi kuandika historia kamili ya vitu hivi ambavyo vimeandikwa, kwa hivyo, ninatosheka kusema kwamba Yesu alijionyesha kwa mtu huyu katika roho, hata jinsi [a]alivyojionyesha kwa Wanefi.

18 Na alimhudumia kama alivyowahudumia Wanefi; na alifanya haya yote, ili huyu mtu ajue kwamba alikuwa Mungu, kwa sababu ya matendo mengi makubwa ambayo Bwana alikuwa amemwonyesha.

19 Na kwa sababu ya ufahamu wa huyu mtu hangeweza kuzuiwa kuona ndani ya [a]pazia; na aliona kidole cha Yesu, ambacho, baada ya kukiona, alianguka kwa woga; kwani alijua kwamba kilikuwa kidole cha Bwana; na hakuwa na imani tena, kwani alijua, bila tashwishi.

20 Kwa hivyo, akiwa na hii elimu kamilifu ya Mungu, [a]hangeweza kuwekwa kwenye pazia; kwa hivyo alimwona Yesu; na akamhudumia.

21 Na ikawa kwamba Bwana alimwambia kaka wa Yaredi: Tazama, hutaruhusu lolote la vitu hivi ambavyo umeona na kusikia kufunuliwa

12 *a* Ebr. 6:18.
13 *a* M&M 67:10–11.
b Eno. 1:6–8.
c MWM Yesu Kristo—Kuwepo kwa Kristo kabla ya kuzaliwa duniani.
14 *a* MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi, Mkombozi.
b Mos. 15:1–4.
c Mos. 16:9.
d MWM Wana na Mabinti za Mungu.
15 *a* MWM Amini, Imani.
b Mwa. 1:26–27; Mos. 7:27; M&M 20:17–18.
16 *a* MWM Roho.
17 *a* 3 Ne. 11:8–10.
19 *a* MWM Pazia.
20 *a* Eth. 12:19–21.

kwa ulimwengu, mpaka [a]wakati utakapotimia nitakapolitukuza jina langu katika mwili; kwa hivyo, utaweka vitu hivi ambavyo umeviona na kusikia kwako, na usimwonyeshe mtu yeyote.

22 Na tazama, utakapokuja kwangu, utaviandika na kufunga, ili mtu yeyote asiweze kuvitafsiri; kwani utaviandika kwa lugha ambayo haiwezi kusomeka.

23 Na tazama, mawe haya [a]mawili nitakukabidhi, nawe utayafunga pia pamoja na vitu utakavyoandika.

24 Kwani tazama, lugha ambayo utaandika nimeichanganya; kwa hivyo nitasababisha kwa wakati wangu unaonifaa kwamba mawe haya yatakuza macho ni pa binadamu vitu hivi ambavyo utaandika.

25 Na baada ya Bwana kusema maneno haya, alimwonyesha kaka wa Yaredi wakazi [a]wote wa dunia ambao walikuwepo, na pia wote watakaokuwepo; na hakuwaficha kutoka kwenye uwezo wake wa kuona, hata hadi kwenye mwisho wa dunia.

26 Kwani alikuwa amemwambia mbeleni, [a]ikiwa [b]atamwamini kwamba angemwonyesha vitu [c]vyote—kwamba ataonyeshwa; kwa hivyo Bwana hakuweza kumzuia lolote, kwani alijua kwamba Bwana angemwonyesha vitu vyote.

27 Na Bwana akamwambia: Andika vitu hivi na uvitie [a]muhuri; na nitavidhihirisha kwa watoto wa watu katika muda wangu unaonifaa.

28 Na ikawa kwamba Bwana alimwamuru kwamba kuyafungia yale [a]mawe mawili ambayo alikuwa amepokea, na asiyaonyeshe kwa yeyote, mpaka Bwana atakapoyadhihirisha kwa watoto wa watu.

MLANGO WA 4

Moroni anaamrishwa kuyafungia maandishi ya kaka wa Yaredi—Hayatafunuliwa mpaka watu wote watakapokuwa na imani kama ya kaka wa Yaredi—Kristo anaamuru watu wote waamini maneno Yake, na yale ya wanafunzi Wake—Watu wanaamriwa watubu, waamini injili, na waokolewe.

Na Bwana alimwamuru kaka wa Yaredi aende chini kutoka mlimani kutoka kwenye uwepo wa Bwana, na [a]aviandike vitu alivyokuwa ameviona; na vilikatazwa kuonekana na watoto wa watu [b]mpaka atakapoinuliwa juu ya msalaba; na kwa sababu hii mfalme Mosia alivificha, kwamba visijulikane duniani mpaka Kristo atakapojidhihirisha kwa watu wake.

2 Na baada ya Kristo kujidhihirisha kwa ukweli kwa watu wake aliamrisha kwamba vijulikane.

3 Na sasa, baada ya hayo, wote

21 *a* Eth. 4:1.
23 *a* MWM Urimu na Thumimu.
25 *a* Musa 1:8.
26 *a* Eth. 3:11–13.
b MWM Amini, Imani.
c Eth. 4:4.
27 *a* 2 Ne. 27:6–8.
28 *a* M&M 17:1.
4 1 *a* Eth. 12:24. MWM Maandiko.
b Eth. 3:21.

wamefifia katika kutoamini; na hakuna yeyote isipokuwa Walamani, na wamekataa injili ya Kristo; kwa hivyo nimeamriwa kwamba [a]nivifiche tena ardhini.

4 Tazama, nimeandika juu ya mabamba haya vitu vivyo hivyo ambavyo kaka wa Yaredi aliviona; na hakujakuwa vitu vikubwa vilivyoonyeshwa kuliko hivyo ambavyo vilionyeshwa kwa kaka wa Yaredi.

5 Kwa hivyo Bwana ameniamuru niviandike; na nimeviandika. Na aliniamuru kwamba [a]nivifunge; na pia ameniamuru kwamba nifungie [b]tafsiri yake; kwa hivyo nimeifungia tafsiri, kulingana na amri ya Bwana.

6 Kwani Bwana aliniambia: Havitawaendea Wayunani mpaka siku watakapotubu uovu wao, na kuwa safi mbele ya Bwana.

7 Na katika siku hiyo watakapofanya imani kwangu, asema Bwana, hata kama kaka wa Yaredi alivyofanya, kwamba [a]watakaswe kupitia kwangu, ndipo nitawaonyesha vitu ambavyo kaka wa Yaredi aliviona, hata kwa kuwakunjulia ufunuo wangu wote, anasema Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, [b]Baba wa mbingu na wa dunia, na vitu vyote vilivyomo.

8 Na yule ambaye [a]atapingana na neno la Bwana, acha alaaniwe; na yule ambaye [b]atakana vitu hivi, acha alaaniwe; kwani kwao, [c]sitaonyesha vitu vikubwa zaidi, anasema Yesu Kristo; kwani ni mimi ninayezungumza.

9 Na kwa amri yangu mbingu hufunguliwa na [a]kufungwa; na kwa neno langu [b]dunia itatetemeka; na kwa amri yangu wakazi wake watakufa, kama waliochomwa na moto.

10 Na yule ambaye haamini maneno yangu, haamini wanafunzi wangu; na ikiwa hivyo kwamba sisemi, hukumu wewe; kwani utajua kwamba ni mimi ninayezungumza, katika [a]siku ya mwisho.

11 Lakini yule [a]aaminiye maneno haya ambayo nimesema, yeye nitamtembelea na ufunuo wa Roho yangu, na atajua na kushuhudia. Kwani kwa sababu ya Roho yangu [b]atafahamu kwamba vitu hivi ni vya [c]kweli; kwani huwashawishi watu kutenda mema.

12 Na kitu chochote ambacho hushawishi watu kutenda mema ni changu; kwani [a]mema hayatoki kwa yeyote isipokuwa kwangu. Mimi ni yule yule ambaye huongoza watu kwa wema wote; yule ambaye [b]hataamini maneno yangu hataniamini—kwamba ni mimi; na yule ambaye hataniamini

3 *a* Morm. 8:14.
5 *a* Eth. 5:1.
b M&M 17:1; JS—H 1:52. MWM Urimu na Thumimu.
7 *a* MWM Utakaso.
b Mos. 3:8.
8 *a* 3 Ne. 29:5–6; Morm. 8:17.
b 2 Ne. 27:14; 28:29–30.
c Alma 12:10–11; 3 Ne. 26:9–10.
9 *a* 1 Fal. 8:35; M&M 77:8.
b Hel. 12:8–18; Morm. 5:23.
10 *a* 2 Ne. 33:10–15.
11 *a* M&M 5:16.
b MWM Ushuhuda.
c Eth. 5:3–4; Moro. 10:4–5.
12 *a* Alma 5:40; Moro. 7:16–17.
b 3 Ne. 28:34.

hatamwamini Baba ambaye alinituma. Kwani tazama, mimi ni Baba, mimi ni [c]mwangaza, na [d]maisha, na ukweli wa dunia.

13 [a]Njooni kwangu, Ee ninyi Wayunani, na nitawaonyesha vitu vikuu zaidi, ufahamu ambao umefichwa kwa sababu ya kutoamini.

14 Njooni kwangu, Ee ninyi nyumba ya Israeli, na itafanywa [a]kujulikana kwenu jinsi Baba alivyoweka vitu kwenu, kutokea msingi wa dunia; na haijawafikia, kwa sababu ya kutoamini.

15 Tazama, wakati mtakapopasua lile pazia la kutoamini ambalo linawasababisha kubaki katika hali yenu ya kutisha ya uovu, na ugumu wa moyo, na upofu wa akili, ndipo vitu vikubwa na vya kustaajabisha ambavyo [a]vilifichwa kutokea mwanzo wa dunia kutoka kwenu—ndiyo, wakati mtakapomlingana Baba katika jina langu, na moyo uliopondeka na roho iliyovunjika, ndipo mtajua kwamba Baba amekumbuka agano ambalo alifanya na babu zenu, Ee nyumba ya Israeli.

16 Na ndipo [a]ufunuo wangu ambao nimesababisha kuandikwa na mtumishi wangu Yohana utakunjuliwa machoni mwa watu wote. Kumbuka, wakati mtakapoona vitu hivi, mtajua kwamba wakati uko karibu kwamba vitafanywa kuwa wazi kabisa.

17 Kwa hivyo, [a]mtakapopokea maandishi haya mjue kwamba kazi ya Baba imeanza juu ya uso wa nchi.

18 Kwa hivyo, [a]tubuni enyi miisho ya dunia, na mje kwangu, na mwamini katika injili yangu, na [b]mbatizwe katika jina langu; kwani yule ambaye anaamini na kubatizwa atakombolewa; lakini yule ambaye haamini atalaaniwa; na [c]ishara zitaonyeshwa kwa wale ambao wanaamini katika jina langu.

19 Na ana baraka yule atakayepatikana akiwa [a]mwaminifu kwa jina langu katika siku ya mwisho, kwani atainuliwa kuishi katika ufalme uliotayarishwa [b]kutokea mwanzo wa dunia. Na tazama ni mimi ambaye nimezungumza. Amina.

MLANGO WA 5

Mashahidi watatu na kazi yenyewe watasimama kama ushuhuda wa ukweli wa Kitabu cha Mormoni.

Na sasa mimi, Moroni, nimeandika maneno ambayo niliamriwa, kulingana na uwezo wangu wa kukumbuka; na nimekwambia vitu ambavyo [a]nimevifungia; kwa hivyo usiviguse ili

12 *c* MWM Nuru, Nuru ya Kristo.
d Yn. 8:12; Alma 38:9.
13 *a* 3 Ne. 12:2–3.
14 *a* M&M 121:26–29.
15 *a* 2 Ne. 27:10.
16 *a* Ufu. 1:1; 1 Ne. 14:18–27.
17 *a* 3 Ne. 21:1–9, 28.
18 *a* 3 Ne. 27:20; Moro. 7:34.
b Yn. 3:3–5. MWM Batiza, Ubatizo—Muhimu.
c MWM Vipawa vya Roho.
19 *a* Mos. 2:41; M&M 6:13. MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
b 2 Ne. 9:18.
5 1 *a* 2 Ne. 27:7–8, 21; Eth. 4:4–7.

uvitafsiri; kwani kitu kile kimekatazwa kwako, isipokuwa baadaye itakuwa hekima kwa Mungu.

2 Na tazama, ungekubaliwa kwamba ungeonyesha mabamba kwa [a]wale ambao watasaidia kwa kuileta mbele hii kazi;

3 Na kwa [a]watatu wataonyeshwa kwa uwezo wa Mungu; kwa hivyo [b]watajua kwa hakika kwamba vitu hivi ni vya [c]kweli.

4 Na kwa vinywa vya [a]mashahidi watatu vitu hivi vitadhihirishwa; na ushuhuda wa watatu, na kazi hii, ambamo kwake kutaonyeshwa uwezo wa Mungu na pia neno lake, ambalo Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu wanashuhudia—na haya yote yatasimama kama ushuhuda dhidi ya dunia katika siku ya mwisho.

5 Na ikiwa itakuwa kwamba watatubu na [a]kurudi kwa Baba katika jina la Yesu, watapokelewa kwenye ufalme wa Mungu.

6 Na sasa, ikiwa sina mamlaka kwa vitu hivi, hukumuni ninyi; kwani mtajua kwamba ninayo mamlaka mtakaponiona, na tutasimama mbele ya Mungu katika siku ya mwisho. Amina.

MLANGO WA 6

Boti za Wayaredi zinaendeshwa kwa upepo hadi kwenye nchi ya ahadi—Watu wanamsifu Bwana kwa wema Wake—Oriha anateuliwa kuwa mfalme juu yao—Yaredi na kaka yake wanafariki.

Na sasa mimi, Moroni, ninaendelea kutoa maandishi ya Yaredi na kaka yake.

2 Kwani ikawa baada ya Bwana kutayarisha [a]mawe ambayo kaka wa Yaredi alikuwa amebeba juu ya mlima, kaka wa Yaredi alishuka chini kutoka kwenye mlima, na kuweka mawe katika boti ambazo zilitayarishwa, moja kwa kila boti; na tazama, yalitoa mwangaza ndani ya boti.

3 Na hivyo Bwana alisababisha mawe kutoa nuru gizani, kutoa mwangaza kwa wanaume, wanawake, na watoto, ili wasivuke maji mengi gizani.

4 Na ikawa kwamba baada ya kutayarisha namna yote ya vyakula, kwamba wangeishi kwenye maji, na pia vyakula kwa wanyama wao na mifugo yao, na kila mnyama au ndege ambao watawachukua—na ikawa kwamba baada ya kufanya vitu hivi vyote waliingia kwenye vyombo au boti, na kuanza safari kuelekea baharini, wakimtegemea Bwana Mungu wao awalinde.

5 Na ikawa kwamba Bwana Mungu alisababisha kwamba kuweko na [a]upepo mkali utakaovuma juu ya maji kuelekea ile

2*a* 2 Ne. 27:12–14; M&M 5:9–15.
3*a* 2 Ne. 11:3; 27:12.
b M&M 5:25.
c Eth. 4:11.
4*a* Tazama M&M 17 kichwa cha habari na aya ya 1–3; tazama pia "Ushuhuda wa Mashahidi Watatu" katika kurasa tangulizi za Kitabu cha Mormoni.
5*a* Morm. 9:27; Moro. 10:30–32.
6 2*a* Eth. 3:3–6.
5*a* Eth. 2:24–25.

nchi ya ahadi; na hivyo walitupwa juu ya mawimbi ya bahari mbele ya upepo.

6 Na ikawa kwamba mara nyingi walizikwa kwenye kilindi cha bahari, kwa sababu ya milima ya mawimbi ambayo iliwaangukia, na pia tufani kubwa za kuogofya ambazo zilisababishwa na ukali wa upepo.

7 Na ikawa kwamba walipozikwa katika kilindi hakukuwa na maji ambayo yangewaumiza, jinsi vyombo vyao vilivyokuwa [a]vimekazwa kama bakuli, na pia vilikazwa kama [b]safina ya Nuhu; kwa hivyo wakati walizingirwa na maji mengi walimwomba Bwana, na aliwaleta tena nje juu ya maji.

8 Na ikawa kwamba upepo haukukoma kamwe kuvuma kuelekea ile nchi ya ahadi wakati walikuwa juu ya maji; na hivyo walipelekwa mbele ya upepo.

9 Na [a]waliimba nyimbo za sifa kwa Bwana; ndiyo, kaka wa Yaredi aliimba sifa kwa Bwana, na [b]alimshukuru na kumsifu Bwana siku yote nzima; na usiku ulipofika, hawakukoma kumsifu Bwana.

10 Na hivyo walisukumwa mbele; na hakuna mnyama mkubwa wa baharini ambaye angewavunja, wala nyangumi ambaye angewaharibu; na walikuwa na mwangaza daima, hata wakiwa chini ya maji au juu ya maji.

11 Na hivyo ndivyo walivyopelekwa mbele, kwa siku mia tatu arubaini na nne juu ya maji.

12 Na walitua kwenye ukingo wa nchi ya ahadi. Na baada ya kuweka miguu yao juu ya ukingo wa nchi ya ahadi walisujudu chini juu ya nchi, na wakajinyenyekeza mbele ya Bwana, na machozi ya shangwe yakatiririka mbele ya Bwana, kwa sababu ya wingi wa wororo wa rehema yake juu yao.

13 Na ikawa kwamba walienda juu ya uso wa nchi, na wakaanza kulima ardhi.

14 Na Yaredi alikuwa na wana wanne; na waliitwa Yakomu, na Gilga, na Maha, na Oriha.

15 Na kaka wa Yaredi pia alizaa wana na mabinti.

16 Na [a]marafiki za Yaredi na kaka yake walikuwa idadi ya karibu watu ishirini na wawili; na pia walizaa wana na mabinti kabla ya kuja kwenye nchi ya ahadi; na kwa sababu hiyo walianza kuwa wengi.

17 Na walifundishwa [a]kujinyenyekeza mbele ya Bwana; na pia [b]walifundishwa kutoka juu.

18 Na ikawa kwamba walianza kuenea juu ya nchi, na kuongezeka na kulima ardhi; na walikuwa na nguvu katika nchi.

19 Na kaka wa Yaredi alianza kuzeeka, na akaona kwamba karibu ataenda chini kwenye kaburi; kwa hivyo alisema kwa

7 *a* Eth. 2:17.
b Mwa. 6:14; Musa 7:43.
9 *a* MWM Imba.
b 1 Nya. 16:7–9; Alma 37:37; M&M 46:32.
16 *a* Eth. 1:41.
17 *a* MWM Tembea, Tembea na Mungu.
b MWM Ufunuo.

Yaredi: Acheni tukusanye pamoja watu wetu ili tuweze kuwahesabu; ili tuwaulize ni kitu gani watakachohitaji kutoka kwetu kabla hatujaenda kwenye makaburi yetu.

20 Na kwa hivyo watu walikusanywa pamoja. Sasa idadi ya wana na mabinti wa kaka wa Yaredi walikuwa watu ishirini na wawili; na idadi ya wana na mabinti wa Yaredi walikuwa kumi na wawili, yeye akiwa na wana wanne.

21 Na ikawa kwamba walihesabu watu wao; na baada ya kuwahesabu, waliwauliza vitu ambavyo wangependa wafanyiwe kabla ya kwenda kwao kwenye makaburi yao.

22 Na ikawa kwamba watu walitaka waweke [a]wakfu mmoja wa wana wao kuwa mfalme juu yao.

23 Na sasa tazama, hii ilikuwa ngumu kwao. Na kaka wa Yaredi akasema kwao: Kwa kweli kitu hiki [a]kitawaongoza kwenye utumwa.

24 Lakini Yaredi alisema kwa kaka yake: Wakubalie kwamba wawe na mfalme. Na kwa hivyo akawaambia: Chagueni kutoka miongoni mwa wana wetu mfalme, yeyote mtakayemtaka.

25 Na ikawa kwamba walimchagua hata mwana wa kwanza wa kaka wa Yaredi; na jina lake lilikuwa Pagagi. Na ikawa kwamba alikataa na hakutaka kuwa mfalme wao. Na watu walitaka kwamba baba yake amlazimishe, lakini baba yake hakumlazimisha; na akawaamuru kwamba wasimlazimishe mtu yeyote kuwa mfalme wao.

26 Na ikawa kwamba waliwachagua kaka wote wa Pagagi, na hawakukubali.

27 Na ikawa kwamba hata wana wa Yaredi, nao wote walikataa isipokuwa tu mmoja; na Oriha alitawazwa kuwa mfalme juu ya watu.

28 Na alianza kutawala, na watu walianza kufanikiwa; na wakawa matajiri sana.

29 Na ikawa kwamba Yaredi alifariki, na kaka yake pia.

30 Na ikawa kwamba Oriha alijinyenyekeza mbele ya Bwana, na alikumbuka vitu gani vikubwa Bwana alikuwa amemfanyia baba yake, na pia aliwafundisha watu wake vitu gani vikubwa Bwana alikuwa amewafanyia babu zao.

MLANGO WA 7

Oriha anatawala kwa haki—Katika hali ya mapinduzi na mzozo, falme za upinzani za Shule na Kohori zinaanzishwa—Manabii wanalaani uovu na kuabudu kwa sanamu kwa watu, ambao kisha wanatubu.

Na ikawa kwamba Oriha alitoa hukumu kwenye nchi kwa haki siku zake zote, ambaye siku zake zilikuwa nyingi sana.

2 Na alizaa wana na mabinti; ndiyo, alizaa thelathini na mmoja, miongoni mwao walikuwa wana ishirini na watatu.

3 Na ikawa kwamba pia

22*a* MWM Paka mafuta. | 23*a* 1 Sam. 8:10–18; Mos. 29:16–23.

alimzaa Kibu katika umri wake wa uzee. Na ikawa kwamba Kibu alitawala badala yake; na Kibu akamzaa Korihori.

4 Na wakati Korihori alipokuwa na miaka thelathini na miwili aliasi dhidi ya baba yake, na akaenda kuishi katika nchi ya Nehori; na alizaa wana na mabinti, na wakawa warembo sana; kwa hivyo Korihori aliwavutia wengi kumfuata.

5 Na baada ya kukusanya pamoja jeshi alikuja kwenye nchi ya Moroni ambapo mfalme aliishi, na kumchukua mateka, ambako kulileta kutimia [a]msemo wa kaka wa Yaredi kwamba watawekwa kwenye utumwa.

6 Sasa nchi ya Moroni, ambako mfalme aliishi, ilikuwa karibu na nchi inayoitwa Ukiwa na Wanefi.

7 Na ikawa kwamba Kibu aliishi utumwani, na watu wake chini ya Korihori mwana wake, mpaka alipokuwa mzee sana; walakini Kibu alimzaa Shule katika umri wake wa uzee, wakati alipokuwa bado utumwani.

8 Na ikawa kwamba Shule alimkasirikia kaka yake; na Shule akaongezeka nguvu, na akawa mwenye nguvu kulingana na nguvu ya mwanaume; na pia alikuwa mkuu kwa kuhukumu.

9 Kwa hivyo, alienda kwenye kilima cha Efraimu, na akayeyusha chuma kutoka kwa kile kilima, na kutengeneza mapanga kutoka kwa chuma cha pua kwa wale ambao alikuwa amekuja nao; na baada ya kuwahami kwa panga alirejea kwenye mji wa Nehori, na kupigana vita na kaka yake Korihori, kwa njia ambayo alijipatia ufalme na kuurudisha kwa baba yake Kibu.

10 Na sasa kwa sababu ya kitu ambacho Shule alifanya, baba yake alimpa ufalme; kwa hivyo alianza kutawala badala ya baba yake.

11 Na ikawa kwamba alitoa hukumu kwa haki; na alisambaza ufalme wake juu ya nchi yote, kwani watu walikuwa wameongezeka sana.

12 Na ikawa kwamba Shule pia alizaa wana na mabinti wengi.

13 Na Korihori alitubu kutoka kwa maovu mengi ambayo alikuwa ameyafanya; kwa hivyo Shule alimpatia uwezo katika ufalme wake.

14 Na ikawa kwamba Korihori alikuwa na wana wengi na mabinti wengi. Na miongoni mwa wana wa Korihori kulikuwa na mmoja ambaye jina lake lilikuwa Nuhu.

15 Na ikawa kwamba Nuhu aliasi dhidi ya Shule, mfalme, na pia baba yake Korihori, na kumvuta kaka yake Kohori kumfuata, na pia ndugu zake wote na wengi wa watu wengine.

16 Na alifanya vita na Shule, mfalme, ambamo kwake alipata nchi ya urithi wa kwanza; na akawa mfalme juu ya sehemu hiyo ya nchi.

17 Na ikawa kwamba alifanya vita tena na Shule, mfalme; na akamshika Shule, mfalme, na

7 5*a* Eth. 6:23.

kumchukua mbali hadi Moroni kama mateka.

18 Na ikawa wakati alipokuwa karibu kumuua, wana wa Shule walienda polepole hadi kwenye nyumba ya Nuhu usiku na kumuua, na walivunja mlango wa gereza na kumtoa nje baba yao, na kumweka kwenye kiti cha enzi cha ufalme wake.

19 Kwa hivyo, mwana wa Nuhu aliimarisha ufalme wake badala yake; walakini hawakupata uwezo tena juu ya Shule, mfalme, na watu waliokuwa chini ya utawala wa Shule, mfalme, walifanikiwa sana na walikuwa na nguvu.

20 Na nchi iligawanywa; na kukawa na falme mbili, falme ya Shule, na falme ya Kohori, mwana wa Nuhu.

21 Na Kohori, mwana wa Nuhu, alisababisha kwamba watu wake wapigane na Shule, ambapo Shule aliwashinda na kumuua Kohori.

22 Na sasa Kohori alikuwa na mwana aliyeitwa Nimrodi; na Nimrodi alisalimisha ufalme wa Kohori kwa Shule, na alipata fadhila za Shule; kwa hivyo Shule alimpatia mapendeleo mengi, na alifanya chochote kulingana na kutaka kwake katika ufalme wa Shule.

23 Na pia katika utawala wa Shule kulikuwa na manabii miongoni mwa watu, ambao walitumwa kutoka kwa Bwana, wakitabiri kwamba uovu na kuabudu [a]sanamu kwa watu kulikuwa kumeleta laana juu ya nchi, na wangeangamizwa kama hawangetubu.

24 Na ikawa kwamba watu walitoa matusi dhidi ya manabii, na kuwafanyia mzaha. Na ikawa kwamba mfalme Shule aliwaadhibu wale wote waliotoa matusi dhidi ya manabii.

25 Na aliweka sheria kote nchini, ambayo iliwapatia manabii uwezo kwamba wangeenda popote walipotaka; na katika njia hii watu waliletwa kwenye toba.

26 Na kwa sababu watu walitubu kutoka kwa uovu wao na kuabudu sanamu kwao Bwana aliwasamehe, na wakaanza kufanikiwa tena nchini. Na ikawa kwamba Shule alizaa wana na mabinti katika umri wake wa uzee.

27 Na hapakuwepo na vita tena katika siku za Shule; na alikumbuka vitu vikubwa ambavyo Bwana alikuwa amewafanyia babu zake katika kuwaleta [a]kuvuka kilindi kikubwa hadi kwenye nchi ya ahadi; kwa hivyo alitoa hukumu katika haki siku zake zote.

MLANGO WA 8

Kuna mzozo na ubishi kuhusu ufalme—Akishi anaunda kundi la siri kwa kiapo ambalo wanachama wake walipanga kumuua mfalme—Makundi ya siri ni ya ibilisi na yanasababisha uharibifu wa mataifa—Wayunani wa siku hizi wanaonywa dhidi ya kundi ovu la siri ambalo litataka kugeuza

23*a* MWM Kuabudu sanamu.

27*a* Eth. 6:4, 12.

uhuru wa ardhi, mataifa, na nchi zote.

Na ikawa kwamba alimzaa Omeri, na Omeri alitawala badala yake. Na Omeri akamzaa Yaredi; na Yaredi akazaa wana na mabinti.

2 Na Yaredi aliasi dhidi ya baba yake, na akaenda kuishi katika nchi ya Hethi. Na ikawa kwamba aliwadanganya watu wengi, kwa sababu ya ujanja wa maneno yake, mpaka alipopata nusu ya ule ufalme.

3 Na baada ya kupata nusu ya ufalme alifanya vita na baba yake, na akamweka baba yake kwenye utumwa, na akamfanya kutumika katika utumwa;

4 Na sasa, katika siku za utawala wa Omeri alikuwa katika utumwa nusu ya maisha yake. Na ikawa kwamba alizaa wana na mabinti, miongoni mwao ambamo walikuwa Esromu na Koriantumuri;

5 Na walikasirika sana kwa sababu ya vitendo vya Yaredi kaka yao, mpaka kwamba waliunda jeshi na kufanya vita na Yaredi. Na ikawa kwamba walifanya vita na yeye wakati wa usiku.

6 Na ikawa kwamba baada ya kuua jeshi la Yaredi walikuwa karibu kumuua yeye pia; na aliwasihi kwamba wasimuue, na angetoa ufalme kwa baba yake. Na ikawa kwamba walimwachia maisha yake.

7 Na sasa Yaredi alihuzunika sana kwa sababu ya kupoteza utawala, kwani alikuwa ameweka moyo wake kwa ufalme na utukufu wa ulimwengu.

8 Sasa binti wa Yaredi akiwa mrembo sana, na akiona huzuni wa baba yake, alifikiria kutafuta mpango ambamo kwake angerudisha utawala kwa baba yake.

9 Sasa binti wa Yaredi alikuwa mrembo sana. Na ikawa kwamba aliongea na baba yake, na kusema kwake: Kwa nini baba yangu una huzuni sana? Hujasoma maandishi ambayo babu zetu walileta kutoka ng'ambo ya kilindi kikubwa? Tazama, hakuna historia kuhusu wale wa kale, kwamba wao kwa mipango yao ya [a]siri walipata falme na utukufu mkuu?

10 Na sasa, kwa hivyo, acha baba yangu amtumainie Akishi, mwana wa Kimnori; na tazama, mimi ni mrembo, na [a]nitacheza mbele yake, na nitampendeza, kwamba atatamani kwamba niwe mke wake; kwa hivyo ikiwa atataka kwamba umpatie mimi kama mke wake, ndipo utasema: Nitakupatia tu ikiwa utaniletea kichwa cha baba yangu, mfalme.

11 Na sasa Omeri alikuwa rafiki ya Akishi; kwa hivyo, wakati Yaredi alipokuwa amemtumainia Akishi, binti wa Yaredi alicheza mbele yake kwamba akampendeza, mpaka kwamba alimtaka awe mke wake. Na ikawa kwamba alisema kwa Yaredi: Nipatie mimi awe mke wangu.

12 Na Yaredi akamwambia:

8 9*a* Hel. 6:26–30; 3 Ne. 6:28; Musa 5:51–52.
10*a* Mk. 6:22–28.

Nitamkabidhi kwako, ikiwa utanileteа kichwa cha baba yangu, mfalme.

13 Na ikawa kwamba Akishi alikusanya kwenye nyumba ya Yaredi jamaa zake wote, na kuwaambia: Mtaapa kwangu kwamba mtakuwa waaminifu kwangu kwa kitu ambacho nitataka kutoka kwenu?

14 Na ikawa kwamba wote [a]waliapa kwake, katika yule Mungu wa mbinguni, na pia na mbingu, pia na dunia, na vichwa vyao, kwamba yeyote atakayetofautiana na usaidizi ambao Akishi alitaka atapoteza kichwa chake; na yeyote atakayetoa wazi kitu chochote ambacho Akishi amewafahamisha, huyo huyo atapoteza maisha yake.

15 Na ikawa kwamba hivyo ndivyo walikubaliana na Akishi. Na Akishi alitoa [a]kiapo kwao ambacho kilitolewa na wale wa kale ambao pia walitaka uwezo, ambao ulitolewa hata kutoka kwa [b]Kaini, ambaye alikuwa muuaji kutoka mwanzo.

16 Na yalihifadhiwa kwa uwezo wa ibilisi kutoa hivi viapo kwa watu, kuwaweka gizani, kuwasaidia wale wanaotafuta nguvu kupata uwezo, na kuua, na kupora, na kudanganya, na kutenda aina yote ya maovu na ukahaba.

17 Na alikuwa binti wa Yaredi aliyemwekea moyo wa kutafuta hivi vitu vya zamani; na Yaredi akaiweka kwenye moyo wa Akishi; kwa hivyo, Akishi aliwaambia jamaa zake na marafiki akiwapotosha mbali na ahadi zisizo za haki kufanya kitu chochote alichotaka.

18 Na ikawa kwamba waliunda [a]kundi la siri, hata kama vile watu wa zamani walivyofanya; kundi ambalo lilikuwa la kuchukiza sana na ovu kushinda yote, machoni pa Mungu;

19 Kwani Bwana hafanyi kazi katika makundi maovu ya siri, wala hataki kwamba mtu amwage damu, lakini katika vitu vyote amevikataza tangu mwanzo wa binadamu.

20 Na sasa mimi, Moroni, siandiki aina ya viapo na makundi, kwani imefanywa kujulikana kwangu kwamba viko miongoni mwa watu wote, na viko miongoni mwa Walamani.

21 Na vimesababisha [a]kuangamizwa kwa watu hawa ambao ninawazungumzia sasa, na pia kuangamia kwa watu wa Nefi.

22 Na taifa lolote litakalokubali makundi maovu ya siri kama haya, kupata uwezo na utajiri, hadi kuenea juu ya taifa, tazama, wataangamizwa; kwani Bwana hatakubali kwamba [a]damu ya watakatifu wake, ambayo itamwagwa na hao, ilie siku zote kutoka mchangani kwa kulipiza [b]kisasi juu yao na bado halipizi kisasi.

23 Kwa hivyo, Ee ninyi Wa-

14 *a* MWM Kukufuru, Kufuru.
15 *a* MWM Kiapo.
b Mwa. 4:7–8; Musa 5:28–30.
18 *a* MWM Makundi maovu ya siri.
21 *a* Hel. 6:28.
22 *a* Morm. 8:27, 40–41.
b MWM Kisasi.

yunani, ni hekima kwa Mungu kwamba vitu hivi vionyeshwe kwenu, kwamba kwa sababu hiyo mngetubu kutoka kwa dhambi zenu, na msikubali kwamba haya makundi maovu ya siri yawe juu yenu, ambayo yamejengwa kupata [a]uwezo na utajiri—na kazi, ndiyo, hata kazi ya uharibifu, ije kwenu, ndiyo, hata upanga wa haki ya Mungu wa milele utawaangukia, kwa upinduaji wenu na uharibifu ikiwa mtakubali vitu hivi kuweko.

24 Kwa hivyo, Bwana anawaamrisha, wakati mtakapoona vitu hivi vikija miongoni mwenu kwamba mtaamka kwa ufahamu wa hali yenu ya kutisha, kwa sababu ya kundi hili la siri ambalo litakuwa miongoni mwenu; au ole kwake, kwa sababu ya damu ya wale ambao wameuawa; kwani hulia kutoka mavumbini kwa kisasi juu yake, na pia juu ya walioliunda.

25 Kwani inakuwa kwamba yeyote anayeijenga hutaka kuangusha [a]uhuru wa ardhi, mataifa na nchi zote; na huleta kutimizwa uangamizo wa watu wote, kwani inaanzishwa na ibilisi, ambaye ni baba wa uwongo wote; hata yule yule mdanganyifu [b]aliyedanganya wazazi wetu wa kwanza, ndiyo, hata ndiye yule yule mdanganyifu ambaye alisababisha binadamu kutenda mauaji tangu mwanzo; ambaye ameshupaza mioyo ya watu kwamba wamewaua manabii, na kuwapiga kwa mawe, na kuwatupa nje tangu mwanzo.

26 Kwa hivyo, mimi, Moroni, nimeamriwa kuandika vitu hivi ili uovu ungeondolewa mbali, na ili wakati ungekuja ambapo Shetani [a]hawezi kuwa na uwezo kwa mioyo ya watoto wa watu, lakini kwamba [b]wangeshawishiwa kutenda mema siku zote, kwamba wangekuja kwenye chemichemi ya ukweli wote na kuokolewa.

MLANGO WA 9

Utawala unaendelea mbele kutoka kwa mmoja hadi kwa mwingine kufuatana na ukoo, hila, na mauaji—Emeri alimuona Mwana wa Haki—Manabii wengi wanahubiri toba—Njaa na nyoka wa sumu wanaua watu.

Na sasa mimi, Moroni, naendelea na maandishi yangu. Kwa hivyo, tazama, ikawa kwamba kwa sababu ya [a]makundi maovu ya siri ya Akishi na marafiki zake, tazama, walipindua utawala wa Omeri.

2 Walakini, Bwana alikuwa na huruma kwa Omeri, na pia kwa wanawe na mabinti zake ambao hawakutaka kuangamizwa naye.

3 Na Bwana alimwonya Omeri kwenye ndoto kwamba aondoke nje ya nchi; kwa hivyo Omeri aliondoka nje ya nchi na jamaa

23 *a* 1 Ne. 22:22–23; Musa 6:15.
25 *a* MWM Huru, Uhuru.
b Mwa. 3:1–13; 2 Ne. 9:9; Mos. 16:3; Musa 4:5–19.
26 *a* 1 Ne. 22:26.
b 2 Ne. 33:4; Moro. 7:12–17.
9 1 *a* Eth. 8:13–17.

zake, na kusafiri siku nyingi, na akaja juu na kupita kando ya kilima cha [a]Shimu, na akaja juu kando ya mahali [b]ambapo Wanefi waliangamizwa, na kutoka hapo akaenda upande wa mashariki, na akaja mahali palipoitwa Ablomu, kando ya ukingo wa bahari, na hapo akapiga hema lake, na pia wanawe na mabinti zake, na jamaa yake yote, isipokuwa Yaredi na jamaa zake.

4 Na ikawa kwamba Yaredi alitawazwa kuwa mfalme juu ya watu, na wale walio waovu; na akampatia Akishi binti wake kuwa mke wake.

5 Na ikawa kwamba Akishi alitaka kutoa maisha ya baba mkwe wake; na akauliza usaidizi kutoka kwa wale ambao alikuwa amewaapisha kwa kiapo cha watu wa kale, na walipata kichwa cha baba mkwe wake, wakati alipokuwa akikalia kiti cha enzi, akikutana na watu wake.

6 Kwani uenezaji wa hiki chama kiovu na cha siri ulikuwa mkuu kwamba kilikuwa kimebadilisha mioyo ya watu wote; kwa hivyo Yaredi aliuawa akiwa juu ya kiti chake cha enzi, na Akishi akatawala badala yake.

7 Na ikawa kwamba Akishi alianza kuwa na wivu kwa mwana wake, kwa hivyo alimfunga gerezani, na kumpatia chakula kidogo au bila mpaka aliposhindwa na kufariki.

8 Na sasa kaka wa yule aliyeumia hadi kifo, (jina lake lilikuwa Nimra) alikasirika na baba yake kwa sababu ya yale ambayo baba yake alimfanyia kaka yake.

9 Na ikawa kwamba Nimra alikusanya idadi ndogo ya watu, na wakatoroka kutoka nchini, na wakaja kuishi na Omeri.

10 Na ikawa kwamba Akishi alizaa wana wengine, na walipendelewa na watu, ingawaje walikuwa wameapa kwake kufanya aina yote ya uovu kulingana na yale aliyokuwa anataka.

11 Sasa watu wa Akishi walitaka utajiri, hata vile Akishi alivyotaka uwezo; kwa hivyo, wana wa Akishi waliwapatia pesa, kwa njia ambayo ilishawishi sehemu kubwa ya watu kuwafuata.

12 Na kulianza kuwa na vita baina ya watoto wa Akishi na Akishi, ambavyo vilidumu kwa muda wa miaka mingi, ndiyo, hadi kwenye maangamizo ya watu karibu wote wa ufalme, ndiyo, hata wote isipokuwa watu thelathini, na wale waliotoroka na nyumba ya Omeri.

13 Kwa hivyo, Omeri alirudishwa tena kwenye nchi ya urithi wake.

14 Na ikawa kwamba Omeri alianza kuzeeka; walakini, katika umri wake wa uzee alimzaa Emeri; na alimtawaza Emeri kuwa mfalme kutawala badala yake.

15 Na baada ya kumtawaza Emeri kuwa mfalme aliona amani nchini kwa muda wa

3 *a* Morm. 1:3; 4:23. | *b* Morm. 6:1–15.

miaka miwili, na akafariki, akiwa ameona siku nyingi, ambazo zilikuwa na huzuni mwingi. Na ikawa kwamba Emeri alitawala mahala pake, na akachukua nafasi ya baba yake.

16 Na Bwana akaanza tena kutoa laana kutoka kwa nchi, na nyumba ya Emeri ilifanikiwa sana wakati wa utawala wa Emeri; na kwa muda wa miaka sitini na mbili walikuwa na nguvu sana, hadi wakawa matajiri kupita kiasi—

17 Wakiwa na kila aina ya matunda, na nafaka, na hariri, na kitani kizuri, na dhahabu, na fedha, na vitu vya thamani;

18 Na pia kila aina ya mifugo, ya ng'ombe wa kiume, na ng'ombe wa kike, na kondoo, na nguruwe, na mbuzi, na pia aina nyingi za wanyama ambao walikuwa wa kufaa kwa chakula cha binadamu.

19 Na pia walikuwa na [a]farasi, na punda, na kulikuwa na ndovu na kurelomu na kumomu; wote ambao walikuwa wa kufaa kwa binadamu, na zaidi ndovu na kurelomu na kumomu.

20 Na hivyo Bwana alitoa baraka zake kwa nchi hii, ambayo ilikuwa [a]nzuri kuliko nchi zote; na aliamuru kwamba yeyote atakayeimiliki ile nchi aimiliki kwa kusudi la Bwana, au [b]wangeangamia baada ya kuwa waovu wa kutosha; kwani juu ya watu kama hawa, asema Bwana: Nitatoa utimilifu wa ghadhabu yangu.

21 Na Emeri alitoa uamuzi wake kwa haki siku zake zote, na alizaa wana na mabinti wengi; na alimzaa Koriantumu, na akamtawaza Koriantumu kutawala badala yake.

22 Na baada ya kumtawaza Koriantumu kutawala badala yake aliishi miaka minne, na aliona amani katika nchi; ndiyo, na hata alimwona [a]Mwana wa Ukweli, na alifurahi na kusifu katika maisha yake; na alikufa katika hali ya amani.

23 Na ikawa kwamba Koriantumu aliishi kama baba yake, na alijenga miji mingi mikubwa, na alitoa kile ambacho kilikuwa kizuri kwa watu wake katika siku zake zote. Na ikawa kwamba hakupata watoto hadi akawa mzee kabisa.

24 Na ikawa kwamba mke wake alifariki akiwa na miaka mia moja na miwili. Na ikawa kwamba Koriantumu, katika miaka yake ya uzee, alioa mwanamwali, na akazaa wana na mabinti; kwa hivyo aliishi mpaka alipokuwa na miaka mia moja na arubaini na miwili.

25 Na ikawa kwamba alimzaa Komu, na Komu akatawala badala yake; na alitawala kwa miaka arubaini na tisa, na akamzaa Hethi; na pia alizaa wana na mabinti wengine.

26 Na watu walikuwa wameenea tena juu ya uso wa nchi, na kukaanza tena kuwa na uovu mkuu sana juu ya uso wa nchi, na Hethi alianza kujiingiza kwenye mipango ya siri tena ya

19 *a* 1 Ne. 18:25.
20 *a* Eth. 2:15.
b Eth. 2:8–11.
22 *a* 3 Ne. 25:2.

zamani, kumwangamiza baba yake.

27 Na ikawa kwamba alimwondoa baba yake, kwani alimchinja kwa upanga wake mwenyewe; na akatawala badala yake.

28 Na kukatokea manabii nchini tena, wakihubiri toba kwao—kwamba watayarishe njia ya Bwana au kungetokea laana juu ya uso wa nchi; ndiyo, hata kungekuwa na njaa kuu, ambamo kwake wangeangamizwa kama hawakutubu.

29 Lakini watu hawakuamini maneno ya manabii, lakini waliwatupa nje; na wengine wao waliwatupa kwenye mashimo na kuwaacha waangamie. Na ikawa kwamba walifanya vitu hivi vyote kufuatana na amri ya mfalme, Hethi.

30 Na ikawa kwamba kulianza kuwa na upungufu mkuu juu ya nchi, na wakazi wakaanza kuangamizwa kwa haraka sana kwa sababu ya upungufu huo, kwani haikuwepo mvua juu ya uso wa ardhi.

31 Na kukatokea nyoka wa sumu pia juu ya uso wa nchi, na waliwauma watu wengi. Na ikawa kwamba mifugo yao ilikimbilia mbele ya nyoka wenye sumu, kuelekea nchi iliyokuwa upande wa kusini, ambayo iliitwa na Wanefi [a]Zarahemla.

32 Na ikawa kwamba kulikuwa na wengi wao waliokufa njiani; walakini, kulikuwa na baadhi yao waliotorokea kwenye nchi ya kusini.

33 Na ikawa kwamba Bwana alisababisha [a]nyoka wasiwafuate tena, lakini wafunge njia ili watu wasiweze kupita, kwamba yeyote atakayejaribu kupita angeuawa na nyoka wa sumu.

34 Na ikawa kwamba watu walifuata njia ya mifugo, na walikula mizoga ya wale waliokufa njiani, mpaka walipokula wote. Sasa wakati watu walipoona kwamba lazima wafe walianza [a]kutubu uovu wao na kumwomba Bwana.

35 Na ikawa kwamba baada ya [a]kujinyenyekeza vya kutosha mbele ya Bwana alileta mvua juu ya uso wa ardhi; na watu wakaanza kufanikiwa tena, na kukaanza kuwa na matunda katika upande wa nchi za kaskazini, na katika nchi zote zilizokuwa karibu. Na Bwana alionyesha uwezo wake kwao katika kuwaokoa kutoka kwenye njaa.

MLANGO WA 10

Mfalme mmoja anamfuata mwingine—Wafalme wengine ni wenye haki; wengine ni waovu—Wakati haki inaenea, watu hubarikiwa na kufanikishwa na Bwana.

Na ikawa kwamba Shezi, ambaye alikuwa ukoo wa Hethi—kwani Hethi aliangamia kwa njaa, na jamaa yake yote isipokuwa Shezi—kwa hivyo Shezi alianza tena kuwaleta wale watu ambao walikuwa wamegawanyika pamoja.

2 Na ikawa kwamba Shezi

31*a* Omni 1:13.
33*a* Hes. 21:6–9.
34*a* Alma 34:34; M&M 101:8.
35*a* M&M 5:24.

alikumbuka kuangamizwa kwa babu zake, na akaweka utawala wa haki; kwani alikumbuka kile Bwana alichofanya kuwaleta Yaredi na kaka yake [a]kuwavusha kilindi; na alitembea katika njia za Bwana; na alizaa wana na mabinti.

3 Na mwana wake mkubwa, ambaye jina lake lilikuwa Shezi, aliasi dhidi yake; hata hivyo, Shezi aliuawa na mwizi, kwa sababu ya utajiri wake mwingi, ambao ulileta tena amani kwa baba yake.

4 Na ikawa kwamba baba yake alijenga miji mingi juu ya uso wa nchi, na watu walianza tena kuenea kwenye uso wa nchi. Na Shezi aliishi na kuwa na umri mkubwa sana; na alimzaa Riplakishi. Na alikufa, na Riplakishi alitawala badala yake.

5 Na ikawa kwamba Riplakishi hakufanya yale yaliyo mema machoni mwa Bwana, kwani alikuwa na wake wengi na wanawake wengi wa [a]kinyumba, na aliwawekea watu mizigo mizito ambayo ilikuwa migumu kuhimili; ndiyo, aliwatoza kodi kubwa; na kwa ile kodi alijenga nyumba nyingi kubwa.

6 Na alijitengenezea enzi maridadi sana; na alijenga magereza mengi, na yeyote ambaye alikataa kulipa ushuru alitiwa gerezani; na yeyote ambaye hakuweza kulipa ushuru alitiwa gerezani; na alisababisha kwamba wafanye kazi siku zote kwa mategemeo yao; na yeyote aliyekataa kufanya kazi alisababisha auawe.

7 Kwa hivyo alipata kazi yake nzuri, ndiyo, hata dhahabu yake laini alisababisha kusafishwa gerezani; na kila aina ya kazi alisababisha kutengenezwa gerezani. Na ikawa kwamba aliwatesa watu kwa ukahaba wake na machukizo yake.

8 Na baada ya kutawala kwa muda wa miaka arubaini na miwili watu waliasi dhidi yake; na kulianza kuwa na vita tena nchini, mpaka kwamba Riplakishi aliuawa, na ukoo wake ulifukuzwa kutoka nchini.

9 Na ikawa baada ya muda wa miaka mingi, Moriantoni, (ambaye alikuwa wa ukoo wa Riplakishi) alikusanya pamoja jeshi la wasiofukuzwa, na akaenda mbele na kupigana na watu; na akapata uwezo juu ya miji mingi; na vita vilikuwa vikali sana, na vilikuwako kwa muda wa miaka mingi; na akachukua nchi yote, na akajiweka mfalme wa nchi yote.

10 Na baada ya kujiweka kuwa mfalme alirahisisha mizigo ya watu, ambako alipata mapendeleo ya watu, na walimtawaza kuwa mfalme wao.

11 Na aliwafanyia watu haki, lakini sio kwake mwenyewe kwa sababu ya ukahaba wake mwingi; kwa hivyo alikatwa kutoka kwenye uwepo wa Bwana.

12 Na ikawa kwamba Moriantoni alijenga miji mingi, na watu walitajirika sana chini ya

10 2*a* Eth. 6:1–12. | 5*a* Yak. (KM) 3:5; Mos. 11:2.

utawala wake, katika majengo, na katika dhahabu na fedha, na katika kukuza nafaka, na katika mifugo, na wanyama, na vitu kama hivyo vilivyorudishwa kwao.

13 Na Moriantoni aliishi akawa na umri mkubwa sana, na ndipo akamzaa Kimu; na Kimu akatawala badala ya baba yake; na alitawala kwa miaka minane, na baba yake akafariki. Na ikawa kwamba Kimu hakutawala kwa haki, kwa hivyo hakupendelewa na Bwana.

14 Na kaka yake aliasi dhidi yake, ambako alimweka kifungoni; na alibaki kifungoni siku zake zote; na alizaa wana na mabinti katika utumwa, na katika umri wake wa uzee alimzaa Lawi; na akafa.

15 Na ikawa kwamba Lawi alitumika kwenye utumwa baada ya kifo cha baba yake, kwa muda wa miaka arubaini na miwili. Na alifanya vita dhidi ya mfalme wa nchi, ambayo kwayo alishinda na kujipatia utawala.

16 Na baada ya kujipatia utawala alifanya yale yaliyokuwa sawa kwa maoni ya Bwana; na watu walifanikiwa katika nchi; na aliishi kwa umri mzuri wa uzee, na alizaa wana na mabinti; na pia alimzaa Koromu, ambaye alimtawaza mfalme badala yake.

17 Na ikawa kwamba Koromu alifanya yale yaliyokuwa mema kwa maoni ya Bwana siku zake zote; na alizaa wana na mabinti wengi; na baada ya kuishi siku nyingi alifariki, kama vile kila kitu ambacho huwa duniani, na Kishi alitawala badala yake.

18 Na ikawa kwamba Kishi alikufa pia, na Libu alitawala badala yake.

19 Na ikawa kwamba Libu pia alifanya yale yaliyokuwa mema katika macho ya Bwana. Na katika siku za Libu nyoka wenye [a]sumu waliangamizwa. Kwa hivyo walienda katika nchi iliyokuwa upande wa kusini, kuwinda chakula kwa watu wa nchi, kwani nchi ilifunikwa na wanyama wa misitu. Na Libu pia alikuwa mwindaji mkuu.

20 Na walijenga mji mkubwa kando ya shingo nyembamba ya nchi, kando ambapo bahari hutenga nchi.

21 Na walihifadhi nchi upande wa kusini kwa jangwa, kupata mawindo. Na uso wote wa nchi upande wa kaskazini ulifunikwa na wakazi.

22 Na walikuwa wenye bidii sana, na walinunua na kuuziana biashara wao kwa wao, ili wapate faida.

23 Na walifanya kazi katika kila aina ya madini, na walitengeneza dhahabu, na fedha, na [a]chuma, na shaba nyeupe, na kila aina ya madini; na waliichimba kutoka udongoni; kwa hivyo, walitupa rundo kubwa za mchanga ili wapate madini, ya dhahabu, na ya fedha, na ya chuma, na ya shaba nyekundu. Na walifanya kazi yote iliyo laini.

24 Na walikuwa na hariri, na

19 *a* Eth. 9:31.

23 *a* 2 Ne. 5:15.

vitani vilivyoshonwa vizuri; na walishona aina yote ya nguo, ili wajivike kutokana na uchi wao.

25 Na walitengeneza kila aina ya vyombo kulimia mashamba, pia vya kulimia na kupanda, kuvuna na kupalilia, na pia kupura.

26 Na walitengeneza kila aina ya vyombo ambavyo wanyama wao walifanyia kazi.

27 Na walitengeneza kila aina ya silaha za vita. Na walifanya aina yote ya ufundi wa hali ya juu.

28 Na hakungekuwa na watu waliobarikiwa kuliko hao, na kufanikishwa zaidi kwa mkono wa Bwana. Na walikuwa katika nchi iliyokuwa nzuri kuliko nchi zote, kwani Bwana alikuwa ameizungumza.

29 Na ikawa kwamba Libu aliishi miaka mingi, na alizaa wana na mabinti; na pia alimzaa Hearthomu.

30 Na ikawa kwamba Hearthomu alitawala badala ya baba yake. Na baada ya Hearthomu kutawala kwa miaka ishirini na minne, tazama, ufalme ulitolewa kutoka kwake. Na alitumikia miaka mingi kwenye utumwa, ndiyo, hata siku zake zote zilizosalia.

31 Na alimzaa Hethi, na Hethi aliishi kwenye utumwa maisha yake yote. Na Hethi alimzaa Haruni, na Haruni aliishi utumwani maisha yake yote; na alimzaa Amnigada, na Amnigada pia aliishi kwenye utumwa siku zake zote; na alimzaa Koriantumu, na Koriantumu aliishi kwenye utumwa siku zake zote; na alimzaa Komu.

32 Na ikawa kwamba Komu alivuta nusu ya ule utawala kumfuata. Na alitawala juu ya nusu ya ufalme kwa miaka arubaini na miwili; na akapigana na mfalme, Amgidi, na walipigana kwa muda wa miaka mingi, wakati ambao Komu alimshinda Amgidi, na akawa na uwezo juu ya utawala uliosalia.

33 Na katika siku za Komu, kulianza kuwa na wanyang'anyi katika nchi; na walianza kutumia mipango ya zamani, na kupeana "viapo kwa njia ya wale wa kale, na kutaka tena kuharibu ufalme.

34 Sasa Komu alipigana sana dhidi yao; walakini, hakuwashinda.

MLANGO WA 11

Vita, mafarakano, na uovu unatawala maisha ya Wayaredi—Manabii watabiri kuangamizwa kabisa kwa Wayaredi wasipotubu—Watu wanakataa maneno ya manabii.

Na kulitokea pia katika siku za Komu manabii wengi, na walitoa unabii wa uharibifu wa wale watu wakuu isipokuwa watubu, na kumgeukia Bwana, na kuacha mauaji yao na uovu.

2 Na ikawa kwamba manabii walikataliwa na watu, na walimkimbilia Komu kwa ulinzi, kwani watu walitaka kuwaangamiza.

33*a* MWM Kiapo; Makundi maovu ya siri.

3 Na walitoa unabii wa vitu vingi kwa Komu; na alibarikiwa kwa siku zake zote zilizosalia.

4 Na aliishi kwa umri mzuri wa uzee, na alimzaa Shiblomu; na Shiblomu akatawala badala yake. Na kaka wa Shiblomu aliasi dhidi yake, na kukaanza kuwa na vita vikubwa katika nchi yote.

5 Na ikawa kwamba kaka wa Shiblomu alisababisha kwamba manabii wote waliotoa unabii wa uharibifu wa watu wauawe;

6 Na kulikuwa na msiba mkubwa katika nchi yote, kwani walikuwa wameshuhudia kwamba laana kubwa ingekuja kwenye nchi, na pia juu ya watu, na kwamba kungekuwa na uharibifu mkuu miongoni mwao, mkubwa kuliko yote iliyowahi kuwa usoni mwa dunia, na mifupa yao ingekuwa kama [a]mafungu ya mchanga usoni mwa nchi isipokuwa watubu uovu wao.

7 Na hawakusikiliza sauti ya Bwana, kwa sababu ya makundi yao maovu; kwa hivyo, kulianza kuwa na vita na mabishano katika nchi yote, na pia njaa nyingi na maradhi ya kuambukiza, mpaka kwamba kukawa na uharibifu mkuu, ambao haujawahi kujulikana usoni mwa dunia; na haya yote yalikuja kutimia katika siku za Shiblomu.

8 Na watu walianza kutubu uovu wao; na kadiri walivyofanya hivyo, Bwana alikuwa na [a]huruma kwao.

9 Na ikawa kwamba Shiblomu aliuawa, na Sethi akaletwa kwenye utumwa, na aliishi kwenye utumwa siku zake zote.

10 Na ikawa kwamba Aha, mwana wake, alichukua ufalme; na akawatawala watu siku zake zote. Na alifanya aina yote ya uovu katika siku zake, ambamo kwake alisababisha umwagaji wa damu nyingi; na siku zake zilikuwa chache.

11 Na Ethemu, akiwa wa ukoo wa Aha, alichukua ufalme; na pia alifanya yale yaliyokuwa maovu katika siku zake.

12 Na ikawa kwamba katika siku za Ethemu kulitokea manabii wengi, na wakatoa unabii tena kwa watu; ndiyo, walitabiri kwamba Bwana angewaharibu kabisa kutoka kwa uso wa dunia isipokuwa watubu uovu wao.

13 Na ikawa kwamba watu walishupaza mioyo yao, na [a]hawangesikiliza maneno yao; na manabii waliomboleza na kujitoa miongoni mwa watu.

14 Na ikawa kwamba Ethemu alitoa hukumu katika uovu siku zake zote; na alimzaa Moroni. Na ikawa kwamba Moroni alitawala badala yake; na Moroni alifanya yale ambayo yalikuwa maovu mbele ya Bwana.

15 Na ikawa kwamba kulitokea [a]uasi miongoni mwa watu, kwa sababu ya lile kundi ovu la siri ambalo lilianzishwa kupata uwezo na faida; na kulitokea mtu mkubwa wa uovu miongoni mwao, na akapigana na Moroni, ambamo kwake alipindua

11 6*a* Omni 1:22; Eth. 14:21.
8*a* MWM Rehema, enye Rehema.
13*a* Mos. 16:2.
15*a* MWM Uasi.

nusu ya ufalme; na akashika nusu ya ule ufalme kwa miaka mingi.

16 Na ikawa kwamba Moroni alimpindua, na kupata ufalme tena.

17 Na ikawa kwamba kulitokea mtu mwingine mwenye nguvu; na alikuwa uzao wa kaka wa Yaredi.

18 Na ikawa kwamba alimwondoa Moroni na kuchukua ufalme; kwa hivyo, Moroni aliishi katika utumwa siku zake zote zilizosalia; na alimzaa Koriantori.

19 Na ikawa kwamba Koriantori aliishi katika utumwa siku zake zote.

20 Na katika siku za Koriantori kulitokea manabii wengi, na wakaagua vitu vikubwa na vya ajabu, na kuhubiri toba kwa watu, na isipokuwa watubu Bwana Mungu angetoa [a]hukumu dhidi yao hadi watakapoharibiwa kabisa.

21 Na kwamba Bwana Mungu angewatuma au kuwaleta mbele watu [a]wengine kumiliki nchi, kwa uwezo wake, kwa njia sawa ambayo aliwaleta babu zao.

22 Na walikataa maneno yote ya manabii, kwa sababu ya kundi lao la siri na machukizo yao maovu.

23 Na ikawa kwamba Koriantori alimzaa [a]Etheri, na akafariki, akiwa ameishi katika utumwa siku zake zote.

MLANGO WA 12

Nabii Etheri anawasihi watu waamini katika Mungu—Moroni anasimulia maajabu na miujiza inayofanywa kwa imani—Imani ilimwezesha kaka wa Yaredi kumwona Kristo—Bwana huwapa watu udhaifu ili wawe wanyenyekevu—Kaka wa Yaredi aliusogeza mlima Zerini kwa imani—Imani, tumaini, na hisani ni muhimu kwa wokovu—Moroni alimwona Yesu uso kwa uso.

Na ikawa kwamba siku za Etheri zilikuwa katika siku za utawala wa Koriantumuri; na [a]Koriantumuri alikuwa mfalme wa nchi yote.

2 Na [a]Etheri alikuwa nabii wa Bwana; kwa hivyo Etheri alijitokeza katika siku za Koriantumuri, na akaanza kutabiri kwa watu, kwani hangeweza [b]kuzuiliwa kwa sababu ya Roho wa Bwana ambayo ilikuwa ndani yake.

3 Kwani [a]alihubiri kutoka asubuhi, hata mpaka kwenda chini kwa jua, akihimiza watu kuamini katika Mungu kwenye toba wasije [b]wakaharibiwa, na akiwaambia kwamba kwa [c]imani vitu vyote hutimizwa—

4 Kwa hivyo, yeyote aaminiye katika Mungu angeweza kwa hakika [a]kutumaini ulimwengu bora, ndiyo, hata mahali katika mkono wa kulia wa Mungu, tumaini ambalo huja kutokana na

20*a* MWM Amua, Hukumu.
21*a* Eth. 13:20–21.
23*a* Eth. 1:6; 15:33–34.
12 1*a* Eth. 13:13–31.
2*a* MWM Etheri.
b Yer. 20:9; Eno. 1:26; Alma 43:1.
3*a* M&M 112:5.
b Eth. 11:12, 20–22.
c MWM Amini, Imani.
4*a* MWM Tumaini.

imani, hutengeneza [b]nanga kwa roho za watu, ambayo ingewafanya kuwa imara na thabiti, wakizidi sana kutenda [c]kazi njema, wakiongozwa [d]kumtukuza Mungu.

5 Na ikawa kwamba Etheri alitabiri vitu vikubwa vya ajabu kwa watu, ambavyo hawakuamini, kwa sababu hawakuviona.

6 Na sasa, mimi, Moroni, nitazungumza machache kuhusu vitu hivi; ninataka kuonyesha ulimwengu kwamba [a]imani ni vitu ambavyo [b]vinatumainiwa na [c]havionekani; kwa hivyo, msishindane kwa sababu hamwoni, kwani hamtapata ushahidi wowote mpaka baada ya [d]majaribu ya imani yenu.

7 Kwani ilikuwa kwa imani kwamba Kristo alijionyesha kwa babu zetu, baada ya kuamka kutoka kwa wafu; na hakujionyesha kwao mpaka walipokuwa na imani ndani yake; kwa hivyo, lazima iwe kwamba wengine walikuwa na imani ndani yake, kwani hakujionyesha kwa ulimwengu.

8 Lakini kwa sababu ya imani ya watu amejionyesha kwa watu wa ulimwengu, na kulitukuza jina la Baba, na alitayarisha njia ambayo kwake wengine wangeshiriki kwa mwito wa zawadi ya mbinguni, kwamba wangetumainia vitu hivyo ambavyo hawajaviona.

9 Kwa hivyo, mnaweza kuwa pia na tumaini, na muwe washiriki wa zawadi, ikiwa mtakuwa tu na imani.

10 Tazama ilikuwa kwa imani kwamba wale wa kale [a]waliitwa kwa mpango mtakatifu wa Mungu.

11 Kwa hivyo, kwa imani, sheria ya Musa ilitolewa. Lakini katika kipawa cha Mwana wake Mungu ametayarisha njia [a]bora zaidi; na ni kwa imani kwamba imetimizwa.

12 Kwani kama hakuna [a]imani miongoni mwa watoto wa watu, Mungu hawezi kufanya [b]miujiza miongoni mwao; kwa hivyo, hakujionyesha mpaka baada ya imani yao.

13 Tazama, ilikuwa imani ya Alma na Amuleki ambayo ilisababisha [a]gereza kuanguka chini.

14 Tazama, ilikuwa imani ya Nefi na Lehi ambayo ilileta [a]mabadiliko juu ya Walamani, kwamba walibatizwa kwa moto na kwa [b]Roho Mtakatifu.

15 Tazama, ilikuwa imani ya [a]Amoni na ndugu zake ambayo [b]ilileta muujiza mkuu miongoni mwa Walamani.

16 Ndiyo, na hata wote waliofanya [a]miujiza waliifanya kwa

4 *b* Ebr. 6:19.
c 1 Kor. 15:58.
d 3 Ne. 12:16.
6 *a* Ebr. 11:1.
b Rum. 8:24–25.
c Alma 32:21.
d 3 Ne. 26:11; M&M 105:19; 121:7–8.
10 *a* Alma 13:3–4.
MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
11 *a* 1 Kor. 12:31.
12 *a* 2 Ne. 27:23; Mos. 8:18; Moro. 7:37; M&M 35:8–11.
b Mt. 13:58; Morm. 9:20.
13 *a* Alma 14:26–29.
14 *a* Hel. 5:50–52.
b Hel. 5:45; 3 Ne. 9:20.
15 *a* Alma 17:29–39.
b MF kama ilivyotajwa katika Alma 17–26.
16 *a* MWM Muujiza.

sababu ya [b]imani, hata wale walioishi kabla ya Kristo na pia wale waliokuwako baadaye.

17 Na ilikuwa kwa imani kwamba wale wanafunzi watatu walipata ahadi kwamba [a]hawangeona kifo; na hawakupokea ahadi hiyo mpaka baada ya wao kuwa na imani.

18 Na wala kwa muda wowote hakujawa na yeyote ambaye amefanya miujiza mpaka awe na imani; kwa hivyo waliamini kwanza katika Mwana wa Mungu.

19 Na kulikuwa na wengi ambao imani yao ilikuwa na nguvu sana, hata [a]kabla ya Kristo kuja, ambao hawangeweza kuwekwa nyuma ya [b]pazia, lakini kwa ukweli waliona kwa macho yao vitu ambavyo walikuwa wameona kwa jicho la imani, na walifurahi.

20 Na tazama, tumeona katika maandishi haya kwamba mmoja wa hao alikuwa kaka wa Yaredi; kwani imani yake ilikuwa kubwa sana katika Mungu, kwamba Mungu alipoweka [a]kidole chake mbele hakuweza kukificha kutoka kwa uwezo wa kuona wa kaka wa Yaredi, kwa sababu ya neno lake ambalo alikuwa amemzungumzia, neno ambalo alikuwa amepokea kwa imani.

21 Na baada ya kaka wa Yaredi kuona kidole cha Bwana, kwa sababu ya [a]ahadi ambayo kaka wa Yaredi alikuwa amepata kwa imani, Bwana hangeweza kumzuia kuona chochote; kwa hivyo alimwonyesha vitu vyote, kwani hangeweza tena kuwekwa nje ya [b]pazia.

22 Na ni kwa imani kwamba babu zangu wamepata [a]ahadi kwamba vitu hivi vitakuja kwa ndugu zao kupitia kwa Wayunani; kwa hivyo Bwana ameniamuru, ndiyo, hata Yesu Kristo.

23 Na nikasema kwake: Bwana, Wayunani watachekelea vitu hivi, kwa sababu ya [a]unyonge wetu katika maandishi; kwani Bwana umetufanya [b]wakubwa katika neno kwa imani, lakini hujatufanya wakubwa kwenye maandishi; kwani umefanya watu hawa wote kwamba wanaweza kusema sana, kwa sababu ya Roho Mtakatifu ambaye umewapatia.

24 Na umetufanya kwamba tuweze kuandika tu machache, kwa sababu ya mikono yetu kutokuwa miepesi. Tazama, hujatufanya mabingwa kwa [a]uandishi kama kaka wa Yaredi, kwani ulimfanya ili vitu ambavyo aliandika viwe vikubwa hata vile wewe ulivyo, kwa kushinda mtu kuvisoma.

25 Umefanya pia maneno yetu yawe yenye nguvu na makubwa, hata kwamba hatuwezi kuyaandika; kwa hivyo, tunapoandika tunaona udhaifu wetu, na kuanguka kwa sababu

16 *b* Ebr. 11:7–40.
17 *a* 3 Ne. 28:7; Morm. 8:10–12.
19 *a* 2 Ne. 11:1–4; Yak. (KM) 4:4–5; Yar. 1:11; Alma 25:15–16.
b Eth. 3:6. MWM Pazia.
20 *a* Eth. 3:4.
21 *a* Eth. 3:25–26.
b Eth. 3:20; M&M 67:10–13.
22 *a* Eno. 1:13.
23 *a* Morm. 8:17; 9:33.
b 2 Ne. 33:1.
24 *a* MWM Lugha.

ya upangaji wa maneno yetu; na ninaogopa Wayunani wasije [a]wakacheka maneno yetu.

26 Na nilipokuwa nimesema hivi, Bwana alinizungumzia, akisema: Wajinga [a]hucheka, lakini wataomboleza; na neema yangu unatosha kwa walio wanyenyekevu, kwamba hawatafaidika na udhaifu wenu;

27 Na ikiwa watu watakuja kwangu nitawaonyesha [a]udhaifu wao. [b]Ninawapatia watu udhaifu ili katika udhaifu wao wawe wanyenyekevu; na [c]neema yangu inatosha watu wote ambao [d]hujinyenyekeza mbele yangu; kwani wakijinyenyekeza mbele yangu, na kuwa na imani ndani yangu, ndipo nitafanya vitu [e]dhaifu kuwa vya nguvu kwao.

28 Tazama, nitawaonyesha Wayunani udhaifu wao, na nitawaonyesha kwamba [a]imani, tumaini na hisani huwaleta kwangu—chimbuko la haki yote.

29 Na mimi, Moroni, baada ya kusikia maneno haya, nilifarijika, na kusema: Ee Bwana, haki yako itafanyika, kwani najua kwamba unafanya miujiza kwa watoto wa watu kufuatana na imani yao;

30 Kwani kaka wa Yaredi alisema kwa mlima Zerini, [a]Nenda—na ulisonga. Na ikiwa hangekuwa na imani haungesonga; kwa hivyo unafanya miujiza baada ya watu kuwa na imani.

31 Kwa njia hii ulijionyesha kwa wanafunzi wako; kwani baada ya wao kuwa na [a]imani, na kuzungumza katika jina lako, ulijidhihirisha kwao kwa uwezo mkuu.

32 Na ninakumbuka kwamba umesema kwamba umetayarisha [a]nyumba kwa watu, ndiyo, hata miongoni mwa nyumba za Baba yako, ambamo kwake binadamu angekuwa na [b]tumaini kamili; kwa hivyo lazima binadamu atumaini, au hatapokea urithi mahali ambapo umetayarisha.

33 Na tena, ninakumbuka kwamba umesema kwamba [a]unawapenda watu wote duniani, hata kwenye kuweka maisha yako chini kwa ajili ya walimwengu, ili ungeyachukua tena kutayarisha mahali kwa watoto wa watu.

34 Na sasa najua kwamba huu [a]upendo ambao umekuwa nao kwa watoto wa watu ni hisani; kwa hivyo, isipokuwa watu wawe na hisani hawawezi kurithi pale mahali ambapo umetayarisha nyumbani kwa Baba yako.

35 Kwa hivyo, ninajua kwa

25*a* 1 Kor. 2:14.
26*a* Gal. 6:7.
27*a* Yak. (KM) 4:7.
b Ku. 4:11; 1 Kor. 1:27.
c MWM Neema.
d Lk. 18:10–14; M&M 1:28. MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu.
e Lk. 9:46–48; 2 Kor. 12:9.
28*a* 1 Kor. 13; Moro. 7:39–47.
30*a* Mt. 17:20; Yak. (KM) 4:6; Hel. 10:6, 9. MWM Uwezo.
31*a* MWM Amini, Imani.
32*a* Yn. 14:2; Eno. 1:27; M&M 72:4; 98:18.
b MWM Tumaini.
33*a* Yn. 3:16–17.
34*a* Moro. 7:47. MWM Hisani; Upendo.

kitu hiki ambacho umesema, kwamba ikiwa Wayunani hawana hisani, kwa sababu ya unyonge wetu, kwamba utawahukumu, na kuchukua kutoka kwao [a]talanta zao, ndiyo, hata ile ambayo wamepokea, na uwapatie wale ambao watakuwa na nyingi zaidi.

36 Na ikawa kwamba niliomba kwa Bwana kwamba awape [a]neema Wayunani, ili wapate kuwa na hisani.

37 Na ikawa kwamba Bwana akasema nami: Kama hawana hisani haikuhusu wewe, umekuwa mwaminifu; kwa hivyo, nguo zako zitafanywa [a]safi. Na kwa sababu umeuona [b]udhaifu wako utafanywa kuwa mwenye nguvu, hata kwa kukaa mahali ambapo nimepatayarisha katika nyumba ya Baba yangu.

38 Na sasa mimi, Moroni, ninaaga kwa Wayunani, ndiyo, na pia kwa ndugu zangu ambao ninawapenda, mpaka tutakapokutana mbele ya [a]kiti cha hukumu cha Kristo, ambapo watu wote watajua kwamba [b]mavazi yangu hayajawekwa mawaa na damu yenu.

39 Na ndipo mtakapojua kwamba [a]nimemwona Yesu, na kwamba amenizungumzia [b]uso kwa uso, na kwamba aliniambia katika unyenyekevu ulio wazi, hata vile mtu humwambia mwenzake kwa lugha yangu, kuhusu vitu hivi;

40 Na ni vichache tu ambavyo nimeandika, kwa sababu ya udhaifu wangu kwa kuandika.

41 Na sasa, nimekupendekeza [a]kumtafuta huyu Yesu ambaye manabii na mitume wameandika kumhusu, kwamba neema ya Mungu Baba, na pia Bwana Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu, ambaye [b]anashuhudia kwao, iwe na kuishi ndani yenu milele. Amina.

MLANGO WA 13

Etheri anazungumzia Yerusalemu Mpya kujengwa katika Marekani na uzao wa Yusufu—Anatoa unabii, anatupwa nje, anaandika historia ya Wayaredi, na anatabiri kuangamizwa kwa Wayaredi—Vita vinaendelea kote nchini.

Na sasa mimi, Moroni, naendelea kumaliza maandishi yangu kuhusu uharibifu wa watu ambao nimekuwa nikiandika juu yao.

2 Kwani tazama, walikataa maneno yote ya Etheri; kwani aliwaambia kwa kweli vitu vyote, kutokea mwanzoni mwa binadamu; na kwamba wakati maji yalipokuwa [a]yamepungua kutoka juu ya uso wa nchi ilikuwa nchi iliyochaguliwa kuliko zingine zote, nchi iliyochaguliwa na Bwana; kwa hivyo Bwana

35 *a* Mt. 25:14–30. MWM Karama; Talanta.
36 *a* MWM Neema.
37 *a* M&M 38:42; 88:74–75; 135:4–5.
b Eth. 12:27.
38 *a* MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
b Yak. (KM) 1:19.
39 *a* MWM Yesu Kristo—Kuonekana kwa Kristo baada ya kifo.
b Mwa. 32:30; Ku. 33:11.
41 *a* M&M 88:63; 101:38.
b 3 Ne. 11:32.
13 2 *a* Mwa. 7:11–24; 8:3.

alitaka kwamba watu wote [b]wangemtumikia, wale ambao wanaishi juu yake;

3 Na kwamba ilikuwa mahali pa [a]Yerusalemu Mpya, ambayo [b]ingekuja chini kutoka mbinguni, na utakatifu wa wakfu wa Bwana.

4 Tazama, Etheri aliona siku za Kristo, na alizungumza kuhusu [a]Yerusalemu Mpya juu ya nchi hii.

5 Na alizungumza pia kuhusu nyumba ya Israeli, na [a]Yerusalemu ambako [b]Lehi angetokea—baada ya kuharibiwa kwake itajengwa tena, [c]mji mtakatifu wa Bwana; kwa hivyo, haingekuwa Yerusalemu mpya kwani ilikuwa wakati wa kale; lakini ingejengwa tena, na uwe mji mtakatifu wa Bwana; na ingejengwa kwa ajili ya nyumba ya Israeli—

6 Na kwamba [a]Yerusalemu Mpya ingejengwa juu ya nchi hii, kwa ajili ya baki la uzao wa [b]Yusufu, kwa vitu ambavyo kumekuwa na [c]mfano.

7 Kwani vile Yusufu alimleta baba yake chini katika nchi ya [a]Misri, hata hivyo alikufa huko; kwa hivyo, Bwana alileta baki la uzao wa Yusufu kutoka nchi ya Yerusalemu, kwamba angekuwa na huruma kwa uzao wa Yusufu kwamba [b]wasiangamie, hata vile alikuwa na huruma kwa baba ya Yusufu ili asiangamie.

8 Kwa hivyo, baki la nyumba ya Yusufu litajengwa juu ya [a]nchi hii; na itakuwa nchi ya urithi wao; na watajenga mji mtakatifu kwa Bwana, kama Yerusalemu ya kale; na [b]hawatachanganywa tena, mpaka mwisho utakapofika wakati dunia itakapoisha.

9 Na kutakuwa na mbingu [a]mpya na dunia mpya; na zitakuwa kama za kale ijapokuwa ya kale imepita mbali, na vitu vyote vimekuwa vipya.

10 Na ndipo kutatokea Yerusalemu Mpya; na heri wanaoishi ndani yake, kwani ni hao ambao mavazi yao ni [a]safi kupitia kwa damu ya Mwanakondoo; na ni hao hao ambao wamehesabiwa miongoni mwa baki la uzao wa Yusufu, ambao walikuwa wa nyumba ya Israeli.

11 Na hapo pia kutatokea Yerusalemu ya kale; na wakazi wake, wamebarikiwa, kwani wameoshwa kwenye damu ya Mwanakondoo; ni hawa ambao walitawanywa na [a]kukusanywa kutoka pande nne za dunia, na kutoka katika nchi za [b]kaskazini, na ni washiriki wa lile agano

2 *b* Eth. 2:8.
3 *a* 3 Ne. 20:22; 21:23–24. MWM Yerusalemu Mpya.
b Ufu. 3:12; 21:2.
4 *a* MWM Sayuni.
5 *a* MWM Yerusalemu.
b 1 Ne. 1:18–20.
c Ufu. 21:10; 3 Ne. 20:29–36.
6 *a* M&M 42:9; 45:66–67; 84:2–5; M ya I 1:10.
b MWM Yusufu, Mwana wa Yakobo.
c Alma 46:24. MWM Uashiriaji.
7 *a* Mwa. 46:2–7; 47:6.
b 2 Ne. 3:5.
8 *a* MWM Nchi ya Ahadi.
b Moro. 10:31.
9 *a* 2 Pet. 3:10–13; Ufu. 21:1; 3 Ne. 26:3; M&M 101:23–25.
10 *a* Ufu. 7:14; 1 Ne. 12:10–11; Alma 5:27.
11 *a* MWM Israeli—Kukusanyika kwa Israeli.
b M&M 133:26–35.

ambalo Mungu alifanya na baba yao, [c]Ibrahimu.

12 Na wakati vitu hivi vitakapokuja, huletwa kutimizwa andiko ambalo linasema, wako wale walio wa [a]kwanza, watakaokuwa wa mwisho; na wako wale waliokuwa wa mwisho, ambao watakuwa wa kwanza.

13 Na nilikuwa karibu kuandika zaidi, lakini nimekatazwa; lakini kuu na wa ajabu ulikuwa unabii wa Etheri; lakini walimdhania kuwa bure, na wakamtupa nje; na alijificha kwenye pango la mwamba wakati wa mchana, na wakati wa usiku alienda akiangalia vitu ambavyo vitawajia watu.

14 Na vile alivyoishi kwenye pango la mwamba aliandika maandishi haya yaliyosalia, akitazama uharibifu ambao uliwajia watu, wakati wa usiku.

15 Na ikawa kwamba katika mwaka huo huo ambamo alitupwa nje kutoka miongoni mwa watu vita vikubwa vilianza miongoni mwa watu, kwani kulikuwa na wengi walioasi, ambao walikuwa watu wenye nguvu, na walitafuta kumwangamiza Koriantumuri kwa mipango yao ya siri na maovu, ambayo yamezungumziwa.

16 Na sasa Koriantumuri, akiwa amesoma, mwenyewe, katika ustadi wote wa vita na ujanja wote wa ulimwengu, kwa hivyo alifanya vita na wale waliotaka kumwangamiza.

17 Lakini hakutubu, wala wanawe wenye sura nzuri na mabinti zake; wala wana na mabinti za Kohori waliokuwa na sura nzuri; wala wana na mabinti za Korihori ambao walikuwa na sura nzuri; na kwa kifupi, hakukuwa na wana na mabinti waliokuwa na sura nzuri juu ya uso wa dunia nzima ambao walitubu dhambi zao.

18 Kwa hivyo, ikawa kwamba katika mwaka wa kwanza ambamo Etheri aliishi kwenye pango la mwamba, kulikuwa na watu wengi waliouawa kwa upanga wa wale wa [a]kundi ovu la siri, likipigana dhidi ya Koriantumuri ili wangepata ufalme.

19 Na ikawa kwamba wana wa Koriantumuri walipigana sana na walitokwa na damu sana.

20 Na katika mwaka wa pili neno la Bwana lilimjia Etheri, kwamba aende na amtabirie [a]Koriantumuri kwamba, ikiwa angetubu, na nyumba yake yote, Bwana angempatia ufalme wake na kuwaachilia watu—

21 La sivyo wangeangamizwa, na nyumba yake yote isipokuwa yeye. Na angeishi tu kushuhudia utimizaji wa unabii ambao umezungumziwa kuhusu watu [a]wengine kupokea nchi kwa urithi wao; na Koriantumuri angezikwa na hao; na kila mtu angeangamizwa isipokuwa [b]Koriantumuri.

22 Na ikawa kwamba Koriantumuri hakutubu, wala

11 *c* MWM Agano la Ibrahimu.
12 *a* Mk. 10:31; 1 Ne. 13:42; Yak. (KM) 5:63; M&M 90:9.
18 *a* Eth. 8:9–26.
20 *a* Eth. 12:1–2.
21 *a* Omni 1:19–21; Eth. 11:21.
b Eth. 15:29–32.

nyumba yake, wala watu; na vita havikuisha; na walitaka kumuua Etheri, lakini alitoroka kutoka kwao na kujificha tena kwenye pango la ule mwamba.

23 Na ikawa kwamba kulitokea mtu ambaye aliitwa Sharedi, na alifanya vita na Koriantumuri; na alimshinda, mpaka kwamba katika mwaka wa tatu alimweka kwenye utumwa.

24 Na wana wa Koriantumuri, katika mwaka wa nne, walimshinda Sharedi, na kumrudisha baba yao kwenye ufalme.

25 Sasa kulianza kuwa na vita juu ya uso wa nchi yote, kila mtu na kundi lake akipigania kile alichotaka.

26 Na kulikuwa na wanyang'anyi, na kwa kifupi, kila aina ya uovu juu ya uso wa nchi yote.

27 Na ikawa kwamba Koriantumuri alimkasirikia sana Sharedi, na akamwendea na jeshi lake kupigana; na walikutana kwa hasira kubwa, na walikutania kwenye bonde la Gilgali; na vita vikawa vikali sana.

28 Na ikawa kwamba Sharedi alipigana dhidi yake kwa muda wa siku tatu. Na ikawa kwamba Koriantumuri alimshinda, na kumfukuza mpaka alipofikia mahali tambarare pa Heshloni.

29 Na ikawa kwamba Sharedi alimfanyia vita tena juu ya tambarare; na tazama, alimshinda Koriantumuri, na kumrudisha nyuma tena hadi kwenye bonde la Gilgali.

30 Na Koriantumuri alifanya vita na Sharedi tena kwenye bonde la Gilgali, ambamo kwake alimshinda Sharedi na kumuua.

31 Na Sharedi alimjeruhi Koriantumuri katika paja lake, kwamba hangepigana tena kwa muda wa miaka miwili, wakati ambamo watu wote juu ya uso wa nchi walikuwa wanamwaga damu, na hakukuwa na yeyote ambaye angewazuia.

MLANGO WA 14

Ubaya wa watu unaleta laana juu ya nchi—Koriantumuri anajihusisha kwa vita dhidi ya Gileadi, halafu Libu, na kisha Shizi—Damu na mauaji yanafunika nchi.

Na sasa kulianza kuwa na [a]laana kuu juu ya nchi yote kwa sababu ya uovu wa watu, ambamo kwake, ikiwa mtu angeweka chombo chake au upanga wake juu ya rafu yake, au mahali ambapo angeiweka, tazama, kufikia kesho yake, hangeipata, kubwa hivyo ilikuwa laana juu ya nchi.

2 Kwa hivyo kila mtu alishikilia kile kilichokuwa chake, kwa mikono yake, na hangeomba wala kuazima; na kila mtu aliweka kipini cha upanga wake kwenye mkono wa kulia, katika kulinda mali yake na maisha yake, na ya mabibi zake na watoto wake.

3 Na sasa, baada ya muda wa miaka miwili, na baada ya kifo cha Sharedi, tazama, kulitokea kaka wa Sharedi na akafanya

14 1 *a* Hel. 12:18; 13:17–23; Morm. 1:17–18; 2:10–14.

vita na Koriantumuri, ambamo Koriantumuri alimshinda na kumfukuza hadi kwenye jangwa la Akishi.

4 Na ikawa kwamba kaka wa Sharedi alifanya vita dhidi yake katika jangwa la Akishi; na vita vilikuwa vikubwa sana, na maelfu wengi walianguka kwa upanga.

5 Na ikawa kwamba Koriantumuri alizingira jangwa; na kaka wa Sharedi alitoka nje ya jangwa wakati wa usiku, na kuua sehemu ya jeshi la Koriantumuri, wakati walipokuwa wamelewa.

6 Na akaja mbele hadi kwenye nchi ya Moroni, na kujiweka kwenye kiti cha enzi cha Koriantumuri.

7 Na ikawa kwamba Koriantumuri aliishi na jeshi lake katika jangwa kwa muda wa miaka miwili, wakati ambapo alipata nguvu nyingi kwa jeshi lake.

8 Sasa kaka wa Sharedi, ambaye jina lake lilikuwa Gileadi, pia alipata nguvu nyingi kwa jeshi lake, kwa sababu ya vikundi vyake vya siri.

9 Na ikawa kwamba kuhani mkuu wake alimuua wakati alipokuwa amekalia kiti chake cha enzi.

10 Na ikawa kwamba mmoja wa wale wa kundi ovu la siri alimuua katika njia ya siri, na akajipatia ufalme; na jina lake lilikuwa Libu; na Libu alikuwa mtu mnene, kuliko mtu yeyote miongoni mwa watu wote.

11 Na ikawa kwamba katika mwaka wa kwanza wa Libu, Koriantumuri alikuja kwenye nchi ya Moroni, na kufanya vita na Libu.

12 Na ikawa kwamba alipigana na Libu, ambamo kwake Libu alimpiga mkono wake kwamba alimjeruhi; walakini, jeshi la Koriantumuri lilimshambulia Libu, kwamba alikimbia hadi kwenye mipaka juu ya ukingo wa bahari.

13 Na ikawa kwamba Koriantumuri alimfuata; na Libu akafanya vita na yeye juu ya ukingo wa bahari.

14 Na ikawa kwamba Libu alishinda jeshi la Koriantumuri, kwamba walikimbia tena hadi kwenye nyika ya Akishi.

15 Na ikawa kwamba Libu alimfuata mpaka akafikia nchi wazi ya Agoshi. Na Koriantumuri alikuwa amechukua watu wote na yeye wakati alikimbia mbele ya Libu katika ile sehemu ya nchi ambapo alikimbilia.

16 Na baada ya kuja kwenye tambarare za Agoshi alifanya vita na Libu, na kumpiga mpaka akafa; walakini, kaka wa Libu alimshambulia Koriantumuri badala yake, na vita vikawa vikali sana, ambapo Koriantumuri alikimbia mbele ya jeshi la kaka wa Libu.

17 Sasa jina la kaka wa Libu lilikuwa Shizi. Na ikawa kwamba Shizi alimfukuza Koriantumuri, na kuangamiza miji mingi, na aliua wote wanawake na watoto, na alichoma miji hiyo.

18 Na kukaenea woga juu ya Shizi katika nchi nzima; ndiyo, mlio ulienda kote nchini—Ni nani anaweza kushindana na

jeshi la Shizi? Tazama, husafisha dunia mbele yake!

19 Na ikawa kwamba watu walianza kujikusanya pamoja kwa majeshi, kote kwenye uso wa nchi.

20 Na waligawanyika; na sehemu yao moja ilikimbilia jeshi la Shizi, na sehemu nyingine ikakimbilia jeshi la Koriantumuri.

21 Na vita vilikuwa vikubwa na vya kudumu, na kuonekana kwa damu kuliendelea kwa muda mrefu na mauaji, kwamba uso wa nchi ulifunikwa na [a]miili ya waliokufa.

22 Na vita vilikuwa vya upesi sana na haraka kwamba hakukuwa na aliyebaki kuzika waliokufa, lakini walienda mbele kutoka kwa umwagaji wa damu hadi kwa umwagaji wa damu mwingine, wakiacha miili ya wote wanaume, wanawake, na watoto imetawanywa juu ya uso wa nchi, kuwa mawindo ya [a]minyoo ya mwili.

23 Na uvundo kutoka hapo ulienea juu ya uso wa nchi, hata juu ya uso wote wa nchi; kwa hivyo watu walisumbuliwa mchana na usiku, kwa sababu ya uvundo wa wafu.

24 Walakini, Shizi hakuacha kumkimbiza Koriantumuri; kwani alikuwa ameapa kujilipiza kisasi juu ya Koriantumuri kwa damu ya kaka yake, ambaye alikuwa amemuua, na neno la Bwana ambalo lilimjia Etheri kwamba Koriantumuri hangeuawa kwa upanga.

25 Na hivyo tunaona kwamba Bwana aliwatembelea katika utimilifu wa ghadhabu yake, na uovu wao na machukizo yao yalitayarisha njia kwa maangamizo yao yasiyo na mwisho.

26 Na ikawa kwamba Shizi alimfuata Koriantumuri kwa upande wa mashariki, mpaka kufika kwenye mipaka kando ya ukingo wa bahari, na kule alifanya vita na Shizi kwa muda wa siku tatu.

27 Na uharibifu ulikuwa wa kutisha sana miongoni mwa majeshi ya Shizi kwamba watu walianza kuogopa, na kuanza kukimbia mbele ya majeshi ya Koriantumuri; na walikimbia hadi kwa nchi ya Korihori, na kuangamiza wakazi mbele yao, wale wote ambao hawakujiunga nao.

28 Na walipiga hema zao katika bonde la Korihori; na Koriantumuri akapiga hema zake katika bonde la Shuri. Sasa bonde la Shuri lilikuwa karibu na kilima Komnori; kwa hivyo, Koriantumuri alikusanya majeshi yake juu ya kilima Komnori, na akapiga tarumbeta kuelekea kwa majeshi ya Shizi kuwakaribisha kupigana.

29 Na ikawa kwamba walikuja mbele, lakini walikimbizwa tena; na wakaja tena safari ya pili, na wakakimbizwa tena safari ya pili. Na ikawa kwamba walikuja tena safari ya tatu, na vita vikawa vikali sana.

30 Na ikawa kwamba Shizi alimpiga Koriantumuri kwamba

21 *a* Eth. 11:6.

22 *a* Isa. 14:9–11.

alimpatia majeraha mengi ya vidonda vikubwa; na Koriantumuri, kwa sababu ya kupoteza damu yake, alizirai, na alibebwa na kupelekwa mbali kama aliyekufa.

31 Sasa mauaji ya wanaume, wanawake na watoto pande zote mbili yalikuwa makubwa sana kwamba Shizi aliamuru watu wake wasiyafuatilie majeshi ya Koriantumuri; kwa hivyo, walirudi kwenye kambi yao.

MLANGO WA 15

Mamilioni ya Wayaredi wanauawa katika vita—Shizi na Koriantumuri wanawakusanya watu wote kwenye vita vya kufa—Roho wa Bwana inakoma kushughulika nao—Taifa la Wayaredi linaangamizwa kabisa—Koriantumuri pekee anabaki.

Na ikawa baada ya Koriantumuri kupona kutokana na majeraha yake, alianza kukumbuka [a]maneno ambayo Etheri alikuwa amemzungumzia.

2 Aliona kwamba walikuwa wameuawa kwa upanga kitambo karibu milioni mbili ya watu wake, na alianza kuhuzunika moyoni mwake; ndiyo, walikuwa wameuawa milion mbili ya watu wakuu, na pia wake zao na watoto wao.

3 Alianza kutubu kwa uovu ambao alikuwa amefanya; alianza kukumbuka maneno ambayo yalizungumzwa kwa midomo ya manabii wote, na aliona kwamba yametimizwa hadi sasa, kila chembe; na nafsi yake iliomboleza na kukataa kutulizwa.

4 Na ikawa kwamba aliandika barua kwa Shizi, akimwuliza awasamehe watu, na angeacha ufalme kwa ajili ya maisha ya watu.

5 Na ikawa kwamba baada ya Shizi kupokea barua yake aliandika barua kwa Koriantumuri, kwamba kama angejisalimisha, ili amuue kwa upanga wake mwenyewe, kwamba angeacha maisha ya watu.

6 Na ikawa kwamba watu hawakutubu kutoka kwa maovu yao; na watu wa Koriantumuri walichochewa kuwa na hasira dhidi ya watu wa Shizi; na watu wa Shizi walichochewa kuwa na hasira dhidi ya watu wa Koriantumuri; kwa hivyo, watu wa Shizi walifanya vita na watu wa Koriantumuri.

7 Na wakati Koriantumuri alipoona kwamba alikuwa karibu kushindwa alikimbia tena mbele ya watu wa Shizi.

8 Na ikawa kwamba alifikia maji ya Ripliankumu, ambayo, kwa tafsiri, ni kubwa, au kushinda yote; kwa hivyo, walipofikia maji haya walipiga hema zao; na Shizi pia akapiga hema zake karibu na wao; na kwa hivyo kesho yake walipigana.

9 Na ikawa kwamba walipigana vita vikali sana, ambamo kwake Koriantumuri alijeruhiwa tena, na akazirai kwa kupoteza damu.

10 Na ikawa kwamba majeshi

15 1*a* Eth. 13:20–21.

ya Koriantumuri yalizidi kushambulia majeshi ya Shizi kwamba waliwashinda, kwamba waliwasababisha kukimbia kutoka mbele yao; na walikimbilia upande wa kusini, na kupiga hema zao mahali palipoitwa Ogathi.

11 Na ikawa kwamba jeshi la Koriantumuri lilipiga hema zao kando ya kilima Rama; na kilikuwa kile kile kilima ambapo baba yangu Mormoni [a]alificha maandishi kwa ulinzi wa Bwana, ambayo yalikuwa matakatifu.

12 Na ikawa kwamba waliwakusanya watu wote pamoja juu ya uso wa nchi, wale ambao walikuwa hawajauawa, isipokuwa Etheri.

13 Na ikawa kwamba Etheri aliona matendo yote ya watu; na aliona kwamba watu ambao walikuwa wafuasi wa Koriantumuri walikusanywa pamoja kuwa jeshi la Koriantumuri; na watu waliokuwa wafuasi wa Shizi walikusanyika pamoja kwenye jeshi la Shizi.

14 Basi, walikusanya watu pamoja kwa muda wa miaka minne, kwamba wangepata wale wote ambao walikuwa juu ya uso wa nchi, na ili wapate nguvu yote ambayo iliwezekana kupata.

15 Na ikawa kwamba baada ya wote kukusanyika pamoja, kila mtu kwenye jeshi ambalo alitaka, na wake zao na watoto wao—wote wanaume, wanawake na watoto wakijihami na silaha za vita, wakiwa na ngao, na [a]dirii, na vyapeo, na wakiwa wamevalia kwa njia ya vita—walisonga mbele mmoja dhidi ya mwingine kupigana; na walipigana ile siku yote, na hakuna aliyeshinda.

16 Na ikawa kwamba wakati ilipokuwa usiku walikuwa wamechoka, na wakarudi kwenye vituo vyao; na baada ya kurudi kwenye vituo vyao walianza kulia na kuomboleza kwa sababu ya watu wao ambao walikuwa wameuawa; na vilio vyao vilikuwa vikuu sana, pamoja na maombolezo yao na makelele, kwamba vilipenya anga kwa wingi.

17 Na ikawa kwamba kesho yake walienda tena kupigana, na siku hiyo ilikuwa kubwa na ya kutisha; walakini, hawakushinda, na wakati usiku ulipowadia tena walipenya anga na vilio vyao, na kulia kwao, na maombolezo yao, kwa vifo vya watu wao.

18 Na ikawa kwamba Koriantumuri aliandika tena barua kwa Shizi, akitaka kwamba asije tena kwa vita, lakini akubali ufalme, na kuhurumia maisha ya watu.

19 Lakini tazama, Roho wa Bwana ilikuwa imekoma kuwaongoza, na [a]Shetani alikuwa na uwezo kamili juu ya mioyo ya watu; kwani walikuwa wamejisalimisha kwa ugumu wa mioyo yao, na upofu wa akili zao kwamba waharibiwe; kwa hivyo walienda tena vitani.

11*a* Morm. 6:6. | 15*a* Mos. 8:7–10. | 19*a* MWM Ibilisi.

20 Na ikawa kwamba walipigana ile siku yote, na usiku ulipowadia walilalia panga zao.

21 Na kesho yake walipigana mpaka hata usiku ukafika.

22 Na usiku ulipofika [a]walikuwa na hasira, kama vile mtu aleweshwavyo na divai; na walilalia tena panga zao.

23 Na kesho yake walipigana tena; na usiku ulipofika wote walikuwa wameuawa isipokuwa watu wa Koriantumuri hamsini na wawili, na watu wa Shizi sitini na tisa.

24 Na ikawa kwamba walilalia panga zao usiku huo, na kesho yake wakapigana tena, na walipigana kwa nguvu zao zote kwa panga na ngao zao, siku hiyo yote.

25 Na wakati usiku ulipofika kulikuwa na watu wa Shizi thelathini na wawili, na watu wa Koriantumuri ishirini na saba.

26 Na ikawa kwamba walikula na kulala, na kujitayarishia kifo kesho yake. Na walikuwa wanene na wenye nguvu wakilinganishwa na watu wa kawaida.

27 Na ikawa kwamba walipigana kwa muda wa masaa matatu, na walizirai kwa kupoteza damu.

28 Na ikawa kwamba baada ya watu wa Koriantumuri kupata nguvu ya kutosha tena kwamba wangeweza kutembea, walikuwa karibu kukimbia kwa maisha yao; lakini tazama, Shizi aliamka, na pia watu wake, na akaapa kwa ghadhabu yake kwamba angemuua Koriantumuri au sivyo angeuawa kwa upanga.

29 Kwa hivyo, aliwafuata, na kesho yake akawapata; na wakapigana tena kwa upanga. Na ikawa kwamba [a]wote walipokuwa wamekufa, isipokuwa Koriantumuri na Shizi, tazama Shizi alikuwa amezirai kwa kupoteza damu.

30 Na ikawa kwamba wakati Koriantumuri alikuwa amelalia upanga wake, ili apumzike kidogo, alikata kichwa cha Shizi.

31 Na ikawa kwamba baada ya kukata kichwa cha Shizi, kwamba Shizi alijiinua kwa mikono yake na kisha akaanguka; na baada ya kujitahidi kuvuta pumzi, akafa.

32 Na ikawa kwamba [a]Koriantumuri alianguka ardhini, na kuwa kama hana uhai.

33 Na Bwana akamzungumzia Etheri, na kumwambia: Nenda mbele. Na akaenda mbele, na aliona kwamba maneno ya Bwana yalikuwa yote yametimizwa; na akamaliza [a]maandishi yake; (na ile sehemu moja kwa mia sijaandika) na akayaficha kwa njia ambayo watu wa Limhi waliyapata.

34 Sasa maneno ya mwisho ambayo yameandikwa na [a]Etheri ni haya: Kama Bwana anataka kunichukua nikiwa hai, au kama nitavumilia mapenzi ya Bwana kimwili, haijalishi, ikiwa nitaokolewa katika ufalme wa Mungu. Amina.

22*a* Moro. 9:23.
29*a* Eth. 13:20–21.
32*a* Omni 1:20–22.
33*a* Mos. 8:9; Alma 37:21–31; Eth. 1:1–5.
34*a* Eth. 12:2.

KITABU CHA MORONI

MLANGO WA 1

Moroni anaandika kwa manufaa ya Walamani—Wanefi ambao hawatamkana Kristo wanauawa. Karibia mwaka 401–421 B.K.

SASA mimi, [a]Moroni, baada ya kumaliza kufupisha historia ya watu wa Yaredi, sikudhania kama ningeandika zaidi, lakini bado sijafa; na sitaki kujionyesha kwa Walamani wasije wakaniangamiza.

2 Kwani tazama, [a]vita vyao ni vikali sana miongoni mwao wenyewe; na kwa sababu ya chuki yao [b]wanaua kila Mnefi ambaye hatamkana Kristo.

3 Na mimi, Moroni, [a]sitamkana Kristo; kwa hivyo, ninarandaranda popote niwezapo kwa usalama wa maisha yangu.

4 Kwa hivyo, ninaandika vitu vingine vichache, kinyume cha kile nilichotarajia; kwani nilidhani kuwa sitaandika zaidi ya hayo; lakini ninaandika vitu vichache zaidi, kwamba vingekuwa vya manufaa kwa ndugu zangu, Walamani, katika siku zijazo, kulingana na mapenzi ya Bwana.

MLANGO WA 2

Yesu aliwapa wale wanafunzi kumi na wawili Wanefi uwezo wa kutoa kipawa cha Roho Mtakatifu. Karibia mwaka 401–421 B.K.

MANENO ya Kristo, aliyowazungumzia [a]wanafunzi wake, kumi na wawili ambao alikuwa amewateua, wakati alipowawekea mikono yake juu yao—

2 Na aliwaita kwa majina, akisema: Mtamwita Baba katika jina langu, katika sala ya nguvu; na baada ya kufanya hivi mtakuwa na [a]uwezo kwamba kwa yule ambaye mtamwekea [b]mikono yenu, [c]mtampa Roho Mtakatifu; na katika jina langu mtamtoa, kwani hivyo ndivyo mitume wangu hufanya.

3 Sasa Kristo alisema maneno haya kwao wakati wa kwanza wa kuonekana kwake; na umati haukusikia, lakini wanafunzi walisikia; na kwa wengi ambao [a]waliwawekea mikono yao, Roho Mtakatifu aliwashukia.

MLANGO WA 3

Wazee wanawatawaza makuhani na walimu kwa kuwawekea mikono. Karibia mwaka 401–421 B.K.

NJIA ambayo wanafunzi, ambao waliitwa [a]wazee wa kanisa, [b]waliwatawaza makuhani na walimu—

2 Baada ya wao kuomba kwa Baba katika jina la Kristo,

1 1*a* MWM Moroni, Mwana wa Mormoni.
2*a* 1 Ne. 12:20–23.
b Alma 45:14.
3*a* Mt. 10:32–33; 3 Ne. 29:5.
2 1*a* 3 Ne. 13:25.
2*a* MWM Uwezo.
b MWM Mikono, Kuweka juu ya.
c 3 Ne. 18:37.
3*a* Mdo. 19:6.
3 1*a* Alma 6:1. MWM Mzee.
b MWM Kutawaza, Kutawazwa.

waliwawekea mikono, na kusema:

3 Katika jina la Yesu Kristo ninakutawaza uwe kuhani (au kama atakuwa mwalimu, ninakutawaza uwe mwalimu) kuhubiri toba na [a]msamaha wa dhambi kupitia kwa Yesu Kristo, kwa kuvumilia kwa imani kwa jina lake hadi mwisho. Amina.

4 Na katika njia hii [a]waliwatawaza makuhani na walimu, kulingana na [b]karama na wito wa Mungu kwa watu; na waliwatawaza kwa [c]uwezo wa Roho Mtakatifu, ambaye alikuwa ndani yao.

MLANGO WA 4

Namna wazee na makuhani wanavyohudumia sakramenti ya mkate inaelezwa. Karibia mwaka 401–421 B.K.

[a]Njia ya [b]wazee wao na makuhani wakibariki mwili na damu ya Kristo kwa washiriki; na [c]waliubariki kulingana na amri za Kristo; kwa hivyo tunajua njia ni ya kweli; na mzee au kuhani aliibariki—

2 Na walipiga magoti chini na washiriki, na kuomba kwa Baba katika jina la Kristo, wakisema:

3 Ee Mungu, Baba wa Milele, tunakuomba katika jina la Mwanao, Yesu Kristo, ubariki na utakase [a]mkate huu kwa roho za wale wote watakaoula, ili waweze kuula kwa [b]ukumbusho wa mwili wa Mwanao, na wakushuhudie, Ee Mungu, Baba wa Milele, kwamba wako radhi kujichukulia juu yao [c]jina la Mwanao, na daima kumkumbuka, na kushika amri zake ambazo amewapa, ili daima [d]Roho wake apate kuwa pamoja nao. Amina.

MLANGO WA 5

Njia ya kutoa divai ya sakramenti inaelezwa. Karibia mwaka 401–421 B.K.

[a]Njia ya kubariki divai—Tazama, walichukua kikombe, na kusema:

2 Ee Mungu, Baba wa Milele, tunakuomba katika jina la Mwanao, Yesu Kristo, ubariki na utakase [a]divai hii kwa roho za wale wote watakaoinywa, ili waweze kufanya hivi kwa [b]ukumbusho wa damu ya Mwanao, ambayo ilimwagwa kwa ajili yao; kwamba washuhudie kwako, Ee Mungu, Baba wa Milele, kwamba daima wamkumbuke, ili Roho wake apate kuwa pamoja nao. Amina.

MLANGO WA 6

Watu waliotubu wanabatizwa

3a MWM Ondoleo la Dhambi.
4a M&M 18:32; 20:60.
b MWM Karama.
c 1 Ne. 13:37; Moro. 6:9.
4 1a 3 Ne. 18:1–7.
b MWM Mzee.
c M&M 20:76–77.
3a MWM Sakramenti.
b Lk. 22:19; 1 Kor. 11:23–24; 3 Ne. 18:7.
c MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
d MWM Roho Mtakatifu.
5 1a 3 Ne. 18:8–11; M&M 20:78–79.
2a M&M 27:2–4. MWM Sakramenti.
b Lk. 22:19–20; 1 Kor. 11:25.

na kushirikishwa—Washiriki wa Kanisa wanaotubu wanasamehewa—Mikutano inaendeshwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu. Karibia mwaka 401–421 B.K.

NA sasa ninazungumza kuhusu [a]ubatizo. Tazama, wazee, makuhani, na walimu walibatizwa; na hawangebatizwa kama hawangezaa matunda [b]yapasayo toba.

2 Wala hawakumpokea yeyote kwenye ubatizo kama hangekuja na moyo [a]uliopondeka na roho iliyovunjika, na kushuhudia kwa kanisa kwamba wametubu kwa kweli kutoka kwenye dhambi zao.

3 Na hakuna waliopokelewa kwenye ubatizo isipokuwa [a]wajivike juu yao jina la Kristo na kukata kauli kumtumikia hadi mwisho.

4 Na baada ya hao kupokewa kwenye ubatizo, na kupokelewa na [a]kusafishwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, walihesabiwa miongoni mwa watu wa kanisa la Kristo; na [b]majina yao yalichukuliwa ili wakumbukwe na kulishwa na neno nzuri la Mungu, kuwaweka kwenye njia nzuri, kuwaweka [c]waangalifu siku zote kwenye sala, [d]wakitegemea tu katika nguvu ya wokovu wa Kristo, ambaye alikuwa [e]mwanzilishi na mtimizaji wa imani yao.

5 Na washiriki wa [a]kanisa walikutana pamoja [b]mara kwa mara, [c]kufunga na kuomba, na kuzungumza mmoja na mwingine kuhusu ustawi wa nafsi zao.

6 Na walikutana pamoja mara kwa mara kushiriki kwa mkate na divai, katika kumkumbuka Bwana Yesu.

7 Na walikuwa waangalifu kwamba [a]kusiwe na uovu miongoni mwao; na yeyote aliyepatikana akitenda uovu, na mashahidi [b]watatu wa kanisa waliwahukumu mbele ya [c]wazee, na kama hawakutubu, na [d]hawakukiri, majina yao [e]yalitolewa nje, na hawakuhesabiwa miongoni mwa watu wa Kristo.

8 Lakini kila [a]mara walipotubu na kutafuta msamaha, na kusudi halisi, [b]walisamehewa.

9 Na mikutano yao [a]iliendeshwa na kanisa kulingana na njia ambayo Roho aliwaongoza, na kwa uwezo wa [b]Roho Mtakatifu; kwani vile uwezo

6 1*a* MWM Batiza, Ubatizo.
b MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki.
2*a* MWM Moyo Uliovunjika.
3*a* MWM Yesu Kristo—Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu.
4*a* MWM Safi na Isiyo safi.
b M&M 20:82.
c Alma 34:39; 3 Ne. 18:15–18.
d 2 Ne. 31:19; M&M 3:20.
e Ebr. 12:2.
5*a* MWM Kanisa la Yesu Kristo.
b 3 Ne. 18:22; 4 Ne. 1:12; M&M 88:76.
c MWM Funga, Kufunga.
7*a* M&M 20:54.
b M&M 42:80–81. MWM Shahidi, Ushahidi.
c Alma 6:1. MWM Mzee.
d MWM Kiri, Kukiri.
e Ku. 32:33; M&M 20:83. MWM Kutengwa na Kanisa.
8*a* Mos. 26:30–31.
b MWM Samehe.
9*a* M&M 20:45; 46:2.
b MWM Roho Mtakatifu.

wa Roho Mtakatifu ulivyowaongoza kuhubiri, au kuhimiza, au kuomba, hata hivyo ndivyo ilivyofanywa.

MLANGO WA 7

Karibisho linapewa kuingia kwenye makao ya Bwana—Ombeni na nia ya kweli—Roho wa Kristo huwezesha watu kujua mema na maovu—Shetani anawashawishi watu wamkane Kristo na wafanye uovu—Manabii wanadhihirisha kuja kwa Kristo—Kwa imani, miujiza hufanyika na malaika wanahudumu—Watu wanapaswa kutumaini uzima wa milele na kuambatana kwenye hisani. Karibia mwaka 401–421 B.K.

Na sasa mimi, Moroni, naandika machache ya maneno ya baba yangu Mormoni, ambayo alisema kuhusu [a]imani, tumaini, na hisani; kwani hii ndiyo njia aliyozungumza kwa watu, wakati alipowafundisha katika sinagogi ambayo walikuwa wamejenga kama mahali pa kuabudu.

2 Na sasa mimi, Mormoni, nazumgumza kwenu ndugu zangu wapendwa; na ni kwa neema ya Mungu Baba, na Bwana wetu Yesu Kristo, na mapenzi yake matakatifu, kwa sababu ya karama yake [a]kuniita, kwamba nimekubaliwa kuzungumza kwenu wakati huu.

3 Kwa hivyo, ningewazungumzia wale ambao ni wa kanisa, ambao ni wafuasi wa imani ya Kristo, ambao wamepata tumaini la kutosha ambalo kwalo mnaweza kuingia kwenye [a]makao ya Bwana, kutoka wakati huu kwenda mbele mpaka mtakapopumzika na yeye mbinguni.

4 Na sasa ndugu zangu, nahukumu vitu hivi kwenu kwa sababu ya [a]matembezi yenu matulivu na watoto wa watu.

5 Kwani nakumbuka neno la Mungu ambalo linasema kwa matunda yao [a]mtawatambua; kwani kama matunda yao ni mema, basi ni wema pia.

6 Kwani tazama, Mungu amesema mtu akiwa [a]mwovu hawezi kufanya yale ambayo ni mema; kwani ikiwa atatoa karama, au [b]kuomba kwa Mungu, isipokuwa aifanye kwa kusudi jema haimfaidii chochote.

7 Kwani tazama, haihesabiwi kwake kwa haki.

8 Kwani tazama, ikiwa mtu [a]mwovu anatoa zawadi, huifanya [b]bila kupenda; kwa hivyo inahesabiwa kwake sawa kama angeiweka ile zawadi; kwa hivyo anadhaniwa mwovu mbele ya Mungu.

9 Na kadhalika huhesibiwa pia uovu kwa mtu, ikiwa ataomba bila [a]nia kamili ya moyo; ndiyo, na haimfaidii chochote, kwani Mungu hampokei yeyote wa aina hii.

7 1*a* 1 Kor. 13; Eth. 12:3–22, 27–37; Moro. 8:14; 10:20–23.
2*a* MWM Ita, Itwa na Mungu, Wito.
3*a* MWM Pumzika.
4*a* 1 Yoh. 2:6; M&M 19:23.
5*a* 3 Ne. 14:15–20.
6*a* Mt. 7:15–18.
b Alma 34:28. MWM Sala.
8*a* Mit. 15:8.
b M&M 64:34.
9*a* Yak. (Bib.) 1:6–7; 5:16; Moro. 10:4.

10 Kwa hivyo, mtu akiwa mwovu hawezi kufanya kile ambacho ni chema; wala hawezi kutoa karama nzuri.

11 Kwani tazama, [a]chimbuko chungu haliwezi kutoa maji mazuri; wala chimbuko zuri haliwezi kutoa maji chungu; kwa hivyo, mtu akiwa mtumishi wa ibilisi hawezi akamfuata Kristo; na akiwa [b]anamfuata Kristo hapo hawezi akawa mtumishi wa ibilisi.

12 Kwa hivyo, vitu vyote vilivyo [a]vizuri vinatoka kwa Mungu; na kile kilicho [b]kiovu hutoka kwa ibilisi; kwani ibilisi ni adui wa Mungu, na hupigana dhidi yake siku zote, na hukaribisha na hushawishi kufanya [c]dhambi, na kufanya kile kilicho kiovu siku zote.

13 Lakini tazama, kile kilicho cha Mungu hukaribisha na hushawishi kufanya mema siku zote; kwa hivyo, kila kitu kinachokaribisha na [a]kushawishi kufanya mema, na kumpenda Mungu, na kumtumikia, [b]kinaongozwa na Mungu.

14 Kwa hivyo, muwe waangalifu, ndugu zangu wapendwa, kwamba msione kile ambacho ni [a]kiovu kuwa cha Mungu, au kile ambacho ni kizuri na cha Mungu kuwa cha ibilisi.

15 Kwani tazama, ndugu zangu, mmepewa uhuru [a]kuhukumu, kwamba mjue mema na maovu; na njia ya kuhukumu ni wazi, kwamba mjue na ufahamu kamili, kama mwangaza wa mchana kutoka kwa giza la usiku.

16 Kwani tazama, [a]Roho ya Kristo imetolewa kwa kila mtu, ili [b]ajue mema na maovu; kwa hivyo, ninawaonyesha njia ya kuhukumu; kwani kila kitu kinachokaribisha kufanya mema, na kushawishi kuamini katika Kristo, kinasababishwa na uwezo na thawabu ya Kristo; kwa hivyo mngejua na ufahamu kamili kwamba ni cha Mungu.

17 Lakini kitu chochote ambacho hushawishi watu kufanya [a]maovu, na kutoamini katika Kristo, na kumkana, na kutomtumikia Mungu, hapo mtajua na ufahamu kamili kwamba ni cha ibilisi; kwani kwa njia hii ndiyo ibilisi hufanya kazi, kwani hamshawishi mtu yeyote kufanya mema, la, sio mmoja; wala malaika wake; wala wale ambao hujiweka chini yake.

18 Na sasa, ndugu zangu, nikiona kwamba mnajua nuru ambayo kwake mnaweza kuhukumu, nuru ambayo ni [a]nuru ya Kristo, mhakikishe kwamba

11 *a* Yak. (Bib.) 3:11–12.
b Mt. 6:24; 2 Ne. 31:10–13; M&M 56:2.
12 *a* Yak. (Bib.) 1:17; 1 Yoh. 4:1–2; Eth. 4:12.
b Alma 5:39–42.
c Hel. 6:30.
MWM Dhambi.
13 *a* 2 Ne. 33:4; Eth. 8:26.
b MWM Maongozi ya Mungu, Shawishi.
14 *a* Isa. 5:20; 2 Ne. 15:20.
15 *a* MWM Utambuzi, Kipawa cha.
16 *a* MWM Dhamiri; Nuru, Nuru ya Kristo.
b Mwa. 3:5; 2 Ne. 2:5, 18, 26; Mos. 16:3; Alma 29:5; Hel. 14:31.
17 *a* MWM Dhambi.
18 *a* Mos. 16:9; M&M 50:24; 88:7–13.
MWM Nuru, Nuru ya Kristo.

hamhukumu kwa makosa; kwani [b]hukumu ile mnayohukumu nayo ndiyo mtakayohukumiwa.

19 Kwa hivyo, ninawasihi ninyi, ndugu, kwamba mtafute kwa bidii katika [a]nuru ya Kristo kwamba mngejua mema na maovu; na ikiwa utashikilia kila kitu kizuri, na usilaumu, hapo utakuwa bila shaka [b]mtoto wa Kristo.

20 Na sasa, ndugu zangu, inawezekanaje kwamba mshikilie kila kitu kizuri?

21 Na sasa naja kwa ile imani, ambayo nilisema nitaizungumzia; na nitawaambia njia ambayo kwake mnaweza kushikilia kwa kila kitu kizuri.

22 Kwani tazama, Mungu [a]akijua vitu vyote, akiwa amekuwepo kutoka milele hadi milele, tazama, alimtuma [b]malaika kuhudumu kwa watoto wa watu, kuwajulisha kuhusu kuja kwa Kristo; na katika Kristo kutatokea kila kitu kizuri.

23 Na Mungu pia aliwatangazia manabii, kwa mdomo wake mwenyewe, kwamba Kristo sharti aje.

24 Na tazama, kulikuwa na njia tofauti ambazo kwake alijulisha vitu kwa watoto wa watu, ambavyo vilikuwa vyema; na vitu vyote ambavyo ni vyema hutoka kwa Kristo; la sivyo watu wangebaki kwenye hali ya [a]kuanguka, na hakuna kitu chochote kizuri ambacho kingewajia.

25 Na kwa hivyo, kwa huduma ya [a]malaika, na kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu, watu walianza kutenda imani katika Kristo; na hivyo kwa imani, walishikilia kila kitu kizuri; na hivi ndivyo ilivyokuwa mpaka kuja kwa Kristo.

26 Na baada ya yeye kuja watu pia waliokolewa kwa imani katika jina lake; na kwa kupitia kwa imani, wakawa wana wa Mungu. Na kwa kweli kadiri Kristo aishivyo alisema maneno haya kwa babu zetu, akisema: Kitu [a]chochote mtakachomwuliza Baba katika jina langu, ambacho ni kizuri, kwa imani mkiamini kwamba mtapata, tazama, mtakipokea.

27 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, je, [a]miujiza imekoma kwa sababu Kristo amepanda mbinguni, na ameketi mkono wa kulia wa Mungu, [b]kudai kutoka kwa Baba haki zake za huruma ambazo anazo juu ya watoto wa watu?

28 Kwani amejibu mwisho wa sheria, na hudai wale wote ambao wana imani ndani yake; na wale ambao wana imani ndani yake [a]watajishikilia kwa kila kitu kizuri; kwa hivyo

18 *b* TJS Mt. 7:1–2 (Kiambatisho); Lk. 6:37; Yn. 7:24.
19 *a* M&M 84:45–46.
b Mos. 15:10–12; 27:25. MWM Wana na Mabinti za Mungu.
22 *a* MWM Mungu, Uungu.
b Musa 5:58. MWM Malaika.
24 *a* 2 Ne. 2:5.
25 *a* Alma 12:28–30.
26 *a* 3 Ne. 18:20. MWM Sala.
27 *a* MWM Muujiza.
b Isa. 53:12; Mos. 14:12.
28 *a* Rum. 12:9; M&M 98:11.

[b]huzungumza akipendelea watoto wa watu; na huishi mbinguni milele.

29 Na kwa sababu amefanya hivi, ndugu zangu wapendwa, je, miujiza imekoma? Tazama ninawaambia, La; wala malaika hawajakoma kuwahudumia watoto wa watu.

30 Kwani tazama, wako chini yake, kuhudumu kulingana na neno la amri yake, wakijidhihirisha kwa wale walio na imani ya nguvu na akili imara katika kila kitu cha uchamungu.

31 Na kazi ya huduma yao ni kuita watu katika toba, na kutimiza na kufanya kazi ya agano la Baba, ambalo amefanya kwa watoto wa watu, kutayarisha njia miongoni mwa watoto wa watu, kwa kutangaza neno la Kristo kwa vyombo viteule vya Bwana, kwamba wangekuwa na ushahidi kumhusu.

32 Na kwa kufanya hivyo, Bwana Mungu hutayarisha njia kwamba watu wengine wangekuwa na [a]imani katika Kristo, kwamba Roho Mtakatifu angekuwa na mahali katika mioyo yao, kulingana na uwezo alio nao; na kwa njia hii ndiyo Baba hutimiza, maagano ambayo amefanya kwa watoto wa watu.

33 Na Kristo amesema: [a]Ikiwa mtakuwa na imani ndani yangu mtakuwa na uwezo wa kufanya kitu chochote ambacho ni cha [b]kufaa kwangu.

34 Na amesema: [a]Tubuni enyi miisho ya dunia, na mje kwangu, na mbatizwe katika jina langu, na muwe na imani ndani yangu, ili muokolewe.

35 Na sasa, ndugu zangu wapendwa, ikiwa hivi ndivyo itakuwa kwamba vitu hivi ni kweli ambavyo nimewazungumzia, na Mungu atawaonyesha, kwa [a]uwezo na fahari kuu katika [b]siku ya mwisho, kwamba ni kweli, na ikiwa ni kweli, je, wakati wa miujiza umekoma?

36 Au malaika wamekoma kuonekana kwa watoto wa watu? Au [a]amesimamisha uwezo wa Roho Mtakatifu kutoka kwao? Au atasimamisha, kadiri muda utakapokuwepo au dunia itakapokuwepo, au kutakuwa na mtu mmoja juu ya uso wake kuokolewa?

37 Tazama ninawaambia, La; kwani ni kwa imani kwamba [a]miujiza hufanyika; na ni kwa imani kwamba malaika huonekana na kuhudumia watu; kwa hivyo, kama vitu hivi vimekoma msiba uwe kwa watoto wa watu, kwani ni kwa sababu ya [b]kutoamini, na yote ni bure.

38 Kwani hakuna atakayeokoka, kulingana na maneno ya Kristo, isipokuwa awe na imani katika jina lake; kwani,

28 *b* 1 Yoh. 2:1; 2 Ne. 2:9. MWM Mtetezi.
32 *a* MWM Amini, Imani.
33 *a* Mt. 17:20.
b M&M 88:64–65.
34 *a* 3 Ne. 27:20; Eth. 4:18.
35 *a* 2 Ne. 33:11.
b M&M 35:8.
36 *a* Moro. 10:4–5, 7, 19.
37 *a* Mt. 13:58; Morm. 9:20; Eth. 12:12–18.
b Moro. 10:19–24.

ikiwa hivi vitu vimekoma, basi imani imekoma pia; na kutisha ni hali ya mtu, kwani ni kama hakujakuwepo na ukombozi uliofanywa.

39 Lakini tazama, ndugu zangu wapendwa, ninaweza kuona vitu vyema zaidi kwenu, kwani ninaona kwamba mna imani katika Kristo kwa sababu ya uvumilivu wenu; kwani kama hamna imani ndani yake [a]hamfai kuhesabiwa miongoni mwa watu wa kanisa lake.

40 Na tena, ndugu zangu wapendwa, ninataka kuwazungumzia kuhusu [a]tumaini. Inawezekanaje kwamba mtafikia imani, isipokuwa muwe na tumaini?

41 Na ni kitu gani [a]mtakachotumainia? Tazama nawaambia kwamba mtakuwa na [b]tumaini kupitia upatanisho wa Kristo na uwezo wa kufufuka kwake, kuinuliwa kwa [c]maisha ya milele, na hii kwa sababu ya imani yenu kwake kulingana na ile ahadi.

42 Kwa hivyo, ikiwa mtu ana [a]imani [b]lazima ahitaji kuwa na tumaini; kwani bila imani hakuwezi kuwepo na tumaini lolote.

43 Na tena, tazama ninawaambia kwamba hawezi kuwa na imani na tumaini, isipokuwa awe [a]mnyenyekevu, na mpole katika moyo.

44 Ikiwa hivyo, [a]imani na tumaini lake ni bure, kwani hakuna yeyote anayekubaliwa mbele ya Mungu, isipokuwa yule aliye myenyekevu na mpole katika moyo; na mtu akiwa myenyekevu na mpole katika moyo, na [b]kukiri kwa uwezo wa Roho Mtakatifu kwamba Yesu ni Kristo, lazima awe na ahisani; kwani kama hana hisani yeye si kitu; kwa hivyo lazima awe na hisani.

45 Na [a]hisani huvumilia, na ni karimu, na haina [b]wivu, na haijivuni, haitafuti mambo yake, haifutuki kwa upesi, haifikirii mabaya, na haifurahii uovu lakini hufurahi katika ukweli, huvumilia vitu vyote, huamini vitu vyote, hutumaini vitu vyote, hustahamili vitu vyote.

46 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, kama hamna hisani, ninyi si kitu, kwani hisani haikosi kufaulu kamwe. Kwa hivyo, ambatana na hisani, ambayo ni kubwa kuliko yote, kwani vitu vyote lazima vishindwe—

47 Lakini [a]hisani ni [b]upendo msafi wa Kristo, na inavumilia milele; na yeyote atakayepatikana nayo katika siku ya mwisho, itakuwa vyema kwake.

39 *a* MWM Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki.
40 *a* Eth. 12:4.
MWM Tumaini.
41 *a* M&M 138:14.
b Tit. 1:2; Yak. (KM) 4:4; Alma 25:16; Moro. 9:25.
c MWM Uzima wa Milele.
42 *a* MWM Amini, Imani.
b Moro. 10:20.
43 *a* MWM Pole, Upole.
44 *a* Alma 7:24; Eth. 12:28–34.
b Lk. 12:8–9.
MWM Kiri, Kukiri; Ushuhuda.
45 *a* 1 Kor. 13.
b MWM Husuda.
47 *a* 2 Ne. 26:30.
MWM Hisani.
b Yos. 22:5.
MWM Upendo.

48 Kwa hivyo, ndugu zangu wapendwa, [a]ombeni kwa Baba kwa nguvu zote za moyo, kwamba mjazwe na upendo huu, ambao ametoa kwa wote ambao ni [b]wafuasi wa kweli wa Mwana wake, Yesu Kristo; ili muwe wana wa Mungu; kwamba wakati atakapoonekana [c]tutakuwa kama yeye, kwani tutamwona vile alivyo; ili tuwe na tumaini hili; ili [d]tutakaswe hata vile alivyo mtakatifu. Amina.

MLANGO WA 8

Ubatizo wa watoto wachanga ni uovu wa machukizo—Watoto wachanga wameokolewa na Kristo kwa sababu ya Upatanisho—Imani, toba, unyenyekevu na upole wa moyo, kupokea Roho Mtakatifu, na kuvumilia hadi mwisho yanaelekeza kwa wokovu. Karibia mwaka 401–421 B.K.

Barua ya [a]baba yangu Mormoni, iliyoandikwa kwangu, Moroni; na iliandikwa kwangu mara baada nilipoitwa kwa huduma. Na kwa njia hii aliniandikia, akisema:

2 Mwana wangu mpendwa, Moroni, ninafurahi sana kwamba Bwana wako Yesu Kristo amekuwa mwangalifu kwako, na amekuita kwa huduma yake, na kwa kazi yake takatifu.

3 Ninakukumbuka wewe kila siku katika sala zangu, siku zote nikisali kwa Mungu Baba katika jina la Mtoto wake Mtakatifu, Yesu, kwamba yeye, kupitia kwa [a]uzuri wake na [b]neema usio na mwisho, atakulinda kupitia uvumilivu wa imani kwa jina lake milele.

4 Na sasa, mwana wangu, ninakuzungumzia kuhusu lile ambalo linanisikitisha sana; kwani ninasikitishwa kwamba [a]ugomvi unaweza kutokea miongoni mwenu.

5 Kwani, ikiwa nimejulishwa ukweli, kumekuwa na ugomvi miongoni mwenu kuhusu ubatizo wa watoto wenu wachanga.

6 Na sasa, mwana wangu, ninataka ufanye kazi kwa bidii, ili hili kosa kubwa litolewe miongoni mwenu; kwani, kwa kusudi hili nimeandika hii barua.

7 Kwani mara moja nilipojua vitu hivi kuwahusu nilimwuliza Bwana kuhusu jambo hili. Na [a]neno la Bwana lilinijia kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, likisema:

8 Sikiliza maneno ya Kristo, Mkombozi wako, Bwana wako na Mungu wako. Tazama, nilikuja duniani sio kuwaita walio na haki bali wenye dhambi kwenye toba; wenye [a]afya hawahitaji tabibu, bali wale walio wagonjwa; kwa hivyo, [b]watoto wachanga ni [c]wazima, kwani hawana uwezo wa kutenda

48 *a* MWM Sala.
b MWM Mtiifu, Tii, Utii; Yesu Kristo—Mfano wa Yesu Kristo.
c 1 Yoh. 3:1–3; 3 Ne. 27:27.
d 3 Ne. 19:28–29.

MWM Safi na Isiyo safi.

8 1 *a* M. ya Morm. 1:1.
3 *a* Mos. 4:11.
b MWM Neema.
4 *a* 3 Ne. 11:22, 28; 18:34.

7 *a* MWM Neno la Mungu.
8 *a* Mk. 2:17.
b Mk. 10:13–16.
c Mos. 3:16; M&M 74:7.

[d]dhambi; kwa hivyo laana ya [e]Adamu imetolewa kwao ndani yangu, kwamba haina uwezo juu yao; na sheria ya [f]kutahiriwa imeisha kwa ajili yangu.

9 Na katika njia hii Roho Mtakatifu alidhihirisha neno la Mungu kwangu; kwa hivyo, mwana wangu mpendwa, ninajua kwamba ni mzaha wa unadhiri mbele ya Mungu, kwamba mbatize watoto wachanga.

10 Tazama ninakwambia kwamba kitu hiki utafundisha—toba na ubatizo kwa wale ambao [a]wanawajibika wenye uwezo wa kutenda dhambi; ndiyo, fundisha wazazi kwamba lazima watubu na wabatizwe, na wajinyenyeze kama [b]watoto wao wachanga.

11 Na [a]watoto wao wachanga hawahitaji toba yoyote, wala ubatizo. Tazama, ubatizo upo katika toba ili kutimiza amri kwa [b]msamaha wa dhambi.

12 Lakini [a]watoto wachanga ni wazima katika Kristo, hata kutokea mwanzo wa dunia; ikiwa si hivyo, Mungu ni Mungu wa upendeleo, na pia Mungu wa kugeuka, na mwenye [b]kupendelea watu; kwani ni watoto wangapi wachanga wamekufa bila kubatizwa!

13 Kwa hivyo, ikiwa watoto wachanga hawangeweza kuokolewa bila ubatizo, hao lazima wangeenda kwenye jehanamu ya milele.

14 Tazama ninawaambia, yule ambaye anadhani kwamba watoto wachanga wanahitaji ubatizo yuko kwenye nyongo chungu na katika kifungo cha uovu; kwani hana [a]imani, wala tumaini, wala hisani; kwa hivyo, ikiwa atakufa kama bado anafikiria hivyo, ataenda jehanamu.

15 Kwani kutisha ni uovu kudhani kwamba Mungu huokoa mtoto mmoja kwa sababu ya ubatizo, na mwingine lazima aangamie kwa sababu hakubatizwa.

16 Laana iwe kwa wale ambao wataharibu njia za Bwana kwa utaratibu huu, kwani wataangamia wasipotubu. Tazama, naongea kwa ujasiri, nikiwa na [a]uwezo kutoka kwa Mungu; na siogopi kile watu wanachoweza kufanya; kwani [b]upendo ulio kamili [c]hutupa nje hofu.

17 Na nimejaa na [a]hisani, ambayo ni upendo usio na mwisho; kwa hivyo, watoto wote ni kama mimi; kwa hivyo, ninapenda [b]watoto wachanga

8 *d* MWM Dhambi.
e 2 Ne. 2:25–27. MWM Anguko la Adamu na Hawa.
f Mwa. 17:10–11. MWM Tohara.
10 *a* MWM Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
b MWM Mnyenyekevu, Unyenyekevu; Mtoto, Watoto.
11 *a* MWM Batiza, Ubatizo—Sifa zinazotakiwa kwa ajili ya ubatizo; Mtoto, Watoto.
b MWM Ondoleo la Dhambi.
12 *a* M&M 29:46–47; 93:38.
b Efe. 6:9; 2 Ne. 26:33; M&M 38:16.
14 *a* 1 Kor. 13; Eth. 12:6; Moro. 7:25–28; 10:20–23.
16 *a* MWM Mamlaka.
b MWM Upendo.
c 1 Yoh. 4:18.
17 *a* MWM Hisani.
b Mos. 3:16–19.

na upendo ulio kamili; na wote wako sawa na washiriki wa wokovu.

18 Kwani najua kwamba Mungu si Mungu wa kupendelea, wala kiumbe [a]kinachobadilika; lakini habadiliki kutoka milele hadi milele [b]yote.

19 [a]Watoto wachanga hawawezi kutubu; kwa hivyo, ni uovu wa kutisha kukana rehema safi ya Mungu kwao, kwani wote ni wazima ndani yake kwa sababu ya [b]rehema yake.

20 Na yule anayesema kwamba watoto wachanga wanahitaji ubatizo anakana huruma za Kristo, na huweka bure [a]upatanisho wake na nguvu ya ukombozi wake.

21 Ole kwa hawa, kwani wako katika hatari ya kifo, [a]jehanamu, na maumivu ya [b]milele. Ninazungumza kwa ujasiri; Mungu ameniamrisha. Yasikilize na uyafuate, au yatatumiwa kwako kwa kiti cha [c]hukumu cha Kristo.

22 Kwani tazama kwamba watoto wote wachanga ni [a]wazima katika Kristo; na pia wale wote ambao hawana [b]sheria. Kwani nguvu ya [c]ukombozi huja kwa wote ambao hawana sheria; kwa hivyo, yule ambaye hahukumiwi, au yule ambaye hayuko chini ya hukumu yoyote, hawezi kutubu; na kwa hao ubatizo hauleti chochote—

23 Lakini ni mzaha mbele ya Mungu, kukana huruma za Kristo, na nguvu za Roho Mtakatifu wake, na kuweka tumaini katika [a]kazi zisizo na uhai.

24 Tazama, mwana wangu, kitu hiki kisifanyike; kwani [a]toba ni kwa wale ambao wako chini ya hukumu na chini ya laana ya sheria iliyovunjwa.

25 Na matokeo ya kwanza ya [a]toba ni [b]ubatizo; na ubatizo huja na imani kwa kutimiza amri; na kule kutimiza amri huleta [c]kusamehewa kwa dhambi;

26 Na kusamehewa kwa dhambi huleta [a]unyenyekevu, na upole wa moyo; na kwa sababu ya unyeyekevu na upole wa moyo huja [b]Roho Mtakatifu, [c]Mfariji ambaye hujaza [d]tumaini na upendo kamili, [e]upendo ambao huvumilia kwa [f]sala ya [g]bidii, mpaka mwisho utakapo-

18 *a* Alma 7:20; Morm. 9:9. MWM Mungu, Uungu.
b Moro. 7:22.
19 *a* Lk. 18:15–17.
b MWM Rehema, enye Rehema.
20 *a* MWM Lipia dhambi, Upatanisho; Mpango wa Ukombozi.
21 *a* MWM Jehanamu.
b Yak. (KM) 6:10; Mos. 28:3; M&M 19:10–12.
c MWM Yesu Kristo—Mwamuzi.
22 *a* MWM Wokovu—Wokovu wa watoto.
b Mdo. 17:30; M&M 76:71–72.
c MWM Komboa, Kombolewa, Ukombozi.
23 *a* M&M 22:2.
24 *a* MWM Toba, Tubu.
25 *a* MWM Batiza, Ubatizo—Sifa zinazotakiwa kwa ajili ya ubatizo.
b Musa 6:58–60.
c M&M 76:52. MWM Ondoleo la Dhambi.
26 *a* MWM Pole, Upole.
b MWM Roho Mtakatifu.
c MWM Mfariji.
d MWM Tumaini.
e 1 Pet. 1:22; 1 Ne. 11:22–25.
f MWM Bidii.
g MWM Sala.

kuja, wakati [h]watakatifu wote watakapoishi na Mungu.

27 Tazama, mwana wangu, nitakuandikia tena ikiwa sitaenda nje tena mapema dhidi ya Walamani. Tazama, [a]kiburi cha taifa hili, au watu wa Wanefi, kimeleta uangamizo wao isipokuwa watubu.

28 Waombee, mwana wangu, kwamba toba ije kwao. Lakini tazama, ninaogopa isiwe Roho amekoma [a]kujitahidi nao; na katika sehemu hii ya nchi wanataka kuweka chini nguvu zote na mamlaka ambayo inatoka kwa Mungu; na [b]wanamkana Roho Mtakatifu.

29 Na baada ya kukataa elimu kubwa hivyo, mwana wangu, lazima waangamie karibuni, kwa kutimiza unabii ambao ulizungumzwa na manabii, na pia maneno ya Mwokozi wetu mwenyewe.

30 Kwaheri, mwana wangu, mpaka nitakapokuandikia, au nitakapokutana nawe tena. Amina.

Waraka wa pili wa Mormoni kwa mwanawe Moroni.

Yenye mlango wa 9.

MLANGO WA 9

Wote Wanefi na Walamani wana tabia mbaya na wamedhoofika—Wanatesana na kuuana—Mormoni anaomba kwamba neema na uzuri uwe kwa Moroni milele. Karibia mwaka 401 B.K.

Mwana wangu mpendwa, ninakuandikia tena ili ujue kwamba mimi bado ni mzima; lakini ninaandika kidogo kwa yale ambayo ni mazito.

2 Kwani tazama, nimekuwa na vita vikali na Walamani, ambavyo hatukushinda; na Arkeanto ameuawa kwa upanga, na pia Luramu na Emroni; ndiyo, na tumepoteza idadi kubwa ya watu wetu wazuri.

3 Na sasa tazama, mwana wangu, ninaogopa kwamba Walamani watawaangamiza hawa watu; kwani hawatubu, na Shetani anawachochea siku zote kukasirikiana wao kwa wao.

4 Tazama, ninajaribu kuwafundisha siku zote; na ninaposema neno la Mungu kwa [a]ukali wanatetemeka na kukasirika dhidi yangu; na nisipotumia ukali wanashupaza mioyo yao dhidi yake; kwa hivyo, ninaogopa isiwe Roho wa Bwana amekoma [b]kujitahidi nao.

5 Kwani wamekuwa na hasira sana kwamba inaonekana kwangu kwamba hawaogopi kifo; na wamepoteza mapenzi yao, mmoja kwa mwingine; na wana [a]kiu cha damu na kulipiza kisasi siku zote.

6 Na sasa, mwana wangu mpendwa, hata kwa ugumu wao, acha tuwafundishe kwa [a]bidii;

26 *h* mwm Mtakatifu.
27 *a* M&M 38:39.
mwm Kiburi.
28 *a* Morm. 5:16.
b Alma 39:6.
mwm Dhambi isiyo sameheka.
9 4 *a* 2 Ne. 1:26–27; M&M 121:41–43.
b M&M 1:33.
5 *a* Morm. 4:11–12.
6 *a* mwm Bidii.

kwani tukikoma kufanya [b]kazi, tungewekwa kwenye laana; kwani tuna kazi ya kufanya kama tungali kwenye hema hii ya udongo, kwamba tuweze kumshinda adui wa haki yote, na kupumzisha nafsi zetu katika ufalme wa Mungu.

7 Na sasa naandika kidogo kuhusu mateso ya hawa watu. Kwani kulingana na elimu ambayo nimepokea kutoka kwa Amoroni, tazama, Walamani wanao wafungwa wengi sana, ambao walikamatwa kutoka kwa mnara wa Sheriza; na kulikuwa na wanaume, wanawake, na watoto.

8 Na waume na baba za wale wanawake na watoto ambao wamewaua; na wanawalisha wanawake nyama za waume zao, na watoto nyama za baba zao; na hakuna maji, isipokuwa machache tu, wanayowapatia.

9 Na ijapokuwa haya machukizo makubwa ya Walamani, hayawezi kuzidi yale ya watu wetu walio Moriantumu. Kwani tazama, wengi wa mabinti za Walamani wamechukuliwa wafungwa na hao; na baada ya kuwanyang'anya kile ambacho kilikuwa cha thamani sana kuliko vitu vyote, ambacho ni [a]usafi wa kimwili na [b]wema—

10 Na baada ya hao kufanya kitu hiki, waliwauwa kwa njia ya kikatili sana, wakitesa miili yao hata hadi kifo; na baada ya kufanya haya, wanakula miili yao kama wanyama wa mwitu, kwa sababu ya ugumu wa mioyo yao; na wanaifanya kama ishara ya ushujaa.

11 Ee mwana wangu mpendwa, inawezekanaje watu kama hawa, ambao hawana ustaarabu—

12 (Na miaka michache tu imepita, tangu wawe wastaarabu na watu wazuri)

13 Lakini Ee mwana wangu, inawezekanaje watu kama hawa, ambao hupendezwa sana na machukizo mengi—

14 Tunawezaje kutumaini kwamba Mungu [a]atajizuia kutoa hukumu yake dhidi yetu?

15 Tazama, moyo wangu unalia: Ole kwa watu hawa. Njoo nje na uwahukumu, Ee Mungu, na ufiche dhambi zao, na uovu, na machukizo kutoka mbele ya uso wako!

16 Na tena, mwana wangu, kuna [a]wajane wengi na mabinti zao ambao wamebaki Sheriza; na sehemu ile ya vyakula ambayo Walamani hawakubeba, tazama, jeshi la Zenefi limebeba, na limewaacha wakizunguka kote ambako wangepata chakula; na wanawake wengi wazee wanazirai na kufia njiani.

17 Na jeshi ambalo liko na mimi ni dhaifu; na majeshi ya Walamani yako katikati ya Sheriza na mimi; na kwa vile wengi walikimbilia jeshi la [a]Haruni wamekuwa madhabuha kwa ukorofi wao wa kutisha.

18 Ee upotovu wa watu

6 *b* Yak. (KM) 1:19; Eno. 1:20. MWM Wajibu.

9 *a* MWM Usafi wa Kimwili. *b* MWM Wema.

14 *a* Alma 10:23.

16 *a* MWM Mjane.

17 *a* Morm. 2:9.

wangu! Hawana msimamo na hawana huruma. Tazama, mimi ni mtu tu, na ninazo nguvu tu za mtu, na siwezi tena kulazimisha amri zangu.

19 Na wamejiimarisha kwa upotovu wao; na ni wakorofi sawasawa, bila kuachilia yeyote, si wazee wala vijana; na wanafurahia kila kitu isipokuwa kile ambacho ni kizuri; na kuumia kwa wanawake wetu na watoto wetu juu ya uso wote wa nchi hii kunazidi kila kitu; ndiyo, ulimi hauwezi kusema, wala haiwezekani kuandikwa.

20 Na sasa, mwana wangu, sitaendelea kueleza hii tamasha ya kuogofya. Tazama, unajua uovu wa hawa watu; unajua kwamba hawana msimamo, na wamekufa ganzi, na uovu wao [a]unazidi ule wa Walamani.

21 Tazama, mwana wangu, siwezi kuwapendekeza kwa Mungu asije akaniua.

22 Lakini tazama, mwana wangu, ninakupendekeza kwa Mungu, na ninaamini katika Kristo kwamba utaokolewa; na ninamwomba Mungu kwamba [a]atakuhurumia maisha yako, kushuhudia kurudi kwa watu wake kwake, au uharibifu wao halisi; kwani najua kwamba lazima waangamie isipokuwa [b]watubu na wamrudie.

23 Na ikiwa wataangamia itakuwa kama ilivyotendeka kwa Wayaredi, kwa sababu ya ukaidi wa mioyo yao, [a]wakitazamia kuua na kulipiza [b]kisasi.

24 Na ikiwa kwamba wataangamia, tunajua kwamba wengi wa ndugu zetu [a]wametoroka na kujiunga na Walamani, na wengi zaidi pia watatorokea kwao; kwa hivyo, uandike vitu vidogo zaidi, ikiwa utaachwa na nife bila kukuona; lakini ninaamini kwamba nitakuona hivi karibuni; kwani ninayo maandishi matakatifu ambayo [b]nitakupatia.

25 Mwana wangu, uwe mwaminifu katika Kristo; na vitu ambavyo nimeandika visikusikitishe, na kukuwekea mzigo wa kukuua; lakini Kristo akuinue juu, na [a]kuumia kwake na kifo chake, na kudhihirisha kwa mwili wake kwa babu zetu, na rehema yake na uvumilivu, na matumaini ya utukufu wake na [b]uzima wa milele, yawe katika [c]akili yako milele.

26 Na ninaomba neema ya Mungu Baba, ambaye kiti chake cha enzi kiko juu mbinguni, na Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye huketi kwenye [a]mkono wake wa kulia wa uwezo wake, mpaka vitu vyote vitakapokuwa chini yake, iwe, na kiishi nawe milele. Amina.

MLANGO WA 10

Ushuhuda wa Kitabu cha Mormoni huja kwa uwezo wa Roho

20 *a* Hel. 6:34–35.
22 *a* Morm. 8:3.
b Mal. 3:7; Hel. 13:11; 3 Ne. 10:6; 24:7.
23 *a* Morm. 4:11–12.
b Eth. 15:15–31.
24 *a* Alma 45:14.
b Morm. 6:6.
25 *a* MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
b MWM Uzima wa Milele.
c MWM Nia.
26 *a* Lk. 22:69; Mdo. 7:55–56; Mos. 5:9; Alma 28:12.

Mtakatifu—Vipawa vya Roho hutolewa kwa walio waaminifu—Karama za kiroho kila mara huambatana na imani—Maneno ya Moroni yanazungumza kutoka mavumbini—Njooni kwa Kristo, mkamilishwe ndani Yake, na mtakase nafsi zenu. Karibia mwaka 421 B.K.

Sasa mimi, Moroni, naandika machache ambayo naona ni ya kufaa; na ninaandika kwa ndugu zangu, [a]Walamani; na ningependa kwamba wajue kwamba zaidi ya miaka mia nne na ishirini imepita tangu ishara ilipotolewa ya kuja kwa Kristo.

2 Na ninaweka [a]muhuri maandishi haya, baada ya kuzungumza maneno machache kwa njia ya ushauri kwenu.

3 Tazama, ningewashauri kwamba mtakaposoma vitu hivi, ikiwa itakuwa hekima katika Mungu kwamba myasome, kwamba mngekumbuka jinsi vile Bwana amekuwa na huruma kwa watoto wa watu, kutokea kuumbwa kwa Adamu hadi chini mpaka wakati ambapo mtapokea vitu hivi, na [a]kuitafakari katika [b]mioyo yenu.

4 Na mtakapopokea vitu hivi, ningewashauri kwamba [a]mngemwuliza Mungu, Baba wa Milele, katika jina la Kristo, ikiwa vitu hivi [b]si vya kweli; na ikiwa mtauliza na [c]moyo wa kweli, na [d]kusudi halisi, mkiwa na [e]imani katika Kristo, [f]atawaonyesha [g]ukweli wake kwenu, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

5 Na kwa uwezo wa Roho Mtakatifu [a]mtajua [b]ukweli wa vitu vyote.

6 Na kitu chochote kilicho kizuri ni haki na kweli; kwa hivyo, hakuna chochote ambacho ni kizuri ambacho humkana Kristo, lakini hukubali kwamba yuko.

7 Na mngejua kwamba yuko, kwa uwezo wa Roho Mtakatifu; kwa hivyo ningewashauri kwamba msikatae uwezo wa Mungu; kwani hufanya kazi kwa uwezo, [a]kulingana na imani ya binadamu, sawa leo na kesho, na milele.

8 Na tena, ninawashauri, ndugu zangu, kwamba msikatae [a]karama za Mungu, kwani ni nyingi; na zinatoka kwa yule yule Mungu. Na kuna njia [b]tofauti ambazo karama hizi hutolewa; lakini ni yule yule Mungu azitendaye kazi zote katika wote; na hupewa kwa ufunuo wa Roho wa Mungu kwa watu, kuwasaidia.

9 Kwani tazama, [a]kwa mmoja

10 1*a* M&M 10:48.
2*a* Morm. 8:4, 13–14. MWM Maandiko—Maandiko yaliyotolewa unabii kwamba yatakuja.
3*a* Kum. 11:18–19. MWM Tafakari.
b Kum. 6:6–7.
4*a* MWM Sala.
b 1 Ne. 13:39; 14:30; Mos. 1:6; Eth. 4:10–11; 5:3.
c MWM Mwaminifu, Uaminifu.
d Yak. (Bib.) 1:5–7; Moro. 7:9.
e MWM Amini, Imani.
f MWM Ufunuo.
g MWM Ukweli.
5*a* M&M 35:19. MWM Ushuhuda; Utambuzi, Kipawa cha.
b Yn. 8:32.
7*a* 1 Ne. 10:17–19.
8*a* MWM Vipawa vya Roho.
b M&M 46:15.
9*a* 1 Kor. 12:8–11; M&M 46:8–29.

inatolewa kwa Roho wa Mungu, kwamba [b]afundishe neno la hekima;

10 Na kwa mwingine, kwamba afundishe neno la elimu na Roho yule yule;

11 Na kwa mwingine, [a]imani kubwa sana; na kwa mwingine, karama za [b]kuponya na Roho yule yule;

12 Na tena, kwa mwingine, kwamba aweze kufanya [a]miujiza mikuu;

13 Na tena, kwa mwingine, kwamba aweze kutoa unabii kuhusu vitu vyote;

14 Na tena, kwa mwingine; kuona kwa malaika na kutumikia roho;

15 Na tena, kwa mwingine, lugha za aina zote;

16 Na tena, kwa mwingine, kutafsiri kwa lugha na [a]ndimi za aina tofauti.

17 Na karama hizi zote huja kwa Roho ya Kristo; na huja kwa kila mtu moja kwa moja, kulingana na vile anavyotaka.

18 Na ningewashauri ninyi, ndugu zangu wapendwa, kwamba mkumbuke kwamba [a]kila karama nzuri hutoka kwa Kristo.

19 Na ningewashauri ninyi, ndugu zangu wapendwa, kwamba mkumbuke kwamba yeye ndiye [a]yule yule jana, leo, na milele, na kwamba karama hizi zote ambazo nimezungumzia, ambazo ni za kiroho, hazitatolewa mbali, kadiri dunia itakavyokuwepo, kulingana tu na [b]kutoamini kwa watoto wa watu.

20 Kwa hivyo, lazima kuwe na [a]imani; na ikiwa kutakuwa na imani lazima kuwe pia na tumaini; na ikiwa kutakuwa na tumaini lazima kuwe pia na hisani.

21 Na msipokuwa na [a]hisani hamwezi kwa vyovyote kuokolewa katika ufalme wa Mungu; wala hamwezi kuokolewa katika ufalme wa Mungu kama hamna imani; wala hamwezi ikiwa hamna tumaini.

22 Na kama hamna tumaini lazima iwe ni kwa kukata tamaa; na kukata tamaa huja kwa sababu ya uovu.

23 Na Kristo kwa kweli alisema kwa babu zetu: [a]Mkiwa na imani mnaweza kufanya vitu vyote ambavyo vinatakikana kwangu.

24 Na sasa ninazungumzia watu wote waliomo duniani—kwamba ikiwa siku itakuja kwamba uwezo na karama za Mungu zitaondolewa kutoka miongoni mwenu, itakuwa ni kwa [a]sababu ya [b]kutoamini.

25 Na ole kwa watoto wa watu ikiwa itakuwa hivyo; kwani hakutakuwa [a]yeyote ambaye hufanya mema miongoni mwenu, la hata mmoja. Kwani ikiwa

9*b* M&M 88:77–79, 118.
11*a* MWM Amini, Imani.
b MWM Ponya, Uponyaji.
12*a* MWM Muujiza.
16*a* MWM Ndimi, Kipawa cha.
18*a* Yak. (Bib.) 1:17.
19*a* Ebr. 13:8.
b Moro. 7:37.
20*a* Eth. 12:3–37.
21*a* 1 Kor. 13; Moro. 7:1, 42–48. MWM Hisani.
23*a* Moro. 7:33.
24*a* Moro. 7:37.
b MWM Kutoamini.
25*a* TJS Zab. 14:1–7 (Kiambatisho); Rum. 3:10–12.

kuna mmoja miongoni mwenu ambaye hufanya mema, atafanya kwa uwezo na karama za Mungu.

26 Na ole kwa hao ambao watatoa vitu hivi na kufa, kwani [a]wanakufa katika [b]dhambi zao, na hawawezi kuokolewa katika ufalme wa Mungu; na ninaizungumzia kulingana na maneno ya Kristo; na sidanganyi.

27 Na ninawashauri mkumbuke vitu hivi; kwani wakati unafika haraka kwamba mtajua kwamba sidanganyi, kwani mtaniona katika kiti cha hukumu cha Mungu; na Bwana Mungu atasema kwenu: Je, si mimi nilitangaza [a]maneno yangu kwenu, ambayo yaliandikwa na mtu huyu, kama mmoja [b]anayelia kutoka kwa wafu, ndiyo, hata kama mmoja asemaye kutoka [c]mavumbini?

28 Ninatangaza vitu hivi kwa kutimiza unabii. Na tazama, yatatoka nje ya mdomo wa Mungu asiye na mwisho; na neno lake [a]litaenda mbele kutoka kwa kizazi hadi kingine.

29 Na Mungu atawaonyesha, kwamba yale ambayo nimeandika ni ya kweli.

30 Na tena ninawashauri kwamba [a]mngekuja kwa Kristo, na kushikilia juu ya kila karama nzuri, na [b]msiguse ile karama mbovu, wala kitu kichafu.

31 Na [a]amka, na kutoka kwenye mavumbi, Ee Yerusalemu; ndiyo, na ujivike mavazi ya kurembesha, Ee binti wa [b]Sayuni; na [c]imarisha [d]vigingi vyako na ongeza mipaka yako milele, kwamba [e]hutachanganywa tena, kwamba agano la Baba wa milele ambalo amefanya kwako, Ee nyumba ya Israeli, liwezekane kutimizwa.

32 Ndiyo, [a]mje kwa Kristo na [b]mkamilishwe ndani yake, na mjinyime ubaya wote; na ikiwa mtajinyima ubaya wote, na [c]kumpenda Mungu na mioyo yenu, akili na nguvu zenu zote, basi neema yake inawatosha, kwamba kwa neema yake mngekamilishwa katika Kristo; na ikiwa kwa [d]neema ya Mungu mnakamilika katika Kristo, hamwezi kwa njia yoyote kukana uwezo wa Mungu.

33 Na tena, ikiwa ninyi kwa neema ya Mungu ni kamili katika Kristo, na hamkani uwezo wake, ndipo [a]mmetakaswa katika Kristo kwa neema ya Mungu, kupitia kwa [b]upatanisho wa Kristo, ambayo ni agano la Baba kwa [c]kusamehewa kwa dhambi zenu, kwamba muwe [d]watakatifu, bila waa.

26 *a* Eze. 18:26–27; 1 Ne. 15:32–33; Mos. 15:26.
b Yn. 8:21.
27 *a* 2 Ne. 33:10–11.
b 2 Ne. 3:19–20; 27:13; 33:13; Morm. 9:30.
c Isa. 29:4.
28 *a* 2 Ne. 29:2.
30 *a* 1 Ne. 6:4; Morm. 9:27; Eth. 5:5.
b Alma 5:57.
31 *a* Isa. 52:1–2.
b MWM Sayuni.
c Isa. 54:2.
d MWM Kigingi.
e Eth. 13:8.
32 *a* Mt. 11:28; 2 Ne. 26:33; Yak. (KM) 1:7; Omni 1:26.
b Mt. 5:48; 3 Ne. 12:48. MWM Kamilifu.
c M&M 4:2; 59:5–6.
d 2 Ne. 25:23.
33 *a* MWM Utakaso.
b MWM Lipia dhambi, Upatanisho.
c MWM Ondoleo la Dhambi.
d MWM Utakatifu.

34 Na sasa ninasema kwenu nyote, kwa herini. Hivi karibuni nitaenda [a]kupumzika katika [b]peponi ya Mungu, mpaka [c]roho yangu na mwili [d]vitakapounganishwa tena, na niinuliwe juu kwa ushindi kupitia [e]angani, kukutana na ninyi mbele ya kiti cha enzi cha [f]kupendeza cha yule [g]Yehova mkuu, [h]Mwamuzi wa Milele wa wanaoishi na waliokufa. Amina.

34 *a* мwм Pumzika.
b мwм Peponi.
c мwм Roho.
d мwм Ufufuko.
e 1 The. 4:17.
f Yak. (KM) 6:13.
g мwм Yehova.
h мwм Yesu Kristo—Mwamuzi.

MWISHO

KIAMBATISHO

MWONGOZO WA MAANDIKO

WENDO

UPATANIFU WA INJILI

MWONGOZO WA MAANDIKO

Mwongozo wa Maandiko hutoa maana fupi ya mafundisho, kanuni, watu, na mahali vinapopatikana katika Biblia Takatifu, Kitabu cha Mormoni, Mafundisho na Maagano, na Lulu ya Thamani Kuu. Na pia hutoa marejeo muhimu ya kimaandiko kwa ajili ya mafundisho yako kwa kila mada. Mwongozo huu waweza kukusaidia wewe katika mafundisho yako ya maandiko kibinafsi na kifamilia. Unaweza kukusaidia kujibu maswali juu ya injili, kujifunza mada katika maandiko, kutayarisha mahubiri na masomo, na kuongeza maarifa na ushuhuda wa injili.

Mchoro ufuatao unaelezea mfano wa ingizo katika Mwongozo wa Maandiko:

Mada zipo katika herufi nzito.

Dunia. *Ona pia* Ulimwengu; Umba, Uumbaji

Nyakati zingine mada zingine katika mwongozo zinazo habari ambazo zinahusiana na mada ambayo wewe unajifunza. Maneno ya hefuri mlazo ya kiitaliki Ona pia hukuelekeza wewe kwenye mada hizi zinazohusiana nayo.

Mada zinajumuisha maana kwa ufupi.

Sayari ambayo juu yake tunaishi, iliumbwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo ili itumiwe na mwanadamu wakati wa kuzaliwa katika mwili wenye kufa na kwa majaribio yake. Hatima yake ni kuwa iliyotukuzwa na kuinuliwa. (M&M 77:1–2; 130:8–9). Dunia itakuwa ni urithi wa milele wa wale walioishi wakistahili fahari ya selestia (M&M 88:14–26). Watafurahia uwepo wa Baba na Mwana (M&M 76:62).

Baadhi ya mada zina mada ndogo. Mada hizi ziko katika herufi aina ya mlazo za italiki.

Iliumbwa kwa ajili ya mwanadamu: Mungu alimpa mwanadamu utawala juu ya dunia, **Mwa.** 1:28 (Musa 2:28). Dunia ni ya Bwana, **Ku.** 9:29 (Zab. 24:1). Bwana amewapa dunia wanadamu, **Zab.** 115:16. Mimi nimeiumba dunia na nimemtunuku mwanadamu juu yake, **Isa.** 45:12.

Marejeo ya kimaandiko yanayofanana yametolewa katika mabano.

Kwa uwezo wa neno lake mwanadamu akaja juu ya dunia, **Yak. (KM)** 4:9.

Kila rejeo la kimaandiko limetanguliwa na dondoo fupi kutoka andiko au ufupisho wa andiko.

Dunia itatolewa kwa wale waliomchukua Roho Mtakatifu kuwa kiongozi wao, **M&M** 45:56–58 (M&M 103:7). Wale ambao wameitii injili wanapokea ujira wa mambo mema ya dunia, **M&M** 59:3. Walio maskini na wapole wa dunia watairithi, **M&M** 88:17 (Mt. 5:5; 3 Ne. 12:5).

Marejeo ya maandiko ambayo hukusaidia wewe kufahamu maana yapo katika mabano.

Sisi tutaifanya dunia, nasi tutawajaribu hao, **Ibr.** 3:24–25.

Nyakati zingine habari juu ya somo halijumuishwi chini ya mada uliyoiangalia. Neno la herufi mlazo la kiitaliki Tazama hukuelekeza kwenye mada ambako habari zake hupatikana.

Kalvari. *Ona* Golgotha

Kanisa, Lililo Kuu na Lenye Kuchukiza. *Ona* Ibilisi—Kanisa la ibilisi

Neno la herufi mlazo la kiitaliki Ona (au Ona pia) likifuatiwa na dashi hii hukuambia wewe kwamba taarifa hiyo inapatikana katika mlango mdogo ("Kanisa la ibilisi") wa mada kuu ("Ibilisi").

Abednego. *Ona pia* Danieli

Katika Agano la Kale, Shadraki, Meshaki, na Abednego walikuwa vijana watatu wa Kiisraeli ambao, pamoja na Danieli, waliletwa katika jumba la Nebukadneza, mfalme wa Babilonia. Jina la Abednego katika Kiebrania lilikuwa Azaria. Vijana hawa wanne walikataa kujinajisi kwa kula chakula na mvinyo wa mfalme (Dan. 1). Mfalme aliwatupa Shadraka, Meshaki, na Abednego katika tanuru lenye kuwaka moto lakini kimiujiza wakaokolewa (Dan. 3).

Abinadi. *Ona pia* Kifo cha kishahidi, Mfiadini

Nabii wa Kinefi katika Kitabu cha Mormoni.

Alitoa unabii kwamba Mungu angewaadhibu watu wa mfalme mwovu Nuhu isipokuwa kama watatubu, **Mos.** 11:20–25. Alitiwa gerezani kwa kutoa unabii wa angamizo la Mfalme Nuhu na watu wake, **Mos.** 12:1–17. Aliwafundisha makuhani waovu wa Mfalme Nuhu juu ya sheria ya Musa na juu ya Kristo, **Mos.** 12–16. Alma Mkubwa aliamini na kuandika maneno yake, **Mos.** 17:2–4. Aliunguzwa kwa moto hadi kufa na Mfalme Nuhu, **Mos.** 17:20.

Abramu. *Ona* Ibrahimu

Adamu. *Ona pia* Adamu-ondi-Amani; Anguko la Adamu na Hawa; Edeni; Hawa; Malaika mkuu; Mikaeli

Mwanadamu wa kwanza kuumbwa duniani.

Adamu ndiye baba na patriaki wa jamii ya wanadamu duniani. Uvunjaji wa sheria katika Bustani ya Edeni (Mwa. 3; M&M 29:40–42; Musa 4) ulimsababisha "aanguke" na kuwa mwenye kufa, hatua iliyo muhimu kwa mwanadamu kukua hapa duniani (2 Ne. 2:14–29; Alma 12:21–26). Kwa sababu hiyo Adamu na Hawa yapaswa waheshimiwe kwa kazi yao waliyofanya katika kuwezesha makuzi yetu ya milele. Adamu ndiye Mzee wa Siku na pia hujulikana kama Mikaeli (Dan. 7; M&M 27:11; 107:53–54; 116; 138:38). Yeye ndiye malaika mkuu (M&M 107:54) na atakuja tena duniani kama patriaki wa familia ya wanadamu, kama matayarisho kwa ujio wa pili wa Yesu Kristo (M&M 116).

Mungu alimwumba mwanadamu kwa sura yake mwenyewe, **Mwa.** 1:26–28 (Musa 2:26–28; Ibr. 4:26–28). Mungu akampa mwanadamu utawala juu ya vitu vyote na akamwamuru aongezeke na akaijaze dunia, **Mwa.** 1:28–31 (Musa 2:28–31; Ibr. 4:28–31). Mungu akawaweka Adamu na Hawa katika Bustani ya Edeni na akawakataza wasile matunda ya mti wa ujuzi wa mema na maovu, **Mwa.** 2:7–9, 15–17 (Musa 3:7–9, 15–17; Ibr. 5:7–13). Adamu akawapa majina kila kiumbe kilichokuwa hai, **Mwa.** 2:19–20 (Musa 3:19–20; Ibr. 5:20–21). Adamu na Hawa waliozwa na Mungu, **Mwa.** 2:18–25 (Musa 3:18–25; Ibr. 5:14–21). Adamu na Hawa walijaribiwa na Shetani, wakala lile tunda lililokatazwa, nao wakafukuzwa nje ya Bustani ya Edeni, **Mwa.** 3 (Musa 4). Adamu alikuwa na umri wa miaka 930 wakati wa kifo chake, **Mwa.** 5:5 (Musa 6:12).

Adamu alikuwa mwanadamu wa kwanza, **M&M** 84:16. Kabla ya kifo chake damu aliwaita wazao wake waliokuwa wenye haki pamoja huko Adamu-ondi-Amani na akawabariki, **M&M** 107:53–57.

Adamu alitoa dhabihu, **Musa** 5:4–8. Adamu alibatizwa, akapokea Roho Mtakatifu, na akatawazwa katika ukuhani, **Musa** 6:51–68.

Adamu-ondi-Amani. *Ona pia* Adamu

Mahali ambapo Adamu aliwabariki wazao wake waliokuwa na haki miaka mitatu kabla ya kufariki (M&M 107:53–56) na ni mahali ambapo atafikia kabla ya wakati wa Ujio wa Pili (M&M 116).

Adhabu Kuu. *Ona pia* Mauaji

Adhabu ya kifo kwa kosa la jinai lililotendeka, hususani linahusiana na adhabu ya kuua.

Atakaye mwaga damu ya mwana-

damu, damu yake huyo itamwagwa na mwanadamu, **Mwa.** 9:6 (TJS, Mwa. 9:12–13). Mwuaji hakika atauawa, **Hes.** 35:16.

Wauaji wanaouwa kwa makusudi watakufa, **2 Ne.** 9:35. Wewe umehukumiwa kufa kulingana na sheria, **Alma** 1:13–14. Yule aliyeua aliadhibiwa kwa kifo, **Alma** 1:18. Sheria inahitaji uhai wa yule aliyeua, **Alma** 34:12.

Yule anayeua atakufa, **M&M** 42:19.

Adui. *Ona* Ibilisi

Afya. *Ona* Neno la Hekima

Agano. *Ona pia* Agano Jipya; Agano Jipya na Lisilo na Mwisho; Agano la Ibrahimu; Agano la Kale; Kiapo; Kiapo na Agano la Ukuhani

Makubaliano kati ya Mungu na mwanadamu, lakini hawatendi kama walio sawa katika makubaliano hayo. Mungu hutoa masharti ya agano, na wanadamu hukubali kutenda yale Yeye aliyowaagiza kuyafanya. Ndipo Mungu huwaahidi wanadamu baraka fulani kwa utiifu wao.

Kanuni na ibada hupokelewa kwa agano. Waumini wa Kanisa wafanyao maagano ya namna hiyo huahidi kuyaheshimu. Kwa mfano, waumini huagana na Bwana wakati wa ubatizo na kurudia agano hilo kwa kupokea sakramenti. Hufanya maagano mengine zaidi katika hekalu. Watu wa Bwana ni watu wa agano nao hubarikiwa sana kadiri wanavyoshika maagano yao na Bwana.

Nitafanya agano langu nawe, **Mwa.** 6:18. Lishikeni agano langu; ndipo mtakapokuwa hazina ya thamani, **Ku.** 19:5. Usifanye maagano pamoja nao wala pamoja na miungu yao, **Ku.** 23:32. Ishikeni sabato kwa agano la milele, **Ku.** 31:16. Mimi, milele sitalivunja agano langu pamoja nawe, **Amu.** 2:1. Watakatifu wangu waliofanya agano nami kwa dhabihu, **Zab.** 50:5 (M&M 97:8).

Kumbukeni agano lake takatifu, **Lk.** 1:72 (M&M 90:24).

Nguvu za Mungu zikashuka juu ya watu wa Bwana wa agano, **1 Ne.** 14:14. Agano lililofanywa kwa Ibrahimu litatimizwa katika siku za mwisho, **1 Ne.** 15:18 (3 Ne. 16:5, 11–12; 21:7; Morm. 9:37). Watu wa Benjamini walikuwa radhi kuingia katika agano na Mungu la kutenda mapenzi yake, **Mos.** 5:5. Ubatizo ni ushuhuda kwamba mwanadamu ameingia katika agano na Mungu la kumtumikia Yeye, **Mos.** 18:13. Ninyi ni watoto wa agano, **3 Ne.** 20:25–26. Malaika hutimiza na kutenda kazi za maagano ya Baba, **Moro.** 7:29–31. Kumwagika kwa damu ya Kristo ni agano, **Moro.** 10:33.

Kila mtu aliye wa kanisa hili la Kristo ataangalia maagano yote, **M&M** 42:78. Heri wao walioshika agano, **M&M** 54:6. Yule avunjaye agano hili atapoteza nafasi yake na uanachama wake katika Kanisa, **M&M** 78:11–12. Wale wote waupokeao ukuhani hupokea kiapo hiki na agano hili, **M&M** 84:39–40. Wao wako radhi kuyatunza maagano yao kwa dhabihu, **M&M** 97:8. Agano la ndoa laweza kuwa la milele, **M&M** 132. Hili ndilo litakuwa agano letu, ya kwamba tutatembea katika maagizo yote, **M&M** 136:4.

Agano Jipya. *Ona pia* Biblia; Maandiko

Mkusanyiko wa maandishi yaliyoandikwa kwa kuongozwa na Mungu (mwanzoni yalikuwa ya Kiyunani) juu ya maisha na huduma ya Yesu Kristo, Mitume, na wanafunzi wengine wa Yesu Kristo. Agano Jipya kwa ujumla limegawanyika katika Injili, Matendo ya Mitume, nyaraka za Paulo, nyaraka za jumla, na kitabu cha Ufunuo.

Injili nne—vitabu vya Mathayo, Marko, Luka, na Yohana—ni taarifa juu ya maisha ya Kristo. Kitabu cha Matendo kinaandika historia ya Kanisa na Mitume, hususani safari za Paulo za kimisionari, baada ya kifo cha Kristo. Barua za Paulo hutoa mafundisho kwa viongozi wa Kanisa na waumini. Barua nyingine ziliandikwa na Mitume

wengine nazo zinatoa nyongeza ya ushauri kwa Watakatifu wa awali. Kitabu cha Ufunuo, ambacho kiliandikwa na Mtume Yohana kina unabii zaidi uhusuo siku za mwisho.

Agano Jipya na Lisilo na Mwisho. *Ona pia* Agano

Utimilifu wa injili ya Yesu Kristo (M&M 66:2). Ni mpya kila wakati inapofunuliwa upya kufuatia kipindi cha ukengeufu. Ni lisilo na mwisho katika maana ya kwamba ni Agano la Mungu na limekuwa likifurahiwa katika kila kipindi cha maongozi ya injili ambapo watu wamekuwa radhi kuipokea. Agano jipya na lisilo na mwisho lilifunuliwa tena kwa wanadamu duniani na Yesu Kristo kupitia Joseph Smith Nabii. Inazo ibada takatifu zinazoendeshwa kwa mamlaka ya ukuhani—kama vile ubatizo na ndoa ya hekaluni—ambazo humpa mwanadamu wokovu, mwili usiokufa, na uzima wa milele. Watu wanapoikubali injili na kuahidi kushika amri za Mungu, Mungu hutoa agano na kuwapa baraka za agano Lake jipya na lisilo na mwisho.

Nitalifanya agano langu kati ya mimi na wewe, **Mwa.** 17:7. Atakuwa na agano la ukuhani wa usio na mwisho, **Hes.** 25:13. Watu wameyabadili maagizo na wamevunja agano lisilo na mwisho, **Isa.** 24:5 (M&M 1:15). Nitafanya agano lisilo na mwisho pamoja nanyi, **Isa.** 55:3 (Yer. 32:40). Litakuwa agano lisilo na mwisho, **Eze.** 37:26.

Bwana alifanya agano jipya, na la zamani likapita, **Ebr.** 8:13. Yesu ndiye mpatanishi wa agano jipya, **Ebr.** 12:24 (M&M 76:69).

Hili ni agano jipya na lisilo na mwisho, **M&M** 22:1. Nimelipeleka agano langu lisilo na mwisho ulimwenguni, **M&M** 45:9 (M&M 49:9). Bwana alipeleka utimilifu wa injili yake, agano lake lisilo na mwisho, **M&M** 66:2 (M&M 133:57). Ili kupata daraja la juu zaidi katika ufalme wa selestia, mwanadamu ni lazima aingie katika agano jipya na lisilo na mwisho la ndoa, **M&M** 131:1–2. Agano jipya na lisilo na mwisho lilianzishwa kwa ajili ya utimilifu wa utukufu wa Bwana, **M&M** 132:6, 19.

Agano la Ibrahimu. *Ona pia* Agano; Ibrahimu; Tohara

Ibrahimu aliipokea injili na akatawazwa katika ukuhani wa juu (M&M 84:14; Ibr. 2:11), naye akaingia katika ndoa ya selestia, ambayo ni agano la kuinuliwa (M&M 131:1–4; 132:19, 29). Ibrahimu alipokea ahadi ya kwamba baraka zote za maagano haya zitatolewa kwa wazao wake watakaozaliwa duniani (M&M 132:29–31; Ibr. 2:6–11). Kwa pamoja, maagano na ahadi hizi ndiyo huitwa agano la Ibrahimu. Urejesho wa agano hili ulikuwa ndiyo Urejesho wa injili katika siku za mwisho, kwani kwa hiyo mataifa yote ya dunia yamebarikiwa (Gal. 3:8–9, 29; M&M 110:12; 124:58; Ibr. 2:10–11).

Agano la Kale. *Ona pia* Biblia; Maandiko; Torati

Maandishi ya manabii wa kale waliofanya hivyo chini ya ushawishi wa Roho Mtakatifu na ambao kwa karne nyingi walimshuhudia Kristo na huduma Yake ya wakati ujao. Pia linayo kumbu kumbu ya historia ya Ibrahimu na uzao wake, ikianzia na Ibrahimu, na agano, au ushuhuda, ambao Bwana aliufanya na Ibrahimu na uzao wake.

Vitabu vitano vya kwanza vya Agano la Kale viliandikwa na Musa. Navyo ni Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu, na Kumbukumbu la Torati. Mwanzo kinaelezea asili ya dunia, mwanadamu, lugha, jamii, na mwanzo wa nyumba ya Israeli.

Vitabu hivi vya kihistoria vinasimulia juu ya matukio ya Israeli. Vitabu hivyo ni Yoshua, Waamuzi, Rutu, 1 na 2 Samweli, 1 na 2 Wafalme, 1 na 2 Mambo ya Nyakati, Ezra, Nehemia, na Esta.

Vitabu vya kishairi vinaandika baadhi ya hekima na ustadi wa lugha wa manabii. Navyo ni Ayubu, Zaburi, Mithali,

Mhubiri, Wimbo wa Suleimani, na Maombolezo.

Manabii walimwonya Israeli juu ya dhambi zake na wakatoa ushuhuda juu ya baraka zinazokuja kutokana na utii. Walitoa unabii juu ya kuja kwa Kristo, ambaye angelipia dhambi za wale ambao wanatubu, kupokea ibada, na kuishi kulingana na injili. Vitabu vya manabii ni Isaya, Yeremia, Ezekieli, Danieli, Hosea, Yoeli, Amosi, Obadia, Yona, Mika, Nahumu, Habakuki, Zefania, Hagai, Zekaria, na Malaki.

Vitabu vingi vya Agano la Kale viliandikwa katika Kiebrania. Maandishi machache yalikuwa ya Kiaramaya, lugha inayofanana na Kiebrania.

Agano Lisilo na Mwisho. *Ona* Agano; Agano Jipya na Lisilo na Mwisho

Agripa. *Ona pia* Paulo

Katika Agano Jipya, ni mwana wa Herodi Agripa I na nduguye Bernika na Drusila. Alikuwa mfalme wa Chalsi, iliyoko katika milima ya Lebanoni. Alimsikiliza Mtume Paulo naye alikaribia kushawishika kuwa Mkristo (Mdo. 25–26; JS—H 1:24).

Ahabu. *Ona pia* Yezebeli

Mmoja kati ya wafalme waovu na aliyekuwa na nguvu nyingi katika Israeli ya kaskazini, katika Agano la Kale. Alimwoa Yezebeli, binti mfalme wa Sidoni, ambaye kwa ushawishi wake kuabudiwa kwa Baali na Ashtorethi kulianza katika Israeli (1 Fal. 16:29–33; 2 Fal. 3:2) na alijaribu kuwaangamiza manabii na kuabudiwa kwa Yehova (1 Fal. 18:13).

Aliitawala Israeli katika Samaria kwa miaka ishirini na miwili, **1 Fal.** 16:29 (1 Fal. 16–22). Alifanya uovu mbele ya uso wa Bwana kuliko wale wote waliokuwa kabla yake, **1 Fal.** 16:30. Aliuawa vitani, **1 Fal.** 22:29–40.

Akida

Ofisa katika jeshi la Kirumi ambaye aliongoza kikundi cha watu hamsini hadi mia moja. Kikundi cha aina hii kilifanya sehemu moja ya sita ya kikosi cha jeshi la Kirumi. (Ona Mt. 8:5; Lk. 23:47; Mdo. 10:1–8.)

Akidi. *Ona pia* Ukuhani

Neno akidi linaweza kutumika katika njia mbili: (1) Kikundi fulani maalumu cha wanaume waliomo katika ofisi moja ya ukuhani. (2) Wingi, au idadi ya chini kabisa ya washiriki katika kikundi cha ukuhani ambacho ni lazima kiwe katika mahudhurio ya mkutano ili kuendesha shughuli ya Kanisa (M&M 107:28).

Akidi za Urais wa Kwanza, ya wale Kumi na Wawili, na ya wale Sabini na uhusiano wake unaelezwa, **M&M** 107:22–26, 33–34 (M&M 124:126–128). Maamuzi ya akidi hizi lazima yawe ya kauli moja, **M&M** 107:27. Maamuzi ya akidi yatafanyika katika uadilifu wote, **M&M** 107:30–32. Kazi za marais wa akidi za ukuhani zinaelezwa, **M&M** 107:85–96. Akidi ya wazee imewekwa kwa ajili ya wahudumu wasimamizi, **M&M** 124:137.

Akili, Viumbe-akili-asilia. *Ona pia* Nuru, Nuru ya Kristo; Roho; Ukweli

Akili ina maana kadhaa, tatu kati ya hizo ni: (1) Ni nuru ya kweli itoayo uzima na mwangaza kwa vitu vyote katika ulimwengu. Daima imekuwepo. (2) Neno viumbe-akili-asilia laweza pia kumaanisha watoto wa kiroho wa Mungu. (3) Maandiko pia husema akili yakionyesha vitu vya asili kiroho ambavyo viliishi kabla hatujazaliwa kama watoto wa kiroho.

Akili huambatana na akili, **M&M** 88:40. Akili haikuumbwa au kutengenezwa, **M&M** 93:29. Akili zote zinajitegemea katika mazingira yale ambayo Mungu ameziweka, **M&M** 93:30. Utukufu wa Mungu ni akili, **M&M** 93:36–37. Akili tuipatayo katika maisha haya itainuka pamoja nasi katika ufufuko, **M&M** 130:18–19.

Bwana hutawala juu ya viumbe-akili-asilia vyote, **Ibr.** 3:21. Bwana alimwonyesha Ibrahimu viumbe-akili-asilia vilivyoumbwa kabla ya ulimwengu kuwako, **Ibr.** 3:22.

Alfa na Omega. *Ona pia* Yesu Kristo

Alfa ni herufi ya kwanza katika alfabeti za Kiyunani; Omega ni ya mwisho. Haya pia ni majina yaliyotolewa kwa Yesu Kristo na yanatumika kama ishara za kuonyesha kwamba Kristo ndiye mwanzo na mwisho (Ufu. 1:8; M&M 19:1).

Alichagua, Chagua, Chaguliwa (kitenzi). *Ona pia* Haki ya uamuzi; Huru, Uhuru; Ita, Itwa na Mungu, Wito

Bwana ateuapo, au kuchagua, mtu au kikundi, kwa kawaida pia Yeye huwaita kutumikia.

Chagueni hivi leo mtakayemtumikia, **Yos.** 24:15 (Alma 30:8; Musa 6:33). Nimekuchagua katika tanuru ya mateso, **Isa.** 48:10 (1 Ne. 20:10).

Waitwao ni wengi, bali wateule ni wachache, **Mt.** 22:14 (Mt. 20:16; M&M 95:5; 121:34, 40). Si ninyi mlio nichagua mimi, bali mimi niliyewachagua ninyi, **Yn.** 15:16. Mungu aliyachagua mambo mapumbavu ya dunia awaaibishe wenye hekima, **1 Kor.** 1:27. Alituchagua sisi kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, **Efe.** 1:4.

Tuko huru kuchagua uhuru na uzima wa milele au utumwa na mauti, **2 Ne.** 2:27.

Watu mashuhuri na walio wakuu walichaguliwa toka mwanzo, **M&M** 138:55–56.

Israeli alichaguliwa na Mungu, **Musa** 1:26. Ibrahimu alichaguliwa kabla hajazaliwa, **Ibr.** 3:23.

Aliye Mahali Pote. *Ona pia* Mungu, Uungu

Uwezo wa Mungu wa kuwa kila mahali kwa njia ya roho Wake (Zab. 139:7–12; M&M 88:7–13, 41).

Alma, Mwana wa Alma. *Ona pia* Alma Mzee; Amuleki; Mosia, Wana wa

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwamuzi mkuu wa kwanza na nabii katika taifa la Wanefi. Katika miaka yake ya mwanzoni yeye alitafuta kuliangamiza Kanisa (Mos. 27:8–10). Hata hivyo malaika akamtokea naye akaongolewa katika injili (Mos. 27:8–24; Alma 36:6–27). Baadaye aliiacha nafasi yake kama mwamuzi mkuu ili kuwafundisha watu (Alma 4:11–20).

Kitabu cha Alma: Kitabu kimojawapo katika Kitabu cha Mormoni, kina ufupisho wa kumbukumbu ya nabii Alma, mwana wa Alma, na mwanawe Helamani. Matukio yaliyoelezwa katika kitabu hicho yalitokea Karibia mwaka 91 hadi 52 kabla ya Kristo. Kitabu hiki kina milango 63. Mlango wa 1–4 inaelezea uasi wa wafuasi wa Nehori na Amlisi dhidi ya Wanefi. Vita vilivyotokea kama matokeo yake vilikuwa miongoni mwa vita vilivyoleta uharibifu mkubwa katika historia ya Wanefi. Mlango wa 5–16 ina historia ya safari za awali za kimisionari za Alma, ikiwa ni pamoja na mahubiri yake juu ya Mchungaji Mwema (Alma 5) na kuhubiri kwake akiwa pamoja na Amuleki katika mji wa Amoniha. Mlango wa 17–27 ina kumbukumbu ya wana wa Mosia na huduma yao miongoni mwa Walamani. Mlango wa 28–44 ina baadhi ya mahubiri muhimu zaidi ya Alma. Katika mlango wa 32 Alma analinganisha neno na mbegu; katika mlango wa 36 anasimulia mwanawe Helamani hadithi ya kuongolewa kwake. Mlango wa 39–42 anaandika maonyo ya Alma kwa mwanawe Koriantoni, ambaye amekuja kujihusisha na uzinzi; mahubiri haya muhimu yanaelezea juu ya haki, huruma, Ufufuko, na Upatanisho. Mlango wa 45–63 inaelezea vita vya Wanefi vya kipindi hicho na uhamiaji chini ya Hagothi. Viongozi maarufu kama vile Kapteni Moroni, Teankumu, na Lehi walisaidia katika kuwalinda Wanefi

kwa njia ya ujasiri wao na matendo yao katika wakati uliofaa.

Alma Mzee

Nabii Mnefi aliye katika Kitabu cha Mormoni ambaye alilianzisha kanisa katika siku za Mfalme mwovu Nuhu.

Alikuwa kuhani wa Mfalme mwovu Nuhu na wa uzao wa Nefi, **Mos.** 17:1–2. Baada ya kumsikiliza na kumwamini Abinadi aliondolewa na mfalme. Alitoroka, akajificha, na aliyaandika maneno ya Abinadi, **Mos.** 17:3–4. Alitubu na kuyafundisha maneno ya Abinadi, **Mos.** 18:1. Alibatiza katika maji ya Mormoni, **Mos.** 18:12–16. Alianzisha kanisa, **Mos.** 18:17–29. Alifika Zarahemla pamoja na watu wake, **Mos.** 24:25. Alipewa mamlaka juu ya kanisa, **Mos.** 26:8. Alihukumu na kuliongoza Kanisa, **Mos.** 26:34–39. Alimpatia mwanawe ofisi ya ukuhani mkuu, **Alma** 4:4 (Mos. 29:42; Alma 5:3).

Amalikia

Katika Kitabu cha Mormoni, ni msaliti wa Kinefi aliyejipatia uwezo miongoni mwa Walamani na akawaongoza katika vita dhidi ya Wanefi (Alma 46–51).

Amani. *Ona pia* Milenia; Msuluhishi; Pumzika

Katika maandiko, amani yaweza kumaanisha uhuru kutokana na kutokuwepo ugomvi na misukosuko au utulivu na faraja ya ndani inayoletwa na Roho Mtakatifu ambayo Mungu huwapa Watakatifu Wake walio waaminifu.

Uhuru kutokana na ugomvi na misukosuko: Avikomesha vita, **Zab.** 46:9. Wala hawatajifunza vita tena kamwe, **Isa.** 2:4.

Muishi kwa amani na watu wote; msijilipize kisasi, **Rum.** 12:18–21.

Bado kulikuwa na amani katika nchi, **4 Ne.** 1:4, 15–20.

Ikataeni vita na tangazeni amani, **M&M** 98:16. Inueni bendera ya amani, **M&M** 105:39.

Amani kutoka kwa Mungu kwa watiifu: Mwokozi ataitwa Mfalme wa Amani, **Isa.** 9:6. Hapana amani kwa waovu, **Isa.** 48:22.

Kulikuwa na jeshi la mbinguni, likimsifu Mungu na kusema, Utukufu kwa Mungu juu, na amani duniani, **Lk.** 2:13–14. Amani nawaachieni, **Yn.** 14:27. Amani ya Mungu ipitayo akili zote, **Flp.** 4:7.

Watu wa Mfalme Benjamini walipata amani katika dhamira zao, **Mos.** 4:3. Jinsi gani ilivyo mizuri juu ya milima miguu yao watangazao amani, **Mos.** 15:14–18 (Isa. 52:7). Alma alilia kwa Bwana na akapata amani, **Alma** 38:8. Roho za walio waadilifu hupokelewa katika hali ya amani, **Alma** 40:12.

Sikusema amani akilini mwako kuhusiana na jambo hili, **M&M** 6:23. Enenda katika unyenyekevu wa Roho wangu, nawe utapata amani, **M&M** 19:23. Yule afanyaye kazi za haki atapokea amani, **M&M** 59:23. Jivikeni wenyewe kwa kifungo cha hisani, ambacho ni kifungo cha ukamilifu na amani, **M&M** 88:125. Mwanangu, amani iwe moyoni mwako, **M&M** 121:7.

Nilipoona kulikuwa na amani kuu zaidi, nilitafuta baraka za mababu, **Ibr.** 1:2.

Amina. *Ona pia* Sala

Humaanisha "na iwe hivyo" au "hivyo ndivyo." Amina husemwa ili kuonyesha makubaliano na maafikiano ya moyo au ya dhati (Kum. 27:14–26) au ukweli (1 Fal. 1:36). Siku hizi mwishoni mwa sala, shuhuda, na mahubiri wale wote waliosikia sala au ujumbe husema amina ya kusikika ili kuonyesha makubaliano na maafikiano.

Katika nyakati za Agano la Kale, mtu alipaswa kusema amina wakati anapotoa kiapo (1 Nya. 16:7, 35–36; Neh. 5:12–13; 8:2–6). Kristo anaitwa "aliye Amina, aliye mwaminifu na shahidi wa kweli" (Ufu. 3:14). Amina pia ilitumika kama ishara ya agano katika Shule ya Manabii (M&M 88:133–135).

Amini, Imani. *Ona pia* Kutoamini; Tegemea; Tumaini; Yesu Kristo

Kuwa na imani au kutumaini katika

mtu fulani au kukikubali kitu fulani kuwa ni kweli. Kama itumikavyo mara kwa mara katika maandiko, imani ni matumaini na mategemeo katika Yesu Kristo ambayo humwongoza mtu katika kumtii yeye, ili apate kuolekewa katika uflame wa Mungu (M&M 20:29). Imani lazima ilenge katika Yesu Kristo ili iweze kumwongoza mtu kwenye wokovu. Watakatifu wa siku za mwisho pia wanayo imani katika Mungu Baba, Roho Mtakatifu, uwezo wa ukuhani, na vipengele vingine muhimu vya injili ya urejesho.

Imani ni pamoja na matumaini juu ya vitu visivyoonekana, lakini ni vya kweli (Ebr. 11:1; Alma 32:21; Eth. 12:6). Imani huwashwa kwa kusikia injili ifundishwayo na wahudumu walio na mamlaka waliotumwa na Mungu (Rum. 10:14–17). Miujiza haizai imani, bali imani iliyo imara huendelezwa na utiifu kwa injili ya Yesu Kristo. Kwa maneno mengine, imani huja kwa maisha ya haki (Alma 32:40–43; Eth. 12:4, 6, 12; M&M 63:9–12).

Imani ya kweli huleta miujiza, maono, ndoto, uponyaji, na vipawa vyote vya Mungu vile ambavyo Yeye huvitoa kwa Watakatifu Wake. Kwa imani mtu hupata ondoleo la dhambi na mwishowe huweza kukaa mbele za Mungu. Ukosefu wa imani humpelekea mtu katika kukata tamaa, ambako huja kwa sababu ya dhambi (Moro. 10:22).

Mwaminini Bwana Mungu wenu; waaminini manabii wake, **2 Nya.** 20:20. Daniel hakuumia katika tundu la simba kwa sababu alimwamini Mungu, **Dan.** 6:23. Mwenye haki ataishi kwa imani, **Hab.** 2:4.

Na ifanyike kwako kama ulivyoamini, **Mt.** 8:13. Imani yako imekuponya, **Mt.** 9:22 (Mk. 5:34; Lk. 7:50). Na iwe kwenu kulingana na imani yenu, **Mt.** 9:29. Kama mna imani kiasi cha punje ya haradali, hakutakuwako jambo lisilowezekana kwenu, **Mt.** 17:20 (Lk. 17:6). Na yoyote mtakayoomba katika sala, mkiamini, mtapokea, **Mt.** 21:22. Usiogope, amini tu, **Mk.** 5:36. Yote yawezekana kwake aaminiye, **Mk.** 9:23–24. Aaminiye na kubatizwa ataokolewa, **Mk.** 16:16 (2 Ne. 2:9; 3 Ne. 11:33–35). Nimekuombea wewe, ili imani yako isitindike, **Lk.** 22:32. Amwaminiye Mwana yu na uzima wa usio na mwisho, **Yn.** 3:16, 18, 36 (Yn. 5:24; M&M 10:50). Tunaamini na tuna uhakika kwamba wewe ndiwe Kristo, **Yn.** 6:69. Yeye aniaminiye mimi, ajapokufa, atakuwa anaishi, **Yn.** 11:25–26. Imani katika jina la Kristo limemtia nguvu mtu huyu, **Mdo.** 3:16. Imani huja kwa kusikia neno la Mungu, **Rum.** 10:17. Kama Kristo hakufufuka imani yenu pia ni bure, **1 Kor.** 15:14. Imani hutenda kazi kwa upendo, **Gal.** 5:6. Kwa neema mnaokolewa kwa njia ya imani, **Efe.** 2:8 (2 Ne. 25:23). Itwaeni ngao ya imani, **Efe.** 6:16 (M&M 27:17). Mwendo wangu nimeumaliza, imani nimeilinda, **2 Tim.** 4:7. Maana sisi ambao tumeamini tunaingia katika raha ile, **Ebr.** 4:3. Imani ni kuwa na matumaini ya mambo yatarajiwayo, **Ebr.** 11:1. Pasipo imani haiwezekani kumpendeza yeye, **Ebr.** 11:6. Imani, kama haina matendo, imekufa, **Yak. (Bib.)** 2:17–18, 22. Tuamini juu ya Yesu Kristo, na kupendana, **1 Yoh.** 3:23.

Nitakwenda na kufanya mambo ambayo Bwana ameniamuru, **1 Ne.** 3:7. Bwana anao uwezo kufanya mambo yote kwa ajili ya wanadamu, kama watakuwa na imani naye, **1 Ne.** 7:12. Mishale katika Liahona ilifanya kazi kulingana na imani, **1 Ne.** 16:28. Masiya hatamwangamiza yeyote yule atakayemwamini, **2 Ne.** 6:14. Tubuni, na mkabatizwe katika jina lake, mkiwa na imani kamilifu katika Yeye aliye Mtakatifu, **2 Ne.** 9:23. Wayahudi watateswa hadi watakaposhawishika kumwamini Kristo, **2 Ne.** 25:16. Kristo alitenda miujiza mikubwa miongoni mwa wanadamu kulingana na imani yao, **2 Ne.** 26:13 (Eth. 12:12; Moro. 7:27–29, 34–38). Dhambi za Enoshi zilisamehewa kwa sababu ya imani yake katika Kristo, **Eno.** 1:3–8. Wokovu hauji kwa yeyote isipokuwa kwa njia ya imani juu ya Bwana Yesu Kristo, **Mos.** 3:12. Kama mnayaamini mambo haya,

oneni kwamba mnayatenda, **Mos.** 4:10. Mioyo hubadilika kwa njia ya imani juu ya jina lake, **Mos.** 5:7. Sala za watumishi wa Bwana hujibiwa kulingana na imani yao, **Mos.** 27:14. Mwana atajitwalia juu yake dhambi zao waaminio katika jina lake, **Alma** 11:40. Tupe nguvu kulingana na imani yetu katika Kristo, **Alma** 14:26. Mlilingane jina la Mungu katika imani, **Alma** 22:16. Amebarikiwa yule aaminiye katika neno la Mungu pasipo kulazimishwa, **Alma** 32:16. Imani siyo kuwa na ufahamu kamili wa mambo, **Alma** 32:21 (Eth. 12:6). Hata ikiwa hamwezi zaidi ya kutamani kuamini, acheni tamaa hii ifanye kazi ndani yenu, **Alma** 32:27. Litakavyoanza kumea hata hivyo ndivyo mtalilisha kwa imani yenu, **Alma** 33:23 (Alma 32:28). Kulindwa kwao kulitokana na uwezo wa kimiujiza wa Mungu kwa sababu ya imani yao iliyopita kiasi, **Alma** 57:25–27. Kadiri wengi watakavyoangalia juu kwa Mwana wa Mungu kwa imani watapata kuwa hai, **Hel.** 8:15. Kama mnaamini katika jina la Kristo, mtatubu, **Hel.** 14:13. Wale waaminio katika Kristo huamini katika Baba pia, **3 Ne.** 11:35. Ninaona kwamba imani yenu inatosha kwamba ningewaponya, **3 Ne.** 17:8. Kamwe mwanadamu hajapata kuamini katika Bwana kama kaka wa Yaredi alivyofanya, **Eth.** 3:15. Imani ni mambo yanayotarajiwa na hayaonekani, **Eth.** 12:6. Wote waliofanya miujiza waliifanya kwa imani, **Eth.** 12:12–18. Kama wanayo imani nami, ndipo nitafanya mambo dhaifu kuwa imara kwao, **Eth.** 12:27–28, 37. Mormoni alifundisha juu ya imani, matumaini, na hisani, **Moro.** 7. Kila kitu kinachokushawishi kuamini katika Kristo kimeletwa kwa uwezo wa Kristo, **Moro.** 7:16–17. Kitu chochote mtakacho mwomba Baba katika jina langu, kilicho chema, katika imani mkiamini kwamba mtapata, tazama, itafanyika hivyo kwenu, **Moro.** 7:26. Walio na imani katika Kristo watashikilia kwa kila kitu kilicho chema, **Moro.** 7:28. Kama mtaomba, mkiwa na imani katika Kristo, yeye atakufunulieni ukweli, **Moro.** 10:4.

Wale waaminio katika neno la Bwana watapewa mawasiliano ya Roho, **M&M** 5:16. Pasipo imani huwezi kufanya chochote; kwa hiyo ombeni kwa imani, **M&M** 8:10. Itakubaliwa kwao kulingana na imani yao katika sala zao, **M&M** 10:47, 52. Wale waaminio katika jina la Bwana watakuwa wana wa Mungu, **M&M** 11:30 (Yn. 1:12). Wanadamu wote lazima wastahimili katika imani katika jina lake hadi mwisho, **M&M** 20:25, 29. Roho atatolewa kwenu kwa sala ya imani, **M&M** 42:14. Kwa wengine imetolewa kuamini juu ya maneno ya wengine, **M&M** 46:14. Ishara huwafuata wale waaminio, **M&M** 58:64 (M&M 63:7–12). Imani haiji kwa ishara, bali ishara huwafuata wale waaminio, **M&M** 63:9–12. Wazazi watawafundisha watoto wao imani katika Kristo, **M&M** 68:25. Tafuteni maarifa, hata kwa kujifunza na pia kwa imani, **M&M** 88:118.

Wale wenye kuamini, kutubu, na wakabatizwa watampokea Roho Mtakatifu, **Musa** 6:52. Imani katika Bwana Yesu Kristo ndiyo kanuni ya kwanza ya injili, **M ya I** 1:4.

Amlisi, Waamlisi

Mtu aliye katika Kitabu cha Mormoni ambaye aliongoza kikundi cha Wanefi waliotaka kuwa na mfalme wakati wa utawala wa waamuzi. Wanefi hawa, waliojiita Waamlisi, walikuwa wakimwasi Mungu wazi wazi, kwa sababu hiyo walilaaniwa (Alma 2–3).

Amoni, Mwana wa Mosia. *Ona pia* Mosia, Mwana wa Benjamini; Mosia, Wana wa; Waanti-Nefi-Lehi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana wa Mfalme Mosia. Amoni aliyefanya kazi kama mmisionari ambaye bidii ya jitihada zake zilisaidia kuziongoa roho nyingi kwa Kristo.

Alikuwa mtu asiyeamini na aliyetafuta kuliangamiza Kanisa, **Mos.** 27:8–10, 34. Malaika alimtokea yeye na wenzi wake, **Mos.** 27:11. Akatubu na kuanza kulihubiri neno la Mungu, **Mos.** 27:32–28:8. Alikataa kuwa mfalme na badala

yake alikwenda katika nchi ya Walamani kuhubiri neno la Mungu, **Alma** 17:6–9. Alifunga na kusali kwa ajili ya kupata mwongozo, **Alma** 17:8–11. Alichukuliwa akiwa amefungwa hadi kwa Mfalme Lamoni, **Alma** 17:20–21. Aliokoa kundi la mifugo ya Lamoni, **Alma** 17:26–39. Alimhubiria Lamoni, **Alma** 18:1–19:13. Alimshukuru Mungu na akazidiwa na shangwe, **Alma** 19:14. Aliowaongoa kamwe hawakuanguka, **Alma** 23:6. Alijawa shangwe kuwa chombo mikononi mwa Mungu cha kuwaleta maelfu kwenye ukweli, **Alma** 26:1–8 (Alma 26). Aliwaongoza watu Anti-Nefi-Lehi kwenye usalama, **Alma** 27. Alijisikia shangwe kuu katika kukutana na Alma, **Alma** 27:16–18.

Amoni, wa Uzao wa Zarahemla. *Ona pia* Limhi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mtu jasiri na mwenye nguvu aliyeongoza msafara maalumu kutoka Zarahemla kwenda nchi ya Lehi-Nefi (Mos. 7:1–16). Alionyeshwa maandiko ya kale na akaelezea kuwa mwonaji ni mtu wa namna gani (Mos. 8:5–18). Na baadaye alisaidia kuwaweka huru mfalme Limhi na watu wake kutoka kwa Walamani na kuwarejesha tena Zarahemla (Mos. 22).

Amosi

Nabii wa Agano la Kale aliyetoa unabii karibia mwaka 792 hadi 740 K.K. Katika siku za Uzia, mfalme wa Yuda, na Yeroboamu, mfalme wa Israeli.

Kitabu cha Amosi: Ni kitabu katika Agano la Kale. Unabii mwingi wa Amosi unawaonya Waisraeli na mataifa ya jirani yake kuigeukia haki.

Mlango wa 1–5 inaiita Israeli na mataifa ya jirani yake kwenye toba. Mlango wa 3 unaeleza kwamba Bwana huwafunulia siri Zake manabii na kwamba kwa sababu ya dhambi, Israeli ataangamizwa na adui. Mlango wa 6–8 inatoa unabii juu ya anguko la Israeli miaka mingi kabla ya uvamizi wa Waashuru. Mlango wa 9 unatoa unabii kwamba Israeli watarejeshwa katika nchi yao yenyewe.

Amri Kumi. *Ona pia* Amri za Mungu; Musa

Sheria kumi zilizotolewa na Mungu kupitia nabii Musa ili kudhibiti tabia za kimwili.

Jina la Kiebrania kwa amri hizi ni "Maneno Kumi." Pia zinaitwa Agano (Kum. 9:9) au ushuhuda (Ku. 25:21; 32:15). Namna Mungu alivyotoa Amri Kumi kwa Musa, na kupitia yeye kwenda kwao Waisraeli, inaelezwa katika Ku. 19:9–20:23; 32:15–19; 34:1. Amri hizi zilikuwa zimechongwa juu ya mabamba mbili ya mawe, ambazo ziliwekwa katika Sanduku; kwa sababu hiyo Sanduku hilo liliitwa Sanduku la Agano (Hes. 10:33). Bwana, akinukuu kutoka Kum. 6:4–5 na Law. 19:18 amezifupisha Amri Kumi hizi katika "amri kuu mbili" (Mt. 22:37–39).

Amri kumi hizi zimerudiwa tena katika ufunuo wa siku za mwisho (TJS, Ku. 34:1–2, 14 [Kiambatisho]; Mos. 12:32–37; 13:12–24; M&M 42:18–28; 59:5–13).

Amri za Mungu. *Ona pia* Amri Kumi; Dhambi; Mtiifu, Tii, Utii; Neno la Mungu; Sheria

Sheria na matakwa ambayo Mungu huyatoa kwa wanadamu, kwa mtu binafsi au kwa kikundi. Kushika amri za Mungu kutamletea baraka za Bwana na kwa aliye mtiifu (M&M 130:21).

Nuhu alifanya kulingana na yale yote ambayo Mungu alimwamuru, **Mwa.** 6:22. Enendeni katika sheria zangu, na kushika amri zangu, **Law.** 26:3. Shika amri zangu, na ukaishi, **Mit.** 4:4 (Mit. 7:2).

Kama mnanipenda, mtazishika amri zangu, **Yn.** 14:15 (M&M 42:29). Lolote tuombalo, twalipokea kwake, kwa sababu tunazishika amri zake, **1 Yoh.** 3:22. Amri zake si nzito, **1 Yoh.** 5:3.

Uwe imara katika kushika amri, **1 Ne.** 2:10. Bwana hatoi amri isipokuwa amewatayarishia njia, **1 Ne.** 3:7. Lazima nifanye kulingana na amri kali za Mungu, **Yak. (KM)** 2:10. Ilimradi mtazishika amri zangu, mtastawi katika nchi, **Yar.**

1:9 (Alma 9:13; 50:20). Jifunze katika ujana wako kuzishika amri za Mungu, **Alma** 37:35.

Amri hizi ni zangu, **M&M** 1:24. Zitafuteni amri hizi, **M&M** 1:37. Wale wasiozishika amri hawawezi kuokolewa, **M&M** 18:46 (M&M 25:15; 56:2). Amri zangu ni za kiroho; siyo za asili au za kimwili, **M&M** 29:35. Amri hutolewa ili tupate kufahamu mapenzi ya Bwana, **M&M** 82:8.

Sielewi, isipokuwa Bwana ameniamuru, **Musa** 5:6. Bwana atawapima wanadamu ili kuona kama watafanya yale yote atakayo waamuru, **Ibr.** 3:25.

Amua, Hukumu. *Ona pia* Hukumu ya mwisho; Shutuma, Shutumu; Yesu Kristo—Mwamuzi

Kupima tabia kwa kuilinganisha na kanuni za injili; kuamua; kutambua mema na maovu.

Musa aliketi ili awahukumu watu, **Ku.** 18:13. Kwa haki utamhukumu jirani yako, **Law.** 19:15.

Msihukumu, nanyi msije mkahukumiwa, **Mt.** 7:1 (TJS, Mt. 7:1–2; Lk. 6:37; 3 Ne. 14:1). Kadiri wengi walivyotenda dhambi katika sheria, watahukumiwa kwa sheria, **Rum.** 2:12. Watakatifu watauhukumu ulimwengu, **1 Kor.** 6:2–3.

Mwana wa Mungu asiye na mwisho alihukumiwa na ulimwengu, **1 Ne.** 11:32. Mitume Kumi na Wawili wa Mwanakondoo watayahukumu makabila kumi na mawili ya Israeli, **1 Ne.** 12:9 (M&M 29:12). Mauti, jehanamu, ibilisi, na wale wote walioshikiliwa hao lazima watahukumiwa, **2 Ne.** 28:23 (1 Ne. 15:33). Kama utamhukumu mtu akuombaye msaada wa kitu, laana yako itakuwa nyingi kiasi gani kwa kumnyima hicho kitu chako, **Mos.** 4:22. Wanadamu watahukumiwa kulingana na matendo yao, **Alma** 41:3. Hukumu kwa haki, nawe utarejeshewa haki tena, **Alma** 41:14. Ulimwengu utahukumiwa na vitabu vitakavyoandikwa, **3 Ne.** 27:23–26 (Ufu. 20:12). Mabaki la watu hawa watahukumiwa na wale kumi na wawili ambao Yesu aliwachagua katika nchi hii, **Morm.** 3:18–20. Mormoni alielezea jinsi ya kuhukumu kati ya mema na maovu, **Moro.** 7:14–18.

Weka imani yako katika yule Roho aongozaye katika kuhukumu kwa haki, **M&M** 11:12. Mnapaswa kusema mioyoni mwenu—Mungu na ahukumu kati yangu mimi na wewe, **M&M** 64:11. Kanisa la Bwana litayahukumu mataifa, **M&M** 64:37–38. Mwana alizitembelea roho zilizokuwa kifungoni ili zipate kuhukumiwa kulingana na mwanadamu katika mwili, **M&M** 76:73 (1 Pet. 4:6). Askofu atakuwa mwamuzi wa wote, **M&M** 107:72–74. Bwana atawahukumu watu wote kulingana na matendo yao, kulingana na tamaa za mioyo yao, **M&M** 137:9.

Amuleki. *Ona pia* Alma, Mwana wa Alma

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mmisionari mwenza wa Alma, mwana wa Alma.

Alitembelewa na malaika, **Alma** 8:20; 10:7. Alimkaribisha Alma nyumbani mwake, **Alma** 8:21–27. Alihubiri kwa nguvu kwa watu wa Amoniha, **Alma** 8:29–32; 10:1–11. Alikuwa wa uzao wa Nefi, Lehi, na Manase, **Alma** 10:2–3. Alishuhudia juu ya ukweli, **Alma** 10:4–11. Aliwasihi watu watubu na akakataliwa, **Alma** 10:12–32. Alipambana na Zezromu, **Alma** 11:20–40. Alifundisha juu ya ufufuko, hukumu, na urejesho, **Alma** 11:41–45. Alitaka kukomesha mauaji ya waumini, **Alma** 14:9–10. Alifungwa gerezani pamoja na Alma, **Alma** 14:14–23. Alivunja kamba za gereza na kuwa huru kwa njia ya imani, **Alma** 14:24–29. Alishuhudia juu ya Upatanisho, neema, na haki, **Alma** 34:8–16. Alifundisha juu ya sala, **Alma** 34:17–28. Aliwahimiza watu wasiahirishe toba, **Alma** 34:30–41. Imani ya Alma na Amuleki ilisababisha kuta za gereza kuanguka, **Eth.** 12:13.

Ana

Katika Agano Jipya, ni nabii mwanamke wa kabila la Asheri. Katika

wakati wa kuzaliwa kwa Yesu, mwanamke huyu alikuwa mzee na mjane. Alimwona mtoto mchanga Yesu wakati wa kutolewa Kwake hekaluni na kutambuliwa Kwake kama ni Mkombozi (Lk. 2:36–38).

Anania wa Dameski. *Ona pia* Paulo

Mwanafunzi Mkristo wa Dameski aliyembatiza Paulo (Mdo. 9:10–18; 22:12).

Anania wa Yerusalemu

Katika Agano Jipya, yeye na mkewe, Safira, walimdanganya Bwana kwa kuzuia sehemu ya fedha ambayo waliiweka wakfu kwa Bwana. Wakati Petro alipowauliza, wote wawili walianguka chini na wakafa (Mdo. 5:1–11).

Anasi. *Ona pia* Kayafa

Katika Agano Jipya, ni mtu aliyekuwa na uwezo mkuu katika Sanhedrini. Yesu, alipokamatwa, kwanza aliletwa kwake (Yn. 18:13); yeye pia alikuwa mstari wa mbele katika kuwashtaki mitume (Mdo. 4:3–6).

Andrea

Katika Agano Jipya, ni kaka wa Simoni Petro na ni mmoja wa Mitume Kumi na Wawili aliyeitwa na Yesu Kristo wakati wa huduma Yake hapa duniani (Mt. 4:18–19; Mk. 1:16–18, 29).

Anguko la Adamu na Hawa. *Ona pia* Adamu; Hali ya Kufa, enye Kufa; Hawa; Komboa, Kombolewa, Ukombozi; Lipia dhambi, Upatanisho; Mauti ya Kimwili; Mauti ya Kiroho; Mpango wa Ukombozi; Mwanadamu wa Tabia ya Asili; Yesu Kristo

Njia ambayo kwayo mwanadamu akawa na mwili wenye kufa hapa duniani. Wakati Adamu na Hawa walipokula tunda lililokatazwa, wakawa wenye mwili wenye kufa, ambako, ni kujiweka chini ya dhambi na mauti. Adamu akawa "mwenye mwili" wa kwanza juu ya dunia (Musa 3:7). Ufunuo wa siku za mwisho unaweka wazi kwamba Anguko ni baraka na kwamba Adamu na Hawa yapaswa waheshimiwe kama wazazi wa kwanza wa wanadamu wote.

Anguko lilikuwa ni hatua muhimu katika makuzi ya mwanadamu. Kwa sababu Mungu alijua kwamba Anguko lingetokea, alipanga katika maisha kabla ya kuzaliwa kuwepo kwa Mwokozi. Yesu Kristo alikuja wakati wa meridiani ili kulipia kosa la Anguko la Adamu na pia kwa ajili ya dhambi za mtu binafsi kwa sharti la toba ya mtu.

Siku utakapokula matunda yake hakika utakufa, **Mwa.** 2:17 (Musa 3:17). Alitwaa katika matunda yake, na akala, **Mwa.** 3:6 (Musa 4:12).

Kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuhishwa, **1 Kor.** 15:22.

Wanadamu wote walikuwa katika hali ya kupotea na katika hali ya kuanguka, **1 Ne.** 10:6. Njia imetayarishwa kutoka anguko la mwanadamu, **2 Ne.** 2:4. Baada ya Adamu na Hawa kula tunda lililokatazwa, walifukuzwa kutoka Bustani ya Edeni, **2 Ne.** 2:19. Adamu alianguka ili wanadamu wapate kuwa, **2 Ne.** 2:15–26. Mwanadamu wa asili ni adui kwa Mungu, na amekuwa hivyo tangu anguko la Adamu, **Mos.** 3:19. Haruni alimfundisha baba yake Lamoni juu ya Anguko, **Alma** 22:12–14. Palilazimika kufanyika upatanisho au vinginevyo wanadamu wote wangeanguka na kupotea, **Alma** 34:9. Wazazi wetu wa kwanza walikatiliwa mbali kimwili na kiroho kutoka mbele za Bwana, **Alma** 42:2–15 (Hel. 14:16). Kwa sababu ya Anguko maumbile yetu yamekuwa maovu, **Eth.** 3:2.

Kwa sababu ya uvunjaji wa sheria hizi takatifu mwanadamu akawa mtu aliyeanguka, **M&M** 20:20 (M&M 29:34–44).

Kwa vile wewe umeanguka nawe utapata kukombolewa, **Musa** 5:9–12. Kwa sababu ya uvunjaji wa sheria likaja Anguko, **Musa** 6:59. Wanadamu wataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao wenyewe, **M ya I** 1:2.

Apa. *Ona* Kiapo; Kukufuru, Kufuru; Lugha chafu

Apokalisi. *Ona pia* Ufunuo wa Yohana

Kitabu cha Ufunuo, kitabu cha mwisho katika Agano Jipya; linaweza pia kumaanisha ufunuo wowote wa kusifika; linatoka katika neno la Kiyunani "funua" au "fichua."

Apokrifa. *Ona pia* Biblia; Maandiko

Vitabu vitakatifu vya watu wa Kiyahudi ambavyo havikujumuishwa katika Biblia ya Waebrania lakini vimewekwa katika Biblia za baadhi ya makanisa ya Kikristo. Vitabu hivi daima ni vya muhimu katika kuunganisha Agano la Kale na Jipya na vinachukuliwa katika kanisa kama vitabu vyenye manufaa.

Apokrifa kwa kiasi kikubwa vimetafsiriwa kwa usahihi lakini kinanyongeza na mabaliko yasiyo sahihi, **M&M** 91:1–3. Apokrifa zaweza kuwafaa wale wenye kuongozwa na Roho, **M&M** 91:4–6.

Asa

Katika Agano la Kale, ni mfalme wa tatu wa Yuda. Maandiko yameandikwa ya kuwa "moyo wake ulikuwa mkamilifu kwa Bwana siku zake zote" (1 Fal. 15:14). Wakati wa utawala wake aliliunda jeshi imara, na akaweka huru ufalme wake toka kwenye kongwa za Ethiopia, akawaondoa miungu wa uongo, na akawaalika watu kufanya agano la kumtafuta Yehova (1 Fal. 15–16; 2 Nya. 14–16). Hata hiyo, wakati alipokuwa mgonjwa wa miguu yake, hakumwomba Bwana msaada naye akafa (1 Fal. 15:23–24; 2 Nya. 16:12–13).

Asheri. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Yakobo na Zilpa, mjakazi wa Lea (Mwa. 30:12–13).

Kabila la Asheri: Yakobo akambariki Asheri (Mwa. 49:20), na Musa akawabariki wazao wa Asheri (Kum. 33:1, 24–29). Wazao hawa waliitwa "watu hodari wa vita" (1 Nya. 7:40).

Ashuru

Ufalme wa kale ambao, pamoja na mpinzani wake Babiloni, walitawala sehemu kubwa ya mataifa ya zamani ya Shamu na Palestina karibu kipindi chote cha nyakati za Agano la Kale. Ingawa Waashuru walikuwa na nguvu kubwa katikati ya karne ya 12 K.K. hadi karibu mwishoni mwa karne ya 7 K.K., kamwe hawakuweza kujenga muundo imara wa kisiasa. Walitawala kwa vitisho, wakiwasaga maadui zao kwa moto na upanga au kwa kuwadhoofisha kwa kuwahamisha sehemu kubwa ya idadi ya watu kwenda sehemu nyingine ya ufalme wao. Watu wale ambao waliwekwa chini ya utawala wa Washuru mara kwa mara walipigana dhidi ya ile milki. (Ona 2 Fal. 18–19; 2 Nya. 32; Isa. 7:17–20; 10; 19; 37.)

Asiye na Hatia, Hali ya Kutojua

Kuwa bila lawama au bila dhambi.

Kabla ya anguko, Adamu na Hawa walikuwa katika hali ya kutojua, **2 Ne.** 2:23. Damu ya mtu asiye na hatia itasimama kama ushahidi, **Alma** 14:11.

Kila roho ya mwanadamu ilikuwa haina hatia mwanzoni, **M&M** 93:38. Watu wasio na hatia wasihukumiwe pamoja na wasio na haki, **M&M** 104:7. Joseph na Hyrum Smith walikuwa hawana hatia ya kosa lolote la jinai, **M&M** 135:6–7.

Watoto ni wazima tangu kuwekwa kwa msingi wa dunia, **Musa** 6:54.

Askofu. *Ona pia* Ukuhani wa Haruni

Humaanisha "msimamizi," ni ofisi au nafasi yenye madaraka. Askofu ni ofisi iliyotawazwa katika Ukuhani wa Haruni (M&M 20:67; 107:87–88), na askofu ni mwamuzi wa wote katika Israeli (M&M 107:72, 74).

Roho Mtakatifu amewafanya ninyi kuwa waangalizi, **Mdo.** 20:28. Sifa za kuwa maaskofu zawekwa, **1 Tim.** 3:1–7 (Tit. 1:7).

Askofu atatawazwa, **M&M** 20:67. Edward Partridge atahudumu kama askofu kwa Kanisa, **M&M** 41:9. Askofu atatambua vipawa vya kiroho, **M&M** 46:27, 29. Kuhani mkuu anaweza kuzitenda kazi katika ofisi ya askofu, **M&M** 68:14, 19 (M&M 107:17). Askofu huteuliwa na Bwana, **M&M** 72. Askofu atawaangalia maskini, **M&M** 84:112. Askofu atasimamia mambo yote ya kimwili, **M&M** 107:68. Askofu ndiye rais wa Ukuhani wa Haruni, **M&M** 107:87–88.

Askofu Kiongozi

Kiongozi Mkuu katika Kanisa. Anao wajibu mkuu juu ya mambo ya ustawi wa Kanisa (M&M 107:68). Askofu Kiongozi na washauri wake, ambao pia ni Viongozi Wakuu, huongoza juu ya Ukuhani wa Haruni wa Kanisa (M&M 68:16–17; 107:76, 87–88).

Edward Partridge atawazwa kuwa askofu, **M&M** 41:9. Maaskofu wataitwa na kutegwa rasmi na Urais wa Kwanza, **M&M** 68:14–15. Wazawa halisi wa Haruni, walio wazaliwa wa kwanza, wanayo haki ya kuongoza kama wataitwa, kutengwa rasmi, na kutawazwa na Urais wa Kwanza, **M&M** 68:16, 18–20. Aweza kushtakiwa tu mbele ya Urais wa Kwanza, **M&M** 68:22–24 (M&M 107:82).

Ayubu

Katika Agano la Kale, ni mtu mwadilifu aliyeteseka kwa mateso makubwa lakini alibakia mwaminifu katika imani yake kwa Mungu. Historia yake inasimuliwa katika kitabu cha Ayubu.

Kitabu cha Ayubu: Ingawa kitabu hiki ni juu ya mateso ya Ayubu, hakijibu moja kwa moja swali la kwa nini Ayubu (au mtu mwingine yeyote) anaweza kuteseka kwa maumivu na kupoteza familia yake na mali. Kitabu kinafafanua kwamba kupata mateso maana yake siyo lazima kwamba mtu huyo ametenda dhambi. Bwana anaweza kutumia mateso kwa ajili ya kutupa uzoefu, kutufundisha nidhamu, na kufundisha vile vile kama adhabu (M&M 122).

Kitabu hiki chaweza kugawanywa katika sehemu nne. Mlango wa 1–2 ni utangulizi wa hadithi hii. Mlango wa 3–31 inaelezea mfuatano wa majadiliano kati ya Ayubu na marafiki zake watatu. Mlango wa 32–37 ina mahubiri ya Elihu, rafiki wa nne, ambaye anamshutumu Ayubu kwa sababu nyingine tofauti na zile za marafiki watatu wa kwanza. Mlango wa 38–42 inahitimisha kitabu kwa uhakikisho kwa Ayubu kwamba mwenendo wake wa maisha ulikuwa mwema tangu mwanzo.

Kitabu cha Ayubu hufundisha kwamba kama mtu anao ufahamu sahihi juu ya Mungu na anaishi maisha ambayo yanakubalika kwa Mungu, itakuwa bora kwake kustahimili majaribu yanayokuja juu yake. Imani isiyotindika ya Ayubu inayoonekana wazi katika matamko kama "Japokuwa ataniua, bado nitamtumaini yeye." (Ayu. 13:15). Ayubu pia ametajwa katika Ezekieli 14:14; Yak. (Bib.) 5:11; Mafundisho na Maagano 121:10.

Baali. *Ona pia* Kuabudu sanamu

Ni mungu-jua mwanamume aliyekuwa akiabudiwa kwa kawaida katika Fonisia (1 Fal. 16:31) lakini pia aliabudiwa katika njia tofauti katika sehemu mbali mbali na Wamoabii kama Baali-Peori (Hes. 25:1–3), huko Shekemu kama Baali-bethiri (Amu. 8:33; 9:4), huko Ekroni kama Baali-Zebubu (2 Fal. 1:2). Baali aweza kuwa huyo huyo Beli wa Babilonia na Zayo wa Uyunani. Neno Baali linaelezea uhusiano kati ya bwana na mtumwa wake. Alama ya kawaida ya Baali ilikuwa ng'ombe dume. Ashtorethi alikuwa mungu mwanamke ambaye kwa kawaida aliabudiwa pamoja na Baali.

Baali nyakati zingine liliunganishwa na jina jingine au neno ili kuonyesha uhusiano na Baali, kama vile mahali alipokuwa akiabudiwa, au mtu aliyefikiriwa kuwa na tabia kama za Baali.

Baadaye, kwa sababu Baali lilikuja kuwa na maana ovu sana, neno Boshethi lilichukua mahali pake katika majina yale yaliyounganishwa nayo. Boshethi maana yake "aibu."

Baba, Mwili wenye kufa. *Ona pia* Baraka za Kipatriaki; Familia; Kipatriaki, Patriaki; Wazazi

Cheo kitakatifu kinachomhusu mwanamume ambaye amezaa au amepanga mtoto kisheria.

Waheshimu baba yako na mama yako, **Ku.** 20:12 (Kum. 5:16; Mt. 19:19; Mos. 13:20). Baba humrudi mwanawe ampendaye, **Mit.** 3:12.

Akina baba, msiwachokoze watoto wenu ili wakasirike, **Efe.** 6:1–4.

Nilifundishwa katika ujuzi wote wa baba yangu, **1 Ne.** 1:1. Baba yangu alikuwa mtu wa haki—kwani alinifundisha, **Eno.** 1:1. Alma alisali kwa ajili ya mwanawe, **Mos.** 27:14. Alma alitoa amri kwa wanawe, **Alma** 36–42. Helamani aliwapa wanawe majina ya mababu zao, **Hel.** 5:5–12. Mormoni daima alikuwa akiwakumbuka wanawe katika sala zake, **Moro.** 8:2–3.

Mambo makuu yaweza kuhitajika kutoka mikononi mwa akina baba, **M&M** 29:48. Kila mwanamume analazimika kuitunza familia yake yeye mwenyewe, **M&M** 75:28.

Aliniamuru niende kwa baba yangu, **JS—H** 1:49.

Baba wa Mbinguni. *Ona pia* Mungu, Uungu

Baba wa roho za wanadamu wote (Zab. 82:6; Mt. 5:48; Yn. 10:34; Rum. 8:16–17; Gal. 4:7; 1 Yoh. 3:2). Yesu ndiye Mwanawe wa Pekee katika mwili. Mwanadamu ameamriwa kutii na kutoa heshima kwa Baba na kumwomba Yeye katika jina la Yesu.

Kama mkiwasamehe watu, Baba yenu wa Mbinguni pia atawasamehe ninyi, **Mt.** 6:14 (Mt. 18:35; 3 Ne. 13:14). Baba yenu wa Mbinguni anajua ya kuwa mnahitaji haya yote, **Mt.** 6:26–33 (3 Ne. 13:26–33). Je, Baba wa Mbinguni hatazidi sana kuwapa Roho Mtakatifu hao Wamwombao, **Lk.** 11:11–13. Atukuzwe Mungu, na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo, **Efe.** 1:3.

Mnadaiwa milele na Baba yenu wa Mbinguni, **Mos.** 2:34. Kristo alilitukuza jina la Baba, **Eth.** 12:8.

Watakatifu wanapaswa kutoa ushuhuda wa mateso yao kabla Baba hajaja kutoka katika mahali pa maficho yake, **M&M** 123:1–3, 6.

Tulipata baraka kuu na tukufu kutoka kwa Baba yetu wa Mbinguni, **JS—H** 1:73.

Baba wa Milele. *Ona* Baba wa Mbinguni; Mungu, Uungu

Babeli, Babilonia. *Ona pia* Nebukadneza; Ulimwengu

Mji mkuu wa Babilonia.

Babeli ulianzishwa na Nimrodi na ulikuwa mmoja kati ya miji ya zamani zaidi katika nchi ya Mesopotania, au Shinari (Mwa. 10:8–10). Bwana aliivuruga lugha wakati watu walipokuwa wakijenga Mnara wa Babeli (Mwa. 11:1–9; Eth. 1:3–5, 33–35). Babilonia baadaye ukaja kuwa mji mkuu wa Nebukadneza. Alijenga mji mkubwa kupita kiasi ambao magofu yake bado yapo. Babilonia ukawa mji mwovu sana na toka hapo umekuwa ishara ya uovu wa ulimwengu.

Kimbieni kutoka kati ya Babilonia, **Yer.** 51:6.

Babilonia itaanzishwa na itaanguka, **Ufu.** 17–18.

Babilonia itaangamizwa, **2 Ne.** 25:15.

Babilonia itaanguka, **M&M** 1:16. Sitamwacha yeyote atakayebaki katika Babilonia, **M&M** 64:24. Ondokeni kutoka Babilonia, **M&M** 133:5, 7, 14.

Bahari ya Chumvi

Bahari ya chumvi iliyo mwisho upande wa kusini wa Bonde la Yordani. Pia ilijulikana kama Bahari ya chumvi. Eneo lake lapata karibu futi 1300 (mita 395) chini ya usawa wa Bahari

ya Mediteraniani. Miji ya Sodoma, Gomora, na Soari au Bela ilikuwa karibu na pwani yake (Mwa. 14:2–3).

Katika kutimia kwa unabii na kama moja ya ishara za Ujio wa Pili wa Mwokozi, maji haya ya Bahari ya Chumvi yataponywa, na maisha yatashamiri huko (Eze. 47:8–9).

Bahari ya Shamu. *Ona pia* Musa

Mkusanyiko wa maji kati ya Misri na Arabia. Ghuba zake mbili upande wa kaskazini zinafanya ufukwe wa Rasi ya Sinai. Kimiujiza Bwana aliigawanya Bahari ya Shamu ili Waisraeli chini ya uongozi wa Musa waweze kupita katika nchi kavu (Ku. 14:13–31; Ebr. 11:29). Kugawanywa kwa Bahari na Musa kunathibitishwa katika ufunuo wa siku za mwisho (1 Ne. 4:2; Hel. 8:11; M&M 8:3; Musa 1:25).

Bahati Nasibu

Njia ya kuchagua au kuondosha uchaguzi kadhaa wa chaguo, mara kwa mara unafanywa kwa kuchagua kipande cha karatasi au kipande cha ubao kutoka katika vipande vingi. Hii huitwa kupiga kura.

Waligawa mavazi yake, wakipiga kura, **Mt.** 27:35 (Zab. 22:18; Mk. 15:24; Lk. 23:34; Yn. 19:24). Walipiga kura zao, na kura ikamwangukia Mathiya, **Mdo.** 1:23–26.

Tulipiga kura—nani kati yetu ataingia katika nyumba ya Labani, **1 Ne.** 3:11.

Balaamu

Nabii katika Agano la Kale ambaye alitaka kuilaani Israeli kwa ajili ya fedha. Aliamriwa na Bwana asiilaani Israeli (Hes. 22–24).

Punda wa Balaamu alikataa kwenda mbele kwa sababu malaika alisimama katika njia yake, **Hes.** 22:22–35.

Baraba

Jina la mtu aliyeachiwa huru badala ya Yesu wakati ule wa Kusulubiwa. Baraba alikuwa mwasi, mwuaji, na mnyang'anyi (Mt. 27:16–26; Mk. 15:6–15; Lk. 23:18–25; Yn. 18:40).

Baraka, Bariki, Barikiwa. *Ona pia* Baraka za Kipatriaki; Huduma kwa Wagonjwa; Neema; Sheria; Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani

Kutunuku upendeleo wa kiungu juu ya mtu fulani. Kitu chochote kichangiacho kwenye furaha ya kweli, hali njema, au ustawi hiyo ni baraka.

Baraka zote zimewekwa juu ya sheria ya milele (M&M 130:20–21). Kwa sababu Mungu anataka watoto Wake wapate furaha katika maisha (2 Ne. 2:25), huwapatia baraka kama matokeo ya utiifu wao katika amri Zake (M&M 82:10), katika kujibu sala au agizo la ukuhani (M&M 19:38; 107:65–67), au kwa njia ya neema Zake (2 Ne. 25:23).

Orodha inayofahamika vyema na taarifa juu ya hali ya kuwa na heri ni Mahubiri ya Heri (Mt. 5:1–12; 3 Ne. 12:1–12).

Kwa ujumla: Nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, **Mwa.** 12:2–3 (1 Ne. 15:18; Ibr. 2:9–11). Baraka humkalia mwenye haki kichwani, **Mit.** 10:6. Mtu mwaminifu atakuwa na baraka tele, **Mit.** 28:20. Bwana atayafungua madirisha ya mbinguni na kuwamwagieni baraka, **Mal.** 3:10 (3 Ne. 24:10).

Mahubiri ya Heri yanaahidi baraka, **Mt.** 5:1–12 (3 Ne. 12:1–12). Heri walioalikwa kwenye karamu ya harusi ya Mwanakondoo, **Ufu.** 19:9.

Yule aliye mwenye haki hupendwa na Mungu, **1 Ne.** 17:35 (Mos. 10:13). Kama mtamsikiliza, nitawaachia baraka, **2 Ne.** 1:28. Ninawapatia baraka kama ile, **2 Ne.** 4:9. Yeye papo hapo atawabariki, **Mos.** 2:24. Bwana huwabariki na kuwafanikisha wale ambao huweka imani yao kwake, **Hel.** 12:1.

Saidia kuianzisha kazi yangu, nawe utabarikiwa, **M&M** 6:9. Sali daima, na baraka zako zitakuwa kubwa, **M&M** 19:38. Ukabatizwe, nawe utampokea

Roho wangu na baraka kuu namna ambayo kamwe hujapata kuijua, **M&M** 39:10. Baada ya taabu nyingi, huja baraka, **M&M** 58:4. Wanadamu wasipotii; naifuta nao hawapokei hiyo baraka, **M&M** 58:32. Ninyi hamjajua ni baraka kubwa jinsi gani ambayo Baba ameitayarisha kwa ajili yenu, **M&M** 78:17. Kutoka ukuhani mkuu huja huduma za ibada na baraka juu ya kanisa, **M&M** 107:65–67. Kuna sheria ambayo juu yake baraka zote hutolewa, **M&M** 130:20. Wote watakaopata baraka mikononi mwangu watatii sheria, **M&M** 132:5. Baraka zimewekwa kwa ajili ya wale wenye kumpenda Bwana, **M&M** 138:52.

Ibrahimu alijaribu kupata baraka za mababu na haki ya kusimamia baraka hiyo, **Ibr.** 1:2.

Baraka za watoto: Aliwanyanyua mikononi mwake na akawabariki, **Mk.** 10:16.

Aliwachukua watoto wao wadogo mmoja mmoja, na akawabariki, **3 Ne.** 17:21.

Wazee watawabariki watoto katika jina la Yesu Kristo, **M&M** 20:70.

Baraka za Kipatriaki. *Ona pia* Baba, Mwili wenye kufa; Kipatriaki, Patriaki; Mwinjilisti

Baraka zitolewazo kwa waumini wa Kanisa wenye kustahili na mapatriaki waliotawazwa. Baraka za kipatriaki zina ushauri wa Bwana kwa yule mtu anayepokea baraka na kutamka kabila la mtu huyo katika nyumba ya Israeli. Akina baba wanaweza kutoa baraka maalumu kama mapatriaki wa familia zao, lakini baraka za aina hiyo haziandikwi au haziwekwi na Kanisa.

Israeli alinyoosha mkono wa kuume na kuuweka juu ya kichwa cha Efraimu, **Mwa.** 48:14. Yakobo aliwabariki wanawe na uzao wao, **Mwa.** 49.

Lehi alibariki uzao wake, **2 Ne.** 4:3–11.

Baraza Kuu

Baraza la makuhani wakuu kumi na wawili.

Katika siku za mwanzoni za urejesho wa Kanisa, neno baraza kuu lilitumika kwa makundi mawili tofauti ya utawala: (1) Akidi ya Mitume Kumi na Wawili wa Kanisa (M&M 107:33, 38) na (2) baraza kuu lenye kuhudumu ndani ya kila kigingi (M&M 102; 107:36).

Baraza la Mitume Kumi na Wawili. *Ona* Mtume

Baraza Mbinguni. *Ona pia* Maisha kabla ya kuzaliwa; Mpango wa Ukombozi; Vita Mbinguni

Tukio katika maisha yetu kabla ya kuzaliwa hapa duniani wakati Baba alipotoa mpango Wake kwa watoto Wake wa kiroho ambao wangekuja katika dunia hii.

Na wana wa Mungu walipopiga kelele kwa shangwe, **Ayu.** 38:4–7. Nitakiinua kiti changu cha enzi juu ya nyota za Mungu, **Isa.** 14:12–13.

Palikuwa na vita mbinguni, **Ufu.** 12:7–11.

Kabla hawajazaliwa, walipata masomo yao ya awali katika ulimwengu wa Roho, **M&M** 138:56.

Shetani aliasi katika maisha ya kabla ya kuzaliwa hapa duniani, **Musa** 4:1–4. Viumbe-akili-asilia viliumbwa kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu, **Ibr.** 3:22. Na Miungu wakashauriana wenyewe, **Ibr.** 4:26. Miungu wakamaliza kazi waliyoshauriana kuifanya, **Ibr.** 5:2.

Barnaba

Jina aliopewa kwa Yusufu (pia aliitwa Yusufi), Mlawi wa Kipro, aliyeuza shamba lake na kutoa mapato yake kwa Mitume (Mdo. 4:36–37). Ingawa hakuwa mmoja wa Mitume Kumi na Wawili wa mwanzoni, alikuja kuwa Mtume (Mdo. 14:4, 14) na alikwenda katika safari kadhaa za kimisionari (Mdo. 11:22–30; 12:25; 13–15; 1 Kor. 9:6; Gal. 2:1, 9; Kol. 4:10).

Bartholomayo. *Ona pia* Nathanaeli

Katika Agano Jipya, ni mmoja wa Mitume Kumi na Wawili wa mwanzo wa Yesu Kristo (Mt. 10:2–4).

Bath-sheba. *Ona pia* Daudi

Mke wa Uria; baadaye, mke wa Daudi na mama wa Suleimani. Mfalme Daudi alitenda uzinzi pamoja naye. Pia alipanga ili mume wake auawe vitani (2 Sam. 11), dhambi ambayo ilikuwa na madhara ya kudumu kwa Daudi (M&M 132:39).

Batiza, Ubatizo. *Ona pia* Ibada; Roho Mtakatifu; Ubatizo wa Watoto Wachanga; Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena

Neno lililotumika katika maandishi halisi ya Kiyunani linaanisha "chovya" au "zamisha." Ubatizo kwa uzamisho katika maji na mtu mwenye mamlaka ni ibada ya kwanza ya injili na ni ya muhimu ili kuwa muumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Hutanguliwa na imani katika Yesu Kristo na katika toba. Ni lazima ufuatiwe na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu ili uweze kuwa kamili (2 Ne. 31:13–14). Ubatizo kwa maji na Roho ni muhimu kabla mtu hajaingia katika ufalme wa selestia. Adamu alikuwa mtu wa kwanza kubatizwa (Musa 6:64–65). Yesu pia alibatizwa ili kutimiza haki yote na ili kuonyesha njia kwa ajili ya wanadamu wote (Mt. 3:13–17; 2 Ne. 31:5–12).

Kwa sababu si watu wote duniani hupata nafasi ya kuipokea injili wakiwa duniani, Bwana ametoa mamlaka ubatizo kufanyika kwa watu walio hai kwa niaba ya wale waliokufa. Kwa hiyo, wale waipokeao injili katika ulimwengu wa roho wanaweza kustahili kuingia katika ufalme wa Mungu.

Muhimu: Kubali hivi sasa ili kutimiza haki yote, **Mt.** 3:15. Yesu alikuja na akabatizwa na Yohana, **Mk.** 1:9. Mafarisayo na wanasheria walipinga shauri la Mungu, kwa kutobatizwa, **Lk.** 7:30. Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu, **Yn.** 3:5. Tubuni, na mkabatizwe kila mmoja wenu, **Mdo.** 2:38.

Anawaamuru watu wote kwamba lazima wakabatizwe katika jina lake, **2 Ne.** 9:23–24. Wanadamu lazima wamfuate Kristo, wabatizwe, wampokee Roho Mtakatifu, na kustahmili hadi mwisho ili wapate kuokolewa, **2 Ne.** 31. Mafundisho ya Kristo ni kwamba wanadamu yawapasa kuamini na kubatizwa, **3 Ne.** 11:20–40.

Wale wasio amini maneno yako na wasiobatizwa katika maji katika jina langu watahukumiwa, **M&M** 84:74.

Mungu alimwelezea Adamu kwa nini toba na ubatizo ni muhimu, **Musa** 6:52–60.

Ubatizo kwa kuzamishwa: Yesu alipokwisha kubatizwa, mara akapanda kutoka majini, **Mt.** 3:16 (Mk. 1:10). Yohana alikuwa akibatiza katika Enoni kwa sababu huko kulikuwa na maji tele, **Yn.** 3:23. Filipo na yule towashi wakateremka ndani ya maji, **Mdo.** 8:38. Tunazikwa pamoja naye kwa ubatizo, **Rum.** 6:4 (Kol. 2:12).

Mfuateni Bwana wenu na Mwokozi wenu chini ndani ya maji, **2 Ne.** 31:13. Alma, Helamu na wengineo walizikwa ndani ya maji, **Mos.** 18:12–16. Na kisha mtawazamisha ndani ya maji, **3 Ne.** 11:25–26.

Namna sahihi ya ubatizo imeelezwa, **M&M** 20:72–74. Walibatizwa kwa namna ya kuzikwa kwake, wakizikwa ndani ya maji katika jina lake, **M&M** 76:50–51.

Adamu alilazwa ndani ya maji na kutolewa kutoka majini, **Musa** 6:64. Ubatizo ni kwa kuzamishwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi, **M ya I** 1:4.

Ubatizo kwa ajili ya maondoleo ya dhambi: Simama na ubatizwe, na ukaoshe dhambi zako, **Mdo.** 22:16.

Baada ya ubatizo huja ondoleo la dhambi zenu kwa moto na kwa Roho Mtakatifu, **2 Ne.** 31:17. Njooni na mkabatizwe ubatizo wa toba ili mpate kuoshwa kutokana na dhambi zenu, **Alma** 7:14. Wamebarikiwa wao watakao amini na kubatizwa, kwa maana watapokea ondoleo la dhambi zao, **3 Ne.** 12:1–2.

Tangazeni toba na imani juu ya Mwokozi na ondoleo la dhambi kwa ubatizo, **M&M** 19:31.

Tunaamini katika ubatizo kwa kuzamishwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi, **M ya I** 1:4.

Mamlaka sahihi: Enendeni na mkayafundishe mataifa yote, mkiwabatiza katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, **Mt.** 28:19 (M&M 68:8).

Limhi na wengi wa watu wake walikuwa wakitamani kubatizwa, lakini hapakuwa na yeyote katika nchi ile aliyekuwa na mamlaka kutoka kwa Mungu, **Mos.** 21:33. Ninakupa uwezo kwamba utawabatiza, **3 Ne.** 11:19–21.

Ukuhani wa Haruni una funguo za ubatizo kwa kuzamisha kwa ajili ya ondoleo la dhambi, **M&M** 13. Hao ndiyo waliotawazwa nami ili kubatiza katika jina langu, **M&M** 18:29.

Yohana Mbatizaji alimpa Joseph Smith na Oliver Cowdery mamalaka ya kubatiza, **JS—H** 1:68–69.

Sifa zinazotakiwa kwa ajili ya ubatizo: Tubuni, na mkabatizwe katika jina la Mwanangu Mpendwa, **2 Ne.** 31:11. Lazima mtubu na kuzaliwa tena, **Alma** 7:14. Angalieni kwamba hambatizwi bila kustahili, **Morm.** 9:29. Fundisha wazazi kwamba lazima watubu na wabatizwe na wajinyenyekeze wenyewe, **Moro.** 8:10.

Sifa za wale wanaotamani ubatizo zawekwa, **M&M** 20:37. Watoto watabatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao wafikapo umri wa miaka minane, **M&M** 68:25, 27.

Agano lifanywalo kwa njia ya ubatizo: Mmeingia katika agano pamoja naye ya kwamba mtamtumikia yeye na kuzishika amri zake, **Mos.** 18:8–10, 13.

Wale wanaotubu, hujichukulia juu yao jina la Kristo, na wakadhamiria kumtumikia yeye watapokelewa kwa njia ya ubatizo, **M&M** 20:37.

Ubatizo kwa ajili ya wafu: Wenye kubatizwa kwa ajili ya wafu watafanyeje, **1 Kor.** 15:29.

Ubatizo kwa ajili ya wafu hufanywa kwa ajili ya ondoleo la dhambi, **M&M** 124:29; 127:5–9; 128:1; 138:33.

Ubatizo siyo kwa ajili ya watoto wachanga: Ni dhihaka iliyo nzito mbele za Mungu kwamba yawapasa kubatiza watoto wadogo, **Moro.** 8:4–23.

Watoto watabatizwa wakiwa na umri wa miaka minane, **M&M** 68:27. Watoto wote wanaokufa kabla ya miaka ya uwajibikaji wanaokolewa katika ufalme wa selestia, **M&M** 137:10.

Belshaza. *Ona pia* Babeli, Babilonia

Katika Agano la Kale, ni mfalme wa mwisho wa Babeli, aliyetawala kabla Koreshi hajaiteka Babilonia; ni mwana na mrithi wa Nebukadneza (Dan. 5:1–2).

Bendera

Katika maandiko ni bendera au kiwango ambacho watu hukusanyika katika umoja wa dhamira au kufunganishwa. Katika nyakati za kale bendera ilitumika kama kambi ya kukusanyika askari katika vita. Kitabu cha Mormoni na Kanisa la Yesu Kristo ni ishara ya bendera kwa mataifa yote ya dunia.

Atawatwekea bendera mataifa, **Isa.** 5:26 (2 Ne. 15:26). Shina la Yese litasimama kuwa bendera, **Isa.** 11:10 (2 Ne. 21:10; M&M 113:6).

Itwekeni bendera ya amani, **M&M** 105:39.

Bendera ya Uhuru. *Ona pia* Moroni, Kapteni

Bendera iliyoinuliwa na Moroni, amiri jeshi mkuu wa majeshi ya Wanefi katika Kitabu cha Mormoni. Moroni aliitengeneza ile bendera ili kuwashawishi watu wa Nefi kulinda dini yao, uhuru, amani na familia zao.

Moroni alitengeneza hati ya uhuru kutokana na koti lake lililochanika, **Alma** 46:12–13. Wale watakaoidumisha ile hati waliingia katika agano, **Alma** 46:20–22. Moroni alifanya ile hati itundikwe juu ya kila mnara, **Alma** 46:36 (Alma 51:20).

Benjamini, Baba wa Mosia. *Ona pia* Mosia, Mwana wa Benjamini

Nabii katika Kitabu cha Mormoni na ni mfalme (Mos. 1–6).

Alijishughulisha na matatizo makubwa katika kustawisha amani katika nchi, **Omni** 1:23–25 (M. ya Morm. 1:12–18). Aliwafundisha wanawe, **Mos.** 1:1–8. Aliuweka ufalme juu ya mwanawe Mosia, **Mos.** 1:9–18. Watu wake walikusanyika ili kusikiliza hotuba yake ya mwisho, **Mos.** 2:1–8. Aliwahutubia watu wake, **Mos.** 2:9–4:30. Watu wake walifanya agano na Bwana, **Mos.** 5–6.

Benjamini, Mwana wa Yakobo. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mwana wa pili wa Yakobo wa Raheli (Mwa. 35:16–20).

Kabila la Benjamini: Yakobo akambariki Benjamini (Mwa. 49:27). Wazao wa Benjamini walikuwa watu wapigana vita. Wabenjamini wawili maarufu ni Sauli, mfalme wa kwanza wa Waisraeli (1 Sam. 9:1–2), na Paulo, Mtume wa Agano Jipya (Rum. 11:1).

Bethania

Kijiji ambacho Yesu Kristo alikaa katika wiki ya mwisho ya maisha yake hapa duniani. (Mt. 21:17; Mk. 11:11). Kipo upande wa kusinimashariki mwa mteremko wa Mlima wa Mizeituni, Bethania kulikuwa ndiyo nyumbani kwa Lazaro, Maria, na Martha (Yn. 11:1–46; 12:1).

Betheli

Katika Kiebrania, maana yake "nyumba ya Mungu" na ni moja ya maeneo matakatifu sana katika Israeli. Uko kiasi maili kumi (kilometa kumi na sita) kaskazini mwa Yerusalemu. Hapa Ibrahimu alijenga madhabahu yake alipofika Kanaani kwa mara ya kwanza (Mwa. 12:8; 13:3). Hapa Yakobo aliona katika ono ngazi ifikayo mbinguni (Mwa. 28:10–19). Pia palikuwa mahali patakatifu katika siku za Samweli (1 Sam. 7:16; 10:3).

Bethlehemu

Mji mdogo ulioko maili tano (kilometa nane) kusini mwa Yerusalemu. Katika Kiebrania, Bethlehemu maana yake "nyumba ya mkate"; pia unaitwa Efrathi, maana yake "wenye kuzaa matunda." Yesu Kristo alizaliwa katika Bethlehemu (Mika 5:2; Mt. 2:1–8). Ni mahali alipozikwa Raheli (Mwa. 35:19; 48:7).

Ruthu na Boazi waliishi hapa, **Rut.** 1:22. Samweli alimpaka mafuta Daudi hapo, **1 Sam.** 16:1–13; 17:12, 15; 20:6, 28.

Herode aliwaua watoto hapo, **Mt.** 2:16.

Biblia. *Ona pia* Agano Jipya; Agano la Kale; Apokrifa; Efraimu—Kijiti cha Efraimu au Yusufu; Kanoni; Maandiko; Yuda—Kijiti cha Yuda

Mkusanyiko wa maandiko ya Kiebrania na Kikristo ambayo yana mafunuo matakatifu. Neno biblia maana yake "vitabu." Biblia ni kazi ya manabii wengi na waandishi wengine waliokuwa wakiandika chini ya maongozi ya Roho Mtakatifu (2 Pet. 1:21).

Biblia ya Kikristo ina pande mbili, hujulikana kama Agano la Kale na Jipya. Agano la Kale linajumuisha vitabu vya maandiko yaliyotumika miongoni mwa Wayahudi wa Filisti wakati wa huduma ya Bwana hapa duniani. Agano Jipya lina maandiko yaliyoandikwa nyakati za Kitume na huheshimika kama yana utakatifu na mamlaka sawa sawa na yale maandiko ya Kiyahudi. Vitabu vya Agano la Kale vimechukuliwa kutoka vitabu vya maandiko mbali mbali ya kitaifa yaliyoendelezwa kwa karne nyingi nayo yalikuwa kwa ujumla yameandikwa katika Kiebrania, wakati vile vitabu vya Agano Jipya ni kazi ya kizazi kimoja tu, nayo kwa kiwango kikubwa yalikuwa yameandikwa katika Kiyunani.

Katika Agano la Kale neno ushuhuda liliwakilisha neno la Kiebrania lenye maana ya "agano." Agano la Kale ni torati iliyotolewa kwa Musa wakati

Israeli walipokataa utimilifu wa injili iliyokuwa na watu wa Mungu kutoka mwanzo wa uhai. Agano Jipya ni injili kama ilivyofundishwa na Yesu Kristo.

Katika Biblia ya Kiebrania (Agano la Kale) vitabu hivi viligawanywa katika makundi matatu: Sheria, Manabii, na Maandiko. Biblia iliyotumiwa na ulimwengu wa Wakristo imeweka vitabu hivi katika madaraja kulingana na mada, kama vile vya kihistoria, vya kishairi, na vya kinabii.

Vitabu vya Agano Jipya kwa ujumla viko katika mpangilio huu: Injili nne na Matendo ya Mitume; nyaraka za Paulo; nyaraka kwa watu wote za Yakobo, Petro, Yohana, na Yuda; na Ufunuo wa Yohana.

Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho linatukuza na kuheshimu sana Biblia na linasisitiza pia kwamba Bwana anaendelea kutoa ufunuo wa nyongeza kupitia manabii Wake katika siku hizi za mwisho ufunuo ambao unaunga mkono na kuthibitisha yaliyoandikwa katika biblia juu ya matendo ya Mungu kwa wanadamu.

Kijiti cha Yuda (Biblia) na kijiti cha Yusufu (Kitabu cha Mormoni) vitakuwa kimoja mkononi mwa Bwana, **Eze.** 37:15–20.

Ukweli wa Biblia utaimarishwa kwa maandiko ya siku za mwisho, **1 Ne.** 13:38–40. Biblia itaungana na Kitabu cha Mormoni katika kuyaagusha mafundisho ya uongo, **2 Ne.** 3:12. Biblia! Biblia! Tunayo Biblia, **2 Ne.** 29:3–10. Wote waiaminio Biblia pia watakiamini Kitabu cha Mormoni, **Morm.** 7:8–10.

Wazee watafundisha kanuni za Injili yangu, ambazo zipo katika Biblia na katika Kitabu cha Mormoni, **M&M** 42:12.

Tunaamini Biblia kuwa ni neno la Mungu ilimradi imetafsiriwa kwa usahihi, **M ya I** 1:8.

Bidii

Msimamo thabiti, jitihada za ujasiri hasa katika kumtumikia Bwana na kutii neno Lake.

Nisikilizeni kwa bidii, **Isa.** 55:2.

Mungu ndiye mtoa thawabu kwao wale wamtafutao kwa bidii, **Ebr.** 11:6. Mkifanya bidii yote, katika imani yenu ongezeni na wema, **2 Pet.** 1:5.

Tulifundishe neno la Mungu kwa bidii yote, **Yak. (KM)** 1:19. Waliyapekua maandiko kwa bidii, **Alma** 17:2. Walitamani kwa bidii yote kushika amri, **3 Ne.** 6:14. Tufanye kazi kwa bidii, **Moro.** 9:6.

Jiingizeni kwa shauku katika kazi njema, **M&M** 58:27. Wala msikae bure pasipo kazi bali fanyeni kazi kwa nguvu zenu, **M&M** 75:3. Fanyeni bidii ya kuwa wasikivu kwa maneno ya uzima wa milele, **M&M** 84:43. Kila mtu na ajifunze wajibu wake, na kutenda kazi kwa bidii yote, **M&M** 107:99.

Bikira. *Ona pia* Maria, Mama wa Yesu

Mwanamume au mwanamke wa umri wa kuweza kuolewa ambaye kamwe hajapata kujamiiana. Katika maandiko, bikira anaweza kumwakilisha mtu ambaye ni msafi kimaadili (Ufu. 14:4).

Bikira atachukuwa mimba na atazaa mwana, **Isa.** 7:14 (Mt. 1:23; 2 Ne. 17:14).

Ufalme wa mbinguni unafananishwa na wanawali kumi, **Mt.** 25:1–13.

Katika mji wa Nazarethi nilimwona bikira, ambaye alikuwa mama wa Mwana wa Mungu, **1 Ne.** 11:13–18. Maria alikuwa bikira, chombo cha thamani na kilichochaguliwa, **Alma** 7:10.

Bikira Maria. *Ona* Maria, Mama wa Yesu

Boazi. *Ona pia* Rutu

Mumewe Ruthu (Rut. 4:9–10); babumkuu wa Daudi, mfalme wa Israeli (Rut. 4:13–17); na babu wa Kristo, mfalme wa wafalme (Lk. 3:32).

Bustani ya Edeni. *Ona* Edeni

Bustani ya Gethsemani. *Ona* Gethsemani

Bwana. *Ona pia* Mungu, Uungu; Yesu Kristo

Jina lenye hadhi na ni heshima kubwa

kwa Mungu Baba na Mwokozi Yesu Kristo. Jina hili linaonyesha nafasi Zao kama watawala wakuu na wenye upendo wa viumbe Vyao.

Hakuna kitu kigumu zaidi kwa Bwana, **Mwa.** 18:14. Bwana alisema na Musa uso kwa uso, **Ku.** 33:11. Mpende Bwana Mungu wako, **Kum.** 6:5 (Mt. 22:37; Mk. 12:30). Lakini mimi na nyumba yangu, tutamtumikia Bwana, **Yos.** 24:15. Bwana ndiye mchungaji wangu, **Zab.** 23:1. Bwana ni hodari na mwenye uwezo, uwezo wa vita, **Zab.** 24:8. Bwana Yehova ndiye nguvu yangu, **Isa.** 12:2 (2 Ne. 22:2). Mimi, Bwana ni Mwokozi wako na Mkombozi wako, **Isa.** 60:16.

Utamwabudu Bwana Mungu wako, **Mt.** 4:10 (Lk. 4:8). Ni makuu jinsi gani makuu aliyotutendea Bwana, **Mk.** 5:19. Kuna Bwana mmoja Yesu Kristo, **1 Kor.** 8:6. Kuna Bwana mmoja, imani moja, ubatizo mmoja, **Efe.** 4:5. Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni, **1 The.** 4:16.

Nitakwenda na kufanya mambo yale Bwana ameyoniamuru, **1 Ne.** 3:7. Bwana atawahukumu maskini kwa haki, **2 Ne.** 30:9. Bwana Mungu, Mungu wa Ibrahimu, aliwakomboa Waisraeli kutoka utumwani, **Alma** 29:11. Hakuna kinachoweza kuwaokoa watu isipokuwa toba na imani juu ya Bwana, **Hel.** 13:6 (Mos. 3:12).

Sikiliza maneno ya Yesu Kristo, Bwana wako, **M&M** 15:1. Utafuteni uso wa Bwana daima, **M&M** 101:38. Bwana atakuwa mwekundu katika mavazi yake wakati wa Ujio wa Pili, **M&M** 133:48 (Isa. 63:1–4).

Ibrahimu aliongea na Bwana uso kwa uso, **Ibr.** 3:11. Tunaamini kuwa kanuni ya kwanza ya injili ni imani katika Bwana Yesu Kristo, **M ya I** 1:4.

Bwana Harusi. *Ona pia* Yesu Kristo

Yesu Kristo amepewa ishara katika maandiko kama Bwana Harusi. Kanisa ni ishara ya bibi harusi Wake.

Wanawali kumi walienda ili kumlaki Bwana Harusi, **Mt.** 25:1–13. Aliye naye bibi harusi ndiye Bwana Harusi, **Yn.** 3:27–30. Heri walioalikwa kwenye karamu ya harusi ya Mwanakondoo, **Ufu.** 19:5–10.

Kuweni tayari wakati wa kuja kwa Bwana Harusi, **M&M** 33:17. Jitayarisheni kwa ajili ya Bwana Harusi, **M&M** 65:3.

Bwana wa Majeshi. *Ona pia* Yesu Kristo

Jina jingine la Yesu Kristo. Hutawala juu ya majeshi ya mbinguni na duniani na huwaongoza wenye haki dhidi ya uovu (M&M 29:9; 121:23).

Bwana wa majeshi ndiye Mfalme wa utukufu, **Zab.** 24:10.

Mungu wa Israeli ndiye Bwana wa Majeshi, **1 Ne.** 20:2.

Roho yangu haitashindana daima na mwanadamu, asema Bwana wa Majeshi, **M&M** 1:33.

Chafu, Uchafu. *Ona pia* Dhambi; Kutokuwa Adilifu, Siyo Adilifu; Ovu, Uovu; Safi na Isiyo safi; Sio mcha mungu

Kutokuwa safi kiroho kwa sababu ya kukosa utiifu kwa makusudi kwa Mungu.

Bwana atakapokuwa ameuosha uchafu wa hao mabinti wa Sayuni, **Isa.** 4:4 (2 Ne. 14:4).

Ufalme wa Mungu siyo mchafu, **1 Ne.** 15:34 (Alma 7:21). Wale walio wachafu watabakia wachafu, **2 Ne.** 9:16 (Morm. 9:14). Utajisikia vipi, kama utasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Mungu, ukiwa na mavazi yaliyo machafu, **Alma** 5:22.

Wao lazima wabaki kuwa wachafu, **M&M** 88:35.

Lini nitapumzika, na kusafishwa kutokana na uchafu, **Musa** 7:48.

Chagua, Chaguliwa. *Ona* Alichagua, Chagua, Chaguliwa (kitenzi)

Chaguo. *Ona* Alichagua, Chagua, Chaguliwa (kitenzi); Haki ya uamuzi

Chuki, Chukia. *Ona pia* Kisasi; Uadui; Upendo

Chukia ni hali yenye nguvu ya kutompenda mtu fulani au kitu fulani.

Mimi, Mungu huupatiliza uovu wa baba juu ya watoto wao wale wanichukiao, **Ku.** 20:5. Mambo haya sita Bwana huyachukia, **Mit.** 6:16. Mtu mjinga humdharau mama yake, **Mit.** 15:20. Amedharauliwa na kukataliwa na wanadamu, **Isa.** 53:3.

Watendeeni mema wale wanao wachukia, **Mt.** 5:44. Ama atamchukia mmoja na kupenda mwingine, au atashikamana na mmoja, na kumdharau mwingine, **Mt.** 6:24. Nanyi mtakuwa mkichukiwa na watu wote kwa ajili ya jina langu, **Mt.** 10:22. Kila mtu atendaye uovu huichukia nuru, **Yn.** 3:20. Mtu awaye yote asiudharau ujana wako, **1 Tim.** 4:12.

Kwa sababu wao ni matajiri, wanawadharau maskini, **2 Ne.** 9:30. Usidharau mafunuo ya Mungu, **Yak. (KM)** 4:8. Walikuwa na chuki ya milele dhidi yetu, **Yak. (KM)** 7:24.

Wanadamu waliyapuuza mashauri ya Mungu, na kudharau maneno yake, **M&M** 3:7.

Nilichukiwa na kuteswa kwa kusema kwamba niliona ono, **JS—H** 1:25.

Chukiza, Chukizo. *Ona pia* Dhambi

Katika maandiko, ni kitu ambacho kinasababisha kuchafuka moyo au chuki kwa wenye haki na wasafi.

Midomo ya uongo ni chukizo kwa Bwana, **Mit.** 12:22.

Kiburi ni chukizo machoni pa Bwana, **Yak. (KM)** 2:13–22. Waovu hutolewa waone machukizo yao wenyewe, **Mos.** 3:25. Uzinzi unachukiza kuliko dhambi zote isipokuwa kuua na kumkufuru Roho Mtakatifu, **Alma** 39:3–5.

Hasira ya Bwana inawaka dhidi ya machukizo yao, **M&M** 97:24.

Chumvi

Ilitumika kama kilinda chakula muhimu katika ulimwengu wa kale; ilifikiriwa kuwa kitu muhimu katika maisha.

Mke wa Lutu akawa nguzo ya chumvi, **Mwa.** 19:26.

Ninyi ni chumvi ya dunia, **Mt.** 5:13 (Lk. 14:34; 3 Ne. 12:13).

Watu wa agano wa Bwana wanahesabika kama chumvi ya dunia, **M&M** 101:39–40. Kama Watakatifu sio njia ya wokovu kwa wanadamu, wao ni sawa na chumvi iliyopoteza ladha yake, **M&M** 103:9–10.

Cowdery, Oliver

Mzee wa pili wa Kanisa lililorejeshwa na ni mmoja kati ya Mashahidi Watatu wa chimbuko na ukweli wa kiungu wa Kitabu cha Mormoni. Alitumika kama mwandishi wakati Joseph Smith alipokuwa akitafsiri Kitabu cha Mormoni kutoka katika mabamba yale ya dhahabu (JS—H 1:66–68).

Alipata ushahidi wa ukweli wa tafsiri ya kitabu cha Mormoni, **M&M** 6:17, 22–24. Alitawazwa na Yohana Mbatizaji, **M&M** 13 (M&M 27:8; JS—H 1:68–73, ona maelezo mstari wa 71). Baada ya kupata imani na kuyashuhudia kwa macho yako, utashuhudia ya kwamba umeyaona, **M&M** 17:3, 5. Nimeyafunua kwako, kwa Roho wangu, kwamba mambo uliyoyaandika kuwa ni ya kweli, **M&M** 18:2. Aliteuliwa na kutawazwa kuwa mmoja wa wasimamizi wa mafunuo, **M&M** 70:3. Alipokea funguo za ukuhani pamoja na Joseph Smith, **M&M** 110.

Dada. *Ona pia* Kaka, Ndugu; Mwanadamu, Wanadamu; Mwanamke, Wanawake

Kama watoto wa baba yetu wa Mbinguni, wanaume na wanawake wote ni kaka na dada wa kiroho. Katika Kanisa, waumini wanawake na marafiki wa Kanisa mara kwa mara hutambulika kama dada.

Wale wafanyao mapenzi ya Baba yangu, hao ndiyo kaka na dada yangu, **Mt.** 12:50 (Mk. 3:35).

Sheria zinazotawala maungamo ya dhambi kati ya kaka na dada katika Kanisa zinawekwa, **M&M** 42:88–93.

Dameski

Mji wa kale wa Shamu.

Dameski husimama juu ya uwanda wenye rutuba ukingoni mwa jangwa na humwagiliwa vyema kwa maji ya mto Barada. Umetajwa mara nyingi katika maandiko (kuanzia Mwa. 14:15). Paulo alikuwa katika safari yake ya kwenda Dameski wakati alipotokewa na Bwana mfufuka (Mdo. 9:1–27; 22:5–16; 26:12–20).

Damu. *Ona pia* Dhabihu; Lipia dhambi, Upatanisho; Yesu Kristo

Huchukuliwa na Waisraeli wa zamani na tamaduni nyingi za leo kama chanzo muhimu cha uhai au nguvu muhimu kwa uzima wa wenye mwili wote. Katika nyakati za Agano la Kale Bwana aliwakataza Israeli wasile damu kama chakula (Law. 3:17; 7:26–27; 17:10–14).

Uwezo wa kulipia dhambi kwa dhabihu ulikuwa katika damu kwa sababu damu ilichukuliwa kama kitu muhimu katika uzima. Dhabihu za wanyama wakati wa Agano la Kale ilikuwa ishara ya dhabihu kuu ambayo baadaye ilifanywa na Yesu Kristo (Law. 17:11; Musa 5:5–7). Damu ya kulipia dhambi ya Yesu Kristo humsafisha mwenye kutubu kutokana na dhambi (1 Yoh. 1:7).

Jasho lake likawa kama matone makubwa ya damu, **Lk.** 22:44. Tunatakaswa kwa kumwagika kwa damu ya Kristo, **Ebr.** 10:1–22.

Damu ikatoka katika kila kitundu, **Mos.** 3:7 (M&M 19:18).

Damu ya Bwana ilimwagika kwa ajili ya ondoleo la dhambi, **M&M** 27:2. Yesu alifanya upatanisho mkamilifu kwa kumwaga damu yake, **M&M** 76:69.

Kwa damu yake mnatakaswa, **Musa** 6:60.

Danganya, Kudanganya, Udanganyifu. *Ona pia* Hila; Kusema uongo

Katika maandiko, kudanganya ni kusababisha mtu aamini kitu ambacho si cha kweli.

Yule asiyeapa kwa hila atapanda katika mlima wa Bwana, **Zab.** 24:3–4. Uniokoe na mtu wa hila, **Zab.** 43:1. Ole wao waitao uovu ni wema, na wema ni uovu, **Isa.** 5:20 (2 Ne. 15:20).

Na mtu asijidanganye mwenyewe, **1 Kor.** 3:18. Na mtu asiwadanganye kwa maneno yasiyo na maana, **Efe.** 5:6. Watu waovu watadanganya na watadanganyika, **2 Tim.** 3:13. Shetani, ambaye aliudanganya ulimwengu wote, alitupwa nje, **Ufu.** 12:9. Shetani alifungwa ili asipate kuwadanganya tena mataifa, **Ufu.** 20:1–3.

Bwana hawezi kudanganywa, **2 Ne.** 9:41. Kama mtamfuata Mwana, pasipo kutenda udanganyifu mbele za Mungu, mtampokea Roho Mtakatifu, **2 Ne.** 31:13. Sheremu alikiri kwamba alidanganywa kwa nguvu za ibilisi, **Yak. (KM)** 7:18. Watu wa Mfalme Nuhu walidanganywa kwa maneno ya ulaghai, **Mos.** 11:7.

Wenye hekima wamemchukua Roho Mtakatifu kuwa kiongozi wao, nao hawajadanganyika, **M&M** 45:57. Ole wao wale walio wadanganyifu, **M&M** 50:6.

Akawa Shetani, baba wa uongo wote, kudanganya na kuwapofusha wanadamu, **Musa** 4:4.

Dani. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, huyu ni mwana wa Yakobo na Bilha, mjakazi wa Raheli (Mwa. 30:5–6).

Kabila la Dani: Kwa baraka za Yakobo juu ya Dani, ona Mwanzo 49:16–18. Kwa baraka za Musa juu ya kabila la Dani, ona Kumbukumbu la Torati 33:22. Baada ya kukaa katika Kanaani, kabila la Dani lilipata kipande kidogo cha ardhi lakini chenye rutuba (Yos. 19:40–48). Walikuwa na kazi ngumu ya kuulinda dhidi ya Waamori (Amu. 1:34) na dhidi

ya Wafilisti (Amu. 13:2, 25; 18:1). Kama matokeo yake, Wadani walihamia kaskazini ya Palestina (Amu. 18), karibu ya Laishi, na wakauita mji ule Dani. Mji huu unajulikana vizuri kama mpaka wa kaskazini wa Palestina, ambao ulienea "kutoka Dani hadi Beer-sheba."

Danieli

Mhusika mkuu wa kitabu cha Danieli katika Agano la Kale; ni nabii wa Mungu na ni mtu aliyekuwa na imani kubwa.

Hakuna kitu kinachojulikana juu ya wazazi wake, ingawa anaonekana kuwa ametokana na uzao wa kifalme (Dan. 1:3). Alichukuliwa mateka kwenda Babeli, mahali ambako alipata jina la Belteshaza (Dan. 1:6–7). Danieli na mateka wengine watatu walikataa chakula cha mfalme kwa sababu za kidini (Dan. 1:8–16).

Danieli alipata kukubalika na Nebukadneza na Dario kutokana na uwezo wake wa kutafsiri ndoto (Dan. 2; 4; 6). Pia alisoma na kutafsiri maandiko ya mkono yaliyoandikwa ukutani (Dan. 5). Maadui zake walikula njama dhidi yake, naye akatupwa katika tundu la simba, lakini Bwana akayalinda maisha yake (Dan. 6).

Kitabu cha Danieli: Kitabu hiki kina sehemu mbili: mlango wa 1–6 ni hadithi juu ya Danieli na wenzake watatu; mlango wa 7–12 ni maono ya kinabii ambayo Danieli aliyaona. Kitabu hiki kinafundisha umuhimu wa kuwa wa kweli kwa Mungu na kinaelezea kwamba Bwana huwabariki walio waaminifu.

Mchango mkubwa wa kitabu hiki ni tafsiri ya ndoto ya Mfalme Nebukadneza. Katika ndoto hiyo, ufalme wa Mungu katika siku za mwisho unasimama kama jiwe ambalo limekatwa kutoka mlimani. Jiwe hilo litabiringika hadi liijaze dunia yote (Dan. 2; ona pia M&M 65:2).

Dario. *Ona pia* Babeli, Babilonia

Katika Agano la Kale, ni Mfalme wa Wamedi aliyetawala katika Babilonia baada ya kifo cha Belshaza (Dan. 5:31; 6:9, 25–28; 9:1; 11:1).

Daudi. *Ona pia* Bath-sheba; Zaburi

Mfalme wa kale wa Israeli katika Agano la Kale.

Daudi alikuwa mwana wa Yese wa kabila la Yuda. Alikuwa kijana jasiri aliyemwua simba, dubu, na jitu kubwa la Kifilisti Goliathi (1 Sam. 17). Daudi alichaguliwa na kupakwa mafuta kuwa mfalme wa Israeli. Kama Sauli, katika utu uzima wake alikuwa na hatia ya kufanya makosa makubwa ya jinai, lakini, tofauti na Sauli, yeye alikuwa na uwezo wa kuonyesha majuto ya kweli. Hivyo basi aliweza kupata msamaha, isipokuwa katika mauaji ya Uria (M&M 132:39). Maisha yake yanaweza kugawanywa katika sehemu nne: (1) huko Bethlehemu, ambako alikuwa mchungaji wa kondoo (1 Sam. 16–17); (2) katika baraza la Mfalme Sauli (1 Sam. 18:1–19:18); (3) kama mtoro (1 Sam. 19:18–31:13; 2 Sam. 1); (4) kama mfalme juu ya Yuda huko Hebroni (2 Sam. 2–4) na mwishowe kama mfalme juu ya Israeli yote (2 Sam. 5–24; 1 Fal. 1:1–2:11).

Dhambi ya uzinzi ya Daudi na Bath-sheba ilifuatiwa na mfuatano wa mabalaa ambayo yaliiharibu miaka ishirini ya mwisho ya uhai wake. Taifa kwa ujumla lilistawi wakati wa utawala wake, lakini Daudi mwenyewe aliteseka kutokana na matokeo ya dhambi zake. Daima kulikuwepo na ugomvi mkubwa wa kifamilia, ambao, katika shauri la Absalomu na Adonia, uliishia katika uasi wa wazi. Matukio haya ni utimilifu wa laana iliyotamkwa na Nathani nabii juu ya Daudi kwa sababu ya dhambi yake (2 Sam. 12:7–13).

Ingawa kulikuwa na mabalaa haya, utawala wa Daudi ulikuwa utawala ulio mzuri kuliko wowote katika historia ya Israeli, kwa sababu (1) aliyaunganisha makabila kuwa katika taifa moja, (2) alipata milki ya nchi pasipo mabishano, (3) aliiweka serikali juu ya misingi ya dini ya kweli kiasi kwamba mapenzi ya

Mungu yakawa ndiyo sheria ya Israeli. Kwa sababu hizi, utawala wa Daudi mwishowe uliheshimiwa kama enzi ya dhahabu ya taifa na iliyo kuwa mfano wa enzi tukufu zaidi wakati Masiya atakapokuja (Isa. 16:5; Yer. 23:5; Eze. 37:24–28).

Maisha ya Daudi hutufundisha umuhimu kwa watu wote kustahmili hadi mwisho. Alipokuwa kijana, alisemekana kuwa mtu aliye mfano wa "moyo wa Bwana mwenyewe" (1 Sam. 13:14); kama mwanadamu, alinena kwa Roho naye alikuwa na mafunuo mengi. Lakini alilipa gharama nzito kwa ajili ya utovu wake wa utiifu kwa amri za Mungu (M&M 132:39).

Debora

Katika Agano la Kale, ni nabii mwanamke aliyewahukumu Waisraeli na alimtia moyo Baraka ili apigane dhidi ya Wakanaani (Amu. 4). Wimbo wa Debora na Baraka wakisherehekea kukombolewa kwa Waisraeli kutoka utumwani (Amu. 5).

Delila. *Ona pia* Wafilisti

Mwanamke Mfilisti katika Agano la Kale ambaye alimdanganya na kumsaliti Samsoni (Amu. 16).

Deni. *Ona pia* Samehe

Kama lilivyotumika katika maandiko, fedha au mali inayodaiwa na mtu mwingine husababisha aliyekopeshwa kuwa katika hali ya utumwa. Kwa maana nyingine, Yesu alifundisha kwamba tumwombe Baba atusamehe madeni yetu, au atufungulie sisi kutoka katika kulipa malipo ya dhambi zetu—kupitia Upatanisho wa Yesu Kristo—baada ya kuwa sisi tumewasamehe wengine kwa ajili ya makosa yao dhidi yetu (Mt. 6:12; 3 Ne. 13:11).

Mtu muovu hukopa wala asilipe tena, **Zab.** 37:21. Akopaye ni mtumwa wake akopeshaye, **Mit.** 22:7.

Nalikusamehe wewe deni lile lote: Nawe je, haikukupasa kumrehemu, **Mt.** 18:23–35. Msidai na mtu chochote, isipokuwa pendaneni, **Rum.** 13:8.

Mnadaiwa milele na Baba yenu wa Mbinguni, **Mos.** 2:21–24, 34. Mtu yeyote aazimaye kutoka kwa jirani yake yampasa kurudisha kitu kile alichokiazima, **Mos.** 4:28.

Lipa deni, na ujifungue mwenyewe kutoka utumwani, **M&M** 19:35. Umekatazwa kujiingiza katika deni kwa maadui zako, **M&M** 64:27. Lipeni madeni yenu yote, **M&M** 104:78. Msiingie katika deni ili kujenga nyumba ya Bwana, **M&M** 115:13.

Dera ya kifuani. *Ona pia* Urimu na Thumimu

Maandiko yanataja aina mbili za dera ya kifuani: (1) Ni vazi ama silaha ya sehemu ya mbele inayomlinda askari. Katika maana ya ishara, Watakatifu wanapaswa kuvaa dirii ya haki ili kujikinga wenyewe dhidi ya maovu (Isa. 59:17; Efe. 6:14). (2) Ni kipande cha vazi kinachovaliwa na kuhani mkuu katika sheria ya Musa (Ku. 28:13–30; 39:8–21). Ilitengenezwa kwa kitani nzuri na kilibeba mawe ya vito kumi na viwili. Wakati mwingine inaelezwa kuwa katika uhusiano na Urimu na Thumimu (M&M 17:1; JS—H 1:35, 42, 52).

Deraya

Vazi linalovaliwa ili kuulinda mwili kutokana na kipigo au kupenywa na silaha. Neno hili pia linatumiwa ili kumaanisha sifa ya kiroho ambayo humlinda mtu kutokana na majaribu au maovu.

Vaeni deraya zote za Mungu, **Efe.** 6:10–18 (M&M 27:15–18).

Desereti. *Ona pia* Wayaredi

Katika kitabu cha Mormoni hili ni neno la Kiyaredi lenye maana ya "nyuki wa asali" (Eth. 2:3).

Dhabihu. *Ona pia* Damu; Lipia dhambi, Upatanisho; Moyo Uliovunjika; Sakramenti; Yesu Kristo

Katika siku za kale, dhabihu ilikuwa

na nia ya kufanya kitu fulani au mtu fulani kuwa mtakatifu. Sasa inamaanisha kuacha au kukubali kupotea kwa mambo ya kiulimwengu kwa ajili ya Bwana na ufalme Wake. Waumini wa Kanisa la Bwana yawapasa kuwa tayari kutoa dhabihu vitu vyote kwa ajili ya Bwana. Joseph Smith alifundisha kwamba "dini ambayo hailazimu kutoa dhabihu ya vitu vyote kamwe haina uwezo wa kutosha kuzalisha imani muhimu kwa ajili ya uzima na wokovu." Katika mtazamo wa milele, baraka zinazopatikana kwa kujitoa dhabihu ni kubwa zaidi kuliko kitu chochote ambacho tumekitoa.

Baada ya Adamu na Hawa kutupwa nje ya Bustani ya Edeni, Bwana aliwapa amri ya dhabihu. Sheria hii ilijumuisha kutoa sadaka mzaliwa wa kwanza wa mifugo yao. Dhabihu hii ilikuwa ni ishara ya dhabihu ambayo ingelifanywa na Mwana Mzaliwa Pekee wa Mungu (Musa 5:4–8). Desturi hii iliendelea hadi kile kifo cha Yesu Kristo, ambacho kilimaliza dhabihu za wanyama kama agizo la injili (Alma 34:13–14). Katika Kanisa siku hizi waumini hushiriki sakramenti ya mkate na maji katika ukumbusho wa dhabihu ya Yesu Kristo. Waumini wa Kanisa la Kristo siku hizi pia wanaombwa kutoa dhabihu ya moyo uliovunjika na roho iliyopondeka (3 Ne. 9:19–22). Hii maana yake ni kwamba watakuwa wanyenyekevu, wenye kutubu, na walio tayari kutii amri za Mungu.

Ibrahimu akamfunga Isaka mwanawe na akamlaza juu ya madhabahu, **Mwa.** 22:1–18 (Yak. [KM] 4:5). Utatoa dhabihu za kuteketeza, **Ku.** 20:24. Wanyama wa dhabihu lazima wawe wale wasio na kilema, **Kum.** 15:19–21. Kutii ni bora kuliko dhabihu, **1 Sam.** 15:22.

Kupenda ni bora zaidi kuliko sadaka za kuteketeza kwa moto na dhabihu, **Mk.** 12:32–33. Tumetakaswa kwa dhabihu ya Kristo, **Ebr.** 10:10–14.

Kristo alijitoa yeye mwenyewe kama dhabihu kwa ajili ya dhambi, **2 Ne.** 2:6–7. Dhabihu kuu na ya mwisho itakuwa Mwana wa Mungu, ndiyo, isiyo na mwisho na iliyo ya milele, **Alma** 34:8–14. Msitoe tena sadaka za kuteketeza kwa moto; toeni kwa Mungu dhabihu ya moyo uliovunjika na roho iliyopondeka, **3 Ne.** 9:19–20 (Zab. 51:16–17; M&M 59:8).

Leo ni siku ya dhabihu, **M&M** 64:23 (M&M 97:12). Wale wote walio radhi kushika maagano yao kwa dhabihu watakubaliwa kwa Bwana, **M&M** 97:8. Joseph F. Smith aliona roho za wenye haki, ambao walikuwa wametoa dhabihu katika mfano wa dhabihu ya Mwokozi, **M&M** 138:13. Ukombozi ulipatikana kupitia dhabihu ya Mwana wa Mungu juu ya msalaba, **M&M** 138:35.

Dhambi. *Ona pia* Chafu, Uchafu; Chukiza, Chukizo; Kosea; Kutokuwa Adilifu, Siyo Adilifu; Ovu, Uovu; Sio mcha mungu; Uasi

Kutotii amri za Mungu kwa makusudi.

Mtu afichaye dhambi zake hatafanikiwa, **Mit.** 28:13. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji, **Isa.** 1:18. Wenye dhambi watakufa, na wenye haki wataokolewa, **Eze.** 18.

Mwanakondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu, **Yn.** 1:29. Ubatizwe, na ukaoshe dhambi zako, **Mdo.** 22:16. Mshahara wa dhambi ni mauti, **Rum.** 6:23. Kwa yeye ajuaye kutenda mema, na wala hayatendi, kwake huyo ni dhambi, **Yak. (Bib.)** 4:17.

Je, utanifanya kwamba nitetemeke nionapo dhambi, **2 Ne.** 4:31. Ole wao wale wafao katika dhambi zao, **2 Ne.** 9:38. Hawakuweza kuitazama dhambi isipokuwa kwa chuki, **Alma** 13:12. Usidhani utarejeshwa kutoka katika dhambi kwenda katika furaha, **Alma** 41:9–10. Bwana hawezi kuiangalia dhambi na kuivumilia hata kidogo, **Alma** 45:16 (M&M 1:31). Watoto wadogo hawana uwezo wa kutenda dhambi, **Moro.** 8:8.

Ili kutubu, wanadamu ni lazima

waungame na kuacha dhambi zao, **M&M** 58:42–43. Dhambi kuu zaidi hubaki ndani yake yeye asiye samehe, **M&M** 64:9. Mtu atendaye dhambi dhidi ya ile nuru kuu zaidi atapata hukumu kuu zaidi, **M&M** 82:3. Kwa nafsi ile ambayo hutenda dhambi, na dhambi za awali zitamrudia, **M&M** 82:7. Tunapojaribu kuficha dhambi zetu, mbingu hujitoa zenyewe, **M&M** 121:37.

Dhambi isiyo sameheka. *Ona pia* Kukufuru, Kufuru; Mauaji; Roho Mtakatifu; Wana wa Upotevu

Dhambi ya kumkana Roho Mtakatifu, ni dhambi ambayo haiwezi kusamehewa.

Kufuru dhidi ya Roho Mtakatifu haitasamehewa kwa wanadamu, **Mt.** 12:31–32 (Mk. 3:29; Lk. 12:10). Haiwezekani kwa wale waliofanywa washiriki wa Roho Mtakatifu kuwafanya upya tena hata katika toba, **Ebr.** 6:4–6. Kama tutafanya dhambi kwa makusudi baada ya kupokea ufahamu wa ukweli haibaki tena dhabihu kwa ajili ya dhambi, **Ebr.** 10:26.

Kama mtamkana Roho Mtakatifu na ukajua kwamba unamkana, hii ni dhambi ambayo isiyosameheka, **Alma** 39:5–6 (Yak. [KM] 7:19).

Hawana msamaha, wakiwa wamemkana Mwana wa Pekee, wakiwa wanamsulubisha kwa nafsi zao, **M&M** 76:30–35. Kufuru dhidi ya Roho Mtakatifu haitasamehewa, ambayo ni kumwaga damu isiyo na hatia baada ya kupokea agano langu jipya na lisilo na mwisho, **M&M** 132:26–27.

Dhamiri. *Ona pia* Nuru, Nuru ya Kristo

Hisia ya ndani kabisa ya sahihi na baya, inayokuja kutokana na Nuru ya Kristo katika wanadamu wote (Moro. 7:16). Tunazaliwa tukiwa na uwezo wa asili wa kutofautisha kati ya mema na mabaya kwa sababu ya Nuru ya Kristo ambayo hutolewa kwa kila mtu (M&M 84:46). Uwezo huu unaitwa dhamiri. Kuwa nayo ndiyo hutufanya sisi kuwa viumbe wenye kuwajibika. Kama uwezo mwingine, dhamiri zetu zaweza kudhoofishwa kwa njia ya dhambi au matumizi mabaya.

Wale waandishi na Mafarisayo walishtakiwa na dhamiri zao wenyewe, **Yn.** 8:9. Dhamiri yao ikiwashuhudia, **Rum.** 2:14–15. Waasi wamezichoma dhamiri zao kwa moto mkali, **1 Tim.** 4:2.

Wanadamu wanafundishwa vya kutosha ili wapate kujua mema na maovu, **2 Ne.** 2:5. Mfalme Benjamini alikuwa na dhamiri iliyo safi mbele za Mungu, **Mos.** 2:15. Wanefi walijawa na shangwe, wakiwa na amani katika dhamiri, **Mos.** 4:3. Zeezromu alihuzunishwa na dhamiri ya ufahamu wa hatia yake mwenyewe, **Alma** 14:6. Tunapewa shangwe au majuto ya dhamiri kulingana na tamaa zetu, **Alma** 29:5. Adhabu na sheria ya haki huleta majuto ya dhamiri, **Alma** 42:18. Roho ya Kristo hutolewa kwa kila mwanadamu ili apate kujua mema na maovu, **Moro.** 7:16.

Kila mtu yapaswa kupata uhuru wa kuitumia dhamiri yake, **M&M** 134:2. Nina dhamiri isiyokuwa na hatia, **M&M** 135:4.

Tunadai haki ya kumwabudu Mungu kulingana na mwongozo wa dhamiri zetu wenyewe, **M ya I** 1:11.

Dharau. *Ona* Chuki, Chukia

Dhiraa

Kipimo cha kawaida cha urefu miongoni mwa Waebrania—kwa asili ni urefu kutoka kiwiko cha mkono hadi ncha za vidole.

Dunia. *Ona pia* Ulimwengu; Umba, Uumbaji

Sayari ambayo juu yake tunaishi, iliumbwa na Mungu kwa njia ya Yesu Kristo ili itumiwe na mwanadamu wakati wa kuzaliwa katika mwili wenye kufa na kwa majaribio yake. Hatima yake ni kuwa iliyotukuzwa na kuinuliwa. (M&M 77:1–2; 130:8–9). Dunia itakuwa ni urithi wa milele wa wale walioishi wakistahili fahari ya selestia

(M&M 88:14–26). Watafurahia uwepo wa Baba na Mwana (M&M 76:62).

Iliumbwa kwa ajili ya mwanadamu: Mungu alimpa mwanadamu utawala juu ya dunia, **Mwa.** 1:28 (Musa 2:28). Dunia ni ya Bwana, **Ku.** 9:29 (Zab. 24:1). Bwana amewapa dunia wanadamu, **Zab.** 115:16. Mimi nimeiumba dunia na nimemtunuku mwanadamu juu yake, **Isa.** 45:12.

Kwa uwezo wa neno lake mwanadamu akaja juu ya dunia, **Yak. (KM)** 4:9.

Dunia itatolewa kwa wale waliomchukua Roho Mtakatifu kuwa kiongozi wao, **M&M** 45:56–58 (M&M 103:7). Wale ambao wameitii injili wanapokea ujira wa mambo mema ya dunia, **M&M** 59:3. Walio maskini na wapole wa dunia watairithi, **M&M** 88:17 (Mt. 5:5; 3 Ne. 12:5).

Sisi tutaifanya dunia, nasi tutawajaribu hao, **Ibr.** 3:24–25.

Kitu Kinachoishi: Dunia hukaa milele, **Mh.** 1:4.

Bahari ya kioo ni dunia katika hali yake ya kutakaswa, isiyokufa, na ya milele, **M&M** 77:1. Dunia lazima itakaswe na kuandaliwa kwa ajili ya utukufu wa selestia, **M&M** 88:18–19.

Dunia iliomboleza kwa sauti, **Musa** 7:48.

Kugawanywa kwa dunia: Maji na yakusanyike mahali pamoja, **Mwa.** 1:9. Katika siku za Pelegi dunia iligawanyika, **Mwa.** 10:25.

Baada ya maji kupungua, ikawa nchi teule, **Eth.** 13:2.

Dunia itakuwa kama ilivyokuwa kabla ya kugawanyika, **M&M** 133:24.

Kutakaswa kwa dunia: Mvua ikaanguka juu ya dunia kwa siku arobaini, **Mwa.** 7:4.

Dunia imewekwa akiba kwa moto hata siku ya hukumu, **2 Pet.** 3:7.

Baada ya leo kwaja kuungua, **M&M** 64:24.

Dunia yatamani kusafishwa kutokana na uchafu, **Musa** 7:48.

Hali ya mwisho ya dunia: Dunia itakunjwa pamoja kama karatasi na kupita, **3 Ne.** 26:3 (M&M 29:23). Patakuwepo na mbingu mpya na dunia mpya, **Eth.** 13:9 (M&M 29:23).

Bahari ya kioo ni dunia katika hali yake ya kutukaswa, kutokufa, na ya milele, **M&M** 77:1. Dunia lazima itakaswe na kuandaliwa kwa ajili ya fahari ya utukufu wa selestia, **M&M** 88:18–19. Dunia hii itafanywa kuwa mfano wa jiwe angavu nayo itakuwa Urimu na Thumimu, **M&M** 130:8–9.

Kwa miaka elfu moja dunia itapumzika, **Musa** 7:64. Dunia itafanywa upya, **M ya I** 1:10.

Edeni. *Ona pia* Adamu; Hawa

Nyumbani kwa wazazi wetu wa kwanza, Adamu, na Hawa (Mwa. 2:8–3:24; 4:16; 2 Ne. 2:19–25; Musa 3–4; Ibr. 5), Edeni ilitengenezwa kama bustani, nayo ilikuwa katika upande wa mashariki. Adamu na Hawa walitolewa nje ya Edeni baada ya kula tunda lililokatazwa na wakawa na miili yenye kufa (Musa 4:29). Ufunuo wa siku za mwisho unathibitisha maelezo ya biblia juu ya Bustani ya Edeni. Unaongezea taarifa muhimu kwamba bustani hiyo ilikuwa mahali ambako sasa ni bara la Marekani ya Kaskazini.

Efraimu. *Ona pia* Israeli; Kitabu cha Mormoni; Manase; Yusufu, Mwana wa Yakobo

Katika Agano la Kale, huyu ni mwana wa pili wa Yusufu na Asinathi (Mwa. 41:50–52; 46:20). Kinyume na taratibu za kimila, Efraimu alipokea baraka ya haki ya uzaliwa wa kwanza badala ya Manase, ambaye ndiye alikuwa mwana mkubwa (Mwa. 48:17–20). Efraimu akawa baba wa kabila la Efraimu.

Kabila la Efraimu: Efraimu alipewa haki ya uzaliwa wa kwanza katika Israeli (1 Nya. 5:1–2; Yer. 31:9). Katika siku za mwisho nafasi yao na wajibu wao ni kuushikilia ukuhani, kupeleka ujumbe wa injili ya urejesho kwa ulimwengu, na kuipeperusha bendera ili kuwakusanya Israeli waliotawanyika

(Isa. 11:12–13; 2 Ne. 21:12–13). Watoto wa Efraimu watawavisha taji pamoja na utukufu wale watokao nchi za kaskazini wanaorejea katika siku za mwisho (M&M 133:26–34).

Kijiti cha Efraimu au Yusufu: Historia ya kikundi kimoja kutoka kabila la Efraimu ambacho kiliongozwa kutoka Yerusalemu hadi Marekani karibu miaka 600 K.K. Historia ya kikundi hiki inaitwa kijiti cha Efraimu au Yusufu au Kitabu cha Mormoni. Hiki na kijiti cha Yuda (Biblia) huunda ushuhuda wa pamoja wa Bwana Yesu Kristo, Ufufuko Wake, na kazi Yake takatifu miongoni mwa sehemu hizi mbili za nyumba ya Israeli.

Tawi la Efraimu litajitenga na litaandika ushuhuda mwingine wa Kristo, **TJS, Mwa.** 50:24–26, 30–31. Kijiti cha Yuda na Kijiti cha Yusufu vitakuwa kimoja, **Eze.** 37:15–19.

Maandiko ya Yuda na ya Yusufu yatakua pamoja, **2 Ne.** 3:12. Bwana hunena kwa mataifa mengi, **2 Ne.** 29.

Funguo za historia ya kijiti cha Efraimu zilikabidhiwa kwa Moroni, **M&M** 27:5.

Egipto

Jina la wote mke na binti wa Hamu, mwana wa Nuhu. Kwa Kikaldayo, jina hili linasimama badala ya "Misri", au "kile kilichokatazwa" (Ibr. 1:23–25).

Eli. *Ona pia* Samweli, Nabii wa Agano la Kale

Kuhani mkuu na mwamuzi katika Agano la Kale wakati Bwana alipomwita Samweli kuwa nabii (1 Sam. 3). Bwana alimkemea kwa sababu ya kuachilia uovu wa wanae (1 Sam. 2:22–36; 3:13).

Elia. *Ona pia* Eliya

Kuna matumizi kadha wa kadha ya jina hili au cheo cha Elia katika Maandiko:

Eliya: Elia ni mtindo wa Agano Jipya (Kiyunani) ya Eliya (Kiebrania), kama katika Mt. 17:3–4, Lk. 4:25–26, na Yak. (Bib.) 5:17. Katika matukio haya, Elia alikuwa ndiye nabii wa kale Eliya ambaye huduma yake imeandikwa katika Wafalme 1 na 2.

Mtangulizi: Elia pia ni cheo cha mtu aliye mtangulizi. Kwa mfano, Yohana Mbatizaji alikuwa Elia, kwa sababu yeye alitumwa kuitengeneza njia kwa ajili ya Yesu (Mt. 17:12–13).

Mrejeshaji: Cheo cha Elia pia kimetumiwa kwa wengine ambao walikuwa na kazi maalumu ya kutimiza, kama vile Yohana Mfunuzi (M&M 77:14) na Gabrieli (Lk. 1:11–20; M&M 27:6–7; 110:12).

Mtu aliyekuwa katika kipindi cha Ibrahimu: Nabii aliyeitwa Esaiya au Elia ambaye ni dhahiri aliishi katika siku za Ibrahimu (M&M 84:11–13; 110:12).

Elisabeti. *Ona pia* Yohana Mbatizaji

Katika Agano Jipya, ni mke wa Zakaria, mama yake Yohana Mbatizaji, na jamaa wa kike wa Maria (Lk. 1:5–60).

Elisha

Nabii wa Agano la Kale wa ufalme wa Kaskazini wa Israeli na mshauri wa kuaminika wa wafalme kadhaa wa nchi hiyo.

Elisha alikuwa na tabia ya upole na mwenye moyo wa kupenda, pasipo ari ya moto mkali ambayo bwana wake, Eliya, walitofautiana. Miujiza yake yenye kutambulika (2 Fal. 2–5; 8) inashuhudia kwamba hakika alipokea nguvu za Eliya wakati yeye alipomrithi Eliya kama nabii (2 Fal. 2:9–12). Kwa mfano, aliyaponya maji ya chemchemi ya maji machungu, aliyagawanya maji ya Mto Yordani, alizidisha mafuta ya mjane, alimfufua mvulana kutoka kwa wafu, alimponya mtu wa ukoma, alisababisha shoka la chuma kuelea majini, na akawapiga Washuri kwa upofu (2 Fal. 2–6). Huduma yake ilidumu kwa zaidi ya miaka hamsini wakati wa utawala wa Yehoramu, Yehu, Yohoahazi, na Yoashi.

Alipokea vazi la Eliya, **2 Fal.** 2:13. Alizidisha mafuta ya mjane, **2 Fal.** 4:1–7. Alimfufua kutoka kwa wafu mvulana

wa mwanamke Mshunami, **2 Fal.** 4:18–37. Alimponya Naamani, Mshamu, **2 Fal.** 5:1–14. Aliwapofusha askari wa Shamu, na macho ya mtumishi wake yakafunguliwa, **2 Fal.** 6:8–23.

Eliya. *Ona pia* Elia; Kufunga, Muhuri, Tia; Wokovu

Nabii katika Agano la Kale ambaye alirudi katika siku za mwisho kuwatunukia funguo za uwezo wa kufunga Joseph Smith na Oliver Cowdery. Katika siku zake, Eliya alihudumu katika Ufalme wa Kaskazini wa Israeli (1 Fal. 17–22; 2 Fal. 1–2). Alikuwa na imani kuu katika Bwana na anajulikana kwa ajili ya miujiza mingi. Kutokana na maombi yake, Mungu aliizuia mvua kwa miaka mitatu 3½. Alimfufua mvulana kutoka kwa wafu na aliita moto kutoka mbinguni (1 Fal. 17–18). Watu wa Uyahudi bado wanasubiri kuja kwa Eliya, kama Malaki alivyotoa unabii kuwa angekuja (Mal. 4:5). Yeye anabakia mgeni mwalikwa katika Karamu ya Pasaka ya Kiyahudi, ambapo mlango ulio wazi na kiti kikiwa wazi daima vikimsubiri yeye.

Joseph Smith Nabii alisema kwamba Eliya alishikilia nguvu za kufunga za ukuhani wa Melkizedeki na alikuwa nabii wa mwisho kufanya hivyo kabla ya wakati wa Yesu Kristo. Yeye alionekana juu ya Mlima wa Kugeuka Sura pamoja na Musa na wakaweka funguo za ukuhani huo juu ya Petro, Yakobo, na Yohana (Mt. 17:3). Alionekana tena pamoja na Musa na wengine mnamo 3 Aprili 1836, katika Hekalu la Kirtland Ohio na akatunukia funguo hizo hizo juu ya Joseph Smith na Oliver Cowdery (M&M 110:13–16). Hii yote ilikuwa katika maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Bwana, kama ilivyonenwa katika Malaki 4:5–6.

Uwezo wa Eliya ni uwezo wa kufunga wa ukuhani ambao kwa huo mambo ambayo yanafungwa au kufunguliwa duniani hufungwa au kufunguliwa mbinguni (M&M 128:8–18). Watumishi wateule wa Bwana walio duniani leo wanao uwezo huu wa kufunga na kufanya ibada za injili zenye kuokoa kwa ajili ya walio wazima na wafu (M&M 128:8).

Akazifunga mbingu na akalishwa na kunguru, **1 Fal.** 17:1–7. Akaamuru pipa la unga la mjane na chupa ya mafuta yasiishe, **1 Fal.** 17:8–16. Akamfufua mwana wa mjane kutoka katika mauti, **1 Fal.** 17:17–24. Aliwashinda makuhani wa Baali, **1 Fal.** 18:21–39. Sauti ndogo tulivu ikasema naye, **1 Fal.** 19:11–12. Alipaa mbinguni katika gari la moto, **2 Fal.** 2:11. Malaki alitoa unabii juu ya kurudi kwake katika siku za mwisho, **Mal.** 4:5–6 (3 Ne. 25:5).

Alionekana katika Hekalu la Kirtland katika mwaka 1836, **M&M** 110:13–16.

Elohimu. *Ona* Baba wa Mbinguni; Mungu, Uungu

Emanueli. *Ona* Imanueli

Endaomenti. *Ona pia* Hekalu, Nyumba ya Bwana

Katika maana ya ujumla, ni kipawa cha uwezo kutoka kwa Mungu. Waumini wa Kanisa wenye kustahili wanaweza kupokea kipawa cha uwezo kwa njia ya ibada katika hekalu ambayo huwapa wao mafundisho na maagano ya Ukuhani Mtakatifu ambayo wao huhitaji ili waweze kupata kuinuliwa. Endaomenti hii hujumuisha mafundisho juu ya mpango wa wokovu.

Humo mtavikwa uwezo utokao juu, **M&M** 38:32, 38 (Lk. 24:49; M&M 43:16). Jengeni nyumba, ambamo ndani yake ninapanga kuwapa endaomenti wale ambao nimewachagua, **M&M** 95:8. Nimetayarisha endaomenti na baraka iliyo kuu, **M&M** 105:12, 18, 33. Wengi watafurahi kwa sababu ya endaomenti ambayo watumishi wangu wamevikwa, **M&M** 110:9. Utukufu, heshima, na endaomenti hutawazwa kwa ibada ya nyumba yangu takatifu, **M&M** 124:39. Wale walioitwa na Baba, kama alivyoitwa Haruni, hupewa endaomenti kwa funguo za ukuhani, **M&M** 132:59.

Enoshi, Mwana wa Yakobo

Nabii Mnefi na mtunza kumbukumbu katika Kitabu cha Mormoni ambaye alisali na kupata msamaha wa dhambi zake kwa njia ya imani yake katika Kristo (Eno. 1:1–8). Bwana aliagana na Enoshi kukitoa Kitabu cha Mormoni kwa Walamani (Eno. 1:15–17).

Kitabu cha Enoshi: Ni kitabu katika Kitabu cha Mormoni ambacho huzungumzia juu ya sala ya Enoshi kwa Bwana kwa ajili ya msamaha wa kibinafsi, kwa ajili ya watu wake, na kwa ajili ya wengine. Bwana akamwahidi kwamba Kitabu cha Mormoni kingehifadhiwa na kitolewe kwa Walamani katika siku zijazo. Ingawa kitabu hicho kuna mlango moja pekee, kinaandika hadithi yenye nguvu ya mtu ambaye alimtafuta Mungu wake katika sala, aliishi kwa kutii amri za Mungu, na kabla ya kifo chake alifurahia katika kumjua kwake Mkombozi.

Esau. *Ona pia* Isaka; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mwana mkubwa wa Isaka na Rebeka na kaka pacha wa Yakobo. Kaka hawa wawili walikuwa wapinzani tangu kuzaliwa kwao (Mwa. 25:19–26). Wazao wa Esau, ni Waedomu, na wazao wa Yakobo ni Waisraeli, wakawa mataifa pinzani (Mwa. 25:23).

Esau aliuza haki yake ya uzaliwa wa kwanza kwa Yakobo, **Mwa.** 25:33 (Ebr. 12:16–17). Esau akaoa wake wa Kihita na kusababisha uchungu kwa wazazi wake, **Mwa.** 26:34–35. Yakobo na Esau wakapatanishwa, **Mwa.** 33.

Esaya

Muundo wa jina la Isaya katika Agano Jipya (Kiyunani) (Lk. 4:17). Esaya alikuwa nabii aliyeishi katika siku za Ibrahimu (M&M 76:100; 84:13).

Esta

Mwanamke wa imani kuu na mhusika mkuu katika kitabu cha Esta.

Kitabu cha Esta: Kitabu kilichoko katika Agano la Kale ambacho kina hadithi ya ujasiri mkuu wa Malkia Esta katika kuwaokoa watu wake kutokana na angamizo.

Mlango wa 1–2 hutuambia namna Esta, mwanamke wa Kiyahudi na binti wa kupanga wa mwanamume wa Kiyahudi aliyeitwa Mordekai, alichaguliwa kuwa Malkia wa Uajemi kwa sababu ya urembo wake. Mlango wa 3 unaelezea kwamba Hamani; kiongozi katika baraza la mfalme, alimchukia Mordekai na akafaulu kupata agizo kutoka kwa mfalme ya kuuawa kwa watu walio Wayahudi wote. Mlango wa 4–10 inaelezea namna Esta, kwa hatari kubwa ya maisha yake, aliifichua asili yake mwenyewe kwa mfalme na akafaulu kubadilisha agizo hilo.

Etheri. *Ona pia* Wayaredi

Nabii wa mwisho wa Wayaredi katika kitabu cha Mormoni (Eth. 12:1–2).

Kitabu cha Etheri: Kitabu katika Kitabu cha Mormoni ambacho kina sehemu za kumbukumbu ya Wayaredi. Wayaredi walikuwa ni kikundi cha watu walioishi katika dunia ya magharibi karne nyingi zilizopita kabla ya watu wa Lehi. Kitabu cha Etheri kilichukuliwa kutoka katika mabamba ishirini na manne yaliyogunduliwa na watu wa Limhi (Mos. 8:8–9).

Mlango wa 1–2 inaeleza namna Wayaredi walivyoacha nyumba zao wakati wa Mnara wa Babeli na kuanza safari yao kwenda mahali ambako sasa kunajulikana kama bara la Marekani. Mlango wa 3–6 inaeleza kwamba kaka wa Yaredi alimwona Mwokozi kabla hajazaliwa na kwamba Wayaredi walisafiri katika boti nane. Mlango wa 7–11 inaendeleza historia ya uovu ambao ulitawala kiasi kikubwa cha historia ya Wayaredi. Moroni ambaye alihariri kumbukumbu ya Etheri, aliandika katika mlango wa 12–13 juu ya maajabu yaliyofanywa kwa imani na juu ya Kristo na Yerusalemu Mpya ijayo. Mlango wa 14–15 inaelezea jinsi Wayaredi walivyokuja kuwa taifa

lenye nguvu lakini likaangamizwa kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe kwa sababu ya uovu.

Ezekieli

Nabii aliyeandika kitabu cha Ezekieli katika Agano la Kale. Yeye alikuwa kuhani katika familia ya Sadoki na ni mmoja wa mateka wa Kiyahudi waliohamishwa na Nebukadneza. Aliishi pamoja na wakimbizi wa Kiyahudi katika Babilonia na alitoa unabii katika kipindi cha miaka ishirini na miwili, tangu mwaka 592 hadi mwaka 570 K.K.

Kitabu cha Ezekieli: Kitabu cha Ezekieli chaweza kugawanywa katika mafungu manne. Mlango wa 1–3 inaelezea juu ya Ono la Mungu na wito wa Ezekieli wa kuhudumu; mlango wa 4–24 inanena juu ya hukumu za Yerusalemu na sababu ya kutolewa kwake; mlango wa 25–32 inatangaza hukumu juu ya mataifa; na mlango wa 33–48 imeandikwa maono ya Israeli ya siku za mwisho.

Ezra

Kuhani na mwandishi katika Agano la Kale ambaye aliwarejesha Yerusalemu baadhi ya Wayahudi kutoka utumwa wa Babilonia (Ezra 7–10; Neh. 8; 12). Katika mwaka 458 K.K. alipata ruhusa kutoka kwa Artashasta, mfalme wa Uajemi kuwapeleka Yerusalemu mkimbizi yeyote wa Kiyahudi aliyetaka kwenda (Ezra 7:12–26).

Kabla ya wakati wa Ezra, makuhani walikuwa na udhibiti kamili juu ya kusoma mkusanyiko wa maandiko yaliyoandikwa yaliyoitwa "sheria." Ezra alisaidia kufanya maandiko yapatikane kwa kila Myahudi. Usomaji wa umma wa "kitabu cha sheria" hatimaye ukawa ni sehemu muhimu ya maisha ya taifa la Kiyahudi. Pengine mafundisho makubwa zaidi ya Ezra yalikuja kutokana na mfano wake yeye mwenyewe wa kuutayarisha moyo wake kwa kutafuta sheria za Bwana, kuzitii, na kuifundisha kwa wengine (Ezra 7:10).

Kitabu cha Ezra: Mlango wa 1–6 inaelezea matukio ambayo yalitokea kutoka miaka sitini hadi themanini kabla Ezra hajafika katika Yerusalemu—agizo la Koreshi katika mwaka 537 K.K. na kurejea kwa Wayahudi chini ya Zerubabeli. Mlango wa 7–10 inaonyesha namna Ezra alivyokwenda Yerusalemu. Yeye, pamoja na kikundi chake, walifunga na kusali kwa ajili ya kupata ulinzi. Huko Yerusalemu waliwakuta watu Wayahudi wengi waliokuwa wamekwenda Yerusalemu mapema chini ya Zerubabeli na walikuwa wameoa wanawake nje ya agano na hivyo kujichafua wenyewe. Ezra akawaombea na akawaweka chini ya agano la kuwataliki wake zao wale. Historia ya mwisho ya Ezra inapatikana katika kitabu cha Nehemia.

Familia. *Ona pia* Baba, Mwili wenye kufa; Mama; Mtoto; Watoto; Ndoa, Oa, Olewa

Kama linavyotumika katika maandiko, familia ndani yake kuna mume na mke, watoto, na wakati mwingine jamaa wengine wanaoishi katika nyumba moja au chini ya kiongozi mmoja wa familia. Familia pia yaweza kuwa ya mzazi mmoja pamoja na watoto, mume na mke bila watoto, au hata mtu mmoja aishiye peke yake.

Kwa ujumla: Katika wewe jamaa zote za duniani zitabarikiwa, **Mwa.** 12:3 (Mwa. 28:14; Ibr. 2:11). Nitakuwa Mungu wa familia zote za Israeli, **Yer.** 31:1.

Familia zote mbinguni na duniani zaitwa ni za Baba, **Efe.** 3:14–15.

Adamu na Hawa wamezaa familia yote ya duniani, **2 Ne.** 2:20.

Utukufu wako utakuwa kuendelea kwa uzao wako milele, **M&M** 132:19. Nitampa taji la uzawa wa milele katika dunia za milele, **M&M** 132:55. Kufunganishwa kwa watoto kwa wazazi ni sehemu ya kazi kuu ya utimilifu wa nyakati, **M&M** 138:48.

Mwana mume na mwanamke niliwaumba, na nikawaambia: Zaeni na mkaongezeke, **Musa** 2:27–28. Si vyema

kwa mtu huyo kuwa pekee yake, **Musa** 3:18. Adamu na Hawa walifanya kazi pamoja, **Musa** 5:1.

Wajibu wa wazazi: Ibrahimu atawaamuru watoto wake, nao wataishika njia ya Bwana, **Mwa.** 18:17–19. Nawe uwafundishe watoto wako maneno haya kwa bidii, **Kum.** 6:7 (Kum. 11:19). Yeye ampendaye mwanawe humrudi, **Mit.** 13:24 (Mit. 23:13). Mlee mtoto katika njia impasayo, **Mit.** 22:6. Uishi kwa furaha pamoja na mke umpendaye, **Mh.** 9:9. Watoto wako watafundishwa na Bwana, **Isa.** 54:13 (3 Ne. 22:13).

Waleeni katika malezi ya Bwana, **Efe.** 6:1–4 (Eno. 1:1). Kama mtu yeyote hawatunzi walio wake, ameikana imani, **1 Tim.** 5:8.

Aliwasihi kwa huruma zote za mzazi mwenye upendo, **1 Ne.** 8:37. Tunazungumza juu ya Kristo ili watoto wetu wapate kujua chanzo kipi wapate kukitazamia, **2 Ne.** 25:26. Waume zao na wake zao wanawapenda watoto wao, **Yak. (KM)** 3:7. Wafundisheni kupendana na kutumikiana, **Mos.** 4:14–15. Mtazilinda familia zenu hata kwa kumwaga damu, **Alma** 43:47. Salini katika familia zenu ili wake zenu na watoto wenu wapate kubarikiwa, **3 Ne.** 18:21.

Wazazi watafundisha injili kwa watoto wao, **M&M** 68:25. Kila mtu analazimika kutunza familia yake yeye mwenyewe, **M&M** 75:28. Watoto wote wanayo haki ya madai juu ya wazazi wao, **M&M** 83:4. Waleeni watoto wenu katika nuru na kweli, **M&M** 93:40. Iweke sawa nyumba yako wewe mwenyewe, **M&M** 93:43–44, 50. Makuhani yawapasa tu kuwashawishi wengine kwa upendo usio na unafiki, **M&M** 121:41.

Adamu na Hawa waliwajulisha watoto wao mambo yote, **Musa** 5:12.

Wajibu wa mtoto: Waheshimu baba yako na mama yako, **Ku.** 20:12. Mwanangu, sikiliza mafundisho ya baba yako, **Mit.** 1:8 (Mit. 13:1; 23:22).

Yesu alikuwa chini ya wazazi wake, **Lk.** 2:51. Yesu alifanya mapenzi ya baba yake, **Yn.** 6:38 (3 Ne. 27:13). Watiini wazazi wenu katika Bwana, **Efe.** 6:1 (Kol. 3:20).

Kama watoto watatubu, hasira yako itakoma, **M&M** 98:45–48. Mabinti waaminifu wa Hawa walimwabudu Mungu wa kweli aliye hai, **M&M** 138:38–39.

Familia ya milele: Mafundisho na Maagano yanaelezea asili ya umilele wa uhusiano wa ndoa na familia. Ndoa ya selestia na uendelezo wa familia unawawezesha waume na wake kuwa miungu (M&M 132:15–20).

Fanywa Upya, Urejesho. *Ona pia* Urejesho wa Injili

Kurudi kwa kitu au hali ambayo iliondolewa au kupotea.

Roho na mwili vitaungana tena katika umbile lake kamilifu, **Alma** 11:43–44. Urejesho ni kuurudisha uovu kwa uovu, haki kwa haki, **Alma** 41:10–15.

Tunaamini katika urejesho wa Makabila Kumi na Mawili na kwamba dunia itafanywa upya na kupokea utukufu wake wa kiparadiso, **M ya I** 1:10 (M&M 133:23–24).

Farao. *Ona pia* Egipto; Misri

Mwana mkubwa wa Egipto, binti wa Hamu (Ibr. 1:25). Pia, ni jina walilopewa wafalme wa Misri (Ibr. 1:27).

Fayette, New York (Marekani)

Eneo la shamba lililomilikiwa na Peter Whitmer Mkubwa, mahali ambapo mafunuo mengi yalitolewa kwa Joseph Smith Nabii Mdogo. Hapo ndipo mahali Kanisa lilipoanzishwa mnamo 6 Aprili 1830 na sauti ya Bwana ilisikika (M&M 128:20).

Fedha. *Ona pia* Lipa zaka, Zaka; Malimwengu; Sadaka, Utoaji sadaka; Ukwasi

Sarafu, noti, hati, au kitu fulani ambacho watu hutumia kama malipo kwa ajili ya bidhaa au huduma. Wakati mwingine ni ishara ya tamaa ya vitu au anasa.

Nanyi mtakombolewa bila fedha, **Isa.** 52:3.

Wale Kumi na Wawili waliambiwa wasichukue chochote kwa ajili ya safari yao, si mkoba, si mkate, wala fedha, **Mk.** 6:8. Petro alimwambia Simoni mchawi ya kwamba pesa zake zingepotelea mbali pamoja naye, **Mdo.** 8:20. Kupenda fedha ndiyo shina la uovu wote, **1 Tim.** 6:10.

Msitumie fedha kwa yale yasiyo na thamani, **2 Ne.** 9:50–51 (Isa. 55:1–2; 2 Ne. 26:25–27). Kama watafanya kazi kwa ajili ya fedha, wataangamia, **2 Ne.** 26:31. Kabla ya kutafuta utajiri, utafuteni ufalme wa Mungu, **Yak. (KM)** 2:18–19. Makanisa yatasema kwamba kwa fedha zako utasamehewa dhambi zako, **Morm.** 8:32, 37.

Yule awapaye fedha zake kwa ajili ya kusudi la sayuni kwa vyovyote vile hatapoteza thawabu yake, **M&M** 84:89–90.

Filemoni. *Ona pia* Paulo

Mkristo katika Agano Jipya aliyekuwa akimiliki mtumwa Onesimo, aliyetoroka na kuungana na Paulo. Paulo alimrudisha tena Onesimo kwa Filemoni pamoja na barua akimwomba Filemoni amsamehe yule mtumwa.

Filemoni, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo

Kitabu katika Agano Jipya, kilichochukuliwa kutoka katika barua iliyoandikwa na Paulo. Barua ya Paulo kwa Filemoni ni barua binafsi juu ya Onesimo, mtumwa aliyemwibia Bwana wake, Filemoni, na akatorokea Roma. Paulo alimrudisha tena kwa Bwana wake huko Kolosai akiwa pamoja na Tikiko, aliyebeba barua ya Paulo kwa Wakolosai. Paulo aliomba kwamba Onesmo asamehewe na kupokelewa tena kama Mkristo mwenzao. Paulo aliandika barua hii wakati akiwa gerezani Roma kwa mara ya kwanza.

Filipo

Katika Agano Jipya, Filipo, wa Bethsaida, alikuwa mmoja wa Mitume Kumi na Wawili wa mwanzo wa Mwokozi (Mt. 10:2–4; Yn. 1:43–45).

Filipo mwingine alikuwa mmoja wa watu saba waliochaguliwa kuwasaidia Mitume Kumi na Wawili (Mdo. 6:2–6). Alihubiri katika Samaria na kwa towashi wa Ethiopia (Mdo. 8).

Fundisha, Mwalimu. *Ona pia* Roho Mtakatifu

Kutoa maarifa kwa wengine, hususani juu ya kweli za injili, na kuwaongoza katika uadilifu. Watu wanaofundisha injili yawapasa kuongozwa na Roho. Wazazi wote ni walimu ndani ya familia zao wenyewe. Watakatifu wanapaswa kuomba na kuwa radhi kukubali mafundisho kutoka kwa Bwana na viongozi Wake.

Uyafundishe kwa wana wako, **Kum.** 4:8–9. Wewe uwafundishe watoto wako kwa bidii, **Kum.** 6:7 (Kum. 11:18–19). Mlee mtoto katika njia impasayo kwenda, **Mit.** 22:6. Watoto wako watafundishwa na Bwana, **Isa.** 54:13 (3 Ne. 22:13).

Twajua ya kuwa yu mwalimu kutoka kwa Mungu, **Yn.** 3:2. Basi wewe umfundishaye mwingine, je, hujifundishi mwenyewe, **Rum.** 2:21.

Nilikuwa nimefundishwa kiasi fulani katika mafundisho yote ya baba yangu, **1 Ne.** 1:1 (Eno. 1:1). Makuhani na walimu lazima wafundishe kwa bidii au wajibu dhambi za watu juu ya vichwa vyao, **Yak. (KM)** 1:18–19. Nisikilizeni, na mfungue masikio yenu, **Mos.** 2:9. Mtawafundisha watoto wenu kupendana na kutumikiana, **Mos.** 4:15. Msimwamini yeyote kuwa mwalimu wenu isipokuwa amekuwa mtu wa Mungu, **Mos.** 23:14. Bwana aliimwaga roho yake juu ya nchi yote ili kuitayarisha mioyo yao kulipokea neno, **Alma** 16:16. Walifundisha kwa nguvu na mamlaka ya Mungu, **Alma** 17:2–3. Walikuwa wamefundishwa na mama zao, **Alma** 56:47 (Alma 57:21).

Kadiri watakavyoitafuta hekima waweze kuelekezwa, **M&M** 1:26. Fundishaneni kulingana na ofisi ambayo ninawateua, **M&M** 38:23. Fundisha kanuni za injili yangu, ambazo zimo katika

Biblia na Kitabu cha Mormoni, **M&M** 42:12. Mtafundishwa kutoka juu, **M&M** 43:15–16. Wazazi watawafundisha watoto wao, **M&M** 68:25–28. Fundishaneni mafundisho ya ufalme, **M&M** 88:77–78, 118. Chagueni miongoni mwenu mwalimu, **M&M** 88:122. Hujawafundisha watoto wako nuru na kweli, na hii ndiyo chanzo cha mateso yako, **M&M** 93:39–42.

Yafundishe bure mambo haya kwa watoto wako, **Musa** 6:57–61.

Kufundisha kwa Roho: Si ninyi msemao, bali ni Roho asemaye ndani yenu, **Mt.** 10:19–20. Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu wakati alipotufungulia maandiko, **Lk.** 24:32. Injili inahubiriwa kwa uwezo wa Roho, **1 Kor.** 2:1–14.

Alinena kwa uwezo na mamlaka kutoka kwa Mungu, **Mos.** 13:5–9 (Alma 17:3; Hel. 5:17).

Utapata Roho wangu kwa kuwashawishi wanadamu, **M&M** 11:21. Wewe utasikilizwa katika mambo yote utakayofundisha kwa uwezo wa Mfariji, **M&M** 28:1 (M&M 52:9). Kama hamtampokea Roho, msifundishe, **M&M** 42:14 (M&M 42:6). Wafundisheni watoto wa watu mambo haya kwa uwezo wa Roho wangu, **M&M** 43:15. Wazee watahubiri injili kwa uwezo wa Roho, **M&M** 50:13–22. Mtapewa katika saa ile ile mtakayosema, **M&M** 84:85 (M&M 100:5–8).

Funga, Kufunga. *Ona pia* Maskini; Sadaka, Utoaji sadaka; Ustawi

Kwa hiari kuacha kula au kunywa kwa madhumuni ya kujisogeza karibu na Bwana na kuomba baraka Zake. Wakati mtu binafsi na vikundi wafungapo, wanapaswa pia kusali ili kuyafahamu mapenzi ya Mungu na kukuza nguvu kubwa zaidi za kiroho. Kufunga daima kumekuwa kukifanywa na waumini wa kweli.

Katika Kanisa leo, siku moja ya Sabato kila mwezi imetengwa kwa madhumuni ya kufunga. Katika wakati huu, waumini wa Kanisa wanaacha kula chakula na kunywa maji kwa kipindi fulani. Kisha wao huchangia katika Kanisa fedha ambazo wao wangelizitumia kwa chakula kwa milo hiyo. Fedha hizi huitwa toleo la mfungo. Kanisa hutumia toleo hili la mfungo kwa kuwasaidia maskini na wenye shida.

Tulifunga na kumwomba Mungu wetu, **Ezra** 8:21–23, 31. Nilifunga na kusali mbele za Mungu wa mbinguni, **Neh.** 1:4. Mkafunge kwa ajili yangu, msile wala kunywa kwa muda wa siku tatu, **Esta** 4:16. Niliinyenyekeza nafsi yangu kwa kufunga, **Zab.** 35:13. Je, saumu niliyoichagua siyo hii, **Isa.** 58:3–12. Nikauelekeza uso wangu kwa Bwana Mungu, ili kuomba kwa sala, kwa kufunga, **Dan.** 9:3. Nirudieni mimi kwa moyo wenu wote, na kwa kufunga, **Yoe.** 2:12. Ninawi wakamsadiki Mungu, na wakatangaza kufunga, **Yon.** 3:5.

Yesu alifunga kwa muda wa siku arobaini, **Mt.** 4:2 (Ku. 34:28; 1 Fal. 19:8; Lk. 4:1–2). Usionekane kwa watu kuwa unafunga, **Mt.** 6:18 (3 Ne. 13:16). Wa namna hii haitoki ila kwa kusali na kufunga, **Mt.** 17:21.

Dumuni katika kufunga na kusali, **Omni** 1:26 (4 Ne. 1:12). Wakaanza kufunga, na kusali kwa Bwana Mungu wao, **Mos.** 27:22. Nimefunga na kusali kwa siku nyingi ili nipate kujua mambo haya, **Alma** 5:46. Watoto wa Mungu wakajiunga katika kufunga na kusali kwa nguvu, **Alma** 6:6. Wana wa Mosia wakajitolea wenyewe kwa kusali na kufunga sana, **Alma** 17:3, 9. Wakati wa kufunga na wa sala ulifuatia mauti ya Wanefi wengi, **Alma** 28:5–6. Walifunga sana na kusali sana, **Alma** 45:1 (Hel. 3:35).

Na chakula chako kiandaliwe kwa moyo mmoja ili kufunga kwako kupate kukamilika, **M&M** 59:13–14. Mtadumu katika sala na kufunga, **M&M** 88:76.

Funguo za Ukuhani. *Ona pia* Kipindi; Ukuhani; Urais wa Kwanza

Funguo ni haki za urais, au uwezo unaotolewa kwa mtu na Mungu ili kuongoza, kudhibiti, au kutawala ukuhani wa Mungu duniani. Watu wenye

ukuhani walioitwa katika nafasi za urais hupokea funguo kutoka kwa wale walio na mamlaka juu yao. Watu wenye ukuhani huutumia ukuhani huo ndani tu ya mipaka iliyowekwa na wale wanaoshikilia funguo hizo. Rais wa Kanisa ndiye mtu pekee ambaye anashikilia na anaye ruhusiwa kutumia funguo zote za ukuhani (M&M 107:65–67, 91–92; 132:7).

Petro alipokea funguo za ufalme, **Mt.** 16:19.

Mikaeli (Adamu) alipokea funguo za wokovu chini ya maelekezo ya Yesu Kristo, **M&M** 78:16. Funguo za ufalme daima ni mali ya Urais wa Kwanza, **M&M** 81:2. Ukuhani wa Melkizedeki hushikilia funguo ya siri za ufahamu wa Mungu, **M&M** 84:19. Funguo maalumu zinashikiliwa na Mitume Kumi na Wawili, **M&M** 107:35; 112:16, 32; 124:128. Joseph Smith na Oliver Cowdery walipokea funguo juu ya kukusanyika kwa Israeli, injili ya Ibrahimu, na za uwezo wa kufunga, **M&M** 110:11–16. Urais wa Kwanza na wale Kumi na Wawili wanashikilia funguo za kipindi cha utimilifu wa nyakati, **M&M** 112:30–34. Maofisa katika ukuhani hushika funguo, **M&M** 124:123. Mtu aliye na funguo anaweza kupata maarifa, **M&M** 128:11.

Ukuhani wa Haruni hushikilia funguo za kupokea huduma ya malaika na ya injili ya toba na ubatizo, **JS—H** 1:69 (M&M 13).

Gabrieli. *Ona pia* Malaika; Maria, Mama wa Yesu; Nuhu, Patriaki wa Biblia

Malaika aliyetumwa kwa Danieli (Dan. 8:16; 9:21), Zakaria (Lk. 1:11–19; M&M 27:7), Maria (Lk. 1:26–38), na wengine (M&M 128:21). Joseph Smith Nabii alionyesha kwamba Gabrieli ni nabii Nuhu wa Agano la Kale.

Gadhabu. *Ona* Hasira

Gadi, Mwana wa Yakobo. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Yakobo na Zilpa (Mwa. 30:10–11). Wazao wake wakawa kabila la Israeli.

Kabila la Gadi: Kwa ajili ya baraka za Yakobo juu ya mwanawe Gadi, ona Mwanzo 49:19. Kwa ajili ya baraka za Musa juu ya kabila la Gadi, ona Kumbukumbu la Torati 33:20–21. Kulingana na baraka hizi, wazao wa Gadi walikuwa wawe watu wa vita. Ardhi iliyogawiwa kwao katika nchi ya Kanaani ilikuwa mashariki ya Mto Yordani nayo ilikuwa nchi ya malisho mazuri na yenye maji mengi.

Gadi Mwonaji. *Ona pia* Maandiko—Maandiko yaliyopotea

Nabii na rafiki mwaminifu na mshauri wa Daudi katika Agano la Kale (1 Sam. 22:5; 2 Sam. 24:11–19). Yeye aliandika kitabu cha matendo ya Daudi, ambacho kimekuwa maandiko yaliyopotea (1 Nya. 29:29).

Galilaya

Katika nyakati za zamani na za kisasa hii ni wilaya ya kaskazini kabisa ya Israeli magharibi ya Mto Yordani na bahari ya Galilaya. Galilaya ina ukubwa upatao maili sitini (kilometa tisini na saba) urefu wa maili thelathini (kilometa arobaini na nane) upana. Hapo zamani ilikuwa na ardhi iliyokuwa bora na miji iliyokuwa na shughuli nyingi zaidi katika Israeli. Barabara kubwa muhimu zinazoelekea Dameski, Misri, na Israeli ya mashariki zilipitia Galilaya. Hali yake ya hewa nzuri na udongo wenye rutuba ilizaa mazao mengi ya mizeituni, ngano, shayiri, na zabibu. Uvuvi katika bahari ya Galilaya ulitoa biashara kubwa ya kusafirisha nje ya nchi na ilikuwa ni chanzo kikubwa cha utajiri. Mwokozi alitumia muda wake mwingi katika Galilaya.

Nuru kuu itaangaza katika Galilaya, **Isa.** 9:1–3 (2 Ne. 19:1–3).

Yesu alikuwa akizunguka katika Galilaya yote, akihubiri, akifundisha, na kuponya, **Mt.** 4:23. Baada ya kufufuka, Yesu alionekana katika Galilaya, **Mk.** 14:28 (Yn. 21:1–14). Habari za Yesu

zikaenea kote Galilaya, **Lk.** 4:14. Yesu alianza kufanya miujiza yake katika Kana ya Galilaya, **Yn.** 2:11.

Bahari ya Galilaya: Bahari ya Galilaya iko katika Israeli ya kaskazini. Pia katika Agano la Kale ilikuwa ikiitwa Bahari ya Kinerethi na Ziwa la Genesareti au Tiberia katika Agano Jipya. Yesu alifundisha mahubiri kadhaa mahali hapo (Mt. 13:2). Bahari hii ina umbile la pea, maili 12.5 (kilometa 20) urefu na maili 7.5 (kilometa 12) upana, katika mapana yake makubwa. Iko futi 680 (mita 207) chini ya usawa wa bahari, ambayo mara kwa mara hufanya hewa inayolizunguka kuwa na joto kali. Hewa baridi inayoteremka kutoka vilimani na kukutana na hewa ya joto juu ya maji mara kwa mara husababisha tufani (Lk. 8:22–24).

Gamalieli. *Ona pia* Mafarisayo

Mfarisayo maarufu katika Agano Jipya aliyeijua na kuifundisha torati ya Kiyahudi. Mtume Paulo alikuwa mmoja wa wanafunzi wake (Mdo. 22:3). Yeye alikuwa mtu mwenye nguvu sana katika Sanhedrini (Mdo. 5:34–40).

Gereza la Carthage (Marekani). *Ona pia* Smith, Hyrum; Smith, Joseph, Mdogo

Joseph na Hyrum Smith waliuawa na kundi la wahuni mnamo 27 Juni 1844 gerezani la Carthage, Illinois, Marekani (M&M 135).

Gereza la Liberty, Missouri (Marekani). *Ona pia* Smith, Joseph, Mdogo

Gereza dogo ambamo ndani yake Joseph Smith Nabii na wengine walifungwa bila makosa kutoka Novemba 1838 hadi Aprili 1839. Wakati wakiwa katika hali hii ngumu, Joseph alipokea mafunuo kadha, alitoa unabii, na aliongozwa kuandika barua muhimu kwa Watakatifu, sehemu zake zimo katika Mafundisho na Maagano 121–123.

Gereza la Roho. *Ona* Jehanamu

Gethsemani. *Ona pia* Lipia dhambi, Upatanisho; Mizeituni, Mlima wa

Bustani inayosemwa katika Agano Jipya kama iko karibu na Mlima wa Mizeituni. Katika Kiaramaiki, neno *gethsemani* maana yake "kinu cha kukamulia zeituni." Yesu alikwenda katika bustani hii usiku ule ambao Yuda alimsaliti. Hapo alisali na kuteseka katika Gethsemani kwa ajili ya dhambi za wanadamu (Mt. 26:36, 39; Mk. 14:32; Yn. 18:1; Alma 21:9; M&M 19:15–19).

Ghala. *Ona pia* Ustawi

Mahali ambapo askofu hupokelea, hutunza, na kugawa kwa maskini sadaka zilizowekwa wakfu za Watakatifu wa Siku za Mwisho. Kila ghala yaweza kuwa kubwa au ndogo kulingana na hali ya mahitaji. Watakatifu waaminifu hutoa vipaji, ujuzi, mali, na fedha kwa askofu ili kuwasaidia maskini wakati wa shida. Kwa hiyo, ghala yaweza kujumuisha orodha ya huduma zinazopatikana, pesa, chakula, au bidhaa nyinginezo. Askofu ndiye wakala wa ghala na hugawa bidhaa na huduma kulingana na mahitaji na kama atakavyoongozwa na Roho wa Bwana (M&M 42:29–36; 82:14–19).

Na wajikusanyie chakula kwa ajili ya akiba dhidi ya miaka hii saba ya njaa, **Mwa.** 41:34–36, 46–57. Leteni zaka zote ghalani, **Mal.** 3:10 (3 Ne. 24:10).

Na askofu aanzishe ghala kwa Kanisa hili, **M&M** 51:13. Bidhaa za ziada zipelekwe katika ghala yangu, **M&M** 70:7–8. Watakatifu wanapaswa kuanzisha na kuimarisha ghala, **M&M** 78:1–4. Watoto wana haki juu ya ghala ya Bwana kama wazazi wao hawana cha kuwapa, **M&M** 83:5.

Gharika katika Wakati wa Nuhu. *Ona pia* Nuhu, Patriaki wa Biblia; Safina; Upinde wa mvua

Katika wakati wa Nuhu dunia ilifunikwa kabisa na maji. Huu ndiyo ulikuwa ubatizo wa dunia na ilikuwa ishara ya kuoshwa (1 Pet. 3:20–21).

Mungu ataleta gharika ya maji juu ya dunia ili kuharibu vyote vyenye mwili, **Mwa.** 6:17 (Musa 7:34, 43, 50–52; 8:17, 30). Maji ya gharika yakawa juu ya dunia, **Mwa.** 7:10. Mungu akaweka upinde katika mawingu kama ishara ya agano, **Mwa.** 9:9–17.

Baada ya maji kupungua, nchi ya Marekani ikawa nchi teule, **Eth.** 13:2.

Waovu wataangamia katika gharika, **Musa** 7:38; 8:24.

Gideoni (Agano la Kale)

Kiongozi aliye wakomboa Israeli kutoka kwa Wamidiani (Amu. 6:11–40; 7–8).

Gideoni (Kitabu cha Mormoni)

Kiongozi Mnefi aliyekuwa mwaminifu.

Alikuwa mtu hodari na adui wa Mfalme Nuhu, **Mos.** 19:4–8. Alishauriana na Mfalme Limhi, **Mos.** 20:17–22. Alipendekeza mpango wa kutoroka kutoka utumwa wa Walamani, **Mos.** 22:3–9. Aliuawa na Nehori, **Alma** 1:8–10.

Giza, Kiroho. *Ona pia* Ovu, Uovu

Uovu au ujinga wa mambo ya kiroho.

Ole wao watiao giza badala ya nuru, **Isa.** 5:20 (2 Ne. 15:20). Giza litaifunika dunia, na giza kuu litawafunika watu, **Isa.** 60:2.

Yesu atatoa nuru kwa wale wakaao gizani, **Lk.** 1:79. Nuru yang'aa gizani, na giza halikuiweza, **Yn.** 1:5 (M&M 45:7). Tuyavue matendo ya giza na kuzivaa silaha za nuru, **Rum.** 13:12. Msishirikiane na matendo yasiyozaa ya giza, **Efe.** 5:8–11.

Kwa sababu ninyi hamuombi, hamjaletwa kwenye nuru lakini lazima mwangamie gizani, **2 Ne.** 32:4. Shetani hueneza matendo ya giza, **Hel.** 6:28–31.

Nguvu za giza zinaenea juu ya dunia, **M&M** 38:8, 11–12. Ulimwengu wote unagumia chini ya giza na dhambi, **M&M** 84:49–54. Kama jicho lako likiwa tu katika utukufu wangu, hapatakuwa na giza ndani yako, **M&M** 88:67.

Matendo ya giza yalianza kuenea miongoni mwa wana wote wa watu, **Musa** 5:55.

Gizani, Nje. *Ona* Ibilisi; Jehanamu; Mauti ya Kiroho; Wana wa Upotevu

Gogu. *Ona pia* Magogu; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo

Mfalme wa Magogu. Ezekieli alitoa unabii kwamba Gogu angeivamia Israeli katika wakati wa Ujio wa Pili wa Bwana (Eze. 38–39). Vita nyingine, iitwayo vita vya Gogu na Magogu, vitatokea mwishoni mwa Milenia (Ufu. 20:7–9; M&M 88:111–116).

Golgotha. *Ona pia* Kusulubiwa; Yesu Kristo

Golgotha maana yake "fuvu" katika lugha ya Kiaramaiki. Ni jina la mahali ambapo Kristo alisulubiwa (Mt. 27:33; Mk. 15:22; Yn. 19:17). Jina la Kilatini la mahali hapa ni Kalvari (Lk. 23:33).

Goliathi. *Ona pia* Daudi

Katika Agano la Kale, ni jitu la Kifilisti ambalo lilikuwa likiyashinda majeshi ya Waisraeli. Daudi alikubali kupambana naye kwa msaada wa Bwana akaliuwa (1 Sam. 17).

Gomora. *Ona pia* Sodoma

Katika Agano la Kale, ni mji wa uovu ambao uliangamizwa na Bwana (Mwa. 19:12–29).

Habakuki

Nabii wa Agano la Kale katika Uyahudi aliyenena juu ya hali ya dhambi ya watu inawezekana wakati wa utawala wa Yohoyakini (karibu mwaka 600 K.K.).

Kitabu cha Habakuki: Mlango wa 1 ni majadiliano kati ya Bwana na nabii Wake, sawa sawa na yale yaliyomo katika Yeremia 12 na Mafundisho na Maagano 121. Habakuki alikuwa akisumbuka kwamba waovu wanaonekana kustawi. Katika mlango wa 2 Bwana anamshauri Habakuki kuwa

mvumilivu—watu wenye haki lazima wajifunze kuishi kwa imani. Mlango wa 3 unaandikwa sala ya Habakuki ambamo ndani yake anakiri kuwa Mungu ni mwenye haki.

Habili. *Ona pia* Adamu; Kaini

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Adamu na Hawa.

Alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora kuliko alivyofanya Kaini kaka yake, **Mwa.** 4:4–5 (Ebr. 11:4; Musa 5:16–21). Aliuawa na Kaini, **Mwa.** 4:8 (Musa 5:32).

Alipokea ukuhani kutoka kwa Adamu, **M&M** 84:16.

Shetani alikula njama na Kaini ili kumwua Habili, **Musa** 5:28–31 (Hel. 6:27).

Hagai

Nabii wa Agano la Kale ambaye alitoa unabii katika karibu mwaka 520 K.K. katika Yerusalemu, mara baada ya watu wa Uyahudi waliporudi kutoka katika uhamisho wa Babilonia (Ezra 5:1; 6:14). Alisema juu ya kujengwa hekalu la Bwana katika Yerusalemu na akawakemea watu kwa sababu hawakuwa wamemaliza. Naye pia aliandika juu ya hekalu la milenia na utawala wa Mwokozi.

Kitabu cha Hagai: Katika mlango wa 1, Bwana anawakemea watu kwa kuishi katika nyumba zao zilizomalizika wakati hekalu limebaki bila kujengwa. Mlango wa 2 unaandikwa unabii wa Hagai kwamba Bwana atatoa amani katika hekalu Lake.

Hagothi

Mnefi mjenga meli katika Kitabu cha Mormoni (Alma 63:5–7).

Hajiri. *Ona pia* Ibrahimu; Ishmaili, Mwana wa Ibrahimu

Katika Agano la Kale, ni mjakazi wa Sarai aliyekuwa Mmisri. Alikuja kuwa mkewe Ibrahimu na mama wa Ishmaeli (Mwa. 16; 25:12; M&M 132:34, 65). Bwana alimwahidi Hajira kwamba taifa kubwa litakuja kutoka kwa mwanawe (Mwa. 21:9–21).

Haki, Uadilifu, enye Uadilifu. *Ona pia* Amri za Mungu; Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki; Kutokuwa Adilifu, Siyo Adilifu; Lipia dhambi, Upatanisho; Mwaminifu, Uaminifu; Rehema, enye Rehema; Tembea, Tembea na Mungu

Kuwa mwenye haki, mtakatifu, wema, wima, unyofu, uaminifu; kutenda katika utii kwa amri za Mungu; kuepuka dhambi.

Matokeo yasiyotindika ya baraka kwa ajili ya mawazo na matendo ya uadilifu, na adhabu kwa dhambi zisizofanyiwa toba. Haki ni sheria ya milele ambayo huhitaji adhabu kila mara sheria ya Mungu inapovunjwa (Alma 42:13–24). Mtenda dhambi ni lazima alipe adhabu kama hatubu (Mos. 2:38–39; M&M 19:17). Kama anatubu, Mwokozi humlipia ile adhabu kupitia upatanisho kwa kuomba rehema (Alma 34:16).

Hadi nitakapokufa, sitajiondelea uadilifu wangu, **Ayu.** 27:5. Bwana atawabariki wenye haki, **Zab.** 5:12. Macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, **Zab.** 34:15, 17 (1 Pet. 3:12). Mwenye haki huenda katika uadilifu wake, **Mit.** 20:7. Wakati wenye haki wawapo katika mamlaka, watu hufurahi, **Mit.** 29:2 (M&M 98:9–10). Roho ile itendayo dhambi itakufa, **Eze.** 18:4. Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, **Mika** 6:8.

Heri wenye njaa na kiu ya haki, **Mt.** 5:6 (3 Ne. 12:6). Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu na haki zake, **Mt.** 6:33. Wenye haki huenda katika uzima wa milele, **Mt.** 25:46. Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, **Yak. (Bib.)** 5:16. Yesu atakuwa wa haki na atatusamehe dhambi zetu, **1 Yoh.** 1:9.

Haki ya Mungu iliwatenga waovu na wenye haki, **1 Ne.** 15:30. Aliye na haki hupendelewa na Mungu, **1 Ne.** 17:35. Atawalinda wenye haki; hawahitaji kuogopa, **1 Ne.** 22:17, 22. Shetani hatakuwa na nguvu kwa sababu ya uadilifu

wa watu wa Bwana, **1 Ne.** 22:26. Kama hakutakuwa na uadilifu hapatakuwepo na furaha, **2 Ne.** 2:13. Wenye haki wataurithi ufalme wa Mungu, **2 Ne.** 9:18. Upatanisho hutosheleza mahitaji ya haki yake, **2 Ne.** 9:26. Wenye haki hawaogopi maneno ya kweli, **2 Ne.** 9:40. Watu wote lazima wabadilike na kuwa katika hali ya uadilifu, **Mos.** 27:25–26. Majina ya wenye haki yataandikwa katika kitabu cha uzima, **Alma** 5:58. Wanadamu wote wameanguka na wameshikwa na haki, **Alma** 42:14. Upatanisho huridhisha mahitaji ya haki, **Alma** 42:15. Ninyi mwadhani rehema yaweza kuiibia haki, **Alma** 42:25. Walikuwa watu waliokuwa wakweli katika nyakati zote na katika mambo yote waliyoaminiwa, **Alma** 53:20. Haki ya Mungu huning'inia juu yako isipokuwa utubu, **Alma** 54:6. Mmetafuta furaha kwa kufanya uovu, kitu ambacho ni kinyume cha asili ya uadilifu, **Hel.** 13:38.

Wimbo wa mwenye haki ni sala kwangu, **M&M** 25:12. Simama ukiwa umevaa dirii ya uadilifu, **M&M** 27:16 (Efe. 6:14). Mauti ya wenye haki ni matamu kwao, **M&M** 42:46. Wenye haki watakusanywa kutoka miongoni mwa mataifa yote, **M&M** 45:71. Wanadamu wanapaswa kutenda mengi ya uadilifu kwa mapenzi yao wenyewe, **M&M** 58:27. Yule afanyaye matendo ya uadilifu atapokea amani katika ulimwengu huu na uzima wa milele katika ulimwengu ujao, **M&M** 59:23. Katika Ujio wa Pili, kutakuwako utengano mkamilifu wa wenye haki na wale waovu, **M&M** 63:54. Haki na hukumu ni adhabu zilizowekwa kwa sheria yangu, **M&M** 82:4. Haki huchukua mkondo wake na kudai chake, **M&M** 88:40. Hakuna atakayesamehewa kutokana na haki na sheria za Mungu, **M&M** 107:84. Nguvu za mbinguni zaweza kudhibitiwa tu juu ya kanuni za uadilifu, **M&M** 121:36. Bwana alimpenda Hyrum Smith kwa sababu ya uadilifu wa moyo wake, **M&M** 124:15. Miongoni mwa wenye haki palikuwepo na amani, **M&M** 138:22.

Watu wa Sayuni waliishi katika uadilifu, **Musa** 7:18. Ibrahimu alikuwa mfuasi wa uadilifu, **Ibr.** 1:2.

Haki ya Kuzaliwa. *Ona pia* Agano; Mzaliwa wa Kwanza

Haki ya urithi ni mali ya mzaliwa wa kwanza wa kiume. Kwa maana pana, haki ya uzawa ni pamoja na chochote au haki zote au urithi unahamishiwa kwa mtu anapozaliwa katika familia na jamii.

Niuzie leo hii haki yako ya uzaliwa wa kwanza, **Mwa.** 25:29–34 (Mwa. 27:36). Mzaliwa wa kwanza alikaa kulingana na haki yake ya uzaliwa wa kwanza, **Mwa.** 43:33. Akamweka Efraimu mbele ya Manase, **Mwa.** 48:14–20 (Yer. 31:9). Haki ile ya uzaliwa wa kwanza ilikuwa ya Yusufu, **1 Nya.** 5:2.

Esau aliiuza haki yake ya uzaliwa wa kwanza, **Ebr.** 12:16.

Ninyi ni warithi kisheria, **M&M** 86:9. Sayuni anayo haki ya ukuhani kwa njia ya nasaba, **M&M** 113:8 (Ibr. 2:9–11).

Haki ya uamuzi. *Ona pia* Huru, Uhuru; Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika

Uwezo na nafasi Mungu awapayo watu ili kujichagulia na kutenda wao wenyewe.

Mna uhuru wa kula kila mti, **Mwa.** 2:16. Chagueni hivi leo mtakayemtumikia, **Yos.** 24:15 (Alma 30:8; Musa 6:33).

Mwanadamu asingeweza kujiamulia mwenyewe bila kuvutiwa, **2 Ne.** 2:15–16. Wanadamu wako huru kuchagua uhuru na uzima wa milele, au utumwa na mauti, **2 Ne.** 2:27. Ninyi mko huru; mmeruhusiwa kujichagulia wenyewe, **Hel.** 14:30.

Theluthi moja ya majeshi ya mbinguni aliyageuza kwa sababu ya haki yao ya kujiamulia, **M&M** 29:36. Ilikuwa ni muhimu kwamba ibilisi awajaribu wanadamu, au la sivyo wasingeliweza kujiamulia wenyewe, **M&M** 29:39. Kila mtu na ajiamulie mwenyewe, **M&M** 37:4. Kila mtu aweza kutenda kulingana na

haki ya kujiamulia niliyompatia, **M&M** 101:78.

Shetani alitafuta kuiangamiza haki ya mwanadamu ya kujiamulia, **Musa** 4:3. Bwana akampatia mwanadamu haki yake ya uamuzi, **Musa** 7:32.

Hali ya Kufa, enye Kufa. *Ona pia* Anguko la Adamu na Hawa; Mauti ya Kimwili; Mwili; Ulimwengu

Muda tangu kuzaliwa hadi kifo cha kimwili. Hii wakati mwingine huitwa hali ya pili.

Siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika, **Mwa.** 2:16–17 (Musa 3:16–17). Katika mauti roho itarudi kwa Mungu na mwili katika mavumbi ya dunia, **Mh.** 12:7 (Mwa. 3:19; Musa 4:25).

Msiache dhambi itawale katika mili yenu yenye kufa, **Rum.** 6:12. Mwili huu wenye kufa lazima uvae kutokufa, **1 Kor.** 15:53 (Eno. 1:27; Mos. 16:10; Morm. 6:21).

Hali ya mwanadamu ikawa hali ya majaribio, **2 Ne.** 2:21 (Alma 12:24; 42:10). Adamu alianguka ili wanadamu wawepo, **2 Ne.** 2:25. Je, ninyi mnatazamia na kuona mwili huu wenye kufa ukiinuliwa katika kutokufa, **Alma** 5:15. Maisha haya ndiyo wakati wa kujitayarisha kukutana na Mungu, **Alma** 34:32.

Msiogope mauti, kwani shangwe yenu si kamilifu katika ulimwengu huu, **M&M** 101:36.

Wale wanaoitunza hali yao ya pili watakuwa na utukufu, **Ibr.** 3:26.

Hali ya Kutojua. *Ona* Asiye na Hatia, Hali ya Kutojua

Hali ya Pili. *Ona* Hali ya Kufa, enye Kufa

Hamaki. *Ona* Hasira

Hamu. *Ona pia* Nuhu, Patriaki wa Biblia

Katika Agano la Kale, ni mwana wa tatu wa Nuhu (Mwa. 5:32; 6:10; Musa 8:12, 27).

Nuhu, wanawe, na familia zao wakaingia katika safina, **Mwa.** 7:13. Kanaani, mwanawe Hamu, alilaaniwa, **Mwa.** 9:18–25.

Utawala wa Hamu ulikuwa wa kipatriaki nao ulibarikiwa kwa vitu vya dunia na hekima lakini siyo kwa ukuhani, **Ibr.** 1:21–27. Mke wa Hamu, Egipto, alikuwa wa uzao wa Kaini, wana wa binti yao Egipto waliishi katika Misri, **Ibr.** 1:23, 25 (Zab. 105:23; 106:21–22).

Hana. *Ona pia* Samweli, Nabii wa Agano la Kale

Mama yake Samweli, nabii wa Agano la Kale. Bwana alimtoa Samweli kwa Hana katika kujibu sala yake (1 Sam. 1:11, 20–28). Hana alimweka wakfu Samweli kwa Bwana. Wimbo wake wa kutoa shukrani waweza kulinganishwa na ule wa Maria, mama wa Yesu (1 Sam. 2:1–10; Lk. 1:46–55).

Har-Magedoni. *Ona pia* Gogu; Magogu; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo

Jina Har-Magedoni linatoka katika neno la Kiebrania *Har-Megidoni* maana yake "mlima wa Megido." Bonde la Megido lipo katika sehemu ya magharibi mwa mbuga za Esdraloni, maili hamsini (kilometa themanini) kaskazini ya Yerusalemu, na ni sehemu ya mapigano kadhaa muhimu katika nyakati za Agano la Kale. Pigano kuu na la mwisho ambalo litakuwepo karibu na wakati wa Ujio wa Pili wa Bwana linaitwa vita vya Har-Magedoni kwa sababu vitaanzia mahali hapa. (Ona Eze. 39:11; Zek. 12–14, hususani 12:11; Ufu. 16:14–21.)

Harris, Martin. *Ona pia* Mashahidi wa Kitabu cha Mormoni

Mmoja wa Mashahidi Watatu wa asili ya utakatifu na wa ukweli wa Kitabu cha Mormoni. Alimsaidia kifedha Joseph Smith na Kanisa. Bwana alimwambia Martin Harris auze shamba lake na kutoa fedha hizo ili kulipia uchapishaji wa Kitabu cha Mormoni (M&M 19:26–27, 34–35), ili awe mfano kwa Kanisa

(M&M 58:35), na ili kusaidia kulipia gharama za huduma (M&M 104:26).

Martin Harris alitengwa na Kanisa lakini baadaye alirejea na kuwa muumini kamili. Hadi mwisho wa maisha yake aliendelea kutoa ushahidi kwamba alimwona malaika Moroni na yale mabamba ya dhahabu ambayo kutoka hayo Joseph Smith alitafsiri Kitabu cha Mormoni.

Haruni, Kaka wa Musa. *Ona pia* Musa; Ukuhani wa Haruni

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Amramu na Yokebedi, wa kabila la Lawi (Ku. 6:16–20); kaka mkubwa wa Musa (Ku. 7:7).

Aliteuliwa na Bwana ili kumsaidia Musa katika kuwaleta wana wa Israeli kutoka Misri na kuwa msemaji wake, **Ku.** 4:10–16, 27–31; 5:1–12:51. Juu ya Mlima Sinai, Musa alipokea maelekezo juu ya uteuzi wa Haruni na wanawe wanne kwenye Ukuhani wa Haruni, **Ku.** 28:1–4. Kwa maombi ya watu alitengeneza ndama wa dhahabu, **Ku.** 32:1–6, 21, 24, 35. Alikufa juu ya Mlima Hori akiwa na umri wa miaka 123, **Hes.** 20:22–29 (Hes. 33:38–39).

Bwana alithibitisha ukuhani pia juu ya Haruni na uzao wake, **M&M** 84:18, 26–27, 30. Wale wenye kukuza miito ya ukuhani huwa wana wa Musa na Haruni, **M&M** 84:33–34.

Haruni, Mwana wa Mosia. *Ona pia* Mosia, Mwana wa Benjamini; Mosia, Wana wa

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana wa Mfalme Mosia. Haruni alitumika kama mmisionari ambaye jitihada zake zilisaidia kuziongoa roho za wengi kuja kwa Kristo.

Alikuwa ni mtu asiyeamini aliyetafuta kuliangamiza Kanisa, **Mos.** 27:8–10, 34. Malaika aliwatokea yeye na wenzi wake, **Mos.** 27:11. Wakatubu na kuanza kulihubiri neno la Mungu, **Mos.** 27:32–28:8. Alikataa kuitwa mfalme na badala yake alikwenda katika nchi ya Walamani kuhubiri neno la Mungu, **Alma** 17:6–9. Akafunga na kusali ili kupata mwongozo, **Alma** 17:8–11. Alimfundisha baba wa Mfalme Lamoni, **Alma** 22:1–26. Alikwenda kuhubiri kwa Wazorami, **Alma** 31:6–7.

Hasira. *Ona pia* Chuki, Chukia; Upendo

Hasira ni onyesho la tabia ya ukali. Bwana aliwatahadharisha watakatifu Wake kudhibiti hasira zao (Mt. 5:22). Si mzazi wala mtoto anayepaswa kuwatukana wengine katika familia. Katika maandiko, hasira daima imepewa sura ya moto (2 Ne. 15:25; M&M 1:13).

Na Kaini akaghadhibika sana, na uso wake ukakunjamana, **Mwa.** 4:5. Bwana si mwepesi wa hasira, na ni mwingi wa rehema, **Zab.** 145:8. Jawabu la upole hugeuza hasira, **Mit.** 15:1. Mtu wa hasira huchochea ugomvi, bali asiye mwepesi wa hasira hutuliza ugomvi, **Mit.** 15:18 (Mit. 14:29). Kwa ajili ya jina langu nitaahirisha hasira yangu, **Isa.** 48:9. Nimewanyooshea mikono yangu watu wanikasirishao daima, **Isa.** 65:2–3.

Yeyote akupigaye shavu lako la kuume, mgeuzie na jingine pia, **Mt.** 5:39. Nanyi akina baba, msiwachokoze watoto wenu wakakasirika, **Efe.** 6:4.

Kwa sababu nimewaambia ukweli, mnanikasirikia, **Mos.** 13:4. Nitawatembelea watu hawa katika hasira yangu, **Alma** 8:29.

Hasira yake haiwaki dhidi ya yeyote isipokuwa wale wasiokiri mkono wake katika mambo yote, **M&M** 59:21. Mimi, Bwana, nimewakasirikia waovu, **M&M** 63:32.

Hatia. *Ona pia* Toba, Tubu

Hali ya kuwa umetenda baya, au hisia za kujuta na kuhuzunika ambayo huambatana na dhambi.

Ametenda dhambi naye anayo hatia, **Law.** 6:1–6.

Yeyote apokeaye sakramenti isivyostahili, atakuwa anajipatia hatia ya mwili na damu ya Yesu, **1 Kor.** 11:27.

Wenye hatia huichukulia kweli kuwa ngumu, **1 Ne.** 16:2. Tutakuwa na ufahamu kamili juu ya hatia zetu zote, **2 Ne.** 9:14. Hatia yangu ilifagiliwa mbali, **Eno.** 1:6. Kulikuwa na adhabu iliyowekwa, ambayo ilileta majuto ya dhamiri, **Alma** 42:18. Dhambi zako na zikusumbue, usumbufu ambao utakuleta chini kwenye toba, **Alma** 42:29.

Baadhi yenu mna hatia mbele yangu, lakini nitakuwa mwenye rehema, **M&M** 38:14.

Mwana wa Mungu amelipia kosa kwa ajili ya hatia ya mwanzo, **Musa** 6:54.

Hawa. *Ona pia* Adamu; Anguko la Adamu na Hawa; Edeni

Mwanamke wa kwanza kuishi katika dunia hii (Mwa. 2:21–25; 3:20). Alikuwa mke wa Adamu. Katika Kiebrania jina hili linaamanisha "uhai." Aliitwa hivyo kwa sababu yeye alikuwa "mama wa wote wenye uhai" (Musa 4:26). Yeye na Adamu, mwanaume wa kwanza, watashiriki kwa pamoja utukufu wa milele kwa ajili ya nafasi yao katika kuwezesha uendeleaje wa milele wa wanadamu wote.

Hawa alijaribiwa naye akala tunda lililokatazwa, **Mwa.** 3 (2 Ne. 2:15–20; Musa 4).

Rais Joseph F. Smith alimwona Hawa katika ono lake la ulimwengu wa roho, **M&M** 138:39.

Hawa alitambua umuhimu wa Anguko na shangwe ya ukombozi, **Musa** 5:11–12.

Hebroni

Mji wa Kale wa Yuda, maili ishirini (kilomita thelathini na mbili) kusini mwa Yerusalemu. Palikuwa mahali pa kuzikia pa Ibrahimu na familia yake (Mwa. 49:29–32). Ulikuwa mji mkuu wa Daudi katika sehemu ya kwanza ya utawala wake (2 Sam. 5:3–5).

Hekalu, Nyumba ya Bwana. *Ona pia* Endaomenti; Hema; Ibada; Patakatifu pa Patakatifu

Kwa maana iliyo wazi ni nyumba ya Bwana. Bwana daima amekuwa akiwaamuru watu Wake kujenga mahekalu, majumba matakatifu ambamo ndani yake Watakatifu wenye kustahili wanafanya sherehe na ibada takatifu za injili kwa ajili yao wenyewe na kwa ajili ya wafu. Bwana huyatembelea mahekalu Yake, nayo ni matakatifu zaidi ya sehemu nyingine zote za kuabudu.

Hema lililojengwa na Musa na wana wa Israeli lilikuwa ni hekalu linalobebeka. Waisraeli walilitumia wakati wa uhamaji wao kutoka Misri.

Hekalu linalofahamika vizuri zaidi na kutajwa katika Agano la Kale ni lile lililojengwa na Sulemani katika Yerusalemu (2 Nya. 2–5). Liliangamizwa katika mwaka 587 K.K. na Wababilonia na likajengwa upya na Zerubabeli takribani miaka 70 baadaye. (Ezra 1–6). Sehemu ya hekalu hili ilichomwa moto katika mwaka 37 K.K.; na Herode Mkuu baadaye akalijenga tena. Warumi wakaliangamiza hekalu hilo katika mwaka 70 B.K.

Katika Kitabu cha Mormoni, wafuasi waadilifu wa Mungu waliongozwa kujenga na kuabudu katika hekalu (2 Ne. 5:16; Mos. 1:18; 3 Ne. 11:1). Kujenga na kutumia hekalu kiusahihi ni ishara za Kanisa la kweli katika kipindi chochote, ikiwa ni pamoja na Kanisa la urejesho katika siku zetu. Hekalu la Kirtland lilikuwa ndiyo hekalu la kwanza kujengwa na kuwekwa wakfu kwa Bwana katika kipindi hiki. Toka wakati huo mahekalu yamekuwa yakiwekwa wakfu katika nchi nyingi kote duniani.

Ni nani atakayesimama katika mahali pake patakatifu, **Zab.** 24:3–5. Twende juu nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, **Isa.** 2:2–3 (Mika 4:1–2; 2 Ne. 12:2–3). Bwana atalijia hekalu lake ghafla, **Mal.** 3:1 (3 Ne. 24:1; M&M 36:8; 42:36).

Yesu alilisafisha hekalu, **Mt.** 21:12–16 (Mk. 11:15–18; Lk. 19:45–48).

Watakatifu waliamriwa kujenga hekalu katika Missouri, **M&M** 57:3 (M&M 84:3–5). Ijengeni nyumba ya Mungu, **M&M** 88:119 (M&M 109:8). Bwana

aliwarudi Watakatifu kwa kushindwa kujenga hekalu, **M&M** 95:1–12. Sitakuja ndani ya mahekalu yasiyo matakatifu, **M&M** 97:15–17. Nimeikubali nyumba hii, na jina langu litakuwa hapa, **M&M** 110:7–8. Watu wa Bwana daima wanaamriwa kujenga nyumba kwa jina lake, **M&M** 124:39. Kazi kubwa itakayofanyika katika mahekalu ni pamoja na kuwafunga watoto kwa wazazi wao, **M&M** 138:47–48. Kazi kubwa ya siku za mwisho ni pamoja na ujenzi wa mahekalu, **M&M** 138:53–54.

Hekalu la Kirtland, Ohio (Marekani)

Hekalu la kwanza lililojengwa na kanisa katika nyakati za sasa. Watakatifu walilijenga huko Kirtland, kulingana na amri ya Bwana (M&M 94:3–9). Dhumuni mojawapo lilikuwa ni kupata mahali ambapo waumini wa Kanisa wanaostahili waweze kupokea nguvu za kiroho, mamlaka, na maarifa (M&M 109–110). Liliwekwa wakfu, mnamo 27 Machi 1836; sala ya kuweka wakfu ilitolewa na Joseph Smith Nabii kwa ufunuo (M&M 109). Bwana alitoa mafunuo kadhaa yaliyo muhimu na kurejesha funguo za ukuhani zilizohitajika katika hekalu hili (M&M 110; 137). Halikutumiwa kwa ibada kamilifu za hekalu kama zinavyotolewa katika mahekalu siku hizi.

Hekima. *Ona pia* Maarifa; Ufahamu; Ukweli

Uwezo au kipawa kutoka kwa Mungu cha kuhukumu kwa usahihi. Mtu hupata hekima kwa njia ya uzoefu na kujifunza na kwa kufuata ushauri wa Mungu. Pasipo msaada wa Mungu, mwanadamu hawezi kuwa na hekima ya kweli (2 Ne. 9:28; 27:26).

Mungu alimpa Sulemani hekima, **1 Fal.** 4:29–30. Hekima ndicho kitu muhimu; kwa hiyo jipatie hekima, **Mit.** 4:7. Apataye hekima huipenda nafsi yake mwenyewe, **Mit.** 19:8.

Yesu aliongezeka hekima, **Lk.** 2:40, 52. Kama mtu yeyote kati yenu akipungukiwa na hekima, na aombe kwa Mungu, **Yak. (Bib.)** 1:5 (M&M 42:68; JS—H 1:11).

Ninawaambia mambo haya ili mpate kujifunza kuwa na hekima, **Mos.** 2:17. Jifunze hekima katika ujana wako, **Alma** 37:35.

Watakatifu watapata hekima na hazina kuu ya maarifa, **M&M** 89:19. Acheni yule ambaye yu mjinga ajifunze hekima kwa kujinyenyekeza mwenyewe na kumlingana Bwana, **M&M** 136:32.

Helamani, Mwana wa Alma. *Ona pia* Alma, Mwana wa Alma; Helamani, Wana wa; Waanti-Nefi-Lehi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana mkubwa wa Alma, aliyekuwa mwana wa Alma (Alma 31:7). Helamani alikuwa nabii na kiongozi wa kijeshi.

Alma alimkabidhi mwanawe Helamani taarifa iliyoandikwa ya watu wake na pamoja na mabamba ya Wayaredi, **Alma** 37:1–2, 21. Alma alimwamuru Helamani kuendelea kuandika historia ya watu wake, **Alma** 45–62. Helamani alilianzisha tena kanisa, **Alma** 45:22–23. Vijana mashujaa wa vita elfu mbili wa Kiamoni walitamani Helamani kuwa kiongozi wao, **Alma** 53:19, 22. Helamani na wavulana wajasiri wake wa Kiamoni walipigana vita na Walamani na wakalindwa na imani, **Alma** 57:19–27.

Helamani, Mwana wa Helamani

Nabii na mtunza kumbu kumbu katika Kitabu cha Mormoni ambaye aliwafundisha watu wa Nefi. Yeye alikuwa mjukuu wa kiume wa Alma Mdogo na baba wa Nefi aliyepewa uwezo juu ya vitu vyote vya asili. Pamoja na mwanawe Nefi, Helamani aliandika Kitabu cha Helamani.

Kitabu cha Helamani: Mlango wa 1–2 inaelezea wakati wa matatizo makubwa ya kisiasa. Mlango wa 3–4 inaandika kwamba, Helamani na Moroniha, jemadari mkuu wa majeshi ya Wanefi, waliweza hatimaye kupata amani kwa

muda. Hata hivyo licha ya uongozi wa watu hawa wema, watu walizidi kuongezeka kuwa waovu. Katika Helamani 5:1–6:14 Nefi aliachia kiti cha hukumu, kama babu yake Alma alivyofanya, ili awafundishe watu. Kwa muda watu wakatubu. Katika Helamani 6:15–12:26, hata hivyo, taifa la Wanefi wakawa waovu. Milango ya mwisho, yaani 13–16, ina historia isiyo ya kawaida ya nabii aliyeitwa Samweli Mlamani ambaye alitabiri kuzaliwa na Kusulubiwa kwa Mwokozi na ishara ambazo zingekuwa dalili ya matukio hayo.

Helamani, Mwana wa Mfalme Benjamini. *Ona pia* Benjamini, Baba wa Mosia

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mmoja kati ya wana watatu wa Mfalme Benjamini (Mos. 1:2–8).

Helamani, Wana wa. *Ona pia* Helamani, Mwana wa Alma; Waanti-Nefi-Lehi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni wana wa Walamani walioongolewa waliojulikana kama Waamoni ambao walikuwa askari wa vita chini ya uongozi wa Helamani (Alma 53:16–22).

Helamani aliwaona kuwa wanastahili kuitwa wanawe, **Alma** 56:10. Mama zao walikuwa wamewafundisha kutokuwa na mashaka na uwezo wa Bwana wa kuwakomboa, **Alma** 56:47. Waliwashinda Walamani na walilindwa na imani yao kiasi kwamba hakuna yeyote aliyeuawa, **Alma** 56:52–54, 56; 57:26.

Hema. *Ona pia* Hekalu, Nyumba ya Bwana; Patakatifu pa Patakatifu; Sanduku la Agano

Nyumba ya Bwana, kituo cha kuabudu cha Waisraeli wakati wa kuhama Kutoka Misri. Hema hili kwa kweli lilikuwa ni hekalu linalohamishika na walikuwa wanaweza kulibomoa na kulijenga tena upya. Wana wa Israeli walilitumia hema hadi walipojenga hekalu la Sulemani (M&M 124:38).

Mungu alimfunulia Musa ramani ya hema (Ku. 26–27), na wana wa Israeli walilijenga kulingana na ramani hiyo (Ku. 35–40). Wakati hema lilipokwisha kujengwa, wingu liliifunika hema hilo, na utukufu wa Bwana ukaijaza hema (Ku. 40:33–34). Wingu lilikuwa ni ishara ya uwepo wa Mungu. Usiku, lilikuwa na sura ya moto. Wakati wingu lilipokaa juu ya hema, wana wa Israeli walifanya kambi. Lilipoondoka nao waliondoka pamoja nalo (Ku. 40:36–38; Hes. 9:17–18). Wana wa Israeli waliibeba ile hema wakati wa kutangatanga kwao jangwani na katika utekaji wa nchi ya Kanani. Baada ya utekaji, hema iliwekwa katika Shilo, sehemu ambayo Bwana aliichagua (Yos. 18:1). Baada ya wana wa Israeli kujenga hekalu la Sulemani, hema ilipotea kabisa katika historia.

Bwana na Isaya walitumia hema kama ishara ya miji ya Sayuni na Yerusalemu katika wakati wa Ujio wa Pili wa Bwana (Isa. 33:20; Musa 7:62).

Henoko. *Ona pia* Sayuni

Nabii aliyewaongoza watu wa mji wa Sayuni. Huduma yake inaongelewa kote katika Agano la Kale na Lulu ya Thamani Kuu. Yeye alikuwa patriaki wa saba baada ya Adamu. Alikuwa mwana wa Yaredi na baba wa Methusela (Mwa. 5:18–24; Lk. 3:37).

Henoko alikuwa mtu maarufu na alikuwa na huduma iliyokuwa muhimu zaidi kuliko historia fupi inayoonyeshwa katika Biblia juu yake. Biblia inaandika kwamba yeye alihamishwa (Ebr. 11:5) lakini haitoi maelezo juu ya huduma yake. Yuda 1:14 inayo nukuu za unabii alioufanya. Ufunuo wa siku za mwisho unaelezea zaidi juu ya Henoko, hususani juu ya mahubiri yake, mji wake uliitwa Sayuni, maono yake, na unabii wake (M&M 107:48–57; Musa 6–7). Sayuni ulitwaliwa mbinguni kwa sababu ya haki ya wale walioishi ndani yake (Musa 7:69).

Mungu alijifunua mwenyewe kwa Henoko, **Musa** 6:26–37. Henoko alifundisha injili, **Musa** 6:37–68. Henoko

aliwafundisha watu na kuianzisha Sayuni, **Musa** 7:1–21. Henoko aliona mambo yote, hatab mwisho wa ulimwengu, **Musa** 7:23–68.

Heri. *Ona* Baraka, Bariki, Barikiwa

Herode

Ni jamaa ya watawala katika Yuda iliyokuwepo karibu na wakati wa Yesu Kristo. Walikuwa ni watu muhimu katika matukio mengi ya Agano Jipya. Familia hii ilianzishwa na Herode Mkuu, ambaye alikuwa mwoga kwa kuzaliwa kwa Mwokozi (Mt. 2:3) na akatoa agizo la mauaji ya kimbari ya watoto wachanga katika Bethlehemu. Wanawe wa kiume ni pamoja na Aristobulo; Herode Filipo (Mt. 14:3; Mk. 6:17); Herode Antipasi, mfalme (Mt. 14:1; Lk. 9:7; pia ialijulikana kama Mfalme Herode, Mk. 6:14); Arkelao (Mt. 2:22); na Filipo, mfalme wa Iturea (Lk. 3:1). Herod Agrippa I (Mdo. 12:1–23) na dada yake Herodia (Mt. 14:3; Mk. 6:17) walikuwa watoto wa Aristobulo. Herode Agrippa I pia alikuwa na watoto kadhaa ambao wametajwa katika Agano Jipya, akijumuishwa na Herod Agrippa II (Mdo. 25:13), Bernike (Mdo. 25:13), na Drusila, mke wa Feliki (Mdo. 24:24).

Herodia

Dada wa Herode Agripa katika Agano Jipya. Aliolewa na baba mdogo wake, Herode Filipo, kwake yeye alimzaa mtoto wa kike, Salome. Yeye na Salome walipanga njama ili Yohana Mbatizaji akatwe kichwa (Mt. 14:3–11).

Hesabu. *Ona pia* Torati

Kitabu cha nne katika Agano la Kale. Musa aliandika kitabu hiki cha Hesabu. Kitabu cha Hesabu kinaelezea hadithi ya safari ya Israeli kutoka Mlima Sinai hadi nyanda za Moabu juu ya mpaka wa Kanaani. Moja ya masomo muhimu kinacho fundisha ni kwamba watu wa Mungu lazima watembee kwa imani, wakiamini ahadi Zake, kama wanataka kuendelea kwa mafanikio. Kinaelezea adhabu za Mungu kwa Israeli kwa sababu ya utovu wa utiifu na hutoa taarifa juu ya sheria za Waisraeli. Jina la kitabu linatokana na tarakimu ya sensa maarufu (Hes. 1–2; 26).

Mlango wa 1–10 inasimulia juu ya maandilizi ya Waisraeli ya kuondoka toka Sinai. Mlango wa 11–14 inaelezea juu ya msafara wenyewe, kutumwa kwa wapelelezi ndani ya Kanaani, na kukataliwa kwa Israeli kuingia nchi ya ahadi. Mlango wa 15–19 inaonyesha sheria kadha wa kadha na matukio ya kihistoria. Mlango wa 20–36 ni historia ya mwaka wa mwisho wa watu hawa nyikani.

Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki. *Ona pia* Lipia dhambi, Upatanisho; Utakaso

Kusamehewa adhabu kwa ajili ya dhambi na kutamkwa kuwa huna hatia. Mtu anahesabiwa haki kwa neema ya Mwokozi kwa njia ya imani katika Yeye. Imani hii huonyeshwa katika toba na utiifu kwa sheria na ibada ya injili. Upatanisho wa Yesu Kristo huwawezesha wanadamu kutubu na kuhesabiwa haki au kusamehewa kutokana na adhabu ambayo vinginevyo wangeipata.

Katika Bwana Israeli wote watahesabiwa haki, **Isa.** 45:25.

Sio wale waisikiao sheria bali ni wale waitendao sheria watakaohesabiwa haki, **Rum.** 2:13. Mwanadamu anahesabiwa haki kupitia damu ya Kristo, **Rum.** 5:1–2, 9. Mwanadamu anahesabiwa haki katika jina la Bwana Yesu, **1 Kor.** 6:11. Tukihesabiwa haki kwa neema yake, tutafanywa warithi, **Tit.** 3:7. Je, baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, **Yak. (Bib.)** 2:21. Kwa matendo mwanadamu anahesabiwa haki, na siyo kwa imani pekee, **Yak. (Bib.)** 2:14–26.

Kwa sheria hakuna aliye na mwili ahesabiwaye kuwa na haki, **2 Ne.** 2:5. Mtumishi wangu mwenye haki atawahesabia wengi haki, kwani atayachukua maovu yao, **Mos.** 14:11 (Isa. 53:11). Je, mwaweza kusema kuwa mavazi yenu

yameoshwa kwa njia ya Kristo, **Alma** 5:27.

Kuhesabiwa haki kupitia neema ya Yesu Kristo ni kweli, **M&M** 20:30–31 (M&M 88:39).

Kwa Roho ninyi mnahesabiwa haki, **Musa** 6:60.

Heshima. *Ona pia* Tukuza; Uchaji

Kama kawaida litumikavyo katika maandiko, kuonyesha staha na uchaji kwa mtu fulani au kitu fulani.

Waheshimu baba yako na mama yako, **Ku.** 20:12 (1 Ne. 17:55; Mos. 13:20). Mheshimu Bwana kwa mali zako, **Mit.** 3:9.

Kama mtu yeyote atanitumikia mimi, Baba yangu atamheshimu mtu huyo, **Yn.** 12:26. Waume yawapasa kuwaheshimu wake zao, **1 Pet.** 3:7.

Humheshimu Bwana kwa midomo yao tu, **2 Ne.** 27:25 (Isa. 29:13). Sitafuti heshima ya ulimwengu, **Alma** 60:36.

Ibilisi aliniasi, akisema, Nipe mimi heshima yako, ambayo ndiyo uwezo wangu, **M&M** 29:36. Walio waaminifu watavikwa taji la heshima, **M&M** 75:5 (M&M 124:55). Bwana hufurahi kuwapa heshima wale wamtumikiaye, **M&M** 76:5. Hawakuchaguliwa kwa sababu wao wanatafuta heshima ya wanadamu, **M&M** 121:34–35.

Tunaamini katika kuheshimu na kuzi unga mkono sheria, **M ya I** 1:12 (M&M 134:6).

Hezekia

Mfalme mwenye haki wa taifa la Yuda katika Agano la Kale. Alitawala kwa miaka ishirini na tisa, wakati ambao Isaya alikuwa nabii katika Yuda (2 Fal. 18–20; 2 Nya. 29–32; Isa. 36–39). Isaya alimsaidia katika kulirekebisha kanisa na taifa. Alikomesha ibada za masanamu na kurejesha ibada za hekalu. Uhai wa Hezekia uliongezwa kwa miaka kumi na mitano kwa njia ya sala na imani (2 Fal. 20:1–7). Sehemu ya kwanza ya utawala wake ilikuwa yenye kustawi, lakini uasi wake dhidi ya mfalme wa Ashuru (2 Fal. 18:7) ilileta kuvamiwa na Waashuru mara mbili: wa kwanza unaelezwa katika Isaya 10:24–32, na wa pili katika 2 Wafalme 18:13–19:7. Katika uvamizi wa pili, Yerusalemu iliokolewa na malaika wa Bwana (2 Fal. 19:35).

Hila. *Ona pia* Danganya, Kudanganya, Udanganyifu

Katika maandiko, ni ujanja wa ulaghai.

Heri mtu yule ambaye rohoni mwake hamna hila, **Zab.** 32:2 (Zab. 34:13; 1 Pet. 2:1).

Nathanaeli alikuwa Mwisraeli ambaye hamna hila ndani yake, **Yn.** 1:47 (M&M 41:9–11).

Maarifa safi huikuza nafsi isiyo na hila, **M&M** 121:42.

Himiza, Kikwazo. *Ona pia* Roho Mtakatifu

Kumsihi sana mtu ili afanye au asifanye jambo fulani, hususani kwa muongozo au nguvu za Roho Mtakatifu.

Roho iliyo ndani yangu hunihimiza, **Ayu.** 32:18.

Upendo wa Kristo watubidisha, **2 Kor.** 5:14.

Nilishurutishwa na Roho kwamba nimuue Laban, **1 Ne.** 4:10. Roho ananizuia, **Alma** 14:11. Nilishurutishwa kulingana na agano, **Alma** 60:34. Amaroni, akiwa anashurutishwa na Roho Mtakatifu, aliyaficha maandishi yale, **4 Ne.** 1:48.

Kile ambacho huja hutoka juu lazima kisemwe kwa kushawishiwa na Roho, **M&M** 63:64.

Himni. *Ona pia* Mosia, Mwana wa Benjamini; Mosia, Wana wa

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana wa Mfalme Mosia. Himni alienda na kaka zake kuhubiri kwa Walamani (Mos. 27:8–11, 34–37; 28:1–9).

Hisani. *Ona pia* Huruma; Upendo; Ustawi; Utumishi

Upendo halisi wa Kristo (Moro. 7:47); ni upendo ambao Kristo alikuwa nao kwa watoto wa watu na kwamba watoto wa watu wanapaswa kuwa nao baina

yao (2 Ne. 26:30; 33:7–9; Eth. 12:33–34); ni upendo wa hali ya juu, wa kipekee, na wenye nguvu, siyo tu urafiki.

Ujuzi huleta majivuno, bali hisani hujenga, **1 Kor.** 8:1. Hisani, upendo halisi, hupita na kuzidi karibu vitu vingine vyote, **1 Kor.** 13. Mwisho wa agizo hilo ni hisani itokayo katika moyo safi, **1 Tim.** 1:5. Ongeza juu ya upendano wa kindugu hisani, **2 Pet.** 1:7.

Bwana ameamuru kwamba watu wote wawe na hisani, **2 Ne.** 26:30 (Moro. 7:44–47). Angalieni ya kwamba mnayo imani, tumaini, na hisani, **Alma** 7:24. Upendo ambao Bwana anao kwa wanadamu ni hisani, **Eth.** 12:33–34. Pasipo hisani wanadamu hawawezi kurithi mahali pale palipo tayarishwa katika makao ya Baba, **Eth.** 12:34 (Moro. 10:20–21). Moroni aliandika maneno ya Mormoni juu ya imani, tumaini, na hisani, **Moro.** 7.

Hisani huwapasisha wanadamu kwa ajili ya kazi ya Bwana, **M&M** 4:5–6 (M&M 12:8). Jivikeni wenyewe kifungo cha hisani, **M&M** 88:125. Mioyo yenu na ijae hisani, **M&M** 121:45.

Hisi. *Ona pia* Roho Mtakatifu

Kutambua ushawishi wa Roho.

Hisia ziliwapata, kwamba hamkuweza kuhisi maneno yake, **1 Ne.** 17:45. Mtakapo hisi mienendo hii ya kuvimba, mtaanza kusema kwamba hii ni mbegu njema, **Alma** 32:28.

Mtahisi kwamba ni sahihi, **M&M** 9:8. Watu wote watakaoingia katika nyumba ya Bwana wapate kuhisi uwezo wako, **M&M** 109:13.

Historia ya Familia. *Ona* Nasaba; Wokovu kwa ajili ya Wafu

Hofu. *Ona pia* Amini, Imani; Uchaji; Ushujaa, enye Ushujaa

Hofu yaweza kuwa na maana mbili: (1) hofu juu ya Mungu ni kujisikia uchaji na heshima Kwake na kutii amri Zake; (2) kumhofia mtu, hatari za kimwili, maumivu, na uovu ni kuwa na woga na mambo ya jinsi hiyo na kuyaogopa sana.

Hofu juu ya Mungu: Hakika hapana hofu ya Mungu mahali hapa, **Mwa.** 20:11. Nawe utakuwa na hofu na Bwana Mungu wako, **Kum.** 6:13 (Yos. 24:14; 1 Sam. 12:24). Mtumikieni Bwana kwa hofu, **Zab.** 2:11. Hofu ya Bwana ndiyo mwanzo wa hekima, **Zab.** 111:10. Mhofieni Bwana na mkajiepushe na uovu, **Mit.** 3:7. Itakuwa heri kwao wenye hofu ya Mungu, **Mh.** 8:12.

Timizeni wokovu wenu ninyi wenyewe kwa hofu na kutetemeka, **Flp.** 2:12. Mwogopeni Mungu, na mpeni yeye utukufu, **Ufu.** 14:7 (M&M 88:104).

Manabii waliwachochea watu daima ili kuwaweka katika hofu ya Bwana, **Eno.** 1:23. Alma na wana wa Mosia walianguka chini, kwani hofu ya Bwana ilikuja juu yao, **Alma** 36:7. Timizeni wokovu wenu kwa hofu na kutetemeka, **Morm.** 9:27.

Wao wasio kuwa na hofu na mimi, nitawasumbua na kuwafanya watetemeke, **M&M** 10:56. Yule mwenye hofu na mimi atazitazamia ishara za kuja kwa Mwana wa Mtu, **M&M** 45:39.

Hofu ya mwanadamu: Usihofu, kwani mimi niko pamoja nawe, **Mwa.** 26:24 (Isa. 41:10). Bwana yu pamoja nasi: msiwaogope, **Hes.** 14:9. Usihofu: maana wao walio pamoja nasi ni zaidi, **2 Fal.** 6:16. Siwezi kuogopa kile ambacho mwanadamu anaweza kufanya, **Zab.** 56:4. Msiogope matukano ya watu, **Isa.** 51:7 (2 Ne. 8:7).

Mungu hajatupa roho wa hofu, **2 Tim.** 1:7. Upendo kamili hufukuza hofu, **1 Yoh.** 4:18 (Moro. 8:16).

Wana wa Helamani hawakuogopa mauti, **Alma** 56:46–48. Hofu ya mauti huvijaza vifua vya waovu, **Morm.** 6:7. Usiogope mwanadamu anaweza kukutenda nini?, **Moro.** 8:16.

Usingemwogopa mwanadamu zaidi kuliko Mungu, **M&M** 3:7 (M&M 30:1, 11; 122:9). Usihofu kutenda mema, **M&M** 6:33. Yeyote aliye mali ya kanisa langu hahitaji kuogopa, **M&M** 10:55. Kama mmejiandaa, hamtaogopa, **M&M** 38:30. Jivueni wenyewe katika

hofu, **M&M** 67:10. Furahini, na msiogope, kwani Mimi Bwana niko pamoja nanyi, **M&M** 68:6. Msiwaogope maadui zenu, **M&M** 136:17.

Hosana

Neno la Kiebrania ambalo maana yake ni "tafadhali utuokoe" na hutumika katika kusifu na maombi ya unyenyekevu.

Katika Sikukuu ya Tabernakulo ambayo walikuwa wakisherehekea kukombolewa kwa Israeli na Bwana na kuingizwa katika nchi ya ahadi, watu walikuwa wakiimba maneno ya Zaburi 118 na kupepea matawi ya mitende. Bwana alipoingia kwa shangwe katika Yerusalemu, makutano waliimba "Hosana" na kutandika matawi ya mitende ili Yesu akanyage juu yake, hivyo ndivyo walivyoonyesha kufahamu kwao kwamba Yesu alikuwa ndiye yule yule Bwana aliyekuwa amewaokoa Israeli hapo kale (Zab. 118:25–26; Mt. 21:9, 15; Mk. 11:9–10; Yn. 12:13). Watu hawa walimtambua Kristo kama Masiya aliyesubiriwa kwa muda mrefu. Neno Hosana limekuwa likitumika katika kumsherehekea Masiya katika zama zote. (1 Ne. 11:6; 3 Ne. 11:14–17). Kelele za hosana zilijumuishwa katika ibada ya kuweka wakfu kwa Hekalu la Kirtland (M&M 109:79) na sasa ni sehemu ya ibada za uwekaji wakfu wa mahekalu ya kisasa.

Hosea

Nabii wa Agano la Kale aliyekuwa akitoa unabii katika ufalme wa kaskazini wa Israeli katika kipindi cha mwisho cha utawala wa Yeroboamu II. Aliishi katika wakati wa kuporomoko kwa taifa na maangamizi, kama matokeo ya dhambi ya Israeli.

Kitabu cha Hosea: Mada kuu ya kitabu hiki ni upendo wa Mungu kwa watu Wake. Kuwatia adabu Kwake kote kulifanyika katika upendo, na urejesho wa Israeli utatokana na upendo Wake (Hos. 2:19; 14:4). Kinyume chake, Hosea anaonyesha udanganyifu na uzinzi wa Israeli. Lakini Mungu bado anaweza kuangalia hatima ya ukombozi wa Israeli (Hos. 11:12–14:9).

Hubiri. *Ona pia* Injili; Kazi ya kimisionari

Kutoa ujumbe ambao hutoa ufahamu bora juu ya kanuni au mafundisho ya injili.

Bwana amenipaka mafuta niwahubirie habari njema wanyenyekevu, **Isa.** 61:1 (Lk. 4:16–21). Inuka, uende Ninawi, na ukawahubirie, **Yona** 3:2–10.

Tangu saa ile Yesu alianza kuhubiri, **Mt.** 4:17. Enendeni ulimwenguni kote, na mkaihubiri injili kwa kila kiumbe, **Mk.** 16:15. Sisi tunamhubiri Kristo aliyesulubiwa, **1 Kor.** 1:22–24. Alikwenda na akazihubiria Roho zilizokuwa kifungoni, **1 Pet.** 3:19.

Hapakuwa na chochote isipokuwa kulikuwa na kuhubiri na kuwachochea ili daima wawe katika woga wa kumwogopa Mungu, **Eno.** 1:23. Aliwaamuru wasihubiri chochote isipokuwa toba na imani juu ya Bwana, **Mos.** 18:20. Kuhubiriwa kwa neno kulikuwa na uelekeo mkubwa wa kuwaongoza watu kufanya yale yaliyo ya haki, **Alma** 31:5.

Hupaswi kudhani ya kuwa umeitwa kuhubiri hadi pale unapoitwa, **M&M** 11:15. Haitatolewa kwa yeyote kwenda kuhubiri injili isipokuwa ametawazwa, **M&M** 42:11. Injili hii itahubiriwa kwa kila taifa, **M&M** 133:37.

Injili ilianza kuhubiriwa tangu mwanzo, **Musa** 5:58.

Huduma kwa Wagonjwa. *Ona pia* Mafuta; Mikono, Kuweka juu ya; Paka mafuta; Ponya, Uponyaji; Ukuhani

Baraka itolewayo kwa mgonjwa na watu wenye Ukuhani wa Melkizedeki, inayojumuisha matumizi ya mafuta yaliyotakaswa na kuwekwa wakfu.

Weka mkono wako juu yake, **Mt.** 9:18. Yesu aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache na akawaponya, **Mk.**

6:5. Mitume wa Kristo waliwapaka kwa mafuta watu wengi walio kuwa wagonjwa na wakawaponya, **Mk.** 6:13. Wazee watawapaka mafuta na kuwaponya walio wagonjwa, **Yak. (Bib.)** 5:14–15.

Hamtawaponya wagonjwa isipokuwa mmeombwa na watakao kuponywa, **M&M** 24:13–14. Wazee wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, **M&M** 42:44. Weka mikono yako juu ya wagonjwa, nao watapona, **M&M** 66:9.

Huisha. *Ona pia* Ufufuko

Kufanya kuwa hai, kufufua, au kumbadilisha mtu ili aweze kuwa katika uwepo wa Mungu.

Mungu alituhuisha pamoja na Kristo, **Efe.** 2:4–5 (Kol. 2:6, 12–13). Kristo aliuawa katika mwili, bali alihuishwa na Roho, **1 Pet.** 3:18 (M&M 138:7).

Hakuna mtu aliyemwona Mungu, isipokuwa alihuishwa na Roho, **M&M** 67:11. Ukombozi ni kupitia kwake yeye ambaye huhuisha vitu vyote, **M&M** 88:16–17. Watakatifu watahuishwa na kutwaliwa kumlaki Kristo, **M&M** 88:96.

Adamu alihuishwa katika utu wa ndani, **Musa** 6:65.

Hukumu. *Ona pia* Amua, Hukumu; Ibilisi; Jehanamu; Mauti ya Kiroho; Wana wa Upotevu

Hali ya kuwa mtu amesimamishwa katika makuzi yake na kukataliwa kuingia mbele ya uso wa Mungu na utukufu Wake. Hukumu ipo katika viwango tofauti. Wale wote ambao hawapati utimilifu wa utukufu wa selestia, kwa kiwango fulani watakuwa wamezuiliwa katika makuzi na haki zao, nao watakuwa wamehukumiwa kwa kiwango hicho.

Ole wenu wanafiki! ninyi mtapata hukumu iliyo kubwa zaidi, **Mt.** 23:14. Mtu yule atakayemkufuru Roho Mtakatifu yu katika hatari ya hukumu ya milele, **Mk.** 3:29. Wale waliotenda maovu watatoka kwa ufufuo wa hukumu, **Yn.** 5:29 (3 Ne. 26:5). Alaye na kunywa pasipo kustahili, hula na kunywa hukumu yake mwenyewe, **1 Kor.** 11:29 (3 Ne. 18:28–29).

Asiye tubu, akabatizwa, na kustahmili hadi mwisho lazima atahukumiwa, **2 Ne.** 9:24 (Mk. 16:16; Eth. 4:18; M&M 68:9; 84:74). Waovu wangelikuwa na huzuni kubwa zaidi kwa kuishi pamoja na Mungu kuliko roho zilizo laaniwa katika jehanamu, **Morm.** 9:4.

Yule ambaye hafanyi lolote hadi ameamrishwa, huyo atahukumiwa, **M&M** 58:29. Mtu apokeaye utimilifu wa agano jipya na lisilo na mwisho lazima aishi kulingana na sheria, au la atahukumiwa, **M&M** 132:6.

Hukumu ya mwisho. *Ona pia* Amua, Hukumu; Shutuma, Shutumu; Yesu Kristo—Mwamuzi

Hukumu ya Mwisho ambayo itakuja baada ya Ufufuko. Mungu, kupitia Yesu Kristo, atamhukumu kila mtu ili kuamua utukufu wa milele atakao pokea. Hukumu hii itategemea utiifu wa kila mtu kwa amri za Mungu, ikiwa ni pamoja na kukubali kwake dhabihu ya Yesu Kristo ya kutulipia dhambi.

Baba amekabidhi hukumu yote kwa Mwana, **Yn.** 5:22. Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, **Rum.** 14:10. Wafu walihukumiwa kutokana na mambo yale yaliyokuwa yameandikwa, **Ufu.** 20:12 (M&M 128:6–7).

Kwa ajili ya matendo yako yote utaletwa katika hukumu, **1 Ne.** 10:20. Mitume Kumi na Wawili na wale wanafunzi Wanefi kumi na wawili watahukumu Israeli, **1 Ne.** 12:9–10 (M&M 29:12). Wote lazima waonekane mbele ya kiti cha hukumu cha yule aliye Mtakatifu, **2 Ne.** 9:15. Tayarisheni nafsi zenu kwa ajili ya ile siku tukufu, **2 Ne.** 9:46. Mnaweza kujifikiria ninyi wenyewe mkiwa mbele ya baraza la hukumu ya Mungu, **Alma** 5:17–25. Yesu Kristo atasimama kuuhukumu ulimwengu, **3 Ne.** 27:16.

Bwana atashuka chini na laana kwa hukumu juu ya wasiomcha mungu, **M&M** 133:2.

Huru, Uhuru. *Ona pia* Haki ya uamuzi; Ufungwa

Hali ya kuweza kujiamulia na kufikiri kwa uhuru au nguvu au uwezo wa kufanya maamuzi binafsi pasipo kulazamishwa. Katika maana ya kiroho, mtu anayetubu na kutii mapenzi ya Mungu anakuwa huru kutoka katika utumwa wa dhambi kwa njia ya Upatanisho wa Yesu Kristo (Mos. 5:8; Yn. 8:31–36).

Nitakwenda kwa uhuru: kwa kuwa nimejifunza mausia yako, **Zab.** 119:45.

Kweli itawaweka huru, **Yn.** 8:32. Wale wanaokuwa huru kutoka katika dhambi hupokea uzima wa milele, **Rum.** 6:19–23. Alipo roho wa Bwana ndipo, penye uhuru, **2 Kor.** 3:17. Simameni imara katika uhuru ambao kwa huo Kristo ametuweka huru, **Gal.** 5:1 (M&M 88:86).

Wanadamu wako huru kuchagua uhuru na uzima wa milele, **2 Ne.** 2:27. Tawi la wenye haki la nyumba ya Israeli litatolewa kutoka utumwani na kuwa katika uhuru, **2 Ne.** 3:5. Nchi hii itakuwa nchi ya uhuru, **2 Ne.** 10:11. Walimlilia Bwana kwa ajili ya uhuru wao, **Alma** 43:48–50. Moroni alisimika bendera ya uhuru miongoni mwa Wanefi, **Alma** 46:36. Moroni alijawa shangwe katika uhuru wa nchi yake, **Alma** 48:11. Roho wa Mungu ni roho ya uhuru, **Alma** 61:15.

Nifuateni, nanyi mtakuwa watu huru, **M&M** 38:22. Bwana na watumishi wake hutangaza uhuru kwa roho zilizo kifungoni, **M&M** 138:18, 31, 42.

Huruma. *Ona pia* Hisani; Rehema, enye Rehema; Upendo

Katika maandiko, huruma kwa maana halisi humaanisha "kuteseka pamoja na." Pia inamaanisha ni kuonyesha utu wema, kusikitika, na rehema kwa mtu mwingine.

Bwana aliwaagiza watu wake kuonyesha huruma, **Zek.** 7:8–10.

Yesu aliwahurumia, **Mt.** 9:36 (Mt. 20:34; Mk. 1:41; Lk. 7:13). Msamaria mmoja alimhurumia, **Lk.** 10:33. Mhurumiane, **1 Pet.** 3:8.

Kristo amejawa na huruma kwa watoto wa watu, **Mos.** 15:9. Matumbo yangu yamejawa na huruma juu yenu, **3 Ne.** 17:6.

Joseph Smith alisali kwa ajili ya huruma ya Bwana, **M&M** 121:3–5.

Husuda. *Ona pia* Tamani; Wivu, enye Wivu

Kulingana na maandiko, kutamani kitu fulani ambacho ni cha mtu mwingine ni kosa.

Mapatriaki, walisukumwa na husuda, wakamwuza Yusufu katika Misri, **Mdo.** 7:9. Hisani haihusudu, **1 Kor.** 13:4 (Moro. 7:45). Husuda hutokana na majivuno, **1 Tim.** 6:4. Palipo na husuda ndipo palipo na machafuko na kila tendo ovu, **Yak. (Bib.)** 3:16.

Bwana aliwaamuru wanadamu kwamba wasiwe na husuda, **2 Ne.** 26:32. Hapakuwa na husuda miongoni mwa watu wa Nefi, **4 Ne.** 1:15–18.

Husuda na ghadhabu za wanadamu zimekuwa ni jambo la kawaida siku zote za maisha yangu, **M&M** 127:2.

Hyde, Orson

Mshiriki wa Akidi ya kwanza ya Mitume Kumi na Wawili walioitwa katika kipindi hiki (M&M 68:1–3; 75:13; 102:3; 124:128–129). Alitumikia misheni nyingi kwa ajili ya Kanisa pamoja na kuiweka wakfu Nchi Takatifu katika mwaka 1841 kwa ajili ya kurudi kwa watu wa Kiyahudi.

Iba, Wizi

Kuchukua kitu fulani kutoka kwa mtu mwingine kinyume cha uaminifu au kinyume cha sheria. Bwana daima amewaamuru watoto Wake kuwa wasiibe (Ku. 20:15; Mt. 19:18; 2 Ne. 26:32; Mos. 13:22; M&M 59:6).

Jiwekeeni hazina mbinguni, mahali ambako wevi hawavunji wala kuiba, **Mt.** 6:19–21.

Kushindwa kwa Wanefi kulikuja kwa sababu ya kiburi, utajiri, uporaji, wizi, **Hel.** 4:12.

Mtu anayeiba na asitubu atatupwa nje, **M&M** 42:20. Wale wanaoiba watatolewa kwa sheria za nchi, **M&M** 42:84–85.

Ibada. *Ona pia* Hekalu, Nyumba ya Bwana; Kufunga, Muhuri, Tia; Nasaba; Wokovu; Wokovu kwa ajili ya Wafu

Kanuni au taratibu takatifu za kidini. Ibada inakuwa na matendo ambayo yana maana za kiroho. Ibada pia yaweza kumaanisha sheria na taratibu za Mungu.

Ibada katika Kanisa hujumuisha huduma kwa wagonjwa (Yak. [Bib.] 5:14–15), kubariki sakramenti (M&M 20:77, 79), ubatizo kwa kuzamishwa (Mt. 3:16; M&M 20:72–74), kubariki watoto (M&M 20:70), kutunukiwa Roho Mtakatifu (M&M 20:68; 33:15), kutunukiwa ukuhani (M&M 84:6–16; 107:41–52), ibada za hekaluni (M&M 124:39), na ndoa katika agano jipya na lisilo na mwisho (M&M 132:19–20).

Wafundisheni amri na sheria, **Ku.** 18:20. Waende katika amri zangu, na kushika maagizo yangu, **Eze.** 11:20.

Watu walikuwa wakamilifu katika kuzishika ibada za Mungu, **Alma** 30:3. Je, tumefaidika na nini kwa kuzishika ibada zake, **3 Ne.** 24:13–14.

Yule aombaye na ikiwa roho yake imependeka ninamkubali kama anazitii ibada zangu, **M&M** 52:14–19.

Wanadamu wote wanaweza kuokolewa, kwa utii kwa sheria na ibada za injili, **M ya I** 1:3.

Ibada zifanywazo kwa niaba ya wafu: Ibada za kidini zifanywazo na mtu aliye hai kwa niaba ya mtu aliyekufa. Ibada hizo huwa na matokeo tu pale wale ambao hufanyiwa ibada hizi wanapozikubali, kushika maagano yanayohusiana, na wanapokuwa wamefungwa kwa yule Roho Mtakatifu wa ahadi. Nazo hufanyika leo ndani ya mahekalu.

Je, wenye kubatizwa kwa ajili ya wafu watafanyaje, kama wafu hawafufuliwi kamwe, **1 Kor.** 15:29.

Ubatizo kwa ajili ya wafu utafanywa mahekaluni, **M&M** 124:29–36. Roho katika ulimwengu wa roho walifundishwa ubatizo kwa niaba ya wafu kwa ajili ya ondoleo la dhambi, **M&M** 138:29–34.

Ibada Iliyofanywa kwa Niaba ya. *Ona* Ibada—Ibada zifanywazo kwa niaba ya wafu; Wokovu kwa ajili ya Wafu

Ibilisi. *Ona pia* Jehanamu; Lusiferi; Mpinga Kristo; Mwangamizi; Roho—Pepo wachafu; Wana wa Upotevu

Shetani. Ibilisi ndiye adui wa haki na wa wale watafutao kutenda mapenzi ya Mungu. Huyu ni mwana halisi wa kiroho wa Mungu na wakati fulani alikuwa malaika mwenye mamlaka mbele za Mungu (Isa. 14:12; 2 Ne. 2:17). Hata hivyo, yeye aliasi kule mbinguni kabla ya maisha ya hapa duniani na akashawishi theluthi moja ya watoto wa kiroho wa Baba ili waasi pamoja naye (M&M 29:36; Musa 4:1–4; Ibr. 3:27–28). Wakafukuzwa kutoka mbinguni, wakanyimwa nafasi ya kupata miili yenye kufa na kupata uzoefu wa maisha ya mwili wenye kufa, nao watalaaniwa milele. Toka wakati ibilisi alipofukuzwa kutoka mbinguni, yeye wakati wote amekuwa akitafuta kuwadanganya wanaume na wanawake wote na kuwapeleka mbali na kazi za Mungu ili apate kuwafanya wanadamu wote wawe na huzuni kama yeye alivyo (Ufu. 12:9; 2 Ne. 2:27; 9:8–9).

Yesu akamkemea pepo, **Mt.** 17:18. Moto usio na mwisho uliowekwa tayari kwa ajili ya ibilisi na malaika zake, **Mt.** 25:41. Mpingeni ibilisi, naye atawakimbia, **Yak. (Bib.)** 4:7.

Waovu wataangushwa chini utumwani mwa ibilisi, **1 Ne.** 14:7. Ibilisi ndiye baba wa uongo wote, **2 Ne.** 2:18 (Musa 4:4). Ibilisi hutafuta wanadamu wote wapate kuwa na huzuni kama yeye alivyo, **2 Ne.** 2:27. Kama wenye mwili hawataamka tena, roho zetu lazima zingekuwa chini ya yule ibilisi, **2 Ne.** 9:8–9. Ibilisi ataghadhibika,

atasuluhisha, na atadanganya, **2 Ne.** 28:20–23. Lile lililo ovu latoka kwa yule ibilisi, **Omni** 1:25 (Alma 5:40; Moro. 7:12, 17). Jihadharini yasije mabishano yakaibuka miongoni mwenu, nanyi mkatii pepo mchafu, **Mos.** 2:32. Kama ninyi si kondoo wa mchungaji mwema, basi ibilisi ndiye mchungaji wenu, **Alma** 5:38–39. Ibilisi hatawasaidia watoto wake, **Alma** 30:60. Salini daima ili msipate kupotoshwa kwa majaribu ya yule ibilisi, **Alma** 34:39 (3 Ne. 18:15, 18). Jengeni msingi wenu juu ya Mkombozi ili dhoruba kali ya ibilisi isipate kuwa na nguvu juu yenu, **Hel.** 5:12. Ibilisi ndiye mwanzilishi wa dhambi zote, **Hel.** 6:26–31.

Ibilisi atafuta kuweka mpango wa hila, **M&M** 10:12. Na hapana budi kwamba ibilisi lazima awajaribu watoto wa watu, vinginevyo wasingeliweza kujiamulia wenyewe, **M&M** 29:39. Adamu akawa chini ya mamlaka ya ibilisi kwa sababu alijiingiza majaribuni, **M&M** 29:40. Wana wa upotevu watatawala pamoja na ibilisi na malaika zake katika milele, **M&M** 76:32–33, 44. Ibilisi atafungwa kwa miaka elfu moja, **M&M** 88:110 (Ufu. 20:2). Yule mwovu huondoa nuru na kweli, **M&M** 93:39.

Shetani hakuitunza hali yake ya kwanza, **Ibr.** 3:28.

Kanisa la ibilisi: Kila ovu na shirikisho la kilimwengu duniani ambalo hupotosha injili safi na kamili na ambalo hupingana na Mwanakondoo wa Mungu.

Ibilisi ndiye aliyeanzisha lile kanisa lililo kuu na la kuchukiza, **1 Ne.** 13:6 (1 Ne. 14:9). Kuna makanisa mawili tu, moja la Mwanakondoo wa Mungu na moja la ibilisi, **1 Ne.** 14:10 (Alma 5:39).

Usishindane na kanisa lolote, isipokuwa lile kanisa la ibilisi, **M&M** 18:20. Kanisa lile kuu na lenye kuchukiza litatupwa chini, **M&M** 29:21.

Ibrahimu. *Ona pia* Agano la Ibrahimu

Mwana wa Tera, aliyezaliwa katika Uru ya Ukaldayo (Mwa. 11:26, 31; 17:5). Nabii wa Bwana ambaye Bwana alifanya naye maagano ya milele, ambayo kupitia kwake mataifa yote ya dunia yamebarikiwa. Ibrahimu mwanzoni aliitwa Abramu.

Alihamia Harani, mahali ambapo Tera alikufa, **Mwa.** 11:31–32 (Ibr. 2:1–5). Aliitwa na Mungu asafiri kwenda Kanaani na kupokea agano takatifu, **Mwa.** 12:1–8 (Ibr. 2:4, 15–17). Alisafiri kwenda Misri, **Mwa.** 12:9–20 (Ibr. 2:21–25). Alikaa katika Hebroni, **Mwa.** 13:18. Alimkomboa Lutu, **Mwa.** 14:1–16. Alikutana na Melkizedeki, **Mwa.** 14:18–20. Hajiri alimzalia mwana wa kiume Ismaili, **Mwa.** 16:15–16. Jina lake lilibadilishwa na kuwa Ibrahimu, **Mwa.** 17:5. Bwana aliwaambia Ibrahimu na Sara ya kwamba wangepata mtoto mwanaume, **Mwa.** 17:15–22; 18:1–14. Sara akamzaa mwanawe wa kiume Isaka, **Mwa.** 21:2–3. Aliamriwa kumtoa dhabihu Isaka, **Mwa.** 22:1–18. Sara alikufa na akazikwa, **Mwa.** 23:1–2, 19. Ibrahimu alikufa na akazikwa, **Mwa.** 25:8–10.

Kukubali kwa Ibrahimu kumtoa sadaka Isaka ulikuwa ni mfano wa Mungu na Mwanawe wa Pekee, **Yak. (KM)** 4:5. Alilipa fungu la kumi kwa Melkizedeki, **Alma** 13:15. Alitabiri na kutoa ushuhuda wa kuja kwa Kristo, **Hel.** 8:16–17.

Alipokea ukuhani kutoka kwa Melkizedeki, **M&M** 84:14. Waaminifu hufanyika kuwa uzao wa Ibrahimu, **M&M** 84:33–34 (Gal. 3:27–29). Alipokea mambo yote kwa ufunuo na amepokea kuinuliwa kwake, **M&M** 132:29.

Alitafuta baraka za mababu na kuteuliwa katika ukuhani, **Ibr.** 1:1–4. Aliteswa na makuhani wa uongo wa Ukaldayo, **Ibr.** 1:5–15. Akaokolewa na Bwana, **Ibr.** 1:16–20. Alijifunza juu ya jua, mwezi, na nyota, **Ibr.** 3:1–14. Alijifunza juu ya maisha yetu kabla ya kuja duniani na juu ya Uumbaji, **Ibr.** 3:22–28.

Kitabu cha Ibrahimu: Maandishi ya Kale yalioandikwa na Ibrahimu ambayo yalikuja kuwa katika milki ya kanisa katika mwaka 1835. Maandishi hayo na maiti kadhaa zilizotiwa mumiani katika

makaburi ya watu huko Misri na Antonio Lebolo ambaye aliandika wosia kuwa yawe mali ya Michael Chandler. Chandler aliyaonyesha katika maonyesho ya mwaka 1835 huko Marekani. Baadhi ya marafiki wa Joseph Smith waliyanunua kutoka kwa Chandler na kumpa Nabii, ambaye aliyatafsiri. Baadhi ya maandishi haya sasa yanapatikana katika Lulu ya Thamani Kuu.

Mlango wa 1 umeandikwa juu ya matukio ya Ibrahimu katika Uru ya Ukaldayo, mahali ambako makuhani waovu walijaribu kumtoa yeye kuwa kafara. Mlango wa 2 unaelezea juu ya safari yake ya Kanaani. Bwana alimtokea na kufanya agano naye. Mlango wa 3 umeandikwa kwamba Ibrahimu aliuona uumbaji wote na akatambua mahusianao kati ya sayari za mbinguni. Mlango wa 4–5 ni maandiko mengine juu ya Uumbaji.

Uzao wa Ibrahimu: Watu ambao, kwa utiifu katika sheria na ibada za injili ya Yesu Kristo, hupokea ahadi na maagano yaliyofanywa na Mungu kwa Ibrahimu. Wanaume na wanawake wanaweza kupokea baraka hizi ikiwa wao ni wa uzao halisi wa Ibrahimu au ikiwa wao wamepangwa katika familia yake kwa kuikubali injili na kwa kubatizwa (Gal. 3:26–29; 4:1–7; M&M 84:33–34; 103:17; 132:30–32; Ibr. 2:9–11). Wazao halisi wa Ibrahimu pia wanaweza kupoteza baraka zao kwa kukosa utiifu (Rum. 4:13; 9:6–8).

Imani. *Ona* Amini, Imani

Imanueli. *Ona pia* Yesu Kristo

Mojawapo ya majina ya Yesu Kristo. Linatokana na maneno ya Kiebrania ambayo maana yake "Mungu pamoja nasi."

Imanueli ni jina na cheo kilichotolewa kama ishara ya kukombolewa na Mungu (Isa. 7:14). Maneno ya Isaya kwa Imanueli yametambuliwa hususani na Mathayo kama unabii juu ya kuzaliwa kwa Yesu katika mwili wa kufa (Mt. 1:18–25). Jina hili pia linaonekana katika maandiko ya siku za mwisho (2 Ne. 17:14; 18:8; M&M 128:22).

Imba. *Ona pia* Muziki; Wimbo

Kuabudu na kumsifu Mungu katika wimbo na beti za muziki.

Mwimbieni Bwana, **1 Nya.** 16:23–36 (Zab. 96). Mwimbieni Bwana, na mpeni shukrani, **Zab.** 30:4. Mfanyieni Bwana sauti za furaha, **Zab.** 100:1.

Walipokuwa wamekwisha kuimba wimbo wa Kanisa, walitoka kwenda katika mlima wa Mizeituni, **Mt.** 26:30.

Roho Mtakatifu aliwaongoza kuimba, **Moro.** 6:9.

Wimbo wa mwenye haki ni sala kwangu, **M&M** 25:12. Kama mmefurahi, msifuni Bwana kwa kuimba, **M&M** 136:28.

Injili. *Ona pia* Kipindi; Mafundisho ya Kristo; Mpango wa Ukombozi

Mpango wa Mungu wa wokovu, uliowezekana kwa njia ya Upatanisho wa Yesu Kristo. Injili inajumuisha kweli za milele au sheria za milele, maagano, na ibada zilizohitajika kwa mwanadamu kuingia tena katika uwepo wa Mungu. Mungu alirejesha utimilifu wa injili duniani katika karne ya 19 kupitia Joseph Smith Nabii.

Enendeni ulimwenguni kote na mkaihubiri injili, **Mk.** 16:15.

Sehemu za injili ya mwanakondoo na zenye thamani zilizuiliwa, **1 Ne.** 13:32. Hii ndiyo injili yangu, **3 Ne.** 27:13–21 (M&M 39:6).

Kitabu cha Mormoni kina utimilifu wa injili, **M&M** 20:8–9 (M&M 42:12). Hii ndiyo injili, **M&M** 76:40–43. Ukuhani wa Melkizedeki husimamia injili, **M&M** 84:19. Kila mtu atausikia utimilifu wa injili katika lugha yake mwenyewe, **M&M** 90:11. Mwana alihubiri injili kwa roho za wafu, **M&M** 138:18–21, 28–37.

Injili ilihubiriwa tangu mwanzo, **Musa** 5:58. Kanuni na ibada ya kwanza za injili zinaelezwa, **M ya I** 1:4.

Injili, Urejesho wa. *Ona* Urejesho wa Injili

Injili, Vitabu vya Biblia. *Ona pia* Luka; Marko; Mathayo; Yohana, Mwana wa Zebedayo

Taarifa nne zilizoandikwa au shuhuda za maisha ya duniani ya Yesu na matukio yahusuyo huduma Yake, iliyomo katika vitabu vinne vya kwanza vya Agano Jipya. Vimeandikwa na Mathayo, Marko, Luka, na Yohana, hizi ni shuhuda zilizoandikwa za maisha ya Kristo. Kitabu cha 3 Nefi katika Kitabu cha Mormoni kinalingana kwa namna nyingi na Injili hizi nne za Agano Jipya.

Vitabu vya Agano Jipya mwanzoni viliandikwa katika Kiyunani. Neno la Kiyunani injili maana yake "habari njema." Habari njema ni kwamba Yesu Kristo anafanya upatanisho ambao utawakomboa wanadamu wote kutokana na mauti na kumzawadia kila mtu kulingana na matendo yake (Yn. 3:16; Rum. 5:10–11; 2 Ne. 9:26; Alma 34:9; M&M 76:69).

Ona pia Upatanifu wa Injili katika kiambatisho.

Isaka. *Ona pia* Ibrahimu—Uzao wa Ibrahimu

Patriaki wa Agano la Kale. Kuzaliwa kwake kwa Ibrahimu na Sara wakiwa katika umri wa uzee ulikuwa ni muujiza (Mwa. 15:4–6; 17:15–21; 21:1–8). Kukubali kwa Ibrahimu kumtoa sadaka Isaka kulikuwa ni mfano wa Mungu na Mwanawe wa Pekee (Yak. [KM] 4:5). Isaka alikuwa mrithi wa ahadi za agano la Ibrahimu (Mwa. 21:9–12; 1 Ne. 17:40; M&M 27:10).

Isaka alizaliwa, **Mwa.** 21:1–7. Ilikuwa atolewe dhabihu juu ya Mlima Moria, **Mwa.** 22:1–19 (M&M 101:4). Alioa, **Mwa.** 24. Aliwakanya wanawe, **Mwa.** 27:1–28:9.

Amepokea kuinuliwa kwake pamoja na Ibrahimu na Yakobo, **M&M** 132:37 (Mt. 8:11).

Isakari. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Mwana wa Yakobo na Lea katika Agano la Kale (Mwa. 30:17–18; 35:23; 46:13). Wazao wake walikuja kuwa moja ya makabila kumi na mawili ya Israeli.

Kabila la Isakari: Baraka za Yakobo kwa Isakari zinapatikana katika Mwanzo 49:14–15. Baada ya kufanya makazi Kaanani, kabila hili lilipata baadhi sehemu ya nchi iliyo kuwa tajiri sana katika Palestina ikiwa pamoja na nyanda za Esdraloni. Ndani ya mipaka ya Isakari kulikuwa na sehemu kadhaa muhimu katika historia ya Uyahudi, kwa mfano, Karmeli, Megido, Dothani, Gilboa, Yezereeli, Taboa, na Nazarethi (Yos. 19:17–23).

Isaya

Nabii wa Agano la Kale aliyetoa unabii tangu mwaka 740–701 K.K. Kama mshauri mkuu wa Mfalme Hezekia, Isaya alikuwa na nguvu kubwa za kidini na kisiasa.

Yesu alikuwa akimnukuu Isaya mara nyingi zaidi kuliko Alivyomnukuu nabii mwingine yeyote. Petro, Yohana, na Paulo pia mara kwa mara walimnukuu Isaya, katika Agano Jipya. Kitabu cha Mormoni na Mafundisho na Maagano vina nukuu nyingi kutoka kwa Isaya kuliko kutoka kwa nabii mwingine yeyote navyo hutoa msaada mkubwa katika kumfafanua Isaya. Nefi aliwafundisha watu wake kutoka kwenye maandiko ya Isaya (2 Ne. 12–24; Isa. 2–14). Bwana aliwaambia Wanefi ya kwamba "maneno ya Isaya ni makuu" na kwamba mambo yote aliyoyatolea unabii yangetimia (3 Ne. 23:1–3).

Kitabu cha Isaya: Kitabu katika Agano la Kale. Unabii mwingi wa Isaya unahusiana na kuja kwa Mkombozi katika huduma Yake ya duniani (Isa. 9:6) na kama Mfalme Mkuu katika siku ya mwisho (Isa. 63). Pia alitoa unabii mwingi juu ya hali ya baadaye ya Israeli.

Mlango wa 1 ni utangulizi wa kitabu chote. Isaya 7:14; 9:6–7; 11:1–5; 53; na 61:1–3 zinaonyesha misheni ya Mwokozi. Mlango wa 2, 11, 12, na 35 hujishughulisha na matukio katika siku za mwisho, wakati injili itakaporejeshwa,

Israeli itakusanywa, na nchi yenye kiu itakapochanua kama ua la waridi. Mlango wa 29 ina unabii wa ujio wa Kitabu cha Mormoni (2 Ne. 27). Mlango wa 40–46 inatangaza ukuu wa Yehova kama Mungu wa kweli aliye juu ya miungu sanamu waabudiwao na wapagani. Milango inayobaki 47–66, hujishughulisha na matukio katika urejesho wa mwisho wa Israeli na kuanzishwa kwa Sayuni, pamoja na Bwana kukaa miongoni mwa watu Wake.

Ishara. *Ona pia* Ishara za Nyakati; Kanisa, Ishara za Kanisa la Kweli; Muujiza

Tukio au jambo ambalo watu wanalielewa kuwa ni ushahidi au thibitisho wa kitu fulani. Ishara kwa kawaida ni ono la kimuujiza kutoka kwa Mungu. Shetani pia anao uwezo wa kuonyesha ishara katika hali fulani. Watakatifu yawapasa kutafuta vipawa vya Roho lakini hawapaswi kutafuta ishara ili kuridhisha udadisi au kudumisha imani yao. Ila Bwana atatoa ishara kama Yeye aonavyo kuwa sahihi kwa wale wanaoamini (M&M 58:64).

Bwana mwenyewe atawapa ishara, **Isa.** 7:14 (2 Ne. 17:14). Mungu hutenda ishara na maajabu mbinguni na duniani, **Dan.** 6:27.

Kizazi kiovu na cha uzinzi chatafuta ishara, **Mt.** 12:39 (Mt. 16:4; Lk. 11:29). Ishara hizi zitawafuata wale wanaoamini, **Mk.** 16:17 (Morm. 9:24; Eth. 4:18; M&M 84:65).

Sheremu aliomba ishara, **Yak. (KM)** 7:13–20. Korihori aliuliza aone ishara, **Alma** 30:48–60. Tuonyeshe ishara ndipo tutaamini, **Alma** 32:17. Sehemu kubwa zaidi ya watu waliamini ishara na maajabu, **3 Ne.** 1:22. Watu walisahau ishara na maajabu yale, **3 Ne.** 2:1. Hamtapata ushahidi hadi baada ya jaribu la imani yenu, **Eth.** 12:6.

Msiombe miujiza, isipokuwa nitakapoamuru, **M&M** 24:13. Imani haiji kwa ishara, bali ishara huwafuata wale waaminio, **M&M** 63:7–11.

Katika siku zile watainuka Makristo wa uongo, na manabii wa uongo, na wataonyesha ishara kuu na maajabu, **JS—M** 1:22.

Ishara za Kanisa la Kweli. *Ona* Kanisa, Ishara za Kanisa la Kweli

Ishara za Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo. *Ona pia* Yesu Kristo

Matukio ambayo yaliambatana na kuzaliwa na kifo cha Yesu Kristo.

Kuzaliwa: Bikira atachukua mimba na kuzaa mtoto mwanamume, **Isa.** 7:14. Kutoka Bethlehemu atatokea mtawala katika Israeli, **Mika** 5:2.

Samweli Mlamani alitoa unabii juu ya mchana, usiku, na siku ya mwangaza; nyota mpya; na ishara nyingine, **Hel.** 14:2–6. Ishara zilitimia, **3 Ne.** 1:15–21.

Kifo: Samweli Mlamani alitoa unabii wa giza, ng'urumo za radi, na radi, na kutetemeka kwa dunia, **Hel.** 14:20–27. Ishara zilitimia, **3 Ne.** 8:5–23.

Ishara za Nyakati. *Ona pia* Ishara; Siku za Mwisho; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo

Matukio au uzoefu ambao Mungu huwapa watu ili kuonyesha kwamba kitu fulani muhimu katika kazi Zake kimetokea au karibu kitatokea. Katika siku za mwisho, ishara nyingi kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Mwokozi zimetolewa unabii. Ishara hizi huwaruhusu watu walio waaminifu kutambua mpango wa Mungu, kuonywa, na kujitayarisha.

Mlima wa nyumba ya Bwana utawekwa imara juu ya milima, **Isa.** 2:2–3. Bwana atatweka bendera na kuwakusanya Israeli, **Isa.** 5:26 (2 Ne. 15:26–30). Jua litatiwa giza na mwezi utaacha nuru yake isiangaze, **Isa.** 13:10 (Yoe. 3:15; M&M 29:14). Watu watavunja sheria na watalivunja agano lisilo na mwisho, **Isa.** 24:5. Wanefi watanena kama sauti kutoka mavumbini, **Isa.** 29:4 (2 Ne. 27). Israeli itakusanywa kwa nguvu, **Isa.** 49:22–23 (1 Ne. 21:22–23; 3 Ne. 20–21). Mungu atausimamisha ufalme ambao

hautaangamizwa, **Dan.** 2:44 (M&M 65:2). Vita, ndoto, na maono vitautangulia Ujio wa Pili, **Yoe.** 2. Mataifa yote yatakusanyika kupigana na Yerusalemu, **Zek.** 14:2 (Eze. 38–39). Siku ile inakuja ambayo itawaka kama tanuri, **Mal.** 4:1 (3 Ne. 25:1; M&M 133:64; JS—H 1:37).

Majanga makuu yatautangulia Ujio wa Pili, **Mt.** 24 (JS—M 1). Paulo aliuelezea ukengeufu na nyakati za siku za mwisho zenye hatari, **2 Tim.** 3–4. Manabii wawili watauawa na kufufuka katika Yerusalemu, **Ufu.** 11 (M&M 77:15). Injili itarejeshwa katika siku za mwisho kwa huduma ya malaika, **Ufu.** 14:6–7 (M&M 13; 27; 110:11–16; 128:8–24). Babilonia itaimarishwa na kuanguka, **Ufu.** 17–18.

Israeli itakusanywa kwa nguvu, **1 Ne.** 21:13–26 (Isa. 49:13–26; 3 Ne. 20–21). Hii ni ishara, ili mpate kujua ule wakati, **3 Ne.** 21:1. Kitabu cha Mormoni kitatokea kwa uwezo wa Mungu, **Morm.** 8.

Walamani watachanua, **M&M** 49:24–25. Waovu watawaua waovu, **M&M** 63:32–35 (Ufu. 9). Vita vitamiminwa juu ya mataifa yote, **M&M** 87:2. Ishara, mabadiliko ya vitu vya asili, na malaika kutengeneza njia kwa ajili ya ujio wa Bwana, **M&M** 88:86–94. Giza kufunika dunia, **M&M** 112:23–24. Bwana amewaamuru Watakatifu kujitayarisha kwa ajili ya Ujio wa Pili, **M&M** 133.

Ishmaili, Baba Mkwe wa Nefi. *Ona pia* Lehi, Baba wa Nefi

Mtu katika Kitabu cha Mormoni, ambaye pamoja na familia yake, aliungana na familia ya Lehi katika safari yao ya kwenda nchi ya ahadi.

Nefi na kaka zake walirudi Yerusalemu na kuwashawishi Ishmaili na familia yake waambatane na Lehi na familia yake kwenda nchi ya ahadi, **1 Ne.** 7:2–5. Familia hizi mbili walioana wao kwa wao, **1 Ne.** 16:7. Ishmaili alikufa nyikani, **1 Ne.** 16:34.

Ishmaili, Mwana wa Ibrahimu. *Ona pia* Hajiri; Ibrahimu

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Ibrahimu na Hajiri, Mmisri aliyekuwa mjakazi wa Sara (Mwa. 16:11–16). Bwana aliwaahidi wote Ibrahimu na Hajiri kwamba Ishmaili angelikuwa baba wa taifa kubwa (Mwa. 21:8–21).

Agano lilikuja kupitia Isaka na siyo Ishmaeli, **Mwa.** 17:19–21 (Gal. 4:22–5:1). Mungu alimbariki Ishmaili ili angekuwa mwenye kuzaa, **Mwa.** 17:20. Ishmaili alisaidia kumzika Ibrahimu, **Mwa.** 25:8–9. Wana kumi na wawili wa Ishmaili walipewa majina, **Mwa.** 25:12–16. Ishmaili alikufa, **Mwa.** 25:17–18. Esau alimchukua binti wa Ishmaili, Mahalati, kuwa mke wake, **Mwa.** 28:9.

Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa. *Ona pia* Hali ya Kufa, enye Kufa; Lipia dhambi, Upatanisho; Ufufuko; Wokovu; Yesu Kristo

Hali ya kuishi milele katika hali ya aliyefufuka, kutokuwa tena chini ya kifo cha kimwili.

Amefufuka, **Mk.** 16:6. Kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa, **1 Kor.** 15:22. Mauti humezwa wakati huu wa kufa utakapovaa kutokufa, **1 Kor.** 15:53–54. Kristo ameishinda mauti na kuleta hali ya kutokufa, **2 Tim.** 1:10.

Hali ya kutokufa ni kurejeshwa kwa roho katika mwili, **2 Ne.** 9:13. Roho zikiunganika pamoja na miili yao huwa na hali ya kutokufa, kamwe haifi tena, **Alma** 11:45.

Watu walio waaminifu watavikwa taji la hali ya kutokufa na uzima wa milele, **M&M** 75:5. Dunia itatakaswa na kuwa isiyo kufa, **M&M** 77:1 (M&M 130:9).

Kazi na utukufu wa Mungu ni kuleta hali ya kutokufa na uzima wa milele wa mwanadamu, **Musa** 1:39.

Isiyo Safi. *Ona* Safi na Isiyo safi

Israeli. *Ona pia* Ibrahimu—Uzao wa Ibrahimu; Upangaji watoto; Yakobo, Mwana wa Isaka

Bwana alimpa Yakobo jina la Israeli, mwana wa Isaka na mjukuu wa Ibrahimu katika Agano la Kale (Mwa. 32:28; 35:10). Jina Israeli laweza kutumiwa kwa Yakobo mwenyewe, wazao wake,

au kwa ufalme ambao wazao wake wakati fulani waliumiliki katika nyakati za Agano la Kale (2 Sam. 1:24; 23:3). Baada ya Musa kuwaongoza wana wa Israeli kutoka katika utumwa wa Misri (Ku. 3–14), walitawaliwa na waamuzi kwa zaidi ya miaka mia tatu. Wakianza na Mfalme Sauli, wafalme waliutawala muungano wa Israeli hadi kifo cha Sulemani, wakati makabila kumi yalipoasi kutoka kwa Rehoboamu ili kuanzisha taifa jingine. Baada ya ufalme wa Israeli kuwa umegawanyika, makabila ya kaskazini, kama sehemu iliyokuwa kubwa zaidi, yalishikilia jina la Israeli, wakati ule ufalme wa kusini ukaitwa Yuda. Nchi ya Kanaani pia siku hizi inaitwa Israeli. Katika maana nyingine, Israeli maana yake muumuni wa kweli wa Kristo (Rum. 10:1; 11:7; Gal. 6:16; Efe. 2:12).

Makabila kumi na mawili ya Israeli: Mjukuu wa Ibrahimu, Yakobo, ambaye jina lake lilibadilishwa na kuwa Israeli, alikuwa na wana kumi na wawili. Wazao wao wamekuja kujulikana kama makabila kumi na mawili ya Israeli au wana wa Israeli. Haya ndiyo makabila hayo kumi na mawili: Reubeni, Simeoni, Lawi, Yuda, Isakari, na Zebuluni (wana wa Yakobo na Lea); Dani, na Naftari (wana wa Yakobo na Bilha); Gadi na Asheri (wana wa Yakobo na Zilpa); Yusufu na Benjamini (wana wa Yakobo na Raheli) (Mwa. 29:32–30:24; 35:16–18).

Yakobo alimpa kila kiongozi wa kikabila baraka kabla ya kifo chake (Mwa. 49:1–28). Kwa taarifa zaidi, ona jina la kila mwana wa Yakobo.

Reubeni, mwana wa kiume wa kwanza wa mke wa kwanza wa Yakobo, Lea, alipoteza baraka ya haki yake ya uzaliwa wa kwanza na sehemu mbili ya urithi kwa sababu ya ukosefu wa maadili (Mwa. 49:3–4). Haki hiyo ya uzaliwa wa kwanza hatimaye ilikwenda kwa Yusufu, ambaye alikuwa mwana wa kwanza wa mke wa pili wa Yakobo, Raheli (1 Nya. 5:1–2). Lawi, ambaye kabila lake Bwana alikuwa amelichagua kumtumikia kama makuhani walio wahudumu Wake, hakupokea urithi kwa sababu ya wito wao maalumu wa kuhudumu miongoni mwa makabila yote. Hii iliruhusu sehemu mbili zigawiwe kwa wana wa Yusufu, Efraimu na Manase (1 Nya. 5:1; Yer. 31:9), ambao walihesabiwa kama makabila tofauti ya Israeli (TJS, Mwa. 48:5–6).

Watu wa kabila la Yuda walitakiwa kuwa watawala hadi Masiya alipokuja (Mwa. 49:10; TJS Mwa. 50:24 [Kiambatisho]). Katika siku za mwisho, kabila la Efraimu litakuwa na nafasi ya kupeleka ujumbe wa Urejesho wa injili ulimwenguni na kuwakusanya Israeli waliotawanyika (Kum. 33:13–17). Wakati utafika ambao kupitia injili ya Yesu Kristo, Efraimu atakuwa katika nafasi ya uongozi katika kuyaunganisha makabila yote ya Israeli (Isa. 11:12–13; M&M 133:26–34).

Kutawanyika kwa Israeli: Bwana aliwatawanya na kuwatesa makabila kumi na mawili ya Israeli kwa sababu ya uovu na uasi wao. Hata hivyo, Bwana pia alitumia kutawanyika huku kwa watu wateule Wake miongoni mwa mataifa ya ulimwengu ili kuyabariki mataifa hayo.

Nitawatawanya miongoni mwa walimwengu, **Law.** 26:33. Bwana atawatawanya miongoni mwa watu wote, **Kum.** 28:25, 37, 64. Nitawatoa watupwe huku na huko katika falme zote za dunia, **Yer.** 29:18–19. Nitaipepeta nyumba ya Israeli katika mataifa yote, **Amo.** 9:9 (Zek. 10:9).

Yesu alitumwa kwa kondoo waliopotea wa nyumba ya Israeli, **Mt.** 15:24. Kondoo wengine ninao ambao si wa kundi hili, **Yn.** 10:16.

Israeli atatawanyika juu ya uso wote wa dunia, **1 Ne.** 22:3–8. Yakobo anasimulia fumbo la Zenosi la miti ya mizeituni ya kupandikiza na ya porini, **Yak. (KM)** 5–6. Kazi ya Baba itaanza miongoni mwa makabila yaliyotawanywa, **3 Ne.** 21:26.

Kukusanyika kwa Israeli: Nyumba ya Israeli itakusanywa pamoja katika siku za mwisho kabla ya ujio wa Kristo (M ya I

1:10). Bwana huwakusanya watu Wake Israeli wanapomkubali Yeye na kuzishika amri Zake.

Atawatwekea bendera nao watakuja, **Isa.** 5:26. Kwa rehema nyingi nitawakusanya, **Isa.** 54:7. Israeli na Yuda watakusanywa katika nchi zao, **Yer.** 30:3. Bwana ataikusanya nyumba ya Israeli kutoka miongoni mwa watu walio tawanyika, **Eze.** 28:25.

Katika kipindi cha utimilifu wa nyakati atakusanya vitu vyote sehemu moja katika Kristo, **Efe.** 1:10.

Baada ya Israeli kutawanywa, watakusanywa, **1 Ne.** 15:12–17. Bwana atawakusanya ndani watu wote wa nyumba ya Israeli, **1 Ne.** 19:16 (3 Ne. 16:5). Watatolewa kutoka gizani na watajua kwamba Bwana ndiye Mwokozi wao, **1 Ne.** 22:12. Mungu huwakusanya na kuwahesabu watoto wake, **1 Ne.** 22:25. Mataifa ya Wayunani watawapeleka Israeli katika nchi zao za urithi, **2 Ne.** 10:8 (3 Ne. 16:4). Watu wangu na neno langu watakusanywa kama kitu kimoja, **2 Ne.** 29:13–14.

Wazee wameitwa ili kuwakusanya wateule, **M&M** 29:7 (M&M 39:11). Nitawakusanya wateule wangu, **M&M** 33:6. Kusanyikeni ili nipate kuwapa ninyi sheria yangu, na kwamba ili mpate kupewa endaumenti, **M&M** 38:31–33. Nitawarudisha tena watu wangu, ambao ni wa nyumba ya Israeli, **M&M** 39:11. Watakatifu watakuja, **M&M** 45:46. Musa alileta funguo za kukusanya, **M&M** 110:11.

Haki na kweli zitaifagia dunia na kuwakusanya wateule wa Bwana, **Musa** 7:62. Kukusanyika kunalinganishwa na kukusanyika kwa tai kwenye mzoga, **JS—M** 1:27.

Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea: Makabila haya kumi ya Israeli yaliunda ufalme wa kaskazini wa Israeli na walichukuliwa mateka katika Ashuru mwaka 721 K.K. Wakati huo walikwenda katika "nchi za kaskazini" na wakawa wamepotea katika ufahamu wa wenzao. Katika siku za mwisho watarudi.

Nitaiambia kaskazini, Toa, **Isa.** 43:6. Hawa watakuja kutoka kaskazini, **Isa.** 49:12 (1 Ne. 21:12). Yuda na Israeli watakuja pamoja kutoka nchi ya kaskazini, **Yer.** 3:18. Bwana yu hai, yeye aliyewaleta wana wa Israeli kutoka nchi ya kaskazini, **Yer.** 16:14–16. Nitawaleta kutoka nchi ya kaskazini, **Yer.** 31:8.

Wanefi na Wayahudi watapata maneno ya makabila yaliyopotea ya Israeli, **2 Ne.** 29:12–13. Ninakwenda kujionyesha mwenyewe kwa makabila yaliyopotea ya Israeli, **3 Ne.** 17:4. Injili ihubiriwapo kwa mabaki ya nyumba ya Israeli, makabila yaliyopotea yatakusanyika nyumbani katika nchi ya urithi wao, **3 Ne.** 21:26–29.

Musa alikabidhi funguo za kukusanyika kwa Israeli kwa Joseph Smith na Oliver Cowdery, **M&M** 110:11. Wale walio katika nchi za kaskazini watakumbukwa mbele za Bwana, **M&M** 133:26–32.

Tunaamini katika kukusanyika kuihalisi kwa Israeli, **M ya I** 1:10.

Ita, Itwa na Mungu, Wito. *Ona pia* Alichagua, Chagua, Chaguliwa (kitenzi); Kutawaza, Kutawazwa; Mamlaka; Msimamizi, Usimamizi; Teule, Wateule

Kuitwa na Mungu ni kupokea uteuzi au mwaliko kutoka Kwake au kiongozi Wake wa Kanisa aliye na mamlaka kisheria ya kumtumikia Yeye katika njia husika.

Akaweka mikono yake na akampa mausia, **Hes.** 27:23. Nimekutawaza kuwa nabii, **Yer.** 1:5.

Nimewachagua ninyi na kuwatawaza, **Yn.** 15:16. Paulo aliitwa kuwa Mtume, **Rum.** 1:1. Hapana mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima hii, ila yule aliyeitwa na Mungu, **Ebr.** 5:4. Yesu aliitwa na Mungu kwa mfano wa Melkizedeki, **Ebr.** 5:10.

Nimeitwa kulihubiri neno la Mungu kulingana na roho wa ufunuo na unabii, **Alma** 8:24. Makuhani waliitwa na kutayarishwa tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, **Alma** 13:3.

Kama unayo hamu ya kumtumikia

Mungu, umeitwa, **M&M** 4:3. Simama imara katika kazi niliyokuitia, **M&M** 9:14. Usidhani kwamba umeitwa kuhubiri, hadi pale utakapoitwa, **M&M** 11:15. Wazee wameitwa kutimiza kusanyiko la wateule, **M&M** 29:7. Hakuna atakaye hubiri injili yangu au kulijenga Kanisa langu isipokuwa ametawazwa, **M&M** 42:11. Walioitwa ni wengi, lakini wateule ni wachache, **M&M** 121:34.

Mtu lazima aitwe na Mungu, **M ya I** 1:5.

Jaribu, Majaribu. *Ona pia* Haki ya uamuzi; Ibilisi; Stahimili

Pima uwezo wa mtu wa kuchagua mema badala ya maovu; kishawishi cha kutenda dhambi na kumfuata Shetani badala ya Mungu.

Usitutie majaribuni, lakini utuokoe na ovu, **Mt.** 6:13 (3 Ne. 13:12). Mungu hatawaacha mjaribiwe kupita mwezayo kuvumilia, **1 Kor.** 10:13. Kristo alijaribiwa kama sisi, **Ebr.** 4:14–15. Heri mtu yule mwenye kustahmili majaribu, **Yak. (Bib.)** 1:12–14.

Majaribu ya adui hayawezi kuwalemea wale wanaosikiliza neno la Mungu, **1 Ne.** 15:24 (Hel. 5:12). Mwanadamu hangeweza kujichagulia mwenyewe isipokuwa alishawishiwa na kimoja au kingine, **2 Ne.** 2:11–16. Kesheni na kusali daima, ili msipate kujaribiwa kupita lile mnaloweza kuvumilia, **Alma** 13:28. Wafundisheni kuhimili kila jaribu la ibilisi, kwa imani yao juu ya Bwana Yesu Kristo, **Alma** 37:33. Salini daima msije mkaingia majaribu, **3 Ne.** 18:15, 18 (M&M 20:33; 31:12; 61:39).

Jihadhari na kiburi, usije ukaingia majaribuni, **M&M** 23:1. Adamu akawa chini ya mapenzi ya ibilisi kwa sababu alikubali majaribu, **M&M** 29:39–40.

Niliachwa katika namna zote za majaribu, **JS—H** 1:28.

Jehanamu. *Ona pia* Hukumu; Ibilisi; Mauti ya Kiroho; Wana wa Upotevu

Ufunuo wa siku za mwisho huzungumzia jehanamu katika maana zipatazo karibu mbili. Ya kwanza, ni mahali pa makazi ya muda katika ulimwengu wa roho kwa wale ambao hawakuwa watiifu katika maisha ya duniani. Katika maana hii, jehanamu ina mwisho. Roho hizo zitafundishwa injili, na wakati mwingine baada ya toba zao wataweza kufufuka katika daraja la utukufu ambalo watakuwa wanastahili. Wale ambao hawatatubu, lakini hata hivyo wao siyo wana wa upotevu, watabakia katika jehanamu wakati wote wa milenia. Baada ya miaka hii elfu moja ya mateso, watafufuliwa katika utukufu wa telestia (M&M 76:81–86; 88:100–101).

Ya pili, ni mahali pa kudumu pa wale wasiokombolewa kwa Upatanisho wa Yesu Kristo. Katika maana hii, jehanamu ni ya kudumu. Ni kwa ajili ya wale wanaopatikana kuwa "bado wachafu" (M&M 88:35, 102). Hapa ni mahali ambapo Shetani, malaika zake, na wana wa upotevu—wale ambao wamemkataa Mwana baada ya Baba Kumfunua kwao—watakaa hapo milele (M&M 76:43–46).

Maandiko wakati mwingine huitaja jehanamu kama giza la nje.

Nafsi ya Daudi haitaachwa katika jehanamu, **Zab.** 16:10 (Zab. 86:13).

Nenda zako jehanamu, kwenye ule moto ambao kamwe hautazimika, **Mk.** 9:43 (Mos. 2:38). Yule tajiri aliyekuwa katika jehanamu akainua macho yake, akiwa katika mateso, **Lk.** 16:22–23 (M&M 104:18). Mauti na jehanamu ikawatoa wafu waliokuwamo, **Ufu.** 20:13.

Kuna mahali palipotayarishwa, ndiyo, hata ile jehanamu ya kutisha, **1 Ne.** 15:35. Matakwa ya mwili humpa roho wa ibilisi uwezo wa kututumbukiza jehanamu, **2 Ne.** 2:29. Kristo aliitengeneza njia ya ukombozi wetu kutoka katika mauti na jehanamu, **2 Ne.** 9:10–12. Wale wanaobaki wachafu huingia katika mateso yasiyo na mwisho, **2 Ne.** 9:16. Ibilisi huzidanganya nafsi zao na kwa uangalifu mkubwa huwaongoza jehanamu, **2 Ne.** 28:21. Yesu ameikomboa nafsi yangu kutoka jehanamu,

2 Ne. 33:6. Jifungueni wenyewe kutoka katika uchungu wa jehanamu, **Yak. (KM)** 3:11. Kuchukuliwa mateka na ibilisi na kuongozwa na matakwa yake hadi kuangamizwa ndiyo minyororo ya jehanamu, **Alma** 12:11. Waovu watatupwa katika giza la nje hadi wakati wa ufufuko wao, **Alma** 40:13–14. Wachafu wangekuwa na huzuni zaidi kukaaa pamoja na Mungu kuliko kukaa jehanamu, **Morm.** 9:4.

Adhabu itolewayo kutoka mkononi mwangu ni adhabu isiyo na mwisho, **M&M** 19:10–12. Jehanamu ni mahali palipo andaliwa kwa ajili ya ibilisi na malaika zake, **M&M** 29:37–38. Wale wenye kumtambua Mungu watakombolewa kutoka mauti na minyororo ya jehanamu, **M&M** 138:23.

Jicho, Macho

Katika maandiko, jicho daima limetumika kama ishara ya uwezo wa mtu kupokea nuru ya Mungu. Kama ishara, jicho la mtu pia huonyesha hali ya kiroho na uelewa wa mambo ya Mungu.

Amri ya Bwana ni safi, huyatia macho nuru, **Zab.** 19:8. Wajinga wana macho na hawaoni, **Yer.** 5:21 (Mk. 8:18).

Taa ya mwili ni jicho, **Mt.** 6:22 (Lk. 11:34; 3 Ne. 13:22; M&M 88:67). Heri macho yenu, kwa kuwa yanaona, **Mt.** 13:16. Macho yenu ya ufahamu yatatiwa nuru, **Efe.** 1:17–18.

Ole wao walio na hekima katika macho yao wenyewe, **2 Ne.** 15:21 (Isa. 5:21). Walianza kufunga na kusali ili macho ya watu yapate kufunguliwa, **Mos.** 27:22. Shetani aliyapofusha macho yao, **3 Ne.** 2:2. Hakuna anayeweza kuwa na uwezo wa kukitoa Kitabu cha Mormoni isipokuwa kwa jicho kuwa tu kwa utukufu wa Mungu, **Morm.** 8:15.

Kwa uwezo wa Roho macho yetu yakafunguliwa na ufahamu wetu ukaangazwa, **M&M** 76:12. Nuru hutoka kwake yeye aangazaye macho yako, **M&M** 88:11. Kama jicho lako likiwa katika utukufu wangu, mwili wako wote utajawa na nuru, **M&M** 88:67.

Jina la Kanisa. *Ona* Kanisa, Jina la; Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

Jiwe la pembeni. *Ona pia* Yesu Kristo

Jiwe kuu lifanyalo kona ya msingi wa jengo. Yesu Kristo anaitwa jiwe kuu la pembeni (Efe. 2:20).

Jiwe walilolikataa waashi limekuwa jiwe kuu la pembeni, **Zab.** 118:22 (Mt. 21:42–44; Mk. 12:10; Lk. 20:17; Mdo. 4:10–12).

Wayahudi walilikataa jiwe la pembeni, **Yak. (KM)** 4:15–17.

Joseph Smith Mdogo. *Ona* Smith, Joseph, Mdogo

Jumapili. *Ona* Siku ya Sabato

Kaburi. *Ona pia* Ufufuko

Mahali pa kuzika mwili ufao. Kwa sababu ya Upatanisho, kila mtu atafufuka kutoka kaburini.

Baada ya ufufuko wa Kristo, makaburi yakafunuka na miili mingi ikainuka, **Mt.** 27:52–53 (3 Ne. 23:9–13). Ewe kaburi, u wapi ushindi wako, **1 Kor.** 15:55.

Kaburi ni lazima liwatoe wafu wake, **2 Ne.** 9:11–13.

Wale waliolala kaburini watatoka, **M&M** 88:97–98. Kisima cha ubatizo ni ishara ya kaburi, **M&M** 128:12–13.

Kaini. *Ona pia* Adamu; Habili; Makundi maovu ya siri; Mauaji

Mwanawe Adamu na Hawa ambaye alimuua kaka yake mdogo Habili (Mwa. 4:1–16).

Sadaka yake ilikataliwa na Bwana, **Mwa.** 4:3–7 (Musa 5:5–8, 18–26). Alimwua kaka yake Habili, **Mwa.** 4:8–14 (Musa 5:32–37). Bwana akaweka laana na alama juu yake, **Mwa.** 4:15 (Musa 5:37–41).

Adamu na Hawa walikuwa na wana na mabinti wengi kabla ya kuzaliwa yeye, **Musa** 5:1–3, 16–17. Alimpenda Shetani zaidi kuliko Mungu, **Musa** 5:13,

18. Akaingia katika agano lisilo takatifu na Shetani, **Musa** 5:29–31.

Kaisari

Katika Agano Jipya, ni cheo ambacho baadhi ya wafalme wa Kirumi walijulikana. Nacho hutumika katika maandiko kama ishara ya serikali za kiulimwengu au nguvu.

Mlipeni Kaisari yaliyo ya Kaisari, **Mt.** 22:21 (Mk. 12:17; Lk. 20:25; M&M 63:26).

Kaka, Ndugu. *Ona pia* Dada; Mwanadamu, Wanadamu; Mwanamke, Wanawake

Kama watoto wa Baba yetu wa Mbinguni, wanaume na wanawake wote ni kaka na dada kiroho. Katika Kanisa, waumini wa kiume na marafiki wa Kanisa mara kwa mara huitwa kama akina kaka.

Utakapoongoka, waimarishe ndugu zako, **Lk.** 22:32. Yeye asiyempenda nduguye akaa katika mauti, **1 Yoh.** 3:10–17.

Fikirieni ndugu zenu kama mjifikiriavyo ninyi wenyewe, **Yak. (KM)** 2:17.

Na kila mtu amheshimu kaka yake kama anavyojiheshimu mwenyewe, **M&M** 38:24–25. Waimarishe ndugu zako katika mazungumzo yako yote, **M&M** 108:7.

Kalebu

Mmoja wa wale waliotumwa na Musa kuchunguza nchi ya Kanaani katika mwaka wa pili baada ya Kutoka. Yeye na Yoshua pekee yao walirudisha taarifa ya kweli juu ya nchi (Hes. 13:6, 30; 14:6–38). Wao pekee yao kati ya wale wote waliondoka Misri walisalia katika ile miaka arobaini ya nyikani (Hes. 26:65; 32:12; Kum. 1:36) na kuingia Kanaani (Yos. 14:6–14; 15:13–19).

Kalvari. *Ona* Golgotha

Kamilifu

Kamili, nzima, na iliyo komaa; adilifu kabisa. Kamilifu inaweza pia kumaanisha pasipo dhambi au uovu. Ni Kristo pekee ndiye aliyekuwa mkamilifu kabisa. Wafuasi wa kweli wa Kristo wanaweza kuwa wakamilifu kwa njia ya neema na Upatanisho Wake.

Mioyo yenu na iwe kamili kwa Bwana, **1 Fal.** 8:61.

Basi ninyi mtakuwa wakamilifu hata kama Baba yenu wa mbinguni alivyo mkamilifu, **Mt.** 5:48 (3 Ne. 12:48). Mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu, **Yak. (Bib.)** 3:2.

Imani sio kuwa na ufahamu mkamilifu juu ya mambo, **Alma** 32:21, 26. Upatanisho ulifanyika ili Mungu apate kuwa Mungu mkamilifu, **Alma** 42:15. Moroni alikuwa mtu mwenye ufahamu mkamilifu, **Alma** 48:11–13, 17–18. Roho ya Kristo imetolewa kwa kila mtu ili apate kuhukumu na kujua kwa ufahamu kamili ikiwa kitu fulani ni cha Mungu au cha ibilisi, **Moro.** 7:15–17. Njooni kwa Kristo, na mkakamilike ndani yake, **Moro.** 10:32.

Endeleeni katika subira hadi mtakapokuwa mmekamilika, **M&M** 67:13. Hawa ndiyo wale watu wenye haki waliokamilishwa kwa njia ya Yesu, **M&M** 76:69. Ofisi zilizoko katika Kanisa ni kwa ajili ya kuwakamilisha Watakatifu, **M&M** 124:143 (Efe. 4:11–13). Walio hai hawakamiliki pasipo wafu wao, **M&M** 128:15, 18.

Nuhu alikuwa mtu mwenye haki, na mkamilifu katika kizazi chake, **Musa** 8:27.

Kanaani, Mkananayo

Katika nyakati za Agano la Kale, ni mtoto wa nne wa kiume wa Hamu (Mwa. 9:22; 10:1, 6) na ni mjukuu wa Nuhu. Mkananayo humwelezea mtu aliyetoka nchi ambako Kanaani mwanzoni aliishi na pia kwa wazao wake. Mkananayo lilikuwa pia jina la watu ambao waliishi nchi za bondeni kando ya pwani ya Mediterania ya Palestina. Jina hili wakati mwingine lilitumika kuwaelezea watu wasio Waisraeli walio wakazi wa nchi ya magharibi mwa Yordani, ambao Wayunani waliwaita Wafoeniki.

Kanisa, Ishara za Kanisa la Kweli.
Ona pia Ishara; Kanisa la Yesu Kristo; Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

Mafundisho na matendo ya Kanisa ambayo yanaonyesha kuwa limekubaliwa na Mungu na ni njia ambayo Bwana ameiweka kwa ajili ya watoto Wake kupata utimilifu wa baraka Zake. Baadhi ya ishara za Kanisa la kweli ni kama zifuatazo:

Ufahamu sahihi wa Uungu: Mungu akamwumba mtu kwa mfano wake mwenyewe, **Mwa.** 1:26–27. Bwana akasema na Musa uso kwa uso, **Ku.** 33:11.

Na uzima wa milele ni kumjua Mungu Baba na Yesu Kristo, **Yn.** 17:3.

Baba na Mwana wana miili ya nyama na mifupa, **M&M** 130:22–23.

Baba na Mwana walimtokea Joseph Smith, **JS—H** 1:15–20. Tunaamini katika Mungu Baba wa Milele, **M ya I** 1:1.

Kanuni na ibada za Kwanza: Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, **Yn.** 3:3–5. Tubuni na mkabatizwe, kila mmoja wenu, katika jina la Yesu Kristo, **Mdo.** 2:38. Ndipo wakaweka mikono yao juu yao, nao wakampokea Roho Mtakatifu, **Mdo.** 8:14–17. Mmekuwa watoto wa Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo, **Gal.** 3:26–27.

Tubuni, na mkabatizwe katika jina la Mwanangu mpendwa, **2 Ne.** 31:11–21.

Wale walioamini walibatizwa na kumpokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono, **M&M** 76:50–53.

Ukuhani sahihi unahitajika ili kubatiza na kutoa kipawa cha Roho Mtakatifu, **JS—H** 1:70–72. Kanuni na maagizo ya Kwanza ya injili yanaelezwa, **M ya I** 1:4.

Ufunuo: Mahali pasipo na maono, watu huangamia, **Mit.** 29:18. Bwana hufunua siri zake kwa manabii wake, **Amo.** 3:7.

Kanisa limejengwa juu ya mwamba wa ufunuo, **Mt.** 16:17–18 (M&M 33:13).

Ole kwa yule atakayesema Bwana hafanyi kazi tena kwa ufunuo, **3 Ne.** 29:6.

Mafunuo na amri huja tu kupitia kwa mtu aliyeteuliwa, **M&M** 43:2–7.

Tunaamini yale yote Mungu aliyoyafunua, **M ya I** 1:9.

Manabii: Kanisa limejengwa juu ya msingi wa Mitume na manabii, **Efe.** 2:19–20. Mitume na manabii ni muhimu kwa Kanisa, **Efe.** 4:11–16.

Joseph Smith aliitwa kuwa mwonaji, nabii, na Mtume, **M&M** 21:1–3.

Tunaamini katika manabii, **M ya I** 1:6.

Mamlaka: Yesu aliwapa wanafunzi wake uwezo na mamlaka, **Lk.** 9:1–2 (Yn. 15:16).

Nefi, mwana wa Helamani, alikuwa na mamlaka makubwa kutoka kwa Mungu, **Hel.** 11:18 (3 Ne. 7:17).

Nabii atapokea amri kwa ajili ya Kanisa, **M&M** 21:4–5. Hapana mtu atakaye hubiri injili au kujenga Kanisa isipokuwa yeye ametawazwa na mtu aliye na mamlaka, **M&M** 42:11. Wazee watahubiri injili, wakitenda hivyo kwa mamlaka, **M&M** 68:8.

Mtu yeyote anayehubiri au kuhudumu kwa ajili ya Mungu ni lazima awe ameitwa na Mungu kupitia wale walioko katika mamlaka, **M ya I** 1:5.

Maandiko nyongeza ya yatakuja: Kijiti cha Yuda kitaungana na kijiti cha Yusufu, **Eze.** 37:15–20.

Kutokea kwa maandiko siku za mwisho kulitabiriwa, **1 Ne.** 13:38–41.

Tunaamini kwamba Mungu bado atafunua mambo mengi yaliyo makubwa na muhimu, **M ya I** 1:9.

Muundo wa Kanisa: Kanisa limejengwa juu ya msingi wa Mitume na manabii, **Efe.** 2:19–20. Mitume na manabii ni muhimu kwa Kanisa, **Efe.** 4:11–16. Kristo ni Kichwa cha Kanisa, **Efe.** 5:23.

Kanisa la Kristo ni lazima liitwe katika jina lake, **3 Ne.** 27:8.

Tunaamini katika muundo ule ule ambao ulikuwepo katika Kanisa la Awali, **M ya I** 1:6.

Kazi ya Umisionari: Kwa hiyo, enendeni, na mkawafundishe mataifa yote,

Mt. 28:19–20. Sabini waliitwa ili kuhubiri injili, **Lk.** 10:1.

Wao walitamani kwamba wokovu utangazwe kwa kila kiumbe, **Mos.** 28:3.

Wazee watakwenda, wakiitangaza injili yangu, wawili wawili, **M&M** 42:6. Injili lazima ihubiriwe kwa kila kiumbe, **M&M** 58:64.

Vipawa vya Kiroho: Wakaanza kunena kwa lugha nyingine, **Mdo.** 2:4. Wazee watawaponya wagonjwa, **Yak. (Bib.)** 5:14.

Msikatae karama za Mungu, **Moro.** 10:8.

Vipawa vya kiroho vimeorodheshwa, **M&M** 46:13–26 (1 Kor. 12:1–11; Moro. 10:9–18).

Mahekalu: Nitafanya agano nao na kuweka patakatifu pangu katikati yao milele daima, **Eze.** 37:26–27. Bwana atalijilia hekalu lake ghafla, **Mal.** 3:1.

Nefi alijenga hekalu, **2 Ne.** 5:16.

Watakatifu wanarudiwa kwa kushindwa kujenga nyumba ya Bwana, **M&M** 95 (M&M 88:119). Watu wa Bwana daima walijenga mahekalu kwa ajili ya utendaji wa ibada takatifu, **M&M** 124:37–44. Kujenga mahekalu na kufanya ibada ni sehemu ya kazi kubwa ya siku za mwisho, **M&M** 138:53–54.

Kanisa, Jina la. *Ona pia* Kanisa la Yesu Kristo; Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho; Wamormoni

Katika Kitabu cha Mormoni, ni wakati Yesu Kristo alipowatembelea Wanefi wenye haki muda mfupi baada ya Ufufuko Wake, Yeye alisema kwamba Kanisa Lake lapaswa kubeba jina Lake (3 Ne. 27:3–8). Katika nyakati za sasa Bwana alifunulia jina la Kanisa kuwa ni "Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho" (M&M 115:4).

Kanisa, Lililo Kuu na Lenye Kuchukiza. *Ona* Ibilisi—Kanisa la ibilisi

Kanisa Kuu na Lenye Machukizo. *Ona* Ibilisi—Kanisa la ibilisi

Kanisa la Yesu Kristo. *Ona pia* Kanisa, Ishara za Kanisa la Kweli; Kanisa, Jina la; Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho; Mtakatifu; Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni; Urejesho wa Injili

Kundi lililoasisiwa la waamio ambao wamejichukulia juu yao wenyewe jina la Yesu Kristo kwa ubatizo na uthibitisho. Ikiwa litakuwa la kweli sharti liwe Kanisa la Bwana; sharti liwe na mamlaka Yake, mafundisho yake, sheria zake, ibada zake, na jina lake; na sharti litawaliwa na Yeye kupitia kwa wawakilishi ambao Yeye amewateua.

Bwana akalizidisha kanisa kila siku, **Mdo.** 2:47. Sisi tulio wengi tu mwili mmoja katika Kristo, **Rum.** 12:5. Katika Roho mmoja sisi sote tulibatizwa kuwa mwili mmoja, **1 Kor.** 12:13. Kanisa limejengwa juu ya msingi wa Mitume na manabii, **Efe.** 2:19–20. Mitume na manabii ni muhimu kwa Kanisa, **Efe.** 4:11–16. Kristo ni Kichwa cha Kanisa, **Efe.** 5:23.

Licha ya kuwa na makanisa mengi, yote yalikuwa kanisa moja, **Mos.** 25:19–22. Kanisa lilitakaswa na kuratibiwa, **Alma** 6:1–6. Kanisa la Kristo ni lazima liitwe katika jina lake, **3 Ne.** 27:8. Washiriki wa Kanisa walikutana pamoja kila mara, kufunga na kuomba na kuzungumza, **Moro.** 6:5.

Hili ndilo kanisa la pekee na lililo hai, **M&M** 1:30. Kanisa la Kristo liliibuka katika hizi siku za mwisho, **M&M** 20:1. Bwana huwaita watumishi wake kulijenga Kanisa lake, **M&M** 39:13. Kwani hivyo ndivyo, Kanisa langu litakavyoitwa katika siku za mwisho, **M&M** 115:4.

Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. *Ona pia* Kanisa, Ishara za Kanisa la Kweli; Kanisa, Jina la; Kanisa la Yesu Kristo; Urejesho wa Injili

Jina lililotolewa kwa Kanisa la Kristo katika siku za mwisho ili kutofautisha na Kanisa katika vipindi vingine (M&M 115:3–4).

Bwana atamwaga maarifa juu ya Watakatifu wa Siku za Mwisho, **M&M** 121:33. Joseph Smith ni nabii na mwonaji wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, **M&M** 127:12. Siku ile kuu ya Bwana i karibu kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho, **M&M** 128:21, 24. Joseph Smith amesaidia kuwakusanya Watakatifu wa Siku za Mwisho, **M&M** 135:3. Makundi ya Watakatifu wa Siku za Mwisho yaundwe kwa ajili ya safari ya kwenda nchi ya magharibi ya Marekani, **M&M** 136:2. Sheria za ndoa zinafafanuliwa kwa ajili ya Watakatifu wa Siku za Mwisho, **TR** 1. Ukuhani unatolewa kwa wanaume wote wenye kustahili walio waumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, M&M **TR**—2.

Maelezo ya juu ya Ono la Kwanza kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho yatolewa, **JS—H** 1:1.

Kanisa Lenye Kuchukiza. *Ona* Ibilisi—Kanisa la ibilisi

Kanoni. *Ona pia* Biblia; Kitabu cha Mormoni; Lulu ya Thamani Kuu; Maandiko; Mafundisho na Maagano

Mkusanyiko wa vitabu vitakatifu vinavyotambuliwa, na vinavyoaminika. Katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, vitabu vya kanoni vinaitwa vitabu vitakatifu navyo vinajumuisha Agano la Kale na Jipya, Kitabu cha Mormoni, Mafundisho na Maagano, na Lulu ya Thamani Kuu.

Kanuni. *Ona pia* Injili

Mafundisho, kweli, au sheria ya msingi. Kanuni za kwanza za injili ni imani katika Bwana Yesu Kristo na toba (M ya I 1:4).

Bila kuacha kanuni za mafundisho ya Kristo, tukaze mwendo ili tuufikie utimilifu, **TJS, Ebr.** 6:1.

Wazee, makuhani, na walimu watafundisha kanuni za injili yangu, zilizoko katika maandiko, **M&M** 42:12. Fundishaneni kwa ukamilifu zaidi katika kanuni, katika mafundisho, katika mambo yote, **M&M** 88:78 (M&M 97:14). Kila mtu anaweza kutenda katika mafundisho na kanuni kulingana na uhuru wa kujiamulia niliompa, **M&M** 101:78. Kanuni yoyote ile ya maarifa tujifunzayo katika maisha haya itafufuka pamoja nasi katika ufufuko, **M&M** 130:18–19.

Kanuni za Kwanza za Injili. *Ona* Amini, Imani; Batiza, Ubatizo; Roho Mtakatifu; Toba, Tubu

Karama. *Ona pia* Kipawa cha Roho Mtakatifu; Vipawa vya Roho

Mungu humpa mwanadamu baraka nyingi na karama.

Kuna karama nyingi za kiroho, **1 Kor.** 12:4–10. Takeni sana karama zilizo bora, **1 Kor.** 12:31. Kila kitolewacho kilicho kamili, hutoka kwa Mungu, **Yak. (Bib.)** 1:17.

Uwezo wa Roho Mtakatifu ni karama ya Mungu, **1 Ne.** 10:17. Wale wasemao hakuna karama hawajui injili ya Kristo, **Morm.** 9:7–8. Kila karama iliyo njema yatoka kwa Kristo, **Moro.** 10:8–18.

Uzima wa milele ndicho kipawa kilicho kikuu kuliko vyote, **M&M** 14:7 (1 Ne. 15:36). Karama hutolewa kwa wale wenye kumpenda Bwana, **M&M** 46:8–11. Wote hawana kila karama iliyotolewa kwao, **M&M** 46:11–29.

Karamu ya Bwana. *Ona* Sakramenti

Karamu ya Mwisho. *Ona pia* Pasaka; Sakramenti

Kulingana na Agano Jipya, ni chakula cha mwisho ambacho Yesu alikula kabla ya kukamatwa Kwake na kusulubiwa (Lk. 22:14–18). Yeye pamoja na Mitume Wake Kumi na Wawili walikula mlo huu wakati wa Pasaka (Mt. 26:17–30; Mk. 14:12–18; Lk. 22:7–13).

Mwokozi aliubariki mkate na divai na akawapa Mitume, **Mt.** 26:26–29 (Mk. 14:22–25; Lk. 22:7–20). Yesu aliosha miguu ya Mitume, **Yn.** 13. Yuda alitajwa kama ndiye msaliti wa Yesu, **Yn.** 13:21–26 (Mt. 26:20–25).

Katiba. *Ona pia* Sheria; Utawala

Katika kitabu cha Mafundisho na Maagano, "Katiba" inamaanisha Katiba ya Muungano wa Mataifa ya Marekani, ambayo iliandikwa kwa mwongozo wa kiungu ili kutengeneza njia kwa ajili ya urejesho wa injili.

Sheria ya kikatiba haina budi kuungwa mkono, **M&M** 98:5–6. Bwana ndiye aliyesababisha katiba hii iwekwe, **M&M** 101:77, 80.

Kayafa. *Ona pia* Anasi; Masadukayo

Katika Agano Jipya, ni kuhani mkuu na mkwewe Anasi. Kayafa alichukuwa nafasi muhimu katika kuwapinga Yesu Kristo na wanafunzi Wake (Mt. 26:3–4; Yn. 11:47–51; 18:13–14).

Kazi ya kimisionari. *Ona pia* Hubiri; Injili

Kuhubiri injili ya Yesu Kristo kwa neno na kwa mfano.

Jinsi gani ilivyo mizuri juu ya milima miguu yake yeye autangazaye, wokovu, **Isa.** 52:7. Nitawatafuta kondoo wangu na kuwaulizia, **Eze.** 34:11.

Mkaihubiri injili kwa kila kiumbe, **Mk.** 16:15 (Morm. 9:22). Mashamba ni meupe tayari kwa mavuno, **Yn.** 4:35. Na watahubirije pasipo kupelekwa, **Rum.** 10:15.

Wafundisheni neno la Mungu kwa bidii yote, **Yak. (KM)** 1:19. Bwana huwakubalia mataifa yote kufundisha neno lake, **Alma** 29:8.

Injili ipate kutangazwa na watu walio dhaifu na wa kawaida, **M&M** 1:23. Kazi ya ajabu i karibu kuanza, **M&M** 4:1. Kama utafanya kazi katika siku zako zote na kuileta, japo iwe nafsi moja kwangu, shangwe yako ni kuu namna gani!, **M&M** 18:15. Wateule wangu huisikia sauti yangu na hawaishupazi mioyo yao, **M&M** 29:7. Enendeni mkiihubiri injili yangu, wawili wawili, **M&M** 42:6. Sauti lazima iende kutoka mahali hapa, **M&M** 58:64. Mfungue vinywa vyenu katika kuitangaza injili yangu, **M&M** 71:1. Tangazeni ukweli kulingana na mafunuo na amri, **M&M** 75:4. Kila mtu aliyeonywa anapaswa amwonye jirani yake, **M&M** 88:81 (M&M 38:40–41). Bwana atazitunza familia za wale wanaohubiri injili, **M&M** 118:3. Watumishi wa Bwana watakwenda mbele, **M&M** 133:38. Wazee walio waaminifu, wanapoondoka kutoka maisha haya ya kufa, huendelea kufanya kazi zao, **M&M** 138:57.

Kesha, Walinzi. *Ona pia* Onya, Onyo

Kuwa macho, kujihadhari. Mtu anayekesha na kutii yu tayari na amejitayarisha. Walinzi ni viongozi walioitwa na ni wawakilishi wa Bwana na wanakuwa na wajibu maalumu kwa ustawi wa wengine. Wale walioitwa kama viongozi wana wajibu maalumu pia wa kuwa walinzi kwa ulimwengu uliobakia.

Nimekufanya wewe kuwa mlinzi, **Eze.** 3:17–21. Walinzi wapazao sauti za onyo huokoa roho zao wenyewe, **Eze.** 33:7–9.

Kwa hiyo kesheni; kwa maana hamjui saa Bwana atakapokuja, **Mt.** 24:42–43 (Mt. 25:13; Mk. 13:35–37; M&M 133:10–11). Kesheni na kusali msije mkaingia majaribuni, **Mt.** 26:41 (3 Ne. 18:15, 18).

Msipojichunga wenyewe, na mawazo yenu, maneno yenu, matendo yenu, lazima mtaangamia, **Mos.** 4:30. Alma aliwatawaza makuhani na wazee ili kulisimamia na kulichunga Kanisa, **Alma** 6:1.

Mtu asiyemtazamia Mwokozi atakatiliwa mbali, **M&M** 45:44. Askofu na wengine wameitwa na kutawazwa na Mungu ili kulichunga Kanisa, **M&M** 46:27. Bwana amewaweka walinzi juu ya shamba la mizabibu, **M&M** 101:44–58.

Kiapo. *Ona pia* Agano; Kiapo na Agano la Ukuhani

Kama linavyotumika katika maandiko, kwa kawaida hili ni agano takatifu au ahadi takatifu. Hata hivyo, watu waovu, pamoja na Shetani na malaika wake, pia hufanya viapo ili kutimiza nia zao ovu. Katika nyakati za Agano la Kale viapo vilikubalika; hata hivyo,

Yesu Kristo alifundisha kwamba watu wasiape katika jina la Mungu au viumbe Vyake (Mt. 5:33–37).

Nitafanya kiapo nilichomwapia Ibrahimu, **Mwa.** 26:3. Kama mtu atafanya kiapo ili kuifunga nafsi yake, asikivunje, **Hes.** 30:2. Wakaingia katika kiapo cha kutembea katika sheria ya Mungu, **Neh.** 10:29.

Mtimizie Bwana viapo vyako, **Mt.** 5:33 (Mh. 5:4–5; 3 Ne. 12:33). Mungu huapa kwa kiapo kwamba waaminifu wataokolewa, **Ebr.** 6:13–18.

Zoramu alipofanya kiapo, hofu yetu ilikoma, **1 Ne.** 4:37. Watu wa Amoni walichukua kiapo ya kuwa kamwe hawatamwaga damu, **Alma** 53:11. Wanefi waovu walifanya viapo na maagano ya siri pamoja na Shetani, **Hel.** 6:21–30.

Wanadamu hupata uzima wa milele kwa njia ya kiapo na agano la ukuhani, **M&M** 84:33–42. Maagano yote, mikataba, mapatano, ahadi, na viapo ambavyo havikutiwa muhuri na yule Roho Mtakatifu wa ahadi wakati wanadamu wanapokufa, **M&M** 132:7.

Kiapo na Agano la Ukuhani. *Ona pia* Agano; Kiapo; Ukuhani

Kiapo ni uthibitisho ulioapwa kuwa mtu atakuwa mkweli na mwaminifu katika ahadi zake. Agano ni ahadi ya dhati kati ya pande mbili. Ukuhani wa Haruni hupokelewa kwa agano peke yake. Wenye Ukuhani wa Melkizedeki hupokea ukuhani kwa kiapo na kwa agano lisilotamkwa. Kama wenye ukuhani watakuwa waaminifu na wenye kuikuza miito yao kama Mungu anavyoelekeza, Yeye huwabariki. Wale wanao kuwa waaminifu hadi mwisho na watendao yote Anayo waagiza kufanya watapata yale yote Baba aliyo nayo (M&M 84:33–39).

Bwana aliagana na Ibrahimu, na Ibrahimu alitii, **Mwa.** 15:18; 17:1; 22:16–18. Makuhani katika wakati wa Ezekieli hawakuwalisha kondoo, **Eze.** 34:2–3. Makuhani katika wakati wa Malaki walililiharibu agano, **Mal.** 1–2.

Kiburi. *Ona pia* Fedha; Majivuno, Siofaa; Malimwengu; Mnyenyekevu, Unyenyekevu; Ukwasi

Upungufu au ukosefu wa unyenyekevu au kutofundishika. Kiburi huwaweka watu katika upinzani wao kwa wao na kwa Mungu. Mtu mwenye majivuno hujiweka yeye mwenyewe juu ya wale wanaomzunguka na hufuata mapenzi yake zaidi kuliko mapenzi ya Mungu. Makuu, husuda, ugumu wa moyo, na maringo pia ni tabia za mtu mwenye majivuno.

Jihadhari kwamba usije ukamsahau Bwana na moyo wako ukainuka, **Kum.** 8:11–14. Kiburi na majivuno navichukia, **Mit.** 8:13 (Mit. 6:16–17). Kiburi hutangulia uangamivu, **Mit.** 16:18. Siku ya Bwana itakuwa juu ya wenye kiburi, **Isa.** 2:11–12 (2 Ne. 12:11–12). Kiburi cha moyo wako kimekudanganya, **Oba.** 1:3. Wote wenye kiburi watakuwa makapi, **Mal.** 4:1 (1 Ne. 22:15; 3 Ne. 25:1; M&M 29:9).

Yeyote atakayejikweza, atadhiliwa, **Mt.** 23:12 (M&M 101:42). Mungu huwapinga wenye kiburi, **1 Pet.** 5:5.

Lile jengo kuu na pana lilikuwa ni kiburi cha ulimwengu, **1 Ne.** 11:36 (1 Ne. 12:18). Wanapoelimika wanadhani kwamba wana hekima, **2 Ne.** 9:28–29. Mmejiinua katika kiburi cha mioyo yenu, **Yak. (KM)** 2:13, 16 (Alma 4:8–12). Mmevuliwa kiburi, **Alma** 5:28. Kiburi kikubwa kupita kiasi kimeingia katika mioyo ya watu, **Hel.** 3:33–36. Je, ni haraka ya jinsi gani watoto wa watu huinuliwa katika kiburi?, **Hel.** 12:4–5. Kiburi cha taifa hili kinathibitisha angamizo lao, **Moro.** 8:27.

Jihadharini na kiburi, msije mkawa kama Wanefi, **M&M** 38:39. Acheni kiburi na upuuzi wenu wote, **M&M** 88:121.

Kiebrania. *Ona pia* Israeli

Lugha ya Kisemiti iliyozungumzwa na wana wa Israeli.

Kiebrania kilikuwa kikizungumzwa

na Waisraeli hadi kurudi kwao kutoka utumwa wa Babilonia, wakati ambapo Kiaramai kilikuja kuwa lugha ya mazungumzo ya kila siku. Wakati wa Yesu, Kiebrania kilikuwa ni lugha ya wasomi, ya sheria, na ya maandiko ya kidini.

Kifo cha Kiroho. *Ona* Mauti ya Kiroho

Kifo cha kishahidi, Mfiadini

Mtu aliye tayari kufa kuliko kumtupa Kristo, injili, au imani yake ya uadilifu au kanuni.

Damu zote za haki tangu Abeli hadi Zakaria zitashuhudia dhidi ya uovu, **Mt.** 23:35 (Lk. 11:50). Mtu yeyote atakayeupoteza uhai wake kwa ajili ya Kristo na injili ataokolewa, **Mk.** 8:35 (M&M 98:13). Nao walimtupia mawe Stefano, **Mdo.** 7:59 (Mdo. 22:20). Maana agano la urithi lilipo, lazima iwepo na mauti yake aliyelifanya, **Ebr.** 9:16–17.

Abinadi alianguka, akiwa amekufa kwa moto, **Mos.** 17:20. Waamoniha walioongoka walitupwa katika moto, **Alma** 14:8–11. Wengi waliuawa kwa sababu walishuhudia juu ya mambo haya, **3 Ne.** 10:15.

Mtu yeyote autoaye uhai wake katika kazi yangu atapata uzima wa milele, **M&M** 98:13–14. Joseph Smith na Hyrum Smith walikufa kifo cha kishahidi kwa urejesho wa injili, **M&M** 135. Joseph Smith alitia muhuri ushuhuda wake kwa damu yake, **M&M** 136:39.

Kigingi

Kitengo kimojawapo cha utaratibu na utawala wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Kigingi kinaundwa na idadi kadhaa ya wadi au matawi. Kwa ujumla kina mipaka ya kijiografia iliyowekwa na inafanana na taswira ya hema inayoelezewa katika Isaya 54:2: "Refusha kamba zako na kuimarisha vigingi vyako." Kila kigingi cha Sayuni kinahimili na kusaidia kushikia Kanisa kwa namna ambayo hema au maskani linavyoshikiliwa na vigingi. Kigingi ni mahali pa kukusanyikia kwa ajili ya mabaki ya Israeli waliotawanywa (M&M 82:13–14; 101:17–21).

Imarisha vigingi vyako na upanue mipaka yako, **Moro.** 10:31 (M&M 82:14).

Ichagulie Sayuni vigingi vingine licha ya hiki, **M&M** 109:59. Kukusanyika pamoja juu ya Sayuni, na juu ya vigingi vyake, kupate kuwa kwa ajili ya kujilinda, **M&M** 115:6 (M&M 101:21). Mahali pengine pateuliwe kwa ajili ya vigingi, **M&M** 115:18. Rais wa akidi ya makuhani wakuu aliteuliwa ili kuwatayarisha wale watakaoteuliwa kuwa marais wa vigingi, **M&M** 124:133–134. Enendeni nchi ya Sayuni, ili vigingi vyake vipate kuimarika, **M&M** 133:9.

Kijisitu Kitakatifu. *Ona* Ono la Kwanza

Kijiti cha Efraimu. *Ona* Efraimu—Kijiti cha Efraimu au Yusufu

Kijiti cha Yuda. *Ona* Yuda—Kijiti cha Yuda

Kijiti cha Yusufu. *Ona* Efraimu—Kijiti cha Efraimu au Yusufu

Kikwazo. *Ona* Himiza, Kikwazo

Kileo. *Ona* Neno la Hekima

Kimball, Spencer W. *Ona pia* Tamko Rasmi 2

Rais wa kumi na mbili wa Kanisa tangu lilipoanzishwa katika mwaka 1830. Spencer W. Kimball alitumikia kama Rais kutoka Desemba 1973 hadi Novemba 1985. Alizaliwa katika mwaka 1895 na alifariki katika mwaka 1985 akiwa na umri wa miaka tisini.

Juni 1978, Urais wa Kwanza ulitangaza kwamba ufunuo umepokolewa na Rais Kimball unaotoa ukuhani na baraka za hekaluni kwa wanaume wote walio wanachama wenye kustahili, **TR** 2.

Kinywaji, Lewa. *Ona* Neno la Hekima

Kipatriaki, Patriaki. *Ona pia* Baba, Mwili wenye kufa; Baraka za Kipatriaki; Mwinjilisti; Ukuhani wa Melkizedeki

Maandiko huzungumzia juu ya aina mbili za mapatriaki: (1) ofisi iliyo katika Ukuhani wa Melkizedeki, wakati mwingine huitwa mwinjilisti; (2) baba za familia. Mapatriaki waliotawazwa hutoa baraka maalumu kwa waumini wa Kanisa wanaostahili.

Mapatriaki wa kutawazwa: Alitoa wengine kuwa mitume na wengine kuwa wainjilisti, **Efe.** 4:11 (M ya I 1:6).

Ni wajibu wa wale Kumi na Wawili kuwatawaza wahudumu wainjilisti, **M&M** 107:39. Hyrum anaweza kuchukua ofisi ya ukuhani na patriaki, **M&M** 124:91–92, 124; 135:1.

Baba: Yakobo aliwabariki watoto wake na uzao wao, **Mwa.** 49:1–28.

Acha niseme kwa uhuru kwenu juu ya patriaki wenu Daudi, **Mdo.** 2:29.

Lehi alishauri na kuwabariki uzao wake, **2 Ne.** 4:3–11.

Nikawa mrithi sahihi nikishikilia haki zilizokuwa mali za mababu, **Ibr.** 1:2–4.

Kipawa. *Ona* Karama

Kipawa cha Roho Mtakatifu. *Ona pia* Karama; Mungu, Uungu; Roho Mtakatifu; Vipawa vya Roho

Haki ya kila muumini wa Kanisa aliyebatizwa na aliye mstahilivu kuwa na ushawishi wa daima wa Roho Mtakatifu. Kufuatia ubatizo wa mtu katika Kanisa la kweli la Yesu Kristo, mtu huyo hupokea kipawa cha Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono kutoka kwa mtu aliye na mamlaka sahihi (Mdo. 8:12–25; Moro. 2; M&M 39:23). Kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu mara nyingi hunenwa kama ubatizo kwa moto (Mt. 3:11; M&M 19:31).

Wanadamu wanaamriwa kutubu, kubatizwa, na kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu, **Mdo.** 2:38. Petro na Yohana walitoa kipawa cha Roho Mtakatifu kwa kuwekea mikono, **Mdo.** 8:14–22. Roho Mtakatifu hutolewa kwa kuwekea mikono, **Mdo.** 19:2–6.

Ondoleo la dhambi huja kwa moto na kwa Roho Mtakatifu, **2 Ne.** 31:17.

Tunaamini katika kuwekea mikono kwa ajili ya kupewa kipawa cha Roho Mtakatifu, **M ya I** 1:4.

Kipindi. *Ona pia* Funguo za Ukuhani; Injili; Ukuhani; Urejesho wa Injili

Kipindi cha injili ni wakati ambamo ndani yake Bwana anakuwa na angalao mtumishi mmoja mwenye mamlaka hapa duniani mwenye kushikilia funguo za ukuhani mtakatifu.

Adamu, Henoko, Nuhu, Ibrahimu, Musa, Yesu Kristo, Joseph Smith, na wengineo kila mmoja wao alianzisha kipindi kipya cha injili. Wakati Bwana aanzishapo kipindi, injili hufunuliwa upya ili watu wa kipindi hicho cha maongozi hawahitaji kutegemea vipindi vilivyopita kwa elimu ya mpango wa wokovu. Kipindi kilichoanzishwa na Joseph Smith kinajulikana kama "kipindi cha utimilifu wa nyakati."

Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme, **Dan.** 2:44 (M&M 65).

Katika siku za mwisho nitawamwagia wote wenye mwili Roho yangu, **Mdo.** 2:17 (Yoe. 2:28). Mbingu lazima impokee Kristo hadi nyakati za kufanywa upya mambo yote, **Mdo.** 3:21. Katika kipindi cha utimilifu wa nyakati, Mungu atavikusanya pamoja vitu vyote katika Kristo, **Efe.** 1:10.

Nitalianzisha kanisa langu miongoni mwao, **3 Ne.** 21:22.

Bwana alikabidhi funguo za ufalme wake na za kipindi cha injili kwa nyakati za mwisho, **M&M** 27:13. Funguo za kipindi hiki zimekabidhiwa mikononi mwenu, **M&M** 110:12–16. Funguo zote za vipindi vilivyopita zimerejeshwa katika kipindi hiki cha utimilifu wa nyakati, **M&M** 128:18–21.

Kiri, Kukiri. *Ona pia* Samehe; Toba, Tubu

Maandiko hutumia neno kukiri katika njia zipatazo mbili. Katika maana moja,

kukiri ni mtu kueleza imani yake katika kitu fulani, kama vile kukiri kwamba Yesu ndiye Kristo (Mt. 10:32; Rum. 10:9; 1 Yoh. 4:1–3; M&M 88:104).

Katika maana nyingine, kukiri ni mtu kukubali hatia, kama vile katika maungamo ya dhambi. Ni wajibu wa watu wote kuungama dhambi zao kwa Bwana na kupata msamaha Wake (M&M 58:42–43). Inapokuwa muhimu, dhambi yapaswa zikiriwa kwa mtu au watu uliowakosea. Dhambi kubwa yapaswa zikiriwe kwa viongozi wa Kanisa (hasa askofu).

Ataikiri dhambi hiyo aliyotenda, **Law.** 5:5. Wataukiri uovu wao, **Law.** 26:40–42. Umtukuze Bwana Mungu wa Israeli, na ukaungame kwake, **Yos.** 7:19.

Watu walibatizwa naye katika mto wa Jordani, wakiziungama dhambi zao, **Mt.** 3:5–6.

Na mvunja sheria atakayeungama dhambi zake atasamehewa, **Mos.** 26:29.

Ungama dhambi zako, usije ukateseka kwa adhabu, **M&M** 19:20. Mwenye toba atakiri na kuziacha dhambi zake, **M&M** 58:43. Bwana ni mwenye huruma kwa wale wanaoungama dhambi zao kwa moyo mnyenyekevu, **M&M** 61:2. Bwana husamehe dhambi za wale wenye kukiri na kuomba msamaha, **M&M** 64:7.

Kisasi. *Ona pia* Uadui

Lipiza kisasi au rudishia mabaya kwa majeraha au mabaya yaliyofanywa.

Mungu wenu atakuja na kisasi, **Isa.** 35:4.

Kisasi ni juu yangu mimi, mimi nitalipa, **Rum.** 12:19 (Morm. 3:15; 8:20).

Upanga wa kisasi unaning'inia juu yenu, **Morm.** 8:40–41.

Nitalipiza kisasi juu ya waovu, kwa kuwa hawatatubu, **M&M** 29:17.

Bwana alikuja katika siku za uovu na kisasi, **Musa** 7:45–46.

Kishkumeni. *Ona pia* Wanyang'anyi wa Gadiantoni

Katika Kitabu cha Mormoni, ni kiongozi wa kikundi cha watu waovu ambao baadaye walijulikana kama wanyang'anyi wa Gadiantoni (Hel. 1:9–12; 2).

Kitabu cha Amri. *Ona pia* Mafundisho na Maagano; Ufunuo

Mnamo mwaka 1833, idadi ya ufunuo ulizopokea Joseph Smith Nabii zilitayarishwa kwa kuchapishwa chini ya jina A Book of Commandments for the Government of the Church of Christ. Bwana aliendelea kuwasiliana na Watumishi Wake, na mkusanyiko uliokuzwa wa ufunuo ulichapishwa miaka miwili baadaye kama Mafundisho na Maagano.

M&M 1 ni utangulizi wa Bwana kwa Kitabu chake cha amri, **M&M** 1:6. Bwana alitoa changamoto kwa watu wenye hekima kuiga japo moja ya mafunuo yake madogo katika Kitabu cha Amri, **M&M** 67:4–9. Wasimamizi waliteuliwa ili kuchapisha mafunuo hayo, **M&M** 70:1–5.

Kitabu cha Mormoni. *Ona pia* Efraimu—Kijiti cha Efraimu au Yusufu; Kanoni; Maandiko; Mabamba; Mabamba ya Dhahabu; Mashahidi wa Kitabu cha Mormoni; Mormoni, Nabii Mnefi; Smith, Joseph, Mdogo

Moja ya vitabu vinne vya maandiko yanayokubalika na Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Ni ufupisho uliofanywa na nabii wa kale aliyeitwa Mormoni juu ya kumbukumbu ya wakazi wa kale wa bara la Marekani. Kiliandikwa ili kushuhudia ya kuwa Yesu ndiye Kristo. Kuhusu kitabu hiki, Joseph Smith Nabii, ambaye alikitafsiri kwa kipawa na uwezo wa Mungu, alisema: "Niliwaambia ndugu zangu kwamba Kitabu cha Mormoni kilikuwa kitabu kilicho sahihi kuliko kingine chochote duniani, na ni jiwe la tao la dini yetu, na mtu angelikuwa karibu zaidi na Mungu kwa kuishi kulingana na maagizo yake, kuliko kitabu kingine chochote" (ona dibaji mwanzoni mwa Kitabu cha Mormoni).

Kitabu cha Mormoni ni kumbukumbu

ya kidini ya makundi matatu ya watu ambao walihamia kutoka Ulimwengu wa Zamani kwenda mabara ya Marekani. Makundi haya yaliongozwa na manabii ambao waliandika historia zao za kidini na kijamii kwenye mabamba ya chuma. Kitabu cha Mormoni kinaelezea juu ya Yesu Kristo kuwatembelea watu katika Marekani baada ya Ufufuko Wake. Kipindi cha miaka mia mbili ya amani kilifuatia matembezi haya ya Kristo.

Moroni, nabii Mnefi na mwanahistoria wa mwisho, alizifunga kumbukumbu hizi zilizofanyiwa ufupisho za watu hawa na kuzificha karibu mwaka 421 B.K. Katika mwaka 1823, Moroni mfufuka alimtokea Joseph Smith na baadaye akampatia kumbukumbu hizi zilizo takatifu na za kale ili azitafsiri na kuzitoa ulimwenguni kama ushuhuda mwingine wa Yesu Kristo.

Yusufu ni mti mchanga wenye kuzaa ambao matawi yake yametanda ukutani, **Mwa.** 49:22–26. Kweli itachipuka duniani, **Zab.** 85:11 (Morm. 8:16; Musa 7:62). Bwana atawainulia bendera mataifa naye atawapigia mluzi, **Isa.** 5:26. Sauti itanena kutoka ardhini, **Isa.** 29:4 (2 Ne. 26:14–17). Maono ya wote yamekuwa kama maneno ya kitabu kilichotiwa muhuri, **Isa.** 29:11 (Isa. 29:9–18; 2 Ne. 27:6–26). Vijiti vya Yusufu na Yuda vitakuwa kimoja mkononi mwa Bwana, **Eze.** 37:15–20.

Kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili, **Yn.** 10:16 (3 Ne. 15:16–24).

Kitabu cha Mormoni na Biblia vitakuwa kwa pamoja, **2 Ne.** 3:12–21. Maneno ya Bwana yatapigwa mluzi hata miisho ya dunia, **2 Ne.** 29:2. Bwana alifanya agano na Enoshi ili kukileta Kitabu cha Mormoni kwa Walamani, **Eno.** 1:15–16. Kitabu cha Mormoni kiliandikwa kwa madhumuni ya kuwa tupate kuiamini Biblia, **Morm.** 7:9. Kitabu cha Mormoni kitasimama kama ushuhuda dhidi ya ulimwengu, **Eth.** 5:4. Mwulizeni Mungu kama mambo haya si ya kweli, **Moro.** 10:4.

Kristo alitoa ushuhuda ya kwamba Kitabu cha Mormoni ni cha kweli, **M&M** 17:6. Kitabu cha Mormoni kina utimilifu wa injili ya Yesu Kristo, **M&M** 20:9 (M&M 20:8–12; 42:12).

Tunaamini ya kuwa Kitabu cha Mormoni ni neno la Mungu, **M ya I** 1:8.

Kitabu cha Ukumbusho. *Ona pia* Kitabu cha Uzima; Nasaba

Kitabu kilichoanzishwa na Adamu ambamo ndani yake mliandikwa kumbukumbu za kazi za wazao wake; pia kumbukumbu ya aina hiyo hiyo ilitunzwa na manabii na waumini walio waaminifu kutoka wakati huo. Adamu na watoto wake walitunza kitabu cha ukumbusho, ambamo ndani yake waliandika kwa kuongozwa na roho, na kitabu cha vizazi, ambacho kilikuwa na nasaba (Musa 6:5, 8). Kumbukumbu ya namna hiyo yaweza kuwa na sehemu katika kuamua hukumu yetu ya mwisho.

Na kitabu cha ukumbusho kikaandikwa, **Mal.** 3:16–18 (3 Ne. 24:16–18).

Wale wote wasioandikwa katika kitabu cha ukumbusho hawatapata urithi katika siku hiyo, **M&M** 85:9. Wafu walihukumiwa kwa vitabu vilivyo kuwa na kumbukumbu za matendo yao, **M&M** 128:7. Acha tulete kitabu chenye kumbukumbu ya wafu wetu, **M&M** 128:24.

Na kitabu cha ukumbusho kiliandikwa, **Musa** 6:5–8. Tunacho kitabu cha ukumbusho, **Musa** 6:46. Ibrahimu alijitahidi sana kuandika kumbukumbu kwa ajili ya wazao wake, **Ibr.** 1:31.

Kitabu cha Uzima. *Ona pia* Kitabu cha Ukumbusho

Kwa maana moja Kitabu cha Uzima ni jumla ya mawazo na matendo ya mtu—kumbukumbu ya maisha yake. Hata hivyo, maandiko pia yanaonyesha kwamba kumbukumbu imewekwa mbinguni ya waaminifu, ikijumuisha majina yao na hesabu ya matendo yao ya haki.

Bwana atawafuta watenda dhambi kutoka katika kitabu chake, **Ku.** 32:33.

Yeye ashindaye hatafutwa katika kitabu cha uzima, **Ufu.** 3:5. Kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima, **Ufu.** 20:12 (M&M 128:6–7).

Majina ya wenye haki yataandikwa katika kitabu cha uzima, **Alma** 5:58.

Sala zenu zimeandikwa katika kitabu cha majina ya wale waliotakaswa, **M&M** 88:2.

Kolobu

Nyota iliyo karibu zaidi na kiti cha enzi cha Mungu (Ibr. 3:2–3, 9).

Ibrahimu aliona Kolobu na nyota, **Ibr.** 3:2–18. Wakati wa Bwana unahesabiwa kulingana na wakati wa Kolobu, **Ibr.** 3:4, 9 (Ibr. 5:13).

Komboa, Kombolewa, Ukombozi. *Ona pia* Anguko la Adamu na Hawa; Lipia dhambi, Upatanisho; Mauti ya Kimwili; Mauti ya Kiroho; Wokovu; Yesu Kristo

Kuokoa, kununua, au kufidia, kama vile kumweka mtu huru kutokana na utumwa kwa kufanya malipo. Ukombozi unahusu Upatanisho wa Yesu Kristo na kuokolewa kutoka katika dhambi. Upatanisho wa Yesu huwakomboa wanadamu wote kutoka katika mauti ya kimwili. Kupitia Upatanisho Wake, watu walio na imani katika Yeye na wenye kutubu pia hukombolewa kutoka katika mauti ya kiroho.

Nimekukomboa, **Isa.** 44:22. Nitawaokoa na mauti, **Hos.** 13:14 (Zab. 49:15).

Tunao ukombozi kwa njia ya damu yake, **Efe.** 1:7, 14 (Ebr. 9:11–15; 1 Pet. 1:18–19; Alma 5:21; Hel. 5:9–12).

Bwana ameikomboa nafsi yangu kutoka jehanamu, **2 Ne.** 1:15. Ukombozi huja katika na kupitia Masiya Mtakatifu, **2 Ne.** 2:6–7, 26 (Mos. 15:26–27; 26:26). Waliimba upendo wa ukombozi, **Alma** 5:9 (Alma 5:26; 26:13). Waovu watabaki kama kana kwamba hakuna ukombozi uliofanyika, **Alma** 11:40–41 (Alma 34:16; 42:13; Hel. 14:16–18). Yesu Kristo amefanikisha ukombozi wa ulimwengu, **Morm.** 7:5–7. Uwezo wa ukombozi huja kwa wale wote wasio na sheria, **Moro.** 8:22 (M&M 45:54).

Wasioamini hawawezi kukombolewa kutokana na anguko lao la kiroho, **M&M** 29:44. Watoto wadogo wamekombolewa tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, **M&M** 29:46. Bwana amewakomboa watu wake, **M&M** 84:99. Joseph F. Smith aliona katika ono ukombozi wa wafu, **M&M** 138.

Adamu na Hawa walifurahia ukombozi wao, **Musa** 5:9–11.

Komunyo. *Ona* Sakramenti

Koreshi

Katika Agano la Kale, ni mfalme wa Uajemi ambaye aliutimiza unabii wa Isaya (2 Nya. 36:22–23; Isa. 44:28; 45:1) kwa kuwaruhusu Wayahudi kurudi Yerusalemu ili kulijenga tena hekalu, na hivyo alipendelea kumalizika kwa utumwa wa Babilonia. Unabii wa Isaya ulifanyika kiasi cha miaka 180 kabla ya tendo hili la mfalme.

Koriantoni. *Ona pia* Alma, Mwana wa Alma

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana wa Alma, aliyekuwa mwana wa Alma.

Alikwenda kwa Wazorami, **Alma** 31:7. Aliitekeleza huduma kwa kumfuata kahaba, **Alma** 39:3. Alma alimfundisha hali ya maisha baada ya kifo, ufufuko, na upatanisho, **Alma** 39–42. Aliitwa tena kuhubiri, **Alma** 42:31. Alikwenda nchi ya upande wa kaskazini kwa merikebu, **Alma** 63:10.

Koriantumuri. *Ona pia* Wayaredi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mfalme wa Wayeredi na ni mtu wa mwisho kuwa hai katika taifa la Wayeredi.

Aligunduliwa na watu wa Zarahemla, **Omni** 1:21. Alikuwa mfalme juu ya nchi yote, **Eth.** 12:1–2. Alikamatwa na Sharedi na kuachiwa huru na wanawe, **Eth.** 13:23–24. Alipigana vita na maadui mbali mbali, **Eth.** 13:28–14:31. Alitubu,

Eth. 15:3. Alipigana vita vyake vya mwisho na Shizi, **Eth.** 15:15–32.

Korihori. *Ona pia* Mpinga Kristo

Mpinga Kristo katika Kitabu cha Mormoni aliyedai ishara kama uthibitisho wa uwezo wa Mungu; Bwana akamfanya Korihori kuwa bubu (Alma 30:6–60).

Kornelio. *Ona pia* Akida; Petro; Wayunani

Akida katika Kaisaria, aliyebatizwa na Petro (Mdo. 10). Yawezekana kuwa yeye alikuwa Myunani wa kwanza kujiunga na Kanisa pasipo kwanza kuongelewa katika dini ya Kiyahudi. Ubatizo wa Kornelio na familia yake uliashiria kufunguka kwa njia kwa injili kuhubiriwa kwa Wayunani. Petro, Mtume kiongozi, aliyeshikilia funguo za ufalme wa Mungu duniani kwa wakati huo, alielekeza mahubiri haya.

Kosea

Kuvunja sheria takatifu, kutenda dhambi, au kusababisha kukosekana kwa faraja, au kujeruhi, pia kuchukiza au kuudhi.

Ndugu aliyekosewa ni mgumu zaidi kumpata kuliko mji wenye nguvu, **Mit.** 18:19.

Kama jicho lako la kuume likikukosesha, ling'oe ulitupe, **Mt.** 5:29. Yoyote atakayewakosea mmoja wapo wa wadogo hawa waniaminio, ingekuwa heri kuzama baharini, **Mt.** 18:6 (M&M 121:19–22).

Kama kaka au dada yako amekukosea na akakiri, patana naye, **M&M** 42:88. Katika lolote mwanadamu hamkosei Mungu, isipokuwa wale wasiokiri mkono wake na wasiotii amri zake, **M&M** 59:21.

Kristo. *Ona* Yesu Kristo

Kuabudu. *Ona pia* Mungu, Uungu

Kumpenda, kumnyenyekea, kumtumikia, na kujitoa kwa Mungu (M&M 20:19). Kuabudu kunajumuisha sala, kufunga, ibada ya kanisani, kushiriki katika ibada za injili, na matendo mengine yanayoonyesha kuabudu na upendo kwa Mungu.

Usiwe na miungu wengine mbele yangu, **Ku.** 20:3 (Ku. 32:1–8, 19–35; Zab. 81:9).

Watamwabudu Baba katika roho na katika kweli, **Yn.** 4:23. Mwabuduni yeye aliyezifanya mbingu na dunia, **Ufu.** 14:7 (M&M 133:38–39).

Mwabuduni yeye kwa uwezo, akili, na nguvu zenu zote, **2 Ne.** 25:29. Waliamini katika Kristo na walimwabudu Baba katika jina lake, **Yak. (KM)** 4:5. Zeno alifundisha kwamba watu wanapaswa kusali na kuabudu katika mahali pote, **Alma** 33:3–11. Mwabudu Bwana, katika mahali popote utakapokuwa, katika roho na katika kweli, **Alma** 34:38. Watu walianguka miguuni pa Yesu na wakamwabudu, **3 Ne.** 11:17.

Watu wote lazima watubu, wamwamini Yesu Kristo, na kumuabudu Baba katika jina lake, **M&M** 20:29. Ninawapa maneno haya ili mpate kufahamu na kujua namna ya kuabudu, na kujua nini mnachokiabudu, **M&M** 93:19.

Ni Mungu huyu mmoja tu ndiye nitakayemwabudu, **Musa** 1:12–20. Tunadai haki ya kumwabudu Mwenyezi Mungu, **M ya I** 1:11.

Kuabudu sanamu

Ibada ya masanamu au upenzi uliopita kiasi au upendo kwa kitu chochote.

Usiwe na miungu mingine ila mimi, **Ku.** 20:3 (Mos. 12:35; 13:12–13). Ikiwa mtaandama na miungu mingine, hakika mtaangamia, **Kum.** 8:19. Ukaidi ni kama dhambi na kuabudu masanamu, **1 Sam.** 15:23. Umejifunua nafsi yako kwa mwingine kuliko Mimi, **Isa.** 57:8. Umeisifu miungu ya fedha na ya dhahabu, **Dan.** 5:23.

Hamwezi kumtumikia Mungu na mali, **Mt.** 6:24. Tamaa mbaya ndiyo ibada ya sanamu, **Kol.** 3:5. Watoto, jilindeni nafsi zenu na sanamu, **1 Yoh.** 5:21.

Ole wao wale waabuduo masanamu,

2 Ne. 9:37. Kuabudu sanamu kwa watu wa Nefi kuliwaletea juu yao vita na maangamizo yao, **Alma** 50:21.

Kila mtu anaenenda akifuata sura ya Mungu wake mwenyewe, **M&M** 1:16. Acha wafanye kazi kwa mikono yao wenyewe ili pasiwepo na kuabudu sanamu, **M&M** 52:39.

Baba yake Ibrahimu alitekwa na ibada ya sanamu, **Ibr.** 1:27.

Kudanganya. *Ona* Danganya, Kudanganya, Udanganyifu

Kufa. *Ona* Hali ya Kufa, enye Kufa

Kufunga. *Ona* Funga, Kufunga

Kufunga, Muhuri, Tia. *Ona pia* Eliya; Ibada; Ukuhani

Kufanya ibada zilizofanyika kwa mamlaka ya ukuhani duniani ziwe na nguvu mbinguni. Ibada zinatiwa mahuri zinapokuwa zimepokea idhini ya Roho Mtakatifu wa Ahadi, ambaye ni Roho Mtakatifu.

Lolote utakalolifunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni, **Mt.** 16:19 (Mt. 18:18; M&M 124:93; 132:46). Mmekwishatiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa Ahadi, **Efe.** 1:13.

Ninakupa wewe uwezo, kwamba lolote utakalolifunga duniani litakuwa limefungwa mbinguni, **Hel.** 10:7.

Kwao umetolewa uwezo wa kuwafunga kote mbinguni na duniani, **M&M** 1:8. Wale walio katika utukufu wa selestia wametiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa Ahadi, **M&M** 76:50–70. Eliya anakabidhi funguo za uwezo wa kufunga katika mikono ya Joseph Smith, **M&M** 110:13–16. Huu ni uwezo wa kufunga na kuunganisha, **M&M** 128:14. Neno la unabii lililo imara zaidi linamaanisha kujua kwamba mtu ametiwa muhuri kwa uzima wa milele, **M&M** 131:5. Maagano yote yasiyotiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa Ahadi yanakoma wakati wanadamu wanapokufa, **M&M** 132:7. Kazi kuu itakayofanyika katika mahekalu ni pamoja na kuunganishwa kwa watoto kwa wazazi wao, **M&M** 138:47–48.

Kugeuka sura. *Ona pia* Funguo za Ukuhani; Yesu Kristo

Hali ya watu ambao kwa muda wanageuka katika sura na hali ya asili—ambako ni, kuinuliwa kwa kiwango cha juu zaidi kiroho—ili kwamba waweze kustahmili uwepo na utukufu wa viumbe wa mbinguni.

Kugeuka sura kwa Kristo: Petro, Yakobo, na Yohana walimwona Bwana akitukuzwa na kugeuka sura mbele yao. Kabla yake Mwokozi alikuwa amemwahidi Petro kwamba angepokea funguo za ufalme wa mbinguni (Mt. 16:13–19; 17:1–9; Mk. 9:2–10; Lk. 9:28–36; 2 Pet. 1:16–18). Katika tukio hili muhimu, Mwokozi, Musa, na Elia (Eliya) walitoa funguo za ukuhani ambazo ziliahidiwa kwa Petro, Yakobo, na Yohana. Kwa funguo hizi za ukuhani, Mitume walikuwa na uwezo wa kuendeleza kazi ya ufalme baada ya Kupaa kwa Yesu.

Joseph Smith alifundisha kwamba juu ya ule Mlima wa Kugeuka sura, Petro, Yakobo, na Yohana pia waligeuka sura. Waliona ono la dunia kama itakavyoonekana katika hali yake ya baadaye ya kutukuzwa (M&M 63:20–21). Waliwaona Musa na Eliya, viumbe wawili waliobadilishwa, na walisikia sauti ya Baba. Baba alisema, "Huyu ndiye Mwanangu Mpendwa wangu ninayependezwa sana naye; msikilizeni yeye" (Mt. 17:5).

Viumbe Waliogeuka Sura: Walimwona Mungu wa Israeli, **Ku.** 24:9–11. Ngozi ya uso wake iling'ara wakati alipokuwa akizungumza na Mungu, **Ku.** 34:29 (Mk. 9:2–3).

Uso wake uling'aa, **Mt.** 17:2 (Mk. 9:2–3). Israeli hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa kwa sababu ya utukufu wake, **2 Kor.** 3:7.

Uso wa Abinadi ulimetameta kwa mng'aro uliopita kiasi, **Mos.** 13:5–9. Walikuwa wamezingirwa kama vile kwa

moto, **Hel.** 5:23, 36, 43–45 (3 Ne. 17:24; 19:14). Walikuwa weupe kama ule uso wa Yesu, **3 Ne.** 19:25. Kwao ilionekana kama kugeuka sura, **3 Ne.** 28:15.

Hakuna mtu aliyemwona Mungu katika mwili, isipokuwa amehuishwa na Roho, **M&M** 67:10–12. Kwa uwezo wa Roho macho yetu yalifunguka, **M&M** 76:12.

Utukufu wa Mungu ulikuwa juu ya Musa, **Musa** 1:2. Utukufu wake ulikuwa juu yangu; nami nikauona uso wake, kwa maana nilikuwa nimegeuka sura, **Musa** 1:11. Niliona mbingu zikifunguka nami nilivikwa utukufu, **Musa** 7:3–4.

Kuhani, Ukuhani wa Haruni. *Ona pia* Haruni, Kaka wa Musa; Kuhani Mkuu; Ukuhani wa Haruni

Ofisi ya Ukuhani wa Haruni. Hapo zamani, ofisi ya juu kabisa katika Ukuhani wa Walawi ilishikiliwa na Haruni na wazao wake tu. Kristo alipotimiza torati ya Musa, kizuizi hiki kiliondolewa.

Kazi za Kuhani katika Kanisa la urejesho zinaelezwa, **M&M** 20:46–52.

Kuhani, Ukuhani wa Melkizedeki. *Ona pia* Kuhani Mkuu; Ukuhani wa Melkizedeki

Mtu anayefanya ibada za kidini kwa ajili ya wengine na huzielekeza kwa Mungu. Mara kwa mara katika maandiko, makuhani kwa kweli ni makuhani wakuu kwa mfano wa Melkizedeki (Alma 13:2). Wale wapokeao utimilifu wa utukufu wa Mungu baada ya Ufufuko huwa makuhani na wafalme katika ulimwengu wa selestia.

Melkizedeki alikuwa kuhani wa Mungu Aliye Juu Sana, **Mwa.** 14:18. Wewe ni kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki, **Zab.**110:4 (Ebr. 5:6; 7:17, 21).

Kristo ametufanya sisi kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu na Baba yake, **Ufu.** 1:6 (Ufu. 5:10; 20:6).

Kumbuka kwamba Bwana Mungu aliwatawaza makuhani kwa mfano wake mtakatifu, **Alma** 13:1–20.

Wale watakaofufuka katika ufufuko wa wenye haki ni makuhani na wafalme, **M&M** 76:50, 55–60.

Kuhani Mkuu. *Ona pia* Ukuhani wa Haruni; Ukuhani wa Melkizedeki

Ofisi katika ukuhani. Maandiko huzungumza juu ya "kuhani mkuu" katika maana mbili: (1) ofisi katika Ukuhani wa Melkizedeki; na (2) chini ya sheria ya Musa, ni ofisa msimamizi wa Ukuhani wa Haruni.

Maana ya kwanza hutumika kwa Yesu Kristo kama Kuhani Mkuu maarufu. Adamu na mapatriaki wote pia walikuwa makuhani wakuu. Siku hizi, makuhani wakuu watatu wasimamizi huunda Urais wa Kanisa na huwasimamia makuhani wengine wote na waumini wa Kanisa. Nyongeza ya wanaume wengine wenye kustahili hutawazwa kuwa makuhani wakuu kulingana na utaratibu kote katika Kanisa leo. Makuhani wakuu waweza kuitwa, kusimikwa, na kutawazwa kuwa maaskofu (M&M 68:19; 107:69–71).

Katika maana ya pili, chini ya torati ya Musa, ofisa msimamizi wa Ukuhani wa Haruni aliitwa kuhani mkuu. Ofisi hii ilirithiwa na ilikuja kupitia kwa mzaliwa wa kwanza miongoni mwa familia ya Haruni, Haruni mwenyewe akiwa kuhani mkuu wa kwanza wa ukuhani wa Haruni (Ku. 28–29; Law. 8; M&M 84:18).

Melkizedeki alikuwa kuhani wa Mungu Aliye Juu Sana, **Mwa.** 14:18 (Alma 13:14).

Makuhani wakuu waliitwa na kuandaliwa tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, **Alma** 13:1–10.

Makuhani wakuu huhudumu katika mambo ya kiroho, **M&M** 107:10, 12, 17.

Kuhesabiwa Haki. *Ona* Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki

Kuhudumu. *Ona pia* Ukuhani; Utumishi

Kufanya kazi ya Bwana duniani. Watumishi wateule wa Bwana ni lazima

waitwe na Mungu ili kuhudumu katika kazi Yake. Wahudumu wa kweli wafanyapo mapenzi ya Bwana, humwakilisha Bwana katika kazi zao rasmi na humwakilisha kama mawakala Wake (M&M 64:29), hivyo basi huendesha kazi muhimu kwa wokovu wa wanadamu. Bwana ametoa mitume, manabii, wainjilisti, makuhani wakuu, sabini, wazee, maaskofu, makuhani, walimu, mashemasi, wasaidizi na utawala kwa ajili ya kuwakamilisha Watakatifu, kwa ajili ya kazi ya huduma (1 Kor. 12:12–28; Efe. 4:11–16; M&M 20; 107).

Bwana amemchagua yeye atumike katika jina la Bwana, **Kum.** 18:5. Watu watakuiteni Wahudumu wa Mungu wetu, **Isa.** 61:6.

Mwana wa Mtu hakuja kuhudumiwa, bali kuhudumu, **Mt.** 20:26–28. Nimekutokea ili kukuweka wewe uwe mtumishi na shahidi, **Mdo.** 26:16–18. Mungu si dhalimu hata asahau kazi yenu ya upendo mliyowahudumia Watakatifu, **Ebr.** 6:10. Kama mtu yeyote akihudumu, na afanye hivyo kwa uwezo anaojaliwa na Mungu, **1 Pet.** 4:10–11.

Walifundisha, na kuhudumiana, **3 Ne.** 26:19.

Ni kazi ya wale Kumi na Wawili kuwatawaza wahudumu wa kiinjilisti, **M&M** 107:39–40. Kuhani mkuu aweza kuwekwa rasmi kwa kusimamia mambo ya kimwili, **M&M** 107:71–72. Hawa sabini watakuwa wahudumu wanao safiri, **M&M** 107:93–97. Wazee ni wahudumu wa kudumu wa kanisa langu, **M&M** 124:137.

Kuinuliwa. *Ona pia* Lipia dhambi, Upatanisho; Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni; Taji; Utukufu wa Selestia; Uzima wa Milele

Hali ya furaha iliyo ya juu zaidi na utukufu katika ufalme wa selestia.

Katika uwepo wako ziko utimilifu wa shangwe, **Zab.** 16:11.

Wao ndiyo miungu, hata wana wa Mungu—kwa hiyo, vitu vyote ni vyao, **M&M** 76:58–59. Watakatifu watapata urithi wao na watafanywa kuwa sawa naye, **M&M** 88:107. Malaika hawa hawakuishi kulingana na sheria zangu; kwa hiyo, watabaki wametengana mmoja mmoja, pasipo kuinuliwa, **M&M** 132:17. Wanaume na wanawake lazima waoe na kuoana kulingana na sheria ya Mungu ili kupata kuinuliwa, **M&M** 132:19–20. Mlango ni mwembamba na njia imesonga iongozayo katika kuinuliwa, **M&M** 132:22–23. Ibrahimu, Isaka, na Yakobo wameingia ndani ya kuinuliwa kwao, **M&M** 132:29, 37. Ninafunga juu yako kuinuliwa kwao, **M&M** 132:49.

Kujisifu. *Ona* Kiburi

Kujua yote. *Ona pia* Mungu, Uungu

Sifa ya kiungu ya kuwa na maarifa yote (Mt. 6:8; 2 Ne. 2:24).

Kukiri. *Ona* Kiri, Kukiri

Kukufuru, Kufuru. *Ona pia* Dhambi isiyo sameheka; Lugha chafu

Kuongea bila heshima au staha juu ya Mungu au vitu vitakatifu.

Yesu alituhumiwa mara kadhaa na Wayahudi kwa madai ya kukufuru kwa sababu Yeye alidai haki ya kusamehe dhambi (Mt. 9:2–3; Lk. 5:20–21), kwa sababu Yeye alijiita Mwenyewe kuwa ni Mwana wa Mungu (Yn. 10:22–36; 19:7), na kwa sababu Yeye alisema wao watamwona Yeye ameketi mkono wa kuume wa nguvu na kuja juu ya mawingu ya mbinguni (Mt. 26:64–65). Tuhuma hizi zingekuwa kweli kama Yeye hakika Hakuwa kile Alichosema Alikuwa. Tuhuma ililetwa dhidi Yake na mashahidi waongo katika kesi mbele ya Sanhedrini (Mt. 26:59–61) ilikuwa kukufuru dhidi ya hekalu la Mungu. Kukufuru dhidi ya Roho Mtakatifu, ambavyo ni kumkana Kristo makusudi baada ya kupokea elimu kamili juu Yake ni dhambi isiyosameheka (Mt. 12:31–32; Mk. 3:28–29; M&M 132:27).

Yule ambaye anakufuru jina la Bwana atauawa, **Law.** 24:11–16.

Maadui wa Bwana hawataachiliwa kukufuru jina lake, **M&M** 105:15. Kisasi kitakuwa juu ya wale ambao wanakufuru dhidi ya Bwana, **M&M** 112:24–26.

Kukusanyika kwa Israeli. *Ona* Israeli—Kukusanyika kwa Israeli

Kumbukumbu la Torati. *Ona pia* Torati

Kitabu cha tano katika Agano la Kale. Kumbukumbu la torati inazo hotuba tatu za mwisho za Musa, ambazo alizitoa katika nyanda za Moabu muda mfupi kabla ya kuhamishwa kwake. Hotuba ya kwanza (mlango wa 1–4) ni utangulizi. Hotuba ya pili (mlango wa 5–26) ina sehemu mbili: (1) mlango wa 5–11—ni zile Amri Kumi na maelekezo ya utekelezaji wake; na (2) mlango 12–26—ni mfumo wa sheria, ambazo zinaunda kiini cha kitabu chote. Hotuba ya tatu (mlango wa 27–30) zina marudio ya moyo wa dhati ya agano kati ya Israeli na Mungu na tangazo la baraka ambazo zinafuata utiifu na laana ambazo hufuatia kutotii. Mlango wa 31–34 inaelezea kutolewa kwa sheria kwa Walawi, wimbo wa Musa na baraka ya mwisho, na kuondoka kwa Musa.

Kumi na Wawili, Akidi ya Wale. *Ona* Mtume

Kumora, Mlima. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni; Moroni, Mwana wa Mormoni; Smith, Joseph, Mdogo

Kilima kidogo kilichoko magharibi ya New York, Marekani. Hapa ndipo nabii wa kale aliyeitwa Moroni alipoyaficha yale mabamba ya dhahabu yaliyokuwa na maandiko ya mataifa ya Wanefi na Wayaredi. Joseph Smith alielekezwa kwenda katika kilima hiki katika mwaka 1827 na Moroni mfufuka ili kuchukua mabamba haya na kutafsiri sehemu yake. Tafsiri hii ndicho Kitabu cha Mormoni.

Wanefi walikusanyika huko Kumora, **Morm.** 6:2–4. Kumora ilikuwa kwenye nchi ya maji mengi, **Morm.** 6:4. Mormoni alificha maandiko yake katika Kilima Kumora, **Morm.** 6:6. Wote isipokuwa Wanefi ishirini na wanne waliuawa huko Kumora, **Morm.** 6:11.

Tunasikia habari njema kutoka Kumora, **M&M** 128:20.

Joseph Smith alichukua mabamba kutoka Kilima Kumora, **JS—H** 1:42, 50–54, 59.

Kupaa. *Ona pia* Ujio wa Pili wa Yesu Kristo; Yesu Kristo

Kuondoka rasmi kwa Mwokozi kutoka duniani, siku arobaini baada ya Ufufuko Wake. Kupaa kulifanyika kutoka kileleni juu ya Mlima wa Mizeituni mbele ya wanafunzi wake (Mk. 16:19; Lk. 24:51). Wakati huo malaika wawili kutoka mbinguni walishuhudia kwamba hapo baadaye Bwana atarejea "jinsi hiyo hiyo" (Mdo. 1:9–12).

Kupenda anasa, Matamanio ya anasa. *Ona pia* Tamaa mbaya; Uasherati; Usafi wa Kimwili; Utovu wa maadili ya kujamiiana; Uzinzi

Hali ya kupenda au kutamani kusiko kwa haki kwa starehe ya kimwili, hususani kwa utovu wa maadili ya kujamiiana.

Mke wa Bwana wake akamtamani Yusufu, **Mwa.** 39:7.

Mtu yeyote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha tenda uzinzi, **Mt.** 5:28 (3 Ne. 12:28). Ziepukeni tamaa za mwili, zipiganazo dhidi ya roho, **1 Pet.** 2:11. Tamaa za mwili na tamaa za macho siyo za Baba, **1 Yoh.** 2:16.

Usizifuate tena tamaa za macho yako, **Alma** 39:9.

Kwa uvunjaji wa sheria hizi takatifu, mwanadamu akawa mwenye tamaa, **M&M** 20:20. Iwapo yeyote atafanya uzinzi mioyoni mwao, hawatakuwa na Roho Mtakatifu, **M&M** 63:16. Acheni tamaa zenu zote zilizo mbaya, **M&M** 88:121.

Watu wakaanza kuwa na tamaa za

kimwili, kupenda anasa, na uovu, **Musa** 5:13 (Mos. 16:3; Musa 6:49).

Kura. *Ona* Ridhaa ya Wengi

Kurudiwa. *Ona* Rudi, Kurudiwa

Kusema uongo. *Ona pia* Danganya, Kudanganya, Udanganyifu; Kusema uovu; Mwaminifu, Uaminifu

Taarifa yoyote yenye uongo au isiyo kweli kwa madhumuni ya kudanganya.

Msiibe, wala msidanganye, wala msiambiane uongo, **Law.** 19:11. Ninauchukia uongo na umekithiri, **Zab.** 119:163. Midomo ya uongo ni chukizo kwa Bwana, **Mit.** 12:22. Ni watu wangu hao ambao hawatasema uongo, **Isa.** 63:8.

Ibilisi ndiye mwongo na baba wa uongo, **Yn.** 8:44 (2 Ne. 2:18; Eth. 8:25; Musa 4:4). Hukumwambia uongo mwanadamu, bali Mungu, **Mdo.** 5:4 (Alma 12:3). Kama mtu akisema, Nampenda Mungu, naye anamchukia ndugu yake, yeye ni mwongo, **1 Yoh.** 4:20. Waongo wote wanayo sehemu yao katika mauti ya pili, **Ufu.** 21:8 (M&M 63:17).

Ole wako mwongo, kwani atatupwa chini jehanamu, **2 Ne.** 9:34. Wengi watafundisha mafundisho ya uongo, wakisema: danganyeni kidogo na hakuna baya ndani yake, **2 Ne.** 28:8–9 (M&M 10:25). Je, wadhani waweza kudanganya kwa Bwana, **Alma** 5:17. Wewe u Mungu wa ukweli nawe huwezi kudanganya, **Eth.** 3:12 (Hes. 23:19; 1 Sam. 15:29; Tit. 1:2; Ebr. 6:18; Eno. 1:6).

Mtu adanganyaye na hatubu atatupwa nje, **M&M** 42:21. Waongo watarithi utukufu wa telestia, **M&M** 76:81, 103–106.

Tunaamini katika kuwa waaminifu, **M ya I** 1:13.

Kusema uovu. *Ona pia* Kusema uongo; Sengenya; Ushindani; Uvumi

Kusema mambo ambayo siyo sahihi, yenye kuumiza, na yaliyo mabaya. Mara kwa mara katika maandiko misemo ya jinsi hii huelekezwa kwa mtu kwa dhamira maalumu ya kumsababishia maumivu.

Uzuie ulimi wako na uovu, **Zab.** 34:13 (1 Pet. 3:10). Mtu asiye mchamungu huchimba uovu, **Mit.** 16:27.

Heri ninyi watu watakapo wanenea kila neno ovu kwa uongo, **Mt.** 5:11 (3 Ne. 12:11). Moyoni hutoka mawazo maovu, **Mt.** 15:19 (Mk. 7:21). Usinene mabaya ya mtawala, **Mdo.** 23:5. Na maneno maovu yote yaondoke kwenu, **Efe.** 4:31. Msineneane uovu, **Yak. (Bib.)** 4:11.

Angalieni kwamba hakuna masengenyo, wala kusema uovu, **M&M** 20:54.

Kusengenya. *Ona* Kusema uovu

Kustahili, enye Kustahili, Ustahiliki. *Ona pia* Haki, Uadilifu, enye Uadilifu

Kuwa mwadilifu kibinafsi na kuwa mwenye kukubalika mbele za Mungu na viongozi Wake wateule.

Mtu asiyechukua msalaba wake hanistahili, **Mt.** 10:38. Mtenda kazi anastahili kupewa ujira wake, **Lk.** 10:7 (M&M 31:5).

Angalieni kwamba mnafanya mambo yote katika ustahmilivu, **Morm.** 9:29. Hawakubatizwa isipokuwa walipokuwa wamekuwa wenye kustahili, **Moro.** 6:1.

Yule aliye mzembe hatahesabika kuwa mwenye kustahili kusimama, **M&M** 107:100. Mtu ambaye hakustahimili kurudiwa haustahili ufalme wangu, **M&M** 136:31. Ukuhani uliruhusiwa kutolewa kwa waumini wanaume wote wenye kustahili, **TR** 2.

Kusulubiwa. *Ona pia* Golgotha; Lipia dhambi, Upatanisho; Msalaba; Yesu Kristo

Mtindo wa uuaji wa Kirumi uliokuwa maarufu katika nyakati za Agano Jipya, ambamo mtu alikuwa akiuawa kwa kufungwa au kupigiliwa misumari katika mikono yake na miguu yake kwenye msalaba. Kwa kawaida ilikuwa ikifanyika kwa watumwa tu na wahalifu wa daraja la chini kabisa. Kusulubiwa

daima kulitanguliwa na kupigwa kwa mijeledi (Mk. 15:15). Mtu aliyekuwa akisulubiwa kwa kawaida alikuwa akibebeshwa msalaba wake kwenda mahali pa kuulia (Yn. 19:16–17). Mavazi yake kwa kawaida yalichukuliwa na askari waliokuwa wakitekeleza hukumu yake (Mt. 27:35). Msalaba ulisimamishwa kwa kufukiwa chini ardhini ili miguu ya mtu huyo iwe futi moja au mbili tu kutoka ardhini. Msalaba ulilindwa na askari hadi mtu wa juu ya msalaba amekufa, kitu ambacho mara nyingine kilichukua hadi siku tatu (Yn. 19:31–37).

Yesu Kristo alisulibiwa kwa sababu kikundi cha wasioamini kimakosa kabisa walimshtaki kwa uasi dhidi ya Kaisari na kukufuru kwa sababu Yeye alisema kuwa Yeye alikuwa Mwana wa Mungu. Joho la zambarau (Yn. 19:2), taji la miiba, na matukano mengine yalitolewa kwa Yesu (Mt. 26:67; Mk. 14:65).

Waovu wataitoboa mikono na miguu ya Masiya, **Zab.** 22:11–18. Kristo atakwenda kama mwanakondoo kwa mchinjaji, **Isa.** 53:7.

Yesu alitabiri kusulubiwa kwake, **Mt.** 20:18–19. Kusulubiwa kwa Kristo kwaelezwa, **Mt.** 27:22–50 (Mk. 15:22–37; Lk. 23:26–46; Yn. 19:17–30).

Nefi aliona katika ono kusulubiwa kwa Mwanakondoo wa Mungu, **1 Ne.** 11:33. Nefi alisema juu ya mateso na kusulibiwa kwa Kristo, **1 Ne.** 19:9–14. Yakobo alinena juu ya huduma na kusulibiwa kwa Mtakatifu wa Israeli, **2 Ne.** 6:9. Dhoruba, matetemeko ya ardhi, moto, na matufani katika Marekani vilithibitisha kusulubiwa kwa Kristo katika Yerusalemu, **3 Ne.** 8.

Mimi ndiye Kristo aliyesulubiwa, **M&M** 45:51–52. Huduma ya Kristo miongoni mwa roho zilizokuwa kifungoni ilidumu kwa muda kati ya kifo chake na ufufuko, **M&M** 138:27.

Kutaamali. *Ona* Tafakari

Kutawanyika kwa Israeli. *Ona* Israeli—Kutawanyika kwa Israeli

Kutawaza, Kutawazwa. *Ona pia* Ita, Itwa na Mungu, Wito; Mamlaka; Mikono, Kuweka juu ya; Ofisa, Ofisi; Ukuhani

Kuteua au kutunuku mamlaka au ofisi. Ili kutumia mamlaka katika Kanisa la Bwana, mtu lazima aitwe na Mungu, kwa njia ya unabii, na kuwekewa mikono na wale walio katika mamlaka (M ya I 1:5). Ingawa mtu anaweza kupokea ukuhani kwa kutawazwa, atayatumia mamlaka hayo chini ya maelekezo ya wale wenye kushikilia funguo hizo kwa mamlaka hiyo.

Nimekutawaza kuwa nabii kwa mataifa, **Yer.** 1:5.

Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi, **Yn.** 15:16.

Akiwa na mamlaka kutoka kwa Mungu, Alma aliwatawaza makuhani, **Mos.** 18:18. Wanaume wametawazwa katika ukuhani mkuu kwa agizo takatifu, **Alma** 13:1–9. Yesu aliwaita na kuwatawaza wanafunzi kumi na wawili, **3 Ne.** 12:1. Wazee huwatawaza makuhani na walimu kwa kuwawekea mikono, **Moro.** 3.

Ngojeni bado kitambo kidogo, kwani bado hamjatawazwa, **M&M** 5:17. Joseph Smith alitawazwa kuwa Mtume wa Yesu Kristo, **M&M** 20:2 (M&M 27:12). Mtu asitawazwe pasipo kura ya Kanisa, **M&M** 20:65. Haitatolewa kwa yeyote kuihubiri injili yangu, isipokuwa ametawazwa na mtu aliye na mamlaka, **M&M** 42:11. Wazee wametawazwa ili kuihubiri injili yangu, **M&M** 50:13–18. Ni wajibu wa wale Kumi na Wawili kuwatawaza na kuwaweka katika utaratibu maofisa wengine wote wa Kanisa, **M&M** 107:58.

Nilitafuta baraka za mababu, na haki ambayo kwayo nilipaswa kutawazwa, **Ibr.** 1:2. Joseph Smith na Oliver Cowdery walitawazana katika Ukuhani wa Haruni, **JS—H** 1:68–72.

Kutawazwa. *Ona* Kutawaza, Kutawazwa

Kutawazwa Katika Ukuhani. *Ona* Kutawaza, Kutawazwa

Kutengwa na Kanisa. *Ona pia* Uasi; Ukengeufu

Hatua ya kumtenga mtu na Kanisa ni hatua ya kinidhamu iliyo kali kupita zote. Mtu anayetengwa na Kanisa si muumini tena wa Kanisa. Mamlaka za Kanisa humtenga mtu na Kanisa pale tu anapochagua kuishi kinyume na amri za Bwana na hivyo hujiondolea haki yeye mwenyewe ya kuendelea kuwa muumini katika Kanisa.

Mioyo ya wengi ilishupaa, na majina yao yakafutwa, **Alma** 1:24 (Alma 6:3). Kama hatatubu hatahesabika kuwa miongoni mwa watu wangu, **3 Ne.** 18:31 (Mos. 26).

Wazinzi wasio tubu watafukuzwa, **M&M** 42:24. Yule atendaye dhambi na hatubu atafukuzwa, **M&M** 42:28. Taratibu zatolewa kwa ajili ya kutatua matatizo muhimu katika Kanisa, **M&M** 102 (M&M 42:80–93). Askofu huteuliwa kuwa mwamuzi katika Israeli, **M&M** 107:72. Jumuiya za kidini zinayo haki ya kuwashughulikia waumini wake kwa makosa yao, **M&M** 134:10.

Kutoamini. *Ona pia* Amini, Imani

Ukosefu wa imani kwa Mungu na injili Yake.

Hakufanya miujiza mingi huko kwa sababu ya kutoamini kwao, **Mt.** 13:58. Kwa sababu ya kutokuamini kwao wanafunzi wa Yesu hawakuweza kumtoa ibilisi, **Mt.** 17:14–21. Nisaidie kutokuamii kwangu, **Mk.** 9:23–24. Yesu akawakemea mitume wake kwa kutokuamini kwao na ugumu wa mioyo yao, **Mk.** 16:14. Je, kutokuamini kutaibatili imani ya Mungu, **Rum.** 3:3.

Ni bora mtu mmoja aangamie kuliko taifa kufifia na kuangamia katika kutokuamini, **1 Ne.** 4:13. Wakati utapofika ambapo wao watafifia katika kutoamini, atasababisha wao watawanywe na kupigwa, **2 Ne.** 1:10–11 (M&M 3:18). Kwa sababu ya kutokuamini kwao hawakuweza kulielewa neno la Mungu, **Mos.** 26:1–5. Sikuweza kuwaonyesha Wayahudi miujiza mikuu kwa sababu ya kutokuamini kwao, **3 Ne.** 19:35.

Mawazo yenu katika nyakati zilizopita yalitiwa giza kwa sababu ya kutokuamini, **M&M** 84:54–58.

Kutoka. *Ona pia* Torati

Kitabu kilichoandikwa na Musa katika Agano la Kale ambacho kinaelezea kuondoka kwa Waisraeli kutoka Misri. Historia ya awali ya Israeli kama ilivyoandikwa katika kutoka inaweza kugawanywa katika sehemu tatu: (1) utumwa wa watu hawa kwa Misri, (2) kuondoka kwao kutoka Misri chini ya uongozi wa Musa, na (3) kujitolea kwao kwa dhati katika huduma ya Mungu katika maisha yao ya kidini na maisha yao ya kisiasa.

Sehemu ya kwanza, Kutoka 1:1–15:21, inafafanua ukandamizwaji wa Israeli katika Misri; historia ya awali na wito wa Musa; Kutoka na kuanzishwa kwa Pasaka; na msafara wa kwenda Bahari ya Shamu, angamizo la jeshi la Farao, na wimbo wa Musa wa ushindi.

Sehemu ya pili, Kutoka 15:22–18:27, inaelezea juu ya ukombozi wa Israeli na matukio ya safarini kutoka Bahari ya Shamu hadi Sinai, maji machungu ya Mara, kutolewa kwa kware na mana, kuishika Sabato, zawadi ya kimuujiza ya maji huko Refidimu, na pambano lao hapo na Waamaleki; kuwasili kwa Yethiro kambini na ushauri wake juu ya kuwatawala watu na matatizo yao ya kila siku.

Sehemu ya tatu, mlango wa 19–40, hujishughulisha na kujiweka wakfu kwa Israeli kwa huduma ya Mungu wakati wa matukio mazito katika Sinai. Bwana aliwatenga watu kama ufalme wa makuhani na taifa takatifu; Yeye akatoa Amri Kumi; na Akatoa mafundisho juu ya hema, samani zake, na kuabudu ndani yake. Hatimaye inafuata historia ya dhambi za watu hawa katika kuabudu ndama wa dhahabu, na mwishowe historia ya ujenzi wa hema na kutolewa kwa vifaa vyote vya huduma yake.

Kutokuwa Adilifu, Siyo Adilifu.
Ona pia Chafu, Uchafu; Dhambi; Haki, Uadilifu, enye Uadilifu; Ovu, Uovu; Sio mcha mungu

Ovu, sio haki; watu ambao hawampendi Mungu au mambo ya Mungu na ambao hawaungi mkono kazi Yake.

Wadhalimu hawatarithi ufalme wa Mungu, **1 Kor.** 6:9–10. Wale ambao hufurahia katika udhalimu watahukumiwa, **2 The.** 2:12. Yesu Kristo anaweza kutusafisha kutokana na udhalimu wote, **1 Yoh.** 1:9.

Mfalme dhalimu huzichafua njia zote za haki, **Mos.** 29:23. Msingi wa angamizi unawekwa na udhalimu wa wanasheria na waamuzi, **Alma** 10:27.

Ninawatuma ninyi kuwakemea walimwengu juu ya matendo yao ya udhalimu, **M&M** 84:87. Nafsi lazima itakaswe kutokana na udhalimu wote, **M&M** 88:17–18. Tabia ya karibu wanadamu wote ni kuanza kutumia utawala pasipo haki, **M&M** 121:39.

Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika.
Ona pia Haki ya uamuzi

Bwana amesema kwamba watu wote wanawajibika kwa nia zao wenyewe, mitazamo yao, tamaa zao, na matendo yao.

Umri wa uwajibikaji ni umri ule ambapo watoto wanafikiriwa kuwajibika kwa ajili ya matendo yao na kuweza kutenda dhambi na kutubu.

Nitamhukumu kila mmoja kwa kadiri ya njia zake, **Eze.** 18:30.

Watatoa hesabu ya kila neno lisilo maana, **Mt.** 12:36. Toa hesabu ya uwakili wako, **Lk.** 16:2. Kila mmoja wetu atatoa hesabu yake mwenyewe kwa Mungu, **Rum.** 14:12. Wafu watahukumiwa kulingana na matendo yao, **Ufu.** 20:12.

Maneno, matendo na mawazo yetu yatatushtaki, **Alma** 12:14. Tunajiamulia sisi wenyewe kufanya mema au maovu, **Alma** 41:7. Mmeruhusiwa kujiamulia ninyi wenyewe, **Hel.** 14:29–31. Jambo hili lifundisheni—toba na ubatizo kwa wale wenye kuwajibika, **Moro.** 8:10.

Wote lazima watubu na kubatizwa wafikiapo katika miaka ya uwajibikaji, **M&M** 18:42. Shetani hawezi kuwajaribu watoto wadogo, hadi waanzapo kuwajibika mbele zangu, **M&M** 29:46–47. Watoto wabatizwe wakiwa na miaka minane, **M&M** 68:27. Kila mtu atawajibika kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe katika siku ya hukumu, **M&M** 101:78.

Imetolewa kwa wanadamu kujua mema na maovu; kwa sababu hiyo wao ni mawakala kwao wenyewe, **Musa** 6:56. Wanadamu wataadhibiwa kwa ajili ya dhambi zao wenyewe, **M ya I** 1:2.

Kuwakubali Viongozi wa Kanisa.
Ona pia Ridhaa ya Wengi

Kutoa ahadi ya kuwaunga mkono viongozi wakuu wa Kanisa au wa maeneo yetu walio katika nafasi za uongozi.

Ukamweke Yoshua mbele ya mkutano wote, na ukampe mausia mbele ya macho yao, **Hes.** 27:18–19. Watu wote wakapiga kelele, na kusema, Mungu mwokoe mfalme, **1 Sam.** 10:24. Waamini manabii wake, ndivyo mtakavyofanikiwa, **2 Nya.** 20:20.

Watiini wao walio watawala juu yenu, **Ebr.** 13:17.

Wewe utapendelewa na Bwana, kwa sababu wewe hujanung'unika, **1 Ne.** 3:6. Waliowapokea manabii walihurumiwa, **3 Ne.** 10:12–13. Sikilizeni maneno ya hawa Kumi na wawili, **3 Ne.** 12:1.

Kwa sauti yangu mimi mwenyewe au kwa sauti ya watumishi wangu, yote ni sawa, **M&M** 1:38. Maneno yake mtayapokea, kama vile yatoka kinywani mwangu mwenyewe, **M&M** 21:5. Yeye awapokeaye watumishi wangu, hunipokea mimi, **M&M** 84:35–38. Yeyote anipokeaye mimi, huwapokea wale niliowatuma, **M&M** 112:20. Kama watu wangu hawatasikiliza sauti za watu hawa ambao nimewateua, hawatabarikiwa, **M&M** 124:45–46.

Kuwekea Mikono. *Ona* Mikono, Kuweka juu ya

Kuzamisha. *Ona* Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa kuzamishwa

Laani, Laana. *Ona pia* Hukumu; Lugha chafu

Katika maandiko, laana ni matumizi ya sheria takatifu ambayo huruhusu au huleta adhabu na matokeo yake juu ya kitu, au mtu, au watu kimsingi ni kwa sababu ya utovu wa haki. Laana ni kuonekana kwa upendo mtakatifu na haki ya Mungu. Zaweza kutolewa moja kwa moja na Mungu au kutamkwa na mtumishi Wake mwenye mamlaka. Wakati mwingine, sababu kamilifu za laana hujulikana tu kwa Mungu. Kwa nyongeza, hali ya laana huwatokea wale ambao kwa makusudi hawamtii Mungu na hivyo kujiengua wao wenyewe kutoka kwa Roho wa Bwana.

Bwana aweza kuiondoa laana kwa sababu ya imani ya mtu mmoja au ya watu katika Yesu Kristo na utiifu wao katika sheria na ibada za injili (Alma 23:16–18; 3 Ne. 2:14–16; M ya I 1:3).

Mungu alimlaani yule nyoka kwa kwa sababu ya kuwadanganya Adamu na Hawa, **Mwa.** 3:13–15 (Musa 4:19–21). Ardhi ikalaaniwa kwa ajili ya Adamu na Hawa, **Mwa.** 3:17–19 (Musa 4:23–25). Bwana akamlaani Kaini kwa kumuua Abili, **Mwa.** 4:11–16 (Musa 5:22–41). Bwana akamlaani Kanaani na wazao wake, **Mwa.** 9:25–27 (Musa 7:6–8; Ibr. 1:21–27). Israeli atabarikiwa kama atakuwa mtiifu kwa Mungu, na kulaaniwa kama hatakuwa mtiifu, **Kum.** 28 (Kum. 29:18–28). Gehazi na wazao wake walilaaniwa kwa ukoma wa Naamani, **2 Fal.** 5:20–27. Bwana alilaani taifa la kale la Israeli kwa kutokulipa zaka na matoleo, **Mal.** 3:6–10.

Yesu aliulaani mti wa mtini nao ukafa, **Mk.** 11:11–14, 20–21. Yesu akailaani miji ya Korazini, Bethsaida na Kapernaumu, **Lk.** 10:10–15.

Kwa sababu Walamani hawangemsikiliza Bwana, wakatengwa kutoka mbele za Bwana na kulaaniwa, **2 Ne.** 5:20–24. Wote anawaalika kuja kwa Bwana, **2 Ne.** 26:33. Bwana atawalaani wale watendao uasherati, **Yak. (KM)** 2:31–33. Wanefi watapokea laana kuu kuliko Walamani endapo hawatatubu, **Yak. (KM)** 3:3–5. Watu waasi hujiletea laana juu yao wenyewe, **Alma** 3:18–19 (Kum. 11:26–28). Korihori alilaaniwa kwa kuwapotosha watu kutoka kwa Mungu, **Alma** 30:43–60. Bwana alilaani nchi na utajiri wa Wanefi kwa sababu ya ouvu wa watu, **Hel.** 13:22–23 (2 Ne. 1:7; Alma 37:31). Bwana aliwalaani Wayaredi waovu, **Eth.** 9:28–35. Upatanisho wa Kristo huondoa laana ya Adamu kutoka kwa watoto wadogo, **Moro.** 8:8–12.

Wale wageukao mbali na Bwana wamelaaniwa, **M&M** 41:1. Dunia itapigwa kwa laana isipokuwa pamekuwepo na muunganiko imara kati ya baba na watoto, **M&M** 128:18 (Mal. 4:5–6).

Kutumia lugha chafu: Kulaani pia na kutumia lugha ambayo ni chafu, ya kukufuru, au ya dharau.

Watu wasitukane baba au mama zao, **Ku.** 21:17 (Mt. 15:4). Usiwatukane wale wanaotawala juu yako, **Ku.** 22:28 (Mh. 10:20). Wanaume na Wanawake wasimlaani Mungu, **Law.** 24:13–16.

Petro alilaani wakati alipokana kumjua Yesu, **Mt.** 26:69–74.

Wanefi waovu walimlaani Mungu na wakataka kufa, **Morm.** 2:14.

Labani, Kaka wa Rebeka. *Ona pia* Rebeka

Katika Agano la Kale, ni kaka wa Rebeka na baba wa Lea na Raheli, wakeze Yakobo (Mwa. 24:29–60; 27:43–44; 28:1–5; 29:4–29; 30:25–42; 31).

Labani, Mtunza Mabamba ya Shaba Nyeupe. *Ona pia* Mabamba ya Shaba Nyeupe

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mtu aliyetunza mabamba ya shaba nyeupe huko Yerusalemu katika wakati wa familia ya Lehi. Labani aliwazuia na kujaribu kuwaua Nefi na kaka zake (1 Ne. 3:1–27). Roho alimwongoza Nefi amwue

Labani ili apate hayo mabamba (1 Ne. 4:1–26).

Lamani. *Ona pia* Lehi, Baba wa Nefi; Walamani

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana mkubwa wa Lehi na Saria na kaka mkubwa wa Nefi (1 Ne. 2:5). Kwa kawaida Lamani alichagua kufanya uovu badala ya mema.

Lamani alimnung'unikia baba yake, **1 Ne.** 2:11–12. Aliasi dhidi ya kaka yake Nefi ambaye alikuwa mwaminifu, **1 Ne.** 7:6 (1 Ne. 3:28–29). Hakula tunda la mti wa uzima katika ono la Lehi, **1 Ne.** 8:35–36. Laana ikaja juu ya Lamani na wafuasi wake, **2 Ne.** 5:21 (Alma 3:7).

Lamoni. *Ona pia* Amoni, Mwana wa Mosia

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mfalme wa Kilamani aliyeongolewa na Roho wa Bwana na kazi takatifu na mafundisho ya Amoni (Alma 17–19).

Lawi. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mwana wa tatu wa Yakobo na Lea (Mwa. 29:34; 35:23). Lawi akawa baba wa mmojawapo wa makabila ya Israeli.

Kabila la Lawi: Yakobo akambariki Lawi na wazao wake (Mwa. 49:5–7, 28). Wazao wa Lawi walihudumu katika mahali patakatifu pa Israeli (Hes. 1:47–54). Haruni alikuwa Mlawi, na wazao wake walikuwa makuhani (Ku. 6:16–20; 28:1–4; 29). Walawi waliwasaidia wale makuhani, wana wa Haruni (Hes. 3:5–10; 1 Fal. 8:4). Wakati mwingine walikuwa kama wanamuziki (1 Nya. 15:16; Neh. 11:22); walichinja dhabihu (2 Nya. 29:34; Ezra 6:20); na kwa ujumla walisaidia katika kazi za hekaluni (Neh. 11:16). Walawi waliwekwa rasmi kwa huduma ya Bwana kutenda ibada kwa ajili ya wana wa Israeli. Walawi wenyewe walitolewa sadaka kwa niaba ya wana wa Israeli (Hes. 8:11–22); hivyo basi wao wakawa mali ya thamani ya Mungu, iliyotolewa Kwake mahali pa mzaliwa wa kwanza (Hes. 8:16). Hawakuwekwa wakfu bali walitakaswa kwa ajili ya ofisi yao (Hes. 8:7–16). Hawakuwa na urithi wa nchi katika Kanaani (Hes. 18:23–24), lakini wao walipokea fungu la kumi (Hes. 18:21), miji arobaini na nane (Hes. 35:6), na haki ya kupokea sadaka za watu katika nyakati za karamu (Kum. 12:18–19; 14:27–29).

Lazaro. *Ona pia* Maria wa Bethania; Martha

Katika Agano Jipya, ni kaka wa Martha na Maria. Yesu alimfufua kutoka kwa wafu (Yn. 11:1–44; 12:1–2, 9–11). Huyu siye Lazaro yule ombaomba katika mfano ambao Yesu alifundisha (Lk. 16:19–31).

Lea. *Ona pia* Labani, Kaka wa Rebeka; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni binti mkubwa wa Labani na ni mmoja wa wake za Yakobo (Mwa. 29). Lea alikuja kuwa mama wa wana sita na binti mmoja (Mwa. 29:31–35; 30:17–21).

Lehi, Baba wa Nefi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni nabii Mwebrania aliyeiongoza familia yake na waliomfuata kutoka Yerusalemu hadi nchi ya ahadi katika Marekani yapata mwaka 600 K.K. Lehi alikuwa ndiye nabii wa kwanza miongoni mwa watu wake katika Kitabu cha Mormoni.

Lehi alitoroka Yerusalemu pamoja na familia yake kwa amri ya Bwana (1 Ne. 2:1–4). Alikuwa ni wa uzao wa Yusufu, aliyeuzwa Misri (1 Ne. 5:14). Bwana alimpa ono la mti wa uzima (1 Ne. 8:2–35). Lehi na wanawe walijenga mashua na wakasafiri hadi Marekani (1 Ne. 17–18). Yeye na wazao wake wakastawi katika nchi mpya (1 Ne. 18:23–25). Kabla ya kufa, Lehi aliwabariki wanawe na aliwafundisha juu ya Kristo na juu ya kutokea kwa Kitabu cha Mormoni katika siku za mwisho (2 Ne. 1:1–4:12).

Kitabu cha Lehi: Joseph Smith alianza na Kitabu cha Lehi wakati alipokuwa

akitafsiri Kitabu cha Mormoni. Ilikuwa ni historia ambayo Mormoni aliifanyia ufupisho kutoka katika mabamba ya Lehi. Baada ya kupata kurasa 116 za muswada uliotafsiriwa kutoka katika kitabu hiki, Joseph alimpa muswada Martin Harris, ambaye kwa muda mfupi alitumika kama mwandishi wa Joseph katika tafsiri ya Kitabu cha Mormoni. Kurasa hizi ndizo zilipotezwa. Joseph hakurudia kutafsiri tena kitabu cha Lehi ili kufidia zile zilizopotea lakini badala yake alitafsiri historia nyingine inayofanana nayo kutoka katika mabamba ya dhahabu (ona utangulizi wa M&M 3; 10). Historia hizi nyingine ndivyo vitabu sita vya mwanzo vya Kitabu cha Mormoni.

Lehi, Jemedari wa Jeshi la Wanefi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni jemedari wa jeshi la Nefi (Alma 43:35–53; 49:16–17; 52:27–36; 53:2; 61:15–21).

Lehi, Mmisionari wa Kinefi. *Ona pia* Helamani, Mwana wa Helamani

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwanawe Helamani, aliyekuwa mwana wa Helamani. Lehi alikuwa mmisionari mkuu (Hel. 3:21; 4:14).

Alipewa jina la Lehi ili apate kumkumbuka mhenga wake, **Hel.** 5:4–6. Pamoja na Nefi, aliwafanya wengi waongoke, alitiwa gerezani, alizingirwa na moto, na alinena na malaika, **Hel.** 5:14–48. Alipokea mafunuo mengi kila siku, **Hel.** 11:23.

Lemueli. *Ona pia* Lamani; Lehi, Baba wa Nefi; Walamani

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana wa pili wa Lehi na ni mmoja kati ya kaka wakubwa wa Nefi. Aliungana na Lamani ili kumpinga Nefi.

Lehi alimwonya Lemueli ili awe imara, kama bonde, **1 Ne.** 2:10. Alimkasirikia Nefi na akamsikiliza Lamani, **1 Ne.** 3:28. Walemueli walijumuishwa miongoni mwa Walamani, **Yak. (KM)** 1:13–14 (Alma 47:35).

Liahona

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mpira wa shaba nyeupe wenye mishale miwili yenye kuonyesha mwelekeo—kama vile dira—na pia maelekezo ya kiroho kwa Lehi na wafuasi wake wakati walipokuwa waaminifu. Bwana aliwapa Liahona na kutoa maelekezo kupitia hiyo.

Lehi aliona mpira wa shaba nyeupe wenye mishale miwili iliyoonyesha njia ambayo Lehi na familia yake walipaswa kwenda, **1 Ne.** 16:10. Mpira ulifanya kazi kulingana na imani na bidii, **1 Ne.** 16:28–29 (Alma 37:40). Benjamini alimpa Mosia mpira, **Mos.** 1:16. Mpira au mwelekezi kiliitwa Liahona, **Alma** 37:38. Liahona ilifananishwa na neno la Kristo, **Alma** 37:43–45.

Mashahidi Watatu wa Kitabu cha Mormoni watamwona mwelekezi aliyepewa Lehi, **M&M** 17:1.

Limhi. *Ona pia* Nuhu, Mwana wa Zenifu

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mfalme mwadilifu wa Wanefi katika nchi ya Nefi; alikuwa mwana wa Mfalme Nuhu (Mos. 7:7–9). Mfalme Limhi aliingia katika agano la kumtumikia Mungu (Mos. 21:32). Aliwaongoza watu wake kutoka katika utumwa wa Walamani na kurejea Zarahemla (Mos. 22).

Lipa zaka, Zaka. *Ona pia* Fedha; Sadaka, Utoaji sadaka

Sehemu moja ya kumi ya mapato ya mtu kwa mwaka aitoayo kwa Bwana kupitia katika Kanisa. Fedha za zaka hutumika kwa kujenga makanisa na mahekalu, kusaidia kazi ya kimisionari, na kujenga ufalme wa Mungu duniani.

Ibrahimu alitoa zaka ya vyote alivyokuwa navyo kwa Melkizedeki, **Mwa.** 14:18–20 (Ebr. 7:1–2, 9; Alma 13:15). Zaka yote ni ya Bwana: ni takatifu kwa Bwana, **Law.** 27:30–34. Hakika utatoa fungu la kumi la maongezo yako yote, **Kum.** 14:22, 28. Na zaka za vitu vyote walivileta kwa wingi, **2 Nya.** 31:5. Je,

mwanadamu atamwibia Mungu? Tumekuibia katika nini? Katika zaka na matoleo, **Mal.** 3:8–11 (3 Ne. 24:8–11).

Mtu alipaye zaka hataungua moto wakati wa ujio wake, **M&M** 64:23 (M&M 85:3). Nyumba ya Bwana itajengwa kwa zaka ya watu wake, **M&M** 97:11–12. Bwana aliifunua sheria ya zaka, **M&M** 119. Matumizi ya zaka yatapangwa na Baraza, **M&M** 120.

Lipia dhambi, Upatanisho. *Ona pia* Anguko la Adamu na Hawa; Damu; Dhabihu; Gethsemani; Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki; Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa; Komboa, Kombolewa, Ukombozi; Kusulubiwa; Mpango wa Ukombozi; Msalaba; Neema; Ondoleo la Dhambi; Rehema, enye Rehema; Sakramenti; Samehe; Toba, Tubu; Ufufuko; Utakaso; Wana na Mabinti za Mungu; Watoto wa Kristo; Wokovu; Yesu Kristo

Kumpatanisha mwanadamu kwa Mungu.

Kama ilivyotumika katika maandiko, kulipia dhambi ni kuadhibiwa kwa ajili ya tendo la dhambi, kwa njia hiyo unaondoa athari ya dhambi kutoka kwa mtenda dhambi na kumruhusu apate kupatanishwa na Mungu. Yesu Kristo alikuwa mtu pekee mwenye uwezo wa kufanya upatanisho mkamilifu kwa ajili ya wanadamu wote. Aliweza kufanya hivyo kwa sababu ya kuchaguliwa Kwake na kuteuliwa kabla katika Baraza Kuu kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu (Eth. 3:14; Musa 4:1–2; Ibr. 3:27), uungu Mwana Wake, na maisha Yake yasiyo na dhambi. Upatanisho Wake ulijumuisha kuteseka Kwake kwa ajili ya dhambi za wanadamu, katika, kumwagika kwa damu Yake, na kifo Chake na hatimaye ufufuko kutoka kaburini (Isa. 53:3–12; Lk. 22:44; Mos. 3:5–11; Alma 7:10–13; M&M 19:16–19). Kwa sababu ya Upatanisho, watu wote watafufuka kutoka wafu wakiwa na miili isiyokufa (1 Kor. 15:22). Upatanisho pia umeleta njia ambayo kwayo sisi tunaweza kusamehewa dhambi zetu na kuishi pamoja na Mungu milele. Lakini mtu aliyefikia umri wa uwajibikaji na kupokea sheria anaweza kupata baraka hizi endapo tu atakuwa na imani katika Yesu Kristo, akatubu dhambi zake, na kupokea ibada za wokovu, na kutii amri za Mungu. Wale ambao hawafikii umri wa uwajibikaji na wale wasio na sheria wamekombolewa kwa njia ya Upatanisho (Mos. 15:24–25; Moro. 8:22). Maandiko kwa uwazi kabisa yanatufundisha kama Kristo asingelipa kwa ajili ya dhambi zetu, hakuna sheria, ibada, au dhabihu ambayo ingeridhisha matakwa ya haki, na mwanadamu kamwe asingeweza kufika tena katika uwepo wa Mungu (2 Ne. 2; 9).

Hii ni damu yangu, iliyomwagika kwa ajili ya wengi kwa ajili ya maondoleo ya dhambi, **Mt.** 26:28. Jasho lake lilikuwa kama vile yalikuwa matone makubwa ya damu, **Lk.** 22:39–44. Nitautoa mwili wangu kwa ajili ya uzima wa ulimwengu, **Yn.** 6:51. Mimi ni ufufuko, na uzima, **Yn.** 11:25. Kristo ndiye sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii, **Ebr.** 5:9. Tunatakaswa kwa kumwagika kwa damu ya Kristo, **Ebr.** 9; 10:1–10. Kristo pia mara moja ameteseka kwa ajili ya dhambi, **1 Pet.** 3:18. Damu ya Yesu Kristo yatusafisha dhambi zote, **1 Yoh.** 1:7.

Aliinuliwa juu ya msalaba na kuuawa kwa ajili ya dhambi, **1 Ne.** 11:32–33. Ukombozi huja kwa wale wenye moyo uliovunjika na roho iliyo pondeka, **2 Ne.** 2:3–10, 25–27. Alijitoa yeye mwenyewe kuwa dhabihu kwa ajili ya dhambi, **2 Ne.** 2:7. Upatanisho hufidia wanadamu kutokana na Anguko na kuwaokoa kutokana na mauti na jehanamu, **2 Ne.** 9:5–24. Unahitajika uwe upatanisho usio na kipimo, **2 Ne.** 9:7. Patanishweni kwa Mungu kwa kupitia upatanisho wa Kristo, **Yak. (KM)** 4:11. Damu yake hulipia kwa ajili ya dhambi za wale ambao kwa ujinga wametenda dhambi, **Mos.** 3:11–18. Mwanadamu

alipokea wokovu kwa njia ya Upatanisho, **Mos.** 4:6–8. Kama isingelikuwa kwa Upatanisho, lazima bila kuepuka wangeangamia, **Mos.** 13:27–32. Atalipia kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, **Alma** 34:8–16. Mungu mwenyewe hulipia dhambi za ulimwengu, ili kutimiza mpango wa rehema, **Alma** 42:11–30. Mimi ni Mungu wa dunia yote, niliyeuawa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, **3 Ne.** 11:14.

Mimi, Mungu, nimeteseka mambo haya yote kwa ajili ya wote, **M&M** 19:16. Watoto wadogo wamekombolewa kwa njia ya Mwanangu wa Pekee, **M&M** 29:46–47. Tazama mateso na kifo chake yeye ambaye hakutenda dhambi, **M&M** 45:3–5.

Jambo hili ni mfano wa dhabihu ya Mwana Pekee, **Musa** 5:7. Kwa Upatanisho wa Kristo, wanadamu wote wapate kuokolewa, **M ya I** 1:3.

Lugha

Maneno, yaliyoandikwa au kunenwa, yaliyowekwa pamoja katika mpangilio maalumu ili kuwasilisha taarifa, mawazo, au hoja. Namna tunavyoitumia lugha huonyesha hisia zetu kwa Mungu na kwa watu wengine. Wakati wa Ujio wa Pili wa Yesu Kristo Bwana ataitoa kwa wanadamu wote lugha iliyo safi (Sef. 3:8–9).

Dunia yote ilikuwa na lugha moja, **Mwa.** 11:1. Bwana aliichanganyisha lugha ya dunia yote, **Mwa.** 11:4–9.

Kila mtu akawasikia wakinena katika lugha yake mwenyewe, **Mdo.** 2:1–6.

Bwana hunena kwa wanadamu kulingana na lugha yao, **2 Ne.** 31:3 (M&M 1:24). Benjamini aliwafundisha wanawe lugha ya baba zake, ili wapate kuwa watu wenye kuelewa, **Mos.** 1:2–5.

Yeye aliye na lugha ya upole na yenye kujenga ni wa Mungu kama anatii maagizo yangu, **M&M** 52:16. Kuzifahamu lugha, ndimi na watu, **M&M** 90:15.

Adamu na watoto wake walikuwa na lugha iliyokuwa safi na isiyo chafuliwa, **Musa** 6:5–6, 46. Mungu alimpa Henoko uwezo mkubwa wa lugha, **Musa** 7:13.

Lugha chafu. *Ona pia* Kukufuru, Kufuru

Utovu wa heshima au dharau kwa mambo matakatifu; hususani, kutoheshimu jina la Mungu.

Usilitaje bure jina la Bwana Mungu wako, **Ku.** 20:7 (2 Ne. 26:32; Mos. 13:15; M&M 136:21). Kwa nini tunakufuru agano la baba zetu, **Mal.** 2:10.

Kila neno lisilo na maana watakalolinena wanadamu, watatoa hesabu ya neno hilo katika hukumu, **Mt.** 12:34–37. Katika kinywa kile kile hutoka baraka na laana, haifai mambo hayo kuwa hivyo, **Yak. (Bib.)** 3:10.

Maneno yetu yatatuhukumu sisi, **Alma** 12:14 (Mos. 4:30).

Na watu wote wajihadhari namna wanavyolichukua jina langu katika midomo yao, **M&M** 63:61–62.

Luka. *Ona pia* Injili, Vitabu vya Biblia; Matendo ya Mitume

Mwandishi wa Injili ya Luka na kitabu cha Matendo katika Agano Jipya na mmisionari mwenza wa Paulo. Alizaliwa kwa wazazi wa Kiyunani na alikuwa tabibu (Kol. 4:14). Luka alikuwa msomi mzuri. Alijitambulisha mwenyewe kama mwenza wa Mtume Paulo wakati alipoungana na Paulo huko Troasi (Mdo. 16:10–11). Luka alikuwa pia pamoja na Paulo huko Filipi katika safari ya mwisho ya Paulo ya kwenda Yerusalemu (Mdo. 20:6), nao wawili walikuwa pamoja hadi walipowasili Roma. Luka alikuwa pia pamoja na Paulo wakati wa kifungo chake cha pili gerezani huko Roma (2 Tim. 4:11). Mapokeo yanasema alikufa kifo cha kishahidi.

Injili ya Luka: Taarifa ambayo Luka aliandika juu ya Yesu Kristo na huduma Yake alipokuwa katika mwili wenye kufa. Kitabu cha Matendo ya Mitume ni endelezo la Injili ya Luka. Luka aliacha taarifa iliyoandikwa vyema juu ya

huduma ya Yesu, akimwelezea Yesu kama Mwokozi wa wote Wayahudi na Wayunani. Aliandika mengi juu ya mafundisho ya Yesu na matendo Yake. Katika Luka tunapata tu habari za Gabrieli kuwatembelea Zakaria na Maria (Lk. 1); matembezi ya wachunga kondoo kwa mtoto Yesu (Lk. 2:8–18); Yesu hekaluni akiwa na umri wa miaka kumi na miwili (Lk. 2:41–52); kuamriwa na kutumwa kwa wale sabini (Lk. 10:1–24). Yesu anatoka jasho la damu (Lk. 22:44); majadiliano ya Yesu na mwizi juu ya msalaba (Lk. 23:39–43); na Yesu anakula samaki na asali baada ya Ufufuko Wake (Lk. 24:42–43).

Kwa orodha ya matukio katika maisha ya Mwokozi yaliyoelezwa katika Injili ya Luka, ona Upatanifu wa Injili katika kiambatisho.

Lulu ya Thamani Kuu. *Ona pia* Kanoni; Maandiko; Smith, Joseph, Mdogo

Ufalme wa Mungu duniani unalinganishwa na "lulu ya thamani kuu" (Mt. 13:45–46).

Lulu ya Thamani Kuu pia ni jina lililotolewa kwa moja ya vitabu vinne vya maandiko yanayoitwa "vitabu vitakatifu" vya Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Toleo la kwanza la Lulu ya Thamani Kuu lilichapishwa katika mwaka 1851 na lilikuwa na baadhi ya mambo ambayo sasa yapo katika Mafundisho na Maagano. Matoleo yaliyochapishwa tangu mwaka 1902 yana (1) dondoo kutoka tafsiri ya Joseph Smith ya Kitabu cha Mwanzo, kinachoitwa Kitabu cha Musa, na cha Mathayo 24, kinachoitwa Joseph Smith—Mathayo; (2) tafsiri ya Joseph Smith ya papiri fulani ya Kimisri ambayo aliiipata katika mwaka 1835, kinachoitwa Kitabu cha Ibrahimu; (3) dondoo kutoka katika historia ya Joseph Smith juu ya Kanisa ambayo aliiandika katika mwaka wa 1838, inayoitwa Joseph Smith—Historia ya; na (4) Makala ya Imani, matamko kumi na matatu juu ya imani na mafundisho.

Lusiferi. *Ona pia* Ibilisi; Jehanamu; Mpinga Kristo; Mwangamizi; Wana wa Upotevu

Jina hili maana yake "Mwenye Kung'ara" au "Mbebanuru." Pia hujulikana kama Mwana wa Asubuhi. Lusiferi alikuwa mwana wa kiroho wa Baba wa Mbinguni na aliongoza uasi katika maisha kabla ya kuzaliwa duniani. Jina Lusiferi linatokea mara moja tu katika Biblia (Isa. 14:12). Ufunuo wa siku za mwisho hutoa maelezo zaidi juu ya anguko la Lusiferi (M&M 76:25–29).

Lusiferi alianguka mbinguni, **Isa.** 14:12 (Lk. 10:18; 2 Ne. 24:12).

Baada ya anguko lake akawa Shetani na ibilisi, **M&M** 76:25–29 (Musa 4:1–4).

Lutu. *Ona pia* Ibrahimu

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Harani na mpwawe Ibrahimu (Mwa. 11:27, 31; Ibr. 2:4). Harani alikufa kwa sababu ya baa la njaa katika Uru (Ibr. 2:1). Lutu aliondoka Uru pamoja na Ibrahimu na Sara na akasafiri pamoja nao hadi Kaanani (Mwa. 12:4–5). Lutu alichagua kuishi Sodoma. Bwana aliwatuma wajumbe kwenda kumwonya Lutu aikimbie Sodoma kabla Bwana hajaiteketeza kwa sababu ya uovu wa watu (Mwa. 13:8–13; 19:1, 13, 15), hata hivyo, mkewe Lutu aliangalia nyuma wakati wa angamizo na akawa nguzo ya chumvi (Mwa. 19:26). Agano Jipya linayo marejeo kwa Lutu (Lk. 17:29; 2 Pet. 2:6–7). Maisha yake baada ya kutengana na Ibrahimu yanaelezwa katika Mwanzo 13, 14 na 19.

Maadili. *Ona* Uasherati; Usafi wa Kimwili; Utovu wa maadili ya kujamiiana; Uzinzi

Maandiko. *Ona pia* Biblia; Kanoni; Kitabu cha Mormoni; Lulu ya Thamani Kuu; Mafundisho na Maagano; Neno la Mungu

Maneno, yaliyoandikwa na kusemwa, na watu watakatifu wa Mungu wakiwa wanaongozwa na Roho Mtakatifu.

Maandiko matakatifu yanayotambuliwa rasmi na Kanisa siku hizi ni pamoja na Biblia, Kitabu cha Mormoni, Mafundisho na Maagano, na Lulu ya Thamani Kuu. Yesu na waandishi wa Agano Jipya waliviheshimu vitabu vya Agano Jipya kama maandiko (Mt. 22:29; Yn. 5:39; 2 Tim. 3:15; 2 Pet. 1:20–21). Ona pia Wendo katika kiambatisho.

Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, wakati alipotufungulia maandiko?, **Lk.** 24:32. Mwayachunguza maandiko; kwa sababu mnadhani kwamba ninyi ndani yake mnao uzima wa milele, **Yn.** 5:39.

Maneno ya Kristo yatawaeleza mambo yote mpaswayo kuyatenda, **2 Ne.** 32:3. Kadiri wengi wanavyoongozwa kuamini maandiko wanakuwa imara na thabiti katika imani, **Hel.** 15:7–8.

Wanadamu hukosea katika kuyapinda maandiko na hawayaelewi, **M&M** 10:63. Maneno haya si ya wanadamu wala si ya mwanadamu, bali yangu mimi, **M&M** 18:34–36. Kuibuka kwa kitabu cha Mormoni kunathibitisha kwa ulimwengu kwamba maandiko ni ya kweli, **M&M** 20:2, 8–12. Muda wenu na utumike kwa kujifunza maandiko, **M&M** 26:1. Maandiko yanatolewa kwa ajili ya maelekezo kwa watakatifu, **M&M** 33:16. Maandiko hutolewa kwa wokovu wa wateule, **M&M** 35:20. Fundisheni kanuni za injili yangu, ambazo ziko katika Biblia na Kitabu cha Mormoni, **M&M** 42:12. Sheria zangu juu ya mambo haya zimetolewa katika maandiko yangu, **M&M** 42:28. Lolote wanalosema chini ya mwongozo wa Roho Mtakatifu ni maandiko, **M&M** 68:4.

Maandiko yaliyopotea: Kuna maandishi mengi matakatifu yaliyotajwa katika maandiko ambayo hatunayo leo, miongoni mwake ni vitabu hivi na waandishi hawa: agano (Ku. 24:7), vita vya Bwana (Hes. 21:14); Yashari (Yos. 10:13; 2 Sam. 1:18), matendo ya Sulemani (1 Fal. 11:41), Samweli mwonaji (1 Nya. 29:29), Nathali nabii (2 Nya. 9:29), Shemaya nabii (2 Nya. 12:15), Ido nabii (2 Nya. 13:22), Yehu (2 Nya. 20:34), misemo ya waonaji (2 Nya. 33:19), Henoko (Yuda 1:14), na maneno ya Zenoki, Neumu, na Zeno (1 Ne. 19:10), Zeno (Yak. [KM] 5:1), Zenoki na Ezia (Hel. 8:20), na kitabu cha ukumbusho (Musa 6:5); na nyaraka kwa Wakorintho (1 Kor. 5:9), kwa Waefeso (Efe. 3:3), na kutoka Laodikia (Kol. 4:16), na kutoka Yuda (Yuda 1:3).

Maandiko yahifadhiwe: Yatupasa kuzipata kumbukumbu hizi ili tupate kuyahifadhi maneno yaliyonenwa na manabii, **1 Ne.** 3:19–20. Yanipasa kuyahifadhi mabamba haya, **Yak. (KM)** 1:3. Vitu hivi vimetunzwa na kuhifadhiwa kwa mkono wa Mungu, **Mos.** 1:5. Vitunze vitu hivi vitakatifu, **Alma** 37:47.

Maandiko yatunzwe katika usalama, **M&M** 42:56.

Nitatumia jitihada zangu zote kuyalinda, **JS—H** 1:59.

Thamani ya maandiko: Utasoma torati hii mbele ya Israeli wote, **Kum.** 31:10–13. Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako, **Yos.** 1:8. Sheria ya Bwana ni kamilifu, huiongoa nafsi, **Zab.** 19:7. Neno lako ni taa ya miguu yangu, **Zab.** 119:105.

Maandiko hunishuhudia mimi, **Yn.** 5:39. Maandiko yote hutolewa kwa mwongozo wa Mungu na yafaa kwa mafundisho na maelekezo, **2 Tim.** 3:15–16.

Niliyalinganisha maandiko yote na sisi, ili yapate kuwa kwa manufaa na mafundisho yetu, **1 Ne.** 19:23. Moyo wangu hufurahia katika maandiko, **2 Ne.** 4:15–16. Tunaandika kwa bidii, ili kuwashawishi watoto wetu, na pia ndugu zetu, kuamini katika Kristo, **2 Ne.** 25:23. Waliyachunguza maandiko, na hawakusikiliza tena maneno ya huyu mtu mwovu, **Yak. (KM)** 7:23 (Alma 14:1). Kama siyo kwa ajili ya mabamba haya, lazima tungeliteseka katika ujinga, **Mos.** 1:2–7. Walikuwa wameyachunguza maandiko kwa bidii, ili wapate kujua neno la Mungu, **Alma** 17:2–3. Maandiko yanalindwa ili kuzileta roho katika wokovu, **Alma** 37:1–19 (2 Ne. 3:15). Neno

la Mungu litamwongoza mtu wa Kristo, **Hel.** 3:29.

Lolote watakalonena kwa uwezo wa Roho Mtakatifu litakuwa andiko takatifu na uwezo wa Mungu katika wokovu, **M&M** 68:4. Pigeni chapa utimilifu wa injili yangu kwa madhumuni ya kulijenga Kanisa langu na kuwatayarisha watu wangu, **M&M** 104:58–59.

Yeyote mwenye kulithamini neno langu hatadanganywa, **JS—M** 1:37.

Maandiko yaliyotolewa unabii kwamba yatakuja: Isaya alitabiri kuja kwa Kitabu cha Mormoni, **Isa.** 29:11–14. Twaa kijiti kimoja, na ukaandike juu yake, kwa Yuda, **Eze.** 37:15–20.

Vitabu vingine vitakuja, **1 Ne.** 13:39. Hamna haja ya kudhani kwamba Biblia ina maneno yangu yote, **2 Ne.** 29:10–14. Muikubali injili ya Kristo, itakayowekwa mbele yenu katika kumbukumbu zile zitakazokuja, **Morm.** 7:8–9. Heri yule ambaye atadhihirisha jambo hili, **Morm.** 8:16. Yaandike mambo haya nami nitayaonyesha katika wakati wangu mwenyewe utakapofika, **Eth.** 3:27 (Eth. 4:7).

Tunaamini kwamba bado atafunua mambo mengi, **M ya I** 1:9.

Maandiko, Yalipotea. *Ona* Maandiko—Maandiko yaliyopotea

Maarifa. *Ona pia* Hekima; Ufahamu; Ukweli

Ufahamu na uelewa, hususani wa ukweli kama ulivyofundishwa au kuthibitishwa na Roho.

Bwana ni Mungu wa maarifa, **1 Sam.** 2:3. Bwana ni mkamilifu, katika maarifa, **Ayu.** 37:16. Kumcha Bwana ni chanzo cha maarifa, **Mit.** 1:7. Yule mwenye maarifa huyazuia maneno yake, **Mit.** 17:27. Dunia itajawa na kumjua Bwana, **Isa.** 11:9 (2 Ne. 21:9; 30:15).

Mmeuondoa ufunguo wa maarifa, **Lk.** 11:52. Upendo wa Kristo wapita ufahamu, **Efe.** 3:19. Katika imani yenu tieni na wema, na katika wema wenu maarifa, **2 Pet.** 1:5.

Nefi alikuwa na ufahamu mkubwa wa wema wa Mungu, **1 Ne.** 1:1. Watakapomfahamu Mkombozi wao, **2 Ne.** 6:11. Wenye haki watakuwa na ufahamu ulio kamili wa uadilifu wao, **2 Ne.** 9:14. Roho hutupa maarifa, **Alma** 18:35. Ufahamu wenu ni mkamilifu katika lile jambo, **Alma** 32:34. Walamani watarejeshwa katika ufahamu wa kweli wa Mkombozi wao, **Hel.** 15:13. Mpate kujua kwa ufahamu ulio kamili kuwa ni ya Mungu, **Moro.** 7:15–17.

Watakatifu watapata hazina kubwa ya maarifa, **M&M** 89:19. Maarifa safi huikuza sana nafsi, **M&M** 121:42. Mtu aliye na funguo za ukuhani mtakatifu hana ugumu katika kupata maarifa ya kweli, **M&M** 128:11. Kama mtu anapata maarifa katika maisha haya, atakuwa na heri katika ulimwengu ujao, **M&M** 130:19. Haiwezekani kuokolewa katika ujinga, **M&M** 131:6.

Mabamba. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni; Mabamba ya Dhahabu

Hapo kale baadhi ya mataifa yalikuwa yakiandika historia yao na kumbukumbu zao juu ya mabamba ya chuma, kama ilivyokuwa kwa Kitabu cha Mormoni. Kwa taarifa zaidi, ona "Maelezo Mafupi kuhusu Kitabu cha Mormoni" katika kurasa za utangulizi za Kitabu cha Mormoni.

Mabamba ya Dhahabu. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni; Mabamba

Taarifa iliyoandikwa juu ya mabamba ya dhahabu. Inaelezea historia ya mataifa makubwa mawili ya mabara ya Marekani. Joseph Smith alitafsiri na kuchapisha sehemu ya mabamba haya. Tafsiri hii inaitwa Kitabu cha Mormoni (Kwa habari zaidi, ona "Utangulizi" na "Ushuhuda wa Joseph Smith Nabii" katika Kitabu cha Mormoni).

Mabamba ya Shaba Nyeupe. *Ona pia* Mabamba

Kumbukumbu ya Wayahudi kutoka mwanzo hadi miaka 600 K.K., yenye maandishi mengi ya manabii (1 Ne. 5:10–16). Kumbukumbu hii ilikuwa

ikitunzwa na Labani, mmoja wa wazee wa Kiyahudi katika Yerusalemu. Wakati Lehi na familia yake walipokuwa nyikani, Lehi aliwatuma wanawe kurudi Yerusalemu ili kuzileta kumbukumbu hizi (1 Ne. 3–4). (Kwa habari zaidi ona, "Maelezo Mafupi kuhusu Kitabu cha Mormoni," yaliyoko katika Kitabu cha Mormoni.)

Macho. *Ona* Jicho, Macho

Madaraja ya Utukufu. *Ona pia* Utukufu wa Selestia; Utukufu wa Telestia; Utukufu wa Terestria

Tofauti za falme katika mbingu. Wakati wa Hukumu ya Mwisho, kila mtu atarithi mahali pake pa kuishi milele katika utukufu wa ufalme maalumu, isipokuwa wale walio wana wa Upotevu.

Yesu alisema, Katika nyumba ya Baba yangu mna makao mengi, **Yn.** 14:2 (Eth. 12:32). Kuna utukufu mmoja wa jua, na mwingine wa mwezi, na mwingine wa nyota, **1 Kor.** 15:40–41. Paulo alinyakuliwa juu katika mbingu ya tatu, **2 Kor.** 12:2.

Kuna mahali pasipokuwa na utukufu na penye adhabu isiyo na mwisho, **M&M** 76:30–38, 43–45. Kuna madaraja matatu ya utukufu, **M&M** 76:50–113; 88:20–32.

Madhabahu. *Ona pia* Dhabihu

Kitu mfano wa meza kilichotumiwa kwa ajili ya kutolea dhabihu, matoleo, na kuabudu.

Nuhu akamjengea Bwana madhabahu na akamtolea sadaka za kuteketezwa, **Mwa.** 8:20. Abramu akamjengea Bwana madhabahu, **Mwa.** 12:7–8. Ibrahimu akamfunga mwanawe Isaka juu ya madhabahu, **Mwa.** 22:9 (Mwa. 22:1–13). Yakobo akajenga hapo madhabahu na akapaita mahali pale Eli-Betheli, **Mwa.** 35:6–7. Eliya akajenga madhabahu na akawataka makuhani wa Baali kufanya vivyo hivyo, **1 Fal.** 18:17–40.

Ukileta sadaka yako madhabahuni, kwanza patana na ndugu yako, **Mt.** 5:23–24. Niliona chini ya madhabahu roho zao waliochinjwa kwa ajili ya neno la Mungu, **Ufu.** 6:9 (M&M 135:7).

Lehi akajenga madhabahu ya mawe na akamtolea Mungu shukrani, **1 Ne.** 2:7.

Ibrahimu aliokolewa kutoka katika na mauti juu ya madhabahu ya Elkana, **Ibr.** 1:8–20.

Mafarisayo. *Ona pia* Wayahudi

Katika Agano Jipya, ni kundi la kidini miongoni mwa Wayahudi ambao jina lao lilieleza kujitenga au tofauti. Mafarisayo walijisifia wao wenyewe juu ya kushika kikamilifu torati ya Musa na kujiepusha na kitu chochote kinachohusiana na Wayunani. Waliamini katika maisha baada ya kifo, Ufufuko, na kuwepo kwa malaika na roho. Waliamini kwamba sheria za mdomo na mila zilikuwa na umuhimu sawa kama sheria zilizoandikwa. Mafundisho yao yaliipunguza dini kuwa kitu cha kutii kanuni na walihimiza kiburi cha kiroho. Walisababisha watu wengi wa Kiyahudi kumtilia mashaka Kristo na injili yake. Bwana aliwakana Mafarisayo na matendo yao katika Mathayo 23; Marko 7:1–23; na Luka 11:37–44.

Mafundisho na Maagano. *Ona pia* Kanoni; Kitabu cha Amri; Maandiko; Smith, Joseph, Mdogo

Mkusanyiko wa mafunuo matakatifu na maazimio ya kuongozwa na Mungu katika siku za mwisho. Bwana aliyatoa haya kwa Joseph Smith na wengine kadhaa waliomrithi kwa ajili ya kuanzisha na kusimamia ufalme wa Mungu hapa duniani katika siku hizi za mwisho. Mafundisho na Maagano ni moja ya vitabu vitakatifu vya maandiko katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho pamoja na Biblia, Kitabu cha Mormoni, na Lulu ya Thamani Kuu. Mafundisho na Maagano ni cha kipekee, hata hivyo, kwa sababu hiki siyo tafsiri ya maandiko ya zamani; Bwana ametoa mafunuo haya kwa manabii Wake wateule katika siku hizi za sasa ili kuurejesha ufalme Wake. Katika mafunuo

mtu husikia sauti laini lakini iliyo imara ya Bwana Yesu Kristo (M&M 18:35–36).

Historia ya Joseph Smith inasema kwamba Mafundisho na Maagano ni msingi wa Kanisa katika siku za mwisho na ni kwa manufaa ya ulimwengu (M&M 70 kichwa cha habari). Mafunuo yaliyomo yanaianzisha kazi ya kuitengeneza njia kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Bwana, katika utimilifu wa maneno yote yaliyonenwa na manabii tangu ulimwengu kuanza.

Mafundisho ya Kristo. *Ona pia* Injili; Mpango wa Ukombozi

Kanuni na mafundisho ya injili ya Yesu Kristo.

Mafundisho yangu yatadondoka kama mvua, **Kum.** 32:2. Hao wanung'unikao watajifunza elimu, **Isa.** 29:24.

Watu walishangaa mno kwa mafundisho yake, **Mt.** 7:28. Mafundisho yangu si yangu mimi, ila ni yake yeye aliyenituma, **Yn.** 7:16. Kila andiko lafaa kwa mafundisho, **2 Tim.** 3:16.

Hili ndilo fundisho la Kristo, na ndilo fundisho pekee na la kweli la Baba, **2 Ne.** 31:21 (2 Ne. 32:6). Hapatakuwa na ugomvi miongoni mwenu kuhusu mambo ya mafundisho yangu, **3 Ne.** 11:28, 32, 35, 39–40.

Shetani huichochea mioyo ya watu ili wabishe kuhusu mambo ya mafundisho yangu, **M&M** 10:62–63, 67. Wafundisheni watoto mafundisho ya toba, imani katika Kristo, ubatizo, na kipawa cha Roho Mtakatifu, **M&M** 68:25. Fundishaneni mafundisho ya ufalme, **M&M** 88:77–78. Mafundisho ya ukuhani yatatonatona juu ya roho yako, **M&M** 121:45.

Mafuta. *Ona pia* Huduma kwa Wagonjwa; Mzeituni; Paka mafuta

Kwa kawaida humaanishwa mafuta ya mzeituni yanapotajwa kama mafuta katika maandiko. Tangu nyakati za Agano la kale, mafuta ya mzeituni yamekuwa yakitumika kwa ibada za hekaluni na majumbani, kwa ajili ya upakaji wa mafuta, kwa kuwasha taa, na kwa chakula. Mafuta ya mzeituni wakati mwingine ni ishara ya usafi na ya Roho Mtakatifu na uwezo wake (1 Sam. 10:1, 6; 16:13; Isa. 61:1–3).

Kuhani atatia mafuta katika ncha ya sikio la kuume, **Law.** 14:28–29. Bwana amenituma nikupake mafuta uwe mfalme juu ya watu wake, **1 Sam.** 15:1. Ile chupa ya mafuta ya mjane haikupungua, **1 Fal.** 17:10–16. Bwana amenipaka mafuta kichwani pangu, **Zab.** 23:5.

Waliwapaka mafuta wengi waliokuwa wagonjwa, **Mk.** 6:13. Acha wazee wamwombee, na kumpaka mafuta, **Yak. (Bib.)** 5:13–15.

Zitengenezeni taa zenu na kuziwasha mkiwa pamoja na mafuta yake, **M&M** 33:17 (Mt. 25:1–13).

Magogu. *Ona pia* Gogu; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo

Katika Biblia, ni nchi na watu walio karibu na Bahari Nyeusi. Mfalme wao, Gogu, atayaongoza majeshi ya Magogu katika pambano kuu la mwisho kabla ya Ujio wa Pili wa Kristo (Eze. 38:2; 39:6). Maandiko yanazungumza juu ya pambano jingine kuu la Gogu na Magogu mwishoni mwa Milenia kati ya majeshi ya Mungu na majeshi ya uovu (Ufu. 20:7–9; M&M 88:111–116).

Magugu

Nyasi au majani yenye sumu ambayo yanafanana kwa sura na ngano. Hayawezi kutofautishwa na ngano hadi yamekuwa na kukomaa (Mt. 13:24–30; M&M 86:1–7).

Mahubiri ya hali ya Heri. *Ona pia* Mahubiri ya Mlimani

Mfululizo wa mafundisho ambayo Yesu aliyatoa katika Mahubiri ya Mlimani ambayo yanaelezea tabia ya kiroho iliyotakaswa (Mt. 5:3–12; Lk. 6:20–23). Sifa za Heri zimepangwa katika namna ambayo kila maelezo yamejengwa juu ya yale yaliyoitangulia. Kumbukumbu iliyokamilifu na sahihi juu ya Sifa za Heri inapatikana katika 3 Nefi 12.

Mahubiri ya Mlimani. *Ona pia* Mahubiri ya hali ya Heri; Yesu Kristo

Mafundisho yaliyotolewa na Bwana Yesu Kristo kwa wanafunzi Wake ambao walikuwa wanakaribia kutumwa katika misheni (Mt. 5–7; Lk. 6:20–49). Bwana alitoa mahubiri haya muda mfupi baada ya kuitwa kwa Wale Kumi na Wawili.

Mahubiri haya yanafafanuliwa na Tafsiri ya Joseph Smith ya Biblia na kwa mahubiri ya aina hiyo hiyo yaliyoandikwa katika 3 Nefi 12–14, ambayo yanaonyesha kwamba sehemu muhimu ya mahubiri hayo yamepotezwa kutoka katika kumbu kumbu iliyoko katika Mathayo.

Maisha kabla ya kuzaliwa. *Ona pia* Baraza Mbinguni; Mwanadamu, Wanadamu; Mwanzo; Vita Mbinguni

Maisha kabla ya maisha ya duniani. Wanaume na wanawake wote waliishi na Mungu kama watoto Wake wa kiroho kabla ya kuja duniani kuwa viumbe wenye mwili wenye kufa. Hii wakati mwingine huitwa hali ya kwanza (Ibr. 3:26).

Mungu alipoweka misingi ya dunia, wana wote wa Mungu walipiga kelele kwa shangwe, **Ayu.** 38:4–7. Roho itarudi kwa Mungu aliyeitoa, **Mh.** 12:7. Kabla sijakuumba tumboni nalikujua, **Yer.** 1:4–5.

Sisi sote tu wazao wake, **Mdo.** 17:28. Mungu alituchagua kabla ya kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, **Efe.** 1:3–4. Tujitie chini ya Baba wa Roho zetu, **Ebr.** 12:9. Malaika ambao hawakutunza hali yao ya kwanza, amewaweka katika minyororo isiyo na mwisho, **Yuda** 1:6 (Ibr. 3:26). Ibilisi na malaika zake walitupwa nje, **Ufu.** 12:9.

Waliitwa na kuandaliwa tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, **Alma** 13:3.

Kristo aliliangalia eneo pana la milele na majeshi ya mbinguni kabla ya ulimwengu kufanyika, **M&M** 38:1. Mwanadamu pia alikuwa pamoja na Mungu mwanzoni, **M&M** 93:29 (Hel. 14:17; M&M 49:17). Roho maarufu walichaguliwa hapo mwanzoni ili kuwa watawala katika Kanisa, **M&M** 138:53–55. Wengi walipokea masomo yao ya mwanzo katika ulimwengu wa roho, **M&M** 138:56.

Vitu vyote viliumbwa kiroho kabla ya kuwekwa juu ya dunia, **Musa** 3:5. Niliumba ulimwengu, na wanadamu kabla hawajawa katika mwili, **Musa** 6:51. Ibrahimu aliwaona viumbe-akili-asilia waliokuweko kabla ya ulimwengu kuwako, **Ibr.** 3:21–24.

Maisha ya Kutokufa. *Ona* Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa

Majaaliwa. *Ona* Uteuzi kabla

Majaribu. *Ona* Jaribu, Majaribu

Maji ya Uzima. *Ona pia* Yesu Kristo

Mfano wa Bwana Yesu Kristo na mafundisho Yake. Kama vile maji yalivyo muhimu kwa kutupa uzima wa kimwili, Mwokozi na mafundisho Yake (maji ya uzima) ni muhimu kwa uzima wa milele.

Kwa shangwe mtachota maji kutoka katika visima vya wokovu, **Isa.** 12:3. Wameniacha mimi, niliye chemchemi ya maji ya uzima, **Yer.** 2:13.

Kama mtu yeyote akiona kiu, na aje kwangu, na anywe, **Yn.** 4:6–15. Kama mtu yeyote akiona kiu, na aje kwangu, na anywe, **Yn.** 7:37.

Fimbo ya chuma iliongoza kwenye chemchemi ya maji ya uzima, **1 Ne.** 11:25.

Kunyweni maji ya uzima bure, **M&M** 10:66. Amri zangu zitakuwa kisima cha maji ya uzima, **M&M** 63:23.

Majivuno, Siofaa. *Ona pia* Kiburi; Malimwengu

Uwongo au udanganyifu; kiburi. Siofaa na majivuno yanaweza pia kumaanisha bure au yasiyo na thamani.

Mtu asiyeiinua nafsi kwa kiburi atasimama katika mahali patakatifu pa Bwana, **Zab.** 24:3–4.

Wakati mnaposali, msitumie kurudia maneno yasiyofaa, **Mt.** 6:7.

Lile jengo kubwa na lililo pana ni mawazo yasiyofaa na kiburi, **1 Ne.** 12:18. Je, mtaendelea kuiweka mioyo yenu juu ya mambo ya ulimwengu yasiyofaa, **Alma** 5:53. Msiyafuate mambo yasiyofaa ya ulimwengu huu, kwa maana hamwezi kwenda nayo, **Alma** 39:14.

Kiburi na kutoamini vimeleta Kanisa chini ya hukumu, **M&M** 84:54–55. Wakati tunapojaribu kuridhisha tamaa zetu zisizofaa, mbingu hujitoa, **M&M** 121:37.

Makabila Kumi. *Ona* Israeli

Makabila Kumi na Mawili ya Israeli. *Ona* Israeli—Makabila kumi na mawili ya Israeli

Makabila Yaliyopotea. *Ona* Israeli—Makabila Kumi ya Israeli yaliyopotea

Makala ya Imani. *Ona pia* Lulu ya Thamani Kuu; Smith, Joseph, Mdogo

Vipengele vya msingi kumi na vitatu vya imani ambavyo waumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho wanaviamini.

Joseph Smith kwanza aliviandika katika barua aliyomwandikia John Wentworth, mhariri wa gazeti la *Chicago Democrat,* katika kujibu maombi yake ya kutaka kujua nini wanachama wa Kanisa wanaamini. Barua hiyo ilikuja kujulikana kama Barua ya Wentworth na kwanza ilichapishwa katika gazeti la *Times and Seasons* mnamo Machi 1842. Mnamo 10 Oktoba 1880, Makala ya Imani yalikubalika rasmi kama maandiko matakatifu kwa kura ya waumini wa Kanisa na yakajumuishwa kama sehemu ya Lulu ya Thamani Kuu.

Makerubi

Maumbo yanayowakilisha viumbe wa mbinguni, umbile lenyewe halisi likiwa halijulikani. Makerubi waliitwa ili kulinda maeneo matakatifu.

Bwana akaweka makerubi kuilinda njia ya mti wa uzima, **Mwa.** 3:24 (Alma 12:21–29; 42:2–3; Musa 4:31). Sanamu ziwakilishazo makerubi ziliwekwa juu ya kiti cha rehema, **Ku.** 25:18, 22 (1 Fal. 6:23–28; Ebr. 9:5). Makerubi wametajwa katika maono ya Ezekieli, **Eze.** 10; 11:22.

Makundi. *Ona* Makundi maovu ya siri

Makundi maovu ya siri. *Ona pia* Kaini; Wanyang'anyi wa Gadiantoni

Kikundi cha watu walioungana pamoja kwa viapo ili kutekeleza malengo maovu ya kikundi hicho.

Baba wa uongo huwachochea watoto wa watu kuwa katika makundi maovu ya siri, **2 Ne.** 9:9. Sina budi kuangamiza matendo ya siri ya gizani, **2 Ne.** 10:15. Hukumu ya Mungu ilikuja juu ya watendaji hawa wa makundi maovu ya siri, **Alma** 37:30. Gadiantoni alidhihirisha angamizo lote la watu wa Nefi, **Hel.** 2:4–13. Shetani aliweka katika mioyo ya watu waunde viapo na maagano ya siri, **Hel.** 6:21–31. Bwana hafanyi kazi katika makundi maovu ya siri, **Eth.** 8:19. Mataifa yanayokubali makundi maovu ya siri yataangamizwa, **Eth.** 8:22–23. Waliyakataa maneno yote ya manabii, kwa sababu ya umoja wao wa siri, **Eth.** 11:22.

Tangu siku za Kaini, palikuwepo makundi ya siri, **Musa** 5:51.

Malaika

Kuna aina mbili za viumbe katika mbingu vinavyoitwa malaika: wale ambao ni roho na wale wenye miili ya nyama na mifupa. Malaika walio roho tu bado hawajapata mwili wa nyama na mifupa, au ni roho wale ambao mwanzo walikuwa na miili ya kuharibika na sasa wanasubiri ufufuko. Malaika walio na miili ya nyama na mifupa ni kwamba ama wamekwisha kufufuka kutoka kwa wafu au wamehamishwa.

Kuna kumbukumbu nyingi katika maandiko ya kazi za malaika. Wakati mwingine malaika huongea kwa sauti ya radi kama wanatoa ujumbe wa

Mungu (Mos. 27:11–16). Watu walio duniani wenye haki waweza pia kuitwa malaika (TJS, Mwa. 19:15 [Kiambatisho]). Baadhi ya malaika hutumikia kuzunguka kiti cha enzi cha Mungu mbinguni (Alma 36:22).

Maandiko pia huzungumzia juu ya malaika wa ibilisi. Hawa ni roho wale waliomfuata Lusiferi nao wakafukuzwa kutoka katika uwepo wa Mungu katika maisha kabla ya kuzaliwa na wakatupwa chini duniani (Ufu. 12:1–9; 2 Ne. 9:9, 16; M&M 29:36–37).

Yakobo aliona malaika wa Mungu wakipanda na kushuka, **Mwa.** 28:12. Malaika wa Mungu wakamlaki Yakobo, **Mwa.** 32:1–2. Gideoni alimwona malaika wa Bwana uso kwa uso, **Amu.** 6:22. Malaika alinyoosha mkono wake juu ya Yerusalemu ili kuiangamiza, **2 Sam.** 24:16. Malaika alimgusa Eliya na akamwambia, Amka na ule, **1 Fal.** 19:5–7. Danieli alimwona malaika Gabrieli katika ono, **Dan.** 8:15–16. Malaika Mikaeli alimsaidia Danieli, **Dan.** 10:13.

Malaika Gabrieli alitumwa kutoka kwa Mungu, **Lk.** 1:19, 26–27. Malaika wa ibilisi watabakizwa katika minyororo hadi hukumu, **Yuda** 1:6 (2 Pet. 2:4).

Watu waliwaona malaika wakishuka kutoka mbinguni, **3 Ne.** 17:24. Moroni aliandika kuhusu huduma za malaika, **Moro.** 7:25–32.

Ukuhani wa Haruni hushikilia funguo za kuhudumiwa na malaika, **M&M** 13. Moroni, Yohana Mbatizaji, Petro, Yakobo, Yohana, Musa, Eliya, na Elia wote walimhudumia Joseph Smith kama malaika, **M&M** 27:5–12. Ninyi hamwezi kustahmili kuhudumiwa na malaika, **M&M** 67:13. Mikaeli, yule malaika mkuu, ni Adamu, **M&M** 107:54. Malaika ni watu waliofufuka, walio na miili ya nyama na mifupa, **M&M** 129. Hakuna malaika wanaohudumia katika dunia hii isipokuwa wale waliokuwa wa dunia hii, **M&M** 130:5. Watu ambao hawatii sheria ya Mungu ya ndoa ya milele si kuoa wala kuolewa; bali huwa malaika wateule mbinguni, **M&M** 132:16–17.

Malaika mkuu. *Ona pia* Adamu; Mikaeli

Mikaeli, au Adamu, ndiye yule malaika mkuu au malaika kiongozi.

Bwana atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, kwa sauti ya malaika mkuu, **1 The.** 4:16. Mikaeli ndiye malaika mkuu, **Yuda** 1:9 (M&M 29:26; 88:112; 128:20–21).

Malaika Wahudumu. *Ona* Malaika

Malaki

Nabii wa Agano la Kale ambaye aliandika na kutoa unabii karibu ya mwaka 430 K.K.

Kitabu cha Malaki: Kitabu au unabii wa Malaki ni kitabu cha mwisho katika Agano la Kale. Kinaelekea kufuatilia mada kuu nne: (1) dhambi za Israeli—Malaki 1:6–2:17; 3:8–9; (2) hukumu zitakazokuja juu ya Israeli kwa sababu ya kutotii kwao—Malaki 1:14; 2:2–3, 12; 3:5; (3) ahadi kwa ajili ya kutii—Malaki 3:10–12, 16–18; 4:2–3; na (4) unabii uhusuo Israeli—Malaki 3:1–5; 4:1, 5–6 (M&M 2; 128:17; JS—H 1:37–39).

Katika unabii wake, Malaki aliandika juu ya Yohana Mbatizaji (Mal. 3:1; Mt. 11:10), sheria ya zaka (Mal. 3:7–12), Ujio wa Pili wa Bwana (Mal. 4:5), na kurejea kwa Eliya (Mal. 4:5–6; M&M 2; 128:17; JS—H 1:37–39). Mwokozi alinukuu milango yote ya Malaki mlango wa 3 na 4 kwa Wanefi (3 Ne. 24–25).

Mali. *Ona pia* Fedha

Neno la Kiaramaya maana yake "utajiri" (Mt. 6:24; Lk. 16:9; M&M 82:22).

Malimbuko

Mavuno ya kwanza yaliyokusanywa katika msimu. Katika nyakati za Agano la Kale, yalitolewa kwa Bwana (Law. 23:9–20). Yesu Kristo alikua limbuko kwa Mungu katika hilo, kwamba Yeye alikuwa wa kwanza kufufuliwa (1 Kor. 15:20, 23; 2 Ne. 2:9). Wale ambao wanaipokea injili na kustahimili hadi mwisho katika uaminifu ni njia ya ishara

ya malimbuko, kwani wao ni mali ya Mungu.

Wale wamfuatao Mwanakondoo kila aendako ndiyo malimbuko kwa Mungu, **Ufu.** 14:4.

Wao watakao shuka kwanza pamoja na Kristo ndiyo malimbuko, **M&M** 88:98.

Malimwengu. *Ona pia* Fedha; Kiburi; Majivuno, Siofaa; Mali; Ukwasi

Tamaa isiyo haki na jitihada za kujipatia mali za kimwili na vitu wakati ukisahau mambo ya kiroho.

Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote na kupoteza nafsi yake mwenyewe, **Mt.** 16:26.

Waliweka mioyo yao juu ya mambo yasiyofaa ya ulimwengu, **Alma** 4:8 (Alma 31:27).

Yaweke kando mambo ya ulimwengu huu, **M&M** 25:10. Mioyo ya wanadamu imewekwa sana juu ya mambo ya ulimwengu huu, **M&M** 121:35.

Mama. *Ona pia* Familia; Hawa; Wazazi

Jina takatifu kwa mwanamke mwenye kuzaa au kupanga watoto. Akinamama husaidia katika mpango wa Mungu kwa kutoa miili yenye kufa kwa ajili ya watoto wa kiroho wa Mungu.

Adamu alimwita mke wake jina la Hawa, kwa sababu yeye alikuwa mama wa wote walio hai, **Mwa.** 3:20 (Musa 4:26). Waheshimu baba na mama yako, **Ku.** 20:12 (Efe. 6:1–3; Mos. 13:20). Usiache sheria ya mama yako, **Mit.** 1:8. Mpumbavu humdharau mama yake, **Mit.** 15:20 (Mit. 10:1). Usimdharau mama yako akiwa mzee, **Mit.** 23:22. Watoto wake na mumewe huinuka na kumwita heri na mumewe naye humsifia, **Mit.** 31:28.

Mama wa Yesu alisimama pembeni ya msalaba, **Yn.** 19:25–27.

Askari elfu mbili wa Walamani walifundishwa na mama zao, **Alma** 56:47 (Alma 57:21).

Mama yetu mtukufu Hawa alikuwa ni miongoni mwa wale maarufu na wakuu ambao Bwana aliwafundisha katika ulimwengu wa roho, **M&M** 138:38–39.

Mambo ya Nyakati

Vitabu viwili katika Agano la Kale. Vinatoa historia fupi ya matukio kutoka Uumbaji hadi tangazo la Koreshi lililowaruhusu Wayahudi kurudi Yerusalemu.

Kitabu cha Kwanza cha Mambo ya Nyakati: Mlango wa 1–9 inaorodhesha nasaba kutoka Adamu mpaka Sauli. Mlango wa 10 unaelezea kifo cha Sauli. Mlango wa 11–12 inasimulia matukio yanayohusiana na utawala wa Daudi. Mlango wa 23–27 inaelezea kwamba Suleimani alifanywa kuwa mfalme na Walawi wakapangiwa kazi. Mlango wa 28 unaelezea kwamba Daudi alimwamuru Suleimani kujenga hekalu. Mlango wa 29 unandika kuhusu kifo cha Daudi.

Kitabu cha Pili cha Mambo ya Nyakati: Mlango wa 1–9 ni matukio yanayohusiana na utawala wa Suleimani. Mlango wa 10–12 inaelezea juu ya utawala wa Rehoboamu mwana wa Suleimani, wakati ambao muungano wa ufalme wa Israeli uligawanyika katika falme za kaskazini na kusini. Mlango wa 13–36 inafafanua tawala za falme mbali mbali hadi kukamatwa kwa ufalme wa Yuda na Nebukadneza. Kitabu hiki kinaishia na tangazo la Koreshi kwamba wana wa Israeli walio utumwani wanaweza kurudi Yerusalemu.

Mamlaka. *Ona pia* Funguo za Ukuhani; Ita, Itwa na Mungu, Wito; Kutawaza, Kutawazwa; Ukuhani; Uwezo

Ruhusa iliyotolewa kwa wanaume duniani walioitwa au kutawazwa ili kutenda kwa ajili ya, na kwa niaba ya Mungu Baba au Yesu Kristo katika kutenda kazi ya Mungu.

Mimi nimekutuma, **Ku.** 3:12–15. Utanena hayo yote nikuagizayo, **Ku.** 7:2.

Akawapa wanafunzi kumi na wawili

uwezo, **Mt.** 10:1. Si ninyi mlionichagua mimi, bali mimi nimewachagua ninyi, na kuwatawaza, **Yn.** 15:16.

Nefi na Lehi walihubiri kwa mamlaka makubwa, **Hel.** 5:18. Nefi, mwana wa Helamani, alikuwa mtu wa Mungu, mwenye uwezo mkubwa na mamlaka kutoka kwa Mungu, **Hel.** 11:18 (3 Ne. 7:17). Yesu alitoa uwezo na mamlaka kwa Wanefi kumi na wawili, **3 Ne.** 12:1–2.

Joseph Smith aliitwa na kutawazwa na Mungu, **M&M** 20:2. Hakuna atakaye hubiri injili yangu au kulijenga Kanisa langu isipokuwa ametawazwa nayo ijulikane kwa kanisa ya kuwa anayo mamlaka, **M&M** 42:11. Wazee wahubiri injili, wakitenda katika mamlaka, **M&M** 68:8. Ukuhani wa Melkizedeki unayo mamlaka ya kuhudumu katika mambo ya kiroho, **M&M** 107:8, 18–19. Lile lifanywalo kwa mamlaka ya kiungu huwa sheria, **M&M** 128:9.

Yeyote anaye hubiri au kuhudumu kwa ajili ya Mungu lazima aitwe na Mungu na wale waliomo katika mamlaka, **M ya I** 1:5.

Mana. *Ona pia* Kutoka; Mkate wa Uzima

Vipande vidogo, vya mviringo vya aina ya chakula chenye ladha ya asali (Ku. 16:14–31) au mafuta mapya (Hes. 11:7–8). Bwana alikitoa kwa ajili ya kuwalisha mwana wa Israeli wakati wa miaka yao arobaini nyikani (Ku. 16:4–5, 14–30, 35; Yos. 5:12; 1 Ne. 17:28).

Wana wa Israeli walikiita mana (au *man-hu* katika Kiebrania)—ambayo maana yake ni "Nini hiki?"—kwa sababu hawakujua ni kitu gani (Ku. 16:15). Pia kiliitwa "chakula cha malaika" na "mkate kutoka mbinguni" (Zab. 78:24–25; Yn. 6:31). Kilikuwa ni mfano wa Kristo, ambaye angekuwa Mkate wa Uzima (Yn. 6:31–35).

Manase. *Ona pia* Efraimu; Israeli; Yusufu, Mwana wa Yakobo

Katika Agano la Kale, ni mwana mkubwa wa Asinati na Yusufu aliyeuzwa Misri (Mwa. 41:50–51). Yeye na kaka yake Efraimu walikuwa ni wajukuu wa Yakobo (Israeli) lakini walichukuliwa na kubarikiwa naye kama vile walikuwa wanawe mwenyewe (Mwa. 48:1–20).

Kabila la Manase: Wazao wa Manase walihesabiwa miongoni mwa makabila ya Israeli (Hes. 1:34–35; Yos. 13:29–31). Baraka za Musa kwa kabila la Yusufu, ambazo zilitolewa pia kwa Efraimu na Manase, zimeandikwa katika Kumbukumbu la Torati 33:13–17. Nchi waliyopangiwa ilikuwa sehemu kidogo upande wa magharibi ya Yordani na karibu na nchi ya Efraimu. Pia walikuwa na makoloni mashariki ya Yordani katika nchi yenye rutuba ya Bashani na Gileadi. Katika siku za mwisho, kabila la Manase litasaidia kabila la Efraimu katika kuwakusanya Israeli waliotawanyika (Kum. 33:13–17). Nabii Lehi wa Kitabu cha Mormoni alikuwa ni wa uzao wa Manase (Alma 10:3).

Manifesto. *Ona pia* Ndoa, Oa, Olewa—Ndoa ya wake wengi; Woodruff, Wilford

Tamko rasmi lililotolewa na Rais Wilford Woodruff katika mwaka 1890 akisema kwa uwazi kabisa kwamba Kanisa na waumini wake wamejiweka chini ya sheria ya nchi na hawataingia tena katika ndoa za wake wengi (TR 1). Rais Woodruff alitoa Manifesto hii kufuatia ono na ufunuo kutoka kwa Mungu.

Manung'uniko. *Ona pia* Uasi

Kunung'unika na kulalamika dhidi ya makusudi, mipango au watumishi wa Mungu.

Watu wakamnung'unikia Musa, **Ku.** 15:23–16:3.

Wayahudi wakamnung'unikia Yesu, **Yn.** 6:41.

Lamani na Lemueli walinung'unika katika mambo mengi, **1 Ne.** 2:11–12 (1 Ne. 3:31; 17:17).

Usinung'unike kwa sababu ya vitu ambavyo hujaviona, **M&M** 25:4.

Maombolezo, Kitabu cha

Kitabu katika Agano la Kale, kilichoandikwa na Yeremia. Ni mkusanyiko wa mashairi au nyimbo za huzuni kwa sababu ya anguko la Yerusalemu na taifa la Israeli. Kitabu hiki kiliandikwa baada ya anguko la mji huo kiasi cha mwaka 586 K.K.

Maongozi ya Mungu, Shawishi. *Ona pia* Roho Mtakatifu; Ufunuo

Mwongozo mtakatifu utolewao na Mungu kwa mwanadamu. Maongozi mara kwa mara huja mawazoni au moyoni mwa mtu katika njia tofauti ya kiroho.

Baada ya moto ikaja sauti ndogo tulivu, **1 Fal.** 19:12.

Roho Mtakatifu atawafundisha mambo yote na kuwakumbusha mambo yote, **Yn.** 14:26. Roho wa kweli atawaongoza katika kweli yote, **Yn.** 16:13.

Niliongozwa na Roho, bila ya kufahamu mapema mambo ambayo nitayafanya, **1 Ne.** 4:6. Sauti ya Bwana ikanijia mawazoni mwangu, **Eno.** 1:10. Kila kitu chenye kukaribisha na kushawishi kutenda mema kimeongozwa na Mungu, **Moro.** 7:13–16.

Sikusema amani akilini mwako, **M&M** 6:23. Nitakuambia mawazoni mwako na moyoni mwako, **M&M** 8:2. Roho wangu atayaangaza mawazo yako, ambayo yataijaza nafsi yako kwa shangwe, **M&M** 11:13. Utapewa katika saa ile kile utakachozungumza au kuandika, **M&M** 24:6 (M&M 84:85). Sauti ndogo tulivu hunong'ona na kupenya vitu vyote, **M&M** 85:6.

Mapokeo

Imani na desturi ambazo hurithishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine (2 The. 2:15). Katika maandiko, Bwana daima huwaonya walio waaminifu kuepuka mapokeo maovu ya wanadamu (Law. 18:30; Mk. 7:6–8; Mos. 1:5; M&M 93:39–40).

Maria, Mama wa Marko. *Ona pia* Marko

Katika Agano Jipya, ni mama wa Yohana Marko, aliyeandika Injili ya Marko (Mdo. 12:12).

Maria, Mama wa Yesu. *Ona pia* Yesu Kristo; Yusufu, Mume wa Maria

Katika Agano Jipya, ni bikira aliyechaguliwa na Mungu Baba kuwa mama wa Mwanawe katika mwili. Baada ya kuzaliwa kwa Yesu, Maria alipata watoto wengine (Mk. 6:3).

Aliposwa na Yusufu, **Mt.** 1:18 (Lk. 1:27). Yusufu aliambiwa asimpe talaka Maria au asimfungue posa ile, **Mt.** 1:18–25. Mamajusi walimtembelea Maria, **Mt.** 2:11. Maria na Yusufu walikimbia pamoja na mtoto Yesu hadi Misri, **Mt.** 2:13–14. Baada ya kifo cha Herode, familia ilirejea Nazarethi, **Mt.** 2:19–23. Malaika Gabrieli alimtembelea, **Lk.** 1:26–38. Alimtembelea Elizabethi, binamu yake, **Lk.** 1:36, 40–45. Maria alitoa zaburi ya sifa kwa Bwana, **Lk.** 1:46–55. Maria alikwenda Bethlehemu pamoja na Yusufu, **Lk.** 2:4–5. Maria akamzaa Yesu na akamlaza horini, **Lk.** 2:7. Wachunga kondoo wakaenda Bethlehemu kumwona mtoto Yesu, **Lk.** 2:16–20. Maria na Yusufu walimpeleka Yesu hekaluni huko Yerusalemu, **Lk.** 2:21–38. Maria na Yusufu walimpeleka Yesu katika Pasaka, **Lk.** 2:41–52. Maria alikuwepo katika harusi huko Kana, **Yn.** 2:2–5. Mwokozi, alipokuwa juu ya msalaba, alimwomba Yohana amtunze mama yake, **Yn.** 19:25–27. Maria alikuwa pamoja na Mitume baada ya Yesu kutwaliwa mbinguni, **Mdo.** 1:14.

Maria alikuwa bikira, mrembo sana na mwenye haki zaidi ya mabikira wengine wote, **1 Ne.** 11:13–20. Mama wa Kristo angeitwa Maria, **Mos.** 3:8. Maria angekuwa bikira, mzuri na chombo kiteule, **Alma** 7:10.

Maria Magdalena

Mwanamke katika Agano Jipya ambaye alijitoa kwa moyo kuwa mwanafunzi wa Yesu Kristo. Magdalena linatokana na Magdala ni mahali ambapo huyu Maria alitoka. Iko

upande wa magharibi wa pwani ya Bahari ya Galilaya.

Alikuwepo karibu na msalaba, **Mt.** 27:56 (Mk. 15:40; Yn. 19:25). Alikuwepo katika mazishi ya Kristo, **Mt.** 27:61 (Mk. 15:47). Alikuwepo kaburini asubuhi ya ufufuko, **Mt.** 28:1 (Mk. 16:1; Lk. 24:10; Yn. 20:1, 11). Yesu alijionyesha kwake kwanza baada ya ufufuko wake, **Mk.** 16:9 (Yn. 20:14–18). Pepo wabaya saba walimtoka, **Lk.** 8:2.

Maria wa Bethania. *Ona pia* Lazaro; Martha

Katika Agano Jipya, ni dada wa Lazaro na Martha.

Maria aliketi na kusikiliza miguuni pa Yesu, **Lk.** 10:39, 42. Maria na dada yake Martha walituma ujumbe kwa Yesu, **Yn.** 11:1–45. Akampaka Yesu miguu kwa mafuta, **Yn.** 12:3–8.

Marko. *Ona pia* Injili, Vitabu vya Biblia

Katika Agano Jipya, Yohana Marko alikuwa mwanawe Maria, aliyeishi Yerusalemu (Mdo. 12:12); yawezekana pia akawa binamu (au mpwa) wa Barnaba (Kol. 4:10). Alikwenda pamoja na Paulo na Barnaba kutoka Yerusalemu katika safari yao ya kwanza ya kimisionari na akawaacha wao huko Perga (Mdo. 12:25; 13:5, 13). Baadaye aliongozana na Barnaba kwenda Kipro (Mdo. 15:37–39). Alikuwa pamoja na Paulo huko Rumi (Kol. 4:10; Flm. 1:24), na alikuwa pamoja na Petro huko Babiloni (huenda huko Rumi) (1 Pet. 5:13). Mwishoni, alikuwa pamoja na Timotheo huko Efeso (2 Tim. 4:11).

Injili ya Marko: Kitabu cha pili katika Agano Jipya. Injili ya Marko yawezekana kuwa iliandikwa kwa maelekezo ya Petro. Lengo lake ni kumwelezea Bwana kama ndiye Mwana wa Mungu aliye hai na akitenda miongoni mwa watu. Marko anaelezea, kwa nguvu na unyenyekevu, picha ambayo Yesu aliifanya kwa watazamaji. Mapokeo yanaelezea ya kuwa baada ya kifo cha Petro, Marko alitembelea Misri, akaanzisha Kanisa katika Iskanderia, na akafa kifo cha kishahidi.

Kwa orodha ya matukio katika maisha ya Mwokozi kama yaliyoelezwa na Marko, ona Upatanifu wa Injili katika kiambatisho.

Marsh, Thomas B.

Rais wa Kwanza wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili baada ya Urejesho wa Kanisa katika mwaka 1830. Alishikilia funguo za ufalme kwa niaba ya wale Kumi na Wawili (M&M 112:16) na, katika mwaka 1838, aliamriwa kwa ufunuo kuchapisha neno la Bwana (M&M 118:2). Sehemu ya 31 ya Mafundisho na Maagano inaelekezwa kwake yeye. Marsh alitengwa na Kanisa katika mwaka 1839 lakini alibatizwa upya tena katika mwezi wa Julai 1857.

Martha. *Ona pia* Lazaro; Maria wa Bethania

Dada wa Lazaro na Maria katika Agano Jipya (Lk. 10:38–42; Yn. 11:1–46; 12:2).

Masadukayo. *Ona pia* Wayahudi

Kundi dogo lakini kundi lenye nguvu sana kisiasa miongoni mwa Wayahudi. Wao labda walikuwa mashuhuri sana kwa ukakamavu wa Imani yao katika kutii kwa dhati sharia ya Musa na kwa kukataa uhalisi wa roho na malaika na pia mafundisho ya Ufufuko na uzima wa milele (Marko 12:18–27; Matendo ya Mitume 4:1–3; 23:7–8).

Mashahidi wa Kitabu cha Mormoni. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni; Shahidi, Ushahidi

Bwana aliwaamuru wengine licha ya Joseph Smith Nabii kutoa ushuhuda wa utakatifu wa Kitabu cha Mormoni (M&M 17; 128:20). Ona shuhuda za mashahidi hawa katika "Utangulizi" mwanzoni mwa Kitabu cha Mormoni.

Kwa maneno ya watatu nitalithibitisha neno langu, **2 Ne.** 11:3. Mashahidi wa kutoa ushuhuda wa neno lake kwa

watoto wa watu, **2 Ne.** 27:12–13. Katika vinywa vya mashahidi watatu mambo haya yatathibitika, **Eth.** 5:4.

Kwa imani Mashahidi Watatu watayaona mabamba, **M&M** 17.

Masiya. *Ona pia* Mpakwa mafuta; Yesu Kristo

Aina ya neno la Kiaramai na Kiebrania lenye maana ya "mpakwa mafuta." Katika Agano Jipya Yesu anaitwa Kristo, ambalo ni la Kiyunani lililo sawa na *Masiya.* Maana yake Nabii mpakwa mafuta, Kuhani, Mfalme na Mkombozi ambaye kuja kwake Wayahudi walikutarajia kwa hamu kubwa.

Wayahudi wengi walitazamia tu mkombozi kutoka mamlaka ya Kirumi na kwa ustawi mkubwa zaidi wa kitaifa; hivyo basi, wakati Masiya alipokuja, viongozi na watu wengine wengi Walimkataa. Wale waliokuwa wanyenyekevu na waaminifu tu, waliweza kuona ndani ya Yesu wa Nazarethi Kristo wa kweli (Isa. 53; Mt. 16:16; Yn. 4:25–26).

Masiya atakuwa na Roho, atahubiri injili, na kutangaza uhuru, **Isa.** 61:1–3 (Lk. 4:18–21).

Tumemwona Masiya, ambaye, maana yake Kristo, **Yn.** 1:41 (Yn. 4:25–26).

Mungu alimwinua Masiya miongoni mwa Wayahudi, au, katika maneno mengine, Mwokozi, **1 Ne.** 10:4. Mwana wa Mungu alikuwa Masiya ambaye angekuja, **1 Ne.** 10:17. Ukombozi huja ndani ya na kupitia Masiya mtakatifu, **2 Ne.** 2:6. Masiya atakuja katika utimilifu wa nyakati, **2 Ne.** 2:26. Masiya atafufuka kutoka kwa wafu, **2 Ne.** 25:14.

Katika jina la Masiya ninawatunukia Ukuhani huu wa Haruni, **M&M** 13.

Bwana akasema, Mimi ndimi Masiya, Mfalme wa Sayuni, **Musa** 7:53.

Maskini. *Ona pia* Funga, Kufunga; Mnyenyekevu, Unyenyekevu; Sadaka, Utoaji sadaka; Ustawi

Katika maandiko, maskini yaweza kutumika kwa (1) watu ambao hawana vitu vya mahitaji muhimu, kama vile chakula, mavazi, na malazi, au (2) watu walio wanyenyekevu na wasio na kiburi.

Maskini katika mahitaji ya muhimu: Usimfumbie mkono wako nduguyo maskini, **Kum.** 15:7. Mwovu katika kiburi chake huwatesa walio maskini, **Zab.** 10:2. Mwenye kuwagawia maskini hatapungukiwa, **Mit.** 28:27. Walete maskini nyumbani kwako, **Isa.** 58:6–7.

Ukitaka kuwa mkamilifu, wape maskini, **Mt.** 19:21 (Mk. 10:21; Lk. 18:22). Je, Mungu hakuwachagua maskini wa ulimwengu huu, **Yak. (Bib.)** 2:5.

Kwa sababu wao ni matajiri wanawadharau maskini, **2 Ne.** 9:30. Kupata msamaha wa dhambi zenu, wapeni maskini mali zenu, **Mos.** 4:26. Waligawa mali zao kwa maskini, **Alma** 1:27. Mkiwanyima wenye shida, sala zenu si kitu, **Alma** 34:28. Wanefi walikuwa na vitu vyote sawa baina yao; hapakuwa na maskini na tajiri, **4 Ne.** 1:3.

Mtawakumbuka maskini, **M&M** 42:30 (M&M 52:40). Ole kwa maskini ambao mioyo yao haijavunjika, **M&M** 56:17–18. Maskini watakuja katika harusi ya Mwanakondoo, **M&M** 58:6–11. Askofu atawatafuta maskini, **M&M** 84:112. Sheria ya injili hutawala misaada kwa maskini, **M&M** 104:17–18.

Hapakuwa na maskini miongoni mwao, **Musa** 7:18.

Maskini katika roho: Heri zaidi kwao wale wanaojinyenyekeza wenyewe pasipo kulazimishwa kwa sababu ya ufukara, **Alma** 32:4–6, 12–16. Heri maskini wa roho wajao kwangu, **3 Ne.** 12:3 (Mt. 5:3).

Injili itahubiriwa kwao walio maskini na wapole, **M&M** 35:15.

Matamanio ya Anasa. *Ona* Kupenda anasa, Matamanio ya anasa

Matendo

Matendo ya mtu, yawe mabaya au mema. Kila mtu atahukumiwa kwa matendo yake mwenyewe.

Bwana atamlipa kila mtu kulingana na matendo yake, **Mit.** 24:12.

Nuru yenu na iangaze mbele za watu, ili wapate kuyaona matendo ya Mungu wenu, **Mt.** 5:16 (3 Ne. 12:16). Mtu yule atendaye mapenzi ya Baba ataingia katika ufalme wa mbinguni, **Mt.** 7:21. Imani pasipo matendo imekufa, **Yak. (Bib.)** 2:14–26.

Lazima wahukumiwe juu ya matendo yao, **1 Ne.** 15:32 (Mos. 3:24). Tunajua ya kuwa kwa neema tunaokolewa, baada ya kufanya yote tuwezayo kufanya, **2 Ne.** 25:23. Wafundisheni kuwa kamwe wasichoke kufanya matendo mema, **Alma** 37:34. Ni lazima kwamba wanadamu wahukumiwe kulingana na matendo yao, **Alma** 41:3. Kwa matendo yao mtawajua, **Moro.** 7:5 (M&M 18:38).

Mimi, Bwana, nitawahukumu watu wote kulingana na matendo yao, **M&M** 137:9.

Matendo ya Mitume. *Ona pia* Luka

Kitabu hiki ni cha pili kati ya sehemu mbili za kazi zilizoandikwa na Luka kwa Theofili. Sehemu ya kwanza hujulikana kama Injili kulingana na Luka. Mlango wa 1–12 imeandikwa baadhi ya kazi muhimu za kimisionari za Mitume Kumi na Wawili chini ya maelekezo ya Petro mara baada ya kifo na ufufuko wa Mwokozi. Mlango wa 13–28 inaelezea baadhi ya safari na kazi za kimisionari za Mtume Paulo.

Mateso, Tesa. *Ona pia* Shida

Kusababisha uchungu au maumivu kwa wengine kwa sababu ya imani yao au hadhi yao kijamii; kusumbua au kukandamiza.

Heri wenye kuteswa kwa ajili ya haki, **Mt.** 5:10 (3 Ne. 12:10). Waombeeni wanaowatumia vibaya na wenye kuwatesa, **Mt.** 5:44 (3 Ne. 12:44).

Kwa sababu wao ni matajiri, huwatesa walio wapole, **2 Ne.** 9:30 (2 Ne. 28:12–13). Waaminifu wamtazamiao Kristo licha ya mateso yote hawataangamia, **2 Ne.** 26:8.

Mambo haya yote yatakupa wewe uzoefu, **M&M** 122:7.

Mathayo. *Ona pia* Injili, Vitabu vya Biblia

Mtume wa Yesu Kristo na mwandishi wa kitabu cha kwanza katika Agano Jipya. Mathayo ni Myahudi ambaye alikuwa mtoza ushuru kwa ajili ya Warumi huko Kapernaumu, yawezekana alikuwa katika huduma ya Herode Antipasi. Alijulikana kama Lawi kabla ya uongofu wake mwana wa Alfayo (Mk. 2:14). Mara baada ya wito wake wa kuwa mwanafunzi wa Yesu, alitengeneza karamu ambayo Bwana naye alikuwepo (Mt. 9:9–13; Mk. 2:14–17; Lk. 5:27–32). Huenda Mathayo alikuwa na ujuzi mpana wa maandiko ya Agano la Kale na aliweza kuona kwa uwazi utimilifu wa unabii katika maisha ya Bwana. Juu ya maisha ya baadaye ya Mtume huyu yanajulikana kidogo. Pokeo moja linadai kwamba alikufa mauti ya mfiadini.

Injili ya Mathayo: Kitabu cha kwanza katika Agano Jipya. Injili ya Mathayo huenda mwanzoni aliiandika kwa matumizi ya Wayahudi katika Palestina. Inatumia nukuu nyingi kutoka katika Agano la Kale. Lengo kuu la Mathayo lilikuwa kuonyesha kwamba Yesu alikuwa ndiye Masiya ambaye manabii wa Agano la Kale walimzungumzia. Yeye pia alisisitiza kuwa Yesu ni Mfalme na Mwamuzi wa watu.

Kwa orodha ya matukio katika maisha ya Mwokozi kama yalivyoelezwa katika Injili ya Mathayo, ona Upatanifu wa Injili katika kiambatisho.

Mathiya. *Ona pia* Mtume—Uteuzi wa Mitume

Mtu aliyechaguliwa kujaza nafasi ya Yuda Iskarioti kama mshiriki wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili (Mdo. 1:15–26). Alikuwa mwanafunzi katika kipindi chote cha huduma ya Yesu duniani (Mdo. 1:21–22).

Matumaini. *Ona pia* Amini, Imani; Tegemea

Kuwa na uhakikisho, kuwa na imani,

kuamini katika, au imani katika jambo fulani, hususani Mungu na Yesu Kristo.

Ni heri kuamini katika Bwana kuliko kumtumainia mwanadamu, **Zab.** 118:8. Bwana atakuwa tumaini lako, **Mit.** 3:26.

Atapoonekana Kristo, tupate kuwa na tumaini, **1 Yoh.** 2:28.

Wanefi waovu wamepoteza matumaini ya watoto wao, **Yak. (KM)** 2:35.

Ndipo tumaini lako litakapokuwa mbele ya Mungu, **M&M** 121:45.

Mauaji. *Ona pia* Adhabu Kuu; Kaini

Kwa makusudi na pasipo uhali mtu anatwaa uhai wa mtu mwingine. Mauaji ni dhambi iliyolaaniwa tangu nyakati za mwanzo (Mwa. 4:1–12; Musa 5:18–41).

Yeyote atakaye mwaga damu ya mwanadamu, damu yake huyo itamwagwa na mwanadamu, **Mwa.** 9:6 (TJS, Mwa. 9:12–13; Ku. 21:12; Alma 34:12). Usiue, **Ku.** 20:13 (Kum. 5:17; Mt. 5:21–22; Mos. 13:21; M&M 59:6).

Yesu alisema, usiue, **Mt.** 19:18. Wauaji watakuwa na sehemu yao katika mauti ya pili, **Ufu.** 21:8.

Ninyi ni wauaji mioyoni mwenu, **1 Ne.** 17:44. Ole kwa muuaji anayeua kwa kutaka, **2 Ne.** 9:35. Mungu ameamuru kwamba wanadamu wasiue, **2 Ne.** 26:32. Mauaji ni chukizo kwa Bwana, **Alma** 39:5–6.

Yule anayeua hatapata msamaha, **M&M** 42:18. Mtu yeyote atakayeua atolewe na kushughulikiwa kulingana na sheria za nchi, **M&M** 42:79.

Mauti ya Kimwili. *Ona pia* Anguko la Adamu na Hawa; Hali ya Kufa, enye Kufa; Ufufuko; Wokovu

Kutengana kwa mwili na roho. Anguko lilileta hali ya kufa na mauti duniani (2 Ne. 2:22; Musa 6:48). Upatanisho wa Yesu Kristo uliishinda mauti ili kwamba kila mmoja atafufuka (1 Kor. 15:21–23). Ufufuko ni zawadi ya bure kwa watu wote bila kujali kama wametenda mema au maovu katika maisha haya (Alma 11:42–44). Kila mtu huteseka mara moja tu kwa mauti ya kimwili kwa vile mara tufufukapo, miili yetu haiwezi kufa tena (Alma 11:45).

Wenye mwili wote wataangamia, na mwanadamu atageuka tena mavumbini, **Ayu.** 34:15. Enye thamani machoni pa Bwana ni mauti ya Watakatifu wake, **Zab.** 116:15. Mavumbi yatairudia dunia, nayo roho itamrudia Mungu, **Mh.** 12:7.

Mauti ililetwa na mtu, **1 Kor.** 15:21. Mwokozi hushikilia funguo za jehanamu na mauti, **Ufu.** 1:18. Mauti haitakuwepo tena, wala maombolezo, **Ufu.** 21:4.

Mauti yamewapata wanadamu wote, **2 Ne.** 9:6, 11 (Alma 12:24). Kamwe hawakuangalia juu ya mauti kwa hofu, **Alma** 27:28. Alma alielezea hali ya roho kati ya mauti na ufufuko, **Alma** 40:11.

Wale wanaokufa kwangu hawataonja mauti, **M&M** 42:46. Wale ambao hawakuteuliwa kufa wataponywa, **M&M** 42:48. Nitawajaribu ninyi katika mambo yote hata mpaka kifo, **M&M** 98:14.

Mavumbini nawe utarudi, **Musa** 4:25. Adamu alianguka, na kwa anguko lake ikaja mauti, **Musa** 6:48.

Mauti ya Kiroho. *Ona pia* Anguko la Adamu na Hawa; Hukumu; Ibilisi; Jehanamu; Wana wa Upotevu; Wokovu

Kutengwa na Mungu na nguvu Zake; ni kufa kwa mambo yahusuyo haki. Lusiferi na theluthi moja ya majeshi ya mbinguni walikubali mauti ya kiroho wakati walipotupwa kutoka mbinguni (M&M 29:36–37).

Mauti ya kiroho yaliletwa ulimwenguni kwa Anguko la Adamu (Musa 6:48). Wenye mwili wenye kufa na mawazo, maneno, na matendo maovu wamekufa kiroho wakati wangali hai hapa duniani (1 Tim. 5:6). Kwa Upatanisho wa Yesu Kristo na kwa kutii kanuni na ibada za injili, wanaume na wanawake wanaweza kuwa safi kwa kutoka katika dhambi na kushinda mauti ya kiroho.

Mauti ya kiroho pia hutokea kufuatia kifo cha mwili wenye kufa. Viumbe

wafufuka na ibilisi na malaika zake wote watahukumiwa. Wale wote walioasi kwa makusudi dhidi ya nuru na kweli ya injili watateseka mauti ya kiroho. Kifo hiki mara nyingi huitwa kifo cha pili (Alma 12:16; Hel. 14:16–19; M&M 76:36–38).

Watenda mabaya watakiliwa, **Zab.** 37:9.

Kuwa na mawazo ya kimwili ni mauti, **Rum.** 8:6 (2 Ne. 9:39). Tamaa huwatosa wanadamu katika uharibifu na upotevu, **1 Tim.** 6:9. Dhambi huzaa mauti, **Yak. (Bib.)** 1:15. Yeye ashindaye hatapatikana na madhara ya mauti ya pili, **Ufu.** 2:11. Juu ya hao mauti ya pili haina nguvu, **Ufu.** 20:6, 12–14. Waovu watakuwa na sehemu yao katika lile ziwa liwakalo moto na kiberiti: ambayo ndiyo mauti ya pili, **Ufu.** 21:8 (M&M 63:17–18).

Wanadamu wako huru kuchagua uhuru na uzima wa milele au kuchagua utumwa na mauti, **2 Ne.** 2:27 (2 Ne. 10:23; Alma 29:5; Hel. 14:30–31). Mungu ametutayarishia njia yetu ya kuepuka mauti na jehanamu, **2 Ne.** 9:10. Jifungueni wenyewe kutoka uchungu wa jehanamu ili msije mkateseka kwa mauti ya pili, **Yak. (KM)** 3:11. Mwanadamu wa asili ni adui kwa Mungu, **Mos.** 3:19. Bwana na awape toba ili msipate kuteseka mauti ya pili, **Alma** 13:30. Alma alizungukwa na minyororo ya mauti isiyo na mwisho, **Alma** 36:18. Waovu hufa kulingana na mambo yaliyo ya haki, **Alma** 40:26 (Alma 12:16). Anguko lilileta mauti ya kiroho juu ya wanadamu wote, **Alma** 42:9 (Hel. 14:16–18).

Adamu alipoanguka, alikuwa amekufa kiroho, **M&M** 29:40–41, 44.

Mauti ya Pili. *Ona* Mauti ya Kiroho

Mavuno

Maandiko wakati mwingine hutumia neno mavuno kama ishara ili kumaanisha kuwaleta watu katika Kanisa, ambalo ndilo ufalme wa Mungu duniani, au kwa wakati wa hukumu, kama vile Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.

Mavuno yamepita, kiangazi kimekwisha, na sisi hatujaokoka, **Yer.** 8:20 (M&M 56:16).

Mavuno ni mengi, lakini watenda kazi ni wachache, **Mt.** 9:37. Mavuno ni mwisho wa ulimwengu, **Mt.** 13:39. Chochote apandacho mtu, ndicho atakachovuna, **Gal.** 6:7–9 (M&M 6:33).

Shamba ni jeupe tayari kwa mavuno, **M&M** 4:4. Mavuno yamekwisha na roho zenu hazijaokolewa, **M&M** 45:2. Wakati wa mavuno umefika, na neno langu lazima litimilike, **M&M** 101:64.

Mawazo. *Ona pia* Haki ya uamuzi; Tafakari

Dhana, fikra, na taswira katika akili ya mtu. Uwezo wa kufikiri ni kipawa kutoka kwa Mungu, nasi tuko huru kuchagua namna tunavyotumia uwezo wetu wa kufikiri. Namna tunavyofikiri kwa kiwango kikubwa huathiri mitazamo na tabia, na vile vile nafasi yetu baada ya maisha haya. Mawazo yenye uadilifu hutuongoza kwenye wokovu; mawazo mabaya hutuongoza kwenye laana.

Bwana hufahamu fikira zote za mawazo, **1 Nya.** 28:9. Maana afikirivyo moyoni mwake, ndivyo alivyo, **Mit.** 23:7. Mawazo yangu si mawazo yenu, **Isa.** 55:7–9.

Yesu aliyajua mawazo yao, **Mt.** 12:25 (Lk. 5:22; 6:8). Ndani ya mioyo ya watu hutoka mawazo maovu, **Mk.** 7:20–23. Tukiteka nyara kila wazo lipate kumtii Kristo, **2 Kor.** 10:5. Mambo yoyote yaliyo ya kweli, ya haki, safi, au yenye kupendeza, yatafakarini hayo, **Flp.** 4:8.

Kumbuka, kuwa na mawazo ya kimwili ni mauti, na kuwa na mawazo ya kiroho ni uzima wa milele, **2 Ne.** 9:39. Kama msipojichunga wenyewe, na mawazo yenu, lazima mtaangamia, **Mos.** 4:30. Mawazo yetu yatatushtaki, **Alma** 12:14.

Mungu pekee ndiye ajuaye mawazo na makusudi ya moyo wako, **M&M** 6:16 (M&M 33:1). Nitazame mimi katika kila wazo, **M&M** 6:36. Yahifadhini katika akili zenu maneno ya uzima, **M&M** 84:85. Yatupeni mbali mawazo

yenu potovu, **M&M** 88:69. Mawazo ya mioyo ya wanadamu yatafunuliwa, **M&M** 88:109. Wema na uyarembe mawazo yako bila kukoma, **M&M** 121:45.

Mawazo ya kila mwanadamu yalikuwa maovu siku zote, **Musa** 8:22.

Mbatizaji. *Ona* Yohana Mbatizaji

Mbegu ya Haradali

Mbegu za mche wa haradali. Ingawa mbegu ni ndogo sana, lakini urefu wa mmea unaokua kutokana nayo ni mkubwa sana. Yesu alilinganisha ufalme wa mbinguni na mbegu ya haradali (Mt. 13:31).

Mkiwa na imani kiasi cha punje ya haradali, mtaweza kuihamisha milima, **Mt.** 17:20.

Mbinguni. *Ona pia* Peponi; Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni; Utukufu wa Selestia

Neno mbinguni lina maana mbili za msingi katika maandiko. (1) Ni mahali ambapo Mungu huishi na nyumbani kwa baadaye Watakatifu (Mwa. 28:12; Zab. 11:4; Mt. 6:9). (2) Ni anga liizungukalo dunia (Mwa. 1:1, 17; Ku. 24:10). Mbinguni ni wazi kabisa kuwa siyo peponi, ambapo ni mahali pa muda kwa ajili ya roho aminifu za wale wote walioishi na kufa katika dunia hii. Yesu Kristo alitembelea peponi baada ya kifo Chake msalabani, lakini katika siku ya tatu alimjulisha Maria kwamba Yeye bado alikuwa Hajaenda kwa Baba (Lk. 23:39–44; Yn. 20:17; M&M 138:11–37).

Nikiziangalia mbingu zako, kazi za vidole vyako, **Zab.** 8:3. Kwa neno la Bwana mbingu zilifanyika, **Zab.** 33:6. Jinsi gani ulianguka kutoka mbinguni, Ewe Lusiferi, **Isa.** 14:12 (2 Ne. 24:12). Mbingu zitakunjwa pamoja kama karatasi, **Isa.** 34:4. Mimi naumba mbingu mpya na dunia mpya, **Isa.** 65:17. Mungu atayafungua madirisha ya mbinguni, **Mal.** 3:10.

Baba yetu aliye mbinguni, jina lako litukuzwe, **Mt.** 6:9 (3 Ne. 13:9). Paulo alinyakuliwa katika mbingu ya tatu, **2 Kor.** 12:2. Kukawa kimya mbinguni, **Ufu.** 8:1 (M&M 88:95–98).

Kama watavumilia kwa uaminifu hadi mwisho watapokelewa mbinguni, **Mos.** 2:41. Mpate kuwa watoto wa Baba yenu aliye mbinguni, **3 Ne.** 12:45.

Nitakuja katika mawingu ya mbinguni, **M&M** 45:16. Eliya alitwaliwa mbinguni pasipo kuonja mauti, **M&M** 110:13. Haki za ukuhani zimeunganishwa pamoja na nguvu za mbinguni, **M&M** 121:36. Kuna aina mbili za viumbe vya mbinguni, **M&M** 129:1.

Sayuni ilitwaliwa mbinguni, **Musa** 7:23.

Mchungaji. *Ona pia* Mchungaji Mwema; Yesu Kristo

Kiishara huyu ni mtu awatunzaye watoto wa Bwana.

Bwana ndiye mchungaji wangu, **Zab.** 23:1. Wachungaji yawapasa kuwalisha kondoo, **Eze.** 34:2–3.

Mchungaji Mwema. *Ona pia* Yesu Kristo

Yesu Kristo ndiye Mchungaji Mwema. Kimfano, wafuasi wake ni kama kondoo ambao Yesu anawachunga.

Bwana ndiye mchungaji wangu, **Zab.** 23:1. Atalilisha kundi lake kama mchungaji, **Isa.** 40:11. Ndivyo nitakavyo watafuta kondoo wangu, **Eze.** 34:12.

Mimi ndiye mchungaji mwema, **Yn.** 10:14–15. Yesu ndiye yule mchungaji mkuu wa kondoo, **Ebr.** 13:20.

Huwahesabu kondoo wake nao humjua yeye, **1 Ne.** 22:25. Mchungaji mwema huwaita ninyi katika jina lake, ambalo ni Kristo, **Alma** 5:38, 60. Kutakuwako na kundi moja, na mchungaji mmoja, **3 Ne.** 15:21 (Yn. 10:16).

Melkizedeki. *Ona pia* Salemu; Ukuhani wa Melkizedeki

Kuhani mkuu, nabii, na kiongozi katika Agano la Kale aliyeishi baada ya Gharika na katika wakati wa Ibrahimu. Aliitwa mfalme wa Salemu (Yerusalemu), mfalme wa amani, mfalme wa

haki (ambayo kwa Kiebrania ndiyo maana ya neno Melkizedeki), na kuhani wa Mungu Aliye Juu Sana.

Ibrahimu alilipa fungu la kumi kwa Melkizedeki, **Mwa.** 14:18–20. Watu wa Melkizedeki walitenda haki, na wakaipata mbingu, **TJS, Mwa.** 14:25–40.

Kristo alikuwa kuhani mkuu kwa mfano wa Melkizedeki, **Ebr.** 5:6. Melkizedeki alikuwa Mfalme wa Salemu, kuhani wa Mungu Aliye Juu Sana, **Ebr.** 7:1–3.

Hakuna waliokuwa wakuu kuliko Melkizedeki, **Alma** 13:14–19.

Ibrahimu alipokea ukuhani kutoka kwa Melkizedeki, **M&M** 84:14. Katika kuheshimu jina la Bwana, Kanisa la kale liliita ukuhani huu wa juu kama Ukuhani wa Melkizedeki, **M&M** 107:1–4.

Meshaki. *Ona pia* Danieli

Katika Agano la Kale, Shadraki, Meshaki, na Abednego walikuwa vijana watatu wa Kiisraeli, ambao, pamoja na Danieli, waliletwa katika kasri ya Nebukadneza, mfalme wa Babilonia. Jina la Meshaki Kiebrania lilikuwa Mishaeli. Vijana hawa wanne walikataa kujichafua wao wenyewe kwa kula chakula na mvinyo wa mfalme (Dan. 1). Shadraki, Meshaki, na Abednego walitupwa katika tanuri ya moto mkali na mfalme, lakini kimiujiza wakaokolewa (Dan. 3).

Methusela. *Ona pia* Henoko

Mwana wa Henoko katika Agano la Kale. Methusela aliishi miaka 969 (Mwa. 5:21–27; Lk. 3:37; Musa 8:7). Alikuwa nabii mwadilifu aliyeachwa duniani wakati mji wa Henoko ulipotwaliwa mbinguni. Alibaki duniani ili kutoa uzao ambao kupitia huo Nuhu angelikuja (Musa 8:3–4).

Mfano

Hadithi fupi iliyotumika kufafanua na kufundisha kweli au kanuni ya Kiroho. Mfano uko katika msingi wa kulinganisha kitu au tukio la kawaida na ukweli, na maana au ujumbe wa mfano unayoonyeshwa bila kutajwa mara kwa mara hufichwa kwa msikilizaji ambaye huwa hayuko tayari kiroho kuupokea (Mt. 13:10–17).

Yesu mara kwa mara alifundisha kwa mifano. Kwa orodha ya mifano yake muhimu, ona Upatanifu wa Injili katika kiambatisho.

Mfariji. *Ona pia* Roho Mtakatifu; Yesu Kristo

Maandiko yanazungumzia juu ya Wafariji wawili. Wa kwanza ni Roho Mtakatifu (Yn. 14:26–27; Moro. 8:26; M&M 21:9; 42:17; 90:11). Mfariji wa pili ni Bwana Yesu Kristo (Yn. 14:18, 21, 23). Mtu ampatapo Mfajiri wa pili, Yesu Kristo atamtokea wakati fulani fulani, atamfunulia Baba, naye atamfundisha uso kwa uso (M&M 130:3).

Mfariji wa Pili. *Ona* Mfariji

Mfiadini. *Ona* Kifo cha kishahidi, Mfiadini

Mhubiri

Kitabu katika Agano la Kale chenye kuonyesha picha ya baadhi ya matatizo makubwa ya maisha.

Mwandishi wa kitabu hiki, ambaye ni Mhubiri, anaandika sehemu kubwa ya kitabu hiki kutokana na mtazamo wa wale ambao wasio na ufahamu wa injili. Anaandika kulingana na hisia za watu wa ulimwengu—ambao ni, wale "walio chini ya jua" (Mh. 1:9). Sehemu kubwa ya kitabu chaonekana kuwa kinyume, na yaonekana kuwa mambo yote ni mabaya (Mh. 9:5, 10). Hii siyo namna ambayo Bwana angetutaka tuyaone maisha, bali ni namna ambayo Mhubiri alivyoona mambo yanavyoonekana kwa wanadamu wasioelimishwa hapa duniani. Sehemu ya kiroho zaidi katika kitabu hiki iko katika milango ya 11 na wa 12, ambamo mwandishi anahitimisha kwamba kitu pekee chenye thamani ya kudumu ni utiifu kwa amri za Mungu.

Mika

Nabii wa Agano la Kale. Alikuwa mwenyeji wa Moresheth-Ghathi, katika

nchi tambarare ya Yuda, naye alitoa unabii wakati Hezekia alipokuwa mfalme (Mika 1:1–2).

Kitabu cha Mika: Mika ndicho kitabu pekee katika Agano la Kale kinachotaja Bethlehemu kama mahali ambapo Masiya angezaliwa (Mika 5:2). Katika kitabu hiki Bwana anasemezana na watu Wake na kukumbusha wema wake uliopita kwao; Yeye alihitaji haki, huruma, na unyenyekevu kutoka kwao (Mika 6:8).

Mikaeli. *Ona pia* Adamu; Malaika mkuu

Jina ambalo kwalo Adamu alijulikana katika maisha mbinguni kabla ya kuzaliwa katika mwili. Yeye huitwa Malaika mkuu. Kwa Kiebrania jina hili maana yake "Aliye kama Mungu."

Mikaeli, mmoja wa hao wakuu wa mbele, alikuja kumsaidia Danieli, **Dan.** 10:13, 21 (M&M 78:16). Katika siku za mwisho Mikaeli atasimama, jemadari mkuu, **Dan.** 12:1.

Mikaeli malaika mkuu alishindana na ibilisi, **Yuda** 1:9. Mikaeli na malaika zake wakapigana na yule joka, **Ufu.** 12:7 (Dan. 7).

Mikaeli ndiye Adamu, **M&M** 27:11 (M&M 107:53–57; 128:21). Mikaeli, malaika mkuu wa Bwana, atapiga tarumbeta, **M&M** 29:26. Mikaeli atakusanya jeshi lake na kupigana na Shetani, **M&M** 88:112–115. Sauti ya Mikaeli ilisikika ikimfichua ibilisi, **M&M** 128:20.

Mikono, Kuweka juu ya. *Ona pia* Huduma kwa Wagonjwa; Kipawa cha Roho Mtakatifu; Kutawaza, Kutawazwa; Usimikaji

Tendo la kuweka mikono ya mtu juu ya kichwa cha mtu mwingine kama sehemu ya ibada ya ukuhani. Ibada nyingi za ukuhani hufanyika kwa kuweka mikono juu ya mtu, kama vile kutawazwa, kubariki, kuhudumia wagonjwa, kuthibitisha uanachama wa Kanisa, na kutoa Roho Mtakatifu.

Musa aliweka mikono yake juu ya kichwa cha Yoshua, kama Bwana alivyomwamuru, **Hes.** 27:18, 22–23 (Kum. 34:9).

Yesu aliweka mikono yake juu ya wagonjwa wachache, na akawaponya, **Mk.** 6:5 (Morm. 9:24). Mitume waliweka mikono yao juu ya watu saba ambao wangewasaidia, **Mdo.** 6:5–6. Roho Mtakatifu alitolewa kwa kuwekea mikono, **Mdo.** 8:14–17. Anania akamwekea mikono Sauli, na akamrejeshea kuona kwake, **Mdo.** 9:12, 17–18. Paulo akamwekea mikono yake juu yake na akamponya, **Mdo.** 28:8. Paulo alifundisha mafundisho ya ubatizo na kuwekea mikono, **Ebr.** 6:2.

Alma aliwatawaza makuhani na wazee kwa kuwawekea mikono, **Alma** 6:1. Yesu alitoa uwezo kwa wanafunzi wake wa kutoa Roho Mtakatifu kwa kuwekea mikono, **3 Ne.** 18:36–37. Ambaye juu yake mtamwekea mikono yenu, mtampa Roho Mtakatifu, **Moro.** 2:2.

Wazee wataweka mikono yao juu ya watoto ili kuwabariki, **M&M** 20:70. Watampokea Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono, **M&M** 35:6 (M ya I 1:4). Wazee wataweka mikono juu ya wagonjwa, **M&M** 42:44 (M&M 66:9). Watoto watapokea kuwekewa mikono baada ya ubatizo, **M&M** 68:27. Ukuhani hupokelewa kwa kuwekewa mikono, **M&M** 84:6–16.

Milenia. *Ona pia* Jehanamu; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo

Kipindi cha amani cha miaka elfu moja ambacho kitaanza wakati Kristo atakaporudi kuitawala dunia yeye mwenyewe (M ya I 1:10).

Watu hawatainua panga, wala hawatajifunza vita tena, **Isa.** 2:4 (Mika 4:3; 2 Ne. 12:4). Nchi ile iliyokuwa ukiwa imekuwa kama bustani ya Edeni, **Eze.** 36:35.

Nao wakaishi na kutawala pamoja na Kristo miaka elfu, **Ufu.** 20:4.

Kwa sababu ya haki, Shetani hana uwezo, **1 Ne.** 22:26.

Nitakaa katika haki duniani kwa miaka elfu, **M&M** 29:11. Miaka elfu itakapokwisha, nitaiachia dunia kwa muda mfupi, **M&M** 29:22. Ile Milenia kuu itakuja, **M&M** 43:30. Watoto wa walio waadilifu watakuwa pasipo dhambi, **M&M** 45:58. Watoto watakua hadi wamekuwa wazee; wanadamu watageuzwa katika muda wa kufumba na kufumbua jicho, **M&M** 63:51. Mwanzoni mwa miaka ya elfu saba, Bwana ataitakasa dunia, **M&M** 77:12. Hawataishi tena hadi ile miaka elfu itakapokwisha, **M&M** 88:101. Shetani atafungwa kwa miaka elfu, **M&M** 88:110. Milenia yaelezwa, **M&M** 101:23–34.

Kwa miaka elfu dunia itapumzika, **Musa** 7:64.

MIMI NIKO. *Ona pia* Yehova; Yesu Kristo

Mojawapo ya majina ya Bwana Yesu Kristo.

Mungu akamwambia Musa, MIMI NIKO AMBAYE NIKO, **Ku.** 3:14–15. Mimi ni Bwana, **Ku.** 6:2–3.

Kabla Ibrahimu hajakuwepo, Mimi niko, **Yn.** 8:56–59.

Sikilizeni sauti ya Yesu Kristo, Mimi Ndimi Mkuu, **M&M** 29:1 (M&M 38:1; 39:1).

Miriamu. *Ona pia* Musa

Katika Agano la Kale, ni dada wa Musa (Hes. 26:59).

Aliangalia kisafina kilichotengenezwa kwa manyasi, **Ku.** 2:1–8. Aliwaongoza wanawake wenye matari, **Ku.** 15:20–21. Alinung'unika dhidi ya Musa na akapigwa kwa ukoma, kisha akaponywa, **Hes.** 12:1–15 (Kum. 24:9).

Misri

Nchi katika kona ya kaskazini mashariki ya Afrika. Sehemu kubwa ya Misri ni jangwa na isiyokaliwa na watu. Wakazi wake wengi huishi katika Bonde la Nile, ambalo lina urefu wa kiasi cha maili 550 (kilometa 890).

Misri ya kale ilikuwa tajiri na yenye kustawi. Miradi mikubwa ya kiuhandisi ilijengwa, ikiwa pamoja na mifereji ya umwagiliaji, miji yenye ngome imara kwa ajili ya ulinzi; na masanamu ya kifalme ya ukumbusho, hususani makaburi ya piramidi na mahekalu, ambayo bado yapo miongoni mwa maajabu ya ulimwengu. Kwa wakati fulani, serikali ya Kimisri ilikuwa katika mfano wa utaratibu wa kipatriaki katika ukuhani (Ibr. 1:21–27).

Ibrahimu na Yusufu waliongozwa kwenda Misri ili kuziokoa familia zao kwa njaa, **Mwa.** 12:10 (Mwa. 37:28). Yusufu aliuzwa Misri, **Mwa.** 45:4–5 (1 Ne. 5:14–15). Yakobo aliongozwa kwenda Misri, **Mwa.** 46:1–7. Musa aliwaongoza wana wa Israeli kutoka Misri, **Ku.** 3:7–10; 13:14 (Ebr. 11:27; 1 Ne. 17:40; Musa 1:25–26). Misri ilikuwa ni ishara ya uovu, **Eze.** 29:14–15 (Hos. 9:3–7; Ibr. 1:6, 8, 11–12, 23).

Malaika alimwambia Yusufu akimbilie Misri yeye pamoja na Maria na Yesu, **Mt.** 2:13 (Hos. 11:1).

Missouri. *Ona* Yerusalemu Mpya

Mitala. *Ona* Ndoa, Oa, Olewa—Ndoa ya wake wengi

Mithali

Misemo mifupi yenye mafundisho au ushauri.

Kitabu cha Mithali: Kitabu cha Agano la Kale ambacho kina mifano mengi, misemo, na mashairi, baadhi yaliandikwa na Sulemani. Kitabu cha Mithali mara kwa mara kimenukuliwa katika Agano Jipya.

Mlango wa 1–9 ina maelezo juu ya hekima ya kweli. Mlango wa 10–24 ina mikusanyiko na misemo juu ya njia sahihi na ambazo si sahihi za kuishi. Mlango wa 25–29 ina mithali za Suleimani ambazo watu wa Hezekia, mfalme wa Yuda, waliziandika. Mlango wa 30–31 inajumuisha maelezo juu ya mwanamke mwadilifu.

Mizeituni, Mlima wa. *Ona pia* Gethsemani

Kilima kilicho katika mashariki ya

Bonde la Kidroni, mashariki ya Yerusalemu. Juu ya miteremko yake ya magharibi, karibu na chini, ndipo ilipo bustani ya Gethsemani. Bethfage na Bethania zipo juu yake na katika mteremko wa mashariki. Mlima huu ulikuwa mahali pa matukio mengi ya kibiblia (Mt. 24:3) na pia patakuwa mahali muhimu katika matukio ya siku za mwisho (Zek. 14:3–5; M&M 45:48–54; 133:20).

Mjane. *Ona pia* Ustawi

Mwanamke ambaye mume wake amefariki na hajaolewa tena.

Yatima na mjane watakuja na watakula, **Kum.** 14:29.

Huyu mjane maskini ametia vyote alivyokuwa navyo, **Mk.** 12:41–44. Kuwatembelea yatima na wajane katika dhiki yao, **Yak. (Bib.)** 1:27.

Bwana atakuwa shahidi mwepesi dhidi ya wale ambao huwanyanyasa wajane, **3 Ne.** 24:5 (Zek. 7:10).

Wajane na mayatima watatunzwa kwa mali hiyo, **M&M** 83:6 (M&M 136:8).

Mkananayo. *Ona* Kanaani, Mkananayo

Mkate wa Uzima. *Ona pia* Sakramenti; Yesu Kristo

Yesu Kristo ni Mkate wa Uzima. Mkate wa Sakramenti ni ishara inayowakilisha mwili wa Kristo.

Mimi ni mkate wa uzima, **Yn.** 6:33–58.

Kuleni na kunyweni mkate na maji ya uzima, **Alma** 5:34. Mkate ni katika ukumbusho wa mwili wa Kristo, **3 Ne.** 18:5–7.

Mkate ni mfano wa mwili wa Kristo, **M&M** 20:40, 77 (Moro. 4).

Mke. *Ona* Familia; Ndoa, Oa, Olewa

Mkombozi. *Ona pia* Mwokozi; Yesu Kristo

Yesu Kristo ndiye Mkombozi mkuu wa wanadamu kwa sababu Yeye, kupitia Upatanisho Wake, alilipia dhambi za wanadamu na akawezesha kupatikana kwa ufufuko wa watu wote.

Ninajua kwamba mkombozi wangu yu hai, **Ayu.** 19:25. Nitakusaidia, asema mkombozi wako, Mtakatifu wa Israeli, **Isa.** 41:14 (Isa. 43:14; 48:17; 54:5; 59:20). Mimi Bwana ndiye Mkombozi wako, **Isa.** 49:26 (Isa. 60:16).

Mtamwita jina lake Yesu: kwa maana atawaokoa watu wake na dhambi zao, **Mt.** 1:21. Mwana wa Mtu amekuja kutoa uhai wake kama fidia kwa ajili ya wengi, **Mt.** 20:28 (1 Tim. 2:5–6). Bwana Mungu wa Israeli amewatembele na kuwakomboa watu wake, **Lk.** 1:68. Tulipatanishwa kwa Mungu kwa kifo cha Mwanawe, **Rum.** 5:10. Yesu Kristo alijitoa mwenyewe kwa ajili yetu, ili apate kutukomboa na uovu wote, **Tit.** 2:13–14. Yesu Kristo alituosha dhambi zetu katika damu yake yeye mwenyewe, **Ufu.** 1:5.

Ukombozi huja katika na kupitia Masiya Mtakatifu, **2 Ne.** 2:6–7, 26. Mwana alijitwalia juu yake uovu na uvunjaji sheria wa wanadamu, akawakomboa, na akatosheleza madai ya haki, **Mos.** 15:6–9, 18–27. Kristo alikuja kuwakomboa wale wote ambao wangebatizwa ubatizo wa toba, **Alma** 9:26–27. Atakuja ulimwenguni kuwakomboa watu wake, **Alma** 11:40–41. Ukombozi huja kwa njia ya toba, **Alma** 42:13–26. Yesu alikuja kuukomboa ulimwengu, **Hel.** 5:9–12. Kristo amewakomboa wanadamu kutokana na kifo cha kimwili na kiroho, **Hel.** 14:12–17. Ukombozi huja kupitia kwa Kristo, **3 Ne.** 9:17. Mimi ndiye niliyetayarishwa tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu ili kuwakomboa watu wangu, **Eth.** 3:14.

Bwana Mkombozi wenu aliteseka mauti katika mwili, **M&M** 18:11. Kristo aliteseka kwa ajili ya wote kama watatubu, **M&M** 19:1, 16–20. Watoto wadogo wamekombolewa kupitia Mwana wa Pekee, **M&M** 29:46. Nimempeleka Mwanangu wa Pekee katika ulimwengu kwa ajili ya ukombozi wa ulimwengu, **M&M** 49:5. Kristo ndiye nuru na Mkombozi wa ulimwengu, **M&M** 93:8–9. Joseph F. Smith alipokea ono juu ya wokovu wa wafu, **M&M** 138.

Tunaamini kwamba kupitia upatanisho wa Kristo, wanadamu wote wanaweza kuokolewa, **M ya I** 1:3.

Mlima wa Mizeituni. *Ona* Mizeituni, Mlima wa

Mmoja. *Ona* Mungu, Uungu; Umoja

Mnyenyekevu, Unyenyekevu. *Ona pia* Kiburi; Maskini; Moyo Uliovunjika; Pole, Upole; Udhaifu

Mtu kuwa mpole na mwenye kufundishika, au hali ya kuwa mpole na mwenye kufundishika. Unyenyekevu ni pamoja na kutambua utegemezi wetu kwa Mungu na kutamani kujiweka katika mapenzi Yake.

Mungu alikuongoza jangwani kwa miaka arobaini ili kukufanya uwe mnyenyekevu, **Kum.** 8:2. Niliinyenyekeza nafsi yangu kwa kufunga, **Zab.** 35:13. Heri kijana maskini mwenye hekima kuliko mfalme mzee mpumbavu, **Mh.** 4:13. Bwana hukaa pamoja na yule aliye mnyenyekevu, **Isa.** 57:15.

Yeyote ajinyenyekezaye mwenyewe kama mtoto mdogo huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni, **Mt.** 18:4. Yeyote atakayejinyenyekeza mwenyewe atakwezwa, **Mt.** 23:12 (Lk. 14:11; 18:14). Yesu alijinyenyekeza mwenyewe na akawa mtii hadi mauti, **Flp.** 2:8 (Lk. 22:42; 23:46). Mungu huwapinga wenye kiburi, na huwapa wanyenyekevu neema, **1 Pet.** 5:5–6 (2 Ne. 9:42).

Jinyenyekezeni wenyewe katika vina vya unyenyekevu, **Mos.** 4:11 (2 Ne. 9:42; 3 Ne. 12:2). Je, mmekuwa wanyenyekevu vya kutosha, **Alma** 5:27–28. Sehemu kubwa ya watu waliokuwa wanyenyekevu zaidi wakawa imara zaidi katika unyenyekevu wao, **Hel.** 3:33–35. Ninawapa wanadamu udhaifu ili wapate kuwa wanyenyekevu, **Eth.** 12:27.

Unyenyekevu ni sifa kwa ajili ya ubatizo, **M&M** 20:37. Jinyenyekezeni mbele yangu na nanyi mtaniona na kujua ya kuwa Mimi ndimi, **M&M** 67:10. Uwe mnyenyekevu na Bwana atakupa jibu la sala zako, **M&M** 112:10. Mtu aliye mjinga na ajifunze hekima kwa kujinyenyekeza mwenyewe, **M&M** 136:32. Roho amepelekwa ili kuwaangaza walio wanyenyekevu, **M&M** 136:33.

Moabu. *Ona pia* Lutu

Nchi katika Agano la Kale iliyokuwa mashariki ya Bahari ya Chumvi. Wamoabu walikuwa ni wazao wa Lutu na walikuwa na uhusiano na Waisraeli. Walizungumza lugha inayofanana na Kiebrania. Kulikuwa na vita vya kudumu baina ya Wamoabu na Waisraeli (Amu. 3:12–30; 11:17; 2 Sam. 8:2; 2 Fal. 3:6–27; 2 Nya. 20:1–25; Isa. 15).

Mormoni, Kitabu cha. *Ona* Kitabu cha Mormoni

Mormoni, Nabii Mnefi. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni

Nabii Mnefi, jemadari wa jeshi, na mtunza kumbukumbu katika Kitabu cha Mormoni. Mormoni aliishi takribani katika miaka ya 311–385 B.K. (Morm. 1:2, 6; 6:5–6; 8:2–3). Alikuwa kiongozi wa jeshi kwa sehemu kubwa ya maisha yake, kuanzia akiwa na umri wa miaka kumi na mitano (Morm. 2:1–2; 3:8–12; 5:1; 8:2–3). Ammaroni alimwamuru Mormoni kujitayarisha kusimamia historia na kuandika historia (Morm. 1:2–5; 2:17–18). Baada ya kuandika historia ya wakati wa uhai wake yeye mwenyewe, Mormoni aliandika kwa ufupi kutoka mabamba mapana ya Nefi juu ya mabamba ya Mormoni. Baadaye aliyatoa maandiko haya matakatifu kwa mwanawe Moroni. Mabamba haya yalikuwa sehemu ya kumbukumbu ambayo kwayo Joseph Smith alitafsiri Kitabu cha Mormoni.

Maneno ya Mormoni: Kitabu kidogo katika Kitabu cha Mormoni. Katikati ya maneno ya mwisho ya Amaleki katika Kitabu cha Omni na maneno ya mwanzo katika kitabu cha Mosia, Mormoni, mhariri wa kumbukumbu zote, ndiye aliyefanya mwingizo huu mdogo. (Ona "Maelezo Mafupi kuhusu Kitabu cha Mormoni" mwanzoni mwa Kitabu cha Mormoni.)

Kitabu cha Mormoni: Kitabu kilichojitenga ndani ya kitabu cha maandiko kinachojulikana kama Kitabu cha Mormoni. Mlango wa 1–2 huzungumzia juu ya Amaroni, nabii wa Wanefi, akimwamuru Mormoni lini na wapi atakapoyapata mabamba hayo. Pia, vita kuu vinaanza, na Wanefi Watatu walitwaliwa na Bwana kwa sababu ya uovu wa watu. Mlango wa 3–4 huzungumzia juu ya Mormoni akililia toba kwa watu, lakini wao walikwisha kufa ganzi, na uovu mkubwa zaidi ulienea kuliko mwanzoni katika Israeli. Mlango wa 5–6 anaandika pambano la mwisho kati ya Wanefi na Walamani. Mormoni aliuawa pamoja na sehemu kubwa ya taifa la Kinefi. Katika mlango wa 7, kabla ya kifo chake, Mormoni aliwasihi watu—wakati huo, na baadaye—watubu. Katika mlango wa 8–9 anaandika kwamba hatimaye mwana wa Mormoni pekee, Moroni, ndiye aliyebaki hai. Aliandika matukio ya mwisho ya mauti na umwagaji damu, pamoja na mwisho wa watu wa Nefi, na akaandika ujumbe kwa vizazi vya wakati ujao na wasomaji wa historia hii.

Moroni, Kapteni. *Ona pia* Bendera ya Uhuru

Katika Kitabu cha Mormoni, ni kamanda mwaminifu wa jeshi la Wanefi aliyeishi takribani miaka 100 K.K.

Moroni aliteuliwa kuwa kapteni mkuu wa majeshi yote ya Wanefi, **Alma** 43:16–17. Aliwatia moyo askari wa Wanefi kupigana kwa ajili ya uhuru wao, **Alma** 43:48–50. Alitengeneza bendera ya uhuru kutokana na kipande cha koti lake, **Alma** 46:12–13. Alikuwa mtu wa Mungu, **Alma** 48:11–18. Alikasirishwa na serikali kwa sababu ya tofauti zao juu ya uhuru wa nchi, **Alma** 59:13.

Moroni, Mwana wa Mormoni. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni; Mormoni, Nabii Mnefi

Nabii wa mwisho Mnefi katika Kitabu cha Mormoni (mnamo mwaka 421 B.K.). Muda mfupi kabla ya kifo cha Mormoni, yeye alikabidhi maandishi ya kihistoria yaliyoitwa mabamba ya Mormoni kwa mwanawe Moroni (M. ya Morm. 1:1). Moroni alimalizia kukusanya mabamba ya Mormoni. Aliongezea mlango wa 8 na wa 9 katika Kitabu cha Mormoni (Morm. 8:1). Aliandika kwa ufupi na kukiongeza Kitabu cha Etheri (Eth. 1:1–2) na akaongeza kitabu chake yeye mwenyewe kinachoitwa Kitabu cha Moroni (Moro. 1). Moroni aliyafunga mabamba hayo na akayaficha katika kilima Kumora (Morm. 8:14; Moro. 10:2). Katika mwaka 1823 Moroni alitumwa kama kiumbe mfufuka ili kukifunua Kitabu cha Mormoni kwa Joseph Smith (M&M 27:5; JS—H 1:30–42, 45). Alimfundisha nabii huyu kijana kila mwaka tangu mwaka 1823 hadi 1827 (JS—H 1:54) na mwishowe akayakabidhi mabamba kwake katika mwaka wa 1827 (JS—H 1:59). Baada ya kumaliza kutafsiri Joseph Smith aliyarudisha mabamba yale kwa Moroni.

Kitabu cha Moroni: Kitabu cha mwisho ndani ya Kitabu cha Mormoni. Kiliandikwa na nabii huyu wa mwisho Mnefi, Moroni. Mlango 1–3 husimulia juu ya angamizo la mwisho la Wanefi, kutoa maelekezo juu ya kutunukiwa kwa Roho Mtakatifu na ukuhani. Mlango wa 4–5 inaeleza kwa mapana namna sahihi ya kuhudumia sakramenti. Mlango wa 6 anafanya muhtasari wa kazi ya Kanisa. Mlango 7–8 ni mafundisho juu ya kanuni za kwanza za injili, pamoja na mafundisho ya Mormoni juu ya imani, tumaini, na hisani na jinsi ya kuhukumu mema na maovu (Moro. 7), na maelezo ya Mormoni kwamba watoto wadogo wako hai katika Kristo na hawahitaji ubatizo (Moro. 8). Mlango wa 9 huelezea kutemwa kwa taifa la Wanefi. Mlango wa 10 ni ujumbe wa mwisho wa Moroni na unajumuisha njia ya kujua ukweli wa Kitabu cha Mormoni (Moro. 10:3–5).

Moroniha, Mwana wa Kapteni Moroni

Kamanda Mnefi mwaminifu katika

Kitabu cha Mormoni (takribani mwaka wa 60 K.K.).

Moroni aliyakabidhi majeshi kwa mwanawe Moroniha, **Alma** 62:43. Aliuchukua tena mji wa Zarahemla, **Hel.** 1:33. Aliwaleta Wanefi kwenye toba na kupata tena udhibiti zaidi ya nusu ya nchi, **Hel.** 4:14–20.

Mosia, Baba wa Benjamini. *Ona pia* Benjamini, Baba wa Mosia; Zarahemla

Katika Kitabu cha Mormoni, ni nabii wa Wanefi aliyefanywa kuwa mfalme juu ya watu wa Zarahemla.

Mosia alionywa aikimbie nchi ya Nefi, **Omni** 1:12. Akawavumbua watu wa Zarahemla, **Omni** 1:14–15. Alifanya watu wa Zarahemla wafundishwe katika lugha yake, **Omni** 1:18. Aliteuliwa kuwa mfalme wa watu wa muungano, **Omni** 1:19. Mwanawe, Benjamini, alitawala baada ya kifo chake, **Omni** 1:23.

Mosia, Mwana wa Benjamini. *Ona pia* Benjamini, Baba wa Mosia; Mosia, Wana wa

Mfalme mwaminifu wa Wanefi na nabii katika Kitabu cha Mormoni. Mosia alifuata mfano mwema wa baba yake (Mos. 6:4–7). Alitafsiri mabamba ishirini na manne ya dhahabu yaliyokuwa na kumbukumbu ya Wayaredi (Mos. 28:17).

Kitabu cha Mosia: Kitabu katika Kitabu cha Mormoni. Mlango wa 1–6 ina mahubiri yenye nguvu ya kwa watu wake. Roho wa Bwana akagusa mioyo yao na watu wakaongolewa na hawakusikia tena tamaa ya kutenda maovu. Mlango wa 7–8 husimulia juu ya kikundi cha Wanefi waliokwenda kuishi katika nchi ya Walamani. Kikundi cha watafutaji kilitumwa kwenda kuwatafuta. Ammoni kiongozi wa kikundi cha watafutaji, aliwaona na akajifunza hadithi juu ya majaribu yao chini ya ukandamizaji wa Walamani. Mlango wa 9–24 inaelezea ukandamizaji huo na namna viongozi wao—Zenifa, Nuhu, na Limhi—walivyoishi chini ya Walamani. Kifo cha kishahidi cha nabii aliyeitwa Abinadi pia kimeandikwa. Alma aliongolewa wakati wa kesi ya Abinadi. Mlango wa 25–28 inaelezea hadithi ya namna mwana wa Alma na wana wanne wa Mfalme Mosia walivyokuja kuongolewa. Katika mlango wa 29 mfalme Mosia alipendekeza kwamba utaratibu wa waamuzi utumike badala ya wafalme. Alma mwana wa Alma aliteuliwa mwamuzi mkuu wa kwanza.

Mosia, Wana wa. *Ona pia* Amoni, Mwana wa Mosia; Haruni, Mwana wa Mosia; Himni; Mosia, Mwana wa Benjamini; Omneri

Katika Kitabu cha Mormoni, ni wana wa nne wa Mfalme Mosia ambao waliongolewa baada ya malaika kuwatokea na kuwaamuru watubu. Majina yao yalikuwa Amoni, Haruni, Omneri, na Himni (Mos. 27:34). Walitumia miaka kumi na minne kwa mafanikio wakihubiri injili kwa Walamani. Kumbukumbu ya huduma yao miongoni mwa Walamani imetolewa katika kitabu cha Alma, mlango wa 17 hadi 26.

Mwanzoni wao hawakuwa waumini hivyo walijaribu kuliangamiza kanisa, **Mos.** 27:8–10 (Alma 36:6). Walikemewa na malaika na wakatubu, **Mos.** 27:11–12, 18–20. Walipata ruhusa ya kuhubiri kwa Walamani, **Mos.** 28:1–7.

Moto. *Ona pia* Batiza, Ubatizo; Dunia—Kutakaswa kwa dunia; Jehanamu; Roho Mtakatifu

Ishara ya kuoshwa, kusafishwa, au kutakaswa. Moto waweza pia kutumika kama ishara ya uwepo wa Mungu.

Mungu wenu ni moto ulao, **Kum.** 4:24. Bwana huwafanya watumishi wake kuwa moto wa miali, **Zab.** 104:4. Bwana wa majeshi atawajilia kwa miale ya moto uteketezao, **Isa.** 29:6 (2 Ne. 27:2). Bwana atakuja na moto, **Isa.** 66:15. Yeye ni mfano wa moto wa mtu asafishaye fedha na kuitakasa, **Mal.** 3:2 (3 Ne. 24:2; M&M 128:24).

Atakubatiza kwa Roho Mtakatifu, na kwa moto, **Mt.** 3:11 (Lk. 3:16).

Wenye haki watahifadhiwa kwa moto, **1 Ne.** 22:17. Waovu wataangamizwa kwa moto, **2 Ne.** 30:10. Nefi alielezea namna gani tunapokea ubatizo wa moto na Roho Mtakatifu, **2 Ne.** 31:13–14 (3 Ne. 9:20; 12:1; 19:13; Eth. 12:14; M&M 33:11).

Utatangaza msamaha wa dhambi kwa ubatizo, na kwa moto, **M&M** 19:31. Kanisa kuu na lenye kuchukiza litatupwa chini kwa moto uteketezao, **M&M** 29:21. Dunia itapita kama vile kwa moto, **M&M** 43:32. Uwepo wa Bwana utakuwa kama moto uyeyushao, **M&M** 133:41.

Adamu alibatizwa kwa moto na Roho Mtakatifu, **Musa** 6:66.

Moyo. *Ona pia* Moyo Uliovunjika; Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena

Ishara ya mawazo na matakwa ya mwanadamu na ishara ya chanzo cha mhemuko wa moyo na hisia zote.

Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, **Kum.** 6:5 (Kum. 6:3–7; Mt. 22:37; Lk. 10:27; M&M 59:5). Bwana amemtafuta mtu ampendezaye moyo wake, **1 Sam.** 13:14. Mwanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo, **1 Sam.** 16:7. Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe atapanda katika mlima wa Bwana naye atabarikiwa, **Zab.** 24:3–5 (2 Ne. 25:16). Mtu awazavyo katika moyo wake, hivyo ndivyo alivyo, **Mit.** 23:7. Eliya ataigeuza mioyo ya baba kwa watoto, na mioyo ya watoto kwa baba zao, **Mal.** 4:5–6 (Lk. 1:17; M&M 2:2; 110:14–15; 138:47; JS—H 1:38–39).

Heri wenye moyo safi, **Mt.** 5:8 (3 Ne. 12:8). Mwanadamu hunena kutoka mema au maovu yaliyo katika moyo wake, **Lk.** 6:45.

Mfuateni Mwana kwa kusudi kamili la moyo, **2 Ne.** 31:13. Je, mmezaliwa kiroho kwa Mungu na kuona mabadiliko makubwa katika mioyo yenu, **Alma** 5:14. Mtoleeni Bwana dhabihu ya moyo uliovunjika na roho iliopondeka, **3 Ne.** 9:20 (3 Ne. 12:19; Eth. 4:15; Moro. 6:2).

Nitakuambia katika mawazo yako na katika moyo wako kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, **M&M** 8:2.

Moyo Uliovunjika. *Ona pia* Dhabihu; Mnyenyekevu, Unyenyekevu; Moyo; Pole, Upole; Toba, Tubu

Kuwa na moyo uliovunjika ni kuwa mwenye kunyenyekea, kupondeka, mwenye kutubu, na mpole—maana yake, ni kuwa msikivu wa mapenzi ya Mungu.

Nakaa pamoja na yeye aliye na roho iliyopondeka na kunyenyekea, **Isa.** 57:15.

Kristo alijitoa mwenyewe kwa ajili ya wale walio na moyo uliovunjika na roho iliyopondeka, **2 Ne.** 2:7. Mtatoa dhabihu kwa Bwana ya moyo uliovunjika na roho iliyopondeka, **3 Ne.** 9:20 (M&M 59:8). Wale tu walio na moyo uliovunjika na roho iliyopondeka wanapokelewa katika ubatizo, **Moro.** 6:2.

Yesu alisulubiwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi kwa moyo uliopondeka, **M&M** 21:9. Yule aliye na roho iliyopondeka hukubalika, **M&M** 52:15. Roho Mtakatifu ameahidiwa kwa wale wenye toba, **M&M** 55:3. Roho wangu amepelekwa ili kuwaangaza walio wanyenyekevu na wenye toba, **M&M** 136:33.

Mpakwa mafuta. *Ona pia* Masiya; Yesu Kristo

Yesu anaitwa *Kristo* (neno la Kiyunani) au *Masiya* (neno la Kiaramaya). Maneno yote mawili yanamaanisha "mpakwa mafuta." Yeye ni mpakwa mafuta wa Baba ili kuwa mwakilishi binafsi wa Baba katika mambo yote yahusuyo wokovu wa wanadamu.

Bwana amenipaka mafuta, **Isa.** 61:1–3.

Amempaka mafuta mmoja ili kuhubiri injili, **Lk.** 4:16–22. Yesu alipakwa mafuta na Mungu Baba, **Mdo.** 4:27. Mungu alimpaka mafuta Yesu wa Nazareti, **Mdo.** 10:38.

Mpango wa Ukombozi. *Ona pia* Anguko la Adamu na Hawa; Injili; Lipia dhambi, Upatanisho; Wokovu; Yesu Kristo

Utimilifu wa injili ya Yesu Kristo, iliyo kusudiwa kumletea mwanadamu kutokufa na uzima wa milele. Unajumuisha Uumbaji, Anguko, na Upatanisho, sambamba na sheria zote zilizotolewa na Mungu, ibada, na mafundisho. Mpango huu hufanya uwezekano kwa watu wote kuinuliwa na kuishi pamoja na Mungu milele (2 Ne. 2; 9); Maandiko pia huonyesha mpango huu kama mpango wa wokovu, mpango wa furaha, na mpango wa rehema.

Alijeruhiwa kwa makosa yetu, **Isa.** 53:5 (Mos. 14:5).

Hapana jina jingine chini ya mbingu ambalo kwalo mwanadamu aweza kuokolewa, **Mdo.** 4:12. Kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa, **1 Kor.** 15:22. Mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani, **Efe.** 2:8 (2 Ne. 25:23). Mungu aliahidi uzima wa milele kabla ya kuanza kwa ulimwengu, **Tit.** 1:2. Yesu ndiye muasisi wa wokovu wa milele, **Ebr.** 5:8–9. Mpango wa ukombozi umepelekwa hadi kwa wafu, **1 Pet.** 3:18–20; 4:6 (M&M 138).

Ni jinsi gani ulivyo mkuu mpango wa Mungu wetu, **2 Ne.** 9:6. Ni jinsi gani ulivyo mkuu mpango wa Mungu wetu!, **2 Ne.** 9:13. Mpango wa ukombozi huleta ufufuko na maondoleo ya dhambi, **Alma** 12:25–34. Haruni alifundisha mpango wa ukombozi kwa baba yake Lamoni, **Alma** 22:12–14. Amuleki alielezea mpango wa wokovu, **Alma** 34:8–16. Alma alielezea mpango wa wokovu, **Alma** 42:5–26, 31.

Mafundisho ya uumbaji, anguko, upatanisho, na ubatizo yanathibitishwa katika mafunuo ya kisasa, **M&M** 20:17–29. Mpango huu uliwekwa kabla ya ulimwengu kuwako, **M&M** 128:22.

Kazi yangu na utukufu wangu ni kuleta kutokufa na uzima wa milele wa mwanadamu, **Musa** 1:39. Huu ndiyo mpango wa wokovu kwa wanadamu wote, **Musa** 6:52–62. Tutawajaribu kwa njia hii, **Ibr.** 3:22–26.

Mpango wa Ushirika. *Ona pia* Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu

Mfumo ambao kupitia huo Watakatifu katika siku za mwanzoni za urejesho wa Kanisa walijaribu kuishi katika sheria ya kuweka wakfu. Watu waliweka na kutumia kwa pamoja, mali, bidhaa, na faida, wakipokea vitu hivi kulingana na vile walivyopangiwa na kulingana na mahitaji yao (M&M 51:3; 78:1–15; 104).

Katika mambo ya kimwili mtakuwa sawa, **M&M** 70:14. Watakatifu walijiandaa kuwa sawa katika mambo yote, **M&M** 78:3–11 (M&M 82:17–20). Bwana alitoa ufunuo na amri kwa mpango wa ushirika, **M&M** 92:1. John Johnson yampasa awe mshirika wa mpango wa ushirika, **M&M** 96:6–9. Bwana alitoa mafundisho ya jumla kwa uendeshaji wa mpango wa ushirika, **M&M** 104. Watu wangu hawajaungana kulingana na muungano unaotakiwa kwa ufalme wa selestia, **M&M** 105:1–13.

Mpango wa Wokovu. *Ona* Mpango wa Ukombozi

Mpatanishi. *Ona pia* Lipia dhambi, Upatanisho; Yesu Kristo

Mwombezi au msuluhishi. Yesu Kristo ni mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu. Upatanisho Wake ulifanya njia iwezekane kwa watu kutubu dhambi zao na kupatanishwa na Mungu.

Hakuna mtu ajaye kwa Baba ila kwa njia ya Yesu Kristo, **Yn.** 14:6. Kuna mpatanishi mmoja kati ya Mungu na wanadamu, **1 Tim.** 2:5. Kristo ni mpatanishi wa agano lililo bora, **Ebr.** 8:6 (Ebr. 9:15; 12:24; M&M 107:19).

Masiya Mtakatifu atafanya maombezi kwa watoto wote wa watu, **2 Ne.** 2:9 (Isa. 53:12; Mos. 14:12). Mtazameni yule Mpatanishi mkuu, **2 Ne.** 2:27–28.

Tunafanywa kuwa wakamilifu kupitia

Yesu yule mpatanishi wa agano jipya, **M&M** 76:69.

Mpinga Kristo. *Ona pia* Ibilisi

Mtu yoyote au kitu chochote ambacho kinaiga mpango wa injili ya kweli ya wokovu na kwamba kwa wazi au kwa siri kinampinga Kristo. Yohana Mfunuzi anamwelezea mpinga Kristo kama mdanganyifu (1 Yoh. 2:18–22; 4:3–6; 2 Yoh. 1:7). Mpinga Kristo mkuu ni Lusiferi, lakini anao wasaidizi wengi, viumbe wa kiroho na wa kimwili.

Mwana wa upotevu hupinga na kujiinua mwenyewe juu ya wote ambao huitwa Mungu, **2 The.** 2:1–12. Huwadanganya wao wakaao ya dunia kwa njia ya miujiza, **Ufu.** 13:13–17.

Sheremu alimkana Kristo naye akawadanganya wengi, **Yak. (KM)** 7:1–23. Nehori alifundisha mafundisho ya uongo, akaanzisha kanisa, na akaanzisha ukuhani wa uongo, **Alma** 1:2–16. Korihori alimdhihaki Kristo, Upatanisho, na roho ya unabii, **Alma** 30:6–60.

Mrithi

Mtu mwenye haki ya kurithi vipawa vya kimwili au kiroho. Katika maandiko, wenye haki wameahidiwa kwamba watakuwa warithi wa vile vyote Mungu alivyo navyo.

Ibrahimu alitamani kuwa na mrithi, **Mwa.** 15:2–5.

Ibrahimu akawa mrithi wa ulimwengu kwa haki aliyohesabiwa kwa imani, **Rum.** 4:13. Sisi tu watoto wa Mungu, na kama tu watoto, basi tu warithi, warithi wa Mungu, na warithi pamoja na Kristo, **Rum.** 8:16–17 (M&M 84:38). Wewe u mwana, mrithi wa Mungu kwa njia ya Kristo, **Gal.** 4:7. Mungu amemweka Mwanawe kuwa mrithi wa mambo yote, **Ebr.** 1:2.

Wale watazamiao msamaha wa dhambi zao ndiyo warithi wa ufalme wa Mungu, **Mos.** 15:11. Watu wakawa watoto wa Kristo na warithi wa ufalme wa Mungu, **4 Ne.** 1:17.

Watu waliokufa pasipo ufahamu wa injili wataweza kuwa warithi wa ufalme wa selestia, **M&M** 137:7–8. Wafu wanaotubu ni warithi wa wokovu, **M&M** 138:58–59.

Ibrahimu akawa mrithi mwenye haki kwa ajili ya haki yake, **Ibr.** 1:2.

Msalaba. *Ona pia* Golgotha; Kusulubiwa; Lipia dhambi, Upatanisho; Sakramenti; Yesu Kristo

Umbile la kitu kilichotengenezwa kwa mbao ambapo juu yake Yesu Kristo alisulubiwa (Mk. 15:20–26). Wengi duniani sasa wanaifikiria hiyo kama ndiyo alama ya Kusulubiwa kwa Kristo na dhabihu ya kulipia dhambi; hata hivyo, Bwana ameweka alama Zake mwenyewe kwa ajili ya Kusulubiwa Kwake na dhabihu Yake—mkate na maji ya sakramenti (Mt. 26:26–28; M&M 20:40, 75–79). Katika maandiko, wale wachukuao msalaba wao ni wale wenye kumpenda Yesu Kristo sana kiasi kwamba hukataa ubaya na tamaa za kidunia na kushika amri Zake (TJS, Mt. 16:25–26 [Kiambatisho]).

Chukua msalaba wako, na ukanifuate, **Mk.** 10:21 (3 Ne. 12:30; M&M 23:6). Yesu aliustahmili msalaba naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu, **Ebr.** 12:2.

Aliinuliwa juu msalabani na akauawa kwa ajili ya dhambi za ulimwengu, **1 Ne.** 11:33. Wale waliostahmili misalaba ya ulimwengu wataurithi ufalme wa Mungu, **2 Ne.** 9:18. Baba wangu alinituma ili nipate kuinuliwa juu ya msalaba, **3 Ne.** 27:14–15.

Yule ambaye hatauchukua msalaba wake na kunifuata na kushika amri zangu, huyo hataokolewa, **M&M** 56:2.

Tazama Mwana wa Mtu ameinuliwa juu ya msalaba, **Musa** 7:55.

Msimamizi, Usimamizi. *Ona pia* Ita, Itwa na Mungu, Wito

Mtu anayeangalia mambo au mali ya mtu mwingine. Kile ambacho msimamizi anakiangalia ndicho huitwa usimamizi. Vitu vyote duniani ni mali

ya Bwana; sisi tu wasimamizi Wake. Sisi tunawajibika kwa Bwana, lakini tunaweza kutoa taarifa juu ya usimamizi wetu kwa wawakilishi wa Mungu walio na mamlaka. Tunapopata wito wa utumishi kutoka kwa Bwana au watumishi Wake wenye mamlaka, usimamizi huo waweza kujumuisha mambo yote kiroho na kimwili (M&M 29:34).

Wewe umekuwa mwaminifu juu ya mambo machache, nitakufanya kuwa mtawala juu ya mambo mengi, **Mt.** 25:14–23. Kila aliyepewa vingi, kwake huyo vitatakiwa vingi, **Lk.** 12:48 (M&M 82:3). Yesu alitoa fumbo la msimamizi asiye na haki, **Lk.** 16:1–8.

Yeyote atakayepatikana kuwa msimamizi mwaminifu ataingia katika shangwe ya Bwana wake, **M&M** 51:19. Kila mtu atatoa hesabu ya usimamizi wake, **M&M** 72:3–5. Yule aliye mwaminifu na msimamizi mwenye hekima atarithi vitu vyote, **M&M** 78:22. Bwana atamfanya kila mtu awajibike kama msimamizi juu ya baraka za kidunia, **M&M** 104:11–17 (M&M 42:32). Fanya bidii ili upate kuwa msimamizi mwenye hekima, **M&M** 136:27.

Msuluhishi. *Ona pia* Amani

Mtu aletaye au ahimizaye amani (Mt. 5:9; 3 Ne. 12:9). Msuluhishi aweza pia kuwa mtu ahubiriye injili (Mos. 15:11–18).

Mtakatifu. *Ona pia* Kanisa la Yesu Kristo; Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho; Wakristo

Muumini mwaminifu wa Kanisa la Yesu Kristo.

Nikusanyieni pamoja Watakatifu wangu, **Zab.** 50:5.

Sauli alifanya mengi maovu kwa Watakatifu huko Yerusalemu, **Mdo.** 9:1–21. Petro pia akawatelemkia Watakatifu waliokuwa wakikaa Lida, **Mdo.** 9:32. Neema na amani kwa wote waliokaa Rumi, walioitwa kuwa Watakatifu, **Rum.** 1:7. Ninyi ni raia wenyeji pamoja na Watakatifu, **Efe.** 2:19–21.

Nililiona Kanisa la Mwanakondoo, ambao walikuwa Watakatifu wa Mungu, **1 Ne.** 14:12. Mtu wa asili ni adui kwa Mungu isipokuwa amekuwa mtakatifu kwa njia ya upatanisho wa Kristo, **Mos.** 3:19.

Mimi, Bwana, nimeibariki nchi kwa ajili ya matumizi ya Watakatifu wangu, **M&M** 61:17. Shetani hufanya vita na Watakatifu wa Mungu, **M&M** 76:28–29. Fanya kazi kwa bidii kwa kuwatayarisha Watakatifu kwa ajili ya hukumu ambayo inakuja, **M&M** 88:84–85. Watakatifu yawapasa kutoa mali zao kwa maskini na walioteseka, **M&M** 105:3. Ofisi zilizoko hapo juu nimezitoa kwa ajili ya kazi ya huduma na ya kuwakamilisha Watakatifu wangu, **M&M** 124:143 (Efe. 4:12).

Mtakatifu wa Israeli. *Ona* Yesu Kristo

Mti wa Uzima. *Ona* Edeni

Mti katika Bustani ya Edeni na ni pepo ya Mungu (Mwa. 2:9; Ufu. 2:7). Katika ndoto ya Lehi mti wa uzima inawakilisha upendo wa Mungu na inaelezwa kuwa kama ndiyo zawadi ya Mungu kubwa kuliko zote (1 Ne. 8; 11:21–22, 25; 15:36).

Makerubi na upanga wa moto hulinda njia ya mti wa uzima, **Mwa.** 3:24 (Alma 12:21–23; 42:2–6).

Yohana aliuona mti wa uzima, na majani yake yalikuwa na uwezo wa kuponya mataifa, **Ufu.** 22:2.

Lehi aliuona mti wa uzima, **1 Ne.** 8:10–35. Nefi aliuona mti ambao baba yake aliuona, **1 Ne.** 11:8–9. Fimbo ya chuma ndiyo iongozayo kwenye mti wa uzima, **1 Ne.** 11:25 (1 Ne. 15:22–24). Shimo refu na la kutisha huwatenga waovu na mti wa uzima, **1 Ne.** 15:28, 36. Ilikuwa hakuna budi kuwepo na tunda lililokatazwa kinyume na mti wa uzima, **2 Ne.** 2:15. Njooni kwa Bwana na mpate kula tunda la mti wa uzima, **Alma** 5:34, 62. Kama wazazi wetu wa

kwanza wangekula tunda la ule mti wa uzima, wangekuwa wenye huzuni milele, **Alma** 12:26. Kama hautalistawisha neno, kamwe hamuweza mkachuma tunda la mti wa uzima, **Alma** 32:40.

Bwana alipanda mti wa uzima katikati ya bustani, **Musa** 3:9 (Ibr. 5:9). Mungu alimtoa Adamu kutoka Edeni asije akala baadhi ya tunda la mti wa uzima na akaishi milele, **Musa** 4:28–31.

Mtiifu, Tii, Utii. *Ona pia* Amri za Mungu; Baraka, Bariki, Barikiwa; Shangwe; Sheria; Sikiliza; Tembea, Tembea na Mungu

Katika maana ya kiroho, utii ni kufanya mapenzi ya Mungu.

Nuhu alifanya kulingana na yote ambayo Mungu alimwamuru, **Mwa.** 6:22. Ibrahimu alimtii Bwana, **Mwa.** 22:15–18. Yote Bwana aliyosema tutayafanya, **Ku.** 24:7. Sikiliza kwa hiyo, Ee Israeli, na angalia uyafanye, **Kum.** 6:1–3. Mpende Bwana na ukatii sauti yake, **Kum.** 30:20. Kutii ni bora kuliko dhabihu, **1 Sam.** 15:22. Mwogope Bwana na ukashike amri zake, **Mh.** 12:13–14.

Si kila mtu ataingia katika ufalme wa mbinguni, bali yeye afanyaye mapenzi ya Baba, **Mt.** 7:21 (3 Ne. 14:21). Kama mtu yeyote atayafanya mapenzi yake, atajua kama mafundisho haya ni ya Mungu, **Yn.** 7:17. Yatupasa kumtii Mungu zaidi kuliko wanadamu, **Mdo.** 5:29. Watoto, watiini wazazi wenu, **Efe.** 6:1 (Kol. 3:20).

Nitakwenda na kufanya mambo ambayo Bwana ameamuru, **1 Ne.** 3:7. Nilitii sauti ya Roho, **1 Ne.** 4:6–18. Kama wanadamu watashika amri za Mungu, yeye atawalisha, **1 Ne.** 17:3. Jihadharini msije mkaitii pepo mchafu, **Mos.** 2:32–33, 37 (M&M 29:45). Wanadamu huvuna thawabu zao kulingana na roho wanayoitii, **Alma** 3:26–27.

Wanadamu yawapasa kufanya mambo mengi kwa ridhaa yao wenyewe, **M&M** 58:26–29. Wanadamu hawamkosei Mungu katika lolote, isipokuwa wale wasioukiri mkono wake na wasiotii amri zake, **M&M** 59:21. Mimi Bwana hufungwa mnapofanya yale nisemayo, **M&M** 82:10. Kila nafsi yenye kutii sauti yangu itauona uso wangu na kunijua Mimi ndimi, **M&M** 93:1. Watu lazima warudiwe hadi wajifunze utii, **M&M** 105:6. Tupatapo baraka yoyote kutoka kwa Mungu ni kwa sababu ya utiifu wetu kwa sheria ile ambayo juu yake hutoka, **M&M** 130:21.

Adamu alikuwa mtiifu, **Musa** 5:5. Tutawajaribu ili kuona kama watafanya mambo yoyote yale ambayo Bwana atawaamuru, **Ibr.** 3:25.

Mto Yordani

Mto Yordani unatoka katika bahari ya Galilaya hadi Bahari ya Chumvi. Mto huu una urefu wa maili 100 (kilometa 160) na unaundwa kwa muunganiko wa chemchemi kadhaa zinazotiririka kutoka Mlima Hermoni. Ni mto muhimu sana katika Israeli.

Matukio muhimu mawili yanayohusiana na mto huu nayo ni Bwana kuugawanya mto huu kwa ajili ya kuwavusha Waisraeli (Yos. 3:14–17) na ubatizo wa Yesu Kristo (Mt. 3:13–17; 1 Ne. 10:9).

Mtoto, Watoto. *Ona pia* Baraka, Bariki, Barikiwa—Baraka za watoto; Familia; Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika; Lipia dhambi, Upatanisho; Ubatizo wa Watoto Wachanga; Wokovu—Wokovu wa watoto

Mtu aliye mdogo, ambaye bado hajafikia balehe. Akina baba na akina mama wawafundishe watoto wao kutii mapenzi ya Mungu. Watoto hawana dhambi hadi wafikiapo umri wa uwajibikaji (Moro. 8:22; M&M 68:27).

Watoto ndiyo urithi kutoka kwa Bwana, **Zab.** 127:3–5. Mlee mtoto katika njia impasayo, **Mit.** 22:6.

Waacheni watoto wadogo waje kwangu na msiwazuie, **Mt.** 19:14. Watiini wazazi wenu, **Efe.** 6:1–3 (Kol. 3:20).

Pasipo Anguko, Adamu na Hawa wasingelikuwa na watoto, **2 Ne.** 2:22–23. Wafundisheni watoto kutembea katika

ukweli na katika kiasi, **Mos.** 4:14–15. Watoto wadogo wanao uzima wa milele, **Mos.** 15:25. Yesu akawachukua watoto wadogo na kuwabariki, **3 Ne.** 17:21. Na watoto wako wote wafundishwe juu ya Bwana, na amani ya watoto wako itakuwa kubwa, **3 Ne.** 22:13 (Isa. 54:13). Watoto wadogo hawahitaji toba au ubatizo, **Moro.** 8:8–24.

Watoto wadogo wamekombolewa tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu kwa njia ya Mwanangu wa Pekee, **M&M** 29:46–47. Wazazi yawapasa wawafundishe watoto wao kanuni za injili na desturi zake, **M&M** 68:25, 27–28. Watoto ni watakatifu kwa njia ya upatanisho wa Kristo, **M&M** 74:7. Wazazi wanaamriwa kuwalea watoto wao katika nuru na kweli, **M&M** 93:40. Watoto wanao kufa kabla ya umri wa uwajibikaji wanaokolewa katika ufalme wa selestia, **M&M** 137:10.

Mtoza Ushuru. *Ona pia* Ufalme wa Kirumi

Katika Rumi ya kale, ni mtoza ushuru kwa ajili ya serikali. Watoza ushuru kwa ujumla walichukiwa na Wayahudi. Baadhi ya watoza ushuru walikuwa tayari kuikubali injili (Mt. 9:9–10; Lk. 19:2–8).

Mtu wa Utakatifu. *Ona pia* Baba wa Mbinguni; Mungu, Uungu; Mwana wa Mtu

Jina jingine la Mungu Baba (Musa 6:57).

Mtume. *Ona pia* Mwanafunzi; Ufunuo

Katika Kiyunani, *Mtume* maana yake "mtu aliyetumwa." Kilikuwa ni cheo ambacho Yesu aliwapa wale Kumi na Wawili ambao Yeye aliwachagua na kuwatawaza kuwa wanafunzi Wake wa karibu sana na wasaidizi wake wakati wa huduma Yake hapa duniani (Lk. 6:13; Yn. 15:16). Aliwatuma kumwakilisha Yeye na kuhudumu kwa niaba Yake baada ya kupaa Kwake mbinguni. Zamani na katika Akidi ya Mitume Kumi na Wawili katika Kanisa lililorejeshwa leo, Mtume ni shahidi maalumu wa Yesu Kristo ulimwenguni kote ili kushuhudia juu ya uungu Wake na ufufuko Wake kutoka kwa wafu (Mdo. 1:22; M&M 107:23).

Kanisa la Yesu Kristo limejengwa juu ya msingi wa Mitume na Manabii, **Efe.** 2:20; 4:11.

Lehi na Nefi waliwaona Mitume kumi na wawili wakimfuata Yesu, **1 Ne.** 1:10; 11:34. Mitume wataihukumu nyumba ya Israeli, **Morm.** 3:18.

Wale wasioyasikia maneno ya manabii na Mitume watakatiliwa mbali, **M&M** 1:14 (3 Ne. 12:1). Wito na huduma wa wale Kumi na Wawili zilifunuliwa, **M&M** 18:26–36. Joseph Smith alitawazwa Mtume, **M&M** 20:2; 21:1. Mitume ni mashahidi maalumu wa jina la Kristo na hushikilia funguo za huduma, **M&M** 27:12 (M&M 112:30–32). Mitume Kumi na Wawili hufanya akidi iliyo sawa katika mamlaka na Urais wa Kwanza, **M&M** 107:23–24. Wale Kumi na Wawili ni Baraza Kuu la viongozi Wasafirio, **M&M** 107:33. Mitume hushikilia funguo za kazi za umisionari, **M&M** 107:35. Baadhi ya kazi za Mitume zafafanuliwa, **M&M** 107:58. Ninasema kwa wote Kumi na Wawili: nifuateni mimi, na walisheni kondoo wangu, **M&M** 112:14–15.

Tunaamini katika mitume, **M ya I** 1:6.

Uteuzi wa Mitume: Mitume huchaguliwa na Bwana (Yn. 6:70; 15:16).

Kutokana na wanafunzi wake, Yesu aliwachagua Mitume kumi na wawili, **Lk.** 6:13–16. Mathiya alikuwa amechaguliwa kuwa Mtume, **Mdo.** 1:21–26.

Oliver Cowdery na David Whitmer waliamriwa kuwatafuta wale Kumi na Wawili, **M&M** 18:37–39.

Muhuri, Tia. *Ona* Kufunga, Muhuri, Tia

Muleki. *Ona pia* Zedekia

Mwana wa mfalme Zedekia wa Agano la Kale (karibia mwaka 589 K.K.). Biblia inaandikwa kwamba wana wote

wa Zedekia waliuawa (2 Fal. 25:7), lakini Kitabu cha Mormoni kinaelezea kwamba Muleki alipona (Hel. 8:21).

Zarahemla alikuwa ni wa uzao wa Muleki, **Mos.** 25:2. Watu wa Muleki waliungana na Wanefi, **Mos.** 25:13. Bwana alimleta Muleki katika nchi ya kaskazini, **Hel.** 6:10. Wana wote wa Zedekia waliuawa isipokuwa Muleki, **Hel.** 8:21.

Mume. *Ona* Familia; Ndoa, Oa, Olewa

Mungu, Uungu. *Ona pia* Baba wa Mbinguni; Bwana; Roho Mtakatifu; Yesu Kristo

Kuna watu watatu tofauti katika Uungu; Mungu, Baba wa Milele; Mwanawe, Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu. Tunaamini katika kila mmoja Wao (M ya I 1:1). Kutokana na ufunuo wa siku za mwisho tunajifunza kwamba Baba na Mwana wana miili yenye kushikika ya nyama na mifupa na kwamba Roho Mtakatifu ni mtu wa kiroho, pasipo nyama na mifupa (M&M 130:22–23). Watu hawa watatu ni wamoja katika umoja mkamilifu na wenye mapatano ya madhumuni na mafundisho (Yn. 17:21–23; 2 Ne. 31:21; 3 Ne. 11:27, 36).

Mungu Baba: Kwa ujumla ni Baba, au Elohimu, ambaye hutajwa kwa jina hili Mungu. Yeye anaitwa Baba kwa sababu Yeye ni baba wa roho zetu (Hes. 16:22; 27:16; Mal. 2:10; Mt. 6:9; Efe. 4:6; Ebr. 12:9). Mungu Baba ndiye mtawala mkuu wa ulimwengu. Yeye ni mweza yote (Mwa. 18:14; Alma 26:35; M&M 19:1–3), mjua yote (Mt. 6:8; 2 Ne. 2:24), na aliye mahali pote kwa njia ya Roho Wake (Zab. 139:7–12; M&M 88:7–13, 41). Mwanadamu anao uhusiano maalumu na Mungu ambao humtenga mwanadamu mbali na vitu vingine vyote vilivyoumbwa: wanaume na wanawake ni watoto wa kiroho wa Mungu (Zab. 82:6; 1 Yoh. 3:1–3; M&M 20:17–18).

Kuna matukio machache ya Mungu Baba kumtokea au kuongea na mwanadamu. Maandiko yanasema kwamba Alinena kwa Adamu na Hawa (Musa 4:14–31) na akamtambulisha Yesu Kristo katika matukio kadha wa kadha (Mt. 3:17; 17:5; Yn. 12:28–29; 3 Ne. 11:3–7). Alimtokea Stefano (Mdo. 7:55–56) na Joseph Smith (JS—H 1:17). Baadaye Aliwatokea wote Joseph Smith na Sidney Rigdon (M&M 76:20, 23). Kwa wale wenye kumpenda Mungu na kujitakasa wenyewe mbele Yake, Mungu wakati mwingine hutoa nafasi ya kumwona na kujua wao wenyewe kwamba Yeye ndiye Mungu (Mt. 5:8; 3 Ne. 12:8; M&M 76:116–118; 93:1).

Mungu wangu, Mungu wangu, kwa nini umeniacha, **Mk.** 15:34. Watu hawa ni watumishi wa Mungu Aliye Juu Sana, **Mdo.** 16:17. Sisi tu wazao wa Mungu, **Mdo.** 17:28–29.

Nanyi mtatoa sakramenti kwa Aliye Juu Sana, **M&M** 59:10–12.

Henoko aliona roho ambazo Mungu aliziumba, **Musa** 6:36. Mtu wa Utakatifu ndilo jina lake, **Musa** 6:57.

Mungu Mwana: Mungu ajulikanaye kama Yehova ni Mwana, Yesu Kristo (Isa. 12:2; 43:11; 49:26; 1 Kor. 10:1–4; 1 Tim. 1:1; Ufu. 1:8; 2 Ne. 22:2). Yesu hutenda kazi chini ya maelekezo ya Baba na wako katika mapatano timilifu na Yeye. Wanadamu wote ni kaka na dada Zake, kwa kuwa Yeye ndiye mkubwa kuliko watoto wote wa kiroho wa Elohimu. Baadhi ya dondoo za maandiko humwita Yeye kwa neno la Mungu. Kwa mfano, andiko lasema kwamba "Mungu aliumba mbingu na dunia" (Mwa. 1:1), lakini ukweli ulikuwa kwamba Yesu ndiye alikuwa Muumba chini ya maelekezo ya Mungu Baba (Yn. 1:1–3, 10, 14; Ebr. 1:1–2).

Bwana alijitambulisha mwenyewe kama MIMI NDIMI, **Ku.** 3:13–16. Mimi ndimi Bwana [Yehova], na zaidi yangu mimi hakuna mwokozi, **Isa.** 43:11 (Isa. 45:21).

Mimi ni nuru ya ulimwengu, **Yn.** 8:12. Kabla ya Ibrahimu kuweko, Mimi Ndimi, **Yn.** 8:58.

Bwana atahudumu miongoni mwa wanadamu katika hema takatifu ya

udongo, **Mos.** 3:5–10. Abinadi alielezea namna Kristo alivyo Baba na Mwana, **Mos.** 15:1–4 (Eth. 3:14). Bwana alimtokea kaka wa Yaredi, **Eth.** 3. Sikilizeni maneno ya Kristo Bwana wako na Mungu wako, **Moro.** 8:8. Yehova ndiye mwamuzi wa walio hai na wafu, **Moro.** 10:34.

Yesu aliwatokea Joseph Smith na Sidney Rigdon, **M&M** 76:20, 23. Bwana Yehova alionekana katika Hekalu la Kirtland, **M&M** 110:1–4.

Yehova aliongea na Ibrahimu, **Ibr.** 1:16–19. Yesu alimtokea Joseph Smith, **JS—H** 1:17.

Mungu Roho Mtakatifu: Roho Mtakatifu pia ni Mungu naye anaitwa Roho Mtakatifu, Roho, na Roho wa Mungu, miongoni mwa majina na vyeo vingine. Kwa msaada wa Roho Mtakatifu, mwanadamu anaweza kujua mapenzi ya Mungu Baba na kujua kwamba Yesu ndiye Kristo (1 Kor. 12:3).

Roho Mtakatifu atakufundisha kile utakachosema, **Lk.** 12:12. Roho Mtakatifu ndiye Mfariji, **Yn.** 14:26 (Yn. 16:7–15). Yesu alitoa amri kwa Mitume kwa njia ya Roho Mtakatifu, **Mdo.** 1:2. Roho Mtakatifu huwashuhudia Mungu na Kristo, **Mdo.** 5:29–32 (1 Kor. 12:3). Roho Mtakatifu pia ni shahidi wetu, **Ebr.** 10:10–17.

Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu mtaweza kujua ukweli wa mambo yote, **Moro.** 10:5.

Roho Mtakatifu ni roho wa ufunuo, **M&M** 8:2–3 (M&M 68:4).

Musa. *Ona pia* Amri Kumi; Haruni, Kaka wa Musa; Kugeuka sura—Kugeuka sura kwa Kristo; Torati; Torati ya Musa

Nabii wa Agano la Kale aliyewaongoza Waisraeli kutoka utumwa wa Misri na akawapa vifungu vya sheria za kidini, kijamii na kilishe kama zilivyofunuliwa na Mungu.

Utumishi wa Musa unaendelea hata ng'ambo ya mipaka ya uhai wake mwenyewe katika mwili wenye kufa. Joseph Smith alifundisha kwamba, wakiwa pamoja na Eliya, alikuja katika Mlima wa Kugeuka Sura na kutunuku funguo za ukuhani juu ya Petro, Yakobo, na Yohana (Mt. 17:3–4; Mk. 9:4–9; Lk. 9:30; M&M 63:21).

Musa aliwatokea Joseph Smith na Oliver Cowdery hapo 3 Aprili 1836, katika hekalu la Kirtland, Ohio, na akawatunukia funguo za kukusanyika kwa Israeli (M&M 110:11).

Ufunuo wa siku za mwisho unazungumzia sana juu ya Musa. Ametajwa mara kwa mara katika Kitabu cha Mormoni, na kutoka katika Mafundisho na Maagano tunajifunza juu ya utumishi wake (M&M 84:20–26) na kwamba alipata ukuhani kutoka kwa baba mkwe wake Yethro (M&M 84:6).

Ufunuo wa siku za mwisho pia unathibitisha historia ya kibiblia ya utumishi wake miongoni mwa wana wa Israeli na unasisitiza ya kuwa yeye ndiye aliyekuwa mwandishi wa vitabu vitano vinavyoanzisha Agano la Kale (1 Ne. 5:11; Musa 1:40–41).

Aliokolewa na binti wa Farao, **Ku.** 2:1–10. Alikimbilia Midiani, **Ku.** 2:11–22. Malaika wa Bwana alimtokea katika kichaka kilichokuwa kikiwaka moto, **Ku.** 3:1–15. Alitangaza mabalaa yatakayokuja juu ya Misri, **Ku.** 7–11. Bwana alianzisha Pasaka, **Ku.** 12:1–30. Aliwaongoza wana wa Israeli kuvuka Bahari Nyekundu, **Ku.** 14:5–31. Bwana alileta mana jangwani, **Ku.** 16. Alipiga mwamba huko Horebu na maji yakatoka, **Ku.** 17:1–7. Haruni na Huri waliishikilia mikono yake ili Joshua apate kumshinda Amuleki, **Ku.** 17:8–16. Yethro alimshauri, **Ku.** 18:13–26. Aliwaandaa watu kwa ajili ya kuonekana kwa Bwana juu ya mlima Sinai, **Ku.** 19. Bwana alimfunulia Amri Kumi, **Ku.** 20:1–17. Yeye na wazee sabini walimwona Mungu, **Ku.** 24:9–11. Alivunja mbao za ushuhuda na akaangamiza sanamu ya ndama wa dhahabu, **Ku.** 32:19–20. Aliongea na Mungu uso kwa uso, **Ku.** 33:9–11.

Alitokea wakati Yesu alipogeuka sura, **Mt.** 17:1–13 (Mk. 9:2–13; Lk. 9:28–36).

Tuwe hodari kama Musa, **1 Ne.** 4:2. Kristo ndiye nabii aliye kama Musa ambaye Bwana atamwinua, **1 Ne.** 22:20–21 (Kum. 18:15; 3 Ne. 20:23).

Aliwaongoza Waisraeli kwa ufunuo, **M&M** 8:3. Alionekana miongoni mwa roho zilizo maarufu, **M&M** 138:41.

Alimwona Mungu uso kwa uso, **Musa** 1:2, 31. Alikuwa katika mfano wa Mwana wa Pekee, **Musa** 1:6, 13. Aliamriwa kuandika mambo yaliyofunuliwa kwake juu ya uumbaji, **Musa** 2:1.

Kitabu cha Musa: Ni Kitabu katika Lulu ya Thamani Kuu ambamo imo tafsiri ya Joseph Smith ya Maongozi ya Mungu ya milango saba ya kwanza ya kitabu cha Mwanzo.

Mlango wa 1 unaandikwa ono ambalo ndani yake Musa alimwona Mungu, ambaye alimfunulia mpango mzima wa wokovu. Mlango wa 2–5 ni maelezo ya Uumbaji na Anguko la mwanadamu. Mlango wa 6–7 ina ono juu ya Henoko na utumishi wake duniani. Mlango wa 8 unalo ono juu ya Nuhu na Gharika kuu.

Vitabu vitano vya Musa: Ona Mwanzo, Kitabu cha Biblia; Kutoka; Walawi; Hesabu; Kumbukumbu la Torati

Vitabu vitano vya kwanza vya Agano la Kale vinajulikana kama vitabu vya Musa. Mabamba ya shaba nyeupe ambayo Nefi aliyachukuwa kutoka kwa Labani yalikuwa na vitabu vya Musa (1 Ne. 5:11).

Nefi alisoma mambo mengi yaliyokuwa yameandikwa katika vitabu hivyo vya Musa, **1 Ne.** 19:23.

Muujiza. *Ona pia* Amini, Imani; Ishara

Tukio lisilo la kawaida linalosababishwa na nguvu za Mungu. Miujiza ni sehemu muhimu katika kazi ya Yesu Kristo. Inajumuisha uponyaji, kurejeshwa kwa wafu katika uhai, na ufufuko. Miujiza ni sehemu ya injili ya Yesu Kristo. Imani ni muhimu ili miujiza iweze kuonekana (Mk. 6:5–6; Morm. 9:10–20; Eth. 12:12).

Farao atakaponena, fanyeni muujiza, **Ku.** 7:9.

Hakuna mtu atakayefanya muujiza kwa jina langu akaweza kuninenea mabaya, **Mk.** 9:39. Kana palikuwa ni mahali ambapo Yesu alifanya muujiza wake wa kwanza, **Yn.** 2:11.

Mimi ni Mungu wa miujiza, **2 Ne.** 27:23. Nguvu za Mungu hutenda miujiza, **Alma** 23:6. Kristo angeliweza kuonyesha miujiza mikuu kwa wale walio katika bara la Marekani kwa sababu walikuwa na imani kubwa, **3 Ne.** 19:35. Mungu hajakoma kuwa Mungu wa miujiza, **Morm.** 9:15.

Usiombe miujiza isipokuwa Bwana akatakapokuamuru, **M&M** 24:13–14. Kwa wengine wamepewa kipawa cha kutenda miujiza, **M&M** 46:21 (Moro. 10:12).

Muumba. *Ona* Umba, Uumbaji; Yesu Kristo

Muziki. *Ona pia* Imba; Wimbo

Tuni na mipigo inayoimbwa na kuchezwa tangu nyakati za mwanzoni za biblia ili kuelezea shangwe, kusifu, na kuabudu (2 Sam. 6:5). Yaweza kuwa katika namna ya sala. Zaburi huenda zilikuwa zikiimbwa kwa tuni rahisi na kuambatanishwa na vyombo.

Miriamu, dada wa Haruni na Musa, akatwaa tari na yeye pamoja na wanawake wenzake wakacheza, **Ku.** 15:20. Walawi waliokuwa waimbaji walikuwa na matoazi na vinanda na makuhani mia moja ishirini walipuliza matarumbeta yao, **2 Nya.** 5:12.

Yesu na wale Kumi na Wawili waliimba wimbo wa dini baada ya Karamu ya Mwisho, **Mt.** 26:30. Mkifundishana na kuonyana ninyi kwa ninyi kwa zaburi na wimbo, na tenzi za rohoni, **Kol.** 3:16.

Je, mmejisikia kuimba wimbo wa upendo wa ukombozi, **Alma** 5:26.

Nafsi ya Mungu hufurahia katika wimbo wa moyo, ndiyo, wimbo wa

mwenye haki ni sala, **M&M** 25:12. Msifuni Bwana kwa kuimba, kwa muziki, na kwa kucheza, **M&M** 136:28.

Mvivu, Uvivu

Asiyejishughulisha na asiyejihusisha katika kazi zilizo za haki.

Ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi asile, **2 The.** 3:10.

Wakawa watu wasiotaka kufanya kazi, waliojawa na fitina, **2 Ne.** 5:24. Epukana na uvivu, **Alma** 38:12.

Mtu asiyetaka kufanya kazi asile mkate wa mfanyakazi, **M&M** 42:42. Ole wenu ninyi ambao hamfanyi kazi kwa mikono yenu wenyewe, **M&M** 56:17. Jishughulisheni kwa bidii katika shughuli zilizo njema, **M&M** 58:27. Acheni uvivu, **M&M** 88:124.

Mwalimu. *Ona* Fundisha, Mwalimu

Mwalimu, Ukuhani wa Haruni. *Ona pia* Ukuhani wa Haruni

Ofisi katika Ukuhani wa Haruni.

Kazi ya mwalimu ni kuliangalia Kanisa, **M&M** 20:53–60. Ofisi ya mwalimu ni sehemu muhimu katika ukuhani, **M&M** 84:30, 111. Rais wa akidi ya walimu husimamia juu ya walimu ishirini na wanne, **M&M** 107:86.

Mwamba. *Ona pia* Injili; Ufunuo; Yesu Kristo

Kitaswira, Yesu Kristo na injili Yake, ambao ndiyo msingi na msaada imara (M&M 11:24; 33:12–13). Mwamba pia waweza kumaanisha ufunuo, ambao kwa huo Mungu hufanya injili Yake ijulikane kwa wanadamu (Mt. 16:15–18).

Yeye ni mwamba, kazi yake ni kamilifu, **Kum.** 32:4. Bwana ni mwamba wangu; nitamwamini yeye, **2 Sam.** 22:2–3. Jiwe likachongwa pasipo mikono, **Dan.** 2:34–35.

Msingi wake ulijengwa juu ya mwamba, **Mt.** 7:25 (3 Ne. 14:25). Yesu Kristo ndiye jiwe lile ambalo lilidharauliwa, **Mdo.** 4:10–11. Mwamba ule ulikuwa Kristo, **1 Kor.** 10:1–4 (Ku. 17:6).

Yule aliyejengwa juu ya mwamba huupokea ukweli, **2 Ne.** 28:28. Wayahudi watalikataa lile jiwe [Kristo] ambalo juu yake wangelijenga, **Yak. (KM)** 4:15–17. Ni juu ya mwamba wa Mkombozi wetu kwamba ni lazima tujenge msingi wetu, **Hel.** 5:12. Yeyote ajengaye juu ya mafundisho ya Kristo hujenga juu ya mwamba wake naye hataanguka wakati mafuriko yatakapokuja, **3 Ne.** 11:39–40 (Mt. 7:24–27; 3 Ne. 18:12–13). Mtu mwenye hekima alijenga nyumba yake juu ya mwamba, **3 Ne.** 14:24.

Kama mmejengwa juu ya mwamba wangu, dunia na jehanamu hazitawashinda, **M&M** 6:34. Yule ajengaye juu ya mwamba huu hataanguka kamwe, **M&M** 50:44.

Mimi ndimi Masiya, Mfalme wa Sayuni, Mwamba wa Mbinguni, **Musa** 7:53.

Mwaminifu, Uaminifu. *Ona pia* Haki, Uadilifu, enye Uadilifu

Kuwa mwaminifu na mkweli, na pasipo udanganyifu.

Watu watendao ukweli ndiyo furaha ya Bwana, **Mit.** 12:22. Lipa kile ambacho umeweka nadhiri, **Mh.** 5:4–5.

Tumeyakataa mambo yasiyo ya uaminifu yaliyositirika, **2 Kor.** 4:1–2. Kuweni na mazungumzo ya uaminifu, **1 Pet.** 2:12.

Ole wake mtu mwongo, kwani atatupwa chini katika jehanamu, **2 Ne.** 9:34. Roho husema ukweli na hasemi uongo, **Yak. (KM)** 4:13. Yeyote aazimaye kitu kwa jirani yake yampasa kurudisha kitu kile alichokiazima, **Mos.** 4:28 (M&M 136:25). Angalieni ya kuwa mnatenda haki mnaamua kwa haki, na mnatenda yaliyo mema, **Alma** 41:14.

Kila mtu na atende kwa uaminifu, **M&M** 51:9. Wote wajuao kuwa katika mioyo yao ni waaminifu wanakubaliwa kwangu, **M&M** 97:8. Walio waaminifu wenye hekima, na watu walio wema yapaswa watafutwe kwa ajili ya ofisi za kisiasa, **M&M** 98:4–10. Kwa bidii

tafuta kurudisha kile ambacho jirani yako amekipoteza, **M&M** 136:26.

Tunaamini katika kuwa waaminifu, **M ya I** 1:13.

Mwana wa Mtu. *Ona pia* Mungu, Uungu; Yesu Kristo

Jina ambalo Yesu Kristo alilitumia wakati alipokuwa akizungumza juu Yake mwenyewe (Lk. 9:22; 21:36). Lilimaanisha Mwana wa Mtu wa Utakatifu. Ni moja ya majina ya Mungu Baba. Wakati Yesu Alipojiita mwenyewe Mwana wa Mtu, lilikuwa ni tamko la wazi la uhusiano Wake mtakatifu na Baba. Jina hili linaonekana mara kwa mara katika vitabu vya Injili. Ufunuo wa siku za mwisho unathibitisha maana rasmi na utakatifu wa jina hili la Mwokozi (M&M 45:39; 49:6, 22; 58:65; Musa 6:57).

Mwana wa Mungu. *Ona* Mungu, Uungu; Yesu Kristo

Mwanadamu wa Tabia ya Asili. *Ona pia* Anguko la Adamu na Hawa; Tamaa za kimwili; Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena

Mtu anayechagua kuongozwa na hisia, tamaa, hamu, na milango ya fahamu ya mwili kuliko kwa miongozo ya Roho Mtakatifu. Mtu wa aina hiyo anaweza kutambua mambo ya kimwili lakini siyo mambo ya kiroho. Watu wote ni wa tamaa za kimwili, au wana miili ile yenye kufa, kwa sababu ya Anguko la Adamu na Hawa. Kila mtu lazima azaliwe tena kwa njia ya Upatanisho wa Yesu Kristo ili kukoma kuwa mtu wa asili.

Mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho, **1 Kor.** 2:14.

Mwanadamu wa tabia za asili ni adui kwa Mungu na lazima aondolewe, **Mos.** 3:19. Mtu ambaye hushikilia katika tamaa zake za mwili wa kiasili hubakia katika hali yake ya kuanguka, **Mos.** 16:5 (Alma 42:7–24; M&M 20:20). Ni mwanadamu gani wa tabia za asili aliyeko ambaye anayajua mambo haya, **Alma** 26:19–22. Watu wa tabia za asili au wenye tamaa za kimwili hawako na Mungu katika ulimwengu, **Alma** 41:11.

Kwa sababu ya uvunjaji wake wa sheria, mwanadamu akawa mfu kiroho, **M&M** 29:41. Wala mwanadamu yeyote wa tabia za asili hawezi kukaa katika uwepo wa Mungu, **M&M** 67:12.

Na mwanadamu akaanza kuwa mwenye tamaa za mwili, mpenda anasa, na uovu, **Musa** 5:13 (Musa 6:49).

Mwanadamu, Wanadamu. *Ona pia* Dada; Kaka, Ndugu; Mungu, Uungu; Mwanamke, Wanawake; Roho; Uumbaji wa Kiroho; Wana na Mabinti za Mungu

Hutumika kwa wanadamu wote, mwanaume na mwanamke. Wanadamu wote wanaume na wanawake ni watoto hasa wa kiroho wa Baba wa Mbinguni. Wanapozaliwa duniani, hupokea maumbile, miili yenye kufa. Miili hii iliumbwa kwa mfano wa Mungu (Mwa. 1:26–27). Wanaume na wanawake walio waaminifu katika kupokea ibada muhimu, kushika maagano yao, na kutii amri za Mungu wataingia katika kuinuliwa kwao na kuwa kama Mungu.

Mungu akamuumba mtu kwa mfano wake yeye mwenyewe, **Mwa.** 1:27 (Mos. 7:27; M&M 20:17–18). Mtu ni kitu gani, hata umkumbuke yeye, **Zab.** 8:4–5. Amelaaniwa mtu yule amtegemeaye mwanadamu, na amfanyaye kuwa kinga yake, **Yer.** 17:5 (2 Ne. 4:34; 28:26, 31).

Nilipokuwa mtu mzima, nimeyabatilisha mambo ya kitoto, **1 Kor.** 13:11.

Watu wapo ili wapate kuwa na shangwe, **2 Ne.** 2:25. Mwanadamu wa asili ni adui kwa Mungu, **Mos.** 3:19. Mnataka kuwa watu wa aina gani, **3 Ne.** 27:27.

Kazi za watu ndizo zenye kubatilika, siyo kazi za Mungu, **M&M** 3:3. Hupaswi kumwogopa mwanadamu zaidi kuliko Mungu, **M&M** 3:7 (M&M 30:11; 122:9). Vitu vyote vimefanywa kwa faida na matumizi ya mwanadamu, **M&M** 59:18.

Najua ya kuwa mwanadamu si kitu,

Musa 1:10. Kazi na utukufu wa Mungu ni kuleta kutokufa na uzima wa milele wa mwanadamu, **Musa** 1:39.

Mwanadamu, mtoto wa kiroho wa Baba wa Mbinguni: Wakaanguka kifudifudi, na kusema, Ee Mungu, Mungu wa roho za wenye mwili wote, **Hes.** 16:22 (Hes. 27:16). Ninyi ni wana wa Bwana Mungu wenu, **Kum.** 14:1. Ninyi ni miungu na ninyi nyote ni watoto wa Aliye Juu Sana, **Zab.** 82:6. Ninyi ni wana wa Mungu aliye hai, **Hos.** 1:10. Je, sisi sote hatuna Baba mmoja? Je, Mungu aliyetuumba si mmoja, **Mal.** 2:10.

Sisi tu wazao wa Mungu, **Mdo.** 17:29. Roho mwenyewe hushuhudia ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu, **Rum.** 8:16. Kujitia chini ya Baba wa roho, **Ebr.** 12:9.

Roho za watu wote huchukuliwa nyumbani kwa yule Mungu aliyezipa uhai, **Alma** 40:11.

Wakazi wa ulimwengu ni wana na mabinti wa Mungu, **M&M** 76:24. Mwanzoni mwanadamu alikuwa pamoja na Baba, **M&M** 93:23, 29.

Mungu aliwaumba wanadamu wote kiroho, kabla hawajakuwa juu ya uso wa dunia, **Musa** 3:5–7. Mimi ndimi Mungu; niliyeufanya ulimwengu, na wanadamu kabla hawajawa katika mwili, **Musa** 6:51.

Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni: Kwa hiyo kuweni wakamilifu, hata kama Baba yenu, **Mt.** 5:48 (3 Ne. 12:48). Je, haikuandikwa katika torati yenu ya kwamba ndinyi miungu, **Yn.** 10:34 (M&M 76:58). Twaweza kuwa warithi wa Mungu na warithi pamoja na Kristo, **Rum.** 8:17. Wewe u mwana, na kama u mwana, basi u mrithi wa Mungu kwa njia ya Kristo, **Gal.** 4:7. Atakapodhihirishwa, tutafanana naye, **1 Yoh.** 3:2. Kwake ashindaye nitampa kuketi pamoja nami katika kiti changu cha enzi, **Ufu.** 3:21.

Kwao nimewapa kuwa wana wa Mungu, **3 Ne.** 9:17.

Wale watakaorithi ufalme wa selestia ndiyo miungu, hata wana wa Mungu, **M&M** 76:50, 58. Kisha watakuwa miungu, kwa sababu wanao uwezo wote, **M&M** 132:20.

Mwanafunzi. *Ona pia* Mtume; Mwongofu, Uongofu; Nira; Wakristo

Mfuasi wa Yesu Kristo ambaye huishi kulingana na mafundisho ya Kristo (M&M 41:5). Mwanafunzi linatumika katika kuwaelezea wale Mitume Kumi na Wawili ambao Kristo aliwaita wakati wa huduma Yake katika mwili wenye kufa (Mt. 10:1–4). Mwanafunzi pia hutumika katika kuwaelezea wale watu kumi na wawili ambao Yesu aliwachagua kuliongoza Kanisa Lake miongoni mwa Wanefi na Walamani (3 Ne. 19:4).

Ukaitie muhuri sheria miongoni mwa wanafunzi wangu, **Isa.** 8:16.

Kama mkikaa katika neno langu, basi mmekuwa wanafunzi wangu, **Yn.** 8:31.

Mormoni alikuwa mwanafunzi wa Yesu Kristo, **3 Ne.** 5:12–13. Ninyi ni wanafunzi wangu, **3 Ne.** 15:12. Wanafunzi watatu hawataonja mauti, **3 Ne.** 28:4–10.

Sauti ya kuonya itakuwa kwa vinywa vya wanafunzi wangu, **M&M** 1:4. Wanafunzi wangu watasimama katika mahali patakatifu, **M&M** 45:32. Wale wasio wakumbuka maskini, wenye shida, wagonjwa na walioathirika siyo wanafunzi wangu, **M&M** 52:40. Yeyote asiye kuwa tayari kuutoa uhai wake siyo mwanafunzi wangu, **M&M** 103:27–28.

Mwanakondoo wa Mungu. *Ona pia* Lipia dhambi, Upatanisho; Pasaka; Yesu Kristo

Jina la Mkombozi ambalo linamwelezea Yesu kama dhabihu iliyotolewa kwa niaba yetu.

Aliletwa kama mwanakondoo apelekwaye machinjoni, **Isa.** 53:7 (Mos. 14:7).

Tazama mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu, **Yn.** 1:29 (Alma 7:14). Ninyi mlikombolewa kwa damu ya thamani ya Kristo, kama ya mwanakondoo asiye na ila, **1 Pet.** 1:18–20. Astahili Mwanakondoo aliyechinjwa, **Ufu.** 5:12. Tunamshinda

Shetani kwa damu ya Mwanakondoo, **Ufu.** 12:11.

Hawa wamefanywa kuwa weupe kwa damu ya Mwanakondoo, kwa sababu ya imani yao katika yeye, **1 Ne.** 12:11. Mwanakondoo wa Mungu ndiye Mwana wa Baba wa milele, na Mwokozi wa ulimwengu, **1 Ne.** 13:40 (1 Ne. 11:21). Lieni kwa Baba kwa nguvu katika jina la Yesu, ili pengine mpate kuoshwa kwa damu ya Mwanakondoo, **Morm.** 9:6 (Ufu. 7:14; Alma 34:36).

Mwana wa Mtu ndiye Mwanakondoo aliyechinjwa tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, **Musa** 7:47.

Mwanamke, Wanawake. *Ona pia* Dada; Kaka, Ndugu; Mwanadamu, Wanadamu

Mtu mzima wa kike, binti wa Mungu. Neno Mwanamke wakati mwingine hutumika katika maandiko kama cheo cha heshima (Yn. 19:26; Alma 19:10).

Mungu alimwumba mwanamume na mwanamke, **Mwa.** 1:27 (Musa 2:27; 6:9; Ibr. 4:27). Mwanamke mwema kima chake chapita cha marijani, **Mit.** 31:10–31.

Mwanamke ni utukufu wa mwanamume, **1 Kor.** 11:7. Walakini si mwanamume pasipo mwanamke, wala mwanamke pasipo mwanaume katika Bwana, **1 Kor.** 11:11. Wanawake wanapaswa kujipamba katika mavazi ya kujisitiri, **1 Tim.** 2:9–10.

Mimi, Bwana Mungu, hufurahia katika usafi wa kimwili wa wanawake, **Yak. (KM)** 2:28.

Dhambi zako zimesamehewa, nawe u mwanamke mteule, **M&M** 25:3. Wanawake wanayo haki ya kupata matunzo kwa waume zao, **M&M** 83:2.

Mwandishi

Agano la Kale na Jipya hutumia neno hili katika njia tofauti kidogo: (1) Katika Agano la Kale, mwandishi wajibu wake wa kimsingi ulikuwa ni kunakili maandiko (Yer. 8:8). (2) Waandishi mara kwa mara wametajwa katika Agano Jipya na wakati mwingine wameitwa wanasheria au madaktari wa sheria. Waliiendeleza sheria katika marefu na kuitumia katika hali za nyakati zao (Mt. 13:52; Mk. 2:16–17; 11:17–18; Lk. 11:44–53; 20:46–47).

Mwangamizi. *Ona pia* Ibilisi

Shetani ndiye mwangamizi.

Bwana hatakubali mwangamizi aingie nyumbani mwenu, **Ku.** 12:23.

Yule mwangamizi atembea juu ya maji, **M&M** 61:19. Yule mlinzi angeliweza kuliokoa shamba langu la mizabibu kutoka kwa yule mwangamizi, **M&M** 101:51–54.

Mwanzo. *Ona pia* Maisha kabla ya kuzaliwa; Umba, Uumbaji; Yesu Kristo

Kwa ujumla humaanisha wakati kabla ya maisha katika mwili wenye kufa ambayo ni maisha kabla ya kuzaliwa. Nyakati zingine Yesu Kristo anatajwa kama Mwanzo.

Hapo mwanzo Mungu aliumba mbingu na dunia, **Mwa.** 1:1 (Musa 2:1).

Hapo mwanzo kulikuwako Neno, **Yn.** 1:1.

Mimi ndimi Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, **3 Ne.** 9:18.

Kristo ndiye mwanzo na mwisho, **M&M** 19:1. Agano jipya na lisilo na mwisho lilikuwako kutoka mwanzo, **M&M** 22:1. Mwanadamu alikuwa mwanzoni pamoja na Mungu, **M&M** 93:23, 29. Roho adilifu na kuu zilichaguliwa mwanzoni kuwa watawala, **M&M** 138:55.

Mwanangu wa Pekee alikuwa pamoja nami kutoka mwanzo, **Musa** 2:26.

Mwanzo, Kitabu cha Biblia. *Ona pia* Torati

Kitabu cha Mwanzo ndiyo kitabu cha kwanza cha Agano la Kale na kiliandikwa na Nabii Musa. Kinatoa historia ya mianzo mingi ya mambo, kama vile uumbaji wa dunia, kuwekwa kwa wanyama na mwanadamu juu ya dunia, anguko la Adamu na Hawa, kufunuliwa

kwa injili kwa Adamu, mwanzo wa makabila na jamii, asili ya lugha mbalimbali katika Babeli, na mwanzo wa familia ya Ibrahimu inayoongoza kuanzishwa kwa nyumba ya Israeli. Nafasi ya Yusufu kama mhifadhi wa Israeli inadhihirishwa katika Mwanzo.

Ufunuo wa siku za mwisho unathibitisha na kubainisha taarifa iliyoandikwa katika Mwanzo (1 Ne. 5; Eth. 1; Musa 1–8; Ibr. 1–5).

Katika Kitabu cha Mwanzo, mlango wa 1–4 inahusisha uumbaji wa ulimwengu na kukua kwa familia ya Adamu. Mlango wa 5–10 inaandika historia ya Nuhu. Mlango wa 11–20 inamtaja Ibrahimu na familia yake hadi wakati wa Isaka. Mlango wa 21–35 inafuatilia familia ya Isaka. Mlango wa 36 unasimulia juu ya Esau na familia yake. Mlango wa 37–50 inasimulia juu ya familia ya Yakobo na kutoa historia ya Yusufu kuuzwa Misri na nafasi yake katika kuiokoa nyumba ya Israeli.

Mwenyezi. *Ona pia* Mungu, Uungu

Tabia ya kiungu ya kuwa na uwezo wote (Mwa. 18:14; Alma 26:35; M&M 19:1–3).

Mwili. *Ona pia* Hali ya Kufa, enye Kufa; Mauti ya Kimwili; Nafsi; Ufufuko

Mwili wenye kufa, umbile la mwili, wa nyama na mifupa liliumbwa katika mfano wa Mungu ambalo limeunganishwa pamoja na roho ili kufanya mtu aliye hai. Miili halisi ya wanaume na wanawake wote itaunganishwa tena milele pamoja na roho zao katika Ufufuko. Maandiko wakati mwingine huielezea mwili na roho zilizoungana pamoja kama nafsi (Mwa. 2:7; M&M 88:15; Musa 3:7, 9, 19; Ibr. 5:7).

Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, **Mwa.** 2:7 (Musa 3:7).

Nishikeni, na mwone kwa maana roho haina mwili na mifupa, **Lk.** 24:39. Nautesa mwili wangu na kuutumikisha, **1 Kor.** 9:27. Kuna mwili wa asili, na kuna mwili wa kiroho, **1 Kor.** 15:44. Mwili pasipo roho umekufa, **Yak. (Bib.)** 2:26.

Mwili wenye kufa utafufuliwa kama mwili usio kufa, **Alma** 11:43–45. Kila sehemu ya mwili itarejeshwa, **Alma** 41:2. Yesu aliuonyesha mwili wake uliofufuka kwa Wanefi, **3 Ne.** 10:18–19; 11:13–15.

Baba anao mwili wa nyama na mifupa unaoshikika kama wa mwanadamu; na Mwana pia, **M&M** 130:22.

Mungu aliwaumba mwanamume na mwanamke katika mfano wa mwili wake yeye mwenyewe, **Musa** 6:9 (Mwa. 9:6).

Mwinjilisti. *Ona pia* Baraka za Kipatriaki; Kipatriaki, Patriaki

Mtu ashuhudiaye au atangazaye habari njema ya injili ya Yesu Kristo. Joseph Smith alifundisha kwamba mwinjilisti ndiye patriaki. Mapatriaki huitwa na kutawazwa chini ya maelekezo ya Mitume Kumi na Wawili ili kutoa baraka maalumu ziitwazo baraka za kipatriaki.

Bwana huwaita watu wengine kuwa Mitume, na wengine manabii, na wengine wainjilisti, **Efe.** 4:11. Fanya kazi ya Uinjilizti, **2 Tim.** 4:5.

Tunaamini katika Mitume, manabii, wachungaji, walimu, na wainjilisti, **M ya I** 1:6.

Mwisho wa Ulimwengu. *Ona* Ulimwengu—Mwisho wa ulimwengu

Mwokozi. *Ona pia* Yesu Kristo

Mtu mwenye kuokoa. Yesu Kristo, kwa njia ya upatanisho Wake, ametoa ukombozi na wokovu kwa wanadamu wote. Yesu Kristo ni Mwokozi wa wanadamu kwa sababu yeye aliwaokoa wote kutoka utumwa wa mauti na wenye kutubu kutokana na adhabu za dhambi. "Mwokozi" ni jina na cheo cha Yesu Kristo.

Bwana ndiye mwamba wangu na mwokozi wangu, **2 Sam.** 22:2 (Zab. 18:2; 144:2). Bwana ni nuru yangu na

wokovu wangu, **Zab.** 27:1 (Ku. 15:1–2; 2 Sam. 22:2–3). Ndiwe msaada wangu na mwokozi wangu, **Zab.** 40:17 (Zab. 70:5). Mimi ndimi Bwana; na zaidi yangu Mimi hapana mwokozi, **Isa.** 43:11 (M&M 76:1).

Utamwita jina lake Yesu: maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake kutoka katika dhambi zao, **Mt.** 1:21. Kwenu amezaliwa leo Mwokozi, ambaye ndiye Kristo Bwana, **Lk.** 2:11. Mungu aliupenda ulimwengu hata Mwanawe wa Pekee akaja kuwaokoa wanadamu, **Yn.** 3:16–17. Hapana jina jingine zaidi ya Kristo ambalo kwalo wanadamu wanaweza kuokolewa, **Mdo.** 4:10–12 (2 Ne. 25:20; Mos. 3:17; 5:8; M&M 18:23; Musa 6:52). Mwokozi atakuja kutoka Sayuni, **Rum.** 11:26. Kutoka mbinguni tunamtazamia Mwokozi, Bwana Yesu Kristo, **Flp.** 3:20. Baba amemtuma Mwana kuwa Mwokozi wa ulimwengu, **1 Yoh.** 4:14.

Bwana amemwinua Masiya, Mwokozi wa ulimwengu, **1 Ne.** 10:4. Mwanakondoo wa Mungu ndiye Mwokozi wa ulimwengu, **1 Ne.** 13:40. Ufahamu juu ya Mwokozi utaenea kote katika kila taifa, koo, lugha na watu, **Mos.** 3:20. Kristo ilibidi afe ili wokovu uweze kuja, **Hel.** 14:15–16.

Kuhesabiwa haki na utakaso kupitia Mwokozi ni haki na kweli, **M&M** 20:30–31. Mimi ndimi Yesu Kristo, Mwokozi wa ulimwengu, **M&M** 43:34. Watakatifu walimshukuru Mwana wa Mungu kama Mkombozi wao na Mwokozi wao, **M&M** 138:23.

Mwanangu wa Pekee ndiye Mwokozi, **Musa** 1:6. Kadiri wengi watakavyoamini katika Mwana na kutubu dhambi zao wataokolewa, **Musa** 5:15.

Mtetezi. *Ona pia* Yesu Kristo

Yesu Kristo ni Mtetezi wetu kwa Baba (Moro. 7:28) na hutuombea Kwake.

Yesu Kristo ni Mtetezi wetu kwa Baba, **1 Yoh.** 2:1 (M&M 110:4).

Yesu anawaombea wote, **2 Ne.** 2:9 (Ebr. 7:25). Yesu alipata ushindi juu ya mauti, uliompa uwezo wa kuwaombea watoto wa watu, **Mos.** 15:8.

Mimi ni mtetezi wenu kwa Baba, **M&M** 29:5. Yesu Kristo anawatetea teto zenu, **M&M** 45:3–5.

Mwonaji. *Ona pia* Nabii; Urimu na Thumimu

Mtu aliyeruhusiwa na Mungu kuona kwa macho ya kiroho mambo yale ambayo Mungu ameyaficha kwa ulimwengu (Musa 6:35–38). Yeye ni mfunuzi na nabii (Mos. 8:13–16). Katika Kitabu cha Mormoni, Amoni alifundisha kwamba mwonaji pekee aliweza kutumia vitafsiri maalumu, au Urimu na Thumimu (Mos. 8:13; 28:16). Mwonaji hujua yaliyopita, yaliyopo, na yajayo. Zamani, nabii mara kwa mara aliitwa mwonaji (1 Sam. 9:9; 2 Sam. 24:11).

Joseph Smith ndiye mwonaji mkuu wa siku za mwisho (M&M 21:1; 135:3). Kwa nyongeza, Urais wa Kwanza na Baraza la wale Kumi na Wawili wanakubalika kama manabii, waonaji, na wafunuzi.

Hawa ni watu waasi, ambao huwaambia waonaji, Msione; na kwa manabii, Msitoe unabii, **Isa.** 30:9–10.

Nabii bora nitamwinua kutoka tunda la viuno vyako, **2 Ne.** 3:6–15.

Hapa ndipo penye hekima; ndiyo, kuwa mwonaji, mfunuzi, mfasiri, na nabii, **M&M** 107:92. Bwana alimteua Hyrum Smith kuwa nabii, mwonaji, na mfunuzi kwa Kanisa, **M&M** 124:91–94.

Mwongofu, Uongofu. *Ona pia* Mwanafunzi; Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena

Mtu kubadili imani, moyo, na maisha kwa kukubali na kufuata mapenzi ya Mungu (Mdo. 3:19).

Uongofu unajumuisha uamuzi wa makusudi wa mtu kuacha njia zake za zamani na kubadilika na kuwa mfuasi wa Kristo. Toba, ubatizo kwa ajili ya ondoleo la dhambi, mapokezi ya Roho Mtakatifu kwa kuwekewa juu mikono, na imani endelevu kwa Bwana Yesu Kristo hufanya uongofu uwe mkamilifu.

Mtu wa asili atabadilika na kuwa mtu mpya aliyetakaswa na aliye safi, aliyezaliwa tena katika Kristo Yesu (2 Kor. 5:17; Mos. 3:19).

Watu lazima waongoke na kuwa kama watoto wadogo, **Mt.** 18:3 (Mos. 3:19). Utakapoongoka, waimarishe ndugu zako, **Lk.** 22:32. Waliolipokea neno lake kwa furaha walibatizwa, **Mdo.** 2:37–41. Mwongoeni mwenye dhambi hata atoke katika njia zake za upotevu, **Yak. (Bib.)** 5:20.

Enoshi aliongolewa, **Eno.** 1:2–5. Maneno ya mfalme Benjamini yalileta mabadiliko makubwa ndani ya watu, **Mos.** 5:2 (Alma 5:12–14). Wanadamu wote ni lazima wazaliwe upya, ndiyo, wazaliwe kwa Mungu, **Mos.** 27:25. Alma na wana wa Mosia waliongolewa, **Mos.** 27:33–35. Baba wa Lamoni aliongolewa, **Alma** 22:15–18. Kwa uwezo na neno la Mungu, wameongolewa kwa Bwana, **Alma** 53:10. Toba huleta badiliko la moyo, **Hel.** 15:7. Kadiri wengi walivyoongolewa kwa kweli walionyesha kwamba walijiliwa na nguvu na Roho wa Mungu, **3 Ne.** 7:21. Kwa sababu ya imani yao katika Kristo wakati wa uongofu wao, walibatizwa kwa moto na kwa Roho Mtakatifu, **3 Ne.** 9:20.

Wataendelea mbele na kufundisha toba, na wengi wataongolewa, **M&M** 44:3–4.

Mzaliwa Pekee. *Ona pia* Yesu Kristo; Zaliwa

Jina jingine la Yesu Kristo. Yeye ni Mwana Mzaliwa Pekee wa Baba (Lk. 1:26–35; Yn. 1:14; 3:16; 1 Ne. 11:18–20; 2 Ne. 25:12; Alma 7:10; 12:33; Musa 7:62).

Mzaliwa wa Kwanza. *Ona pia* Haki ya Kuzaliwa; Yesu Kristo

Katika wakati wa mapatriaki wa kale, mtoto wa kiume wa kwanza ndiye aliyepokea haki ya uzaliwa wa kwanza (Mwa. 43:33) na hivyo alirithi uongozi wa familia mara baada ya kifo cha baba. Mzaliwa wa kwanza alipaswa kuwa mwenye kustahili ili kutwaa wajibu huu (1 Nya. 5:1–2) na angeweza kupoteza haki ya mzaliwa kwa kuwa mtu asiye wa haki.

Chini ya sheria ya Musa, mtoto wa kiume wa kwanza aliheshimika kama mali ya Mungu. Mzaliwa wa kwanza alipokea sehemu mbili ya mali ya baba yake (Kum. 21:17). Baada ya kifo cha baba yake, yeye aliwajibika kwa matunzo ya mama yake na dada zake.

Wanyama madume wazaliwa wa kwanza nao pia walikuwa mali ya Mungu. Wanyama waliokuwa safi walitumika kwa kutolea dhabihu, wakati wanyama walio kuwa siyo safi waliweza kukombolewa au kuuzwa au kuchinjwa (Ku. 13:2, 11–13; 34:19–20; Law. 27:11–13, 26–27).

Mzaliwa wa kwanza alisimama badala ya Yesu Kristo na huduma yake duniani, akiwakumbusha watu kwamba Masiya mkuu angelikuja (Musa 5:4–8; 6:63).

Yesu alikuwa mzaliwa wa kwanza kati ya watoto wa kiroho wa Baba yetu wa Mbinguni, Mzaliwa Pekee wa Baba katika mwili, na ndiye wa kwanza kufufuka kutoka kwa wafu katika Ufufuko (Kol. 1:13–18). Watakatifu waaminifu wanakuwa waumini wa Kanisa la Mzaliwa wa Kwanza milele (M&M 93:21–22).

Mzaliwa wa kwanza katika wanao waume utanipa mimi, **Ku.** 22:29. Nikajiwekea wakfu wazaliwa wa kwanza wote wa Israeli, **Hes.** 3:13.

Yeye aweza kuwa mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi, **Rum.** 8:29. Amletapo mzaliwa wa kwanza ulimwenguni, **Ebr.** 1:6.

Hao ndiyo wao walio Kanisa la Mzaliwa wa Kwanza, **M&M** 76:54, 94.

Ulitunukiwa juu yangu kutoka kwa mababu, hata haki ya mzaliwa wa kwanza, **Ibr.** 1:3.

Mzee. *Ona pia* Ukuhani; Ukuhani wa Melkizedeki

Neno mzee limetumiwa katika njia tofauti katika Biblia. Katika Agano la Kale mara nyingi limetumiwa kwa watu

walio na umri mkubwa katika kabila, ambalo kwa kawaida walikuwa wameaminiwa kwa mambo ya kiutawala (Mwa. 50:7; Yos. 20:4; Rut. 4:2; Mt. 15:2). Umri na uzoefu wao ulifanya ushauri wao kuwa wenye thamani. Nafasi yao haikuwa lazima kwa wito wa ukuhani.

Walikuwepo pia wazee waliotawazwa katika ukuhani wa Melkizedeki katika Agano la Kale (Ku. 24:9–11). Katika Agano Jipya, wazee wametajwa kama ni ofisi ya ukuhani katika kanisa (Yak. [Bib.] 5:14–15). Miongoni mwa Wanefi walikuwepo pia wazee waliotawazwa katika ukuhani (Alma 4:7, 16; Moro. 3:1). Katika kipindi hiki, Joseph Smith na Oliver Cowdery ndiyo walikuwa wazee wa kwanza kutawazwa (M&M 20:2–3).

Mzee sasa ni cheo kilichotolewa kwa wote wanaoshikilia ukuhani wa Melkizedeki. Kwa mfano, wamisionari wanaume wote hujulikana kama wazee. Pia, Mtume ni mzee, na ni sahihi kusema juu ya washiriki wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili au Akidi ya Sabini kwa cheo hiki (M&M 20:38; 1 Pet. 5:1). Wajibu wa wazee waliotawazwa katika Kanisa leo umetolewa katika ufunuo katika siku za mwisho (M&M 20:38–45; 42:44; 46:2; 107:12).

Musa aliwaandikia wazee wote wa Israeli, **Kum.** 31:9.

Barnaba alipeleka msaada kwa wazee wa kanisa, **Mdo.** 11:30. Wazee walitawazwa katika kila kanisa, **Mdo.** 14:23 (Tit. 1:5). Waiteni wazee wamwombee mgonjwa, **Yak. (Bib.)** 5:14.

Wazee walitawazwa kwa kuwekewa mikono, **Alma** 6:1.

Wazee watawabariki watoto, **M&M** 20:70. Wazee wataendesha mikutano kwa Roho Mtakatifu, **M&M** 46:2. Wazee watatoa hesabu ya usimamizi wao, **M&M** 72:5. Wazee watahubiri injili kwa mataifa, **M&M** 133:8.

Mzee wa Siku. *Ona* Adamu

Mzeituni. *Ona pia* Israeli; Mafuta

Mti maarufu katika Israeli na tegemeo muhimu la kilimo katika nchi za Biblia. Hupandwa kwa ajili ya kuni zake, matunda, na mafuta. Mzeituni umetumika mara kwa mara katika maandiko ili kuashiria nyumba ya Israeli.

Nyumba ya Israeli inalinganishwa na mti wa mzeituni ambao matawi yake yamevunjika na kutawanywa, **1 Ne.** 10:12 (1 Ne. 15:12). Bwana alilinganisha nyumba ya Israeli na mti wa mzeituni uliopandwa, **Yak. (KM)** 5–6.

Joseph Smith aliita ufunuo katika sehemu ya 88 jani la mzeituni, **M&M** 88 kichwa cha habari. Mtu maarufu aliwaambia watumishi wake kwenda katika shamba lake la mizabibu na kupanda miti ya mizeituni kumi na miwili, **M&M** 101:43–62.

Mzozo. *Ona* Ushindani

Naamani. *Ona pia* Elisha

Katika Agano la Kale, ni kapteni wa jeshi la Shamu. Pia alikuwa mkoma. Kupitia imani ya mtumishi wake wa kike wa Kiisraeli alikwenda Israeli kumwona nabii Elisha. Aliponywa ukoma kwa kujinyenyekeza yeye mwenyewe na kuoga mara saba katika mto Yordani kama nabii Elisha alivyomwelekeza (2 Fal. 5:1–19; Lk. 4:27).

Nabii. *Ona pia* Mwonaji; Rais; Toa unabii, Unabii; Ufunuo

Mtu aliyeitwa na kuzungumza kwa niaba ya Mungu. Kama mjumbe wa Mungu, nabii hupokea amri, unabii, na mafunuo kutoka kwa Mungu. Wajibu wake ni kuyajulisha mapenzi ya Mungu na kuyatambulisha mapenzi na tabia za kweli za Mungu kwa wanadamu na kuonyesha maana ya matendo Yake kwao. Nabii hukemea dhambi na hutabiri matokeo yake. Yeye ni mhubiri wa haki. Wakati mwingine, manabii wanaweza kupata mwongozo kutoka kwa Mungu wa kutabiri mambo yatakayotokea baadaye kwa manufaa ya wanadamu. Wajibu wake wa msingi, hata hivyo, ni kutoa ushuhuda juu ya Kristo. Rais wa

Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho ndiye nabii wa Mungu duniani siku hizi. Washiriki wa Urais wa Kwanza na Mitume Kumi na Wawili wanakubalika kama ni manabii, waonaji, na wafunuzi.

Ningependa kwa Mungu kwamba watu wote wa Bwana wangekuwa manabii, **Hes.** 11:29. Kama akiwapo nabii, Mimi Bwana nitajifunua kwake katika maono, **Hes.** 12:6. Bwana aliwashuhudia Israeli kwa njia ya manabii wote, **2 Fal.** 17:13 (2 Nya. 36:15–16; Yer. 7:25). Nilikutawaza kuwa nabii kwa mataifa, **Yer.** 1:5, 7. Atawafunulia siri yake watumishi wake manabii, **Amo.** 3:7.

Alisema kwa kinywa cha manabii wake watakatifu, **Lk.** 1:70 (Mdo. 3:21). Manabii wote walimshuhudia Kristo, **Mdo.** 10:43. Mungu ameweka manabii katika Kanisa, **1 Kor.** 12:28 (Efe. 4:11). Kanisa limejengwa juu ya msingi wa Mitume na Manabii, **Efe.** 2:19–20.

Watu wameyakataa maneno ya manabii, **1 Ne.** 3:17–18 (2 Ne. 26:3). Kwa njia ya Roho mambo yote hujulikana kwa manabii, **1 Ne.** 22:1–2. Kristo alikuja kwa Wanefi ili kutimiza yale yote aliyosema kwa vinywa vya manabii wake watakatifu, **3 Ne.** 1:13 (M&M 42:39).

Wale ambao hawatatii maneno ya manabii watakatiliwa mbali, **M&M** 1:14. Wale wenye kuyaamini maneno ya manabii wanao uzima wa milele, **M&M** 20:26. Neno la nabii mtalipokea, kama kwamba kutoka kinywani mwangu mimi mwenyewe, **M&M** 21:4–6. Mafunuo na amri kwa Kanisa huja tu kupitia kwa mtu aliyeteuliwa, **M&M** 43:1–7. Kazi ya Rais ni kuliongoza Kanisa lote na kuwa kama Musa, kuwa nabii, **M&M** 107:91–92.

Tunaamini katika manabii, **M ya I** 1:6.

Nabii Mwanamke. *Ona pia* Toa unabii, Unabii

Mwanamke ambaye amepokea ushuhuda wa Yesu na anayo roho ya ufunuo. Nabii mwanamke hana ukuhani wala funguo zake. Ingawa ni wanawake wachache tu katika maandiko wanaitwa manabii wengi walitoa unabii, kama Rebeka, Ana, Elisabeti, na Maria.

Miriamu aliitwa nabii mwanamke, **Ku.** 15:20. Debora aliitwa nabii mwanamke, **Amu.** 4:4. Hulda aliitwa nabii mwanamke, **2 Fal.** 22:14 (2 Nya. 34:22).

Ana aliitwa nabii mwanamke, **Lk.** 2:36.

Nafsi. *Ona pia* Mwili; Roho

Maandiko huzungumza juu ya nafsi katika njia tatu: (1) viumbe roho, kabla ya kuzaliwa katika mwili wenye kufa na baada ya kufa (Alma 40:11–14; Ibr. 3:23); (2) roho na mwili viliungana katika mwili wenye kufa, (M&M 88:15; Ibr. 5:7); na (3) mtu aliye katika mwili usiokufa, mtu aliyefufuka ambaye roho na mwili vimeungana na kamwe haviwezi kutengana (2 Ne. 9:13; M&M 88:15–16).

Damu inafanya upatanisho kwa ajili ya nafsi, **Law.** 17:11. Hunihuisha nafsi yangu, **Zab.** 23:1–3.

Wewe mpende Bwana Mungu wako kwa nafsi yako yote, **Mt.** 22:37 (Mk. 12:30).

Ibilisi huzidanganya nafsi zao, **2 Ne.** 28:21. Mtolee nafsi yako yote kama sadaka kwake, **Omni** 1:26. Neno linaanza kuikuza nafsi yangu, **Alma** 32:28. Nafsi yake kamwe haitaona njaa wala kiu, **3 Ne.** 20:8. Mkate na maji ya sakramenti vimetakaswa kwa roho za wale watakaoula, **Moro.** 4–5 (M&M 20:77–79).

Watenda kazi katika ufalme huleta wokovu kwa nafsi zao kwa njia ya utumishi wao, **M&M** 4:2, 4. Thamani ya nafsi ni kuu, **M&M** 18:10.

Mlizaliwa duniani kwa maji, damu, na roho, na hivyo mkawa nafsi hai, **Musa** 6:59.

Thamani ya nafsi: Watu wote ni watoto wa Kiroho wa Mungu. Anamjali kila mtoto Wake na humchukulia kuwa kila mmoja ni muhimu. Kwa sababu ni watoto Wake, wanao uwezekano wa kuwa kama Yeye. Kwa sababu hiyo, ni wa thamani kubwa.

Kuna shangwe kwa ajili ya mwenye

dhambi mmoja anayetubu, **Lk.** 15:10. Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe Pekee, **Yn.** 3:16.

Hawakuweza kuvumilia kwamba nafsi yoyote ya mwanadamu iangamie, **Mos.** 28:3. Je, si nafsi kwa wakati huu inathamani kwa Mungu kama nafsi itakavyokuwa wakati wa kuja kwake, **Alma** 39:17.

Kitu cha thamani zaidi kwako ni kuzileta nafsi kwangu, **M&M** 15:6. Kumbuka thamani ya nafsi ni kubwa mbele za Mungu, **M&M** 18:10–15.

Hii ndiyo kazi na utukufu wangu—kuleta mwili usiokufa na uzima wa milele wa mwanadamu, **Musa** 1:39.

Naftali. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Ni wa sita kati ya wana kumi na wawili wa Yakobo na ni mtoto wa pili wa Bilha, mjakazi wa Raheli (Mwa. 30:7–8). Naftali alikuwa na wana wanne (1 Nya. 7:13).

Kabila la Naftali: Baraka za Yakobo juu ya Naftali zimeandikwa katika Mwanzo 49:21. Baraka za Musa juu ya kabila hilo zimeandikwa katika Kumbukumbu 33:23.

Nahumu

Nabii wa Agano la Kale wa Galilaya aliyeandika unabii wake wakati fulani kati ya mwaka 642 na 606 K.K.

Kitabu cha Nahumu: Mlango wa 1 huzungumzia juu ya kuunguzwa kwa dunia wakati wa Ujio wa Pili na juu ya huruma na uwezo wa Bwana. Mlango wa 2 huelezea juu ya angamizo la Ninawi, ambalo ni kivuli cha kile kitakachokuja katika siku za mwisho. Mlango wa 3 unaendelea kutaja angamizo la kuhuzunisha la Ninawi.

Najisi. *Ona* Sio mcha mungu

Naomi. *Ona pia* Rutu

Katika Agano la Kale, ni mwanamke mwaminifu na mke wa Elimeleki (Rut. 1–4). Elimeleki na Naomi walichukua familia yao kwenda Moabu ili kuepuka njaa. Baada ya Elimeleki na wanae wawili kufa, Naomi alirudi Bethlehemu pamoja na mkwewe Rutu.

Nasaba. *Ona pia* Batiza, Ubatizo—Ubatizo kwa ajili ya wafu; Familia; Ibada—Ibada zifanywazo kwa niaba ya wafu; Kitabu cha Ukumbusho; Wokovu; Wokovu kwa ajili ya Wafu

Kumbukumbu iliyoandikwa kufuatia mstari wa uzao katika familia. Ambapo ofisi za ukuhani au baraka fulani zilizuiliwa kwa familia fulani tu, nasaba katika maandiko zilikuwa muhimu sana (Mwa. 5; 10; 25; 46; 1 Nya. 1–9; Ezra 2:61–62; Neh. 7:63–64; Mt. 1:1–17; Lk. 3:23–38; 1 Ne. 3:1–4; 5:14–19; Yar. 1:1–2). Katika Kanisa lililorejeshwa siku hizi, waumini wa Kanisa wanaendelea kufuatilia mstari wa uzao wa familia zao, kwa upande mmoja ili kuwatambua kiusahihi walengwa wao waliofariki ili waweze kufanya ibada za wokovu kwa niaba ya walengwa wao. Ibada hizi zipo kwa ajili ya watu wale waliofariki ambao wanaikubali injili ya Yesu Kristo katika ulimwengu wa roho (M&M 127–128).

Nathanaeli. *Ona pia* Bartholomayo

Mtume wa Kristo na rafiki wa Filipo katika Agano Jipya (Yn. 1:45–51). Alitoka Kana ya Galilaya (Yn. 21:2). Kristo alisema kwamba Nathanaeli alikuwa Mwisraeli asiye na hila (Yn. 1:47). Yeye na Bartholomayo wanafikiriwa kuwa ni mtu huyo huyo mmoja (Mt. 10:3; Mk. 3:18; Lk. 6:14; Yn. 1:43–45).

Nathani. *Ona pia* Daudi

Nabii wa Agano la Kale katika wakati wa Mfalme Daudi. Daudi alipojitolea kujenga hekalu la Bwana, Bwana alimwelekeza Nathani kumwambia Daudi asijenge. Nathani pia alimkemea Daudi kwa kusababisha mauti ya Uria, mmoja wa askari wake, na kwa kumchukua mke wa Uria, Bathsheba (2 Sam. 12:1–15; M&M 132:38–39). Sadoki, pamoja na Nathani, walimpaka mafuta

mfalme Sulemani mwana wa Daudi (1 Fal. 1:38–39, 45).

Nauvoo, Illinois (Marekani)

Mji ulioanzishwa na Watakatifu wa siku za Mwisho katika mwaka 1839 katika jimbo la Illinois. Uko kando ya Mto Mississippi, karibu maili 200 (kilomita 320) juu ya mto kutoka St. Louis.

Kutokana na mateso katika jimbo la Missouri, Watakatifu walihamia karibu maili 200 (kilometa 320) kaskazini mashariki, ng'ambo ya Mto Mississippi, na ndani ya Illinois, mahali ambapo walipata hali iliyowavutia zaidi. Hatimaye, Watakatifu walinunua ardhi karibu na mji ambao haukuendelea wa Commerce. Nchi hii kwa kweli ilikuwa msitu uliojaa maji pamoja na majengo machache ya kawaida. Watakatifu waliyakausha maji katika ardhi na wakajenga majumba. Joseph Smith aliihamishia familia yake katika nyumba ndogo ya mbao. Jina la Commerce la mji huo likabadilishwa kuwa Nauvoo, kwa neno la Kiebrania maana yake "mrembo."

Sehemu kadhaa za Mafundisho na Maagano ziliandikwa Nauvoo (M&M 124–129; 132; 135). Watakatifu waliambiwa kujenga hekalu katika Nauvoo (M&M 124:26–27). Walijenga hekalu na kuunda vigingi vya Sayuni kabla ya kufukuzwa kutoka majumbani mwao katika mwaka 1846. Kama matokeo ya mateso haya, Watakatifu waliondoka katika eneo na kufanya safari yao kwenda magharibi.

Nazarethi. *Ona pia* Yesu Kristo

Kijiji kati kati ya vilima vya magharibi ya Bahari ya Galilaya. Nazarethi kulikuwa nyumbani kwa Yesu wakati wa mwanzoni. (Mt. 2:23). Yesu alifundisha katika sinagogi huko Nazarethi na akatamka kwamba Yeye alikamilisha unabii katika Isaya 61:1–2 (Mt. 13:54–58; Mk. 6:1–6; Lk. 4:16–30).

Nchi ya Ahadi

Nchi ambazo Bwana huahidi kuwa kama urithi kwa wafuasi wake waaminifu, na mara kwa mara pia kwa wazao wao. Kuna nchi nyingi za ahadi. Mara kwa mara katika Kitabu cha Mormoni nchi ya ahadi inayozungumzwa ni nchi ya Marekani.

Uzao wako nitawapa nchi hii, **Mwa.** 12:7 (Ibr. 2:19). Nitakupa wewe na uzao wako nchi ya Kanaani, **Mwa.** 17:8 (Mwa. 28:13). Musa alielezea mipaka ya nchi kwa ajili ya Israeli katika Kanaani, **Hes.** 34:1–12 (Hes. 27:12).

Mtaongozwa hadi nchi ya ahadi, **1 Ne.** 2:20 (1 Ne. 5:5). Bwana huwaongoza walio waadilifu katika nchi nzuri, **1 Ne.** 17:38. Kama wazao wa Lehi watashika amri, watastawi katika nchi ya ahadi, **2 Ne.** 1:5–9. Israeli itarudi katika nchi zao za ahadi, **2 Ne.** 24:1–2 (Isa. 14:1–2). Taifa lolote litakaloimiliki nchi hii ya ahadi yapasa limtumikie Mungu, au watafagiliwa mbali, **Eth.** 2:9–12.

Hii ni nchi ya ahadi na ni mahali pa mji wa Sayuni, **M&M** 57:2. Yuda inaweza kuanza kurudi katika nchi ya Ibrahimu, **M&M** 109:64.

Yerusalemu Mpya itajengwa katika bara la Marekani, **M ya I** 1:10.

Ndimi, Kipawa cha. *Ona* Ulimi; Vipawa vya Roho

Kipawa cha Roho Mtakatifu ambacho huwaruhusu watu walio na mwongozo wa kiuungu kunena katika, au kuelewa, au kutafsiri lugha ngeni. Tunaamini katika kipawa cha ndimi (M ya I 1:7).

Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, na wakaanza kunena kwa ndimi zingine, **Mdo.** 2:4. Mtu anenaye katika ndimi isiyojulikana hasemi na wanadamu, bali na Mungu, **1 Kor.** 14:1–5, 27–28. Ndimi ni ishara kwao wale wasioamini, **1 Kor.** 14:22–28.

Kisha waja ubatizo wa moto na wa Roho Mtakatifu; na ndipo mtakaponena kwa ndimi za malaika, **2 Ne.** 31:13–14. Amaleki aliwasihi watu wote kuamini katika kunena kwa ndimi, **Omni** 1:25.

Imetolewa kwa wengine kunena kwa ndimi; na mwingine kutafsiri ndimi, **M&M** 46:24–25 (1 Kor. 12:10; Moro. 10:8,

15–16). Na kipawa cha ndimi kimwagwe, **M&M** 109:36.

Ndoa, Oa, Olewa. *Ona pia* Familia; Talaka

Agano au mkataba wa kisheria kati ya mwanaume na mwanamke ambalo huwafanya kuwa mume na mke. Ndoa imeamriwa na Mungu (M&M 49:15).

Si vyema mtu huyo kuwa pekee yake, **Mwa.** 2:18 (Musa 3:18). Mwanamume ataambatana na mke wake, nao watakuwa mwili mmoja, **Mwa.** 2:24 (Mt. 19:5; Ibr. 5:18).

Aliowaunganisha Mungu, na mtu yeyote asiwatenganishe, **Mt.** 19:6 (Mk. 10:9). Katika siku za mwisho wengine watajitenga na imani, wakiwazuia watu kuoa au kuolewa, **1 Tim.** 4:1–3. Ndoa na iheshimiwe, **Ebr.** 13:4.

Bwana aliwaamuru wana wa Lehi kuoa mabinti za Ishmaili, **1 Ne.** 7:1, 5 (1 Ne. 16:7–8).

Mungu aliwaumba Adamu na Eva wawe mme na mke, **Musa** 3:7, 18, 21–25.

Agano Jipya na la Lisilo na Mwisho la Ndoa: Ndoa iliyofungwa chini ya sheria ya injili na ukuhani mtakatifu ni kwa maisha ya duniani na kwa milele. Wanaume na wanawake wenye kustahili wakiwa wamefungwa hivi hekaluni katika ndoa wanaweza kuendelea kuwa kama mume na mke kwa milele.

Yesu alifundisha sheria ya ndoa, **Lk.** 20:27–36. Walakini si mwanaume pasipo mwanamke katika Bwana, **1 Kor.** 11:11. Waume na wake ni warithi pamoja wa neema ya uzima, **1 Pet.** 3:7.

Lolote utakalolifunga duniani litafungwa mbinguni, **Hel.** 10:7 (Mt. 16:19).

Ili kupata daraja la juu kabisa la ufalme wa selestia, mtu lazima aingie katika agano jipya na lisilo na mwisho la ndoa, **M&M** 131:1–4. Kama mtu ataoa mke siyo kwa njia yangu mimi, agano na ndoa yao haitakuwa na nguvu wakifa, **M&M** 132:15. Kama mtu ataoa mke kwa njia ya neno langu na kwa agano jipya na lisilo na mwisho, na ikafungwa kwa Roho Mtakatifu wa Ahadi, itakuwa na nguvu kamili wawapo nje ya ulimwengu, **M&M** 132:19.

Ndoa ya imani mbili: Ndoa kati ya mwanamume na mwanamke wa imani za dini na desturi zilizo tofauti.

Hutamtwalia mwanangu mke katika binti za Wakanaani, **Mwa.** 24:3. Kama Yakobo anamtwaa mke katika binti za Hethi, maisha yangu yatanifaidia nini, **Mwa.** 27:46 (Mwa. 28:1–2). Israeli hataoa Wakaanani, **Kum.** 7:3–4. Israeli walioa na kuolewa na Wakanaani, wakaabudu miungu wa uongo, na wakalaaniwa, **Amu.** 3:1–8. Wake za Suleimani waliugeuza moyo wake kuabudu miungu ya uongo, **1 Fal.** 11:1–6. Hatutawaoza binti zetu kwa watu wa nchi, wala tusiwatwalie wana wetu binti zao, **Neh.** 10:30.

Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, **2 Kor.** 6:14.

Bwana aliweka alama Walamani wasipate kuchanganyika na kuamini katika mila zao zisizo sahihi, **Alma** 3:6–10.

Kama mtu akioa mke sio kwa njia yangu, agano na ndoa yao haina nguvu wakifa, **M&M** 132:15.

Wana wa wanadamu walijitwalia wake hata kama walivyojichagulia, **Musa** 8:13–15.

Ndoa ya wake wengi: Ndoa ya mume kwa wake wawili au zaidi walio hai. Ni sheria kwa mwanaume kuwa na mke mmoja tu, isipokuwa Bwana anaamuru vinginevyo kwa ufunuo (Yak. [KM] 2:27–30). Kwa ufunuo, ndoa ya wake wengi ilifanyika katika nyakati za Agano la Kale na katika siku za mwanzoni za Kanisa lililorejeshwa kwa maelekezo ya nabii ambaye alishikilia funguo za ukuhani (M&M 132:34–40, 45). Haifanyiki tena katika Kanisa (TR 1); leo, kuwa na zaidi ya mke mmoja kunamzuia mtu kuwa mwanachama katika Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Sarai alimtoa Hajiri kwa Abramu kama mke wake, **Mwa.** 16:1–11. Yakobo aliwapokea Lea na Raheli na wajakazi wao kama wakeze, **Mwa.** 29:21–28

(Mwa. 30:4, 9, 26). Kama mtu atajitwalia mke mwingine, hatampunguzia mali zake yule mke wa kwanza, **Ku.** 21:10. Daudi na wakeze wawili walipanda kwenda Hebroni, **2 Sam.** 2:1–2.

Ibrahimu, Isaka, na Yakobo walifanya lile ambalo waliamriwa katika kupokea wake wengi, **M&M** 132:37. Daudi na Sulemani hawakutenda dhambi katika lolote isipokuwa kwa mambo yale ambayo hawakupokea kutoka kwa Bwana, **M&M** 132:38–39.

Ndoa ya Hekaluni. *Ona* Ndoa, Oa, Olewa

Ndoa ya Wake Wengi. *Ona* Ndoa, Oa, Olewa—Ndoa ya wake wengi

Ndoto. *Ona pia* Ufunuo

Njia mojawapo ambayo Mungu hufunua mapenzi Yake kwa wanaume na wanawake duniani. Siyo ndoto zote ni mafunuo, hata hivyo. Ndoto za maongozi ya Mungu ni matunda ya imani.

Akaota ndoto, na tazama ngazi imefika mbinguni, **Mwa.** 28:12. Yusufu akaota ndoto, **Mwa.** 37:5. Bwana atasema naye katika ndoto, **Hes.** 12:6. Nebukadneza aliota ndoto, **Dan.** 2:1–3. Wazee wataota ndoto, **Yoe.** 2:28 (Mdo. 2:17).

Malaika wa Bwana akamtokea katika ndoto, **Mt.** 1:20 (Mt. 2:19).

Lehi aliandika mambo mengi aliyoyaona katika ndoto, **1 Ne.** 1:16. Lehi aliota ndoto, **1 Ne.** 8.

Ndugu. *Ona* Kaka, Ndugu

Nebukadneza. *Ona pia* Babeli, Babilonia; Danieli

Katika Agano la Kale, ni mfalme wa Babilonia (604–561 K.K.) aliyeishinda Yuda (2 Fal. 24:1–4) na akaizingira Yerusalemu (2 Fal. 24:10–11). Nabii Lehi aliamriwa kuikimbia Yerusalemu katika karibu mwaka 600 K.K. ili kuepuka kuchukuliwa mateka katika Babilonia (1 Ne. 1:4–13) wakati Nebukadneza alipomteka Mfalme Zedekia na watu (2 Fal. 25:1, 8–16, 20–22). Danieli alitafsiri ndoto ya Nebukadneza (Dan. 2; 4).

Neema. *Ona pia* Lipia dhambi, Upatanisho; Rehema, enye Rehema; Wokovu; Yesu Kristo

Nguvu yenye kuwezesha itokayo kwa Mungu ambayo huwaruhusu wanaume na wanawake kupata baraka katika maisha haya na kupata uzima wa milele na kuinuliwa baada ya kuonyesha imani, kutubu, na kufanya jitihada zao zilizo bora ili kushika amri. Msaada mtakatifu wa aina hii au nguvu hii hutolewa kwa njia ya rehema na upendo wa Mungu. Kila mtu mwenye mwili ufao anahitaji neema takatifu kwa sababu ya Anguko la Adamu na pia kwa sababu ya udhaifu wa mwanadamu.

Neema na kweli zilikuja kwa njia ya Yesu, **Yn.** 1:17. Kupitia neema ya Kristo, tutaokolewa, **Mdo.** 15:11 (Rum. 3:23–24; M&M 138:14). Tumepata kwa njia ya imani kuifikia neema yake, **Rum.** 5:2. Kwa neema mmeokolewa kwa njia ya imani, **Efe.** 2:8. Neema ya Mungu huleta wokovu, **Tit.** 2:11. Kwa ujasiri tukikaribie kiti cha neema, **Ebr.** 4:16. Mungu huwapa neema wanyenyekevu, **1 Pet.** 5:5.

Hakuna mtu awezaye kukaa katika uwepo wa Mungu bali kwa ustahili, rehema, na neema ya Masiya Mtakatifu, **2 Ne.** 2:8. Ni katika na kwa kupitia neema ya Mungu pekee wanadamu wanaokolewa, **2 Ne.** 10:24. Tunaokolewa kwa neema, baada ya kutenda yote tuwezayo, **2 Ne.** 25:23. Ni kwa neema kwamba tunao uwezo wa kufanya mambo haya, **Yak. (KM)** 4:7. Wanadamu wapate kurejeshwa kwa neema juu ya neema, kulingana na matendo yao, **Hel.** 12:24. Neema yangu inatosha kwa walio wasikivu na wote ambao hujinyenyekeza wenyewe, **Eth.** 12:26–27. Moroni aliomba kwamba Wayunani wapewe neema ili wapate kuwa na hisani, **Eth.** 12:36, 41. Kwa neema ya Mungu ninyi mu wakamilifu katika Kristo, **Moro.** 10:32–33.

Yesu alipokea neema juu ya neema, **M&M** 93:12–13, 20.

Nefi, Mwana wa Helamani. *Ona pia* Helamani, Mwana wa Helamani; Lehi, Mmisionari wa Kinefi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni nabii Mnefi na mmsionari.

Alikuwa ni mwana mkubwa wa Helamani, **Hel.** 3:21. Aliteuliwa kuwa mwamuzi mkuu, **Hel.** 3:37. Yeye na kaka wa Lehi waliwaongoa Walamani wengi katika injili, **Hel.** 5:18–19. Alizingirwa kwa moto na kufunguliwa gerezani, **Hel.** 5:20–52. Alisali juu ya mnara wake wa bustani, **Hel.** 7:6–10. Alifichua mauaji ya mwamuzi mkuu, **Hel.** 8:25–28; 9:1–38. Alipewa uwezo mkubwa na Bwana, **Hel.** 10:3–11. Aliomba njaa kwa Bwana na kukoma kwa njaa hiyo, **Hel.** 11:3–18.

Nefi, Mwana wa Lehi. *Ona pia* Lehi, Baba wa Nefi; Wanefi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana mwaminifu wa Lehi na Saria (1 Ne. 1:1–4; 2:5). Nefi alikuwa na imani thabiti katika neno la Mungu (1 Ne. 3:7) na akawa nabii mkubwa, mtunza kumbukumbu, na kiongozi wa watu wake.

Alikuwa mtiifu na alisali kwa imani, **1 Ne.** 2:16. Alirudi Yerusalemu kuchukua mabamba ya shaba nyeupe, **1 Ne.** 3–4. Alirudi Yerusalemu kwenda kuileta familia ya Ismaili nyikani, **1 Ne.** 7. Alipokea ufunuo ule ule ambao Lehi alipokea, **1 Ne.** 10:17–22; 11. Aliona katika ono hali ya baadaye ya watu wake na urejesho wa injili, **1 Ne.** 12–13. Alitafsiri ono la mti wa uzima, **1 Ne.** 15:21–36. Alivunja upinde wake lakini kwa njia ya imani aliweza kupata chakula, **1 Ne.** 16:18–32. Alijenga meli na wakasafiri hadi nchi ya ahadi, **1 Ne.** 17–18. Wanefi na Walamani walitengana, **2 Ne.** 5. Alitoa ushuhuda wa mwisho, **2 Ne.** 33.

Kitabu cha 1 Nefi: Mlango wa 1 hadi 18:8 inajishughulisha zaidi na kuondoka kwa nabii Lehi na familia yake kutoka Yerusalemu. Walisafiri kupitia kwenye jangwa kame hadi walipofika baharini. 1 Nefi 18:9–23 inaelezea juu ya safari yao kwenda nchi ya ahadi, kama walivyoelekezwa na Bwana, licha ya uasi wa Lamani na Lemueli. Mlango wa 19–22 inaelezea madhumuni ya Lehi ya kutunza kumbukumbu (1 Ne. 6; 19:18)—ili kuwashawishi watu wote kumkumbuka Bwana Mkombozi wao. Alimnukuu Isaya (1 Ne. 20–21) na akatafsiri ujumbe wa Isaya, kwa matumaini kwamba watu wote wapate kuja kumjua Yesu Kristo kama Mwokozi na Mkombozi wao (1 Ne. 22:12).

Kitabu cha 2 Nefi: Mlango wa 1–4 ina baadhi ya mafundisho na unabii wake wa mwisho kabla ya kifo chake, ikiwa ni pamoja na baraka juu ya wanawe na wazao wao. Mlango wa 5 unafafanua kwa nini Wanefi walijitenga wenyewe kutoka kwa Walamani. Wanefi walijenga hekalu, walifundisha torati ya Musa, na walitunza kumbukumbu. Mlango wa 6–10 ina maneno ya Yakobo, mdogo wa Nefi. Yakobo alirejea upya historia ya Yuda na alitoa unabii juu ya Masiya, baadhi yake yamechukuliwa kutoka katika maandiko ya nabii Isaya. Katika mlango wa 11–33. Nefi ameandika ushuhuda wake juu ya Kristo, ushuhuda wa Yakobo, unatoa unabii juu ya siku za mwisho, na milango kadhaa kutoka katika Agano la Kale Kitabu cha Isaya.

Mabamba ya Nefi: Ona Mabamba

Nefi, Mwana wa Nefi, Mwana wa Helamani. *Ona pia* Mwanafunzi; Nefi, Mwana wa Helamani

Mmoja wa wale wanafunzi Wanefi kumi na wawili waliochaguliwa na Yesu Kristo mfufuka katika Kitabu cha Mormoni (3 Ne. 1:2–3; 19:4). Nabii huyu alisali kwa bidii sana kwa Bwana kwa niaba ya watu wake. Nefi aliisikia sauti ya Bwana (3 Ne. 1:11–14). Nefi pia alitembelewa na malaika, aliwafukuza pepo wabaya, alimfufua kaka yake kutoka kwa wafu, na alitoa ushuhuda ambao hangeweza kukosa kuaminika (3 Ne. 7:15–19; 19:4). Nefi alitunza kumbukumbu ya kimaandiko (3 Ne. 1:2–3).

Kitabu cha 3 Nefi: Kitabu kilichoandikwa na Nefi, mwana wa Nefi, katika Kitabu cha Mormoni. Mlango wa 1–10

inaonyesha kutimilika kwa unabii juu ya kuja kwa Bwana. Ishara ya kuzaliwa kwa Kristo ilitolewa; watu wakatubu; lakini wakarudi kwenye uovu. Mwishowe tufani, matetemeko ya ardhi, dhoruba kali, na maangamizo makubwa yalikuwa ishara ya kifo cha Kristo. Mlango wa 11–28 inaandikwa ujio wa Kristo katika Marekani. Hii ndiyo sehemu muhimu ya Kitabu cha 3 Nefi. Maneno mengi ya Kristo yanafanana na mahubiri Yake yaliyoandikwa katika Biblia (kwa mfano, Mt. 5–7 na 3 Ne. 12–14). Mlango wa 29–30 ni maneno ya Mormoni kwa mataifa ya siku za mwisho.

Kitabu cha 4 Nefi: Kitabu hiki kina aya arobaini na tisa tu, zote ni katika mlango mmoja, hata hivyo inaelezea taarifa za karibu miaka mia tatu ya historia ya Wanefi (34–321 B.K.). Waandishi wa vizazi kadha wa kadha, ikiwa ni pamoja na Nefi, walichangia katika kumbu kumbu hii. Mstari wa 1–19 inazungumzia kwamba baada ya kuja kwa Kristo mfufuka Wanefi na Walamani wote waliongolewa katika injili. Amani, upendo, na maelewano vilitawala. Wanafunzi Wanefi watatu, ambao Kristo aliwaruhusu kubakia duniani hadi Ujio Wake wa Pili (3 Ne. 28:4–9), waliwahudumia watu. Nefi aliacha kumbukumbu hiyo kwa mwanawe Amosi. Mstari wa 19–47 ni kumbukumbu za utumishi wa Amosi (miaka 84) na ule wa mwanawe Amosi (miaka 112). Katika mwaka 201 B.K. kiburi kikaanza kusababisha matatizo miongoni mwa watu, ambao waligawanyika wenyewe katika madaraja na wakaanzisha makanisa ya uongo ili kupata faida (4 Ne. 1:24–34).

Mstari ya mwisho ya 4 Nefi inaonyesha kwamba watu walikuwa wamerudia tena kwenye uovu (4 Ne. 1:35–49). Katika mwaka 305 B.K., Amosi mwana wa Amosi alikufa na kaka yake Amaroni akazificha kumbukumbu takatifu zote kwa usalama. Amaroni baadaye alizikabidhisha kumbukumbu hizo kwa Mormoni, ambaye aliandika matukio mengi ya wakati wa uhai wake na kisha akazifanyia muhtasari (Morm. 1:2–4).

Nehemia

Muisraeli aliyekuwa mtu maarufu katika Babiloni katika Agano la Kale (alikuwa Mlawi au wa kabila la Yuda) aliyekuwa na ofisi ya mnyweshaji wa mfalme katika baraza la Artashasta, ambaye kutoka kwake alipata mamlaka ya kifalme yaliyomruhusu yeye kujenga upya kuta za Yerusalemu.

Kitabu cha Nehemia: Kitabu hiki ni mwendelezo wa kitabu cha Ezra. Kina maelezo juu ya maendeleo na ugumu wa kazi huko Yerusalemu kikifuatiwa na kurudi kwa Wayahudi kutoka utumwa wa Babilonia. Mlango wa 1–7 inasimulia juu ya safari ya kwanza ya Nehemia huko Yerusalemu na kujengwa upya kwa kuta za jiji licha ya upinzani mkubwa. Mlango wa 8–10 inaelezea marekebisho ya kidini na kijamii ambayo Nehemia alijaribu kuyatekeleza. Mlango wa 11–13 inatoa orodha ya majina ya wale wanaostahili na kutoa taarifa ya kuwekwa wakfu kwa ukuta. Mistari ya 4–31 ya mlango wa 13 inaandikwa juu ya safari ya pili ya Nehemia kwenda Yerusalemu baada ya kuwa mbali kwa miaka kumi na miwili.

Nehori. *Ona pia* Mpinga Kristo; Ukuhani wa uongo

Mtu mwovu katika Kitabu cha Mormoni. Nehori alikuwa mmoja wa watu wa kwanza kufanya ukuhani wa uongo miongoni mwa Wanefi. Baada ya kufundisha mafundisho ya uongo na kumwua Gidioni, Nehori aliuawa kwa ajili ya makosa yake ya jinai (Alma 1). Wafuasi wa Nehori waliendeleza matendo maovu na mafundisho yake kwa muda mrefu baada ya kufa kwa Nehori.

Alma na Amuleki walifungwa gerezani na mwamuzi aliyekuwa wa mfano wa Nehori, **Alma** 14:14–18. Watu waliouawa walikuwa ni wa taaluma ya Nehori, **Alma** 16:11. Wengi walikuwa

wa mfano wa Nehori, **Alma** 21:4. Idadi kubwa zaidi ya wale waliowaua ndugu zao walikuwa watu wa mfano wa Nehori, **Alma** 24:28.

Neno. *Ona* Yesu Kristo—Kuwepo kwa Kristo kabla ya kuzaliwa duniani

Neno la Hekima

Sheria ya afya iliyofunuliwa na Bwana kwa ajili ya manufaa ya kimwili na ya kiroho ya Watakatifu (M&M 89). Imekuwa ni kawaida kuiita kama Neno la Hekima. Bwana daima amekuwa akiwafundisha wafuasi wake kanuni za afya. Bwana alimfunulia Joseph Smith ni vyakula vya aina gani wale na vipi waviepuke, sambamba pamoja na ahadi ya baraka za kimwili na kiroho kwa kutii Neno la Hekima.

Usinywe mvinyo wala kileo, **Law.** 10:9. Mvinyo hudhihaki, na kileo huleta ugomvi, **Mit.** 20:1. Kileo kitakuwa kichungu kwao wakinywao, **Isa.** 24:9. Danieli hangejitia najisi mwenyewe kwa kula chakula na mvinyo wa mfalme, **Dan.** 1:8.

Kama mtu akilichafua hekalu la Mungu, Mungu naye atamharibu, **1 Kor.** 3:16–17. Walevi hawatarithi ufalme wa Mungu, **1 Kor.** 6:10 (Gal. 5:21).

Mtu yeyote akatazaye mtu asile nyama, huyo hakuagizwa na Mungu, **M&M** 49:18–21. Vitu vyote vinavyokuja duniani vitumiwe kwa hekima, siyo kwa ufujaji, **M&M** 59:20. Bwana amewashauri Watakatifu wasitumie mvinyo, kileo, tumbaku, na vinywaji vya moto, **M&M** 89:1–9. Majani ya mimea, matunda, nyama, na nafaka vimekubaliwa kwa matumizi ya mwanadamu na wanyama, **M&M** 89:10–17. Utii kwa Neno la Hekima huleta baraka za kimwili na kiroho, **M&M** 89:18–21.

Neno la Mungu. *Ona pia* Amri za Mungu; Maandiko; Ufunuo

Mafundisho, amri, au ujumbe kutoka kwa Mungu. Watoto wa Mungu wanaweza kulipata neno Lake moja kwa moja kwa njia ya ufunuo kupitia Roho au kutoka kwa watumishi Wake wateule (M&M 1:38).

Mwanadamu huishi kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Bwana, **Kum.** 8:3 (Mt. 4:4; M&M 84:43–44). Neno lako ni taa kwa miguu yangu, na ni mwanga kwa njia yangu, **Zab.** 119:105.

Wote walijazwa na Roho Mtakatifu na wakanena neno la Mungu kwa ujasiri, **Mdo.** 4:31–33.

Fimbo ya chuma ilikuwa ni neno la Mungu ambalo hutuongoza kwenye mti wa uzima, **1 Ne.** 11:25 (1 Ne. 15:23–25). Mlikufa ganzi, kwamba hamkuweza kuyasikia maneno yake, **1 Ne.** 17:45–46. Ole wake yule alikataaye neno la Mungu, **2 Ne.** 27:14 (2 Ne. 28:29; Eth. 4:8). Songa mbele, ukisherehekea neno la Mungu, **2 Ne.** 31:20 (2 Ne. 32:3). Kwa sababu ya kutoamini kwao hawakuweza kuelewa neno la Mungu, **Mos.** 26:3 (Alma 12:10). Waliyapekua maandiko kwa bidii, ili wapate kulijua neno la Mungu, **Alma** 17:2. Jaribu wema wa neno la Mungu, **Alma** 31:5. Alma alilinganisha neno la Mungu na mbegu, **Alma** 32:28–43.

Lolote watakalolisema wakiwa wanaongozwa na Roho Mtakatifu litakuwa ni neno la Mungu, **M&M** 68:4. Ishi kwa kila neno litakalo kinywani mwa Mungu, **M&M** 84:44–45.

Yeyote mwenye kulithamini neno langu, hatadanganywa, **JS—M** 1:37.

Nia

Welekevu wa akili; uwezo wa kufahamu fikira.

Umtumikie kwa moyo mkamilifu na kwa nia ya kumkubali, **1 Nya.** 28:9.

Mpende Bwana Mungu wako kwa akili zako zote, **Mt.** 22:37.

Kufikiria kimwili ni kifo; kufikiria kiroho ni uzima wa milele, **2 Ne.** 9:39. Sauti ya Bwana ilinijia akilini mwangu, **Eno.** 1:10. Neno likawa matokeo na nguvu zaidi akilini mwa watu kuliko upanga, **Alma** 31:5.

Nitakujulisha wewe akilini mwako,

M&M 8:2. Lichunguze katika akili yako, **M&M** 9:8. Acha taadhima ya milele na iwe akilini mwenu, **M&M** 43:34. Akili zenu katika wakati uliopita zilitiwa giza, **M&M** 84:54. Laleni vitandani mwenu mapema, amkeni mapema ili miili yenu na akili zenu zipate kutiwa nguvu, **M&M** 88:124.

Shetani hakujua mawazo ya Mungu, **Musa** 4:6. Bwana aliwaita watu wake Sayuni, kwa sababu walikuwa na moyo mmoja na nia moja, **Musa** 7:18.

Nikodemo. *Ona pia* Mafarisayo

Katika Agano Jipya, ni mtawala mwadilifu wa Wayahudi (labda wa Sanhedrini) na Mfarisayo (Yn. 3:1).

Aliongea na Yesu usiku, **Yn.** 3:1–21. Alimtetea Yesu kwa Mafarisayo, **Yn.** 7:50–53. Alileta manukato katika mazishi ya Yesu, **Yn.** 19:39–40.

Ninawi. *Ona pia* Ashuru; Yona

Katika Agano la Kale, ni mji mkuu wa Ashuru na kwa zaidi ya miaka mia mbili ulikuwa mji maarufu wa kibiashara katika kingo ya mashariki ya mto Tigri. Ulianguka wakati wa kushuka kwa ufalme wa Ashuru, 606 K.K.

Senakeribu, mfalme wa Ashuru, aliishi Ninawi, **2 Fal.** 19:36. Yona alitumwa kuhubiri toba kwa mji ule, **Yon.** 1:1–2 (Yon. 3:1–4). Watu wa Ninawi walitubu, **Yon.** 3:5–10.

Kristo aliitumia Ninawi kama mfano wa toba mbele ya Wayahudi, **Mt.** 12:41.

Nira. *Ona pia* Mwanafunzi

Chombo kinachovikwa kuzunguka shingo ya wanyama au watu ili kufungwa pamoja. Nira ya Kristo ni ishara ya uanafunzi, wakati nira ya utumwa ni ishara ya ukandamizaji.

Nira yangu ni rahisi, na mzigo wangu ni mwepesi, **Mt.** 11:29–30. Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, **2 Kor.** 6:14. Msinaswe kwa nira ya utumwa, **Gal.** 5:1.

Wala hatutamani kumleta yoyote kwenye nira ya utumwa, **Alma** 44:2.

Mateso ya Watakatifu ni nira ya chuma, kamba imara, na minyororo ya jehanamu, **M&M** 123:1–3, 7–8.

Nje Gizani. *Ona* Jehanamu

Njia. *Ona pia* Tembea, Tembea na Mungu; Yesu Kristo

Mapito au uelekeo ambao mtu huufuata. Yesu alisema ya kuwa Yeye ni njia (Yn. 14:4–6).

Uzishike amri za Bwana upate kwenda katika njia zake, **Kum.** 8:6. Mfundishe mtoto katika njia zimpasazo, **Mit.** 22:6 (2 Ne. 4:5). Bwana alisema njia zake ni za juu zaidi kuliko njia zetu, **Isa.** 55:8–9.

Mlango ni mwembamba na njia imesonga iendayo uzimani, **Mt.** 7:13–14 (3 Ne. 14:13–14; 27:33; M&M 132:22, 25). Mungu atawafanyia njia ili mwepuke majaribu, **1 Kor.** 10:13.

Bwana hatoi amri ambayo hatayarishi njia kwa ajili ya watoto wake kuishika, **1 Ne.** 3:7 (1 Ne. 9:6; 17:3, 13). Hakuna njia nyingine isipokuwa kwa kupitia mlangoni, **2 Ne.** 9:41. Mko huru kujiamulia wenyewe—kuchagua njia ya mauti yasiyo na mwisho au uzima wa milele, **2 Ne.** 10:23. Hii ndiyo njia na hakuna njia nyingine au jina jingine, **2 Ne.** 31:21 (Mos. 3:17; Alma 38:9; Hel. 5:9). Kwa zawadi ya Mwanawe Mungu ametayarisha njia iliyo bora zaidi, **Eth.** 12:11 (1 Kor. 12:31).

Kila mtu alitembea katika njia yake mwenyewe, **M&M** 1:16. Lazima ifanyike katika njia yangu mwenyewe, **M&M** 104:16.

Njiwa, Ishara ya. *Ona pia* Roho Mtakatifu

Alama iliyopangwa tangu awali ambayo kwayo Yohana Mbatizaji angeliweza kumtambua Masiya (Yn. 1:32–34). Joseph Smith alifundisha ya kwamba alama ya njiwa ilichaguliwa kabla ya uumbaji wa ulimwengu kama ushahidi kwa ajili ya Roho Mtakatifu; kwa hiyo, ibilisi hawezi kuja katika alama ya njiwa.

Roho wa Mungu alishuka kama njiwa, **Mt.** 3:16.

Baada ya Yesu kubatizwa, Roho Mtakatifu alimshukia katika umbile la njiwa, **1 Ne.** 11:27.

Mimi Yohana, ninashuhudia, na lo, mbingu zikafunguka, na Roho Mtakatifu akashuka juu yake katika umbo la njiwa, **M&M** 93:15.

Njoo. *Ona pia* Mtiifu, Tii, Utii; Mwanafunzi

Katika maandiko, daima humaanisha kusogea karibu na mtu kwa kufuata au kutii, kama vile ilivyo katika usemi "njooni kwa Kristo, na mkakamilishwe ndani yake" (Moro. 10:32).

Tegeni masikio yenu na kunijia, **Isa.** 55:3.

Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao, **Mt.** 11:28. Waacheni watoto wadogo waje kwangu, **Mt.** 19:14. Kama mtu yeyote akitaka kunifuata, na ajikane mwenyewe, **Lk.** 9:23. Yeyote ajaye kwangu hataona njaa kamwe, **Yn.** 6:35.

Kristo anawaalika wote kuja kwake, **2 Ne.** 26:33. Njooni kwangu na muokolewe, **3 Ne.** 12:20. Njooni kwa Kristo, **Moro.** 10:32.

Waalikeni wote waje kwa Kristo, **M&M** 20:59. Njooni kwangu, na nafsi zenu zitakuwa hai, **M&M** 45:46.

Nuhu, Mwana wa Zenifu

Mfalme mwovu katika Kitabu cha Mormoni. Alitawala kikundi cha Wanefi katika nchi ya Nefi.

Nuhu alifanya dhambi nyingi, **Mos.** 11:1–15. Aliamuru nabii Abinadi auawe, **Mos.** 13:1 (Mos. 17:1, 5–20). Nuhu alichomwa moto hadi kufa, **Mos.** 19:20.

Nuhu, Patriaki wa Biblia. *Ona pia* Gabrieli; Gharika katika Wakati wa Nuhu; Safina; Upinde wa mvua

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Lameki na ni patriaki wa kumi kutoka kwa Adamu (Mwa. 5:29–32). Alishuhudia juu ya Kristo na alihubiri toba kwa kizazi kilichokuwa kiovu. Watu walipokataa ujumbe wake, Mungu alimwamuru kujenga safina ili kuihifadhi familia yake na wanyama wote wakati dunia ilipofurika ili kuwaangamiza waovu. (Mwa. 6:13–22; Musa 8:16–30). Joseph Smith Nabii alifundisha ya kwamba Nuhu ndiye malaika Gabrieli na ni wa pili kutoka kwa Adamu katika kushikilia funguo za wokovu.

Yeye na wanawe Yafeti, Shemu, na Hamu, na wake zao waliokolewa walipojenga safina kwa amri ya Mungu, **Mwa.** 6–8 (Ebr. 11:7; 1 Pet. 3:20). Bwana alifanya upya agano alilolifanya pamoja na Henoko kwa Nuhu, **Mwa.** 9:1–17 (TJS, Mwa. 9:15, 21–25; Musa 7:49–52).

Nuhu alitawazwa katika ukuhani alipokuwa na umri wa miaka kumi na Methusela, **M&M** 107:52.

Watu walijaribu kumwua, lakini uwezo wa Mungu ulimwokoa, **Musa** 8:18. Akawa mhubiri wa uadilifu na alifundisha injili ya Yesu Kristo, **Musa** 8:19, 23–24 (2 Pet. 2:5).

Nuru, Nuru ya Kristo. *Ona pia* Akili, Viumbe-akili-asilia; Dhamiri; Roho Mtakatifu; Ukweli; Yesu Kristo

Nguvu za kiungu, uwezo, au ushawishi unaotokana na Mungu kupitia kwa Kristo na kutoa uhai na nuru kwa vitu vyote. Ni sheria ambayo kwayo vitu vyote vinatawaliwa mbinguni na duniani (M&M 88:6–13). Pia huwasaidia watu kuelewa kweli za injili na husaidia kuwaweka katika njia ile ya injili ambayo huwaongoza kwenye wokovu (Yn. 3:19–21; 12:46; Alma 26:15; 32:35; M&M 93:28–29, 31–32, 40, 42).

Nuru ya Kristo isifananishwe pamoja na Roho Mtakatifu. Nuru ya Kristo siyo mtu. Ni ushawishi utokao kwa Mungu na kumtayarisha mtu kumpokea Roho Mtakatifu. Ni ushawishi wa kutenda mema katika maisha ya watu wote (Yn. 1:9; M&M 84:46–47).

Onyesho moja la nuru ya Kristo ni dhamiri, ambayo humsaidia mtu kuchagua kati ya mema na mabaya (Moro. 7:16). Kadiri watu wanavyojifunza zaidi

juu ya injili, dhamiri zao huwa nyepesi zaidi katika kuhisi (Moro. 7:12–19). Watu wanaoifuata nuru ya Kristo huongozwa kwenye injili ya Yesu Kristo (M&M 84:46–48).

Bwana ni nuru yangu, **Zab.** 27:1. Na twendeni katika nuru ya Bwana, **Isa.** 2:5 (2 Ne. 12:5). Bwana atakuwa nuru isiyo na mwisho, **Isa.** 60:19.

Nuru ya kweli humtia nuru kila mtu ajaye katika ulimwengu, **Yn.** 1:4–9 (Yn. 3:19; M&M 6:21; 34:1–3). Mimi ndimi nuru ya ulimwengu, **Yn.** 8:12 (Yn. 9:5; M&M 11:28).

Chochote kilicho nuru, ni chema, **Alma** 32:35. Kristo ndiye uzima na nuru ya ulimwengu, **Alma** 38:9 (3 Ne. 9:18; 11:11; Eth. 4:12). Roho ya kristo imetolewa kwa kila mtu ili apate kujua mema na maovu, **Moro.** 7:15–19.

Kile kilicho cha Mungu ni nuru, nayo huzidi kung'ara hadi mchana mkamilifu, **M&M** 50:24. Roho hutoa nuru kwa kila mtu, **M&M** 84:45–48 (M&M 93:1–2). Yule azishikaye amri zake hupokea nuru na kweli, **M&M** 93:27–28. Nuru na kweli humkataa yule mwovu, **M&M** 93:37.

Nyama. *Ona pia* Hali ya Kufa, enye Kufa; Mwanadamu wa Tabia ya Asili; Mwili; Tamaa za kimwili

Nyama ina maana nyingi: (1) mkusanyiko wa seli ndogo laini ambazo hutengeneza miili ya wanadamu, wanyama, ndege, au samaki; (2) wenye kufa; au (3) maumbile au tamaa za mwanadamu wa asili.

Mkusanyiko wa seli za mwili: Wanyama watakuwa chakula chenu, **Mwa.** 9:3. Wanyama wasiuawe bila sababu, **TJS, Mwa.** 9:10–11 (M&M 49:21).

Wanyama na ndege ni kwa ajili ya chakula na mavazi ya mwanadamu, **M&M** 49:18–19 (M&M 59:16–20). Yatupasa kula nyama kwa kiasi, **M&M** 89:12–15.

Mwili wenye kufa: Yesu ndiye Mwana pekee wa Baba katika mwili wenye kufa, **Yn.** 1:14 (Mos. 15:1–3).

Adamu akawa mwenye mwili wa kwanza, **Musa** 3:7.

Tamaa ya asili ya mwanadamu: Amelaaniwa mwanadamu aufanyaye mwili kuwa mkono wake, **Yer.** 17:5.

Roho iradhi, bali mwili ni dhaifu, **Mk.** 14:38. Tamaa ya mwili haitokani na Baba, **1 Yoh.** 2:16.

Nefi alihuzunika kwa sababu ya mwili wake na dhambi zake, **2 Ne.** 4:17–18, 34. Msijipatanishe wenyewe kwa ibilisi wala mwili, **2 Ne.** 10:24.

Nyaraka za Paulo. *Ona pia* Paulo; majina ya nyaraka moja moja

Vitabu kumi na vinne katika Agano Jipya ambavyo awali vilikuwa ni barua zilizoandikwa na mtume Paulo kwa waumini wa Kanisa. Vinaweza kugawanywa katika makundi kama ifuatavyo:

1 na 2 Wathesalonike (50–51 B.K.)

Paulo aliandika nyaraka hizi kwa Wathesalonike kutoka Korintho wakati wa safari yake ya pili ya kimisionari. Kazi yake katika Thesalonike imeelekezwa katika Matendo 17. Alitaka kurudi tena Thesalonike, lakini hakuweza kufanya hivyo (1 The. 2:18). Kwa hiyo alimtuma Timotheo ili kuwachangamsha waongofu na ili amletee taarifa juu ya namna wanavyoendelea. Waraka wa kwanza ni matokeo ya shukrani zake juu ya kurudi kwa Timotheo. Waraka wa pili uliandikwa muda mfupi baadaye.

1 na 2 Wakorintho, Wagalatia, Warumi (55–57 B.K.)

Paulo aliandika nyaraka hizi kwa Wakorintho wakati wa safari yake ya tatu ya kimisionari ili kujibu maswali na kusahihisha machafuko miongoni mwa Watakatifu katika Korintho.

Waraka kwa Wagalatia yawezekana kuwa uliandikwa kwa vikundi vingi vya Kanisa katika Galatia. Baadhi ya waumini wa Kanisa walikuwa wakiacha injili kwa sababu ya sheria za Kiyahudi. Katika barua hii, Paulo alielezea madhumuni ya torati ya Musa na maana ya dini ya kiroho.

Paulo aliandika waraka kwa Warumi kutoka Korintho, kwa upande mmoja ili kuwatayarisha Watakatifu wa Rumi kwa ajili ya ziara aliyotumaini kuifanya kwao. Barua hii pia inasisitiza usahihi wa mafundisho ambayo yalikuwa yakipingwa na baadhi ya Wayahudi ambao wameongolewa katika Ukristo.

Wafilipi, Wakolosai, Waefeso, Filemoni, Waebrania (60–62 B.K.)

Paulo aliandika nyaraka hizi wakati alipokuwa gerezani kwa mara ya kwanza katika Roma.

Paulo aliandika waraka kwa Wafilipi kwa madhumuni ya kueleza shukrani yake na upendo wake kwa Watakatifu wa Filipi na kuwatia furaha kutokana na kukata kwao tamaa kwa sababu ya kifungo chake cha muda mrefu gerezani.

Paulo aliandika waraka kwa Wakolosai kama matokeo ya taarifa ya kwamba Watakatifu wa Kolosai walikuwa wakianguka katika makosa makubwa. Waliamini kwamba ukamilifu huja kwa kushika, kwa uangalifu, ibada za kimwili pekee yake kuliko kukuza tabia kama za Kristo.

Waraka kwa Waefeso ni wa umuhimu mkubwa, kwani una mafundisho ya Paulo juu ya Kanisa la Kristo.

Waraka kwa Filemoni ni barua ya siri juu ya Onesmo, mtumwa aliyemwibia bwana wake, Filemoni, na akakimbilia Roma. Paulo alimrudisha Onesmo kwa bwana wake pamoja na barua akiomba Onesmo asamehewa.

Paulo aliandika waraka kwa Waebrania waumini wa Kanisa wa Kiyahudi akiwashawishi kwamba torati ya Musa imetimilika katika Kristo na kwamba sheria ya injili ya Kristo imechukua nafasi yake.

1 na 2 Timotheo, Tito (64–65 B.K.)

Paulo aliandika nyaraka hizi baada ya kuachiliwa huru kutoka gerezani katika Roma kwa mara ya kwanza.

Paulo alisafiri kwenda Efeso, ambako alimwacha Timotheo kukomesha ukuaji wa aina fulani ya mafundisho yasiyo ya uhakika, akidhamiria kurudi tena baadaye. Aliandika waraka wake wa kwanza kwa Timotheo, pengine kutoka Makedonia, ili kumshauri na kumtia moyo katika kutimiza wajibu wake.

Paulo aliandika waraka kwa Tito wakati alipokuwa huru kutoka gerezani. Yawezekana alikuwa ametembelea Krete mahali ambapo Tito alikuwa akitumika. Barua hii hususani inashughulika na maisha ya uadilifu na nidhamu ndani ya Kanisa.

Paulo aliandika waraka wake wa pili kwa Timotheo wakati akiwa gerezani kwa mara ya pili, muda mfupi kabla ya kifo cha kishahidi cha Paulo. Waraka huu una maneno ya mwisho ya Paulo na huonyesha ujasiri na matumaini ya ajabu ambayo kwayo alikabili mauti.

Nyoka wa shaba nyeupe. *Ona pia* Musa; Yesu Kristo

Nyoka wa shaba nyeupe aliyetengenezwa na Musa kwa amri ya Mungu ili kuwaponya Waisraeli ambao walikuwa wameumwa na nyoka wakali (nyoka wenye sumu) nyikani (Hes. 21:8–9). Nyoka huyu wa shaba nyeupe alitundikwa kwenye mlingoti na "kuinuliwa juu ili kwamba mtu yeyote ambaye angeliangalia apate kuishi" (Alma 33:19–22). Bwana alielezea kwa kuinuliwa kwa yule nyoka nyikani kama ni ishara yake Yeye mwenyewe akiwa ameinuliwa juu ya msalaba (Yn. 3:14–15). Ufunuo wa siku za mwisho unathibitisha historia juu ya nyoka wakali na jinsi watu walivyokuwa wameponywa (1 Ne. 17:41; 2 Ne. 25:20; Hel. 8:14–15).

Nyumba ya Bwana. *Ona* Hekalu, Nyumba ya Bwana

Nyumba ya Israeli. *Ona* Israeli

Nyumbani. *Ona pia* Familia

Nyumbani panapaswa kuwa ndiyo kituo cha injili na shughuli za kifamilia.

Mwanaume atakuwa huru nyumbani mwake ili amfurahishe mke wake, **Kum.** 24:5.

Alimtuma nyumbani kwake, **Mk.** 8:26. Watoto na wajifunze kuonyesha heshima kwa wazazi wao nyumbani, **1 Tim.** 5:4. Kuwa wenye kiasi, kuwa safi, kufanya kazi nyumbani mwao, **Tit.** 2:5.

Nendeni nyumbani mwenu na mkayatafakari mambo haya niliyoyasema, **3 Ne.** 17:2–3. Niliwasihi wapigane vita kwa ajili ya wake zao, na watoto wao, na nyumba zao, na familia zao, **Morm.** 2:23.

Akina baba wanaamriwa kuwa na bidii na kuwa wenye kuzijali familia zao, **M&M** 93:43–44, 48–50.

Oa. *Ona* Ndoa, Oa, Olewa

Obadia

Nabii wa Agano la kale aliyetabiri maangamizi ya Edomu. Yawezekana alitoa unabii katika wakati wa utawala wa Yehoramu (848–844 K.K.) au wakati wa uvamizi wa Babilonia katika mwaka 586 K.K.

Kitabu cha Obadia: Ni kitabu katika Agano la Kale. Kina mlango mmoja tu. Ndani yake, Obadia aliandika kuanguka kwa Edomu na alitoa unabii kwamba waokozi watakwea juu ya Mlima Sayuni.

Obedi. *Ona pia* Boazi; Rutu

Katika Agano la Kale, mwana wa Boazi na Rutu na ndiye baba wa Yese, aliyekuja kuwa baba wa Mfalme Daudi (Rut. 4:13–17, 21–22).

Ofisa, Ofisi. *Ona pia* Kutawaza, Kutawazwa; Ukuhani

Nafasi ya mamlaka au wajibu katika shirika, mara kwa mara hutumika katika maandiko ili kumaanisha nafasi ya mamlaka ya ukuhani; yaweza pia kumaanisha kazi zilizopangwa katika nafasi au kwa mtu anayeshikilia nafasi hiyo.

Waumini wote hawatendi kazi moja, **Rum.** 12:4.

Tulizitukuza ofisi zetu kwa Bwana, **Yak. (KM)** 1:19. Melkizedeki alipokea ofisi ya ukuhani mkuu, **Alma** 13:18. Ofisi ya huduma ya malaika ni kuwaonya watu ili watubu, **Moro.** 7:31.

Mtu asitawazwe katika ofisi yoyote katika Kanisa hili pasipo kura ya Kanisa hilo, **M&M** 20:65. Acheni kila mtu asimame katika ofisi yake mwenyewe, **M&M** 84:109. Kuna marais au maafisa wasimamizi, walioteuliwa kutoka miongoni mwa wale waliotawazwa kwenye ofisi hizi katika kuhani hizi mbili, **M&M** 107:21. Kazi za wale wanaoongoza juu ya ofisi za akidi za ukuhani zinaelezwa, **M&M** 107:85–98. Na kila mtu ajifunze kazi yake, na kutenda katika ofisi ambayo ameteuliwa, **M&M** 107:99–100. Ninakupeni maofisa walio wa ukuhani wangu, **M&M** 124:123.

Olewa. *Ona* Ndoa, Oa, Olewa

Omba. *Ona pia* Sala

Kuuliza, swali, au kumwomba Mungu kwa ajili ya upendeleo maalumu.

Ombeni, nanyi mtapewa, **Mt.** 7:7. Lakini mtu wa kwenu akipungukiwa na hekima, na aombe dua kwa Mungu, **Yak. (Bib.)** 1:5 (JS—H 1:7–20).

Niombeni kwa imani, **1 Ne.** 15:11. Kama hamwezi kufahamu maneno haya, itakuwa ni kwa sababu hamuombi, **2 Ne.** 32:4. Muombe kwa moyo wa dhati, **Mos.** 4:10. Mungu huwapatia chochote mnachoomba kile kilicho sahihi, kwa imani, **Mos.** 4:21. Mwulizeni Mungu kama mambo haya si ya kweli, **Moro.** 10:4.

Huipenda giza kuliko nuru; kwa hiyo wao hawataniomba mimi, **M&M** 10:21. Mnaamriwa katika mambo yote kumwomba Mungu, **M&M** 46:7.

Omega. *Ona* Alfa na Omega; Yesu Kristo

Omneri. *Ona pia* Mosia, Mwana wa Benjamini; Mosia, Wana wa

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana wa Mfalme Mosia. Omneri alikwenda pamoja na kaka zake kuhubiri kwa Walamani (Mos. 27:8–11, 34–37; 28:1–9).

Omni

Mnefi mtunza kumbukumbu katika Kitabu cha Mormoni aliyeandika katika takribani mwaka wa 361 B.K. (Yar. 1:15; Omni 1:1–3).

Kitabu cha Omni: Kitabu kilichotafsiriwa kutoka katika mabamba madogo ya Nefi katika Kitabu cha Mormoni. Kitabu kina mlango mmoja tu, ambacho kina maelezo ya vita miongoni mwa Wanefi na Walamani. Omni aliandika mistari mitatu tu ya mwanzo ya kitabu hiki. Mabamba hayo kisha yakakabidhiwa kwa kupokezana kwa Amaroni, Kemisha, Abinadomu, na mwishowe Amaleki. Amaleki alikabidhi mabamba hayo kwa mfalme Benjamini, mfalme wa Zarahemla.

Ondoleo la Dhambi. *Ona pia* Lipia dhambi, Upatanisho; Samehe; Toba, Tubu; Yesu Kristo

Msamaha wa makosa unaotokana na masharti ya toba. Ondoleo la dhambi linawezeshwa na Upatanisho wa Yesu Kristo. Mtu hupata msamaha wa dhambi zake kama anayo imani katika Kristo, anatubu dhambi zake, anapokea ibada ya ubatizo na kuwekewa mikono kwa ajili ya kipawa cha Roho Mtakatifu, na anatii amri za Mungu, (M ya I 1:3–4).

Dhambi zenu zijapokuwa kama nyekundu, zitakuwa nyeupe kama theluji, **Isa.** 1:16–18.

Hii ni damu yangu, imwagikayo kwa ajili ya wengi kwa ondoleo la dhambi, **Mt.** 26:28 (Ebr. 9:22–28; M&M 27:2). Tubuni, na mkabatizwe kwa ondoleo la dhambi, **Mdo.** 2:38 (Lk. 3:3; M&M 107:20). Wale waaminio katika Kristo watapata ondoleo la dhambi, **Mdo.** 10:43 (Mos. 3:13).

Kristo ndiye chanzo ambacho wanaweza kutazamia ondoleo la dhambi, **2 Ne.** 25:26. Ili kubakiza ondoleo la dhambi zetu, ni lazima tuwajali maskini na wenye shida, **Mos.** 4:11–12, 26. Yeyote atakayetubu atakuwa na haki ya kupata rehema, hata ondoleo la dhambi zake, **Alma** 12:34. Kutimiza amri huleta ondoleo la dhambi, **Moro.** 8:25.

Ukuhani wa Haruni hushikilia funguo za ubatizo kwa kuzamishwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi, **M&M** 13 (M&M 84:64, 74; M ya I 1:4). Mimi, Bwana, sitazikumbuka tena dhambi zao, **M&M** 58:42–43 (Eze. 18:21–22). Hawa walifundishwa ubatizo unaofanywa kwa niaba ya waliokufa kwa ajili ya ondoleo la dhambi, **M&M** 138:33.

Ono. *Ona pia* Ndoto; Ono la Kwanza; Ufunuo

Ufunuo wa kuona juu ya tukio fulani, mtu, au jambo kwa uwezo wa Roho Mtakatifu.

Mifano ya maono muhimu ni pamoja na yafuatayo: Ono la Ezekieli juu ya siku za mwisho (Eze. 37–39), ono la Stefano juu ya Yesu kusimama mkono wa kuume wa Mungu (Mdo. 7:55–56), ufunuo wa Yohana kuhusu siku za mwisho (Ufu. 4–21), ono la Lehi na Nefi juu ya mti wa uzima (1 Ne. 8; 10–14), ono la Alma Mtoto juu ya malaika wa Bwana (Mos. 27), ono la kaka wa Yaredi juu ya wakazi wote wa dunia (Eth. 3:25), ono la madaraja ya utukufu (M&M 76), maono waliyopewa Joseph Smith na Oliver Cowdery katika hekalu la Kirtland (M&M 110), ono la Joseph F. Smith juu ya ukombozi wa wafu (M&M 138), ono la Musa juu ya Mungu na uumbaji Wake (Musa 1), ono la Enoshi juu ya Mungu (Musa 6–7), na Ono la Kwanza la Joseph Smith (JS—H 1).

Pasipo maono, watu huangamia, **Mit.** 29:18. Vijana wataona maono, **Yoe.** 2:28 (Mdo. 2:17).

Amenipa maarifa kwa maono, **2 Ne.** 4:23.

Alikuwa ni mjumbe aliyetumwa kutoka katika uwepo wa Mungu, **JS—H** 1:33. Tunaamini katika unabii, ufunuo, maono, **M ya I** 1:7.

Ono la Kwanza. *Ona pia* Smith, Joseph, Mdogo; Urejesho wa Injili

Kutokea kwa Mungu Baba na

Mwanawe Yesu Kristo kwa Joseph Smith Nabii katika kijisitu cha miti.

Katika majira ya kuchipua ya mwaka 1820, Joseph Smith Mdogo, alikuwa katika mwaka wake wa kumi na nne. Yeye alikuwa akiishi na familia yake katika eneo la Palmyra, New York. Umbali mfupi magharibi mwa nyumba ya familia hiyo kilikuwepo kijisitu cha miti mikubwa. Joseph alikwenda mahali hapa kusali kwa Mungu ili kujua kanisa lipi lilikuwa la kweli. Alikuwa amevutiwa wakati akisoma Biblia kwamba alilazimika kuomba jibu kutoka kwa Mungu (Yak. [Bib.] 1:5–6). Katika jibu la sala yake, Baba na Mwana wakamtokea yeye na kumwambia asijiunge na lolote kati ya makanisa hayo yaliyokuwepo duniani, kwani yote hayakuwa sahihi uongo (JS—H 1:15–20). Tukio hili takatifu lilianzisha mfuatano wa matukio ambayo yangeleta Urejesho wa injili na Kanisa la kweli la Kristo.

Onya, Onyo. *Ona pia* Kesha, Walinzi

Kutoa taarifa au tahadhari. Manabii, viongozi, na wazazi huonya na kufundisha wengine kuwa watiifu kwa Bwana na mafundisho Yake.

Yakobo aliwaonya watu wa Nefi dhidi ya kila aina ya dhambi, **Yak. (KM)** 3:12.

Sauti ya onyo ni kwa watu wote, **M&M** 1:4. Na kuhubiri kwako kuwe sauti ya onyo, **M&M** 38:41. Hii ni siku ya kuonya, **M&M** 63:58. Kila mtu ambaye amekwisha kuonywa yampasa kumwonya jirani yake, **M&M** 88:81. Nimewaonya na ninawaonya mapema, kwa kuwapa ninyi neno la hekima, **M&M** 89:4.

Osha, Oshwa, Uoshaji. *Ona pia* Batiza, Ubatizo; Lipia dhambi, Upatanisho

Kusafisha, kimwili au kiroho. Kwa ishara, mtu mwenye kutubu anaweza kusafishwa kutokana na maisha yaliyolemewa na mzigo wa dhambi na matokeo ya dhambi kupitia dhabihu ya upatanisho ya Yesu Kristo. Aina fulani ya uoshaji ufanyikao chini ya mamlaka ya ukuhani sahihi hutumika kama ibada takatifu.

Kuhani ataziosha nguo zake na kuoga majini, **Hes.** 19:7. Unioshe kabisa na dhambi zangu, **Zab.** 51:2, 7. Jiosheni, jitakaseni, komeni kutenda uovu, **Isa.** 1:16–18.

Yesu aliosha miguu ya Mitume wake, **Yn.** 13:4–15 (M&M 88:138–139). Mkabatizwe, na kuziosha dhambi zenu, **Mdo.** 22:16 (Alma 7:14; M&M 39:10).

Hakuna mtu awezaye kuokolewa isipokuwa mavazi yake yameoshwa na kuwa meupe, **Alma** 5:21 (3 Ne. 27:19). Mavazi yao yalioshwa na kuwa meupe kwa njia ya damu ya Kristo, **Alma** 13:11 (Eth. 13:10).

Kwa kushika amri waweze kuoshwa na kusafishwa kutoka katika dhambi zao zote, **M&M** 76:52. Kupakwa mafuta kwenu na kuoshwa kwenu kunahalalishwa na ibada ya nyumba yangu takatifu, **M&M** 124:39–41.

Ovu, Uovu. *Ona pia* Chafu, Uchafu; Dhambi; Giza, Kiroho; Kutokuwa Adilifu, Siyo Adilifu; Sio mcha mungu

Dhambi; kutokuwa mtiifu kwa amri za Mungu.

Nawezaje basi kutenda uovu huu mkubwa, na kutenda dhambi kwa Mungu, **Mwa.** 39:7–9. Bwana yu mbali na wasio na haki: bali husikia sala ya wenye haki, **Mit.** 15:29. Mwovu anapotawala, watu huugua, **Mit.** 29:2 (M&M 98:9).

Mwondoeni mtu mwovu miongoni mwenu, **1 Kor.** 5:13. Tunashindana na uovu wa kiroho katika mahali pa juu, **Efe.** 6:12.

Tokeni nje kutoka kwa waovu, na msiguse vitu vyao visivyo safi, **Alma** 5:56–57 (M&M 38:42). Hii ndiyo hali ya mwisho ya waovu, **Alma** 34:35 (Alma 40:13–14). Kamwe uovu haujapata kuwa furaha, **Alma** 41:10. Kwa njia ya waovu, waovu huadhibiwa, **Morm.** 4:5 (M&M 63:33).

Katika saa hiyo waja utengano mkamilifu wa wenye haki na waovu, **M&M** 63:54.

Hivyo waja mwisho wa waovu, **JS—M** 1:55.

Pahorani

Mwamuzi mkuu wa tatu Mnefi katika Kitabu cha Mormoni (Alma 50:39–40; 51:1–7; 59–62).

Paka mafuta. *Ona pia* Huduma kwa Wagonjwa; Mafuta

Katika nyakati za kale, ni manabii wa Bwana waliwapaka kwa mafuta wale ambao wangetenda kazi maalumu, kama vile Haruni au makuhani au wafalme ambao wangeitawala Israeli. Katika Kanisa leo, kupaka ni kuweka kiasi kidogo cha mafuta yaliyotakaswa juu ya kichwa cha mtu kama sehemu ya baraka maalumu. Hii inaweza tu kufanywa chini ya mamlaka na nguvu za Ukuhani wa Melkizedeki. Baada ya mpako, mtu anayefanya chini ya mamlaka ya ukuhani huo huo anaweza kufunga mpako huo na kutoa baraka maalumu kwa yule aliyepakwa.

Uwapake mafuta, na uwatakase ili wapate kunitumikia mimi, **Ku.** 28:41 (Law. 8:6–12, 30). Mpake mafuta ili awe mkuu juu ya watu wangu Israeli, **1 Sam.** 9:16; 10:1.

Wazee watawapaka mafuta na kuwabariki walio wagonjwa, **Yak. (Bib.)** 5:14–15 (M&M 42:44).

Partridge, Edward

Muumini na kiongozi wa mwanzoni wa Kanisa baada ya urejesho wake katika nyakati hizi za sasa. Edward Partridge alitumika kama askofu wa kwanza wa Kanisa (M&M 36; 41:9–11; 42:10; 51:1–18; 115; 124:19).

Pasaka. *Ona pia* Karamu ya Mwisho; Mwanakondoo wa Mungu; Ufufuko; Yesu Kristo

Sikukuu ya Pasaka iliwekwa ili kuwasaidia wana wa Israeli kukumbuka wakati malaika mwangamizaji alipopita juu ya nyumba zao na kuwakomboa kutoka kwa Wamisri (Ku. 12:21–28; 13:14–15). Wanakondoo wasio na doa, ambao damu yao ilitumika kama ishara ya kuwaokoa Israeli hapo kale, ni ishara ya Yesu Kristo, Mwanakondoo wa Mungu, ambaye dhabihu yake imewakomboa wanadamu wote.

Agizo la Pasaka ni hili, **Ku.** 12:43.

Yesu na Mitume wake waliishika Pasaka wakati wa Karamu ya Mwisho, **Mt.** 26:17–29 (Mk. 14:12–25). Ona Mwanakondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya ulimwengu, **Yn.** 1:29, 36. Kristo Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa dhabihu kwa ajili yetu, **1 Kor.** 5:7. Tulikombolewa kwa damu ya Kristo, kama ya mwanakondoo asiye na hila, **1 Pet.** 1:18–19.

Kuweni na imani kwa Mwanakondoo wa Mungu anayeziondoa dhambi za ulimwengu, **Alma** 7:14.

Watakatifu ambao huishi kwa Neno la Hekima watalindwa kama walivyokuwa wana wa Israeli, **M&M** 89:21.

Mwanakondoo amechinjwa tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, **Musa** 7:47.

Patakatifu pa Patakatifu. *Ona pia* Hekalu, Nyumba ya Bwana; Hema

Chumba kilichokuwa kitakatifu zaidi katika hema la Musa na baadaye katika hekalu. Patakatifu pa Patakatifu pia huitwa "mahali patakatifu sana" (Ku. 26:33–34).

Patriaki. *Ona* Kipatriaki, Patriaki

Patten, David W.

Mshiriki wa Akidi ya kwanza ya Mitume Kumi na Wawili waliochaguliwa katika kipindi hiki cha siku za mwisho. David Patten alikufa katika kifo cha kwanza cha kishahidi cha Kanisa lililorejeshwa, akiwa ameuawa katika pambano la Mto Crooked katika Missouri katika mwaka 1838.

Aliitwa kumaliza shughuli zake na kwenda kutumikia misheni, **M&M**

114:1. Alitwaliwa kwa Bwana, **M&M** 124:19, 130.

Paulo. *Ona pia* Nyaraka za Paulo

Mtume katika Agano Jipya. Jina la Paulo la Kiebrania lilikuwa ni Sauli, na alikuwa akijulikana kwa jina hili hadi kuanza kwa misheni yake kwa Wayunani. Mwanzoni alilitesa Kanisa hadi alipoongolewa katika ukweli wake baada ya kuona ono la Yesu Kristo. Paulo alienda katika safari kuu tatu za kimisionari na aliandika barua nyingi kwa Watakatifu. Kumi na nne kati ya barua hizi zimeunda sehemu ya Agano Jipya siku hizi. Hatimaye alichukuliwa kama mfungwa hadi Roma na akauawa, huenda katika majira ya kuchipua ya mwaka 65 B.K.

Aliruhusu Stefano kupigwa kwa mawe, **Mdo.** 7:57–8:1. Aliwatesa Watakatifu, **Mdo.** 8:3. Alikuwa akisafiri kwenda Dameski wakati Yesu alipomtokea, **Mdo.** 9:1–9. Alibatizwa na Anania, **Mdo.** 9:10–18. Baada ya kukaa Uarabuni, alirudi tena Dameski kuhubiri, **Mdo.** 9:19–25 (Gal. 1:17). Miaka mitatu baada ya kuongoka kwake, alirudi tena Yerusalemu, **Mdo.** 9:26–30 (Gal. 1:18–19). Akaenda safari tatu za kimisionari, akihubiri injili na kuunda matawi ya Kanisa katika sehemu mbalimbali za Ufalme wa Kirumi, **Mdo.** 13:1–14:26; 15:36–18:22; 18:23–21:15. Aliporudi Yerusalemu baada ya misheni yake ya tatu, alitiwa nguvuni na kupelekwa Kaisaria, **Mdo.** 21:7–23:35. Alibaki mfungwa katika Kaisaria kwa miaka miwili, **Mdo.** 24:1–26:32. Alipelekwa Roma kujibu mashtaka na alikumbana na kuvunjika kwa meli akiwa njiani, **Mdo.** 27:1–28:11.

Pazia

Neno litumikalo katika maandiko ili kumaanisha (1) kigawanyaji kinachotenga maeneo ya hema takatifu au hekalu, (2) ishara ya utengano kati ya Mungu na mwanadamu, (3) nguo nyembamba inayovaliwa na watu ili kufunika uso au kichwa, au (4) usahaulifu utolewao na Mungu ambao huziba kumbukumbu za watu juu ya maisha kabla ya kuzaliwa duniani.

Lile pazia litawagawanya kati ya patakatifu pa patakatifu na mahali patakatifu, **Ku.** 26:33.

Pazia la hekalu likapasuka vipande viwili wakati wa kusulubiwa kwa Kristo, **Mt.** 27:51 (Mk. 15:38; Lk. 23:45). Sasa tunaona kwa kioo, kwa jinsi ya giza, lakini baadaye tutaona uso kwa uso, **1 Kor.** 13:12.

Pazia la giza ya kutoamini lilikuwa likiondolewa kutoka akilini mwake, **Alma** 19:6. Kaka wa Yaredi hakuweza kuzuiliwa kuona ndani ya pazia, **Eth.** 3:19 (Eth. 12:19).

Lile pazia litapasuliwa nanyi mtaniona, **M&M** 67:10 (M&M 38:8). Lile pazia la kufunikia hekalu langu litaondolewa, **M&M** 101:23. Pazia likaondolewa kutoka akilini mwetu, **M&M** 110:1.

Pazia la giza litaifunika dunia, **Musa** 7:61.

Pelegi

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Eberi na mwana kitukuu wa Shemu. Katika siku zake dunia iligawanyika (Mwa. 10:22–25).

Pentekoste. *Ona pia* Torati ya Musa

Kama sehemu ya torati ya Musa, Sikukuu ya Pentekoste au Mavuno ya Kwanza ilifanyika siku hamsini baada ya Sikukuu ya Pasaka (Law. 23:16). Pentekoste ilikuwa ni kusherehekea mavuno, na katika Agano la Kale inaitwa Sikukuu ya Mavuno au Sikukuu ya Majuma. Ilikuwa ni sikukuu hii ambayo ilikuwa ikisherehekewa wakati wale Mitume katika Yerusalemu walipojazwa na Roho Mtakatifu nao wakanena katika ndimi (Mdo. 2; M&M 109:36–37).

Pepo Wabaya. *Ona* Roho—Pepo wachafu

Peponi. *Ona pia* Mbinguni

Sehemu ile ya ulimwengu wa roho ambamo ndani yake roho walio waadilifu ambao wameondoka katika maisha

haya hungojea ufufuko wa mwili. Ni hali ya furaha na amani.

Peponi pia hutumika katika maandiko ili kumaanisha ulimwengu wa roho (Lk. 23:43), ufalme wa selestia (2 Kor. 12:4), na hali ya dunia iliyotukuzwa kimilenia (M ya I 1:10).

Yeye ashindaye nitampa kula matunda ya mti wa uzima, ulio katikati ya peponi ya Mungu, **Ufu.** 2:7.

Peponi ya Mungu lazima itoe roho za waadilifu, **2 Ne.** 9:13. Roho za wenye haki hupokelewa katika hali ya furaha, ambayo huitwa peponi, **Alma** 40:11–12. Wanafunzi wote wa Yesu wamekwenda peponi kwa Mungu, isipokuwa wale watatu, **4 Ne.** 1:14. Hivi karibuni nitakwenda kupumzika peponi kwa Mungu, **Moro.** 10:34.

Kristo alizihubiria roho za wenye haki peponi, **M&M** 138.

Petro

Katika Agano Jipya, Petro mwanzoni alijulikana kama Simeoni au Simoni (2 Pet. 1:1), mvuvi wa Bethsaida aliyekuwa akiishi Kapernaumu pamoja na mke wake. Yesu alimponya mama wa mke wake (Mk. 1:29–31). Petro aliitwa yeye pamoja na kaka yake Andrea kuwa mfuasi wa Yesu Kristo (Mt. 4:18–22; Mk. 1:16–18; Lk. 5:1–11). Jina lake la Kiaramaya, Kefa, maana yake "mwonaji" au "jiwe" alipewa na Bwana (Yn. 1:40–42; TJS, Yn. 1:42 [Kiambatisho]). Wakati Agano Jipya linataja baadhi ya mapungufu ya Petro katika mwili wenye kufa, pia linatuonyesha kwamba aliyashinda na akaimarishwa kwa imani yake katika Yesu Kristo.

Petro alikiri kwamba Yesu alikuwa ndiye Kristo na Mwana wa Mungu (Yn. 6:68–69), na Bwana alimteua yeye kushikilia funguo za ufalme duniani (Mt. 16:13–19). Juu ya Mlima wa Kugeuka Sura, Petro alimwona Mwokozi aliyegeuka sura, vile vile Musa na Elia (Eliya) (Mt. 17:1–9).

Petro alikuwa ndiye Mtume kiongozi katika siku zake. Baada ya kifo, Ufufuko, na Kupaa kwa Mwokozi, yeye aliliita Kanisa pamoja na akaongoza katika kuitwa kwa Mtume wa kujaza nafasi ya Yuda Iskarioti (Mdo. 1:15–26). Petro na Yohana walimponya mtu aliyekuwa kiwete tangu kuzaliwa (Mdo. 3:1–16) na kimuujiza aliachiliwa huru kutoka gerezani (Mdo. 5:11–29; 12:1–19). Ilikuwa kupitia kwa huduma ya Petro kwamba injili kwa mara ya kwanza ilipelekwa kwa Wayunani (Mdo. 10–11). Katika siku za mwisho, Petro, pamoja na Yakobo na Yohana, walikuja kutoka mbinguni na kutunuku Ukuhani wa Melkizedeki na funguo zake juu ya Joseph Smith na Oliver Cowdery (M&M 27:12–13; 128:20).

Waraka wa Kwanza wa Petro: Waraka wa kwanza uliandikwa kutoka "Babilonia" (huenda ikawa Roma) na ukatumwa kwa Watakatifu katika ile ambayo sasa inaitwa Asia Ndogo mara baada ya Nero kuanza kuwatesa Wakristo.

Mlango wa 1 unazungumzia juu ya nafasi ya Kristo kuteuliwa kabla kuwa Mkombozi. Mlango wa 2–3 inaelezea kwamba Kristo ndiye jiwe kuu la pembeni la Kanisa, kwamba Watakatifu wanaushikilia ukuhani wa Kifalme, na kwamba Kristo alizihubiria roho zilizokuwa gerezani. Mlango wa 4–5 inaelezea ni kwani injili inahubiriwa kwa wafu na ni kwa nini wazee lazima walilishe kundi.

Waraka wa pili wa Petro: Mlango wa 1 unawahimiza Watakatifu kufanya imara miito yao na uteule wao. Mlango wa 2 unaonya dhidi ya walimu wa uongo. Mlango wa 3 unaeleza juu ya siku za mwisho na Ujio wa Pili wa Kristo.

Phelps, William W.

Muumuni na kiongozi wa mwanzo katika Kanisa baada ya kurejeshwa katika mwaka 1830. Bwana alimwita William Phelps kuwa mpiga chapa wa Kanisa (M&M 57:11; 58:40; 70:1).

Pilato, Pontio

Mtawala wa Kirumi katika Yuda,

mwaka 26–36 B.K. (Lk. 3:1). Aliwachukia watu wa Uyahudi na dini yao na akawaua baadhi ya Wagalilaya (Lk. 13:1). Yesu alishtakiwa na kuhukumiwa kusulubiwa mbele ya Pilato (Mt. 27:2, 11–26, 58–66; Mk. 15; Lk. 23; Yn. 18:28–19:38).

Pole, Upole. *Ona pia* Mnyenyekevu, Unyenyekevu; Moyo Uliovunjika; Subira

Mchamungu, mwadilifu, mnyenyekevu, mwenye kufundishika, na mvumilivu chini ya mateso. Watu wapole wako radhi kufuata mafundisho ya injili.

Musa alikuwa mpole sana, **Hes.** 12:3. Wapole watairithi dunia, **Zab.** 37:11 (Mt. 5:5; 3 Ne. 12:5; M&M 88:17). Mtafuteni Bwana, enyi wote mlio wapole; itafuteni haki, tafuteni unyenyekevu, **Sef.** 2:3 (1 Tim. 6:11).

Jifunzeni kwangu kwa kuwa Mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, **Mt.** 11:29. Upole ni tunda la Roho, **Gal.** 5:22–23. Mtumishi wa Bwana lazima awe muungwana, awezaye kufundisha, mvumilivu, akiwaelekeza kwa upole wale wampingao, **2 Tim.** 2:24–25. Roho ya upole na utulivu ni ya thamani kuu mbele za Mungu, **1 Pet.** 3:4.

Uvueni uanadamu wa asili na kuweni wanyenyekevu, **Mos.** 3:19 (Alma 13:27–28). Mungu alimwamuru Helamani kuwafundisha watu kuwa wapole, **Alma** 37:33. Neema ya Bwana yatosha kwa walio wanyenyekevu, **Eth.** 12:26. Mnayo imani katika Kristo kwa sababu ya unyenyekevu wenu, **Moro.** 7:39. Hakuna yeyote anayekubalika mbele za Mungu isipokuwa wapole na wanyenyekevu wa moyo, **Moro.** 7:44. Ondoleo la dhambi huleta unyenyekevu, na kwa sababu ya unyenyekevu huja kujiliwa na Roho Mtakatifu, **Moro.** 8:26.

Enenda katika unyenyekevu wa Roho wangu, **M&M** 19:23. Tawala nyumba yako kwa unyenyekevu, **M&M** 31:9. Nguvu na uwezo wa Ukuhani vyaweza kudumishwa kwa upole na unyenyekevu, **M&M** 121:41.

Ponya, Uponyaji. *Ona pia* Huduma kwa Wagonjwa; Paka mafuta

Kufanya mtu ajisikie vyema au kupata afya tena, kimwili na kiroho. Maandiko yana mifano mingi ya uponyaji wa kimiujiza wa Bwana na watumishi Wake.

Mimi ni Bwana ambaye nimekuponya, **Ku.** 15:26. Naamani alijichovya yeye mwenyewe ndani ya Mto Yordani mara saba na akaponywa, **2 Fal.** 5:1–14. Kwa fimbo zake tumeponywa, **Isa.** 53:5 (Mos. 14:5). Jua la walio na haki litachomoza na uponyaji katika mbawa zake, **Mal.** 4:2.

Yesu aliponya aina zote za magonjwa, **Mt.** 4:23 (Mt. 9:35). Aliwapa uwezo wa kuponya aina zote za magonjwa, **Mt.** 10:1. Amenituma mimi kuwaponya waliovunjika moyo, **Lk.** 4:18.

Waliponywa kwa uwezo wa Mwanakondoo wa Mungu, **1 Ne.** 11:31. Kama unaamini katika ukombozi wa Kristo, unaweza ukaponywa, **Alma** 15:8. Aliwaponya kila mmoja, **3 Ne.** 17:9.

Yule aliye na imani nami ya kuponywa ataponywa, **M&M** 42:48. Katika jina langu watawaponya wagonjwa, **M&M** 84:68.

Tunaamini katika karama ya uponyaji, **M ya I** 1:7.

Pornografia. *Ona* Uasherati; Usafi wa Kimwili; Uzinzi

Pratt, Orson

Mmoja wa Mitume Kumi na Wawili wa kwanza walioitwa baada ya Urejesho wa Kanisa katika nyakati za sasa (M&M 124:128–129). Alikuwa amekuwa muumini wa Kanisa kwa wiki sita tu wakati Bwana alipotoa ufunuo kwake kupitia Joseph Smith (M&M 34). Orson Pratt pia alikuwa mmisionari wa Kanisa (M&M 52:26; 75:14) na alitumikia kama mtunza historia ya Kanisa kwa miaka kadhaa.

Pratt, Parley Parker

Kaka mkubwa wa Orson Pratt na ni mmoja wa Mitume Kumi na Wawili wa

kwanza walioitwa baada ya Urejesho wa Kanisa katika nyakati za sasa (M&M 124:128–129). Parley Pratt aliitwa katika safari kadhaa za kwanza za kimisionari wakati Bwana alipotoa ufunuo kwake kupitia Joseph Smith katika Oktoba 1830 (M&M 32; 50:37).

Pumzika. *Ona pia* Amani; Siku ya Sabato

Kufurahia amani na uhuru kwa kuondokana na usumbufu na ghasia. Bwana ameahidi hivyo kwa wafuasi wake walio waaminifu katika maisha haya. Pia ameandaa mahali pa pumziko kwa ajili yao katika maisha yajayo.

Uwepo wangu utakwenda pamoja nanyi, nami nitawapa pumziko, **Ku.** 33:14.

Njooni kwangu, ninyi nyote wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha, **Mt.** 11:28–29.

Tulifanya kazi kwa bidii ili wapate kuingia katika pumziko lake, **Yak. (KM)** 1:7 (Ebr. 4:1–11). Yeyote atakayetubu ataingia katika pumziko langu, **Alma** 12:34. Kulikuwa na wengi kupita kiasi, waliotakaswa, na wakaingia katika pumziko la Bwana, **Alma** 13:12–16. Peponi ni hali ya pumziko, **Alma** 40:12 (Alma 60:13). Hakuna kiingiacho katika pumziko lake isipokuwa wale waliioosha mavazi yao katika damu yangu, **3 Ne.** 27:19.

Tangaza toba kwa watu hawa, ili upate kupumzika pamoja nao katika ufalme wa Baba yangu, **M&M** 15:6 (M&M 16:6). Wale wanaokufa watapumzika baada ya kazi zao zote, **M&M** 59:2 (Ufu. 14:13). Pumziko la Bwana ni utimilifu wa utukufu wake, **M&M** 84:24.

Rafaeli. *Ona pia* Malaika

Malaika wa Bwana aliyeshiriki katika urejesho wa vitu vyote (M&M 128:21).

Raheli. *Ona pia* Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mke wa Yakobo (Mwa. 29–31; 35). Pia alikuwa mama wa Yusufu na Benjamini.

Rais. *Ona pia* Nabii; Urais wa Kwanza

Jina la ofisa kiongozi wa shirika. Rais wa Kanisa ni nabii, mwonaji, na mfunuzi (M&M 21:1; 107:91–92), na waumini wa Kanisa watamwita nabii wa Kanisa kwa jina la "Rais" (M&M 107:65). Yeye ndiye mtu pekee duniani aliye na mamlaka ya kutumia funguo zote za ukuhani.

Viongozi wa akidi za ukuhani na jumuiya nyingine za Kanisa zaweza pia kuwa na jina la rais.

Bwana alitoa funguo za ufalme kwa Joseph Smith, **M&M** 81:1–2. Marais watatu huunda akidi ya Urais wa Kanisa, **M&M** 107:21–24. Marais walitawazwa kwa mfano wa Melkizedeki, **M&M** 107:29. Kazi za marais juu ya mashemasi, walimu, makuhani, na wazee zinaelezwa, **M&M** 107:85–89 (M&M 124:136–138, 142). Kuna marais saba juu ya sabini wengine wote, **M&M** 107:93–95. Marais wa vigingi waliteuliwa, **M&M** 124:133–135.

Rameumtomu

Katika Kitabu cha Mormoni, ni jukwaa refu ambalo juu yake Wazorami, Wanefi waliokengeuka, walisali (Alma 31:8–14, 21).

Rebeka. *Ona pia* Isaka

Mke wa Isaka, Patriaki katika Agano la Kale (Mwa. 24–27). Rebeka alikuwa mama wa Esau na Yakobo (Mwa. 25:23–26).

Rehema, enye Rehema. *Ona pia* Haki, Uadilifu, enye Uadilifu; Lipia dhambi, Upatanisho; Neema; Samehe; Yesu Kristo

Roho ya huruma, upole, na msamaha. Rehema ni moja ya sifa za Mungu. Yesu Kristo hutoa rehema kwetu kupitia dhabihu Yake ya kutulipia dhambi.

Bwana ni mwingi wa rehema na mwenye fadhili, **Ku.** 34:6 (Kum. 4:31). Rehema yake hudumu milele, **1 Nya.** 16:34. Wema na fadhili zitanifuata, **Zab.** 23:6.

Mtu mwenye huruma juu ya maskini ana heri, **Mit.** 14:21. Nataka fadhili wala si dhabihu, **Hos.** 6:6.

Heri wenye rehema: maana hao watapata rehema, **Mt.** 5:7 (3 Ne. 12:7). Ole wenu wanafiki mlipao zaka na kuacha mambo makuu ya sheria, hukumu, rehema, na imani, **Mt.** 23:23. Basi muweni na rehema, kama Baba yenu pia alivyo na rehema, **Lk.** 6:36. Siyo kwa matendo yetu yaliyo ya haki, bali kulingana na rehema zake ametukomboa sisi, **Tit.** 3:5.

Rehema za upendo wa Bwana zi juu ya wote, **1 Ne.** 1:20. Rehema haina madai juu ya asiyetubu, **Mos.** 2:38–39. Mungu ni mwenye huruma kwa wote wenye kuamini katika jina lake, **Alma** 32:22. Rehema yaweza kuridhisha mahitaji ya haki, **Alma** 34:16. Je, wadhani rehema yaweza kumwibia haki, **Alma** 42:25 (Alma 42:13–25). Watoto wadogo wako hai katika Kristo kwa sababu ya rehema zake, **Moro.** 8:19–20 (M&M 29:46).

Mkono wa rehema wa Yesu Kristo umelipia dhambi zenu, **M&M** 29:1. Kwa wema wa damu niliyoitoa, nimeomba mbele za Baba kwa ajili yao wanao liamini jina langu, **M&M** 38:4. Wale waliolishika agano langu watapata rehema, **M&M** 54:6. Mimi, Bwana, husamehe dhambi, na ni mwingi wa rehema kwa wale wenye kukiri dhambi zao kwa moyo mnyenyekevu, **M&M** 61:2. Mimi, Bwana, huonyesha huruma kwa wote walio wapole, **M&M** 97:2. Na mtu akupokeaye wewe kama mtoto mdogo, huupokea ufalme wangu, kwa maana watapata rehema, **M&M** 99:3.

Neema itakwenda mbele ya uso wako, **Musa** 7:31.

Rehoboamu. *Ona pia* Suleimani

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Mfalme Suleimani. Alimrithi baba yake na alitawala kwa miaka kumi na saba katika Yerusalemu (1 Fal. 11:43; 14:21, 31). Wakati wa utawala wa Rehoboamu, ufalme uligawanyika katika ufalme wa Israeli ya kaskazini na ufalme wa Yuda kusini (1 Fal. 11:31–36; 12:19–20). Rehoboamu alitawala ufalme wa Yuda.

Reubeni. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mwana mkubwa wa Yakobo na Lea (Mwa. 29:32; 37:21–22, 29; 42:22, 37). Ingawa Reubeni alikuwa mzaliwa wa kwanza, alipoteza haki yake ya Uzaliwa wa Kwanza kwa sababu ya dhambi (Mwa. 35:22; 49:3–4).

Kabila la Reubeni: Baraka za Yakobo kwa Reubeni zinapatikana katika Mwanzo 49:3 na Kumbukumbu la Torati 33:6. Idadi ya kabila taratibu ilipungua, na ingawa kabila liliendelea kuwepo, lilipungua umuhimu wake kisiasa. Haki ya uzaliwa wa kwanza ya Reubeni ikamwendea Yusufu na wanawe kwa sababu Yusufu alikuwa mwana wa kwanza wa mke wa pili wa Yusufu, Raheli (1 Nya. 5:1–2).

Reuheli. *Ona* Yethro

Ridhaa ya Wengi. *Ona pia* Kanisa la Yesu Kristo; Kuwakubali Viongozi wa Kanisa

Kanuni ambayo kwayo waumini wa Kanisa huwakubali wale walioitwa kuhudumu katika Kanisa pamoja na maamuzi mengine ya Kanisa ambayo yanahitaji kuungwa mkono na waumini, kwa kawaida huonyeshwa kwa kuinua mkono wa kuume.

Yesu Kristo husimama kama kiongozi wa Kanisa Lake. Kupitia mwongozo wa Roho Mtakatifu, Yeye huwaelekeza viongozi wa Kanisa katika matendo na maamuzi muhimu. Hata hivyo, waumini wote wa Kanisa wanayo haki na nafasi ya kuyakubali, au kutoyakubali matendo na maamuzi ya viongozi wao.

Watu wote walijibu kwa sauti moja, **Ku.** 24:3 (Hes. 27:18–19).

Mitume na wazee walipatana kwa moyo mmoja, **Mdo.** 15:25.

Mtu hasitawazwe pasipo kura ya Kanisa, **M&M** 20:65–66. Mambo yote yalifanyika kwa ridhaa ya wengi, **M&M** 26:2 (M&M 28:13). Na mambo yote yafanyike kwa ridhaa ya umoja, **M&M** 104:21.

Rigdon, Sidney

Mwongofu na kiongozi wa Kanisa wa mwanzoni kabisa katika miaka ya 1830 na mwanzoni mwa miaka ya 1840. Sidney Rigdon alitumikia kwa wakati fulani kama Mshauri wa Kwanza kwa Joseph Smith katika Urais wa Kwanza wa Kanisa (M&M 35; 58:50, 57; 63:55–56; 76:11–12, 19–23; 90:6; 93:44; 100:9–11; 124:126). Baadaye alianguka na akatengwa na Kanisa katika Septemba 1844.

Roho. *Ona pia* Mauti ya Kimwili; Mwanadamu, Wanadamu; Nafsi; Ufufuko

Ile sehemu ya kiumbe hai ambayo ilikuwepo kabla ya kuzaliwa duniani, ile ikaayo ndani ya mwili wa nyama na mifupa wakati wa maisha katika mwili wenye kufa, na itakuwepo baada ya kifo kama kiumbe kinachojitegemea hadi ufufuko. Vitu vyote vyenye uhai—mwanadamu, wanyama, na mimea—vilikuwa roho kabla ya uhai haujakuwepo juu ya dunia (Mwa. 2:4–5; Musa 3:4–7). Mwili wa roho huonekana kama mwili wa kawaida (1 Ne. 11:11; Eth. 3:15–16; M&M 77:2; 129). Roho ni maada, lakini ni angavu zaidi au safi kuliko kitu cha asili cha duniani au maada (M&M 131:7).

Kila mtu ni mwana au binti halisi wa Mungu, akiwa amezaliwa kama roho kwa Wazazi wa Mbinguni kabla ya kuzaliwa kwa wazazi wenye mwili wenye kufa duniani (Ebr. 12:9). Kila mtu duniani anao mwili usiokufa wa kiroho kama nyongeza kwa mwili wa nyama na mifupa. Kama wakati mwingine ilivyofafanuliwa katika maandiko, roho na mwili wa kawaida kwa pamoja hufanya nafsi (Mwa. 2:7; M&M 88:15; Musa 3:7, 9, 19; Ibr. 5:7). Roho inaweza kuishi pasipo mwili, lakini mwili hauwezi kuishi pasipo roho (Yak. [Bib.] 2:26). Kifo cha kimwili ni kujitenga kwa roho kutoka katika mwili. Katika Ufufuko, roho inaungana tena na mwili ule ule wa nyama na mifupa iliokuwa ikiumiliki kama mtu mwenye kufa, ukiwa na tofauti kubwa mbili: havitatengana tena, na ule mwili utakuwa mwili usiokufa na mkamilifu (Alma 11:45; M&M 138:16–17).

Roho haina nyama na mifupa, kama mnionavyo mimi, **Lk.** 24:39. Roho mwenyewe anashuhudia pamoja na roho zetu, kwamba sisi tu watoto wa Mungu, **Rum.** 8:16. Mtukuze Mungu katika mwili wako, na katika roho yako, **1 Kor.** 6:20.

Mwili huu ni mwili wa roho yangu, **Eth.** 3:16.

Mtu ni roho, **M&M** 93:33. Kristo alihudumu kwa roho waadilifu peponi, **M&M** 138:28–30 (1 Pet. 3:18–19).

Mlizaliwa katika ulimwengu kwa maji, na damu, na roho, **Musa** 6:59. Alisimama miongoni mwa wale waliokuwa roho, **Ibr.** 3:23.

Pepo wachafu: Yesu aliwafukuza pepo wachafu wengi, **Mk.** 1:27, 34, 39. Ewe pepo mchafu mtoke mtu huyu, **Mk.** 5:2–13.

Pepo mchafu humfundisha mwanadamu kwamba siyo lazima kusali, **2 Ne.** 32:8. Katika jina la Yesu aliwafukuza ibilisi na roho wachafu, **3 Ne.** 7:19.

Roho wengi waongo wamesambaa wakiudanganya ulimwengu, **M&M** 50:2, 31–32. Joseph Smith alielezea funguo tatu za kupambanua kama roho hiyo ni kutoka kwa Mungu au kwa ibilisi, **M&M** 129.

Roho iliyopondeka. *Ona* Moyo Uliovunjika

Roho Mtakatifu. *Ona pia* Batiza, Ubatizo; Dhambi isiyo sameheka; Kipawa cha Roho Mtakatifu; Maongozi ya Mungu, Shawishi; Mfariji; Mungu, Uungu; Njiwa, Ishara ya; Roho Mtakatifu wa Ahadi; Ufunuo

Mshirika wa tatu wa Uungu (1 Yoh. 5:7; M&M 20:28). Yeye ni mtu wa Roho, hana mwili wa nyama na mifupa (M&M 130:22). Roho Mtakatifu mara nyingi hutajwa kama Roho, au Roho wa Mungu.

Roho Mtakatifu hufanya kazi kadhaa

zilizo muhimu katika mpango wa wokovu. (1) Hutoa ushuhuda juu ya Baba na Mwana (1 Kor. 12:3; 3 Ne. 28:11; Eth. 12:41). (2) Hutufunulia ukweli wa mambo yote (Yn. 14:26; 16:13; Moro. 10:5; M&M 39:6). (3) Huwatakasa wale waliotubu na kubatizwa (Yn. 3:5; 3 Ne. 27:20; Musa 6:64–68). (4) Yeye ndiye Roho Mtakatifu wa Ahadi (M&M 76:50–53; 132:7, 18–19, 26).

Uwezo wa Roho Mtakatifu waweza kuja juu ya mtu kabla ya ubatizo na kumshuhudia kwamba injili ni ya kweli. Lakini haki ya kuwa na Roho Mtakatifu wakati wote, mtu anapokuwa mwenye kustahili, ni karama ambayo inaweza kupokelewa tu kwa kuwekewa mikono na mtu mwenye Ukuhani wa Melkizedeki baada ya kubatizwa na mtu aliye na mamlaka katika Kanisa la kweli la Yesu Kristo.

Yesu alifundisha kwamba dhambi zote zaweza kusamehewa isipokuwa kumkufuru Roho Mtakatifu (Mt. 12:31–32; Mk. 3:28–29; Lk. 12:10; Ebr. 6:4–8; M&M 76:34–35).

Roho huwafanya watu kutembea katika sheria za Mungu, **Eze.** 36:27.

Mitume walipewa mamlaka ya kubatiza katika jina la Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, **Mt.** 28:19. Roho Mtakatifu atawafundisha mambo yote, **Yn.** 14:26. Watu walio watakatifu walinena kama walivyoongozwa na Roho Mtakatifu, **2 Pet.** 1:21.

Nefi aliongozwa na Roho, **1 Ne.** 4:6. Siri za Mungu zitafunuliwa kwanza kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, **1 Ne.** 10:17–19. Roho Mtakatifu atakuonyesha mambo yote yakupasayo kuyafanya, **2 Ne.** 32:5. Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu mtaweza kujua ukweli wa mambo yote, **Moro.** 10:5.

Roho Mtakatifu atakuambia katika mawazo yako na katika akili na moyo wako, **M&M** 8:2. Roho hutuongoza kutenda yaliyo mema, **M&M** 11:12. Roho Mtakatifu anajua mambo yote, **M&M** 35:19. Roho Mtakatifu hufundisha mambo ya ufalme yaliyo ya amani, **M&M** 36:2 (M&M 39:6). Kama hautampokea Roho, usifundishe, **M&M** 42:14. Roho Mtakatifu huwashuhudia Baba na Mwana, **M&M** 42:17 (1 Kor. 12:3; 3 Ne. 11:32, 35–36). Kwa wengine wamepewa na Roho Mtakatifu kujua kwamba Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, **M&M** 46:13. Lolote watakalonena kwa kuongozwa na Roho Mtakatifu litakuwa andiko takatifu, **M&M** 68:4. Roho Mtakatifu atamwagwa katika kutoa ushuhuda wa mambo yote mtakayosema, **M&M** 100:8. Roho Mtakatifu atakuwa mwenzi wako daima, **M&M** 121:45–46.

Roho Mtakatifu wa Ahadi. *Ona pia* Roho Mtakatifu

Roho Mtakatifu ndiye Roho Mtakatifu wa Ahadi (Mdo. 2:33). Yeye huthibitisha matendo mema, ibada, na maagano ya wanadamu, kama yanavyokubalika kwa Mungu. Roho Mtakatifu wa Ahadi hushuhudia kwa Baba kwamba ibada za wokovu zimefanyika kiusahihi na kwamba maagano yahusianayo na hizo yameshikwa.

Wale waliotiwa muhuri na Roho Mtakatifu wa Ahadi hupokea yote Baba aliyo nayo, **M&M** 76:51–60 (Efe. 1:13–14). Maagano yote na utendaji wote lazima utiwe muhuri na Roho Mtakatifu wa Ahadi ili kuwa na nguvu baada ya maisha haya, **M&M** 132:7, 18–19, 26.

Roma. *Ona pia* Ufalme wa Kirumi

Katika Agano Jipya, ni mji mkuu wa Ufalme wa Kirumi, ulioko juu ya Mto Tiberi katika Italia (Mdo. 18:2; 19:21; 23:11). Paulo alifundisha injili katika Roma wakati alipokuwa mfungwa wa serikali ya Kirumi (Mdo. 28:14–31; Rum. 1:7, 15–16).

Rudi, Kurudiwa. *Ona pia* Shida

Rekebisho au fundisho la nidhamu litolewalo kwa watu binafsi au vikundi ili kuwasaidia waweze kujirekebisha au kuwa imara zaidi.

Msidharau kurudiwa na mkono wa Mwenyezi, **Ayu.** 5:17 (Mit. 3:11). Heri

mtu yule umwadhibuye, Ee Bwana, **Zab.** 94:12.

Maandiko yote yametolewa kwa ajili ya kuwaonya, na kuwaadabisha, **2 Tim.** 3:16. Bwana huwarudi wale awapendao, **Ebr.** 12:5–11.

Bwana anaonelea kuwa ni vyema kuwarudi watu wake, **Mos.** 23:21–22. Bwana asipowarudi watu wake, wao hawatamkumbuka yeye, **Hel.** 12:3. Bwana alisema na kaka wa Yaredi, na akamrudi, **Eth.** 2:14.

Aliwarudi ili wapate kutubu, **M&M** 1:27. Wale niwapendao pia huwarudi ili dhambi zao zipate kusamehewa, **M&M** 95:1. Wale wote wasiostahmili kurudiwa hawawezi kutakaswa, **M&M** 101:2–5. Watu wangu yafaa kuwarudi hadi wajifunze utiifu, **M&M** 105:6. Yule ambaye hatavumilia kuadhibiwa haustahili ufalme wangu, **M&M** 136:31.

Rutu. *Ona pia* Boazi

Katika Agano la Kale, ni mkwe Mmoabu wa Naomi na Elimeleki, waliokuwa Waisraeli. Baada ya kifo cha mume wake, Rutu aliolewa na jamaa ya Naomi, Boazi. Mwana wao Obedi alikuwa babu wa Daudi na Kristo. Hadithi ya Rutu inaelezea kwa uzuri zaidi uongofu wa asiye Mwisraeli katika kundi la kondoo la Israeli. Rutu aliachana na Mungu wake wa zamani na maisha yake ya zamani ili kuungana na jamaa ya waaminio katika kumtumikia Mungu wa Israeli (Rut. 1:16).

Kitabu cha Rutu: Mlango wa 1 unaelezea maisha ya Elimeleki na familia yake katika Moabu. Baada ya vifo vya waume zao, Naomi na Rutu walikwenda Bethlehemu. Mlango 2 unaelezea kwamba Rutu alivuna masazo katika mashamba ya Boazi. Mlango wa 3 unasimulia namna Naomi alivyomwagiza Rutu kwenda katika uga wa kupuria na kulala katika miguu ya Boazi. Mlango wa 4 ni historia ya ndoa ya Rutu na Boazi. Wakazaa mwana, Obedi, ambaye toka ukoo wake Daudi na Kristo wamekuja.

Sabini. *Ona pia* Mtume; Ukuhani wa Melkizedeki

Ofisi ambayo wanaume hutawazwa katika Ukuhani wa Melkizedeki. Leo, akidi za Sabini ni Viongozi Wakuu wa Kanisa na Sabini wa Maeneo. Wale Sabini huhudumu katika jina la Bwana chini ya maelekezo ya Uraisi wa Kwanza na Akidi ya Mitume Kumi na Wawili (ona M&M 107:34). Hutoa muda wao wote kwa huduma hii.

Bwana aliteua na wengine sabini, **Lk.** 10:1.

Sabini wanaitwa kuihubiri injili na kuwa mashahidi maalumu wa Yesu Kristo, **M&M** 107:25–26. Sabini hutenda kazi katika jina la Bwana, chini ya maelekezo ya wale Kumi na Wawili, wakilijenga Kanisa na kurekebisha mambo yote yalihusulo katika mataifa yote, **M&M** 107:34. Chagueni sabini wengine, hata saba mara sabini, kama kazi inataka hivyo, **M&M** 107:93–97. Akidi ya sabini imeanzishwa kwa ajili ya wazee wasafirio kutoa ushuhuda wa jina langu ulimwenguni kote, **M&M** 124:138–139.

Sadaka, Utoaji sadaka. *Ona pia* Dhabihu; Funga, Kufunga; Lipa zaka, Zaka; Maskini; Ustawi

Zawadi kwa Bwana. Agano la Kale mara kwa mara lilitumia neno hili ili kumaanisha dhabihu au sadaka ya kuteketeza. Kanisa leo huitumia sadaka ya mfungo na sadaka nyingine za hiari (ikijumuisha muda, vipaji, na mali) ili kuwasaidia maskini na kwa makusudi mengine yaliyo bora.

Mmeniibia katika zaka na matoleo, **Mal.** 3:8–10.

Kwanza ukapatane na ndugu yako na kisha urudi uitoe sadaka yako, **Mt.** 5:23–24. Msitoe sadaka zenu mbele za watu, **Mt.** 6:1–4 (3 Ne. 13:1–4). Huyu mjane maskini ametia zaidi kuliko wao wote, **Mk.** 12:41–44. Ni heri kutoa kuliko kupokea, **Mdo.** 20:33–35.

Mnitoleeni nafsi zenu zote kama sadaka kwa Kristo, **Omni** 1:26. Ningetaka kwamba muwapatie maskini mali yenu,

Mos. 4:26. Watu wa kanisa watoe mali yao, kila mmoja kulingana na kile alichokuwa nacho, **Mos.** 18:27. Kama mtu atatoa sadaka pasipo dhamira ya kweli, haitamfaidia kitu, **Moro.** 7:6.

Ukuhani wa Haruni kamwe hautaondoshwa tena hadi wana wa Lawi watoe tena sadaka kwa Bwana katika haki, **M&M** 13. Katika hii, siku ya Bwana, utatoa sadaka na sakramenti zako kwa Aliye Juu Sana, **M&M** 59:12. Na sisi kama Kanisa na watu tumtolee Bwana sadaka katika haki, **M&M** 128:24.

Safi na Isiyo safi. *Ona pia* Chafu, Uchafu; Torati ya Musa; Utakaso

Katika Agano la Kale, Bwana alimfunulia Musa na Waisraeli wa kale kwamba ni baadhi ya vyakula fulani tu vilionekana kuwa safi, au kwa maneno mengine, kufaa kuliwa. Tofauti ambayo Waisraeli waliifanya kati ya vyakula safi na visivyo safi ilikuwa na athari kubwa juu ya maisha yao ya kidini na kijamii. Baadhi ya wanyama, ndege na samaki walionekana kama ni safi na walikubalika kuliwa wakati wengine walikuwa siyo safi na walikatazwa (Law. 11; Kum. 14:3–20). Baadhi ya watu waliokuwa na ugonjwa fulani pia walifikiriwa kuwa siyo watu safi.

Katika mtazamo wa kiroho, kuwa safi ni kuwa bila dhambi na tamaa za kidhambi. Katika mtazamo huu neno hili linatumika kumwelezea mtu ambaye ni mwema na mwenye moyo mweupe (Zab. 24:4). Watu wa Mungu walio wa agano daima wamekuwa na mafundisho maalumu ili kuwa safi (3 Ne. 20:41; M&M 38:42; 133:5). Mtu aliyetenda dhambi anaweza kuwa safi kupitia imani katika Yesu Kristo, toba, na kupokea ibada za injili.

Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe atapokea baraka kwa Bwana, **Zab.** 24:3–5. Iweni safi, ninyi mnaochukua vyombo vya Bwana, **Isa.** 52:11 (M&M 133:4–5).

Heri wenye moyo safi, **Mt.** 5:8 (3 Ne. 12:8). Usimwite mtu yeyote kuwa najisi au mchafu, **Mdo.** 10:11–28. Mambo yoyote yaliyo safi, yatafakarini mambo haya, **Flp.** 4:8 (M ya I 1:13).

Ninyi nyote mlio weupe moyoni, inueni vichwa vyenu na kupokea neno la kupendeza la Bwana, **Yak. (KM)** 3:2–3. Je, mwaweza kumtazama Mungu siku hiyo kwa moyo mweupe na mikono safi, **Alma** 5:19. Wakiwa weupe na wasio na doa mbele za Mungu, wasingeweza kuiangalia dhambi isipokuwa kwa chuki kubwa, **Alma** 13:12. Mkatakaswe hata kama Kristo alivyo mweupe, **Moro.** 7:48 (Morm. 9:6).

Kristo atajihifadhia watu walio safi, **M&M** 43:14. Bwana atamrudi Sayuni hadi awe safi, **M&M** 90:36. Bwana aliamuru kwamba nyumba ijengwe katika Sayuni ambamo ndani yake walio safi watamwona Mungu, **M&M** 97:10–17. Hii ndiyo Sayuni—walio safi moyoni, **M&M** 97:21. Iweni safi ninyi mchukuao vyombo vya Bwana, **M&M** 133:4–5, 14 (Isa. 52:11).

Safina. *Ona pia* Gharika katika Wakati wa Nuhu; Nuhu, Patriaki wa Biblia; Upinde wa mvua

Katika Agano la Kale, ni safina iliyojengwa na Nuhu ili kulinda uhai wakati wa Gharika kuu.

Ujifanyie safina ya mti wa mvinje, **Mwa.** 6:14. Safina ikatua juu ya milima ya Ararati, **Mwa.** 8:4.

Boti za Wayaredi zilikuwa zimekazwa kama safina ya Nuhu, **Eth.** 6:7.

Sakramenti. *Ona pia* Batiza, Ubatizo; Dhabihu; Karamu ya Mwisho; Lipia dhambi, Upatanisho; Maji ya Uzima; Mkate wa Uzima; Msalaba; Yesu Kristo

Kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho, sakramenti humaanisha ibada ya kushiriki mkate na maji katika ukumbusho wa dhabihu ya Kristo ya kulipia dhambi. Mkate uliokatwakatwa huwakilisha mwili wake uliovunjwa, maji huwakilisha damu yake iliyomwagika kwa kulipia dhambi zetu (1 Kor. 11:23–25; M&M 27:2). Waumini wa Kanisa wenye

kustahili wanapopokea sakramenti, huahidi kujichukulia juu yao jina la Yesu Kristo, ili daima kumkumbuka Yeye, na kuzishika amri Zake. Kupitia ibada hii, waumini wa Kanisa hufanya upya maagano yao ya ubatizo.

Katika Karamu ya Mwisho, Yesu aliielezea ibada ya Sakramenti wakati alipokuwa Akila pamoja na wale Mitume Kumi na Wawili (Mt. 26:17–28; Lk. 22:1–20).

Yesu alitwaa mkate, na akaubariki, na akatwaa kikombe, na akatoa shukrani, **Mt.** 26:26–28 (Mk. 14:22–24; Lk. 22:19–20). Yeyote aulaye mwili wangu, na kuinywa damu yangu, anao uzima wa milele, **Yn.** 6:54. Mtu ambaye huula na kuinywa pasipo kustahili, hula na kuinywa laana kwa nafsi yake, **1 Kor.** 11:29 (3 Ne. 18:29).

Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kumi na wawili wa Kinefi juu ya sakramenti, **3 Ne.** 18:1–11. Yesu aliwafundisha wanafunzi hawa kuwakataza watu wasiostahili kushiriki sakramenti, **3 Ne.** 18:28–29 (Morm. 9:29). Sala za sakramenti zinatolewa, **Moro.** 4–5 (M&M 20:75–79).

Sakramenti ihudumiwe na kuhani au mzee, **M&M** 20:46, 76. Walimu na mashemasi hawana mamlaka ya kubariki sakramenti, **M&M** 20:58. Vimiminika vingine zaidi ya mvinyo vyaweza kutumika kwa ajili ya sakramenti, **M&M** 27:1–4.

Sala. *Ona pia* Amina; Kuabudu; Omba; Tafakari

Mawasiliano ya unyenyekevu kati ya mtu na Mungu wakati ambapo mtu hutoa shukrani na kuomba baraka. Sala hutolewa kwa Baba wa Mbinguni katika jina la Yesu Kristo. Sala zaweza kusemwa kwa sauti au kimya kimya. Mawazo ya mtu yaweza pia kuwa sala kama yanaelekezwa kwa Mungu. Wimbo wa mwenye haki waweza kuwa sala kwa Mungu (M&M 25:12).

Madhumuni ya sala siyo kubadilisha mapenzi ya Mungu, bali kujipatia kwa ajili yetu sisi wenyewe na kwa ajili ya wengine baraka ambazo Mungu tayari anataka kutupa, lakini tunalazimika kuomba ili tuweze kuzipata.

Tunasali kwa Baba katika jina la Kristo (Yn. 14:13–14; 16:23–24). Hakika tunaweza kusali katika jina la Yesu wakati matakwa yetu yanapokuwa matakwa ya Kristo (Yn. 15:7; M&M 46:30). Kisha tunaomba mambo yale yaliyo sahihi na hivyo Mungu huwa radhi kutupatia (3 Ne. 18:20). Sala zingine hubaki pasipo kujibiwa kwa sababu kwa njia yoyote ile hayawakilishi matakwa ya Kristo bali badala yake hutokana na ubinafsi wa mtu huyo (Yak. [Bib.] 4:3; M&M 46:9). Kweli, kama tutamwomba Mungu mambo yasiyo ya haki, yatageuka kuwa lana kwetu (M&M 88:65).

Hapo ndipo wanadamu wakaanza kulilingana jina la Bwana, **Mwa.** 4:26. Mahali pa madhabahu, ndipo hapo Ibrahimu alipoliitia jina la Bwana, **Mwa.** 13:4. Watumishi wa Ibrahimu walisali ili kupata msaada wa kumtafuta mke kwa ajili ya Isaka, **Mwa.** 24:10–19. Mungu apishe mbali kwamba nisimtendee Bwana dhambi kwa kuacha kusali kwa ajili yenu, **1 Sam.** 12:23. Bwana huisikia sala ya mwenye haki, **Mit.** 15:29. Nanyi mtanitafuta na kuniona mtakaponitafuta kwa moyo wenu wote, **Yer.** 29:12–13.

Salini kwa ajili ya wale wanaowatumia vibaya, **Mt.** 5:44 (Lk. 6:28; 3 Ne. 12:44). Salini kwa Baba yenu aliye sirini, **Mt.** 6:5–8 (3 Ne. 13:5–8). Kwa hiyo salini hivi, **Mt.** 6:9–13 (Lk. 11:2; 3 Ne. 13:9). Ombeni, nanyi mtapewa, **Mt.** 7:7 (3 Ne. 14:7; M&M 4:7; 6:5; 66:9). Yesu alipanda mlimani faraghani ili kusali, **Mt.** 14:23. Kesheni na kusali, ili msije mkaingia majaribuni, **Mt.** 26:41 (Mk. 14:38; 3 Ne. 18:15–18; M&M 31:12). Na aombe kwa imani, pasipo mashaka, **Yak. (Bib.)** 1:5–6 (M&M 42:68; 46:7). Sala ya dhati ya mwenye haki yafaa sana, **Yak. (Bib.)** 5:16.

Msikilizeni Roho awafundishaye wanadamu kusali, **2 Ne.** 32:8–9. Nilimlilia

kwa sala kuu, **Eno.** 1:4. Nimefunga na kusali kwa siku nyingi, **Alma** 5:45–46 (Alma 26:22). Walijitoa wenyewe kwa sala nyingi na kufunga, **Alma** 17:3. Je, mnakumbuka Zeno alisema nini kuhusu sala na kuabudu, **Alma** 33:3. Jinyenyekezeni wenyewe, na mdumu katika sala, **Alma** 34:18–27. Mwombe Bwana katika matendo yako yote, **Alma** 37:37. Lazima msali daima kwa Baba katika jina langu, **3 Ne.** 18:19–20. Salini katika familia zenu, **3 Ne.** 18:21. Yesu alisali kwa baba, **3 Ne.** 19:31–34 (Yn. 17; 3 Ne. 18:16). Awaamuru kwamba wasikome kusali mioyoni mwao, **3 Ne.** 20:1. Kama hatasali kwa dhamira halisi ya moyo, haitamsaidia kitu chochote, **Moro.** 7:6–9.

Usiombe kile usichopaswa kuomba, **M&M** 8:10. Sali daima, ili uweze kutoka mshindi, **M&M** 10:5. Ninakuamuru kwamba utasali kwa sauti na vile vile moyoni mwako, **M&M** 19:28. Roho atatolewa kwenu kwa sala ya imani, **M&M** 42:14. Utakwenda kwenye nyumba ya sala na kutoa sakramenti zako, **M&M** 59:9 (Mt. 21:13). Wazazi watawafundisha watoto wao kusali, **M&M** 68:28. Bwana Mungu wao amekuwa mzito kusikiliza sala zao, **M&M** 101:7–8 (Mos. 21:15). Uwe mnyenyekevu; na Bwana Mungu wako atakupa jibu la sala zako, **M&M** 112:10.

Adamu aliamriwa kumlingana Mungu katika jina la Mwana, **Musa** 5:8. Baba na Mwana walimtokea Joseph Smith katika kujibu sala yake, **JS—H** 1:11–20.

Sala ya Bwana. *Ona pia* Sala

Sala iliyotolewa na Mwokozi kwa ajili ya wanafunzi Wake ambayo inatumika kama mfano kwa sala zote (Mt. 6:9–13; 3 Ne. 13:9–13).

Salemu. *Ona pia* Melkizedeki; Yerusalemu

Mji katika Agano la Kale ambao Melkizedeki alitawala. Yawezekana ulikuwa katika eneo ambalo kwa sasa Yerusalemu iko. Jina Salemu linafanana na neno la Kiebrania linalomaanisha "amani."

Melkizedeki mfalme wa Salemu alileta mkate na divai, **Mwa.** 14:18.

Melkizedeki, mfalme wa Salemu, alikuwa kuhani wa Mungu Aliye Juu Sana, **Ebr.** 7:1–2.

Melkizedeki alikuwa mfalme wa nchi ya Salemu, **Alma** 13:17–18.

Samaria. *Ona pia* Wasamaria

Katika Agano la Kale, ni mji mkuu wa ufalme wa kaskazini wa Israeli (1 Fal. 16:23–24). Kwa sababu ya nafasi yake ya uimara wa kijeshi juu ya mlima, Waashuru hawakuweza kuuteka hadi baada ya kuuhusuru kwa miaka mitatu (2 Fal. 17:5–6). Herodi aliujenga upya na akauita Sebaste. Katika nyakati za Agano Jipya, Samaria lilikuwa ndilo jina la sehemu yote ya katikati ya Palestina magharibi ya Yordani.

Samehe. *Ona pia* Kiri, Kukiri; Lipia dhambi, Upatanisho; Ondoleo la Dhambi; Toba, Tubu

Kama linavyotumika katika maandiko, kusamehe kwa ujumla linaamanisha moja ya mambo mawili: (1) Mungu anapowasamehe wanadamu, yeye hufuta au huiweka pembeni adhabu inayotakiwa kwa dhambi ile. Kupitia upatanisho wa Kristo, msamaha wa dhambi unapatikana kwa wote wenye kutubu, isipokuwa wale walio na hatia ya mauaji au ile dhambi isiyo sameheka dhidi ya Roho Mtakatifu. (2) Watu wanaposameheana wao kwa wao, wanafanyiana kwa upendo kama Kristo nao wanakuwa hawana hisia mbaya kwa wale walio wakosea (Mt. 5:43–45; 6:12–15; Lk. 17:3–4; 1 Ne. 7:19–21).

Bwana ni mvumilivu, na mwingi wa rehema, mwenye kusamehe ovu na uvunjaji wa sheria, **Hes.** 14:18. Dhambi zenu zijapokuwa nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji, **Isa.** 1:18.

Tusamehe madeni yetu, kama sisi tunavyo wasamehe wadeni wetu, **Mt.** 6:12 (Lk. 11:4; 3 Ne. 13:11). Mwana wa Mtu

anao uwezo wa kusamehe dhambi, **Mt.** 9:6 (Mt. 18:35; Mk. 2:10; Lk. 5:20–24). Ndugu yangu anikosee mara ngapi, nami nimsamehe?, **Mt.** 18:21–22 (M&M 98:40). Mtu atakaye mkufuru Roho Mtakatifu hana msamaha kamwe, **Mk.** 3:29 (Alma 39:6). Kama ndugu yako akikosa dhidi yako na kutubu, msamehe, **Lk.** 17:3. Baba uwasamehe, kwa maana hawajui watendalo, **Lk.** 23:34.

Ombeni msamaha, **1 Ne.** 7:21. Tumia damu ya Kristo kulipia makosa ili tupate kupokea msamaha wa dhambi zetu, **Mos.** 4:2. Kama atakiri dhambi zake mbele yako na yangu, na kutubu, yeye utamsamehe, **Mos.** 26:29–31.

Mtu anayetubu na kutimiza amri atasamehewa, **M&M** 1:32. Ingiza mundu yako, na dhambi zako zitasamehewa, **M&M** 31:5 (M&M 84:61). Yule aliyetubu dhambi zake amesamehewa, na Mimi, Bwana sizikumbuki tena, **M&M** 58:42. Nitamsamehe yule nitakaye kumsamehe, lakini ninyi mnatakiwa kuwasamehe watu wote, **M&M** 64:10. Kwa kuwa mmesameheana ninyi kwa ninyi makosa yenu, hata Mimi, Bwana, ninawasamehe, **M&M** 82:1. Kwao wao niwapendao Mimi pia huwarudi, ili dhambi zao zipate kusamehewa, **M&M** 95:1.

Nimekusamehe uvunjaji wako wa sheria, **Musa** 6:53.

Samsoni

Katika Agano la Kale, ni mwamuzi wa Kumi na Mbili katika "waamuzi" wa Israeli. Yeye alijulikana kwa ajili ya nguvu zake kuu za kimwili, lakini hakuwa na busara katika baadhi ya maamuzi na matendo ya kimaadili (Amu. 13:24–16:31).

Samu. *Ona pia* Lehi, Baba wa Nefi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana wa tatu wa Lehi (1 Ne. 2:5). Alikuwa mtu wa haki na mtakatifu aliyechagua kumfuata Bwana (1 Ne. 2:17; 2 Ne. 5:5–6; Alma 3:6).

Samweli, Nabii wa Agano la Kale

Mwana wa Elkana na Hanna, Samweli alizaliwa kama jibu la sala za mama yake (1 Sam. 1). Akiwa mdogo aliwekwa katika usimamizi wa Eli, kuhani mkuu katika hema huko Shilo (1 Sam. 2:11; 3:1). Bwana alimwita Samweli kuwa nabii katika umri mdogo (1 Sam. 3). Baada ya kifo cha Eli, Samweli akawa ndiye nabii na mwamuzi mkuu wa Israeli na akarejesha sheria, taratibu, na ibada za kawaida kidini katika nchi (1 Sam. 4:15–18; 7:3–17).

1 Samweli 28:5–20 ni historia ya Samweli alivyoamriwa kurudi kutoka kwa wafu na mchawi wa Endori kwa ombi la Mfalme Sauli. Hili lisingeweza kuwa ono kutoka kwa Mungu, kwa sababu mchawi au mtu mwingine yeyote aliye hai anayedai kuwasiliana na roho za wafu hawezi kumfanya nabii ajitokeze kwa ombi lake.

Kitabu cha 1 na 2 Samweli: Katika baadhi ya Biblia, vitabu 1 na 2 Samweli ni kitabu kimoja. Katika nyingine ni vitabu viwili. Vitabu hivi vinachukua kipindi cha takribani miaka 130, tangu kuzaliwa kwa Samweli hadi kabla tu ya kifo cha Daudi.

Kitabu cha 1 Samweli: Mlango 1–3 inaeleza kwamba Bwana aliilaani na kuiadhibu familia ya Eli na akamwita Samweli kuwa kuhani na mwamuzi mkuu. Mlango 4–6 inaelezea namna sanduku la agano lilivyoangukia katika mikono ya Wafilisti. Mlango wa 7–8 inaandikwa maonyo ya Samweli juu ya kuwa na miungu wa uongo na mfalme mwovu. Mlango 9–15 inaelezea kuvikwa kwa taji la ufalme kwa Sauli na utawala wake kama mfalme. Mlango 16–31 ni historia ya Daudi na kujipatia kwake madaraka—Samweli alimpaka mafuta Daudi aliyemwua Goliati. Sauli alimchukia Daudi, lakini Daudi alikataa kumuua Sauli ingawa alipata nafasi ya kufanya hivyo.

Kitabu cha 2 Samweli: Kitabu kina maelezo marefu juu ya utawala wa Daudi kama mfalme wa Yuda na hatimaye wa Israeli yote. Mlango wa 1–4 inaonyesha mapambano marefu kati ya wafuasi wa

Daudi baada ya kuvikwa taji la kifalme na Yuda, na wafuasi wa Sauli. Mlango wa 5–10 inamwonyesha Daudi anakuwa mwenye nguvu sana katika nchi nyingi. Mlango wa 11–21 inaonyesha kushuka kwa nguvu za kiroho za Daudi kwa sababu ya dhambi zake na uasi ndani ya familia yake mwenyewe. Mlango wa 22–24 inaelezea jaribio la Daudi la kujipatanisha na Bwana.

Samweli Mlamani

Nabii Mlamani katika Kitabu cha Mormoni aliyetumwa na Bwana kufundisha na kuwaonya Wanefi muda mfupi kabla ya kuzaliwa kwa Mwokozi. Samweli alitoa unabii juu ya ishara zilizohusiana na kuzaliwa na kifo cha Yesu Kristo na juu ya angamizo la Wanefi (Hel. 13–16).

Sanduku la Agano. *Ona pia* Hema

Pia hujulikana kama Sanduku la Yehova na Sanduku la Ushuhuda, Sanduku la Agano lilikuwa kasha la mstatili au sanduku lililotengenezwa kwa mbao zilizofunikwa kwa dhahabu. Lilikuwa ni alama iliyokuwa ya zamani na takatifu zaidi katika dini ya Waisraeli. Kiti cha Rehema ambacho kilitengeneza maficho yake kiliheshimiwa kama mahali akaapo Yehova hapa duniani (Ku. 25:22). Wakati hekalu lilipokamilika, sanduku liliwekwa katika Patakatifu pa Patakatifu, mahali patakatifu zaidi kuliko pengine katika jengo lile (1 Fal. 8:1–8).

Musa alilitengeneza sanduku kwa amri ya Mungu, **Ku.** 25. Watoto wa Lawi walipewa jukumu la kulitunza sanduku, **Hes.** 3:15, 31. Sanduku la agano liliwatangulia, **Hes.** 10:33. Twaeni kitabu hiki cha torati, na mkiweke ndani ya sanduku la agano, **Kum.** 31:24–26. Maji ya Yordani yakatindika mbele ya sanduku la agano, **Yos.** 3:13–17; 4:1–7. Makuhani walichukua sanduku la agano katika kuiteka Yeriko, **Yos.** 6:6–20. Wafilisti walilikamata sanduku la Mungu, **1 Sam.** 5. Bwana akaibariki nyumba ya Obed-edomu kwa sababu ya sanduku la Mungu, **2 Sam.** 6:11–12. Uza aliuawa na Bwana wakati kwa kiburi alipojaribu kulituliza sanduku, **1 Nya.** 13:9–12 (M&M 85:8). Mjengeeni Bwana Mungu mahali patakatifu, ili kulileta sanduku la agano, **1 Nya.** 22:19.

Yaliyomo ndani ya sanduku la agano yanaelezwa, **Ebr.** 9:4.

Sanhedrini. *Ona pia* Wayahudi

Seneti ya Kiyahudi na baraza la juu zaidi la Kiyahudi katika mashauri yote ya Kiraia na kidini. Sanhedrini linaundwa na washiriki sabini na mmoja waliochaguliwa kutoka miongoni mwa makuhani wakuu, waandishi, na wazee. Katika maandiko, mara kwa mara huitwa baraza (Mt. 26:59; Mk. 14:55; Mdo. 5:34).

Sara. *Ona pia* Ibrahimu

Katika Agano la Kale, ni mke wa kwanza wa Ibrahimu. Katika umri wake wa uzee akawa mama wa Isaka (Mwa. 18:9–15; 21:2).

Saria. *Ona pia* Lehi, Baba wa Nefi

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mke wa Lehi (1 Ne. 5:1–8; 8:14–16; 18:19) na mama wa Lamani, Lemueli, Samu, Nefi, Yakobo, Yusufu, na mabinti kadhaa (1 Ne. 2:5; 2 Ne. 5:6).

Sauli, Mfalme wa Israeli

Katika Agano la Kale, ni mfalme wa kwanza wa Israeli kabla haijagawanyika. Ingawa alikuwa mwadilifu mwanzoni mwa utawala wake, hatimaye akawa amejaa kiburi na akawa siyo mtiifu kwa Mungu (1 Sam. 9–31).

Sauli wa Tarsisi. *Ona* Paulo

Sauti. *Ona pia* Ufunuo

Kama inavyotumika katika maandiko, wakati mwingine ujumbe unaosikika ukisemwa na Bwana au wajumbe Wake. Sauti ya Roho yaweza pia kuwa isiyosikika na ikaelekezwa moyoni au akilini.

Adamu na Hawa walisikia sauti ya

Bwana Mungu, **Mwa.** 3:8 (Musa 4:14). Bwana alinena na Eliya katika sauti ndogo ya utulivu, **1 Fal.** 19:11–13.

Walio waadilifu huisikia sauti ya Mchungaji Mwema, **Yn.** 10:1–16. Kila mmoja aliye wa kweli huisikia sauti yangu, **Yn.** 18:37.

Niliitii sauti ya Roho, **1 Ne.** 4:6–18. Ikaja sauti kwangu, ikisema: Enoshi, dhambi zako zimesamehewa, **Eno.** 1:5. Ilikuwa sauti tulivu ya ulaini mkamilifu na ilipenya hata kwenye roho, **Hel.** 5:29–33 (3 Ne. 11:3–7).

Iwe kwa sauti yangu mwenyewe au kwa sauti ya watumishi wangu, ni sawa, **M&M** 1:38. Lolote watakalosema wakati wanaongozwa na Roho Mtakatifu litakuwa sauti ya Bwana, **M&M** 68:2–4. Kila mtu ambaye hutii sauti yangu atauona uso wangu na kujua kuwa Mimi ndimi, **M&M** 93:1.

Sayuni. *Ona pia* Henoko; Yerusalemu Mpya

Walio safi moyoni (M&M 97:21). Sayuni pia humaanisha mahali ambapo walio safi moyoni huishi. Mji uliojengwa na Henoko na watu wake ambao hatimaye ulitwaliwa mbinguni kwa sababu ya uadilifu uliitwa Sayuni (M&M 38:4; Musa 7:18–21, 69). Katika siku za mwisho mji uliopewa jina la Sayuni utajengwa karibu na Wilaya ya Jackson, Missouri (Marekani), ambako makabila ya Israeli yatakusanyika (M&M 103:11–22; 133:18). Watakatifu wanashauriwa kuijenga Sayuni mahali popote wanapoishi ulimwenguni.

Mji wa Daudi uliitwa Sayuni, **1 Fal.** 8:1. Kutoka Sayuni itatoka sheria, **Isa.** 2:2–3 (Mika 4:2; 2 Ne. 12:2–3). Mkombozi atakuja Sayuni, **Isa.** 59:20. Nami nitatwaa mtu mmoja wa mji mmoja, na wawili wa familia moja, nami nitawaleta hata Sayuni, **Yer.** 3:14. Katika mlima Sayuni na katika Yerusalemu wataokolewa, **Yoe.** 2:32 (Oba. 1:17).

Heri wale ambao watatafuta kuijenga Sayuni yangu, **1 Ne.** 13:37. Mabinti wa Sayuni wana kiburi, **2 Ne.** 13:16 (Isa. 3:16). Ole wake yule mwenye kustarehe katika Sayuni, **2 Ne.** 28:19–25.

Tafuta kuijenga na kuliimarisha kusudi la Sayuni, **M&M** 6:6 (M&M 11:6). Yeye nimemwongoza kuendesha kusudi la Sayuni katika uwezo mwingi kwa ajili ya mema, **M&M** 21:7. Yerusalemu Mpya itaitwa Sayuni, **M&M** 45:66–67. Independence, Missouri ndipo mahali pa mji wa Sayuni, **M&M** 57:1–3. Mjeledi unabaki juu ya watoto wa Sayuni hadi watakapotubu, **M&M** 84:58.

Bwana aliwaita watu wake Sayuni, kwa sababu walikuwa wenye moyo mmoja na nia moja, **Musa** 7:18–19. Sayuni (Yerusalemu Mpya) itajengwa katika ya bara la Marekani, **M ya I** 1:10.

Sengenya. *Ona pia* Kusema uovu; Uvumi

Kutoa siri za mtu au taarifa juu ya mtu mwingine pasipo idhini ya mtu huyo.

Kila neno lisilofaa ambalo mtu atalisema, atajibu juu yake, **Mt.** 12:36. Watakatifu wanaonywa wasiwe wafitini na wadaku, wakizungumza mambo ambayo hawapaswi kuzungumza, **1 Tim.** 5:11–14.

Usimseme mabaya jirani yako, **M&M** 42:27. Waimarishe ndugu zako katika mazungumzo yako yote, **M&M** 108:7.

Serikali. *Ona* Utawala

Seti. *Ona pia* Adamu

Katika Agano la Kale, ni mwana mwadilifu wa Adamu na Hawa.

Seti alikuwa mtu mkamilifu, na sura yake ilikuwa kwa mfano halisi wa baba yake, **M&M** 107:42–43 (Mwa. 5:3). Seti alikuwa miongoni mwa wenye nguvu katika ulimwengu wa roho, **M&M** 138:40.

Mungu alijifunua mwenyewe kwa Seti, **Musa** 6:1–3, 8–14.

Shadraka. *Ona pia* Danieli

Katika Agano la Kale, Shadraka, Meshaki, na Abednego walikuwa vijana watatu wa Kiisraeli ambao, pamoja na Danieli, waliingizwa katika kasri ya

Nebukadneza, mfalme wa Babiloni. Jina la Kiebrania la Shadraka lilikuwa Hanania. Vijana hawa wanne walikataa kujitia najisi wao wenyewe kwa kula nyama na mvinyo wa mfalme (Dan. 1). Shadraka, Meshaki, na Abednego walitupwa na mfalme katika tanuri la moto mkali lakini kimuujiza wakaokolewa (Dan. 3).

Shahidi, Ushahidi. *Ona pia* Ushuhuda

Taarifa au ushahidi mwingine kwamba jambo fulani ni la kweli; ushuhuda. Shahidi anaweza pia kwani mtu fulani anayetoa taarifa juu ya jambo au ushahidi unaotokana na ufahamu wake; maana yake, ni mtu anayetoa ushuhuda.

Usishuhudie uongo, **Ku.** 20:16.

Injili itahubiriwa ulimwenguni kote kama ushuhuda kwa mataifa yote, **Mt.** 24:14 (JS—M 1:31). Mtakuwa mashahidi kwangu, **Mdo.** 1:8. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, **Rum.** 8:16 (1 Yoh. 5:6).

Mko radhi kusimama kama mashahidi wa Mungu nyakati zote, **Mos.** 18:8–9. Tunapokea sakramenti ili kushuhudia kwa Baba kwamba tutazishika amri na daima tutamkumbuka Yesu, **3 Ne.** 18:10–11 (Moro. 4–5; M&M 20:77–79). Hampati ushahidi hadi baada ya majaribu ya imani yenu, **Eth.** 12:6.

Sheria ya mashahidi: katika vinywa vya mashahidi wawili au watatu kila neno litathibitika, **M&M** 6:28 (Kum. 17:6; Mt. 18:16; 2 Kor. 13:1; Eth. 5:4; M&M 128:3). Nimewatawaza kuwa Mitume na mashahidi maalumu wa jina langu, **M&M** 27:12 (M&M 107:23). Sabini wameitwa ili kuwa mashahidi maalumu kwa Wayunani na ulimwenguni kote, **M&M** 107:25. Acha awepo na mwandishi, naye awe shahidi wa ubatizo wenu kwa kuona kwa macho, **M&M** 127:6 (M&M 128:2–4).

Shamba. *Ona pia* Shamba la mizabibu la Bwana; Ulimwengu

Katika maandiko, ni eneo la wazi la ardhi litumikalo kwa kulima au uchungaji. Mara nyingi linaashiria ulimwengu na watu wake.

Lile shamba ni ulimwengu, **Mt.** 13:38. Ufalme wa mbinguni ni sawa na hazina iliyo sitirika katika shamba, **Mt.** 13:44.

Niliona shamba kubwa na pana, **1 Ne.** 8:9, 20. Shamba lilikuwa limeiva, **Alma** 26:5.

Shamba li jeupe tayari kwa mavuno, **M&M** 4:4 (M&M 6:3; 11:3; 12:3; 14:3; 31:4; 33:3, 7). Shamba lilikuwa ulimwengu, **M&M** 86:1–2. Nitalinganisha falme hizi na mtu mwenye shamba, **M&M** 88:51.

Shamba la mizabibu la Bwana. *Ona pia* Israeli; Shamba

Ishara ya shamba la kazi za kiroho. Katika maandiko shamba la mizabibu la Bwana kwa kawaida humaanisha nyumba ya Israeli au ufalme wa Mungu duniani. Wakati mwingine humaanisha watu wa ulimwengu kwa ujumla.

Shamba la mizabibu la Bwana wa Majeshi ni nyumba ya Israeli, **Isa.** 5:7 (2 Ne. 15:7).

Yesu alitoa mfano wa watumishi katika shamba la mizabibu, **Mt.** 20:1–16.

Israeli ni kama mzeituni uliotunzwa katika shamba la mizabibu la Bwana, **Yak. (KM)** 5. Watumishi wa Bwana watapogoa shamba lake la mizabibu kwa mara ya mwisho, **Yak. (KM)** 6.

Bwana atawabariki wote ambao wanatumika katika shamba la mizabibu, **M&M** 21:9 (Alma 28:14). Tumikeni ninyi katika shamba langu la mizabibu kwa mara ya mwisho, **M&M** 43:28.

Shangwe. *Ona pia* Mtiifu, Tii, Utii

Hali ya furaha kuu inayokuja kutokana na maisha ya uadilifu. Madhumuni ya maisha katika mwili wenye kufa ni kwa watu wote kuwa na shangwe (2 Ne. 2:22–25). shangwe kamilifu itakuja tu kupitia kwa Yesu Kristo (Yn. 15:11; M&M 93:33–34; 101:36).

Wapole pia wataongeza shangwe yao katika Bwana, **Isa.** 29:19 (2 Ne. 27:30).

Ninakuletea habari njema ya shangwe kuu, **Lk.** 2:10. shangwe yenu hakuna mtu awaondoleaye, **Yn.** 16:22. Tunda la Roho ni upendo, shangwe, amani, **Gal.** 5:22.

Tunda lake lilijaza nafsi yangu kwa shangwe isiyo kifani, **1 Ne.** 8:12. Wanadamu wapo ili wapate kuwa na shangwe, **2 Ne.** 2:25. shangwe ya waadilifu itakuwa tele milele, **2 Ne.** 9:18. Wataweza kukaa na Mungu katika hali ya furaha isiyo na mwisho, **Mos.** 2:41. Nitaachia yote ninayo yamiliki ili nipate kupokea shangwe hii iliyo kuu, **Alma** 22:15. Huenda nikawa chombo mikononi mwa Mungu kuzileta baadhi ya nafsi kwenye toba, na hii ndiyo shangwe yangu, **Alma** 29:9. Ni shangwe gani, na nuru gani ya maajabu niliyoiona, **Alma** 36:20.

Roho wangu ataijaza nafsi yako kwa shangwe, **M&M** 11:13. Shangwe itakuwa kubwa namna gani pamoja naye katika ufalme wa Baba yangu, **M&M** 18:15–16. Katika ulimwengu huu furaha yenu si kamilifu, bali ndani yangu shangwe yenu ni kamilifu, **M&M** 101:36.

Katika maisha haya nitakuwa na shangwe, **Musa** 5:10–11.

Shauri

Kama lilivyotumika katika maandiko, shauri maana yake ni nasihi au fundisha.

Nakupa shauri ununue kwangu dhahabu iliyosafishwa kwa moto, **Ufu.** 3:18.

Msijaribu kumshauri Bwana, **Yak. (KM)** 4:10. Yeye hushauri kwa hekima juu ya kazi zake zote, **Alma** 37:12.

Dhambi zako zimepanda juu hadi kwangu kwa sababu unataka shauri katika njia zako mwenyewe, **M&M** 56:14.

Shawishi. *Ona* Maongozi ya Mungu, Shawishi

Shemasi. *Ona pia* Ukuhani wa Haruni

Wito katika huduma ya Kanisa wakati wa Mtume Paulo (Flp. 1:1; 1 Tim. 3:8–13) na ni ofisi katika Ukuhani wa Haruni (M&M 20:38, 57–59; 84:30, 111; 107:85).

Shemu. *Ona pia* Nuhu, Patriaki wa Biblia

Katika Agano la Kale, ni mwana mwadilifu wa Nuhu na, kulingana na desturi, ni mhenga wa Washemiti, au Semiti, pamoja na Waarabu, Waebrania, Wababilonia, Waashuri, Wafoenike, na Waashuru (Mwa. 5:29–32; 6:10; 7:13; 9:26; 10:21–32; Musa 8:12). Katika ufunuo wa siku za mwisho Shemu anaelezwa kama "yule kuhani mkuu sana" (M&M 138:41).

Sheremu. *Ona pia* Mpinga Kristo

Mtu aliye katika Kitabu cha Mormoni ambaye alimkana Kristo na akadai ishara (Yak. [KM] 7:1–20).

Sheria. *Ona pia* Amri za Mungu; Baraka, Bariki, Barikiwa; Mtiifu, Tii, Utii; Torati ya Musa

Amri au masharti ya Mungu ambayo juu yake baraka na adhabu zote husimama kote mbinguni na duniani. Wale wanaotii sheria za Mungu hupokea baraka zilizoahidiwa. Joseph Smith Nabii alifundisha ya kuwa watu ni lazima pia watii, waheshimu, na kuzikubali sheria za nchi (M ya I 1:12).

Torati ya Musa ilikuwa ni sheria ya matayarisho ya kuwaleta wanaume na wanawake kwa Kristo. Ilikuwa sheria yenye maamrisho, maelekezo, na ibada. Siku hizi sheria ya Kristo, ambayo inatimiliza torati ya Musa, ni utimilifu wa injili au "sheria kamilifu iliyo ya uhuru" (Yak. [Bib.] 1:25).

Mungu alitoa amri kwa Adamu, **Mwa.** 1:28; 2:16–17. Mungu alitoa sheria kwa Nuhu, **Mwa.** 9:1. Sheria ya Bwana ni kamilifu, yabadilisha nafsi, **Zab.** 19:7. Bwana ndiye mtoasheria wetu, **Isa.** 33:22.

Kuna mtoasheria mmoja, **Yak. (Bib.)** 4:12.

Pasipokuwa na sheria, hakuna

adhabu, **2 Ne.** 9:25. Kuna sheria iliyotolewa, **Alma** 42:17–22. Wanadamu watahukumiwa kulingana na sheria, **Alma** 42:23. Kristo ndiye sheria, **3 Ne.** 15:9.

Sheria zote ni za kiroho, **M&M** 29:34. Joseph Smith alipokea sheria ya Kanisa kwa ufunuo, **M&M** 42. Mtu ashikaye sheria ya Mungu hana haja ya kuvunja sheria za nchi, **M&M** 58:21. Nuru ya Kristo ndiye sheria ambayo kwayo vitu vyote hutawaliwa, **M&M** 88:7–13. Yeye ametoa sheria kwa vitu vyote, **M&M** 88:42–43. Watu wanapaswa kushika sheria ya nchi, **M&M** 98:4–5. Tupatapo baraka kutoka kwa Mungu, ni kutokana na utiifu kwa sheria, **M&M** 130:20–21. Kanisa lilitangaza imani yake kuhusu sheria za nchi, **M&M** 134.

Mwanadamu anaokolewa kutokana na utiifu kwa sheria na ibada za injili, **M ya I** 1:3.

Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu. *Ona pia* Mpango wa Ushirika; Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni

Kuweka kitu kwa kusudi takatifu, kuifanya iwe takatifu, au kuwa ya haki. Sheria ya kuweka wakfu ni kanuni ya kiungu ambayo kwayo wanaume na wanawake kwa hiari hutoa wakati wao, vipaji, na utajiri wa mali yao kwa ajili ya kustawisha na kuujenga ufalme wa Mungu.

Jiwekeni wakfu kwa Bwana leo, **Ku.** 32:29.

Wote walioamini walikuwa na vitu vyote shirika, **Mdo.** 2:44–45.

Walikuwa na vitu vyote sawa miongoni mwao; kwa sababu hiyo hapakuwa na tajiri na maskini, **4 Ne.** 1:3.

Bwana alifafanua kanuni za kuweka wakfu, **M&M** 42:30–39 (M&M 51:2–19; 58:35–36). Mtu mmoja asimiliki vingi zaidi kuliko mwingine, **M&M** 49:20. Kila mtu alipewa sehemu sawa kulingana na familia yake, **M&M** 51:3. Utaratibu ulianzishwa ili Watakatifu waweze kuwa sawa katika mambo yote ya kimbinguni na ya kidunia, **M&M** 78:4–5. Kila mtu alitakiwa kuwa na haki sawa kulingana na matakwa yake na mahitaji yake, **M&M** 82:17–19. Sayuni yaweza kujengwa tu kwa kanuni za sheria ya selestia, **M&M** 105:5.

Watu wa Henoko walikuwa wa moyo mmoja na akili moja na walikaa katika haki na hapakuwa na maskini miongoni mwao, **Musa** 7:18.

Shetani. *Ona* Ibilisi

Shibloni. *Ona pia* Alma, Mwana wa Alma

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana wa Alma Mdogo. Shibloni alifundisha injili kwa Wazorami na akateswa kwa ajili ya uadilifu wake. Bwana akamwokoa kutoka katika mateso yake kwa sababu ya uaminifu wake na uvumilivu (Alma 38). Shibloni pia alitunza kumbukumbu ya Wanefi kwa wakati fulani (Alma 63:1–2, 11–13).

Shida. *Ona pia* Jaribu, Majaribu; Mateso, Tesa; Rudi, Kurudiwa; Stahimili

Kupitia shida—majaribu, dhiki, na huzuni—mwanadamu aweza kupata matatizo mengi ambayo humpeleka katika makuzi ya kiroho na makuzi ya milele kwa kumgeukia Bwana.

Mungu mwenyewe ndiye aliyewaokoa ninyi katika shida zenu zote na taabu zenu, **1 Sam.** 10:19. Wakamlilia Bwana katika dhiki zao, **Zab.** 107:6, 13, 19, 28. Ingawa Bwana atawapeni chakula cha shida, lakini walimu wako hawataondolewa, **Isa.** 30:20–21.

Kwani lazima kuwe na upinzani katika mambo yote, **2 Ne.** 2:11.

Kama kamwe hawakuonja machungu, wasingeliweza kuyajua matamu, **M&M** 29:39. Shida zako zitakuwa kwa muda mfupi tu, **M&M** 121:7–8. Mambo haya yote yatakupa wewe uzoefu, nayo yatakuwa kwa faida yako, **M&M** 122:5–8.

Wanaonja machungu, ili wapate kujua kutuza chema, **Musa** 6:55.

Shizi. *Ona pia* Wayaredi

Kiongozi wa kijeshi wa Wayaredi katika Kitabu cha Mormoni. Alikufa mwishoni mwa vita vikuu ambavyo viliangamiza taifa zima la Yaredi (Eth. 14:17–15:31).

Shuhudia. *Ona pia* Ushuhuda

Kutoa ushuhuda kwa uwezo wa Roho Mtakatifu; kutoa tamko la dhati la ukweli lililojengwa juu ya ufahamu au imani ya mtu.

Mfariji atanishuhudia mimi, **Yn.** 15:26. Akatuamuru kuhubiri na kushuhudia, **Mdo.** 10:42.

Mashahidi watatu wataushuhudia ukweli, **2 Ne.** 27:12. Uwezo wa Roho Mtakatifu huuchukua hadi katika mioyo ya watoto wa watu, **2 Ne.** 33:1. Maandiko yanamshuhudia Kristo, **Yak. (KM)** 7:10–11 (Yn. 5:39). Ninawashuhudia kwamba ninajua mambo haya ambayo nimesema ni ya kweli, **Alma** 5:45 (Alma 34:8).

Mtayashuhudia kwa uwezo wa Mungu, **M&M** 17:3–5. Kile ambacho Roho hukushuhudia, yakupasa kufanya, **M&M** 46:7. Nimewatuma ninyi kwenda kushuhudia na kuwaonya, **M&M** 88:81.

Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani. *Ona pia* Baraka, Bariki, Barikiwa; Kuabudu

Shukrani kwa baraka zilizopokelewa kutoka kwa Mungu. Kuelezea shukrani kunampendeza Mungu, na ibada ya kweli inajumuisha kumshukuru Yeye. Tunapaswa kutoa shukrani kwa Bwana kwa ajili ya mambo yote.

Ni jambo jema kumshukuru Bwana, **Zab.** 92:1. Tuje mbele zake kwa kutoa shukrani, **Zab.** 95:1–2. Mshukuruni, na kulibariki jina lake, **Zab.** 100.

Siachi kutoa shukrani, **Efe.** 1:15–16. Iweni wenye shukrani, **Kol.** 3:15. Baraka, na utukufu, na shukrani, na heshima ziwe kwa Mungu wetu, **Ufu.** 7:12.

Ee! ni jinsi gani inawapasa kumshukuru Mfalme wenu wa Mbinguni, **Mos.** 2:19–21. Muishi katika kutoa shukrani kila siku, **Alma** 34:38. Uamkapo asubuhi acha moyo wako ujae shukrani kwa Mungu, **Alma** 37:37.

Yawapasa kufanya mambo yote kwa sala na kwa kutoa shukrani, **M&M** 46:7. Lazima mtoe shukrani kwa Mungu, **M&M** 46:32. Fanya mambo haya kwa kutoa shukrani, **M&M** 59:15–21. Pokea baraka hizi kutoka katika mkono wa Bwana, kwa moyo wenye shukrani, **M&M** 62:7. Mwenye kupokea mambo yote kwa shukrani atatukuzwa, **M&M** 78:19. Toa shukrani katika kila jambo, **M&M** 98:1 (1 The. 5:18). Msifuni Bwana kwa sala ya sifa na kwa kutoa shukrani, **M&M** 136:28.

Shule ya Manabii. *Ona pia* Smith, Joseph, Mdogo

Katika Kirtland, Ohio, (Marekani), katika wakati wa majira ya baridi ya mwaka 1832–1833, Bwana alimwamuru Joseph Smith kuanzisha shule kwa madhumuni ya kuwafundisha ndugu viongozi wa kanisa mambo yote yahusuyo injili na ufalme wa Mungu. Viongozi wengi wa mwanzoni wa Kanisa walikuja kutoka miongoni mwa wale waliohudhuria shule hii. Shule nyingine ya manabii au wazee iliendeshwa na Parley P. Pratt katika Wilaya ya Jackson, Missouri (M&M 97:1–6). Shule za aina hiyo hiyo zilianzishwa muda mfupi tu baada ya Watakatifu kuhamia magharibi; hata hivyo, hizi zilikatizwa muda mfupi tu. Kufundisha injili siku hizi kunafanyika majumbani, katika akidi za ukuhani na makundi mengine kadha wa kadha na kupitia shule za Kanisa na seminari na madarasa rasmi ya mafundisho.

Jitakaseni wenyewe na mfundishane mafundisho ya ufalme, **M&M** 88:74–80. Tafuteni kwa bidii, na kufundishana, **M&M** 88:118–122. Utaratibu juu ya shule ya manabii uliwekwa, **M&M** 88:127–141. Urais wa Kwanza

unashikilia funguo za shule ya manabii, **M&M** 90:6–7.

Shutuma, Shutumu. *Ona pia* Amua, Hukumu; Hukumu ya mwisho

Kuamua au kutiwa hatiani na Mungu.

Mungu atamhukumu mtu mwenye hila, **Mit.** 12:2.

Twarudiwa na Bwana, ili tusipaswe kuhukumiwa pamoja na ulimwengu, **1 Kor.** 11:32.

Maneno yetu, matendo, na mawazo yetu yatatuhukumu, **Alma** 12:14. Kwa kujua mambo na kuacha kuyatenda, watu huwa chini ya hukumu, **Hel.** 14:19. Kama tutakoma kufanya kazi, itatupasa kuwekwa chini ya hukumu, **Moro.** 9:6.

Mtu asiye msamehe ndugu yake husimama akiwa na hatia mbele ya Bwana, **M&M** 64:9. Yule atendaye dhambi dhidi ya nuru kubwa zaidi atapokea hukumu kubwa zaidi, **M&M** 82:3. Kanisa lote liko chini ya hatia hadi watakapotubu na kukumbuka Kitabu cha Mormoni, **M&M** 84:54–57.

Sifu. *Ona* Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani; Utukufu

Sikiliza. *Ona pia* Mtiifu, Tii, Utii; Sikio

Kusikia na kutii sauti au mafundisho ya Bwana.

Bwana atamwinua nabii kama Musa, na watu wanapaswa kumsikiliza yeye, **Kum.** 18:15. Kusikia ni bora kuliko mafuta ya beberu wa dhabihu, **1 Sam.** 15:20–23. Hatukuwasikiliza watumishi wa Bwana, manabii, **Dan.** 9:6.

Watu wenye haki wasikilizao maneno ya manabii hawataangamia, **2 Ne.** 26:8. Kama hamtasikia sauti ya mchungaji mwema, ninyi si kondoo wake, **Alma** 5:38 (Hel. 7:18).

Sikilizeni, Enyi watu wa kanisa langu, **M&M** 1:1. Wale waisikilizao sauti ya Roho huangazwa na kuja kwa Baba, **M&M** 84:46–47. Wao walikuwa wavivu kuisikiliza sauti ya Bwana; kwa hiyo, naye amekuwa mzito kuzisikiliza sala zao, **M&M** 101:7–9. Wale ambao hawasikii amri huwarudi, **M&M** 103:4 (Musa 4:4).

Sikio. *Ona pia* Sikiliza

Katika maandiko sikio mara nyingi limetumika kama alama ya uwezo wa mtu wa kusikia na kuelewa mambo ya Mungu.

Wanayo masikio, lakini hawasikii, **Zab.** 115:6. Bwana huniamsha sikio langu lipate kusikia, **Isa.** 50:4–5 (2 Ne. 7:4–5).

Mwenye masikio ya kusikia, na asikie, **Mt.** 11:15. Masikio yao hayasikii, **Mt.** 13:15 (Musa 6:27). Jicho haliyaoni wala sikio halikuyasikia mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao, **1 Kor.** 2:9 (M&M 76:10).

Ibilisi anong'ona masikioni mwao, **2 Ne.** 28:22. Fungueni masikio yenu ili mpate kusikia, **Mos.** 2:9 (3 Ne. 11:5). Niliitwa mara nyingi, na sikutaka kusikia, **Alma** 10:6. Yapeni sikio maneno yangu, **Alma** 36:1 (Alma 38:1; M&M 58:1).

Hakuna sikio ambalo halitasikia, **M&M** 1:2. Masikio hufunguliwa kwa njia ya unyenyekevu na sala, **M&M** 136:32.

Siku ya Bwana. *Ona* Hukumu ya mwisho; Siku ya Sabato; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo

Siku ya Sabato. *Ona pia* Pumzika; Umba, Uumbaji

Siku takatifu iliyotengwa kila wiki kwa ajili ya kupumzika na kuabudu. Baada ya Mungu kuumba vitu vyote, Alipumzika siku ya saba na akaamuru kwamba siku moja katika kila wiki iwe siku ya kupumzika ili kuwasaidia watu kumkumbuka Yeye (Ku. 20:8–11).

Kabla ya kufufuka kwa Yesu Kristo, waumini wa Kanisa waliiheshimu siku ya mwisho ya wiki kama Sabato, kama walivyofanya Wayahudi. Baada ya Ufufuko, waumini wa Kanisa, wawe Wayahudi au Wayunani, waliiheshimu siku ya kwanza ya wiki (ile siku ya Bwana) ili kukumbuka Ufufuko wa Bwana.

Kanisa siku hizi huendelea kuheshimu siku moja ya wiki kama siku takatifu ya Sabato ambapo siku hiyo humuabudu Mungu na kupumzika kutokana na kazi za ulimwengu.

Sabato huwakumbusha watu juu ya umuhimu wao wa chakula cha kiroho na wajibu wao wa kumtii Mungu. Wakati taifa linapokuwa halijali katika kutii Sabato, hali zote za maisha huathirika na maisha yake ya kidini huoza (Neh. 13:15–18; Yer. 17:21–27).

Mungu alipumzika siku ya saba, **Mwa.** 2:1–3. Wana wa Israeli hawakuokota mana katika siku ya sabato, **Ku.** 16:22–30. Kumbuka siku ya sabato, ili kuishika kitakatifu, **Ku.** 20:8–11 (Mos. 13:16–19). Sabato ilitolewa kama ishara kati ya Mungu na mwanadamu, **Ku.** 31:12–17 (Eze. 20:12, 20). Hatupaswi kununua au kuuza siku ya sabato, **Neh.** 10:31. Ita siku ya sabato kuwa siku ya furaha, kwa kumheshimu Bwana na siyo kutafuta furaha yako wewe mwenyewe, **Isa.** 58:13–14.

Sabato ilitengenezwa kwa ajili ya mwanadamu na siyo mwanadamu kwa ajili ya sabato, **Mk.** 2:23–28. Mwana wa mtu ndiye Bwana wa Sabato, **Lk.** 6:1–10. Yesu alifundisha katika sinagogi na kuponya siku ya Sabato, **Lk.** 13:10–14.

Wanefi waliishika kitakatifu siku ya sabato, **Yar.** 1:5. Ikumbukeni siku ya sabato kuishika kitakatifu, **Mos.** 18:23.

Toa sakramenti zako katika siku yangu takatifu, **M&M** 59:9–13. Wakazi wa Sayuni wataiheshimu siku ya sabato, **M&M** 68:29.

Mimi, Mungu, nilipumzika siku ya saba kutokana na kazi yangu yote, **Musa** 3:1–3 (Mwa. 2:1–3; Ibr. 5:1–3).

Siku za Mwisho. *Ona pia* Ishara za Nyakati; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo

Wakati ambao sasa tunaishi. Siku (au kipindi cha wakati) ambazo ni mara kabla ya Ujio wa Pili wa Bwana.

Niwaambie yatakayowapata siku za mwisho, **Mwa.** 49:1. Siku ya mwisho Mkombozi atasimama juu ya dunia, **Ayu.** 19:25. Katika siku za mwisho, nyumba ya Bwana itawekwa imara, **Isa.** 2:2.

Katika siku za mwisho kutakuja nyakati za hatari, **2 Tim.** 3:1–7. Wadhihaki wa siku ya mwisho watakana Ujio wa Pili, **2 Pet.** 3:3–7.

Ninatoa unabii kwenu ninyi kuhusu siku za mwisho, **2 Ne.** 26:14–30.

Hivyo ndivyo kanisa langu litakavyoitwa katika siku za mwisho, hata Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, **M&M** 115:4.

Kristo atakuja katika siku za mwisho, **Musa** 7:60.

Simeoni. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mwana wa pili wa Yakobo na mkewe Lea (Mwa. 29:33; 35:23; Ku. 1:2). Aliungana na Lawi katika mauaji ya kinyama ya Washekemu (Mwa. 34:25–31). Unabii wa Yakobo juu ya Simeoni unapatikana katika Mwanzo 49:5–7.

Kabila la Simeoni: Wazao wa Simeoni mara kwa mara waliishi pamoja na kabila la Yuda na ndani ya mipaka ya ufalme wa Yuda (Yos. 19:1–9; 1 Nya. 4:24–33). Kabila la Simeoni liliungana na Yuda katika vita dhidi ya Wakanaani (Amu. 1:3, 17). Pia baadaye waliungana na majeshi ya Daudi (1 Nya. 12:25).

Simoni Mkanani

Katika Agano Jipya, ni mmoja kati ya Mitume Kumi na Wawili wa mwanzoni wa Yesu Kristo (Mt. 10:2–4).

Simoni Petro. *Ona* Petro

Sinagogi. *Ona pia* Wayahudi

Mahali pa kukutania palipotumika kwa madhumuni ya kidini. Katika nyakati za Agano Jipya, samani zake kwa ujumla zilikuwa za kawaida, zikiwa ni sanduku lenye hati ndefu za kukunja za torati na maandishi mengine

matakatifu, meza ya kusomea, na viti kwa ajili ya wenye kuabudu.

Baraza la wazee wenyeji wa eneo walisimamia kila sinagogi. Wao ndiyo walioamua nani aruhusiwe kuingia na nani atengwe (Yn. 9:22; 12:42). Ofisa muhimu zaidi alikuwa ni yule mtawala wa sinagogi hiyo (Mk. 5:22; Lk. 13:14). Kwa ujumla yeye alikuwa mwandishi, alikuwa mtunzaji wa jengo hilo, na alisimamia ibada hizo. Mhudumu alikuwa akitenda kazi za kiukarani (Lk. 4:20).

Palikuwepo sinagogi katika kila mji ambao Wayahudi walikuwa wakiishi, kote katika Palestina na kwingineko kote. Huu ulikuwa ni msaada mkubwa katika kueneza injili ya Yesu Kristo kwa sababu wamisionari wa kwanza wa Kanisa kwa kawaida waliweza kuzungumza katika masinagogi haya (Mdo. 13:5, 14; 14:1; 17:1, 10; 18:4). Desturi hii ilikuwepo miongoni mwa wamisionari katika Kitabu cha Mormoni (Alma 16:13; 21:4–5; 32:1), vile vile miongoni mwa wamisionari wa mwanzoni katika kipindi hiki (M&M 66:7; 68:1).

Sinai, Mlima. *Ona pia* Musa; Torati ya Musa

Mlima katika Rasi ya Sinai karibu na mahali ambapo Musa na Waisraeli walipiga kambi miezi mitatu baada ya kuondoka kwao Misri; pia huitwa Mlima Horebu (Ku. 3:1). Hapa ndipo Mungu alipompa Musa sheria Yake kwa ajili ya nyumba ya Israeli; hapa pia walijenga hema (Ku. 19:2; 20:18; 24:12; 32:15).

Sio mcha mungu. *Ona pia* Chafu, Uchafu; Dhambi; Kutokuwa Adilifu, Siyo Adilifu; Ovu, Uovu

Mtu fulani au jambo fulani ambalo halilingani na mapenzi au amri za Mungu; mwovu na asiye mtakatifu.

Njia ya asiye mchamungu itapotea, **Zab.** 1:6.

Kama mwenye haki ataokoka kwa shida, yule asiyemcha Mungu ataonekana wapi, **1 Pet.** 4:18.

Mjikane wenyewe kutomcha Mungu kwenu kote, **Moro.** 10:32.

Kisasi chaja upesi juu ya wasiomcha Mungu, **M&M** 97:22. Mwokozi hakupaza sauti yake miongoni mwa wasio mcha Mungu, **M&M** 138:20.

Siofaa. *Ona* Majivuno, Siofaa

Siri za Mungu

Siri za Mungu ni kweli za kiroho zijulikanazo kwa ufunuo tu. Mungu huwafunulia siri Zake wale ambao ni watiifu katika injili. Baadhi ya siri za Mungu zitaendelea kufunuliwa.

Ninyi mmejaliwa kuzijua siri za ufalme wa mbinguni, **Mt.** 13:11. Ijapokuwa nazijua siri zote, na kama sina hisani, mimi si kitu, **1 Kor.** 13:2.

Nefi alikuwa na maarifa makubwa juu ya siri za Mungu, **1 Ne.** 1:1. Wengi wamejaliwa kujua siri za Mungu, **Alma** 12:9. Kwa hao wamejaliwa kujua siri za Mungu, **Alma** 26:22. Siri hizi bado hazijajulikana kwangu kiukamilifu, **Alma** 37:11. Ziko siri nyingi ambazo hakuna mwanadamu azijuaye isipokuwa Mungu mwenyewe, **Alma** 40:3.

Siri za uchamungu ni kuu namna gani, **M&M** 19:10. Ikiwa utaomba, utapokea ufunuo na kujua siri za ufalme, **M&M** 42:61, 65 (1 Kor. 2:7, 11–14). Yeye azishikaye amri atapewa siri za ufalme, **M&M** 63:23. Kwao nitafunua siri zote, **M&M** 76:7. Ukuhani mkuu zaidi hushikilia ufunguo wa siri, **M&M** 84:19. Wakati wa kuja kwake Bwana atafunua mambo yaliyofichika ambayo hakuna mtu aliyejua, **M&M** 101:32–33. Ukuhani wa Melkizedeki utakuwa na fursa ya kupokea siri za ufalme, **M&M** 107:19.

Siyo Adilifu. *Ona* Kutokuwa Adilifu, Siyo Adilifu

Siyo na mwisho. *Ona pia* Mungu, Uungu

Moja ya majina ya Mungu lionyeshalo asili Yake ya milele (M&M 19:10–12; Musa 1:3; 7:35).

Smith, Emma Hale. *Ona pia* Smith, Joseph, Mdogo

Mke wa Joseph Smith Nabii. Bwana alimwamuru Emma kufanya uteuzi wa nyimbo. Pia alitumikia kama rais wa kwanza wa Jumuiya ya usaidizi wa Akina Mama.

Ufunuo ulitolewa juu ya mapenzi ya Bwana kwa Emma Smith, **M&M** 25. Bwana alimshauri Emma Smith juu ya ndoa, **M&M** 132:51–56.

Smith, Hyrum. *Ona pia* Smith, Joseph, Mdogo

Kaka mkubwa na mshirika mwaminifu wa Joseph Smith. Hyrum alizaliwa 9 Februari 1800. Alitumikia kama msaidizi kwa Joseph katika urais wa Kanisa, vile vile kuwa Patriaki wa pili kwa Kanisa. Mnamo 27 Juni 1844, akawa mfia dini mwenza wa Joseph gerezani la Carthage.

Mungu alifunua maelekezo kwa Hyrum kupitia kwa kaka yake Joseph, **M&M** 11; 23:3. Heri mtumishi wangu Hyrum Smith kwa sababu ya uadilifu wa moyo wake, **M&M** 124:15. Hyrum aliamriwa kuchukua ofisi ya Patriaki wa Kanisa, **M&M** 124:91–96, 124. Joseph na Hyrum waliuawa kifo cha kishahidi gerezani ya Carthage, **M&M** 135. Hyrum na roho wengine wateule walihifadhiwa ili kuja katika utimilifu wa nyakati, **M&M** 138:53.

Smith, Joseph, Mdogo. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni; Lulu ya Thamani Kuu; Mafundisho na Maagano; Ono la Kwanza; Tafsiri ya Joseph Smith (TJS); Urejesho wa Injili

Nabii aliyechaguliwa kurejesha Kanisa la kweli la Yesu Kristo duniani. Joseph Smith alizaliwa katika jimbo la Vermont katika Marekani na aliishi tangu mwaka 1805 hadi 1844.

Katika mwaka 1820, Mungu Baba na Yesu Kristo walimtokea Joseph, na alijifunza kwamba katika makanisa ya duniani hakuna hata moja lililokuwa la kweli (JS—H 1:1–20). Kisha baadaye alijiwa na malaika Moroni, aliyemfunulia mahali palipofichwa mabamba ya dhahabu ambayo yalikuwa na kumbu kumbu ya watu wa kale walioishi katika bara la Marekani (JS—H 1:29–54).

Joseph alitafsiri yale mabamba ya dhahabu na katika mwaka 1830 akayachapisha kama Kitabu cha Mormoni (JS—H 1:66–67, 75). Katika mwaka 1829, alipokea mamlaka ya ukuhani kutoka kwa Yohana Mbatizaji na Petro, Yakobo, na Yohana (M&M 13; 27:12; 128:20; JS—H 1:68–70).

Kama alivyoongozwa na Mungu, mnamo 6 Aprili 1830, Joseph na watu wengine kadhaa wakaanzisha Kanisa lililorejeshwa la Yesu Kristo (M&M 20:1–4). Chini ya uongozi wa Joseph, Kanisa lilikua katika Kanada, Uingereza, na sehemu za mashariki za Marekani, hususani katika Ohio, Missiouri, na Illinois. Mateso makali yaliwafuata Joseph na Watakatifu popote walipohamia. Mnamo 27 Juni 1844, Joseph na kaka yake Hyrum waliuawa katika kifo cha kishahidi katika Carthage, Illinois, katika Marekani.

Yusufu, mwana wa Yakobo, alitoa unabii juu ya Joseph Smith, **2 Ne.** 3:6–15.

Kwa sababu ya ufahamu Wake juu ya janga linalokuja, Bwana alimwita mtumishi wake Joseph Smith, **M&M** 1:17 (M&M 19:13). Joseph Smith alitawazwa Mtume wa Yesu Kristo na mzee wa Kwanza wa Kanisa hili, **M&M** 20:2. Joseph alitawazwa katika utume na Petro, Yakobo, na Yohana, **M&M** 27:12. Joseph na Sidney Rigdon walishuhudia ya kuwa walimwona Mzaliwa Pekee wa Baba, **M&M** 76:23. Pamoja na Oliver Cowdery, Joseph Smith alimwona Bwana katika ono, **M&M** 110:1–4. Bwana alimwita Joseph kama mzee kiongozi, mfasiri, mfunuzi, mwonaji, na nabii, **M&M** 124:125. Joseph Smith amefanya mambo zaidi kwa ajili ya wokovu wa wanadamu kuliko

mwanadamu mwingine yeyote, isipokuwa Yesu Kristo pekee, **M&M** 135:3.

Maandiko yaliyoletwa na Joseph Smith Nabii: Joseph alitafsiri sehemu ya yale mabamba ya dhahabu aliyopewa na malaika Moroni, tafsiri ambayo ilichapishwa katika mwaka 1830 kama Kitabu cha Mormoni. Pia alipokea mafunuo mengi kutoka kwa Bwana yakielezea mafundisho ya msingi na muundo wa Kanisa. Mengi ya mafunuo haya yalikusanywa katika kile ambacho sasa kinajulikana kama Mafundisho na Maagano. Pia alihusika katika kuleta Lulu ya Thamani Kuu, yenye tafsiri ya kuongozwa na Mungu ya baadhi ya maandiko ya Musa, Ibrahimu, na Mathayo, dondoo kutoka historia yake binafsi na ushuhuda, na kauli kumi na tatu za mafundisho na imani zinazoshikiliwa na Kanisa.

Smith, Joseph, Mkubwa. *Ona pia* Smith, Joseph, Mdogo; Smith, Lucy Mack

Baba wa Joseph Smith Nabii. Alizaliwa 12 Julai 1771. Alimwoa Lucy Mack, na walizaa watoto tisa (JS—H 1:4). Joseph alikuwa muumini mwaminifu katika Urejesho wa siku za mwisho na Patriaki wa kwanza kwa Kanisa. Alikufa 14 Septemba 1840.

Mungu alimfunulia maelekezo kupitia mwanawe Joseph, **M&M** 4; 23:5. Mwacheni mtumishi wangu mzee aendelee kukaa pamoja na familia yake, **M&M** 90:20. Mtumishi wangu mzee Joseph hukaa pamoja na Ibrahimu katika mkono wake wa kuume, **M&M** 124:19. Joseph Smith Mdogo, alimwona baba yake katika ono la ufalme wa selestia, **M&M** 137:5.

Malaika alimwamuru Joseph Smith Mdogo umwambia baba yake juu ya ono alilopata, **JS—H** 1:49–50.

Smith, Joseph F.

Rais wa sita wa Kanisa; mwana pekee wa Hyrum na Mary Fielding Smith. Alizaliwa 13 Novemba 1838 na alikufa 19 Novemba 1918.

Joseph F. Smith alipata ono la ukombozi wa wafu, **M&M** 138.

Smith, Lucy Mack. *Ona pia* Smith, Joseph, Mdogo; Smith, Joseph, Mkubwa

Mama wa Joseph Smith Nabii na mke wa Joseph Smith Mkubwa (JS—H 1:4, 7, 20). Alizaliwa 8 Julai 1776 na alikufa 5 Mei 1856.

Joseph alimwona mama yake katika ono la ufalme wa selestia, **M&M** 137:5.

Smith, Samuel H. *Ona pia* Smith, Joseph, Mdogo

Kaka mdogo wa Joseph Smith Nabii (JS—H 1:4). Samuel alizaliwa katika mwaka 1808 na alikufa katika mwaka 1844. Alikuwa mmoja wa Mashahidi Wanane wa Kitabu cha Mormoni na alitumikia kama mmoja wa wamisionari wa Kwanza wa Kanisa lililorejeshwa (M&M 23:4; 52:30; 61:33–35; 66:7–8; 75:13).

Sodoma. *Ona pia* Gomora

Katika Agano la Kale, ni mji mwovu ambao uliangamizwa na Bwana (Mwa. 19:12–29).

Staha. *Ona pia* Mnyenyekevu, Unyenyekevu

Tabia au sura ilio nyenyekevu, ya wastani, na ya heshima. Mtu aliye na staha huepuka matendo mabaya ya kupindukia na kujisingizia.

Mungu akafanya mavazi ya ngozi, na akawavika Adamu na Hawa, **Mwa.** 3:21 (Musa 4:27).

Wanawake na wajipambe wenyewe kwa mavazi ya staha, **1 Tim.** 2:9. Kuweni wenye uangalifu, usafi, na kufanya kazi nyumbani, **Tit.** 2:5.

Wengi wamejiinua juu kwa kiburi kwa sababu ya gharama ya mavazi yao, **Yak. (KM)** 2:13.

Na mavazi yenu yote yawe ya kawaida, **M&M** 42:40.

Tunaamini katika kuwa wasafi na wema, **M ya I** 1:13.

Stahimili. *Ona pia* Jaribu, Majaribu; Shida; Subira

Kubaki imara katika ahadi na kuwa mkweli katika amri za Mungu licha ya majaribu, upinzani, na shida.

Mwenye kustahimili hadi mwisho ataokolewa, **Mt.** 10:22 (Mk. 13:13). Hawana mizizi na hivyo hustahimili kwa muda mchache, **Mk.** 4:17. Hisani hustahimili mambo yote, **1 Kor.** 13:7. Baada ya Ibrahimu kustahimili vyema, akapata ahadi, **Ebr.** 6:15.

Kama watavumilia hata mwisho watainuliwa juu katika siku ya mwisho, **1 Ne.** 13:37. Kama mtakuwa watiifu katika amri, na kustahimili hadi mwisho, mtaokolewa, **1 Ne.** 22:31 (Alma 5:13). Kama mtasonga mbele, mkisherehekea karamu ya neno la Kristo, na kustahimili hadi mwisho, mtakuwa na uzima wa milele, **2 Ne.** 31:20 (3 Ne. 15:9; M&M 14:7). Yeyote ajichukuliae juu yake jina langu, na kustahimili hadi mwisho, ataokolewa, **3 Ne.** 27:6.

Yeyote katika Kanisa langu astahimiliye hadi mwisho, huyo nitamstawisha juu ya mwamba wangu, **M&M** 10:69. Yule astahimiliye katika imani ataushinda ulimwengu, **M&M** 63:20, 47. Enzi na utawala zote zitakuwa juu ya wote ambao wamestahimili kwa ujasiri mkubwa kwa ajili ya injili ya Yesu Kristo, **M&M** 121:29.

Stefano

Stephano alikufa kifo cha kishahidi kwa ajili ya Mwokozi na Kanisa Lake katika nyakati za Agano Jipya. Mahubiri yake yalifanyika mapema na yawezekana yaliiongoza kazi kubwa ya Paulo, ambaye alikuwepo wakati Stefano alipokuwa akijitetea mwenyewe mbele ya Sanhedrini (Mdo. 8:1; 22:20).

Stephano alikuwa mmoja kati ya watu saba walioteuliwa kuwasaidia wale Mitume Kumi na Wawili, **Mdo.** 6:1–8. Stephano alifanya maajabu makubwa na miujiza, **Mdo.** 6:8. Stefano aliingia katika mabishano na Wayahudi, **Mdo.** 6:9–10. Mashtaka yaliletwa dhidi yake na alishtakiwa mbele ya Sanhedrini, **Mdo.** 6:11–15. Stefano alitoa utetezi wake, **Mdo.** 7:2–53. Akiwa amejawa na Roho Mtakatifu, alimwona Baba na Mwana katika ono, **Mdo.** 7:55–56. Stefano aliuawa kifo cha kishahidi kwa ajili ya ushuhuda wake, **Mdo.** 7:54–60.

Subira. *Ona pia* Pole, Upole; Stahimili

Ustahimilivu wa utulivu; ni uwezo wa kustahimili mateso, matukano, au majeraha pasipo kulalamika au kulipiza.

Tulia katika Bwana, na umngojee kwa subira, **Zab.** 37:7–8. Asiye mwepesi wa hasira ana fahamu nyingi, **Mit.** 14:29.

Nanyi kwa subira yenu mtaziponya nafsi zenu, **Lk.** 21:19. Tunalo tumaini kwa njia ya subira na faraja ya maandiko, **Rum.** 15:4. Mkawe wafuasi wa hao ambao kwa imani na subira huzirithi ahadi, **Ebr.** 6:12–15. Subira na iwe na kazi kamilifu, ili mpate kuwa wakamilifu na watimilifu, **Yak. (Bib.)** 1:2–4. Mmesikia juu ya subira yake Ayubu, **Yak. (Bib.)** 5:11.

Walitii kwa furaha na kwa subira mapenzi yote ya Bwana, **Mos.** 24:15. Nawe ulivumilia mambo haya yote kwa subira kwa sababu Bwana alikuwa pamoja nawe, **Alma** 38:4–5.

Endeleeni katika subira hadi mtakapokuwa mmekamilika, **M&M** 67:13.

Suleimani. *Ona pia* Bath-sheba; Daudi

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Daudi na Bath-sheba (2 Sam. 12:24). Sulemani kwa wakati fulani alikuwa mfalme wa Israeli.

Daudi alimtaja Sulemani kama mfalme, **1 Fal.** 1:11–53. Daudi alimwamuru Sulemani kutembea katika njia za Bwana, **1 Fal.** 2:1–9. Bwana alimwahidi moyo wa kufahamu, **1 Fal.** 3:5–15. Aliwahukumu akina mama wawili na aliweza kumtambua mama halisi wa mtoto huyo, **1 Fal.** 3:16–28. Anena kwa methali na nyimbo, **1 Fal.** 4:32. Alijenga hekalu, **1 Fal.** 6; 7:13–51. Aliliweka wakfu hekalu, **1 Fal.** 8. Alitembelewa na malkia

wa Sheba, **1 Fal.** 10:1–13. Suleimani alioa nje ya Israeli, na hao wake zake wakaugeuza moyo wake kwa kuwaabudu miungu wa uongo, **1 Fal.** 11:1–8. Bwana alimkasirikia Sulemani, **1 Fal.** 11:9–13. Alikufa, **1 Fal.** 11:43. Daudi alitoa unabii juu ya utukufu wa utawala wa Sulemani, **Zab.** 72.

Sulemani alipokea wake wengi na masuria, lakini wengine hawakuwapokea kutoka kwa Bwana, **M&M** 132:38 (Yak. [KM] 2:24).

Tabia ya Ubasha. *Ona pia* Kupenda anasa, Matamanio ya anasa; Uzinzi

Mahusiano ya kujamiana kwa watu wa jinsia moja. Mungu anakataza shughuli za kujamiana za aina hii.

Walete nje kwetu sisi, ili tupate kuwajua, **Mwa.** 19:1–11 (Musa 5:51–53). Usilale na mwanamume mfano wa kulala na mwanamke; ni machukizo, **Law.** 18:22 (Law. 20:13). Pasiwe na hanithi katika wana wa Israeli, **Kum.** 23:17. Watangaza dhambi yao kama Sodoma, hawaifichi, **Isa.** 3:9 (2 Ne. 13:9).

Wanaume waliwakiana tamaa wao kwa wao, **Rum.** 1:27. Wajitukanao wenyewe kwa kujamiana hawataurithi ufalme wa Mungu, **1 Kor.** 6:9–10. Sheria haikutungwa kwa ajili ya mtu mwenye haki, bali kwa ajili ya wale wajichafuao wenyewe kwa kujamiana wanaume wa jinsia moja, **1 Tim.** 1:9–10. Watu waendao kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili wamewekwa kuwa mfano, watateseka kisasi cha moto wa milele, **Yuda** 1:7.

Tafakari. *Ona pia* Sala; Ufunuo

Kutaamali na kufikiri kwa kina, mara kwa mara ni juu ya maandiko au mambo mengine ya Mungu. Kukiunganika na sala, kutafakari mambo ya Mungu kunaweza kuleta ufunuo na uelewa.

Maria alitafakari mambo haya moyoni mwake, **Lk.** 2:19.

Nilipokuwa nimekaa nikitafakari moyoni mwangu nilinyakuliwa, **1 Ne.** 11:1. Moyo wangu huyatafakari maandiko, **2 Ne.** 4:15. Nefi alienda zake, akitafakari juu ya mambo ambayo Bwana amemwonyesha, **Hel.** 10:2–3. Nendeni majumbani mwenu na mtafakari juu ya mambo ambayo nimeyasema, **3 Ne.** 17:3. Kumbukeni jinsi Bwana alivyo mwenye rehema, na mtafakari mioyoni mwenu, **Moro.** 10:3.

Tafakari juu ya mambo ambayo umeyapokea, **M&M** 30:3. Wakati tukiwa tukitafakari juu ya mambo haya, Bwana akagusa macho ya ufahamu wetu, **M&M** 76:19. Nilikaa chumbani mwangu nikitafakari juu ya maandiko, **M&M** 138:1–11.

Nilifikiri juu ya jambo hili tena na tena, **JS—H** 1:12.

Tafsiri

Kuelezea maana ya wazo moja lililotolewa katika lugha moja na kuyaweka katika maneno yaliyo sawa sawa katika lugha nyingine (Mos. 8:8–13; M ya I 1:8). Katika maandiko mara nyingi inaelezwa kama kipawa kutoka kwa Mungu (Alma 9:21; M&M 8; 9:7–9). Wakati mwingine yaweza kumaanisha kuboresha au kusahihisha tafsiri iliyoko katika lugha au kurejesha sehemu ya maneno yaliyopotea (M&M 45:60–61). Joseph Smith aliamriwa kufanya tafsiri ya kuongozwa na Mungu katika Biblia ya toleo la Mfalme James (M&M 42:56; 76:15).

Joseph Smith alikuwa na uwezo wa kutafsiri kwa njia ya neema ya Mungu, kwa uwezo wa Mungu, **M&M** 1:29. Unacho kipawa cha kutafsiri, **M&M** 5:4. Ninakupa wewe kipawa, kama unataka kutoka kwangu cha kutafsiri, **M&M** 6:25. Mungu alimpa Joseph Smith uwezo kutoka juu kutafsiri Kitabu cha Mormoni, **M&M** 20:8.

Kwa njia ya Urimu na Thumimu nilitafsiri baadhi ya herufi, **JS—H** 1:62 (Mos. 8:13; 28:13).

Tafsiri ya Joseph Smith (TJS). *Ona pia* Smith, Joseph, Mdogo

Marudio au tafsiri ya Toleo la Mfalme James la Biblia katika lugha ya Kiingereza, ambayo Joseph Smith Nabii

alianza mwezi Juni 1830. Aliamriwa na Mungu kufanya tafsiri hiyo na alijichukulia kama sehemu ya wito wake kama nabii.

Ingawa Joseph alimaliza tafsiri hiyo ilipofika Julai 1833, aliendelea hadi kifo chake katika mwaka 1844 akifanya marekebisho wakati akitayarisha muswada kwa ajili ya kuchapisha. Ingawa alichapisha baadhi ya sehemu za tafsiri hiyo wakati wa uhai wake, inawezekana kwamba angelikuwa amefanya nyongeza ya mabadiliko kama angeliishi hadi kuchapisha kazi yote. Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho Lililoundwa Upya lilichapisha toleo la kwanza la tafsiri ya Joseph Smith ya kuongozwa na Mungu katika mwaka 1867. Wamechapisha matoleo kadha wa kadha tokea wakati huo.

Nabii alijifunza mambo mengi wakati wa shughuli ya kutafsiri. Sehemu kadhaa za Mafundisho na Maagano zilipokelewa kwa sababu ya kazi ya kutafsiri (kama vile M&M 76; 77; 91; na 132). Pia, Bwana alimpa Joseph maelekezo maalumu kwa ajili ya tafsiri hiyo, ambayo yameandikwa katika Mafundisho na Maagano (M&M 37:1; 45:60–61; 76:15–18; 90:13; 91; 94:10; 104:58; 124:89). Kitabu cha Musa na Joseph Smith—Mathayo, sasa kimejumuishwa katika Lulu ya Thamani Kuu, zilichukuliwa moja kwa moja kutoka kwa Tafsiri ya Joseph Smith.

Tafsiri ya Joseph Smith imerejesha baadhi ya mambo yaliyo wazi na yenye thamani ambayo yalikuwa yamepotea kutoka katika Biblia (1 Ne. 13). Ingawa siyo Biblia rasmi ya Kanisa, tafsiri hii inatoa utambuzi mwingi ulio mzuri na ni muhimu sana katika kuielewa Biblia. Pia ni ushahidi wa wito mtakatifu na huduma ya Joseph Smith Nabii.

Tafsiri ya Joseph Smith ya Biblia (TJS). *Ona* Tafsiri ya Joseph Smith (TJS)

Taji. *Ona pia* Uzima wa Milele

Pambo la duara linalovaliwa juu ya kichwa cha mtawala. Laweza kuwa alama ya uwezo wa kiselestia, utawala, na umungu. Wale wenye kustahimili hadi mwisho kwa kushika amri zote za Mungu watapokea taji la uzima wa milele. (Ona M&M 20:14; Musa 7:56; JS—M 1:1).

Nimewekewa taji ya haki, **2 Tim.** 4:8. Mtalipokea taji la utukufu, lile lisilofifia, **1 Pet.** 5:4.

Wafu wanaokuja katika Bwana watapokea taji la haki, **M&M** 29:13. Watapokea taji katika makao ya Baba yangu, **M&M** 59:2. Bwana huwatayarisha Watakatifu kuja juu kwenye taji lililotayarishwa kwa ajili yao, **M&M** 78:15. Bwana amewaahidi Watakatifu wake taji la utukufu katika mkono wake wa kuume, **M&M** 104:7.

Takatifu. *Ona pia* Safi na Isiyo safi; Utakaso; Utakatifu

Kuwa na tabia ya kumchamungu, au kuwa safi kiroho na kimwili. Kinyume cha mtakatifu ni kuwa wa ulimwengu au kuwa mchafu.

Mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, na taifa takatifu, **Ku.** 19:5–6 (1 Pet. 2:9). Bwana akamwamuru Israeli: Kuweni watakatifu, kwa kuwa Mimi ni mtakatifu, **Law.** 11:44–45. Wale walio na mikono safi na moyo safi watasimama katika mahali pake patakatifu, **Zab.** 24:3–4. Watawafundisha watu wangu tofauti kati ya vitu vitakatifu na vitu vichafu, **Eze.** 44:23.

Mungu ametuita kwa wito mtakatifu, **2 Tim.** 1:8–9. Tangu utoto umeyajua maandiko, **2 Tim.** 3:15. Wanadamu watakatifu wa Mungu walinena kama walivyoongozwa na Roho Mtakatifu, **2 Pet.** 1:21.

Wanadamu wote watahukumiwa kulingana na ukweli na utakatifu ulioko katika Mungu, **2 Ne.** 2:10. Mwanadamu wa asili huwa mtakatifu kupitia upatanisho wa Kristo, **Mos.** 3:19. Tembea kwa mfano mtakatifu wa Mungu, **Alma** 7:22 (Alma 13:11–12). Wanafunzi watatu walitakaswa katika mwili na

wakafanywa kuwa watakatifu, **3 Ne.** 28:1–9, 36–39.

Usicheze na mambo matakatifu, **M&M** 6:12. Huwezi kuandika lililo takatifu isipokuwa limetolewa kwako kutoka kwangu, **M&M** 9:9. Mtajifunga ninyi wenyewe ili kutenda katika utakatifu wote, **M&M** 43:9. Wanafunzi wangu watasimama katika mahali patakatifu, **M&M** 45:32. Kile kijacho kutoka juu ni kitakatifu, **M&M** 63:64. Watoto wadogo ni watakatifu, **M&M** 74:7. Wekeni wakfu mahali pale napo patafanywa kuwa patakatifu, **M&M** 124:44.

Bwana atawakusanya wateule wake katika mji mtakatifu, **Musa** 7:62.

Talaka. *Ona pia* Ndoa, Oa, Olewa

Kikomo cha ndoa kwa njia ya mamlaka ya kiserikali au sheria ya kidini. Kulingana na Agano Jipya, Mungu aliruhusu talaka chini ya masharti fulani kwa sababu ya ugumu wa mioyo ya watu; hata hivyo, kama Yesu alivyoelezea, "tangu mwanzo haikuwa hivyo" (Mt. 19:3–12). Maandiko kwa ujumla yanatushauri dhidi ya talaka na yanawashauri waume na wake kupendana kwa haki (1 Kor. 7:10–12; M&M 42:22).

Talanta

Kipimo cha kale cha uzito au kiasi cha fedha kilichokuwa cha thamani kuu. Pia hutumika kama ishara kwa kitu fulani chenye thamani kubwa, kama vile injili ya Yesu Kristo (Mt. 25:14–29; Eth. 12:35; M&M 60:2, 13).

Tamaa mbaya. *Ona pia* Kupenda anasa, Matamanio ya anasa

Kuwa na hamu kubwa isiyofaa kwa kitu fulani.

Usiutamani uzuri wake moyoni mwako, **Mit.** 6:25.

Yeyote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini, **Mt.** 5:28 (3 Ne. 12:28). Wanaume waliwakiana tamaa, **Rum.** 1:27. Kwa kufuata tamaa zao wenyewe watajilundikia walimu, **2 Tim.** 4:3–4.

Labani aliona mali yetu na akaitamani, **1 Ne.** 3:25. Usiende tena kufuata tamaa ya macho yako, **Alma** 39:3–4, 9.

Mtu amwangaliaye mwanamke kwa kumtamani ataikana imani, **M&M** 42:23. Acheni tamaa zenu zilizo mbaya, **M&M** 88:121.

Tamaa za kimwili. *Ona pia* Anguko la Adamu na Hawa; Kupenda anasa, Matamanio ya anasa; Mwanadamu wa Tabia ya Asili

Kitu fulani kisicho cha kiroho; hasa neno hili laweza kutumika kumaanisha ama yenye kuharibika na ya kimwili (M&M 67:10) au ya kiulimwengu, ya kimwili, na kupenda anasa (Mos. 16:10–12).

Kuwa na mawazo ya tamaa za kimwili ni kifo, **2 Ne.** 9:39. Ibilisi huwadanganya wanadamu na kuwaingiza katika usalama wa tamaa za kimwili, **2 Ne.** 28:21. Na walikuwa wamejiona wenyewe katika hali yao ya tamaa za kimwili, **Mos.** 4:2. Yule anaye endelea katika kupenda hali yake ya tamaa ya kimwili hubaki katika hali yake ya kuanguka, **Mos.** 16:5. Wote lazima wazaliwe kwa Mungu, wabadilishwe kutoka hali yao ya tamaa za kimwili na hali ya kuanguka, **Mos.** 27:25. Wanadamu wamekuwa wa tamaa za kimwili, wenye kupenda anasa, na uibilisi, **Alma** 42:10.

Wale wafuatao matakwa yao wenyewe na tamaa za kimwili lazima watanguka, **M&M** 3:4. Mwanadamu hawezi kumwona Mungu kwa mawazo yake ya tamaa za kimwili, **M&M** 67:10–12.

Wanadamu wakaanza kuwa wenye tamaa za kimwili wenye kupenda anasa, na uibilisi, **Musa** 5:13; 6:49.

Tamani. *Ona pia* Husuda

Kama lilivyotumika katika maandiko, kutamani ni kumwonea wivu mtu fulani au kuwa na tamaa kupita kiasi kwa ajili ya kitu fulani.

Usitamani, **Ku.** 20:17 (Kum. 5:21; Mos. 13:24; M&M 19:25). Yule achukiaye kutamani ataongeza siku zake, **Mit.** 28:16.

Hutamani mashamba na kuyashika, **Mik.** 2:2.

Jilindeni na choyo, **Lk.** 12:15. Torati ilisema, Usitamani, **Rum.** 7:7. Katika siku za mwisho, wanadamu watakuwa wenye tamaa, **2 Tim.** 3:1–2.

Labani alipoiona mali yetu, aliitamani, **1 Ne.** 3:25.

Usitamani mali yako wewe mwenyewe, **M&M** 19:26. Acheni kuwa na tamaa, **M&M** 88:123. Usitamani kile kilicho cha ndugu yako, **M&M** 136:20.

Tamko Rasmi 1. *Ona pia* Manifesto; Ndoa, Oa, Olewa—Ndoa ya wake wengi; Woodruff, Wilford

Limepigwa chapa katika kurasa za kufungia za Mafundisho na Maagano, sehemu ya kwanza ya Tamko Rasmi 1 pia hujulikana kama Manifesto. Lilitolewa na Rais Wilford Woodruff na kuwasilishwa kwa waumini wa Kanisa katika mkutano mkuu mnamo 6 Oktoba 1890. Kuanzia mwaka 1862, sheria mbalimbali kwa miaka ishirini na mitano iliyofuatia ilifanya ndoa ya wake wengi ifanywe kuwa ni kinyume cha sheria katika Marekani. Bwana alimwonyesha Wilford Woodruff kwa ono na ufunuo nini kingetokea kama Watakatifu wasingeacha desturi ya ndoa ya wake wengi. Manifesto hiyo ilitangaza rasmi kwamba ndoa ya wake wengi haifanyiki tena.

Tamko Rasmi 2. *Ona pia* Kimball, Spencer W.; Ukuhani

Maelezo ya mafundisho ya kidini yanayohusu ni nani anaweza kushika ukuhani wa Mungu, maelezo ambayo sasa yamepigwa chapa katika kurasa za mwisho za Mafundisho na Maagano. Mapema Juni 1978, Bwana alimfunulia Rais Spencer W. Kimball kwamba ukuhani utolewe kwa wanaume wote walio waumini wa Kanisa wenye kustahili. Hii ilifanya ukuhani upatikane kwa waumini wanaume wote wenye kustahili na baraka za hekaluni zipatikane kwa waumini wote wenye kustahili, bila kujali asili au rangi. Mnamo 30 Septemba 1978, tamko hili liliwasilishwa kwenye mkutano mkuu wa Kanisa na lilikubaliwa kwa kura zote.

Tawanyika. *Ona* Israeli—Kutawanyika kwa Israeli

Taylor, John

Rais wa tatu wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Aliitwa katika Baraza la wale Kumi na Wawili, **M&M** 118:6 (M&M 124:128–129). Alijeruhiwa katika mauaji haya ya kishahidi, **M&M** 135:2. Alikuwa miongoni mwa watu maarufu walioonwa na Joseph F. Smith katika ulimwengu wa roho, **M&M** 138:53–56.

Teankumu

Kiongozi mkuu wa jeshi la Wanefi katika Kitabu cha Mormoni (Alma 50:35; 51–52; 61–62).

Tegemea. *Ona pia* Amini, Imani; Matumaini

Kutegemea au kuweka matumaini yako katika mtu fulani au jambo fulani. Katika mambo ya kiroho, kutegemea kunajumuisha kumtegemea Mungu na Roho Wake.

Japo kuwa ataniua, bado nitamtumaini yeye, **Ayu.** 13:15. Mtumaini Bwana kwa moyo wako wote, **Mit.** 3:5. Bwana aliwaokoa watumishi wake ambao walimtumaini yeye, **Dan.** 3:19–28.

Nitakutumaini wewe milele, **2 Ne.** 4:34. Furahini na kuweka matumaini yenu katika Mungu, **Mos.** 7:19. Mtu yeyote awekaye tumaini lake katika Mungu atainuliwa katika ile siku ya mwisho, **Mos.** 23:22. Watu wowote watakao mwamini Mungu watasaidiwa katika majaribu yao, **Alma** 36:3, 27.

Usiuegemee mkono wa mwanadamu, **M&M** 1:19. Weka imani yako katika ile Roho ambayo hutuongoza kufanya yaliyo mema, **M&M** 11:12. Mwache anitumaini mimi, naye hatashindwa, **M&M** 84:116.

Tembea, Tembea na Mungu. *Ona pia* Haki, Uadilifu, enye Uadilifu; Mtiifu, Tii, Utii; Njia

Kuwa katika maafikiano na mafundisho ya Mungu na kuishi kama Mungu anavyopenda watu Wake waishi; kuwa msikivu na mtiifu kwa ushawishi wa Roho Mtakatifu.

Nipate kuwajaribu, kwamba watatembea katika sheria zangu, ama sivyo, **Ku.** 16:4. Hawatanyimwa kitu chema, hao watembeao wima, **Zab.** 84:11. Wale waendao katika amri zangu na kuyashika maagizo yangu watakuwa watu wangu, **Eze.** 11:20–21 (Kum. 8:6). Bwana anataka nini kwako, ila kwamba kwenda kwa unyenyekevu na Mungu, **Mika** 6:8 (M&M 11:12).

Tukienenda nuruni, kama Mungu alivyo katika nuru, **1 Yoh.** 1:7 (2 Yoh. 1:6; 3 Yoh. 1:4; 4 Ne. 1:12).

Enenda katika njia nyembamba iongozayo kwenye uzima, **2 Ne.** 33:9. Mfalme Benjamini alitembea kwa dhamira iliyosafi mbele za Mungu, **Mos.** 2:27. Wajibu wenu ni kutembea bila lawama kwa mfano mtakatifu wa Mungu, **Alma** 7:22.

Waumini wa Kanisa wataonyesha mwenendo na mazungumzo ya kiuchamungu, **M&M** 20:69. Wasikieni manabii na kutembea katika utakatifu wote mbele za Bwana, **M&M** 21:4. Wafundisheni watoto kusali na kutembea wima mbele za Bwana, **M&M** 68:28.

Kaeni ndani yangu, nami ndani yenu; kwa hiyo tembeeni pamoja nami, **Musa** 6:34.

Tenda. *Ona* Mtiifu, Tii, Utii

Tesa. *Ona* Mateso, Tesa

Teule, Wateule. *Ona pia* Ita, Itwa na Mungu, Wito

Wateule ni wale ambao wanampenda Mungu kwa moyo wao wote na kuishi maisha ambayo yanampendeza Yeye. Wale wanaoishi maisha ya jinsi ya uanafunzi siku moja watachaguliwa na Bwana kuwa miongoni mwa watoto Wake waliochaguliwa.

Nimefanya agano na mteule wangu, **Zab.** 89:3.

Kama ingeliwezekana, watawadanganya hata walio wateule haswa, **Mt.** 24:24. Watakatifu ndiyo kizazi kiteule, ukuhani wa kifalme, **1 Pet.** 2:9. Yohana alifurahi kwa sababu watoto wa mwanamke mteule walikuwa wakweli na waaminifu, **2 Yoh.** 1.

Umesamehewa dhambi zako, nawe u mwanamke mteule, **M&M** 25:3. Wateule wangu husikia sauti yangu na hawashupazi mioyo yao, **M&M** 29:7. Hata hivyo ndivyo nitakavyowakusanya wateule wangu kutoka pande nne za dunia, **M&M** 33:6. Maandiko yatatolewa kwa ajili ya wateule wangu, **M&M** 35:20–21. Wale wenye kuitukuza miito ya ukuhani huwa wateule wa Mungu, **M&M** 84:33–34.

Kristo alikuwa Mpendwa na Mteule wa Mungu tangu mwanzo, **Musa** 4:2. Kwa sababu ya wateule, siku za majonzi zitafupishwa, **JS—M** 1:20.

Timotheo. *Ona pia* Paulo

Katika Agano Jipya, ni mmsionari kijana mshirika wa Paulo wakati wa huduma za Paulo (Mdo. 16:1–3; 2 Tim. 1:1–5); mwana wa baba Myunani na mama Myahudi; yeye na wazazi wake waliishi katika Listra.

Paulo alizungumza juu ya Timotheo kama "mwanawe hasa katika imani" (1 Tim. 1:2, 18; 2 Tim. 1:2). Timoteo huenda alikuwa ndiye msaidizi wa Paulo aliyeaminika na mwenye uwezo zaidi (Flp. 2:19–23).

Timotheo, Nyaraka Kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo; Timotheo

Vitabu viwili katika Agano Jipya. Vyote mwanzoni vilikuwa ni barua ambazo Paulo alimwandikia Timotheo.

1 Timotheo: Paulo aliandika waraka wa kwanza baada ya kifungo chake cha kwanza gerezani. Alikuwa amemwacha Timotheo huko Efeso, akitarajia baadaye

arudi (1 Tim. 3:14). Hata hivyo, Paulo alihisi kwamba angeliweza kucheleweshwa, hivyo alimwandikia Timotheo, huenda kutoka Makedonia (1 Tim. 1:3), ili kumpa ushauri na kumtia moyo katika kutekeleza kazi yake.

Mlango wa 1 una salamu za Paulo na pia mafundisho yake juu ya watu waliooeneza mafundisho ya kipumbavu katika Kanisa. Mlango wa 2–3 anaandika mwongozo juu ya ibada ya hadharani na juu ya tabia na mwenendo wa wahudumu. Mlango wa 4–5 anaelezea juu ya ukengeufu wa siku za mwisho na ushauri kwa Timotheo juu ya jinsi ya kuhudumu kwa wale anaowaongoza. Mlango wa 6 anamsihi kuthibitisha uaminifu na kuepuka utajiri wa kilimwengu.

2 Timotheo: Paulo aliandika barua ya pili wakati wa kufungwa kwake mara ya pili, muda mfupi kabla ya kifo chake cha kishahidi. Ina maneno ya mwisho ya Mtume na inaonyesha ujasiri na uaminifu wa ajabu ambao kwa huo alikabiliana na mauti.

Mlango wa 1 una salamu za Paulo na amri kwa Timotheo. Mlango wa 2–3 inatoa maonyo na maelekezo mbalimbali, pamoja na kumtia moyo ili kukabili hatari zinazokuja. Mlango wa 4 ni ujumbe kwa marafiki wa Paulo, wenye ushauri juu ya jinsi ya kuwatendea wakengeufu.

Tito. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo; Tito, Waraka kwa

Katika Agano Jipya, ni Myunani muongofu na muaminifu aliyesafiri kwenda Yerusalemu pamoja na Paulo na baadaye akawa mmsionari (Gal. 2:1–4; 2 Tim. 4:10). Tito alipeleka waraka wa kwanza wa Paulo kwa Watakatifu huko Korintho (2 Kor. 7:5–8, 13–15).

Tito, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo; Tito

Wakati Paulo alipokuwa huru kwa muda kutoka kifungo cha gereza la Kirumi, aliandika waraka kwa Tito, aliyekuwa katika Krete. Barua inaadiri zaidi maswali yanayohusiana na nidhamu ya kibinafsi na muundo wa Kanisa.

Mlango wa 1 una salamu za Paulo na mafundisho ya jumla juu ya sifa za maaskofu. Mlango wa 2–3 ina mafundisho ya kawaida na ujumbe binafsi kwa Tito juu ya jinsi ya kuyatenda makundi mbalimbali ya Kanisa la Krete. Paulo aliwatia moyo Watakatifu ili waushinde ukaidi, wawe na kiasi na waaminifu, na waendeleze matendo mema.

Toa Shukrani. *Ona* Shukrani, enye Shukrani, Asante, Toa shukrani

Toa unabii, Unabii. *Ona pia* Mwonaji; Nabii; Nabii Mwanamke; Ufunuo

Unabii una maneno matakatifu ya kimungu au maandishi, ambayo mtu hupokea kwa njia ya ufunuo kutoka kwa Roho Mtakatifu. Ushuhuda wa Yesu ni roho ya unabii (Ufu. 19:10). Unabii waweza kuwa juu ya mambo yaliyopita, yaliyopo, au yajayo. Mtu anapotoa unabii, hunena au huandika lile ambalo Mungu anataka yeye alijue, kwa manufaa yake mwenyewe au kwa manufaa ya wengine. Watu binafsi wanaweza kupokea unabii au ufunuo kwa ajili ya maisha yao wao wenyewe.

Ningependa kwa Mungu kwamba watu wote wa Bwana wangekuwa manabii, **Hes.** 11:29. Wana na mabinti zenu watatoa unabii, **Yoe.** 2:28 (Mdo. 2:17–18). Huwafunulia siri zake watumishi wake manabii, **Amo.** 3:7.

Hakuna unabii katika maandiko upatao tafsiri yoyote binafsi, **2 Pet.** 1:20.

Wanefi walipata mafunuo mengi na roho wa unabii, **Yak. (KM)** 4:6, 13. Alma na Amuleki walijua dhamira za moyo wa Zezromu kwa roho wa unabii, **Alma** 12:7. Ole wake yeye asemaye Bwana hatendi kazi tena kwa unabii, **3 Ne.** 29:6. Pekueni unabii wa Isaya, **Morm.** 8:23.

Unabii wote utatimia, **M&M** 1:37–38.

Mwanadamu lazima aitwe na Mungu kwa unabii, **M ya I** 1:5.

Toba, Tubu. *Ona pia* Kiri, Kukiri; Lipia dhambi, Upatanisho; Moyo Uliovunjika; Ondoleo la Dhambi; Samehe; Yesu Kristo

Badiliko la mawazo na moyo ambalo huleta mtazamo mpya kwa Mungu, kwa mtu mwenyewe, na maisha kwa ujumla. Toba humaanisha kwamba mtu hugeuka kabisa kutoka katika uovu na kugeuza moyo wake na mapenzi yake kwa Mungu, akijikabidhi katika amri na mapenzi ya Mungu na kutupa dhambi. Toba ya kweli huja kutokana na upendo kwa Mungu na tamaa ya dhati ya kutii amri zake. Watu wote wenye kuwajibika wamefanya dhambi na lazima watubu ili wapate kukua kuelekea katika wokovu. Ni kupitia Upatanisho wa Yesu Kristo pekee toba yetu inaweza kuwa na nguvu na kukubaliwa na Mungu.

Ungameni kwa Bwana, **Ezra** 10:11. Ondoeni uovu wa matendo yenu; acheni kutenda maovu, **Isa.** 1:16. Tubuni na mkageuke wenyewe kutoka kwenye uvunjaji sheria wenu wote, **Eze.** 18:30–31.

Tubuni: kwa maana ufalme wa mbinguni u karibu, **Mt.** 3:2. Kuna shangwe mbinguni mwenye dhambi mmoja anapotubu, **Lk.** 15:7. Mungu anawaamuru wanadamu wote kila mahali kutubu, **Mdo.** 17:30 (2 Ne. 9:23; 3 Ne. 11:31–40; M&M 133:16). Huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba iletayo wokovu, **2 Kor.** 7:10.

Roho wa Bwana Mwenyezi ameleta mabadiliko makubwa mioyoni mwetu, kwamba hatuna hamu tena ya kufanya maovu, **Mos.** 5:2. Kama ataungama dhambi zake na kutubu, huyo mtamsaheme, **Mos.** 26:29. Baada ya mahubiri ya Alma, watu wengi walianza kutubu, **Alma** 14:1. Usiahirishe siku ya toba yako, **Alma** 34:33. Alma alimfundisha Helamani juu ya toba na uongofu wake, **Alma** 36 (Mos. 27:8–32). Toba isingekuja kwa wanadamu isipokuwa pamekuwepo na adhabu, **Alma** 42:16. Acha dhambi zako zikusumbue, kwa usumbufu ambao utakushusha hadi kwenye toba, **Alma** 42:29. Mtatoa kwangu dhabihu ya moyo uliovunjika na roho iliyopondeka, **3 Ne.** 9:20. Yeyote mwenye kutubu na kuja kwangu kama mtoto mdogo, huyo nitampokea, **3 Ne.** 9:22. Tubuni, ninyi miisho yote ya dunia, **3 Ne.** 27:20. Kadiri mara nyingi walivyotubu, walisamehewa, **Moro.** 6:8.

Usiseme lolote, ila toba kwa kizazi hiki, **M&M** 6:9 (M&M 11:9). Furaha yake ni kubwa kiasi gani katika nafsi ambayo hutubu, **M&M** 18:13. Kila mtu lazima atubu au ateseke, **M&M** 19:4. Yule atendaye dhambi na hatubu atatupwa nje, **M&M** 42:28. Yule anayeungama na kuziacha dhambi zake anasamehewa, **M&M** 58:42–43. Wafu wanaotubu watakombolewa, **M&M** 138:58.

Tunaamini katika toba, **M ya I** 1:4.

Tohara. *Ona pia* Agano la Ibrahimu

Ishara ya Agano la Ibrahimu kwa Waisraeli wanaume wakati wa kipindi cha Agano la Kale (Mwa. 17:10–11, 23–27; TJS, Mwa. 17:11 [Kiambatisho]). Tohara ilikuwa ikifanyika kwa kukata "ngozi ya mbeleni" ya mtoto mchanga wa kiume na pia mwanamume mtu mzima. Wale waliofanyiwa walifurahia heshima na kupokea kazi za agano. Tohara kama ishara ya agano ilifutwa kwa misheni ya Kristo (Moro. 8:8; M&M 74:3–7).

Tomaso

Katika Agano Jipya, ni mmoja kati ya Mitume Kumi na Wawili wa mwanzoni waliochaguliwa na Mwokozi wakati wa huduma Yake katika mwili wenye kufa (Mt. 10:2–3; Yn. 14:5). Katika Kiyunani jina lake ni Didimo (Yn. 20:24–29; 21:2). Ingawa Tomaso alitia mashaka juu ya Ufufuko wa Yesu hadi yeye mwenyewe alipomwona Mwokozi, uaminifu wake mkubwa ulimfanya awe radhi kukabiliana na mateso na mauti pamoja na Bwana wake (Yn. 11:16; 20:19–25).

Torati. *Ona pia* Agano la Kale; Hesabu; Kumbukumbu la Torati; Kutoka; Musa; Mwanzo, Kitabu cha Biblia; Walawi

Jina lililotolewa kwa vitabu vitano vya kwanza vya Agano la Kale—Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, Hesabu, na Kumbukumbu la Torati. Wayahudi huvisema vitabu hivi kama ni Torati au sheria ya Israeli. Viliandikwa na Musa (1 Ne. 5:10–11).

Torati ya Musa. *Ona pia* Musa; Safi na Isiyo safi; Sheria; Ukuhani wa Haruni

Mungu alitoa sheria kwa nyumba ya Israeli kupitia kwa Musa ili kuwa badala ya ile sheria ya juu zaidi ambayo walishindwa kuitii (Ku. 34; TJS, Ku. 34:1–2; TJS, Kum. 10:2 [Kiambatisho]). Torati ya Musa ilikuwa na kanuni nyingi, masharti, ibada, matambiko, na ishara nyingi za kuwakumbusha watu kazi na wajibu wao. Ilijumuisha sheria ya tabia njema, maadili, dini, na amri za kimwili na za matendo—ikiwa ni pamoja na dhabihu (Law. 1–7)—ambazo zilikusudiwa kuwakumbusha juu ya Mungu na wajibu wao kwake Yeye (Mos. 13:30). Imani, toba, ubatizo katika maji, na ondoleo la dhambi zilikuwa ni sehemu ya torati, kama zilivyokuwa Amri Kumi na amri nyingine nyingi za maadili ya hali ya juu na tabia njema. Sehemu kubwa ya sheria zihusuzo sherehe zilimalizika katika mauti na Ufufuko wa Yesu Kristo, ambao ulihitimisha dhabihu kwa kumwaga damu (Alma 34:13–14). Torati ilisimamiwa chini ya Ukuhani wa Haruni na ilikuwa ni injili ya matayarisho ili kuwaleta kwa Kristo wenye kuifuata.

Nitawapa sheria kama vile mwanzo, lakini itakuwa kulingana na sheria ya amri ya kimwili, **TJS, Ku.** 34:1–2.

Torati ilikuwa walimu wetu kutuleta kwa Kristo, **Gal.** 3:19–24.

Tunaishika torati ya Musa na tukitazamia kwa uthabiti kuja kwa Kristo, **2 Ne.** 25:24–30. Wokovu hauji kwa torati ya Musa pekee, **Mos.** 12:27–13:32. Ndani yangu torati ya Musa imetimizwa, **3 Ne.** 9:17. Torati aliyopewa Musa mwisho wake ni ndani yangu, **3 Ne.** 15:1–10.

Kwa sababu ya kutotii, Bwana alimchukua Musa na Ukuhani Mtakatifu kutoka kwa wana wa Israeli, akaacha torati ya amri za kimwili, **M&M** 84:23–27.

Tubu. *Ona* Toba, Tubu

Tukuza. *Ona pia* Heshima; Uchaji

Kumchukulia mtu fulani au kitu fulani kama chenye kustahili na chenye thamani, hususani katika mtazamo wa kiinjili.

Alidharauliwa, na hatukumhesabu kuwa kitu, **Isa.** 53:3–4.

Lile ambalo linatukuzwa miongoni mwa wanadamu huwa chukizo mbele za Mungu, **Lk.** 16:15. Kila mtu na amhesabu mwenzie kuwa bora kuliko nafsi yake, **Flp.** 2:3.

Bwana huhesabu wenye mwili wote kuwa kitu kimoja, **1 Ne.** 17:35. Kila mwanadamu yapasa amheshimu jirani yake kama yeye mwenyewe, **Mos.** 27:4 (M&M 38:24–25).

Katika siku ya amani yao waliuchukulia kwa wepesi ushauri wangu, **M&M** 101:8.

Tumaini. *Ona pia* Amini, Imani

Tarajio la hamu ya uhakika la baraka za haki zilizoahidiwa. Maandiko mara kwa mara huzungumza juu ya tumaini kama matarajio ya uzima wa milele kupitia imani katika Yesu Kristo.

Heri mtu yule ambaye tumaini lake ni Bwana, **Yer.** 17:7. Bwana atakuwa ndiye tumaini la watu wake, **Yoe.** 3:16.

Tunalo tumaini kwa njia ya subira na maandiko, **Rum.** 15:4. Mungu ametuzaa sisi kwa tumaini lenye uzima katika ufufuko wa Kristo, **1 Pet.** 1:3. Kila mwanadamu aliye na tumaini hili hujitakasa yeye mwenyewe, **1 Yoh.** 3:2–3.

Lazima msonge mbele, mkiwa na mwangaza kamili wa tumaini, **2 Ne.** 31:20. Angalieni kuwa mnayo imani, tumaini, na hisani, **Alma** 7:24 (1 Kor. 13:13; Moro. 10:20). Ningelitamani muyasikie

maneno yangu, mkiwa na tumaini ya kwamba mtapokea uzima wa milele, **Alma** 13:27–29. Kama mna imani, ninyi mnalo tumaini kwa ajili ya mambo yasiyoonekana, ambayo ni ya kweli, **Alma** 32:21 (Ebr. 11:1). Tumaini huja kwa imani ambayo hufanya nanga kwa roho, **Eth.** 12:4 (Ebr. 6:17–19). Mwanadamu lazima awe na tumaini vinginevyo hataweza kupokea urithi, **Eth.** 12:32. Mormoni alizungumza juu ya imani, tumaini, na hisani, **Moro.** 7:1. Mtakuwa na tumaini kupitia upatanishi wa Yesu Kristo la kufufuliwa katika uzima wa milele, **Moro.** 7:40–43. Roho Mtakatifu hukujaza matumaini, **Moro.** 8:26 (Rum. 15:13).

Waliondoka katika maisha ya mwili wa kuharibika, wakiwa imara katika tumaini la ufufuko wa utukufu, **M&M** 138:14.

Tumbaku. *Ona* Neno la Hekima

Tunda Lililokatazwa. *Ona* Anguko la Adamu na Hawa; Edeni

Ua. *Ona* Adhabu Kuu; Mauaji

Uadilifu. *Ona* Haki, Uadilifu, enye Uadilifu

Uadui. *Ona pia* Husuda; Kisasi; Upendo

Katika maandiko, ni uhasama, kuwa na uadui, na kuchukia.

Nitaweka uadui kati yako wewe na mwanamke, **Mwa.** 3:15 (Musa 4:21).

Mawazo ya kimwili ni uadui dhidi ya Mungu, **Rum.** 8:7. Kuwa rafiki wa dunia ni kuwa adui wa Mungu, **Yak. (Bib.)** 4:4.

Katika siku hiyo uadui utakoma kutoka mbele ya uso wangu, **M&M** 101:26.

Uaminifu. *Ona* Mwaminifu, Uaminifu

Uasherati. *Ona pia* Kupenda anasa, Matamanio ya anasa; Usafi wa Kimwili; Uzinzi

Tendo la ngono lisilo la kisheria kati ya watu wawili wasiooana. Katika maandiko pia mara chache hutumika kama ishara ya ukengeufu.

Jiepusheni na uasherati, **Mdo.** 15:20. Mwili si kwa ajili ya uasherati, bali ni kwa ajili ya Mungu, **1 Kor.** 6:13–18. Kuepuka uasherati, acha kila mtu awe na mke wake mwenyewe, **1 Kor.** 7:2–3. Haya ni mapenzi ya Mungu, kwamba yawapasa mjiepushe na uasherati, **1 The.** 4:3.

Yakobo waliwaonya watu wa Nefi dhidi ya uasherati, **Yak. (KM)** 3:12. Ninyi mnakomaa, kwa sababu ya mauaji yenu na uasherati, kwa kuangamizwa, **Hel.** 8:26.

Washerati lazima watubu ili waweze kujiunga na Kanisa, **M&M** 42:74–78.

Uashiriaji

Kutumia kitu fulani kama mfano au alama ya kitu kingine. Uashiriaji katika maandiko hutumia vitu vinavyofahamika kiurahisi, tukio, au hali fulani ili kuwakilisha kanuni au fundisho la injili. Kwa mfano, Kitabu cha Mormoni nabii Alma alitumia mbegu kuwakilisha neno la Mungu (Alma 32).

Manabii katika maandiko yote wanatumia uashiriaji kwa kufundisha juu ya Yesu Kristo. Baadhi ya ishara hizi ni pamoja na sherehe na ibada (Musa 6:63), dhabihu (Ebr. 9:11–15; Musa 5:7–8), sakramenti (TJS, Mk. 14:20–24 [Kiambatisho]; Lk. 22:13–20), na ubatizo (Rum. 6:1–6; M&M 128:12–13). Majina mengi ya kibiblia ni ya kiishara. Sherehe za hema za Agano la Kale na torati ya Musa zilikuwa zinawakilisha kweli za milele (Ebr. 8–10; Mos. 13:29–32; Alma 25:15; Hel. 8:14–15). Kwa mifano mingine ona, Mathayo 5:13–16; Yohana 3:14–15; Yakobo (KM) 4:5; Alma 37:38–45.

Uasi. *Ona pia* Dhambi; Ibilisi; Manung'uniko; Ukengeufu

Kukataa kata kata au kumpinga Bwana, ikijumuisha kukataa kuwafuata viongozi Wake waliochaguliwa na kwa makusudi kabisa kukataa kutii amri Zake.

Msimwasi Bwana, **Hes.** 14:9. Mtu mwovu hatafuti neno ila kuasi tu, **Mit.** 17:11. Ole wao watoto waasi, **Isa.** 30:1.

Bwana hawakomboi wanao muasi nao hufa katika dhambi zao, **Mos.** 15:26. Waamlisiti walijitokeza katika uasi wa wazi dhidi ya Mungu, **Alma** 3:18–19.

Waasi watachomwa kwa uchungu mwingi, **M&M** 1:3. Hasira ya Bwana inawaka dhidi ya waasi, **M&M** 56:1 (M&M 63:1–6).

Shetani alimwasi Mungu, **Musa** 4:3.

Ubatizo. *Ona* Batiza, Ubatizo

Ubatizo wa Watoto Wachanga. *Ona pia* Batiza, Ubatizo—Ubatizo siyo kwa ajili ya watoto wachanga; Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika; Mtoto, Watoto; Wokovu—Wokovu wa watoto

Desturi isiyofaa ya kubatiza watoto wachanga na watoto walio chini ya umri wa uwajibikaji, ambao ni umri wa miaka minane. Bwana analaani ubatizo wa watoto wachanga (Moro. 8:10–21). Watoto wanazaliwa bila hatia na pasipo dhambi. Shetani hana uwezo wa kuwajaribu watoto hadi wanapoanza kuwajibika (M&M 29:46–47) hivyo hawana haja ya kutubu au kubatizwa. Watoto yapaswa wabatizwe wafikiapo umri wa miaka minane (M&M 68:25–27).

Uchafu. *Ona* Chafu, Uchafu

Uchaji. *Ona pia* Heshima; Hofu

Heshima kubwa kwa vitu vitakatifu; staajabika.

Bwana alimwamuru Musa kuvua viatu vyake, kwa kuwa alisimama juu ya ardhi takatifu, **Ku.** 3:4–5. Mungu huogopwa na ni wa kuhofiwa, **Zab.** 89:7.

Tumtumikie Mungu kwa kumpendeza na kwa kuonyesha unyenyekevu na hofu ya kimungu, **Ebr.** 12:28.

Moroni akajiinamisha chini, na akasali kwa nguvu sana, **Alma** 46:13. Umati ulianguka chini na wakamwabudu Kristo, **3 Ne.** 11:12–19.

Inama mbele zangu, **M&M** 5:24. Vitu vyote husujudu kwa upole na unyenyekevu mbele za kiti cha enzi cha Mungu, **M&M** 76:93. Akili zenu zilikuwa zimetiwa giza kwa sababu mmeyachukua bila uzito mambo mliyoyapokea, **M&M** 84:54–57. Kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri, **M&M** 88:104. Kwa heshima au kwa kuonyesha unyenyekevu kwa jina la Kiumbe Mkuu, Kanisa likauita ukuhani huo Melkizedeki, **M&M** 107:4. Baraka zitamwagwa juu ya wale wenye kuonyesha unyenyekevu kwa Bwana katika nyumba yake, **M&M** 109:21.

Udanganyifu. *Ona* Danganya, Kudanganya, Udanganyifu

Udhaifu. *Ona pia* Mnyenyekevu, Unyenyekevu

Hali ya kuwa katika mwili wenye kufa na kupungukiwa na uwezo, nguvu, au ujuzi. Udhaifu ni hali. Watu wote ni wadhaifu, na ni kwa neema ya Mungu tu kwamba hupokea uwezo wa kufanya matendo ya haki (Yak. [KM] 4:6–7). Udhaifu huu huonekana kwa upande mmoja katika mapungufu ya mtu au kasoro ambazo kila mtu anazo.

Iimarisheni mikono iliyo dhaifu, **Isa.** 35:3–4.

Roho hakika i radhi, lakini mwili ni dhaifu, **Mt.** 26:41 (Mk. 14:38).

Kwa sababu ya udhaifu ulioko ndani yangu, kulingana na mwili, nitajihalalisha mwenyewe, **1 Ne.** 19:6. Nimeamriwa kuandika mambo haya, licha ya udhaifu wangu, **2 Ne.** 33:11. Usimkasirikie mtumishi wako kwa sababu ya udhaifu wake, **Eth.** 3:2. Wayunani watadhihaki mambo haya kwa sababu ya udhaifu wetu katika kuandika, **Eth.** 12:23–25, 40. Nitawaonyesha udhaifu wao, **Eth.** 12:27–28. Kwa sababu umeuona udhaifu wako nawe utafanywa kuwa mwenye nguvu, **Eth.** 12:37.

Mtu aliye dhaifu miongoni mwenu tangu sasa atafanywa kuwa mwenye nguvu, **M&M** 50:16. Yesu Kristo anaujua udhaifu wa mwanadamu, **M&M** 62:1.

Ufahamu. *Ona pia* Hekima; Maarifa; Ukweli

Kupata maarifa juu ya au kutambua maana ya ukweli fulani, ikijumuisha matumizi yake katika maisha.

Usitegemee ufahamu wako mwenyewe, **Mit.** 3:5. Katika kupata kwako kote jipatie ufahamu, **Mit.** 4:7.

Yesu alisema kwa mifano na baadhi hawakufahamu, **Mt.** 13:12–17. Bwana alifungua ufahamu wao, **Lk.** 24:45.

Kama hamwezi kufahamu maneno haya, itakuwa ni kwa sababu hamuombi, **2 Ne.** 32:4 (3 Ne. 17:3). Kumbukumbu ilitunzwa ili kwamba tupate kuisoma na kufahamu, **Mos.** 1:2–5. Kwa sababu ya kutokuamini kwao, hawakuweza kufahamu neno la Mungu, **Mos.** 26:3. Walikuwa watu wenye ufahamu mkamilifu, **Alma** 17:2–3. Neno lile lilianza kuangaza ufahamu wangu, **Alma** 32:28.

Njooni tusemezane ili mpate kufahamu, **M&M** 50:10–12, 19–23. Wazazi lazima wawafundishe watoto wao kufahamu, **M&M** 68:25. Matendo na miujiza ya Mungu yaweza tu kufahamika kwa njia ya Roho Mtakatifu, **M&M** 76:114–116. Shetani hutafuta kuigeuza mioyo ya wanadamu mbali na ufahamu, **M&M** 78:10. Nuru ya Kristo huhuisha ufahamu wetu, **M&M** 88:11.

Ufalme wa Kirumi. *Ona pia* Roma

Milki ya Roma ya Kale. Katika zama za kitume, Milki ya Kirumi ilikuwa yenye nguvu kubwa ulimwenguni. Ulijumuisha kila kitu kilichokuwa kati ya Frati, na Danube, Rine, Atlantiki, na jangwa la Sahara. Palestina ikawa kibaraka katika mwaka 63 K.K., wakati Pompei alipoitwaa Yerusalemu. Ingawa Warumi waliwapa Wayahudi upendeleo mwingi, Wayahudi waliuchukia utawala wa Kirumi na daima walikuwa katika uasi.

Paulo, raia wa Kirumi, alitumia Kiyunani, lugha iliyokuwa ikitumika zaidi katika ufalme huo, ili kueneza injili katika ufalme wote.

Mpeni Kaisari mambo yaliyo ya Kaisari, **Mt.** 22:17–22. Paulo alitetea haki zake kama raia wa Kirumi, **Mdo.** 16:37–39 (Mdo. 22:25–29).

Ufalme wa Mungu au Ufalme wa Mbinguni. *Ona pia* Kanisa la Yesu Kristo; Utukufu wa Selestia

Ufalme wa Mungu duniani ni Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho (M&M 65). Madhumuni ya Kanisa ni kuwaandaa wanachama wake kuishi milele katika ufalme wa selestia au ufalme wa mbinguni. Hata hivyo, maandiko wakati mwingine huliita Kanisa ufalme wa mbinguni, yakimaanisha kwamba Kanisa ni ufalme wa mbinguni juu ya dunia.

Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho ndiyo ufalme wa Mungu duniani, lakini kwa sasa ni ufalme wa kidini pekee. Wakati wa Milenia, ufalme wa Mungu utakuwa wa kisiasa na wa kidini.

Bwana ndiye Mfalme milele na milele, **Zab.** 10:16 (Zab. 11:4). Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme ambao kamwe hautaangamizwa, **Dan.** 2:44 (M&M 138:44).

Tubuni, kwa maana ufalme wa mbingu umekaribia, **Mt.** 3:2 (Mt. 4:17). Ufalme wako uje, mapenzi yako yatimizwe hapa duniani, **Mt.** 6:10. Utafuteni kwanza ufalme wa Mungu, **Mt.** 6:33 (3 Ne. 13:33). Nitakupa wewe funguo za ufalme, **Mt.** 16:19. Njooni, urithini ufalme uliowekwa tayari kwa ajili yenu, **Mt.** 25:34. Ninapokula sakramenti pamoja nanyi katika ufalme wa Baba yangu, **Mt.** 26:26–29. Mtawaona manabii wote katika ufalme wa Mungu, **Lk.** 13:28. Wasio waaminifu hawatarithi ufalme wa Mungu, **1 Kor.** 6:9. Nyama na damu haziwezi kuurithi ufalme wa Mungu, **1 Kor.** 15:50.

Kabla ya kutafuta utajiri utafuteni ufalme wa Mungu, **Yak. (KM)** 2:18. Hakuna kitu kichafu kinachoweza kurithi ufalme wa mbinguni, **Alma** 11:37.

Uweze kupumzika pamoja nao katika

ufalme wa Baba yangu, **M&M** 15:6. Kwenu ninyi ufalme au funguo za Kanisa zimetolewa, **M&M** 42:69 (M&M 65:2). Ufalme wa Mungu na uenee ili ufalme wa mbinguni upate kuja, **M&M** 65:5–6. Funguo za ufalme huu kamwe hazitaondoshwa kutoka kwenu, **M&M** 90:3. Yeyote awapokeaye ninyi kama mtoto mdogo, huupokea ufalme wangu, **M&M** 99:3. Hivyo ndivyo Kanisa langu litakavyoitwa katika siku za mwisho, hata Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho, **M&M** 115:4. Mbingu zikafunguliwa nami nikaona ufalme wa selestia wa Mungu, **M&M** 137:1–4.

Ufufuko. *Ona pia* Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa; Lipia dhambi, Upatanisho; Mauti ya Kimwili; Mwili; Roho; Yesu Kristo

Kuungana tena kwa mwili wa kiroho pamoja na mwili wa kawaida wa nyama na mifupa baada ya kifo. Baada ya ufufuko, roho na mwili kamwe havitatengana tena, na mtu atakuwa mtu asiyekufa. Kila mtu aliyezaliwa duniani atafufuka kwa sababu Yesu alishinda mauti (1 Kor. 15:20–22).

Yesu Kristo alikuwa mtu wa kwanza kufufuka katika dunia hii (Mdo. 26:23; Kol. 1:18; Ufu. 1:5). Agano Jipya linatoa ushahidi wa kutosha kwamba Yesu alifufuka pamoja na mwili Wake wa kawaida: kaburi Lake lilikuwa wazi, Alikula samaki na asali, Alikuwa na mwili wa nyama na mifupa, watu Walimgusa, na malaika walisema Amefufuka (Mk. 16:1–6; Lk. 24:1–12, 36–43; Yn. 20:1–18). Ufunuo wa siku za mwisho unathibitisha ukweli juu ya Ufufuko wa Kristo na wa wanadamu wote (Alma 11:40–45; 40; 3 Ne. 11:1–17; M&M 76; Musa 7:62).

Watu wote hawatafufuka katika utukufu mmoja (1 Kor. 15:39–42; M&M 76:89–98), wala hawatafufuka kwa wakati mmoja (1 Kor. 15:22–23; Alma 40:8; M&M 76:64–65, 85; 88:96–102). Watakatifu wengi walifufuka baada ya Ufufuko wa Kristo (Mt. 27:52). Waadilifu watafufuka kabla ya waovu nao watatoka katika Ufufuko wa Kwanza (1 The. 4:16); wenye dhambi wasiotubu watatoka katika ufufuko wa mwisho (Ufu. 20:5–13; M&M 76:85).

Ingawa mwili huu utaangamizwa, lakini katika mwili wangu nitamwona Mungu, **Ayu.** 19:26 (Musa 5:10). Nitayafunua makaburi yenu, na kuwapandisha, **Eze.** 37:12.

Makaburi yakafunuliwa, na miili mingi ikainuka, **Mt.** 27:52–53 (3 Ne. 23:9). Bwana amefufuka, **Lk.** 24:34. Roho haina mwili wa nyama na mifupa, kama mnionavyo mimi, **Lk.** 24:39. Mimi ndimi ufufuko na uzima, **Yn.** 11:25. Mitume Kumi na Wawili walifundisha kwamba Yesu amefufuka, **Mdo.** 1:21–22 (Mdo. 2:32; 3:15; 4:33). Katika Kristo wote watahuishwa, **1 Kor.** 15:1–22. Wanaokufa katika Kristo watafufuka kwanza, **1 The.** 4:16. Heri na mtakatifu ni yeye atakayeshirika katika ufufuko wa kwanza, **Ufu.** 20:6.

Kristo anauweka chini uhai wake na kuutwaa tena ili apate kuleta ufufuko wa wafu, **2 Ne.** 2:8 (Mos. 13:35; 15:20; Alma 33:22; 40:3; Hel. 14:15). Pasipo ufufuko, tungelikuwa chini ya Shetani, **2 Ne.** 9:6–9. Ufufuko utakuwa kwa wanadamu wote, **2 Ne.** 9:22. Abinadi alifundisha juu ya ufufuko wa kwanza, **Mos.** 15:21–26. Waovu wanabaki kama kwamba hapajakuwepo ukombozi, isipokuwa kwa kufunguliwa kwa kamba za mauti, **Alma** 11:41–45. Alma alieleza hali ya roho kati ya kifo na ufufuko, **Alma** 40:6, 11–24.

Wakati wa ujio wa Bwana, wafu waliokufa katika Kristo watafufuka, **M&M** 29:13 (M&M 45:45–46; 88:97–98; 133:56). Walilieni hususani kwa ajili ya wale wasio na tumaini la ufufuko wa utukufu, **M&M** 42:45. Watu ambao hawakujua sheria watakuwa na sehemu katika ufufuko huu wa kwanza, **M&M** 45:54. Watafufuka kutoka katika wafu na hawatakufa baada ya hapo, **M&M** 63:49. Ufufuko kutoka kwa wafu ndiyo ukombozi wa nafsi, **M&M** 88:14–16. Roho na vitu vya asili, ambavyo vimeungana

na havitenganishwi, hupokea utimilifu wa shangwe, **M&M** 93:33. Malaika walio viumbe waliofufuka wana miili ya nyama na mifupa, **M&M** 129:1. Maarifa yoyote tuyapatayo katika maisha haya yatafufuka pamoja nasi katika ufufuko, **M&M** 130:18–19.

Ufungwa. *Ona pia* Huru, Uhuru

Kuwa katika hali ya utumwa wa kimwili au kiroho.

Nyumba ya Israeli ilienda kifungoni kwa sababu ya uovu wao, **Eze.** 39:23.

Yule aongozaye kifungoni atakwenda kifungoni, **Ufu.** 13:10.

Waovu watatupwa chini katika utumwa wa ibilisi, **1 Ne.** 14:4, 7. Wanadamu wako huru kuchagua uhuru na uzima wa milele au utumwa na mauti, **2 Ne.** 2:27. Mapenzi ya mwili hutoa uwezo kwa roho wa ibilisi kuteka nyara, **2 Ne.** 2:29. Je, mngali mnakumbuka vya kutosha utumwa wa mababu zenu, **Alma** 5:5–6. Wale wenye kushupaza mioyo yao huchukuliwa mateka na ibilisi, **Alma** 12:11. Kesheni na kusali daima, msije mkajaribiwa na ibilisi, nanyi mkaongozwa utumwani na yeye, **3 Ne.** 18:15.

Ufunuo. *Ona pia* Maongozi ya Mungu, Shawishi; Ndoto; Neno la Mungu; Nuru, Nuru ya Kristo; Ono; Roho Mtakatifu; Sauti; Toa unabii, Unabii

Mawasiliano kutoka kwa Mungu kwenda kwa watoto Wake duniani. Ufunuo waweza kuja kupitia Nuru ya Kristo na Roho Mtakatifu kwa njia ya maongozi ya kimungu, maono, ndoto, au kutembelewa na malaika. Ufunuo hutoa mwongozo ambao unaweza kumwongoza aliye mwaminifu kwenye wokovu wa milele katika ufalme wa selestia.

Bwana huwafunulia manabii Wake kazi Yake na huthibitisha kwa waumini kwamba ufunuo huo kwa manabii ni wa kweli (Amo. 3:7). Kwa njia ya ufunuo, Bwana hutoa mwongozo binafsi kwa kila mtu autafutaye na kwa aliye na imani, mwenye kutubu, na aliye mtiifu kwa injili ya Yesu Kristo. "Roho Mtakatifu ndiye mfunuzi," alisema Joseph Smith, na "hakuna mtu anayeweza kupokea Roho Mtakatifu pasipo kupokea ufunuo."

Katika Kanisa la Bwana, Urais wa Kwanza na Akidi ya Mitume Kumi na Wawili ndiyo manabii, waonaji, na wafunuzi kwa Kanisa na kwa ulimwengu. Rais wa Kanisa ndiye mtu pekee ambaye Bwana amempa mamlaka ya kupokea ufunuo kwa ajili ya Kanisa (M&M 28:2–7). Kila mtu anaweza kupokea ufunuo kwa ajili ya manufaa yake yeye mwenyewe.

Mwanadamu huishi kwa kila neno litokalo kinywani mwa Bwana, **Kum.** 8:3 (Mt. 4:4; M&M 98:11). Bwana hunena katika sauti ndogo ya utulivu, **1 Fal.** 19:12. Pasipo na ono, watu huangamia, **Mit.** 29:18. Hakika Bwana Mungu hatafanya jambo lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake, **Amo.** 3:7.

Heri wewe Simoni Ba-Yona: kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu, **Mt.** 16:15–19. Roho atawaongoza awatie katika kweli yote na atawaonyesha mambo yajayo, **Yn.** 16:13. Kama yeyote kati yenu akipungukiwa hekima, na aombe kwa Mungu, **Yak. (Bib.)** 1:5.

Mambo yote yatafunuliwa, **2 Ne.** 27:11. Nitawapa watoto wa watu mstari juu ya mstari, **2 Ne.** 28:30. Hakuna siri ambayo haitafunuliwa, **2 Ne.** 30:17. Roho Mtakatifu atakuonyesha mambo yote, **2 Ne.** 32:5. Hakuna mtu azijuaye njia za Mungu isipokuwa amefunuliwa, **Yak. (KM)** 4:8. Alma alifunga na kusali kwa ajili ya kupata ufunuo, **Alma** 5:46. Mambo ambayo kamwe hayajafunuliwa yatafunuliwa kwa walio waaminifu, **Alma** 26:22. Watu wanaokana ufunuo hawaijui injili ya Yesu Kristo na hawayafahamu maandiko, **Morm.** 9:7–8. Hamtapata ushahidi wowote hadi baada ya majaribu ya imani yenu, **Eth.** 12:6.

Neno langu lote litatimia, **M&M** 1:38. Sikusema amani akilini mwako juu ya

jambo hili, **M&M** 6:22–23. Nitakujulisha akilini mwako na katika moyo wako, **M&M** 8:2–3. Kama ni sahihi nitaufanya moyo wako uwake moto, **M&M** 9:8. Usikatae roho ya ufunuo, **M&M** 11:25. Wale waombao watapokea ufunuo juu ya ufunuo, **M&M** 42:61. Lolote watakalonena wakati wakiongozwa na Roho Mtakatifu litakuwa ni sauti ya Bwana, **M&M** 68:4. Mungu atakupa maarifa, **M&M** 121:26.

Joseph Smith aliwaona Baba na Mwana, **JS—H** 1:17. Tunaamini yale yote Mungu aliyoyafunua na yale atakayoyafunua, **M ya I** 1:7, 9.

Ufunuo wa Yohana. *Ona pia* Apokalisi; Yohana, Mwana wa Zebedayo

Kitabu cha mwisho katika Agano Jipya, kilicho na ufunuo uliotolewa kwa Yohana Mtume. Aliruhusiwa kuona historia ya ulimwengu, hususani siku za mwisho (Ufu. 1:1–2; 1 Ne. 14:18–27; M&M 77). Ufunuo wa Yohana pia hujulikana kama Apokalisi.

Yohana alipokea ufunuo katika siku ya Bwana katika kisiwa cha Patmo (Ufu. 1:9–10), ng'ambo ya pwani ya Asia, siyo mbali na Efeso. Tarehe halisi ya ufunuo huu haijulikani.

Funguo za kukielewa kitabu hiki zimejumuishwa katika 1 Nefi 14:18–27 na Mafundisho na Maagano 77 (Eth. 4:15–16).

Mlango wa 1–3 ni utangulizi kwa kitabu hiki na barua kwa makanisa saba katika Asia. Yohana aliandika barua hizi ili kuwasaidia Watakatifu kutatua matatizo fulani. Mlango wa 4–5 imeandikwa maono ambayo Yohana alipokea yenye kuonyesha ukuu wa enzi na uwezo wa haki ya Mungu na Kristo. Katika mlango wa 6–9, 11, Yohana ameandika kuwa aliona kitabu kilichotiwa mihuri saba, kila muhuri unawakilisha miaka elfu moja ya historia ya muda ya dunia. Mlango huu kimsingi hujishughulisha na matukio yaliyomo katika muhuri wa saba (ona Ufu. 8–9; 11:1–15). Mlango wa 10 unaelezea juu ya kitabu ambacho Yohana alikila. Kitabu kinawakilisha huduma ya baadaye ambayo yeye angeifanya. Mlango wa 12 unaandikwa ono la ule uovu ambao ulianzia mbinguni wakati Shetani alipoasi na kutupwa nje. Vita vilivyoanza huko vinaendelea kupiganwa duniani. Katika mlango 13, 17–19, Yohana anaelezea falme ovu za kidunia zinazodhibitiwa na Shetani na akaandika maangamizo yake, ikijumuisha angamizo la mwisho la uovu. Mlango wa 14–16 huelezea uadilifu wa Watakatifu katikati ya uovu muda mfupi kabla ya ujio wa pili wa Kristo. Mlango wa 20–22 inaelezea juu ya Milenia, mji mzuri wa Yerusalemu Mpya, na matukio ya mwisho ya historia ya dunia.

Ugonjwa. *Ona* Ugonjwa, Ugua

Ugonjwa, Ugua

Kuwa na ugonjwa au maradhi. Katika maandiko, ugonjwa wa kimwili wakati mwingine hutumika kama ishara ya ukosefu wa uzima wa kiroho (Isa. 1:4–7; 33:24).

Nimesikia sala zako, nimeona machozi yako; tazama, nitakuponya, **2 Fal.** 20:1–5 (2 Nya. 32:24; Isa. 38:1–5).

Yesu alienda huku na huku akiponya kila aina ya magonjwa na aina zote za maradhi, **Mt.** 4:23–24 (1 Ne. 11:31; Mos. 3:5–6). Walio wazima hawamhitaji tabibu, bali wao walio wagonjwa, **Mt.** 9:10–13 (Mk. 2:14–17; Lk. 5:27–32). Je, kuna yeyote aliye mgonjwa miongoni kati yenu? na awaite wazee, **Yak. (Bib.)** 5:14–15.

Kristo atajichukulia juu yake maumivu na magonjwa ya watu wake, **Alma** 7:10–12. Yesu aliwaponya wagonjwa wote miongoni mwa Wanefi, **3 Ne.** 26:15.

Mlisheni aliye mgonjwa kwa upendo, madawa, na kwa chakula laini, **M&M** 42:43 (Alma 46:40). Katika mambo yote wakumbukeni walio wagonjwa na wenye kuteseka, **M&M** 52:40. Wekeni mikono yenu juu ya wagonjwa, nao watapona, **M&M** 66:9.

Uhuru. *Ona* Huru, Uhuru

Ujio wa Pili wa Yesu Kristo. *Ona pia* Gogu; Har-Magedoni; Ishara za Nyakati; Magogu; Yesu Kristo

Mwanzoni mwa Enzi ya Milenia, Kristo atarudi duniani. Tukio hili litaonyesha ule mwisho wa kipindi cha majaribu cha mwili wenye kufa cha dunia hii. Waovu wataondolewa kutoka duniani na waadilifu watatwaliwa katika wingu wakati dunia ikisafishwa. Wakati hakuna mwanadamu ajuaye hasa lini Kristo atakuja kwa mara ya pili, Yeye ametupa sisi ishara za kuzitazamia ambazo zinaashiria wakati umekaribia (Mt. 24; JS—M 1).

Ninajua kwamba Mkombozi wangu katika siku ya mwisho atasimama juu ya dunia, **Ayu.** 19:25. Mbele zangu kila goti litapigwa, kila ulimi utaapa, **Isa.** 45:23 (M&M 88:104). Mwana wa Mtu alikuja kwa mawingu ya mbinguni, **Dan.** 7:13 (Mt. 26:64; Lk. 21:25–28). Watanitazama mimi ambaye walimchoma, **Zek.** 12:10. Mtu atasema, Je, jeraha hizi mikononi mwako ni nini, **Zek.** 13:6 (M&M 45:51). Ni nani atakayestahmili hadi katika siku ya kuja kwake? kwa maana yeye ni kama moto wa mtu asafishaye fedha, **Mal.** 3:2 (3 Ne. 24:2; M&M 128:24).

Mwana wa Mtu atakuja katika utukufu wa Baba yake, **Mt.** 16:27 (Mt. 25:31). Juu ya siku ile na saa ile hakuna mtu ajuaye, ila Baba yangu peke yake, **Mt.** 24:36 (M&M 49:7; JS—M 1:38–48). Huyu Yesu atakuja jinsi hiyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni, **Mdo.** 1:11. Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni, **1 The.** 4:16. Siku ya Bwana itakuja kama mwivi ajavyo usiku, **2 Pet.** 3:10. Bwana atakuja pamoja na maelfu kumi ya Watakatifu wake, **Yuda** 1:14. Yuaja na mawingu, na kila jicho litamwona, **Ufu.** 1:7.

Yesu atasimama ili auhukumu ulimwengu, **3 Ne.** 27:14–18.

Jitayarisheni, jitayarisheni, kwa maana Bwana yu karibu, **M&M** 1:12. Nitajifunua mwenyewe kutoka mbinguni kwa uwezo, na kukaa duniani miaka elfu, **M&M** 29:9–12. Pazeni sauti zenu na kutangaza toba, mkimtengenezea Bwana njia kwa ujio wake wa pili, **M&M** 34:5–12. Mimi ndimi Yesu Kristo, nami nitakuja ghafla hekaluni mwangu, **M&M** 36:8 (M&M 133:2). Siku i karibu kuja ambayo mtaniona, na kujua kuwa Mimi ndimi, **M&M** 38:8. Yule aniogopaye mimi atazitazamia ishara za kuja kwa Mwana wa Mtu, **M&M** 45:39. Uso wa Bwana utafunuliwa, **M&M** 88:95. Siku ile iliyo kuu na ya kutisha ya Bwana i karibu, **M&M** 110:16. Wakati Mwokozi atakapoonekana tutamwona yeye kama alivyo, **M&M** 130:1. Mwokozi atasimama katikati ya watu wake na atatawala, **M&M** 133:25. Huyu ni nani ashukaye kutoka kwa Mungu mbinguni akiwa na mavazi yaliyotiwa rangi, **M&M** 133:46 (Isa. 63:1).

Ukengeufu. *Ona pia* Uasi; Urejesho wa Injili

Kugeuka mbali na ukweli kwa mtu binafsi, Kanisa, au taifa lote.

Ukengeufu wa jumla: Israeli walijilinda mioyo yao isigeuke mbali na Bwana, **Kum.** 29:18. Pale pasipo maono, watu huangamia, **Mit.** 29:18. Wamelivunja agano lisilo na mwisho, **Isa.** 24:5.

Pepo zikapiga nyumba ile, nayo ikaanguka, **Mt.** 7:27. Nastaajabu kwamba kwa upesi mmegeukia katika injili nyingine, **Gal.** 1:6.

Walianza katika njia nzuri lakini katikati ya ukungu wakaipoteza njia yao, **1 Ne.** 8:23 (1 Ne. 12:17). Baada ya kuonja lile tunda, wakaangukia katika njia zilizokatazwa, **1 Ne.** 8:28. Ukengeufu wa Wanefi ulisababisha vikwazo kwa wale wasio amini, **Alma** 4:6–12. Waumini wengi wa Kanisa wakawa na kiburi na wakiwatesa waumini wengine, **Hel.** 3:33–34 (Hel. 4:11–13; 5:2–3). Bwana anapowastawisha watu wake nyakati nyingine wao hushupaza mioyo yao na kumsahau yeye, **Hel.** 12:2; 13:38. Wanefi walishupaza mioyo yao na kuanguka chini ya uwezo wa Shetani, **3 Ne.** 2:1–3.

Moroni alitoa unabii juu ya uasi katika siku za mwisho, **Morm.** 8:28, 31–41.

Ukengeufu utatangulia Ujio wa Pili, **M&M** 1:13–16.

Ukengeufu wa Kanisa la awali la Kikristo: Watu hawa hunikaribia kwa vinywa vyao, **Isa.** 29:10, 13. Giza litaifunika dunia, **Isa.** 60:2. Bwana ataileta njaa ya kuyasikia maneno ya Bwana, **Amo.** 8:11.

Watatokea Makristo wa uongo na manabii wa uongo, **Mt.** 24:24. Mbwa mwitu wakali wataingia miongoni mwenu, **Mdo.** 20:29. Nastaajabu kwamba kwa upesi mmeondoshwa kutoka kwake, **Gal.** 1:6. Kutakuwa na ukengeufu kabla ya Ujio wa Pili, **2 The.** 2:3. Baadhi ya watu hukosea juu ya ukweli, **2 Tim.** 2:18. Baadhi ya watu wana mfano wa uchamungu lakini wakikana nguvu zake, **2 Tim.** 3:2–5. Wakati utafika wakati ambao hawatastahimili mafundisho yenye uzima, **2 Tim.** 4:3–4. Patakuwepo na manabii wa uongo na walimu wa uongo miongoni mwa watu, **2 Pet.** 2:1. Kuna watu waliojiingiza kwa siri katika kumkana Bwana Mungu pekee, **Yuda** 1:4. Baadhi ya watu walisema kuwa walikuwa Mitume na hawakuwa, **Ufu.** 2:2.

Nefi aliona kuundwa kwa kanisa lile kuu na lenye machukizo, **1 Ne.** 13:26. Wayunani wamejikwaa na kujenga makanisa mengi, **2 Ne.** 26:20.

Wameenda kinyume na ibada zangu na wamevunja agano langu lisilo na mwisho, **M&M** 1:15. Giza limeifunika dunia na giza nene limezifunika akili za watu, **M&M** 112:23.

Joseph aliambiwa kwamba makanisa yote hayakawa sahihi; mioyo yao ilikuwa mbali na Mungu, **JS—H** 1:19.

Ukoma

Aina ya ugonjwa wa kutisha wa ngozi unaoambukiza umetajwa mara kwa mara katika Agano la Kale na Jipya. Watu wengi maarufu katika Biblia kwa wakati fulani waliathirika nao, ikiwa ni pamoja na Musa (Ku. 4:6–7), dada yake Miriamu (Hes. 12:10), Naamani (2 Fal. 5), na Mfalme Uzia (2 Nya. 26:19–21).

Yesu aliponya ukoma katika watu kadha wa kadha, **Mt.** 8:2–4 (Mk. 1:40–45; Lk. 5:12–15; 3 Ne. 17:7–9). Yesu aliwaponya wakoma kumi, **Lk.** 17:11–19.

Ukombozi. *Ona* Komboa, Kombolewa, Ukombozi

Ukombozi, Mpango wa. *Ona* Mpango wa Ukombozi

Ukosefu wa Maadili. *Ona* Isiyo kufa, Maisha ya kutokufa

Ukuhani. *Ona pia* Funguo za Ukuhani; Kiapo na Agano la Ukuhani; Kutawaza, Kutawazwa; Mamlaka; Ukuhani wa Haruni; Ukuhani wa Melkizedeki; Uwezo

Mamlaka na uwezo ambao Mungu humpa mwanadamu ili atende katika mambo yote kwa ajili ya wokovu wa mwanadamu (M&M 50:26–27). Waumini wa Kanisa wanaume walio na ukuhani wametengwa katika akidi nao wamepewa mamlaka ya kufanya ibada na shughuli fulani za kiutawala katika Kanisa.

Kutiwa mafuta kwao hakika kutakuwa ni kwa ukuhani usio na mwisho, **Ku.** 40:15 (Hes. 25:13).

Mimi nimewachagua ninyi, **Yn.** 15:16. Mmejengwa muwe nyumba ya kiroho, ukuhani mtakatifu, **1 Pet.** 2:5. Ninyi ni zao teule, ukuhani wa kifalme, **1 Pet.** 2:9 (Ku. 19:6).

Wanaume huitwa kama makuhani wakuu kwa sababu ya imani na matendo yao mema yanayopita kiasi, **Alma** 13:1–12. Ninawapa ninyi uwezo wa kubatiza, **3 Ne.** 11:21. Ninyi mtakuwa na uwezo wa kutoa Roho Mtakatifu, **Moro.** 2:2.

Nitaufunua kwenu ukuhani, kwa mkono wa Eliya, **M&M** 2:1 (JS—H 1:38). Bwana alithibitisha ukuhani juu ya Haruni na kizazi chake, **M&M** 84:18. Ukuhani huu mkuu zaidi huhudumia injili, **M&M** 84:19. Alimchukua Musa kutoka katikati yao, na Ukuhani Mtakatifu pia, **M&M** 84:25. Kiapo na agano la ukuhani vinaelezwa, **M&M** 84:33–42. Ukuhani

umedumu kupitia safu ya uzao wa baba zenu, **M&M** 86:8. Katika Kanisa kuna kuhani mbili, **M&M** 107:1. Ukuhani wa kwanza ni Ukuhani Mtakatifu, kwa Mfano wa Mwana wa Mungu, **M&M** 107:2–4. Haki za ukuhani zimeungana na hazitenganishwi na nguvu za mbinguni, **M&M** 121:36. Hakuna nguvu au uwezo unaoweza au upaswao kudumishwa kwa njia ya ukuhani isipokuwa tu kwa ushawishi na upendo usio unafiki, **M&M** 121:41. Kila mwanaume muumini wa kanisa mwenye kustahili anaweza kupokea ukuhani, **TR** 2.

Tunaamini kwamba mwanadamu lazima aitwe na Mungu, **M ya I** 1:5.

Ukuhani, Funguo za. *Ona* Funguo za Ukuhani

Ukuhani Mkuu. *Ona* Ukuhani wa Melkizedeki

Ukuhani wa Haruni. *Ona pia* Haruni, Kaka wa Musa; Torati ya Musa; Ukuhani

Ukuhani mdogo (Ebr. 7:11–12; M&M 107:13–14). Ofisi zake ni askofu, kuhani, mwalimu, na shemasi (M&M 84:30; 107:10, 14–15, 87–88). Hapo zamani, chini ya sheria za Musa, palikuwepo na makuhani wakuu, makuhani, na Walawi. Kwa sababu Waisraeli wa kale walimwasi Mungu. Musa nan a ukuhani mtakatifu waliondolewa kutoka kwao na ukuhani mdogo uliendelea. Wao walikataa kutakaswa na kupokea Ukuhani wa Melkizedeki na ibada zake. (Ona M&M 84:23–26.) Ukuhani wa Haruni hushughulikia ibada za kimwili na za nje katika sheria ya injili (1 Nya. 23:27–32; M&M 84:26–27; 107:20). Una shikilia funguo za huduma ya malaika, za injili ya toba, na ubatizo (M&M 13). Ukuhani wa Haruni ulirejeshwa duniani katika kipindi hiki 15 Mei 1829, Yohana Mbatizaji aliwatunukia Joseph Smith na Oliver Cowdery jirani na Harmony, Pennsylvania (M&M 13; JS—H 1:68–73).

Naye atakuwa na agano la ukuhani usio na mwisho, **Hes.** 25:13. Bwana atawatakasa wana wa Lawi, na kuwasafisha, **Mal.** 3:3 (3 Ne. 24:3).

Na hapana mtu ajitwaliaye mwenyewe heshima hii, **Ebr.** 5:4. Ukamilifu hauji kwa Ukuhani wa Lawi, **Ebr.** 7:11.

Ukuhani huu kamwe hautaondolewa duniani hadi wana wa Lawi wamtolee sadaka, **M&M** 13. Joseph Smith na Oliver Cowdery walitawazwa katika ukuhani wa Haruni, **M&M** 27:8. Ukuhani mdogo unashikilia funguo ya kuhudumiwa na malaika, **M&M** 84:26 (M&M 13). Kuna kuhani mbili, nazo ni, Melkizedeki na Haruni, **M&M** 107:1. Ukuhani wa pili unaitwa Ukuhani wa Haruni, **M&M** 107:13.

Ukuhani wa Lawi. *Ona* Ukuhani wa Haruni

Ukuhani wa Melkizedeki. *Ona pia* Melkizedeki; Mzee; Ukuhani

Ukuhani wa Melkizedeki ni ukuhani wa juu zaidi au mkuu zaidi; Ukuhani wa Haruni ni ukuhani mdogo zaidi. Ukuhani wa Melkizedeki unajumuisha funguo za baraka za kiroho za Kanisa. Kwa njia ya ibada za ukuhani wa juu zaidi nguvu za uchamungu huonekana kwa wanadamu (M&M 84:18–25; 107:18–21).

Mungu kwanza aliufunua ukuhani huu mkuu zaidi kwa Adamu. Mapatriaki na manabii katika kila kipindi walikuwa na mamlaka haya (M&M 84:6–17). Mwanzoni uliitwa Ukuhani Mtakatifu, kwa Mfano wa Mwana wa Mungu. Baadaye ukajulikana kama Ukuhani wa Melkizedeki (M&M 107:2–4).

Wana wa Israeli waliposhindwa kuishi kulingana na heshima na maagano ya Ukuhani wa Melkizedeki, Bwana aliiondoa sheria hii ya juu zaidi na akawapa ukuhani mdogo zaidi na torati ndogo zaidi (M&M 84:23–26). Hizi ziliitwa Ukuhani wa Haruni na torati ya Musa. Yesu alipokuja duniani, Alirejesha Ukuhani wa Melkizedeki kwa Wayahudi na akaanza kulijenga Kanisa miongoni mwao. Hata hivyo, ukuhani na Kanisa ukapotea tena kwa njia ya ukengeufu.

Ukarejeshwa tena baadaye kupitia Joseph Smith Mdogo (M&M 27:12–13; 128:20; JS—H 1:73).

Ndani ya Ukuhani wa Melkizedeki kuna ofisi za mzee, kuhani mkuu, patriaki, Sabini, na Mtume (M&M 107). Ukuhani wa Melkizedeki daima utakuwa ni sehemu ya ufalme wa Mungu duniani.

Rais wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho ndiye rais wa Ukuhani mkuu au wa Melkizedeki, naye hushikilia funguo zote zihusuzo ufalme wa Mungu duniani. Wito wa Rais hushikiliwa na mwanamume mmoja tu kwa wakati mmoja, naye ndiye mtu pekee duniani aliye na mamlaka ya kutumia funguo zote za ukuhani (M&M 107:64–67; 132:7).

Kristo atakuwa kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki, **Zab.** 110:4 (Ebr. 5:6, 10; 7:11).

Ukuhani wa Melkizedeki husimamia injili, **Ebr.** 7 (M&M 84:18–25).

Melkizedeki alionyesha imani kubwa na akapokea ofisi ya ukuhani mkuu, **Alma** 13:18.

Ukuhani wa Melkizedeki ulitunukiwa juu ya Joseph Smith na Oliver Cowdery, **M&M** 27:12–13 (JS—H 1:72). Ukuhani huu hupokelewa kwa kiapo na agano, **M&M** 84:33–42. Kuna migawanyiko au vichwa vikuu viwili, yaani Kuhani za Melkizedeki na Haruni, **M&M** 107:6. Ukuhani wa Melkizedeki hushikilia haki ya kusimamia baraka zote za kiroho, **M&M** 107:8–18. Musa, Elia, na Eliya waliwapa Joseph Smith na Oliver Cowdery funguo za ukuhani, **M&M** 110:11–16. Sasa ninawatoa kwenyu maofisa walio wa ukuhani wangu, ili ninyi mpate kuzishika funguo zake, **M&M** 124:123.

Ukuhani wa uongo

Watu wanaohubiri na kujiweka juu ili kuwa nuru kwa ulimwengu ili waweze kupata faida na sifa za walimwengu; hawatafuti ustawi wa Sayuni (2 Ne. 26:29).

Lichungeni kundi la Mungu, si kwa kutaka fedha ya aibu, **1 Pet.** 5:2.

Makanisa yaliyojengwa kwa ajili ya kujinufaisha lazima yaangushwe, **1 Ne.** 22:23 (Morm. 8:32–41). Kwa sababu ya ukuhani wa uongo na uovu, Yesu atasulubiwa, **2 Ne.** 10:5. Kama ukuhani wa uongo utaingizwa miongoni mwa watu hawa itathibitisha angamizo lao wote, **Alma** 1:12. Wayunani watajawa na kila aina ya ukuhani wa uongo, **3 Ne.** 16:10.

Ukwasi. *Ona pia* Fedha; Kiburi

Mali au kuwa na vitu. Bwana huwashauri Watakatifu wasitafute utajiri wa kiulimwengu isipokuwa kwa kufanya yaliyo mema. Watakatifu lazima wasijiwekwe katika kutafuta utajiri wa kiulimwengu kabla ya kutafuta ufalme wa Mungu, ambao ndiyo hushikila utajiri wa milele (Yak. [KM] 2:18–19).

Mali izidipo, msiiangalie sana moyoni, **Zab.** 62:10. Mali hazifaidi kitu siku ya ghadhabu, **Mit.** 11:4. Mtu azitegemeaye mali zake ataanguka, **Mit.** 11:28. Heri kuchagua jina jema kuliko mali nyingi, **Mit.** 22:1.

Jinsi itakavyokuwa vigumu kwa wenye mali kuingia katika ufalme wa Mungu, **Mk.** 10:23 (Lk. 18:24–25). Kupenda fedha ndiyo shina la uovu wote, **1 Tim.** 6:10.

Ole wao matajiri wenye kuwadharau maskini na ambao hazina zao ndiyo mungu wao, **2 Ne.** 9:30. Wenye haki hawakuiweka mioyo yao juu ya mali, waliwagawia wote, **Alma** 1:30. Watu walianza kuwa na kiburi kwa sababu ya mali, **Alma** 4:6–8. Watu walitambuliwa kwa vyeo, kulingana na mali zao, **3 Ne.** 6:12.

Usitafute mali bali hekima, **M&M** 6:7 (Alma 39:14; M&M 11:7). Mali za dunia zinatolewa na Mungu, lakini jihadharini na kiburi, **M&M** 38:39.

Utajiri wa Milele: Jiwekeeni hazina mbinguni, **Mt.** 6:19–21.

Ni mara ngapi nimewaita kwa mali za uzima wa milele, **M&M** 43:25. Mali za milele ni juu yangu kuzitoa, **M&M** 67:2 (M&M 78:18).

Ukweli. *Ona pia* Akili, Viumbe-akili-asilia; Maarifa; Nuru, Nuru ya Kristo

Ufahamu wa mambo kama yalivyo, na kama yalivyokuwa, na kama yatavyokuwa (M&M 93:24). Ukweli pia unamaanisha nuru na ufunuo kutoka mbinguni.

Ukweli utachipua kutoka duniani, **Zab.** 85:11 (Musa 7:62).

Mtaufahamu ukweli, na ukweli utawafanya muwe huru, **Yn.** 8:32. Mimi ndimi njia, ukweli, na uzima, **Yn.** 14:6. Kama tutasema hatuna dhambi, ukweli hauko ndani yetu, **1 Yoh.** 1:8.

Wenye hatia huuchukulia ukweli kuwa ni mgumu, **1 Ne.** 16:2. Wenye haki hupenda ukweli, **2 Ne.** 9:40. Roho hunena yaliyo ya ukweli na wala hadanganyi, **Yak. (KM)** 4:13. Wewe u Mungu wa ukweli na huwezi kudanganya, **Eth.** 3:12. Kwa uwezo wa Roho Mtakatifu waweza kujua ukweli wa mambo yote, **Moro.** 10:5.

Ukweli hudumu milele na milele, **M&M** 1:39. Wewe umeangaziwa na Roho wa ukweli, **M&M** 6:15. Kitabu cha Mormoni kina ukweli na neno la Mungu, **M&M** 19:26. Mfariji alipelekwa kufundisha ukweli, **M&M** 50:14. Mtu ambaye hulipokea neno kwa Roho wa ukweli huupokea kama linavyohubiriwa na Roho wa ukweli, **M&M** 50:17–22. Tangazeni ukweli kulingana na mafunuo niliyowapeni, **M&M** 75:3–4. Lolote lililo la kweli ni nuru, **M&M** 84:45. Nuru ya Kristo ni nuru ya ukweli, **M&M** 88:6–7, 40. Roho yangu ni ukweli, **M&M** 88:66. Akili, au nuru ya kweli, haikuumbwa, **M&M** 93:29. Utukufu wa Mungu ni akili, au nuru na ukweli, **M&M** 93:36. Nimewaamuru ninyi kuwalea watoto wenu katika nuru na ukweli, **M&M** 93:40.

Mwanangu wa Pekee amejaa neema na ukweli, **Musa** 1:6.

Ulimi. *Ona pia* Ndimi, Kipawa cha

Ishara ya kunena. Watakatifu wazuie ndimi zao, maana yake ni kwamba wazuie kunena kwao. Ulimi pia una maana ya lugha na watu. Hatimaye, kila goti litapigwa na kila ulimi utakiri kwa Mungu (Isa. 45:23; Rum. 14:11).

Uzuie ulimi wako na uovu, **Zab.** 34:13 (1 Pet. 3:10). Mtu azuiaye kinywa chake na ulimi wake atajilinda nafsi yake na taabu, **Mit.** 21:23.

Kama mtu yeyote hauzuii ulimi wake, dini mtu huyo haifai, **Yak. (Bib.)** 1:26. Kama mtu yeyote hawakosei wengine kwa neno, huyo mtu mkamilifu, **Yak. (Bib.)** 3:1–13. Injili hii itahubiriwa kwa kila taifa, kabila, lugha, na watu, **Ufu.** 14:6–7 (2 Ne. 26:13; Mos. 3:13, 20; M&M 88:103; 112:1).

Bwana huyapa mataifa yote, kila taifa na lugha yake, kufundisha neno lake, **Alma** 29:8. Mabamba yatalifikia kila taifa, kabila, lugha, na watu, **Alma** 37:4.

Lipate neno langu, na ndipo ulimi wako utalegezwa, **M&M** 11:21. Kila mtu atausikia utimilifu wa injili katika lugha yake mwenyewe, **M&M** 90:11.

Ulimwengu. *Ona pia* Babeli, Babilonia; Dunia; Hali ya Kufa, enye Kufa

Dunia; mahali pa majaribu kwa wanadamu wenye miili ya kufa. Kama ishara, hutumika kwa wale watu ambao hawatii amri za Mungu.

Maisha ya kuishi duniani: Katika ulimwengu mtapata dhiki, **Yn.** 16:33.

Msiogope hata kama itabidi kufa; kwani katika ulimwengu huu shangwe yenu siyo kamilifu, **M&M** 101:36.

Watu wasiotii amri: Nitauadhibu ulimwengu kwa sababu ya uovu wake, **Isa.** 13:11 (2 Ne. 23:11).

Kama ulimwengu utawachukia, ninajua ya kuwa ulinichukia mimi kabla ya kuwachukia ninyi, **Yn.** 15:18–19.

Jumba kubwa na pana lilikuwa ni kiburi cha ulimwengu, **1 Ne.** 11:36.

Ulimwengu unaiva katika uovu, **M&M** 18:6. Ujilinde na mawaa kutoka ulimwenguni, **M&M** 59:9. Yule aliye mwaminifu na mwenye kustahmili ataushinda ulimwengu, **M&M** 63:47.

Hamtaishi kwa jinsi ya ulimwengu, **M&M** 95:13.

Mwisho wa ulimwengu: Ninaumba dunia mpya: na ya kwanza haitakumbukwa, **Isa.** 65:17 (Ufu. 21:1; M ya I 1:10).

Katika mwisho wa ulimwengu huu, magugu yatakusanywa na kuchomwa katika moto, **Mt.** 13:40, 49 (Mal. 4:1; Yak. [KM] 6:3).

Nitafanya shamba langu la mizabibu lichomwe kwa moto, **Yak. (KM)** 5:77 (M&M 64:23–24).

Bwana atamwangamiza Shetani na kazi zake mwisho wa ulimwengu, **M&M** 19:3. Dunia itakufa, lakini itahuishwa tena, **M&M** 88:25–26.

Bwana alimwonyesha Henoko mwisho wa ulimwengu, **Musa** 7:67.

Ulimwengu wa Roho. *Ona* Jehanamu; Maisha kabla ya kuzaliwa; Peponi

Umba, Uumbaji. *Ona pia* Dunia; Mwanzo; Siku ya Sabato; Uumbaji wa Kiroho; Yesu Kristo

Kupanga. Mungu, akifanya kazi kupitia Mwanawe, Yesu Kristo, alipanga vitu vya asilia katika asili yake ili kutengeneza mbingu na dunia. Baba wa Mbinguni na Yesu Kristo walimuumba mwanadamu katika mfano Wao (Musa 2:26–27).

Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na dunia, **Mwa.** 1:1. Na tufanye mtu kwa mfano wetu, **Mwa.** 1:26 (Musa 2:26–27; Ibr. 4:26).

Vitu vyote vilifanywa kwa njia yake, **Yn.** 1:3, 10. Katika yeye vitu vyote viliumbwa vilivyoko mbinguni, **Kol.** 1:16 (Mos. 3:8; Hel. 14:12). Mungu alizifanya ulimwengu kwa Mwana wake, **Ebr.** 1:2.

Mwanadamu aliumbwa mwanzoni, **Mos.** 7:27. Niliyeumba mbingu na dunia na vitu vyote, **3 Ne.** 9:15 (Morm. 9:11, 17). Wanadamu wote waliumbwa mwanzoni kwa mfano wangu mwenyewe, **Eth.** 3:15.

Yesu Kristo aliziumba mbingu na dunia, **M&M** 14:9. Aliwaumba mtu, mme na mke, kwa mfano wake, **M&M** 20:18.

Na dunia pasipo idadi nimeziumba, **Musa** 1:33. Kwa njia ya Mwanangu wa pekee niliziumba mbingu, **Musa** 2:1. Mimi, Bwana Mungu niliviumba vitu vyote kiroho kwanza kabla havijawa kikawaida juu ya uso wa dunia, **Musa** 3:5. Mamilioni ya dunia kama hii isingelikuwa mwanzo wa hesabu ya viumbe vyako, **Musa** 7:30. Miungu walipanga na kuzitengeneza mbingu, **Ibr.** 4:1.

Umoja. *Ona pia* Mungu, Uungu

Kuwa wamoja katika mawazo, tamaa, na madhumuni kwanza na Baba yetu wa Mbinguni na Yesu Kristo, na kisha na Watakatifu wengine.

Ni vyema kwa ndugu kukaa katika umoja, **Zab.** 133:1.

Mimi na Baba tu wamoja, **Yn.** 10:30 (M&M 50:43). Yesu alisali kwamba wote wapate kuwa wamoja kama yeye na Baba yake walivyo wamoja, **Yn.** 17:11–23 (3 Ne. 19:23). Nawasihi kwamba pasiwe na mgawanyiko miongoni mwenu, bali kwamba muwe mumeungana pamoja kwa ukamilifu, **1 Kor.** 1:10.

Mdhamirie katika nia moja na katika moyo mmoja, mkiungana katika mambo yote, **2 Ne.** 1:21. Watakatifu inapaswa mioyo yao ishonwe pamoja katika umoja, **Mos.** 18:21. Yesu alisali kwa ajili ya umoja miongoni mwa wanafunzi wake Wanefi, **3 Ne.** 19:23. Wanafunzi waliungana katika kusali na kufunga kwa bidii, **3 Ne.** 27:1.

Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu ni wamoja, **M&M** 20:27–28 (M&M 35:2; 50:43). Ni wajibu wako kuungana na Kanisa la kweli, **M&M** 23:7. Lolote mtakaloomba kwa imani, mkiwa mmeungana katika sala, mtapata, **M&M** 29:6. Kama si wamoja ninyi sio wangu, **M&M** 38:27.

Bwana aliwaita watu wake Sayuni kwa sababu walikuwa wenye moyo mmoja na nia moja, **Musa** 7:18.

Umungu. *Ona* Kuinuliwa; Mwanadamu, Wanadamu—Mwanadamu, uwezekano wa kuwa kama Baba wa Mbinguni; Uzima wa Milele

Unabii. *Ona* Toa unabii, Unabii

Unyenyekevu. *Ona* Mnyenyekevu, Unyenyekevu

Uongofu. *Ona* Mwongofu, Uongofu

Uoshaji. *Ona* Osha, Oshwa, Uoshaji

Uovu. *Ona* Ovu, Uovu

Upangaji Uzazi. *Ona pia* Familia; Ndoa, Oa, Olewa

Kupanga idadi ya watoto wa kuzaliwa kwa mke na mume kwa kuweka kikomo au kwa kuzuia utungaji mimba.

Zaeni, na mkaongezeke, na mkaijaze dunia, **Mwa.** 1:28 (Musa 2:28). Watoto ndiyo urithi wa Bwana, **Zab.** 127:3–5.

Familia ya Lehi walitakiwa kumzalia Bwana kizazi, **1 Ne.** 7:1.

Ndoa iliagizwa na Mungu kwa mwanadamu, **M&M** 49:15–17. Walioinuliwa watapokea utimilifu na kuendelea kwa vizazi milele na milele, **M&M** 132:19, 63.

Upangaji watoto. *Ona pia* Ibrahimu—Uzao wa Ibrahimu; Israeli; Wana na Mabinti za Mungu; Watoto wa Kristo

Maandiko huzungumza juu ya aina mbili za upangaji watoto.

(1) Mtu ambaye si wa ukoo wa Kiisraeli huweza kuwa mshirika wa familia ya Ibrahimu na wa nyumba ya Israeli kwa kuwa na imani katika Yesu Kristo, kutubu, kwa kubatizwa kwa kuzamishwa, na kumpokea Roho Mtakatifu (2 Ne. 31:17–18; M&M 84:73–74; Ibr. 2:6, 10–11).

(2) Wale wote waliopokea ibada za injili za wokovu huwa wana na mabinti za Yesu Kristo kwa kuendelea kutii amri Zake (Rum. 8:15–17; Gal. 3:24–29; 4:5–7; Mos. 5:7–8).

Upatanisho. *Ona* Lipia dhambi, Upatanisho

Upendo. *Ona pia* Hisani; Huruma; Uadui

Upenzi na urafiki wa kina. Upendo kwa Mungu ni pamoja na kupenda kwa moyo, kuabudu, heshima kuu, upole, rehema, msamaha, huruma, neema, huduma, shukrani, wema. Mfano mkuu wa upendo wa Mungu kwa watoto wake unaonekana katika Upatanisho usio na mwisho wa Yesu Kristo.

Mpende jirani yako kama nafsi yako, **Law.** 19:18 (Mt. 5:43–44; 22:37–40; Rum. 13:9; Gal. 5:14; Yak. [Bib.] 2:8; Mos. 23:15; M&M 59:6). Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, **Kum.** 6:5 (Moro. 10:32; M&M 59:5). Bwana Mungu wenu yu awajaribu, apate kujua kwamba mwampenda Bwana Mungu wenu, **Kum.** 13:3. Bwana ampendaye humrudi, **Mit.** 3:12. Rafiki hupenda wakati wote, **Mit.** 17:17.

Jinsi gani Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa Pekee, **Yn.** 3:16 (M&M 138:3). Mpendane, kama nilivyowapenda ninyi, **Yn.** 13:34 (Yn. 15:12, 17; Musa 7:33). Kama mnanipenda, zishikeni amri zangu, **Yn.** 14:15 (M&M 42:29). Hakuna mtu aliye na upendo mkuu kana huu, kwamba ananatoa maisha yake kwa marafiki zake, **Yn.** 15:13. Petro, wanipenda kuliko hawa? Lisha kondoo wangu, **Yn.** 21:15–17. Hakuna kitu kitakachotutenga sisi na upendo wa Mungu ulio katika Kristo, **Rum.** 8:35–39. Jicho halijaona mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao, **1 Kor.** 2:9. Tumikianeni kwa upendo, **Gal.** 5:13. Waume, wapendeni wake zenu, **Efe.** 5:25 (Kol. 3:19). Msiipende dunia, **1 Yoh.** 2:15. Mungu ni upendo, **1 Yoh.** 4:8. Sisi twampenda, kwa sababu yeye alitupenda sisi kwanza, **1 Yoh.** 4:19.

Kristo huteseka kwa sababu ya wema wa upendo wake kwa wanadamu, **1 Ne.** 19:9. Songeni mbele kwa upendo wa Mungu na wa wanadamu wote, **2 Ne.** 31:20. Mtawafundisha watoto wenu kupendana na kutumikiana, **Mos.** 4:15. Kama mmejisikia kuimba wimbo wa upendo wa ukombozi, mwaweza kujisikia hivyo hivi sasa, **Alma** 5:26. Mkaongozwe na Roho Mtakatifu,

katika kuwa wenye subira, waliojawa na upendo, **Alma** 13:28. Zuia tamaa zako zote, ili upate kujawa na upendo, **Alma** 38:12. Hapakuwa na ubishi kwa sababu ya upendo wa Mungu uliokaa katika mioyo ya watu, **4 Ne.** 1:15. Kila kitu kikaribishacho kumpenda Mungu kimeongozwa na Mungu, **Moro.** 7:13–16. Hisani ni upendo safi wa Kristo, **Moro.** 7:47. Pendo kamili huitupa nje hofu, **Moro.** 8:16 (1 Yoh. 4:18).

Upendo huwapasisha wanadamu katika kazi ya Mungu, **M&M** 4:5 (M&M 12:8). Utakaso huja kwa wale wote wenye kumpenda na kumtumikia Mungu, **M&M** 20:31. Kama wanipenda, utanitumikia na kushika amri zangu, **M&M** 42:29 (Yn. 14:15). Onyesha ongezeko la upendo kwa wale unaowasahihisha au kuwakemea, **M&M** 121:43.

Wanadamu walimpenda Shetani zaidi kuliko Mungu, **Musa** 5:13, 18, 28.

Upinde wa mvua. *Ona pia* Gharika katika Wakati wa Nuhu; Nuhu, Patriaki wa Biblia; Safina

Ishara au alama ya agano la Mungu na Nuhu (Mwa. 9:13–17). TJS, Mwanzo 9:21–25 (Kiambatisho) inaelezea kwamba agano hilo linajumuisha ahadi kwamba dunia kamwe haitafunikwa tena kwa gharika ya maji, kwamba Sayuni ya Henoko itarudi, na kwamba Bwana atakuja tena kuishi duniani.

Upinzani. *Ona* Shida

Upole. *Ona* Pole, Upole

Upotevu. *Ona* Wana wa Upotevu

Upuuzi. *Ona pia* Kusema uovu

Kuyachukulia bila uzito mambo matakatifu (M&M 84:54).

Watakatifu wasiwe na mawazo yasiyofaa, au vicheko vilivyokithiri, **M&M** 88:69. Acheni kiburi chote na upuuzi wenu wote, **M&M** 88:121.

Urais. *Ona* Urais wa Kwanza

Urais wa Kwanza. *Ona pia* Funguo za Ukuhani; Rais; Ufunuo

Rais wa Kanisa na Washauri wake. Wao ndiyo akidi ya makuhani wakuu watatu na husimamia Kanisa zima. Urais wa Kwanza hushikilia funguo zote za ukuhani.

Funguo za ufalme daima ni mali ya Urais wa Ukuhani Mkuu, **M&M** 81:2. Urais wa Ukuhani Mkuu unayo haki ya kutenda kazi katika ofisi zote, **M&M** 107:9, 22. Yeyote anipokeaye mimi hupokea Urais wa Kwanza, **M&M** 112:20, 30. Urais wa Kwanza utapokea ushauri [mafunuo] kwa ajili ya Kanisa zima, **M&M** 124:126.

Urejesho. *Ona* Fanywa Upya, Urejesho

Urejesho wa Injili. *Ona pia* Injili; Kipindi; Smith, Joseph, Mdogo; Ukengeufu

Ni kurejeshwa upya na Mungu kwa kweli na ibada za injili Yake miongoni mwa wanadamu duniani. Injili ya Yesu Kristo ilipotea duniani kwa njia ya ukengeufu uliotokea baada ya huduma ya Mitume wa Kristo duniani. Ukengeufu huo ulifanya uwepo umuhimu wa urejesho wa injili. Kwa njia ya maono, huduma za malaika, na mafunuo kwa wanadamu duniani, Mungu alirejesha injili. Urejesho ulianza na Joseph Smith Nabii (JS—H 1; M&M 128:20–21) na umeendelea hadi sasa kwa njia ya kazi za manabii wa Bwana wanaoishi.

Nyumba ya Bwana itawekwa imara juu ya milima, **Isa.** 2:2 (Mika 4:2; 2 Ne. 12:2). Mungu atafanya kazi ya ajabu na muujiza, **Isa.** 29:14 (2 Ne. 25:17–18; M&M 4:1). Mungu atausimamisha ufalme, ambao kamwe hautaangamizwa, **Dan.** 2:44.

Elia atakuja, na atarejesha vitu vyote, **Mt.** 17:11 (Mk. 9:12; M&M 77:14). Zitakuja nyakati za kufanywa upya vitu vyote, **Mdo.** 3:21 (M&M 27:6). Katika kipindi cha utimilifu wa nyakati, Mungu atavijumlisha katika kimoja vitu vyote,

Efe. 1:10. Nikaona malaika mwingine, akiwa na injili isiyo na mwisho ili awahubirie, **Ufu.** 14:6.

Utimilifu wa injili utawajia Wayunani, **1 Ne.** 15:13–18. Wayahudi watarejeshwa katika kanisa la kweli, **2 Ne.** 9:2. Katika siku za mwisho ukweli utakuja, **3 Ne.** 16:7.

Juu yenu ninyi ninawatunukia Ukuhani wa Haruni, **M&M** 13 (JS—H 1:69). Nimekabidhi funguo za ufalme kwa mara ya mwisho, **M&M** 27:6, 13–14 (M&M 128:19–21). Atakusanya pamoja makabila ya Israeli na kurejesha mambo yote, **M&M** 77:9. Funguo za kipindi hiki cha maongozi ya Mungu zimekabidhiwa, **M&M** 110:16 (M&M 65:2). Ukuhani umetolewa katika kipindi hiki cha maongozi ya Mungu cha utimilifu wa nyakati, **M&M** 112:30.

Niliona Viumbe wawili, **JS—H** 1:17. Nitaufunua kwenu ukuhani kwa mkono wa Eliya, **JS—H** 1:38 (Mal. 4:5–6).

Urimu na Thumimu. *Ona pia* Dera ya kifuani; Mwonaji

Vifaa vilivyotayarishwa na Mungu ili kumsaidia mtu katika kupata ufunuo na katika kutafsiri lugha. Katika lugha ya Kiebrania maneno haya yanamaanisha venye kutoa "nuru na ukamilifu." Urimu na Thumimu zinajumuisha mawe mawili yaliyowekwa katika pinde za fedha na wakati mwingine zilitumika pamoja na dera ya kifuani (M&M 17:1; JS—H 1:35, 42, 52). Dunia hii itakuwa Urimu na Thumimu kuu katika hali yake ya utakaso na isiyo kufa (M&M 130:6–9).

Wewe utie hizo Urimu na Thumimu katika dera ya kifuani ya hukumu, **Ku.** 28:30.

Kwa yeye ashindaye nitampa jiwe jeupe, **Ufu.** 2:17.

Kuna kitu ambacho kwa kutumia hapo aliweza kuangalia, na kutafsiri, **Mos.** 8:13. Mawe haya mawili nitakupa, **Eth.** 3:23–24, 28 (Eth. 4:5).

Joseph Smith alipokea mafunuo kupitia Urimu na Thumimu, M&M vichwa vya habari vya sehemu ya 6; 11; 14–16. Ulipewa uwezo wa kutafsiri kwa kutumia nyenzo ya Urimu na Thumimu, **M&M** 10:1. Mashahidi Watatu ilikuwa waone Urimu na Thumimu, ambavyo vilitolewa kwa kaka wa Yaredi juu ya mlima, **M&M** 17:1. Mahali ambapo Mungu huishi ni Urimu na Thumimu iliyo kuu. Jiwe jeupe litakuwa Urimu na Thumimu kwa kila mtu atakayepata, **M&M** 130:6–11.

Mimi, Ibrahimu, nilikuwa na Urimu na Thumimu, **Ibr.** 3:1, 4.

Uru

Katika Agano la Kale, Uru ya Wakaldayo ilikuwa ndiyo nyumbani halisi kwa Abramu (Mwa. 11:27–28, 31; 15:7; Neh. 9:7; Ibr. 2:1, 4).

Usafi wa Kimwili. *Ona pia* Kupenda anasa, Matamanio ya anasa; Uasherati; Uzinzi; Wema

Usafi wa maadili ya kujamiiana kwa wanaume na wanawake.

Yusufu alishinda vishawishi vya mke wa Potifa, **Mwa.** 39:7–21 (M&M 42:24; 59:6). Usizini, **Ku.** 20:14. Mwanamke mwema ni taji kwa mumewe, **Mit.** 12:4 (Mit. 31:10).

Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu, **1 Kor.** 6:18–19. Uwe kielelezo kwao katika usafi, **1 Tim.** 4:12.

Hakuna kitu kichafu kiwezacho kuishi na Mungu, **1 Ne.** 10:21. Kwani mimi, Bwana, hupendezwa katika usafi wa kimwili wa wanawake, **Yak. (KM)** 2:28. Dhambi ya ngono ni chukizo, **Alma** 39:1–13. Usafi wa kimwili na wema ni mambo yaliyo mazuri na thamani sana kupita yote, **Moro.** 9:9.

Tunaamini katika kuwa wasafi kimwili, **M ya I** 1:13.

Useja. *Ona* Ndoa, Oa, Olewa

Ushauri. *Ona pia* Nabii

Maonyo madogo, maonyo, ushauri, na mafundisho kutoka kwa Bwana na viongozi Wake aliowaweka.

Nitakupa shauri, **Ku.** 18:19. Mungu ataniongoza kwa shauri lake, **Zab.** 73:24. Pasipo ushauri kutolewa watu huanguka, **Mit.** 11:14.

Mafarisayo na wana-sheria walilipinga shauri la Mungu, **Lk.** 7:30.

Kuelimika ni vyema ikiwa watatii ushauri wa Mungu, **2 Ne.** 9:29.

Sikiliza ushauri wake yeye aliyekutawaza, **M&M** 78:2. Pokea ushauri wake yeye niliyemteua, **M&M** 108:1. Alitamani kuweka baraza lake badala ya baraza ambalo nimelitawaza, **M&M** 124:84. Sikilizeni ushauri wa mtumishi wangu Joseph, **M&M** 124:89. Kama mtu yeyote hatafuti ushauri wangu, hatakuwa na uwezo, **M&M** 136:19.

Ushindani. *Ona pia* Uasi

Mashindano, kubishana, na ugomvi. Ushindani, hususani kati ya waumini wa Kanisa la Bwana au kati ya wana familia, haimpendezi Bwana.

Usiwepo ugomvi kati ya mimi na wewe, **Mwa.** 13:8. Kiburi huleta ushindani, **Mit.** 13:10.

Kama mtu akiwa na sababu ya kumlaumu mwenzake, asamehe kama Kristo alivyowasamehe, **Kol.** 3:13. Jiepushe na maswali ya kipuuzi na magomvi, **Tit.** 3:9.

Bwana anawaamuru wanadamu wasibishane wao kwa wao, **2 Ne.** 26:32. Hamtawaacha watoto wenu wapigane na kuzozana wao kwa wao, **Mos.** 4:14. Alma aliamuru kwamba pasiwepo na ushindani miongoni mwa waumini wa Kanisa, **Mos.** 18:21. Shetani alisambaza uvumi na ushindani, **Hel.** 16:22. Ibilisi ndiye baba wa ushindani na huwachochea wanadamu kubishana wao kwa wao, **3 Ne.** 11:29 (Mos. 23:15).

Ihubirini injili yangu, ili pasiwepo na ushindani mwingi, **M&M** 10:62–64. Komeni kubishana ninyi kwa ninyi, **M&M** 136:23.

Ushirika. *Ona pia* Umoja; Upendo

Kwa Watakatifu wa Siku za Mwisho, ushirika ni pamoja na kutoa ushirikiano wa kirafiki, kuhudumiana, kuinuana, na kuwaimarisha wengine.

Mpende jirani yako kama nafsi yako, **Law.** 19:18 (Mt. 19:19; M&M 59:6).

Utakapoongoka, waimarishe ndugu zako, **Lk.** 22:32. Mmekuwa wanafunzi wangu mkiwa na upendo ninyi kwa ninyi, **Yn.** 13:35. Lisha kondoo wangu, **Yn.** 21:15–17. Waliomba kwamba tujichukulie juu yetu shirika hili la kuwahudumia Watakatifu, **2 Kor.** 8:1–5. Ushirika wetu ni pamoja na Baba, na pamoja na Mwanawe, **1 Yoh.** 1:3.

Wanefi na Walamani walishirikiana, **Hel.** 6:3.

Na kila mtu ampende ndugu yake kama vile ajipendavyo yeye mwenyeye, **M&M** 38:24–25. Kama ninyi si wamoja, si wangu, **M&M** 38:27. Ninakupokea katika shirika kuwa rafiki yako na ndugu yako, **M&M** 88:133.

Ushuhuda. *Ona pia* Roho Mtakatifu; Shahidi, Ushahidi; Shuhudia

Ufahamu na ushahidi wa kiroho unaotolewa na Roho Mtakatifu. Ushuhuda pia waweza kuwa tamko rasmi au la kisheria juu ya kile ambacho mtu hukiona kama kweli (M&M 102:26).

Najua kwamba Mkombozi wangu yu hai, **Ayu.** 19:25–26.

Usiuonee haya ushuhuda wa Bwana wetu, **2 Tim.** 1:8. Ushuhuda wa Yesu ni roho ya unabii, **Ufu.** 19:10.

Simameni kama mashahidi wa Mungu nyakati zote, **Mos.** 18:9. Hapakuwa na njia ya kuwaokoa watu isipokuwa kuwashawishi kwa ushuhuda halisi, **Alma** 4:19–20. Ninavyo vitu vyote kama ushahidi kwamba mambo haya ni ya kweli, **Alma** 30:41–44. Kwani hamtapata ushahidi wowote mpaka baada ya majaribu ya imani yenu, **Eth.** 12:6.

Je, sikusema amani akilini mwako? Ushahidi gani mkubwa unaoweza kupata kuliko ule utokao kwa Mungu, **M&M** 6:22–23. Na sasa, baada ya shuhuda nyingi zilizokwisha kutolewa juu yake, huu ni ushuhuda wa mwisho wa zote ambao tunatoa juu yake, **M&M**

76:22–24. Nimewatuma kwenda kushuhudia na kuonya watu, **M&M** 88:81–82. Mashahidi hawa sasa wamekufa, na ushuhuda wao bado una nguvu, **M&M** 135:4–5.

Henoko aliwaona malaika wakitoa ushuhuda juu ya Baba na Mwana, **Musa** 7:27. Ingawa nilichukiwa na kuteswa kwa kusema kwamba nimeona ono, lakini bado ilikuwa kweli, **JS—H** 1:24–25.

Ushujaa, enye Ushujaa. *Ona pia* Amini, Imani; Hofu

Kutoogopa, hususani katika kutenda kilicho chema.

Uwe hodari na mwenye moyo wa ushujaa, **Kum.** 31:6 (Yos. 1:6–7). Kuweni mashujaa sana kuyashika na kuyatenda yote yalioandikwa, **Yos.** 23:6.

Mungu hakutupa roho ya uoga, **2 Tim.** 1:7.

Moyo wake ulianza kupata ujasiri wakati aliposikia, **Alma** 15:4 (Alma 62:1). Wana wa Helamani walikuwa hodari kwa ushujaa, **Alma** 53:20–21. Kamwe sijapata kuona ushujaa mkuu jinsi hiyo, **Alma** 56:45.

Tuweni majasiri, ndugu, na twende mbele, mbele kwenye ushindi, **M&M** 128:22.

Usimamizi. *Ona* Msimamizi, Usimamizi

Usimikaji. *Ona pia* Ita, Itwa na Mungu, Wito; Mikono, Kuweka juu ya

Kuchaguliwa na kuwekwa wakfu kwa madhumuni yaliyo matakatifu. Uteuzi huu ni kwa utumishi maalumu ndani ya muundo wa Kanisa kwa kuwekewa mikono na mtu aliye na mamlaka sahihi. Wale tu wanaosimamia akidi za ukuhani hupokea funguo kutoka kwa kiongozi wa juu wanaposimikwa. Watu wanaosimikwa katika nafasi tofauti na marais wa akidi za ukuhani wanaweza kupokea baraka za ukuhani, lakini hakuna funguo wanazopewa pamoja na baraka ile.

Nitengeeni Barnaba na Sauli kwa ajili ya kazi ile, **Mdo.** 13:2–3.

Maaskofu wengine watengwe, **M&M** 68:14. Askofu, mwamuzi wa wote, asimikwe kwa huduma hii, **M&M** 107:17, 74.

Mwanadamu lazima aitwe na Mungu kwa unabii na kwa kuwekewa mikono ya, **M ya I** 1:5.

Usingizi

Hali ya pumziko ambapo mtu anakuwa hajishughulishi na hana fahamu. Bwana amewashauri Watakatifu Wake wasilale muda mrefu kuliko inavyohitajika (M&M 88:124). Usingizi waweza pia kuwa ishara ya mauti ya kiroho (1 Kor. 11:30; 2 Ne. 1:13) au kuwa mauti ya kimwili (Morm. 9:13).

Uso

Kwa ujumla ni uonekano wa uso wa mtu, ambao mara nyingi huakisi mtazamo wa kiroho na hali ya mawazo.

Nyuso zao za shuhudia juu yao, **Isa.** 3:9. Uso wa mfalme ukambadilika, na fikra zake zikamfadhaisha, **Dan.** 5:6.

Uso wake ulikuwa kama umeme, **Mt.** 28:3. Uso wake ulikuwa kama jua, **Ufu.** 1:16.

Je, mmepokea mfano wa Mungu katika nyuso zenu, **Alma** 5:14, 19. Amoni akaona uso wa mfalme ulibadilika, **Alma** 18:12.

Fungeni na msali kwa moyo wenye furaha na nyuso zilizo changamka, **M&M** 59:14–15. Uso wake ulingara kuliko mngaro wa jua, **M&M** 110:3.

Ustawi. *Ona pia* Funga, Kufunga; Maskini; Sadaka, Utoaji sadaka; Utumishi

Utaratibu na njia itumikayo kwa ajili ya kuwatunza watu kimahitaji ya kiroho na ya kimwili.

Mfumbulie mkono wako nduguyo, maskini wako, na kwa mhitaji wako katika nchi yako, **Kum.** 15:11. Mtu awapaye maskini hatapungukiwa, **Mit.** 28:27. Je, hii siyo funga niliyoichagua? kuwapa wenye njaa mkate, kuwaleta maskini nyumbani mwangu, **Isa.** 58:6–7.

Nalikuwa na njaa nawe ukanipa

chakula; nalikuwa mgeni nawe ulinikaribisha ndani. Wakati umtendeapo mmoja wa ndugu zangu wadogo hawa, umenitendea mimi, **Mt.** 25:35–40.

Mhudumieni kwa mali zenu yule mwenye shida, **Mos.** 4:16–26. Walipeana vitu vya kimwili na kiroho kulingana na shida na matakwa yao, **Mos.** 18:29. Waliamriwa kujiunga katika kufunga na kusali kwa ajili ya ustawi wa wale ambao hawakumjua Mungu, **Alma** 6:6. Sali kwa ajili ya ustawi wako na kwa ustawi wa wale wanaokuzunguka, **Alma** 34:27–28. Walikuwa na vitu vilivyo sawa miongoni mwao, **4 Ne.** 1:3.

Wakumbuke maskini, **M&M** 42:30–31. Watembelee maskini na wenye shida, **M&M** 44:6. Wakumbukeni katika mambo yote maskini na wenye shida, **M&M** 52:40. Ole wenu ninyi matajiri ambao hamtawapa maskini vitu vyenu, na ole wenu maskini ambao hamridhiki, na mlio wachoyo, na hamfanyi kazi, **M&M** 56:16–17.

Katika Sayuni hapakuwa na maskini miongoni mwao, **Musa** 7:18.

Utajiri. *Ona* Ukwasi

Utakaso. *Ona pia* Hesabu kwa haki, Kuhesabiwa haki; Lipia dhambi, Upatanisho; Yesu Kristo

Njia ya kuwa huru na dhambi, sio na doa, safi, na takatifu kwa njia ya upatanisho wa Yesu Kristo (Musa 6:59–60).

Mungu amewachagua mpate wokovu kwa njia ya utakaso na Roho, **2 The.** 2:13. Tumetakaswa kwa njia ya kutolewa kwa mwili wa Yesu, **Ebr.** 10:10. Yesu aliteseka ili apate kuwatakasa watu kwa damu yake mwenyewe, **Ebr.** 13:12.

Makuhani wakuu walitakaswa na mavazi yao yakaoshwa kuwa meupe kwa njia ya damu ya Mwanakondoo, **Alma** 13:10–12. Utakaso ambao huja kwa wale ambao huiachia mioyo yao kwa Mungu, **Hel.** 3:33–35. Tubuni ili mpate kutakaswa kwa kumpokea Roho Mtakatifu, **3 Ne.** 27:20.

Utakaso kupitia neema ya Yesu Kristo ni haki na kweli, **M&M** 20:31. Yesu alikuja kuutakasa ulimwengu, **M&M** 76:41. Jitakaseni ninyi wenyewe ili mawazo yenu yawe tu kwa Bwana, **M&M** 88:68.

Utakatifu. *Ona pia* Safi na Isiyo safi; Takatifu; Utakaso

Ukamilifu wa kiroho na kimwili. Utakatifu huonyesha usafi wa moyo na dhamiri ya mtu.

Waumini wataonyesha kuwa wenye kustahili katika Kanisa kwa kutembea katika utakatifu mbele za Bwana, **M&M** 20:69. Nyumba ya Bwana ni mahali pa utakatifu, **M&M** 109:13.

Mtu wa utakatifu ni mojawapo ya majina ya Mungu, **Musa** 6:57 (Musa 7:35).

Utambuzi, Kipawa cha. *Ona pia* Vipawa vya Roho

Kufahamu au kujua kitu fulani kwa njia ya uwezo wa Roho. Kipawa cha utambuzi ni moja ya vipawa vya Roho. Inajumuisha kutambulika kwa tabia za kweli za watu na chanzo na maana ya maonyesho ya kiroho.

Mwanadamu huitazama sura ya nje, bali Bwana huutazama moyo, **1 Sam.** 16:7. Ole wao waitao uovu kuwa ni wema, **Isa.** 5:20 (2 Ne. 15:20).

Mambo ya Mungu yatambulika kwa jinsi ya rohoni, **1 Kor.** 2:14. Kwa watu wengine kimetolewa kipawa cha utambizi wa roho, **1 Kor.** 12:10.

Amoni angeweza kutambua mawazo yake, **Alma** 18:18. Ile sauti ndogo tulivu iliwapenya wale walioisikia, **3 Ne.** 11:3.

Ili msipate kudanganyika, zitakeni karama zilizo bora, **M&M** 46:8, 23. Viongozi wa Kanisa hupewa uwezo wa kutambua vipawa vya Roho, **M&M** 46:27. Ule mwili uliojazwa na nuru hufahamu mambo yote, **M&M** 88:67.

Musa aliitazama dunia, na akaitambua kwa uwezo wa Roho wa Mungu, **Musa** 1:27.

Utaratibu

Mfano ambao mtu anaweza akafuata ili kupata matokeo fulani. Katika maandiko,

utaratibu kwa kawaida humaanisha mfano wowote kwa ajili ya kuishi njia fulani au kwa ajili ya kujenga kitu fulani.

Bwana aliwaamuru Israeli kujenga hema takatifu kulingana na utaratibu ulioonyeshwa kwa Musa, **Ku.** 25. Daudi alimpa Suleimani utaratibu wa ujenzi wa hekalu, **1 Nya.** 28:11–13.

Katika mimi Yesu Kristo apate kuonyesha mfano kwa wale watakaomwamini, **1 Tim.** 1:16.

Nitatoa kwenu utaratibu katika mambo yote, ili msidanganyike, **M&M** 52:14.

Utawala. *Ona pia* Katiba

Yesu Kristo atakaporudi, ataanzisha utawala wa haki.

Utawala utakuwa mabegani mwake, **Isa.** 9:6 (2 Ne. 19:6).

Mpeni Kaisari vitu vilivyo vya Kaisari, **Mt.** 22:21 (M&M 63:26). Itiini mamlaka ya juu, **Rum.** 13:1. Salini kwa ajili ya wafalme na wote walio katika mamlaka, **1 Tim.** 2:1–2. Wanyenyekeeni wenye himaya na mamlaka na kuwatii mahakimu, **Tit.** 3:1. Tiini kila sheria ya wanadamu kwa ajili ya Bwana, **1 Pet.** 2:13–14. Yesu Kristo atakuwa ndiye msimamizi wa mwisho wa dunia, **Ufu.** 11:15.

Wafanyeni watu wa haki wawe wafalme wenu, **Mos.** 23:8. Fanyeni mambo yenu kwa kura za watu, **Mos.** 29:26.

Kristo ajapo atakuwa mtawala wetu, **M&M** 41:4. Yule ashikaye amri za Mungu hahitaji kuvunja amri za nchi, **M&M** 58:21. Waovu watawalapo, watu huhuzunika, **M&M** 98:9–10. Tawala zimewekwa na Mungu kwa manufaa ya wanadamu, **M&M** 134:1–5. Watu wana lazimika kuzikubali na kuziunga mkono serikali, **M&M** 134:5.

Tunaamini katika kuwatii wafalme, marais, watawala na mahakimu, **M ya I** 1:12.

Uteuzi. *Ona pia* Wito na Uteuzi

Utegemeao ustahilivu kabla ya kuzaliwa, Mungu aliwachagua wale ambao wangekuwa wazao wa Ibrahimu na wa nyumba ya Israeli na kuwa watu wa agano (Kum. 32:7–9; Ibr. 2:9–11). Watu hawa wanapewa baraka maalumu na wajibu ili waweze kubariki mataifa yote ya ulimwengu (Rum. 11:5–7; 1 Pet. 1:2; Alma 13:1–5; M&M 84:99). Hata hivyo, hata hawa wateule ni lazima waitwe na kuteuliwa katika maisha haya ili wapate wokovu.

Uteuzi kabla. *Ona pia* Maisha kabla ya kuzaliwa

Uteuzi ufanywao na Mungu kwa watoto wake wa kiroho waliokuwa mahodari kabla ya kuzaliwa katika mwili ili kutimiza kazi fulani wakati wa maisha yao katika mwili wenye kufa.

Mungu aliweka mipaka ya watu, **Kum.** 32:8. Kabla sijakuumba katika tumbo, nilikuteua kabla wewe kuwa nabii, **Yer.** 1:5.

Mungu aliziamuru nyakati kabla ya kuwekwa, **Mdo.** 17:26. Maana wale aliowajua tangu asili, yeye pia aliwachagua tangu asili, **Rum.** 8:28–30. Yeye alituchagua sisi katika yeye kabla ya kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu, **Efe.** 1:3–4. Yesu Kristo aliteuliwa kabla kuwa Mkombozi, **1 Pet.** 1:19–20 (Ufu. 13:8).

Wao waliitwa na kutayarishwa tangu kuwekwa kwa misingi ya ulimwengu, **Alma** 13:1–9.

Niliwaangalia watu walio maarufu na wakuu ambao walichaguliwa mwanzoni, **M&M** 138:55–56.

Mwanangu Mpendwa alichaguliwa tangu mwanzo, **Musa** 4:2. Ibrahimu alichaguliwa kabla hajazaliwa, **Ibr.** 3:23.

Uthibitisho. *Ona pia* Mikono, Kuweka juu ya

Utii. *Ona* Mtiifu, Tii, Utii

Utoaji sadaka. *Ona* Sadaka, Utoaji sadaka

Utovu wa maadili ya kujamiiana. *Ona pia* Kupenda anasa, Matamanio ya anasa; Uasherati; Uzinzi

Kushiriki katika uzinzi kwa makusudi, uasherati, tabia za ubasha na

usagaji, kujamiiana kwa maharimu, au nyingine yoyote isiyo takatifu, isiyo ya kawaida, au mambo ya kujamiiana yasiyo safi.

Haya na tumnyweshe baba yetu mvinyo, na tukalale naye, **Mwa.** 19:30–36. Reubeni akaenda na akalala na Bilha suria wa baba yake, **Mwa.** 35:22 (Mwa. 49:4; 1 Nya. 5:1). Tabia za ubasha na utovu mwingine wa kujamiiana ni chukizo, **Law.** 18:22–23. Kama mwanamume atalazimisha mwanamke kulala naye, ni yule mwanamume tu ndiye aliye na hatia ya dhambi, **Kum.** 22:25–27.

Yeyote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amekwisha kuzini naye moyoni mwake, **Mt.** 5:28 (3 Ne. 12:28). Uasherati, uchafu, tamaa mbaya ndiyo ibada ya masanamu, **Kol.** 3:5. Katika siku za mwisho wanadamu watakuwa hawana upendo wa asili, **2 Tim.** 3:1–3.

Dhambi ya kujamiiana ni chukizo, **Alma** 39:3–5.

Utukufu. *Ona pia* Madaraja ya Utukufu; Nuru, Nuru ya Kristo; Ukweli

Katika maandiko, ni utukufu mara kwa mara umetajwa kuwa ni nuru na ukweli wa Mungu. Pia waweza kutajwa kuwa ni sifa au heshima na hali fulani ya uzima wa milele au ya utukufu wa Mungu.

Mtakatifu ni Bwana wa majeshi: dunia yote imejaa utukufu wake, **Isa.** 6:3 (2 Ne. 16:3).

Tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, **2 Kor.** 3:18.

Ataniinua juu ili niishi pamoja naye katika utukufu, **Alma** 36:28.

Tukufu tutakazopokelewa katika ufufuko zitatofautiana kulingana na haki, **M&M** 76:50–119. Utukufu wa Mungu ni akili, **M&M** 93:36.

Utukufu wa Mungu ni kutokufa maisha na uzima wa milele wa mwanadamu, **Musa** 1:39. Niliwaona Watu wawili, ambao uangavu na utukufu wao wapita maelezo yote, **JS—H** 1:17.

Utukufu wa Selestia. *Ona pia* Kuinuliwa; Madaraja ya Utukufu; Uzima wa Milele

Daraja la juu kabisa kati ya madaraja matatu ya utukufu ambalo mtu aweza kupata baada ya maisha haya. Hapa watu wenye haki wataishi katika uwepo wa Mungu Baba na Mwanawe Yesu Kristo.

Utukufu wa selestia ni mmoja, **1 Kor.** 15:40 (M&M 76:96). Paulo alinyakulwa katika mbingu ya tatu, **2 Kor.** 12:2.

Utukufu wa selestia ulionyeshwa katika ono, **M&M** 76:50–70. Kama Watakatifu wanataka kuwa na mahali katika ulimwengu wa selestia, ni lazima wajitayarishe, **M&M** 78:7. Yule asiye weza kutii sheria ya ufalme wa selestia hawezi kuishi katika utukufu wa selestia, **M&M** 88:15–22. Katika utukufu wa selestia kuna mbingu tatu; masharti yamewekwa kwa ajili ya kuufikia ule wa juu zaidi, **M&M** 131:1–2. Watoto wanaokufa kabla ya umri wa uwajibikaji wanaokolewa katika ufalme wa selestia, **M&M** 137:10.

Utukufu wa Telestia. *Ona pia* Madaraja ya Utukufu

Daraja la chini kabisa kati ya madaraja matatu ya utukufu ambamo ndani yake watu wataishi baada ya Hukumu ya Mwisho.

Paulo aliona utukufu wa nyota, **1 Kor.** 15:40–41.

Joseph Smith na Sidney Rigdon waliona utukufu wa telestia, **M&M** 76:81–90. Wakazi wa ulimwengu wa telestia walikuwa wengi pasipo idadi kama vile nyota, **M&M** 76:109–112. Mtu asiyeweza kustahmili sheria za ufalme wa telestia hawezi kustahmili utukufu wa telestia, **M&M** 88:24, 31, 38.

Utukufu wa Terestria. *Ona pia* Madaraja ya Utukufu

Daraja la pili kati ya madaraja matatu ya utukufu ambamo ndani yake watu wataishi baada ya Hukumu ya Mwisho.

Paulo aliona utukufu wa terestria,

ukilinganishwa na utukufu wa mwezi, **1 Kor.** 15:40–41.

Joseph Smith na Sydney Rigdon waliona utukufu wa terestria, **M&M** 76:71–80. Utukufu wa terestria unaupita ule wa telestia, **M&M** 76:91. Wale wasioweza kustahmili sheria ya ufalme wa terestria hawawezi kustahmili utukufu wa terestria, **M&M** 88:23, 30, 38.

Utumishi. *Ona pia* Upendo; Ustawi

Msaada uliotolewa au kazi iliyofanywa kwa manufaa ya Mungu na wengine. Tunapowatumikia wengine, tunamtumikia pia Mungu.

Chagueni hivi leo mtakayemtumikia, **Yos.** 24:15.

Kadiri mlivyomtendea mmoja wa wadogo hawa, mmenitendea mimi, **Mt.** 25:35–45. Itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, ambayo ndiyo utumishi wenu ulio na maana, **Rum.** 12:1. Tumikianeni kwa upendo, **Gal.** 5:13.

Siku zako zitatumika katika utumishi wa Mungu wako, **2 Ne.** 2:3. Wakati mkiwa katika utumishi wa viumbe wenzenu mnakuwa tu katika utumishi wa Mungu wenu, **Mos.** 2:17. Watu wanaoimiliki nchi ya ahadi lazima wamtumikie Mungu au watafagiliwa mbali, **Eth.** 2:8–12.

Wale wajiingizao katika utumishi wa Mungu yawapasa kutumikia kwa moyo wao wote, **M&M** 4:2. Bwana alitoa amri kwamba wanadamu yawapasa kumpenda na kumtumikia yeye, **M&M** 20:18–19. Katika jina la Yesu Kristo nawe utamtumikia Mungu, **M&M** 59:5. Mimi, Bwana, napenda kuwaheshimu wale wanaonitumikia, **M&M** 76:5.

Mwabudu Mungu, kwani ni yeye pekee utamtumikia, **Musa** 1:15.

Uumbaji. *Ona* Umba, Uumbaji

Uumbaji wa Kiroho. *Ona pia* Mwanadamu, Wanadamu; Umba, Uumbaji

Bwana aliumba vitu vyote kiroho kabla Yeye hajaviumba kimwili (Musa 3:5).

Bwana alifanya kila mmea kabla haujakuwepo katika dunia, **Mwa.** 2:4–6 (Ibr. 5:5).

Kwa uwezo wa Roho wangu niliviumba vitu vyote—kwanza kiroho, pili kimwili, **M&M** 29:31–32. Kila kilicho cha kimwili kiko kwa mfano wa kile kilicho cha kiroho, **M&M** 77:2.

Niliuumba ulimwengu na wanadamu kabla hawajawa katika mwili, **Musa** 6:51.

Uungu. *Ona* Mungu, Uungu

Uvivu. *Ona* Mvivu, Uvivu

Uvumi. *Ona* Kusema uovu; Sengenya

Shetani hueneza uvumi na magomvi—wakati mwingine hujengwa kwa sehemu fulani juu ya ukweli—ili kuwageuza watu dhidi ya Mungu na yote yaliyo mema (Hel. 16:22; JS—H 1:1). Moja ya ishara ya Ujio wa Pili wa Yesu Kristo ni kwamba watu watasikia juu ya vita na uvumi wa vita (Mt. 24:6; M&M 45:26; JS—M 1:23).

Uwajibikaji. *Ona* Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika

Uwajibikaji, Umri wa. *Ona* Batiza, Ubatizo—Ubatizo siyo kwa ajili ya watoto wachanga; Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika; Mtoto, Watoto; Ubatizo wa Watoto Wachanga

Uwezo. *Ona pia* Mamlaka; Ukuhani

Kuweza kufanya jambo fulani. Kuwa na uwezo juu ya mtu fulani au kitu fulani ni kuweza kudhibiti au kumwamuru mtu huyo au jambo hilo. Katika maandiko, uwezo daima unaunganishwa na nguvu za Mungu au nguvu za mbingu. Mara kwa mara huhusishwa kwa karibu na mamlaka ya ukuhani, ambayo ni ruhusa au haki ya kutenda jambo kwa niaba ya Mungu.

Kwa sababu hii nilikusimamisha wewe, ili kuonyesha katika wewe uwezo wangu, **Ku.** 9:16. Mungu ndiye nguvu na uwezo wangu, **2 Sam.** 22:33. Usiwanyime watu mema ikiwa katika

uwezo wa mkono wako kuyatenda, **Mit.** 3:27. Mimi hakika nimejaa nguvu kwa roho ya Bwana, **Mika** 3:8.

Nimepewa uwezo wote mbinguni na duniani, **Mt.** 28:18. Wakashangaa mno kwa mafundisho yake: kwa kuwa neno lake lilikuwa na uwezo, **Lk.** 4:32. Kaeni humu mjini, hadi mvikwe uwezo utokao juu, **Lk.** 24:49. Kadiri wengi walivyompokea, aliwapa uwezo wa kuwa wana wa Mungu, **Yn.** 1:12 (M&M 11:30). Mtapokea nguvu, baada ya kujiwa na Roho Mtakatifu, **Mdo.** 1:8. Hakuna nguvu isipokuwa imetoka kwa Mungu, **Rum.** 13:1. Mnalindwa kwa nguvu za Mungu kwa njia ya imani hata mpate wokovu, **1 Pet.** 1:3–5.

Nimejazwa na nguvu za Mungu, **1 Ne.** 17:48. Imedhihirishwa kwangu kwa nguvu za Roho Mtakatifu, **Yak. (KM)** 7:12. Mwanadamu anaweza kuwa na nguvu kuu alizopewa na Mungu, **Mos.** 8:16. Walifundisha kwa nguvu na mamlaka ya Mungu, **Alma** 17:2–3. Nefi alihudumu kwa nguvu na mamlaka kuu, **3 Ne.** 7:15–20 (3 Ne. 11:19–22).

Ingawa mwanadamu aweza kuwa na nguvu za kufanya kazi kubwa, kama akijidai katika nguvu zake mwenyewe lazima ataanguka, **M&M** 3:4. Nguvu za kufanya mema ziko ndani ya kila mtu, **M&M** 58:27–28. Katika ibada zifanywazo kwa Ukuhani wa Melkizedeki nguvu za uchamungu hujidhihirisha, **M&M** 84:19–22. Haki za ukuhani zimeungana na hazitenganishwi na nguvu za mbinguni, **M&M** 121:34–46.

Nitakuongoza kwa mkono wangu, na nguvu zangu zitakuwa juu yako, **Ibr.** 1:18.

Uzao wa Ibrahimu. *Ona* Ibrahimu—Uzao wa Ibrahimu

Uzima. *Ona pia* Nuru, Nuru ya Kristo; Uzima wa Milele

Kuishi kimwili na kiroho kulikowezeshwa kwa uwezo wa Mungu.

Nimekuwekea leo mbele yako uzima na mema, **Kum.** 30:15–20. Utanijulisha njia ya uzima, **Zab.** 16:11. Aandamaye haki anaona uzima, **Mit.** 21:21.

Mwenye kuuona uhai wake ataupoteza: naye aupotezaye uhai wake kwa ajili yangu, atauona, **Mt.** 10:39 (Mt. 16:25; Mk. 8:35; Lk. 9:24; 17:33). Mwana wa Mtu hakuja kuziangamiza roho za watu, bali kuziokoa, **Lk.** 9:56. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu, **Yn.** 1:4. Yeye amwaminiye aliyenipeleka amepita kutoka mautini kuingia uzimani, **Yn.** 5:24. Mimi ni njia, kweli, na uzima, **Yn.** 14:6. Kama katika maisha haya tu tumemtumaini Kristo, sisi tu maskini zaidi, **1 Kor.** 15:19–22. Uchamungu unayo ahadi ya uzima wa sasa, na ya ule utakaokuja baadaye, **1 Tim.** 4:8.

Watoto wetu wapate kutazamia ule uzima uliomo katika Kristo, **2 Ne.** 25:23–27. Maisha haya ndiyo wakati wa wanadamu kujitayarisha kukutana na Mungu, **Alma** 34:32 (Alma 12:24). Mimi ndimi nuru na uzima wa ulimwengu, **3 Ne.** 9:18 (Mos. 16:9; 3 Ne. 11:11; Eth. 4:12).

Heri wale walio waaminifu, katika uzima au katika mauti, **M&M** 50:5. Huu ndiyo uzawa wa milele—kumjua Mungu na Yesu Kristo, **M&M** 132:24.

Hii ndiyo kazi yangu na utukufu wangu—kuleta kutokufa na uzima wa milele wa mwanadamu, **Musa** 1:39.

Uzima Usio na Mwisho. *Ona* Uzima wa Milele

Uzima wa Milele. *Ona pia* Kuinuliwa; Lipia dhambi, Upatanisho; Taji; Utukufu wa Selestia; Uzima

Kuishi milele kama familia katika uwepo wa Mungu (M&M 132:19–20, 24, 55). Uzima wa milele ndiyo tuzo kuu zaidi ya Mungu kwa mwanadamu.

Wewe unayo maneno ya uzima wa milele, **Yn.** 6:68. Uzima wa milele ndiyo huu, kwamba wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo, **Yn.** 17:3 (M&M 132:24). Piga vita vile vizuri vya imani, shika uzima ule wa milele, **1 Tim.** 6:12.

Watu wako huru kuchagua uhuru na uzima wa milele, **2 Ne.** 2:27 (Hel. 14:31). Kujali mambo ya kiroho ndiyo uzima wa milele, **2 Ne.** 9:39. Ndipo ninyi mtakuwa katika ile njia nyembamba ile iongozayo katika uzima wa milele, **2 Ne.** 31:17–20. Kuamini katika Kristo na kustahimili hadi mwisho ndiyo uzima wa milele, **2 Ne.** 33:4 (3 Ne. 15:9).

Yeye aliye na uzima wa milele ndiye tajiri, **M&M** 6:7 (M&M 11:7). Uzima wa milele ndiyo zawadi ya Mungu iliyo kuu kupita zote, **M&M** 14:7 (Rum. 6:23). Wenye haki watapokea amani katika ulimwengu huu, na uzima wa milele katika ulimwengu ujao, **M&M** 59:23. Wale wastahimilio hadi mwisho watavikwa taji la uzima wa milele, **M&M** 66:12 (M&M 75:5). Wote wanaokufa pasipo injili ambao wangeipokea kama wangeliishi ni warithi wa ufalme wa selestia, **M&M** 137:7–9.

Kazi na utukufu wa Mungu ni kuleta kutokufa na uzima wa milele wa mwanadamu, **Musa** 1:39. Mungu hutoa uzima wa milele kwa walio watiifu, **Musa** 5:11.

Uzinzi. *Ona pia* Kupenda anasa, Matamanio ya anasa; Tabia ya Ubasha; Uasherati; Usafi wa Kimwili; Utovu wa maadili ya kujamiiana

Ushirikiano wa kingono usio wa kisheria kati ya wanaume na wanawake. Ingawa uzinzi kwa ujumla huelezea tendo la ngono kati ya mtu aliyeoa au kuolewa na mtu mwingine asiye mme au mke wake, katika maandiko pia yaweza kumaanisha kwa wasiooa au kuolewa.

Nyakati zingine uzinzi unatumika kama ishara ya uasi wa taifa au watu wote kutoka katika njia za Bwana (Hes. 25:1–3; Yer. 3:6–10; Eze. 16:15–59; Hos. 4).

Yusufu asingetenda uovu huu mkubwa, na kumtendea Mungu dhambi, **Mwa.** 39:7–12. Usizini, **Ku.** 20:14.

Kila mtu amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake, **Mt.** 5:28. Si washerati wala wazinzi wataurithi ufalme wa Mungu, **1 Kor.** 6:9–10. Mungu atawahukumu malaya na wazinzi, **Ebr.** 13:4.

Uzinzi ni chukizo lililo kuu kupita dhambi zote isipokuwa kumwaga damu isiyo na hatia au kumkana Roho Mtakatifu, **Alma** 39:3–5.

Atendaye uzinzi, na asitubu, atatupwa nje, **M&M** 42:23–26. Kama mtu yeyote atatenda uzinzi mioyoni mwao, hawatakuwa na Roho Mtakatifu, **M&M** 63:14–16.

Viongozi Wakuu. *Ona* Askofu Kiongozi; Mtume; Sabini; Urais wa Kwanza

Vipawa Vya Kiroho. *Ona* Vipawa vya Roho

Vipawa vya Roho. *Ona pia* Karama

Baraka maalumu zitolewazo na Bwana kwa watu wenye kustahili kwa manufaa yao wenyewe na kuvitumia kwa ajili ya kuwabariki wengine. Kwa maelezo juu ya vipawa vya Roho, jifunze Mafundisho na Maagano 46:11–33; 1 Wakorintho 12:1–12; Moroni 10:8–18.

Takeni kwa dhati karama zilizo bora, **1 Kor.** 12:31 (1 Kor. 14:1).

Wanefi walipewa vipawa vingi vya Roho, **Alma** 9:21. Ole wake asemaye Bwana hatendi kazi tena kwa vipawa au kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, **3 Ne.** 29:6. Mungu hutoa vipawa kwa walio waaminifu, **Morm.** 9:7. Vipawa huja kwa Roho wa Kristo, **Moro.** 10:17.

Kuna vipawa vingi na kwa kila mtu kimetolewa vipawa vya Roho, **M&M** 46:11. Viongozi wa Kanisa wanapewa uwezo wa kupambanua vipawa vya Roho, **M&M** 46:27. Rais wa Kanisa anavyo vipawa vyote ambavyo Mungu huviweka juu ya kichwa cha kiongozi wa Kanisa, **M&M** 107:91–92.

Vita. *Ona pia* Amani

Pambano, au ugomvi wa silaha; kupigana kwa silaha. Bwana hukemea vita isipokuwa tu kama ndiyo njia ya

mwisho kwa Watakatifu Wake ili kuzilinda familia zao, mali, haki, heshima na uhuru wao (Alma 43:9, 45–47).

Moroni alitafuta kuwalinda watu wake, haki zake, nchi yake, na dini yake, **Alma** 48:10–17.

Joseph Smith alipokea ufunuo na unabii juu ya vita, **M&M** 87. Kemeeni vita na tangazeni amani, **M&M** 98:16, 34–46. Tunaamini kwamba wanadamu huhesabiwa haki katika kujilinda wao wenyewe, marafiki zao, na mali, na serikali yao, **M&M** 134:11.

Tunaamini katika kutii, kuheshimu, na kuunga mkono sheria, **M ya I** 1:12.

Vita Mbinguni. *Ona pia* Baraza Mbinguni; Maisha kabla ya kuzaliwa

Ugomvi ambao ulitokea katika maisha kabla ya kuzaliwa miongoni mwa watoto wa kiroho wa Mungu.

Shetani alifukuzwa kutoka mbinguni na akaingia duniani, **Ufu.** 12:4, 7–9.

Ibilisi na theluthi moja ya majeshi ya mbinguni wakatupwa chini, **M&M** 29:36–37. Lusiferi aliasi dhidi ya Mwana wa Pekee, **M&M** 76:25–26.

Shetani alitaka utukufu wa Baba na kuangamiza haki ya mwanadamu kujiamulia, **Musa** 4:1–4 (Isa. 14:12–15; Ibr. 3:27–28). Wale waliomfuata Mungu walitunza hali yao ya kwanza, wakaja duniani, nao wakapokea miili, **Ibr.** 3:26.

Vitabu Vitakatifu. *Ona* Kanoni

Vitabu Vya Maandiko Vilivyopotea. *Ona* Maandiko—Maandiko yaliyopotea

Viumbe-Akili-Asilia. *Ona* Akili, Viumbe-akili-asilia

Viumbe waliobadilishwa

Watu waliobadilishwa ili wao wasionje maumivu au mauti hadi ufufuko wao katika mwili usiokufa.

Henoko akaenda pamoja na Mungu; naye akatoweka; maana Mungu alimtwaa, **Mwa.** 5:24 (Ebr. 11:5; M&M 107:48–49). Hakuna mtu ajuaye juu ya kaburi la Musa hata leo, **Kum.** 34:5–6 (Alma 45:19). Eliya alipanda mbinguni kwa upepo wa kisulisuli, **2 Fal.** 2:11.

Kama ninataka huyu akae hata nijapo, imekupasaje, **Yn.** 21:22–23 (M&M 7:1–3).

Hutaonja mauti kamwe, **3 Ne.** 28:7. Ili wasipate kuonja mauti kulikuwa na mabadiliko yaliyofanyika juu ya miili yao, **3 Ne.** 28:38 (4 Ne. 1:14; Morm. 8:10–11).

Yohana Kipenzi ataishi hadi Bwana atakapokuja, **M&M** 7. Nimeichukua Sayuni ya Henoko kifuani pangu mwenyewe, **M&M** 38:4 (Musa 7:21, 31, 69). Henoko na nduguze ndiyo mji uliohifadhiwa hadi siku ya haki, **M&M** 45:11–12. Eliya alitwaliwa mbinguni pasipo kuonja mauti, **M&M** 110:13.

Roho Mtakatifu alishuka juu ya wengi, nao wakanyakuliwa katika Sayuni, **Musa** 7:27.

Waamaleki (Agano la Kale)

Kabila la Waarabu ambao waliishi katika jangwa la Parani kati ya Araba na Meditarania. Daima walikuwa vitani na Waebrania kutoka wakati wa Musa (Ku. 17:8) hadi wakati wa Sauli na Daudi (1 Sam. 15; 27:8; 30; 2 Sam. 8:11–12).

Waamaleki (Kitabu cha Mormoni)

Kundi la Wanefi wakengeufu waliowaongoza Walamani katika vita dhidi ya Wanefi (Alma 21–24; 43).

Waamlisi. *Ona* Amlisi, Waamlisi

Waamuzi, Kitabu Cha

Kitabu katika Agano la Kale. Kitabu cha Waamuzi kinajishughulisha na Waisraeli kutoka kifo cha Yoshua hadi kuzaliwa kwa Samweli.

Mlango wa 1–3 ni utangulizi wa kitabu chote cha Waamuzi. Inaelezea kwamba kwa sababu Waisraeli hawakuwafukuza maadui zao (Amu. 1:16–35), Waisraeli lazima wapatwe

na matokeo yake; kukosa imani, kufunga ndoa na wasioamini, na ibada za sanamu. Mlango wa 4–5 inahusu matukio ya Debora na Baraka, walioikomboa Israeli kutoka kwa Wakanaani. Mlango wa 6–8 ni matukio ya Gideoni yenye kukuza imani, ambaye Mungu alimbariki ili aikomboe Israeli kutoka kwa Wamidiani. Katika mlango wa 9–12, watu kadhaa tofauti wanatumika kama waamuzi katika Israeli, katika wakati ambao Waisraeli wengi walikuwa katika ukengeufu na wkitawaliwa na watawala wageni. Mlango wa 13–16 inasimulia juu ya kuinuka na kuanguka kwa mwamuzi wa mwisho, Samsoni. Milango ya mwisho, 17–21, inaweza kuelezewa kama ni kiambatisho ambacho kinafichua kina cha dhambi za Israeli.

Waanti-Nefi-Lehi. *Ona pia* Amoni, Mwana wa Mosia; Helamani, Wana wa; Mosia, Wana wa

Katika Kitabu cha Mormoni, ni jina lililotolewa kwa Walamani walioongolewa na wana wa Mosia. Baada ya wongofu wao, watu hawa, ambao pia waliitwa watu wa Amoni, waliendelea kuwa waaminifu katika maisha yao yote (Alma 23:4–7, 16–17; 27:20–27).

Walichukua jina la Waanti-Nefi-Lehi, **Alma** 23:16–17; 24:1. Walikataa kumwaga damu na wakazika silaha zao, **Alma** 24:6–19. Watoto wao wa kiume walijiandaa kwa vita nao wakamchagua Helamani kama kiongozi wao, **Alma** 53:16–19; 56–58 (wana hawa pia walijulikana kama askari wa vita vijana 2,000).

Waebrania, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo

Kitabu katika Agano Jipya. Paulo aliandika barua hii kwa waumini wa Kanisa wa Kiyahudi ili kuwahimiza kwamba sehemu muhimu za sheria ya Musa zimetimia katika Kristo na kwamba sheria ya juu kabisa ya injili imekuja badala yake. Paulo aliporudi Yerusalemu mwishoni mwa safari yake ya tatu ya kuhubiri (karibu mwaka 60 B.K.), alikuta kwamba waumini wa Kanisa wa Kiyahudi wengi walikuwa bado wakiishi kwa sheria ya Musa (Mdo. 21:20). Hii ilikuwa karibu miaka kumi baada ya mkutano wa Kanisa huko Yerusalemu uliokuwa umeazimia kwamba baadhi ya ibada za sheria ya Musa hazikuwa muhimu kwa wokovu wa Wakristo wayunani. Ni dhahiri, mara baada ya hapo, Paulo aliwaandikia Waebrania ili kuwaonyesha andiko lao wenyewe na kwa nguvu ya hoja ya kwa nini wao hawapaswi tena kutenda sheria ya Musa.

Mlango wa 1 na 2 inaeleza kwamba Yesu ni mkuu kuliko malaika. Mlango wa 3–7 inamlinganisha Yesu na Musa na kwa sheria ya Musa na inashuhudia kwamba Yeye ni mkuu kuliko wote. Pia hufundisha kwamba Ukuhani wa Melkizedeki ni mkuu kuliko wa Haruni. Mlango wa 8–9 inaelezea namna ibada za sheria za Musa zilivyokuwa zikiwaandaa watu kwa ajili ya huduma ya Kristo na namna Kristo alivyo mpatanishi wa agano jipya (Alma 37:38–45; M&M 84:21–24). Mlango wa 10 unahimiza bidii na uaminifu. Mlango wa 11 ni mafundisho juu ya imani. Mlango wa 12 unatoa maonyo na salamu. Mlango wa 13 unafundisha juu ya tabia ya kuheshimiwa kwa ndoa na umuhimu wa utiifu.

Waefeso, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo

Katika Agano Jipya ni waraka ulioandikwa na Mtume Paulo kwa Watakatifu wa Efeso. Waraka huu una umuhimu mkubwa, kwani unayo mafundisho ya Paulo juu ya Kanisa la Kristo.

Mlango wa 1 una salamu ya kawaida. Mlango wa 2–3 inaelezea mabadiliko ambayo hutokea ndani ya watu wakati wanapokuwa wanachama wa Kanisa—wanakuwa washirika pamoja na Watakatifu, pamoja na Wayunani na Wayahudi wakiwa wameungana katika Kanisa moja. Mlango wa 4–6 inaelezea nafasi ya Mitume na manabii umuhimu wa umoja, na umuhimu wa kuvaa deraya zote za Mungu.

Wafalme

Vitabu viwili katika Agano la Kale. Vitabu hivi vinasimulia historia ya Israeli kuanzia uasi wa Adoniya, mwana wa nne wa mfalme Daudi (karibu mwaka 1015 K.K.), hadi utumwa wa mwisho wa Yuda (karibu mwaka 586 K.K.). Ni pamoja na historia nzima ya ufalme wa kaskazini (makabila kumi ya Israeli) tangu kutengana kwao hadi Waashuru walipowachukua mateka katika nchi za kaskazini. Ona pia Wendo katika kiambatisho.

Wafalme wa Kwanza: Mlango wa 1 unaelezea siku za mwisho za maisha ya Mfalme Daudi. Mlango wa 2–11 ni juu ya maisha ya Sulemani. Mlango wa 12–16 inazungumzia juu ya warithi wa karibu wa Sulemani, Rehoboamu na Yeroboamu. Yeroboamu alisababisha mgawanyiko wa ufalme wa Israeli. Wafalme wengine pia wametajwa. Mlango wa 17–21 inaelezea sehemu ya huduma ya Eliya kama alivyomwonya Ahabu, mfame wa Israeli. Mlango wa 22 ni juu ya vita dhidi ya Shamu ambayo Ahabu na Yehoshafati, mfalme wa Yuda, alishiriki. Nabii Mika alitoa unabii dhidi ya wafalme hawa.

Wafalme wa Pili: Mlango 1:1–2:11 inaendeleza juu ya maisha ya Eliya, ikiwa pamoja na Eliya kutwaliwa mbinguni katika gari ya kukokotwa na farasi wa moto. Mlango 2–9 ni juu ya huduma ya Eliya ya imani na uwezo mkuu. Mlango 10 unaelezea juu ya Yehu, mfalme, na namna alivyoiangamiza nyumba ya Ahabu na makuhani wa Baali. Mlango 1–13 ni juu ya utawala wa haki ya Yehoashi na kifo cha Elisha. Mlango 14–17 inaeleza juu ya wafalme mbalimbali waliotawala katika Israeli na Yuda, mara kwa mara katika uovu. Mlango 15 unaandikwa juu ya Waashuru kuyateka makabila kumi ya Israeli. Mlango 18–20 inaandikwa juu ya maisha ya haki ya Hezekia, mfalme wa Yuda, na nabii Isaya. Mlango 21–23 inasimulia juu ya wafalme Manase na Yosia. Kulingana na mapokeo, Manase ndiye anayewajibika kwa mauaji ya mfiadini ya Isaya. Yosia alikuwa mfalme mwaminifu aliyeianzisha tena sheria miongoni mwa Wayahudi. Mlango 24–25 inaandika juu ya utumwa katika Babeli.

Wafilipi, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo

Barua ambayo Paulo aliwaandikia Watakatifu wa Filipi wakati alipokuwa gerezani Roma kwa mara ya kwanza. Sasa ni kitabu cha Wafilipi katika Agano Jipya.

Mlango wa 1 una salamu za Paulo na mafundisho yake juu ya umoja, unyenyekevu, na uvumilivu. Mlango wa 2 unasisitiza kwamba wote watainama kwa Kristo na kila mtu lazima autafute wokovu wake mwenyewe. Katika Mlango wa 3, Paulo anasema kwamba yeye amejitolea dhabihu mambo yote kwa ajili ya Kristo. Katika Mlango wa 4, Paulo anawashukuru Watakatifu wa Filipi kwa msaada wao.

Wafilisti

Katika Agano la Kale, ni kabila ambalo kwa asili lilikuja kutoka Kaftari (Amo. 9:7) na wakakaa katika bonde tajiri juu ya pwani ya Mediterania kuanzia Yafa hadi jangwa la Misri kabla ya siku za Ibrahimu (Mwa. 21:32). Kwa miaka mingi palikuwepo vita vya kijeshi kati ya Wafilisti na Waisraeli. Hatimaye Palestina, jina la dola ya Wafilisti, limekuwa jina maarufu kwa Nchi yote Takatifu.

Israeli walikuwa katika utumwa kwa Wafilisti kwa miaka arobaini, **Amu.** 13:1. Samsoni alipigana na Wafilisti, **Amu.** 13–16. Goliati alikuwa Mfilisti wa Gathi, **1 Sam.** 17. Daudi aliwashinda Wafilisti, **1 Sam.** 19:8.

Wafu, Wokovu kwa Ajili ya. *Ona* Wokovu kwa ajili ya Wafu

Wagalatia, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo

Kitabu katika Agano Jipya. Mwanzoni ilikuwa ni barua ambayo Mtume Paulo

aliwaandikia Watakatifu waliokuwa wakiishi Galatia. Mada ya barua hii ni kwamba uhuru wa kweli unaweza kupatikana tu katika kuishi kulingana na injili ya Yesu Kristo. Kama Watakatifu wangeyachukua na kuishi kulingana na mafundisho ya Wakristo wa Kiyahudi ambao walisisitiza juu ya kuziangalia torati ya Musa, wangelijizuia au kuharibu uhuru walioupata katika Kristo. Katika waraka Paulo alielezea nafasi yake yeye mwenyewe kama Mtume, alielezea mafundisho ya haki kwa njia ya imani, na akathibitisha thamani ya dini ya kiroho.

Katika mlango wa 1 na wa 2, Paulo alihuzunishwa na habari aliyoipokea juu ya ukengeufu miongoni mwa Wagalatia na akaelezea kwa ufasaha nafasi yake miongoni mwa Mitume. Mlango wa 3 na wa 4 inajadili mafundisho ya imani na matendo. Mlango wa 5 na wa 6 ina mahubiri juu ya matokeo yanayoweza kutendeka ya mafundisho ya imani.

Wajibika. *Ona* Kuwajibika, Uwajibikaji, Wajibika

Wajibu. *Ona pia* Mtiifu, Tii, Utii

Katika maandiko, ni kazi ya kufanya, kazi iliyopangwa, au jukumu mara nyingi hutolewa na Bwana au na watumishi Wake.

Uzishike amri zake, maana kwa jumla ndiyo wajibu wa mwanadamu, **Mh.** 12:13. Bwana anataka nini kwako, ila kutenda haki, **Mika** 6:8.

Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu, **Mdo.** 5:29.

Walipigwa kwa mateso ili kuwashtua katika kumbukumbu ya wajibu wao, **Mos.** 1:17.

Wajibu wa wazee, makuhani, walimu, na mashemasi umeelezwa, **M&M** 20:38–67. Wenye ukuhani watashughulika na kazi zote za familia, **M&M** 20:47, 51. Wajibu wa wanachama baada ya ubatizo waelezwa, **M&M** 20:68–69. Wazee wangu yawapasa kusubiri kwa muda mfupi ili watu wangu wapate kujua kiukamilifu zaidi juu ya wajibu wao, **M&M** 105:9–10. Kila mtu na ajifunze wajibu wake, **M&M** 107:99–100.

Wakolosai, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo

Kitabu katika Agano Jipya. Kwa asili ilikuwa ni barua ambayo Mtume Paulo aliiandika kwenda kwa Wakolosai baada ya kutembelewa na Epafra, mwinjilisti wa Kanisa katika Kolosai (Kol. 1:7–8). Epafra alimwambia Paulo ya kuwa Wakolosai wanaingia katika kosa lililo kubwa—walijidhania ya kuwa wao ni bora zaidi kuliko watu wengine kwa sababu wao walikuwa waangalifu sana juu ya ibada fulani za kimwili (Kol. 2:16), wakijizuia matakwa fulani ya kimwili, na wakiabudu malaika (Kol. 2:18). Matendo haya yaliwafanya Wakolosai wajisikie kuwa walikuwa wakitakaswa. Wao pia walidhani kuwa walikuwa wakielewa siri za ulimwengu vizuri zaidi kuliko waumini wengine wa Kanisa. Katika barua yake, Paulo aliwasahihisha kwa kuwafundisha kwamba ukombozi waja tu kupitia Kristo na ya kwamba tuwe na hekima na kumtumikia.

Mlango wa 1 ni salamu za Paulo kwa Wakolosai. Mlango wa 2–3 ni ya mafundisho na zina maelezo juu ya Kristo kama ndiye Mkombozi, hatari ya ibada za uongo, na umuhimu wa Ufufuko. Mlango wa 4 unafundisha kwamba Watakatifu wawe na hekima katika mambo yote.

Wakorintho, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo

Vitabu viwili vilivyoko katika Agano Jipya. Mwanzoni zilikuwa ni barua ambazo Paulo aliwaandikia Watakatifu katika Korintho ili kusahihisha mvurugano miongoni mwao. Wakorintho waliishi katika jumuiya ambayo ilikuwa ovu kimaadili.

Wakorintho wa Kwanza: Mlango wa 1 una salamu za Paulo na maonyo yake madogo kwa watakatifu kuungana Mlango wa 2–6 ni masahihisho ya Paulo juu

ya makosa ya Watakatifu wa Korintho. Mlango wa 7–12 ni majibu ya Paulo ya maulizo aliyoulizwa. Mlango wa 13–15 ni mambo yahusuyo hisani, vipawa vya kiroho, na Ufufuko. Mlango wa 16 una maonyo ya Paulo juu ya kusimama imara katika imani.

Wakorintho wa Pili: Mlango wa 1 una salamu za Paulo na ujumbe wa kufariji. Mlango wa 2 una ushauri binafsi kwa Tito. Mlango wa 3–7 inahusu uwezo wa injili katika maisha ya Watakatifu na viongozi wao. Mlango wa 8–9 inawaasa Watakatifu kuwa watoaji wenye moyo wa furaha kwa maskini. Mlango wa 10–12 ni maelekezo ya Paulo mwenye nafasi yake kama Mtume. Mlango wa 13 ni maonyo ya kuwa wakamilifu.

Wakristo. *Ona pia* Mtakatifu; Mwanafunzi

Jina lililotolewa kwa waumini wa Yesu Kristo. Ingawa neno hili hutumika sana kote ulimwenguni, Bwana huwaita wafuasi wa kweli wa Kristo kama Watakatifu. (Mdo. 9:13, 32, 41; 1 Kor. 1:2; M&M 115:4).

Wanafunzi wa Yesu walikuwa wakiitwa Wakristo, **Mdo.** 11:26. Kama mtu yeyote anateseka kama Mkristo, na asione haya, **1 Pet.** 4:16.

Kwa sababu ya agano mtaitwa watoto wa Kristo, **Mos.** 5:7. Waamini wa kweli waliitwa Wakristo na wale ambao hawakuwa waumini wa Kanisa, **Alma** 46:13–16.

Walamani. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni; Lamani; Wanefi

Kikundi cha watu katika Kitabu cha Mormoni, wengi wao wakiwa ni wazao wa Lamani, mwana mkubwa wa Lehi. Walijiona kuwa walikuwa wametendewa makosa na Nefi na wazao wake (Mos. 10:11–17). Kama matokeo yake, wakawaasi Wanefi na mara kwa mara walikataa mafundisho ya injili. Hata hivyo, muda mfupi kabla ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo, Walamani waliikubali injili nao wakawa watu wema zaidi kuliko Wanefi (Hel. 6:34–36). Miaka mia mbili baada ya Kristo kuitembelea Marekani, wote Walamani na Wanefi wakawa waovu na wakaanza kupigana vita baina yao. Karibia mwaka 400 B.K., Walamani waliliangamiza kabisa taifa la Wanefi.

Walamani wakawashinda wazao wa Nefi, **1 Ne.** 12:19–20. Walamani waliwachukia Wanefi, **2 Ne.** 5:14. Walamani watakuwa mjeledi kwa Wanefi, **2 Ne.** 5:25. Kitabu cha Mormoni kitarejesha kwa Walamani ufahamu wao juu ya mababu zao na juu ya injili ya Yesu Kristo, **2 Ne.** 30:3–6 (Ukurasa wa jina la Kitabu cha Mormoni).

Walamani ni mabaki la Wayahudi, **M&M** 19:27. Walamani watachanua kama ua la waridi kabla ya ujio wa Bwana, **M&M** 49:24.

Walawi. *Ona pia* Torati

Kitabu katika Agano la Kale ambacho kinasimulia juu ya kazi za kikuhani katika Israeli. Kinasisitiza utukufu wa Mungu na kanuni ambazo kwazo watu Wake wangeliweza kuishi na kuwa watakatifu. Madhumuni yake ni kufundisha kanuni za tabia njema na kweli za dini za torati ya Musa kwa njia ya ibada. Musa ndiye aliyeandika Kitabu cha Walawi.

Mlango wa 1–7 inaelezea ibada za dhabihu. Mlango wa 8–10 inaelezea ibada iliyofanywa katika kuwaweka wakfu makuhani. Mlango wa 11 unaelezea ni nini kinachoweza au kisichoweza kuliwa na kipi kilicho safi au kisicho safi. Mlango wa 12 unajadili wanawake baada ya kuzaa. Mlango wa 13–15 ni sheria zinazohusu uchafu katika sherehe safi. Mlango wa 16 una ibada inayotakiwa kufanywa katika Siku ya Upatanisho. Mlango wa 17–26 ina mkusanyiko wa kanuni za sheria zinazoshughulikia sherehe za kidini na kijamii. Mlango wa 27 unaelezea kwamba Bwana aliiamuru Israeli kuweka wakfu nafaka zao, kondoo na ng'ombe wao kwa Bwana.

Walinzi. *Ona* Kesha, Walinzi

Wamormoni. *Ona pia* Kanisa la Yesu Kristo; Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho

Jina la utani la Mormoni liliundwa na watu ambao hawakuwa waumini wa Kanisa ili kuwataja waumini wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Jina hili linatokana na kitabu kitakatifu cha maandiko yaliyokusanywa na nabii wa kale Mormoni na kuitwa Kitabu cha Mormoni. Jina lililotolewa na Bwana ambalo kwalo waumini wa Kanisa wanajulikana ni "Watakatifu." Jina sahihi la Kanisa ni Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho.

Wana na Mabinti za Mungu. *Ona pia* Lipia dhambi, Upatanisho; Mwanadamu, Wanadamu; Watoto wa Kristo; Zaliwa; Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena

Maandiko hutumia maneno haya katika njia mbili. Katika maana moja, sisi wote ni watoto halisi wa kiroho wa Baba wa Mbinguni. Katika maana nyingine, wana na mabinti za Mungu ni wale waliozaliwa tena kwa njia ya Upatanisho wa Kristo.

Watoto wa kiroho wa Baba: Ninyi ndinyi miungu, watoto wa Aliye Juu Sana, **Zab.** 82:6.

Sisi wazao wa Mungu, **Mdo.** 17:29. Tujitie chini ya Baba wa roho, **Ebr.** 12:9.

Mimi ni mwana wa Mungu, **Musa** 1:13.

Watoto waliozaliwa tena kupitia Upatanisho: Kadiri wengi walivyompokea aliwapa uwezo wa kuwa wana wa Mungu, **Yn.** 1:12 (Rum. 8:14; 3 Ne. 9:17; M&M 11:30). Sasa tu wana wa Mungu, **1 Yoh.** 3:1–2.

Mtaitwa watoto wa Kristo, wana na mabinti zake, **Mos.** 5:7. Watu wote ni lazima wazaliwe tena, ili kuwa wana na mabinti zake, **Mos.** 27:25. Watakuwa wana wangu na mabinti zangu, **Eth.** 3:14. Wewe hakika utafanyika mtoto wa Kristo, **Moro.** 7:19.

Wale wote wenye kuipokea injili yangu ni wana na mabinti, **M&M** 25:1. Wao ni miungu, hata wana wa Mungu, **M&M** 76:58.

Hivyo wote wapate kufanyika wana wangu, **Musa** 6:68. Wengi wameamini na wamekuwa wana wa Mungu, **Musa** 7:1.

Wana wa Helamani. *Ona* Helamani, Wana wa

Wana wa Israeli. *Ona* Israeli

Wana wa Mosia. *Ona* Mosia, Wana wa

Wana wa Upotevu. *Ona pia* Dhambi isiyo sameheka; Hukumu; Ibilisi; Jehanamu; Mauti ya Kiroho

Wafuasi wa Shetani watakaoteseka pamoja naye milele. Wana wa upotevu ni pamoja na (1) wale waliomfuata Shetani na wakafukuzwa kutoka mbinguni kwa ajili ya uasi katika maisha kabla ya kuwa duniani na (2) wale walioruhusiwa kuzaliwa katika ulimwengu huu wakiwa na miili lakini halafu wakamtumikia Shetani na wakamgeuka kabisa Mungu. Wale walio katika kundi hili la pili watafufuka kutoka kwa wafu lakini hawatakombolewa kutokana na mauti ya pili (kiroho) na hawataweza kukaa katika ufalme wa utukufu (M&M 88:32, 35).

Wala hapana mmoja wao aliyepotea ila yule mwana wa upotevu, **Yn.** 17:12. Haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu, **Ebr.** 6:4–6 (Ebr. 10:26–29).

Rehema haina madai juu ya mtu huyo na hukumu yake ya mwisho ni mateso ambayo kamwe hayana mwisho, **Mos.** 2:36–39. Yeye yuko kama kwamba hapakuwa na ukombozi uliofanyika, **Mos.** 16:5. Wale wanaokataa miujiza ya Kristo ili kujinufaisha watakuwa kama wana wa upotevu, **3 Ne.** 29:7.

Hawatapokea msamaha katika ulimwengu huu au ujao, **M&M** 76:30–34 (M&M 84:41; 132:27). Wao ndiyo pekee ambao hawatakombolewa kutoka katika mauti ya pili, **M&M** 76:34–48. Wana wa

upotevu humkana Roho Mtakatifu baada ya kumpokea, **M&M** 76:35. Wana wa upotevu humkana Mwana baada ya Baba kuwa amekwisha mfunua, **M&M** 76:43.

Kaini ataitwa Upotevu, **Musa** 5:22–26.

Wanadamu. *Ona* Mwanadamu, Wanadamu

Wanafunzi Wanefi. *Ona* Wanafunzi Watatu wa Kinefi

Wanafunzi Watatu wa Kinefi. *Ona pia* Mwanafunzi; Viumbe waliobadilishwa; Wanefi

Watatu kati ya wanafunzi wa Kinefi waliochaguliwa na Kristo waliotajwa katika Kitabu cha Mormoni.

Bwana aliwapa wanafunzi hawa baraka ile ile aliyompatia Yohana Kipenzi—kwamba wapate kubaki duniani ili kuzileta Roho kwa Kristo hadi Bwana atakapokuja tena. Wao walibadilishwa ili wasife ili wasisikie maumivu na wasife (3 Ne. 28).

Kristo aliwapa wanafunzi wale watatu hamu yao ya kukaa hadi kuja kwake, **3 Ne.** 28:1–9. Hawatapata kamwe uchungu wa mauti au majonzi, **3 Ne.** 28:7–9. Watapata utimilifu wa shangwe, **3 Ne.** 28:10. Kwa muda walitwaliwa mbinguni, **3 Ne.** 28:13–17. Walihudumu kwa watu na kuvumilia mateso, **3 Ne.** 28:18–23. Walimhudumia Mormoni, **3 Ne.** 28:24–26 (Morm. 8:10–11). Watahudumu kwa Wayunani, Wayahudi, makabila yaliyotawanyika, na mataifa yote, **3 Ne.** 28:27–29. Shetani hana uwezo juu yao, **3 Ne.** 28:39.

Wanawake. *Ona* Mwanamke, Wanawake

Wanefi. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni; Nefi, Mwana wa Lehi; Walamani

Kikundi cha watu katika Kitabu cha Mormoni, wengi wao wakiwa ni wazao wa nabii Nefi, mwana wa Lehi. Walijitenga na Walamani na kwa ujumla walikuwa waadilifu zaidi kuliko Walamani. Hata hivyo, mwishowe waliangamizwa na Walamani kwa sababu ya uovu.

Wanefi walijitenga na Walamani, **2 Ne.** 5:5–17. Wale wote ambao hawakuwa Walamani walikuwa Wanefi, **Yak. (KM)** 1:13. Wanefi waliongozwa kwa kusudi lililo bora, **Alma** 43:6–9, 45. Wanefi kamwe hawakuwahi kuwa na furaha zaidi kuliko wakati wa Moroni, **Alma** 50:23. Wanefi waliokolewa kwa sababu ya sala za wenye haki, **Alma** 62:40. Wanefi wakaanza kufifia katika kutoamini, **Hel.** 6:34–35. Yesu alifundisha na kuhudumu miongoni mwa Wanefi, **3 Ne.** 11:1–28:12. Wote waliongolewa kwa Bwana na walikuwa na mambo yote sawa, **4 Ne.** 1:2–3. Hapakuwa na ugomvi, upendo wa Mungu ulikaa mioyoni mwao, nao walikuwa watu wenye furaha zaidi, **4 Ne.** 1:15–16. Wanefi wakaanza kuwa wenye kiburi na kuwa bure, **4 Ne.** 1:43. Damu na mauaji ya watu wengi yalienea kote katika uso wote wa nchi, **Morm.** 2:8. Wanefi waliongezeka katika uovu na Mormoni alikataa kuwaongoza, **Morm.** 3:9–11. Wanefi wote, isipokuwa wale ishirini na wanne, waliuawa, **Morm.** 6:7–15. Kila Mnefi ambaye hangeweza kumkana Kristo aliuawa, **Moro.** 1:2.

Wanefi waliangamizwa kwa sababu ya uovu na dhambi zao, **M&M** 3:18. Jihadhari na kiburi kwa kuogopa usije ukawa kama Wanefi, **M&M** 38:39.

Wanyang'anyi wa Gadiantoni. *Ona pia* Makundi maovu ya siri

Katika Kitabu cha Mormoni, ni kundi la wanyang'anyi lililoundwa na Mnefi mwovu aliyeitwa Gadiantoni. Shirikisho lao lilijengwa juu ya usiri na viapo vya kishetani.

Gadiantoni alisababisha kuangamizwa kwa taifa la Wanefi, **Hel.** 2:12–13. Ibilisi alitoa viapo na maagano ya siri kwa Gadiantoni, **Hel.** 6:16–32. Ushirikiano wa siri ulisababisha kuangamia kwa taifa la Wayaredi, **Eth.** 8:15–26.

Warumi, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo

Katika Agano Jipya, ni barua ambayo Paulo aliwaandikia Watakatifu katika

Roma. Alikuwa akiitafakari safari ya Yerusalemu, ambayo ilikuwa dhahiri ni ya hatari. Kama angeokoa maisha yake, alitumaini baadaye kutembelea Roma. Barua ilikuwa na maana kwa sehemu moja ya kulitayarisha Kanisa huko kumpokea yeye wakati alipoenda. Pia yaweza kuchukuliwa kama yenye taarifa ya mafundisho fulani ambayo yalikuwa yakibishaniwa na kwamba Paulo sasa aliyachukulia kana kwamba mwishowe yamefafanua.

Mlango wa 1 una salamu za Paulo kwa Warumi. Mlango wa 2–11 inajumuisha matamko kadhaa juu ya mafundisho ya imani, matendo, na neema. Mlango 12–16 ina mafundisho ya kimatendo juu ya upendo, kazi, na utakatifu.

Wasamaria. *Ona pia* Samaria

Watu wa nyakati za Biblia walioishi katika Samaria baada ya ufalme wa kaskazini wa Israeli kutekwa na Waashuru. Wasamaria walikuwa sehemu ni Waisraeli na sehemu ni Wayunani. Dini yao ilikuwa ni mchanganyiko wa imani na desturi za Kiyahudi na kipagani. Mfano wa Msamaria mwema katika Luka 10:25–37 unaonyesha chuki ambayo Wayahudi waliikuza kwa Wasamaria kwa sababu Wasamaria walikuwa wamekengeuka kutoka dini ya Kiisraeli. Bwana aliwatuma Mitume kufundisha injili kwa Wasamaria (Mdo. 1:6–8). Filipo kwa mafanikio alihubiri injili ya Kristo kwa watu wa Samaria na akafanya miujiza mingi miongoni mwao (Mdo. 8:5–39).

Wateule. *Ona* Teule, Wateule

Wathesalonike, Waraka kwa. *Ona pia* Nyaraka za Paulo; Paulo

Vitabu viwili katika Agano Jipya. Mwanzoni zilikuwa ni barua ambazo Paulo aliziandika kwa Wathesalonike wakati akiwa katika Korintho wakati wa safari yake ya kwanza katika Ulaya takribani mwaka wa 50 B.K. Kazi yake katika Thesalonike inaelezwa katika Matendo 17. Paulo alitaka kurudi Thesalonike lakini alishindwa kufanya hivyo (1 The. 2:18). Kwa hiyo yeye akamtuma Timoteo kuwasalimia waongofu hao na kumletea taarifa ya jinsi walivyokuwa wakiendelea. Paulo aliandika waraka wa kwanza kama matokeo ya shukrani zake juu ya kurudi kwa Timoteo.

Wathesalonike wa Kwanza: Mlango wa 1–2 ina salamu za Paulo na sala yake kwa ajili ya Watakatifu hao; mlango wa 3–5 inafundisha juu ya makuzi ya kiroho, upendo, usafi wa kimwili, juhudi, na Ujio wa Pili wa Yesu Kristo.

Wathesalonike wa Pili: Mlango wa 1 una sala kwa ajili ya Watakatifu. Mlango wa 2 unazungumzia juu ya kuja kwa ukengeufu. Mlango wa 3 una sala ya Paulo kwa ajili ya ushindi wa malengo ya injili.

Watoto. *Ona* Mtoto, Watoto

Watoto wa Kristo. *Ona pia* Wana na Mabinti za Mungu; Yesu Kristo; Zaliwa; Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena

Wale walioikubali injili ya Yesu Kristo.

Yeyote atakayejinyenyekeza mwenyewe kama huyu mtoto mdogo ndiye mkuu, **Mt.** 18:1–4. Iaminini nuru hiyo ili mpate kuwa watoto wa nuru, **Yn.** 12:36.

Mvueni mtu wa asili na kuwa kama mtoto, **Mos.** 3:19; 27:25–26. Kwa sababu ya agano mtaitwa watoto wa Kristo, **Mos.** 5:7. Kama utashikilia kila jambo lililo jema, bila shaka utakuwa mtoto wa Kristo, **Moro.** 7:19.

Kadiri wengi walivyonipokea, niliwapa uwezo wa kuwa wana wangu, **M&M** 39:4. Msiogope, watoto wadogo, kwani ninyi ni wangu, **M&M** 50:40–41.

Wewe u mmoja ndani yangu, mwana wa Mungu, **Musa** 6:68.

Watoto wa Mungu. *Ona* Mwanadamu, Wanadamu; Wana na Mabinti za Mungu

Watu wa Mfalme

Katika Kitabu cha Mormoni, ni

kikundi cha watu waliotaka kuipindua serikali ya Wanefi (Alma 51:1–8).

Wayahudi. *Ona pia* Israeli; Yuda

Wayahudi wanaweza kuwa (1) wazao wa Yuda, mmoja wa wana kumi na wawili wa Yakobo, (2) watu wa kale wa ufalme wa kusini wa Yuda, au (3) watu wenye kushika dini, staili za maisha, na mila za dini ya Kiyahudi lakini aweza kuwa au asiwe Myahudi kwa kuzaliwa. Imekuwa ni kitu cha kawaida kutumia neno Myahudi kwa kuwaonyesha wazao wote wa Yakobo, lakini hili ni kosa. Ni lazima litumike kwa wale walio wa ufalme wa Yuda au, hususani zaidi kwa siku hizi, wale walio wa kabila la Yuda na washirika wake.

Fimbo ya enzi haitaondoka katika Yuda hadi Shilo atakapokuja, **Mwa.** 49:10.

Injili ya Kristo ni uwezo wa Mungu kwa wokovu, kwa Myahudi kwanza, **Rum.** 1:16.

Bwana atamwinua nabii miongoni mwa Wayahudi—hata Masiya, **1 Ne.** 10:4. Kitabu kilipotoka kinywani mwa Myahudi, mambo yaliyoandikwa yalikuwa wazi na safi, **1 Ne.** 14:23. Wayahudi watatawanyika miongoni mwa mataifa yote, **2 Ne.** 25:15. Wayahudi ni watu wangu wa kale wa agano, **2 Ne.** 29:4. Wayahudi waliotawanyika wataanza kumwamini Kristo, **2 Ne.** 30:7. Wayahudi watalikataa jiwe ambalo juu yake wangelijenga, **Yak. (KM)** 4:14–16. Wayahudi watapata ushahidi mwingine ya kuwa Yesu alikuwa ndiye Kristo halisi, **Morm.** 3:20–21.

Manabii wawili watainuliwa kwa taifa la Kiyahudi katika siku za mwisho, **M&M** 77:15. Yasihini mataifa yote, kwanza juu ya Wayunani, na kisha juu ya Wayahudi, **M&M** 133:8.

Katika siku zile kutakuwako na taabu kuu juu ya Wayahudi, **JS—M** 1:18.

Wayaredi. *Ona pia* Kitabu cha Mormoni; Yaredi; Yaredi, Kaka wa

Watu katika Kitabu cha Mormoni ambao walikuwa wazao wa Yaredi, kaka yake, na marafiki zao (Eth. 1:33–41). Waliongozwa na Mungu kutoka Mnara wa Babeli hadi Marekani, nchi ya ahadi (Eth. 1:42–43; 2–3; 6:1–18). Ingawa taifa lao wakati fulani lilikuwa na mamilioni ya watu, wote walijiangamiza kwa vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyoletwa na uovu (Eth. 14–15).

Wayunani

Kama ilivyotumika katika maandiko, *Wayunani* lina maana kadhaa. Wakati mwingine lina maana ya watu wasiokuwa wa ukoo wa Israeli, wakati mwingine watu wasiokuwa wa ukoo wa Kiyahudi, na wakati mwingine ni mataifa ambayo hayana injili, ingawa panaweza pakawa na watu wa damu ya Kiisraeli miongoni mwa watu hao. Matumizi ya hili la mwisho yanaonekana kutumika zaidi katika Kitabu cha Mormoni na Mafundisho na Maagano.

Waisraeli walikatazwa kuoa au kuolewa na wasio Waisraeli (Wayunani), **Kum.** 7:1–3. Bwana angelikuja kuwa nuru ya Wayunani, **Isa.** 42:6.

Petro aliamriwa kuipeleka injili kwa Wayunani, **Mdo.** 10:9–48. Mungu pia alitoa toba kwa Wayunani, **Mdo.** 11:18. Tunabatizwa katika kanisa moja, iwe tu Wayahudi au Wayunani, **1 Kor.** 12:13. Wayunani ni washiriki pamoja nasi katika Kristo kwa injili, **Efe.** 3:6.

Kitabu cha Mormoni kiliandikwa kwa Wayunani, **Ukurasa wa jina la Kitabu cha Mormoni** (Morm. 3:17). Mtu miongoni mwa Wayunani alisafiri juu ya maji, **1 Ne.** 13:12. Vitabu vingine vilikuja kutoka kwa Wayunani, **1 Ne.** 13:39. Utimilifu wa injili utawafikia Wayunani, **1 Ne.** 15:13 (3 Ne. 16:7; M&M 20:9). Nchi hii itakuwa nchi ya uhuru kwa Wayunani, **2 Ne.** 10:11. Wayunani ni mfano wa mti wa mizabibu pori, **Yak. (KM)** 5.

Injili itaenea katika nyakati za Wayunani, **M&M** 45:28 (M&M 19:27). Neno litaenea hata miisho ya dunia, kwa Wayunani kwanza, na kisha kwa Wayahudi, **M&M** 90:8–10. Sabini watakuwa

mashahidi maalumu kwa Wayunani, **M&M** 107:25. Wapelekeni wazee wa kanisa langu kuyaita mataifa yote, kwanza juu ya Wayunani, na kisha juu ya Wayahudi, **M&M** 133:8.

Wazazi. *Ona pia* Baba, Mwili wenye kufa; Mama

Akina baba na akina mama. Waume na wake wenye kustahili ambao wameunganishwa kiusahihi katika ndoa katika hekalu la Mungu wanaweza wakatimiza nafasi yao kama wazazi kwa milele yote. "Wazazi wana wajibu mtakatifu wa kuwalea watoto wao katika upendo na haki, kuwapa mahitaji yao ya kimwili na kiroho, na kuwafundisha kupendana na kutumikiana, kuzishika amri za Mungu, na kuwa raia wenye kuheshimu sheria za nchi yoyote wanayoishi" ("Familia: Tangazo kwa Ulimwengu," *Ensign,* Nov. 2010, 129).

Watoto, watiini wazazi wenu, **Efe.** 6:1–3 (Kol. 3:20).

Adamu na Hawa walikuwa wazazi wetu wa kwanza, **1 Ne.** 5:11. Laana yaweza kuwa juu ya vichwa vya wazazi wenu, **2 Ne.** 4:6. Fundisha wazazi kwamba lazima watubu na wabatizwe, **Moro.** 8:10.

Wazazi wanaamriwa kufundisha injili kwa watoto wao, **M&M** 68:25. Watoto wote wanayo haki ya kudai juu ya wazazi wao, **M&M** 83:4.

Dhambi za wazazi haziwezi kujibiwa juu ya vichwa vya watoto, **Musa** 6:54.

Wazoramu. *Ona* Zoramu, Wazoramu

Weka Wakfu. *Ona* Sheria ya Kuweka wakfu, Weka wakfu

Wema. *Ona pia* Haki, Uadilifu, enye Uadilifu; Usafi wa Kimwili; Uwezo

Uaminifu na uadilifu ulio bora, uwezo na nguvu (Luka 8:46), au usafi wa kimwili (Moro. 9:9).

Wewe u mwanamke mwema, **Rut.** 3:11. Mtu aliye na mikono safi na moyo mweupe atasimama katika mahali patakatifu pa Bwana, **Zab.** 24:3–4. Mwanamke mwema ni taji kwa mume wake, **Mit.** 12:4. Kima cha mke mwema chapita rubi zaidi, **Mit.** 31:10–31.

Katika imani yenu ongezeni wema, **2 Pet.** 1:5 (M&M 4:6).

Jaribu wema wa neno la Mungu, **Alma** 31:5.

Na wema uyarembe mawazo yako bila kukoma, **M&M** 121:45.

Tunaamini katika kuwa wema, **M ya I** 1:13 (Flp. 4:8).

Wendo

Ona Wendo katika kiambatisho.

Whitmer, David

Kiongozi wa mwanzo kabisa katika Kanisa la urejesho na ni mmoja wa Mashahidi Watatu wa asili ya kiungu na ukweli wa Kitabu cha Mormoni (M&M 14; 17–18). Bwana alimpa maelekezo binafsi katika Mafundisho na Maagano sehemu ya 14 na 30:1–4.

Whitmer, John

Kiongozi wa awali kabisa katika Kanisa la Urejesho na ni mmoja wa Mashahidi Wanane wa Kitabu cha Mormoni. Ona "Ushuhuda wa Mashahidi Wanane" katika kurasa za utangulizi za Kitabu cha Mormoni. Pia aliitwa kuhubiri injili (M&M 30:9–11).

Whitmer, Peter, Mdogo

Kiongozi wa awali kabisa katika Kanisa la urejesho na ni mmoja wa Mashahidi Wanane wa Kitabu cha Mormoni. Ona "Ushuhuda wa Mashahidi Wanane" katika kurasa za utangulizi za Kitabu cha Mormoni. Bwana alimpa maelekezo binafsi katika Mafundisho na Maagano sehemu ya 16 na 30:5–8.

Whitney, Newel K.

Kiongozi wa awali kabisa katika Kanisa la urejesho. Newel K. Whitney alikuwa askofu katika Kirtland, Ohio (Marekani), na baadaye alitumikia kama Askofu Msimamizi wa Kanisa (M&M 72:1–8; 104; 117).

Wilaya ya Jackson, Missouri (Marekani). *Ona pia* Yerusalemu Mpya

Mahali pa kukusanyika Watakatifu katika siku za mwisho; maana yake ni, mahali pa kituo cha Yerusalemu Mpya itakapoanzishwa (M&M 57–58; 82; 101:69–71; 105:28).

Williams, Frederick G.

Kiongozi wa awali kabisa katika Kanisa la urejesho ambaye kwa wakati fulani alitumika kama mshauri katika Urais wa Ukuhani Mkuu (M&M 81; 90:6, 19; 102:3).

Wimbo. *Ona pia* Imba; Muziki

Namna ya kumtukuza Mungu.

Wimbo uliimbwa na Mitume Kumi na Wawili kabla ya Bwana hajaenda Gethsemani, **Mt.** 26:30.

Bwana alimwita Emma Smith kufanya uteuzi wa nyimbo takatifu, **M&M** 25:11. Wimbo wa mwenye haki ni sala kwangu, na utajibiwa kwa baraka juu ya vichwa vyao, **M&M** 25:12. Msifuni Bwana kwa kuimba na kwa muziki, **M&M** 136:28.

Wimbo wa Sulemani

Kitabu katika Agano la Kale. Joseph Smith Nabii alifundisha kwamba Wimbo wa Sulemani siyo maandiko ya kuongozwa na Mungu.

Wito. *Ona* Ita, Itwa na Mungu, Wito

Wito na Uteuzi. *Ona pia* Uteuzi

Wafuasi wa Kristo wenye haki wanaweza kuhesabiwa miongoni mwa wateule ambao hupata uhakika wa kuinuliwa. Wito wa uteuzi huu huanza katika toba na ubatizo. Unakamilika pale "wanaposonga mbele, wakisherehekea juu ya neno la Kristo, na wakistahmili hadi mwisho" (2 Ne. 31:19–20). Maandiko huita utaratibu huu kama ni kufanya wito na uteuzi wetu kuwa imara zaidi (2 Pet. 1:4–11; M&M 131:5–6).

Nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani, **Ku.** 19:5–6 (Ufu. 1:6).

Mungu amewachagua wateule tangu mwanzo mpate wokovu, **2 The.** 2:13. Jitahidini zaidi kufanya imara kuitwa kwenu na uteule wenu, **2 Pet.** 1:10.

Bwana awaweke muhuri muwe wake, **Mos.** 5:15. Ninaagana na wewe kwamba utapata uzima wa milele, **Mos.** 26:20.

Makuhani walio waaminifu wanakuwa kanisa na ufalme na wateule wa Mungu, **M&M** 84:33–34. Neno la unabii lililo imara zaidi maana yake ni kujua kwamba mtu ametiwa muhuri kwa uzima wa milele, **M&M** 131:5–6. Ninafunga juu yake kuinuliwa kwako, **M&M** 132:49.

Wivu, enye Wivu. *Ona pia* Husuda

Kama ilivyotumika katika maandiko, neno wivu lina maana mbili: (1) kuwa mwenye kuwaka moto na hisia kali na nzito juu ya mtu fulani au kitu fulani, na ya (2) kuwa mwenye husuda juu ya mtu fulani au kuwa na mashaka kwamba mwingine atapata mafanikio ya aina fulani.

Kuwa mwenye hisia kali: Mimi Bwana ni Mungu mwenye wivu, **Ku.** 20:5 (Kum. 5:9; 6:15; Mos. 11:22). Nitakuwa na wivu kwa ajili ya jina langu takatifu, **Eze.** 39:25. Naona wivu kwa ajili ya Yerusalemu na kwa ajili ya Sayuni, **Zek.** 1:14.

Kuwa mwenye husuda au shaka: Wivu ni ghadhabu ya mtu, **Mit.** 6:32–35.

Akishi alianza kuwa na wivu kwa mwanawe, **Eth.** 9:7.

Jivueni ninyi wenyewe mkaondokane na wivu na woga, **M&M** 67:10.

Wizi. *Ona* Iba, Wizi

Wokovu. *Ona pia* Komboa, Kombolewa, Ukombozi; Kuinuliwa; Lipia dhambi, Upatanisho; Mauti ya Kimwili; Mauti ya Kiroho; Mpango wa Ukombozi; Neema; Yesu Kristo

Kuokolewa kutoka katika mauti ya kimwili na kiroho. Watu wote wataokolewa kutokana na mauti ya kimwili kwa neema ya Mungu, kupitia mauti na Ufufuko wa Yesu Kristo. Kila mtu anaweza pia kuokolewa kutoka katika

mauti ya kiroho kwa neema ya Mungu, kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. Imani hii huonekana katika maisha ya utii kwa sheria na ibada za injili na huduma kwa Kristo.

Bwana ndiye nuru na wokovu wangu, **Zab.** 27:1. Yeye tu ndiye mwamba wangu na wokovu wangu, **Zab.** 62:2.

Injili ni uwezo wa Mungu uletao wokovu, **Rum.** 1:16 (M&M 68:4). Utimizeni wokovu wenu kwa kuogopa, **Flp.** 2:12. Mungu amewachagua mpate wokovu kwa njia ya utakaso, **2 The.** 2:13.

Wokovu ni wa bure, **2 Ne.** 2:4.

Hakuna zawadi iliyo kuu zaidi kuliko zawadi ya wokovu, **M&M** 6:13.

Yesu Kristo ndilo jina pekee ambalo kwalo wokovu utakuja, **Musa** 6:52 (Mdo. 4:10–12). Tunaamini kwamba kupitia upatanisho wa Kristo, wanadamu wote wanaweza kuokolewa, **M ya I** 1:3.

Wokovu wa watoto: Isipokuwa mmekuwa kama watoto wadogo, hamtaingia katika ufalme wa mbinguni, **Mt.** 18:3.

Watoto wadogo pia wanao uzima wa milele, **Mos.** 15:25. Ubatizo wa watoto wachanga ni chukizo, na watoto wadogo wako hai katika Kristo kwa sababu ya Upatanisho, **Moro.** 8:8–24.

Watoto wadogo wamekombolewa kwa njia ya Mwana Pekee; Shetani hawezi kuwajaribu, **M&M** 29:46–47. Watoto wafundishwe injili na wabatizwe wakiwa na umri wa miaka minane, **M&M** 68:25–28. Watoto wadogo wametakaswa kupitia Yesu Kristo, **M&M** 74:7. Wanadamu huwa tena, katika hali ya uchanga, wasio na hatia, **M&M** 93:38. Watoto wote wanaokufa kabla ya umri wa uwajibikaji wataokolewa katika ufalme wa selestia, **M&M** 137:10.

Watoto ni wazima tangu kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, **Musa** 6:54.

Wokovu, Mpango wa. *Ona* Mpango wa Ukombozi

Wokovu kwa ajili ya Wafu. *Ona pia* Kitabu cha Ukumbusho; Mpango wa Ukombozi; Nasaba; Wokovu

Nafasi kwa watu wale waliokufa pasipo kupokea ibada za wokovu za injili ili kupata ibada kufanywa kwa ajili yao katika mahekalu na waumini wa Kanisa wenye kustahili. Wafu hufundishwa injili katika ulimwengu wa roho na inawezekana wakakubali ibada zilizofanywa kwa ajili yao katika mwili wenye kufa.

Waumini wa Kanisa walio waaminifu hutafiti na kutayarisha historia za familia ili kuyajua majina na tarehe za kuzaliwa kwa wahenga wao ili kwamba ibada za wokovu zipate kufanywa kwa ajili yao.

Kuwaambia wafungwa, Haya tokeni, **Isa.** 49:9 (Isa. 24:22; 1 Ne. 21:9). Kuwatangazia mateka uhuru wao, **Isa.** 61:1 (Lk. 4:18). Ataigeuza mioyo ya baba iwaelekee watoto, **Mal.** 4:5–6 (3 Ne. 25:5–6; M&M 110:13–16).

Wafu wataisikia sauti ya Mwana wa Mungu, **Yn.** 5:25. Kwa nini wao hubatizwa kwa ajili ya wafu, **1 Kor.** 15:29. Kristo alizihubiria roho zilizokuwa kifungoni, **1 Pet.** 3:18–20. Kwa sababu hii injili ilihubiriwa pia kwao wale walio wafu, **1 Pet.** 4:6.

Mwana aliwatembelea roho waliokuwa kifungoni, **M&M** 76:73. Halafu utakuja ukombozi wa wale ambao wamepokea sehemu yao katika kile kifungo, **M&M** 88:99. Kisima cha ubatizo hakiko juu ya dunia ili wakatifu wangu wapate kubatizwa kwa ajili ya wale waliokufa, **M&M** 124:29. Wale wote waliokufa na ambao wangeikubali injili watakuwa warithi kwa ufalme wa selestia, **M&M** 137:7–10. Mwana wa Mungu alionekana akitangaza uhuru kwa wafungwa ambao wamekuwa waaminifu, **M&M** 138:18.

Roho nyingi zilizokuwa kifungoni zilitoka, **Musa** 7:57.

Wokovu wa Watoto. *Ona* Mtoto, Watoto; Wokovu—Wokovu wa watoto

Woodruff, Wilford. *Ona pia* Manifesto; Tamko Rasmi 1

Rais wa nne wa Kanisa baada ya

Urejesho wa injili kupitia kwa Joseph Smith Nabii. Alizaliwa katika mwaka 1807 na alifariki katika mwaka 1898.

Aliitwa kujaza nafasi katika Baraza la wale Kumi na Wawili, **M&M** 118:6. Alikuwa miongoni mwa roho teule zilizowekwa ili kuja katika kipindi cha utimilifu wa nyakati, **M&M** 138:53. Alipokea ufunuo wa kusimamisha ndoa za wake wengi katika Kanisa, **TR** 1.

Yafethi. *Ona pia* Nuhu, Patriaki wa Biblia

Mwana mkubwa wa Nuhu, nabii wa Agano la Kale (Musa 8:12).

Nuhu akamzaa Yafethi, **Mwa.** 5:32 (Mwa. 6:10; Musa 8:12). Yafethi na mkewe wakaingia katika safina ya Nuhu, **Mwa.** 7:13. Yafethi akatoka nje ya safina, **Mwa.** 9:18. Mungu atamnafisisha Yafethi, **Mwa.** 9:27.

Yakobo, Kaka wa Bwana

Katika Agano Jipya, ni kaka wa Bwana (Gal. 1:19) na wa Yusufu, Simoni, Juda, na dada kadhaa (Mt. 13:55–56; Mk. 6:3; Yuda 1:1). Pia alijulikana kama Yakobo mwenye Haki na alikuwa na nafasi muhimu katika Kanisa katika Yerusalemu (Mdo. 12:17; 15:13; 1 Kor. 15:7; Gal. 2:9–12). Huenda yeye ndiye aliyeandika waraka wa Yakobo.

Waraka wa Yakobo: Kitabu katika Agano Jipya. Mwanzoni hii ilikuwa ni barua iliyoandikwa kwa makabila kumi na mawili ya Israeli yaliyotawanyika sehemu mbalimbali na huenda kuwa iliandikwa kutoka Yerusalemu. Waraka una mambo yaliyoelezwa wazi juu ya matendo ya dini, ikijumuisha ushauri muhimu katika mlango wa 1 kwamba kama mtu akipungukiwa na hekima, aombe msaada kwa Mungu (Yak. [Bib.] 1:5–6; JS—H 1:9–20). Mlango wa 2 unajishughulisha na imani na matendo. Mlango wa 3–4 inazungumzia juu ya umuhimu wa kuudhibiti ulimi na anawashauri watakatifu wasisemeane mabaya. Mlango wa 5 unawatia moyo Watakatifu kuwa na subira na kuwaita wazee kwa ajili ya kuwabariki wawapo wagonjwa; pia inafundisha juu ya baraka za kusaidia kuwaongoa wengine.

Yakobo, Mwana wa Alfayo

Mmoja wa Mitume Kumi na Wawili waliochaguliwa na Yesu wakati akiwa katika huduma Yake katika mwili ufao (Mt. 10:3; Mk. 3:18; Lk. 6:15; Mdo. 1:13).

Yakobo, Mwana wa Isaka. *Ona pia* Esau; Isaka; Israeli

Patriaki na nabii wa Agano la Kale; ni mdogo kati ya wana mapacha wa Isaka na Rebeka (Mwa. 25:19–26). Yakobo alipata haki ya uzaliwa wa kwanza dhidi ya kaka yake Esau. Hii ilikuwa kwa sababu ya ustahilivu wa Yakobo na kuoa katika agano, wakati Esau alikuwa akidharau haki yake ya uzaliwa wa kwanza na akaoa nje ya agano (Mwa. 25:30–34; 26:34–35; 27; 28:6–9; Ebr. 12:16).

Rebeka alijua kutoka kwa Bwana ya kuwa Esau angelimtumikia Yakobo, **Mwa.** 25:23. Alinunua haki ya uzaliwa wa kwanza kutoka kwa Esau, **Mwa.** 25:29–34. Aliota ndoto ya ngazi ifikayo mbinguni, **Mwa.** 28. Aliwaoa Lea na Raheli, **Mwa.** 29:1–30. Alikuwa na watoto wa kiume kumi na wawili na binti mmoja, **Mwa.** 29:31–30:24; 35:16–20. Aliwaoa Bilha na Zilpa, **Mwa.** 30:3–4, 9. Jina lake lilibadilishwa na kuwa Israeli, **Mwa.** 32:28. Alimwona Mungu uso kwa uso, **Mwa.** 32:30. Alimpendelea Yusufu, **Mwa.** 37:3. Alikwenda Misri pamoja na familia yake, **Mwa.** 46:1–7. Aliwabariki wanawe na wazao wao, **Mwa.** 49. Akafa, **Mwa.** 49:33.

Alizishika amri na hivi leo ameinuliwa juu ya kiti cha enzi huko mbinguni akiwa pamoja na Ibrahimu na Isaka, **M&M** 132:37.

Yakobo, Mwana wa Lehi. *Ona pia* Lehi, Baba wa Nefi

Nabii katika Kitabu cha Mormoni na mtunzi wa mahubiri kadhaa katika

vitabu vya 2 Nefi na Yakobo (2 Ne. 6–11; Yak. [KM] 1–7).

Kitabu cha Yakobo: Kitabu cha tatu katika kitabu cha Mormoni. Mlango wa 1 hutuambia kwamba Nefi alimkabidhi Yakobo kumbukumbu iliyoandikwa na kisha akamweka wakfu Yakobo na kaka yake Yusufu ili wawe makuhani na walimu kwa watu. Mlango wa 2–4 ni mahubiri yanayowasisitizia watu kuwa safi kimaadili. Yakobo pia alifundisha juu ya ujio wa Masiya mkombozi, na akatoa sababu kwa nini baadhi katika Israeli wasingemkubali wakati wa ujio Wake. Mlango wa 5–6 ina ushuhuda wa Yakobo na fumbo la kinabii juu ya historia na misheni ya watu wa Israeli. Mlango wa 7 una historia ya mwasi msomi aliyeitwa Sheremu, ambaye alishindwa kwa ushuhuda mtakatifu wa Yakobo.

Yakobo, Mwana wa Zebedayo

Mmoja wa Mitume Kumi na Wawili waliochaguliwa na Yesu wakati wa huduma Yake katika mwili ufao. Alikuwa kaka yake Yohana. Alikuwa mmoja wa Mitume watatu waliochaguliwa kuwa na Yesu katika matukio fulani maalumu: wakati wa kufufuliwa kwa binti wa Yairo (Mk. 5:37), wakati wa Kugeuka Sura (Mt. 17:1; Mk. 9:2; Lk. 9:28), na wakati wa Gethsemani (Mt. 26:37; Mk. 14:33). Pamoja na Petro na Yohana, alirejesha ukuhani wa Melkizedeki duniani kwa kumtawaza Joseph Smith na Oliver Cowdery (M&M 27:12; 128:20; JS—H 1:72).

Yaredi. *Ona pia* Wayaredi; Yaredi, Kaka wa

Kiongozi katika Kitabu cha Mormoni ambaye, pamoja na kaka yake, waliwaongoza kikundi cha watu kutoka Mnara wa Babeli hadi nchi ya ahadi katika bara la Marekani (Eth. 1:33–2:1).

Yaredi alimwomba kaka yake kusali ili Bwana asizivuruge lugha za familia na marafiki zao, **Eth.** 1:34–37. Alisafiri hadi baharini na kukaa huko kwa miaka minne, **Eth.** 2:13. Alisafiri juu ya maji hadi nchi ya ahadi, **Eth.** 6:4–12.

Yaredi, Kaka wa. *Ona pia* Wayaredi; Yaredi

Nabii wa Kitabu cha Mormoni. Yeye na kaka yake waliasisi taifa la Kiyaredi walipokiongoza kikundi cha watu kutoka katika Mnara wa Babeli hadi katika nchi ya ahadi katika bara la Marekani (Eth. 1–6). Alikuwa mtu mwenye imani kubwa ambaye alinena na Bwana uso kwa uso. (M&M 17:1). Hadithi yake imeandikwa katika kitabu cha Etheri.

Kaka wa Yaredi alikuwa ni mtu mpana na mtu mwenye nguvu, na alipendwa sana na Bwana, **Eth.** 1:34. Kwa sababu ya imani yake, kaka wa Yaredi alikiona kidole cha Bwana, **Eth.** 3:6–9 (Eth. 12:20). Kristo alionyesha mwili wake wa kiroho kwa kaka yake Yaredi, **Eth.** 3:13–20. Kamwe hapakuwahi kuwa na mambo makuu zaidi yaliyoonyeshwa kuliko yale ambayo yalionyeshwa kwa kaka yake Yaredi, **Eth.** 4:4. Kaka yake Yaredi aliwaonya watu wake dhidi ya ufalme, **Eth.** 6:22–23. Bwana alionyesha mambo yote kwa kaka yake Yaredi, **Eth.** 12:21. Kaka wa Yaredi alikuwa mwenye uwezo mkubwa katika kuandika, **Eth.** 12:24. Kwa njia ya imani kaka yake Yaredi aliuhamisha mlima Zerina, **Eth.** 12:30.

Yaromu

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwana wa Enoshi na kijukuu cha Lehi. Alitunza kumbukumbu ya Wanefi kwa miaka sitini, 420–361 K.K. (Eno. 1:25; Yar. 1:13). Alikuwa mtu mwaminifu aliyechagua kutokuandika mengi katika kumbukumbu hiyo ya kihistoria (Yar. 1:2).

Kitabu cha Yaromu: Kuna aya kumi na tano tu katika kitabu hiki, katika Kitabu cha Mormoni. Yaromu aliandika kuwa Wanefi waliendelea kuishi kwa torati ya Musa na walitazamia ujio wa Kristo. Waliongozwa na wafalme waliokuwa watu wenye imani kubwa. Walisitawi walipokuwa wakiwatii manabii wao, makuhani, na walimu.

Yehoshafati

Katika Agano la Kale, ni mfalme mwaminifu wa Wayahudi (1 Fal. 15:24; 22).

Yehova. *Ona pia* MIMI NIKO; Yesu Kristo

Agano au jina sahihi la Mungu wa Israeli. Maana yake "MIMI NIKO wa milele" (Ku. 3:14; Yn. 8:58). Yehova ndiye Yesu Kristo kabla ya kuzaliwa na akaja duniani kama mwana wa Maria (Mos. 3:8; 15:1; 3 Ne. 15:1–5). Kwa kawaida, neno Bwana lionekanapo katika Agano la Kale, linamaanisha "Yehova."

Yehova ndiye Kristo: Yehova alijulikana kwa manabii wa kale (Ku. 6:3; Ibr. 1:16). Mtume Paulo alifundisha ya kuwa Kristo alikuwa ndiye Yehova wa Agano la Kale (Ku. 17:6; 1 Kor. 10:1–4). Kaka yake Yaredi katika Kitabu cha Mormoni alimwona Kristo kabla ya kuzaliwa na Akamwabudu (Eth. 3:13–15). Moroni pia alimwita Kristo "Yehova" (Moro. 10:34). Katika Hekalu la Kirtland, Joseph Smith na Oliver Cowdery walimwona Yehova mfufuka (M&M 110:3–4).

Yeremia. *Ona pia* Maombolezo, Kitabu cha

Nabii wa Agano la Kale aliyezaliwa katika familia ya kikuhani na alitoa unabii wake katika Yuda tangu mwaka 626–586 K.K. Aliishi karibu na wakati wa manabii wengine wakuu: Lehi, Ezekieli, Hosea, na Danieli.

Yeremia alitawazwa kuwa nabii kabla ya kuzaliwa (Yer. 1:4–5). Wakati wa miaka yake ipatayo arobaini kama nabii alifundisha dhidi ya ibada za sanamu na utovu wa maadili miongoni mwa watu wa Uyahudi (Yer. 3:1–5; 7:8–10). Mara zote alikabiliana na upinzani na matukano (Yer. 20:2; 36:18–19; 38:4). Baada ya anguko la Yerusalemu, Wayahudi waliokimbilia Misri walimchukua Yeremia pamoja nao (Yer. 43:5–6), ambako, kulingana na mapokeo, walimpiga kwa mawe hadi kufa.

Kitabu cha Yeremia: Mlango wa 1–6 kuna unabii uliotolewa wakati wa utawala wa Yosia. Mlango wa 7–20 ni unabii wa wakati wa Yehoyakimu. Mlango wa 21–38 ni kuhusu utawala wa Zedekia. Mlango wa 39–44 kuna unabii na inaelezea matukio ya kihistoria baada ya anguko la Yerusalemu. Mlango wa 45 ina ahadi aliyompa Baruku, mwandishi wake, kwamba uhai wa Baruku ungelindwa. Mwishowe, mlango wa 46–51 ni unabii dhidi ya mataifa ya kigeni. Mlango wa 52 ni hitimisho la kihistoria. Sehemu ya unabii wa Yeremia ulikuwa katika mabamba ya shaba nyeupe ya Labani yaliyosalimishwa na Nefi (1 Ne. 5:10–13). Yeremia pia ametajwa mara mbili nyingine katika Kitabu cha Mormoni (1 Ne. 7:14; Hel. 8:20).

Kitabu cha Yeremia pia kinajumuisha uthibitisho wa kuishi kwa mtu kabla ya kuzaliwa na kuteuliwa kabla kwa Yeremia (Yer. 1:4–5); unabii wa kurudi kwa Waisraelii kutoka katika hali ya kutawanyika, kukusanywa kwa mmoja kutoka katika mji na wawili katika familia hadi Sayuni, nchi ya kupendeza ambayo Israeli na Yuda wangeliweza kukaa katika usalama na amani (Yer. 3:12–19); ni unabii wa Bwana wa kuwakusanya Israeli kutoka nchi za kaskazini kwa kuwapeleka "wavuvi" na "wawindaji" wengi kuwatafuta (Yer. 16:14–21). Tukio hili la siku za mwisho litakuwa pana sana kwa uwiano kuliko hata lile la Musa kuwaleta Israeli kutoka katika Misri (Yer. 16:13–15; 23:8).

Yeriko

Mji uliozungushiwa ukuta katika bonde la Yordani ulio futi 800 (mita 245) chini ya usawa wa bahari. Yeriko uko karibu na mahali ambapo Waisraeli walivuka mto wakati walipoingia kwa mara ya kwanza katika nchi ya ahadi (Yos. 2:1–3; 3:16; 6).

Waisraeli walipigana vita hapo Yeriko, **Yos.** 6:1–20. Yoshua aliweka laana juu ya Yeriko, **Yos.** 6:26 (1 Fal. 16:34). Yeriko ilikuwa ndani ya himaya iliyopangiwa kwa Benjamini, **Yos.** 18:11–12, 21.

Bwana aliitembelea Yeriko katika

safari yake ya mwisho ya Yerusalemu, **Mk.** 10:46 (Lk. 18:35; 19:1).

Yeroboamu

Katika Agano la Kale, Yeroboamu alikuwa mfalme wa kwanza wa upande wa kaskazini ya Israeli iliyogawanyika. Alikuwa mshirika wa kabila la Efraimu. Yeroboamu mwovu aliongoza uasi dhidi ya nyumba ya Yuda na familia ya Daudi.

Yeroboamu aliweka sanamu kwa ajili ya watu katika Dani na Betheli kuabudu, **1 Fal.** 12:28–29. Ahiya alimkemea Yeroboamu, **1 Fal.** 14:6–16. Yeroboamu alikumbukwa kwa kuleta dhambi ya kutisha kwa Israeli, **1 Fal.** 15:34 (1 Fal. 12:30).

Yerubaali. *Ona pia* Gideoni (Agano la Kale)

Jina lilitolewa kwa Gideoni katika Agano la Kale baada ya kuyangamiza madhabahu ya Baali (Amu. 6:32; 7:1; 9; 1 Sam. 12:11).

Yerusalemu

Mji ulioko katika Israeli ya sasa. Ni mji maarufu sana katika historia ya Biblia. Baadhi ya maeneo matakatifu sana zaidi kwa Wakristo, Wayahudi na Waislamuu yako katika mji huu na hutembelewa mara kwa mara na waumini wengi walio waaminifu. Mara nyingi unaelezwa kama mji mtakatifu.

Wakati fulani ulijulikana kama Salemu (Mwa. 14:18; Zab. 76:2), Yerusalemu ulikuwa mji wa Myebusi hadi ulipotwaliwa na Daudi (Yos. 10:1; 15:8; 2 Sam. 5:6–7); ambaye aliufanya kuwa makao makuu yake. Hadi wakati huo ulikuwa ukitumika sana kama ngome ya milimani, iliyokuwa kiasi cha futi 2600 (mita 800) juu ya usawa wa bahari. Umezungukwa na mabonde marefu katika pande zake zote isipokuwa kaskazini.

Wakati wa utawala wa Mfalme Daudi katika Yerusalemu, yeye alikaa katika kasri ya mbao. Hata hivyo, wakati wa utawala wa Suleimani, watu walifanya mambo mengi ya kuuremba mji huu, ikiwa ni pamoja na kujenga ikulu ya mfalme na hekalu.

Baada ya falme za Israeli na Yuda kugawanyika, Yerusalemu ulibakia kuwa mji mkuu wa Yuda. Mara kwa mara ulikuwa ukishambuliwa na majeshi ya uvamizi. (1 Fal. 14:25; 2 Fal. 14:13; 16:5; 18–19; 24:10; 25). Chini ya Hezekia, Yerusalemu ikawa kituo cha kuabudu kidini, lakini sehemu ya mji huo iliangamizwa katika mwaka wa 320 K.K., 168 K.K., na 65 K.K., Herode alijenga upya kuta zake na hekalu, lakini katika mwaka 70 B.K. Warumi wakauangamiza kabisa.

Melkizedeki alikuwa mfalme wa Salemu, **Mwa.** 14:18 (Ebr. 7:1–2). Isaya aliita Yerusalemu kujivika mavazi yake mazuri, **Isa.** 52:1. Neno la Bwana lingekuja kutoka Yerusalemu, **Mika** 4:2.

Kristo aliomboleza juu ya maanganizi ya Yerusalemu, **Mt.** 23:37–39 (Lk. 13:34). Yerusalemu ni mji wa Mungu aliye hai, **Ebr.** 12:22.

Yerusalemu ungeangamizwa kama haungetubu, **1 Ne.** 1:4, 13, 18 (2 Ne. 1:4; Hel. 8:20). Yerusalemu ungelikaliwa tena baada ya maangamizo, **3 Ne.** 20:46. Yerusalemu itajengwa tena, **Eth.** 13:5.

Kristo aliwaonya Watakatifu wa Siku za Mwisho kama alivyowaonya watu wa Yerusalemu, **M&M** 5:20. Wale walio wa Yuda watakimbilia Yerusalemu, **M&M** 133:13. Bwana atasema kutoka Yerusalemu, **M&M** 133:21.

Yerusalemu Mpya. *Ona pia* Sayuni

Mahali ambapo Watakatifu watakusanyika na Kristo atatawala yeye mwenyewe pamoja nao wakati wa Milenia. Sayuni (Yerusalemu Mpya) itajengwa katika ya bara la Marekani, na dunia itafanywa upya na kupokea utukufu wake wa kipepo (M ya I 1:10). Pia inamaanisha mji mtakatifu utakaoshuka kutoka mbinguni mwanzoni mwa Milenia.

Katika Sayuni itatoka sheria, **Mika** 4:2.

Jina la mji wa Mungu wangu, ni

Yerusalemu Mpya, **Ufu.** 3:12. Yohana aliuona ule mji mtakatifu, Yerusalemu Mpya, **Ufu.** 21:1–5.

Watu hawa nitawaimarisha katika nchi hii, nayo itakuwa Yerusalemu Mpya, **3 Ne.** 20:22. Yerusalemu mpya itajengwa katika Marekani, **Eth.** 13:3–6, 10.

Mji wa Yerusalemu Mpya utatayarishwa, **M&M** 42:9, 35, 62–69. Watakatifu wakusanyike na kuijenga Yerusalemu Mpya, **M&M** 45:63–75. Yerusalemu Mpya itajengwa katika Missouri, **M&M** 84:1–5 (M&M 57:1–3). Mwanakondoo atasimama juu ya Mlima Sayuni na juu ya mji mtakatifu, wa Yerusalemu Mpya, **M&M** 133:56.

Hema langu litaitwa Sayuni, Yerusalemu Mpya, **Musa** 7:62.

Yese. *Ona pia* Daudi

Katika Agano la Kale, ni baba wa Daudi na ni mhenga wa Kristo na wafalme wote wa Yuda.

Mwanawe Ruth, Obedi, alikuwa ndiye baba wa Yese, **Rut.** 4:17, 22. Wahenga wa Yese walipiginia tena kurudi nyuma hadi kwa Yuda, **1 Nya.** 2:5–12 (Mt. 1:5–6).

Yesu Kristo. *Ona pia* Alfa na Omega; Amini, Imani; Anguko la Adamu na Hawa; Bwana; Bwana Harusi; Damu; Dhabihu; Dhamiri; Golgotha; Imanueli; Injili, Vitabu vya Biblia; Jiwe la pembeni; Komboa, Kombolewa, Ukombozi; Kugeuka sura—Kugeuka sura kwa Kristo; Kupaa; Kusulubiwa; Lipia dhambi, Upatanisho; Mahubiri ya Mlimani; Maji ya Uzima; Maria, Mama wa Yesu; Masiya; Mchungaji Mwema; Mfariji; MIMI NIKO; Mkate wa Uzima; Mkombozi; Mpakwa mafuta; Mpango wa Ukombozi; Mpatanishi; Msalaba; Mtetezi; Mungu, Uungu; Mwamba; Mwana wa Mtu; Mwanakondoo wa Mungu; Mwanzo; Mwokozi; Mzaliwa wa Kwanza; Neema; Njia; Nuru, Nuru ya Kristo; Nyoka wa shaba nyeupe; Ondoleo la Dhambi; Sakramenti; Siyo na mwisho; Toba, Tubu; Ufufuko; Ujio wa Pili wa Yesu Kristo; Umba, Uumbaji; Yehova; Zaliwa

Kristo (neno la Kiyunani) na *Masiya* (neno la Kiebrania) maana yake ni "mpakwa mafuta." Yesu Kristo ndiye Mzaliwa wa kwanza wa Baba katika roho (Ebr. 1:6; M&M 93:21). Yeye ndiye Mzaliwa Pekee wa Baba katika mwili (Yn. 1:14; 3:16). Yeye ndiye Yehova (M&M 110:3–4) na aliteuliwa katika wito wake mkuu kabla ya kuumbwa kwa ulimwengu. Chini ya maelekezo ya Baba, Yesu aliumba dunia na kila kitu kilichopo juu yake (Yn. 1:3, 14; Musa 1:31–33). Alizaliwa na Maria huko Bethlehemu, aliishi maisha yasiyo na dhambi, na akafanya upatanisho kamili kwa ajili ya dhambi za wanadamu wote kwa kumwaga damu Yake na kwa kutoa uhai Wake juu ya msalaba (Mt. 2:1; 1 Ne. 11:13–33; 3 Ne. 27:13–16; M&M 76:40–42). Akafufuka kutoka kwa wafu, hivyo akathibitisha hatima ya kufufuka kwa wanadamu wote. Kupitia Upatanisho na Ufufuko wa Yesu, wale wanaotubu dhambi zao na kutii amri za Mungu wanaweza kuishi milele pamoja na Yesu na Baba (2 Ne. 9:10–12; 21–22; M&M 76:50–53, 62).

Yesu Kristo ndiye mtu mkuu kuliko wote waliozaliwa juu ya dunia. Maisha Yake ni mfano kamili wa jinsi wanadamu wote itupasavyo kuishi. Sala, baraka, na ibada zote za ukuhani zinapaswa kufanyika katika jina Lake. Yeye ni Bwana wa mabwana, Mfalme wa wafalme, Muumba, Mwokozi, na Mungu wa dunia nzima.

Yesu Kristo atakuja tena katika uwezo na utukufu ili kutawala juu ya dunia wakati wa Milenia. Katika siku ya mwisho, yeye atawahukumu wanadamu wote (Alma 11:40–41; JS—M 1).

Muhtasari wa maisha Yake (katika mfuatano wa matukio): Kuzaliwa na huduma ya Yesu vilitabiriwa, **Lk.** 1:26–38 (Isa. 7:14; 9:6–7; 1 Ne. 11). Alizaliwa, **Lk.**

2:1–7 (Mt. 1:18–25). Alitahiriwa, **Lk.** 2:21. Aliletwa hekaluni, **Lk.** 2:22–38. Alitembelewa na mamajusi, **Mt.** 2:1–12. Yusufu na Maria walikimbia pamoja naye hadi Misri, **Mt.** 2:13–18. Aliletwa Nazarathi, **Mt.** 2:19–23. Alitembelea hekaluni katika umri wa miaka kumi na miwili, **Lk.** 2:41–50. Alikuwa na kaka na dada zake, **Mt.** 13:55–56 (Mk. 6:3). Alibatizwa, **Mt.** 3:13–17 (Mk. 1:9–11; Lk. 3:21–22). Alijaribiwa na ibilisi, **Mt.** 4:1–11 (Mk. 1:12–13; Lk. 4:1–13). Aliwaita wanafunzi wake, **Mt.** 4:18–22 (Mt. 9:9; Mk. 1:16–20; 2:13–14; Lk. 5:1–11, 27–28; 6:12–16; Yn. 1:35–51). Aliwapa mamlaka wale Kumi na Wawili, **Mt.** 10:1–4 (Mk. 3:13–19; Lk. 6:12–16). Alitoa Mahubiri ya Mlimani, **Mt.** 5–7. Alitabiri mauti yake na ufufuko, **Mt.** 16:21 (Mt. 17:22–23; 20:17–19; Mk. 8:31; 9:30–32; 10:32–34; Lk. 9:22; 18:31–34). Aligeuka sura, **Mt.** 17:1–9 (Mk. 9:2–8; Lk. 9:28–36). Aliwatuma wale sabini, **Lk.** 10:1–20. Aliingia Yerusalemu kwa shangwe, **Mt.** 21:1–11 (Mk. 11:1–11; Lk. 19:29–40; Yn. 12:12–15). Alianzisha sakramenti, **Mt.** 26:26–29 (Mk. 14:22–25; Lk. 22:19–20). Aliteseka na kusali katika Gethsemani, **Mt.** 26:36–46 (Mk. 14:32–42; Lk. 22:39–46). Alisalitiwa, kukamatwa, na kukimbiwa, **Mt.** 26:47–56 (Mk. 14:43–53; Lk. 22:47–54; Yn. 18:2–13). Alisulubiwa, **Mt.** 27:31–54 (Mk. 15:20–41; Lk. 23:26–28, 32–49; Yn. 19:16–30). Alifufuka, **Mt.** 28:1–8 (Mk. 16:1–8; Lk. 24:1–12; Yn. 20:1–10). Alionekana baada ya ufufuko wake, **Mt.** 28:9–20 (Mk. 16:9–18; Lk. 24:13–48; Yn. 20:11–31; Mdo. 1:3–8; 1 Kor. 15:5–8). Alipaa mbinguni, **Mk.** 16:19–20 (Lk. 24:51–53; Mdo. 1:9–12).

Alionekana kwa Wanefi, **3 Ne.** 11:1–17 (3 Ne. 11–26).

Alionekana kwa Joseph Smith, **JS—H** 1:15–20.

Kichwa cha Kanisa: Kristo ndiye kichwa cha Kanisa, **Efe.** 5:23 (Efe. 1:22; 4:15). Yeye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha Kanisa, **Kol.** 1:18.

Hili ndilo Kanisa langu, **Mos.** 26:22 (Mos. 27:13). Kristo alikuwa ndiye mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yao, **Moro.** 6:1–4.

Kanisa hili Mimi nimelianzisha, **M&M** 33:5 (3 Ne. 27:3–8).

Kujichukulia jina la Yesu Kristo juu yetu: Hakuna jina jingine litupasalo sisi kuokolewa kwalo, **Mdo.** 4:12 (2 Ne. 31:21). Mitume walifurahi kwa sababu walihesabiwa kuwa wamestahili kuaibishwa kwa ajili ya jina lake, **Mdo.** 5:38–42. Hii ndiyo amri yake, Kwamba tuliamini jina la Mwana wake Yesu Kristo, **1 Yoh.** 3:23.

Mtashuhudia ya kwamba mko radhi kujichukulia juu yenu jina la Kristo kwa ubatizo, **2 Ne.** 31:13. Ningeliwataka ninyi mjichukulie juu yenu jina la Kristo, **Mos.** 5:6–12 (Mos. 1:11). Yeyote aliyetamani kujichukulia juu yake jina la Kristo alijiunga na Kanisa la Mungu, **Mos.** 25:23. Wale wote waliokuwa waumini wa kweli katika Kristo walijichukulia juu yao jina la Kristo, **Alma** 46:15. Mlango wa mbinguni u wazi kwa wale watakaao katika jina la Yesu Kristo, **Hel.** 3:28. Heri yule apatikanaye kuwa yu mwaminifu katika jina langu ile siku ya mwisho, **Eth.** 4:19. Wako tayari kujichukulia juu yao jina la mwana, **Moro.** 4:3 (M&M 20:77).

Jichukulie juu yako jina la Kristo, **M&M** 18:21–25.

Kuonekana kwa Kristo baada ya kifo: Yesu alipofufuka, kwanza alimtokea Maria, **Mk.** 16:9 (Yn. 20:11–18). Yesu alitembea na kuzungumza na wawili kati ya wanafunzi wake katika barabara iendayo Emau, **Lk.** 24:13–34. Yesu aliwatokea Mitume, ambao walishikashika mikono na miguu yake, **Lk.** 24:36–43 (Yn. 20:19–20). Yesu alimtokea Tomaso, **Yn.** 20:24–29. Yesu aliwatokea wanafunzi wake katika bahari ya Tiberia, **Yn.** 21:1–14. Yesu alihudumu kwa siku arobaini baada ya ufufuko wake, **Mdo.** 1:2–3. Stefano alimwona Yesu amesisima upande wa mkono wa kuume wa Mungu, **Mdo.** 7:55–56. Yesu alimtokea Sauli, **Mdo.** 9:1–8 (TJS, Mdo. 9:7; Mdo. 26:9–17). Kristo alionekana kwa watu zaidi ya 500, **1 Kor.** 15:3–8.

Yesu Kristo alijionyesha mwenyewe kwa watu wa Nefi, **3 Ne.** 11:1–17. Watu 2500 walimwona na kumsikia Yesu, **3 Ne.** 17:16–25. Mormoni alitembelewa na Bwana, **Morm.** 1:15.

Joseph Smith na Sidney Rigdon walimwona Yesu akiwa mkono wa kuume wa Mungu, **M&M** 76:22–23. Joseph Smith na Oliver Cowdery walimwona Bwana katika Hekalu la Kirtland, **M&M** 110:1–4.

Joseph Smith alimwona Yesu, **JS—H** 1:15–17.

Kuwepo kwa Kristo kabla ya kuzaliwa duniani: Bwana akamtokea Abramu, **Mwa.** 12:7 (Mwa. 17:1; 18:1; Ibr. 2:6–8). Bwana akasema na Musa uso kwa uso, **Ku.** 33:11 (Kum. 34:10; Musa 1:1–2). Nalimwona Bwana amesimama juu ya madhabahu, **Amo.** 9:1.

Hapo mwanzo, Neno alikuwa pamoja na Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, na akakaa miongoni mwenu, **Yn.** 1:1, 14 (1 Yoh. 1:1–3). Kabla Ibrahimu hajakuweko, MIMI niko, **Yn.** 8:58. Nitukuze mimi kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako, **Yn.** 17:5.

Isaya amini alimwona Mkombozi wangu kama vile mimi na ndugu yangu Yakobo tulivyomwona, **2 Ne.** 11:2–3. Kesho naja ulimwenguni, **3 Ne.** 1:12–14. Kristo alikuwako kabla ya ulimwengu kuanza, **3 Ne.** 26:5 (Yn. 6:62). Kama nionekanavyo kwako ndivyo nitakavyoonekana kwa watu wangu katika mwili, **Eth.** 3:14–17.

Henoko alimwona Bwana na alitembea pamoja naye, **M&M** 107:48–49.

Mwana wangu Mpendwa, aliyekuwa Mpendwa wangu na Mteule tangu mwanzo, **Musa** 4:2. Bwana akasema: Nimtume nani? Na mmoja akasema kama Mwana wa Mtu: Niko hapa, nitume mimi, **Ibr.** 3:27.

Mamlaka: Na utawala utakuwa begani mwake, **Isa.** 9:6 (2 Ne. 19:6).

Yesu alifundisha kama mtu mwenye mamlaka, **Mt.** 7:28–29 (Mk. 1:22). Mwana wa Mtu anao uwezo wa kusamehe dhambi hapa duniani, **Mt.** 9:6. Yesu aliamuru mapepo wachafu kwa mamlaka nao walimtii, **Mk.** 1:27 (Lk. 4:33–36). Yesu aliwatawaza wale kumi na wawili wawe na uwezo, **Mk.** 3:14–15. Neno la Yesu lilikuwa na nguvu, **Lk.** 4:32. Baba amekabidhi hukumu zote kwa Mwana, **Yn.** 5:22, 27. Mungu alimpaka mafuta Yesu kwa Roho Mtakatifu na kwa uwezo, **Mdo.** 10:38. Kristo aliteuliwa kabla ya kuwekwa kwa msingi wa ulimwengu, **1 Pet.** 1:20 (Eth. 3:14). Kristo anazo funguo za jehanamu na za mauti, **Ufu.** 1:18.

Wanadamu wote wako chini ya Kristo, **2 Ne.** 9:5. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, ndiye Baba wa mbingu na dunia, Mwumbaji wa vitu vyote tangu mwanzo, **Hel.** 14:12.

Kristo alikuja kwa mapenzi ya Baba ili kufanya mapenzi yake, **M&M** 19:24. Yesu alipokea utimilifu wa utukufu wa Baba; na alipokea uwezo wote, **M&M** 93:3–4, 16–17 (Yn. 3:35–36).

Mfano wa Yesu Kristo: Nimewapa ninyi mfano, **Yn.** 13:15. Mimi ndimi njia, kweli, na uzima, **Yn.** 14:6. Kristo pia aliteswa kwa ajili yetu, akituachia mfano, ili mfuate nyayo zake, **1 Pet.** 2:21.

Isipokuwa mtu amefuata mfano wa Mwana wa Mungu, aliye hai, hawezi kuokolewa, **2 Ne.** 31:16. Ningelipenda muwe wakamilifu hata kama Mimi, **3 Ne.** 12:48. Hivi daima zingateni kufanya, hata kama Mimi nilivyofanya, **3 Ne.** 18:6. Nimeweka mfano kwa ajili yenu, **3 Ne.** 18:16. Kazi ambazo mmeniona nikizifanya nanyi pia mtazifanya, **3 Ne.** 27:21, 27. Wafuasi wa kweli wa Yesu Kristo watakuwa kama yeye, **Moro.** 7:48.

Mifano au ishara za Kristo: Habili alitoa sadaka ya wazao wa kwanza wa wanyama wake, **Mwa.** 4:4 (Musa 5:20). Mchukue mwanao wa pekee Isaka, na ukamtoe sadaka, **Mwa.** 22:1–13 (Yak. [KM] 4:5). Bwana aliwaamuru wana wa Israeli kutoa dhabihu wanakondoo wasio na ila, **Ku.** 12:5, 21, 46 (Hes. 9:12; Yn. 1:29; 19:33; 1 Pet. 1:19; Ufu. 5:6).

Huu ndiyo mkate ambao Bwana amewapa ninyi kula, **Ku.** 16:2–15 (Yn. 6:51). Lipige jabali, nalo litatoa maji, ili watu wapate kunywa, **Ku.** 17:6 (Yn. 4:6–14; 1 Kor. 10:1–4). Huyo mbuzi atajichukulia juu yake maovu yao yote, **Law.** 16:20–22 (Isa. 53:11; Mos. 14:11; 15:6–9). Musa akamweka juu nyoka wa shaba nyeupe ili kuwaokoa wale watakaoitazama, **Hes.** 21:8–9 (Yn. 3:14–15; Alma 33:19; Hel. 8:14–15). Yona alikuwa ndani ya tumbo la yule nyangumi kwa siku tatu, **Yon.** 1:17 (Mt. 12:40).

Jambo hili ni mfano wa dhabihu ya Mzaliwa Pekee wa Baba, **Musa** 5:4–8.

Mwamuzi: Atauhukumu ulimwengu kwa haki, **Zab.** 9:8 (3 Ne. 27:16). Anakuja aihukumu dunia, **Zab.** 96:13. Mungu atawahukumu wenye haki na walio waovu, **Mh.** 3:17. Atahukumu kati ya mataifa, **Isa.** 2:4 (Mika 4:3; 2 Ne. 12:4). Kwa haki atawahukumu maskini, **Isa.** 11:2–4.

Baba amekabidhi hukumu yote kwa Mwana, **Yn.** 5:22. Kama ninahukumu, hukumu yangu ni ya kweli, **Yn.** 8:16. Alitawazwa na Mungu kuwa mwamuzi wa walio hai na wafu, **Mdo.** 10:42 (2 Tim. 4:1). Mungu atazihukumu siri za wanadamu kupitia Yesu Kristo, **Rum.** 2:16. Sisi sote tutasimama mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, **Rum.** 14:10 (2 Kor. 5:10; Alma 12:12; Morm. 3:20; 7:6; Eth. 12:38; M&M 135:5).

Wanadamu wote huja kwa Mungu ili wahukumiwe naye kulingana na ukweli na utakatifu uliomo ndani yake, **2 Ne.** 2:10. Kusimama mbele ya Mungu ili kuhukumiwa kulingana na matendo, **Alma** 5:15 (Alma 12:15; 33:22; 3 Ne. 27:14).

Mungu na Kristo ndiyo waamuzi wa wote, **M&M** 76:68.

Unabii juu ya Kuzaliwa na Kifo cha Yesu Kristo: Bikira atachukua mimba na atazaa mwana, **Isa.** 7:14 (1 Ne. 11:13–20). Kutoka Bethlehemu atatokea mtawala katika Israeli, **Mika** 5:2.

Samweli Mlamani alitoa unabii kuwa mchana, usiku, mchana wa mwanga; nyota mpya; na ishara nyinginezo, **Hel.** 14:2–6. Samweli Mlamani alitoa unabii kuhusu giza, mngurumo na radi, na kutetemeka kwa dunia, **Hel.** 14:20–27. Ishara za kuzaliwa kwa Yesu zilitimia, **3 Ne.** 1:15–21. Ishara za kifo cha Yesu zilitimia, **3 Ne.** 8:5–23.

Ushuhuda uliotolewa juu ya Yesu Kristo: Paulo alishuhudia kwamba Yesu ndiye Kristo, **Mdo.** 18:5. Hata mapepo wabaya walishuhudia kwamba walimjua Yesu, **Mdo.** 19:15. Hapana mtu awezaye kusema kwamba Yesu ni Bwana isipokuwa kwa Roho Mtakatifu, **1 Kor.** 12:3. Kila goti litapiga na kila ulimi utakiri kwamba Yesu Kristo ni Bwana, **Flp.** 2:10–11.

Tunazungumza juu ya Kristo, tunafurahia katika Kristo, tunahubiri juu ya Kristo, tunatoa unabii juu ya Kristo, **2 Ne.** 25:26. Kitabu cha Mormoni ni kwa kuwathibitishia Myahudi na Myunani kwamba Yesu ndiye Kristo, **2 Ne.** 26:12 (Ukurasa wa jina la Kitabu cha Mormoni). Manabii na maandiko matakatifu yanamshuhudia Kristo, **Yak. (KM)** 7:11, 19. Mtafuteni huyu Yesu ambaye manabii na mitume wameandika juu yake, **Eth.** 12:41.

Tulimwona na kusikia sauti ikimshuhudia kwamba yeye ndiye Mwana Pekee, **M&M** 76:20–24. Na huu ndiyo uzawa wa milele—kumjua Mungu na Yesu Kristo, **M&M** 132:24.

Tunaamini katika Mungu Baba wa Milele, na katika Mwanawe, Yesu Kristo, **M ya I** 1:1. Tunaamini kwamba Kristo atatawala yeye mwenyewe duniani, **M ya I** 1:10.

Utawala wa Kristo katika milenia: Utawala utakuwa begani mwake, **Isa.** 9:6 (2 Ne. 19:6). Nitakaa kati yako, asema Bwana, **Zek.** 2:10–12 (Zek. 14:9).

Mungu atampa Yesu kiti cha enzi cha Daudi baba yake, **Lk.** 1:30–33. Kristo atatawala milele na milele, **Ufu.** 11:15. Watakatifu watatawala pamoja na Kristo kwa miaka elfu moja, **Ufu.** 20:4 (M&M 76:63).

Kwa sababu ya haki ya watu, Shetani

hatakuwa na uwezo, **1 Ne.** 22:26 (Ufu. 20:1–3).

Nitakaa katika haki pamoja na wanadamu duniani kwa miaka elfu moja, **M&M** 29:11 (M&M 43:29–30). Mzitii mamlaka zilizopo, hadi atawalapo mwenye haki ya kutawala, **M&M** 58:22 (1 Kor. 15:25).

Kristo atatawala yeye mwenyewe juu ya dunia, **M ya I** 1:10 (Isa. 32:1).

Utukufu wa Yesu Kristo: Utukufu wa Bwana ukajaza hema takatifu, **Ku.** 40:34–38. Dunia yote imejaa utukufu wake, **Isa.** 6:3 (2 Ne. 16:3). Utukufu wa Bwana umekuja juu yenu, **Isa.** 60:1–2.

Mwana wa Mtu atakuja katika utukufu wa Baba yake, **Mt.** 16:27. Unitukuze mimi kwa utukufu ule niliokuwa nao pamoja nawe kabla ya ulimwengu kuwako, **Yn.** 17:5.

Mtakatifu wa Israeli lazima atawale kwa utukufu mkuu, **1 Ne.** 22:24. Tulikuwa na tumaini la utukufu wake, **Yak. (KM)** 4:4. Mwana wa Mungu yu aja katika utukufu wake, **Alma** 5:50. Alielezea mambo yote, kutoka mwanzo hadi atakapokuja katika utukufu wake, **3 Ne.** 26:3.

Mitume wangu watasimama wakiwa wamevikwa katika utukufu hata kama vile Mimi nilivyo, **M&M** 29:12 (M&M 45:44). Tuliuona utukufu wa Mwana, katika mkono wa kuume wa Baba, **M&M** 76:19–23. Yohana aliona na kutoa shuhuda juu ya utimilifu wa utukufu wangu, **M&M** 93:6 (Yn. 1:14). Uso wake uling'ara kupita mwangaza wa jua, **M&M** 110:3.

Utukufu wake ulikuwa juu yangu, nami nikauona uso wake, **Musa** 1:1–11. Hii ndiyo kazi yangu na utukufu wangu, **Musa** 1:39.

Yethro. *Ona pia* Musa

Mwana mfalme na kuhani wa Midiani katika Agano la Kale aliyempa makazi Musa baada ya Musa kutoroka kutoka Misri. Pia anaitwa Reueli (Ku. 2:18). Baadaye Musa alioa binti wa Yethro aliyeitwa Zipora (Ku. 3:1; 4:18; 18:1–12). Yethro alimfundisha Musa kunaibisha mamlaka, (Ku. 18:13–27). Musa alipokea Ukuhani wa Melkizedeki kutoka kwa Yethro (M&M 84:6–7).

Yezebeli. *Ona pia* Ahabu

Mwanamke mwovu katika Agano la Kale kutoka nchi ya Foinike. Alikuwa mke wa Ahabu (1 Fal. 16:30–31), mfalme wa Israeli aliyetawala wakati Eliya alipokuwa nabii.

Kuolewa kwa Yezebeli kwa Ahabu, ni tukio moja kubwa zaidi kuliko tukio jingine lolote, lililosababisha kuanguka kwa ufalme wa kaskazini wa Israeli; Yezebeli alianzisha katika Israeli aina mbaya zaidi ya zote ya ibada ya sanamu kutoka katika nchi yake badala ya kumwabudu Yehova (1 Fal. 18:13, 19).

Yezebeli aliwaua manabii wengi wa Mungu, **1 Fal.** 18:4. Yezebeli alijaribu kumwua Eliya, **1 Fal.** 19:1–3. Uovu wa Yezebeli uliishia kwa mauti yake ya kutisha, **2 Fal.** 9:30–37.

Yoeli

Nabii katika nchi ya Yuda katika Agano la Kale. Siku za maisha yake hazina uhakika—yawezekana kuwa aliishi katikati ya wakati wa utawala wa Yoashi, kabla ya mwaka 850 K.K. na kurudi kwa kabila la Yuda kutoka utumwani Babeli.

Kitabu cha Yoeli: Kitabu hiki kinaelezea juu ya unabii uliotolewa na Yoeli baada ya nchi ya Yuda kuwa imepigwa kwa ukame mkali na nzige (Yoe. 1:4–20). Yoeli aliwahakikishia watu kuwa kupitia toba wangeliweza tena kupokea baraka za Mungu (Yoe. 2:12–14).

Mlango wa 1 ni wito kwa ajili ya kusanyiko la kiroho katika nyumba ya Bwana. Mlango wa 2 unasimulia juu ya vita na ukiwa utakaoitangulia Milenia. Mlango wa 3 unazungumzia juu ya siku za mwisho na inatamka kwa dhati kwamba mataifa yote yatakuwa katika vita lakini mwishowe Bwana atakaa katika Sayuni.

Petro alinukuu unabii wa Yoeli wa kumwagwa kwa roho katika siku ile ya Pentekoste (Yoe. 2:28–32; Mdo. 2:16–21). Malaika Moroni pia alinukuu mistari hii hii kwa Joseph Smith. (JS—H 1:41).

Yohana, Mwana wa Zebedayo.
Ona pia Injili, Vitabu vya Biblia; Mtume; Ufunuo wa Yohana; Ukuhani wa Melkizedeki; Viumbe waliobadilishwa

Mmoja wa Mitume Kumi na Wawili katika Agano Jipya, mwana wa Zebedayo, na ni kaka wa Yakobo. Katika maisha yake ya awali yeye alikuwa mvuvi (Mk. 1:17–20). Huenda yeye ni yule mwanafunzi ambaye hakutajwa wa Yohana Mbatizaji aliyetajwa katika Yohana 1:40. Baadaye alipokea wito wa kuwa mwanafunzi wa Yesu Kristo (Mt. 4:21–22; Lk. 5:1–11). Aliandika Injili ya Yohana, nyaraka tatu, na kitabu cha Ufunuo. Alikuwa mmoja wa wale watu watatu walio kuwa na Bwana wakati wa kufufuliwa kwa binti wa Yairo (Mk. 5:35–42), katika Mlima wa Kugeuka Sura (Mt. 17:1–9), na katika Gethsemani (Mt. 26:36–46). Katika maandiko yake yeye mwenyewe anajieleza kama yule mwanafunzi aliyependwa na Yesu (Yn. 13:23; 21:20) na kama "mwanafunzi mwingine" (Yn. 20:2–8). Yesu pia alimwita yeye na kaka yake kwa jina la Boanerge, maana yake, "wana wa ngurumo" (Mk. 3:17). Kuna marejeo ya mara kwa mara kwake katika taarifa za Kusulubiwa na Ufufuko (Lk. 22:8; Yn. 18:15; 19:26–27; 20:2–8; 21:1–2). Yohana baadaye aliwekwa kizuizini huko Patmo, mahali ambako aliandika kitabu cha Ufunuo. (Ufu. 1:9).

Yohana anatajwa mara kwa mara katika ufunuo wa siku za mwisho (1 Ne. 14:18–27; 3 Ne. 28:6; Eth. 4:16; M&M 7; 27:12; 61:14; 77; 88:141). Mistari hii inathibitisha taarifa iliyoandikwa kibiblia juu ya Yohana na pia inatoa utambuzi wa ukuu wake na umuhimu wa kazi ambayo Bwana amempa kufanya duniani katika nyakati za Agano Jipya na katika siku za mwisho. Maandiko ya siku za mwisho yanafafanua kwamba Yohana hakufa bali aliruhusiwa kubakia duniani kama mtumishi mhudumu hadi wakati wa Ujio wa Pili wa Bwana (Yn. 21:20–23; 3 Ne. 28:6–7; M&M 7).

Nyaraka za Yohana: Ingawa mwandishi wa nyaraka hizi tatu hajitaji mwenyewe kwa jina, lugha inafanana kwa nguvu sana na ile ya Yohana Mtume kwamba inasadikiwa kuwa ameandika zote tatu.

1 Yohana 1 anawaasa Watakatifu kupata ushirika na Mungu. Mlango wa 2 anasisitiza kwamba Watakatifu wamjue Mungu kwa utii na anawafundisha wasiupende ulimwengu. Mlango wa 3 anawaita watu wote kuwa watoto wa Mungu na wapendane. Mlango wa 4 anaelezea kwamba Mungu ni upendo na hukaa ndani ya wale Wampendao. Mlango wa 5 anaelezea kwamba Watakatifu huzaliwa kwa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo.

2 Yohana inafanana na 1 Yohana. Katika hizo Yohana anafurahi kwa sababu ya uaminifu wa watoto wa "bibi mteule."

3 Yohana anamsifu mtu aliyeitwa Gayo kwa uaminifu wake na kwa msaada wake kwa wale wenye kupenda ukweli.

Injili ya Yohana: Katika kitabu hiki cha Agano Jipya, Yohana Mtume alishuhudia kwamba (1) Yesu ndiye Kristo au Masiya na (2) Yesu ndiye Mwana wa Mungu (Yn. 20:31). Matukio kutoka katika maisha ya Yesu ambayo anayaelezea yamechaguliwa na kupangwa kwa uangalifu kwa kusudi hili. Kitabu kinaanza kwa maelezo ya hali ya Kristo kabla ya kuzaliwa: alikuwa pamoja na Mungu, alikuwa Mungu, na alikuwa ndiye mwumbaji wa vitu vyote. Alizaliwa katika mwili kama Mwana Pekee wa Baba. Yohana anafuatilia historia ya huduma ya Yesu, alisisitiza sana uungu Wake na ufufuko Wake kutoka kwa wafu. Kwa uwazi kabisa anathibitisha kwamba Yesu ndiye Mwana wa Mungu,

aliyeshuhudiwa kwa miujiza, na mashahidi, na manabii, na kwa sauti ya Kristo mwenyewe. Yohana anafundisha kwa kutofautisha nuru na giza, ukweli na uongo, wema na uovu, Mungu na ibilisi. Pengine hakuna taarifa nyingine iliyoandikwa ambamo ndani yake utakatifu wa Yesu na ukosefu wa imani wa watawala wa Kiyahudi umetamkwa wazi kabisa kama hii.

Yohana aliandika hasa juu ya huduma ya Kristo katika Yuda, hususani wiki ile ya mwisho ya huduma Yake katika mwili wenye kufa, wakati Mathayo, Marko, na Luka waliandika hasa juu ya huduma yake katika Galilaya. Mambo kadhaa kutoka katika injili hii yamefafanuliwa kwa ufunuo wa siku za mwisho (M&M 7 na M&M 88:138–141).

Kwa orodha ya matukio katika maisha ya Mwokozi yaliyoelezwa katika Injili ya Yohana, ona Upatanifu wa Injili katika kiambatisho.

Kitabu cha Ufunuo: Ona Ufunuo wa Yohana

Yohana Mbatizaji. *Ona pia* Elia; Ukuhani wa Haruni

Mwana wa Zakaria na Elizabethi katika Agano Jipya. Yohana alitumwa kuwaandaa watu kwa kumpokea Masiya (Yn. 1:19–27). Alishikilia funguo za Ukuhani wa Haruni na alimbatiza Yesu Kristo.

Isaya na wengineo walitoa unabii juu ya huduma ya Yohana, **Isa.** 40:3 (Mal. 3:1; 1 Ne. 10:7–10; 2 Ne. 31:4).

Aliwekwa gerezani na akakatwa kichwa, **Mt.** 14:3–12 (Mk. 6:17–29). Gabrieli alitangaza kuzaliwa na huduma ya Yohana kwa Zakaria, **Lk.** 1:5–25. Yesu alifundisha kuwa Yohana Mbatizaji alikuwa nabii mkuu, **Lk.** 7:24–28. Alimtambua Yesu kama ni Mwana wa Mungu, **Yn.** 1:29–34. Wanafunzi wa Yohana wakaja kuwa wanafunzi wa Yesu, **Yn.** 1:25–29, 35–42 (Mdo. 1:21–22). Hakufanya muujiza, **Yn.** 10:41.

Kama mtu mfufuka, alitumwa kuwatawaza Joseph Smith na Oliver Cowdery katika Ukuhani wa Haruni, **M&M** 13 (M&M 27:7–8; JS—H 1:68–72). Alitawazwa na malaika wakati alipokuwa na umri wa siku nane, **M&M** 84:28.

Yona. *Ona pia* Ninawi

Nabii wa Agano la Kale aliyeitwa na Bwana kuhubiri toba katika mji wa Ninawi (Yon. 1:1–2).

Kitabu cha Yona: Kitabu katika Agano la Kale ambacho kinaelezea juu ya tukio moja katika maisha ya Yona. Yona yawezekana hakuandika kitabu hiki yeye mwenyewe. Wazo kuu la kitabu cha Yona ni kwamba Yehova anatawala kila mahali na upendo Wake hauzuiliwi katika taifa moja au watu fulani tu.

Katika mlango wa 1, Bwana anamwita Yona kwenda kuhubiri Ninawi. Badala ya kufanya kama Bwana alivyomwamuru, Yona alitoroka kwa mashua na akamezwa na samaki mkubwa. Katika Mlango wa 2, Yona alisali kwa Bwana, na yule samaki akamtapika Yona nje kwenye ardhi kavu. Mlango wa 3 unaandikwa kuwa Yona alikwenda Ninawi na akatoa unabii wa kuanguka kwa mji huo. Hata hivyo, watu wale wakatubu. Katika Mlango wa 4, Bwana anamkanya Yona kwa kukasirika kwa vile Bwana aliwaokoa wale watu.

Yesu alifundisha kwamba Yona kumezwa na samaki kumetumika kama ishara ya mauti ya Yesu mwenyewe na ufufuko wake (Mt. 12:39–40; 16:4; Lk. 11:29–30).

Yonathani. *Ona pia* Daudi; Sauli, Mfalme wa Israeli

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Sauli, mfalme wa Israeli. Yonathani alikuwa rafiki wa karibu wa Daudi (1 Sam. 13–23; 31).

Yoshua. *Ona pia* Yeriko

Nabii na kiongozi katika Agano la Kale, na mrithi wa Musa. Alizaliwa Misri kabla kutoroka kwa wana wa

Israeli (Hes. 14:26–31). Yeye na Kalebu walikuwa miongoni mwa wapelelezi kumi na wawili waliotumwa Kanani. Wao tu ndiyo waliotoa taarifa nzuri juu ya ile nchi (Hes. 13:8, 16–33; 14:1–10). Alikufa katika umri wa miaka 110 (Yos. 24:29). Yoshua alikuwa mfano mkubwa wa nabii mpiganaji hodari.

Kitabu cha Yoshua: Kitabu hiki kimepewa jina la Yoshua kwa sababu yeye ndiye mtu muhimu ndani yake na siyo kwa sababu yeye alikuwa mtunzi. Mlango wa 1–12 inaelezea kukamatwa kwa Kaanani; mlango wa 13–24 inazungumzia makabila ya Israeli yakigawana nchi na ushauri wa mwisho wa Yoshua.

Mistari miwili maarufu katika kitabu cha Yoshua ni amri ya Bwana kwake ya kuyatafakari maandiko (Yos. 1:8) na wito wa Yoshua kwa watu wa kuwa waaminifu kwa Bwana (Yos. 24:15).

Yosia

Mfalme mwadilifu wa Yuda kutoka mwaka 641–610 K.K. (2 Fal. 22–24; 2 Nya. 34–35). Wakati wa utawala wake, kitabu cha torati kilipatikana katika nyumba ya Bwana (2 Fal. 22:8–13).

Young, Brigham

Mtume wa mwanzoni kabisa katika kipindi hiki na Rais wa pili wa Kanisa la Yesu Kristo la Watakatifu wa Siku za Mwisho. Aliwaongoza Watakatifu kwenda upande wa magharibi kutoka Nauvoo, Illinois, kwenda bonde la Salt Lake na alikuwa mwasisi mkubwa wa miji mipya katika muungano wa magharibi mwa Mataifa ya Marekani.

Brigham Young aliitwa kuwa Rais juu ya Mitume Kumi na Wawili, **M&M** 124:127. Brigham Young alisifiwa kwa kazi zake na alipumzishwa kwa safari za baadaye za nje ya nchi, **M&M** 126. Bwana alimfundisha Brigham Young namna ya kuwaandaa Watakatifu kwa msafara wao wa kuelekea magharibi, **M&M** 136. Brigham Young alikuwa miongoni mwa watu maarufu katika ulimwengu wa roho, **M&M** 138:53.

Yuda. *Ona pia* Biblia; Israeli; Wayahudi

Katika Agano la Kale, ni mwana wa nne wa Yakobo na Lea (Mwa. 29:35; 37:26–27; 43:3, 8; 44:16; 49:8). Yakobo alimbariki Yuda kuwa angekuwa kiongozi wa asili miongoni mwa wana wa Yakobo na kwamba Shilo (Yesu Kristo) angekuwa wa uzao wake (Mwa. 49:10).

Kabila la Yuda: Kabila la Yuda lilichukua uongozi baada ya kuingia na kukaa katika Kaanani. Mpinzani wake mkubwa alikuwa kabila la Efraimu. Musa alilibariki kabila la Yuda (Kum. 33:7). Baada ya utawala wa Sulemani, kabila la Yuda likawa ufalme wa Yuda.

Ufalme wa Yuda: Katika utawala wa Rehoboamu utawala wa Sulemani ulivunjika katika falme mbili tofauti, hasa kwa sababu ya wivu kati ya makabila ya Efraimu na Yuda. Ufalme wa kusini, au ufalme wa Yuda, ilijumuisha ufalme wa Yuda na sehemu kubwa zaidi ya kabila la Benjamini. Yerusalemu yakiwa makao yake makuu. Kwa namna zote ulibaki katika uaminifu zaidi katika kumwabudu Yehova kuliko ulivyofanya ule ufalme wa kaskazini. Yuda ilikuwa imara upande wa kaskazini na mashariki, na mamlaka kuu yalibaki mikononi mwa familia ya Daudi hadi utumwa wa Babilonia. Ufalme wa Yuda ulimudu kudumu kwa miaka 135 baada ya anguko la ufalme wenye watu wengi na wenye nguvu zaidi wa Israeli.

Kijiti cha Yuda: Hii inamaanisha Biblia kama kumbu kumbu ya nyumba ya Yuda (Eze. 37:15–19). Katika siku za mwisho, wakati matawi kadha wa kadha ya nyumba ya Israeli yatakapokuwa yamekusanywa, kumbukumbu zao takatifu pia zitakusanywa pamoja. Kumbu kumbu hizi za maandiko zinakamilishana na kufanya ushuhuda wa umoja kwamba Yesu ndiye Kristo, Mungu wa Israeli na Mungu wa dunia nzima (TJS, Mwa. 50:24–36 [Kiambatisho]; 2 Ne. 3; 29).

Yuda Iskariote

Mmoja wa Mitume Kumi na Wawili wa Yesu katika Agano Jipya (Mt. 10:4; Mk. 14:10; Yn. 6:71; 12:4). Jina lake la ukoo linamaanisha "mtu wa Keriothi." Alitoka katika kabila la Yuda na alikuwa ndiye Mtume pekee ambaye hakuwa Mgalilaya. Yuda alimsaliti Bwana.

Alipokea vipande thelathini vya fedha kwa kumtoa Kristo kwa mmoja wa makuhani wakuu, **Mt.** 26:14–16 (Zek. 11:12–13). Alimsaliti Bwana kwa kumbusu, **Mt.** 26:47–50 (Mk. 14:43–45; Lk. 22:47–48; Yn. 18:2–5). Alijinyonga yeye mwenyewe, **Mt.** 27:5. Shetani aliingia ndani ya Yuda, **Lk.** 22:3 (Yn. 13:2, 26–30). Daudi alinena juu ya usaliti wa Yuda kwa Yesu, **Mdo.** 1:16 (Zab. 41:9).

Yuda, Kaka wa Yakobo

Katika Agano Jipya, ni mmoja wa Mitume Kumi na Wawili wa mwanzoni wa Yesu Kristo (Lk. 6:13–16). Yeye huenda pia alijulikana kama Leboya Thadayo (Mt. 10:2–4).

Yuda, Kaka wa Yesu

Katika Agano Jipya, ni mmoja wa kaka zake Yesu na huenda ndiye mwandishi wa waraka wa Yuda (Mt. 13:55; Yuda 1:1).

Waraka wa Yuda: Kitabu hiki ni nyaraka kutoka kwa Yuda kwenda kwa Watakatifu fulani ambao walikuwa wakidhoofishwa katika imani. Walikuwa wakidhoofishwa na wale miongoni mwao waliokuwa wakidai kuwa ni Wakristo lakini wakitenda ibada za kipagani na wakidai wana ruhusa ya kutotii sheria za maadili. Yuda alitamani kuwaamsha Watakatifu juu ya hali yao ya hatari ya kiroho na kuwatia moyo ili wabaki kuwa waaminifu.

Mistari kadhaa muhimu katika Kitabu cha Yuda ni mstari wa 6, ambayo unakumbusha vita vya mbinguni na kutupwa nje kwa Lusiferi na malaika zake kutoka katika hali ile kabla ya kuzaliwa (Ibr. 3:26–28), na mstari 14–15, ambayo inauelezea unabii uliofanywa na Henoko.

Yusufu, Kijiti Cha. *Ona* Efraimu—Kijiti cha Efraimu au Yusufu; Kitabu cha Mormoni

Yusufu, Mume wa Maria. *Ona pia* Maria, Mama wa Yesu; Yesu Kristo

Mume wa Maria, mama wa Yesu. Yusufu alikuwa ni wa ukoo wa Daudi (Mt. 1:1–16; Lk. 3:23–38) na aliishi Nazareti. Alimposa Maria. Muda mfupi kabla ya ndoa yao, Maria alitembelewa na malaika Gabrieli, aliyemtangazia kwamba Maria amechaguliwa kuwa mama wa Mwokozi (Lk. 1:26–35). Yusufu pia alipokea ufunuo wa kuzaliwa huku kwa kimungu (Mt. 1:20–25).

Maria alikuwa ndiye mzazi pekee wa kidunia wa Yesu kwa sababu Mungu Baba ndiye aliyekuwa baba wa Yesu. Lakini Wayahudi walimdhania Yusufu kuwa ndiye baba wa Yesu, naye Yesu alimheshimu kama ndiye babaye (Lk. 2:48, 51). Akiwa ameonywa kwa ndoto za mbinguni, Yusufu alilinda uhai wa mtoto mchanga Yesu kwa kukimbilia Misri (Mt. 2:13–14). Baada ya kufa kwa Herode, malaika akamwambia Yusufu amchukue mtoto Kristo warudi Israeli (Mt. 2:19–23).

Yusufu, Mwana wa Yakobo. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mwana mzaliwa wa kwanza wa Yakobo na Raheli (Mwa. 30:22–24; 37:3).

Yusufu alijipatia haki ya uzaliwa wa kwanza katika Israeli kwa sababu Reubeni, mwana mzaliwa wa kwanza wa mke wa kwanza wa Yakobo, alipoteza haki hii kwa uvunjaji wa sheria (1 Nya. 5:1–2). Kwa sababu alikuwa mtu mwenye kustahili, Yusufu, kama mwana mzaliwa wa kwanza wa mke wa pili wa Yakobo, alikuwa ndiye anayefuatia katika mstari kwa ajili ya baraka hiyo. Yusufu pia alipokea baraka kutoka kwa baba yake muda mfupi tu kabla ya Yakobo kufa (Mwa. 49:22–26).

Yusufu alikuwa mtu mwadilifu sana "mwangalifu na mwenye hekima" (Mwa. 41:39). Kumkatalia kwake mke wa Potifa

ni mfano wa imani, usafi wa kimwili, na uadilifu wa kibinafsi (Mwa. 39:7–12). Katika Misri, wakati Yusufu alipofunua utambulisho wake wa kweli kwa kaka zake, aliwashukuru badala ya kuwashutumu kwa jinsi walivyomtendea yeye. Aliamini matendo yao yamesaidia kutimiza mapenzi matakatifu ya Mungu (Mwa. 45:4–15).

Ufunuo wa siku za mwisho unafunua huduma ya familia ya Yusufu katika siku za mwisho (TJS, Mwa. 50:24–38 [Kiambatisho]; 2 Ne. 3:3–24; 3 Ne. 20:25–27).

Yakobo alimpenda sana Yusufu na akampa kanzu ya rangi nyingi, **Mwa.** 37:3. Kwa sababu ya wivu, kaka zake Yusufu wakaanza kumchukia na kupanga njama za kumwua, lakini badala yake wakamwuza kwa wafanya biashara, waliokuwa njiani wakienda Misri, **Mwa.** 37:5–36. Akiwa Misri, Bwana alimneemesha Yusufu na akawa mtawala wa nyumba ya Potifa, **Mwa.** 39:1–4. Mke wa Potifa alidanganya, akisema kuwa Yusufu alijaribu kumtongoza yeye; Yusufu alihukumiwa kimakosa na akawekwa gerezani, **Mwa.** 39:7–20. Yusufu alifasiri ndoto za mhudumu mkuu na mwoka mikate wa nyumba ya Farao, **Mwa.** 40. Farao akaanza kumpenda Yusufu kwa sababu Yusufu alifasiri moja kati ya ndoto za Farao; akamfanya Yusufu kuwa mtawala juu ya Misri, **Mwa.** 41:14–45. Efraimu na Manase walizaliwa, **Mwa.** 41:50–52. Yusufu aliungana tena pamoja na baba yake na kaka zake, **Mwa.** 45–46. Yusufu alikufa Misri akiwa na umri wa miaka 110, **Mwa.** 50:22–26.

Yusufu wa Arimathaya

Yusufu wa Arimathaya alikuwa mshirika wa Sanhedrini, mwanafunzi wa Kristo, na Muisraeli aliyekuwa tajiri na mwaminifu ambaye hakushiriki katika kumhukumu Bwana wetu. Baada ya Kusulubiwa, Yusufu aliomba mwili wa Mwokozi aliufunga katika nguo zilizo safi na akamweka katika kaburi lake mwenyewe la mfano wa pango (Mt. 27:57–60; Mk. 15:43–46; Lk. 23:50–53; Yn. 19:38–42).

Zaburi. *Ona pia* Daudi; Muziki

Mashairi au nyimbo zilizotungwa kwa mwongozo wa Mungu.

Kitabu cha Zaburi: Kitabu cha Agano la Kale ambacho kinamkusanyiko wa zaburi, nyingi kati ya hizo ni juu ya Kristo. Kitabu cha Zaburi kimenukuliwa mara kwa mara katika Agano Jipya.

Daudi aliandika nyingi ya Zaburi hizi. Zaburi ziliandikwa kama sifa kwa Mungu. Nyingi zilitungwa kwa mtindo wa muziki.

Zaka. *Ona* Lipa zaka, Zaka

Zakaria. *Ona pia* Elisabeti; Yohana Mbatizaji

Katika Agano Jipya, ni baba wa Yohana Mbatizaji. Zakaria alishikilia ofisi ya kuhani na alitenda kazi katika hekalu.

Zakaria aliuawa kati ya patakatifu na madhabahu, **Mt.** 23:35 (Lk. 11:51). Malaika Gabrieli aliwaahidi Zakaria na mke wake Elizabeti, kuwa watapata mwana, **Lk.** 1:5–25 (M&M 27:7). Ulimi wake ukafunguliwa, **Lk.** 1:59–79.

Zaliwa. *Ona pia* Mzaliwa Pekee; Wana na Mabinti za Mungu; Watoto wa Kristo; Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena

Kuzaliwa. Kuzaa ni kujifungua, kuumba kwa kuzaa, au kuleta katika uhai. Katika maandiko, maneno haya mara kwa mara yanatumika ili kumaanisha kuzaliwa na Mungu. Ingawa Yesu Kristo ni mtoto pekee wa kuzaa wa Mungu katika mwili wa kuharibika, watu wote waweza kuwa wazaliwa kiroho wa Kristo kwa kumkubali Yeye, kwa kutii amri Zake, na kwa kuwa watu wapya kwa njia ya uwezo wa Roho Mtakatifu.

Mimi leo nimekuzaa, **Zab.** 2:7 (Mdo. 13:33; Ebr. 1:5–6; 5:5).

Utukufu wake ulikuwa wa Mzaliwa Pekee wa Baba, **Yn.** 1:14 (2 Ne. 25:12; Alma 12:33–34; M&M 76:23). Jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe Pekee, **Yn.** 3:16 (M&M 20:21).

Kristo amewazaa watu wake kiroho, **Mos.** 5:7.

Wale waliozaliwa kwa njia ya Bwana ndiyo Kanisa la Mzaliwa wa Kwanza, **M&M** 93:22.

Zaliwa na Mungu, Zaliwa Tena. *Ona pia* Batiza, Ubatizo; Mwanadamu wa Tabia ya Asili; Mwongofu, Uongofu; Wana na Mabinti za Mungu; Watoto wa Kristo; Zaliwa

Kuwa na Roho wa Bwana husababisha mabadiliko makubwa katika moyo wa mtu kiasi kwamba akawa hana hamu tena ya kufanya uovu, bali akatamani kutafuta mambo ya Mungu.

Nami nitatia roho mpya ndani yenu, **Eze.** 11:19 (Eze. 18:31; 36:26).

Wale waliaminio jina la Kristo walizaliwa, siyo kwa damu, bali kwa Mungu, **Yn.** 1:12–13. Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho, hawezi kuingia katika ufalme wa Mungu, **Yn.** 3:3–7. Twaweza kuzaliwa tena kwa neno la Mungu, **1 Pet.** 1:3–23. Yeyote aliyezaliwa kwa Mungu haendelei katika dhambi, **TJS, 1 Yoh.** 3:9. Kwani yeyote aliyezaliwa na Mungu huushinda ulimwengu, **1 Yoh.** 5:4.

Wale wazaliwao kwa Kristo hufanya agano na Mungu, **Mos.** 3:19; 5:2–7. Watu wote lazima wazaliwe tena; ndiyo, wazaliwe kwa Mungu, **Mos.** 27:25–26 (Alma 5:49). Je, ninyi kiroho mmezaliwa kwa Mungu, **Alma** 5:12–19. Kama ninyi hamjazaliwa tena, hamwezi kuurithi ufalme wa mbinguni, **Alma** 7:14.

Yeyote yule aaminiye maneno yangu atazaliwa kwangu, hata kwa maji na kwa Roho, **M&M** 5:16.

Lazima mzaliwe tena katika ufalme wa mbinguni, **Musa** 6:59.

Zarahemla. *Ona pia* Amoni, wa Uzao wa Zarahemla; Muleki

Katika Kitabu cha Mormoni, Zarahemla inataja kwa (1) mtu aliyeliongoza koloni la Muleki, (2) mji uliopewa jina lake, (3) nchi ya Zarahemla, au (4) watu waliomfuata yeye.

Zarahemla alifurahi kwamba Bwana alikuwa amewapeleka Wanefi, **Omni** 1:14. Zarahemla alitoa nasaba ya baba zao, **Omni** 1:18. Amoni alikuwa wa uzao wa Zarahemla, **Mos.** 7:3, 13. Kanisa lilianzishwa katika mji wa Zarahemla, **Alma** 5:2. Kwa sababu ya wenye haki waovu waliokolewa katika Zarahemla, **Hel.** 13:12. Mji wa Zarahemla uliunguzwa moto wakati wa kifo cha Kristo, **3 Ne.** 8:8, 24.

Zebuluni. *Ona pia* Israeli; Yakobo, Mwana wa Isaka

Katika Agano la Kale, ni mwana wa Yakobo na Lea (Mwa. 30:19–20).

Kabila la Zebuluni: Yakobo alilibariki kabila la Zebuluni (Mwa. 49:13). Kabila la Zebuluni liliungana na Debora na Baraka katika kupigana dhidi ya maadui wa Israeli (Amu. 4:4–6, 10). Pia waliungana na Gidioni katika kupigana na Wamidiani (Amu. 6:33–35).

Zedekia. *Ona pia* Muleki

Katika Agano la Kale, ni mfalme wa mwisho wa Yuda (2 Fal. 24:17–20; 25:2–7). Zedekia alimfunga gerezani nabii Yeremia (Yer. 32:1–5), na Yeremia alitoa unabii juu ya utumwa wa Zedekia (Yer. 34:2–8, 21). Lehi na familia yake waliishi katika Yerusalemu wakati wa mwaka wa kwanza wa utawala wa Zedekia (1 Ne. 1:4). Watoto wote wa Zedekia waliuawa isipokuwa mmoja; mtoto wake Muleki alitorokea Marekani (Yer. 52:10; Omni 1:15; Hel. 8:21).

Zeezromu

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mwanasheria katika Mji wa Amoniha. Alma na Amuleki walitambua kwa njia ya Roho kwamba Zeezromu alikuwa akidanganya. Hatimaye aliongolewa katika injili ya Kristo (Alma 11:21–46; 15:1–12).

Zefania

Nabii wa Agano la Kale aliyeishi wakati wa utawala wa Yosia (639–608 K.K.).

Kitabu cha Zefania: Mlango wa 1 unazungumzia juu ya siku ile inayokuja

itajawa na ghadhabu na matatizo. Mlango wa 2 unawaonya watu wa Israeli kutafuta haki na uvumilivu. Mlango wa 3 unasimulia juu ya Ujio wa Pili wakati mataifa yote yatakapokusanyika kwa ajili ya vita. Bwana, hata hivyo, atatawala katikati yao.

Zekaria

Nabii wa Agano la Kale aliyetoa unabii mwaka takribani 520 K.K. Aliishi wakati mmoja na nabii Hagai (Ezra 5:1; 6:14).

Kitabu cha Zekaria: Kitabu hiki kinatambulika kwa unabii wake juu ya huduma ya Kristo katika mwili wenye kufa na Ujio Wake wa Pili (Zek. 9:9; 11:12–13; 12:10; 13:6). Mlango wa 1–8 ina mfuatano wa maono ya maisha ya baadaye ya watu wa Mungu. Mlango 9–14 ina maono juu ya Masiya, siku za mwisho, kukusanyika kwa Israeli, vita vikuu vya mwisho, na Ujio wa Pili.

Zenifu

Katika Kitabu cha Mormoni, ni mtu aliyeongoza kikundi kilichorudi kwenye nchi ya Nefi; akawa mfalme wao na akawaongoza kwa haki (Mos. 9–10).

Zeno

Nabii wa Israeli katika nyakati za Agano la Kale ambaye unabii wake juu ya huduma ya Kristo unapatikana katika Kitabu cha Mormoni pekee.

Alitoa unabii wa maziko ya Kristo na siku tatu za giza, **1 Ne.** 19:10, 12. Alitabiri kukusanyika kwa Israeli, **1 Ne.** 19:16. Yakobo alinukuu fumbo la Zeno la mti wa mzeituni wa kupandwa na wa porini, **Yak. (KM)** 5. Yakobo aelezea istiari ya Zeno, **Yak. (KM)** 6:1–10. Alifundisha kuhusu sala na kuabudu, **Alma** 33:3–11. Alifundisha kwamba ukombozi huja kupitia Mwana, **Alma** 34:7. Aliuawa kwa sababu ya ushuhuda wake wa ujasiri, **Hel.** 8:19. Alisema juu ya urejesho wa Walamani, **Hel.** 15:11. Alitoa ushuhuda juu ya angamizo wakati wa kifo cha Kristo, **3 Ne.** 10:15–16.

Zenoki

Nabii wa Israeli katika nyakati za Agano la Kale ambaye ametajwa katika Kitabu cha Mormoni pekee.

Alitoa unabii juu ya kifo cha Kristo, **1 Ne.** 19:10. Alisema juu ya Mwana wa Mungu, **Alma** 33:15 (Alma 34:7). Aliuawa kifo cha kishahidi kwa ajili ya ukweli, **Alma** 33:17. Alitoa unabii kuhusu ujio wa Masiya, **Hel.** 8:20.

Zeri ya Giliadi

Ubani wenye harufu nzuri sana au kiungo kitumikacho kutibu vidonda (Mwa. 43:11; Yer. 8:22; 46:11; 51:8). Kichaka kitoacho utomvu ambao kwao zeri ilitengenezwa iliota kwa wingi sana katika Giliadi katika nyakati za Agano la Kale kiasi kwamba zeri ilikuja kujulikana kama "zeri ya Giliadi" (Mwa. 37:25; Eze. 27:17).

Zerubabeli

Katika Agano la Kale, ni wakati Koreshi alipotoa ruhusa kwa Wayahudi kurudi Palestina, Zerubabeli aliteuliwa kuwa gavana au mwakilishi wa nyumba ya kifalme wa Kiyahudi. Jina lake la Kiajemi lilikuwa Sheshabaza (Ezra 1:8). Alihusika katika kulijenga upya hekalu katika Yerusalemu (Ezra 3:2, 8; 5:2).

Zipora. *Ona pia* Musa

Katika Agano la Kale, mke wa Musa na binti wa Yethro (Ku. 2:21; 18:2).

Zoramu, Wazoramu

Katika Kitabu cha Mormoni, alikuwa mtumishi wa Labani ambaye aliungana pamoja na Nefi na Lehi kuja katika nchi ya ahadi (1 Ne. 4:31–38). Kwa sababu ya uaminifu wa Zoramu, Lehi alimbariki pamoja na wanawe Lehi mwenyewe (2 Ne. 1:30–32). Wazao wake walijulikana kama Wazorami (Yak. [KM] 1:13).

WENDO

Utaratibu mfupi ufuatao waweza kukupa ufahamu wa mfuatano wa matukio katika nyakati za Biblia na Kitabu cha Mormoni. Tarehe nyingi ni za kukadiria, hususani katika nyakati za Agano la Kale.

Matukio katika siku za mapatriaki wa Mwanzo
(Kwa sababu ya ugumu katika kujua tarehe halisi ya matukio katika sehemu hii, tarehe hazikutolewa.)

K.K. (au K.K.K.—Kabla ya Kuzaliwa kwa Kristo)

4000 Adamu alianguka.

Henoko alihudumu.

Nuhu alihudumu; gharika ikaja duniani.

Mnara wa Babeli ulijengwa; Wayaredi walisafiri kwenda Nchi ya Ahadi.

Melkizedeki alihudumu.

Nuhu alikufa.

Abramu (Ibrahimu) alizaliwa.

Isaka alizaliwa.

Yakobo alizaliwa.

Yusufu alizaliwa.

Yusufu aliuzwa Misri.

Yusufu atokea mbele ya Farao.

Yakobo (Israeli) na familia yake waliteremka kwenda Misri.

Yakobo (Israeli) alikufa.

Yusufu alikufa.

Musa alizaliwa.

Musa aliwaongoza wana wa Israeli kutoka Misri (ndiyo Kutoka).

Musa alihamishwa.

Yoshua alikufa.

Baada ya kufa Musa, kipindi cha waamuzi kikaanza, mwamuzi wa kwanza akiwa Othinieli na wa mwisho ni Samweli; mpangalio na tarehe za waliosalia hazifahamiki kwa uhakika.

Sauli alipakwa mafuta kuwa mfalme.

Matukio ya Muungano wa Ufalme wa Israeli

1095 Kuanza kwa utawala wa Sauli.

1063 Daudi alipakwa mafuta na Samweli kuwa mfalme.

1055 Daudi akawa mfalme katika Hebroni.

1047 Daudi akawa mfalme katika Yerusalemu; Nathani na Gadi walitoa unabii.

1015 Suleimani akawa mfalme wa Israeli yote.

991 Hekalu lilimalizika kujengwa.

975 Suleimani alikufa; makabila kumi ya kaskazini yaliasi dhidi ya Rehoboamu, mwanawe, na Israeli ikagawanyika.

Matukio ya Israeli	**Matukio ya Yuda**	**Matukio katika Historia ya Kitabu cha Mormoni**
975 Yeroboamu alikuwa mfalme wa Israeli.		
	949 Shishaki, mfalme wa Misri, aliiteka Yerusalemu.	
875 Ahabu alitawala katika Samaria juu ya Israeli ya kaskazini; Eliya alitoa unabii.		
851 Elisha alifanya miujiza mikubwa.		
792 Amosi alitoa unabii.		
790 Yona na Hosea walitoa unabii.		
	740 Isaya alianza kutoa unabii. (Rumi inaanzishwa; Nabonasari alikuwa mfalme wa Babilonia katika mwaka 747; Tiglathi-pilesa III alikuwa mfalme wa Ashuru tangu mwaka 747 hadi 734.)	
	728 Hezekia alikuwa mfalme wa Yuda. (Shalmanasa IV alikuwa mfalme wa Ashuru.)	
721 Ule Ufalme wa Kaskazini uliangamizwa; yale makabila kumi yalichukuliwa utumwani; Mika alitoa unabii.		
	642 Nahumu alitoa unabii.	

Matukio ya Israeli	Matukio ya Yuda	Matukio katika Historia ya Kitabu cha Mormoni
	628 Yeremia na Zefania walitoa unabii.	
	609 Obadia alitoa unabii; Danieli alichukuliwa mateka utumwani Babiloni. (Ninawi ilianguka katika mwaka 606; Nebukadneza alikuwa mfalme wa Babilonia tangu mwaka 604 hadi 561.)	
		600 Lehi aliondoka Yerusalemu.
	598 Ezekieli alitoa unabii katika Babiloni; Habakuki alitoa unabii; Zedekia alikuwa mfalme wa Yuda.	
		588 Muleki aliondoka kutoka Yerusalemu kwenda nchi ya ahadi.
		588 Wanefi walijitenga wao wenyewe na Walamani (kati ya mwaka 588 na 570).
	587 Nebukadneza aliiteka Yerusalemu.	

Matukio katika Historia ya Uyahudi	Matukio katika Kitabu cha Mormoni
537 Koreshi alitangaza kuwa Wayahudi wanaweza kurudi kwao kutoka Babeli.	
520 Hagai na Zekaria walitoa unabii.	
486 Esta aliishi.	
458 Ezra alipewa mamlaka ya kufanya mageuzi.	
444 Nehemia aliteuliwa kuwa gavana wa Yuda.	
432 Malaki alitoa unabii.	

Matukio katika Historia ya Uyahudi		Matukio katika Kitabu cha Mormoni	
		400	Yaromu alipokea mabamba.
		360	Omni alipokea mabamba.
332	Iskanda Mkuu aliishinda Shamu na Misri.		
323	Iskanda alikufa.		
277	Septaginta, tafsiri ya maandiko ya Kiyahudi katika Kiyunani, ilianza.		
167	Mathalia Mmkabayo aliasi dhidi ya Shamu.		
166	Yuda Makabayo akawa kiongozi wa Wayahudi.		
165	Hekalu lilisafishwa na kuwekwa wakfu upya; Hanuka ikaanza.		
161	Yuda Makabayo alikufa.		
		148	Abinadi aliuawa kwa kifo cha kishahidi; Alma alilianzisha tena Kanisa miongoni mwa Wanefi.
		124	Benjamini alitoa hotuba yake ya mwisho kwa Wanefi.
		100	Alma Mtoto na wana wa Mosia walianza kazi yao.
		91	Utawala wa waamuzi ulianza miongoni mwa Wanefi.
63	Pompi aliishinda Yerusalemu, utawala wa Makabayo ukaisha katika Israeli, na utawala wa Warumi ukaanza.		
51	Cleopatra alitawala.		
41	Herodi na Fasaeli kwa pamoja walifanywa maliwali wa Yuda.		
37	Herodi akawa kiongozi katika Yerusalemu.		
31	Vita vya Aktio vilipiganwa; Augusto alikuwa mfalme mkuu wa Rumi kutoka mwaka wa 31 K.K. hadi mwaka wa 14 B.K.		
30	Cleopatra alikufa.		
17	Herode alirejesha hekalu.		
		6	Samweli Mlamani alitoa unabii juu ya kuzaliwa kwa Kristo.

Matukio katika Historia ya Ukristo		Matukio katika Historia ya Kitabu cha Mormoni	
B.K.		B.K.	
	Kuzaliwa kwa Yesu Kristo.		
30	Huduma ya Kristo ilianza.		
33	Kristo alisulubiwa.	33 au 34	Kristo mfufuka alionekana katika Marekani.
35	Paulo aliongolewa.		
45	Paulo alifanya safari yake ya kwanza ya kimisionari.		
58	Paulo alipelekwa Rumi.		
61	Historia ya Matendo ya Mitume ilifungwa.		
62	Rumi ilichomwa moto; Wakristo waliteswa chini ya Niro.		
70	Wakristo walikimbilia Pela; Yerusalemu ilizingirwa na kukamatwa.		
95	Wakristo waliteswa na Domitia.		
		385	Taifa la Wanefi liliangamizwa.
		421	Moroni alificha mabamba.

UPATANIFU WA INJILI

Mafundisho ya Mwokozi katika Mathayo, Marko, Luka, na Yohana yanaweza kulinganishwa yenyewe kwa yenyewe na ufunuo wa siku hizi za mwisho katika njia ifuatayo.

Tukio	Mathayo	Marko	Luka	Yohana	Ufunuo wa Siku za Mwisho
Nasaba za Yesu	1:1–17		3:23–38		
Kuzaliwa kwa Yohana Mbatizaji			1:5–25, 57–58		
Kuzaliwa kwa Yesu	2:1–15		2:6–7		1 Ne. 11:18–20; 2 Ne. 17:14; Mos. 3:5–8; Alma 7:10; Hel. 14:5–12; 3 Ne. 1:4–22
Unabii wa Simioni na Ana			2:25–39		
Kutembelea hekaluni (Pasaka)			2:41–50		
Mwanzo wa huduma ya Yohana	3:1, 5–6	1:4	3:1–3		M&M 35:4; 84:27–28
Ubatizo wa Yesu	3:13–17	1:9–11	3:21–22	1:31–34	1 Ne. 10:7–10; 2 Ne. 31:4–21
Majaribu ya Yesu	4:1–11	1:12–13	4:1–13		
Ushuhuda wa Yohana Mbatizaji				1:15–36	M&M 93:6–18, 26
Karamu ya harusi huko Kana (Muujiza wa kwanza wa Yesu)				2:1–11	
Kusafishwa kwa hekalu kwa mara ya kwanza				2:14–17	
Matembezi ya Nikodemo				3:1–21	
Mwanamke Msamaria Kisimani				4:1–42	
Yesu akataliwa huko Nazarethi			4:16–30		
Wavuvi wa samaki waitwa kuwa wavuvi wa watu	4:18–22	1:16–20			

Tukio	Mathayo	Marko	Luka	Yohana	Ufunuo wa Siku za Mwisho
Kujazwa kwa nyavu za samaki kimiujiza			5:1–11		
Kumi na Wawili waitwa na kutawazwa	10:1–4	3:13–19	6:12–16		1 Ne. 13:24–26, 39–41; M&M 95:4
Mahubiri ya Mlimani	5–7		6:17–49		3 Ne. 12–14
Sala ya Bwana	6:5–15		11:1–4		3 Ne. 13:5–15
Kufufuliwa kwa mwana wa mjane			7:11–15		
Yesu anapakwa mafuta na mwanamke.			7:36–50		
Mifano ya Yesu ni hadithi ambazo hulinganisha kitu cha kawaida au tukio na ukweli. Mara nyingi Yesu aliitumia kufundisha kweli za kiroho.					
Mpanzi:	13:3–9, 18–23	4:3–9, 14–20	8:4–8, 11–15		
Magugu:	13:24–30, 36–43				M&M 86:1–7
Mbegu ya haradali:	13:31–32	4:30–32	13:18–19		
Chachu:	13:33		13:20–21		
Hazina iliyo shambani:	13:44				
Lulu ya thamani kuu:	13:45–46				
Nyavu ya mvuvi:	13:47–50				
Mwenye nyumba:	13:51–52				
Mtumishi asiye na huruma:	18:23–35				
Mchungaji mwema:				10:1–21	3 Ne. 15:17–24
Msamaria mwema:			10:25–37		
Unyenyekevu: karamu ya harusi:			14:7–11		
Karamu kubwa ya chakula cha jioni			14:12–24		
Kondoo aliyepotea:	ona pia 18:12–14		15:1–7		
Sarafu iliyopotea:			15:8–10		
Mwana mpotevu:			15:11–32		

Tukio	Mathayo	Marko	Luka	Yohana	Ufunuo wa Siku za Mwisho
Msimamizi asiye na haki:			16:1–13		
Lazaro na mtu tajiri:			16:14–15, 19–31		
Mwamuzi asiye na haki:			18:1–8		
Wafanyakazi katika shamba la mizabibu:	20:1–16	ona pia 10:31			
Pauni:			19:11–27		
Wana wawili:	21:28–32				
Wakulima waovu:	21:33–46	12:1–12	20:9–19		
Harusi ya mwana wa mfalme:	22:1–14		linganisha 14:7–24		
Wanawali kumi:	25:1–13		ona pia 12:35–36		M&M 45:56–59
Talanta:	25:14–30				
Kondoo, mbuzi:	25:31–46				
Kutulizwa kwa tufani	8:23–27	4:35–41	8:22–25		
Kufukuzwa kwa kundi la mapepo wabaya na kutiwa katika nguruwe	8:28–34	5:1–20	8:26–29		
Kufufuliwa kwa binti wa Yairo	9:18–20, 23–26	5:21–24, 35–43	8:41–42, 49–56		
Kuponywa kwa mwanamke aliyekuwa akitokwa na damu	9:20–22	5:25–34	8:43–48		
Kazi za wale Kumi na Wawili	10:5–42	6:7–13	9:1–6		M&M 18
Kulisha watu elfu tano	14:16–21	6:33–44	9:11–17	6:5–14	
Yesu anatembea juu ya maji	14:22–33	6:45–52		6:15–21	
Mahubiri ya Mkate wa Uzima				6:22–71	
Ushuhuda wa Petro juu ya Yesu	16:13–16	8:27–29	9:18–21		

Tukio	Mathayo	Marko	Luka	Yohana	Ufunuo wa Siku za Mwisho
Petro aliadiwa funguo za ufalme	16:19				
Kugeuka sura; kukabidhiwa kwa funguo za ukuhani	17:1–13	9:2–13	9:28–36		M&M 63:20–21; 110:11–13
Sabini wateuliwa na kutumwa			10:1–12		M&M 107:25, 34, 93–97; 124:138–140
Kuponywa kwa kipofu siku ya Sabato				9	
Kurejeshwa kwa Lazaro				11:1–53	
Kuponywa kwa wenye ukoma kumi			17:11–19		
Kubarikiwa kwa Watoto	19:13–15	10:13–16	18:15–17		
Maria anapaka mafuta miguu ya Kristo	26:6–13	14:3–9		12:2–8	
Kuingia kwa shangwe	21:6–11	11:7–11	19:35–38	12:12–18	
Wabadilisha fedha wafukuzwa hekaluni	21:12–16	11:15–19	19:45–48		
Mchango mdogo wa mjane		12:41–44	21:1–4		
Angamizo la Yerusalemu na ishara za Ujio wa Pili	24	13	21:5–38		M&M 45:16–60; JS—M 1
Pasaka ya mwisho ya Yesu; kuanzishwa kwa sakramenti; maelekezo kwa wale Kumi na Wawili; kuoshwa miguu kwa wanafunzi	26:14–32	14:10–27	22:1–20	13–17	
Yesu ndiye mizabibu				15:1–8	
Mateso ya Yesu katika Gethsemani	26:36–46	14:32–42	22:40–46	18:1	2 Ne. 9:21–22; Mos. 3:5–12; M&M 19:1–24
Usaliti wa Yuda	26:47–50	14:43–46	22:47–48	18:2–3	
Kesi mbele ya Kayafa	26:57	14:53	22:54, 66–71	18:24, 28	

Tukio	Mathayo	Marko	Luka	Yohana	Ufunuo wa Siku za Mwisho
Kesi mbele ya Pilato	27:2, 11–14	15:1–5	23:1–6	18:28–38	
Kesi mbele ya Herodi			23:7–12		
Yesu alipigwa mijeledi na kudhihakiwa	27:27–31	15:15–20		19:1–12	
Kusulubiwa	27:35–44	15:24–33	23:32–43	19:18–22	Hel. 14:20–27; 3 Ne. 8:5–22; 10:9
Ufufuko	28:2–8	16:5–8	24:4–8		
Yesu awatokea wanafunzi		16:14	24:13–32, 36–51	20:19–23	
Yesu amtokea Thomaso				20:24–29	
Kupaa		16:19–20	24:50–53		